




بلوغ المرام

من أدلة الاحكام

Ufikiaji wa malengo kwa mujibu wa Dalili za kisheria

KUTAMBUA (KUKIRI)

BismiLLaah wasw-swalaatu was-salaamu 'alaa RasuuliLLaah wa
aalihi wa-aswahaabihi wa ba'ad,

Anastahiki Allaah (سبحانه وتعالى) kuhimidiwa, Swalaah na Salaam
zimfikie Nabiyy Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) na jamaa zake, na
Swahaba zake (رضي الله عنهم) na wote waliotangulia kwa wema
mpaka Siku ya Mwisho.

Imekuwa ni waajib wa kila Muislamu kufikisha ujumbe kwa
kuamrisha na kukatazana maovu kama Anavyoamrisha
Allaah (سبحانه وتعالى):

Taasisi la Albayaan Daawa media linapenda kutambua na
kukiri kazi nzuri iliofanywa na alhidaaya.com Tunakiri au
kutambua kuwa manhaj yao ipo sahihi kulingana na wema
waliotangulia. Tumenukuu kitabu hiki kutoka kwao bila ya
kuongeza au kupunguza chochote. Ukitaka unaweza
kufanya reference alhidaaya.com na utapata hayo yote.
Tunatoa katika mfumo wa e book kwa yeyote atakae hitaji.
Usisite kutujua kama utaona mapungufu yoyote kwani
kitabu kilicho kamili bila mapunguf ni Qurani
pekee. Mawasiliano yetu ni [alwastan 7@gmail.com](mailto:alwastan7@gmail.com).

Taasisi la albayan si ya kibiashara ni bure kwa kuisaidia jamii.

Buluwgh Al-Maraam ni mkusanyiko wa Hadiyth zenye hukmu za ki-Fiqhi, alizozikusanya Imaam Al-Haafidwh Ibn Hajar Al-‘Asqalaaniy (رحمه الله) .aliyezaliwa mwaka 773H mji wa Cairo

Hutokuta katika Buluwgh Al-Maraam Hadiyth zinazohusiana na ‘Aqiydah kama kuhusu Rusuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) na Manabii, Malaika, Majini, Jannah, Moto na kadhaalika. Bali ni Hadiyth zinazohusiana na hukmu za ‘ibaadah na mi’aamalaat.

Historia Fupi Ya:

Imaam Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah)

Jina Lake:

Ahmad bin ‘Aliy bin Muhammad, bin Muhammad, bin ‘Aliy, bin Mahmuwd, bin Ahmad, bin Ahmad bin Al-Kinaaniy Al-‘Asqalaaniy. Umaarufu wake ni Ibn Hajar ‘Asqalaaniy.

Babu zake waliishi Asqalaan ambapo walifika huko katika mwaka wa 583H. Jiji la Asqalaan liko Palestina huko Gaza. Neno Hajar ni jina la mmoja wa babu zake. Kun-ya yake ni Abul-Fadhwil na Laqab yake ni Shihaabuddiyn.

Kuzaliwa Kwake:

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu Allaah) alizaliwa tarehe 12 mwezi wa Sha'baan, 773H. Inasemekana pia amezaliwa tarehe 10 Sha'baan. Alizaliwa Misri karibu na ufukoni wa mto wa Nile alikulia huko huko.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alikuwa yatima. Baba yake ambaye alikuwa Mwanazuoni mkubwa na mfanya biashara alifariki katika mwaka wa 777H akimwacha Ibn Hajar (Rahimahu-Allaah) akiwa na miaka minne tu. Mama yake alifariki kabla ya hapo na kwa hivyo alikuwa yatima kutoka kwa wazazi wake wote wawili.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) amekulia katika familia yenye maadili mema na wazazi wenye ‘ilmu na wenye kushajishana katika kutafuta ‘ilmu.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alikuwa ana kaka mkubwa ambaye alikuwa ni ‘Aalim, lakini alifariki kabla ya Ibn Hajar, na kwa sababu hii, baba yake alikuwa na majonzi makubwa na huzuni mno. Mmoja wa Swaalihiyna Shaykh Yahyaa Asw-Swaanifiriy aliota ndoto akambashiria baba yake Ibn Hajar akamwambia kwamba atarithiwa (‘ilmu yake) na mtu ambaye atakuwa bora kuliko yeye, atakayekuwa na maisha marefu na kwamba atatoka katika mgongo wake ‘Aalim atakayejaza dunia kwa ‘ilmu. Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) mwenyewe kisha akasema: "Nilizaliwa kisha Allaah (Subhaanahu wa Ta'aalaa) Akanifungulia mikono." Kwa maana: Allaah Amemjaalia nuru ya 'ilmu kubwa na akili nzuri ya busara.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alilelewa na Zaakiy Al-Kharuwbiy ambaye alikuwa tajiri mfanya biashara maarufu.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) anahesabiwa kuwa ni mmoja wa watu adimu katika Historia ya Kiislamu. Imaam Al-Albaaniy (Rahimahu-Allaah) alisema: "Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alikuwa miongoni mwa ‘Ulamaa wakubwa kabisa, ambaye alihifadhi Hadiyth kwa usahihi kabisa wa hali ya juu."

Elimu Yake:

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alianza madrasa akiwa na umri wa miaka mitano, akahifadhi Qur-aan akiwa na umri wa miaka tisa. Alikuwa na akili nzuri mno ya kuhifadhi; aliweza kuhifahdi Suwraah Maryam kwa siku moja tu.

Mlezi wake; Zaakiy Al-Kharuwbiy alikwenda naye Hajj, akabakia huko na alipofika umri wa miaka kumi na mbili aliimamisha Waislamu Swalaah za Taraawiyh katika Masjid Al-Haram Makkah. Alikuwa ni mtoto tofuati na wenzake kutokana na upeo wa ‘ilmu yake na kuhifadhi kwake Qur-aan na kuweza kuimamisha watu katika umri mdogo kama huo. Hapakuweko na mtoto ambaye aliyelingana sawa naye katika ‘ilmu. Alipokuwa Makkah alihudhuria duruws za ‘Ulamaa waliokuwa wakifundisha huko.

Mnamo mwaka wa 786H Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alihama kutoka Makkah kurudi Misr ambako alihifadhi vitabu kadhaa vya mukhtasari mfano: ‘Umdatul-Ahkaam cha Al-Maqdisiyy na Al-Haawiy ambacho ni cha Fiqh ya Ash-Shaafi’iy na pia Al-Mukhtasar Al-Haajib ambacho ni cha Usuwl Al-Fiqh, na vitabu vingine vya sarufi ya lugha ya Kiarabu.

Alipofika umri wa miaka kumi na tisa aliisoma Qur-aan yote kwa Tajwiyd mbele ya Shihaab Al-Khayuwtwiy na alizisoma Hadiyth za Swahiyh Al-Bukhaariy mbele ya Mashaykh mbali mbali .

Akazidi kutafuta ‘ilmu katika sayansi mbalimbali, kama Tafsiyr na Qiraa-ah. Alikuwa akipenda sana kusoma Historia. Na alipenda sana kusoma fasihi ya lugha ya Kiarabu. Mmoja wa ‘Ulamaa Al-Badr

Al-Bushtakiy alimhimiza kusoma Al-Ghaaniy, ambayo ni vitabu vikubwa vilivyoandikwa katika fasihi ya Kiarabu. Vitabu hivyo vilikuwa ni mjeledi takriban ishirini mpaka thelathini na Ibn Hajar (Rahimahu-Allaah) alivisoma vyote kwa umakinifu hadi akawa, pindi akisikia shairi aliweza kutambua mtunzi wake na kufahamu kwa kina shairi hilo. Alipokaribia kufikia umri wa miaka ishirini na tano alikuwa ameshachuma na kukusanya ‘ilmu ambayo hapakuweco mtu aliyeweza kukusanya ‘ilmu kama yeye.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) aliandika mashairi mwenyewe. Akaanza kusoma zaidi Sayansi ya Hadiyth na Allaah (Subhaanahu wa Ta'aalaa) Akamjaalia mapenzi ya Hadiyth yakamsukuma kujifunza Sayansi ya Hadiyth kuzihifadhi moyoni mwake.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) akazidi kupatwa shauku kubwa na bidii ya kuzidi kutafuta elimu. Aliweza kujifunza elimu kubwa na alibarikiwa na Allaah (Subhaanahu wa Ta'aalaa) mkatika fani hiyo. Alikuwa akitembea sana masafa na safari za asubuhi na jioni kutafuta ‘ilmu kutoka kwa ‘Ulamaa wa zama zake.

Alisafiri kwenda Hijaz Sham, Syria, Misri akifika mpaka Alexandria, na sehemu zingine pia, ambapo aliweza kuchuma faida tele ya ‘ilmu na pia akanufaisha watu kwa ‘ilmu.

Alisafiri pia kwenda Yemen ambako alikutana na baadhi ya ‘Ulamaa kama Fayruwz Aabaadiy ambaye ni ‘Aalim bingwa mkubwa wa sarufi ya Kiarabu ambaye aliandika moja ya kamusi ya Lugha ya Kiarabu inayojulikana kama Qamuws Al-Muhiytw.

Pindi Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alipokuwa na umri wa miaka sitini na kipindi hiki alikuwa tayari ni ‘Aalim mkubwa, lakini hii haikumzuia kusafiri kwa ajili ya kutafuta ‘ilmu. Hii inaonyesha jinsi gani Imaam huyu mkubwa alivyokuwa na shauku na kuthibitika kwake kutafuta ‘ilmu kutoka kwa ‘Ulamaa wengineo.

Daraja Yake ‘Ilmu Na Hadhi Yake:

‘Ulamaa wa zama zake walimpa Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) kipaumbele na walimheshimu na akaheshimika katika zama zake na zama za baada yake.

Al-Buqaa’iy alisema kumhusu Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) kwamba: “Yeye ni Imaam wa Waislaam.”

Ash-Shawkaaniy amesema: “Yeye ni Al-Haafidhw Maarufu mwenye upeo wa ‘ilmu ya Hadiyth.”

Basi ilikuwa anapotajwa mtu kwa “Al-Haafidhw” ilijulikana moja kwa moja kuwa ni Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah)

Kufundisha Kwake:

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alifundisha Sayansi tofauti za Kiislam kama Tafsiyr ya Qur-aan, Qiraa-ah, Hadiyth, Fiqh (Shariy’ah) na kadhaalika. Alikuwa Mufti pia, hivyo alitowa Fatawa kwa watu. Alijishughulisha sana kuendeleza ‘ilmu ya Hadiyth, akiifundisha na akiandika. Alitoa mawaidha mahali pengi kama Al-Azhar, Jami’ ‘Amr, na penginepo. Pia alikuwa akifundisha

wanafunzi wake kwa imla kutoka katika hifdhw yake. ‘Ulamaa wengineo, Qadhi na Mufti walikuwa wakisafiri kwenda kwake kuchota elimu yake.

Walimu Wake Wengineo:

Miongoni mwa ‘Ulamaa mashuhuri ambao alijifunza kutoka kwao alikuwa Al-Hafidhw Al-Iraqi na Ibn Al-Mulaqqin, ambao walikuwa ‘Ulamaa wawili mashuhuri wa Hadiyth na alijifunza kutoka kwa ‘Ulamaa hawa wawili na ‘Ulamaa wengine kama wao. Aliishi pamoja na Az-Zayn Al-Iraqi kwa miaka kumi. Pia alisomeshwa na Al-Balqini, Ibn Al-Mulaqqin, Alijifunza Kiarabu kutoka kwa Al-‘Amari, alijifunza ufasaha wa lugha na mashairi kutoka kwa Al-Badr Al-Mushtaki, na alijifunza uandishi utoka kwa baadhi ya ‘Ulamaa. Pia alikuwa akiisoma Qur-aan katika Viraa vyote saba kutokwa kwa At-Tanuwkhiy.

Kazi Zake:

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) aliandika vitabu vingi vinavyopindukia mia moja na khamsini; vingi kati ya hivyo vilikuwa ni fani ya Hadiyth. Wafalme na wana wafalme wakawa wanapeana zawadi ya vitabu vyake.

Kitabu chake maarufu ni Fat-h Al-Baariy ambacho ni Sharh ya Swahiyh Al-Bukhaariy. Kitabu hiki hakika kilihesabika kuwa ni Kamusi ya Sunnah, bali ni Kamusi ya Sayansi za Kiislaam.

Kitabu hiki kilihesabiwa kuwa na faida kubwa kwa kuwa ilikuwa inapoulizwa maswali, basi Ibn Hajar (Rahimahu-Allaah) alitoa

majibu kutokana na Kitabu hiki na kuwafanya waulizaji wapate fahamu kamili ya maswali yao.

Pia katika kazi zake nyenginezo ni Tahdhiyb At-Tahdhiyb, Taqriyb At-Tahdhiyb, Lisaan Al-Miyzaan, Al-Iyswaabah fiy Tamyiyz Asw-Swahaabah, na Buluwgh Al-Maraam Min Adillat Al-Ahkaam.

Pia kazi zake (Vitabu) vingi mno mbalimbali vya Sayansi za Hadiyth, Tafsiyr, Uluwmul-Qur-aan.

Wadhifa:

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alikuwa Ustaadh, Mwandishi, Mufti na Qadhi wa Misri, kisha Sham, ikaongezewa kwenye eneo la madaraka yake, ambayo aliyashikilia kwa zaidi ya miaka ishirini. Mara ya kwanza, alikataa kukalia kiti cha Uqadhi, mpaka pale Sultani alipompelekea shauri moja makhsusi. Kisha akakubali kumwakilisha Al-Balqini alipomuomba sana awe Qadhi. Tena akashika wadhifa kwa ajili ya watu wengine mpaka alipoteuliwa akalie kiti cha Uqadhi Mkuu. Kisha akaondoka, lakini akalazimika kushika wadhifa wa Uqadhi mara saba, hadi alipoacha karibu na mwaka wa kufariki kwake

Khulqa (Tabia) Zake:

Kuhusu khulqa zake, Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alikuwa mnyenyekevu mno hadi kwamba alipoulizwa: “Je umepata kukutana au kumjua mtu kama wewe?” Alijibu:

فَلَا تُزَكُّوا أَنْفُسَكُمْ ۖ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اتَّقَىٰ (٣٢)

Basi msizitakase nafsi zenu. Yeye Anamjua zaidi aliyekuwa na taqwa. [An-Najm: 32]

Na baadhi ya Swahibu zake walimuuliza: “Je wewe umehifadhi zaidi au Adh-Dhahabiy?” Alinyamaza kimya bila kujibu lolote.

Kwa hiyo, hakuwa mwenye kujigamba kutokana na ‘ilmu yake wala daraja yake katika jamii.

Alikuwa pia mvumilivu, na mwenye subira na ustahamilivu mkubwa sana, mwenye zuhd (kuipa mgongo dunia). Ilisemwa kuwa alikuwa mcheshi, mwaminifu, mwerevu, mtu anaejinyima anasa, asiyejiweka mbele mbele, mkarimu, mtoa swadaqah, na aliyedumu katika Swalaah na Swiyaam za faradhi na za Sunnah. Hakuwacha kamwe Swalaah za jamaa wala hakupata kuacha kuamka kuswali usiku hadi alipofika kupata maradhi yake aliyofia. Imesemekana kwamba alikuwa akifunga Swiyaam siku moja na ya pili yake akila.

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu Allaah) alikuwa akila chakuka kidogo tu. Alikuwa mwangalifu katika kula chakula cha watu wengine, hakuwa na makuu, na alipokuwa safarini alikuwa akila chochote anachokipata. Pindi alipoishiwa na pesa za kununulia chakula, alikuwa akila chakula duni; chakula ambacho watu wa kawaida hawangeweza kula. Alikuwa anatahadhari na kukhofia sana kula chakula cha watu kutokana na chumo la haraam.

Alikuwa na khulqa na desturi nzuri ya kuwasiliana na Imaam, wawe ni wa daraja la juu au watu duni kabisa, na akitaamuli vizuri na watu alioishi nao, wawe wazee au vijana, maskini na mafakiri.

Kwa ujumla Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alikuwa na akhlaaq njema za kila aina, akhlaaq ambazo apasavyo kuwa nazo

Muumini wa kweli. As-Sakhaawiy aliandika mlango mzima kuhusu akhlaaq za Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah)

Kufariki Kwake:

Ibn Hajar ‘Asqalaaniy (Rahimahu-Allaah) alianza kuumwa katika mwezi wa Dhul-Qa’dah mwaka 852H lakini hakuacha kufundisha wala kuacha kazi zake nyenginezo za kunufaisha Waislamu katika mambo ya dunia yao na Aakhirah yao, wala hakuacha Swalaah ya jamaa. Kisha maradhi yakamzidi katika mwezi wa Dhul-Hijjah akashindwa kuhudhuria Swalaah ya ‘Iydul-Adhwhaa, ila aliswali Swaaah ya jamaa usiku wa kabla yake. Kisha ilipofika Jumanne tarehe 14 Dhul-Hijjah akazidiwa mno na maradhi hadi kufika Jumamosi tarehe 18 Dhul-Hijjah akafariki baada ya Swalaah ya ‘Ishaa.

Inasemekana kuwa aliswaliwa Swalaah ya Janaazah na Khaliyfah wa Al-‘Aabasiyy au Qaadhi mkuu al-Baqalaaniy. Mazishi yake Misr yalihudhuria na umati wa Waislamu akiwemo Sultan, pamoja na viongozi wengineo wa Kiislamu na ‘Ulamaa wakubwa na watu wengi mno walihudhuria hadi ilisemekana kwamba idadi ya watu waliohudhuria walifikia maelfu. Na akaswaliwa pia Swalaatul-ghayb (Swalaah ya ghaibu) sehemu kadhaa za Kiislamu ikiwemo Makkah, Sham, na miji mingineyo ya Kisalaam. Siku ya kufariki kwake ilikuwa siku adhimu ya huzuni kubwa kwa Waislamu.

Allaah Amrehemu Alimpe malipo mema ya Jannatul-Firdaws kwa juhudi zake katika Uislaam na kunufaisha kwake Waislamu.

كِتَابُ الطَّهَّارَةِ

Kitabu Cha Twahaarah

01-Mlango Wa Maji

بَابُ الْمِيَاهِ

01-Mlango Wa Maji

1.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الْبَحْرِ: { هُوَ الطُّهُورُ مَاوُهُ، الْجِلُّ مَيِّتُهُ } أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، وَابْنُ أَبِي شَيْبَةَ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ وَالتِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah[1] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu bahari: “Maji yake yanatwahaarisha, na maiti wake ni halaal (kuliwa).” [Imetolewa na Al-Arba’ah: Abuu Daawuwd, At-Tirmidhiy, An-

Nasaa'iy na Ibn Maajah na Ibn Abiy Shaybah na tamshi la Hadiyth hii ni lake Ibn Khuzaymah akaisahihisha na At-Tirmidhiy]

2.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: {إِنَّ الْمَاءَ طَهُورٌ لَا يُنَجِّسُهُ شَيْءٌ} أَخْرَجَهُ الثَّلَاثَةُ وَصَحَّحَهُ أَحْمَدُ

Kutoka kwa Sa'iyd Al-Khudriyy[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika maji ni masafi[3], hayanaajisiwi na kitu.” [Imetolewa na Ath-Thalaathah: Abuu Daawuud, At-Tirmidhiy na An-Nasaa'iy na akaisahihisha Ahmad]

3.

وَعَنْ أَبِي أَمَامَةَ الْبَاهِلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: {إِنَّ الْمَاءَ لَا يُنَجِّسُهُ شَيْءٌ، إِلَّا مَا غَلَبَ عَلَى رِيحِهِ وَطَعْمِهِ، وَلَوْنِهِ} أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَةَ وَضَعَّفَهُ أَبُو حَاتِمٍ

Kutoka kwa Abuu Umaamah Al-Baahiliyy[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika maji hayanaajisiwi na chochote isipokuwa kinachozidi harufu yake, ladha yake na rangi.” [Imetolewa na Ibn Maajah na Abuu Haatim akaidhoofisha]

Aliyepokea Al-Bayhaqiyy: “Maji ni yenye kutwahirisha isipokuwa yakiingia najsi na kuyabadilisha harufu, ladha au rangi[5] yake.”

4.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: {إِذَا كَانَ الْمَاءُ قُلَّتَيْنِ لَمْ يَحْمِلِ الْخَبَثُ}

وَفِي لَفْظٍ: {لَمْ يَنْجُسْ} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Abdullaahi bin ‘Umar[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: Rasuli wa Allaah amesema: “Pindi maji yakiwa qullatayn[7] (viriba au mitungi miwili) huwa hayachukui uchafu.”

Na katika tamshi: “Haifanyi kuwa najisi.” [Imetolewa na Al-Arba’ah na ameisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Maajah]

5.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: { لَا يَغْتَسِلُ أَحَدُكُمْ فِي الْمَاءِ الدَّائِمِ وَهُوَ جُنُبٌ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

وَالْبُخَارِيُّ: { لَا يَبُولَنَّ أَحَدُكُمْ فِي الْمَاءِ الدَّائِمِ الَّذِي لَا يَجْرِي، ثُمَّ يَغْتَسِلُ فِيهِ }

وَلِمُسْلِمٍ: { مِنْهُ }
وَلِأَبِي دَاوُدَ: { وَلَا يَغْتَسِلُ فِيهِ مِنَ الْجَنَابَةِ }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asioge mmoja wenu katika maji yaliyotuwama ilhali ana janaba.” [Imetolewa na Muslim]

Na katika Al-Bukhaariy: “Asikojoe mmoja wenu katika maji yaliyotuwama ambayo hayaendi kisha akaoga ndani yake[8].”

Na katika riwaayah nyengine ya Muslim: “Kutoka humo” (yaani kutoka kwenye maji hayo).

Na kwa Abuu Daawuwd: “Mtu asioge humo janaba.”

6.

وَعَنْ رَجُلٍ صَحِبَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "أَنْ تَغْتَسِلَ الْمَرْأَةُ بِفَضْلِ الرَّجُلِ، أَوْ الرَّجُلُ بِفَضْلِ الْمَرْأَةِ، وَلْيَغْتَرِفَا جَمِيعًا. أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ. وَالنَّسَائِيُّ، وَإِسْنَادُهُ صَحِيحٌ.

Mtu mmoja[9] aliyesuhubiana na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza mwanamke kuoga mabaki ya maji ya mwanamume na mwanamume kuoga mabaki ya maji ya mwanamke, wachote pamoja.”

[Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaa'iy na Isnaad yake ni Swahiyh]

7.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَغْتَسِلُ بِفَضْلِ مَيْمُونَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا. أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ.

وَلِأَصْحَابِ "السُّنَنِ": اغْتَسَلَ بَعْضُ أَزْوَاجِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي جَفْنَةٍ، فَجَاءَ لِيَغْتَسِلَ مِنْهَا، فَقَالَتْ لَهُ: إِنِّي كُنْتُ جُنْبًا، فَقَالَ: {إِنَّ الْمَاءَ لَا يُجْنِبُ} وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) kwamba Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akioga kwa maji yaliyoacha na Maymuwnah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا). [Imetolewa na Muslim]

Na katika mapokezi ya Aswhaab As-Sunan]:

(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) “Mmoja katika ya wake wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alioga kwenye beseni kisha Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akaja kuoga katika chombo hicho, huyo mkewe[11] akamwambia: “Mimi nilikuwa na janaba.” Akasema: “Hakika maji hayapati janaba.” [Ameisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Khuzaymah]

8.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: {طَهُورُ إِنَاءٍ أَحَدِكُمْ إِذْ وَلَغَ فِيهِ الْكَلْبُ أَنْ يَغْسِلَهُ سَبْعَ مَرَّاتٍ، أَوْ لَاهُنَّ بِالتُّرَابِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ.
وَفِي لَفْظٍ لَهُ: {فَلْيُرْقَهُ}
وَلِلتِّرْمِذِيِّ: {أَخْرَاهُنَّ، أَوْ أُولَاهُنَّ بِالتُّرَابِ} .

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwamba Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kutwaharisha chombo cha mmoja wenu ikiwa kimeambwa na mbwa, ni ki kukiosha mara saba[12].”

[Imetolewa na Muslim].

Tamshi jengine la Muslim: “Basi amwage.”

Na katika riwaayah ya Imaam At-Tirmidhiy: “Kwanza au mwisho wake kwa mchanga.”

9.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ فِي الْهَرَّةِ: {إِنَّهَا لَيْسَتْ بِنَجَسٍ، إِنَّمَا هِيَ مِنَ الطَّوَافِينَ عَلَيْكُمْ} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ.
وَابْنُ خُزَيْمَةَ.

Kutoka kwa Abuu Qataadah[13] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwamba Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu paka: “Huyo si najsi bali ni mmoja wa wananchanganyika nanyi.” [Imetolewa na Al-Arba’ah: Abuu Daawuwd, At-Tirmidhiy, An-Nasaa’iy na Ibn Maajah na ameisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Khuzaymah]

10.

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { جَاءَ أَعْرَابِيٌّ فَبَالَ فِي طَائِفَةِ الْمَسْجِدِ، فَزَجَرَهُ النَّاسُ، فَنَهَاَهُمُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَلَمَّا قَضَى بَوْلَهُ أَمَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِذُنُوبٍ مِنْ مَاءٍ، فَأُهْرِيقَ عَلَيْهِ. } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

Kutoka kwa Anas bin Maalik[14] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Bedui mmoja alikuja akakojoa katika pembe ya Msikiti, watu wakamkemea Lakini Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawakataza. Alipomaliza mkojo wake, Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaamrisha iletwe ndoo ya maji, ikamwagiwa[15] juu yake (huo mkojo). [Al-Bukhaariy, Muslim]

11.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أُحِلَّتْ لَنَا مَيِّتَتَانِ وَدَمَانِ، فَأَمَّا الْمَيِّتَتَانِ:

فَالْجَرَادُ وَالْحُوتُ، وَأَمَّا الدَّمَانُ: فَالطَّحَالُ وَالْكَبِدُ { أَخْرَجَهُ
أَحْمَدُ، وَابْنُ مَاجَهَ، وَفِيهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) kwamba Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tumehalalishiwa
maiti za aina bili na damu za aina mbili. Ama maiti mbili ni nzige na
samaki ‘ na ama damu mbili ni bandama na ini.” [Imetolewa na
Ahmad na Ibn Maajah na Hadiyth hii ina yaliyo dhaifu]

12.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا وَقَعَ الذُّبَابُ فِي شَرَابٍ أَحَدِكُمْ
فَلْيَغْمِسْهُ، ثُمَّ لِيْنِزْهُ، فَإِنَّ فِي أَحَدِ جَنَاحَيْهِ دَاءٌ، وَفِي الْآخَرِ
شِفَاءٌ { أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ.

وَأَبُو دَاوُدَ ، وَزَادَ: { وَإِنَّهُ يَتَّقِي بِجَنَاحِهِ الَّذِي فِيهِ الدَّاءُ {

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwamba Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Pindi nzi
akiangukia katika kinywaji cha mmoja wenu, basi amazmishe kisha
amtoe , kwani kuna ugonjwa katika moja ya bawa lake na tiba katika
bawa jengine[16].” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na Abuu Daawuwd ambaye aliongeza:

“Kwani yeye (inzi) huangulikia kwa bawa lake lenye ugonjwa.”

13.

عَنْ أَبِي وَاqِدِ اللَّيْثِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَا قُطِعَ مِنَ الْبَهِيمَةِ وَهِيَ حَيَّةٌ فَهُوَ مَيِّتٌ }
أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ، وَاللَّفْظُ لَهُ.

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Waaqid Al-Laythiyy[17] (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kwamba Nabiyy amesema:
“Kilichokatwa kutoka kwa mnyama aliye hai basi hicho ni maiti.”
[Imetolewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy na ameipa daraja ya Hasan na tamashi hili ni lake]

[1] Abuu Hurayrah: Jina lake halisi ni ni ‘Abdullaah au ‘Abdur-Rahmaan bin Sakhr Ad-Daws, mmoja wa Swahaba wakubwa wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na alipokea Hadiyih nyingi kuliko wote. Zaidi ya watu 800 walipokea kutoka kwake. Alisilimu katika mwaka wa Khaybar (7H) na akawa karibu na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mpaka Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) alipofariki. Akateuliwa kuwa Mufti (Mwanazuoni wa hukumu za Kiislaam) wakati wa Ukhalifa wa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) na baadaye akawa gavana wa Madiynah wakati wa utawala wa Marwaan bin Al-Hakam. Alifariki mwaka 59 H na akazikwa Al-Baqi’.

[2] Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy: Jina lake ni Sa'd bin Maalik bin Sinan Al-Khazraj Al-Answaar. Alikuwa miongoni mwa Swahaba wasomi. Alipokea Hadiyth nyingi, na alitoa rai za kidini kwa muda fulani. Alifariki mwanzoni mwa mwaka wa 74H akiwa na umri wa miaka 86.

[3] Imepokewa na Ahmad, At-Tirmidhiy, na Abuu Daawud kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisema maneno hayo katika kujibu swali kuhusu kisima cha Buda'a, kilicho karibu na Madiynah, na daima kilijaa uchafu. Kilikuwa kwenye eneo lililo chini, na maji ya mvua yalikuwa yanapeleka uchafu na takataka kisimani. Maneno haya bila shaka yanakihusu.

[4] Abuu Umaamah Al-Baahiliy: Jina lake halisi ni Suday bin Ajlaan akiwa ni mmoja wa Swahaba waliopokea Hadiyth nyingi. Aliishi Misri, kisha akahamia Hims (sasa iko Syria), na akafia kule akiwa na umri wa miaka 81 au 86.

[5] Baadhi ya watu wamehoji kwamba, maji yanaweza kupunguka au kuongezeka wingi wake ikiwa huo uchafu au taka zitabadili moja ya sifa zake hizo tatu (rangi, harufu na ladha), na hapo maji yatanajisika. Lakini maoni sahihi katika maudhui haya ni kuwa, iwapo maji yako chini ya kilo 227 (Qulla mbili), basi taka yoyote inayanajisi maji, iwe imebadilisha moja ya sifa zake au laa. Lakini ikiwa maji yana kilo 227, hayanajisiki mpaka ibadilike mojawapo kati ya sifa zake hizo tatu.

[6] 'Abdullaah bin 'Umar alikuwa miongoni mwa wenye kuipa nyongo dunia na mwenye elimu kubwa sana. Alisilimu Makkah wakati akingali kijana mdogo na akahamia Madiynah. Kwanza alishiriki katika vita vya Khandaq, na akafariki mnamo mwaka 73H, akazikwa kule Dhi-Twuwaa.

[7] Qulla ni mtungi mkubwa wa udongo unaoweza kuwa na maji yapatayo viriba viwili na nusu, yaani kilo 113.

[8] Hii inahusu maji kidogo. Iwapo maji ni mengi, yatahesabika kama maji yanayokwenda au kutiririka, ambayo si machafu na ni mazuri kwa kuogea. Imekatazwa kukojolea maji yaliyosimama ardhini, na kwamba mtu

asifanye hivyo ili asizowee kuchafua maji. Maji yanayotiririka kila mara huwa masafi; na hayanajisiki kwa kutiwa takataka au uchafu.

[9] Huyu ni mmoja wa Swahaba, na kutokutajwa jina lake hakuiathiri Hadiyth kwa kuwa Swahaba wote walikuwa waaminifu kabisa.

[10] Ibn ‘Abbaas: Huyu ndiye ‘Abdullaah bin ‘Abbaas bin ‘Abdul-Mutwalib, binammi wa Nabiy (ﷺ) na Mwanazuoni wa Ummah wa Kiislaam, aliyezaliwa miaka 3 kabla ya Hijrah na akafariki mnamo mwaka 67 A.H.

[11] Hadiyth hii inaonekana kama inapingana na ya kwanza, lakini sivyo, kwani amri si ya kukataza moja kwa moja, bali ni mapendekezo ya kukataza ili kuepuka mabaki yoyote ya uchafu.

[12] Ieleweke kwamba, kukosha tu uchafu katika chombo, si lazima kuwe mara saba. Falsafa ya kukiosha kitu kikawaida ni tofauti na kukiosha uchafu mahsusi. Madaktari wa zama hizi wanasema kuwa aghalabu katika matumbo ya mbwa huwa kuna viini vya maradhi na minyoo ipatayo urefu wa milimita 4, na hivi hutoka pamoja na kinyesi na hujishikiza kwenye nywele zizungukazo duburi ya mbwa. Mbwa hujisafisha duburi kwa ndimi zao, huchukua viini na minyoo hiyo, na pindi anapolamba chombo au ukimbusu kinywa chake (kama wazungu wafanyavyo). Viini hivi huhamia kwenye chombo au kwenye mdomo wa mtu anayembusu mbwa, na hatimaye huingia tumboni mwa mwana Adam, na huweza kupenya mpaka kwenye seli za damu na kusababisha magonjwa yanayoweza hata kuua. Kwa kuwa viini hivi havionekani bila darubini. Shariy’ah ya Kiislaam iliamuru kuwa mate ya mbwa kwa ujumla ni najsi, na chochote kinachonajisiwa na mate ya mbwa ni sharti kiohwe mara saba (7), moja ya mara hizi saba, iwe kwa udongo ili kuwa na hakika wa usafi wake. Ili uyajue vyema maudhui haya, tafadhali soma tanbihi chini ya ukurasa wa kitabu cha Ahkaamul-Ahsan, Sharh ‘Umdatul Ahkaam.

[13] Huyu Abuu Qatada ndiye Al-Haarith bin Rib’I Al Answaar, mwangalizi wa farasi wa Nabiy (ﷺ). Alipigana

katika vita vya Uhud, na vita vingine vilivyofuatia. Inasemekana kuwa alifariki Madiynah au Kufa mnamo mwaka 54 A.H.

[14] Anas bin Maalik alikuwa mtumishi wa Nabiyy (ﷺ) kutoka wakati alipokwenda Madiynah mpaka alipofariki. Anajulikana kwa jina la Abuu Hamzah na alikuwa Mkhazrajiy. Aliishi kule Basra wakati wa ukhalifa wa ‘Umar (رضي الله عنه), na akafariki kule akiwa na umri wa miaka 99 au 103, mnamo mwaka wa 91 au 92 au 93 A.H.

[15] Hadiyth hii inathibitisha kwamba, mchanga au udongo husafika ukikauka, kama Abuu Shaybah alivyopokea, hususan iwapo utamwagia maji na yatiririke juu ya mahali palipokojolewa.

[16] Ni wazi kutoka katika Hadiyth hii kwamba endapo inzi kadondokea katika maji au kinywaji, hakitafanywa kichafu, sawa na viumbe vya familia hii ambayo damu yake haitembei, kama mbu, dondola na buibui, hawakifanyi kinywaji kiwe kichafu wakidondokea au kufia humo.

[17] Jina halisi la Abuu Waqiyyd ni Al-Haarith bin ‘Awf, na kizazi cha Banu ‘Aamir bin Layth. Alisilimu mapema sana na anahesabika kuwa ni mtu wa Madiynah. Inasemekana kwamba alipigana katika vita vya Badr, aliishi Makkah, na akafariki Makkah mnamo mwaka 65 au 68 A.H alipokuwa na miaka 57, na akazikwa Funj.

02-Mlango Wa Vyombo Vya Chakula, Kunywea Na Kutawadhia

بَابُ الْأَنْيَةِ

14.

عَنْ حُذَيْفَةَ بْنِ الْيَمَانِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَشْرَبُوا فِي أَنْيَةِ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ، وَلَا تَأْكُلُوا فِي صِحَافِهَا، فَإِنَّهَا لَهُمْ فِي الدُّنْيَا، وَلَكُمْ فِي الْآخِرَةِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Hudhayfah bin Al Yamaaniy[1] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msinywe katika vyombo vya fedha na vya dhahabu na wala msile katika sahani zake[2], kwani hivyo ni vya wasioamini humu duniani na ni vyenu Aakhirah.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

15.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { الَّذِي يَشْرَبُ فِي إِنَاءِ الْفِضَّةِ إِنَّمَا يُجْرَجُ فِي بَطْنِهِ نَارَ جَهَنَّمَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ummu Salamah[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika anayekunywa katika vyombo vya fedha anameza moto wa Jahannam tumboni mwake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

16.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا دُبِغَ الْإِهَابُ فَقَدْ طُهِرَ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ.

وَعِنْدَ الْأَرْبَعَةِ: { أَيُّمَا إِهَابٍ دُبِغَ }

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ngozi ikitengezwa, imetoharika[4].” [Imetolewa na Muslim]

Na kwa Al-Arba’ah: “Ngozi yoyote iliyotengenezwa.”

17.

وَعَنْ سَلَمَةَ بْنِ الْمُحَبِّقِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { دِبَاغُ جُلُودِ الْمَيِّتَةِ طُهْرُهَا } صَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Salamah bin Al-Muhabbig[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuisafisha ngozi ya maiti ni kuitakasa kwake.” [Ameisahihisha Ibn Hibbaan]

18.

وَعَنْ مَيْمُونَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، قَالَتْ: مَرَّ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِشَاةٍ يَجْرُونَهَا، فَقَالَ: {لَوْ أَخَذْتُمْ إِهَابَهَا؟}
فَقَالُوا: إِنَّهَا مَيْتَةٌ، فَقَالَ: {يُطَهَّرُهَا الْمَاءُ وَالْقَرَضُ} أَخْرَجَهُ أَبُو
دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ

Kutoka kwa Maymuwnah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipita mbele ya watu
wanaoburuza mbuzi akasema: “Lau mgelichukua ngozi yake.”
Wakasema: “Huyo ni maiti.” Akasema: “Maji na qaradh huitakasa
(ngozi hiyo).” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy]

19.

وَعَنْ أَبِي ثَعْلَبَةَ الْخُسَنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قُلْتُ: يَا
رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّا بِأَرْضِ قَوْمٍ أَهْلِ كِتَابٍ، أَفَنَأْكُلُ فِي أَنْيَتِهِمْ؟
فَقَالَ: {لَا تَأْكُلُوا فِيهَا، إِلَّا أَنْ لَا تَجِدُوا غَيْرَهَا، فَاغْسِلُوهَا،
وَكُلُوا فِيهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Tha’labah Al-Khushaniyyi[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
amesema: Niliuliza: Ee Rasuli wa Allaah! Tunaishi katika nchi
inayokaliwa na Ahlul-Kitaab. Je tunaweza kula katika vyombo vyao?
Akasema: “Msile katika vyombo vyao[7], isipokuwa msipopata
vingine, hapo basi viosheni na mle katika vyombo hivyo.” [Al-
Bukhaariy, Muslim]

20.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَأَصْحَابَهُ تَوَضَّعُوا مِنْ مَزَادَةِ امْرَأَةٍ مُشْرِكَةٍ.
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، فِي حَدِيثٍ طَوِيلٍ

(رضي الله عنهما) [8] Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn[8]
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na
amesema kwamba Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na
Swahaba zake walitawadha kutoka kwenye maji ya kiriba cha
ngozi[9] cha mwanamke mshirikina.” [Al-Bukhaariy, Muslim] [Hii
ni sehemu ya Hadiyth ndefu]

21.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ قَدَحَ النَّبِيِّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ انْكَسَرَ، فَاتَّخَذَ مَكَانَ الشَّعْبِ سِلْسِلَةً مِنْ فِضَّةٍ.
أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwamba: “Jagi la
Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) lilivunjika, akaziba penye
mwanya kwa mnyororo wa fedha.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

[1] Hudhayfah alipewa jina la utani la Abuu ‘Abdillaah. Yeye na baba yake
walikuwa Swahaba. Alikuwa kuwa maarufu kwa kuwa msiri wa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alifariki Midian (Madain) siku arubaini baada
ya kuuliwa ‘Uthmaan katika mwaka wa 35 au 36.H.

[2] Hadiyth hii imetajwa hapa kwa madhumuni kuwa, iwapo imekatazwa kunywa au kula kwenye vifaa vya metali hizo, basi kutawadhia vyombo vya metali hizo kumekatazwa, vinginevyo Hadiyth hii ingewekwa katika Mlango wa Kula na Kunywa. Lakini kula na kunywa katika vifaa vilivyopambwa na almasi na rubi inaruhusiwa.

[3] Ummu Salamah ni Hindi bint Abiy ‘Umaiyyah. Aliolewa na Abuu Salamah, akahajiri naye hadi Uhabeshi (Ethiopia), na akaja naye hadi Madiynah. Abuu Salamah alipofariki kutokana na jeraha alilolipata katika vita vya Uhud, Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuoa mnamo Shawwaal mwaka 4 A.H. Yasemekana kuwa alifariki mwaka 59 au 62 A.H akiwa na umri wa miaka 84, na akazikwa Al-Baqi’.

[4] Hadiyth hii inathibitisha kuwa ngozi ikishapitia kwa ufundi wa kiwandani (tasnia), huwa inakuwa safi na nadhifu, inaweza kuwa ni ngozi ya mnyama aliye haraam au halaal kuliwa, na kama mnyama huyo alichinjwa au amekufa mwenyewe. Lakini ngozi za wana Aadam na baadhi ya wanyama ni haraam na haziruhusiwi kutumika. Ngozi ya mwana Aadam ni haraam kwa sababu ya utukufu wake. Na ngozi za wanyama kama mbwa au nguruwe ni haraam kwa sababu wamezaliwa najisi na wachafu. Sharti ikumbukwe kwamba nywele, meno na pembe za wanyama walioruhusiwa pia ni halaal kutumika na kwa biashara.

[5] Salamah alipewa jina la utani la Abuu Sinaan wa kabila la Hudhayl. Alihesabika kuwa ni mkazi wa Basra, na Al-Hasan Al-Basr alipokea Hadiyth hii toka kwake.

[6] Abuu Tha’labah ni Swahaba aliyetokana na kizazi cha Khushayn bin An-Nimir wa kabila la Quda’a. Alikuwa mmoja wa Swahaba wa Asw-haab Ash-Shajarah waliombai Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) siku ya Al-Hudaibiyah. Alitumwa kwa watu wake na wote wakashilimu. Aliishi Shaam na akafariki kule mwaka 75 A.H.

[7] Hadiyth hii inaweka wazi kuwa, endapo vipo vyombo vya Muislaam, basi visitumike vya asiye Muislaam kwa kula, kupikia chakula, wala kunywea vinywaji. Iwapo kuna uhakika kuwa asiye Muislaam havitumii

vyombo vile kwa kula au kunywa vitu haraam, basi vyombo vyake hivyo vinaweza kutumika; lakini hata hivyo sharti kuwa na tahadhari.

[8] ‘Imraan alipewa jina la utani la Abuu Nujayd, na anatoka katika kabila la Khuza’a. alisilimu mnamo mwaka wa Khaybar. Alilelewa na kuishi Basra, na akafia hapo mnamo mwaka 52 au 53 A.H.

[9] Hadiyth hii inaweka wazi kuwa, vyombo kama hivyo vya waabuduo miungu wengi, vinaweza kutumika bila kusita, kukiwa hakuna uwezekano wa vyombo hivyo kuwa si visafi.

03-Buluwgh Al-Maraam: Kitabu Cha Twahaarah:Mlango Wa Kuondosha Najisi Na Ubainifu Wake

بَابُ إِزَالَةِ النَّجَاسَةِ وَبَيَانِهَا

22.

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سُئِلَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ الْخَمْرِ تُتَّخَذُ خَلًّا؟ قَالَ: { لَا } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ^{٢٨}

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa kuhusu kutengeneza siki kutokana na mvinyo. Akasema: “Hapana[1].” [Imetolewa na Muslim]

23.

وَعَنْهُ قَالَ: لَمَّا كَانَ يَوْمُ خَيْبَرَ، أَمَرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَبَا طَلْحَةَ، فَنَادَى: {إِنَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ يَنْهَيَانِكُمْ عَنْ أُحُومِ الْحُمُرِ الْأَهْلِيَّةِ، فَإِنَّهَا رِجْسٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Katika siku ya Khaybar, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuamrisha Abuu Twalhah[2] kutangaza: “Hakika Allaah na Rasuli Wake wamekukatazeni kula nyama ya punda vihongwe kwa kuwa ni najisi.[3]” [Al-Bukhaariy, Muslim]

24.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ خَارِجَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {خَطَبَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِمِنَى وَهُوَ عَلَى رَاحِلَتِهِ، وَلَعَابُهَا يَسِيلُ عَلَى كَتِفَيَّ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Amr bin Khaarijah[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitukhutubia kule Minna huku akiwa juu ya kipando chake, na mate yake yanachuruzika mabegani[5] mwangu.” [Imetolewa na Ahmad na ameisahihisha At-Tirmidhiy]

25.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَغْسِلُ الْمَنِيَّ، ثُمَّ يَخْرُجُ إِلَى الصَّلَاةِ فِي ذَلِكَ
التَّوْبِ وَأَنَا أَنْظُرُ إِلَى أَثَرِ الْغُسْلِ فِيهِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَلِمُسْلِمٍ: { لَقَدْ كُنْتُ أَفْرُكُهُ مِنْ تَوْبِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَرَكًا، فَيُصَلِّي فِيهِ }
وَفِي لَفْظٍ لَهُ: { لَقَدْ كُنْتُ أَحْكُهُ يَابِسًا بِظُفْرِي مِنْ تَوْبِهِ }

Kutoka kwa ‘Aaishah[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiosha manii[7], na
kisha alikuwa akielekea katika Swalaah na nguo hiyo, nami nilikuwa
naona mabaki ya athari za maosho ndani yake.” [Al-Bukhaariy,
Muslim]

Na katika Muslim: “Nilikuwa nikikwangua (manii) kutoka kwenye
nguo ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mkwanguo
na huswali na nguo hiyo.”

Na katika riwaayah nyengine ya Muslim: “Mimi (‘Aaishah) nilikuwa
nayakwangua kwa kucha yangu hali ya kuwa yamekauka.”

26.

وَعَنْ أَبِي السَّمْحِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { يُغْسَلُ مِنْ بَوْلِ الْجَارِيَةِ، وَيُرَشُّ مِنْ بَوْلِ
الْغُلَامِ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَالنَّسَائِيُّ وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu As-Samh[8] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkojo wa mtoto mchanga
wa kike uoshwe, na mkojo wa mtoto wa kiume unyunyiziwe

maji[9].” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaa'iy na ameisahihisha Al-Haakim]

27.

وَعَنْ أَسْمَاءَ بِنْتِ أَبِي بَكْرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ فِي دَمِ الْحَيْضِ يُصِيبُ الثَّوْبَ: { تَحْتُهُ ثُمَّ تَقْرُصُهُ بِالْمَاءِ ثُمَّ تَنْضَحُهُ ثُمَّ تُصَلِّي فِيهِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

Kutoka kwa Asmaa' bint Abiy Bakar[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuhusu kwamba Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu damu ya hedhi inayodondokea nguo: “Aikwanguye, aifikiche na maji, na kisha aioshe, na kisha aswali na nguo hiyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

28.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَتْ خَوْلَةُ: { يَا رَسُولَ اللَّهِ، فَإِنْ لَمْ يَذْهَبِ الدَّمُ، قَالَ: "يَكْفِيكَ الْمَاءُ، وَلَا يَضُرُّكَ أَثَرُهُ" } أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَسَنَدُهُ ضَعِيفٌ²⁸

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Khawlah[11] aliuliza: “Ee Rasuli wa Allaah! Je, endapo alama ya damu haitatoweka?” Akasema: “Maji yanakutosha, na athari yake haitokuathiri chochote.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy, na Isnaad yake ni dhaifu]

[1] Kutengeneza siki kwa kuongeza vitu kwenye mvinyo kumekatazwa.

[2] Abuu Twahlah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) ndiye Zayd bin Sahl bin Al-Aswad bin Haraam Al-Answaar An-Najaar, ambaye alikuwa ni mmoja wa Swahaba waandamizi. Alihudhuria Bay'atul-'Aqabah na vita vyote.

Alipigana kishujaa wakati wa Vita Vya Uhud na akamhami Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mpaka mkono wake ukapooza. Pia aliua watu ishirini katika Vita Vya Hunayn. Akijulikana kwa Abuu Twalha Al-Answaawiry na alikuwa ni mume wa Ummu Sulaym ambaye alitaka mahari yake yawe ni kusilimu kwake. Wawili hawa walikuwa wakarimu mno na wenye iymaan za hali ya juu. Walikuwa na visa vizuri vyenye mafunzo na vya kuisisimua, na hata kisa chake kimoja cha kupokea wageni kilikuwa ni sababu ya kuteremshwa kauli ya Allaah (عز وجل):

وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ

Na wanawapendelea kuliko nafsi zao japokuwa wao wenyewe wanahitaji. [Al-Hashr: 9]

Alifariki mwaka 34 au 51 A.H.

[3] Hadiyth hii ni dalili kuwa nyama ya punda vihongwe ni haraam.

[4] 'Amr ndiye 'Amr bin Kharija bin Al-Muntafiq Al-Asad. Alikuwa rafiki wa Abuu Sufyaan. Anahesabika kuwa alitokana na ukoo wa Al-Ash'ar. Yeye ni miongoni mwa Swahaba waliolowea Sham, na Hadiyth yake iliripotiwa na watu wa Basra.

[5] Kutoka katika Hadiyth hii tunatambua kuwa mate ya mnyama ambaye ni halaal (kuliwa) ni masafi. Hadiyth hii iliafikiwa na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[6] ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) ni binti wa Abuu Bakar Asw-Swiddiyq (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) aliyeolewa na Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) miaka miwili kabla ya Hijrah (kuhama) mnamo mwezi wa Shawwaal, lakini akaanza kuishi naye mnamo mwaka wa 1 A.H wakati akiwa na umri wa miaka 9. Alikuwa msomi sana na aliripoti Hadiyth nyingi. Alifariki mnamo tarehe 17 mwezi wa Ramadhwaan mwaka 57 au 58 A.H. Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimswalia Swalaah ya Janaazah, na akazikwa Al-Baq’.

[7] Kuna kutofautiana maoni kuhusu manii ya mwana Aadam, kama ni safi au siyo safi. Wanazuoni wengine wanayahesabu kama mate au makamasi, na kwa mujibu wa wengine ni lazima kuyaosha. Kundi hilo la kwanza linatoa sababu yake katika Hadiyth ya kuwa huwa yanakwanguliwa yakikauka, na kundi la pili linatoa sababu yake kutoka kwenye Hadiyth ya kuyaosha. Kwa hakika manii ni najsi, na lazima yasafishwe kwa kuyaosha, kuyakwangua au kuyapangusa. (Tazama kitabu cha Niyl Al-Awtwaar cha Imaam Shawkaaniy).

[8] Abuu As-Samh jina lake halisi ni Iyyaad. Alikuwa ni mtumwa aliyeachwa huru na akawa mtumishi wa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) (وَسَلَّمَ). Ibn Abdil-Barr alisema aliripotiwa kwamba alipotea na hakuna anayejua alifia wapi au lini.

[9] Hii inamaanisha kuwa ipo tofauti baina ya mkojo wa msichana na mvulana. Katika wakati wa kunyonya, mkojo wa mvulana ni msafi zaidi kuliko mkojo wa msichana.

[10] ‘Asmaa ni Mama wa ‘Abdullaah bin Az-Zubayr na ni dada mkubwa wa ‘Aaishah. Alisilimu mapema sana kule Makkah na akahamia Madiynah. Alifariki chini ya mwezi mmoja baada ya kuuliwa mwanawe Ibn Az-Zubayr mnamo mwaka 73 A.H akiwa na umri wa miaka 100, nab ado hakung’oa jino hata moja wala kuharibika akili kwa uzee.

[11] Khawlah bint Yaasir alikuwa Swahaba, na Abu Salamah bin ‘Abdir-Rahmaan alisimulia Hadiyth hiyo kutoka kwake.

04:-Mlango Wa Wudhuu

بَابُ الْوُضُوءِ

04-Mlango Wa Wudhuu

29.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَوْلَا أَنْ أَشُقَّ عَلَى أُمَّتِي لِأَمْرَتِهِمْ بِالسَّوَاكِ مَعَ كُلِّ وُضُوءٍ } أَخْرَجَهُ مَالِكٌ، وَأَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Lau nisingeugopea uzito ummah wangu, ningeliwaamrisha mswaki[1] kabla ya kila Swalaah.” [Imetolewa na Maalik, Ahmad na An-Nasaaiy. Akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

30.

وَعَنْ حُمْرَانَ: { أَنَّ عُثْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ دَعَا بِوُضُوءٍ، فَغَسَلَ كَفَّيْهِ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، ثُمَّ مَضْمَضَ، وَاسْتَنْشَقَ، وَاسْتَنْثَرَ، ثُمَّ غَسَلَ وَجْهَهُ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، ثُمَّ غَسَلَ يَدَهُ الْيُمْنَى إِلَى الْمِرْفَقِ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، ثُمَّ الْيُسْرَى مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ مَسَحَ بِرَأْسِهِ،

ثُمَّ غَسَلَ رِجْلَهُ الْيُمْنَى إِلَى الْكَعْبَيْنِ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، ثُمَّ الْيُسْرَى
مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ قَالَ: رَأَيْتُمْ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ تَوَضَّأَ
نَحْوَ وُضُوءِي هَذَا { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Humraan[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) mtumwa aliyeachwa huru na ‘Uthmaan[3] amesema kuwa: “Uthmaan alitaka maji ya kutawadhia. Akaosha viganja vyake mara tatu, kisha akasukutua na akatia maji puani, na kisha akapenga. Kisha akaosha uso wake mara tatu. Kisha akaosha mkono wake wa kuume hadi kwenye kiwiko cha mkono wake (fundo kati ya kiganja na bega) mara tatu[4], kisha akauosha hivyo hivyo mkono wake wa kushoto. Kisha akapaka maji kichwa chake. Kisha akauosha mguu wake wa kuume hadi kwenye vifundi viwili mara tatu, kisha akauosha mguu wake wa kushoto hivyo hivyo. Kisha akasema: Nilimuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akitawadha mfano wa wudhuu wangu huu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

31.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي صِفَةِ وُضُوءِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { وَمَسَحَ بِرَأْسِهِ وَاحِدَةً. } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Aliy[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuhusu wasifu wa wudhuu wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuwa: “Nabiy alipangusa kichwa chake kwa maji mara moja tu[6].” [Imetolewa na Abuu Daawuud]

32.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدِ بْنِ عَاصِمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي صِفَةِ
الْوُضُوءِ قَالَ: { وَمَسَحَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِرَأْسِهِ، فَأَقْبَلَ
بِيَدَيْهِ وَأَذْبَرَ. } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي لَفْظٍ: { بَدَأَ بِمُقَدِّمِ رَأْسِهِ، حَتَّى ذَهَبَ بِهِمَا إِلَى قَفَاهُ، ثُمَّ
رَدَّهُمَا إِلَى الْمَكَانِ الَّذِي بَدَأَ مِنْهُ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [7] ‘Abdullaah bin Zayd bin ‘Aaswim
amesema akielezea sifa ya wudhuu: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipangusa kichwa chake kutoka katika paji la uso
mpaka kisogoni na kisha mpaka kwenye paji la uso[8].” [Al-
Bukhaariy, Muslim]

Na katika riwaayah nyengine ya Al-Bukhaariy na Muslim:
“Ameanza mwanzo wa kichwa chake kwa mikono yake hadi
akaipoleka kisogoni mwake, kisha akairudisha mahali alipoanza.”

33.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا فِي صِفَةِ الْوُضُوءِ
قَالَ: { ثُمَّ مَسَحَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِرَأْسِهِ، وَأَدْخَلَ
إِصْبَعَيْهِ السَّبَّاحَتَيْنِ فِي أُذُنَيْهِ، وَمَسَحَ بِإِبْهَامَيْهِ ظَاهِرَ أُذُنَيْهِ {
أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr[9] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuhusu sifa za wudhuu: “Kisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) alipangusa kichwa chake, akaingiza vidole vyake vya Shahaadah katika masikio yake, na akapangusa nje ya masikio yake kwa vidole gumba.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na ameisahihisha Ibn Khuzaymah]

34.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا اسْتَيْقَظَ أَحَدُكُمْ مِنْ مَنَامِهِ فَلْيَسْتَنْثِرْ ثَلَاثًا، فَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَبِيتُ عَلَى خَيْشُومِهِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakapoamka mmoja wenu usingizini, apenge pua mara tatu, kwani shaytwaan hulala kwenye mionzi ya pua[10] yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

35.

وَعَنْهُ: { إِذَا اسْتَيْقَظَ أَحَدُكُمْ مِنْ نَوْمِهِ فَلَا يَغْمِسُ يَدَهُ فِي الْإِنَاءِ حَتَّى يَغْسِلَهَا ثَلَاثًا فَإِنَّهُ لَا يَدْرِي أَيْنَ بَاتَتْ يَدُهُ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ. وَهَذَا لَفْظُ مُسْلِمٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: Rasuli wa Allah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Akiamka mmoja wenu usingizini, asizamishe mikono yake katika chombo chochote, hadi aioshe mara tatu[11], kwani hajui mkono wake ulilala wapi.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

36.

وَعَنْ لَقِيطِ بْنِ صَبْرَةَ، رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَسْبَغُ الْوُضُوءَ، وَخَلَّلُ بَيْنَ الْأَصَابِعِ، وَيَبْلُغُ فِي الْإِسْتِنْشَاقِ، إِلَّا أَنْ تَكُونَ صَائِمًا} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ
وَلِأَبِي دَاوُدَ فِي رِوَايَةٍ: {إِذَا تَوَضَّأْتَ فَمَضْمُضٌ}

Kutoka kwa Laqiytw bin Swabrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tawadha kikamilifu, na pitisha kati ya vidole vyako vya mikono na miguu[12], zidisha katika kuyapandisha maji puani isipokuwa utakapokuwa uko katika Swawm.” [Imetolewa na Al-Arba’ah; Abuu Daawuud, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy na Ibn Maajah na ameisahihisha Ibn Khuzaymah]

Na katika riwaayah ya Abuu Daawuud: “Ukitawadha, sukutua mdomo wako.”

37.

وَعَنْ عُثْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يُخَلِّلُ لِحَيْتَهُ فِي الْوُضُوءِ } أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Uthmaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akitawadha, alikuwa akipitisha vidole kati ya ndevu[13] zake.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na ameisahihisha Ibn Khuzaymah]

38.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَتَى بِثُلُثِي مُدٍّ، فَجَعَلَ يَذْكُ ذِرَاعَيْهِ } أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Zayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliletewa thuluthi mbili za Mudd[14] (kibaba cha maji), akawa anasugua mikono yake.” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

39.

وَعَنْهُ، { أَنَّهُ رَأَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَأْخُذُ لِأُذُنَيْهِ مَاءً غَيْرَ الَّذِي أَخَذَ لِرَأْسِهِ. } أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ

وَهُوَ عِنْدَ "مُسْلِمٍ" مِنْ هَذَا الْوَجْهِ بِلَفْظٍ: وَمَسَحَ بِرَأْسِهِ بِمَاءٍ
غَيْرِ فَضْلِ يَدَيْهِ، وَهُوَ الْمَحْفُوظُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Zayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Alimuona
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akichukua maji kupangusa
masikio, tofauti na maji aliyopangusia kichwa.” [Imetolewa na
Bayhaqqiy]

Na katika riwaayah ya Muslim: “Alipangusa kichwa chake kwa
kuchukua maji yasiyokuwa yaliyosalia kutoka katika maji ya
kuoshea mikono.” [Hadithi hii ni Mahfuwdh]

40.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "إِنَّ أُمَّتِي يَأْتُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
غُرًّا مُحَجَّلِينَ، مِنْ أَثَرِ الْوُضُوءِ، فَمَنْ اسْتَطَاعَ مِنْكُمْ أَنْ
يُطِيلَ غُرَّتَهُ فَلْيَفْعَلْ. } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Nilimsikia
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Ummah
wangu utakuja siku ya Qiyaamah na viungo vinavyong’aa (nyuso,
mikono, miguu) kwa sababu ya alama za wudhuu, basi mwenye
kuweza miongoni mwenu kuirefusha mng’aro wake[15], basi afanye
hivyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

41.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: { كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُعْجِبُهُ التَّيْمُنُ فِي تَنَعُّلِهِ، وَتَرَجُّلِهِ، وَطُهُورِهِ، وَفِي شَأْنِهِ كُلِّهِ. } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anapendezwa sana na kuanza na upande wa kuume katika kuvaa kwake viatu; na katika kuchana nywele, na katika kujitwaharisha kwake, na katika mambo yote[16].” [Al-Bukhaariy, Muslim]

42.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا تَوَضَّأْتُمْ فابدأوا بِمَيِّمِنِكُمْ } أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mnapotawadha, anzeni kulia kwenu.” [Imetolewa na Al-Arba’ah; Abuu Daawuwd, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy na Ibn Maajah na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

43.

وَعَنْ الْمُغِيرَةَ بْنِ شُعْبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ تَوَضَّأَ، فَمَسَحَ بِنَاصِيَّتِهِ، وَعَلَى الْعِمَامَةِ
وَالْخُفَّيْنِ { أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [17] Kutoka kwa Al-Mughiyrah bin Shu'bah
amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitawadha na
akawa ni mwenye kupangusa maji utosi wake na juu ya kilemba, na
juu ya soksi (khofu) mbili za ngozi[18].” [Imetolewa na Muslim]

44.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا فِي صِفَةِ حَجِّ النَّبِيِّ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { ابْدُؤُوا بِمَا
بَدَأَ اللَّهُ بِهِ { أَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ، هَكَذَا بِلَفْظِ الْأَمْرِ وَهُوَ عِنْدَ
مُسْلِمٍ بِلَفْظِ الْخَبَرِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) [19] Kutoka kwa Jaabir bin 'Abdillaah
amesema kuhusu Hijjah ya Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ):
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anzeni
kwa Alichianza nacho Allaah[20].” [Imetolewa na An-Nasaaiy kwa
tamshi hili la amri na imepokewa na Muslim kwa tamko la Al-
Khabar[21]]

45.

وَعَنْهُ قَالَ: { كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا تَوَضَّأَ أَدَارَ الْمَاءَ عَلَى مُرْفَقَيْهِ. } أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anapotawadha hutiririsha maji hadi kwenye kiwiko.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy kwa Isnaad dhaifu]

46.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا وُضُوءَ لِمَنْ لَمْ يَذْكُرِ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ } أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ، بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

وَلِلتِّرْمِذِيِّ: عَنْ سَعِيدِ بْنِ زَيْدٍ
وَأَبِي سَعِيدٍ نَحْوَهُ
قَالَ أَحْمَدُ: لَا يَثْبُتُ فِيهِ شَيْءٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna wudhuu kwa asiyetaja Jina la Allaah wakati wa kutawadha[22].” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuwd, na Ibn Maajah, kwa Isnaad dhaifu]

Na katika At-Tirmidhiy: “amepokea Hadiyth kama hiyo kutoka kwa Sa’iyd bin Zayd[23].”

Na Abuu Sa'iyd na Ahmad wamesema: “Hakujathibitika chochote ndani yake Hadiyth hiyo.”

47.

وَعَنْ طَلْحَةَ بْنِ مُصَرِّفٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: { رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَفْصِلُ بَيْنَ الْمَضْمَضَةِ وَالْإِسْتِنْشَاقِ. } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Twalhah bin Muswarraf[24] amemnuuu baba yake kwa upokezi wa babu yake[25] aliyesema: “Nimemuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akitenganisha kati ya kusukutua na kupandisha maji puani[26].” [Imetolewa na Abuu Daawuud kwa Isnaad dhaifu]

48.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي صِفَةِ الْوُضُوءِ { ثُمَّ تَمَضْمَضَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَاسْتَنْثَرَ ثَلَاثًا، يُمَضِّمُ وَيَنْثِرُ مِنَ الْكَفِّ الَّذِي يَأْخُذُ مِنْهُ الْمَاءُ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَالنَّسَائِيُّ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuhusu wasifu wa kutawadha, “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisukutua kisha akavuta maji puani na kupenga mara tatu. Alisukutua na akapenga pua yake kwa kiganja kilekile alichochukulia maji.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nassaiy]

49.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي صِفَةِ الْوُضُوءِ { ثُمَّ ادْخَلَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَدَهُ، فَمَضَمَضَ وَاسْتَنْشَقَ مِنْ كَفٍّ وَاحِدَةٍ، يَفْعَلُ ذَلِكَ ثَلَاثًا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Zayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuhusu wasifu wa kutawadha: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) alitumbukiza mkono wake (katika chombo), akasukutua na akapandisha maji puani kwa fumbo moja (maji). Alifanya hivyo mara tatu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

50.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { رَأَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَجُلًا، وَفِي قَدَمِهِ مِثْلُ الظُّفْرِ لَمْ يُصِبْهُ الْمَاءُ. فَقَالَ: "ارْجِعْ فَأَحْسِنْ وَضُوءَكَ" } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alimuona mtu katika unyayo wake kuna mfano wa kucha (baka) haikupata maji. Akamwambia: ‘Rejea vizuri wudhuu wako[27].’” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy]

51.

وَعَنْهُ قَالَ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَتَوَضَّأُ بِالْمُدِّ، وَيَغْتَسِلُ بِالصَّاعِ إِلَى خَمْسَةِ أَمْدَادٍ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitawadha kwa kibaba[28] kimoja cha maji, na akikoga kwa pishi[29] moja hadi vibaba (Mudd) vitano.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

52.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ يَتَوَضَّأُ، فَيُسْبِغُ الْوُضُوءَ، ثُمَّ يَقُولُ: أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، إِلَّا فُتِحَتْ لَهُ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ" { أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

وَالْتِّرْمِذِيُّ، وَزَادَ: { اَللّٰهُمَّ اجْعَلْنِي مِنَ التَّوَّابِينَ، وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ {

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna yeyote miongoni mwenu anayetawadha vizuri, kisha akasema: “Ash-hadu an laa ilaaha illa Allaah Wahdahu laa shariyka Lahu, wa ash-hadu anna Muhammad ‘Abduhuu wa Rasuwluhu” (Nashuhudia kuwa hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, Peke Yake, hana mshirika, na

ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja Wake na Rasuli Wake) ila atafunguliwa milango minane ya Jannah.” [Imetolewa na Muslim na At-Tirmidhiy]

At-Tirmidhiy aliongezea: “Allaahummaj-‘alniy minat-tawaabiyna Waj-‘alniy minal-mutatwahhiriyna (Ee Rabi! Nijaalie niwe miongoni mwa wenye kutubia na unijaalie niwe miongoni mwa wenye kujitwaharisha)”

[1] Hii inamaanisha kuwa matumizi ya mswaki kila mtu anapotawadha ni Sunnah, na Hadiyth hii iliyoripotiwa na Muslim inatuambia kwamba, ni sharti kutumia mswaki kabla ya kila Swalaah. Inamaanisha kuwa, haya tule anayekuenda kuswali na ‘udwuu ule ule aliotawadha safari iliyopita, hata hivyo sharti atumie mswaki. Ahadiyth hizi zinathibitisha mkazo mkubwa sana unaowekwa katika matumizi ya mswaki kila mara kwa ajili ya kusafisha meno. Hiyo ni Sunnah na siyo waajibu

[2] Humraan bin Aban alikamatwa na Khaalid bin Al-Waliyd katika vita wakati wa Ukhalifa wa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ), naye akampeleka akamtumikie ‘Uthmaan ambaye alimuacha huru. Ni mwaminifu wa daraja la pili katika kuripoti Hadiyth. Alifariki mwano mwaka wa 75 A.H.

[3] ‘Uthmaan ni Khalifa wa tatu kati ya wanne walio wakuu au walioongozwa. Alisilimu mapema na akamuoa Ruqayyah bint wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na baada ya kufariki kwake akaozwa bint mwingine wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), Ummu-Kulthum na hivyo anaitwa Dhun-Nurayn (yaani mwenye nuru mbili, maana yake mabinti wawili wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)). ‘Uthmaan aliuliwa shahidi siku ya Ijuma tarehe 18 Dhul-Hijjah mwaka 35 A.H.

[4] Katika Hadiyth hii, kuosha uso, mikono na miguu, imetajwa kuwa vioshwe mara tatu kila kiuongo, lakini viungo vingine, inatosha kuviosha mara mbili au hata mara moja kila kiungo. Imaam Nawawi ameandika

kuwa maafikiano ya pamoja ni kwamba kuosha mara moja ni faradhi yaani lazima.

[5] ‘Aliy ni Khalifa wa nne walioongozwa. Alipigana vita zote isipokuwa ya Tabuwk, kwa kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuacha akikaimu kule Madiynah. Mtu mmoja muovu aitwae ‘Abdur-Rahmaan bin Muljam, alimuua ‘Aliy akafa kama ni Shahidi asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 17 mwezi Ramadhwaan mwaka 40 A.H huko Kufa.

[6] Hii maana yake ni kwamba kupangusa maji kichwa wakati wa kutawadha mara moja tu ndiyo faradha.

[7] ‘Abdullaah bin Zayd alikuwa Answaar (watu wa Madiynah waliowapokea Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na wenziwe wa Makkah waliohajiri Madiynah), aliyetoka kwa akina Bani Maazin kutoka katika ukoo wa An-Najaar. Alipigana katika vita vya Uhud alimuua Musailimah Al-Kadhdhaab na pia alimuua Wahshi mnamo Siku ya Al-Yamama. Aliuwawa mnamo siku ya Al-Harraah mnamo mwaka 63 A.H.

[8] Hadiyth hii inatuambia kupangusa maji (mas-h) kichwani sharti kuanzie mbele.

[9] ‘Abdullaah bin ‘Amr mwana wa ‘Amr bin Al-‘Aasw Al-Qurayshiy. Yeye alisilimu kabla ya babake ambaye alikuwa mkubwa kuliko yeye kwa miaka 13. Alikuwa ni ‘Aalim (msomi), alihifadhi Hadiyth na alikuwa mwenye taqwa sana. Alifariki mnamo mwaka 63 au 70 A.H.

[10] Kwa shaytwaan kulala ndani ya pua za mtu kunawezekana, lakini hali halisi inayotokea inajulikana na Mwenyewe Allaah (عز وجل) na Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Huenda huo ni usemi wa kimethali, kwa sababu kamasi mbaya hukusanyika puani na kusababisha uzembe, uvivu, kusahau au kupuuza. Hali hizi zote ni za kishaytwaan.

[11] Hii inamaanisha kuwa, mikono isitumbukizwe katika chombo cha maji ya kutawadhia, kwa kuwa neno “kutawadha” limo katika Hadiyth

zilizoandikwa na Al-Bukhaariy. Ibn Hajar, katika kitabu chake cha Fat-h Al-Baariy amesema kuwa: “Ingawa Hadiyth hii inataja vyombo vya kutawadha, lakini inajumuisha vyombo vyote vingine pamoja na vyombo vya kuogea. Lakini kukiweko bwawa kubwa au tanki la maji, basi inaruhusiwa kutumbukiza mkono humo.”

[12] Hii inamaanisha kuwa vidole vya mikononi na miguuni sharti vioshwe taratibu na kikamilifu.

[13] Wakati wa tendo la kutawadha, kuchanua ndevu zako kwa vidole vyako ni Sunnah na siyo lazima (wajibu).

[14] Katika Hadiyth zingine, Mudd kamili ni zaidi kidogo ya gram 600. Hii ndio idadi ndogo kuliko idadi zote zilizotajwa kwa ajili ya kutawadha, vinginevyo itakuwa tabu kubwa kutawadha kwa maji kidogo zaidi ya hivi. Hakijatajwa kiwango cha juu cha maji. Kiasi chochote cha maji kinaweza kutumika kwa kutawadha na kuoga, lakini inakatazwa kufanya israfu ya maji.

[15] Hii inaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Inaweza kumaanisha kuosha viungo zaidi ya kiwango cha chini, kwa mfano, kuosha mikono hadi mabegani, na kuosha miguu hadi magotini. Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) anaiafiki hii maana ya pili. Pia inaweza kumaanisha kuosha kila kiungo mara tatu, badala ya kuosha viungo kama vile viganja, mdomo na pua kwa uchache mara moja. Pia inaweza kumaanisha kutawadha tena na tena, au hata kubaki na wudhuu huo huo mmoja saa zote.

[16] Mtindo huu (wakuanzia kiungo cha kuume) wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) ulikuwa ni kwa matendo mema. Lakini kwa matendo mengine kama kuenda nje ya Msikiti, au kuingia chooni, ambapo mtu ni sharti atangulize mguu wa kushoto kwanza.

[17] Al-Mughiyrah ndiye Abuu ‘Abdillaah au Abuu Lisa. Al-Mughiyrah bin Shu’bah bin Mas-‘uwd Ath-Thaqaaf alikuwa Swahaba maarufu. Alisilimu mnamo mwaka wa vita ya Khandaq (Handaki), na akahajiri.

Kwanza alishiriki katika vita ya Hdaybiyah. Alifariki mnamo mwaka 50 A.H. kule Kufa.

[18] Hadiyth hii inaweka wazi wazi kwamba, kupangusa maji kidogo juu ya kilemba (kofia) ni sahihi. Kuna aina mbili za tendo hili. Kwanza ni kupangusa kidogo juu ya kilemba na kidogo juu ya kichwa. Hakuna tofauti ya maoni juu ya tendo hili. Pili ni kupangusa juu ya kilemba peke yake. Kuna tofauti ya maoni kwa hili, lakini hii inathibitishwa pia na Hadiyth Swahiyh ya At-Tirmidhiy.

[19] Jaabir alikuwa Answaar aliyetoka katika ukoo wa Sulamiy, na alipewa jina la utani la Abuu ‘Abdillaah. Alikuwa mmoja wa Swahaba maarufu. Alipigana katika vita vya Badr, ingawa wengine wanasema kuwa hakuwahi kuishuhudia vita vya Badr wala ya Uhud, lakini alishiriki katika vita zilizofuata hizo. Pia alikuwako kule Siffin. Alikuwa mmoja wa watu waliohifadhi Hadiyth nyingi. Alipata upofu mnamo mwisho wa maisha yake, alifariki mnamo mwaka wa 74 A.H akiwa na umri wa miaka 94. Inasemekana kuwa yeye ndiye aliyekuwa Swahaba wa mwisho kufariki pale Madiynah.

[20] Qur-aan tukufu imetaja kwanza Asw-Swafaa katika kutaja Asw-Swafaa na Al-Marwaa. Nabiyy (ﷺ) alianza Saa’i (kutembea na kukimbia kati ya Asw-Swafaa na Al-Marwaa wakati wa kuhiji Hijjah kubwa (Hajj) na Hijjah ndogo (‘Umrah) kutokea upande wa Asw-Swafaa). Kwa hivyo anzeni kutawada kwa namna hiyo hiyo – kuanzia kuosha uso, kisha mikono mpaka katika kiwiko, kisha pangusa kichwa, na kisha osha miguu (kama alivyovifanya Nabiyy (ﷺ)).

[21] Katika Hadiyth hii limetumika neno “bada-a” katika maandishi ya Kiarabu, kwa maana ya kutoa taarifa (kwa mfano naanza kwa) na siyo kwa kuamrisha (anza kwa).

[22] Kuhusu kadhia hii, zipo Ahaadiyth zinazopingana ambazo zinaashiria maoni yanayopishana kuhusu kuitamka “BismiLlaah” kabla ya kuanza

kutawadha. Jibu sahihi la kadhia hii ni kusema kuwa, kutamka BismiLlaah ni Sunnah.

[23] Sa'iyd huyu ndiye Sa'iyd bin 'Amr Al-Qurayshiy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ), aliyepewa jina la utani la Abuu Al-A'war. Naye ni mmoja wa wale watu kumi waliyoahidiwa Al-Jannah. Alisilimu mapema sana, na akamuoa Faatwimah, dada wa 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ), na wote hawo (Faatwimah na Sa'iyd) walisababisha 'Umar kujaaliwa na Allaah (عز وجل) kusilimu. Alipigana vita vyote isipokuwa ya Badr, kwa sababu hakuwepo kwa kuwa alikuwa akiutafuta msafara. Alifariki mnamo mwaka 51 A.H na akazikwa Al-Baqi'.

[24] Huyu Twalhah ndiye Abuu Muhammad au Abuu 'Abdillaah Twalhah bin Muswarrif. Alikuwa Taabi' (mfuasi au mrithi ambaye alionana na au aliongozana na Swahaba wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)) mtegemewa sana wa daraja la tano. Alikuwa ni mwenye taqwah na msomaji wa Qur-aan. Alifariki mnamo mwaka wa 112 A.H. Baba yake Muswarrif, hajulikani na hilo limeifanya Hadiyth yake kuwa dhaifu.

[25] Babu wa Twalhah anaitwa Ka'b bin 'Amr au 'Amr bin Ka'b bin Juhdub Al-Yami anayetokana na kabila la Yemen linaloitwa Yam la Hamadan. Ibn 'Abdil-Bar alisema kuwa, yeye (Ka'b) alilowea kule Kufa, naye ni Swahaba.

[26] Hii inamaanisha kwamba, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitwaa maji kwa mikupuo mbalimbali kwa kuosha pua na kusukutua mdomo. Kwa mujibu wa mwandishi, Hadiyth hii ni dhaifu. Kwa mujibu wa Al-Bukhaariy na Muslim, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitumia mkono mmoja tu wa maji kwa kuosha pua na kusukutua mdomo. Imaam Nawawi ameelezea aina zake tano, na akasema hiyo iliyotajwa na Al-Bukhaariy na Muslim ndiyo Swahiyh.

[27] Hadiyth hii inaweka wazi msimamo kwamba, kuuosha mguu mzima kikamilifu ni tendo la lazima. Katika Hadiyth iliyorikodiwa na Muslim inasema kuwa, ni moto kuacha eneo la mguu likiwa kavu. Katika Hadiyth

hii kuna kukana kwa watu wanaosema kuwa kupangusa (mas-h) mguu pamoja na kuuosha vyote ni lazima; au watu wanaosema kuwa kupangusa na kuosha vyote vinaruhusiwa.

[28] Mudd moja ni sawa na takribani gram mia sita, na Sai' moja ni sawa na zaidi kidogo ya kilo mbili unusu, na hiki ndicho kiasi cha chini kabisa cha kutumia. Hii inamaanisha kuwa kila mtu awe muangalifu sana katika matumizi ya maji (bila israaf).

[29] Sai' moja ni sawa na mudd nne au gram 2660.

05-Mlango Wa Kupangusa Juu Ya Khuff Mbili (Soksi)

بَابُ الْمَسْحِ عَلَى الْخُفَّيْنِ

05-Mlango Wa Kupangusa Juu Ya Khuff Mbili (Soksi Za Ngozi)

Tanbihi: Soksi za aina yoyote zinafaa ikiwa za sufi, pamba au katani na mifano hivyo.

53.

عَنْ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كُنْتُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَتَوَضَّأَ، فَأَهْوَيْتُ لِأَنْزِعَ خُفَّيْهِ، فَقَالَ:

"دَعَهُمَا، فَإِنِّي أَدْخَلْتُهُمَا طَاهِرَتَيْنِ" فَمَسَحَ عَلَيْهِمَا { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِلْأَرْبَعَةِ عَنْهُ إِلَّا النَّسَائِيَّ: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَسَحَ أَعْلَى الْخُفِّ وَأَسْفَلَهُ } وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Mughiyra bin Shu'bah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Nilikuwa na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akatawadha, nikaharakia kumvua soksi zake. Akasema: "Ziache, kwani nilizivaa zikiwa twahaara[1]." Akapungusa juu yake." [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na kutoka kwa Al-Arba'ah isipokuwa An-Nasaaiy: "Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipangusa sehemu ya juu na chini ya soksi za ngozi." [Katika Isnaad yake kuna udhaifu].

54.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { لَوْ كَانَ الدِّينُ بِالرَّأْيِ لَكَانَ أَسْفَلُ الْخُفِّ أَوْلَى بِالْمَسْحِ مِنْ أَعْلَاهُ، وَقَدْ رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَمْسَحُ عَلَى ظَاهِرِ خُفِّهِ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa 'Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Lau Dini ingekuwa kwa rai[2], basi ingelikuwa kupangusa chini ya khuff ni bora zaidi kuliko juu yake. Na kwa yakini mimi nimemuona Rasuli wa Allaah

(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akipangusa juu ya khuff zake.”
[Imetolewa na Abuu Daawuud kwa Isnaad Hasan]

55.

وَعَنْ صَفْوَانَ بْنِ عَسَّالٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَأْمُرُنَا إِذَا كُنَّا سَفَرًا أَنْ لَا نَنْزِعَ
خِفَافَنَا ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ وَلَيَالِيَهُنَّ، إِلَّا مِنْ جَنَابَةٍ وَلَكِنْ مِنْ غَائِطٍ،
وَبَوْلٍ، وَنَوْمٍ} أَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَابْنُ
خُزَيْمَةَ وَصَحَّاحُهُ

Kutoka kwa Swafwaan bin ‘Assaal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa
akituamrisha pindi tukiwia safarini, tusivue khuff zetu siku tatu
mfululizo mchana na usiku wak[3]e isipokuwa tukiwa katika janaba,
lakini kwa haja kubwa, mkojo na usingizi (tulikuwa hatuvui).”
[Imetolewa na An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy, na tamshi hili ni lake, na
akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

56.

وَعَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {جَعَلَ النَّبِيُّ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ وَلَيَالِيَهُنَّ لِلْمُسَافِرِ، وَيَوْمًا
وَلَيْلَةً لِلْمُقِيمِ. يَعْنِي: فِي الْمَسْحِ عَلَى الْخُفَّيْنِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alifanya kuwa siku tatu; mchana na usiku wake kwa msafiri, na siku moja; mchana na usiku wake kwa mkaazi yaani katika kufuta juu ya khuff.” [Imetolewa na Muslim]

57.

وَعَنْ ثَوْبَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {بَعَثَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَرِيَّةً، فَأَمَرَهُمْ أَنْ يَمْسَحُوا عَلَى الْعَصَائِبِ يَغْنِي: الْعَمَائِمَ وَالتَّسَاخِينَ يَغْنِي: الْخِفَافَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Thawbaan[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituma kikosi cha jeshi na akawaamrisha wapanguse juu ya vilemba[5] na khuff.” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud, na akaisahihisha Al-Haakim]

58.

وَعَنْ عُمَرَ مَوْقُوفًا وَعَنْ أَنَسٍ مَرْفُوعًا: {إِذَا تَوَضَّأَ أَحَدُكُمْ وَلَبَسَ خُفَّيْهِ فَلْيَمْسَحْ عَلَيْهِمَا، وَلْيُصَلِّ فِيهِمَا، وَلَا يَخْلَعْهُمَا إِنْ شَاءَ إِلَّا مِنْ جَنَابَةٍ} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَالْحَاكِمُ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) katika Hadiyth Mawquwfaa na kutoka kwa Anas katika Hadiyth Marfuw’aa kuwa: “Pindi mmoja

wenu akitawadha na akavaa khuff zake mbili, afanye mas-h (kupangusa kwa maji) juu yake na aswali nazo, na asizivue akipenda[6], isipokuwa kwa janaba.” [Imetolewa na Ad-Daarqutwniy na Al-Haakim, na akaisahihisha Al-Haakim]

59.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَنَّهُ رَخَّصَ لِلْمُسَافِرِ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ وَلَيَالِيَهُنَّ، وَلِلْمُقِيمِ يَوْمًا وَلَيْلَةً، إِذَا تَطَهَّرَ فَلَيْسَ خُفَّيْهِ: أَنْ يَمْسَحَ عَلَيْهِمَا} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Abuu Bakrah[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameruhusu msafiri kupangusa juu ya khuff siku tatu na usiku wake, na kwa mkaazi siku moja; mchana na usiku wake, atakapochukua wudhuu akavaa khuff zake mbili.” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

60.

وَعَنْ أَبِي بَنْ عِمَارَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ قَالَ: {يَا رَسُولَ اللَّهِ أَمْسَحُ عَلَى الْخُفَّيْنِ؟ قَالَ: "نَعَمْ" قَالَ: يَوْمًا؟ قَالَ: "نَعَمْ"، قَالَ: وَيَوْمَيْنِ؟ قَالَ: "نَعَمْ"، قَالَ: وَثَلَاثَةً؟ قَالَ: "نَعَمْ، وَمَا شِئْتَ" أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَقَالَ: لَيْسَ بِالْقَوِيِّ

Kutoka kwa Ubayy bin ‘Imaarah[8] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Ee Rasuli wa Allaah! Je, naweza kupangusa juu ya khuff mbili?” Akasema: “Ndiyo.” Akauliza tena: “Siku moja?” Akasema: “Ndiyo.” Akauliza tena: “Siku mbili je?” Akasema: “Ndiyo.” Akauliza tena: “Na siku tatu?: Akasema: “Ndiyo, na utakavyo[9].” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na akasema: “Hadiyth haina nguvu[10].”]

[1] Kupangusa (Mas-h) juu ya soksi kuna masharti. Hizo soksi lazima uwe ulizivaa ukiwa twahara. Ikiwa ulivaa soksi hizo hauko tohara, basi kupangusa juu yake hakuruhusiwi.

[2] Hadiyth hii inamaanisha kuwa amri za kidini (katika Uislaam) za maamrisho na makatazo hutegemea Wahyi. Mtu huwezi kukubali au kukataa amri kwa sababu ya kuzielewa au kutozielewa. Lakini hii haimaanishi kuwa maamrisho au makatazo hayo ya kidini huenda kinyume na akili na busara. Pia inathibitisha kuwa, pakiwepo Hadiyth Swahiyh, kutoa uamuzi kinyume na Hadiyth hiyo hairuhusiwi. Hili limebainishwa na Shariy’ah ya Kiislaam.

[3] Hadiyth hii inamaanisha kuwa, kupangusa (Mas-h) kunaruhusiwa kwa msafiri mpaka siku tatu, na kwa mkazi wa pale mpaka saa thelathini na nne. Kipindi cha Mas-h huhesabika tangu wudhuu unapobatilika na siyo tangu kuzivaa soksi. Njia ya kupangusa (Mas-h) ni kulowanisha mikono kwa maji, na kuanzia kwenye vidole kuupandisha mpaka chini ya magoti. Baada ya wakati unaoruhusiwa kwisha au ukijamba, ukikojoa, n.k., mas-h hubatilika. Na pia inabatilika kwa mambo yote yanayobatilisha wudhuu.

[4] Huyu Thawbaan ni Thawbaan bin Bujdud bin Jahdar, ambaye alipewa jina la utani la Abuu ‘Abdillaah. Alikuwa mkazi wa As-Surat, ambapo ni mahali kati ya Makkah na Al-Madiynah. Ilisemekana pia kuwa yeye alitoka Himyaar. Aliishi na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) maisha yake yote, baadaye akalowea Sham, na baadaye akahamia Hims alikofia mnamo mwaka 54 A.H.

[5] Katika maandishi ya Kiarabu neno ‘Aswaa-ib maana yake ni bendeji inayotumiwa kufungia vidonda, au ukivunjika mguu au mkono, kufungia juu ya vipande vya mbao viwekwavyo kuuzunguka mfupa uliovunjika.

[6] “Akipenda” maana yake iwapo bado yumo katika wakati ulioruhusiwa kupangusa (Mas-h). Lakini mara wakati huo unapokwisha, lazima azivue soksi zake, akatawadhe upya pamoja na kuosha miguu yake, ndipo azivae tena hizo soksi zake, na kipindi cha kupangusa (Mas-h) kianze upya.

[7] Huyu Abuu Bakrah ndiye Nufai bin Al-Haarith au bin Al-Masruwh. Alishuka kutoka katika ngome ya Twaaiif pamoja na kundi la watumwa na akasilimu, ndipo Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuacha huru. Alikuwa mmoja wa Swahaba wenye taqwa na akafia Basra manmo mwaka 51 au 52 A.H.

[8] Ubay bin ‘Imaarah alikuwa Swahaba wa Kianswaar (wa kutoka Al-Madiynah). Alilowea Misr. Ibn Hibbaan alisema: “Aliswali kwa Qiblah mbili, lakini sichukulii ripoti yake kuwa ni mlolongo kamili wa wapokezi.”

[9] Isnaad ya Hadiyth hii si Swahiyh. Hadiyth ile inayotaja siku moja (saa 24) kwa mkazi, na siku tatu kwa msafiri ni Swahiyh.

[10] Hadiyth hii haikuchukuliwa kama ni ushahidi kwa udhaifu wake na kwa kuipinga Hadiyth Hasan na Swahiyh ambayo imetaja vipindi. An-Nawawi ametaja katika Sharh Al-Muhadhdhab kwamba, Imaam wamekubaliana juu ya udhaifu wa Hadiyth hii, na Ahmad alisema: “Wapokezi wake hawajulikani.”

06-Mlango Wa Kubatilika Wudhuu

بَابُ نَوَاقِضِ الْوُضُوءِ

06-Mlango Wa Kubatilika[1] Wudhuu

61.

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ أَصْحَابُ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى عَهْدِهِ يَنْتَظِرُونَ الْعِشَاءَ حَتَّى تَخْفِقَ رُؤُوسُهُمْ، ثُمَّ يُصَلُّونَ وَلَا يَتَوَضَّئُونَ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَأَصْلُهُ فِي مُسْلِمٍ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Maswahaba wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), katika zama zake (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) walikuwa wakingojea Swalaah ya ‘Ishaa hadi wanainamisha chini vichwa vyao (kwa kusinzia)[2], kisha wanaswali bila kutawadha upya[3].” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Ad-Daaruqutwniy]

[Chanzo chake ni Hadiyth ya Muslim]

62.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {جَاءَتْ فَاطِمَةُ بِنْتُ أَبِي حُبَيْشٍ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي امْرَأَةٌ أُسْتَحَاضُ فَلَا أَطْهَرُ، أَفَادَعُ الصَّلَاةَ؟ قَالَ: "لَا.

إِنَّمَا ذَلِكَ عِرْقٌ، وَلَيْسَ بِحَيْضٍ، فَإِذَا أَقْبَلْتَ حَيْضَتَكَ فَدَعِي
الصَّلَاةَ، وَإِذَا أَذْبَرْتَ فَاغْسِلِي عَنْكَ الدَّمَ، ثُمَّ صَلِّي { مُتَّفَقٌ
عَلَيْهِ

وَلِلْبُخَارِيِّ: { ثُمَّ تَوَضَّئِي لِكُلِّ صَلَاةٍ }
وَأَشَارَ مُسْلِمٌ إِلَى أَنَّهُ حَذَفَهَا عَمْدًا

Kutokwa kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: Faatwimah bint Abiy Hubaysh[4] alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akauliza: “Ee Rasuli wa Allaah! Mimi ni mwanamke nakuwa na istihaadhwah (damu[5] ya haikatiki hata baada ya muda wa hedhi kumalizika) hivyo huwa sitohariki, je, niache kuswali?” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Hapana kwani huo ni mshipa wa damu, wala si hedhi, hivyo, ukiingia katika hedhi, sitisha kuswali, na hedhi ikiisha, osha damu huko iliko, kisha uswali.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Al-Bukhaariy ameongezea: “Kisha tawadha kwa kila Swalaah[6].”

Na Muslim alitaja kuwa ameiondoa nyongeza hii kwa maksudi.

63.

وَعَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { كُنْتُ رَجُلًا
مَذَّاءً، فَأَمَرْتُ الْمِقْدَادَ بْنَ الْأَسْوَدِ أَنْ يَسْأَلَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَسَأَلَهُ فَقَالَ: "فِيهِ الْوُضُوءُ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ
لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa ‘Aliy bin Abuu Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilikuwa mtu wa kutokwa na madhiy[7] (majimaji yatokayo katika dhakari), nikamuamrisha Miqdaad bin Al-Aswad[8] amuulize Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), akamuuliza.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Anapaswa atawadhe.” [Al-Bukhaariy, Muslim]
[Na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

64.

وَعَنْ عَائِشَةَ، رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَبْلَ بَعْضِ نِسَائِهِ، ثُمَّ خَرَجَ إِلَى الصَّلَاةِ وَلَمْ يَتَوَضَّأْ } أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَضَعَفَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimbusu[9] mmoja wa wake zake, na akaenda kuswali bila kutawadha upya.” [Imetolewa na Ahmad, na akaidhoofisha Al-Bukhaariy]

65.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا وَجَدَ أَحَدُكُمْ فِي بَطْنِهِ شَيْئًا، فَأَشْكَلَ عَلَيْهِ: أَخْرَجَ مِنْهُ شَيْءٌ، أَمْ لَا؟ } فَلَا يَخْرُجَنَّ مِنَ الْمَسْجِدِ حَتَّى يَسْمَعَ صَوْتًا، أَوْ يَجِدَ رِيحًا } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akipata kinachomtia shaka katika tumbo lake kuwa anatokwa kitu au la, basi asitoke Msikitini hadi amesikia sauti yake au ahisi harufu[10] yake.” [Imetolewa na Muslim]

66.

وَعَنْ طَلْقِ بْنِ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {قَالَ رَجُلٌ: مَسَسْتُ ذَكَرِي أَوْ قَالَ الرَّجُلُ يَمَسُّ ذَكَرَهُ فِي الصَّلَاةِ، أَعَلَيْهِ وَضُوءٌ؟ فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "لَا، إِنَّمَا هُوَ بَضْعَةٌ مِنْكَ"} أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَقَالَ ابْنُ الْمَدِينِيِّ: هُوَ أَحْسَنُ مِنْ حَدِيثِ بُسْرَةَ.

Kutoka kwa Twalq bin ‘Aliy[11] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mtu mmoja alisema: “Nimeigusa dhakari yangu” au aliuliza: “Mtu aliyegusa dhakari yake wakati wa Swalaah, Je ni lazima kutawadha?” Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Hapana, hiyo ni sehemu ya mwili wako.” [Imetolewa na Al-Khamsah: Ahmad, Abuu Daawud, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy na Ibn Maajah na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

[Na Ibn Al-Madiyniyy amesema: “Hii ni bora kuliko Hadiyth ya Busrah.”]

67.

وَعَنْ بُسْرَةَ بِنْتِ صَفْوَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: "مَنْ مَسَّ ذَكَرَهُ فَلْيَتَوَضَّأْ" } أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ وَقَالَ الْبُخَارِيُّ: هُوَ أَصَحُّ شَيْءٍ فِي هَذَا الْبَابِ.

Kutoka kwa Busrah bint Swafwaan[12] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah amesema: “Atakayegusa dhakari[13] yake basi na atawadhe.” [Imetolewa na Al-Khamsah, na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

[Na Al-Bukhaariy amesema: “Hadiyth hii ni sahihi zaidi kuliko zote katika mlango huu.”]

68.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { مَنْ أَصَابَهُ قِيءٌ أَوْ رُعَافٌ، أَوْ قَلَسٌ، أَوْ مَذْيٌ فَلْيَنْصَرِفْ فَلْيَتَوَضَّأْ، ثُمَّ لِيَبْنِ عَلَى صَلَاتِهِ، وَهُوَ فِي ذَلِكَ لَا يَتَكَلَّمُ } أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَهَ وَضَعَّفَهُ أَحْمَدُ وَغَيْرُهُ.

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Yeyote atakayetapika au kutokwa na damu puani[14] kutokwa na madhiy,

atoke atawadhe kisha aendelee na Swalaah yake[15] (kwa kuendelea kutokea pale alipoiachia hiyo Swalaah), kwa sharti kwamba asizungumze katika wakati wa harakati hiyo.” [Imetolewa na Ibn Maajah]

Na akaidhoofisha Ahmad na wengine.

69.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّ رَجُلًا سَأَلَ
النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَتَوْضَأُ مِنْ لُحُومِ الْغَنَمِ؟ قَالَ: إِنْ
شِئْتَ قَالَ: أَتَوْضَأُ مِنْ لُحُومِ الْإِبِلِ؟ قَالَ: نَعَمْ} أَخْرَجَهُ
مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin Samurah[16] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) anasema kuwa: “Mtu mmoja alimuuliza Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Je! Nitawadhe kwa kula nyama ya kondoo?” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Ukipenda.” Akauliza: “Je nitawadhe kwa kula nyama ya ngamia[17]?” Akasema: “Ndiyo.” [Imetolewa na Muslim]

70.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ غَسَلَ مَيْتًا فَلْيَغْتَسِلْ، وَمَنْ حَمَلَهُ فَلْيَتَوَضَّأْ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ وَقَالَ أَحْمَدُ: لَا يَصِحُّ فِي هَذَا الْبَابِ شَيْءٌ.

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Aliyemuosha maiti[18] na aoge na aliyembeba atawadhe.” [Imetolewa na Ahmad na An-Nassaiy, na ameifanya ‘Hasan’ At-Tirmidhiy]

[Na Ahmad amesema: “Hakuna Hadiyah yoyote iliyosihi katika mlango huu]

71.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي بَكْرٍ رَحِمَهُ اللَّهُ، {أَنَّ فِي الْكِتَابِ الَّذِي كَتَبَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِعَمْرِو بْنِ حَزْمٍ: أَنْ لَا يَمَسَّ الْقُرْآنَ إِلَّا طَاهِرٌ} رَوَاهُ مَالِكٌ مُرْسَلًا، وَوَصَلَهُ النَّسَائِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَهُوَ مَعْلُولٌ.

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Abiy Bakr[19] (رَحِمَهُ اللَّهُ) amesema kuwa: Katika barua ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliyomwandikia “Amr bin Hazm[20]: “Asiiguse Qur-aan[21] isipokuwa aliyekuwa kwenye twahaarah.” [Imetolewa na Maalik Mursalaa, na Mawswul (wameiunganisha) An-Nasaa'iy na Ibn Hibbaan, nayo ina dosari]

72.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُذَكِّرُ اللَّهَ عَلَى كُلِّ أَحْيَانِهِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ، وَعَلَّقَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akimdhukuru Allaah nyakati zake[22] zote.” [Imetolewa na Muslim, na Al-Bukhaariy akaipa daraja la Mu’alaq]

73.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ احْتَجَمَ وَصَلَّى، وَلَمْ يَتَوَضَّأْ} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَلَيْتَهُ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alifanya hijaamah[23] (kumikwa au kupigwa chuku) akaswali wala hakutawadha.” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy, aliyeipa daraja la Dhaifu]

وَعَنْ مُعَاوِيَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْعَيْنُ وَكَأُ السَّهْ، فَإِذَا نَامَتْ الْعَيْنَانِ اسْتَطْلَقَ الْوِكَاءُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالطَّبْرَانِيُّ وَزَادَ {وَمَنْ نَامَ فَلْيَتَوَضَّأْ}

وَهَذِهِ الزِّيَادَةُ فِي هَذَا الْحَدِيثِ عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ مِنْ حَدِيثِ عَلِيٍّ دُونَ قَوْلِهِ: {اسْتَطْلَقَ الْوِكَاءُ} وَفِي كِلَا الْإِسْنَادَيْنِ ضَعْفٌ وَلِأَبِي دَاوُدَ أَيْضًا، عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ مَرْفُوعًا: {إِنَّمَا الْوُضُوءُ عَلَى مَنْ نَامَ مُضْطَجِعًا} وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ أَيْضًا

Kutoka kwa Mu'aawiyah[24] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Jicho lililo macho ni kamba na kizuizi cha kutoka upepo, na macho yote mawili yakilala, hiyo kamba hufunguka (na upepo hutoka bila hisia[25])." [Imetolewa na Ahmad na Atw-Twabaraaniy]

Na Atw-Twabaraaniy aliongezea: "Kila aliyelala atawadhe upya."

Pia imetolewa na Abuu Daawuwd kwa Hadiyth ya 'Aliy bila maneno: "Kamba hufunguka" [Isnaad zote mbili ni dhaifu]

Na kutoka kwa Abuu Daawuwd vile vile kutoka kwa Ibn 'Abbaas ikiwa ni Hadiyth Marfuw'aa: "Hakika wudhuu ungalipo kwa aliyelala kwa makalio yake." [Katika Isnaad yake kuna udhaifu pia]

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {يَأْتِي أَحَدَكُمْ الشَّيْطَانُ فِي صَلَاتِهِ، فَيَنْفُخُ فِي مَقْعَدَتِهِ فَيُخَيِّلُ إِلَيْهِ أَنَّهُ أَحَدَثَ، وَلَمْ يُحْدِثْ، فَإِذَا وَجَدَ ذَلِكَ فَلَا يَنْصَرِفُ حَتَّى يَسْمَعَ صَوْتًا أَوْ يَجِدَ رِيحًا} أَخْرَجَهُ الْبَزَّازُ

وَأَصْلُهُ فِي الصَّحِيحَيْنِ مِنْ حَدِيثِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدٍ وَلِمُسْلِمٍ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ نَحْوَهُ.

وَالْحَاكِمُ. عَنْ أَبِي سَعِيدٍ مَرْفُوعًا: {إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمْ الشَّيْطَانُ، فَقَالَ: إِنَّكَ أَحَدَثْتَ، فَلْيَقُلْ: كَذَبْتَ}

وَأَخْرَجَهُ ابْنُ حِبَّانَ بَلْفَظٍ: {فَلْيَقُلْ فِي نَفْسِهِ}

Kutokwa kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesimulia kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Shaytwaan huja kwa mmoja wenu ndani ya Swalaah, na humpulizia upepo makalioni mwake naye hudhani amepata hadath nae hajapata hadath. Hivyo, akihisi hivyo asiondoke hadi asikie sauti au ahisi harufu[26].” [Imetolewa na Al Bazaar]

[Asili yake ni katika Swahiyh mbili, Al-Bukhaariy na Muslim kuwa ilisimuliwa na ‘Abdullaah bin Zayd]

[Na Muslim amepokea Hadiyth ya Abuu Hurayrah vivyo hivyo]

Na Al-Haakim amemnukuu Abuu Sa’iyd katika Hadiyth Marfuw’aa (yenye upokezi wa wazi): “Endapo shaytwaan atamjia mmoja wenu

na kumwambia: “Wewe umetengua wudhuu wako kwa kutoa upepo”, basi aseme: “Umesema uongo.”” [Imetolewa na Al-Haakim]

Na Ibn Hibbaan pia amepokea Hadiyth hiyo pamoja na tamshi: “Na aseme moyoni mwake.”

[1] Mazingira yote yanayobatilisha wudhuu na kutawadha kwa maji, pia hubatilisha wudhuu wa kutayammam (kutawadha kwa udongo safi itokeapo maji hakuna).

[2] Hii inathibitisha kwamba, kusingia hakubatilishi au hakutangui wudhuu.

[3] Hili suala la iwapo usingizi unabatilisha wudhuu au laa, lina utata sana. Katika kadhia hii, maamuzi ya mwisho ni kuwa, endapo usingizi utakuwa ule mzito, basi wudhuu unabatilika, vinginevyo hautenguki.

[4] Faatwimah bint Abiy Hubaysh ni Swahabiyyah kutoka Quraysh na tena Asad. Babake ni Qays bin ‘Abdil-Mutwalib bin Asad bin ‘Abdil-‘Uzza bin Quswayy. Alikuwa Muhajira (mhamiaji kutoka Makkah) maarufu, na aliolewa na ‘Abdullaah bin Jahsh.

[5] Damu za mwanamke ziko za namna tatu:

a) Hedhi ni damu ya kila mwezi mmoja wa hedhi, ambayo huanza mwanamke akiwa baleghe. Damu ya aina hii husimama wakati mwanamke yu mjamzito.

b) Nifaas, yaani damu ya mwanamke imtokayo akisha kuzaa, ambayo haidumu zaidi ya siku 40.

c) Istihaadhwah, yaani damu inayoweza kutoka kwa sababu zisizokuwa hizo mbili. Hapa inamaanisha inayotajwa mwishoni.

[6] Hii inamaanisha kuwa, damu ya Istihaadhwah hubatilisha wudhuu, ndiyo maana Nabiyy (ﷺ) akaamuru kutawadha upya kabla ya kila Swalaah.

[7] Madhiy ni majimaji meupe kama mafuta ambayo hutoka bila kuzuilika wakati mtu ana ashki ya jimai. Ute huu hubatilisha wudhuu, lakini hauhitaji kuoga rasmi.

[8] Miqdaad bin ‘Amr bin Tha’labah Al-Bahraan alipewa jina la utani la Abul-Aswad au Abuu ‘Amr, na anajulikana kwa jina la Al-Miqdaad bin Al-Aswad. Al-Aswad bin Yaghuwth Az-Zuhr alimlea na wakafanya mkataba wa kujihami na Miqdaad zama za ujaahiliyyah (kabla ya ujio wa Uislaam). Alikuwa ni mmoja wa Swahaba wenye taqwah, wenye busara, na maarufu. Alikuwa wa sita kusilimu, alihama hijrah zote mbili, na alishiriki vita zote kuu. Alikuwa mpanda farasi katika vita vya Badr, na alishiriki katika kuiteka Misri. Alifariki akiwa na miaka 70 mnamo mwaka 33 A.H kule Al-Jawf, maili tatu kutoka Al-Madiynah. Kwa hivyo mwili wake ulipelekwa Al-Madiynah. ‘Uthmaan akasalisha Swalaah yake ya Janaazah, na kuzikwa Al-Baqi’.

[9] Hadiyth hii inathibitisha kwamba, wudhuu haubatiliki kwa kumgusa mwanamke, ukimtamani au usimtamani. Hii inaungwa mkono na ripoti ya Al-Bukhaariy iliyosimuliwa na ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) kuwa Rasuli wa Allaah (ﷺ) “Alikuwa akisali gizani, nami nilikuwa nimepumzika wakati miguu yangu ilining’inia hadi kule ambako Nabiyy (ﷺ) alikokuwa akisujudia juu ya msala wake. Kila anaposujudu alikuwa akigusa miguu yangu, nami nikawa naiondosha.”

[10] Hadiyth hii inataja msingi wa maana kwamba kila kitu hubaki katika amri ya awali, mpaka kitokee kitu dhahiri dhidi yake. Dhana peke yake si ya kuzingatia ukiwa umo ndani ya Swalaah au laa.

[11] Huyu Twalq ni Abuu ‘Aliy Twalq bin ‘Amr Al-Hanaf As-Siheim Al-Yamaam. Alimzuru Nabiyy (ﷺ) mara alipofika Al-

Madiynah, na akafanya naye kazi katika kuujenga Msikiti wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[12] Busrah bint Swafwaan bin Naefal bin Asad bin ‘Abdil-‘Uzza Al-Quraishiyyah Al-Asadiyyah alikuwa ni Swahaba miongoni mwa Waislaam wa kwanza, alihajiri (alihama) mapema, na akaishi hadi katika Ukhalifa wa Mu’aawiyah.

[13] Hadiyth hiyo hapo juu ya Twalq bin ‘Aliy inaelekea inapingana na hii, lakini sivyo hivyo. Kama kiungo hicho kitaguswa bila kufunikwa nguo au kwa nia ya matamanio hapo wudhuu utakuwa umebatilika; vinginevyo haubatiliki.

[14] Hadiyth hii ni dhaifu, na hakuna Hadiyth Swahiyh juu ya kadhia hii.

[15] Hii inamaanisha kwamba, iwapo mtu alishaswali rakaa mbili na Imaam, na ikatokezea kwamba wudhuu wake umebatilika, ataicha Swalaah, na baada ya kutawadha upya, ajiunge na jamaa katika sehemu ile ile alipoachia, kisha amalizie Swalaah na Imaam.

[16] Jaabir ni Swahaba maarufu na ni mtoto wa dada wa Sa’d bin Abiy Waqqaas. Aliloweza Kufa akajenga nyumba kule. Alifariki mnamo mwaka 66 au 74 A.H. Baba yake Samurah bin Junada As-Sawai Al-‘Aamir naye pia ni Swahaba.

[17] Watu wengine wanasema hii inamaanisha kutawadha kamili na wengine wanasema kusukutua mdomo tu. Fikra hii ya mwisho ni sahihi, kwa kuwa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitaja sababu ya amri hii kuwa ni mafuta, na mafuta huganda mdomoni tu.

[18] Kuhusu kadhia hii, hakuna Hadiyth Swahiyh. Wengine wanasema kuwa kuoga ni lazima kwa yule anayeogesha maiti, wengine wanasema ni vizuri, na wengine wanasema kutawadha ni lazima, na wengine wanasema hata hii siyo lazima.

[19] Huyu ni ‘Abdullaah bin Abiy Bakr bin ‘Amr bin Hazm Al-Answaar Al-Madani Al-Qadi. Taabi’ wa daraja la 5. Alifariki mnamo mwaka 135 A.H akiwa na miaka 70.

[20] Huyu ‘Amr bin Hazm ni Mkhazraj, Mnajaar aliyepewa jina la utani la Abuu Ad-Dhwahhaak. Alishiriki kwanza katika vita ya Khandaq, na Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma Najran kuwafundisha watu dini na kukusanya swadaqah. Aliwaandikia kitabu chenye matendo ya lazima na ya hiari, swadaqah na hiki ndicho kitabu kilichotajwa katika Hadiyth hii. Alifariki Madiynah akiwa na miaka hamsini na kitu.

[21] Hadath Akbar: (hadathi au najisi kubwa, yaani majimaji ya kijinsia yanayotoka kwenye sehemu za siri), na Hadath Aswghar: (Hadathi ndogo kutoa upepo, mkojo au kinyesi), vyote hivi vinahitaji kutawadha. Lakini ikiwa hiyo Hadath inatokana na kujamiiiana, basi imeafikiwa na wote kuwa huna ruhusa kuigusa Qur-aan, lakini kuna maoni tofauti kuhusu kufanya hivyo bila kutawadha.

[22] Nyakati za kuenda haja kubwa, kukojoa na za kujamiiiana, hazimo. Katika kunajisika kwa kujamiiiana, dhikr au kutamka jina la Allaah kunaruhusiwa, lakini kuigusa au kuisoma Qur-aan hakuruhusiwi.

[23] Hadiyth hii inaweka wazi kwamba, kutokwa na damu nje ya sehemu mbili kama katika hali hii ya kufanyiwa hijaamah (ukeni na sehemu ya kutolea kinyesi) hakubatilishi wudhuu. Hadiyth za daraja hilo zimesimuliwa pia na Ibn ‘Umar Ibn ‘Abbaas na Abuu Aufa (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ).

[24] Mu’aawiyah huyu pamoja na babake, Abuu Sufyaan Sakhr bin Harb, walisilimu ilipotekwa Makkah. ‘Umar alimteuwa akawa Gavana wa Shaam, baada ya kifo cha kaka yake Yaziyd bin Abuu Sufyaan na alibakia hivyo hadi ‘Aliy alivyojitokeza ili apate kumuondosha kwa nguvu, na akaapishwa kuwa Khalifa wakati wa Al-Hasan alipojiuzulu kwa kumuachia yeye cheo mnamo mwaka wa 40 H. Alifariki mnamo mwezi wa Rajabu mwaka 60 A.H akiwa na miaka 78.

[25] Hii inamaanisha kuwa usingizi ni chanzo cha hadathi (uchafu), lakini siyo uchafu wenyewe.

[26] Hii maana yake ni kwamba, kulala na sambamba na kilalio hupelekea kubatilika kwa wudhuu, ambapo kwenye Hadiyth ya juu inaelezea kuwa usingizi peke yake wowote unabatilisha wudhuu. Kulala sambamba na kilalio ni ishara ya kulala usingizi mzito, wakati viungo vyote vya mwili vinapumzika na kunawezesha upepo kutoka bila kizuizi, ambapo katika usingizi mwepesi au kusinzia, mtu huwa hajapoteza fahamu zote.

07-Mlango Wa Kwenda Kujisaidia Haja Msalani

بَابُ قَضَاءِ الْحَاجَةِ

07-Mlango Wa Kwenda Kujisaidia Haja Msalani

76.

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا دَخَلَ الْخَلَاءَ وَضَعَ خَاتَمَهُ} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، وَهُوَ مَغْلُولٌ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anaivua pete[1]

yake akiingia msalani.” [Imetolewa na Al-Arba’ah: Abuu Daawuwd, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy na Ibn Maajah na ina dosari]

77.

وَعَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا دَخَلَ الْخَلَاءَ قَالَ: "اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْخُبْثِ وَالْخَبَائِثِ"}
أَخْرَجَهُ السَّبْعَةُ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiingia msalani anasema[2]:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْخُبْثِ وَالْخَبَائِثِ

“Allaahumma inniy a’uwdhu ‘Bika minal khubuthi wal khabaaith.”
(Ee Allaah, najikinga Kwako dhidi ya mashaytwani ya kiume na ya kike).” [Imetolewa na As-Sab’ah (Maimamu Saba Wa Hadiyth: Al-Bukhaariy, Muslim, Abuu Daawuwd, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad)]

78.

وَعَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَدْخُلُ الْخَلَاءَ، فَأَحْمِلُ أَنَا وَغُلَامٌ نَحْوِي إِدَاوَةً مِنْ مَاءٍ وَعَنْزَةً، فَيَسْتَنْجِي بِالْمَاءِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiingia msalani, mimi na ghulamu (mtoto mvulana) mwengine tukimchukulia viroba vya maji na mkuki, na anajisafisha kwa maji[3] yale.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

79.

وَعَنْ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {قَالَ لِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "خُذِ الْأَدَاةَ". فَانْطَلَقَ حَتَّى تَوَارَى عَنِّي، فَقَضَى حَاجَتَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Al-Mughiyrah bin Shu'bah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliniambia: “Chukua kiroba cha maji.” Kisha akaenda mbele hadi akanipotea[4], na ndipo akakidhi haja yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

80.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {اتَّقُوا اللَّاعِنِينَ: الَّذِي يَتَخَلَّى فِي طَرِيقِ النَّاسِ، أَوْ فِي ظِلِّهِمْ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ
زَادَ أَبُو دَاوُدَ، عَنْ مُعَاذٍ: {وَالْمَوَارِدُ}
وَلِأَحْمَدَ; عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ: {أَوْ نَقَعَ مَاءً} وَفِيهِمَا ضَعْفٌ

وَأَخْرَجَ الطَّبْرَانِيُّ النَّهْيَ عَنْ تَحْتِ الْأَشْجَارِ الْمُثْمِرَةِ،
وَصَفَّةِ النَّهْرِ الْجَارِي. مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عُمَرَ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ogopeni viwili vyenye kusababisha laana; humpata ambaye hujisaidia (kukojoa au kunya) katika njia za watu[5], na chini ya vivuli vyao.” [Imetolewa na Muslim]

Ameongezea Abuu Daawuwd kuwa ilisimuliwa na Mu’aadh[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwa: “Kujisaidia mahali pa kuchotea maji na hifadhi yake.”

Katika Riwaayah ya Ahmad (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) kuwa: “Kujisaidia palipokusanyika maji.” [Na Hadiyth zote mbili, zina udhaifu]

Atw-Twabaraaniy alitaja kuwa: “Imekatazwa kujisaidia chini ya miti ya matunda na kando kando ya mito inayotiririka[7].” [Imetolewa na Atw-Twabaraaniy kutokana na Hadiyth ya Ibn ‘Umar, kwa Isnaad dhaifu]

81.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا تَغَوَّطَ الرَّجُلَانِ فَلْيَتَوَارَا كُلُّ وَاحِدٍ مِنْهُمَا عَنْ

صَاحِبِهِ، وَلَا يَتَحَدَّثَا. فَإِنَّ اللَّهَ يَمُقْتُ عَلَى ذَلِكَ { رَوَاهُ أَحْمَدُ.
وَصَحَّحَهُ ابْنُ السَّكَنِ، وَابْنُ الْقَطَّانِ، وَهُوَ مَعْلُولٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu wawili wakijisaidia pamoja, kila mmoja ajifiche na mwenzie wala wasiongee, kwani Allaah anachukia hivyo.”” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Ibn As-Sakan na Ibn Al-Qatwaan, lakini ina dosari[8]]

82.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا يُمَسِكَنَّ أَحَدُكُمْ ذَكَرَهُ بِيَمِينِهِ، وَهُوَ يَبُولُ، وَلَا يَتَمَسَّحُ مِنَ الْخَلَاءِ بِيَمِينِهِ، وَلَا يَتَنَفَّسُ فِي الْإِنَاءِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Abuu Qataadah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtu yeyote asishike dhakari[9] yake kwa kulia kwake wakati anakojoa, na asijisafishe (kutokana na haja kubwa au ndogo) kwa kulia kwake, wala asipumulie katika chombo (anachonywea).” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

83.

وَعَنْ سَلْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَقَدْ نَهَانَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "أَنْ نَسْتَقْبِلَ الْقِبْلَةَ بِغَائِطٍ أَوْ بَوْلٍ، أَوْ أَنْ نَسْتَنْجِيَ بِالْيَمِينِ، أَوْ أَنْ نَسْتَنْجِيَ بِأَقْلٍ مِنْ ثَلَاثَةِ أَحْجَارٍ، أَوْ أَنْ نَسْتَنْجِيَ بِرَجِيعٍ أَوْ عَظْمٍ"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَالسَّبْعَةَ مِنْ حَدِيثِ أَبِي أَيُّوبَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {لَا تَسْتَقْبِلُوا الْقِبْلَةَ بِغَائِطٍ وَلَا بَوْلٍ، وَلَكِنْ شَرِّقُوا أَوْ غَرِّبُوا}

Kutoka kwa Salmaan[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitukataza kuelekea Qiblah wakati wa kwenda haja kubwa au ndogo, wala tusijisafishe kwa mkono wa kulia, au kujisafisha kwa mawe yasiyotimia matatu, au kujisafisha kwa kinyesi cha wanyama au mfupa.” [Imetolewa na Muslim]

As-Sab’ah (Maimaam Saba wa Hadiyth) wamenukuu Hadiyth ya Abuu Ayyuub[11] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Usielekee Qiblah[12] wakati unakwenda haja kubwa au ndogo, lakini geukia Mashariki au Mgharibi.”

84.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا; أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ أَتَى الْغَائِطَ فَلْيَسْتَتِرْ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kwenda kujisaidia haja kubwa na ajisitiri.” [Imetolewa na Abuu Daawuud]

85.

وَعَنْهَا: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا خَرَجَ مِنَ الْغَائِطِ قَالَ: "غُفْرَانَكَ" } أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ. وَصَحَّحَهُ أَبُو حَاتِمٍ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema tena: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitoka msalani, anasema: “Ghufraanaka (Ee Allaah! Naomba Unighufurie).” [Imetolewa na Al-Khamsah: (Abuu Daawuud, At-Tirmidhiy, Ibn Maajah, An-Nasaaiy, Ahmad, Ibn Hibbaan, Al-Haakim) Waliipa Hadiyth hii daraja la Swahiyh Abuu Haatim na Al Haakim]

86.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { أَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْغَائِطُ، فَأَمَرَنِي أَنْ آتِيَهُ بِثَلَاثَةِ أَحْجَارٍ، فَوَجَدْتُ حَجَرَيْنِ، وَلَمْ أَجِدْ ثَالِثًا. فَأَتَيْتُهُ بِرَوْثَةٍ. فَأَخَذَهُمَا وَأَلْقَى الرَّوْثَةَ، وَقَالَ: "هَذَا رِكْسٌ" } أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ زَادَ أَحْمَدُ، وَالْذَاقُطْنِيُّ: { ائْتِنِي بِغَيْرِهَا }

Kutoka kwa Ibn Mas-'uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikwenda kujisaidia na akaniamrisha nimpelekee mawe matatu, nikapata mawe mawili na sikupata la tatu. Kwa hivyo nikampelekea kinyesi cha mnyama kilichokauka. Akakirushia mbali[13] kisha akasema: “Hii ni najisi.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Katika nukuu ya Ahmad na Ad-Daaruqutwniy imeongezewa: “Niletee kisichokuwa hiki[14].”

87.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَهَى "أَنْ يُسْتَنْجَى بِعَظْمٍ، أَوْ رَوْثٍ" وَقَالَ: "إِنَّهُمَا لَا يُطَهَّرَانِ" } رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ametukataza kutumia mifupa au kinyesi kikavu cha mnyama kujisafisha, alisema: “Vitu hivi viwili havitwoharishi.”” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy na akaisahihisha]

88.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {اسْتَنْزِهُوا مِنَ الْبَوْلِ، فَإِنَّ عَامَّةَ عَذَابِ الْقَبْرِ مِنْهُ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ
وَالْحَاكِمُ: {أَكْثَرُ عَذَابِ الْقَبْرِ مِنَ الْبَوْلِ} وَهُوَ صَحِيحُ
الْإِسْنَادِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Jitakaseni kutoka na mkojo, kwani ni sababu kuu ya adhabu za kaburini.” [Imetolewa na Ad-Daaruuqutwniy

Na kutoka kwa Al Haakim alisimulia kuwa: “Adhabu nyingi za kaburini ni kutokana na mkojo.” [Na Isnaad yake ni Swahiyh]

89.

وَعَنْ سُرَّاقَةَ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {عَلَّمَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الْخَلَاءِ: " أَنْ نَقْعُدَ عَلَى الْيُسْرَى، وَنَنْصِبَ الْيُمْنَى"} رَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Suraaqah bin Maalik[15] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitufundisha adabu za msalani: kuwa tukalie mguu wa kushoto[16] na tuusimamisha wima mguu wa kulia.” [Imetolewa na Al-Bayhaqiy kwa Isnaad dhaifu[17]]

90.

وَعَنْ عِيسَى بْنِ يَزْدَادَ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا بَالَ أَحَدُكُمْ فَلْيَنْتُرْ ذَكَرَهُ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ } رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa ‘Iysaa bin Yazdaad[18] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kutoka kwa baba yake amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) amesema: “Mmoja wenu akikojoa, anapaswa akung’ute dhakari yake mara tatu.” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa Isnaad dhaifu]

91.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا; { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَأَلَ أَهْلَ قُبَاءٍ، فَقَالَ: "إِنَّ اللَّهَ يُثْنِي عَلَيْكُمْ، فَقَالُوا: إِنَّا نَتَّبِعُ الْحِجَارَةَ الْمَاءَ } رَوَاهُ الْبَزَّازُ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ وَأَصْلُهُ فِي أَبِي دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ بِدُونِ ذِكْرِ الْحِجَارَةِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy aliwauliza watu wa Qubaa akasema: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) “Allaah Anakusifuni.” Wakasema: “Sisi hufuatisha maji baada ya (kujisafisha kwa) mawe.” [Imetolewa na Al Bazaar kwa Isnaad dhaifu]

Na chanzo chake ni Abuu Daawuwd na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Khuzaymah Hadiyth hii kupitia kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) bila kutaja “mawe.”

[1] Pete ile ilikuwa imeandikwa mistari mitatu: “Muhammad Rasulu wa Allaah.” Hii inamaanisha kwamba, Majina ya Allaah (عز وجل) au Aayah za Qur-aan kamwe zisipelekwe chooni au unapokwenda haja yoyote.

[2] Kwa kawaida majini huishi sehemu chafu kama vyooni. Kwa sababu hiyo, Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiomba hifadhi ya Allaah (عز وجل). Mtu sharti aisome du’aa hii kabla ya kuingia chooni kwa sauti ya kusikika. Kwa mujibu wa usimulizi wa Anas (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) maporini na misituni, mtu sharti aisome du’aa hii kabla ya kuchuchumaa na kuenda haja. Wakati wa kuenda haja, mtu sharti aangalie mwili wake na nguo zake.

[3] Baadhi ya Wanazuoni hupendelea kujisafisha kwa dongo pamoja na maji.

[4] Tendo hili la Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) linatufundisha kuwa, wakati wa kuenda kujisaidia ni lazima kuandaa sitara (kificho) ili ufichike kwa watu wengine. Katika Hadiyath nyingine imesema kwamba, mahala palipo wazi, kijilima cha udongo au rundo la mchanga uandaliwe kwa ajili ya kujisitiri. Mtu akijisaidia mahali pa wazi kabisa, shaytwaani atayacheke matakao yake na atachekwa na watu pia.

[5] Imekatazwa kuenda haja njiani au katika njia zilizo karibu na maeneo yenye watu wengi. Mahali penye barabara isiyotumika au magofu ya nyumba zilizohamwa zinaweza kutumika kuendea haja.

[6] Mu’aadh ni Answaar (wa kutoka Al-Madiynah) wa kabila la Al-Khazraj alikuwa mmoja wa Swahaba waadilifu, mtukufu na msomi mkubwa. Alishiriki katika vita za Aqabah, Badr na vita zingine kubwa.

Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimteuwa kuwa mwakilishi wake kule Yaman. Kisha ‘Umar akamteua kuwa Gavana wa Shaam baada ya Abuu ‘Ubaydah bin Al-Jarraah. Alifariki katika mji wa Amwaas mnamo mwaka 17 au 18 A.H akiwa na umri wa miaka 38.

[7] Sehemu zote zinazokatazwa ni sita. Imekatazwa katika Hadiyth kuenda haja kubwa au ndogo karibu na milango ya Misikiti.

[8] Hii inathibitishwa na Hadiyth zingine.

[9] Kuushika uume kwa mkono wa kuume wakati wa kuenda haja ndogo au kuuosha, na kupumulia kwenye chombo cha kunywea imekatazwa, kwa mujibu wa wengine, na kwa mujibu wa wengine wanasema haipendezi. Kutolea pumzi ndani ya chombo kuna madhara kwa sababu hiki ni chanzo cha kuambukiza viini kutoka kwa mtu mmoja mpaka kwa mwingine. Na Hadiyth inayoagiza kuwa na mapumziko matatu wakati wa kunywa, inamaanisha kuwa kinywaji sharti kinywewe taratibu na siyo kukimeza kwa mkupuo mmoja.

[10] Salmaan Al-Faarisii: Alikuwa akijulikana kwa jina la “Salmaan mkarimu”, na akapewa jina la utani la Abuu ‘Abdillaah. Asili yake alitoka Uajemi (Persia). Alisafiri akitafuta dini, na akawa Mkristo. Kisha akahamia Al-Madiynah na akamuamini Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mara tu alipowasili Al-Madiynah. Salmaan Al-Faarisii ndiye aliyetoa fikra ya kuchimbwa mahandaki katika vita vya Al-Khandaq. Alikuwa kiongozi katika Uislaam, na alifariki Al-Madiynah mnamo mwaka 50 au 32 A.H. Imetaarifiwa kwamba aliishi muda mrefu sana, ama miaka 250 au 350.

[11] Abuu Ayuwb jina lake ni Khaalid bin Zayd bin Kulayb. Huyu ndiye aliyemkaribisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipowasili Al-Madiynah mara ya kwanza. Alikuwa ni mmoja wa Swahaba wakubwa na waandamizi sana. Alishiriki katika vita vya Badr, na akafa shahidi wakati alipopigana vita dhidi ya Wabinzantina mnamo mwaka 50 A.H.

Kaburi lake liko katika kuta za Istanbul linajulikana sana na watu wengi hulizuru.

[12] Katika kadhia hii, ‘Makatazo’ yako kwenye maeneo ya wazi. Haikatazwi ikiwa eneo hilo ni ndani ya jengo ambalo lina kuta zinazolizunguka. Kwani kuna Hadiyth ambayo ilisimuliwa na ‘Abdullaah bin ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) kwamba: “Katika nyumba ya dadangu Hafswa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) nilikuenda ghorofani kwenye paa, nikamuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anakuenda haja, ameeleka Shaam.” Hadiyth hii ni ya Sahihi Muslim.

[13] Hadiyth hii inatujulisha kuwa, mtu asisafishe sehemu zake za siri kwa kinyesi au samadi ya mnyama; na pia imekatazwa kujisafisha kwa mifupa.

[14] Hiyo nyongeza inamaanisha kwamba, kwa ajili ya usafi, hutakiwa mabonge matatu ya udongo, ingawa mawili yangetosha, lakini sharti la matatu liko pale pale. Yanaweza kutumika mabonge zaidi ya matatu, ikilazimika, lakini namba iwe Witri. Hadiyth hii pia inathibitisha kuwa kinyesi cha Wanyama hakiwezi kutumika kusafishia sehemu za siri. Na pia kujisafisha kwa mifupa pia kumekatazwa.

[15] Suraaqah bin Maalik bin Ju’shum Al-Mudlaj Al-Kinaan aliyepewa jina la utani la Abuu Sufyaan alikuwa Swahaba maarufu. Huyu ndiye aliyemsaka Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akihama (kuenda zake Madiynah na Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) na mwishowe miguu ya mbele ya farasi wake ikazama ardhini mpaka magotini. Alifariki mnamo mwaka wa 24 A.H.

[16] Katika kila amri ya Uislaam kuna hikma, iwe tunaielewa au laa. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituagiza sisi tuukalie mguu wa kushoto, ili kuweka uzito wa mwili upande wa kushoto kwani hata tumbo liko upande huo wa kushoto, kwa hivyo inalifanya tendo la kijisaidia liwe rahisi, na uyabisi wa tumbo, mama wa mgonjwa pia huondoshwa.

[17] Hadiyth hii ni dhaifu.

[18] ‘Iysaa na babake Yazdaad wote hawajulikani. Ibn ‘Iyn alisema kuwa: “Iysaa na babake hawafahamiki.”

08-Mlango Wa Ghuslu (Kuoga) Na Hukumu Ya Janaba

بَابُ الْغُسْلِ وَحُكْمِ الْجُنُبِ

Mlango Wa Ghuslu (Kuoga) Na Hukumu Ya Janaba

92.

عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْمَاءُ مِنَ الْمَاءِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَأَصْلُهُ فِي الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Maji (ya ghuslu) ni kutokana na maji (ya kutoka manii)[1].” [Imetolewa na Muslim, na chanzo chake ni Al-Bukhaariy]

93.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا جَلَسَ بَيْنَ شُعْبَيْهَا الْأَرْبَعِ، ثُمَّ جَهَذَهَا، فَقَدْ وَجَبَ الْغُسْلُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ زَادَ مُسْلِمٌ: "وَإِنْ لَمْ يُنْزَلْ "

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “(Mwanamume) atakapokaa baina ya sehemu nne za mwanamke, kisha akamfanyia bidii kuingiza dhakari yake[2], itampasa ghuslu.”” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Muslim aliongeza yafuatayo: “Hata kama hakutokwa na manii.”

94.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ؛ أَنَّ أُمَّ سُلَيْمٍ وَهِيَ امْرَأَةُ أَبِي طَلْحَةَ قَالَتْ: { يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ اللَّهَ لَا يَسْتَحِي مِنْ الْحَقِّ، فَهَلْ عَلَى الْمَرْأَةِ الْغُسْلُ إِذَا احْتَلَمَتْ؟ قَالَ: "نَعَمْ. إِذَا رَأَتْ الْمَاءَ" } الْحَدِيثُ مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) kuwa: “Ummu Sulaym[3], mke wa Abuu Twalhah amesema: “Ee Rasuli wa Allaah!

Allaah Haionei haki aibu. Je mwanamke inamlazimu afanye ghuslu akiota ndoto ya kujimai[4]?” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Ndiyo! Akiona maji maji.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

95.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الْمَرْأَةِ تَرَى فِي مَنَامِهَا مَا يَرَى الرَّجُلُ قَالَ: "تَغْتَسِلُ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

زَادَ مُسْلِمٌ: فَقَالَتْ أُمُّ سُلَيْمٍ { وَهَلْ يَكُونُ هَذَا؟ قَالَ: "نَعَمْ فَمِنْ أَيْنَ يَكُونُ الشَّبَهُ؟ {

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu mwanamke anayeota usingizini kujimai[5] kama aotavyo mwanamume: “Basi aoge.”” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Muslim aliongeza yafuatayo: “Ummu Salamah aliuliza: “Hii hutokea (kwa mwanamke pia)?” Akasema: “Ndiyo! Kwani inatoka wapi kushabihiana (kwa mtoto na mama yake)?”

96.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَغْتَسِلُ مِنْ أَرْبَعٍ: مِنَ الْجَنَابَةِ، وَيَوْمَ الْجُمُعَةِ، وَمِنْ الْحِجَامَةِ، وَمِنْ غُسْلِ الْمَيِّتِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akioga kutokana na mambo manne: Kutoka na janaba, siku ya Ijumaa, baada ya hijaamah (kuumika), na baada ya kuosha maiti[6].” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

97.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {فِي قِصَّةِ ثُمَامَةَ بِنِ أَثَالٍ، عِنْدَمَا أَسْلَمَ وَأَمَرَهُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يَغْتَسِلَ} رَوَاهُ عَبْدُ الرَّزَّاقِ وَأَصْلُهُ مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuhusu kisa cha Thumaamah bin Uthaal[7] aliposilimu, Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alimuamrisha aoge[8].” [Imetolewa na ‘Abdur-Razzaaq, na chanzo chake ni kutoka Al-Bukhaariy na Muslim]

98.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {غُسْلُ الْجُمُعَةِ وَاجِبٌ عَلَى كُلِّ مُحْتَلِمٍ} أَخْرَجَهُ السَّبْعَةُ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ghuslu (kuoga) siku ya Ijumaa ni waajib kwa kila mtu aliyebaleghe.”” [Imetolewa na As-Sab’ah (Al-Bukhaariy, Muslim, Abuu Daawuud, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad, At-Tirmidhiy]

99.

وَعَنْ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ تَوَضَّأَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ فَبِهَا وَنِعْمَتْ، وَمَنْ اغْتَسَلَ فَالْغُسْلُ أَفْضَلُ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Samurah[9] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kutawadha siku ya Ijumaa anafanya jambo jema, na yule anayeoga, basi ghuslu (kuoga) ni bora zaidi.” [Imetolewa na Maimaam watano na akaipa daraja la Hasan At-Tirmidhiy]

100.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُقْرِنُنَا الْقُرْآنَ مَا لَمْ يَكُنْ جُنُبًا} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَهَذَا لَفْظُ التِّرْمِذِيِّ وَحَسَنَةٌ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitufundisha Qur-aan, isipokuwa alipokuwa katika janaba[10].” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, na Musnad Ahmad) na hili ni tamshi la At-Tirmidhiy aliyeipa daraja la Hasan na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

101.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا أَتَى أَحَدُكُمْ أَهْلَهُ، ثُمَّ أَرَادَ أَنْ يَعُودَ فَلْيَتَوَضَّأْ بَيْنَهُمَا وَضُوءًا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ زَادَ الْحَاكِمُ: { فَإِنَّهُ أَنْشَطُ لِلْعُودِ }

وَلِلْأَرْبَعَةِ عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَنَامُ وَهُوَ جُنُبٌ، مِنْ غَيْرِ أَنْ يَمَسَّ مَاءً} وَهُوَ مَعْلُومٌ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akijimai na mkewe, na akataka kurudia, basi na atawadhe[11] baina ya mara hizo mbili.” [Imetolewa na Muslim]

Na akaongezea Al Haakim: “Kwani huo (wudhuu) humchangamsha kwa ajili ya kurudia (jimai).”

Na Maimaam wanne wamepokea Hadiyth ya ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa analala na huku ana janaba bila ya kugusa maji[12].” [Imetolewa na Al-Arba’h, Hadiyth hii ina dosari]

102.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا اغْتَسَلَ مِنَ الْجَنَابَةِ يَبْدَأُ فَيَغْسِلُ يَدَيْهِ، ثُمَّ يُفْرَغُ بِيَمِينِهِ عَلَى شِمَالِهِ، فَيَغْسِلُ فَرْجَهُ، ثُمَّ يَتَوَضَّأُ، ثُمَّ يَأْخُذُ الْمَاءَ، فَيُدْخِلُ أَصَابِعَهُ فِي أُصُولِ الشَّعْرِ، ثُمَّ حَفَنَ عَلَى رَأْسِهِ ثَلَاثَ حَفَنَاتٍ، ثُمَّ أَفَاضَ عَلَى سَائِرِ جَسَدِهِ، ثُمَّ غَسَلَ رِجْلَيْهِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

وَلَهُمَا فِي حَدِيثِ مَيْمُونَةَ: {ثُمَّ أَفْرَغَ عَلَى فَرْجِهِ، فَغَسَلَهُ بِشِمَالِهِ، ثُمَّ ضَرَبَ بِهَا الْأَرْضَ} وَفِي رِوَايَةٍ: {فَمَسَحَهَا بِالثُّرَابِ} وَفِي آخِرِهِ: {ثُمَّ أَتَيْتُهُ بِالْمِنْدِيلِ} فَرَدَّهُ، وَفِيهِ: {وَجَعَلَ يَنْفُضُ الْمَاءَ بِيَدِهِ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akioga janaba, akianza kuosha mikono, kisha anamimina kwa kulia kwake juu ya

kushoto kwake na anaosha tupu yake, kisha anatawadha, kisha alichukua maji akapitisha vidole vyake kwenye mizizi ya nywele zake, kisha alitia mafumba matatu ya maji kichwani, kisha anamimina maji sehemu zingine za mwili wake, kisha anaosha miguu yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Nao wawili (Al-Bukhaariy na Muslim) wamesimulia Hadiyth ya Maymuwnah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimwagia tupu yake na akaosha kwa mkono wake wa kushoto. Kisha akapiga mkono wake ardhini.”

Katika Riwaayah nyengine: “Akaupangusa ardhini.”

Na mwisho inasema: “Kisha nikamletea kitambaa[13], akakirudisha, na akaendelea kujipangusa maji kwa mkono wake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

103.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ
إِنِّي امْرَأَةٌ أَشَدُّ شَعْرَ رَأْسِي، أَفَأَنْقِضُهُ لِغُسْلِ الْجَنَابَةِ؟

وَفِي رِوَايَةٍ: وَالْحَيْضَةُ؟ فَقَالَ: "لَا، إِنَّمَا يَكْفِيكَ أَنْ تَحْتِيَ عَلَى
رَأْسِكَ ثَلَاثَ حَثِيَّاتٍ" { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema:
“Nilisema, Ee Rasuli wa Allaah! Mimi ni mwanamke nasuka nywele kichwa changu, Je! Nizifumue ili nipate kuoga janaba?”

Katika Riwaayah nyengine: “Na mwisho wa hedhi?” akasema: “Hapana, inatosha kumwagia mafumba matatuya maji kichwani kwako[14].” [Imetolewa na Muslim]

104.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنِّي لَا أُحِلُّ الْمَسْجِدَ لِحَائِضٍ وَلَا جُنُبٍ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Siruhusu Msikiti kwa mwenye hedhi[15] wala mwenye janaba[16].”” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

105.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {كُنْتُ أَغْتَسِلُ أَنَا وَرَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مِنْ إِنَاءٍ وَاحِدٍ، تَخْتَلِفُ أَيْدِينَا فِيهِ مِنَ الْجَنَابَةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

زَادَ ابْنُ حِبَّانَ: وَتَلَّتْنِي أَيْدِينَا

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema tena: “Mimi na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) tulikuwa tukioa

(ghuslu ya) janaba katika chombo kimoja huku mikono yetu ikipishana.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na akaongezea Ibn Hibbaan: “Na (mikono yetu) ilikuwa inakutana.”

106.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ تَحْتَ كُلِّ شَعْرَةٍ جَنَابَةٌ، فَاغْسِلُوا الشَّعْرَ، وَأَنْقُوا الْبَشَرَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَضَعَفَاهُ
وَلِأَحْمَدَ عَنْ عَائِشَةَ نَحْوَهُ، وَفِيهِ رَأْيٌ مَجْهُولٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuna janaba chini ya kila unywele[17], kwa hivyo osheni nywele na osheni ngozi.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na At-Tirmidhiy, na wote waliidhoofisha]

Na katika Riwaayah ya Ahmad, Hadiyth sawa na hiyo imesimuliwa na ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) na katika Isnaad yake kuna mpokezi mmoja Majhuwl (asiyejulikana).

[1] Inamaanisha baada ya kutokwa na manii, kuoga ni lazima na muhimu. Hadiyth hii inahusiana na “kutokwa kwa usiku” tu, siyo kwa kujamiiana. Wanazuoni wengi wanaamini hivyo. ‘Ubayy bin Ka’b alisema: “Katika

siku za mwanzo za Uislaam, watu wakijamiiana, kuoga hakukuwa lazima hadi manii yawe yametoka; lakini baadaye amri hii ikabatilishwa. Baadhi ya watafiti wameripoti maafikiano ya Muslim juu ya kadhia hii, kwamba, mara kujamiiana kunapoanza, kuoga kunakuwa lazima, hata manii yasipotoka.”

[2] Hii inamaanisha kuwa kujamiiana kukianza tu, kuoga kunakuwa lazima. Hadiyth hii inaibatilisha hiyo iliyopita, ikihusiana na kujamiiana.

[3] Umm Sulaym ni Ar-Rumaysa au Al-Ghumaysa bint Milhaan, Mama wa Anas bin Maalik. Alikuwa miongoni mwa Swahabiyyah waadilifu. Aliolewa na Maalik bin An-Nasr. Kisha akasilimu, na akamualika aingie Uislaam. Lakini yeye alichukia na akaenda zake Shaam ambako alifia. Kisha akachumbiwa na Abuu Twalha Al-Anaswaariy wakati bado ni mshirikina, lakini yeye akampa sharti kuwa awe Muislaam kwanza, kwa hivyo akasilimu na akamuoa. Alifariki zama za Ukhalifa wa ‘Uthmaan.

[4] Kama walivyo wanaume, wanawake pia hupata “Ndoto za kulowana.”

[5] Inamaanisha kuwa wanawake pia hutokwa na maji maji kama manii ya mwanamme, ama sivyo watoto wangukuwa hawafanani na mama zao. Kufanana kwa watoto na wazazi wao kunategemea ukali wa hayo manii.

[6] Kati ya mambo hayo manne, kuoga baada ya kujamiiana ni fardhi (lazima), kuoga siku ya Ijumaa ni Sunnah (kufuata matendo ya Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)), na mawili yanayobaki ni Mustahab (yanapendeza). Ahaadiyth kuhusu ulazima wa kuoga siku ya Ijumaa ni sahihi zaidi, kwa hivyo zifuatwe hizo.

[7] Thumaamah bin Uthaal alikuwa anatoka kwa Banu Hanifa na Sultani wa watu wa Al-Yamaama. Alikuenda kuhiji Hijjah ndogo (‘Umrah) wakati akiwa bado mushrik na akakamatwa na wapanda farasi wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Walimpeleka Al-Madiynah na wakamfungia katika nguzo ya Msikiti. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuachia huru baada ya siku tatu. Basi akawa Muislaam muadilifu sana

na imara sana, zama zile za ukanaji dini, dhidi ya watu wake ambao walighilibiwa na Musailima Al-Kadhdhaab.

[8] Mtu asiyekuwa Muislaam anaposilimu, sharti aoge. Abuu Daawuud aliripoti kuwa, Nabiyy (ﷺ) alimuamuru Thumaamah aoge aliposilimu.

[9] Samurah bin Jundub ni Swahaba maarufu ambaye alipewa jina la utani la Abuu ‘Abdillaah. Alikuwa ni Fazari na alikuwa rafiki wa Answaar. Pia alikuwa mmoja wa mahaafidh waliohifadhi Ahaadiyth nyingi. Alilowea Basra, na alikuwa mkali sana dhidi ya Al-Haruriya. Alifariki mwishoni mwa mwaka 59 A.H.

[10] Kutokana na Hadiyth hii na zingine, inathibitika kwamba kusoma Qur-aan Tukufu kwa mtu anayepasa kuoga josho la baada ya kujamiiana, siyo sawa.

[11] Kutawadha huku kunapendeza lakini siyo lazima. Pia kunaleta raha na uchangamfu au upya katika hali ya tendo. Inasemekana kuwa Nabiyy (ﷺ) akienda kulala na wakeze mbalimbali katika usiku mmoja, alikuwa akioga kabla ya kuenda kwa kila mmoja. Imeripotiwa pia kuwa mara nyingine alikuwa akitawadha baina yao na mara nyingine hakufanya hivyo. Kwa hivyo katika jambo hili, mtu aweza kuchagua mtindo wowote.

[12] Inamaanisha kwamba, kabla ya kuenda kulala, kuoga siyo lazima kwa mtu mwenye janaba. Kuna Hadiyth kutoka kwa Bukhaariy kuhusu kadhia hii kwamba Nabiyy (ﷺ) alikuwa akitawadha kabla ya kula, kunywa au kulala. Kwa hiyo ni ubora kufuata njia za Nabiyy (ﷺ), ingawa jambo hili linapendeza tu (lakini siyo lazima).

[13] Suala la kukausha viungo baada ya kutawadha ni la hiari, kwa hivyo ni hiari ya mtu kujikausha au laa.

[14] Hadiyth hii inaweka wazi kwamba, kwa mwanamke mwenye hedhi na kwa mwanamume mwenye janaba, siyo lazima kuzifumua nywele. Kuna Hadiyth nyingine kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) ambayo inataja kufumua nywele. Hadiyth zote mbili ni kwa mazingira au nyakati tofauti.

[15] Mwanamke mwenye hedhi haruhusiwi kuingia Msikiti wowote wala kutufu (kuizunguka) Ka’bah, na asiswali wala kufunga akiwa katika hedhi. Swalaah anazozikosa nyakati hizi anasamehewa, lakini ni sharti alipe Swawm baada ya hedhi. Wanazuoni wamekhitilafiana kuhusu mwanamke mwenye hedhi kusoma na kugusa Qur-aan, lakini rai iliyo na nguvu zaidi ni kuwa anaruhusika kuisoma kwani hawezi kuharamika kuihifadhi Qur-aan. Na wengineo wameona pia anaruhusika hata kuigusa wakatoa dalili kadhaa ikiwemo Hadiyth ya ‘Aaishah pindi alipokwenda Hajj ikamjia hedhi akaamrisha na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) ateleze yote wanayoyateleza Hujaji isipokuwa kutufu Ka’bah. Ama wengineo wamekubali aisome lakini asiiguse bali anaweza kuikamata kwa kushikia kitambaa au glavu. Kumdhukuru Allaah (عز وجل) imeruhusiwa kwake. Anaruhusiwa kuenda mahali pa kuswalia ‘Iyd.

[16] Inamaanisha kuwa mwanamke mwenye hedhi na mwanamume mwenye janaba hawaruhusiwi kukaa Msikitini lakini kupita tu wanaruhusiwa. Mtu akiwa kalala Msikitini na akaota na akajikojolea huku bado yumo Msikitini, ni lazima atoke nje.

[17] Tunaelewa kuwa Hadiyth hii kwamba, ni lazima kuosha mwili mzima baada ya tendo la ndoa, isipokuwa kusukutua mdomo na kuweka maji puani kwa kuwa haya mawili yana ubishi.

09-Mlango Wa Tayammum (Kujitwaharisha Kwa Mchanga)

بَابُ التَّيَمُّمِ

09-Mlango Wa Tayammum (Kujitwaharisha Kwa Mchanga)

107.

عَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا; أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أُعْطِيتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ قَبْلِي: نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ، وَجُعِلَتْ لِي الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهُورًا، فَأَيُّمَا رَجُلٍ أَدْرَكَتْهُ الصَّلَاةُ فَلْيُصَلِّ} وَذَكَرَ الْحَدِيثَ

وَفِي حَدِيثٍ حُذِيفَةَ عِنْدَ مُسْلِمٍ: {وَجُعِلَتْ ثُرْبَتُهَا لَنَا طَهُورًا، إِذَا لَمْ نَجِدِ الْمَاءَ}

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عِنْدَ أَحْمَدَ: {وَجُعِلَ التُّرَابُ لِي طَهُورًا}

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Nimepewa mambo matano hakupewa yeyote kabla yangu: Nimenusuriwa na (kutiwa) kizaazaa (nyoyoni mwa maadui) kwa mwendo wa mwezi. Na nimefanyiwa ardhi kuwa sehemu ya kufanyia ‘ibaadah na kujitwaharishia[1], basi mtu mtu yeyote katika ummah wangu akifikiwa na Swalaah, aswali.”[2]

Katika Hadiyth ya Khudhayfah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) iliyoandikwa na Muslim inaeleza:

“Mchanga[3] wake (au udongo) umefanywa kitoharisho changu ikiwa hatukupata maji.”

Na Hadiyith ya ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) iliyoandikwa na Ahmad inasema: “Ardhi (mchanga) wake umefanywa kitoharisho kwa ajili yangu.”

108.

وَعَنْ عَمَّارِ بْنِ يَاسِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {بَعَثَنِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي حَاجَةٍ، فَأَجْنَبْتُ، فَلَمْ أَجِدِ الْمَاءَ، فَتَمَرَّغْتُ فِي الصَّعِيدِ كَمَا تَمَرَّغُ الدَّابَّةُ، ثُمَّ أَتَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَذَكَرْتُ ذَلِكَ لَهُ، فَقَالَ: "إِنَّمَا كَانَ يَكْفِيكَ أَنْ تَقُولَ بِيَدَيْكَ هَكَذَا" ثُمَّ ضَرَبَ بِيَدَيْهِ الْأَرْضَ ضَرْبَةً وَاحِدَةً، ثُمَّ مَسَحَ الشَّمَالَ عَلَى الْيَمِينِ، وَظَاهَرَ كَفَّيْهِ وَوَجْهَهُ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

وَفِي رِوَايَةِ لِلْبُخَارِيِّ: وَضَرَبَ بِكَفَّيْهِ الْأَرْضَ، وَنَفَخَ فِيهِمَا، ثُمَّ مَسَحَ بِهِمَا وَجْهَهُ وَكَفَّيْهِ

Kutoka kwa ‘Ammar bin Yaasir[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alinituma katika haja fulani, kisha nikapata janaba na sikupata maji, nilijiviringisha kwenye mchanga kama mnyama, nikarejea kwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) nikamtajia tukio hilo. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaniambia: “Inakutosha kufanya hivi kwa mikono.” Akapiga mikono yake mara moja juu ya mchanga, na akaupangusa mkono wa kushoto juu ya kiganja cha mkono wake wa kulia mbele na nyuma na uso wake.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi ni la Muslim]

Na katika Riwaayah ya Al-Bukhaariy: “Na (Nabiy ﷺ) akapiga viganja vyake viwili ardhini[5], halafu akavipuliza, akapangusa navyo usoni na viganja vyake.”

109.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {التَّيْمُمُ ضَرْبَتَانِ ضَرْبَةٌ لِلْوَجْهِ، وَضَرْبَةٌ لِلْيَدَيْنِ إِلَى الْمِرْفَقَيْنِ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَصَحَّحَ الْأَيْمَنُ وَقَفَّهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tayammum (kujitwaharisha kwa mchanga), ni mapigo mawili, pigo moja kwa ajili ya uso jingine kwa ajili ya mikono hadi kwenye viwiko viwili[6].”” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy, na akaisahihisha Imaam kama Mawquwf]

110.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الصَّعِيدُ وَضُوءُ الْمُسْلِمِ، وَإِنْ لَمْ يَجِدِ الْمَاءَ عَشْرَ سِنِينَ، فَإِذَا وَجَدَ الْمَاءَ فَلْيَتَّقِ اللَّهَ، وَلْيُمِسَّهُ

بَشَرَتُهُ { رَوَاهُ الْبَزَّازُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْقَطَّانِ، وَ لَكِنْ صَوَّبَ
الْدَّارَقُطْنِيُّ إِرْسَالَهُ
وَلِلتِّرْمِذِيِّ: عَنْ أَبِي ذَرٍّ نَحْوَهُ، وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mchanga ni
wudhuu wa Muislamu hata kama hatapata maji kwa miaka kumi[7],
akiyapata amche Allaah na ayagusishe ngozi yake.” [Imetolewa na
Al-Bazaar, na akaisahihisha Ibn Al-Qatwaan. Lakini aliidhinisha
Ad-Daaruuqtwniy kama Mursal]

Na katika Riwaayah ya At-Tirmidhiy amepokea Hadiyth inayofanana
na hiyo kutoka kwa Abuu Dharr[8], ambayo aliisahihisha.

111.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { خَرَجَ
رَجُلَانِ فِي سَفَرٍ، فَحَضَرَتِ الصَّلَاةُ وَلَيْسَ مَعَهُمَا مَاءٌ فَتَيَمَّمَا
صَعِيدًا طَيِّبًا، فَصَلَّيَا، ثُمَّ وَجَدَا الْمَاءَ فِي الْوَقْتِ. فَأَعَادَا
أَحَدُهُمَا الصَّلَاةَ وَالْوُضُوءَ، وَلَمْ يُعِدِ الْآخَرُ، ثُمَّ أَتَيَا رَسُولَ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَذَكَرَا ذَلِكَ لَهُ، فَقَالَ لِلَّذِي لَمْ يُعِدْ:
"أَصَبْتَ السُّنَّةَ وَأَجْزَأُكَ صَلَاتُكَ" وَقَالَ لِلْآخَرِ: "لَكَ الْأَجْرُ
مَرَّتَيْنِ" { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَ النَّسَائِيُّ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al Khudriy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Watu wawili walikwenda safarini, Swalaah ikawadia, hawakuwa na
maji. Walitayammam kwa mchanga safi na wakaswali. Baadaye

wakapata maji wakati wa Swalaah. Mmoja wao akarudia Swalaah na kutawadha, mwenzie hakurudia. Walipofika kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wakamueleza hilo, akamgeukia yule ambaye hakurudia akamwambia kuwa: “Umefuata Sunnah, na Swalaah yako ya kwanza imekutosheleza[9].” Akamwambia yule aliyerudia kutawadha na kuswali akamwambia: “Wewe una malipo mara mbili[10].” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy]

112.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا فِي قَوْلِهِ عَزَّ وَجَلَّ (وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَى أَوْ عَلَى سَفَرٍ) قَالَ: "إِذَا كَانَتْ بِالرَّجُلِ الْجِرَاحَةُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْقُرُوحُ، فَيُجَنَّبُ، فَيَخَافُ أَنْ يَمُوتَ إِنْ اغْتَسَلَ: تَيْمَمٌ". رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ مَوْقُوفًا، وَرَفَعَهُ الْبَزَّازُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn “Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuhusu kauli yake Allaah (عَزَّ وَجَلَّ): “...Na mkiwa wagonjwa[11] au mko safarini...” [Al-Maaidah (5: 6)] kuwa: “Ikiwa mtu ana jeraha aloumia akiwa katika (jihaad) njia ya Allaah, kisha akapata janaba, na akaogopa kuwa atakufa endapo ataoga, basi atayammam.” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy katika Hadiyth Mawquwf, na Al-Bazaar katika Hadiyth Marfuw’aa, na wakaisahihisha Ibn Khuzaymah na Al Haakim]

113.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {انْكَسَرَتْ إِحْدَى زَنْدَيَّ
فَسَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَأَمَرَنِي أَنْ أُمْسَحَ
عَلَى الْجَبَائِرِ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ بِسَنَدٍ وَاهٍ جَدًّا

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mkono wangu
mmoja ulivunjika, nikamuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ)
nifanyeje, akaniamrisha nipanguse juu ya bendeji[12].”
[Imetolewa na Ibn Maajah kwa Isnaad dhaifu sana]

114.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا فِي الرَّجُلِ الَّذِي
شُجَّ، فَاغْتَسَلَ فَمَاتَ: {“إِنَّمَا كَانَ يَكْفِيهِ أَنْ يَتَيَمَّمَ، وَيَعْصِبَ
عَلَى جُرْحِهِ خِرْقَةً، ثُمَّ يَمْسَحَ عَلَيْهَا وَيَغْسِلَ سَائِرَ جَسَدِهِ”}
رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ بِسَنَدٍ فِيهِ ضَعْفٌ، وَفِيهِ اخْتِلَافٌ عَلَى رُؤَاتِهِ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema
kuhusu mtu aliyejeruhiwa kichwani akaoga na akafariki, kwamba
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ilikuwa
inamtosha kutayammam, kisha afunge bendeji na apanguse maji juu
yake, kisha aoshe sehemu nyingine za mwili wake.” [Imetolewa na
Abuu Daawuwd, Isnaad yake ni dhaifu, na kuna kutofautiana
wasimulizi wake]

115.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {مَنْ السُّنَّةُ أَنْ لَا يُصَلِّيَ الرَّجُلُ بِالتَّيَمُّمِ إِلَّا صَلَاةً وَاحِدَةً، ثُمَّ يَتَيَمَّمُ لِلصَّلَاةِ الْآخَرَى} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ جَدًّا

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Ni Sunnah mtu kutokuswali zaidi ya Swalaah moja[13] kwa Tayammum moja, kisha atayammam kwa ajili ya Swalaah nyingine.” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy kwa Isnaad dhaifu sana[14]]

[1] Maana yake ni kwamba, kama maji hakuna, mtu asipoteze nusu ya wakati wa Swalaah kwa kutafuta maji.

[2] Vitu vingine hivi vitatu ni: (a) Ngawira amefanyiwa ziwe Halaal, (b) Shufaa siku ya Qiyaamah, (c) Unabii kwa ulimwengu wote.

[3] Mchanga au udongo na vitu vyote vingine vitokanavyo na udongo vinahesabika kuwa sawa, na Tayammam kwayo inaruhusiwa. Lakini siyo metali kama antimoni, arseniki, n.k. ambavyo havimo katika fungu la udongo.

[4] ‘Ammaar alipewa jina la utani la Abul-Yaqzaan, na alikuwa miongoni mwa Swahaba waandamizi wa mwanzo, aliteswa kule Makkah kwa ajili ya Iymaan yake. Alishiriki katika Hijrah zote mbili, na katika vita vya Badr na vita vyote muhimu. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia kuwa: “Ee ‘Ammaar, kundi la wapotofu litakuua wewe.” Hiyo ilitokea Siffiyn mnamo mwaka wa 36 A.H wakati akiwa na ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ), aliuawa na askari wa Mu’aawiya akiwa na umri wa miaka 73.

[5] Hadiyth hii inaongelea kuhusu Tayammam (kujitwaharisha kwa udongo). 'Ulamaa wa Fiqh wanasema kuwa pigo moja tu linatosha kwa uso na mikono yote miwili. Wengine wanasema kuwa mapigo mawili ni lazima, moja kwa uso na jingine kwa mikono, kama inavyotajwa katika Hadiyth hii inayofuata. Lakini Hadiyth zote zinazotaja mapigo mawili ni dhaifu.

[6] 'Ulamaa wa Hadiyth wameihesabu Hadiyth hii kuwa ni dhaifu na milolongo yake yote ni dhaifu.

[7] Inamaanisha kwamba, wakati wa dharura, mchanga (udongo) ni badala kamili ya maji, na unakidhi shughuli zote za utwahirishaji, uwe ni kutawadha, au kuoga. Kwa kila Tayammam moja, matendo mengi ya faradhi yanaweza kufanywa, iwapo hakuna mazingira yanayoubatilisha.

[8] Jina la Abuu Dharr lilikuwa ni Jundub bin Junaadah, naye alikuwa miongoni mwa Swahaba maarufu na ni mtu aliyejinyima anasa za kimwili. Alisilimu mapema sana kule Makkah, kisha akaenda kwa watu wake. Alikuwa kwa Nabiy (ﷺ) Al-Madiynah, na baadaye akalowe na akafia Rabdha mnamo mwaka wa 32 A.H.

[9] Inamaanisha kwamba, ikiwa mtu amekwisha kuswali Swalaah moja kwa kutumia Tayammam, basi hakuna haja ya kurudia kuswali, hata kama maji yamepatikana baadaye tena kabla wakati wa Swalaah ile haujapita.

[10] Haikuwa lazima kurudia kuiswali Swalaah ile, kama Swalaah ile iliswaliwa kwa wudhuu wa kutayammam. Huyu mtu wa pili alipata malipo maradufu siyo kwa sababu kaswali mara mbili Swalaah moja, bali kwa sababu ya kufanya uamuzi kuhusu tatizo lililowakabili, hata kama uamuzi ule haukuwa sahihi, lakini kuna malipo zaidi kwa uamuzi usiyo sahihi. Sababu ya pili ya kupata malipo mara mbili, inawezekana ni kwamba aliswali mara mbili, mara moja kwa wudhuu wa Tayammam na mara ya pili kwa wudhuu wa maji.

[11] Inamaanisha kuwa ukiwa unataka kuswali lakini kuna kizuizi katika kutawadha au kuoga, Tayammam huwa ni lazima. Hapa ugonjwa ni

ugonjwa kweli, siyo vipele au vijipu tu. (Kulingana na Maalik, Hanafi na moja katika maneno ya Imaam Shaafi'). Wengine kama (Ahmad na moja katika maneno ya Imaam shaafi') kuwa Tayammam hairuhusiwi isipokuwa kwa mgonjwa anayehofia kuwa maji yatamsababishia kifo. Daawuud anaona kuwa Tayammam inaruhusiwa kwa mgonjwa yoyote bila kujali kama anadhurika na maji au la.

[12] Neno la Kiarabu ni **الْجَبَائِرُ** ambalo hutumika kwa vile vipande vya mbao vinavyowekwa kuuzunguka mkono au mguu uliovunjika ili kuufanya ukae umenyooka saa zote.

[13] Kwa kuwa kutawadha kwa kutayammam ni badala ya kutawadha kwa maji, hufanya kazi namna ile ile. Swalaah nyingi zinaweza kuswaliwa kwa kutawadha kwa maji mara moja tu. Halikadhalika, Swalaah nyingi zinaweza kuswaliwa kwa kutayamamu mara moja tu. Watu wengine baada ya kutayamamu kwa kujamiiiana au kwa kuota na kutoa manii husita kuingia Msikitini au kusoma Qur-aan. Hii ni kutia shaka kuovu na ni ushawishi wa shaytwaan tu, na wala usiujali. Hadiyth hii ya Hasan bin 'Ammar ni dhaifu katika mlolongo wa wapokezi. Kuna Hadiyth mbili zingine kuhusu kadhia hii hii na zote ni dhaifu.

[14]

Hadiyth hii ni dhaifu kwa sababu ilisimuliwa na Hasan bin 'Ammar ambaye alikuwa dhaifu. Kwa sababu hii 'Ulamaa walisema hawaitegemei lakini wakasema kwamba: "Allaah (عز وجل) Ameturuhusu tutumie udongo kukiwa hakuna maji. Na kwa kuwa kutawadha ni lazima baada ya kuenda haja ndogo au haja kubwa au kutoa upepo, basi halikadhalika kwa kutayammam."

10-Mlango Wa Hedhi

بَابُ الْحَيْضِ

116.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {إِنَّ فَاطِمَةَ بِنْتَ أَبِي حُبَيْشٍ كَانَتْ تُسْتَحَاضُ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "إِنَّ دَمَ الْحَيْضِ دَمٌ أَسْوَدُ يُعْرِفُ، فَإِذَا كَانَ ذَلِكَ فَأَمْسِكِي مِنَ الصَّلَاةِ، فَإِذَا كَانَ الْآخِرُ فَتَوَضَّئِي، وَصَلِّي"} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ، وَاسْتَنْكَرَهُ أَبُو حَاتِمٍ

وَفِي حَدِيثِ أَسْمَاءَ بِنْتِ عُمَيْسٍ عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ: {لَتَجْلِسَ فِي مِرْكَنٍ، فَإِذَا رَأَتْ صُفْرَةً فَوْقَ الْمَاءِ، فَلَتَغْتَسِلَ لِلظُّهْرِ وَالْعَصْرِ غُسْلًا وَاحِدًا، وَتَغْتَسِلَ لِلْمَغْرِبِ وَالْعِشَاءِ غُسْلًا وَاحِدًا، وَتَغْتَسِلَ لِلْفَجْرِ غُسْلًا، وَتَتَوَضَّأُ فِيمَا بَيْنَ ذَلِكَ }

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: Fatwmah bint Abiy Hubaysh alikuwa na hedhi ya kudumu[1], Rasulu wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Damu ya hedhi ni nyeusi inatambulika, kwa hivyo ikiwa ndiyo hiyo, jizuie kuswali, na ikiwa ni nyingine (iliyopauka), basi tawadha na uswali.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy, wakaisahihisha Ibn Hibbaan na Al Haakim, na akaiita Munkar (si ya kawaida) Abuu Haatim]

Na katika Hadiyth ya Asmaa bint ‘Umays[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) iliyopokewa na Abuu Daawuud, amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

(Mwanamke) Akae ndani ya bafu lenye maji, na akiona rangi ya njano hivi juu ya maji, basi afanye ghuslu moja kwa Swalaah ya Adhuhuri na Alasiri na afanye ghuslu moja tena kwa Swalaah ya Magharibi na 'Ishaa, na afanye ghuslu kwa Swalaah ya Alfajiri, na baina ya nyakati hizi atawadhe.”

117.

وَعَنْ حَمْنَةَ بِنْتِ جَحْشٍ قَالَتْ: {كُنْتُ أُسْتَحَاضُ حَيْضَةً كَبِيرَةً شَدِيدَةً، فَأَتَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَسْتَفْتِيهِ، فَقَالَ: "إِنَّمَا هِيَ رَكْضَةٌ مِنَ الشَّيْطَانِ، فَتَحْيِضِي سِتَّةَ أَيَّامٍ، أَوْ سَبْعَةً، ثُمَّ اغْتَسِلِي، فَإِذَا اسْتَنْقَأْتَ فَصَلِّي أَرْبَعَةً وَعِشْرِينَ، أَوْ ثَلَاثَةً وَعِشْرِينَ، وَصُومِي وَصَلِّي، فَإِنَّ ذَلِكَ يُجْزِئُكَ، وَكَذَلِكَ فَافْعَلِي كَمَا تَحِيضُ النِّسَاءُ، فَإِنْ قَوِيَتْ عَلَى أَنْ تُؤَخَّرِي الظُّهْرَ وَتُعْجَلِي الْعَصْرَ، ثُمَّ تَغْتَسِلِي حِينَ تَطْهُرِينَ وَتُصَلِّينَ الظُّهْرَ وَالْعَصْرَ جَمِيعًا، ثُمَّ تُؤَخَّرِينَ الْمَغْرِبَ وَتُعْجَلِينَ الْعِشَاءَ، ثُمَّ تَغْتَسِلِينَ وَتَجْمَعِينَ بَيْنَ الصَّلَاتَيْنِ، فَافْعَلِي. وَتَغْتَسِلِينَ مَعَ الصُّبْحِ وَتُصَلِّينَ. قَالَ: وَهُوَ أَعْجَبُ الْأَمْرَيْنِ إِلَيَّ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَحَسَنَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Hamnah bint Jahsh[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: Nilikuwa na hedhi yangu ilikuwa nyingi mno na kali, kwa hivyo nilikwenda kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kumtaka fatwa, akasema: “Hii ni athari ya shaytwaan, kwa hivyo wewe

zingatia hedhi yako kwa siku sita au saba, kisha fanya ghuslu na ukitwahaika, swali kwa siku ishirini na tatu au ishirini na nne, na ufunge na uswali, kwani hiyo itakutosheleza wewe, na ufanye hivyo hivyo kila mwezi kama wanavyopata hedhi wanawake wengine.

Lakini ukiwa na nguvu[4] unaweza kuakhirisha Swalaah ya Adhuhuri na kutanguliza Alasiri, kisha fanya ghuslu na uswali Adhuhuri na Alasiri pamoja kisha akhirisha Magharibi na kutanguliza ‘Ishaa, fanya hivyo, na ufanye ghuslu na ukusanye baina ya Swalaah mbili, fanya hivyo na fanya ghuslu asubuhi na uswali Alfajiri.” Rasuli wa Allaah (ﷺ) amesema: “Mimi hii ninaipendelea zaidi, (yaani kufanya ghuslu kwa kila Swalaah).” [Imetolewa na Al Khamsah (Maimaam watano wa Hadiyth) ila An-Nasaaiy. Na akaisahihisha At-Tirmidhiy, na akaipa daraja la Hasan, Al-Bukhaariy]

118.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا; { أَنَّ أُمَّ حَبِيبَةَ بِنْتَ جَحْشٍ
شَكَتْ إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الدَّمَ، فَقَالَ:
"أَمْكُثِي قَدْرَ مَا كَانَتْ تَحْبِسُكِ حَيْضَتُكَ، ثُمَّ اغْتَسِلِي" فَكَانَتْ
تَغْتَسِلُ كُلَّ صَلَاةٍ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَفِي رِوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: { وَتَوَضَّيْتُ لِكُلِّ صَلَاةٍ } وَهِيَ لِأَبِي
دَاوُدَ وَغَيْرِهِ مِنْ وَجْهِ آخَرٍ.

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Ummu
Habiyyah bint Jahsh[5] alimshtakia Rasuli wa Allaah (ﷺ) damu (iliyokuwa ikitoka zaidi ya kipindi cha

hedhi); akasema: “Kaa kadiri ilivyokuwa hedhi yako inakuzuia kuswali, kisha fanya ghuslu.” Akawa anafanya ghuslu kila Swalaah[6]. [Imetolewa na Muslim]

Na katika Riwaayah ya Al-Bukhaariy: “Tawadha kwa kila Swalaah.” [Pia ameipokea na Abuu Daawuwd na wengine kwa namna nyingine.]

119.

وَعَنْ أُمِّ عَطِيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كُنَّا لَا نَعُدُّ الْكُذْرَةَ
وَالصُّفْرَةَ بَعْدَ الظُّهْرِ شَيْئًا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ، وَأَبُو دَاوُدَ
وَاللَّفْظُ لَهُ

Kutoka kwa Ummu ‘Aatwiyyah[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema:
“Hatukuwa tukihesabu unjano na ukahawia kuwa ni chochote
(majimaji yanayotokea ukeni[8]) baada ya Twahaarah.” [Imetolewa
na Al-Bukhaariy na Abuu Daawuwd, na tamshi hili ni lake]

120.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ الْيَهُودَ كَانُوا إِذَا حَاضَتْ
الْمَرْأَةُ لَمْ يُؤَاكِلُوهَا، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
"اصْنَعُوا كُلَّ شَيْءٍ إِلَّا النِّكَاحَ"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Mayahudi walikuwa hawali na mwanamke wakati ana hedhi, kwa hivyo Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Fanyeni kila kitu (na wake zenu) isipokuwa kujamiiana.” [Imetolewa na Muslim]

121.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَأْمُرُنِي فَأَتَزِرُ، فَيُبَاشِرُنِي وَأَنَا حَائِضٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiniamrisha kuvaa Izaar[9] (gagulo) kisha ananipapasa kwa mahaba[10] wakati nina hedhi.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

122.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الَّذِي يَأْتِي امْرَأَتَهُ وَهِيَ حَائِضٌ قَالَ: {يَتَصَدَّقُ بِدِينَارٍ، أَوْ نِصْفِ دِينَارٍ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ وَابْنُ الْقَطَّانِ، وَرَجَّحَ غَيْرُهُمَا وَقَفَّه

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu mume anayejamiiana na mkewe akiwa na hedhi: “Atoe dinari moja au nusu dinari kama Swadaqah.” [Imetolewa na Al-Khamsah (watano). Wakaisahihisha Al-Haakim na Ibn Al-Qatwaan, na wengine waliita kuwa Mawquwf[11]]

123.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَلَيْسَ إِذَا حَاضَتْ لَمْ تُصَلِّ وَلَمْ تَصُمْ؟} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ فِي حَدِيثٍ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Je si kweli kuwa mwanamke aliye katika hedhi haswali wala hafungi[12]?” [Al-Bukhaariy, Muslim na ni sehemu ya Hadiyth ndefu]

124.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {لَمَّا جِئْنَا سَرَفَ حِضَّتُ، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "إِفْعَلِي مَا يَفْعَلُ

الْحَاجُّ، غَيْرَ أَنْ لَا تَطُوفِي بِالْبَيْتِ حَتَّى تَطْهُرِي" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ فِي حَدِيثٍ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Tulipofika mahali paitwapo Sarif, mimi nilipata hedhi, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akaniambia: “Wewe fanya analolifanya Haji isipokuwa usifanya twawaaf (kutufu Ka’bah) mpaka ukishatwahirika.” [Al-Bukhaariy, Muslim, na ni sehemu ya Hadiyth ndefu]

125.

وَعَنْ مُعَاذٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ سَأَلَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَا يَحِلُّ لِلرَّجُلِ مِنْ امْرَأَتِهِ، وَهِيَ حَائِضٌ؟ قَالَ: "مَا فَوْقَ الْإِزَارِ" { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَضَعَفَهُ

Kutoka kwa Mu’aadh (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuuliza Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kitu gani halali kwa mwanamume kwa mkewe wakati ana hedhi? Akasema: “Kilicho juu ya Izaar[13].” [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaidhoofisha]

126.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَتْ النَّفْسَاءُ تَقْعُدُ فِي عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعْدَ نِفَاسِهَا أَرْبَعِينَ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَاللَّفْظُ لِأَبِي دَاوُدَ وَفِي لَفْظٍ لَهُ: {وَلَمْ يَأْمُرْهَا النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِقِضَاءِ صَلَاةِ النَّفَاسِ} وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Wanawake wenye nifaas zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) walikuwa wakikaa (bila kuswali) kwa siku arubaini[14].” [Imetolewa na Al Khamsah isipokuwa An-Nisaa'iy, na tamshi hili ni la Abuu Daawuud]

Na katika Riwaayah nyengine ya Abuu Daawuud anasema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) hakumuamrisha (mzazi) aliye Swalaah alizoacha wakati wa nifaas yake.” [Aliisahihisha Al Haakim]

[1] Istihaadhawah (damu imtokayo mwanamke ukeni) ni damu inayodumu muda mrefu na inaweza kuwa ni damu ya uzazi au ya hedhi, na huhesabika kuwa ni kutokwa na damu kati kati ya vipindi. Kipindi cha hedhi, kwa mujibu wa ‘Ulamaa ni kutoka siku moja mpaka siku kumi na tano; na kwa mujibu wa wengine ni kutoka siku tatu mpaka siku kumi. Uzoefu unaonyesha kuwa huo usemi wa pili ni sahihi zaidi. Kila mwanamke huwa anafahamu vipindi vyake, na akitokwa damu zaidi ya wakati wake, basi hiyo ni Istihaadhawah.

[2] Asmaa alikuwa mke wa Ja'far bin Abiy Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ). Alihajiri pamoja naye hadi Habashah (Abyssinia Ethiopia), na alimzalia watoto watatu, na kati ya hao ni 'Abdullaah. Baada ya Ja'far (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kufa Shahidi katika vita vya Mut'a, Abuu Bakar Swiddiyq (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuoa Asmaa ambaye alimzalia mtoto mmoja Muhammad. Na baada ya kufariki Abuu Bakar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ), 'Aliy bin Abiy Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuoa Asmaa ambaye alimzalia Yahyaa. 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alizowea kumuuliza Asmaa tafsiri ya ndoto. Alikufa baada ya kifo cha 'Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ).

[3] Hamnah bint Jahsh ni dada wa "Mama wa Waumini", Zaynab bint Jahsh. Alioelewa na Musw'ab bin 'Umayr ambaye alikufa Shahidi katika vita vya Uhud, na baada ya hivyo akaolewa na Twalhah bin 'Ubaydillaah.

[4] Katika Hadiyth hii Hamnah aliamriwa kuoga mara tatu kila siku. Aoge mara moja kwa ajili ya Swalaah za Adhuhuri na Alasiri, na aoge mara ya pili kwa Swalaah za Magharibi na 'Ishaa, na aoge mara ya tatu kwa Swalaah ya Alfajiri. Katika Hadiyth iliyopita, Faatwimah binti Abiy Hubaysh aliamuriwa achukue wudhuu tu kabla ya kila Swalaah. Hii inamaanisha kuwa, kwa mwanamke anayekuwa na Istihaadhwah kuoga siyo lazima, lakini kuchukuwa wudhuu ni lazima kwa kila Swalaah. Kuoga ni bora ikiwa hali ya afya na ya hewa itaruhusu, vinginevyo hakuna haja ya kuoga.

[5] Habiyyah bint Jahsh alikuwa dada mwingine wa "Mama wa Waumini" Zaynab bint Jahsh, naye aliolewa na 'Abdur-Rahmaan bin 'Awf. Mulsim alisimulia kuwa alikuwa na damu iliyodumu miaka saba. Alifariki mnamo mwaka wa 44 A.H.

[6] Ilikuwa ni hatua ya hiari na ya tahadhari tu kwa Umm Habiyyah kuoga kwa kila Swalaah. Uamuzi sahihi kuhusu kadhia hii ni kuoga baada ya hedhi na atawadhe. Kuhusu kutokwa damu kwa muda mrefu mno, ipo amri ya kuosha damu na kuchukua wudhuu katika kila Swalaah.

[7] Ummu ‘Atwiyyah ni jina la Nusaybah Ka’b bint Al-Haarith Al-Ansariyya. Alikuwa ni miongoni mwa Swahaba wa kike maarufu, na alikuwa akiongozana na Nabiyy (ﷺ) vitani akiwauguza wagonjwa na kuwatibu majeruhi. Alipigana katika Vita vya Uhud kama shujaa. Alishuhudia kuoshwa kwa maiti ya binti wa Nabiyy (ﷺ) ambako alieleza na alitusimulia, na Swahaba, Taabi’, ‘Ulamaa wa Basra walirikodi kutoka kwake. Hadiyih yake inahesabika kuwa ndiyo msingi wa kuosha maiti. Alikuwa mmoja wa Swahaba wa kike walioloweza kule Basra.

[8] Katika usimulizi wa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) majimaji ya rangi ya njano au na vumbi yanahesabika kuwa ni damu ya hedhi, lakini Hadiyih hii inasema: **“Tuliyahesabu kuwa siyo kitu.”** Hadiyih hizi mbili zaelekea kujipinga, lakini zote mbili ni sahihi katika muktadha wa kila moja. Ikiwa majimaji ya rangi ya njano au ya vumbi yatajitokeza wakati wa kipindi cha hedhi, yatahesabika kuwa ni “damu ya hedhi.” Lakini yakijitokeza baada ya kipindi cha hedhi basi si chochote kama maneno ya Kiarabu ya بَعْدَ الطُّهْرِ yanavyodokeza.

[9] Vazi linalovaliwa kutoka kiunoni kuenda chini kama gagulo au sketi.

[10] Wale ambao hawazisadiki Hadiyih, yaani wakanushaji wa Sunnah, wanaleta utata na mashaka hapa, na wanawafanya watu wazishuku Hadiyih. Wanasema kuwa tendo la ndoa katika kipindi cha hedhi limekatazwa na Qur-aan lakini kwa mujibu wa Hadiyih hii Nabiyy (ﷺ) (اللَّهُ عَلَيْهِ وَالْآلِ وَسَلَّمَ) alifanya wakati ule, kwa hiyo Hadiyih hiyo siyo sahihi. Maana ya maneno ya ‘Mubaasharat’ ni kugusa na kuukanda mwili kwa mwili, na kwa kifumbo maana yake ni kufanya tendo la ndoa. Katika Hadiyih imewekwa wazi kwamba tendo la ndoa limekatazwa wakati ya

hedhi ya mwanamke. Kwa hivyo ni udanganyifu tu kutafsiri neno hilo ‘mubashaarat’ kuwa ni ‘tendo la ndoa’ badala ya kulitafsiri kuwa ni ‘kushikashika kwa mahaba’ na kuleta mashaka.

[11] Hii ni Hadiyth dhaifu, kwa hivyo wengi wa ‘Ulamaa hawadhani kuwa ni lazima kufidia, ingawa baadhi ya ‘Ulamaa hudhani inafaa kufidia, lakini rai ya kwanza ni sahihi kwa kuwa amri hiyo ni kwa kuhamasisha Swadaqah.

[12] Hii ni sehemu ndogo tu ya Hadiyth ndefu. Alipokuwa akitoa khutbah kwa wanawake Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaambia kuwa dini yao haijakamilika. Walipouliza kwa namna gani, kwa kusema maneno yanayomaanisha kuwa wanawake walio na hedhi wasiswali wala wasifunge Swawm.

[13] Kila kilicho juu ya Izaar (Nguo inayovaliwa chini ya kiuno) inaweza kuwa na maana mbili: kwanza inaweza kuwa na maana ya jimai. Kwa maneno mengine, kila kitu kinaruhusiwa isipokuwa jimai. Pili: ina maana ya ile sehemu inayovaliwa Izaar. Ila maana hii inaweza kupingana na Hadiyth isemayo: “Fanyeni kila kitu isipokuwa jimai.” Kwa hivyo basi ni vizuri kutumia maana ya kwanza.

[14] Hii inamaanisha ni kile kiwango cha juu cha siku za damu ya uzazi, na hakuna kiwango chake cha chini. Laiti ikiendelea zaidi ya siku arubaini, basi itakuwa ni Istihaadhwah (damu ya ugonjwa), ambayo siyo kizuizi kwa Swalaah, wala kufunga Swawm, wala kufanya tendo la ndoa. Kila amri kuhusu damu na uzazi ni sawa na ile ya damu ya hedhi.

كِتَابُ الصَّلَاةِ

Kitabu Cha Swalaah

01-Mlango Nyakati Za Swalaah

بَابُ الْمَوَاقِيتِ

Mlango Nyakati Za Swalaah

127.

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا ، أَنَّ نَبِيَّ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {وَقْتُ الظُّهْرِ إِذَا زَالَتْ الشَّمْسُ، وَكَانَ ظِلُّ الرَّجُلِ كَطُولِهِ مَا لَمْ يَحْضُرِ الْعَصْرُ، وَوَقْتُ الْعَصْرِ مَا لَمْ تَصْفُرْ الشَّمْسُ، وَوَقْتُ صَلَاةِ الْمَغْرِبِ مَا لَمْ يَغِبِ الشَّفَقُ، وَوَقْتُ صَلَاةِ الْعِشَاءِ إِلَى نِصْفِ اللَّيْلِ الْأَوْسَطِ، وَوَقْتُ صَلَاةِ الصُّبْحِ مِنْ طُلُوعِ الْفَجْرِ مَا لَمْ تَطْلُعِ الشَّمْسُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَلَهُ مِنْ حَدِيثِ بُرَيْدَةَ فِي الْعَصْرِ: {وَالشَّمْسُ بَيَضاءُ نَقِيَّةٌ} وَمِنْ حَدِيثِ أَبِي مُوسَى: {وَالشَّمْسُ مُرْتَفَعَةٌ}

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wakati wa Swalaah ya Adhuhuri[1] ni jua linapopinduka (meridani) na kivuli cha mtu kuwa kama urefu wake, madamu haujaingia wakati wa Swalaah ya Alasiri. Wakati wa Swalaah ya Alasiri ni muda jua halijawa njano (machweo). Wakati wa Swalaah ya Magharibi (machweo)[2] ni katika wakati wa mawingu hayajapotea[3]. Wakati wa Swalaah ya

‘Ishaa hadi nusu ya usiku. Wakati wa Swalaah ya Alfajiri ni tangu kuchomoza Alfajiri mpaka wakati wa kuchomoza jua.’ [Imetolewa na Muslim]

Buraydah[4] amesema katika Hadiyth nyengine kuhusu Alasiri kuwa: “Jua likiwa jeupe angavu[5].” [Imetolewa na Muslim]

Na Hadiyth ya Abuu Muwsaa[6] amesema kuhusu wakati wa Swalaah ya Alasiri: “Wakati jua liko juu.”[7] [Imetolewa na Muslim katika Hadiyth ndefu inayosema: “Kisha akamuamrisha akakimu Alasiri”]

128.

وَعَنْ أَبِي بَرْزَةَ الْأَسْلَمِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي الْعَصْرَ، ثُمَّ يَرْجِعُ أَحَدُنَا إِلَى رَحْلِهِ فِي أَقْصَى الْمَدِينَةِ وَالشَّمْسُ حَيَّةٌ، وَكَانَ يَسْتَحِبُّ أَنْ يُؤَخَّرَ مِنَ الْعِشَاءِ، وَكَانَ يَكْرَهُ النَّوْمَ قَبْلَهَا وَالْحَدِيثَ بَعْدَهَا، وَكَانَ يَنْفَتِلُ مِنْ صَلَاةِ الْغَدَاةِ حِينَ يَعْرِفُ الرَّجُلُ جَلِيسَهُ، وَيَقْرَأُ بِالسَّتِّينَ إِلَى الْمِائَةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَعِنْدَهُمَا مِنْ حَدِيثِ جَابِرٍ: {وَالْعِشَاءُ أَحْيَانًا وَأَحْيَانًا: إِذَا رَأَوْهُمْ اجْتَمَعُوا عَجَلًا، وَإِذَا رَأَوْهُمْ أَبْطَأُوا آخَرَ، وَالصُّبْحُ: كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي بِهَا بِغَلَسٍ}

وَلِمُسْلِمٍ مِنْ حَدِيثِ أَبِي مُوسَى: {فَأَقَامَ الْفَجْرَ حِينَ انْشَقَّ
الْفَجْرُ، وَالنَّاسُ لَا يَكَادُ يَعْرِفُ بَعْضُهُمْ بَعْضًا}

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Barzah Al-Aslamiy[8] amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiswali Swalaah ya Alasiri na baada ya Swalaah, mmoja wetu alirejea nyumbani kwake mwisho kabisa wa Madiynah na kufika wakati jua bado linang’aa, na alipenda kuichelewesha Swalaah ya ‘Ishaa, na hakupenda kulala usingizi kabla yake na kuzungumza baada yake.[9] Na baada ya Swalaah ya Fajr alikuwa akitoka wakati mtu aliweza kumtambua mwenzie aliyekaa karibu naye, na alikuwa akisoma Aayah sitini hadi mia za Qur-aan katika Swalaah ya Fajr.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Kwao wawili (Al-Bukhaariy na Muslim) wamepokea Hadiyth ya Jaabir kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiwahisha Swalaah ya ‘Ishaa na mara nyingine akiichelewesha, kila alipowaona watu wamekusanyika ili kuswali ‘Ishaa, aliiswali mapema, na watu wakiwa wamechelewa, naye aliichelewesha. Swalaah ya Fajr aliiswali wakati bado kungali kiza.”[10]

Muslim alimnukuu Abuu Muwsaa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiswali Fajr wakati wa kupambazuka ambapo watu hawakutambuana.”

وَعَنْ رَافِعِ بْنِ خَدِيجٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كُنَّا نُصَلِّي
الْمَغْرِبَ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَيَنْصَرِفُ أَحَدُنَا
وَأَنَّهُ لَيُبْصِرُ مَوَاقِعَ نَبْلِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Raafi' bin Khadiyy[11] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
Tulikuwa tukiswali Magharibi na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
وَسَلَّمَ) halafu mmoja wetu alitoka nje ya Msikiti akaweza kuona
mahali mshale ulipoangukia.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

130.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {أَعْتَمَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ذَاتَ لَيْلَةٍ بِالْعِشَاءِ، حَتَّى ذَهَبَ عَامَّةُ اللَّيْلِ،
ثُمَّ خَرَجَ، فَصَلَّى، وَقَالَ: "إِنَّهُ لَوْ قُتِلَ لَوْلَا أَنْ أَشُقَّ عَلَى
أُمَّتِي"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alichelewesha Swalaah ya ‘Ishaa hadi
sehemu kubwa ya usiku ilipopita, halafu akenda nje akaswali
Swalaah ya ‘Ishaa akasema: “Huu ndio wakati wake[12] ingekuwa
siyo kuogopea mashaka kwa Ummah wangu.” [Imetolewa na
Muslim]

131.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا اشْتَدَّ الْحَرُّ فَأَبْرِدُوا بِالصَّلَاةِ، فَإِنَّ شِدَّةَ الْحَرِّ مِنْ فَيْحِ جَهَنَّمَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Joto likiwa kali lipoze kwa Swalaah[13] kwani ukali wa joto hutoka kwenye pumzi ya Jahannam.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

132.

وَعَنْ رَافِعِ بْنِ خَدِيجٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَصْبَحُوا بِالصُّبْحِ فَإِنَّهُ أَعْظَمُ لِأَجُورِكُمْ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Raafi' bin Khadiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Pambazukeni kwa Swalaah ya Alfajiri[14] kwani hiyo ndio kubwa zaidi kwa ujira wenu.” [Imetolewa na Al-Khamsah na wakaipa daraja la Swahiyh At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

133.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ أَدْرَكَ مِنَ الصُّبْحِ رَكْعَةً قَبْلَ أَنْ تَطْلُعَ الشَّمْسُ فَقَدْ أَدْرَكَ الصُّبْحَ، وَمَنْ أَدْرَكَ رَكْعَةً مِنَ الْعَصْرِ قَبْلَ أَنْ تَغْرُبَ الشَّمْسُ فَقَدْ أَدْرَكَ الْعَصْرَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَلِمُسْلِمٍ عَنْ عَائِشَةَ نَحْوَهُ، وَقَالَ: "سَجْدَةٌ" بَدَل "رَكْعَةٍ". ثُمَّ قَالَ: وَالسَّجْدَةُ إِنَّمَا هِيَ الرَّكْعَةُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuipata Rakaa moja ya Swalaah ya Alfajiri kabla jua halijachomoza, anakuwa ameipata Swalaah ya Alfajiri kwa wakati wake, na mtu anayeswali Rakaa ya Alasiri kabla ya jua halijatua anakuwa ameipata Swalaah ya Alasiri.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Muslim alipokea masimulizi kama hayo kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) na amesema: “Sajdah badala ya Rakaa.” Kisha amesema: “Sajdah inaashiria Rakaa.”

134.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {لَا صَلَاةَ بَعْدَ الصُّبْحِ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ وَلَا صَلَاةَ بَعْدَ الْعَصْرِ حَتَّى تَغِيبَ الشَّمْسُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَلَفْظُ مُسْلِمٍ: {لَا صَلَاةَ بَعْدَ صَلَاةِ الْفَجْرِ}

وَلَهُ عَنْ عُقْبَةَ بْنِ عَامِرٍ: {ثَلَاثُ سَاعَاتٍ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَنْهَانَا أَنْ نُصَلِّيَ فِيهِنَّ، وَأَنْ نَقْبُرَ فِيهِنَّ مَوْتَانَا: حِينَ تَطْلُعُ الشَّمْسُ بَارِغَةً حَتَّى تَرْتَفِعَ، وَحِينَ يَقُومُ قَائِمُ الظَّهِيرَةِ حَتَّى تَزُولَ الشَّمْسُ، وَحِينَ تَتَضَيَّفُ الشَّمْسُ لِلْغُرُوبِ}

وَالْحُكْمُ الثَّانِي عِنْدَ "الْشَّافِعِيِّ" مِنْ:

حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ. وَزَادَ: {إِلَّا يَوْمَ الْجُمُعَةِ} وَكَذَا لِأَبِي دَاوُدَ: عَنْ أَبِي قَتَادَةَ نَحْوُهُ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: "Hakuna Swalaah baada ya Swalaah ya Alfajiri hadi jua kuchomoza[15], wala hakuna Swalaah baada ya Swalaah ya Alasiri hadi jua lizame." [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na tamshi la Muslim amesema: "Hakuna Swalaah baada ya Swalaah ya Alfajiri."

Na Muslim amenukuu Hadiyth ya 'Uqbah bin 'Aamir[16] kuwa: "Nyakati tatu ambazo Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitukataza kuswali wala kuzika[17] wafu wetu: (a) Wakati wa kuchomoza jua mpaka lipae. (b) Wakati jua liko juu kati kati hadi lipinduke. (c) Wakati jua linakaribia kuzama (kuingia Magharibi)."

Hukmu ya pili kwa Ash-Shaafi'y[18] inatokana na Hadiyth ya Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwa Isnaad dhaifu, akaongezea:

“Isipokuwa siku ya Ijumaa.” Kadhalika Abuu Daawuud alisimulia hivyo kutoka kwa Abuu Qataadah.

135.

وَعَنْ جُبَيْرِ بْنِ مُطْعِمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يَا بَنِي عَبْدِ مَنَافٍ، لَا تَمْنَعُوا أَحَدًا طَافَ بِهَذَا الْبَيْتِ وَصَلَّى آيَةً سَاعَةً شَاءَ مِنْ لَيْلٍ أَوْ نَهَارٍ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Jubayr bin Mutw'im[19] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Enyi Baniy ‘Abdil-Manaaf, msimzuie yeyote kutufu Nyumba (Al-Ka’bah) hii na akaswali saa yoyote anayotaka, usiku au mchana.” [Imetolewa na Al-Khamsah, na wakaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

136.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الشَّفَقُ الْحُمْرَةُ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَصَحَّحَ ابْنُ خُزَيْمَةَ وَغَيْرُهُ وَقَفَّهْ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mawingu (ya machweo ya jua) ni wekundu.” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy, na

akaisahihisha Ibn Khuzaymah, na wengine waliipa daraja la Mawquwf]

137.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْفَجْرُ فَجْرَانِ: فَجْرٌ يُحَرِّمُ الطَّعَامَ وَتَحِلُّ فِيهِ الصَّلَاةُ، وَفَجْرٌ تَحْرُمُ فِيهِ الصَّلَاةُ أَيُّ: صَلَاةُ الصُّبْحِ وَيَحِلُّ فِيهِ الطَّعَامُ} رَوَاهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَالْحَاكِمُ، وَصَحَّاحُهُ

وَالْحَاكِمُ فِي حَدِيثِ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ نَحْوُهُ، وَزَادَ فِي الَّذِي يُحَرِّمُ الطَّعَامَ: {إِنَّهُ يَذْهَبُ مُسْتَطِيلًا فِي الْأُفُقِ} وَفِي الْآخِرِ: {إِنَّهُ كَذَنْبُ السَّرْحَانِ}

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Alfajiri ni Alfajiri mbili: Alfajiri moja inaharamisha chakula na inahalalisha Swalaah, na Alfajiri nyingine inaharamisha kuswali ndani yake: yaani Swalaah ya Alfajiri wakati huo chakula kinakuwa halali.” [Imetolewa na Ibn Khuzaymah na Al-Haakim aliyeisahihisha]

Na Al-Haakim alipokea Hadiyth ya Jaabir mfano wake, na ikaongeza katika ambayo inaharamisha kula: “Kumesambaa sana katika pambizo upeo.”

Na katika nyingine amesema: “Ni kama mkia wa mbwa.”

138.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَفْضَلُ الْأَعْمَالِ الصَّلَاةُ فِي أَوَّلِ وَقْتِهَا} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالْحَاكِمُ. وَصَحَّاحُهُ .
وَأَصْلُهُ فِي "الصَّحِيحَيْنِ"

Kutoka kwa Ibn Mas'ud (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Amali bora kabisa ni Swalaah mwanzo wa wakati wake[20].” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na Al-Haakim aliyeisahihiisha] na chanzo chake ni katika Swahiyh mbili.

139.

وَعَنْ أَبِي مَحْذُورَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَوَّلُ الْوَقْتِ رِضْوَانُ اللَّهِ، وَأَوْسَطُهُ رَحْمَةُ اللَّهِ، وَآخِرُهُ عَفْوُ اللَّهِ} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ جِدًّا وَلِلتِّرْمِذِيِّ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عُمَرَ نَحْوُهُ، دُونَ الْأَوْسَطِ، وَهُوَ ضَعِيفٌ أَيْضًا

Kutoka kwa Abuu Mahdhuwrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabi (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wakati wa mwanzo ni radhi ya Allaah, wa katikati yake ni wa Rahmah za Allaah, na wa

mwisho wake ni msamaha wa Allaah.” [Imetolewa na Ad-Daaruqutwniy kwa Isnaad dhaifu sana]

Na At-Tirmidhiy alisimulia hivyo hivyo, na kutokana na Hadiyth ya Ibn ‘Umar, bila kutaja wakati wa kati na kati. [Hii Hadiyth pia ni dhaifu]

140.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا صَلَاةَ بَعْدَ الْفَجْرِ إِلَّا سَجْدَتَيْنِ} أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ، إِلَّا النَّسَائِيُّ

وَفِي رِوَايَةٍ عَبْدِ الرَّزَّاقِ: {لَا صَلَاةَ بَعْدَ طُلُوعِ الْفَجْرِ إِلَّا رَكْعَتَيِ الْفَجْرِ}

وَمِثْلُهُ لِلدَّارَقُطْنِيِّ عَنْ ابْنِ عُمَرَ بْنِ الْعَاصِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna Swalaah baada ya Alfajiri isipokuwa sajdah mbili (Rakaa mbili za Alfajr) [21].” [Imetolewa na Al-Khamsah isipokuwa An-Nasaaiy]

Katika Riwaayah nyingine ‘Abdur-Razzaaq pia alisimulia: “Hakuna Swalaah baada ya kupambazuka Alfajiri isipokuwa Rakaa mbili za Sunnah ya Alfajir[22]i.”

Mfano wa Hadiyth hiyo imepokewa na Ad-Daaruqutwniy kutoka kwa ‘Amr bin Al-‘Aasw.

141.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {صَلَّى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْعَصْرَ، ثُمَّ دَخَلَ بَيْتِي، فَصَلَّى رَكْعَتَيْنِ، فَسَأَلْتُهُ، فَقَالَ: "شُغِلْتُ عَنْ رَكْعَتَيْنِ بَعْدَ الظُّهْرِ، فَصَلَّيْتُهُمَا الْآنَ"، قُلْتُ: أَفَنَقُضِيهِمَا إِذَا فَاتَتْنَا؟ قَالَ: "لَا" { أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ

وَلِأَبِي دَاوُدَ عَنْ عَائِشَةَ بِمَعْنَاهُ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali Alasiri, kisha akaja nyumbani kwangu, akaswali Rakaa mbili, halafu nikamuuliza juu ya hizo, naye akasema: “Nilishughulishwa na Rakaa mbili za Sunnah baada ya Swalaah ya Adhuhuri, kwa hivyo nimeziswali sasa.” Nikasema: Tuzilipe tukizikosa? Akasema: “Hapana[23].” [metolewa na Ahmad]

Naye Abuu Daawuwd amepokea Hadiyth ya ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) yenye maana sawa na hiyo.

[1] Inamaanisha kuwa wakati wa Swalaah ya Adhuhuri ni hadi kivuli kiwe na ukubwa sawa (kutoka wakati jua linapanda mpaka wakati ukubwa wa mtu na wa kivuli chake viwe sawa), na baada ya pale,

wakati wa Swalaah ya ‘Aswr huanza. Baadhi ya ‘Ulamaa wanahesabu wakati wa Swalaah ya Adhuhuri ni mpaka kivuli kiwe na ukubwa mara mbili, lakini hii haijathibitishwa na Hadiyth yoyote sahihi.

[2] Hadiyth hii inasema kuwa, Swalaah ya Maghrib pia ina nyakati mbili, mwanzo na mwisho. Katika Hadiyth ya Jibriyl wakati mmoja tu umetajwa kwa ajili ya Swalaah ya Maghribi mara zote mbili, lakini hii ilikuwa ni wakati wa mwanzo wa Uislaam. Baadaye kule Al-Madiynah, wakati wa Swalaah ya Maghribi ulirefushwa.

[3] الشَّفَقُ Wakati wa mwanga wa jua unapofifia yaani ni ule wekundu katika upeo wa Maghribi wakati wa jioni jua linapotua, kama maelezo yanavyosimuliwa na Ad-Daaraqutniy.

[4] Huyu Buraydah ndiye Abuu ‘Abdillaah Buraydah bin Al-Husayb Al-Aslami. Alisilimu yeye pamoja na wenziwe themanini pale Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipompita yeye wakati akihama kwenda Al-Madiynah. Baadaye alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) baada ya Vita vya Uhud, na akashiriki katika Vita zingine. Na pia alihudhuria Al-Hudaybiyyah na pia Bay’atu Ar-Ridhwaan. Alilowea Basra, kisha akaenda na msafara hadi Khurasaan na akalowea Marwa alikofia na akazikwa mnamo mwaka 62 au 63 A.H.

[5] Inamaanisha kuwa Swalaah ya ‘Aswr ni sharti iswaliwe mapema. Baada ya kivuli chenye ukubwa sawa, wakati unatosheleza kuswali rakaah nne tu ambayo ndiyo kawaida kati ya Swalaah ya Dhuhuri na ya ‘Aswr. Baada ya hapo, wakati wa Swalaah ya ‘Aswr huanza.

[6] Abuu Muwsaa ndiye ‘Abdullaah bin Qays Al-Ash’ariyy aliyekuwa mmoja wa Swahaba maarufu kabisa. Alihamia Habasha

(Abyssinia) na baadaye akaja kwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kule Khaybar. Aliteuliwa kutawala Zabid na ‘Aden, na kisha akawa Gavana wa ‘Umar kule Kuwfah na Basra. Alisaidia kuikomboa Tatar na miji mingine kadhaa. Huenda alifariki mnamo mwaka 42 A.H

[7] Simulizi zote zilizotajwa zimethibitisha kuwa kila Swalaah ina “Wakati wa mwanzo” na “Wakati wa mwisho” kuiswali Swalaah ile; lakini kila Swalaah sharti iswaliwe katika wakati wake wa mwanzo.

[8] Abuu Barzah Al-Aslamiyy ndiye Nadla bin ‘Ubayd. Alisilimu mapema sana na akashuhudia kutekwa kwa Makkah na Vita zingine muhimu. Alilowea Basra, na baadaye Khurasaan, na akafia Marwa au Basra mnamo mwaka 60 au 64 A.H.

[9] Baada ya Swalaah ya ‘Ishaa imekatazwa kuongea. Sababu ya katazo hili ni kwamba dhambi za Muumini zimesamehewa baada ya kuswali, na bora kuenda kitandani kuliko kuongea na kushiriki katika mambo ya kidunia. Baada ya kuswali ‘Ishaa, mtu kuenda zake kulala kunampa faida maradufu; kwanza ni kujiepusha na dhambi, na pili ubora Swalaah ndiyo ihesabiwe kuwa ni tendo lake la mwisho kabla hajalala.

[10] Kuhusu wakati wa Swalaah ya Fajr, yapo maoni tofauti ya Swahaba wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Katika Hadiyih hii, hilo neno la Kiarabu la غَلَسَ inamaanisha wakati ambao kupambazuka kunaonekana katika giza la usiku.

[11] Raafi’ bin Khadiyy ndiye Ansari aliyeitwa Abuu ‘Abdillaah. Alikosa Vita ya Badr kwa sababu ya umri wake kuwa mdogo, lakini akashiriki katika Vita ya Uhud na Vita vilivyofuata. Alifariki mnamo mwaka wa 73 au 74 A.H akiwa na umri wa miaka 86.

[12] Ni ubora kuiswali Swalaah ya ‘Ishaa wakati wa mwisho kadiri iwezekanavyo. Amri hii ni maalumu kwa Swalaah ya ‘Ishaa tu, na siyo kwa Swalaah nyingine yoyote. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akingoja na kuichelewesha Swalaah hii.

[13] Kuna maoni tofauti kuhusu kuswali Dhuhuri mapema au mwishoni wakati wa majira ya joto. Lakini ni sawa kuichelewesha kidogo hadi mtu aweze kutembea katika vivuli vya kuta. Kwa mujibu wa Abuu Daawud na An-Nasaaiy: “Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiichelewesha Swalaah ya Dhuhuri hadi kivuli kilipokuwa na urefu wa hatua tatu au tano.”

[14] Hii inamaanisha kuwa mwanga wa Alfajiri sharti uonekane waziwazi na kusiweko shaka yoyote juu yake. Kwa hivyo Hadiyih hii haipingani na hiyo Hadiyih ya “Giza” hapo nyuma. Kipengele kingine ni kuwa Swalaah sharti ianze kuswaliwa wakati ikiwa giza, na visomo virefushwe mpaka mwanga wa Alfajiri uonekane waziwazi.

[15] . Maana yake hii ni kuwa, tangu kunapopambazuka mpaka kuchomoza jua, na tangu ‘Asr hadi jua linapokuchwa, Swalaah za khiari (Nawaafil) zozote haziruhusiwi. Rakaah mbili kabla ya Swalaah ya faradhi ya Fajr hazimo katika amri hii, kama ilivyothibitishwa kutoka kwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Ingawa Rakaah hizi mbili huswaliwa kabla ya Swalaah ya faradhi (Fajr), ukizikosa hizi unaweza kuziswali baada ya Swalaah ya fardhi kama ilivyoripotiwa katika At-Tirmidhiy.

[16] ‘Uqbah bin ‘Aamir alikuwa ni Junani aliyepewa jina la utani Abuu Hammad au Abu ‘Aamir. Alisilimu, akahama na kuandamana

na Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mwanzoni kabisa. Aliisoma sana Qur-aan na alikuwa mtaalamu wa Kanuni za Shariy'ah na mirathi, na alikuwa msomi na mshairi. Alipewa ardhi Basra, na alishiriki katika Siffin pamoja na Mu'aawiyah. Baadaye aliitawala Misri kwa niaba ya Mu'aawiyah kwa miaka mitatu, na akawa mkuu wa misafara ya baharini. Alifariki mwaka 58 A.H. kule Misri, na akazikwa Al-Muqtam.

[17] Hapa, "Kuzika" maana yake ni "Swalaah za maiti". Swalaah za maiti zisiswaliwe katika nyakati hizo, lakini kumzika maiti inaruhusiwa. Lakini kwa mujibu wa Wanazuoni wengine, hata kuzika hakuruhusiwi. Kwa hivyo, katika hali hizo, inamaanisha kuwa hata maziko yasifanyike katika nyakati hizo. Lakini iwapo nyakati hizi zimewadia katikati ya shughuli za maziko, au hakuna njia nyingine, basi kuzika kunaruhusiwa.

[18] Amri ya pili maana yake wakati wa katikati ya siku, ambapo hakuna Swalaah inayoruhusiwa kuswaliwa wakati huu. Lakini Ijumaa haimo katika amri hii. Siku za Ijumaa inaruhusiwa kuswali wakati jua liko juu kabisa, kama inavyodhihirisha Hadiyith iliyoripotiwa na Abuu Hurayrah.

[19] Jubayr bin Mutw'im ndiye Abuu Muhammad au Abuu 'Umayyah Jubayr bin Mutw'im bin 'Aad bin Nawfal Al-Quraysh. Alikuwa mstahamilivu sana, mjuzi wa ukoo wa Maquraysh. Alisilimu kabla ya Fat-h (kutekwa kwa Makkah) na alilowea Al-Madiynah, na akafia huko mnamo mwaka 54 au 57 au 59 A.H.

[20] Katika Hadiyith hii, Swalaah inayoswaliwa katika nyakati zake za mwanzo huhesabika kuwa ni tendo bora sana. Katika Hadiyith zingine, Iymaan, Swadaqah na Jihaad huhesabika kuwa matendo bora sana. Hizi Hadiyith zinaonyesha Iymaan ni tendo la sifa, Swalaah ni tendo la mwili, Swadaqah ni tendo la mali, na Jihaad ni

tendo la ujana na afya. Kwa hivyo haya yote ni matendo makubwa na bora kwa namna zake na mahala pake; na hakuna mapingano.

[21] Maana yake ni kwamba, baada ya kupambazuka, Swalaah za khiari (Nawaafil) haziruhusiwi, lakini Rakaa mbili za Sunnah zinakubaliwa, na zinaweza kuswaliwa baada ya Swalaah ya Fajr, kama rejeo la At-Tirmidhiy lilivyotaja hapo nyuma

[22] Hizo Rakaa mbili ni zile za Sunnah kabla ya Swalaah ya faradhi ya Fajr, ambayo Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kamwe hakuwa anaikosa hata iwe baada ya kupambazuka, kama ilivyoonyeshwa na Hadiyth hii na Hadiyth zingine.

[23] Hadiyth hii inatuarifu kwamba, baada ya Swalaah ya ‘Aswr, kuswali Swalaah za ziada au za khiari tulizozikosa ni kwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) tu, watu wengine hawaruhusiwi kulipa Swalaah za khiari. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliiswali Swalaah ile kwa sababu watu fulani wa kabila la Abdul-Qays walimzuru na walileta vitu vya Swadaqah, kwa hivyo ziara yao ile na ugawanyaji wa vitu walivyoleta ulimchelewesha.

02-Mlango Wa Adhaan

بَابُ الْأَذَانِ

02-Mlango Wa Adhaan[1]

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدِ بْنِ عَبْدِ رَبِّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {طَافَ بِي وَأَنَا نَائِمٌ رَجُلٌ فَقَالَ: تَقُولُ: "اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ، فَذَكَرَ الْأَذَانَ بِتَرْبِيعِ التَّكْبِيرِ بغيرِ تَرْجِيعٍ، وَالْإِقَامَةَ فُرَادَى، إِلَّا قَدْ قَامَتِ الصَّلَاةُ قَالَ: فَلَمَّا أَصْبَحْتُ أَتَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: "إِنَّهَا لَرُؤْيَا حَقٌّ..." } الْحَدِيثُ. أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ

وَزَادَ أَحْمَدُ فِي آخِرِهِ قِصَّةَ قَوْلِ بِلَالٍ فِي آذَانِ الْفَجْرِ: {الصَّلَاةُ خَيْرٌ مِنَ النَّوْمِ}

وَلِابْنِ خُزَيْمَةَ: عَنْ أَنَسٍ قَالَ: {مِنْ السُّنَّةِ إِذَا قَالَ الْمُؤَذِّنُ فِي الْفَجْرِ: حَيَّ عَلَى الْفَلَاحِ، قَالَ: الصَّلَاةُ خَيْرٌ مِنَ النَّوْمِ}

رَضِيَ اللَّهُ (Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Zayd bin ‘Abdi-Rabbih[2]) amesema: Mtu mmoja alinitembelea wakati nimelala[3], akaniambia: Sema:

اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ

“Allaahu Akbar, Allaahu Akbar” (Allaah ni Mkubwa zaidi, Allaah ni Mkubwa zaidi). Akataja Adhaan kwa tamko la

اللَّهُ أَكْبَرُ

“Allaahu Akbar”

mara nne bila Tarjiy’[4] na Iqaamah mara moja, isipokuwa

قَدْ قَامَتِ الصَّلَاةُ

“Qad Qaamati Swalaah”[5]

(Swalaah imekwishakimiwa), ‘Abdullaah akasema: Asubuhi yake nilikwenda kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) naye akasema: “Hiyo ni ndoto ya kweli.” [Hadiyth hii imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuwd, na wakaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Khuzaymah]

Ahmad aliongeza mwishoni wa Hadiyth hiyo, Hadiyth ya msemu wa Bilaal[6] katika Adhaan ya Alfajiri:

الصَّلَاةُ خَيْرٌ مِنَ النَّوْمِ

“*Asw-Swalaatu khayrun minan-nawm* (Swalaah ni bora kuliko usingizi).”

Ibn Khuzaymah alisimulia kuwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Ni Sunna Muadhini anaposema:

حَيٍّ عَلَى الْفَلَّاحِ

“*Hayya ‘alal falaah*” (Njooni kwenye kufaulu), aongeze:

الصَّلَاةُ خَيْرٌ مِنَ النَّوْمِ

“*Asw-Swalaatu khayrun minan-nawm*”
(Swalaah ni bora kuliko usingizi).”

عَنْ أَبِي مَحْذُورَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {عَلَّمَهُ الْأَذَانَ، فَذَكَرَ فِيهِ التَّرْجِيعَ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ. وَلَكِنْ ذَكَرَ التَّكْبِيرَ فِي أَوَّلِهِ مَرَّتَيْنِ فَقَطْ وَرَوَاهُ الْخَمْسَةُ فَذَكَرُوهُ مُرَبَّعًا

Kutoka kwa Abuu Mahdhuwrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:

“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimfundisha Adhaan, na yeye (msimuliaji) akataja Tarjiy’ ndani yake.” [Imetolewa na Muslim, lakini alitaja Takbiyra, mwanzo wake mara mbili tu^[7]]

[Imetolewa na Al-Khamsah, lakini wamesema Takbiyra hutajwa mara nne]

144.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَمَرَ بِلَالٌ أَنْ يَشْفَعَ الْأَذَانَ، وَيُوتِرَ الْإِقَامَةَ، إِلَّا الْإِقَامَةَ، يَعْنِي قَوْلَهُ: قَدْ قَامَتِ الصَّلَاةُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَلَمْ يَذْكُرْ مُسْلِمٌ الْإِسْتِثْنَاءَ وَلِلنَّسَائِيِّ: {أَمَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِبِلَالٍ}

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Bilaal aliamrisha aitamke Adhaan kwa shufwa (mara mbili)[8], na Iqaamah kwa witr[9] isipokuwa “*Qad Qaamati Swalaah*” (yaani Swalaah imekwishakimiwa).” [Al-Bukhaariy, Muslim; lakini Muslim hakutaja huko kuvua]

Na An-Nasaaiy alipokea: “Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuamrisha Bilaal.”

145.

وَعَنْ أَبِي جُحَيْفَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {رَأَيْتُ بِلَالًا يُؤَدِّنُ
وَأَتَتَّبِعُ فَاهُ، هَاهُنَا وَهَاهُنَا، وَإِصْبَعَاهُ فِي أُذُنَيْهِ} رَوَاهُ
أَحْمَدُ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ
وَلِابْنِ مَاجَةَ: وَجَعَلَ إِصْبَعَيْهِ فِي أُذُنَيْهِ
وَلِأَبِي دَاوُدَ: {لَوَى عُنُقَهُ، لَمَّا بَلَغَ "حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ"
يَمِينًا وَشِمَالًا وَلَمْ يَسْتَدِرْ}
وَأَصْلُهُ فِي الصَّحِيحَيْنِ

Kutoka kwa Abuu Juhayfah[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Nimemuona Bilaal akiadhini, nami nilikuwa nikifuatisha kwa
kumtazama mdomo wake akiugeuza upande huu (kuume), na upande
ule (kushoto)[11], kaweka vidole vyake masikioni.” [Imetolewa na
Ahmad na At-Tirmidhiy aliyeipa daraja la Swahiyh]

Na katika mapokezi ya Ibn Maajah: “Na aliweka vidole vyake viwili
kwenye masikio yake.”

Na mapokezi ya Abuu Daawuud: “Aligeuza shingo yake kuumeni na
kushotoni alipofika: “Hayya ‘alasw-Swalaah” (njoo katika
Swalaah), na hakugeuza mwili wake.” Na chanzo chake ni katika
Swahiyh mbili.

146.

وَعَنْ أَبِي مَحْذُورَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَعْجَبَهُ صَوْتُهُ، فَعَلَّمَهُ الْأَذَانَ } رَوَاهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Abuu Mahdhuwrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipenda sauti yake[12] kwa hivyo akamfundisha Adhaan.” [Imetolewa na Ibn Khuzaymah]

147.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { صَلَّيْتُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْعِيدَيْنِ، غَيْرَ مَرَّةٍ وَلَا مَرَّتَيْنِ، بِغَيْرِ أَذَانٍ وَلَا إِقَامَةٍ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَنَحْوُهُ فِي الْمُتَّفَقِ: عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، وَغَيْرُهُ

Kutoka kwa Jaabir bin Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema:
“Nimeswali na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ‘Iyd mbili, siyo mara moja au mara mbili tu[13], bila Adhaan wala Iqaamah.”
[Imetolewa na Muslim]

Hadiyth kama hiyo imo katika Al-Bukhaariy na Muslim kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) na wengineo.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ فِي الْحَدِيثِ الطَّوِيلِ، {فِي نَوْمِهِمْ عَنْ الصَّلَاةِ ثُمَّ أَذَّنَ بِلَالٌ، فَصَلَّى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَمَا كَانَ يَصْنَعُ كُلَّ يَوْمٍ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَلَهُ عَنْ جَابِرٍ: {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَتَى الْمُزْدَلِفَةَ فَصَلَّى بِهَا الْمَغْرِبَ وَالْعِشَاءَ، بِأَذَانٍ وَاحِدٍ وَإِقَامَتَيْنِ}

وَلَهُ عَنْ ابْنِ عُمَرَ: {جَمَعَ بَيْنَ الْمَغْرِبِ وَالْعِشَاءِ بِإِقَامَةٍ وَاحِدَةٍ}

زَادَ أَبُو دَاوُدَ: {لِكُلِّ صَلَاةٍ}

وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ: {وَلَمْ يُنَادِ فِي وَاحِدَةٍ مِنْهُمَا}

Kutoka kwa Abuu Qataadah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) katika Hadiyith ndefu kuhusu: Maswahaba kulala kwao wakapitwa na Swalaah, kisha Bilaal akaadhini na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaswalisha kama alivyokuwa akifanya kila siku[14].” [Imetolewa na Muslim]

Na Jaabir alihadithia: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipofika Muzdalifah[15] aliswali hapo Maghrib na ‘Ishaa kwa Adhaan moja na Iqaamah mbili.”

Alihadithia Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikusanya Swalaah ya Maghrib na ya ‘Ishaa kwa Iqaamah moja.”

Na Abuu Daawuud akaongezea: “Kwa kila Swalaah[16].”

Na katika Riwaayah nyingine: “Adhaan haikuadhiniwa katika Swalaah yoyote kati ya hizo mbili.”

149.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ، وَعَائِشَةَ قَالَا: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ بِلَالًا يُؤَذِّنُ بَلِيلٌ، فَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى يُنَادِيَ ابْنُ أُمِّ مَكْتُومٍ}، وَكَانَ رَجُلًا أَعْمَى لَا يُنَادِي، حَتَّى يُقَالَ لَهُ: أَصْبَحْتَ، أَصْبَحْتَ {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَفِي آخِرِهِ إِدْرَاجٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar na ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) wamesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Bilaal huadhini usiku[17], kwa hivyo kuleni na kunyweni mpaka Ibn Ummi Maktuwm[18] aadhini.” Na Ibn Ummi Maktuwm alikuwa kipofu na kwa hivyo hakuadhini mpaka aambiwe: “Kumekucha, kumekucha.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika sehemu yake ya mwishoni mwake kuna Idraaj[19]

150.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ: {إِنَّ بِلَالاً أَدْنَقَبْلَ الْفَجْرِ، فَأَمَرَهُ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يَرْجِعَ، فَيُنَادِي: "أَلَا إِنَّ الْعَبْدَ نَامَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَضَعَّفَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Bilaal aliadhini kabla ya kupambazuka, na Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akamwambia arejee[20] na aadhini: Mja wa Allaah (Yaani Bilaal), amelala (na hiyo ndiyo sababu ya kosa lile).” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na ikapewa daraja la dhaifu]

151.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا سَمِعْتُمُ النَّدَاءَ، فَقُولُوا مِثْلَ مَا يَقُولُ الْمُؤَذِّنُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِلْبُخَارِيِّ: عَنْ مُعَاوِيَةَ

وَلِمُسْلِمٍ: {عَنْ عُمَرَ فِي فَضْلِ الْقَوْلِ كَمَا يَقُولُ الْمُؤَذِّنُ كَلِمَةً كَلِمَةً، سِوَى الْحَيَعَتَيْنِ، فَيَقُولُ: "لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ"} بِاللَّهِ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriy (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) kwamba Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:

“Mkisikia Adhaan semeni[21] kama anavyosema Muadhini.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Al-Bukhaariy amepokea hivyo hivyo kutokana na uslimulizi wa Mu’aawiyah.

Na Muslim alipokea usimulizi wa ‘Umar kuhusu fadhila ya kusema kama anavyotamka Muadhini isipokuwa pale Muadhini anaposema: “Hayya ‘alasw-Swalaah” (Njoo katika Swalaah) na “Hayya ‘alal-falaah” (Njoo kwenye kufaulu) ambapo mtu hutakiwa aseme: “Laa hawla wa laa quwwata illaa biLLaah” (Hakuna uwezo wala nguvu ila kwa msaada wa Allaah).”

152.

وَعَنْ عُثْمَانَ بْنِ أَبِي الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ قَالَ : يَا رَسُولَ اللَّهِ اجْعَلْنِي إِمَامَ قَوْمِي . قَالَ : "أَنْتَ إِمَامُهُمْ، وَاقْتَدِ بِأَضْعَفِهِمْ، وَاتَّخِذْ مُؤَدِّنًا لَا يَأْخُذُ عَلَى أَذَانِهِ أَجْرًا { أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Uthmaan bin Abiy Al-‘Aasw[22] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Ee Rasuli wa Allaah! Niteue niwe Imaam wa watu wangu. Akasema: “Wewe ni Imaam wao, zingatia wadhaifu wao zaidi[23], na uteue Muadhini asiye chukua ujira[24] kutokana na kuadhini.” [Imetolewa na Al-Khamsah, na aliipa daraja la Hasan At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Al-Haakim]

153.

وَعَنْ مَالِكِ بْنِ الْحُوَيْرِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ لَنَا النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {وَإِذَا حَضَرَتِ الصَّلَاةُ فَلْيُؤْذِنْ لَكُمْ أَنْحَادُكُمْ . . . } الْحَدِيثَ أَخْرَجَهُ السَّبْعَةُ

Kutoka kwa Maalik bin Al-Huwayrith[25] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ametuambia: “Ukifika wakati wa Swalaah, mmoja wenu aadhini[26]....” [Imetolewa na Maimaam Saba]

154.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لِبِلَالٍ : {إِذَا أَذْنَتَ فَتَرَسَّلْ ، وَإِذَا أَقَمْتَ فَاحْدُرْ ، وَاجْعَلْ بَيْنَ أَذَانِكَ وَإِقَامَتِكَ قَدْرَ مَا يَفْرُغُ الْأَكِلُ مِنْ أَكْلِهِ } الْحَدِيثَ . رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَضَعَفَهُ .

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimwambia Bilaal: “Unapoadhini, tamka taratibu, na unapokimu kimu haraka, na acha muda baina ya Adhaan na Iqaamah kiasi cha mlaji amalize kula[27] kwake.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy, na akaidhoofisha]

155.

وَلَهُ : عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : { لَا يُؤَذِّنُ إِلَّا مُتَوَضِّئٌ } وَضَعَّفَهُ أَيْضًا

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asiadhini isipokuwa mwenye wudhuu[28].” [Pia ameidhoofisha]

156.

وَلَهُ : عَنْ زِيَادِ بْنِ الْحَارِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { وَمَنْ أَدَّنَ فَهُوَ يُقِيمُ } وَضَعَّفَهُ أَيْضًا

Tena At-Tirmidhiy amepokea kuwa Ziyaad bin Al-Haarith[29] (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mwenye kuadhini ndiye mwenye kukimu[30].” [Pia ameidhoofisha]

157.

وَلِأَبِي دَاوُدَ: فِي حَدِيثِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدٍ أَنَّهُ قَالَ : أَنَا رَأَيْتُهُ يَعْني : الْأَذَانُ وَأَنَا كُنْتُ أُرِيدُهُ . قَالَ : "فَأَقِمِ أَنْتَ " وَفِيهِ ضَعْفٌ أَيْضًا

Abuu Daawuwd amepokea kutokana na Hadiyth ya ‘Abdullaah bin Zayd kuwa amesema: “Niliiona (yaani Adhaan) ndotoni, nami

nilikuwa naitaka (kuitumia), Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ) akasema: “Kimu wewe (Swalaah).” [Hadiyth hii pia ni dhaifu]

158.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْمُؤَذِّنُ أَمْلَكُ بِالْأَذَانِ ، وَالْإِمَامُ أَمْلَكُ بِالْإِقَامَةِ} رَوَاهُ ابْنُ عَدِيٍّ وَضَعَّفَهُ وَلِلْبَيْهَقِيِّ نَحْوُهُ : عَنْ عَلِيٍّ مِنْ قَوْلِهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muadhini ana haki zaidi ya kuadhini na Imaam ana haki zaidi ya kukimu.” [Imetolewa na Ibn ‘Adiy na akaidhoofisha]

Na Al-Bayhaqiyy mfano wake: kutoka kwa ‘Aliy kutoka katika kauli yake.

159.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا يُرَدُّ الدُّعَاءُ بَيْنَ الْأَذَانِ وَالْإِقَامَةِ} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Dua baina ya Adhaan na Iqaamah haikataliwi.” [Imetolewa na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

160.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : {مَنْ قَالَ حِينَ يَسْمَعُ النِّدَاءَ : اَللّٰهُمَّ رَبِّ هَذِهِ الدَّعْوَةِ التَّامَّةِ، وَالصَّلَاةِ الْقَائِمَةِ، اَتِ مُحَمَّدًا الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ، وَابْعَثْهُ مَقَامًا مَحْمُودًا الَّذِي وَعَدْتَهُ، حَلَّتْ لَهُ شَفَاعَتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kusema anaposikia Adhaan:

اَللّٰهُمَّ رَبِّ هَذِهِ الدَّعْوَةِ التَّامَّةِ، وَالصَّلَاةِ الْقَائِمَةِ، اَتِ مُحَمَّدًا الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ، وَابْعَثْهُ مَقَامًا مَحْمُودًا الَّذِي وَعَدْتَهُ

Allaahumma Rabba haadhihi-d-da'watit-taamah, wasw-Swaalaatil qaaimah, aati Muhammada al-wasiylata wal fadhwiylah, wab-'ath-hu maqaaman mahmuwdan alladhiy wa'adtah[31].

(Ee Allaah, Rabb wa mwito huu uliotimia, na Swalaah iliyosimama, mpe (Nabiy) Muhammad al-Wasiylah (cheo, daraja), na fadhila[32], na mfikishe daraja yenye kuhimidiwa, ambayo Umemuahidi).

Ash-Shafaa'ah (Uombezi) wangu umehalalika kwake Siku ya Qiyaamah.” [Imetolewa na Al-Arba'ah]

[1] Maneno yanayounda “Adhaan” yamepangiliwa Kiilaahi. Hayaruhusiwi kuongezwa, kupunguzwa wala kubadilishwa. Maneno hayo alipewa ‘Abdullaah bin Zayd Answaariy na ‘Umar bin Khattwaab na Malaika ndotoni, na yakathibitishwa na Nabiy (ﷺ), yakakwezwa kufikia hadhi ya Wahyi. Kuna dalili pia katika Qur-aan juu ya hili.

[2] ‘Abdullaah bin Zayd ni Answaar Mkhariji (wa Al-Madiynah). Alipewa jina la utani, Abuu Muhammad. Alishuhudia Al-‘Aqaba, Badr na Vita vingine muhimu. Alionyeshwa ndotoni namna ya kuita watu kuenda kuswali katika mwaka wa kwanza wa Hijrah, baada ya kujengwa kwa Msikiti wa Rasuli wa Allaah (ﷺ). Alifariki mwaka 32 A.H. akiwa na umri wa miaka 64.

[3] Waislaam walipoongezeka, tatizo la kuwaita watu waende kuswali likajitokeza. Mapendekezo mengi yalitolewa. Wengine wakapendekeza kupuliza kombe (gamba ya wanyama wa baharini) au pembe, na Nabiy (ﷺ) akasema hiyo ilikuwa njia ya Mayahudi. Wengine wakapendekeza kuwasha moto, Nabiy (ﷺ) akasema hiyo ilikuwa njia ya Majusi. Hawakufikia uamuzi wowote. Lakini usiku ule, ‘Abdullaah bin Zayd akamuota mtu amesimama na kombe mkononi mwake. ‘Abdullaah akamuuliza iwapo anaweza kumuuzia lile. Yule mtu akamuuliza ni kwa ajili gani? ‘Abdullaah akajibu kwa kuwaitia Waislaam kuja kuswali. Akamuuliza iwapo anataka amfunze njia nzuri kuliko hiyo; na akasoma maneno ya Adhaan. Asubuhi yake ‘Abdullaah akamuambia Rasuli wa Allaah (ﷺ), naye akasema ndoto ilikuwa ni ya kweli.

[4] تَرْجِيع (Kurudia) Ni kutamka maneno ya Shahada mbili Yaani

أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمدا رسول الله

mara mbili kwa sauti ya chini, halafu utamke kwa sauti kubwa.

[5] Katika Iqaamah (mwito wa kuanza Swalaah), maneno yote ya Takbiyr (kumtukuza Allaah) lakini hapa ina maana ya Iqaamah hutamkwa mara moja isipokuwa maneno

قد قامت الصلاة

(yaani Swalaah iko tayari kuanza) ambayo hutamkwa mara mbili.

[6] Bilaal bin Rabbaah, mtumwa aliyeachwa huru wa Banu Taym. Alisilimu mapema sana, na akateswa sana katika jihaad ya njia za Allaah (عز وجل). Alipigana katika Vita ya Badr na Vita vingine vikuu. Alikuwa muadhini wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na hakuadhini kwa ajili ya mtu yeyote mwingine isipokuwa mara moja aliporejea Madiynah kutoka Damascus alikolowea. Inasemekana hakuwahi kuimaliza Adhaan hiyo kwa sababu ya kelele za Swahaba waliokuwa wakilia waliposikia sauti ya Bilaal, kwa sababu ya mazowea na kumbukumbu. Bilaal alifia Shaam mnamo mwaka 17 au 18 au 20 A.H akiwa na umri wa miaka sitini hivi, na hakuacha watoto wowote.

[7] Mwanzo wa Adhaan, maneno haya

اللهُ أَكْبَرُ

Allaahu Akbar (Allaah ni Mkuu Zaidi kuliko wote)

hutakiwa yarudiwe mara nne. Kuyarudia mara mbili tu siyo sahihi kama walivyosimulia Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad)

[8] Adhaan iliyo na Tarji' au hata isiwe na Tarji' inaruhusiwa, na hali kadhalika Iqaamah nayo inaruhusiwa ikiwa mara moja au mara mbili.

Lakini ni vizuri kuitangaza Adhaan pamoja na Tarji' na kuitangaza Iqaamah bila marudio.

[9] Inamaanisha kwamba, maneno

قد قامت الصلاة

(Yaani Swalaah iko tayari kuanza) yarudiwe mara mbili, na maneno mengine yatangazwe mara moja tu.

[10] Huyu Abuu Juhayfah ndiye Wahaab bin 'Abdillaah As-Suwa'i Al-'Aamir, ambaye alikuwa miongoni mwa Swahaba vijana. Alilowea Kufa. 'Aliy alimfanya awe mkuu wa Baytul-Maal; na alishuhudia pamoja naye vita vyote. Alifia Kuwfah mnamo mwaka 74 A.H.

[11] Wakati anatamka maneno haya

حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ

(njoo katika Swalaah) na

حَيَّ عَلَى الْفَلَاحِ

(njoo kwenye kufaulu),

kugeuza uso kuume na kisha kushoto ni Sunnah. Kugeuza mwili mzima hakuruhusiwi. Hadiyth zinazokataza kugeuka, zinamaanisha kugeuza mwili wote na siyo kugeuza uso tu.

[12] Inamaanisha kuwa awe anateuliwa Muadhini mwenye sauti nzuri.

[13] Hii ina maana kwamba, Swalaah za 'Iyd zote mbili (ya Fitwr na ya Adhwhaa) huswaliwa bila Adhaan wala Iqaamah

[14] Ikiwa Swalaah ya Qadhwa (Swalaah inayolipwa) inataka kuswaliwa kwa jamaa, basi ni Sunnah kutoa Adhaan kwa ajili yake. Siku moja Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na Swahaba zake walisafiri usiku sana.

Waliposimama na wakataka kuenda kulala, walikuwa hawana hakika ya kuwahi kuamka Alfajiri iliyofuata ili kuiswali. Kwa hivyo wakamuomba Bilaal abakie macho, lakini naye akazidiwa na usingizi akalala. Nabiyy (ﷺ) alikuwa wa kwanza kuamka baada ya jua kuchomoza akawaamsha Swahaba. Walisogelea pembeni wakaswali baada ya kuadhini.

[15] Muzdalifah ni mahali kati ya Makkah na ‘Arafah. Usiku wa tarehe 9 kuamkia tarehe 10 ya mwezi wa Dhul-Hijjah, baada ya kurudi kutoka ‘Arafah, Mahujaji hubakia hapo. Swalaah za Maghribi na ‘Ishaa huswaliwa hapo kwa pamoja kwa Adhaan moja tu, bali hutolewa Iqaamah moja kwa kila Swalaah. Hii yamaanisha kuwa, kila panaposwaliwa Swalaah ya jamaa, lazima ikimiwe.

[16] Hadiyth hii inatofautiana na Hadiyth iliyosimuliwa na Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) ambapo imetajwa Adhaan moja na Iqaamah mbili.

[17] Katika mwezi wa Ramadhwaan Nabiyy (ﷺ) aliteua Waadhini wawili, wa kwanza kuadhini ili kujulisha wakati wa kula daku, na Muadhini wa pili kuadhini ili kuwaita watu waende kuswali.

[18] Ibn Umm Maktuwm ndiye ‘Amr au ‘Abdullaah bin Qays Al-Qurayshiy Al-‘Aamir, yule mtu kipofu anayetajwa katika Suwrah ‘Abasa. Alisilimu zamani na akafanya Hijrah (kuhama). Nabiyy (ﷺ) alimteua yeye awe Mkuu wa Madiynah mara 13 akiwaswalisha watu. Alikufa shahidi kule Al-Qadisiya wakati akishika bendera siku ile.

[19] Neno إِدْرَاجٌ Idraaj (kilichoongezwa) linamaanisha kwamba, maneno hayo: "Na alipokuwa kipofu." Hayakusemwa na Nabiyy (ﷺ) mwenyewe, bali msimulizi aliongeza maneno haya kwa utashi wake mwenyewe.

[20] Hii inamaanisha kuwa kama kumeadhiniwa kabla ya wakati, kuadhiniwe tena ukifika wakati wake sahihi.

[21] Ni amri kwamba, tunaposikia Adhaan, watu warudie yale maneno ya Adhaan kwa kujibu kila mara, kama mtu anao wudhuu au asiwe nao, awe msafi bila najsi au awe na najsi ya kijinsia; lakini wakati mtu anafanya tendo la ndoa au akiwa chooni, haifai kujibu.

[22] ‘Uthmaan bin Abiy Al-‘Aasw ndiye aliyepewa jina la utani la Abuu ‘Abdillaah. Alikuwa mdogo kuliko watu waliokuwa katika ujumbe wa Twaaif wa Banu Thaqif. Nabiyy (ﷺ) alimteua awe mkuu wa Twaaif, na aliwazuia watu wake wasiasi, na kwa hivyo wabakie katika Uislaam. ‘Umar alimteua awe Gavana wa Bahrayn na Oman. Alifariki mnamo mwaka 51 A.H.

[23] Imaam (anayeswalisha) ni sharti awajali watu dhaifu na wazee kwa kutorefusha sana Swalaah, kiasi cha kuwafanya wafikirie kuacha jamaa.

[24] Inamaanisha kwamba, Muadhini sharti asiwe analipwa kwa kazi hiyo ya kuadhini. Lakini huku siyo kukataza, bali ni pendekezo linalopendeza.

[25] Maalik bin Al-Huwayrith alikuwa wa Banu Layth, na alipewa jina la utani la Abuu Salmaan. Alimzuru Nabiyy (ﷺ) na akakaa naye kwa siku ishirini. Alilowea Basra na akafia huko mnamo mwaka wa 74 A.H.

[26] Inamaanisha kuwa, wakati wa safari pia, kuadhini na kukimu ni Sunnah.

[27] Mambo mengine yanajulikana kuhusu Hadiyth hii:

a) Adhaan sharti itolewe kwa sauti kubwa, pakiweko mapumziko kidogo kati ya maneno yake.

(b) Iqaamah itolewe haraka haraka.

(c) Sharti kuweko muda wa kutosha kati ya Adhaan na Swalaah, ili mtu aweze kuja kujiunga na jamaa baada ya kumaliza kula au baada ya kuenda na kutoka msalani na kutawadha. ‘Ulamaa wengine wamekisia wakati huo uwe sawa na muda wa Rakaa nne.

[28] Ni Sunnah kwa Muadhini kutoa Adhaan akiwa na wudhuu, lakini isipowezekana, Adhaan itolewe bila wudhuu. Hili ni pendekezo tu siyo lazima.

[29] Ziyaad bin Al-Haarith alikuwa Swahaba kutoka Yaman aliyekubaliana na Nabiyy (ﷺ) na akatoa Adhaan mbele yake. Inasemekana alilowea Basra.

[30] Ni Sunnah kwa mtu mmoja huyo huyo atoe Adhaan na Iqaamah; lakini akiruhusu, mtu mwingine anaweza kutoa Iqaamah.

[31] Du’aa kamili (الدَّعْوَةُ التَّامَّةُ) maana yake ni ung’avu wa Umoja wa Allaah (عز وجل) na Nuru ya Unabiy.

[32] Baki ya kumaanisha ‘uombezi na ukuu (wasiylah)’, hilo pia ni jina la mahali. Nabiyy (ﷺ) alisema kwamba, ni mtu mmoja tu miongoni mwa viumbe wa Allaah (عز وجل) atakayefika kule, naye alitegemea, kwa Rahmah za Allaah (عز وجل), mtu huyo atakuwa yeye Nabiyy (ﷺ).

03- Mlango Wa Masharti Ya Swalaah

بَابُ شُرُوطِ الصَّلَاةِ

03-Mlango Wa Masharti Ya Swalaah

161.

عَنْ عَلِيِّ بْنِ طَلْقٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا فَسَا أَحَدُكُمْ فِي الصَّلَاةِ فَلْيَنْصَرِفْ ، وَلْيَتَوَضَّأْ ، وَلْيُعِدْ الصَّلَاةَ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Aliy bin Twalq[1] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akitoa upepo katika Swalaah aondoke akatawadhe, na arudie kuswali[2].” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

162.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : { لَا يَقْبَلُ اللَّهُ صَلَاةَ حَائِضٍ إِلَّا بِخِمَارٍ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah haikubali

Swalaah ya mwanamke aliye baleghe mpaka avae khimaar[3] (shungi la kufunika kichwa na mwili).” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

163.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لَهُ : {إِنْ كَانَ الثَّوْبُ وَاسِعًا فَالْتَحِفْ بِهِ} يَغْنِي : فِي الصَّلَاةِ وَلِمُسْلِمٍ : {فَخَالَفَ بَيْنَ طَرَفَيْهِ وَإِنْ كَانَ ضَيِّقًا فَاتَّزَرَ بِهِ} . مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ .

وَلَهُمَا مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {لَا يُصَلِّي أَحَدُكُمْ فِي الثَّوْبِ الْوَاحِدِ لَيْسَ عَلَى عَاتِقِهِ مِنْهُ شَيْءٌ}

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Iwapo nguo ni pana, jizungushie mwili wote (yaani wakati wa kuswali)

Na katika tamshi la Muslim: “Kutanisha ncha mbili, na ikiwa inabana, izungushie kiunoni.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Nao wawili (Al-Bukhaariy na Muslim) wamenukuu Hadiyth ya Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Asiswali mmoja wenu na vazi moja tu lisilofunika mabega.”

164.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا : أَنَّهَا سَأَلَتْ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَتُصَلِّي الْمَرْأَةُ فِي دِرْعٍ وَخِمَارٍ ، بَغَيْرِ إِزَارٍ ؟ قَالَ : " إِذَا كَانَ الدَّرْعُ سَابِغًا يُغْطِي ظُهُورَ قَدَمَيْهَا } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَصَحَّحَ الْأَيْمَنُ وَقَفَّهُ .

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa alimuuliza Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Je, mwanamke anaweza kuswali na vazi refu na ushungi bila kuvaa nguo ya chini? Akasema: “Ikiwa hilo vazi ni refu linalofunika miguu yake.[4]” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na wakaisahihisha Maimaam kuwa ni Mawquwf]

165.

وَعَنْ عَامِرِ بْنِ رَبِيعَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { كُنَّا مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي لَيْلَةٍ مَظْلَمَةٍ ، فَأَشْكَلَتْ عَلَيْنَا الْقِبْلَةَ ، فَصَلَّيْنَا . فَلَمَّا طَلَعَتِ الشَّمْسُ إِذَا نَحْنُ صَلَّيْنَا إِلَى غَيْرِ الْقِبْلَةِ ، فَنَزَلَتْ : (فَأَيْنَمَا تُوَلُّوا فَثَمَّ وَجْهُ اللَّهِ) } أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَضَعَفَهُ

Kutoka kwa ‘Aamir bin Rabiyy’ah[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulikwa na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika usiku wa giza na hatukuwa na hakika ya Qiblah, tukaswali, jua lilipochomoza tukagundua tulielekea upande usiokuwa Qiblah, ikateremka Aayah: (basi popote mnapogeuka kuna Wajihi wa Allaah) [Al-Baqarah: 115].” [Imetolewa na At-Tirmidhiy, na akaidhoofisha]

166.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَا بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ قِبْلَةٌ } رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ ، وَقَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Baina ya Mashariki na Magharibi ni Qiblah[6].” [Imetolewana At-Tirmidhiy, na akaipa daraja la Qawiy Al-Bukhaariy]

167.

وَعَنْ عَامِرِ بْنِ رَبِيعَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي عَلَى رَاحِلَتِهِ حَيْثُ تَوَجَّهَتْ بِهِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ زَادَ الْبُخَارِيُّ : { يُومِي بِرَأْسِهِ ، وَلَمْ يَكُنْ يَصْنَعُهُ فِي الْمَكْتُوبَةِ }

وَلِأَبِي دَاوُدَ : مِنْ حَدِيثِ أَنَسٍ : { كَانَ إِذَا سَافَرَ فَأَرَادَ أَنْ يَتَطَوَّعَ اسْتَقْبَلَ بِنَاقَتِهِ الْقِبْلَةَ ، فَكَبَّرَ ، ثُمَّ صَلَّى حَيْثُ كَانَ وَجْهَ رِكَابِهِ } وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ

Kutoka kwa ‘Aamir bin Rabiyy’ah[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nimemuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiswali huku kapanda mnyama wake akielekea kokote alikoelekea mnyama wake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Al-Bukhaariy akaongeza: “Huku akiashiria kwa kichwa, hakufanya hivyo (kuswali huku kapanda mnyama) kwa Swalaah za faradhi.”

Na Abuu Daawuud amepokea Hadiyth ya Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Aliposafiri na akataka kuswali Swalaah ya Sunnah, alikuwa akimuelekeza ngamia wake Qiblah[8], akapiga takbiyra na kuendelea kuswali huku akielekea kokote ngamia wake alikoelekea.” [Isnaad yake ni Hasan]

168.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْأَرْضُ كُلُّهَا مَسْجِدٌ إِلَّا الْمَقْبَرَةَ وَالْحَمَّامَ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَلَهُ عِلَّةٌ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ardhi yote ni Msikiti, isipokuwa makaburini na msalani.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy, na ina dosari]

169.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {نَهَى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يُصَلَّى فِي سَبْعِ مَوَاطِنَ: الْمَزْبَلَةِ، وَالْمَجْزَرَةِ

، وَالْمَقْبَرَةَ، وَقَارِعَةَ الطَّرِيقِ، وَالْحَمَّامَ، وَمَعَاظِنَ الْإِبِلِ،
وَفَوْقَ ظَهْرِ بَيْتِ اللَّهِ { رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَضَعَّفَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza kuswali katika
sehemu saba[9]: (a) jalalani (b) machinjioni (c) makaburini (d)
katikati ya njia (e) msalani (bafuni, chooni) (f) wanapokaa ngamia,
katika sehemu ya kunywa maji, na (g) juu ya paa la Ka’bah.”
[Imetolewa na At-Tirmidhiy, na akaidhoofisha]

170.

وَعَنْ أَبِي مَرْثَدٍ الْغَنَوِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : سَمِعْتُ رَسُولَ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ : { لَا تُصَلُّوا إِلَى الْقُبُورِ ، وَلَا
تَجْلِسُوا عَلَيْهَا } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Marthad Al-Ghanawiyy[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
amesema: Nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
akisema: “Msiswali kuelekea makaburi[11], wala
msiyakalie[12].” [Imetolewa na Muslim]

171.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا جَاءَ أَحَدُكُمْ الْمَسْجِدَ ، فَلْيَنْظُرْ ، فَإِنْ رَأَى

فِي نَعْلَيْهِ أَذَى أَوْ قَدْرًا فَلْيَمْسَحْهُ ، وَلْيُصَلِّ فِيهِمَا } أَخْرَجَهُ
أَبُو دَاوُدَ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Mmoja wenu anapokuja Msikitini na atazame, na akiona uchafu katika viatu vyake, basi avipanguse na kisha aswali navyo.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

172.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا وَطِئَ أَحَدُكُمْ الْأَذَى بِخَفِيِّهِ فَطَهَّرْهُمَا
الْتِّرَابُ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akikanyaga uchafu kwa khofu yake (soksi zake za ngozi), basi kitakaso chake ni mchanga[13].” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

173.

وَعَنْ مُعَاوِيَةَ بْنِ الْحَكَمِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِنَّ هَذِهِ الصَّلَاةَ لَا يَصْلَحُ فِيهَا شَيْءٌ

مِنْ كَلَامِ النَّاسِ ، إِنَّمَا هُوَ التَّسْبِيحُ ، وَالتَّكْبِيرُ ، وَقِرَاءَةُ
الْقُرْآنِ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Mu'aawiyah bin Al-Hakam[14] amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika hii Swalaah ndani yake haifai chochote katika maneno ya watu, kwa kuwa hiyo ni Tasbiyh, Takbiyra na kusoma Qur-aan.” [Imetolewa na Muslim]

174.

وَعَنْ زَيْدِ بْنِ أَرْقَمَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { إِن كُنَّا لَنَتَكَلَّمُ فِي
الصَّلَاةِ عَلَى عَهْدِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُكَلِّمُ أَحَدُنَا
صَاحِبَهُ بِحَاجَتِهِ، حَتَّى نَزَلَتْ : (حَافِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ
وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَى وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ) [البقرة : 238] ،
فَأَمَرْنَا بِالسُّكُوتِ، وَنُهِينَا عَنْ الْكَلَامِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ
لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Zayd bin Arqama[15] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Sisi tulikuwa tukiongea ndani ya Swalaah zama za uhai wa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na mtu alikuwa akiongea na mwenzake kuhusu mahitaji yake, ilipoteremka Aayah:

(حَافِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَى وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ)

(Shikamaneni na Swalaah na khaswa Swalaah ya katikati (Alasiri), na simameni mbele ya Allaah katika hali ya utiifu) [Al-Baqarah:

238] tukaamrisha kunyamaza na tukakatazwa kuongea[16].” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

175.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {التَّسْبِيحُ لِلرِّجَالِ، وَالتَّصْفِيقُ لِلنِّسَاءِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

زَادَ مُسْلِمٌ {فِي الصَّلَاةِ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tasbiyh (Kusema Subhaana-Allaah) ni kwa mwanamume, na kupiga makofi[17] ni kwa wanawake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Muslim akaongezea: “Ndani ya Swalaah[18].”

176.

وَعَنْ مُطَرِّفِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ الشَّخِيرِ ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ :
{رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي، وَفِي صَدْرِهِ
أَزِيْرٌ كَأَزِيْرِ الْمَرْجَلِ، مِنْ الْبُكَاءِ}
أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ ، إِلَّا ابْنُ مَاجَةَ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Mutwarriif bin ‘Abdillaah bin Shikh-khiyr[19] (رَضِيَ) ame-
 sema kutoka kwa baba yake[20] amesema:
 “Nimemuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiswali, na nikasikia sauti kifuani mwake kama kuchemka kwa chungu, kwa sababu ya kulia[21].” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ahmad) isipokuwa Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

177.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { كَانَ لِي مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَدْخَلَانِ ، فَكُنْتُ إِذَا أَتَيْتُهُ وَهُوَ يُصَلِّي تَخَنَّحَ لِي } رَوَاهُ النَّسَائِيُّ ، وَابْنُ مَاجَهَ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilipata ruhusa ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kumwona nyumbani kwake mara mbili, na kila nilipokwenda na kumkuta anaswali, alikuwa anajikohoza kwa ajili yangu[22] (kuwa anaswali).” [Imetolewa na An-Nasaaiy na Ibn Maajah]

178.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : { قُلْتُ لِبِلَالٍ : كَيْفَ رَأَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَرُدُّ عَلَيْهِمْ حِينَ يُسَلِّمُونَ عَلَيْهِ ، وَهُوَ يُصَلِّي ؟ قَالَ : يَقُولُ هَكَذَا ، وَبَسَطَ كَفَّهُ { أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Nilimuuliza Bilaal hivi: “Ulimuona Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anawajibu vipi Mswahaba zake pindi wanapomsalimia akiwa anaswali? Bilaal akasema: alikuwa akifanya hivi, naye Bilaal akaonyesha kwa kupanua kiganja chake[23].” [Imetolewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy naye aliisahihisha]

179.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي وَهُوَ حَامِلٌ أُمَامَةَ بِنْتِ زَيْنَبَ ، فَإِذَا سَجَدَ وَضَعَهَا ، وَإِذَا قَامَ حَمَلَهَا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِمُسْلِمٍ : { وَهُوَ يَوْمُ النَّاسِ فِي الْمَسْجِدِ }

Kutoka kwa Abuu Qataadah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anaswali huku kambeba Umaamah bint Zaynab[24], na aliposujudu[25] alimweka chini, na aliposimama alimnyanyua.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Muslim amesema: “Na yeye (Nabiy) anaswalisha watu.”

180.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أُقْتُلُوا الْأَسْوَدَيْنِ فِي الصَّلَاةِ: الْحَيَّةُ،
وَالْعُقْرَبُ} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ueni vyeusi
viwili mkiwa ndani ya Swalaah: nyoka na nge[26].” [Imetolewa na
Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn
Maajah) na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

[1] Aliy bin Twalq bin Al-Mundhir bin Qays Al-Hanafiyy ni ambaye kutoka
kwa Banu Hanifa, As-Sahimi, na Al-Yamami. Alikuwa ni Swahaba, na
inasemekana kuwa ndiye aliyekuwa baba wa Twalq bin ‘Aliy, lakini
ilisemekana kuwa majina hayo mawil ni ya mtu mmoja huyo huyo.

[2] Hii maana yake ni kwamba, ikiwa wudhuu umetanguka wakati wa
Swalaah, lazima kuchukua wudhuu upya na Swalaah hiyo irudiwe. Hii
ndiyo bora zaidi.

[3] Khimaar ni mtandio au kipande cha nguo ambacho kwacho mwanamke
hujifunikia eneo la kichwa na la shingo lake. Hiyo inamaanisha kuwa
mwili mzima wa mwanamke sharti ufunikwe pamoja na kichwa na nywele
zake.

[4] Hii iko pamoja na masharti ya Swalaah kuwa, mwanamke sharti pia
afunike miguu yake mpaka kwenye visigino, vinginevyo Swalaah yake
haitokubaliwa.

[5] ‘Aamir bin Rabiyy’ah bin Maalik Al-‘Inzy, na inasemekana ni Al-
‘Adawy. Alisilimu na akafanya Hijrah mara mbili. Alihudhuria Vita vyote.
Alifariki wakati alipokufa ‘Uthmaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ).

[6] Kwa maneno hayo, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameelezea upande iliko Qiblah (Ka'bah) kwa ulimwengu mzima. Watu wanaoishi Mashariki au Magharibi ya Qiblah, wachukue maana ya Hadiyth hii kwamba Qiblah iko kati ya kunakochomozea jua na kunakochwea jua mnamo majira ya baridi na joto. Na wale wanaoishi kaskazini na kusini ya Qiblah, wachukue maaana ya kuwa, wakisimama huku Mashariki na Magharibi iko upande wao wa kuume na kushoto, basi Qiblah yao iko katikati ya pande hizi mbili.

[7] 'Aamir bin Rabiyy'a alikuwa mmoja wa wana wa 'Anz bin Wa'il, ambaye alikuwa ndugu ya Bakr na Taghlib, wana wa Wa'il. Alikuwa Swahaba aliyesilimu mapema sana na akafanya Hijrah (kuhama) zote mbili. Alishiriki katika Badr na vita zote nyingine, na akafariki mnamo mwaka 32 au 35 A.H

[8] Hii maana yake ni kwamba, Swalaah ya Sunnah (Nafl) ndiyo inayoweza kuswaliwa huku mtu kapanda mnyama au chombo, kwa sharti kuwa pale anapoanza kuswali, mnyama yule au chombo kile akielekeze Qiblah, na baada ya hapo badiliko lolote la mwelekeo haliathiri kitu. Lakini Swalaah za faradhi zisiswaliwe mtu akiwa kampanda mnyama, lakini meli, majahazi, mitumbwi, na ndege, vinaruhusiwa.

[9] Hadiyth hii ni ushahidi kuwa kuswali makaburini hairuhusiwi, uwe unaswali juu ya makaburi au katikati ya makaburi, na si hoja ikiwa makaburi hayo ni ya Waislaamu au wasiokuwa Waislaamu. Kuswalia makaburini kunatoa picha ya kuabudu asiyekuwa Allaah, ambalo ni kosa kubwa la ushirikina. Imekatazwa kuswali msalani kwa sababu ya najisi na uchafu uliyoko huko; na isitoshe Hadiyth zinasema kuwa msalani ni mahala pa shaytwaan.

[10] Jina la Abuu Marthad Al-Ghanawiyy ni Kannaz bin Hussayn bin Yarnu' Al-Ghanawiyy kizazi cha Ghani bin Ya'sur, kabila la Ghatafan. Alikuwa ni Swahaba ambaye alishuhudia Badr na alikuwa sahibu wa Hamza bin 'Abdil-Muttwalib, na alikuwa sawa naye ki umri. Alishiriki katika Vita vyote, na akafa mnamo mwaka 12 A.H. akiwa na umri wa miaka 66.

[11] Ina maana kuwa, imekatazwa kuswali huku ukielekea makaburi. Watu wengine wanajenga Misikiti karibu na makaburi ya watakatifu ili kupata fadhila za roho zilizokufa. Hii pia imekatazwa. Katika Hadiyth ya ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) imesemwa waziwazi kuwa: “Allaah (عز وجل) Awalaani Mayahudi na Wakristo, kwani walifanya makaburi ya Manabii wao kuwa mahali pa kusalia.” Inaweza kumaanisha pia kwamba matendo yatakiwayo kuyafanya mbele ya Allaah (عز وجل) Misikitini kamwe yasitendwe katika makaburi. Au pia yaweza kumaanisha kuwa kamwe mtu asiswali mahala ambapo kuna makaburi mbele yake.

[12] Kukalia juu ya makaburi kuna maana mbili: moja ni kupumzika au kuegemea makaburi; na pili ni kuyamiliki makaburi kama Mujawwir (mwangalizi wa makaburi ambaye pia hukusanya pesa na vitu vingine kutoka kwa watu wanaozuru makaburi ili kupata radhi za roho zilizozikwa). Aina zote hizo mbili zimekatazwa, inaweza kuwa na maana nyingine kwamba mtu yoyote asikae juu ya kaburi au asijisaidie haja kubwa au ndogo. Hii pia imekatazwa.

[13] Hadiyth hizi mbili zinaonyesha kuwa kuswali huku mtu amevaa soksi na au viatu inaruhusiwa. Zinasema pia kuwa endapo viatu hivyo vitachafuliwa na uchafu wowote, vinyesi vya wanyama au bin Adam, inatosha kusugua kwa vumbi na hakuna haja ya kuosha kwa maji.

[14] Huyu Mu’aawiyah bin Al-Hakam alikuwa Swahaba aliyehesabika miongoni mwa wakazi wa Hijaaz. Alikuwa akizuru Madiynah na akawa anakaa kwa akina Banu Sulaym. Alifariki mnamo mwaka 117 A.H.

[15] Zayd bin Arqam alipewa jina la utani la Abuu ‘Amr, na alikuwa Answaar Mkhazraj. Kwanza alishiriki katika Vita vya Al-Khandaq, na akaongozana na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika misafara 17. Alihudhuria Vita vya Siffin pamoja na ‘Aliy kwa kuwa alikuwa mmoja wa wafuasi wake. Alilowea kule Kuwfah, na akafia huko mnamo mwaka 66 A.H.

[16] Inamaanisha kuwa kuongea wakati wa Swalaah kumekatazwa. Mnamo siku za mwanzo mwanzo za Uislaam, watu walikuwa wakiongea tu ndani ya Swalaah, kisha likaja katazo.

[17] Inamaanisha kwamba, iwapo Imaam akitenda kosa kwa bahati mbaya ndani ya Swalaah, wanaume maamuma wake (wanaokuwa nyuma ya huyo Imaam) hutakiwa waseme hivi:

سبحان الله

(kumkumbusha Imaam alisahihishe kosa lake hilo), na wanawake wanatakiwa wapige makofi kidogo (kwa maana hiyo hiyo ya kumkumbusha Imaam), ili sauti (ya mwanamke) isisikike na wanaume.

[18] Yaani ikiwa mtu anataka kumkumbusha Imaam jambo alilolisahau, ndani ya Swalaah, sharti aseme:

سبحان الله

Lakini ikiwa ni mwanamke anayetaka kumkumbusha Imaam, basi sharti mwanamke huyo apige makofi kwa kuvipiga pamoja na vidole vya kiganja chake cha kuume kwa cha kushoto.

[19] Huyu Mutwarrif ndiye Mutwarrif bin ‘Abdillaah bin Ash-Shikhkhir Al-Harashi Al-‘Aamir Al-Basr, miongoni mwa Taabi’iyna wa zamani. Aliaminika sana, alikua muadilifu, na alifanya matendo mengi ya sifa nzuri nzuri. Alikufa mnamo mwaka 95 A.H

[20] Baba yake Mutwarrif alikuwa ni ‘Abdullaah bin Ash-Shikhkhir bin ‘Awf bin Ka’b Al-Harashi Al-‘Aamir, huyo wa mwisho ni Swahaba. Alikuwa ni mjumbe wa ujumbe wa Banu ‘Aamir na anaaminiwa kuwa alilowea Basra.

[21] Kwa mujibu wa Hadiyth, kulia ndani ya Swalaah kwa kumuogopa Allaah kunaruhusiwa; lakini kulia kwa sababu ya ugonjwa au adha yoyote kunabatilisha Swalaah.

[22] Inamaanisha kuwa kutoa dalili ya kukohoa hasa mara moja moja au mbili, hakutangui Swalaah. Kitabu cha Musaffa cha ufafanuzi wa Mu’atta

kinaelezea kuwa, kukohoa, kulia, au kucheka kwa mfululizo, ingawa huko siyo kusema, kunatangua Swalaah.

[23] Inamaanisha kuwa matendo madogo madogo hayabatilishi Swalaah.

[24] Umaamah ni mjukuu wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), binti wa Zaynab kwa Abdul-‘Aass bin Ar-Rabi’. Aliolewa na ‘Aliy baada ya kifo cha Faatwimah (رَضِيَ اللهُ عَنْهَا) kwa mujibu wa mapendekezo ya Faatwimah. Na ‘Aliy alipouliwa, aliolewa na Al-Mughiyrah bin Nawfal, na akafariki wakati akiwa kwa mume huyu.

[25] Shah Waliyu-Allaah wa Delhi aliandika katika kitabu chake حجة الله kuwa, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alifanya vitendo vidogo vidogo kwa maksudi ili kuonyesha kuwa vitendo vidogo vidogo havitengui Swalaah. Hadiyth zinasema kuwa, kukiwa na dharura, yafuatayo hayaathiri wala kutangua Swalaah: (a) Tamko dogo, (b) Kuhama kidogo mahali ulipo, vitendo vidogo, (c) Badiliko dogo la mahala uliko kuenda mbele au nyuma, (d) Kutoa ishara au kuashiria kitu kwa mguu, (e) Kufungua mlango kwa kuhama kidogo tu, (f) Kusogea nyuma wakati mtu (wa tatu) anajiunga nanyi (kuswali jamaa), (g) Kulia kwa kumuogopa Allaah, (h) Kutoa ishara ili kuelewesha kitu fulani, (i) Kuua nge au nyoka, (j) Kutazama pembeni bila kugeuza shingo.

[26] Hadiyth hii inathibitisha vitu viwili: (a) Swalaah haitanguki kwa kuua nge na nyoka, (b) Mtu asiwaonee huruma. Sharti wauawe na wasiachwe kwani wao wana madhara.

04-Mlango Wa Sutrah (Kizuzi) Ya Mwenye Kuswali

بَابُ سُتْرَةِ الْمُصَلِّي

04-Mlango Wa Sutra[1] (Kizuzi) Ya Mwenye Kuswali

181.

عَنْ أَبِي جُهَيْمٍ بْنِ الْحَارِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَوْ يَعْلَمُ الْمَارُّ بَيْنَ يَدَيِ الْمُصَلِّي مَاذَا عَلَيْهِ مِنَ الْإِثْمِ لَكَانَ أَنْ يَقِفَ أَرْبَعِينَ خَيْرًا لَهُ مِنْ أَنْ يَمُرَّ بَيْنَ يَدَيْهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ وَوَقَعَ فِي "الْبَزَّازِ" مِنْ وَجْهِ آخَرَ : {أَرْبَعِينَ خَرِيفًا}

Kutoka kwa Abuu Juhaym bin Al-Haarith[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah amesema: “Lau angejua anayepita mbele ya anayeswali, dhambi kubwa aliyo nayo ingekuwa bora kwake kusimama (siku) arubaini, kuliko kupita mbele yake.[3]” [Al-Bukhaariy, Muslim, na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na imetajwa katika Al-Bazzaar kwa njia nyingine na imeongezwa: “Miaka arubaini.”

182.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : {سُئِلَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي غَزْوَةِ تَبُوكَ عَنْ سِتْرَةِ الْمُصَلِّي . فَقَالَ : "مِثْلُ مُؤَخِرَةِ الرَّحْلِ" } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa katika vita vya Tabuwk kuhusu Sutra (kizuizi) ya anayeswali, akasema: ni kama sehemu ya nyuma ya tandiko la mnyama[4].” [Imetolewa na Muslim]

183.

وَعَنْ سَبْرَةَ بْنِ مَعْبَدٍ الْجُهَنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَيْسَتْ أَحَدُكُمْ فِي صَلَاتِهِ وَلَوْ بِسَهْمٍ} أَخْرَجَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Sabrah bin Ma’bad Al-Juhaniyy[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu aweke sutrah[6] katika Swalaah, japo kwa kuweka mshale.” [Imetolewa na Al-Haakim]

184.

وَعَنْ أَبِي ذَرٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يَقْطَعُ صَلَاةَ الْمَرْءِ الْمُسْلِمِ إِذَا لَمْ يَكُنْ بَيْنَ يَدَيْهِ مِثْلُ مُؤَخِرَةِ الرَّحْلِ الْمَرْأَةِ ، وَالْجِمَارِ ، وَالْكَلْبِ

الْأَسْوَدُ . . . " الْحَدِيثُ { وَفِيهِ { الْكَلْبُ الْأَسْوَدُ شَيْطَانٌ } .
أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

وَلَهُ : عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ نَحْوُهُ دُونَ : " الْكَلْبُ " .
وَلِأَبِي دَاوُدَ ، وَالنَّسَائِيِّ : عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا
نَحْوُهُ ، دُونَ آخِرِهِ . وَقَيَّدَ الْمَرْأَةَ بِالْحَائِضِ

Kutoka kwa Abuu Dharr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Itakapokuwa
hakuna mbele yake, (Sutrah) mfano wa sehemu ya nyuma ya tandiko
la mnyama[7], basi Swalaah ya Muislamu itakatika ikiwa atapita
mwanamke au punda na mbwa mweusi." Na Hadiyth inasema pia:
"Na mbwa mweusi ni shaytwaan.[8]" [Imetolewa na Muslim]

Naye amepokea Hadiyth ya Abuu Hurayrah kama hiyo pasi na kutaja
"mbwa."

Nao Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy wamepokea Hadiyth ya Ibn
'Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) pasi na mwisho wake, na
akafungamanisha mwanamke na hedhi.

185.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ إِلَى شَيْءٍ يَسْتُرُهُ
مِنْ النَّاسِ ، فَأَرَادَ أَحَدٌ أَنْ يَجْتَازَ بَيْنَ يَدَيْهِ فَلْيَدْفَعْهُ ، فَإِنْ أَبَى
فَلْيَقَاتِلْهُ ، فَإِنَّمَا هُوَ شَيْطَانٌ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ .

وَفِي رِوَايَةٍ : {فَإِنَّ مَعَهُ الْقَرِينَ}

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akiswali kuelekea kitu kinachomsitiri dhidi ya watu wengine, na mtu akataka kupita mbele yake, basi amzuie, akikataa, apigane naye[9], kwani huyo ni shaytwaan.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine: “Kwani shaytwaan yuko pamoja naye.”

186.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ فَلْيَجْعَلْ تَلَقَاءَ وَجْهِهِ شَيْئًا ، فَإِنْ لَمْ يَجِدْ فَلْيَنْصِبْ عَصًا ، فَإِنْ لَمْ يَكُنْ فَلْيَخُطْ خَطًّا ، ثُمَّ لَا يَضُرُّهُ مَنْ مَرَّ بَيْنَ يَدَيْهِ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ وَابْنُ مَاجَةَ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ ، وَلَمْ يُصِبْ مَنْ زَعَمَ أَنَّهُ مُضْطَرِبٌ ، بَلْ هُوَ حَسَنٌ .

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Endapo mmoja wenu anaswali, basi aweke kitu mbele yake, na iwapo hana kitu cha kuweka, basi asimamishe fimbo, na akiwa hana fimbo basi achore msitari, ndipo hatadhuriwa na anayepita mbele yake[10].” [Imetolewa na Ahmad na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Hibbaan, wala hakupatia aliyesema ni Mudhw-twarib, bali hiyo ni Hasan]

187.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا يَقْطَعُ الصَّلَاةَ شَيْءٌ ، وَادْرَأْ مَا اسْتَطَعْتَ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَفِي سَنَدِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna chochote kinachokatisha Swalaah, lakini epusha kadiri mnavyoweza (vitu vinavyokatisha Swalaah).” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na katika Isnaad yake kuna udhaifu]

[1] Sutra (kizuizi) ni kitu chochote ambacho mtu anayeswali hukiweka mbele yake iwe kama kizuizi kati yake yeye na wengine.

[2] Inasemekana kuwa huyu Abuu Juhaym jina lake ni ‘Abdullaah bin Al-Haarith bin As-Simma Al-Answaar Al-Khazraj. Alikuwa ni Swahaba anayejulikana sana, ambaye aliishi hadi wakati wa Ukhalifa wa Mu’aawiyah.

[3] “Mpaka” wa mtu anayeswali ni mahala pale mahali anaposujudia. Kukatisha mbele zaidi ya mpaka huu siyo kosa. Onyo hili ni la mtu anayekatisha, siyo mtu aliyekwisha kukaa au anaswali mbele yake, na anayefanya vitendo vingine (visivyostahiki ndani ya Swalaah).

[4] Urefu wa Sutra ni sharti uwe kwa uchache sawa sawa na sehemu ya nyuma ya tandiko. Hiyo ni sawa na takribani futi moja. Endapo hakuna kitu kingine, basi fimbo inaweza kufanya kazi badala ya Sutra. Na iwapo

hata fimbo hakuna, msitari waweza kuchorwa kama anavyoelezea Abuu Daawuud.

[5] Sabrah bin Ma'yad Al-Juhaniyy alikuwa ni Swahaba kutoka Al-Madiynah aliyelowea kule Dhi Marwa. Alipewa jina la utani la Abuu Thuraiya. Kwanza alishiriki katika vita vya Al-Khandaq (Vita vya Handaki). Aliyekuwa ndiye mjumbe wa 'Aliy kuenda kwa Mu'aawiyah, alipoteuliwa kuwa Khalifa, kumtaka athibitishe utii wa watu wa shaam kwa 'Aliy. Alikufa mnamo mwish wa Ukhalifa wa Mu'aawiyah.

[6] Wakati mtu anaposwali, Baraka za Allaah (عز وجل) humuelekea yeye. Sutrath huwa kama ukingo, na Baraka za Allaah (عز وجل) hubakia ndani ya eneo la ukingo huo. Mtu yoyote anayekatisha njia nje ya Sutrath hiyo, haikabili Baraka ya Allaah (عز وجل) na Swalaah haiathiriki. Kusipokuwepo Sutrath (kizuizi), basi huwa hakuna mpaka wa Baraka za Allaah (عز وجل), na mtu anayekatisha mbele ya mtu anayeswali hugongana na Baraka hiyo, na umakini kwa Allaah wa mtu wa anayeswali huvurugika. Kwa hivyo Sutrath ilifanywa iwe lazima.

[7] Inamaanisha kwamba inaathiri unyenyekevu kwa Allaah (عز وجل) tu, lakini hakuathiri Swalaah.

[8] Katika Hadiyth hii kuna ushahidi kuwa, bila kuwepo Sutrath viumbe vilivyotajwa hapo juu vikipita mbele ya mtu anayeswali, Swalaah yake hukatishwa. Lakini kuna Hadiyth iliyoafikiwa inayosema kuwa, Ibn 'Abbaas (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) huku akiwa amempanda punda alipita mbele ya msururu wa Waumini wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anaswali, naye Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakuirudia Swalaah yake wala hakuwaamuru Swahaba zake warudie Swalaah zao.

[9] Kupita mbele ya mtu anayeswali imeafikiwa kunahesabika ni kumtengeua. Iwapo mtu anaswali nyuma ya Sutrath (kizuizi), na mtu kukatisha njia apite ndani yake, asimamishwe kwa ishara, na aking'ang'ania kupita, azuiwe kwa nguvu. "Kupigana". Endapo Muumini anaswali bila ya kuwa na Sutrath mbele yake, ni kosa na Muumini anayeswali na siyo kosa la mpitaji. Pia Hadiyth hii inaonyesha kuwa

Swalaah ya Muumini huyo haikatishwi kwa kitendo hicho kidogo, lakini kitendo hicho kinaathiri umakinifu.

[10] Inaonyeshwa kuwa Swalaah haikatishwi kwa mtu kupita mbele, lakini huathiri umakinifu.

05-Mlango Sisitizo La Khushuw' (Unyenyekevu) Katika Swalaah

بَابُ الْحَثِّ عَلَى الْخُشُوعِ فِي الصَّلَاةِ

05-Mlango Sisitizo La Khushuw'[1] (Unyenyekevu) Katika Swalaah

188.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يُصَلِّيَ الرَّجُلُ مُخْتَصِرًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ وَمَعْنَاهُ: أَنْ يَجْعَلَ يَدَهُ عَلَى خَاصِرَتِهِ وَفِي الْبُخَارِيِّ: عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا أَنَّ ذَلِكَ فَعَلَ الْيَهُودُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza mtu kuswali hali

ya kuweka mikono kiunoni.[2]” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Na maana yake ni: “Mtu kuweka mikono yake kwenye kiuno.”

Na katika Al-Bukhaariy kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا):
“Kuwa ni kitendo cha Mayahudi katika Swalaah zao.”

189.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : { إِذَا قُدِّمَ الْعِشَاءُ فَأَبْدِءُوا بِهِ قَبْلَ أَنْ تُصَلُّوا الْمَغْرِبَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kikiwadia chakula cha jioni (na huku Swalaah imewadia) kianzeni kabla hamjaswali[3] Magharibi.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

190.

وَعَنْ أَبِي ذَرٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا قَامَ أَحَدُكُمْ فِي الصَّلَاةِ فَلَا يَمْسَحِ الْخَصْيَ، فَإِنَّ الرَّحْمَةَ تَوَاجَهُ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ بِإِسْنَادٍ صَحِيحٍ

وَزَادَ أَحْمَدُ : "وَاحِدَةً أَوْ دَعً"

وَفِي "الصَّحِيح" عَنْ مُعَيْقِبٍ نَحْوَهُ بِغَيْرِ تَعْلِيلٍ

Kutoka kwa Abuu Dharr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anaposimama mmoja wenu katika Swalaah, asijipanguse vijiwe[4] kwani Rahmah inamuelekea yeye.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) kwa Isnaad swahiyh]

Na akaongezea Ahmad: “(Ondosha) mara moja tu, au acha.”

Na ndani ya Swahiyh (Al-Bukhaariy) kuna Hadiyih kama hiyo, kutoka kwa Mu’ayqib[5] bila kutajwa sababu.

191.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : {سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ الْإِلْتِفَاتِ فِي الصَّلَاةِ ؟ فَقَالَ : "هُوَ اخْتِلَاسٌ يَخْتَلِسُهُ الشَّيْطَانُ مِنْ صَلَاةِ الْعَبْدِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَلِلتِّرْمِذِيِّ: عَنْ أَنَسٍ وَصَحَّحَهُ {إِيَّاكَ وَالْإِلْتِفَاتِ فِي الصَّلَاةِ، فَإِنَّهُ هَلَكَةٌ، فَإِنْ كَانَ فَلَا بُدَّ فِي التَّطَوُّعِ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilimuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) juu ya kugeuka geuka ndani ya Swalaah naye akasema: Huko ni kunyakua ambako

shaytwaan hunyakua kutoka katika Swalaah ya mja.” [Imetolew na Al-Bukhaariy]

Na katika At-Tirmidhiy kutoka kwa Anas aliisahihisha ameandika: “Epuka kugeuka geuka ukiwa ndani ya Swalaah, kwani kutazama pembeni ni uharibifu, na ikiwa ni lazima[6] basi iwe katika Swalaah ya Sunnah.[7]”

192.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا كَانَ أَحَدُكُمْ فِي الصَّلَاةِ فَإِنَّهُ يُنَاجِي رَبَّهُ، فَلَا يَبْزُقَنَّ بَيْنَ يَدَيْهِ وَلَا عَنْ يَمِينِهِ، وَلَكِنْ عَنْ شِمَالِهِ تَحْتَ قَدَمِهِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَفِي رِوَايَةٍ : { أَوْ تَحْتَ قَدَمِهِ }

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akiwa ndani ya Swalaah, anakuwa anamnong’oneza Allaah, kwa hivyo asiteme mate mbele yake[8], wala upande wa kuume, lakini kushotoni kwake na chini ya mguu wake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine: “Au chini ya mguu wake.”

193.

وَعَنْهُ قَالَ : {كَانَ قِرَامٌ لِعَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا سَتَرَتْ بِهِ جَانِبَ بَيْتِهَا فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَمِيطِي عَنَّا قِرَامَكَ هَذَا، فَإِنَّهُ لَا تَزَالُ تَصَاوِيرُهُ تَعْرِضُ لِي فِي صَلَاتِي} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ
وَاتَّفَقَا عَلَى حَدِيثِهَا فِي قِصَّةِ أَنْبِجَانِيَّةِ أَبِي جَهْمٍ ، وَفِيهِ :
{فَإِنَّهَا أَلْهَتْنِي عَنْ صَلَاتِي}

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Aaishah alikuwa na Qiraam[9] aliyoitumia kusitiri upande mmoja wa nyumba yake, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamwambia: “Ondoa[10] pazia lako, kwani picha zake hazijaacha kunitokea katika Swalaah yangu.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Al-Bukhaariy na Muslim pia waliafikiana Hadiyith iliyosimuliwa naye (‘Aaishah) amabayo inataja kisa cha Anbijaaniyyah[11] Abiy Jahm[12], ikieleza pia: “Hiyo[13] imenivurugia umakinifu[14] wa Swalaah yangu.”

194.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَيَنْتَهَيْنَ قَوْمٌ يَرْفَعُونَ أَبْصَارَهُمْ إِلَى السَّمَاءِ فِي الصَّلَاةِ أَوْ لَا تَرْجِعَ إِلَيْهِمْ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَلَهُ : عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ : {لَا صَلَاةَ بِحَضْرَةِ طَعَامٍ ، وَلَا هُوَ يُدَافِعُهُ الْأَخْبَثَانِ}

Kutoka kwa Jaabir bin Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu wanaoelekeza macho yao mbinguni wanapokuwa ndani ya Swalaah, waache, au sivyoy kuona kwao hakutawarudia[15].” [Imetolewa na Muslim]

Pia (Muslim) amenukuu Hadiyth ya ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) kuwa amesema: “Nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema hakuna Swalaah wakati wa kuhudhuria chakula, wala mtu anapojizuia haja mbili (kubwa na ndogo)[16].”

195.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : {التَّائِبُ مِنَ الشَّيْطَانِ فَإِذَا تَتَاءَبَ أَحَدُكُمْ فَلْيَكْظَمْ مَا اسْتَطَاعَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَالْتِّرْمِذِيُّ ، وَزَادَ : {فِي الصَّلَاةِ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kupiga miayo hutokana na shaytwaan[17], kwa hivyo mmoja wenu anapopiga miayo ajizuie kadiri anavyoweza.” [Imetolewa na Muslim]

Na katika At-Tirmidhiy ameongeza: “Ndani ya Swalaah[18].”

[1] Khushuw' maana yake ni unyenyekevu, utulivu, ushwari, na kumakinia mwili mzima na akili yote kwa Allaah (سبحانه وتعالى).

[2] Kuweka mikono pembeni au kiunoni ni kitendo cha kujiona, wakati unyenyekevu na upole ndio unaotakiwa katika Swalaah. Nukta nyingine iliyofafanuliwa katika Hadiyth inayofuata ni kuwa hii inafanana na desturi ya Mayahudi, na kuwaiga wao imekatazwa.

[3] Ikiwa chakula kimeandaliwa, kula chakula hicho ni afadhali hata kama huna njaa. Falsafa ya kufanya hivi ni kwamba, mtu anatakiwa asimame mbele ya Allaah (سبحانه وتعالى) huku akiwa karidhika kikamilifu na akiwa juu ya mahitaji yoyote ya kidunia. Lakini hairuhusiwi kuenda kula wakati wa Swalaah ilhali hicho chakula hakijaandaliwa.

[4] Kuondosha changarawe kutoka mahala pa kusujudia kumekatazwa ikiwa vijiwe vyenyewe ni vidogo na havina madhara. Ama ikiwa vijiwe ni vikubwa na vinaleta adha na vinazuia umakinifu, basi hakuna dhara kuviondosha.

[5] Mu'ayqiyb bin Abiy Faatwimah Ad-Daws alisilimu zamani sana kule Makkah, na akahama Abyssinia wakati wa Hijrah ya pili. Alishuhudia Badr. Alikuwa akihiifadhi lakiri ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na baadaye Abuu Bakr (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) na baadaye tena 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) walimfanya mkuu wa Baytul-Maal. Alikufa wakati wa Ukhalifa wa 'Uthmaan (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ).

[6] Iwapo ni lazima, waweza kugeuka katika Swalaah ya Sunnah (nafl) lakini siyo katika Swalaah ya fardhi. Kwa sababu kuna madhara kidogo zaidi kufanya kitendo hicho katika Swalaah ya Sunnah. Katika dharura muhimu sana, huruhusiwa, kama ilivyodhihirika katika ugonjwa wa mwisho wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipotoka nje ya nyumba yake ili akaswali Msikitini, Abuu Bakr Swiddiyq (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) aliyekuwa akiswalisha wakati huo alitaka arudi nyuma kumpisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aswalishe, lakini aliashiriwa na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) asirudi nyuma akaendelea kuswalisha, naye Nabiyy (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) hakumkosoa Abuu Bakr (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ).

[7] Hata katika Swalaah ya khiari, uso ukigeuka mbali na Qiblah, Swalaah inakatika.

[8] Sharti ikumbukwe kwamba mtu kamwe asiteme mate kuelekea Qiblah, au upande wa kuume, awe ndani ya Swalaah au nje ya Swalaah.

[9] Kipande cha nguo laini chenye nakhsi rangi.

[10] Inamaanisha kuwa kitu chochote kinachovuruga khushuw' ni lazima kiondoshwe kutoka katika mahala pa kuswalia. Ikiwa hii haiwezekani, basi epuka mahala hapo na uende kwengine.

[11] Vazi la sufi lisilokuwa na nakshi wala picha au maandishi.

[12] Abuu Jahm ndiye Ibn Hudhayfah bin Ghaniym Al-'Adawi. Jina lake ni 'Aamir au 'Ubayd. Alisilimu katika mwaka ule ilipotekwa Makkah. Alikuwa miongoni mwa Swahaba walioishi umri mrefu, kwani huyu alihudhuria ujenzi wa Ka'bah wa Maqurayshi kabla ya ujio wa Nabiy (ﷺ), na akashuhudia ujenzi wake upya wa 'Abdullaah bin Az-Zubayr ambaye Abuu Jahm alifariki mwanzoni mwa Ukhalifa wake.

[13] Kipande cha nguo laini chenye nakshi na rangi.

[14] Inamaanisha kwamba Misikiti isipambwe kwa nakshi na urembo n.k. kwa kuwa vinazuwia umakinifu. Imaam Nawawi amenukuu maafikiano ya 'Ulamaa wa Kiislamu kuwa katazo hili ni halisi.

[15] Imaam An-Nawawi ameripoti maafikiano ya 'Ulamaa wa Kiislamu kwamba katazo hili ni halisi. Ibn Hazm anasema kuwa Swalaah inabatilika.

[16] Endapo mtu anahisi kutaka kuenda haja (choo), kukojoa au kutoa upepo, na akiwa anao muda wa kutosha, basi afanye hivyo kabla hajaanza kuswali, vinginevyo itakuwa karaha. Kwa mujibu wa wengine, hiyo haitahesabika kuwa ni Swalaah kabisa kwa sababu ya kutokuwepo umakinifu na unyenyekevu kwa Allaah (عز وجل). Iwapo muda ni mfupi sana na mtu ana haraka sana, basi aswali ile Swalaah kuliko kuchelewa.

[17] Kutoa mwayo ni matokeo ya kujaa tumbo ni uvivu. Shaytwaan hufurahi kumuona mwana Adam yuko hivyo, kwa hivyo kupiga mwayo kunahesabika kuwa ni tabia ya kishaytwaan.

[18] Kuzuia mwayo ndani ya Swalaah au katika wakati wowote ni Sunnah

06-Mlango Wa Misikiti

بَابُ الْمَسَاجِدِ

06-Mlango Wa Misikiti

196.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {أَمَرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِبِنَاءِ الْمَسَاجِدِ فِي الدُّوْرِ، وَأَنْ تُنْظَفَ، وَتُطَيَّبَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَ إِرْسَالَهُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amsema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliamrisha Misikiti ijengwe katika maeneo ya makazi[1], na kwamba isafishwe na itiwe manukato.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuwd, At-Tirmidhiy, naye aliithibitisha kama Mursal]

197.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَاتِلَ اللَّهِ الْيَهُودَ : اتَّخَذُوا قُبُورَ أَنْبِيَائِهِمْ مَسَاجِدَ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَزَادَ مُسْلِمٌ { وَالنَّصَارَى }

وَلَهُمَا : مِنْ حَدِيثِ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا : { كَانُوا إِذَا مَاتَ فِيهِمُ الرَّجُلُ الصَّالِحُ بَنَوْا عَلَى قَبْرِهِ مَسْجِدًا } وَفِيهِ : { أَوْلَئِكَ شِرَارُ الْخَلْقِ }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah awalaani Mayahudi, wamefanya makaburi ya Manabii wao kuwa Misikiti.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Muslim akaongeza: “Na Manaswara.”

Nao (Al-Bukhaariy, Muslim) wamepokea kuwa: “Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: Walikuwa akifariki mtu mwema miongoni mwao (Mayahudi na Manaswara) wanajenga juu ya kaburi lake Msikiti.”

Katika Hadiyth hiyo hiyo iliongezwa: “Hao ni viumbe waovu kabisa katika viumbe[2].”

198.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {بَعَثَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خَيْلاً، فَجَاءَتْ بِرَجُلٍ، فَرَبَطُوهُ بِسَارِيَةٍ مِنْ سَوَارِي الْمَسْجِدِ} الْحَدِيثُ . مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituma wapanda farasi ambao walirudi na mtu mmoja, kisha wakamfunga[3] katika moja ya nguzo za Msikiti.[4]” [Al-Bukhaariy, Muslim]

199.

وَعَنْهُ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ مَرَّ بِحَسَّانَ يَنْشُدُ فِي الْمَسْجِدِ ، فَلَحَظَ إِلَيْهِ ، فَقَالَ : "قَدْ كُنْتُ أَنْشُدُ ، وَفِيهِ مَنْ هُوَ خَيْرٌ مِنْكَ" مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena: “Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimkuta Hassan[5] akiimba mashairi Msikitini, akamtazama kwa jicho kali, akasema Nilikuwa naimba

Msikitini[6] akiwemo mbora zaidi kuliko wewe (yaani Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

200.

وَعَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَنْ سَمِعَ رَجُلًا يَنْشُدُ ضَالَّةً فِي الْمَسْجِدِ فَلْيَقُلْ : لَا رَدَّهَا اللَّهُ عَلَيْكَ، فَإِنَّ الْمَسَاجِدَ لَمْ تُبْنَ لِهَذَا { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kumsikia mtu anatangaza Msikitini kupoteza kitu, aseme: Allaah Asikurejeshee[7] ulichopoteza, kwani Misikiti haikujengwa kwa ajili ya hilo.” [Imetolewa na Muslim]

201.

وَعَنْهُ : أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا رَأَيْتُمْ مَنْ يَبِيعُ ، أَوْ يَبْتَاعُ فِي الْمَسْجِدِ، فَقُولُوا: لَا أَرْبَحَ اللَّهُ تِجَارَتَكَ { رَوَاهُ النَّسَائِيُّ ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkimuona anayenunua au anauza[8] vitu Msikitini, semeni” “Allaah Asiipe faida biashara yako[9]” [Imetolewa na An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy, naye aliita Hasan]

202.

وَعَنْ حَكِيمِ بْنِ حِزَامٍ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَا تُقَامُ الْحُدُودُ فِي الْمَسَاجِدِ ، وَلَا يُسْتَقَادُ فِيهَا { رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَأَبُو دَاوُدَ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Hakiym bin Hizaam[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Adhabu hazitekelezwi Msikitini wala kisasi hakilipwi humo.” [Imetolewa na Ahmad, na Abuu Daawuwd, kupitia Isnaad dhaifu]

203.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : { أُصِيبَ سَعْدٌ يَوْمَ الْخَنْدَقِ ، فَضَرَبَ عَلَيْهِ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خِيَمَةً فِي الْمَسْجِدِ ، لِيَعُودَهُ مِنْ قَرِيبٍ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Katika siku ya Al-Khandaq (vita vya mahandaki), Sa’d[11] aliumia, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamwekea hema Msikitini ili awe karibu[12] kumzuru.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

204.

وَعَنْهَا قَالَتْ : {رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
يَسْتُرُنِي، وَأَنَا أَنْظُرُ إِلَى الْحَبَشَةِ يَلْعَبُونَ فِي الْمَسْجِدِ . . . }
الْحَدِيثُ . مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema tena:
“Nilimuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
akinikinga wakati nikiangalia Wahabeshi[13] waliokuwa wanacheza
Msikitini[14].” [Al-Bukhaariy, Muslim]

205.

وَعَنْهَا : {أَنَّ وَلِيدَةً سَوْدَاءَ كَانَ لَهَا خِבَاءٌ فِي الْمَسْجِدِ ،
فَكَانَتْ تَأْتِينِي ، فَتَحَدَّثُ عِنْدِي . . . } الْحَدِيثُ . مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema tena: “Mjakazi
mmoja mweusi alikuwa na hema Msikitini na alikuwa akinijia na
kuongea nami[15].” [Al-Bukhaariy, Muslim]

206.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْبُزَاقُ فِي الْمَسْجِدِ خَطِيئَةٌ وَكَفَّارَتُهَا دَفْنُهَا}
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kutema mate Msikitini
ni dhambi, na kafara yake ni kuyazika.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

207.

وَعَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَقُومُ
السَّاعَةُ حَتَّى يَتَبَاهَى النَّاسُ فِي الْمَسَاجِدِ } أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ
إِلَّا التِّرْمِذِيَّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Qiyaamah
hakitasimama hadi watu wajifakharishe (kuhusiana na majengo na
mapambo ya) Misikitini[16].” [Imetolewa na Al-Khamsah (An-
Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa At-
Tirmidhiy, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

208.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَا أَمِرْتُ بِتَشْيِيدِ الْمَسَاجِدِ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ
، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mimi
sikuamrisha kurefusha na kupamba Misikiti[17].” [Imetolewa na
Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

209.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {عُرِضَتْ عَلَيَّ أَجُورُ أُمَّتِي ، حَتَّى الْقَذَاةُ يُخْرِجُهَا الرَّجُلُ مِنَ الْمَسْجِدِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَاسْتُغْرِبَهُ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Nilionyeshwa malipo ya Ummah wangu, hadi punje ya vumbi anayoiondoa mtu Msikitini.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na At-Tirmidhiy aliyeipa daraja la Ghaarib (ngeni), na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

210.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا دَخَلَ أَحَدُكُمْ الْمَسْجِدَ فَلَا يَجْلِسْ حَتَّى يُصَلِّيَ رَكْعَتَيْنِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Qataadah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu anapoingia Msikitini, asiketi mpaka aswali Rakaa mbili[18].” [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Ili mtu aswali karibu na nyumbani kwake.

[2] “Kugeuza makaburi kuwa Misikiti” kuna maana mbili. Kwanza, matendo ambayo yanatakiwa kufanywa mbele ya Allaah (سبحانه وتعالى) ndani ya Misikiti, yanafanywa karibu au juu ya makaburi kwa mfano kusujudu, kuinama, kukalia mapaja, au kusimama huku mikono imekunjwa kama ishara ya heshima. Pili, kujenga Misikiti karibu na makaburi kwa maana yoyote iwayo, kumekatazwa kabisa.

[3] Maana yake: kwa muda mfupi Msikiti unaweza kutumika kama mahabusu.

[4] Hadiyth hii inaonyesha kuwa mtu asiyekuwa Muislamu anaweza kuingia Msikitini kwa kuwa si msafi kiasili bali kidhahiri; lakini haruhusiwi kuingia ndani ya Ka’bah takatifu na hawezi kuhiji.

[5] Hassan huyu ndiye Hassan bin Thaabit Al-Answaar Al-Khazraj, aliyekuwa mshairi wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Abuu ‘Ubayda alisema kuwa: “Waarabu wameafiki kuwa Hassan bin Thaabit alikuwa mshairi mzuri kuliko wote.” Alikufa kabla ya mwaka 40 A.H zama za Ukhalifa wa ‘Aliy. Pia inasemekana kuwa alikufa mnamo mwaka 50 A.H. akiwa na umri wa miaka 120 ambayo miaka 60 ya hiyo alikuwa yumo bado katika ujahili, na miaka 60 alikuwa katika Uislaam.

[6] Huu ni ushahidi kuwa maadili mema na ushairi wa juu vyaweza kusomwa ndani ya Msikiti. Hassan bin Thaabit alikuwa akisoma mashairi muhimu kujibu mashairi ya makafiri yanayoudhihaki Uislaam, naye Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) daima alikuwa akimsifu Hassan kwa kusema kuwa: “Jibriyl anakusaidia.”

[7] Hii ni kuwalaumu wanaosema upuuzi Msikitini. Kwa mfano, itokeapo ng'ombe wamepotea, mwenyewe asiulize ndani ya Msikiti kutoka kwa watu kwa kuwavurugia utulivu wao kwa Allaah (سبحانه وتعالى). Akitaka, asimame kwenye lango la Msikiti aulize.

[8] Inamaanisha Misikiti isitumike kama masoko, kwa sababu itaathiri heshima ya Misikiti.

[9] Kufanya biashara Msikitini kumekatazwa. Yoyote anayefanya biashara mle, atahesabika kuwa ni mwenye dhambi, lakini mauziano yatakuwa Halaal.

[10] Huyu Hakiym bin Hizaam ndiye Abuu Khaalid Al-Qurashi Al-Asadi, kaka yake Khadiyjah "Mama wa Waumini". Alikuwa miongoni mwa watu watukufu wa Maquraysh, na alizaliwa ndani ya Ka'bah miaka 13 kabla ya tukio la tembo. Alisilimu mnamo mwaka wa kutekwa Makkah, na alikufa Madiynah mnamo mwaka 54 A.H. akiwa na umri wa miaka 120.

[11] Sa'd bin Mu'aadh alikuwa kiongozi wa Al- Aws na mmoja wa Swahaba wakuu. Alisilimu kati ya 'Aqaba ya kwanza na ya Bukhaariy na Muslim pili, na Banu 'Abdul-Ashhar wakasilimu kwa athari ya Uislaam. Alikuwa anaheshimiwa na anatiiwa sana na watu wake. Alipigwa mshale katika Vita vya Handaki, na kafariki kwa jeraha lile baada ya Vita vya Banu Quraydha mnamo mwezi wa Dhul-Hijjah mwaka wa 5 A.H

[12] Hadiyth hii ni ushahidi kuwa kuweka hema ndani ya Msikiti la mtu mgonjwa au aliyejeruhiwa kukaa mle inaruhusiwa.

[13] Yaani mwanamke anaweza kumtazama mwanamume bila niyyah maalumu.

[14] Mazoezi yanayosaidia katika vita vya Jihaad yaruhusiwa kufanyiwa Msikitini, na wale Wahabeshi walikuwa wakicheza michezo ya kivita.

[15] Hadiyth kamili imesimuliwa katika Swahiyh Al-Bukhaariy. Lengo la kuisimulia hapa ni kufahamisha kuwa mwanamke pia anaweza kukaa Msikitini na kuweka hema Msikitini imeruhusiwa.

[16] Inamaanisha kuwa, watu watashindana kifahari, na watajivunia upambaji na uzuri wa Misikiti yao. Pia inaweza kumaanisha kuwa watajivunia uku una umaarufu wao ndani ya Misikiti.

[17] Inaonyesha kuwa, kwa kuwa ni desturi ya Kiyahudi, imekatazwa kuchora na kuiremba Misikiti.

[18] Hii ni wazi kuwa Rakaa hizi mbili ni za Tahiyyatul-Masjid (maamkizi ya Msikiti). Baadhi ya ‘Ulamaa wanazihesabu hizi ni za lazima, wakati wengine wengi wanazihesabu kuwa ni za hiari. Ukichunguza maana ya Hadiyth utaona kuwa ‘Ulamaa wengine wameiruhusu Swalaah hii iswaliwe hata nyakati za makruwh (zinazokatazwa kuswali), ambapo wengine wanakataza isiswaliwe nyakati hizo.

07-Mlango Wa Sifa Ya Swalaah

بَابُ صِفَةِ الصَّلَاةِ

07-Mlango Wa Sifa Ya Swalaah

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا قُمْتُ إِلَى الصَّلَاةِ فَأَسْبِغِ الْوُضُوءَ ، ثُمَّ اسْتَقْبِلِ الْقِبْلَةَ، فَكَبِّرْ، ثُمَّ اقْرَأْ مَا تيسَّرَ مَعَكَ مِنَ الْقُرْآنِ ، ثُمَّ ارْكَعْ حَتَّى تَطْمِئِنَّ رَاكِعًا، ثُمَّ ارْفَعْ حَتَّى تَعْتَدِلَ قَائِمًا، ثُمَّ أَسْجُدْ حَتَّى تَطْمِئِنَّ سَاجِدًا، ثُمَّ ارْفَعْ حَتَّى تَطْمِئِنَّ جَالِسًا، ثُمَّ أَسْجُدْ حَتَّى تَطْمِئِنَّ سَاجِدًا، ثُمَّ ارْفَعْ حَتَّى تَطْمِئِنَّ جَالِسًا، ثُمَّ أَسْجُدْ حَتَّى تَطْمِئِنَّ سَاجِدًا، ثُمَّ افْعَلْ ذَلِكَ فِي صَلَاتِكَ كُلِّهَا} أَخْرَجَهُ السَّبْعَةُ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

وَلِابْنِ مَاجَةَ بِإِسْنَادٍ مُسْلِمٍ : {حَتَّى تَطْمِئِنَّ قَائِمًا} وَمِثْلُهُ فِي حَدِيثِ رِفَاعَةَ عِنْدَ أَحْمَدَ وَابْنِ حِبَّانَ {حَتَّى تَطْمِئِنَّ قَائِمًا}

وَفِي لَفْظٍ لِأَحْمَدَ : {فَاقِمِ صُلْبَكَ حَتَّى تَرْجِعَ الْعِظَامُ} وَلِلنَّسَائِيِّ ، وَأَبِي دَاوُدَ مِنْ حَدِيثِ رِفَاعَةَ بْنِ رَافِعٍ : {إِنَّهَا لَنْ تَتِمَّ صَلَاةُ أَحَدِكُمْ حَتَّى يُسْبِغَ الْوُضُوءَ كَمَا أَمَرَهُ اللَّهُ، ثُمَّ يُكَبِّرَ اللَّهَ، وَيَحْمَدَهُ ، وَيُثْنِي عَلَيْهِ}

وَفِيهَا {فَإِنْ كَانَ مَعَكَ قُرْآنٌ فَاقْرَأْ وَإِلَّا فَاحْمَدِ اللَّهَ ، وَكَبِّرْهُ ، وَهَلِّلْهُ}

وَلِأَبِي دَاوُدَ : {ثُمَّ اقْرَأْ بِأَمِّ الْقُرْآنِ وَبِمَا شَاءَ اللَّهُ} وَلِابْنِ حِبَّانَ : {ثُمَّ بِمَا شِئْتَ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ukisimama kuswali, tawadha vizuri na kikamilifu, kisha elekea Qiblah, na piga

takbiyra kisha soma unachoweza katika Qur-aan[1], kisha rukuu hadi utulie ukiwa katika rakaa, kisha inuka na usimame wima, kisha sujudu hadi utulie ukiwa katika sajdah, kisha inuka na utulie ukiwa umeketi[2], kisha sujudu tena na utulie katika sajdah, kisha ufanye vivyo hivyo katika Swalaah yako yote.” [Imetolewa na As-Sab’ah (Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Pia ni tamshi la Ibn Maajah kwa Isnaad ya Muslim: “Mpaka utulie ukiwa umesimama wima.”

Hadiyth ya Rifaa’ah[3] iliyoko kwa Ahmad na Ibn Hibbaan: “Mpaka utulie hali ya kuwa umesimama.”

Naye Ahmad amesema: “Unyooshe mgongo wako hadi mifupa irejee nafasi zake.”

Nao An-Nasaaiy na Abuu Daawuud wamepokea Hadiyth ya Rifaa’ah bin Raafi’ inasema: “Swalaah ya mmoja wenu haitatimia hadi atawadhe sawasawa kama Allaah Alivyoamrisha, kisha apige takbiyra na amhimidi na kumsifu Yeye.”

Pia inatajwa katika Hadiyth hiyo kuwa: “Ukiwa unajua sehemu yoyote ya Qur-aan, isome, vinginevyo mhimidi Allaah (AlhamduliLLaah), mpigie takbiyra (Allaahu Akbar) na mpwekeshe kwa tahliyl (laa ilaaha illa-Allaah).”

Na Abuu Daawuud amesema: “Kisha soma Ummul-Qur-aan[4] (Suwrah Al-Faatihah) na kisha kila Atakacho Allaah.”

Na Ibn Hibbaan akasema: “na (usome) chochote unachotaka”

وَعَنْ أَبِي حُمَيْدٍ السَّاعِدِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {رَأَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا كَبَّرَ جَعَلَ يَدَيْهِ حَذْوَ مَنْكَبَيْهِ ، وَإِذَا رَكَعَ أَمَكَّنَ يَدَيْهِ مِنْ رُكْبَتَيْهِ ، ثُمَّ هَصَرَ ظَهْرَهُ ، فَإِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ اسْتَوَى حَتَّى يَعُودَ كُلُّ فَقَارٍ مَكَانَهُ ، فَإِذَا سَجَدَ وَضَعَ يَدَيْهِ غَيْرَ مُفْتَرَشٍ وَلَا قَابِضِهِمَا ، وَاسْتَقْبَلَ بِأَطْرَافِ أَصَابِعِ رِجْلَيْهِ الْقِبْلَةَ ، وَإِذَا جَلَسَ فِي الرُّكْعَتَيْنِ جَلَسَ عَلَى رِجْلِهِ الْيُسْرَى وَنَصَبَ الْيُمْنَى ، وَإِذَا جَلَسَ فِي الرُّكْعَةِ الْآخِرَةِ قَدَّمَ رِجْلَهُ الْيُسْرَى وَنَصَبَ الْآخَرَى ، وَقَعَدَ عَلَى مَقْعَدَتِهِ { أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [5] Kutoka kwa Abuu Humayd As-Saa'idiyy[5] (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) [6] amesema: “Nimemuona Nabiy[6] akipiga Takbiyra aliweka mikono yake sambamba na mabega yake[7], na aliporukuu aliweka mikono yake kwenye magoti, na alikunja mgongo wake, alipoinuka alisimama wima hadi mifupa ya uti wa mgongo ikarejea mahali pake, aliposujudu, aliweka mikono yake bila kuisambaza wala kuifumba; na ncha za vidole vyake vya miguu vikawa vinaelekea Qiblah, alipoketi katika rakaa mbili, alikalia mguu wake wa kushoto na kusimamisha wa kuume, na alipoketi katika rakaa ya mwisho alitanguliza mbele mguu wake wa kushoto na akasimamisha wa kuume na akakalia makalio yake. “ [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

وَعَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ كَانَ إِذَا قَامَ إِلَى الصَّلَاةِ قَالَ : "وَجَّهْتُ وَجْهِي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ" . . . إِلَى قَوْلِهِ : "مِنْ الْمُسْلِمِينَ ، اَللَّهُمَّ أَنْتَ الْمَلِكُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ ، أَنْتَ رَبِّي وَأَنَا عَبْدُكَ . . . } إِلَى آخِرِهِ . رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ : أَنَّ ذَلِكَ فِي صَلَاةِ اللَّيْلِ

Kutoka kwa ‘Aliy bin Abiy Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akisimama kuswali, alikuwa akisema[8]: “*Wajjahtu wajhiya li-Lladhiy fatwaras-samaawaati...*” mpaka: “*minal muslimiyna. Allaahumma Antal-Maliku laa ilaaha illaa Anta, Anta Rabbiy wa anaa ‘abduka*” mpaka mwisho wake. (Nimeelekeza uso wangu kwa Aliyeumba mbingu na ardhi”, hadi kauli yake: “miongoni mwa Waislamu. Ee Allaah, Wewe Ndiye Mfalme, hapana mwabudiwa wa haki ila Wewe, Wewe ni Rabb wangu na mimi ni mja wako[9]).” [Imetolewa na Muslim]

Na katika mapokezi yake (Muslim) mengine: “Hayo ni katika Swalaah ya usiku.”

214.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا كَبَّرَ لِلصَّلَاةِ سَكَتَ هُنَيْئَةً ، قَبْلَ أَنْ يَقْرَأَ ، فَسَأَلْتُهُ ، فَقَالَ : "أَقُولُ : اَللَّهُمَّ بَاعِدْ بَيْنِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ ، اَللَّهُمَّ نَقِّنِي مِنْ

خَطَايَايَ كَمَا يُنْقَى التَّوْبُ الْأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ ، اَللَّهُمَّ اغْسِلْنِي
مِنْ خَطَايَايَ بِالْمَاءِ وَالتَّلْجِ وَالْبَرَدِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akishasoma
Takbiyra ya Swalaah alinyamaza kidogo kabla ya kusoma Qur-aan.
Nikamuuliza juu ya hilo, akasema: Nasema:

*“Allaahumma baa'id bayniy wa bayna khatwaayaaya kamaa
baa'adta baynal-Mashriqi wal-Maghrib. Allaahumma naqqiniy min
khatwaayaaya kamaa yunaqqath-thawbul abyadhwu minad-danasi.
Allaahumma-ghsiliniy min khatwaayaaya bil-maai wath-thalji wal-
barad.”*

(Ee Allaah niweke mbali na makosa yangu kama Ulivyoweka mbali
baina ya Mashariki na Magharibi, Ee Allaah nisafishe makosa yangu
kama vile inavyosafishwa nguo nyeupe kutokana na uchafu, Ee
Allaah nisafishe makosa yangu kwa maji na theluji na barafu). [Al-
Bukhaariy, Muslim]

215.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ كَانَ يَقُولُ : {سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ
وَبِحَمْدِكَ ، تَبَارَكَ إِسْمُكَ ، وَتَعَالَى جَدُّكَ ، وَلَا إِلَهَ غَيْرُكَ}
رَوَاهُ مُسْلِمٌ بِسَنَدٍ مُنْقَطِعٍ ، وَالْأَدَارِقُطْنِيُّ مَوْصُولًا وَهُوَ
مَوْقُوفٌ

وَنَحْوُهُ عَنْ أَبِي سَعِيدٍ مَرْفُوعًا عِنْدَ الْخَمْسَةِ

وَفِيهِ : وَكَانَ يَقُولُ بَعْدَ التَّكْبِيرِ : {أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ
مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ، مِنْ هَمْزِهِ ، وَنَفْخِهِ ، وَنَفْثِهِ }

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisema:

”Subhaanaka-LLaahumma wabihamdika wa Tabaarakas-Smuka wa Ta’aalaa Jadduka walaa ilaaha Ghayruka.”

(Utakasifu ni Wako Ee Allaah, na Himdi ni Zako, na Limebarikika Jina Lako, na Utukufu Wako uko juu, na hapana mwabudiwa wa haki ghairi Yako) [Imetolewa na Muslim kwa Isnaad iliyo Munqatwi’ (iliyokatika). Na katika Riwaayah ya Ad-Daaraqutwniy ina Isnaad Mawsuwl na Mawquwf]

Hadiyth kama hiyo ameisimulia Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy ambayo ni Marfuw’ kwa Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) imesema: “(Nabiy) alikuwa akisema baada ya Takbiyra:

”‘Auwdhu biLLaahis-Samiy’il ‘Aliymi mina-sh-shaytwaanir-rajiym min hamzihi wa nafkhihi, wa nafthihi.”

(Najilindia na Allaah kutokana na shaytwaan aliyefukuzwa na kulaaniwa, najilinda na kutokana na wazimu wake au ushauri wake muovu, na upulizaji wake, na kutabana kwake au uchawi wake).

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَسْتَفْتِحُ الصَّلَاةَ بِالتَّكْبِيرِ ، وَالْقِرَاءَةِ : بِ (الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ) وَكَانَ إِذَا رَكَعَ لَمْ يُشْخِصْ رَأْسَهُ ، وَلَمْ يُصَوِّبْهُ ، وَلَكِنْ بَيْنَ ذَلِكَ . وَكَانَ إِذَا رَفَعَ مِنَ الرُّكُوعِ لَمْ يَسْجُدْ حَتَّى يَسْتَوِيَ قَائِمًا . وَإِذَا رَفَعَ مِنَ السُّجُودِ لَمْ يَسْجُدْ حَتَّى يَسْتَوِيَ جَالِسًا . وَكَانَ يَقُولُ فِي كُلِّ رَكَعَتَيْنِ التَّحِيَّةَ . وَكَانَ يَفْرَشُ رِجْلَهُ الْيُسْرَى وَيَنْصِبُ الْيُمْنَى . وَكَانَ يَنْهَى عَنْ عُقْبَةِ الشَّيْطَانِ ، وَيَنْهَى أَنْ يَفْتَرِشَ الرَّجُلُ زَرَاعِيهِ إِفْتِرَاشَ السَّبْعِ . وَكَانَ يُخْتَمُ الصَّلَاةُ بِالتَّسْلِيمِ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ ، وَلَهُ عِلَّةٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akianza Swalaah kwa Takbiyra na kusoma:

“*AlhamduliLlaahi Rabbil ‘Aalamiyn*[10]

Na aliporukuuu, hakuinua kichwa chake wala hakiinamishi, bali alikiweka baina ya sehemu hizi mbili. Alipoinua kichwa chake kutoka katika kurukuu, hokusujudu hadi aliposimama wima, na alipoinua kichwa chake baada ya kusujudu, hakurudia kusujudu mpaka alipoinuka na kuketi kitako, alikuwa akisoma katika Rakaa mbili At-Tahiyyah. Na alikuwa akitandika mguu wake wa kushoto na kuusimamisha wima wa kuume; na alikuwa alikataza mkao wa shaytwaan wa kukalia[11] makalio, na akakataza watu kutandika mikono yao kama wanyama, na alikuwa akikhitimisha Swalaah kwa tasliym (Assalaamu ‘alaykum).” [Imetolewa na Muslim, na ina dosari]

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَرْفَعُ يَدَيْهِ حَذْوَ مَنْكِبَيْهِ إِذَا افْتَتَحَ الصَّلَاةَ، وَإِذَا كَبَّرَ لِلرُّكُوعِ، وَإِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي حَدِيثِ أَبِي حُمَيْدٍ، عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ: { يَرْفَعُ يَدَيْهِ حَتَّى يُحَازِيَ بِهِمَا مَنْكِبَيْهِ، ثُمَّ يُكَبِّرُ }

وَلِمُسْلِمٍ عَنْ مَالِكِ بْنِ الْحُوَيْرِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ نَحْوُ حَدِيثِ ابْنِ عُمَرَ، وَلَكِنْ قَالَ: { حَتَّى يُحَازِيَ بِهِمَا فُرُوعَ أُذُنَيْهِ }

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akinyanyua mikono yake usawa wa mabega[12] yake, anapoanza Swalaah, na anapopiga Takbiyra kwa ajili ya kurukuu, na aliponyanya kichwa chake baada ya kurukuu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Hadiyth aliyopokea Abuu Daawuwd kutoka kwa Abuu Humayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “(Nabiy) alikuwa akinyanyua mikono yake na kuiweka sambamba na mabega yake, kisha anapiga takbiyra.”

Katika Hadiyth ya Muslim iliyosimuliwa na Maalik bin Al-Huwayrith (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) ni sawa sawa kama Hadiyth iliyosimuliwa na Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) lakini yeye (Maalik bin Al-Huwayrith) alitaja kuwa: “Nabiy alikuwa akinyanyua mikono yake sambamba na mwisho wa masikio yake.”

218.

وَعَنْ وَائِلِ بْنِ حُجْرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { صَلَّيْتُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَوَضَعَ يَدَهُ الْيُمْنَى عَلَى يَدِهِ الْيُسْرَى عَلَى صَدْرِهِ } أَخْرَجَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Waail bin Hujr[13] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mimi niliswali na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) naye aliweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto, na kisha akaiweka juu ya kifua[14] chake.” [Imetolewa na Ibn Khuzaymah]

219.

وَعَنْ عُبَادَةَ بْنِ الصَّامِتِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَا صَلَاةَ لِمَنْ لَمْ يَقْرَأْ بِأَمِّ الْقُرْآنِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ ، لِابْنِ حِبَّانَ وَالْدَّارَقُطْنِيِّ : { لَا تَجْزِي صَلَاةٌ لَا يُقْرَأُ فِيهَا بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ }

وَفِي أُخْرَى ، لِأَحْمَدَ وَأَبِي دَاوُدَ ، وَالتِّرْمِذِيِّ ، وَابْنِ حِبَّانَ : { لَعَلَّكُمْ تَقْرَأُونَ خَلْفَ إِمَامِكُمْ ؟ " قُلْنَا : نَعَمْ . قَالَ : " لَا تَفْعَلُوا إِلَّا بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ ، فَإِنَّهُ لَا صَلَاةَ لِمَنْ لَمْ يَقْرَأْ بِهَا }

Kutoka kwa ‘Ubaadah bin Asw-Swaamit[15] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna Swalaah kwa mtu asiyesoma *Ummul-Qur-aan* (Suwrah Al-Faatihah)[16].” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Ibn Hibbaan na Ad-Daaraqutwniy: “Haijuzu Swalaah isiyosomwa ndani yake Suwrah Al-Faatihah.”

Na Riwaayah nyingine ya Ahmad, Abuu Daawuud, At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan: “Huenda mnasoma nyuma ya Imaam wenu? Tukasema: “Ndiyo.” Akasema: “Msifanye hivyo, isipokuwa kwa Suwrah Al-Faatihah kwani hana Swalaah asiyeisoma.”

220.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَأَبَا بَكْرٍ وَعُمَرَ كَانُوا يَفْتَتِحُونَ الصَّلَاةَ بِ (الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ) { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

زَادَ مُسْلِمٌ: { لَا يَذْكُرُونَ : (بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ) فِي أَوَّلِ قِرَاءَةٍ وَلَا فِي آخِرِهَا }

وَفِي رِوَايَةٍ لِأَحْمَدَ ، وَالنَّسَائِيَّ وَابْنِ خُزَيْمَةَ : { لَا يَجْهَرُونَ بِبِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ }

وَفِي أُخْرَى لِابْنِ خُزَيْمَةَ : { كَانُوا يُسِرُّونَ }

وَعَلَى هَذَا يُحْمَلُ النَّفْيُ فِي رِوَايَةِ مُسْلِمٍ ، خِلَافًا لِمَنْ أَعْلَاهَا

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) , Abuu Bakr na ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا)

walikuwa wakianza Swalaah kwa: “*AlhamduliLLaahi Rabbil ‘Aalamiyn.*” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Muslim aliongezea: “Walikuwa hawasomi “*BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiym*” mwanzoni, wala mwishoni wake.[17]”

Na katika Riwaayah ya Ahmad, An-Nasaaiy na Ibn Khuzaymah: “Hawadhihirishi *BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiym* kwa sauti.”

Na katika Riwaayah ya Ibn Khuzaymah: “Walikuwa wanasoma (*BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiym*)[18]”

Na juu ya hili katika Riwaayah ya Muslim, tofauti na wenye kuitia dosari.

221.

نُعِيْمُ الْمُجَمَّرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { صَلَّيْتُ وَرَاءَ أَبِي
هُرَيْرَةَ فَقَرَأَ : (بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ) . ثُمَّ قَرَأَ بِأَمِّ
الْقُرْآنِ ، حَتَّى إِذَا بَلَغَ : (وَلَا الضَّالِّينَ) ، قَالَ : "أَمِينَ"
وَيَقُولُ كُلَّمَا سَجَدَ ، وَإِذَا قَامَ مِنَ الْجُلُوسِ : اللَّهُ أَكْبَرُ . ثُمَّ
يَقُولُ إِذَا سَلَّمَ : وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ إِنِّي لَأَشْبَهُكُمْ صَلَاةَ بِرَسُولِ
اللَّهِ } رَوَاهُ النَّسَائِيُّ وَابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Nu’aym Al-Mujammir[19] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)

amesema: “Niliswali nyuma ya Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)

alisoma: “*BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiym*”, kisha Ummul-Qur-
aan (Al-Faatihah), alipofika: “*Waladhw-dhwaalliyna*” alisema:

“Aamiyn.”[20] Akawa anasema: “*Allaahu Akbar*” kila aliposujudu na alipoinuka na kusimama kutoka katika Sijdah, na alipotoa salaam yaani kusema: “Assalaam ‘alaykum” alisema: “Ninaapa kwa Ambaye roho yangu iko Mkononi Mwake, Swalaah yangu inafanana sana na ile ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuliko yeyote miongoni mwenu.” [Imetolewa na An-Nasaaiy na Ibn Khuzaymah]

222.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا قَرَأْتُمْ الْفَاتِحَةَ فَاقْرَءُوا : (بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ) ، فَإِنَّهَا إِحْدَى آيَاتِهَا { رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ ، وَصَوَّبَ وَقَفَهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mnaposoma Suwrah Al-Faatihah someni “*BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiyim*”, kwani hiyo ni moja ya Aayah zake.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy, aliyeipa daraja la Mawquwf]

223.

وَعَنْهُ قَالَ : { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا فَرَغَ مِنْ قِرَاءَةِ أَمِّ الْقُرْآنِ رَفَعَ صَوْتَهُ وَقَالَ : "أَمِينَ" . } رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَحَسَّنَهُ ، وَالْحَاكِمُ وَصَحَّحَهُ

- وَلِأَبِي دَاوُدَ وَالتِّرْمِذِيِّ مِنْ حَدِيثِ وَائِلِ بْنِ حُجْرٍ نَحْوُهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipomaliza kusoma *Ummul-Qur-aan* alipaza sauti yake na kusema “Aaamiyn.”
[21] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy, aliyeipa daraja la Hasan, na akaisahihisha Al-Haakim]

Na Abuu Daawuwd na At-Tirmidhiy wamepokea masimulizi ya Waail bin Hujri mfano wake.

224.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي أَوْفَى رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : { جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ : إِنِّي لَا أَسْتَطِيعُ أَنْ أَخُذَ مِنَ الْقُرْآنِ شَيْئًا ، فَعَلَّمَنِي مَا يُجْزئُنِي مِنْهُ . قَالَ : "سُبْحَانَ اللَّهِ ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ ، وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ ، وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ . . . } الْحَدِيثَ . رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَأَبُو دَاوُدَ ، وَالتِّرْمِذِيُّ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ ، وَالْحَاكِمُ .

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Abiy Awfaa[22] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Mtu mmoja alikuja kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Mimi siwezi kuhifadhi chochote katika Qur-aan, kwa hivyo nifundishe kitakachonitosha humo, akasema: Sema:

“*Subhaana-Allaah*, (Utakasifu ni wa Allaah), “*Wal-Hamdu liLLaah* (Himdi ni za Allaah) *wa laa ilaaha illa Allaah* (na hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah) *wa-Allaahu Akbar* (na Allaah ni Mkubwa Zaidi), *wa laa hawla wa laa quwwata illa biLLaahil-‘Aliyyil-‘Adhwiym* (na hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Allaah Aliyetukuka Aliye ‘Adhimu).[23]” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuwd, na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan, Ad-Daaraqutwniy na Al-Haakim]

225.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي بِنَا ، فَيَقْرَأُ فِي الظُّهْرِ وَالْعَصْرِ فِي الرَّكْعَتَيْنِ الْأُولَيَيْنِ بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ وَسُورَتَيْنِ ، وَيُسْمِعُنَا الْآيَةَ أَحْيَانًا ، وَيُطَوِّلُ الرَّكْعَةَ الْأُولَى ، وَيَقْرَأُ فِي الْآخِرَتَيْنِ بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ. } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Qataadah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akituswalisha anasoma katika Swalaah ya Adhuhuri na Alasiri, Suwrah Al-Faatihah katika Rakaa mbili za mwanzo, pamoja na Suwrah zingine mbili, na mara nyingine alitusikilizisha Aayah[24], alikuwa akiirefusha Rakaa ya mwanzo, na alikuwa akisoma Suwrah Al-Faatihah tu katika Rakaa mbili za mwisho.[25]” [Al-Bukhaariy, Muslim]

226.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {كُنَّا نَحْزُرُ قِيَامَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الظُّهْرِ وَالْعَصْرِ ، فَحَزَرْنَا قِيَامَهُ فِي الرُّكْعَتَيْنِ الْأُولَيَيْنِ مِنَ الظُّهْرِ قَدْرَ : (الْمِ تَنْزِيلُ) السَّجْدَةِ . وَفِي الْآخِرَتَيْنِ قَدْرَ النِّصْفِ مِنْ ذَلِكَ . وَفِي الْأُولَيَيْنِ مِنَ الْعَصْرِ عَلَى قَدْرِ الْآخِرَتَيْنِ مِنَ الظُّهْرِ ، وَالْآخِرَتَيْنِ عَلَى النِّصْفِ مِنْ ذَلِكَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Tulikuwa tukikisia urefu wa kisimamo cha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika Swalaah za Adhuhuri na Alasiri na tukapata ni kadiri ya kusoma Suwrah ya "Alif Laam Miym Tanziyl" (Suwrah As-Sajdah)[26], na katika Rakaa za mwisho mbili kadiri ya nusu ya hivyo, na katika Rakaa mbili za mwanzo za Swalaah ya Alasiri, alikuwa akisimama kwa muda kadiri ya Rakaa mbili za Swalaah ya Adhuhuri, na Rakaa mbili za mwisho kadiri ya nusu ya urefu wa Rakaa mbili za mwanzo." [Imetolewa na Muslim]

227.

وَعَنْ سُلَيْمَانَ بْنِ يَسَارٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {كَانَ فُلَانٌ يُطِيلُ الْأُولَيَيْنِ مِنَ الظُّهْرِ ، وَيُخَفِّفُ الْعَصْرَ ، وَيَقْرَأُ فِي الْمَغْرِبِ بِقِصَارِ الْمَفْصَلِ وَفِي الْعِشَاءِ بَوَسْطِهِ وَفِي الصُّبْحِ بِطُولِهِ . فَقَالَ أَبُو هُرَيْرَةَ : "مَا صَلَّيْتُ وَرَاءَ أَحَدٍ أَشَبَّهَ صَلَاةَ بِرَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مِنْ هَذَا} أَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ بِإِسْنَادٍ صَحِيحٍ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Sulaymaan bin Yasaar[27] amesema: “Fulani alikuwa akirefusha Rakaa mbili za mwanzo za Swalaah ya Adhuhuri, na akifupisha Alasiri na akisoma Suwrah fupi ya *Mufasw-swal*[28] wakati wa Swalaah ya Magharibi, na Suwrah za wastani kwa Swalaah ya ‘Ishaa, na Suwrah ndefu wakati wa Alfajiri.” Kisha Abuu Hurayrah akasema: “Sijaswali nyuma ya yeyote ambaye Swalaah yake inafanana zaidi na Swalaah ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuliko huyu.” [Imetolewa na An-Nasaaiy kwa Isnaad Swahiyh]

228.

وَعَنْ جُبَيْرِ بْنِ مُطْعِمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ فِي الْمَغْرِبِ بِالطُّورِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jubayr bin Mutw'im (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisoma Suwrah “Atw-Twuwr” katika Swalaah ya Magharibi.[29]” [Al-Bukhaariy, Muslim]

229.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ فِي صَلَاةِ الْفَجْرِ يَوْمَ الْجُمُعَةِ: (الْمُتَزِيلُ) السَّجْدَةَ، وَ (هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ) مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِلطَّبَرَانِيِّ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ مَسْعُودٍ : {يُدِيمُ ذَلِكَ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisoma katika Swalaah ya Alfajiri siku ya Ijumaa “*Alif-Laam-Miym Tanziyl...*” (As-Sajdah) na “Hal ataa ‘alal Insaani” (ambayo pia huitwa Suwrah Ad-Dahr)?[30]” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Atw-Twabaraaniyy imepokea Hadiyth ya Ibn Mas-‘uwd ikiwa na nyongeza kuwa: “Rasuli akidumisha hivyo.[31]”

230.

وَعَنْ حُذَيْفَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {صَلَّيْتُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَمَا مَرَّتْ بِهِ آيَةُ رَحْمَةٍ إِلَّا وَقَفَ عِنْدَهَا يَسْأَلُ، وَلَا آيَةَ عَذَابٍ إِلَّا تَعَوَّذَ مِنْهَا} أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Hudhayfah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nimeswali pamoja na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na hakuipita Aayah ya Rahmah ila alisimama hapo na kuomba (Rahmah), wala Aayah ya adhabu ila aliomba kinga nayo (adhabu hiyo).” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaipa daraja la Hasan At-Tirmidhiy]

231.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَلَا وَإِنِّي نُهِيتُ أَنْ أَقْرَأَ الْقُرْآنَ رَاكِعًا أَوْ سَاجِدًا ، فَأَمَّا الرُّكُوعُ فَعِظْمُوهَا فِيهِ الرَّبُّ ، وَأَمَّا السُّجُودُ فَاجْتَهِدُوا فِي الدُّعَاءِ ، فَقَمِنْ أَنْ يُسْتَجَابَ لَكُمْ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Jueni nimekatazwa kusoma Qur-aan[32] nikiwa nimerukuu au nimesujudu, ama katika kurukuu Muadhimisheni humo Rabb, na wakati wa kusujudu jitahidini kuomba du’aa, kwani hakika mtajibiwa.” [Imetolewa na Muslim]

232.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: فِي رُكُوعِهِ وَسُجُودِهِ : "سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ ، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anasema wakati wa kurukuu na kusujudu:

“Subhaanaka-Allaahumma Rabbanaa wa bi-Hamdika, Allaahummagh-firliy”

(Kutakasika ni Kwako, ee Allaah, Rabb wetu, na kuhimidiwa ni Kwako, ee Allaah nighufirie).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

233.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا قَامَ إِلَى الصَّلَاةِ يُكَبِّرُ حِينَ يَقُومُ ، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَرْكَعُ ، ثُمَّ يَقُولُ : " سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ " حِينَ يَرْفَعُ صُلْبَهُ مِنَ الرُّكُوعِ ، ثُمَّ يَقُولُ وَهُوَ قَائِمٌ : " رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ " ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَهْوِي سَاجِدًا ، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَرْفَعُ رَأْسَهُ ، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَسْجُدُ ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَرْفَعُ ، ثُمَّ يَفْعَلُ ذَلِكَ فِي الصَّلَاةِ كُلِّهَا ، وَيُكَبِّرُ حِينَ يَقُومُ مِنْ اثْنَتَيْنِ بَعْدَ الْجُلُوسِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anaposimama kuswali, alikuwa anapiga Takbiyra[33] ilhali amesimama wima, kisha anitamka Takbiyra wakati akirukuu, kisha anasema:

“Sami’a-Allaahu liman Hamidah.”

(Allaah Amemsikia mwenye kumhimidi).

Wakati anainua mgongo wake kutoka katika rukuu akishasimama wima (I’tidaal) anasema:

“Rabbanaa wa-Lakal Hamd.”

(Rabb wetu kuhimidiwa ni kwako).

Kisha anapiga Takbiyra anapoinama kwa ajili ya kusujudu, kisha anapiga takbiyra anapoinua kichwa, kisha anapiga takbiyra anaposujudu mara ya pili, kisha anapiga takbiyra anapoinua kichwa mara nyingine. Na alifanya hivyo hivyo katika Swalaah yote. Na

alipiga takbiyra aliposimama toka katika kikao, baada ya Rakaa mbili.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

234.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ قَالَ : " اللَّهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ مِلءَ السَّمَوَاتِ وَمِلءَ الْأَرْضِ ، وَمِلءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ ، أَهْلَ الثَّنَاءِ وَالْمَجْدِ ، أَحَقُّ مَا قَالَ الْعَبْدُ وَكُلُّنَا لَكَ عَبْدٌ اللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أُعْطِيَْتَ ، وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anapoinua kichwa chake baada ya rukuu alikuwa anasema:

“Allaahumma Rabbanaa Lakal-Hamd, mil-as-samawaati wal-ardhwi, wa mil-a maa Shii-ta min shay-in ba’du, ahlath-thanaai wal-Majdi, ahaqqu maa qaalal-‘abdu, wa kullunaa Laka ‘abdu, Allaahumma laa maani’a limaa A’twayta, wa laa mu’twiya limaa Mana’ta, wa laa yanfa’u dhal-jaddi Minkal-jaddu.”

(Ee Allaah! Rabb wetu, Himdi ni Zako, ujazo wa mbingu na ardhi, na ujazo wa chochote Ulichotaka (kuumba) baadaye. Ee Mwenye Sifa na Utukufu, Mwenye kustahiki kuliko vyote kwa kila alilolisema mja Wako, Ee Allaah hakuna mwenye kuzuia Ulichotoa, au kutoa Ulichozuia, wala mali[34] haziwezi kumnufaisha tajiri Kwako).[35]” [Imetolewa na Muslim]

235.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أُمِرْتُ أَنْ أَسْجُدَ عَلَى سَبْعَةِ أَعْظَمٍ: عَلَى الْجَبْهَةِ وَأَشَارَ بِيَدِهِ إِلَى أَنْفِهِ وَالْيَدَيْنِ، وَالرُّكْبَتَيْنِ، وَأَطْرَافِ الْقَدَمَيْنِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Nimeamrisha kusujudu juu ya mifupa saba: paji la uso, akaashiria kwa mikono yake miwili juu ya pua yake[36], magoti mawili na vidole vya miguu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

236.

وَعَنْ ابْنِ بُحَيْنَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {كَانَ إِذَا صَلَّى فَرَجَ بَيْنَ يَدَيْهِ، حَتَّى يَبْدُوَ بَيَاضُ إِبْطَيْهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn Buhaynah[37] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisujudu anaposwali, hupanua mikono yake hadi weupe wa kwapa zake ukaonekana.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

237.

وَعَنْ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا سَجَدْتَ فَضَعْ كَفَّيْكَ ، وَارْفَعْ مِرْفَقَيْكَ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Al-Baraai bin ‘Aazib[38] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Unaposujudu, weka viganja vya mikono yako juu ya ardhi na unyanyue viwiko vyako.” [Imetolewa na Muslim]

238.

وَعَنْ وَائِلِ بْنِ حُجْرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { كَانَ إِذَا رَكَعَ فَرَجَّ بَيْنَ أَصَابِعِهِ ، وَإِذَا سَجَدَ ضَمَّ أَصَابِعَهُ } رَوَاهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Waail bin Hujr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alipokuwa akirukuu anapanua vidole vyake, anaposujudu alivikusanya.” [Imetolewa na Al-Haakim]

239.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : { رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي مُتَرَبِّعًا } رَوَاهُ النَّسَائِيُّ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilimuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiswali akiwa amekaa huku kakunja miguu.[39]” [Imetolewa na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

240.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَقُولُ بَيْنَ السَّجْدَتَيْنِ : {اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ، وَارْحَمْنِي ، وَاهْدِنِي ، وَعَافِنِي ، وَارْزُقْنِي} رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيُّ ، وَاللَّفْظُ لِأَبِي دَاوُدَ ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anasoma baina ya Sijda mbili:

“Allaahummagh-fir-liy Warhamniy, Wahdiniy, Wa’aafiniy, Warzuqniy.”

(Ee Allaah! Nighufirie, Nirehemu, Nihidi, Nijaalie ‘Aafiyah (siha, amani nk.) na Niruzuku).” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy, na tamshi hili ni la Abuu Daawuud, na aliisahihisha Al-Haakim

241.

وَعَنْ مَالِكِ بْنِ الْحُوَيْرِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ {رَأَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي ، فَإِذَا كَانَ فِي وَثْرِ مِنْ صَلَاتِهِ لَمْ يَنْهَضْ حَتَّى يَسْتَوِيَ قَاعِدًا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Maalik bin Al-Huwayrith (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Alimuona Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiswali, na alipokuwa katika Rakaa za Swalaah ya Witr, hakusimama wima hadi alipokaa chini sawasawa.”[40] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

242.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {قَنَتَ شَهْرًا بَعْدَ الرُّكُوعِ ، يَدْعُو عَلَى أَحْيَاءِ مِنْ أَحْيَاءِ الْعَرَبِ ، ثُمَّ تَرَكَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَلِأَحْمَدَ وَالْدَّارَقُطْنِيِّ نَحْوُهُ مِنْ وَجْهِ آخَرَ ، وَزَادَ : {فَأَمَّا فِي الصُّبْحِ فَلَمْ يَزَلْ يَقْنُتُ حَتَّى يَفَارِقَ الدُّنْيَا}

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisoma Qunuwt mwezi mmoja, baada ya kurukuu, akilaani makabila fulani ya Waarabu[41], kisha akaiacha.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Katika Riwaayah ya Ahmad na Ad-Daaraqutwniyy kuna Hadiyth kama hiyo kwa njia nyingine, na kuna ziada hii: “Ama katika Alfajiri aliendelea kusoma Qunuwt mpaka alipoaga dunia.”

243.

وَعَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { كَانَ لَا يَقْنُتُ إِلَّا إِذَا
دَعَا لِقَوْمٍ ، أَوْ دَعَا عَلَى قَوْمٍ } صَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) hakutekeleza Qunuwt isipokuwa alipokuwa akiomba du’aa dhidi ya watu[42] baada ya kuinuka kutoka katika rukuu isipokuwa alipowaombea watu, au kuwalaani watu.”
[Aliisahihisha Ibn Khuzaymah]

244.

وَعَنْ سَعْدِ بْنِ طَارِقِ الْأَشْجَعِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { قُلْتُ
لِأَبِي : يَا أَبَتِ ! إِنَّكَ قَدْ صَلَّيْتَ خَلْفَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَأَبِي بَكْرٍ ، وَعُمَرُ ، وَعُثْمَانُ ، وَعَلِيٌّ ، أَفَكَانُوا
يَقْنُتُونَ فِي الْفَجْرِ ؟ قَالَ : أَيُّ بَنِيَّ ، مُحَدَّثٌ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ ،
إِلَّا أَبَا دَاوُدَ

Kutoka kwa Sa’d[43] bin Twaariq[44] Al-Ashja’iyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nilimuuliza baba yangu: Ee baba yangu! Wewe umeswali nyuma ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), Abuu Bakr, ‘Umar, ‘Uthmaan na ‘Aliy, Je walikuwa wakifanya Qunuwt katika Swalaah ya Alfajiri? Akasema: Ee mwanangu! Huo ni uzushi.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa Abuu Daawuwd]

وَعَنْ الْحَسَنِ بْنِ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا : قَالَ : {عَلَّمَنِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَلِمَاتٍ أَقُولُهُنَّ فِي قُنُوتِ الْوُتْرِ : "اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيمَنْ هَدَيْتَ ، وَعَافِنِي فِيمَنْ عَافَيْتَ ، وَتَوَلَّنِي فِيمَنْ تَوَلَّيْتَ ، وَبَارِكْ لِي فِيمَا أَعْطَيْتَ ، وَقِنِي شَرَّ مَا قَضَيْتَ ، فَإِنَّكَ تَقْضِي وَلَا يُقْضَى عَلَيْكَ ، إِنَّهُ لَا يَذِلُّ مَنْ وَالَيْتَ ، تَبَارَكْتَ رَبَّنَا وَتَعَالَيْتَ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ . وَزَادَ الطَّبْرَانِيُّ وَالْبَيْهَقِيُّ : {وَلَا يَعْزُّ مَنْ عَادَيْتَ } زَادَ النَّسَائِيُّ مِنْ وَجْهِ آخَرَ فِي آخِرِهِ : {وَصَلَّى اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ } وَلِلْبَيْهَقِيِّ عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا : {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُعَلِّمُنَا دُعَاءَ نَدْعُو بِهِ فِي الْقُنُوتِ مِنْ صَلَاةِ الصُّبْحِ } وَفِي سَنَدِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Al-Hasan bin ‘Aliy[45] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alinifundisha maneno ya kusema katika Qunuwt ya Swalaah ya Witr:

“Allaahumma-hdniy fiyman Hadayta, wa-‘Aafiniy fiyman ‘Aafayta, wa-Tawallaniy fiyman Tawallayta, wa-Baarik liy fiymaa A’twayta, wa-Qiniy sharra maa Qadhwayta, fa-Innaka Taqdhwiyy walaa yuqdhwaa ‘Alayka, innahu laa yadhillu man Waalayta, Tabaarakta Rabbanaa wa-Ta’aalayta.”

(Ee Allaah! Nihidi pamoja na Uliowahidi, na Unipe 'aafiyah pamoja na Uliowapa 'aafiyah, na Nifanye kuwa ni mpenzi Wako pamoja na Uliowafanya wapenzi Wako, na Nibariki katika Ulichonipa na Nikinge na shari ya Ulilolihukumu kwani Wewe Unahukumu wala Huhukumiwi. Hakika hadhaliliki Uliyemfanya mpenzi, Umebarikika Ee Rabb wetu na Umetukuka) [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad)]

Atw-Twabaraaniyy na Al-Bayhaqiyy wakaongeza:

“Wa laa ya 'izzu man 'aadayta.”

(Wala hana 'izzah (hadhi) Unayemfanya adui).

Katika Riwaayah iliyopokewa na An-Nasaaiy aliongezea:

“Wa Swalla Allaahu 'alan-Nabiyy.”

(na Allaah Amaswalie Nabiyy).[46]

Na Bayhaqiyy amepokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anatufundisha du'aa tunaiomba katika Qunuwt ya Swalaah ya asubuhi.” Katika Isnaad yake kuna udhaifu.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا سَجَدَ أَحَدُكُمْ فَلَا يَبْرُكْ كَمَا يَبْرُكُ الْبَعِيرُ، وَلِيَضَعَ يَدَيْهِ قَبْلَ رُكْبَتَيْهِ} أَخْرَجَهُ الثَّلَاثَةُ

وَهُوَ أَقْوَى مِنْ حَدِيثِ وَائِلٍ: {رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا سَجَدَ وَضَعَ رُكْبَتَيْهِ قَبْلَ يَدَيْهِ} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ فَإِنَّ لِلأَوَّلِ شَاهِدًا مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا صَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ ، وَذَكَرَهُ الْبُخَارِيُّ مُعَلَّقًا مَوْقُوفًا

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu anaposujudu, asipige magoti kama afanyavyo ngamia, bali aweke viganja vyake chini kabla ya kuweka magoti yake.” [Imetolewa na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud)]

Nayo ina nguvu (kwa usahihi) zaidi^[47] kuliko Hadiyth ya Waail bin Hujr: “Nilimuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiweka magoti yake chini kabla ya kuweka viganja vyake akisujudu.” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah)]

Hadiyth ya kwanza inashuhudiwa na Hadiyth ya Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) (inayofuata chini), ambayo Ibn Khuzaymah amesema ni Swahiyh, Al-Bukhaariy aliitaja kuwa ni Mu’allaq Mawquwf.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا قَعَدَ لِلتَّشَهُّدِ وَضَعَ يَدَهُ الْيُسْرَى عَلَى رُكْبَتِهِ الْيُسْرَى ، وَالْيُمْنَى عَلَى الْيُمْنَى ، وَعَقَدَ ثَلَاثَةً وَخَمْسِينَ ، وَأَشَارَ بِإِصْبَعِهِ السَّبَّابَةِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ
 وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ : { وَقَبَضَ أَصَابِعَهُ كُلَّهَا ، وَأَشَارَ بِأَلْتِي تَلِي الْإِبْهَامَ }

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa anakaa kwa ajili ya Tashahhud aliweka kiganja chake cha kushoto juu ya goti lake la kushoto, na cha kuume juu ya goti lake la kuume, na akakunja vidole vyake[48] na akaashiria kwa kidole chake cha kulia cha Shahaadah.”
 [Imetolewa na Muslim]

Na katika mapokezi yake mengine tamshi la Muslim ilisema: “Na alikunja vidole vyake vyote vya mkono wa kuume, na akaashiria kwa kidole chake cha Shahaadah.”

248.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { التَّفَتَ إِلَيْنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ : "إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ فَلْيَقُلْ : التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ ، وَالصَّلَوَاتُ ، وَالطَّيِّبَاتُ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ }

وَرَسُولُهُ ، ثُمَّ لِيَتَخَيَّرَ مِنَ الدُّعَاءِ أَعْجَبُهُ إِلَيْهِ ، فَيَدْعُو { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ .

وَالنِّسَائِيُّ : { كُنَّا نَقُولُ قَبْلَ أَنْ يُفَرَضَ عَلَيْنَا التَّشَهُّدُ }
وَلِأَحْمَدَ : { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَّمَهُ التَّشَهُّدَ ،
وَأَمَرَهُ أَنْ يُعَلِّمَهُ النَّاسَ }

وَلِمُسْلِمٍ : عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : { كَانَ
رَسُولُ اللَّهِ ﷺ يُعَلِّمُنَا التَّشَهُّدَ : " اَلتَّحِيَّاتُ الْمُبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ
... } إِلَى آخِرِهِ

Kutoka kwa Abdullaah bin Mas- ‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Alitugeukia Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم)
akasema: “Mmoja wenu anaposwali aseme:

“At-tahiyyaatu liLLaah, wasw-Swalawaatu, watw-Twayyibaatu. As-salaamu ‘alayka ayyuhan-Nabiy wa-RahmatuLLaahi wa Barakaatuh, As-salaamu ‘alaynaa wa ‘alaa ‘ibaadi-LLaahi-sw-Swaalihiyn. Ash-hadu an-laa ilaaha illaa Allaah wa ash-hadu anna Muhammadan ‘Abduhu wa Rasuwluhu.”

(Maamkizi mema ni ya Allaah, na Swalaah na maneno mema yote. Amani iwe juu yako Ee Nabiy[49] na Rahmah za Allaah na Baraka Zake. Amani iwe juu yetu na juu ya waja Swalihina wa Allaah, Ninashuhudia kwamba hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, na ninashuhudia kwamba Muhammad ni mja Wake na Rasuli Wake).

Kisha achague dua yoyote[50] aipendayo aisome.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Katika mapokezi ya An-Nassaiy: “Tulikuwa tukisema kabla ya kufaradhishwa (At-Tashahhud).[51]”

Na katika mapokezi ya Ahmad: “Kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ) alimfundisha At-Tashahhud na akamuamrisha kuwafundisha watu.”

Na katika Muslim kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitufundisha At-Tashahhud:

“At-Tahiyyaatu, Al-Mubaarakatu, Asw-Swalawaatu, Atw-Twayyibaatu liLLaah...”

(Maamkizi mema, maneno yenye baraka na mazuri yote, Swalaah ni kwa ajili ya Allaah).

Mpaka mwisho wake.

249.

وَعَنْ فَضَالَةَ بْنِ عُبَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { سَمِعَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَجُلًا يَدْعُو فِي صَلَاتِهِ ، لَمْ يَحْمَدِ اللَّهَ ، وَلَمْ يُصَلِّ عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ : " عَجَلَ هَذَا " ثُمَّ دَعَاهُ ، فَقَالَ : " إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ فَلْيُبْدَأْ بِتَحْمِيدِ رَبِّهِ وَالتَّنَاءِ عَلَيْهِ ، ثُمَّ يُصَلِّي عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ثُمَّ يَدْعُو بِمَا شَاءَ } رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَالثَّلَاثَةُ ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ ، وَابْنُ حِبَّانَ ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Fadhwaalah bin ‘Ubayd[52] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimsikia mtu akiomba du’aa ndani ya Swalaah na hakumhimidi Allaah wala hakumswalia Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), akasema: “Huyu ameharakisha.” Kisha akamuita yule mtu na akasema: “Mmoja wenu anaposwali, aanze kwa kumhimidi Rabb wake na kumsifu, kisha amswalie Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kisha aombe anachotaka.” [Imetolewa na Ahmad na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na waliisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

250.

وَعَنْ أَبِي مَسْعُودٍ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { قَالَ بَشِيرُ بْنُ سَعْدٍ: يَا رَسُولَ اللَّهِ ! أَمَرَنَا اللَّهُ أَنْ نُصَلِّيَ عَلَيْكَ ، فَكَيْفَ نُصَلِّيَ عَلَيْكَ ؟ فَسَكَتَ ، ثُمَّ قَالَ: " قُولُوا : اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ ، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ ، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ . وَالسَّلَامُ كَمَا عَلَّمْتُمْ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَزَادَ ابْنُ خُزَيْمَةَ فِيهِ : { فَكَيْفَ نُصَلِّيَ عَلَيْكَ ، إِذَا نَحْنُ صَلَّيْنَا عَلَيْكَ فِي صَلَاتِنَا }

Kutoka kwa Abuu Mas-‘uud Al-Answaariyy[53] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Bashiyr bin Sa’d[54] amesema Ee Rasuli wa Allaah!

Allaah Ametuamrisha tukuswalie, sasa tukuswalie namna gani?
(Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akanyamaza,
kisha akasema: Semeni[55]:

*“Allaahumma Swalli ‘alaa Muhammad, wa ‘alaa aali Muhammad,
kamaa Swallayta ‘alaa Ibraahiym, wa Baarik ‘alaa Muhammad wa
‘alaa aali Muhammad, kamaa Baarakta ‘alaa Ibraahiym fil
‘Aalamiyna Innaka Hamiydun Majiyyd.”*

(Ee Allaah! Mswalie Muhammad na ahli wa Muhammad, kama
ulivyomswalia Ibraahiym na Umbariki Muhammad na ahli wa
Muhammad kama Ulivyombariki Ibraahiym Ulimwenguni kote,
hakika Wewe ni Mwenye Kuhimidiwa, Mtukufu)[56]

na kusalimiana ni kama mnavyojua.” [Imetolewa na Muslim]

Na akaongezea Ibn Khuzaymah: “Namna gani tukuswalie wakati
tushakuswalia katika Swalaah zetu.”

251.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا تَشَهَّدَ أَحَدُكُمْ فَلْيَسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنْ أَرْبَعٍ ،
يَقُولُ : اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ جَهَنَّمَ ، وَمِنْ عَذَابِ
الْقَبْرِ ، وَمِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ ، وَمِنْ شَرِّ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ
الْدَّجَالِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ : { إِذَا فَرَغَ أَحَدُكُمْ مِنَ التَّشَهُّدِ الْأَخِيرِ }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu anapomaliza Tashahhud, aombe isti’aadhah (kinga) kwa Allaah dhidi ya mambo manne aseme:

“Allaahumma inniy a’uwdhubika min ‘adhaabi Jahannama, wamin ‘adhaabil qabri, wamin fitnatil-mahyaa wal-mamaati, wamin sharri fitnatil-masiyhid-dajjaal.”

(Ee Allaah, naomba kinga Kwako dhidi ya adhabu ya Jahannam na adhabu ya kaburi[57], na dhidi ya mitihani ya uhai na mauti, na dhidi ya mitihani ya Masiyh Ad-Dajjaal[58]).[59] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Akimaliza mmoja wenu Tahiyyaat ya mwisho.”

252.

وَعَنْ أَبِي بَكْرٍ الصِّدِّيقِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ قَالَ لِرَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { عَلَّمَنِي دُعَاءَ أَدْعُو بِهِ فِي صَلَاتِي . قَالَ قُلْ : "اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْمًا كَثِيرًا ، وَلَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ ، فَاعْفِرْ لِي مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ ، وَارْحَمْنِي ، إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Bakr Asw-Swiddiyq (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amepokea[60] kuwa alimuambia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ

(وَالِهِ وَسَلَّمَ): “Nifundishe du’aa ya kuomba katika Swalaah yangu.
Akasema: Sema:

“Allaahumma inniy dhwalamtu nafsiy dhwulman kathiyran, walaa yaghfirudh-dhunuwba illaa Anta, faghfir-liy maghfiratan min ‘Indika, war-hamniy, Innaka Antal-Ghafuwrur-Rahiyim.”

(Ee Allaah, hakika mimi nimedhulumu nafsi yangu dhulma nyingi, wala hapana wa kughufiria dhambi isipokuwa Wewe, kwa hivyo naomba unighufirie maghfirah Yako na unirehemu, Hakika Wewe ni Mwingi wa kughufuria, Mwenye kurehemu).[61] [Al-Bukhaariy, Muslim]

253.

وَعَنْ وَائِلِ بْنِ حُجْرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { صَلَّيْتُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَكَانَ يُسَلِّمُ عَنْ يَمِينِهِ : " السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ " وَعَنْ شِمَالِهِ : " السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ بِسَنَدٍ صَحِيحٍ

Kutoka kwa Waail bin Hujr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Nimeswali pamoja na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitoa Salaam kulia kwake[62] akisema:

“Assalaam ‘alaykum wa-RahmatuLLaahi wa-Barakaatuh.”

(Amani iwe juu yenu na Rahmah za Allaah na Baraka Zake)

na kushoto akisema:

“Assalaam ‘alaykum wa-RahmatuLLaahi wa-Barakaatuh.”
[Imetolewa na Abuu Daawuud kwa Isnaad Swahiyh]

254.

وَعَنْ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { كَانَ يَقُولُ فِي دُبُرِ كُلِّ صَلَاةٍ مَكْتُوبَةٍ : " لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ ، وَلَهُ الْحَمْدُ ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ، اَللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ ، وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Al-Mughiyrah bin Shu’bah
amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alikuwa akisema mwisho wa kila Swalaah ya faradhi:

“Laa ilaaha illaa Allaah Wahdahu laa shariyka Lah, Lahul-Mulk wa-Lahul-Hamd wa Huwa ‘alaa kulli shay-in Qadiyr, Allaahumma laa maani’a limaa A’twayta, wa laa mu’twiya limaa Mana’ta, wa laa yanfa’u dhal-jaddi Minkal-jaddu.”

(Hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, Peke Yake Hana mshirika, Ufalme ni Wake, Kuhimidiwa ni Kwake, Naye ni Mweza wa kila kitu. Ee Allaah, hakuna wa kuzuia Ulilotoa, wala wa kulitoa Ulilozuia, wala mwenye utajiri hatanufaishwa chochote Kwako na utajiri wake)[63]. [Al-Bukhaariy, Muslim]

255.

وَعَنْ سَعْدِ بْنِ أَبِي وَقَّاصٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { إِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَتَعَوَّذُ بِهِنَّ دُبْرَ الصَّلَاةِ : " اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْبُخْلِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْجُبْنِ ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ أَنْ أُرَدَّ إِلَى أَرْذَلِ الْعُمُرِ ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الدُّنْيَا ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [64] Kutoka kwa Sa'd bin Abii Waqqaasw[64] amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akijikinga (kwa Allaah) baada ya kila Swalaah:

“Allaahumma inniy a’uwdhubika minal-bukhli, wa a’uwdhubika minal-jubni, wa a’uwdhubika min an uradda ilaa ardhilil-‘umuri, wa a’uwdhubika min fitnatid-dunyaa wa adhaabil-qabri.”

(Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kutokana na ubakhili, na najikinga Kwako kutokana na uoga, na najikinga Kwako kurudishwa katika umri wa kudhalilika [uzee][65], na najikinga Kwako fitnah za dunia na adhabu za kaburi). [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

256.

وَعَنْ ثَوْبَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا أَنْصَرَفَ مِنْ صَلَاتِهِ اسْتَغْفَرَ اللَّهُ ثَلَاثًا ، وَقَالَ : " اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ . تَبَارَكْتَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Thawbaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa alipomaliza Swalaah yake, anaomba maghfirah kwa Allaah mara tatu[66], na anasema:

“Allaahumma Antas-Salaam, wa Minkas-Salaam, Tabaarakta yaa Dhal Jalaali wal Ikraam.”

(Ee Allaah, Wewe Ndiye Amani, na Amani hutoka Kwako, Umebarikika ee Mwenye Ujalali na Utukufu).[67] [Imetolewa na Muslim]

257.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : { مَنْ سَبَّحَ اللَّهَ دُبْرَ كُلِّ صَلَاةٍ ثَلَاثًا وَثَلَاثِينَ ، وَحَمِدَ اللَّهَ ثَلَاثًا وَثَلَاثِينَ ، وَكَبَّرَ اللَّهَ ثَلَاثًا وَثَلَاثِينَ ، فَتِلْكَ تِسْعٌ وَتِسْعُونَ ، وَقَالَ تَمَامَ الْمِائَةِ : لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ ، وَلَهُ الْحَمْدُ ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ، غُفِرَتْ لَهُ خَطَايَاهُ ، وَإِنْ كَانَتْ مِثْلَ زَبَدِ الْبَحْرِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَفِي رِوَايَةٍ أُخْرَى: أَنَّ التَّكْبِيرَ أَرْبَعٌ وَثَلَاثُونَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakaye Sabbih (Subhaana Allaah) kila baada ya Swalaah mara thelathini na tatu[68], akaleta tahmiyd (AlhamduliLLaah) mara thelathini na tatu

akaleta takbiyra (*Allaahu Akbar*) mara thelathini na tatu, akamalizia itimie mia kwa:

“Laa ilaaha illa-Allaahu Wahdahu laa shariyka Lah, Lahul-Mulku wa Lahul-Hamdu wa-Huwa ‘alaa kulli shay-in Qadiyr.”

(Hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, Hana mshirika, ufalme wote ni Wake, na Himdi zote ni Zake, Naye ni Mweza wa kila kitu), ataghufuriwa makosa yake japokuwa ni mfano wa povu la bahari.” [Imetolewa na Muslim]

Na katika mapokezi mengine: “Takbiyra ni mara thelathini na nne.”

258.

وَعَنْ مُعَاذِ بْنِ جَبَلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لَهُ : " أَوْصِيكَ يَا مُعَاذُ : لَا تَدْعَنَّ دُبْرَ كُلِّ صَلَاةٍ أَنْ تَقُولَ : اللَّهُمَّ أَعْنِي عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ } رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَأَبُو دَاوُدَ ، وَالنَّسَائِيُّ بِسَنَدٍ قَوِيٍّ

Kutoka kwa Mu’aadh bin Jabal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia: “Nakuusia ee Mu’aadh! Usiache abadani baada ya kila Swalaah kusema:

“Allaahumma a’inniy ‘alaa Dhikrika wa Shukrika, wa husni ‘ibaadatika.”

(Ee Allaah! Nisaidie kukudhukuru, na kukushukuru, na kukuabudu kwa uzuri upasao). [Imetolewa na Amad, Abuu Daawuud na An-Nasaaiy kwa Isnaad yenye nguvu (Qawiyy)]

259.

وَعَنْ أَبِي أُمَامَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ قَرَأَ آيَةَ الْكُرْسِيِّ دُبَّرَ كُلَّ صَلَاةٍ مَكْتُوبَةٍ
لَمْ يَمْنَعَهُ مِنْ دُخُولِ الْجَنَّةِ إِلَّا الْمَوْتُ} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ ،
وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ
وَزَادَ فِيهِ الطَّبْرَانِيُّ : {وَقُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ}

Kutoka kwa Abuu Umaamah[69] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:
“Mwenye kusoma Aayatul kursiyy[70] mwisho wa kila Swalaah ya
faradhi, hakuna kitakachomzuia kuingia Jannah isipokuwa[71]
mauti.”[72] [Imetolewa na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn
Hibbaan]

At-Twabaraaniyy aliongezea: “Na *Qul-Huwa-Allaahu Ahad*.”[73]

260.

وَعَنْ مَالِكِ بْنِ الْحُوَيْرِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ
اللَّهُ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {صَلُّوا كَمَا رَأَيْتُمُونِي أُصَلِّي} رَوَاهُ
الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Maalik bin Al-Huwayrith (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalini kama mlivyoniona nikiswali.”[74] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

261.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { قَالَ لِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ " صَلِّ قَائِمًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَقَاعِدًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَعَلَى جَنْبٍ وَإِلَّا فَأَوْمٌ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) kwamba Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swali huku umesimama, na ukiwa huwezi swali kwa kukaa, na ukiwa huwezi, swali kwa ubavu, laa sivyo swali kwa ishara.”[75] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

262.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { قَالَ لِمَرِيضٍ صَلَّى عَلَى وَسَادَةٍ ، فَرَمَى بِهَا وَقَالَ : " صَلِّ عَلَى الْأَرْضِ إِنْ اسْتَطَعْتَ ، وَإِلَّا فَأَوْمِيْ إِيْمَاءً ، وَاجْعَلْ سُجُودَكَ أَخْفَضَ مِنْ رُكُوعِكَ } رَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ بِسَنَدٍ قَوِيٍّ وَلَكِنْ صَحَّحَ أَبُو حَاتِمٍ وَقَفَّهْ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia mgonjwa aliyekuwa

anaswali juu ya mto (tandiko) Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه) aliutupa, akasema: “Swali juu ya ardhi ukiweza, vinginevyo swali kwa ishara na uzifanye Sijdah zako ziwe chini zaidi kuliko rukuu zako.” [Imetolewa na Al-Bayhaq kwa Isnaad yenye nguvu, lakini Abuu Haatim aliisahihisha iliyo Mawquwf]

[1] Ni wazi kwamba kuisoma Qur-aan ni lazima. Kuna Hadiyth inayosema:

((ثُمَّ اقْرَأْ بِأَمِّ الْقُرْآنِ))

((Kisha soma kwa Mama wa Qur-aan))

Ni wazi kuwa inamaanisha Suwrah Al-Faatihah.

[2] Wale watu ambao hawarukuu vizuri, hawasujudu vizuri, na hawakai vizuri, n.k katika Swalaah zao, waizingatie Hadiyth hii. Vitendo vinavyofanywa ovyo-ovyo, na harakaharaka siyo sahihi. Hivi vitendo vya ovyo-ovyo huharibu Swalaah zao. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisema Swalaah kama hiyo ni “Swalaah ya mnafiki” na wanaotenda hivyo ni “Wezi wa aina mbaya kabisa.”

[3] Huyu Rifaa’ah alipewa jina la utani la Abuu Mu’aadh na alikuwa Az-Zurqi Al-Answaar Al-Madaniy, Swahaba mkubwa ambaye alishiriki katika Al-‘Aqabah pamoja na babake ambaye alikuwa Answaar wa kwanza kusilimu. Rifaa’ah alishiriki katika vita vya Badr na vita vyote vilivyofuata; na pia alikuwa pamoja na ‘Aliy katika vita vya Al-Jamal na Siffiyn. Alikufa mwanzoni mwa Ukhalifa wa Mu’aawiyah mnamo mwaka 41 A.H.

[4] *Ummul-Qur-aan* ni jina lingine la Suwrah Al-Faatihah. Hadiyth hii ya kusoma Al-Faatihah na Suwrah au Aayah zingine za Qur-aan ni muhimu. Kwa mujibu wa ‘Ulamaa wengine, baada ya kuisoma Al-Faatihah ni muhimu kusoma zaidi, na wengine wanasema inapendeza. Ukitaka kujua zaidi soma vitabu vya Hadiyth.

[5] Abuu Humayd anaitwa ‘Amr au Mundhir bin Sa’d bin Al-Mundir au Maalik Al-Answaar Al-Khazraj Al-Madaniy. Ametoka katika kizazi cha Saa’idah ambaye ndiye baba wa Al-Khazraj. Alishiriki katika Uhud na vita vilivyofuatia, na akafariki ima mwishoni mwa Ukhalifa wa Mu’aawiyah au mwanzoni mwa utawala wa Yaziyd mnamo mwaka 61 A.H.

[6] Ummah wote wa kiislamu unatakiwa uswali kama alivyokuwa akiswali mwenyewe Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alikuwa akiswali kwa amani na utulivu wa akili na ukamilifu. Kuswali kwa papara, harakaharaka kunakatazwa.

[7] Katika Hadiyth hii, “Raf’u yadayni” (kunyanyua mikono) imetajwa kuwa ifike hadi mabegani. Usimulizi wa Waail bin Hujr, umetaja hadi masikioni.

[8] Katika mwisho wa Hadiyth hii, inatajwa kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisoma du’aa hii wakati wa kuswali Tahajjud iswaliwayo katikati ya usiku. Mtunzi, katika kitabu chake cha Talkhiys, ameripoti kutoka kwa Imaam Shaafi’iy na Ibn Khuzaymah kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliisoma du’aa hiyo katika Swalaah zote za faradhi. Katika usimulizi wa ‘Aliy (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) anasema uwezekano wa kusoma du’aa hii katika Swalaah zote mbili upo.

[9] Katika maneno haya matukufu, Muislamu anaagizwa aombe maghfirah kutoka kwa Allaah (سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى) juu ya dhambi zake, anazozijua na asizozijua, hata awe mtiifu sana kuliko wote.

[10] Suwrah Al-Faatihah:

[11] “Uqbat ash-shaywaan” (mkao wa shaytwaan) ni kuweka matakao ardhini na kunyanyua magoti na mguu uliyoko chini ya goti na viganja vikiwa ardhini pande zote mbili. “Iftiraash As-Sab’i” (kutandaza mikono kama mnyama mwitu) ni kukalia sehemu za nyuma za mguu wa chini na sehemu ya nyuma ya paja na kisha kuinamia mbele huku ukinyoosha viganja mbele yako juu ya ardhi.

[12] Simulizi hii ya ‘Abdullaah bin ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) ni dhahiri kabisa kuthibitisha kwa kila mwanzo wa Swalaah, wakati wa kurukuu, kuinuka baada ya kurukuu, kunyanyua mikono mpaka kwenye masikio ni Sunnah. Hayo maneno:

كَانَ يَرْفَعُ

“alikuwa akinyanyua...”

Yanaonyesha udumishaji. Inathibitisha unyanyuaji wa mikono haukuwahi kufutwa wala kuachwa. Ahaadiyth zote zinazopinga “kunyanyua mikono” ni dhaifu au mawdhu’ (zimetungwa). Miongoni mwa Hadiyth dhaifu, udhaifu wa zingine umeafikiwa na wengi, na zingine zina kukhitilafiana. Katika zote hizo, usimulizi wa ‘Abdullaah bin Mas-‘uwd huhesabika kuwa bora zaidi. Imaam Al-Bukhaariy alinukuu maoni ya kishariy’ah ya mwalimu wake ‘Ali bin Al-Madiniy kwa msingi wa simulizi za ‘Abdullaah bin ‘Umar ni lazima kwa kila Muislamu kunyanyua mikono. Ikhtilaaf kuhusu kadhia hii ni pana mno kujadaliwa hapa.

[13] Waail bin Hujr au Abuu Hunayda au Abuu Hinda, alikuwa Swahaba mkubwa, na babake alikuwa mmoja wa wafalme wa Hadhramaut. Alimzuru Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ambaye alitandika shali (nguo ya juu) yake ili akalie, na akamuomba Baraka yeye na wanawe, na kisha akamteua awe mkuu wa Aqyal ya Hadhramaut. Alilowea mji wa Kufa, na akafariki wakati wa Ukhalifa wa Mu’aawiyah.

[14] Hadiyth hii inaweka wazi mambo mawili: Kwanza kuikunja mikono ndani ya Swalaah ni Sunnah, na kutokuikunja ni kuipinga Sunnah. Watu wengine wameipokea Hadiyth hii kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) lakini siyo sahihi. Pili, mkono ikunjwe juu ya kifua, siyo chini ya kitovu, kama

wanavyofanya watu wengine. Usimulizi wanaotegemeza ubishani wao pia siyo sahihi.

[15] ‘Ubaadah bin Asw-Swaamit alikuwa mmoja wa viongozi wa ki-Answaar katika ‘Aqabah (Maktaba) wa kwanza na wa pili wa Aqaba. Pia alihudhuria katika vita vya Badr na vita vilivyofuata. ‘Umar alimpeleka Shaam awe Kadhi na mwalimu. Kwa hivyo alilowea Hims na baadaye alikwenda Palestina na akafia Ramlah au Bayt Al-Maqdis mnamo mwaka 34 A.H. akiwa na miaka 72.

[16] Hadiyth iliyotajwa hapo juu ni ushahidi tosha kuwa bila kusoma Suwrah Al-Faatihah Swalaah haiswihi. Maswahaba wa Nabiyy (ﷺ), na wafuasi wa Maswahaba na wengi wa ‘Ulamaa waliamini desturi hii. Katika Hadiyth ijulikanayo kama (مسء الصلاة) - maneno yenyewe ni:

إِقْرَأْ بِأَمِّ الْكِتَابِ

(Soma kwa Ummul-Kitaab)

Nabiyy (ﷺ) aliamrisha kuswali kwa kusoma Al-Faatihah katika kila Rakaa. Imaam na Maqtadi (Maamuma) wote sharti waisome Al-Faatihah. Hakuna mtu yoyote aliyeepushiwa kusoma, na yatakiwa isomwe katika kila Swalaah, kimyakimya (Sirran) au kwa sauti (Jahran), ni lazima kuisoma Al-Faatihah. Muslim amesimulia Hadiyth aliyoipokea Abuu Hurayrah (رضي الله عنه), aliulizwa juu ya kuisoma Al-Faatihah, endapo Swalaah inaswaliwa nyuma ya Imaam. [Abuu Hurayrah alijibu kuwa: ni lazima isomwe kwa siri kwa sauti ya chini.](#) At-Tirmidhiy, Abuu Daawud na An-Nasaaiy wameripoti [Hadiyth kutoka kwa ‘Ubaadah \(رضي الله عنه\) Rasuli wa Allaah \(ﷺ\) aliwahi kuwauliza: “Je mnasoma chochote mkiwa nyuma ya Imaam?”](#) Maswahaba wakajibu: ‘Ndiyo,’ Ndipo Rasuli wa Allaah (ﷺ) akawaambia: [Someni Al-Faatihah na siyo nyingine yoyote, kwa kuwa bila kuisoma Suwrah hiyo Swalaah haiswihi.](#) Kuna Hadiyth nyingine nyingi tu ambazo zinathibitisha kuwa kuisoma Al-Faatihah ni lazima hata ukiwa nyuma ya Imaam pia. Ama kuhusu Hadiyth inayosema kuwa kusoma kwa Imaam kunatosheleza kwa Maamuma pia, ni dhaifu. Miongoni mwa wale wanaoamini maoni haya (kuisoma Al-Faatihah), kwengine wanaona kuwa

Al-Faatihah isomwe katikati ya mapumziko ya visomo vya Imaam, na wengine wanasema kuwa isomwe baada ya kumaliza Imaam kusoma Al-Faatihah.

[17] Inamaanisha kuwa walikuwa hawaisomi kwa sauti, bali waliisoma kimyakimya kama ilivyosema Hadiyith iliyofuatia.

[18] Mtu anaweza kufanya yoyote kati ya hizo njia, ni sahihi.

[19] Nu'aym huyu ndiye Abuu 'Abdillaah Nu'aym 'Abdillaah Al-Mujmir, ambaye ni mtumwa aliyeachwa huru na 'Umar bin Al-Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ). Alikuwa akifukiza manukato katika Msikiti wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kila siku ya Ijumaa saa sita mchana, kwa hivyo alipewa jina la utani la Al-Mujmir. Alikuwa Taabi'i na Abuu Haatim, Ibn Ma'ayn, Ibn Sa'd na An-Nasaaiy walimthibitisha kuwa ni wa kutegemewa.

[20] Baada ya kuisoma Suwrah Al-Faatihah ni Sunnah kusema "Aamiyn". Ikiwa ni Imaam au Maamuma, kila mtu ni wajibu kusema "Aamiyn" ambayo maana yake ni: "Ee Allaah Ikubali du'aa hii au kisomo hiki."

[21] "Aamiyn" inajuzu kwa sauti au kimyakimya. Kuna kutofautiana maoni juu ya kadhia hii. Hanafiyah wanaisoma kimyakimya. Shaafi'i na Ahlul-Hadiyith huisoma kwa sauti kubwa. Sauti kubwa (Jahr) maana yake, ni sauti ya mtu wa pili kuweza kuisikia. Kusoma "Aamiyn" kwa sauti kubwa kumethibitishwa na Ahaadiyith nyingi zingine. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisoma kwa sauti na alikuwa akiirefusha. At-Tirmidhiy aliipa Hadiyith hii kuwa ni Hasan, na Ad-Daaraqutwniy aliipa daraja la Swahiyh. Maulana Abdul-Hayy Lucknowi alisema kuwa, kwa mujibu wa kutopendela upande wowote, kuisoma Aamiyn kwa sauti kubwa ni sahihi zaidi. Ama kuhusu kuisoma Aamiyn kimya kimya, Imaam At-Tirmidhiy amesimulia Hadiyith ambayo kwayo Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliisoma Aamiyn na akatumia sauti ya chini. Kwa hivyo baadhi ya Wahanafi wanahoji matumizi ya Hadiyith hii, ingawa At-Tirmidhiy mwenyewe ameikanusha Hadiyith hii kwa nukta nne za maoni. Hata hivyo,

kila mtu ana uhuru na anawajibika kwa desturi na matendo yake mwenyewe.

[22] ‘Abdullaah bin Abiy Awfaa ndiye aliyepewa jina la utani la Abuu Mu’aawiyah, na jina la babake ilikuwa ‘Alqamah bin Al-Haarith Al-Aslamiy. Yeye na babake wote walikuwa Maswahaba wa Nabiyy (ﷺ). Alihudhuria Al-Hudaybiyyah, Khaybar, na vita vilivyofuata. Aliishi katika mji wa Kufa nchini ‘Iraq na alifariki huko katika mwaka 87H. Alipofuka macho na alikuwa Swahaba wa mwisho kufariki katika mji wa Kufa huko ‘Iraq.

[23] Watu wengine hutumia Hadiyth hii kudai kuwa kusioma Suwrah Al-Faatihah ndani ya Swalaah siyo lazima kwa sababu Nabiyy (ﷺ) hakusema kuwa alilazimika kujifunza Al-Faatihah. Hii na ikumbukwe kwamba kuna kuwahurumia walemavu katika Shariy’ah. Makatazo na amri huwa hazibadili Shariy’ah za kuhurumia kama hizo. Iwapo mtu anasema kuwa hawezi kutawadha kwa sababu asizoweza kuzizuia, basi huambiwa ajitwahirishe kwa kutayammam (kwa mchanga); na hii haimaanishi kuwa kuchukua wudhuu siyo lazima.

[24] Hii imeafikiwa na wengi kuwa kuisoma Al-Faatihah kwa Swalaah za Adhuhuri na Alasiri huwa kwa sauti ya chini au kimyakimya.

[25] Inaelekea kutoka katika Hadiyth hii kuwa, hakuisoma Suwrah yoyote baada ya Al-Faatihah katika Rakaa mbili za mwisho. Lakini Hadiyth ya Abuu Sa’iyd katika Swahiyh Muslim inaripoti kwamba, walikisia urefu wa Rakaa ya mwisho ni kama Aayah 15 wakati wa Aayah za Al-Faathah ni Aayah 7 tu. Kwa hivyo, yaelekea kuwa Nabiyy (ﷺ) alizisoma Aayah zingine na wakati mwingine hakuzisoma. Yaani, kusoma katika Rakaa za mwisho ni Sunnah.

[26] Suwrah As-Sajdah (32: 1-30) ambayo ina Aayah thelathini (30).

[27] Sulaymaan bin Yasaar alikuwa ni mmoja wa ‘Ulamaa saba wa Fiqh na miongoni mwa Taabi’iyn maarufu. Alikuwa ni wa kutegemewa, mwenye

taqwa, msomi, na alihifadhi Hadiyth nyingi. Alipewa jina la utani la Abuu Ayyuwb, na alikuwa mtumwa alieachwa huru na Maymuwnah, (Mama wa Waumini). Alifariki mnamo mwaka wa 107A.H. akiwa na umri wa miaka 73.

[28] Kutoka Suwrah ya Al-Hujuraat mpaka mwisho, Suwrah zote zinaitwa “Mufasw-swal” (zilizopambanuliwa), kwa sababu ya nafasi ndefu kati ya BismiLLaahi mbili. Na kutoka Suwrah ya Al-Hujuraat hadi Al-Buruwj zinaitwa “Twiwaal Mufasw-swal” (ndefu zilizopambanuliwa) na kutoka Al-Buruwj mpaka Al-Bayyinah mpaka mwisho zinaitwa “Awsaatw Mufasw-swal” (zenye urefu wa wastani). Na kutoka Al-Bayyinah mpaka mwisho zinaitwa “Qiswaar Mufasw-swal” (Fupi zilizopambanuliwa). Kuisoma Twiwaal katika Swalaah za Alfajiri, Awsaatw katika Swalaah za ‘Ishaa, na Qiswaar katika Swalaah ya Magharibi ni Sunnah. Mara nyingine hutokea kinyume chake kama inavyoelezewa katika Hadiyth ifuatayo.

[29] Hadiyth zingine zinaripoti kwamba, Suwrah Al-A’raaf, Asw-Swaffaat, na Ad-Dukhaan pia zilizomwa kwenye Swalaah ya Magharibi. Inamaanisha kuwa Suwrah ndefu pia zimewahi kusomwa katika Swalaah ya Magharibi; na Mu’awwidhatayn (Suwrah Al-Falaq na An-Naas) zilizosomwa katika Swalaah ya Alfajiri. Lakini kawaida ilikuwa ni kusoma kama ilivyoelezwa hapo juu.

[30] Katika Suwrah hizi yametajwa mambo ya kuumbwa kwa Aadam, maajabu ya uumbaji, na Siku ya Mkusanyiko, na Siku ya kufufuliwa itatokea siku ya Ijumaa. Kwa sababu hii, Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akizisoma Suwrah hizi mnamo siku ya Ijumaa, ili watu waweze kufikiri kuwa kitu chaweza kutokea leo na wamuogope Allaah (سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى).

[31] Inamaanisha kuwa, Suwrah hizi zisomwe kila siku ya Ijumaa katika Swalaah ya Alfajiri, Suwrah zozote maalumu ambazo Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akizisoma katika Swalaah yoyote maalumu kwa mpangilio maalumu na kila mara, ni vizuri kuzisoma hizo kwa namna ile ile kwa kila Swalaah kwa kuwa hiyo ndiyo Sunnah. Kuzisoma Suwrah nyingine pia inaruhusiwa.

[32] Katika Rukuu na Sijdah, kusoma Qur-aan ni haraam na inachukiza. Kuna sehemu nyingi za Qur-aan, na kila sehemu ina namna yake, na kwa kila sehemu imeelezwa du'aa na maombi maalumu. Katika Rukuu yatakiwa kusomwa:

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ

na katika Sijdah isomwe:

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى

Katika Sijdah inaruhusiwa kuomba du'aa.

[33] Takbiyra ya kwanza inaitwa *Takbiyraatul-Ihraam* (ya kukataza kufanya lolote liwalo isipokuwa Swalaah tu), au huitwa *Takbiyratul-Iftitaah* (ya kufungulia), au *Takbiyratul-Uwlaa* (ya mwanzo), na Takbiyra zingine zote zinaitwa *Takbiyratul-Intiqaal*, maana yake ni ya kuhamia ndani ya Swalaah kwa mfano kutoka katika kisimamo hadi kwenda Rukuu, na kutoka Rukuu kwenda Sijdah, n.k. Ile Takbiyra ya mwanzo (Takbiyratul-Ihraam) imeshurutishwa kuwajibika, na Takbiyra zinazobakia ni za Sunnah, na kwa mujibu wa wengine ni waajib (lazima).

[34] Neno hilo جَد linatumika katika lugha ya Kiarabu kwa maana mbili; Kwanza babu na mababu, na pili utukufu na hadhi. Maana zote mbili ni sahihi katika muktadha huu kwa sababu mali au utajiri, utukufu wa kuzaliwa na taadhima, vyote havina thamani mbele ya Allaah (سُبْحَانَهُ). 'Amali njema pekee ndiyo dira ya kuepukia adhabu. Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) alimuambia binti yake Faatwimah (رَضِيَ اللهُ عَنْهَا) kutenda 'amali njema ili kujiokoa yeye mwenyewe kutokana na adhabu ya Allaah (سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى), na wala asimtegemee babake (Yeye Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wala unasaba wake. Kuokoka kunategemea 'amali njema tu, sasa iwapo Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kamuambia hivyo binti wa kumzaa yeye mwenyewe namna hii, basi nani mwingine tena anaweza kujivunia hadhi ya kuzaliwa?

[35] Du'aa hii ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ni ushahidi tosha wa kukanusha dhana ya wale wanaosimama wima moja kwa moja baada ya kurukuu, na kuchukulia kwamba ucheleweshaji wa kutamka Tasbiyh tatu (yaani kusema سبحان الله) utafanya Sijdah ya kulipia ni lazima. Inapokuwa imethibitishwa na Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) basi tena hakuna nafasi ya maoni ya mtu mwingine binafsi.

[36] Hadiyth hii inaweka wazi kuwa paji la uso na pua, vyote vinahesabika kuwa ni kiungo kimoja. Ukihesabu paji la uso mbali na pua, utapata viungo vinane.

[37] Huyu Ibn Buhaynah ni Abuu Muhammad ‘Abdillaah bin Maalik bin Al-Qishb Al-Azdi, na hilo Buhaynah ni jina la mamake. Alisilimu zamani na akawa mtawa, mwenye taqwa, na alikuwa akifunga (Swawm) siku zote. Alifariki chini ya bonde la Rim, maili tatu kutoka Al-Madiynah, mnamo mwaka wa 54 au 58 A.H.

[38] Huyu Al-Baraa ndiye Abuu ‘Ammaara Al-Baraa bin ‘Aazib bin Al-Haarith bin ‘Adiy Al-Answariy Al-Aws, ambaye alikuwa Swahaba na pia mwana wa Swahaba. Aliachwa kwenye vita vya Badr kwa sababu ya umri wake ulikuwa mdogo, na kushiriki kwake mara ya kwanza kulikuwa katika vita vya Uhud au Al-Khandaaq. Aliteka Ar-Ray na alishiriki katika vita vya Al-Jamaal, Siffiyn, na Naharwaan pamoja na ‘Aliy. Alifia Kufa mnamo mwaka wa 72 A.H.

[39] Hii ilikuwa kwa ajili ya kutojiweza kwa sababu alianguka kutoka juu ya farasi wake, na akateguka kiunganishi cha mguu wake.

[40] Inamaanisha katika Rakaa ya kwanza na ya tatu. Na hii inaitwa *Jalsatul-Istiraahah* (mkao wa kupumzika). Kwa mujibu wa usimulizi, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akikaa katika mkao huu kwa muda mrefu kiasi kwamba watu walifikiri ni kwa ajili ya kusahau kwake. Haikuwa kwa sababu ya umri wake, kwani yeye Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kamwe hakurahisisha wajibu wake wowote kwa ajili ya udhaifu utokanao na uzee.

[41] Makabila haya yalikuwa ya رعل (Ri'il), ذكوان (Dhakwaan) na عصية ('Uswayyah). Haya yalifanya bay'ah (mkataba) na Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) lakini yakavunja ahadi yao na yakawaua Wahubiri sabiini wa Kiislamu baada ya kuwategea kwa kuwaalika. Tukio hili linajulikana kama Bi'r Ma'uwnah.

[42] Inaelekea kuwa kuna ikhtilaaf miongoni mwa Hadiyth hizi. Ya kwanza inasema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) daima alikuwa akisoma Qunuwt katika Swalaah ya Alfajiri kisha akaacha. Hadiyth nyengine inasema kuwa aliisoma Qunuwt kila alipokuwa akiomba ustawi wa kijamii wa taifa au kuwalaani watu fulani kwa ufisadi wao. Hadiyth ya tatu inasema kuwa, kusoma Qunuwt katika Swalaah ya Alfajiri ni uzushi. Lakini iliyo sahihi ni kwamba haikuwa ni waajib zama hizo kuisoma Qunuwt kama wafanyavyo baadhi ya watu sasa kuidumisha Qunuwt katika Swalaah ya Alfajiri, bali lililo sahihi ni kuwa Qunuwt inasomwa pale inapotokea shida fulani kwa Waislamu, kisha inapomalizika huachwa kutekelezwa Qunuwt kama ilivyotajwa katika Hadiyth namba (242) ya Al-Bukhaariy na Muslim.

[43] Sa'd huyu ndiye Abuu Maalik Sa'd bin Twaariq bin Ashyaam bin Mas-'uwd Al-Ashja'iy Al-Kuwfi. Alikuwa miongoni mwa Taabi'iyn waliotegemewa. Alifariki mnamo mwaka 140 A.H.

[44] Twaariq ni Swahaba aliyesimulia Hadiyth chache. Hadiyth kumi nne tu ndizo zilizosimuliwa kutoka kwake, na zote zilisimuliwa na mwanac huyo aliyetajwa hapo juu, Sa'd. Alistakir kule Kufa.

[45] Al-Hasan ni mjukuu kipenzi wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na ni mmoja wa vijana wa Jannah. Alizaliwa mnamo mwezi wa Ramadhwaan mwaka wa 3 A.H; na aliapishwa kuwa Khalifa baada ya kuuliwa baba yeke 'Aliy (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ), lakini alimkabidhi Mu'aawiyah Ukhalifa mnamo mwezi wa Jumaadal-Uwlaa mwaka 41 baada ya miezi saba tu kwa kuchukia kumwaga damu ya Waislamu. Alikufa mnamo mwaka 49 A.H., na akazikwa Al-Baqiy'.

[46] Ifahamike kuwa baadhi ya watu husoma Qunuwt mikono yao ikiwa wazi kabla ya kurukuu. Lakini sahihi yake ni kusoma kwanza Qunuwt huku mikono imeinuliwa juu baada ya kusimama wima kutoka katika Rukuu. Watu wengine husoma Qunuwt kila wanaposwali Witr, wakati wengine husoma Qunuwt katika wiki mbili za mwisho za mwezi wa Ramadhwaan tu. Watu wengine huhesabu Qunuwt kama ni Waajib (lazima), na wengine huihesabu kuwa ni Sunnah. Ukweli ni kwamba hiyo ni Sunnah.

[47] Kitabu cha Fathul-‘Uluwm kinasema kuwa, Hadiyth zote mbili ni imara, na zinatumiwa sawasawa. Hata hivyo tendo la Muhaddithiyn (‘Ulmaa Wasimulizi wa Hadiyth) na Hanaabilah (wafuasi wa Hanbali) imeegemezwa kwenye Hadiyth ya Abuu Hurayrah. Msimamo wa Shafi’iyya, Hanafiyya na Malikiyya ummegemezea katika rejea ya Waail.

[48] Sharti ikunjwe kwa njia ambayo mtu aweke kidole gumba chake chini (kifunikwe na) kidole chake cha Shahaadah huku akiwa kavifumba vidole vitatu vilivyobaki. Kisha ainue kidole chake cha Shahaadah wakati akisoma sehemu ya Tahiyaaat inayosema:

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

“Ash-hadu an laa ilaaha illa Allaah”

Na wakati anapokishusha asome hivyo hivyo.

[49] Mwanzoni, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitufundisha tumswalie yeye, kwa sababu haki yake kwa Ummah wake ni zaidi kuliko mtu yoyote awaye, zaidi kuliko Muumini mwenyewe.

[50] Hadiyth hii inaelezea kuwa, du’aa yoyote ndani ya Swalaah ni kufuata mwendo wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), hii pia inaweka wazi kuwa hakuna jambo lolote makhsusi ambalo mja anaweza kuomba ndani ya Swalaah. Mtu anaweza kuomba chochote akitakacho, iwe cha hapahapa duniani au cha Aakhirah.

[51] Yale maneno ambayo watu walikuwa wakiyasoma kabla ya kufaradhishwa At-Tashahhud hayajatajwa na msimulizi. Lakini kwa mujibu wa Hadiyth zingine, walikuwa wakisema hivi:

السَّلَامُ عَلَى جِبْرِيلَ، السَّلَامُ عَلَى مِيكَائِيلَ ...

Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwazuia kusema hivyo, ndipo akawafundisha At-Tashahhud.

[52] Fadhwaalah bin ‘Ubayd bin Naafidh bin Qays alipewa jina la utani la Abuu Muhammad Al-Answaar Al-Aws. Mwanzo alipigana vita vya Uhud na vita vingine vilivyofuata. Alichukua Bay’atur-Ridhwaan. Alilowea Damascus, Shaam na akawa Kadhi wake akiwa aliteuliwa na Mu’aawiyah wakati alipokuwa akienda kwenye vita vya As-Siffiyn. Alifariki mnamo mwaka wa 56 A.H.

[53] Abuu Mas-‘uwd ndiye ‘Uqbah bin ‘Amr bin Tha’alabah Al-Answaar Al-Badri, alikuwa ni mmoja wa Maswahaba maarufu. Alishiriki ‘Aqabah ya pili wakati angali kijana. Alilowea Kufa na akafia huko au Al-Madiynah baada ya miaka ya arubaini ya Hijrah.

[54] Bashiyr Ibn Sa’d huyu ndiye Abuu An-Nu’mān Bashiyr bin Sa’d bin Tha’alabah bin Al-Jullaas au Al-Khallaas Al-Answaar Al-Khazraj. Alipigana vita vya Badr, na alihudhuria Bay’atul-‘Aqabah. Pia alishiriki katika vita vya Uhud, Al-Khandaq, na vita vingine vilivyofuata. Aliuwawa kule ‘Ayn At-Tamr mnamo mwaka wa 13 A.H.

[55] Maneno ya kumswalia Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) yametajwa namna tofauti katika Hadiyth mbalimbali. Kwenye Hadiyth moja huweko neno au maneno zaidi kuliko kwenye Hadiyth nyingine.

[56] Hii inaweka wazi kuwa hiyo kumswalia Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) yatakiwa isomwe baada ya kusoma At-Tashahhud ndani ya Swalaah, na kuomba du’aa sharti iwe katika Tashahhud ya mwisho tu. Tuna arifiwa zaidi kwamba, kumswalia Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Swalaah ndani ya Swalaah ni Waajib (lazima).

[57] Hadiyth hii inatuarifu kwamba, mtu akishafariki hukumbana na adhabu kaburini, halikadhalika inatuarifu kuwa Muumin wa kweli huwa hana khofu yoyote kaburini. Hii inatibitishwa na Hadiyth nyingi tu.

[58] Al-Masiyh Ad-Dajjaal atakuwa ni kafiri atakayezuka kabla ya Siku ya Qiyaamah ili kuijaribu Iymaan za Waumini. Waumini wakweli watabakia wameishikilia Iymaan yao kwa dhati kabisa juu ya madhila makubwa, ambapo watu wenye Iymaan dhaifu na yenye kuyumba, na makafiri na wanafiki, watafuata amri zake huyo Masiyh Ad-Dajjaal. Huyo ataitwa Masiyh na Nabiyy ‘Iysaa (عليه السلام) pia anaitwa Masiyh. Ingawa matamshi ya haya majina mawili ni sawa, lakini maana zake hapo ni tofauti. Nabiyy ‘Iysaa (عليه السلام) anaitwa Masiyh kwa sababu aliwaponya wagonjwa kwa kuwagusa. Maana ya Masiyh ni kugusa. Lakini Ad-Dajjaal ataitwa Masiyh kwa sababu jicho lake moja limeguswa au limeharibiwa na kwa hivyo limegeuka umbo.

[59] Katika Ahaadiyth zingine maneno yafuatayo yameongezwa:

مِنَ الْمَغْرَمِ وَالْمَأْتَمِ

“Minal maghrami wal ma-athami” (dhidi ya madeni na mwenye dhambi). Imeripotiwa katika Al-Bukhaariy kwamba Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa kwamba kwa nini alikuwa anaomba hifadhi dhidi ya kuwa na madeni kwa namna hiyo? Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema kwamba: “Mtu mwenye deni siyo tu huwa anaongopa, bali pia huwa anavunja ahadi zake. Maafa ya maisha yapo kwenye mwisho wa maisha (huku mtu ukiwa huna Iymaan), na maafa ya kifo yapo katika ukali wa maswali aulizwayo mtu kaburini.”

[60] Huyu ndiye ‘Abdullaah bin ‘Uthmaan Abuu Quhaafah bin ‘Aamir bin At-Taymiy, ambaye ndiye Khalifa wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na mwenzi wake aliyekuwa naye pamoja pangoni, na ndiye mzuri kuliko watu wote wa Ummah huu baki ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mweyewe. Alikuwa mweupe na nywele za singa, mzuri na mwembamba.

Anajulikana sana, na hahitaji kujulishwa. Alikufa mnamo Jumaada Al-Aakhir mwaka wa 13 A.H.

[61] Hadiyith hii inafahamisha kuwa, mwana Aadam anapaswa awe muombaji wa maghfirah hata kama amepata daraja la juu kabisa la taqwa, ukweli na ikhlasi.

[62] Kuna simulizi kutoka kwa Maswahaba kumi na tano wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuhusu Tasliym (kumalizia kwa Salaam). Baadhi ya hizo ni Swahiyh, zingine ni Hasan, na zingine ni dhaifu. Hakuna hata moja ya hizo zilikuwa na maneno ya

وَبَرَكَاتِهِ

“wa Barakaatuh.”

Kuna usimulizi mmoja tu kati ya hizi unaohesabika kuwa ni wa kuaminika na unakubalika.

[63] Maneno ya

ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ

Ina maana: “Endapo Kuridhia Kwako Allaah, hakupo, basi ukuu wote, ufakhari, na mali za kidunia zote, huwa hazina maana, yaani vitu vyovyote vya kidunia utakavyokuwa navyo (mali, vizazi, hadhi na uwezo), haisaidii katika uokovu. Uokovu utapatikana kutokana na Rahmah na Baraka Zako Wewe tu.”

[64] Sa’d bin Abiy Waqqaasw ndiye aliyepewa jina la utani la Abuu Is-haaq bin Maalik, na alikuwa ni Zuhri na Quraysh. Alikuwa ni Muislamu wa tano au wa saba, na ni mmoja wa wale watu kumi ambao waliahidiwa kuingia Jannah. Yeye ni mtu wa kwanza kupiga silaha katika njia ya Allaah, na alishiriki katika vita vyote muhimu. Alikomboa ‘Iraaq kwa ajili ya Uislamu, na du’aa zake zilitakabaliwa. Alikuwa mfupi, mnene, na mwenye nywele nyingi. Alifia Al-‘Aqiyq ambayo iko maili kumi kutoka Al-Madiynah, na alibebwa juu ya mabega ya watu hadi Al-Madiynah, na akazikwa Al-Baqi’y mnamo mwaka 55 H.

[65] Maana ya

Ni pale uzee unamfikia mtu anapokuwa uwezo wa ndani ya mwili wake au nje yake, na akili, unadhoofika ima wote au baadhi yake.

[66] Kuonyesha kutubu na kuomba maghfirah kwa Allaah (سبحانه وتعالى) baada ya kumaliza Swalaah, ni dalili ya kuwa Swalaah ya mtu anayoswali haina hadhi ya kuiwakilisha mbele ya Allaah (سبحانه وتعالى), khasa kwa vile mja huwa amekwisha kutenda makosa, ukhalifu na dosari katika Swalaah yake.

[67] Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alionyesha kutubu na aliomba maghfirah kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kama njia ya kutoa shukrani kwa Allaah (سبحانه وتعالى), pamoja na kuwafundisha watu maadili mema. Basi na Muumini wa kawaida naye hufanya vivyo hivyo kutubia kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kutokana na utovu wa khushuw' (unyenyekavu) kwa kumjia fikra na mawazo yanayomtoa nje ya Swalaah na kumweka mbali wakati anaswali.

[68] Adkhaar hizi zinawakilisha mambo yote mazuri ya dunia hii na Aakhirah. Inaelekea kuwa mtu sharti atamke Adhkaar baada ya kila Swalaah ya fardhi na Swalaah ya Sunnah. Lakini baadhi ya Wanachuoni wamependekeza kusoma Adkhaar hizi katika Swalaah za fardhi tu. Kwa hivyo umuhimu wa du'aa baada ya Swalaah za fardhi umethibitishiwa, lakini Ahaadiyth hazithibitishi kuwepo kwa kusoma Adhkaar hizi au du'aa zozote zile kwa pamoja (kwa jamaa) wala kwa kuinua mikono juu. Bali kila mtu anatakiwa asome Adhkaar hizi na du'aa zake binafi peke yake na bila ya kuinua mikono.

[69] Abuu Umaamah ndiye Iyaas bin Tha'labah Al-Balawiyy na Swahibu wa Banu Haarithah wa wa Answaar. Yeye ni Swahaba, na alisimulia Hadiyth nyingi. Hakushiriki katika vita vya Badr kwa kuwa alikuwa akimuuguza Mama yake.

[70] Aayat-ul-Kursiyy ni ya katika Suwrah Al-Baqarah (2: 255).

[71] Hii inamanisha kuwa ataingia Jannah mara atakapofariki. Yaani, kinachomzuia kuingia Jannah ni kuweko kwake duniani.

[72] Umuhimu wa Aayatul-Kursiyy ni kutokana na Aayah hii kuweko Majina ‘Adhimu kabisa na Sifa za Allaah (سبحانه وتعالى) na pia yanaelezea Tawhiyd ya Allaah (سبحانه وتعالى) ambayo Yeye Anapenda zaidi Apwekeshwe. Suwrah Ikhlaasw pia ina Majina na Sifa kama hizo.

[73] Suwrah Ikhlaasw ni Suwrah namba (112).

[74] Hadiyth hii Swahiyyh na ‘adhimu inatuambia kuwa kauli zote na matendo yote ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ni maelezo ya kutulengea, kutuongoza na kutuamrisha kutekeleza Swalaah kama ilivyoamrishwa katika Qur-aan na Sunnah. Juu ya hivyo, ni dalili kwamba Muislamu anapaswa lazima afuate Sunnah za Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika ‘ibaadah zake zote katika kila kitendo na kauli. Hivyo basi matendo yote aliyoyatenda Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na kauli zote alizotamka katika Swalaah ni waajib kwetu isipokuwa zile ambazo zimethibitishwa vinginevyo kwa dalili ya wazi kabisa.

[75] Endapo mtu yoyote, kwa sababu zisizokuwa za maradhi, hawezi kusimama wima, anaruhusiwa yeye kuswali huku amekaa, kama ambavyo mtu hufanya akiwa katika safari ya treni, ilimradi awe akikamilisha vizuri vitendo vya kurukuu na kusujudu. Akiwa hawezi kufanya hivyo kwa sababu ya maradhi, lazima afanye hivyo kwa kuashiria na kuinama. Akiwa anataka kusujudu mathalani, ni lazima ainamishe kichwa chake mbali zaidi kuliko kuinamisha kwa ajili ya kurukuu. Hii imeripotiwa katika Hadiyth iliyosimuliwa na Jaabir (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ).

08-Mlango Wa Sajdatus-Sahw Na Nyingine

بَابُ سُجُودِ السَّهْوِ وَغَيْرِهِ

263.

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ بُحَيْنَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى بِهِمُ الظُّهْرَ ، فَقَامَ فِي الرَّكْعَتَيْنِ الْأُولَيَيْنِ ، وَلَمْ يَجْلِسْ ، فَقَامَ النَّاسُ مَعَهُ ، حَتَّى إِذَا قَضَى الصَّلَاةَ ، وَانْتَظَرَ النَّاسُ تَسْلِيمَهُ ، كَبَّرَ وَهُوَ جَالِسٌ . وَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ ، قَبْلَ أَنْ يُسَلَّمَ ، ثُمَّ سَلَّمَ } أَخْرَجَهُ السَّبْعَةُ ، وَهَذَا لَفْظُ الْبُخَارِيِّ وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ : { يُكَبِّرُ فِي كُلِّ سَجْدَةٍ وَهُوَ جَالِسٌ وَسَجَدَ النَّاسُ مَعَهُ ، مَكَانَ مَا نَسِيَ مِنَ الْجُلُوسِ }

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Buhaynah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaswalisha Adhuhuri, akasimama mwisho wa Rakaa mbili za mwanzo na hakuketi chini.[2] Watu walimfuata wakasimama pamoja naye. Swalaah ilipomalizika, watu wakangojea atoe salaam. Akapiga Takbiyra hali akiwa ameketi. Huku akiwa amekaa, akasujudu Sajdah mbili kabla hajatoa salaam,[3], kisha akatoa salaam.” [Imetolewa na As-Sab’ah (Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad), na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipiga Takbiyra kwa kila Sajdah alipiga akiwa amekaa. Kisha alisujudu na Maamuma wote walisujudu pamoja naye kwa kufidia kule kuketi alikosahau.”

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {صَلَّى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِحْدَى صَلَاتِي الْعِشِيِّ رَكْعَتَيْنِ ، ثُمَّ سَلَّمَ ، ثُمَّ قَامَ إِلَى خَشَبَةٍ فِي مُقَدِّمِ الْمَسْجِدِ ، فَوَضَعَ يَدَهُ عَلَيْهَا ، وَفِي الْقَوْمِ أَبُو بَكْرٍ وَعُمَرُ ، فَهَابَا أَنْ يُكَلِّمَاهُ ، وَخَرَجَ سَرْعَانَ النَّاسِ ، فَقَالُوا : أَقْصِرْتَ . الصَّلَاةُ ، وَرَجُلٌ يَدْعُوهُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ذَا الْيَدَيْنِ ، فَقَالَ : يَا رَسُولَ اللَّهِ ، أَنْسَيْتَ أَمْ قُصِرْتَ ؟ فَقَالَ : " لَمْ أَنْسَ وَلَمْ تُقْصِرْ " فَقَالَ : بَلَى ، قَدْ نَسِيتُ ، فَصَلَّى رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ سَلَّمَ ، ثُمَّ كَبَّرَ ، فَسَجَدَ مِثْلَ سُجُودِهِ ، أَوْ أَطْوَلَ ثُمَّ رَفَعَ رَأْسَهُ فَكَبَّرَ ، ثُمَّ وَضَعَ رَأْسَهُ ، فَكَبَّرَ ، فَسَجَدَ مِثْلَ سُجُودِهِ ، أَوْ أَطْوَلَ . ثُمَّ رَفَعَ رَأْسَهُ وَكَبَّرَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ : {صَلَاةُ الْعَصْرِ} وَلِأَبِي دَاوُدَ ، فَقَالَ : {أَصْدَقَ ذُو الْيَدَيْنِ ؟} " فَأَوْمَأُوا : أَيْ نَعَمْ

وَهِيَ فِي " الصَّحِيحَيْنِ " لَكِنْ بِلَفْظٍ : فَقَالُوا وَهِيَ فِي رِوَايَةٍ لَهُ : {وَلَمْ يَسْجُدْ حَتَّى يَقْنَهُ اللَّهُ تَعَالَى ذَلِكَ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswalisha Rakaa mbili za Swalaah mojawapo kati ya mbili za Al-‘Ashiyy (yaani Adhuhuri au Alasiri), kisha akatoa salaam. Akasimama karibu na kipande kimoja cha ubao

kilichokuwa mbele ya Msikiti akaweka mkono wake juu yake. Abuu Bakr na ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) walikuwa miongoni mwa watu waliokuwepo pale, wakaogopa kumsemesha lolote Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Wenye haraka wakatoka na wakasema Swalaah imefupishwa. Miongoni mwa watu hao alikuwepo mtu ambaye Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akimwita Dhul-Yadayn[4] (mtu mwenye mikono mirefu), akauliza: Ee Rasuli wa Allaah! Umesahau au Swalaah imefupishwa? Akasema: “Sijasahau[5] wala haijafupishwa.” Akasema: “Bali umesahau.”[6], Kisha Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaswali Rakaa mbili zilizobakia, kisha akatoa salaam. Akapiga Takbiyra, akasujudu kama anavyosujudu Sajdah yake kawaida au ndefu zaidi. Kisha akainua kichwa chake na akatamka Takbiyra[7], akasujudu, akapiga Takbiyra, akasujudu kama Sajdah yake ya kawaida au ndefu zaidi. Akainua kichwa chake na akapiga Takbiyra.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Swalaah ya Alasiri.”

Na katika upokezi wa Abuu Daawuud: “Je Dhul-Yadayn amesema kweli? Nao wakasema “Ndio” kwa kuashiria.

Na hiyo imo katika Swahiyhayn lakini kwa neno فَقَالُوا (wakasema). Na katika mapokezi yake (Abuu Daawuud) mengine: “Hakusujudu hadi Allaah (تَعَالَى) alipompa uhakika wa hilo.”

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى
 اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى بِهِمْ ، فَسَهَا فَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ ، ثُمَّ تَشَهَّدَ ،
 ثُمَّ سَلَّمَ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ ، وَالْحَاكِمُ
 وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema
 kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaswalisha wao,
 akasahau kitu. Akasujudu Sajdah mbili, akasoma, kisha akatoa
 Tashahhud na salaam.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na At-
 Tirmidhiy aliipa daraja la Hasan, na Al-Haakim akaipa daraja la
 Swahiyh]

266.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ
 اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ فِي صَلَاتِهِ ، فَلَمْ
 يَذَرْكُمْ صَلَّيْ أَثَلَاثًا أَوْ أَرْبَعًا ؟ فَلْيَطْرَحِ الشَّكَّ وَلْيَبْنِ عَلَى مَا
 اسْتَيْقَنَ ، ثُمَّ يَسْجُدْ سَجْدَتَيْنِ قَبْلَ أَنْ يُسَلَّمَ ، فَإِنْ كَانَ صَلَّي
 خَمْسًا شَفَعْنَ لَهُ صَلَاتَهُ ، وَإِنْ كَانَ صَلَّي تَمَامًا كَانَتَا تَرْغِيمًا
 لِلشَّيْطَانِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema
 Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja
 wenu akitia shaka katika Swalaah yake, hajui Rakaa ngapi ameswali,
 ni tatu au nne, basi aache mashaka na ajengee idadi aliyo na yakini
 nayo[8]. Kisha asujudu Sajdah mbili kabla hajatoa salaam. Ikiwa
 aliswali Rakaa tano, basi Swalaah yake itamuomba[9], na ikiwa

aliswali Rakaa nne kamili zitakuwa zimentahayarisha shaytwaan.”
[Imetolewa na Muslim]

267.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {صَلَّى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَلَمَّا سَلَّمَ قِيلَ لَهُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، أَحَدَثَ فِي الصَّلَاةِ شَيْءٌ؟} قَالَ: "وَمَا ذَلِكَ؟". قَالُوا: صَلَّيْتَ كَذَا، قَالَ: فَتَنَى رَجُلِيهِ وَاسْتَقْبَلَ الْقِبْلَةَ، فَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ، ثُمَّ سَلَّمَ، ثُمَّ أَقْبَلَ عَلَيْنَا بِوَجْهِهِ فَقَالَ: "إِنَّهُ لَوْ حَدَّثَ فِي الصَّلَاةِ شَيْءٌ أَنْبَأْتُكُمْ بِهِ، وَلَكِنْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ، أَنْسَى كَمَا تَنْسَوْنَ، فَإِذَا نَسِيتُ فَذَكِّرُونِي، وَإِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ فِي صَلَاتِهِ فَلْيَتَحَرَّ الصَّوَابَ، فَلْيُتِمَّ عَلَيْهِ، ثُمَّ لِيَسْجُدْ سَجْدَتَيْنِ {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: {فَلْيُتِمَّ، ثُمَّ يُسَلِّمْ، ثُمَّ يَسْجُدْ} وَلِمُسْلِمٍ: {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَجَدَ سَجْدَتَيْنِ السَّهْوِ بَعْدَ السَّلَامِ وَالْكَلامِ}

وَلِأَحْمَدَ، وَأَبِي دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيَّ؛ مِنْ حَدِيثِ عَبْدِ بْنِ جَعْفَرٍ مَرْفُوعاً: {مَنْ شَكَّ فِي صَلَاتِهِ، فَلْيَسْجُدْ سَجْدَتَيْنِ بَعْدَ مَا يُسَلِّمُ} وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Ibn Mas‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswalisha, na alipotoa salaam aliulizwa: Ee Rasuli wa Allaah! Kuna jambo jipya limetokea

katika Swalaah? Akasema: “Kitu gani?” Wakasema: “Umeswali Rakaa kadhaa.” Hapo akakunja miguu yake akaeleka Qiblah na akasujudu Sajdah mbili, akatoa salaam. Akaelekea watu akasema: “Endapo kitu kipyaa kingeletwa katika Swalaah, ningekujulisheni, lakini mimi ni mwana Adam kama nyinyi,[10] ninasahau kama nyinyi mnavyosahau. Kwa hivyo nikisahau mnikumbushe. Na ikiwa yeyote kati yenu ana mashaka katika Swalaah yake, basi afuate lililo sawa na aikamilishe, kisha alete Sajdah mbili.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika mapokezi ya Al-Bukhaariy: “Akamilishe (Swalaah yake) kisha atoe salaam, kisha asujudu.”

Na katika Riwaayah ya Muslim: “**صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** (Nabiy) alisujudu Sajdah mbili za Sahw baada ya kutoa salaam na kuongea.”

Na katika mapokezi ya Ahmad, Abuu Daawuud na An-Nasaaiy kutokana Hadiyth Marfuw’ ya ‘Abdullaah bin Ja’far[11] ilisema: “Mwenye kutia shaka katika Swalaah yake, basi asujudu sijda mbili baada ya salaam.” [Akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

268.

وَعَنِ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ {إِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ ، فَقَامَ فِي الرُّكْعَتَيْنِ ، فَاسْتَتَمَ قَائِمًا ، فَلْيَمُضِ ، وَلْيَسْجُدْ سَجْدَتَيْنِ ، وَإِنْ لَمْ يَسْتَتِمَ

قَائِمًا فَلْيَجْلِسْ وَلَا سَهْوَ عَلَيْهِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَابْنُ مَاجَةَ ،
وَالدَّارَقُطْنِيُّ ، وَاللَّفْظُ لَهُ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Al-Mughiyrah bin Shu'bah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesimulia kuwa Rasuli wa Allaah amesema: “Endapo mmoja wenu atapata mashaka akasimama katika Rakaa mbili, akikumbuka wakati ameshasimama basi aendelee[12] na asirejee kwenye kukaa, na asujudu katika Sajdah mbili. Lakini endapo hakuwahi kusimama wima kabisa basi akae na hana Sajdah mbili za kusahau.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, Ibn Maajah na Ad-Daaraqutwniy na tamshi ni lake, kwa Isnaad dhaifu]

269.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَيْسَ عَلَى مَنْ خَلَفَ الْإِمَامَ سَهْوٌ فَإِنْ سَهَا الْإِمَامُ فَعَلَيْهِ وَعَلَى مَنْ خَلَفَهُ} رَوَاهُ الْبَزَّازُ وَالْبَيْهَقِيُّ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna Sijdatus-sahw kwa anayeswali[13] nyuma ya Imaam, Imaam akisahau, ni juu yake na juu ya Imaam na wanaomfuata kuileta.” [Imetolewa na Al-Bazaar na Al-Bayhaqiyy kwa Isnaad dhaifu]

270.

وَعَنْ ثَوْبَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لِكُلِّ سَهْوٍ سَجْدَتَانِ بَعْدَمَا يُسَلِّمُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَابْنُ مَاجَهَ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Thawbaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kila sahau ni Sajdah mbili baada ya salaam.[14]” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na Ibn Maajah kwa Isnaad dhaifu]

271.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {سَجَدْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي: (إِذَا السَّمَاءُ انْشَقَّتْ) ، وَ: (اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ)} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulisujudu pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akisoma Suwrah:[15]

إِذَا السَّمَاءُ انْشَقَّتْ (١) [16].

na

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ [17]

.” [Imetolewa na Muslim]

272.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { (ص) لَيْسَتْ مِنْ عَزَائِمِ السُّجُودِ ، وَقَدْ رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَسْجُدُ فِيهَا } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutokwa kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Kusujudu wakati inaposomwa Suwrah Swaad[18] si katika ‘azaaaim (zilizoamrisha kusujudu)[19], lakini nilimuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisujudu katika Suwrah hiyo.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

273.

وَعَنْهُ: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَجَدَ بِالنَّجْمِ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) tena amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisujudu kwa kusoma Suwrah An-Najm.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

274.

وَعَنْ زَيْدِ بْنِ ثَابِتٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { قَرَأْتُ عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ النَّجْمَ ، فَلَمْ يَسْجُدْ فِيهَا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Zayd bin Thaabit[20] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilisoma mbele ya Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Suwrah

An-Najm[21], na hakusujudu ndani yake.[22]” [Al-Bukhaariy, Muslim]

275.

وَعَنْ خَالِدِ بْنِ مَعْدَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {فُضِّلَتْ سُورَةُ الْحَجِّ بِسَجْدَتَيْنِ} . رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ فِي " الْمَرَاسِيلِ " وَرَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَالتِّرْمِذِيُّ مَوْصُولًا مِنْ حَدِيثِ عُقْبَةَ بْنِ عَامِرٍ ، وَزَادَ: {فَمَنْ لَمْ يَسْجُدْهُمَا ، فَلَا يَقْرَأَهَا} وَسَنَدُهُ ضَعِيفٌ

Kutoka kwa Khaalid bin Ma'daan[23] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Suwrah Al-Hajj[24] imefadhilishwa kwa kuwa na Sajdah mbili.” [Imetolewa na Abuu Daawuud katika Al-Maraasiyl]

Na waliipokea Ahmad na At-Tirmidhiy katika Hadiyth Mawsuwl kutoka kwa ‘Uqbah bin ‘Aamir, akaongezea: “Asiyesujudu Sajdah hizo mbili (za Suwrah Al-Hajj), basi asiisome.” [Isnaad yake ni dhaifu]

276.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا نَمُرُّ بِالسُّجُودِ فَمَنْ سَجَدَ فَقَدْ أَصَابَ ، وَمَنْ لَمْ يَسْجُدْ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ} . رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ . وَفِيهِ: {إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى لَمْ يَفْرِضْ السُّجُودَ إِلَّا أَنْ نَشَاءَ} . وَهُوَ فِي " الْمَوْطَأِ "

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Enyi watu, katika visomo vyetu tunapita Aayah za kusujudu. Hivyo, anayesujudu amefanya sawa na asiyesujudu hana dhambi.[25]” [Imetolewa na Al-Bukhaariy] na ndani yake kuna: “Allaah (تعالى) Hakufaradhisha kusujudu, ila tukipenda.” [Ipo katika kitabu Al-Muwatwa’ cha Imaam Maalik]

277.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ عَلَيْنَا الْقُرْآنَ ، فَإِذَا مَرَّ بِالسَّجْدَةِ ، كَبَّرَ ، وَسَجَدَ ، وَسَجَدْنَا مَعَهُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ بِسَنَدٍ فِيهِ لِيْنٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitusomea Qur-aan, na kila alipofika mahali pa kusujudu alipiga Takbiyra na akasujudu, nasi tukasujudu pamoja naye.[26]” [Imetolewa na Abuu Daawuwd kwa Isnaad laini]

278.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا جَاءَهُ أَمْرٌ يَسْرُهُ خَرَّ سَاجِدًا لِلَّهِ { رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ

Kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa likimjia jambo lililomfurahisha anaporomoka, akisujudu.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy]

279.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَوْفٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {سَجَدَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَأَطَالَ السُّجُودَ ، ثُمَّ رَفَعَ رَأْسَهُ وَقَالَ: " إِنَّ جِبْرِيلَ آتَانِي ، فَبَشِّرْنِي ، فَسَجَدْتُ لِلَّهِ شُكْرًا " }
رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Awf[27] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisujudu na akarefusha Sajdah, kisha akainua kichwa chake akasema: “Jibriyl amekuja na akanibashiria habari nzuri, kwa hiyo nimesujudu kumshukuru Allaah.” [Imetolewa na Ahmad, na akaisahihisha Al-Haakim]

280.

وَعَنْ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعَثَ عَلِيًّا إِلَى الْيَمَنِ فَذَكَرَ الْحَدِيثَ قَالَ : فَكَتَبَ عَلِيٌّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ بِإِسْلَامِهِمْ ، فَلَمَّا قَرَأَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى

الله عليه وسلم الْكِتَابَ خَرَّ سَاجِدًا { رَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ وَأَصْلُهُ فِي الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Al-Baraa bin ‘Aazib (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma ‘Aliy kwenda Yaman. Msimuliaji akaitaja Hadiyth.[28] Alisema: “‘Aliy akaandika barua kuhusu kusilimu kwao. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akasoma barua hiyo akasujudu kumshukuru[29] Allaah (تعالى) kwa ajili ya hilo.” [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy na chanzo chake kimo katika Al-Bukhaariy]

[1] Sijdatus-sahw (Sajdah ya kusahau) huwa ni waajib iwapo mtu anayeswali anaongeza au anapunguza tendo fulani ndani ya Swalaah kwa makosa.

[2] Yapasa tuelewe kwamba tafsiri ya maneno ya kiarabu “Sahw” na “Nisyaan” ni “Kusahau”. Lakini “Sahw” inamaanisha kutenda mambo zaidi, na “Nisyaan” kwa kawaida inamaanisha sehemu ndogo ya taarifa. Lakini maneno yote haya mawili yanahesabika kuwa ni visawe, yaani moja ni sawasawa na jingine. Miongoni mwa ‘Ulamaa, hakuna hata mmoja anayelitumia neno “Nisyaan” kwa ajili ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Kwa hivyo Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kamwe hakuwahi kuugua maradhi ya kuchanganyikiwa katika mambo yahasuyo kulingania Risala ya Uislamu. Angewezaje kuugua maradhi kama hayo wakati Allaah, Anasema katika Suwrah Al-A’laa:

سَنُقَرِّئُكَ فَلَا تَنْسَى (٦)

Tutakusomesha (Qur-aan ee Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) basi hutoisahau

[Al-A’laa: 6].

‘Ulamaa waadilifu wanasema kuwa, matumizi ya neno ‘Sahw’ kwa ajili ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) inaruhusiwa kwa kuwa zipo rejea nyingi kutoka katika Hadiyth nyingi kuhusu kadhia hii. Maimaamu wote wane wanaafiki kwamba, mazingira yanayohusu kusahau (Sahw) kwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) yamethibitishwa. Hakuna ubaya katika hili; bali kuna niyyah njema (inamaanisha, usahau wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)).

[3] Hadiyth hii inatufunza kuwa, mtu anaweza kufidia katika kuacha Tashahhud ya kwanza kwa kuleta Sijdatus-Sahw. Wengine wanasema iletwe kabla ya Salaam, na wengine wanasema iletwe baada ya Salaam. Hali zote hizi mbili zina ushahidi kutoka kwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ambaye hakuweka kanuni thabiti kuhusu hili. Katika kitabu cha Niyl Al-Awtwaar kuwa endapo kumeondoshwa jambo ndani ya Swalaah basi Sajdah iletwe baada ya Salaam. Wanazuoni wengine wanasema kuwa, ushahidi wa Sajdah kabla ya Salaam ni sahihi na sawa zaidi.

[4] Huyu Dhul-Yadayn ndiye Al-Khirbaq bin ‘Amr As-Sulaymiyy wa kabila la Baniyy Sulaym. Alifariki zama za Ukhalifa wa Mu’aawiyah (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ). Inasemekana pia kuwa alifia kule Dhi Khashab zama za Ukhalifa wa ‘Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ). Alikuwa na mikono mirefu mno; ndiyo maana akaitwa kiutani Dhul-Yadayn

[5] Kwa mujibu wa ufahamu wangu, sijaugua usahaulifu wala haikuja amri la Shariy’ah kwa Swalaah kufupishwa.

[6] Usahaulifu wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiwa ndani ya Swalaah, juu ya ukweli kwamba alikuwa kazama sana katika tafakuri wakati akiomba Du’aa kwa Allaah (سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى) inaweza kueleweka kikweli kuwa ilikuwa tendo la haki na lilikuwa kwa niyyah njema. Kwanza tendo lile lilikuwa la kuuelimisha Ummah kimatendo juu ya mambo yanayohusu kusahau (Sahw) na ni yapi maagizo yake na jinsi ya kuyarekebisha pindi mtu yeyote atakabiliwa na hali kama ile. Pili, alitaka

kuufundisha Ummah kwamba, juu ya heshima zake, hadhi, na nafasi ya juu sana ya kuwa zaidi kuliko viumbe wote, na yeye ni mwana Adam, na amerithi hisia zote za kibinadamu kwa mfano kula, kunywa, kulala, kuamka, kutembea tembea, kwenda haja, kupata magonjwa na kuponywa, n.k. sifa zote zilizotajwa hapo juu zimedhihirishwa kwa nafsi yake. Yeye mwenyewe alilitaja jambo hili la busara na kama hilo litakalotajwa katika Hadiyth iliyosimuliwa na Ibn Mas-'uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ).

[7] Hadiyth hii inaweka wazi kwamba, pindi mtu akifikiri ana hakika amekamilisha Swalaah yake, anatoa Salaam, anaanza hata kuzungumza, na kisha ghafla anatambua kosa lake kwa kukumbuka yeye mwenyewe au mtu mwingine anamkumbusha kosa lake, Swalaah yake inabakia kuwa sahihi ilimradi tu aikamilishe mara moja.

[8] Hii ina maana mbili: Kwanza, kukiweco mashaka, mtu achukue namba ndogo zaidi. Kwa mfano, akiwa hana hakika ameshaziswali Rakaa tatu au nne, basi achukulie kuwa ni Rakaa tatu, kwani hii ni karibu zaidi na ukweli. Pili afanye lile ambalo ana hakika zaidi kuwa ndiyo sawa.

[9] Inamaanisha kuwa iwapo mtu kaziswali Rakaa tano, zitakuwa sita kwa kujumlisha na Sijdatus-Sahw. Inaonekana kutoka katika Hadiyth hii kuwa mtu sharti awe akichukulia namba ya Rakaa ya chini zaidi, kwani hiyo ndiyo huwa karibu zaidi na ukweli.

[10] Kwa mujibu wa rejea hii, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitumia maneno ya:

"إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ"

((Mimi ni mwanadamu kama nyinyi))."

Hii huenda itawashangaza sana watu wasiomchukulia yeye kama mwana Adam, na wanadai kuwa kauli ya Allaah (سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى) katika Qur-aan:

إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ

“Hakika mimi ni mtu kama nyinyi;” [Fusw-Swilat: 6],

Unawania kuwanyamazisha tu washirikina wengi, ambapo ukweli ni kwamba watu wanaohusika hapa ni Waumini na wala sio washirikina.

[11] ‘Abdullaah bin Ja’far ndiye Abuu Ja’far ‘Abdullaah bin Ja’far bin Abiy Twaalib, na mama yake ni Asmaa’ bint ‘Umayy. Huyu ni Mwislamu wa mwanzo kuzaliwa kule Abyssinia, na baba yake alitoka Al-Madiynah mnamo mwaka wa 7 A.H. alikuwa mcheshi sana, mwenye taqwa, na mkarimu sana. Alikuwa mkarimu kuliko wote miongoni mwa Waislamu. Alifariki Al-Madiynah mnamo mwaka 80 A.H. akiwa na umri wa miaka 80.

[12] Endapo mtu amesahau kusoma Tashahhud ya kati na akasimama wima kabisa, lazima aendeleo na Swalaah yake. Lakini akiwa hakuwahi kusimama wima kikamilifu, achunguze kama yuko karibu na kusimama au karibu na kukaa. Akiwa karibu zaidi na kusimama, lazima asimame na alete Sijdatus-Sahw. Akiwa karibu na kukaa basi lazima akae chini kabisa, asome Tashahhud, na hana haja ya kuleta zile Sajdah mbili za Sahw.

[13] Hadiyth hii inatufunza kwamba, kuleta Sijdatus-Sahw huwa ni lazima kwa Muqtadi (mtu anayeswalishwa yaani Maamuma) pale tu ambapo Imaam kasahau, na wala siyo ikiwa yeye mtu mwenyewe kasahau.

[14] Hadiyth hii haina maana ya kuwa endapo mtu kafanya makosa mawili au manne, basi lazima alete Sijdatus-Sahw mbili kwa kila kosa. Inamaanisha tu kwamba, bila kujali aina na wingi wa makosa ambayo mtu kayafanya, Sajdah mbili tu zinatoshleza kufidia makosa yote. (Baadhi ya Wanazuoni wanaona kuwa Hadiyth hii inakubalika. Tazama Subulus-Salaam, (1/418-419), namba (319) na Irwaa’ Al-Ghaliyl, (2/47- 48) namba (339).

[15] Kama Sijdatut-Tilaawa (Sajdah ya kusoma baada ya Aayah maalumu za Qur-aan) itahesabika kama Mashruw’ (ya kuamrishwa), Sunnah (ya khiayri), au Waajib (ya kuwajibika), Wanazuoni wengi wanahesabu ile ni

Sunnah, lakini Imaam Abuu Haniyfah amesema kuwa ni Waajib. Pia kuna kutofautiana maoni mtu sharti awe na wudhuu au hata akiwa hana wudhuu, anaweza kuleta Sajdah hii.

[16] Al-Inshiqaaq (84: 21)

[17] Al-‘Alaq (96: 19)

[18] Swaad (38: 88)

[19] Kwa mujibu wa Imaam wengine, Sajdah hii ni lazima kama Sajdah zingine. Hadiyth hii inaashiria tu kwamba hii haikuamriwa kuwa iwe ni tendo la ‘Ibaadah; lakini Sajdah hii inatekelezwa mpaka sasa ikiwa kama ukumbusho wa mwenendo wa Nabiyy Daawuud (عليه السلام).

[20] Zayd bin Thaabit ni Answaar na Najjaar, alipewa jina la utani la Abuu Sa’iyd au Abuu Khaarijah. Alikuwa muandishi mzuri wa Qur-aan, na alijua sana elimu ya Mirathi. Alipigana kwanza katika vita vya Al-Khandaq. Alikusanya Qur-aan zama za Ukhalifa wa Abuu Bakr, na aliinakili katika Ukhalifa wa ‘Uthmaan. Alijifunza maandishi ya Kiyahudi kwa nusu mwezi. Kwa amri ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na alikuwa akimuandikia na kumsomea maandishi hayo. Alifia Al-Madiynah mnamo mwaka wa 45 A.H. Imesemekana pia kuwa alikufa katika mwaka mwingine.

[21] An-Najm (53: 62).

[22] Hii ndiyo maana Wanazuoni wameihesabu Sijdatut-Tilaawah inayofanywa wakati wa kusoma Aayah maalumu za Qur-aan kuwa ni Sunnah, kwa sababu Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakuitekeleza hii mara zote. Wakati mwingine alisujudu, na wakati mwingine hakisujudu kabisa.

[23] Khaalid bin Ma'daan ndiye Abuu 'Abdillaah Al-Kalaa'i kutoka Hims, Syria. Alikuwa miongoni mwa kizazi cha Taabi'iy (watu waliokuja baada ya Maswahaba) maarufu na wenye elimu na ujuzi sana. Alisema kuwa aliwahi kukutana na Maswahaba sabini wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alifariki mwaka 103 au 104 au 108 A.H

[24] Al-Hajj (22: 18 , 77).

[25] Hadiyth hii ni ushahidi wa wazi kuwa Sijdatut-Tilaawah siyo tendo la lazima. 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) alisema hivyo alipokuwa akiwahutubia Maswahaba waliokusanyika kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na hakuna hata mmoja kati yao aliyenena neno juu yake, hiyo ilithibitisha kuwa wote walibaki kimya kuhusu jambo hili.

[26] Hii inatufahamisha kuwa kusujudu ni waajib wa msomaji na hata msikilizaji, kwa sharti kwamba watu wawe ndani ya Swalaah. Na vivyo hivyo huwa kwa Sijdatut-Tilaawah (Sajdah ndani ya kisomo) na Sajdah Ash-Shukr.

[27] 'Abdur-Rahmaan bin 'Awf (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) ndiye aitwaye Abuu Muhammad Az-Zuhriy Al-Qarayshiy. Alisilimu mapema, akahamia Abyssinia mara mbili. Alishiriki katika vita vya Badr na vita vingine vikubwa. Huyu ni mmoja katika wale watu kumi walioahidiwa Jannah, na ni mmoja wa watu sita ambao 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) aliwateua kuwa Makhalifa baada yake. Alitoa dinari elfu nne, kisha elfu arubaini, na kisha farasi mia tano na ngamia mia tano waliobebeshwa kama Swadaqah wakati Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akingali hai. Aliacha wasia wa bustani la thamani ya elfu mia nne kwa "Akina Mama wa Waumini." Alikufa mnamo mwaka wa 34 A.H. na akazikwa Al-Baqi'.

[28] Imeripotiwa kuwa 'Aliy (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) alikwenda Yemen na watu wake mia tatu. Akawaita Wayemeni kusilimu. Jibu la Wayemeni lilikuwa kuwashambulia akina 'Aliy kwa mishale, 'Aliy alijibu mashambulizi yale,

na wanaharakati wake maarufu 20 wakauliwa. Kukazuka mfarakano katika kambi ya ‘Aliy, na wengine wakakimbia kutoka uwanja wa vita. Wakaitwa kusilimu mara ya pili, nao wakakubali. ‘Aliy alikutana na Nabiyy (ﷺ) kule Makkah wakati wa Hijjah, mwaka ule ule, baada ya kurejea salama toka katika ujumbe huo.

[29] Hii inatoa jibu watu wale wasioamini usahihi uliothibitishwa wa Sajdah Ash-Shukr

09-Mlango Wa Swalaah Za Sunnah

بَابُ صَلَاةِ التَّطَوُّعِ

09-Mlango Wa Swalaah Za Sunnah

281.

عَنْ رَبِيعَةَ بْنِ كَعْبٍ الْأَسْلَمِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { قَالَ لِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَلْ . فَقُلْتُ : أَسْأَلُكَ مُرَافَقَتَكَ فِي الْجَنَّةِ . فَقَالَ : أَوْغَيْرَ ذَلِكَ ؟ ، قُلْتُ : هُوَ ذَاكَ ، قَالَ : " فَأَعِنِّي عَلَى نَفْسِكَ بِكَثْرَةِ السُّجُودِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Rabiyy’ah bin Ka’b Al-Aslamiyy[1] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiyy (ﷺ) aliniambia: “Ombe.” Nikasema: “Ninakuomba niwe pamoja nawe Jannah.” Aksema: “Hakuna zaidi ya hilo?” Nikasema: “Hilo tu basi.”

Akasema: “Basi nisaidie mimi juu ya nafsi yako[2] kwa kukithirisha kusujudu.” (Yaani Swalaah)[3] [Imetolewa na Muslim][4]

282.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : { حَفِظْتُ مِنَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَشْرَ رَكَعَاتٍ : رَكَعَتَيْنِ قَبْلَ الظُّهْرِ ، وَرَكَعَتَيْنِ بَعْدَهَا ، وَرَكَعَتَيْنِ بَعْدَ الْمَغْرَبِ فِي بَيْتِهِ ، وَرَكَعَتَيْنِ بَعْدَ الْعِشَاءِ فِي بَيْتِهِ ، وَرَكَعَتَيْنِ قَبْلَ الصُّبْحِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَفِي رِوَايَةٍ لَهُمَا : { وَرَكَعَتَيْنِ بَعْدَ الْجُمُعَةِ فِي بَيْتِهِ } وَلِمُسْلِمٍ : { كَانَ إِذَا طَلَعَ الْفَجْرُ لَا يُصَلِّي إِلَّا رَكَعَتَيْنِ خَفِيفَتَيْنِ }

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) “Nimehifadhi kutoka kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Rakaa kumi (za Sunnah): Rakaa mbili kabla ya Adhuhuri, na mbili baada yake; Rakaa mbili baada ya Magharibi nyumbani kwake, na Rakaa mbili baada ya ‘Ishaa nyumbani kwake; na Rakaa mbili kabla ya Alfajiri.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika mapokezi yao (Al-Bukhaariy, Muslim) mengine: “Rakaa mbili baada ya Ijumaa nyumbani kwake.”

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Haswali baada ya kutoka jua ila Rakaa mbili khafifu.”

283.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا : أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { كَانَ لَا يَدْعُ أَرْبَعًا قَبْلَ الظُّهْرِ وَرَكَعَتَيْنِ قَبْلَ الْغَدَاةِ }
رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Hakuacha Rakaa nne kabla ya Swalaah ya Adhuhuri, na Rakaa mbili kabla ya Swalaah ya Alfajiri.[5]”
[Imetolewa na Al-Bukhaariy]

284.

وَعَنْهَا قَالَتْ: { لَمْ يَكُنْ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى شَيْءٍ مِنَ النَّوَافِلِ أَشَدَّ تَعَاهُدًا مِنْهُ عَلَى رَكَعَتَيِ الْفَجْرِ }
عَلَيْهِ

وَلِمُسْلِمٍ: { رَكَعَتَا الْفَجْرِ خَيْرٌ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا }

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakuwahi kukaza niyyah ya kuswali Rakaa mbili za Swalaah yoyote ya khiari kuliko Rakaa mbili kabla ya Alfajiri. [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Rakaa mbili za Alfajiri ni bora kuliko dunia na vilivyomo ndani yake.”

وَعَنْ أُمِّ حَبِيبَةَ أُمِّ الْمُؤْمِنِينَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : سَمِعْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ : { مَنْ صَلَّى اثْنَتَا عَشْرَةَ رَكْعَةً فِي يَوْمٍ وَلَيْلَةٍ بُنِيَ لَهُ بِهِنَّ بَيْتٌ فِي الْجَنَّةِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ . وَفِي رِوَايَةٍ " تَطَوُّعًا "

وَلِلتِّرْمِذِيِّ نَحْوُهُ ، وَزَادَ : { أَرْبَعًا قَبْلَ الظُّهْرِ وَرَكْعَتَيْنِ بَعْدَهَا ، وَرَكْعَتَيْنِ بَعْدَ الْمَغْرَبِ ، وَرَكْعَتَيْنِ بَعْدَ الْعِشَاءِ ، وَرَكْعَتَيْنِ قَبْلَ صَلَاةِ الْفَجْرِ }

وَالْخَمْسَةَ عَنْهَا : { مَنْ حَافِظٌ عَلَى أَرْبَعٍ قَبْلَ الظُّهْرِ وَأَرْبَعٍ بَعْدَهَا حَرَّمَهُ اللَّهُ عَلَى النَّارِ }

Kutoka kwa Ummu Habiyyah[6] Mama wa Waumini (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nimemsikia Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akisema: “Mwenye kuswali Rakaa kumi na mbili mchana na usiku atajengewa nyumba Jannah kwa sababu ya hizo Rakaa.” [Imetolewa na Muslim]

Katika mapokezi mengine: “...Za Sunnah....”

Na At-Tirmidhiy alisimulia hivyo hivyo ila akaongezea: “Rakaa nne kabla ya adhuhuri na mbili baada yake; na Rakaa mbili baada ya Magharibi, na Rakaa mbili baada ya ‘Ishaa, na Rakaa mbili kabla ya Swalaah ya Alfajiri.”

Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) wamepokea toka kwake (Ummu Habiyyah):

“Mwenye kuhifadhi (kuswali) Rakaa nne kabla ya Adhuhuri na nne baada yake, Allaah (تعالى) Atamharamishia Moto.”

286.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { رَحِمَ اللَّهُ إِمْرَأً صَلَّى أَرْبَعًا قَبْلَ الْعَصْرِ } رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَأَبُو دَاوُدَ وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah Anamrehemu mtu anayeswali Rakaa nne kabla ya Alasiri.[7]” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud, na At-Tirmidhiy naye aliipa daraja la Hasan. Na Ibn Khuzaymah aliipa daraja la Swahiyh]

287.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مُغَفَّلٍ الْمُزَنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : { صَلُّوا قَبْلَ الْمَغْرِبِ ، صَلُّوا قَبْلَ الْمَغْرِبِ } ثُمَّ قَالَ فِي الثَّلَاثَةِ : " لِمَنْ شَاءَ " كَرَاهِيَةً أَنْ يَتَّخِذَهَا النَّاسُ سُنَّةً { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَفِي رِوَايَةِ ابْنِ حِبَّانَ : { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى قَبْلَ الْمَغْرِبِ رَكْعَتَيْنِ }

وَلِمُسْلِمٍ عَنْ أَنَسٍ قَالَ: {كُنَّا نُصَلِّي رَكْعَتَيْنِ بَعْدَ غُرُوبِ الشَّمْسِ ، فَكَانَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَرَانَا ، فَلَمْ يَأْمُرْنَا وَلَمْ يَنْهَانَا}

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mughaffal Al-Muzaniyy[8] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalini kabla ya Magharibi, swalini kabla ya Magharibi.”[9] Na mara ya tatu amesema: “Kwa anayetaka.” Kwa kuchelea watu wasiifanye kuwa ni Sunnah.[10] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Ibn Hibbaan: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali Rakaa mbili kabla ya Magharibi.”

Na Muslim kupitia kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulikuwa tukiswali Rakaa mbili baada ya kuchwa jua, na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akituona naye hakutumrisha wala hakutukataza.”

288.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُخَفِّفُ الرِّكَعَتَيْنِ اللَّتَيْنِ قَبْلَ صَلَاةِ الصُّبْحِ ، حَتَّى إِنِّي أَقُولُ : أَقْرَأَ بِأَمِّ الْكِتَابِ ؟} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akihafifisha Rakaa mbili kabla ya

Alfajiri hadi mimi ninasema: Amesoma Ummul-Kitaab? (Al-Faatihah).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

289.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ : { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَرَأَ فِي رَكْعَتَيِ الْفَجْرِ : (قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ) وَ (قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ) } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisoma:

قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ (١)

Sema: “Enyi makafiri!”[11]

Na:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ (١)

“Sema: “Yeye ni Allaahu Mmoja Pekee.”[12] katika Rakaa mbili za Alfajiri.” [Imetolewa na Muslim]

290.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : { كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا صَلَّى رَكْعَتَيِ الْفَجْرِ اضْطَجَعَ عَلَى شِقِّهِ الْأَيْمَنِ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Pindi Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiswali Rakaa mbili za Alfajiri analalia ubavu wake wa kulia.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

291.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ الرُّكْعَتَيْنِ قَبْلَ صَلَاةِ الصُّبْحِ ، فَلْيُضْطَجِعْ عَلَى جَنْبِهِ الْأَيْمَنِ } رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَأَبُو دَاوُدَ ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakaposwali mmoja wenu Rakaa mbili kabla ya Swalaah ya Alfajiri, basi alalie upande wake wa kuume.”[13] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud, na At-Tirmidhiy naye aliipa daraja la Swahiyh]

292.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { صَلَاةُ اللَّيْلِ مَثْنَى مَثْنَى ، فَإِذَا خَشِيَ أَحَدُكُمْ الصُّبْحَ صَلَّى رَكْعَةً وَاحِدَةً ، تُؤْتِرُ لَهُ مَا قَدْ صَلَّى } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَالْخَمْسَةِ وَصَحَّحَهُ ابْنُ حَبَّانَ: {صَلَاةُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ مَثْنَى مَثْنَى} وَقَالَ النَّسَائِيُّ: "هَذَا خَطَأً"

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah za usiku ni Rakaa mbili mbili, na mmoja wenu akikhofia Swalaah ya Alfajiri, basi aswali Rakaa moja ambayo itakuwa ni Witr ya Rakaa alizoswali.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Imepokewa Hadiyth na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad), ambayo Ibn Hibbaan aliipa daraja la Swahiyh: “Swalaah za (Sunnah za) usiku na mchana ni Rakaa mbili mbili.”

An-Nasaaiy amesema: “Hili ni kosa.[14]”[15]

293.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَفْضَلُ الصَّلَاةِ بَعْدَ الْفَرِيضَةِ صَلَاةُ اللَّيْلِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah bora zaidi baada ya Swalaah ya faradhi ni Swalaah ya usiku.” [Imetolewa na Muslim]

294.

وَعَنْ أَبِي أَيُّوبَ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الْوُتْرُ حَقٌّ عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ، مَنْ أَحَبَّ أَنْ يُوتِرَ بِخَمْسٍ فَلْيَفْعَلْ، وَمَنْ أَحَبَّ أَنْ يُوتِرَ بِثَلَاثٍ فَلْيَفْعَلْ، وَمَنْ أَحَبَّ أَنْ يُوتِرَ بِوَاحِدَةٍ فَلْيَفْعَلْ} رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَرَجَّحَ النَّسَائِيُّ وَقَفَّهُ

Kutoka kwa Abuu Ayyuwb Al-Anaswaariy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah ya Witr ni haki juu ya kila Muislamu.[16] Anayependa kuswali kwa Rakaa tano, na afanye hivyo, na anayetaka kuiswali kwa Witr ya Rakaa tatu na afanye hivyo, na anayetaka kuiswali kwa Rakaa moja na afanye hivyo.[17]” [Imetolewa na Al-Arba’ah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan, na An-Nasaaiy aliipa daraja la Mawquwf]

295.

وَعَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَيْسَ الْوُتْرُ بِحَتْمٍ كَهَيْئَةِ الْمَكْتُوبَةِ، وَلَكِنْ سُنَّةٌ سَنَّهَا رَسُولُ اللَّهِ} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَّنَهُ وَالْحَاكِمُ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Aliy bin Abiy Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Swalaah ya Witr siyo lazima kama Swalaah ya faradhi, lakini ni Sunnah iliyowekwa na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).” [Imetolewa na An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy naye aliipa daraja la Hasan, na Al-Haakim akaisahihisha]

296.

وَعَنْ جَابِرٍ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَامَ فِي شَهْرِ رَمَضَانَ، ثُمَّ انْتَظَرُوهُ مِنَ الْقَابِلَةِ فَلَمَّا يَخْرُجُ، وَقَالَ: " إِنِّي خَشِيتُ أَنْ يُكْتَبَ عَلَيْكُمُ الْوُتْرُ } رَوَاهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali katika mwezi wa Ramadhwaan kisha Maswahaba zake wakamngojea usiku wa pili, lakini hakutoka (nyumbani kwake) akasema: Niliogopa isije[18] Witr ikafaradhishwa kwenu[19].” [Imetolewa na Ibn Hibbaan]

297.

وَعَنْ خَارِجَةَ بِنِ حُذَافَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِنَّ اللَّهَ أَمَدَّكُمْ بِصَلَاةٍ هِيَ خَيْرٌ لَكُمْ مِنْ حُمْرِ النَّعَمِ " قُلْنَا : وَمَا هِيَ يَا رَسُولَ اللَّهِ ؟ قَالَ: " الْوُتْرُ ، مَا بَيْنَ صَلَاةِ الْعِشَاءِ إِلَى طُلُوعِ الْفَجْرِ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

وَرَوَى أَحْمَدُ: عَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ ، عَنْ أَبِيهِ ، عَنْ جَدِّهِ نَحْوَهُ

Kutoka kwa Khaarijah bin Hudhaafah[20] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah Amekupeni Swalaah ya ziada iliyo bora kwenu kuliko ngamia wekundu.” Tukasema: “Ni ipi Ee Rasuli wa Allaah?”

Akasema: “Ni Witr iliyo baina ya Swalaah ya ‘Ishaa na Alfajiri.[21]” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha Al-Haakim]

Na Ahmad amepokea Hadiyth inayofanana na hiyo kutoka kwa ‘Amr[22] bin Shu’ayb[23] kwa usimulizi wa baba yake aliyeipokea kutoka kwa babu yake ‘Amr.

298.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ بُرَيْدَةَ ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { الْوُتْرُ حَقٌّ ، فَمَنْ لَمْ يُوتِرْ فَلَيْسَ مِنَّا } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ بِسَنَدٍ لَيْثٍ ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ وَلَهُ شَاهِدٌ ضَعِيفٌ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ عِنْدَ أَحْمَدَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Buraydah[24] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amepokea kutoka kwa baba yake kuwa, Rasuli wa Allaa (صَلَّى اللَّهُ) amesema: “Witr ni haki kwa hivyo asiyeiswali si miongoni mwetu.” [Imetolewa na Abuu Daawuud kwa Isnaad laini, na akaisahihisha Al-Haakim]

Na ina ushahidi dhaifu kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ) uliopokewa na Ahmad.

299.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {مَا كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَزِيدُ فِي رَمَضَانَ وَلَا فِي غَيْرِهِ عَلَى إِحْدَى عَشْرَةِ رَكْعَةٍ، يُصَلِّي أَرْبَعًا، فَلَا تَسْأَلُ عَنْ حُسْنِهِنَّ وَطُولِهِنَّ، ثُمَّ يُصَلِّي أَرْبَعًا، فَلَا تَسْأَلُ عَنْ حُسْنِهِنَّ وَطُولِهِنَّ، ثُمَّ يُصَلِّي ثَلَاثًا. قَالَتْ عَائِشَةُ، فَقُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، أَتَنَامُ قَبْلَ أَنْ تُؤْتِرَ؟ قَالَ: "يَا عَائِشَةُ، إِنَّ عَيْنَيَّ تَنَامَانِ وَلَا يَنَامُ قَلْبِي." { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لَهُمَا عَنْهَا: {كَانَ يُصَلِّي مِنَ اللَّيْلِ عَشْرَ رَكْعَاتٍ، وَيُؤْتِرُ بِسَجْدَةٍ، وَيَرْكَعُ رَكْعَتَيَ الْفَجْرِ، فَتِلْكَ ثَلَاثُ عَشْرَةٍ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakuzidisha Rakaa kumi na moja za Sunnah katika mwezi wa Ramadhwaan wala katika miezi mingine, Aliswali Rakaa nne, usiulize uzuri wake wala urefu wake. Kisha Rakaa nne usiulize uzuri na urefu wake. Kisha akswali Rakaa tatu za Witr.” ‘Aaishah akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Utalala usingizi kabla ya kuswali Witr?” Akasema: “Ee ‘Aaishah macho yangu hulala, lakini moyo wangu haulali.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika mapokezi ya Al-Bukhaariy na Muslim: “Alikuwa akiswali usiku Rakaa kumi, na anamalizia Witr kwa kuswali Rakaa moja, na alikuwa akiswali Rakaa mbili za Alfajiri, kwa hiyo hizo ni Rakaa kumi na tatu.[25]”

300.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي مِنْ اللَّيْلِ ثَلَاثَ عَشْرَةَ رَكْعَةً، يُؤْتِرُ مِنْ ذَلِكَ بِخَمْسٍ، لَا يَجْلِسُ فِي شَيْءٍ إِلَّا فِي آخِرِهَا}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema tena: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiswali Rakaa kumi na tatu usiku, akiswali Witr Rakaa tano kati ya hizo, na hakai popote isipokuwa katika Rakaa ya mwisho.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

301.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {مِنْ كُلِّ اللَّيْلِ قَدْ أُوتِرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَأَنْتَهَى وَثَرُهُ إِلَى السَّحَرِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِمَا

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Katika usiku mzima Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameswali Witr, na Witr yake iliishia wakati wa suhuwr.” (Saa ya mwisho kabla ya Alfajiri)[26] [Al-Bukhaariy, Muslim]

302.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو بْنِ الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يَا عَبْدَ اللَّهِ! لَا تَكُنْ مِثْلَ فُلَانٍ، كَانَ يَقُومُ مِنَ اللَّيْلِ، فَتَرَكَ قِيَامَ اللَّيْلِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amri bin Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliniambia: “Ee ‘Abdullaah! Usiwe kama fulani alikuwa akiswali usiku akaacha kuswali usiku.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

303.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَوْثِرُوا يَا أَهْلَ الْقُرْآنَ، فَإِنَّ اللَّهَ وَثِرٌ يُحِبُّ الْوَثِرَ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Enyi watu wa Qur-aan! Swalini Swalaah ya Witr kwa sababu Allaah ni Witr (Mmoja)[27] na Anapenda Witr.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Khuzayma]

304.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا; عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { اجْعَلُوا آخِرَ صَلَاتِكُمْ بِاللَّيْلِ وَثِرًا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Fanyeni mwisho wa Swalaah zenu usiku ni Witr.”[28] [Al-Bukhaariy, Muslim]

305.

وَعَنْ طَلْقِ بْنِ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {لَا وَثْرَانِ فِي لَيْلَةٍ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالثَّلَاثَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Twalq bin ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) “Nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Hakuna Witr mbili katika usiku mmoja.” [Imetolewa na Ahmad, na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud), na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

306.

وَعَنْ أَبِي بِنِ كَعْبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُوتِرُ بِـ "سَبَّحَ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى"، وَ: "قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ"، وَ: "قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ"} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ. وَزَادَ: {وَلَا يُسَلَّمُ إِلَّا فِي آخِرِهِنَّ} وَلِأَبِي دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيِّ نَحْوُهُ عَنْ عَائِشَةَ وَفِيهِ: {كُلَّ سُورَةٍ فِي رَكْعَةٍ، وَفِي الْآخِرَةِ: "قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ"، وَالْمُعَوَّذَتَيْنِ}

Kutoka kwa Ubayy bin Ka’b[29] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akiswali Witr anasoma Suwrah Al-A’laa[30] katika Rakaa ya kwanza, na Suwrah Al-Kaafiruwn katika Rakaa ya pili na Suwrah Al-Ikhlaasw katika Rakaa ya tatu.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu

Daawuud na An-Nasaaiy] Naye akaongeza: “Wala hatoi Salaam isipokuwa mwishoni.”

Na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy wamepokea Hadiyth kama hiyo kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisoma kila Suwrah moja katika kila Rakaa, na katika Rakaa ya mwisho alikuwa akisoma Al-Ikhlaasw pamoja na Al-Mu’awwidhatayn.[31]”

307.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَوْتِرُوا قَبْلَ أَنْ تُصْبِحُوا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَلِابْنِ حِبَّانَ: {مَنْ أَدْرَكَ الصُّبْحَ وَلَمْ يُوتِرْ فَلَا وَتَرَ لَهُ}

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalini Witr kabla ya Alfajiri.” [Imetolewa na Muslim]

Na Ibn Hibbaan amepokea: “Mwenye kudiriki Alfajiri na hakuiswali Witr, basi hana Witr.”[32]

308.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَنْ نَامَ
عَنِ الْوَيْتْرِ أَوْ نَسِيَهُ فَلْيُصَلِّ إِذَا أَصْبَحَ أَوْ ذَكَرَ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ
إِلَّا النَّسَائِيَّ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema
tena Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:
“Mwenye kulala akakosa Witr au akaisahau, basi na aiswali
asubuhi[33] au hapo atakapokumbuka.” [Imetolewa na Al-Khamsah
(At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-
Nasaaiy]

309.

وَعَنْ جَابِرٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَنْ
خَافَ أَنْ لَا يَقُومَ مِنْ آخِرِ اللَّيْلِ فَلْيُوتِرْ أَوَّلَهُ، وَمَنْ طَمَعَ أَنْ
يَقُومَ آخِرَهُ فَلْيُوتِرْ آخِرَ اللَّيْلِ، فَإِنَّ صَلَاةَ آخِرِ اللَّيْلِ مَشْهُودَةٌ،
وَذَلِكَ أَفْضَلُ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuchelea
kuamka mwishoni mwa usiku, basi aswali Witr mwanzoni mwa
usiku, na mwenye azma ya kuamka mwisho mwa usiku basi aiswali
Witr mwishoni mwa usiku, kwani Swalaah iswaliwayo mwishoni
mwa usiku hushuhudiwa (Na Malaika) nayo ni bora zaidi.”
[Imetolewa na Muslim]

310.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا ، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا طَلَعَ الْفَجْرُ فَقَدْ ذَهَبَ كُلُّ صَلَاةِ اللَّيْلِ وَالْوَتْرِ، فَأَوْتِرُوا قَبْلَ طُلُوعِ الْفَجْرِ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Alfajiri ikichomoza Swalaah zote za usiku pamoja na Witr zimeondoka, basi swalini Witr kabla ya kuchomoza Alfajiri.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy]

311.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي الضُّحَى أَرْبَعًا، وَيَزِيدُ مَا شَاءَ اللَّهُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَلَهُ عَنْهَا: {أَنَّهَا سُئِلَتْ: هَلْ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي الضُّحَى؟ قَالَتْ: لَا، إِلَّا أَنْ يَجِيءَ مِنْ مَغِيبِهِ}

وَلَهُ عَنْهَا: {مَا رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي سُبْحَةَ الضُّحَى قَطُّ، وَإِنِّي لَأَسْبَحُهَا}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiswali Dhwhuhaa Rakaa nne[34] na akizidisha kiasi apendacho Allaah.” [Imetolewa na Muslim]

Katika upokezi wake (Muslim) mwingine: “Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) aliulizwa: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiswali Dhwuhaa? Akasema: “Laa isipokuwa awe kutoka safarini.”

Na katika upokezi wake (Muslim) mwingine: 'Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Sikumuona kamwe Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiswali Dhwuhaa, lakini mimi ninaiswali.”[35]

312.

وَعَنْ زَيْدِ بْنِ أَرْقَمَ: أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {صَلَاةُ الْأَوَّابِينَ حِينَ تَرْمَضُ الْفِصَالُ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Zayd bin Arqam (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimuliwa kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah ya Al-Awwaabiyn (wanaotubia) huswaliwa wakati ndama wa ngamia wanapochomwa na jua.”[36] [Imetolewa na At-Tirmidhiy]

313.

وَعَنْ أَنَسٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ صَلَّى الضُّحَى ثِنْتَيْ عَشْرَةَ رَكْعَةً بَنَى اللَّهُ لَهُ قَصْرًا فِي الْجَنَّةِ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَاسْتَعْرَبَهُ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuswali Rakaa kumi na mbili za Dhwuhaa, Allaah atamjengea nyumba Jannah.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy, na aliipa daraja la Ghaarib (ngeni)]

314.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {دَخَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَيْتِي، فَصَلَّى الضُّحَى ثَمَانِي رَكَعَاتٍ} رَوَاهُ ابْنُ حِبَّانَ فِي "صَحِيحِهِ"

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliingia nyumbani kwangu akaswali Rakaa nane za Dhwuhaa.” [Imetolewa na Ibn Hibbaan katika Swahiyh yake]

[1] Jina la utani la Rabiyy’ah bin Ka’b Al-Aslamiyy ni Abuu Firaas Al-Madaniy. Alikuwa Swahaba alitoka katika Maswahaba wa Suffa. Alikuwa mtumishi wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na alikuwa akimhudumia na kuongozana naye katika safari na nyumbani. Alifariki mnamo mwaka wa 3 A.H.

[2] Hii inatufunza kuwa, iwapo mtu anataka kumkurubia sana Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), ni lazima aswali Swalaah za khiari (Nawaafil) kwa wingi.

[3] Hadiyth hii ina ushahidi kwa watu wale wanaohesabu kwamba kusujudu ni bora kabisa kuliko vitendo vingine vya Swalaah.

[4] Maana ya Hadiyth hii ni kwamba: “Mimi ninaomba kwa Allaah ili Akupe wewe kile unachokitaka, na nitamuomba Yeye Akupe wewe, lakini

kwa kuwa ni kitu kikubwa sana kuomba hicho, basi ni sharti uswali Swalaah nyingi sana za khiari ili du'aa zangu zipate kukubalika.”

[5] Hadiyth hii inatuarifu kuhusu Rakaa nne za Sunnah kabla ya Swalaah ya faradhi wakati wa Adhuhuri. Imetajwa kupitia katika rejea ya ‘Abdullaah bin ‘Umar kuwa kuna Rakaa mbili za kuswaliwa kabla ya Swalaah ya faradhi. Kama ufafanuzi kuhusu hali hii, inasemwa kwamba Rasuli wa Allaah (ﷺ) alikuwa akiswali Rakaa nne kama tendo la kuonyesha unyenyekevu na kufunguliwa kwa milango ya Jannah, na Rakaa mbili za Sunnah Msikitini. Wengine wanasema Rasuli wa Allaah (ﷺ) alikuwa akiswali Rakaa nne nyumbani, na kuhusu Rakaa mbili ambazo alikuwa akiziswali Msikitini, hazikuwa zingine ila ni ile Swalaah ya Tahiyyatul-Masjid (Maamkizi ya Msikiti). Wengine wanasema kwamba, zote mbili zilikuwa ni Sunnah za Swalaah ya Adhuhuri, na kwamba Nabiyy (ﷺ) mara nyingine alikuwa akiziswali Rakaa nne na mara nyingine mbili tu. Zote mbili ni sawa, lakini nne ni bora zaidi kuliko mbili. Hakuna tofauti ya maoni juu ya Rakaa mbili za Swalaah ya Alfajiri, kwa kuwa zinahesabika kuwa ni Sunnah Muakkadah (Sunnah iliyosisitizwa iliyoswaliwa mara kwa mara na Nabiyy (ﷺ)). Imeripotiwa kuwa Nabiyy (ﷺ) alikuwa haziachi hizo hata akiwa safarini, na kwa hivyo ni Waajib kwa msafiri kutoiacha Swalaah ya Witr ya usiku na pia Sunnah ya Swalaah ya Alfajiri.

[6] Ummu Habiyyah anaitwa Ramla bint Abuu Sufyaan ni dada wa Mu’aawiyah. Alisilimu zamani, akahamia Abyssinia, na mumewe ‘Ubaydullaah bin Jahsh alirtadi na akawa Mkristo akafia huko. Kisha Rasuli wa Allaah (ﷺ) alimuoa mnamo mwaka wa 7A.H. wakati yeye Ramla yuko kule, kisha akaja Al-Madiynah pamoja na wahamiaji wa Abyssinia. Alifariki mnamo mwaka wa 42, au 44 au 50 A.H.

[7] Hadiyth hii inatuarifu kuwa, desturi ya Rakaa nne kuswaliwa kabla ya Swalaah ya Alasiri pia ilikuwepo. Endapo mtu yeyote ataziswali hizo, atapata thawabu, lakini asipozswali hana lawama.

[8] ‘Abdullaah bin Mughaffal alikuwa miongoni mwa Aswhaab Ash-Shajara (Waliofanya bay’ah yaaani kula kiapo kuutetea Uislamu dhidi ya Maquraysh kule Hdaybiyah). Aliishi Al-Madiynah na baadae Basra. Alikuwa ni mmoja wa wale watu kumi waliopolekwa na ‘Umar Basra kuwafundisha watu Dini. Alikufa mnamo mwaka wa 60 A.H

[9] Kuna tofauti ya maoni miongoni mwa Wanazuoni kuhusu ubora wa kuswali Rakaa mbili kabla ya Swalaah ya Magharibi. Wale wanaokubali kusihi kwake wanachukua ushahidi kutoka katika Swahiyhayn (Al-Bukhaariy na Muslim). Na wale wanaokanusha wanalinganisha na Hadiyth ya Abuu Daawud kuwa, alipoulizwa ‘Abdullaah bin ‘Umar juu ya hizo Rakaa mbili za kabla ya Swalaah ya Magharibi alisema hakuwahi kumuona yeyote akiziswali Rakaa hizo wakati Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa bado yu hai. Ukweli ni kuwa, usahihi unathibitishwa, lakini zisihesabike kuwa ni Sunnah Muakkadah (Zilosisitizwa), kwa sababu Anas, msimuliaji wa Hadiyth za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisema kuwa: “Kila Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipotuona sisi tunaswali Rakaa hizo, hakutuamrisha sisi kuwa lazima tuwe tukiziswali, wala hakutuamrisha sisi tuache tusiziswali.” Kwa hivyo inaonekana kuwa mtu anaweza kuziswali iwapo tu bado upo muda kabla ya Swalaah ya Jamaa lakini si sawa kuichelewesha Swalaah ya faradhi kwa ajili yake.

[10] Hadiyth hii inatuambia sisi kuwa, kujuzu na usahihi wa Rakaa hizo mbili kabla ya Swalaah ya Magharibi umethibitishwa.

[11] Suwrah Al-Kaafiruwn (109)

[12] Suwrah Al-Ikhlaasw (113)

[13] Kuna tofauti ya maoni juu ya tatizo hili ambalo ni la kipekee. Wengine wanakuhesabu kule kulala chini kuwa ni Waajib (Lazima); wengine wanasema ni Sunnah (khiari), na wapo wanaosema hiyo ni Mustahab (iliyopendekezwa). Kwa mujibu wa maoni ya Imaam Nawawi, ni Sunnah ambayo inaingia akilini pia. Ama ripoti ya Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) kutokuafiki, ni sababu ya kuhusiana na Msikiti. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alilala chini hivyo nyumbani kwake tu. Vitendo vyote viwili vya kuswalia hizo Rakaa mbili Msikitini na akalala chini mle, havijathibitishwa.

[14] An-Nasaaiy anasema kuwa yale maneno ya

صَلَاةُ اللَّيْلِ مَثْنَى مَثْنَى

(Swalaah za usiku ni Rakaa mbili, mbili)

ni sawa, lakini maneno ya

صَلَاةُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ مَثْنَى مَثْنَى

(Swalaah za usiku na za mchana ni Rakaa mbili, mbili) siyo sawa. Yaani kule kuongezwa kwa neno “Wan-nahaar” kunahisabika kuwa ni kwingi mno na kwa hivyo ni makosa, kwa mujibu wa maoni ya Imaam An-Nasaaiy.

[15] Maoni ya Imaam An-Nasaaiy kuhusu usimulizi huo na kukiri kuwa sio sahihi haukubaliki na hauna uthibitisho kwa kuwa Bayhaqiy amekiri kuwa ni sahihi. Tena Imaam Muslim, kwa kunukuu usimulizi wa ‘Aliy bin ‘Abdullaah Bariqi, msimuliaji wa Ahaadiyth za Nabiyy (ﷺ) aliidhinisha kwa hiyo akauthibitisha usahihi wake. Imaam Al-Bukhaariy ameripoti Hadiyth nane kuhusu kadhia hii, na zote zinaiunga mkono. Hata hivyo, bila kujali kuwa Rakaa hizo zitaswaliwa mchana au usiku, ni ubora kuziswali hizo Nawaafil (Swala za khiari, yaani Sunnah) kwa Swalaah za Rakaa mbili mbili, na inaruhusika pia kuziswali kwa Swalaah za Rakaa nne.

[16] Hadiyth hii inatuarifu kwamba kuswali Witr ni lazima. Wale Ahnaaf (Wafuasi wa Imaam Abuu Haniyfah yaani Wahanafi) wanafuata fikra hizo hizo. Maimaam waliobaki na Wanazuoni wengi wengine wanaihesabu Witr kuwa ni Sunnah. Kwa hivyo Hadiyth inayofuata, ambayo ni imara zaidi katika mlolongo wa wapokezi, nayo inaunga mkono.

[17] Kwa mujibu wa ripoti, namba ya Rakaa za Swalaah ya Witr ni kati ya moja na kumi na moja. Wanazuoni wengine hupendelea kuswali Rakaa tatu. Wengi wa Maswahaba wa Nabiyy (ﷺ), wafuasi wao, Imaam Shaafi’, Imaam Ahmad, na Imaam Maalik, wanatambua na wanapendelea Rakaa moja.

[18] Kwa mujibu wa Hadiyth hii, Rasuli wa Allaah (ﷺ) aliswalisha Swalaah ya Taraawiyh katika Jamaa kwa mausiku matatu tu katika maisha yake yote, na kuiswali Swalaah hii kila siku katika mwezi wa Ramadhwaan, kulianzishwa baadaye na Khalifa ‘Umar (رضي الله عنه)

[19] Hadiyth hii inaelezea Swalaah ya Taraawiyh ambayo wingi wa Rakaa zake ni kumi na moja, na Witr nayo wingi wa Rakaa zake ni kumi na moja pia. ‘Aaishah (رضي الله عنها) aliripoti kuwa Nabiyy (ﷺ) hakiswali zaidi ya Rakaa kumi na moja za Witr mnamo mwezi wa Ramadhwaan na katika miezi mingine. ‘Umar (رضي الله عنه)

alimuamrisha ‘Ubay bin Ka’b (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuswalisha Rakaa nane za Taraawiyh. Kwa hivyo inaweza kusemwa kuwa watu walikuwa wakiswali kwa uwingi Rakaa ishirini (20) pia mnamo zama za ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) (ilimradi hii pia ilithibitishwa na mlolongo wa wapokezi). Lakini hakuna Hadiyth Swahiyh inayojulikana chanzo inayothibitisha Rakaa ishirini za Taraawiyh.

[20] Khaarijah bin Hudhaafah ni Qurayshi na ni ‘Adawi ambaye alifananishwa na wapanda farasi elfu moja. ‘Amr bin Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuomba ‘Umar bin Al-Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ), ampelekee wapanda farasi elfu tatu, lakini yeye akampelekea watu watatu tu, nao ni Az-Zubayr bin Al-‘Awwaam, Al-Miqdaad bin Al-Aswad, na Khaarijah. Alikuwa Qadhi kule Misri kwa ‘Amr bin Al-‘Aasw na akauliwa kule mnamo Ramadhwaan mwaka 40 A.H, na mmoja wa Khawaarij aliyemdhania kuwa yeye ndiye ‘Amr bin Al-‘Aasw. Hii ilikuwa wakati ule wale Makhawaarij walipokula njama ya kuwaua ‘Amr, ‘Aliy na Mu’aawiyah.

[21] Kwa mujibu wa Hadiyth hii, wakati wa ‘Ishaa ni kutokea wakati wa Swalaah ya ‘Ishaa mpaka wakati wa dalili za kwanza za Alfajiri. Wakati wake mzuri ni usiku zaidi; lakini iwapo mtu hatokuwa na hakika kuwa atawahi kuamka toka usingizini, basi ni ubora aiswali Witr mara baada ya kuiswali ‘Ishaa.

[22] ‘Amr huyu ndiye Abuu Ibraahiym ‘Amr bin Shu’ayb bin ‘Abdillaah bin ‘Amr bin Al-‘Aasw As-Sahmiy Al-Qurayshiy Al-Madaniy, aliyelowea Twaaf. An-Nasaaiy alimthibitisha kuwa ni wa kutegemewa. Alikufa mnamo mwaka 118 A.H.

[23] Shu’ayb alikuwa mmoja wa Taabi’iyn wa kutegemewa. Inasemekana kuwa babake Muhammad alikufa zama za utoto wake; kwa hivyo babu yake ‘Abdullaah bin ‘Amr yule Swahaba maarufu ndiye alimlea. Na imethibitika kuwa yeye aliisikia hasa hii Hadiyth kutoka kwake. Kwa hiyo hii siyo Munqatwi’ wala siyo Mursal, bali ni Mutwassil ambayo haiendi chini ya daraja la Hassan.

[24] ‘Abdullaah bin Buraydah ndiye Abuu Sahl, Qadhi wa Marw, ambaye alikuwa ni mmoja wa Taabi’iyn wa daraja la tatu wa kutegemewa sana na maarufu kabisa. Alifia Marw mnamo mwaka wa 115 A.H.

[25] Kuna tofauti ya maoni iwapo Swalaah ya Tahajjud (Swalaah ya usiku wa manane) ina Rakaa kumi na moja au kumi na tatu. Kumi na moja

zimeafikiwa, lakini kumi na tatu zina mtafaruku. Ukweli ni kwamba, Nabiyy (ﷺ) wakati mwingine aliswali kumi na moja za Tahajjud kujumlisha na Witr na wakati mwingine kumi na tatu.

[26] Suwhur inajulikana pia ni kula daku.

[27] Inamaanisha Sifa za Allaah, yaani Yeye ni wa Kipekee, na “Hakuna chochote kinachofanana na Yeye”

[28] Kwa mujibu wa simulizi zingine, Nabiyy (ﷺ) alikuwa akiswali Rakaa mbili za Sunnah (Naafil) baada ya Swalaah ya Witr kwa hivyo amesamehewa. Wengine wanasema kuwa mtu ni bora aswali Rakaa mbili za Swalaah ya Sunnah katika sehemu ya mwisho ya usiku, akiwa ameshaswali Swalaah ya Witr sehemu ya mwanzo ya usiku. Endapo ataswali Witr katika sehemu ya mwisho ya usiku, basi hana haja ya kuswali hiyo Swalaah ya Sunnah.

[29] Ubayy bin Ka'b ni Answaar, na ni Khazraj, alipewa jina la utani la Abu Al-Mundhir. Alikuwa ndiye Sayyid wa Wanazuoni wa Qur-aan na alikuwa mmoja wa waandishi wa Wahy. Na alikuwa pia mmoja wa watu walioikusanya Qur-aan na alitoa Fatwa (uamuzi wa kisheria) zama za uhai wa Rasuli wa Allaah (ﷺ). Alishiriki katika vita vya 'Aqabah, Badr na vita vilivyofuatia hivi. Mwaka wa kufa kwake kumetofautiana; wengine wakisema alikufa mnamo mwaka wa 19, au 20, au 22, au 30, au 32, au 33 A.H

[30] Suwrah Al-A'laa (87).

[31] Suwrah za Al-Mu'awwidhatayn ni: Al-Falaq (113) na An-Naas (114).

[32] Hadiyth hii inatuambia kuwa wakati wa Witr unakwisha kunapopambazuka; na Hadiyth hii inamaanisha kuwa Witr anayoiswali mtu huku wakati huo umepita basi inakuwa haikuswaliwa kwa mujibu wa Sunnah ya Rasuli wa Allaah (ﷺ). Haimaanishi kuwa iwapo mtu hakuwahi kuswali Witr kabla ya Alfajiri basi asiiswali kabisa. Tukio moja linalowahusu Maswahaba linasimuliwa na Hadiyth isemayo kwamba, wakati fulani alilala na akachelewa kuamka. Akamtuma Mtumwa wake akaone kama Swalaah ya Jamaa imekwisha kuswaliwa; na Mtumwa akarejea na kumjibu kuwa imekwisha kuswaliwa. Baada ya kuambiwa hivi, aliswali hiyo Witr kwanza, kisha Sunnah na kisha akaiswali Swalaah ya faradhi ya Alfajiri. Kwa hivyo inaeleweka kwamba, mtu asipowahi kuswali Witr katika wakati wake, ni lazima aiswali kama

kadhaa baadaye. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisisitiza kuwa Witr ni lazima iswaliwe katika wakati wake bila kukosa. Na aliagiza kuwa kwa wale waliokuwa na shaka ya kuwahi kuamka kuiswali, basi waiswali usiku (kabla hawajalala). Kwa hivyo akamuamrisha Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) aswali Witr usiku.

[33] Ieleweke kwamba, mtu akiikosa Swalaah kwa sababu ya kusahau au usingizi, hatotiwa hatiani na atapata thawabu na kama aliiswali Swalaah ile kwa wakati wake; lakini imekatazwa kwenda kulala wakati ambao unakaribia Swalaah fulani. Itokeapo kwamba hili linatokea kwa bahati mbaya na kwa hali ambayo yeye hawezi kuiepuka, basi hatolaumiwa.

[34] Ifahamike kwamba Ishraaq, Swalaatul-Awwaabiyn, na Dhwhuhaa ni majina tofauti yanayomaanisha Swalaah zile zile za kabla ya Swalaah ya Adhuhuri. Wakati wa Swalaah hiyo ni mara baada ya kuchomoza jua na huendelea hadi robo moja ya mchana. Idadi ya chini kabisa ya Rakaa za Dhwhuhaa ni Rakaa mbili, na idadi ya juu kabisa ni Rakaa kumi na mbili. Inayopendelewa ni Rakaa nne, ambayo inaungwa mkono na Hadiyth za Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Ikumbukwe pia kuwa Swalaah hii ni Sunnah ya Manabiy waliotangulia kwa vile walikuwa wakiziswali hizo katika zama zao. Kwa hivyo Swalaah hii ni Sunnah na Mustahabb (inayopendekezwa). Ama ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuiita Swalaah hii ni Bid’ah (uzushi), inamaanisha tu kuwa ikiwa mtu atazowea kuiswali hiyo kila siku zote, yaweza kuhesabika ni Bid’ah kwa kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakuiswali siku zote.

[35] Ingawa Hadiyth hii na hizo mbili zilizoitangulia zinaonekana kupingana, zinaonyesha tu kuwa Swalaah ya Dhwhuhaa ni Swalaah ya khiari kama inavyohibitishwa na Wanazuoni wa Hadiyth.

[36] Hadiyth hii inaonyesha kuwa wakati mzuri kuliko wote wa Swalaah ya Dhwhuhaa ni kabla tu ya saa sita mchana.

10- Mlango Wa Swalaah Ya Jamaa Na Uimaamu

بَابُ صَلَاةِ الْجَمَاعَةِ وَالْإِمَامَةِ

10- Mlango Wa Swalaah Ya Jamaa Na Uimaamu1

315.

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا; أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {صَلَاةُ الْجَمَاعَةِ أَفْضَلُ مِنْ صَلَاةِ الْفَذِّ بِسَبْعٍ وَعِشْرِينَ دَرَجَةً} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلَهُمَا عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ: {بِخَمْسٍ وَعِشْرِينَ جُزْءًا} وَكَذَا لِلْبُخَارِيِّ: عَنْ أَبِي سَعِيدٍ، وَقَالَ: "دَرَجَةً"

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah ya Jamaa ina fadhila zaidi kuliko ya peke yake kwa daraja ishirini na saba[1].” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Nao (Al-Bukhaariy na Muslim) tena wamepokea Hadiyth ya Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Kwa mafungu ishirini na tano.”

Kadhalika Al-Bukhaariy amepokea Hadiyth ya Abuu Sa’iyyd Al-Khudriyy, amesema: “...daraja...”

316.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَقَدْ هَمَمْتُ أَنْ أَمُرَّ بِحَطَبٍ فَيُحْتَطَبَ، ثُمَّ أَمُرَ بِالصَّلَاةِ فَيُؤَذَّنَ لَهَا، ثُمَّ أَمُرَ رَجُلًا فَيُؤَمِّمَ النَّاسَ، ثُمَّ أَخَالَفُ إِلَى رَجَالٍ لَا يَشْهَدُونَ الصَّلَاةَ، فَأُحَرِّقَ عَلَيْهِمْ بُيُوتَهُمْ، وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوْ يَعْلَمُ أَحَدُهُمْ أَنَّهُ يَجِدُ عَرَقًا سَمِينًا أَوْ مَرْمَاتَيْنِ حَسَنَتَيْنِ لَشَهِدَ الْعِشَاءَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Naapa kwa Ambaye nafsi yangu imo Mkononi Mwake, nimetamani kuamuru kukusanywa kuni, kisha kuamrisha kwa Swalaah kuadhiniwe, kisha nimuamrishe mtu mmoja aongoze watu, kisha niwaendee watu wasiohudhuria Swalaah nichome[2] nyumba zao. Naapa kwa Ambaye Nafsi yangu ipo Mkononi Mwake, angejua mmoja wao atapata mfupa ulionona au miguu mizuri ya kondoo angehudhuria Swalaah ya ‘Ishaa.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

317.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَثْقَلُ الصَّلَاةِ عَلَى الْمُنَافِقِينَ: صَلَاةُ الْعِشَاءِ، وَصَلَاةُ الْفَجْرِ، وَلَوْ يَعْلَمُونَ مَا فِيهِمَا لَأَتَوْهُمَا وَلَوْ حَبَوًّا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) tena amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah nzito zaidi kwa wanafiki[3] ni ‘Ishaa na Alfajiri, na laiti wangelijua yaliyomo humo, wangeziendea, hata kwa kutambaa kwa magoti.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

318.

وَعَنْهُ قَالَ: { أَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَجُلٌ أَعْمَى فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! لَيْسَ لِي قَائِدٌ يَقُودُنِي إِلَى الْمَسْجِدِ، فَرَخَّصْ لَهُ، فَلَمَّا وَلَّى دَعَاهُ، فَقَالَ: "هَلْ تَسْمَعُ النِّدَاءَ بِالصَّلَاةِ؟" قَالَ: نَعَمْ. قَالَ: "فَاجِبٌ" { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena: “Mtu kipofu[4] alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Mimi sina mwongozaji anayeniongoza Msikitini. Na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akamruhusu (kuswali nyumbani). Kisha mtu yule alipogeuka kwenda zake Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuuliza: “Je, unaisikia Adhana?” Akasema: “Ndiyo.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Basi itikia.” [Imetolewa na Muslim]

319.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ سَمِعَ النِّدَاءَ فَلَمْ يَأْتِ فَلَا صَلَاةَ لَهُ إِلَّا مِنْ عُذْرٍ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ، وَإِسْنَادُهُ عَلَى شَرْطِ مُسْلِمٍ، لَكِنْ رَجَّحَ بَعْضُهُمْ وَقْفَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kusikia[5] Adhana asije, hana Swalaah isipokuwa kwa udhuru.” [Imetolewa na Ibn Maajah, Ad-Daaraqutwniy, Ibn Hibbaan na Al-Haakim. Isnaad yake ni kwa sharti la Muslim, lakini baadhi ya wapokezi wa Hadiyth waliipa daraja la Mawquwf]

320.

وَعَنْ يَزِيدَ بْنِ الْأَسْوَدِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ صَلَّى مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَاةَ الصُّبْحِ، فَلَمَّا صَلَّى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا هُوَ بِرَجُلَيْنِ لَمْ يُصَلِّيَا، فَدَعَا بِهِمَا، فَجِئَا بِهِمَا تَرَعْدُ فَرَأَيْتُهُمَا، فَقَالَ لَهُمَا: "مَا مَنَعَكُمَا أَنْ تُصَلِّيَا مَعَنَا؟" قَالَا: قَدْ صَلَّيْنَا فِي رَحَالِنَا. قَالَ: "فَلَا تَفْعَلَا، إِذَا صَلَّيْتُمَا فِي رَحَالِكُمَا، ثُمَّ أَدْرَكْتُمُ الْإِمَامَ وَلَمْ يُصَلِّ، فَصَلِّيَا مَعَهُ، فَإِنَّهَا لَكُمْ نَافِلَةٌ" رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَاللَّفْظُ لَهُ، وَالثَّلَاثَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Yaziyd bin Al-Aswad[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alisema kuwa: “Yeye aliswali Swalaah ya Fajr pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ), Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipomaliza kuswali, aliwaona watu wawili ambao hawakuswali pamoja naye. Akaamrisha waletwe, na wakaletwa huku wakitetemeka[7] (kwa uoga). Akawauliza: “Jambo gani lilowazuia msiswali pamoja nasi?” Wakasema: “Tumeswali majumbani mwetu.” Akasema: “Msifanye hivyo, mkiswali majumbani mwenu, kisha mkaja Msikitini wakati Imaam hajamaliza kuswalisha watu, swalini pamoja naye, na hiyo itakuwa ni Swalaah ya Sunnah kwenu.” [Imetolewa na Ahmad, na tamshi hili ni lake, na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd) na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

321.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّمَا جُعِلَ الْإِمَامُ لِيُؤْتَمَّ بِهِ، فَإِذَا كَبَّرَ فَكَبِّرُوا، وَلَا تُكَبِّرُوا حَتَّى يُكَبِّرَ، وَإِذَا رَكَعَ فَارْكَعُوا، وَلَا تَرْكَعُوا حَتَّى يَرْكَعَ، وَإِذَا قَالَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ، فَقُولُوا: اللَّهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ، وَإِذَا سَجَدَ فَاسْجُدُوا، وَلَا تَسْجُدُوا حَتَّى يَسْجُدَ، وَإِذَا صَلَّى قَائِمًا فَصَلُّوا قِيَامًا، وَإِذَا صَلَّى قَاعِدًا فَصَلُّوا قُعُودًا أَجْمَعِينَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَهَذَا لَفْظُهُ وَأَصْلُهُ فِي الصَّحِيحَيْنِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Imaam

amefanywa ili afuatwe, kwa hivyo akipiga Takbiyra nanyi pigeni, lakini nyie msipige Takbiyra hadi yeye apige. Na akirukuu nanyi mrukuu, wala msirukuu hadi amerukuu. Imaam akisema:

سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ

“Sami’a-Allaahu liman hamidah” (Allaah Amemsikia aliyemhimidi),

Semeni:

اللَّهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ

“Allaahumma Rabbanaa Lakal-Hamd.” (Ee Allaah! Rabb wetu, ni Zako Wewe Himd).

Na akisujudu, nanyi msujudu, wala msisujudu hadi amesujudu. Akiswali akiwa amesimama nanyi simameni, na akiswali huku amekaa, nanyi swalini huku mmekaa.[8]” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na hili ni tamshi lake, na chanzo chake kimo katika Swahiyhayn (Al-Bukhaariy na Muslim)]

322.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {رَأَى فِي أَصْحَابِهِ تَأْخُرًا. فَقَالَ: "تَقَدَّمُوا فَأَتَمُّوا بِي، وَلْيَأْتَمَّ بِكُمْ مَنْ بَعْدَكُمْ"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipoona Maswahaba zake wanachelewa, alisema: “Njooni mbele na

mnifuata, na wale wa nyuma wawafuate nyinyi.”[9] [Imetolewa na Muslim]

323.

وَعَنْ زَيْدِ بْنِ ثَابِتٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {اِحْتَجَرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حُجْرَةً بِخَصْفَةٍ، فَصَلَّى فِيهَا، فَتَتَبَعَ إِلَيْهِ رَجَالٌ، وَجَاءُوا يُصَلُّونَ بِصَلَاتِهِ...} الْحَدِيثُ، وَفِيهِ: {أَفْضَلُ صَلَاةِ الْمَرْءِ فِي بَيْتِهِ إِلَّا الْمَكْتُوبَةُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Zayd bin Thaabit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitengeneza mswala akaswali ndani yake. Watu wakamfuata na wakawa wanaswali nyuma yake...”[10] Msimuliaji aliitaja Hadiyth yote na ina maneno: “Swalaah bora ya mtu ni (anayoiswali) nyumbani kwake isipokuwa Swalaah ya faradhi.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

324.

وَعَنْ جَابِرٍ قَالَ: {صَلَّى مُعَاذُ بِأَصْحَابِهِ الْعِشَاءَ، فَطَوَّلَ عَلَيْهِمْ، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: "أَتُرِيدُ أَنْ تَكُونَ يَا مُعَاذُ فَتَنَانًا؟ إِذَا أَمَمْتَ النَّاسَ فَاقْرَأْ: بِالشَّمْسِ وَضُحَاهَا، وَ: سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى، وَ: اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ، وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mu’aadh aliwaswalisha Maswahaba wenziwe Swalaah ya ‘Ishaa na akawarefushia Swalaah. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Ee Mu’aadh! Unataka uwe Fattaan[11]? Ukiswalisha watu[12] soma:

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا [13]

na

سَبَّحَ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى [14]

na

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ [15]

na

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى [16]

[Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim[17]]

325.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا فِي قِصَّةِ صَلَاةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِالنَّاسِ، وَهُوَ مَرِيضٌ قَالَتْ: {فَجَاءَ حَتَّى جَلَسَ عَنْ يَسَارِ أَبِي بَكْرٍ، فَكَانَ يُصَلِّي بِالنَّاسِ جَالِسًا وَأَبُو بَكْرٍ قَائِمًا، يَقْتَدِي أَبُو بَكْرٍ بِصَلَاةِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَيَقْتَدِي النَّاسُ بِصَلَاةِ أَبِي بَكْرٍ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuhusu Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuswalisha watu wakati

akiwa mgonjwa. Amesema: “Alikuwa na akaketi upande wa kushoto wa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ). Akawa anaswalisha watu huku amekaa na Abuu Bakr amesimama. Abuu Bakr alikuwa anamfuata Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na watu wanafuata Swalaah ya Abuu Bakr.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

326.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا أَمَّ أَحَدُكُمْ النَّاسَ فَلْيُخَفِّفْ، فَإِنَّ فِيهِمُ الصَّغِيرَ وَالْكَبِيرَ وَالضَّعِيفَ وَذَا الْحَاجَةِ، فَإِذَا صَلَّى وَحْدَهُ فَلْيُصَلِّ كَيْفَ شَاءَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu atakaposwalisha watu, afupishe, kwani miongoni mwao wapo watoto, wazee, wadhooфу, na wenye shida. Lakini akiwa anaswali peke yake, na aswali kadiri anavyotaka.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

327.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ سَلَمَةَ قَالَ: قَالَ أَبِي: {جِئْتُكُمْ مِنْ عِنْدِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حَقًّا. قَالَ: "فَإِذَا حَضَرْتَ الصَّلَاةَ فَلْيُؤَذِّنْ أَحَدُكُمْ، وَلْيُؤَمِّكُمْ أَكْثَرُكُمْ قُرْآنًا"، قَالَ: فَانْظَرُوا فَلَمْ

يَكُنْ أَحَدُ أَكْثَرَ قُرْآنًا مِنِّي، فَقَدَّمُونِي، وَأَنَا ابْنُ سِتٍّ أَوْ سَبْعِ
سِنِينَ { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ

Kutoka kwa ‘Amr bin Salamah[18] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
Baba yangu amesema: “Nimekuleteeni haki kutoka kwa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kwa hivyo wakati wa Swalaah
ukiwadia, mmoja wenu aadhini, na mmoja wenu na aliye hifadhi Qur-
aan kuliko wote awe Imaam.” ‘Amr akaendelea kusema:
Wakaangalia lakini hakuwepo mtu aliyejua Qur-aan kuliko mimi.
[19]. Wakanitanguliza nami nikiwa na umri wa miaka sita au saba tu.
”[20] [Imetolewa na Al-Bukhaariy, Abuu Daawuud na An-Nasaaiy]

328.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يَوْمُ الْقَوْمِ أَقْرَوْهُمْ لِكِتَابِ اللَّهِ، فَإِنْ كَانُوا فِي
الْقِرَاءَةِ سَوَاءً فَأَعْلَمُهُمُ بِالسُّنَّةِ، فَإِنْ كَانُوا فِي السُّنَّةِ سَوَاءً
فَأَقْدَمُهُمْ هِجْرَةً، فَإِنْ كَانُوا فِي الْهِجْرَةِ سَوَاءً فَأَقْدَمُهُمْ سِلْمًا
وَفِي رِوَايَةٍ: سِنًا وَلَا يَوْمَنَّ الرَّجُلُ. الرَّجُلُ فِي سُلْطَانِهِ، وَلَا
يَقْعُدُ فِي بَيْتِهِ عَلَى تَكْرِمَتِهِ إِلَّا بِإِذْنِهِ". { رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَلَاِبْنُ مَاجَةَ: مِنْ حَدِيثِ جَابِرٍ: {وَلَا تَوْمَنَّ امْرَأَةٌ رَجُلًا، وَلَا
أَعْرَابِيٌّ مُهَاجِرًا، وَلَا فَاجِرٌ مُؤْمِنًا. { وَإِسْنَادُهُ وَاه

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uud (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa:
“Anaswalisha watu msomaji wao zaidi wa Qur-aan. Ikiwa wako
sawa katika usomaji, basi anayejua Sunnah zaidi, na ikiwa wako

sawa katika Sunnah basi mtu aliyetangulia Hijrah[21], na kama wako sawa katika uhamiaji basi aliyetangulia kusilimu.”

Na katika mapokezi mengine: “Kwa umri.” Na mtu asiswalishe mtu aliyekaa katika milki yake au asikae nyumbani kwa mwenyeji wake penye nafasi ya heshima isipokuwa kwa ruhusa yake.” [Imetolewa na Muslim]

Na Ibn Maajah amepokea kutokana na Hadiyth ya Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Mwanamke asimswalishe kamwe mwanamume, wala Bedui (Mwarabu wa jangwani) asimswalishe mhamiaji, na muovu asimswalishe Muumini.” [Isnaad yake ni Waahin (Dhaifu sana)]

329.

وَعَنْ أَنَسٍ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {رُصُّوا صُفُوفَكُمْ، وَقَارِبُوا بَيْنَهَا، وَحَاذُوا بِالْأَعْنَاقِ}. {رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Pangeni safu zenu na karibieni baina yake[22], na muwe shingo kwa shingo.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

330.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { خَيْرُ صُفُوفِ الرِّجَالِ أَوَّلُهَا، وَشَرُّهَا آخِرُهَا، وَخَيْرُ صُفُوفِ النِّسَاءِ آخِرُهَا، وَشَرُّهَا أَوَّلُهَا } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Safu bora kwa wanaume ni ya kwanza, na mbaya zaidi ni ya mwisho; na kwa mwanamke safu bora zaidi ni ya mwisho na mbaya zaidi ni ya mwanzo.” [Imetolewa na Muslim]

331.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { صَلَّيْتُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ذَاتَ لَيْلَةٍ، فَقُمْتُ عَنْ يَسَارِهِ، فَأَخَذَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِرَأْسِي مِنْ وَرَائِي، فَجَعَلَنِي عَنْ يَمِينِهِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Niliswali pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) usiku mmoja, nikasimama kushoto kwake, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akanishika kisogoni[23] na akaniweka upande wake wa kulia.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

332.

وَعَنْ أَنَسٍ قَالَ: {صَلَّى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
فَقُمْتُ وَيَتِيمٌ خَلْفَهُ، وَأُمُّ سُلَيْمٍ خَلْفَنَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ
لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali nikasimama mimi na yatima[24] nyuma yake, na Ummu Sulaym nyuma yetu[25].” [Al-Bukhaariy, Muslim, na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

333.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ انْتَهَى إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَهُوَ رَاكِعٌ، فَرَكَعَ قَبْلَ أَنْ يَصِلَ إِلَى الصَّفِّ،
فَقَالَ لَهُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَادَكَ اللَّهُ حِرْصًا. وَلَا
تَعُدْ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَزَادَ أَبُو دَاوُدَ فِيهِ: {فَرَكَعَ دُونَ الصَّفِّ، ثُمَّ مَشَى إِلَى
الصَّفِّ}

Kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwamba alikwenda kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiwa anarukuu. Akarukuu kabla hajakuta safu. Akamtajia hayo Nabiyy , (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hapo akamuambia: “Allaah Akuongezee himma, lakini usirudie.[26]” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na Abuu Daawud akaongezea: “Alirukuu kabla hata ya kuifikia safu, kisha akatembea hadi kwenye safu.”

334.

وَعَنْ وَابِصَةَ بْنِ مَعْبَدٍ الْجُهَنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {رَأَى رَجُلًا يُصَلِّي خَلْفَ الصَّفِّ وَخَذَهُ، فَأَمَرَهُ أَنْ يُعِيدَ الصَّلَاةَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَلَهُ عَنْ طَلْقٍ {لَا صَلَاةَ لِمُنْفَرِدٍ خَلْفَ الصَّفِّ} وَزَادَ الطَّبْرَانِيُّ مِنْ حَدِيثِ وَابِصَةَ: {أَلَا دَخَلْتَ مَعَهُمْ أَوْ اجْتَرَرْتَ رَجُلًا؟}

Kutoka kwa Waabiswah bin Ma'bad[27] Al-Juhaniyy (رَضِيَ اللَّهُ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuona mtu mmoja anaswali peke yake nyuma ya safu, na akamuamrisha arudie kuswali.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuwd, na At-Tirmidhiy naye akaipa daraja la Hasan, Ibn Hibbaan akaipa daraja la Swahiyh]

Naye (Ibn Hibbaan) amepokea Hadiyth ya Twalq bin ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Hakuna Swalaah ya mtu peke yake nyuma ya safu.[28]”

Na akaongezea Atw-Twabaraaniyy kwenye usimulizi wa Waabiswah: “Kwa nini hukujiunga nao au kumvuta mtu (ajiunge nawe?).”

335.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا سَمِعْتُمُ الْإِقَامَةَ فَامْشُوا إِلَى الصَّلَاةِ، وَعَلَيْكُمْ السَّكِينَةُ وَالْوَقَارُ، وَلَا تُسْرِعُوا، فَمَا أَدْرَكْتُمْ فَصَلُّوا، وَمَا فَاتَكُمْ فَأَتِمُّوا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkisikia Iqaamah, nendeni kuswali kwa utulivu na taadhima, na msifanye haraka, na swalini sehemu yoyote ya Swalaah mtakayoiwahi[29], kisha timizeni sehemu iliyokupiteni.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

336.

وَعَنْ أَبِي بِنِ كَعْبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {صَلَاةُ الرَّجُلِ مَعَ الرَّجُلِ أَزْكَى مِنْ صَلَاتِهِ وَحْدَهُ، وَصَلَاتُهُ مَعَ الرَّجُلَيْنِ أَزْكَى مِنْ صَلَاتِهِ مَعَ الرَّجُلِ، وَمَا كَانَ أَكْثَرَ فَهُوَ أَحَبُّ إِلَى اللَّهِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Ubayy bin Ka’b (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah ya mtu anayoiswali pamoja na mtu mwingine ni bora zaidi kuliko anayoswali peke yake. Na Swalaah ya mtu anaiswali pamoja na watu wawili ni bora zaidi kuliko anayoswali na mtu mmoja; na Swalaah inapokuwa na watu wengi zaidi humpendeza zaidi Allaah (عَزَّ

وجل” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

337.

وَعَنْ أُمِّ وَرَقَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَمَرَهَا أَنْ تَوُمَّ أَهْلَ دَارِهَا } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Ummu Waraqah[30] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuamrisha Ummu Waraqah awaswalishe watu wa nyumba yake.”[31] [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

338.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ؛ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ اسْتَخْلَفَ ابْنَ أُمِّ مَكْتُومٍ، يَوْمَ النَّاسِ، وَهُوَ أَعْمَى } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ وَنَحْوُهُ لِابْنِ حِبَّانَ: عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimteua Ibn Ummu Maktuwm (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) aswalishe, alipokuwa hayupo, naye (Ibn Ummu Maktuwm) alikuwa kipofu.[32]” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud]

Ibn Hibbaan pia amepokea Hadiyth kama hiyo, kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا)

339.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { صَلُّوا عَلَيَّ مَنْ قَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَصَلُّوا خَلْفَ مَنْ قَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ } رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mswalieni mtu aliyetamka (aliyesilimu) Laa ilaaha illa Allaah (hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah) na swalini nyuma ya mtu aliyesema: Laa ilaaha illa Allaah.”[33] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy kwa Isnaad dhaifu]

340.

وَعَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا أَتَى أَحَدُكُمْ الصَّلَاةَ وَالْإِمَامُ عَلَى حَالٍ، فَلْيَصْنَعْ كَمَا يَصْنَعُ الْإِمَامُ } رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akiingia katika Swalaah, na Imaam yuko katika kitendo fulani, basi afanye anavyofanya Imaam.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy kwa Isnaad dhaifu]

[1] Katika simulizi zinazofuata, thawabu zimeripotiwa kuwa ni kubwa mara ishirini na tano. Inategemeana na hali ya huyo anayeswali. Mtu mwenye hadhi ya juu hupata mara ishirini na saba zaidi, na yule mwenye hadhi ya chini hupata mara ishirini na tano tu zaidi.

[2] Tunaarifiwa katika Hadiyth hii kwamba, kuswali katika jamaa ni *Fardhw 'Ayn* (wajibu wa binafsi). Ingelikuwa ni *Fardhw Kifaaya* (wajibu wa wengi) au Sunnah Muakkadah (iliyosisitizwa), Nabiyy (ﷺ) asingetumia maneno makali vile kwa watu wasiohudhuria Swalaah za Jamaa.

[3] Neno hilo “unafiki” hapa limetumika kuhusu unafiki wa matendo na siyo unafiki wa uaminifu, kwani mnafiki ni mtu asiyeamini moyoni mwake, na huenda Msikitini kwa ajili ya kujionyesha tu kwa watu.

[4] Mtu huyo asiyeona hakuwa mwengine bali ni ‘Abdullaah bin Ummi Maktuwm. Baada ya amri hiyo ya Nabiyy (ﷺ) alikuwa akienda kuswali Msikitini kila mara hadi akateuliwa kuwa Muadhini. Kwa kuwa hata walemavu wanaamrisha wahudhurie Swalaah ya Jamaa Msikitini, je wale wasiohudhuria Swalaah za jamaa bila kisingizio chochote? Swalaah ya mlemavu inakubalika iswaliwe nyumbani, lakini yeye pia hazipati thawabu za jamaa.

[5] Hadiyth hii inadhihirisha kwamba, ni waajib kwa kwa anayesikia Adhana kuitikia kwa kuwenda kuswali Jamaa Msikitini. Hakuna kisingizio cha kutokwenda kuswali jamaa madamu tu kasikia Adhana. Miongoni mwa nyudhuru zinazokubalika mtu asiende Msikitini kuswali Jamaa, ni kimbunga, mvua, njaa kali sana, kwenda haja kubwa, kukojoa, kuugua maradhi n.k.

[6] Yaziyd bin Al-Aswad ndiye Jaabir As-Sawaaiy Al-‘Aamiriy, ambaye alikuwa sahiba wa Maquraysh. Alikuwa ni Swahaba aliyeishi Twaaif, na hii ndiyo Hadiyth pekee kutoka kwake kupitia kwa mwanawe Jaabir.

[7] Miili yao ilianza kusiimka kwa sababu ya woga kutokana na haiba ya Nabiyy (ﷺ), kama ambavyo hutokea kwa sababu ya mshituko wa woga.

[8] Shariy'ah hii sasa imefutwa. Nabiyy (ﷺ) aliswalisha watu huku kaketi chini kwa sababu ya maradhi yake (ambayo ndiyo yaliyomuua), ambapo Maamuma (wafuasi) wake waliswali huku wamesimama wima kama ilivyo kawaida.

[9] Hadiyth hii inaweza kunukuliwa kuwa ndiyo ushahidi wa Maamuma ambao wanaweza kumuona Imaam lakini hawawezi kumsikia. Maamuma kama hao lazima wafuate Maamuma mwingine walio mbele yao. Pia inatufundisha kuwa msitari wa mbele kabisa ndiyo mbora, na mtu sharti afuate kuujaza huo kwanza ikiwezekana, na kwamba msitari wa pili usiwe mbali na msitari wa kwanza, na halikadhalika msitari wa kwanza usiwe mbali na Imaam.

[10] Hadiyth hii inaonyesha kuwa, ikiwa upo ukuta au kitenganisho au umbali fulani kati ya Imaam na Maamuma, Swalaah itabakia kuwa halali. Watu wengine hawaafiki maneno yote ya Hadiyth hii, lakini usahihi wake unatosha kuwashawishi watu hao.

[11] Inamaanisha: “Kwa kukirefusha kisomo unataka kuwatesa watu unaowaswalisha, na kwa hivyo unawakatisha tamaa wasiwe wanahudhuria Swalaah za Jamaa?”

[12] Hadiyth hii inatufundisha kwamba, Imaam asirefushe kisomo chake ndani ya Swalaah asiwakere Maamuma wake, wasije kuiepuka Swalaah ya Jamaa. Hadiyth nyingine inayoifuatia hii inatoa sababu za kutorefusha kisomo, lakini pia kisifupishwe kwa kiasi cha Maamuma kushindwa hata kukamilisha kisomo chake au Swalaah yake. Njia iliyo sahihi ni kuswalisha kwa namna ya wastani kwa mujibu wa Sunnah ya Nabiyy (ﷺ)

[13] [Ash-Sams (91)]

[14] [Al-A'laa (87)]

[15] [Al-'Alaq (96)]

[16] [Al-Layl: (92)]

[17] Hadiyth nyingine inaripoti kwamba, Mu'aadh alikuwa kwanza anaswali nyuma ya Nabiyy (ﷺ), kisha anaswali Nafl (Swalaah ya khiari, ya Sunnah), na kisha alikuwa anakwenda kuswalisha katika Msikiti mwingine. Hii inaonyesha kuwa, mtu anaweza kuswali

Swalaah yake ya faradhi nyuma ya Imaam anayeswali Swalaah yake ya Nafl.

[18] ‘Amr bin Salamah ndiye Abu Yazid au Abuu Burayd. Alikuwa na baba yake kwa Rasuli wa Allaah (ﷺ). Inasemekana pia kuwa hakuja na baba yake. Alikuwa katika kabila la Jarum, na akawa anaishi Basra.

[19] Hadiyth hii inaeleza kuwa, mtu anayestahili zaidi kuliko wengine wote kuwa Imaam ni yule anayejua **Shari’a** zaidi kuliko wote. Ikiwa watu wawili wana ujuzi sawa, yule ambaye ni mwenye taqwa zaidi ndiye awe Imaam. Vigezo hivyo pia vimetajwa katika usimulizi wa Ibn Mas-‘uwd.

[20] Hadiyth hii inaonyesha kuwa mtoto ambaye bado hajabaleghe anaweza kumswalisha mtu mkubwa au kundi la watu wakubwa iwapo anatokezea kuwa mjuzi zaidi kuliko wale wakubwa kwenye mambo ya **Shariy’ah**.

[21] Nabiyy (ﷺ) na Maswahaba walipohamia Madiynah kutoka Makkah.

[22] Imeripotiwa katika Swahiyh mbili kuwa Nabiyy (ﷺ) aliwakhutubia watu huku uso wake umewaelekea wao, na akawaamrisha wanyooshe safu (misitari) zao vinginevyo Allaah (عز وجل) Atafanya kutopatana ndani ya nyoyo zenu. Msimuliaji anasema aliwaona watu wanaoswali jamaa walikuwa wakisogezeana vifundo vya miguu na mikono yao karibu karibu. Nabiyy (ﷺ) alisema huku akimuapia Allaah (عز وجل) kuwa iwapo safu za ndani ya Swalaah zinaacha mapengo, anaweza kumuona shaytwaan mle. Pamoja na hii, zipo Hadiyth nyingi zinazozungumzia mpangilio wa safu katika Swalaah.

[23] Safu ya mwisho ya wanaume ni mbaya kwa sababu kwa kuwa imenyimwa fadhila za kuwa katika safu ya kwanza. Safu ya mwisho kuliko zote kwa mwanamke ndio bora zaidi kwa sababu iko mbali zaidi kuweza kuchanganyika na wanaume. Lakini iwapo jamaa ni ya wanawake watupu na Swalaah hiyo ya jamaa inaswalishwa na mwanamke, basi kanuni hiyo hiyo inahusika kwa wanawake pia, yaani safu ya kwanza ya wanawake hao ni bora zaidi kuliko safu ya mwisho sawa sawa na wanaume.

[24] Hukmu ni kwamba, wanaume sharti wapange safu kwanza, kisha watoto na kisha wanawake. Endapo yupo mwanamme mmoja na mtoto mmoja, basi wote wawili wasimame safu moja.

[25] Mwanamke mmoja tu anaruhusiwa aswali nyuma ya safu ya mwisho ya wanaume kukiwa hakuna mwanamke mwingine wa kuungana naye.

[26] Maana yake ni kuwa: “Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) na Aongeze shauku au himma yako ya kufanya matendo ya uadilifu, lakini tendo hilo lisikiuke mipaka.”

[27] Waabiswah bin Ma’bad ndiye Answaar kutoka katika ukoo wa Asad bin Khuzaymah. Alipewa jina la utani la Abuu Qirswaafah. Kwanza aliishi Kufa, kisha akahamia Al-Hira na akafariki mnamo mwaka 90 A.H.

[28] Kama Swalaah ya mtu anayeswali peke yake nyuma ya safu inakubalika au laa ni suala lenye kutofautiana na linalohitaji majadiliano zaidi. Ukweli ni kuwa mtu asiswali kwa kusimama peke yake wakati Swalaah ya Jamaa inaendelea.

[29] Nukta nyingine yenye kutofautiana ni kama sehemu ya Swalaah iliyobakia anayoiswali mtu nyuma ya Imaam katika Swalaah ya jamaa, ihesabike kuwa ni sehemu ya mwanzo ya Swalaah au kama ihesabike kuwa ni sehemu ya mwisho.

[30] Umm Waraqah huyu ndiye Bint Nawfal, au Bint ‘Abdillaah bin Al-Haarith bin ‘Uwaymr Al-Answaariyyah. Alikusanya Qur-aan na akamuomba Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amruhusu ashiriki katika vita vya Badr. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akimzuru na akimwita “Shahidi”. Aliuliwa na watumwa wake wa kiume na wa kike kwa kumziba pumzi na nguo. Kisha wakakimbia, lakini walikamatwa na wakauliwa kwa amri ya ‘Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ)

[31] Hadiyth hii inaeleza kuwa inaruhusiwa kwa mwanamke kuswalisha. Ni ukweli uliothibitishwa kuwa ‘Aaishah na Ummu Salamah (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) waliwahi kuswalisha. Imaam Shawkaan alisema kuwa, mwanamke akiswalisha, asisimame peke yake mbele ya safu, bali naye asimame ndani ya safu. Iwapo katika Maamuma wake wamo wanaume pia, basi ni sharti wawe Mahaarim (wasioweza kuwaoa). Mwanamke hawezi hadhara ya watu ambao kuna watu wageni au watu wasio mahaarim wake.

[32] Hadiyth hii inaweka wazi kabisa kuwa kipofu asiyeona anafaa kuswalisha. Wanazuoni wengine huafiki hili, lakini hiyo ni kinyume cha

desturi. Wanazuoni wengine husema kuwa, pakiwepo Mwanazuoni mwenye uwezo kamili wa kuona, si sahihi kumuomba Mwanazuoni asiyeona kuswalisha na oni hili ni batili pia. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuamrisha ‘Abdallaah bin Umm Maktwum (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) pamoja na kutoona kwake aswalishe kiasi cha mara kumi na tatu.

[33] Nukta inayodhihirishwa hapa ni kuwa, inaruhusiwa kuswali nyuma ya mtu anayepuuza kutekeleza mambo ya waajib. Lakini mtu kama huyo asiteuliwe kamwe kuwa Imaam, yaani asipewe kazi ya kuswalisha.

11-Mlango Wa Swalaah Ya Msafiri Na Mgonjwa

بَابُ صَلَاةِ الْمُسَافِرِ وَالْمَرِيضِ

11-Mlango Wa Swalaah Ya Msafiri Na Mgonjwa

341.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهَا قَالَتْ: {أَوَّلُ مَا فُرِضَتْ الصَّلَاةُ رَكْعَتَيْنِ ، فَأُقِرَّتْ صَلَاةُ السَّفَرِ وَأُتِمَّتْ صَلَاةُ الْحَضَرِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَالْبُخَارِيُّ: {ثُمَّ هَاجَرَ، فَفَرَضْتُ أَرْبَعًا، وَأُقِرَّتْ صَلَاةُ
السَّفَرِ عَلَى الْأَوَّلِ}
زَادَ أَحْمَدُ: {إِلَّا الْمَغْرِبَ فَإِنَّهَا وَثَرُ النَّهَارِ، وَإِلَّا الصُّبْحَ،
فَإِنَّهَا تَطُولُ فِيهَا الْقِرَاءَةُ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Mwanzo kufaradhishwa Swalaah ni Rakaa mbili[1], baadaye zikabakishwa (Hizo Rakaa mbili) kuwa Swalaah ya safari. Na Swalaah ya mkazi ikatimizwa (kwa kuongezwa Rakaa mbili nyingine).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika mapokezi ya Al-Bukhaariy: “Kisha (صَلَّى اللَّهُ) (Nabiy) akahajiri kwa hiyo Rakaa zikafaradhishwa nne, na Swalaah ya safari ikaachwa juu ya hali yake ya mwanzo.”

Na Ahmad aliongezea: “Isipokuwa Swalaah ya Magharibi kwani hiyo ni (Swalaah ya) Witr ya mchana, na isipokuwa Swalaah ya Alfajiri kwani hurefushwa ndani yake kisomo.”

342.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ كَانَ يَقْصُرُ فِي السَّفَرِ وَيُتِمُّ، وَيَصُومُ وَيُفْطِرُ.} رَوَاهُ
الدَّارَقُطْنِيُّ، وَرَوَاهُ ثِقَاتٌ. إِلَّا أَنَّهُ مَعْلُولٌ

وَالْمَحْفُوظُ عَنْ عَائِشَةَ مِنْ فِعْلِهَا، وَقَالَتْ: {إِنَّهُ لَا يَشُقُّ عَلَيَّ} أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akifupisha Swalaah safarini, na pia alikuwa akitimiza (Rakaa)[2], na alikua akifunga Swawm na akifuturu.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy, na wapokezi wake ni waaminifu, isipokuwa ni Hadiyth yenye ila]

Na imehifadhiwa kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) na ndivyo alivyokuwa anafanya na amesema (‘Aaishah): “Hakika (kufanya) hivyo si mashaka kwangu.” [Imetolewa na Al-Bayhqayy[3]]

343.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ أَنْ تُؤْتَى رُخْصَتُهُ كَمَا يَكْرَهُ أَنْ تُؤْتَى مَعْصِيَتُهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ .
وَفِي رِوَايَةٍ: {كَمَا يُحِبُّ أَنْ تُؤْتَى عَزَائِمُهُ}

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Allaah Anapenda rukhusa Zake zitumiwe, kama Anavyochukia kufanywa maasi Yake[4].” [Imetolewa na Ahmad, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan]

Katika mapokezi mengine: “Kama Anavyopenda utekelezwe wajibu Wake.”

344.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا خَرَجَ مَسِيرَةَ ثَلَاثَةِ أَمْيَالٍ أَوْ فَرَاسِخَ، صَلَّى رَكْعَتَيْنِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Pindi Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akisafiri safari ya maili tatu[5] au faraasikh[6] tatu, anaswali Rakaa mbili.” [Imetolewa na Muslim]

345.

وَعَنْهُ قَالَ: {خَرَجْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مِنَ الْمَدِينَةِ إِلَى مَكَّةَ، فَكَانَ يُصَلِّي رَكْعَتَيْنِ رَكْعَتَيْنِ حَتَّى رَجَعْنَا إِلَى الْمَدِينَةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) tena amesema: “Tulitoka pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) toka Madiynah kwenda Makkah, akawa anaswali Rakaa mbili mbili mpaka tuliporejea Madiynah.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

346.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {أَقَامَ النَّبِيُّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ تِسْعَةَ عَشَرَ يَقْصُرُ} وَفِي لَفْظٍ: {بِمَكَّةَ تِسْعَةَ
عَشَرَ يَوْمًا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَفِي رِوَايَةٍ لِأَبِي دَاوُدَ: {سَبْعَ عَشْرَةَ}

وَفِي أُخْرَى: {خَمْسَ عَشْرَةَ}

وَلَهُ عَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ: {ثَمَانِي عَشْرَةَ}

وَلَهُ عَنْ جَابِرٍ: {أَقَامَ بَتَّبُوكَ عِشْرِينَ يَوْمًا يَقْصُرُ الصَّلَاةَ}
وَرُوَاتُهُ ثِقَاتٌ، إِلَّا أَنَّهُ اخْتَلَفَ فِي وَصْلِهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikaa siku kumi na tisa (safari
ambapo alikuwa) akifupisha (Swalaah zake).” Katika tamshi lingine:
“Alikaa siku kumi na tisa Makkah.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Abuu Daawud: “...Siku kumi na saba...[7]”

Na katika mapokezi mengine tena: “...Siku kumi na tano...”

Yeye (Abuu Daawud) tena amepokea kutokana na masimulizi ya
‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “...Siku kumi na nane...”

(Abuu Daawud) tena amepokea Hadiyth ya Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikaa Tabuwk siku
ishirini, akifupisha Swalaah.” [Wapokezi wake wanategemewa,
isipokuwa wamekhitilafiana kuhusu muunganiko wake]

وَعَنْ أَنَسٍ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا ارْتَحَلَ قَبْلَ أَنْ تَزِيغَ الشَّمْسُ آخِرَ الظُّهْرِ إِلَى وَقْتِ الْعَصْرِ، ثُمَّ نَزَلَ فَجَمَعَ بَيْنَهُمَا، فَإِنْ زَاغَتِ الشَّمْسُ قَبْلَ أَنْ يَرْتَحِلَ صَلَّى الظُّهْرَ، ثُمَّ رَكِبَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةِ الْحَاكِمِ فِي "الْأَرْبَعِينَ" بِإِسْنَادٍ الصَّحِيحِ: {صَلَّى الظُّهْرَ وَالْعَصْرَ، ثُمَّ رَكِبَ}.

وَلِأَبِي نُعَيْمٍ فِي "مُسْتَخْرَجِ مُسْلِمٍ": {كَانَ إِذَا كَانَ فِي سَفَرٍ، فَزَالَتِ الشَّمْسُ صَلَّى الظُّهْرَ وَالْعَصْرَ جَمِيعًا، ثُمَّ ارْتَحَلَ}

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa safarini na akaendelea safari kabla jua halijapinduka, aliakhirisha Swalaah ya Adhuhuri hadi wakati wa Alasiri. Kisha alishuka na akaziunganisha Swalaah zote mbili. Jua likipinduka kabla hajaondoka anaswali Adhuhuri kisha anapanda mnyama wake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Katika mapokezi ya Al-Haakim iliyonukuliwa katika Al-Arba’iyn kwa Isnaad Swahiyh: “Aliswali Adhuhuri na Alasiri kisha akapanda mnyama wake na akaendelea na safari yake.”

Na Abuu Nu’aym (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alisimulia katika matoleo ya Muslim: “Akiwa safarini, kama jua limevuka, alikuwa akiswali Dhuhuri na Alasiri pamoja, kisha aliendelea na safari yake.”

348.

وَعَنْ مُعَاذِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {خَرَجْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي غَزْوَةِ تَبُوكَ، فَكَانَ يُصَلِّي الظُّهْرَ وَالْعَصْرَ جَمِيعًا، وَالْمَغْرِبَ وَالْعِشَاءَ جَمِيعًا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Mu'aadh (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tuliondoka pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika vita vya Tabuwk akawa anaswali Adhuhuri na Alasiri pamoja[8], na Swalaah ya Magharibi na ‘Ishaa pamoja.” [Imetolewa na Muslim]

349.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: {لَا تَقْصُرُوا الصَّلَاةَ فِي أَقَلِّ مِنْ أَرْبَعَةِ بُرْدٍ; مِنْ مَكَّةَ إِلَى عُسْفَانَ} رَوَاهُ الدَّارِقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ وَالصَّحِيحُ أَنَّهُ مَوْقُوفٌ، كَذَا أَخْرَجَهُ ابْنُ خُرَيْمَةَ.

Kutoka kwa Ibn ‘Abaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msifupishe Swalaah katika umbali usiozidi burud nne[9] kutoka Makkah mpaka ‘Usfaan.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy kwa Isnaad dhaifu, lililo sahihi ni kuwa hiyo ni Mawquwf, kadhalika ameipokea Ibn Khuzaymah]

350.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {خَيْرُ أُمَّتِي الَّذِينَ إِذَا أَسَاءُوا اسْتَغْفَرُوا، وَإِذَا سَافَرُوا قَصَرُوا وَأَفْطَرُوا} أَخْرَجَهُ الطَّبْرَانِيُّ فِي "الْأَوْسَطِ" بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ.

وَهُوَ فِي مُرْسَلٍ سَعِيدِ بْنِ الْمُسَيَّبِ عِنْدَ الْبَيْهَقِيِّ مُخْتَصَرٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Walio bora katika Ummah wangu ni wale ambao wakitenda dhambi huomba maghfirah kwa Allaah, na wakiwa safarini, wanafupisha Swalaah na kuacha kufunga Swawm.” [Imetolewa na Atw-Twabaraaniyy ameiandika katika Al-Aswatw kwa Isnaad dhaifu]

Al-Bayhaqiyy ameipokea kwa ufupi kuwa ni Mursal kutoka kwa Sa’iyd bin Al-Musayyib.

351.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَتْ بِي بَوَاسِيرٌ، فَسَأَلْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ الصَّلَاةِ؟ فَقَالَ: "صَلِّ قَائِمًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَقَاعِدًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَعَلَى جَنْبٍ"} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ.

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nilikuwa na maradhi ya bawasiri, nikamuuliza Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) juu ya Swalaah. Akasema: “Swali kwa kusimama, na ukiwa huwezi hivyo swali kwa kukaa, na ukiwa

huwezi hivyo, swali kwa kulalia ubavu.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

352.

وَعَنْ جَابِرٍ قَالَ: {عَادَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَرِيضًا، فَرَأَاهُ يُصَلِّي عَلَى وَسَادَةٍ، فَرَمَى بِهَا، وَقَالَ: "صَلِّ عَلَى الْأَرْضِ إِنْ اسْتَطَعْتَ، وَإِلَّا فَأَوْمِ إِمَاءً، وَاجْعَلْ سُجُودَكَ أَخْفَضَ مِنْ رُكُوعِكَ"} رَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ. وَصَحَّحَ أَبُو حَاتِمٍ وَقَفَّهُ.

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alizuru mgonjwa, akamkuta anaswali juu ya mto (tandiko). Akalitupa na akamuambia: “Swalia juu ya ardhi ukiweza, laa sivyo swali kwa ishara[10], na zifanye Sijdah zako kuwa chini zaidi kuliko rukuu zako.” [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy, na Abuu Haatim akaipa daraja Mawquwf]

353.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {رَأَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي مُتَرَبِّعًا} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ. وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilimuona Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) anaswali huku ameketi chini kwa kuikunja miguu yake.[11]” [Imetolewa na An-Nasaa'iy na akaisahihisha Al-Haakim]

[1] Hii inajulisha kwamba hapo mwanzoni, Swalaah ya fardhi ilikuwa inaswaliwa kwa Rakaa mbili tu (kama Swalaah ya safari). Baadaye urefu wa Swalaah za wakazi wa kudumu uliongezwa na urefu wa Swalaah ya safari ukabakia Rakaa mbili, Haijathibitishwa na mlolongo wa wapokezi kwamba Nabiyy (ﷺ) aliswali Swalaah kamili wakati wa safari.

[2] Mlolongo wa wapokezi kuhusu Hadiyih hii ni pamoja na ‘Alaa bin Zuhayr ambaye juu ya kujulikana kwake kuwa haifai, anajulikana kuwa si mkweli. Imaam Ibn Taymiyyah anasema kuwa anayosingiziwa Rasuli wa Allaah (ﷺ) ni ‘Uongo’. Katika Swahiyy mbili kupitia kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar (رضي الله عنهما) amesema kuwa Nabiyy (ﷺ) hakuwali kamwe zaidi ya Rakaa mbili alipokuwa safarini.

[3] Hadiyih hii haiwezi kutumika kama ushahidi kwa sababu katika mlolongo wa wapokezi yupo ‘Alaa bin Zuhayr ambaye si wa kutegemewa. Pia inaipinga Hadiyih iliyosimuliwa na Ibn ‘Umar (رضي الله عنه) na iliripotiwa na Al-Bukhaariy na Muslim kwamba, Nabiyy (ﷺ) kamwe hakuwali Rakaa zaidi ya mbili ya Swalaah za Rakaa nne.

[4] Hadiyih hii inadhihirisha kuwa, ni bora zaidi kuswali Swalaah ya Rakaa mbili, na kuswali kamili ni kukosa kutumiza Sunnah.

[5] Kuna mashaka katika Hadiyih hii kama ilitajwa maili tatu au farsakh tatu. Hadiyih ya awali haikutaja hili, lakini ni mashaka ya msimuliaji wa mlolongo wa wapokeaji kama Anas (رضي الله عنه) alitumia maneno: “Maili tatu” au “farsakh tatu”. Ni lazima tujue hilo ili tuweze “kuswali Swalaah ya Rakaa mbili.” Hakuna umbali uliotajwa katika Hadiyih yoyote, kama ile ruhusa ya kuchukua wudhuu kwa Tayammum (kutwawadha kwa mchanga) wakati mtu yumo safarini, umbali wakati wa safari umeachwa wazi sana kiasi kwamba imeruhusiwa kuswali Rakaa

mbili wakati wa safari yoyote ile. Inaelekea Hadiyth hii inaonyesha kuwa “Safari ya maili tatu” ni safari khasa, lakini kwa kuwa Shu’ba anaitilia shaka, Wanazuoni wengine wameamua kuwa umbali uwe farsakh tatu (yaani maili tisa). Wanazuoni wengine wamependekea maili 36, wengine maili 48, na wengine maili 52. Rejea ya kuhusu maili 48 ni imara zaidi, kwa kuwa Ahnaf na Wanazuoni wa Hadiyth wanapendekeza hiyo. Lakini hizi zote ni makisio ya kubahatisha tu, na hayajatolewa ushahidi wowote.

[6] Faraasikh (uwingi wa farsakh) ni kipimo cha Kiajemi cha umbali ambacho ni sawa na takribani maili tatu.

[7] Kuna khitilafu pia kuhusu urefu wa kukaa safarini. Wengine wametaja siku tatu, wengine siku kumi na nane. Kwa hakika ni swala walokhotilafiana.

[8] Hadiyth hii inadhirisha kuwa inaruhusiwa kuunganisha Adhuhuri na Alasiri pamoja na Magharibi na ‘Ishaa wakati wa safari, bila kujali kuwa Swalaah hizo zinaswaliwa wakati mahususi wa Swalaah ya mwanzo au wakati wa Swalaah ya pili. Hali zote hizi mbili zinathibitishwa kwa mfano au desturi za Nabiyy (ﷺ). Wafuasi wa Kihanafi hawaafiki desturi hii, ambayo inamaanisha kuwa wao hawaiafiki Hadiyth hii.

[9] Burud ni wingi wa barid, ambayo inamaanisha farsakh tatu, na farsakh moja ni sawa na maili tatu.

[10] Endapo mtu hawezi hata kutoa ishara, basi husamehewa kwa muda wajibu wa kuswali. Lakini mara atakavyopona na kurejesha afya na nguvu zake, lazima aziswali zote kama deni. Ikiwa mtu amezirai na amepotewa na fahamu kabisa, husamehewa Swalaah zake kadiri anavyokuwa hana fahamu.

[11] Nabiyy (ﷺ) aliketi chini vile kwa sababu maalumu. Hadiyth nyingine inasema kwamba, Rasuli wa Allaah (ﷺ) aliugua jipu pajani, na kadiri mtu anavyougua maradhi, anaweza kuswali kwa mkao wowote anaouweza bila kushurutishwa vyovyote. Hiyo ni zawadi kutoka kwa Allaah (عز وجل).

12-Mlango Wa Swalaatul-Jumu'ah (Swalaah Ya Ijuma)

بَابُ صَلَاةِ الْجُمُعَةِ

12-Mlango Wa Swalaatul-Jumu'ah [1]

354.

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ، وَأَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّهُمَا سَمِعَا رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ عَلَى أَعْوَادِ مَنبَرِهِ "لَيَنْتَهِيَنَّ أَقْوَامٌ عَنْ وَدْعِهِمُ الْجُمُعَاتِ، أَوْ لَيَخْتَمَنَّ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ، ثُمَّ لَيَكُونَنَّ مِنَ الْغَافِلِينَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar na Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) wamesema: “Walimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akisema huku akiwa juu ya Minbar: “Watu lazima waache kupuuza Swalaah za Ijumaa, vinginevyo Allaah Atapiga muhuri nyoyo zao, na kisha watakuwa miongoni mwa walioghafilika.” [Imetolewa na Muslim]

355.

وَعَنْ سَلَمَةَ بْنِ الْأَكْوَعِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كُنَّا نُصَلِّي مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْجُمُعَةَ، ثُمَّ نَنْصَرِفُ وَلَيْسَ لِلْحَيَّطَانِ ظِلٌّ نَسْتَضِلُّ بِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

وَفِي لَفْظٍ لِمُسْلِمٍ: {كُنَّا نَجْمَعُ مَعَهُ إِذَا زَالَتِ الشَّمْسُ، ثُمَّ نَرْجِعُ، نَتَّبَعُ الْفَيْءَ }

Kutoka kwa Salamah[2] bin Al-Akwa' (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulikuwa tukiswali Swalaah ya Ijumaa pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kisha tunaondoka wakati kuta hazijawa na kivuli[3] tunachojihifadhi[4].” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Tulikuwa tukikusanyika pamoja naye jua linapoondoka halafu tunarejea tunatafuta vivuli.”

356.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {مَا كُنَّا نَقِيلُ وَلَا نَتَغَدَّى إِلَّا بَعْدَ الْجُمُعَةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ وَفِي رِوَايَةٍ: {فِي عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ}

Kutoka kwa Sahl bin Sa'd[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Tulikuwa hatulali mchana wala hatuli chakula cha mchana isipokuwa baada ya kuswali Ijumaa.”[6] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Katika Riwaayah nyingine: “...zama za uhai wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).”

357.

وَعَنْ جَابِرٍ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَخْطُبُ قَائِمًا، فَجَاءَتْ عِيرٌ مِنَ الشَّامِ، فَاَنْفَقَلَ النَّاسُ إِلَيْهَا، حَتَّى لَمْ يَبْقَ إِلَّا اثْنَا عَشَرَ رَجُلًا } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anatoa khutuba kwa kusimama siku ya Ijumaa. Ukaja msafara kutoka Sham (Syria, Palestina, Lebanon na Jordan). Watu wakaukimbia hadi hakuna aliyebakia na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) isipokuwa watu kumi na wawili.” [Imetolewa na Muslim]

358.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَنْ أَدْرَكَ رَكْعَةً مِنْ صَلَاةِ الْجُمُعَةِ وَغَيْرِهَا فَلْيُضِفْ إِلَيْهَا أُخْرَى، وَقَدْ تَمَّتْ صَلَاتُهُ } رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَاللَّفْظُ لَهُ، وَإِسْنَادُهُ صَحِيحٌ، لَكِنْ قَوَّى أَبُو حَاتِمٍ إِرْسَالَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Endapo mtu yeyote kawahi Rakaa ya Swalaah ya Ijumaa au Swalaah yoyote nyingine[7], basi aongeze kuswali Rakaa ingine ndipo Swalaah yake itakamilika.[8]” [Imetolewa na An-Nasaaiy, Ibn Maajah na Ad-Daaraqutwniy na tamshi hili ni lake. Isnaad yake ni sahihi; lakini Al-Haatim aliipa nguvu kama Mursal]

359.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَخْطُبُ قَائِمًا، ثُمَّ يَجْلِسُ، ثُمَّ يَقُومُ فَيَخْطُبُ قَائِمًا، فَمَنْ أَنْبَأَكَ أَنَّهُ كَانَ يَخْطُبُ جَالِسًا، فَقَدْ كَذَبَ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitoa Khutbah akiwa amesimama[9], kisha anaketi, halafu anasimama tena. Na yeyote anayekuarifu kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitoa khutbah huku amekaa chini, amedanganya.” [Imetolewa na Muslim]

360.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا خَطَبَ، أَحْمَرَّتْ عَيْنَاهُ، وَعَلَا صَوْتُهُ، وَاشْتَدَّ غَضَبُهُ، حَتَّى كَأَنَّهُ مُنْذِرُ جَيْشٍ يَقُولُ: صَبَّحَكُمْ وَمَسَّأَكُمْ، وَيَقُولُ: "أَمَّا بَعْدُ، فَإِنَّ خَيْرَ الْحَدِيثِ كِتَابُ اللَّهِ، وَخَيْرَ الْهَدْيِ هَدْيُ مُحَمَّدٍ، وَشَرُّ الْأُمُورِ مُحْدَثَاتُهَا، وَكُلُّ

بِدْعَةٍ ضَالَّةٌ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَفِي رَوَايَةٍ لَهُ كَانَتْ خُطْبَةُ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ: {يَحْمَدُ اللَّهُ وَيُثْنِي عَلَيْهِ، ثُمَّ يَقُولُ عَلَى إِثْرِ ذَلِكَ، وَقَدْ عَلَا صَوْتُهُ}

وَفِي رَوَايَةٍ لَهُ: {مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ، وَمَنْ يُضِلَّ فَلَا هَادِيَ لَهُ}

وَالنَّسَائِيُّ: {وَكُلَّ ضَلَالَةٍ فِي النَّارِ}

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdullaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akitoa khutbah, macho yake huwa mekundu, na sauti yake hupanda[10], na ghadhabu yake huwa kali, kama vile mtu anayelionya jeshi akiwaambia: “(Adui) atakushambulieni asubuhi na jioni.” Na anasema: Ammaa Ba’du[11], Hakika mazungumzo bora ni Kitabu cha Allaah, na uongozi bora kabisa ni wa Muhammad, na mambo maovu ni ya uzushi (Bid’ah) na kila Bid’ah ni upotevu.[12]” [Imetolewa na Muslim]

Na katika Riwaayah yake nyingine: “Khutbah ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) siku ya Ijumaa ilikuwa hivi: Anamhimidi Allaah na anamsifu. Kisha anakhutubiu baada ya hayo na sauti yake inapanda.”

Na katika Riwaayah yake (Muslim) nyingine: “Na ambaye Allaah Amemhidi, basi hapana wa kumpotoa.” [Az-Zumar: 37], “Ambao Allaah Amewapotoa, basi hakuna wa kuwahidi” [Al-A’raaf: 186] na Ambaye Allaah Anampotosha hakuna yeyote anayeweza kumhidi.”

Na tamshi la An-Nasaaiy: “...na kila upotovu ni Motoni.”

361.

وَعَنْ عَمَّارِ بْنِ يَاسِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {إِنَّ طُولَ صَلَاةِ الرَّجُلِ، وَقِصَرَ خُطْبَتِهِ مِئَنَةٌ مِنْ فِقْهِهِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Ammmaar bin Yaasir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anasema: “Urefu wa Swalaah ya mtu, na ufupi wa khutbah yake ni alama ya Fiqhi yake (uelewa)[13] katika Dini.” [Imetolewa na Muslim]

362.

وَعَنْ أُمِّ هِشَامٍ بِنْتِ حَارِثَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {مَا أَخَذْتُ: "ق وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ"، إِلَّا عَنْ لِسَانِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرُوهَا كُلَّ جُمُعَةٍ عَلَى الْمِنْبَرِ إِذَا خُطِبَ النَّاسُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ.

Kutoka kwa Umm Hishaam[14] bint Haarithah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Sikuihifadhi Suwrah Qaaf[15] isipokuwa kutoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliyekuwa akiisoma kila siku ya Ijumaa juu ya Minbar[16] anapowakhutubia watu.” [Imetolewa na Muslim]

363.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَنْ تَكَلَّمَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ وَالْإِمَامُ يَخْطُبُ فَهُوَ كَمَثَلِ الْحِمَارِ يَحْمِلُ أَسْفَارًا، وَالَّذِي يَقُولُ لَهُ: أَنْصِتْ، لَيْسَتْ لَهُ جُمُعَةٌ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، بِإِسْنَادٍ لَا بَأْسَ بِهِ

وَهُوَ يُفَسِّرُ حَدِيثَ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي "الصَّحِيحَيْنِ" مَرْفُوعًا: { إِذَا قُلْتَ لِصَاحِبِكَ: أَنْصِتْ يَوْمَ الْجُمُعَةِ وَالْإِمَامُ يَخْطُبُ، فَقَدْ لَغَوْتَ }

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuzungumza siku ya Ijumaa wakati Imaam anakhutubia yeye ni kama punda aliyebeba vitabu[17], na anayemuambia: “Nyamaza!” basi hana Ijumaa.[18] [Imetolewa na Ahmad, kwa Isnaad isiyo na ubaya wowote]

Hadiyth hii inafanana na Hadiyth Marfuw’ ya Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) iliyopokewa katika Swahiyyh mbili: “Utakapomuambia mwenzako: “Nyamaza!” wakati Imaam anakhutubia, basi umefanya upuuzi.”

364.

وَعَنْ جَابِرٍ قَالَ: { دَخَلَ رَجُلٌ يَوْمَ الْجُمُعَةِ، وَالنَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَخْطُبُ. فَقَالَ: "صَلَّيْتَ؟" قَالَ: لَا. قَالَ: "قُمْ فَصَلِّ رَكَعَتَيْنِ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mtu mmoja aliingia Msikitini siku ya Ijumaa wakati Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akikhutubia. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akasema: “Umeswali?” Akajibu: “Hapana.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akasema: “Simama uswali Rakaa mbili.”[19] [Al-Bukhaariy, Muslim]

365.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ؛ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَقْرَأُ فِي صَلَاةِ الْجُمُعَةِ سُورَةَ الْجُمُعَةِ، وَالْمُنَافِقِينَ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَلَهُ: عَنْ النُّعْمَانِ بْنِ بَشِيرٍ: { كَانَ يَقْرَأُ فِي الْعِيدَيْنِ وَفِي الْجُمُعَةِ: بِ "سَبَّحَ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى"، وَ: "هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ" }

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anasoma katika Swalaah ya Ijumaa Suwrah Al-Jumu’ah na Al-Munaafiquwn.

Suwrah Al-Jumua’ah[20] na Al-Munaafiquwn[21].” [Imetolewa na Muslim]

Naye (Muslim) amenukuu Hadiyth ya Nu’maan bin Bashiyr[22] amesema: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anasoma katika Swalaah ya ‘Iyd mbili na Swalaah ya Ijumaa[23]

سَبَّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى [24]

na

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ [25]

366.

وَعَنْ زَيْدِ بْنِ أَرْقَمَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {صَلَّى النَّبِيُّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْعِيدَ، ثُمَّ رَخَّصَ فِي الْجُمُعَةِ، فَقَالَ: "مَنْ شَاءَ
أَنْ يُصَلِّيَ فَلْيُصَلِّ"} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ
ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Zayd bin Arqam (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali ‘Iyd (Siku ya Ijumaa), na
akaruhusu iswaliwe Swalaah ya Ijumaa akasema: Anaetaka kuiswali
aswali.”[26] [Imetolewa na Al-Khamsah (An-Nasaaiy, Abuu
Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa At-Tirmidhiy. Na
akaisahihisha Ibn Khuzaymah]

367.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمُ الْجُمُعَةَ فَلْيُصِلْ بَعْدَهَا أَرْبَعًا } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Yeyote kati yenu ataswali Swalaah ya Jumua’ah basi na aswali Rakaa nne baadaye.” [27] [Imetolewa na Muslim]

368.

وَعَنْ السَّائِبِ بْنِ يَزِيدَ، أَنَّ مُعَاوِيَةَ قَالَ لَهُ: { إِذَا صَلَّيْتَ الْجُمُعَةَ فَلَا تَصِلْهَا بِصَلَاةٍ، حَتَّى تُكَلِّمَ أَوْ تَخْرُجَ، فَإِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَمَرَنَا بِذَلِكَ: أَنْ لَا نُوصِلَ صَلَاةً بِصَلَاةٍ حَتَّى نَتَكَلَّمَ أَوْ نَخْرُجَ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa As-Saaib bin Yaziyd[28] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Mu’aawiyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuambia: “Unaposwali Ijumaa usiunganishe na Swalaah nyingine hadi umeongea au umekwenda nje. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituamrisha hivyo, kuwa tusiunganishe Swalaah moja na Swalaah nyingine, mpaka mtu tumeongea au tumetoka nje.”[29] [Imetolewa na Muslim]

369.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَنْ اغْتَسَلَ، ثُمَّ أَتَى الْجُمُعَةَ، فَصَلَّى مَا قُدِّرَ لَهُ، ثُمَّ أَنْصَتَ، حَتَّى يَفْرُغَ الْإِمَامُ مِنْ خُطْبَتِهِ، ثُمَّ يُصَلِّي مَعَهُ: غُفِرَ لَهُ مَا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجُمُعَةِ الْأُخْرَى، وَفُضِّلَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuoga, kisha akaja kuswali Ijumaa na akaswali alichopangiwa[30], halafu akanyamaza mpaka Imaam amemaliza khutbah, halafu akaswali pamoja naye, ataghufiriwa (madhambi) kati ya Ijumaa hiyo na inayofuatia na kwa siku tatu zaidi.”[31] [Imetolewa na Muslim]

370.

وَعَنْهُ; أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ذَكَرَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ فَقَالَ: { فِيهِ سَاعَةٌ لَا يُوَافِقُهَا عَبْدٌ مُسْلِمٌ وَهُوَ قَائِمٌ يُصَلِّي، يَسْأَلُ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ شَيْئًا إِلَّا أَعْطَاهُ إِيَّاهُ، وَأَشَارَ بِيَدِهِ يُقَلِّلُهَا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ: { وَهِيَ سَاعَةٌ خَفِيفَةٌ }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliitaja siku ya Ijumaa akasema: “Katika siku hii kuna muda ambapo hakuna mja Muislamu atakayesimama kuswali na anamuomba lolote isipokuwa Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) Atampa hilo jambo”[32] Akaashiria kwa mkono wake kuwa muda huo ni mdogo sana.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Na muda huo ni hafifu.”

371.

وَعَنْ أَبِي بُرْدَةَ عَنْ أَبِيهِ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { هِيَ مَا بَيْنَ أَنْ يَجْلِسَ الْإِمَامُ إِلَى أَنْ تُقْضَى الصَّلَاةُ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ،

وَرَجَّحَ الدَّارَقُطْنِيُّ أَنَّهُ مِنْ قَوْلِ أَبِي بُرْدَةَ
وَفِي حَدِيثِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ سَلَامٍ عِنْدَ ابْنِ مَاجَهَ

وَجَابِرٍ عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيِّ : { أَنَّهَا مَا بَيْنَ صَلَاةِ
الْعَصْرِ إِلَى غُرُوبِ الشَّمْسِ }

وَقَدْ اخْتَلَفَ فِيهَا عَلَى أَكْثَرِ مَنْ أَرْبَعِينَ قَوْلًا، أَمْلَيْتُهَا فِي
"شَرْحِ الْبُخَارِيِّ"

Kutoka kwa Abuu Burdah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa baba yake amesema: “Nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akisema: “Muda huo ni baina ya Imaam anapokaa mpaka mwisho wa Swalaah.” [Imetolewa na Muslim]

Na Ad-Daaraqutwniyy ana kauli kama ya Abuu Burdah.

Katika Hadiyth ya ‘Abdullaah bin Salaam iliyopokewa na Ibn Maajah

Pia Hadiyth ya Jaabir iliyopokewa na Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy: “Muda huo ni baina ya Swalaah ya Alasiri na kukuchwa kwa jua (Magharibi).”

Kuna kauli zaidi ya arubaini kuhusu muda huo, na nimezinukuu katika “Sharh Al-Bukhaariy”

372.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مَضَتِ السُّنَّةُ أَنْ فِي كُلِّ أَرْبَعِينَ فَصَاعِدًا جُمُعَةً} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Sunnah[33] imekuwa ni kuwa katika kila watu arubaini au zaidi ni Ijumaa.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy kwa Isnaad dhaifu[34]]

373.

وَعَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَسْتَغْفِرُ لِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ كُلِّ جُمُعَةٍ} رَوَاهُ الْبَزَّازُ بِإِسْنَادٍ لَيْئٍ

Kutoka kwa Samurah bin Jundub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiombea maghufirah Waumini wanaume na Waumini wanawake katika kila Ijumaa.” [Imetolewa na Al-Bazzaar kwa Isnaad laini]

374.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ فِي الْخُطْبَةِ يَقْرَأُ آيَاتٍ مِنَ الْقُرْآنِ، وَيَذْكُرُ النَّاسَ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَأَصْلُهُ فِي مُسْلِمٍ

Kutoka kwa Jaabir bin Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa anakhutubia alisoma Aayah kadhaa za Qur-aan, na anawakumbusha watu[35].” [Imetolewa na Abuu Daawuud, na chanzo chake ni katika Swahiyh Muslim]

375.

وَعَنْ طَارِقِ بْنِ شِهَابٍ; أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { الْجُمُعَةُ حَقٌّ وَاجِبٌ عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ فِي- جَمَاعَةٍ- إِلَّا أَرْبَعَةً: مَمْلُوكٌ، وَامْرَأَةٌ، وَصَبِيٌّ، وَمَرِيضٌ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَقَالَ: لَمْ يَسْمَعْ طَارِقٌ مِنَ النَّبِيِّ وَأَخْرَجَهُ الْحَاكِمُ مِنْ رِوَايَةِ طَارِقٍ الْمَذْكُورِ عَنْ أَبِي مُوسَى

Kutoka kwa Twaariq bin Shihaab[36] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah ya Ijumaa kwa jamaa ni waajibu kwa kila Muislamu isipokuwa wane: mtumwa, mwanamke, mtoto na mgonjwa.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na akasema: Twaariq hakusikia (haya) kwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)]

Al-Haakim ameyapokea haya kutoka kwa Twaariq aliyetajwa hapa, naye kutoka kwa Abuu Muwsaa.

376.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَيْسَ عَلَى مُسَافِرٍ جُمُعَةٌ} رَوَاهُ الطَّبْرَانِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah ya Ijumaa si lazima kwa msafiri.”[37] [Imetolewa na Atw-Twabaraaniyy kwa Isnaad dhaifu]

377

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا اسْتَوَى عَلَى الْمِنْبَرِ اسْتَقْبَلْنَاهُ بِوُجُوهِنَا} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ وَلَهُ شَاهِدٌ مِنْ حَدِيثِ الْبَرَاءِ عِنْدَ ابْنِ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa sawasawa juu ya minbar, sisi tunamuelekea kwa nyuso zetu.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy kwa Isnaad dhaifu]

Nayo ina ushahidi wa Hadiyth ya Al-Baraa iliyopokelewa na Ibn Khuzaymah.

378.

وَعَنِ الْحَكَمِ بْنِ حَزْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {شَهِدْنَا الْجُمُعَةَ
مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَامَ مُتَوَكِّئًا عَلَى عَصَا أَوْ
قَوْسٍ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa Al-Hakam bin Hazn[38] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Tulihudhuria Swalaah ya Ijumaa pamoja na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), naye akasimama wima akiegemea fimbo au
upinde.”[39] [Imetolewa na Abuu Daawuud]

[1] Siku ya Ijumaa ilikuwa ikijulikana kama Al-‘Aruwbah zama za Jaahiliyyah (kipindi kabla ya Uislamu kuja). Uislamu ukaita Jumua’ah kwa kuwa Waislamu wa mji hukusanyika (Jamaa) ili kuswali na kumwabudu Allaah (عَزَّ وَجَلَّ). Zaidi ya hizi, zipo sababu zingine pia.

[2] Salamah bin Al-Akwa’ ndiye Abuu Muslim, Salamah bin ‘Amr bin Al-Akwa’ Sinaan bin ‘Abdillaah Al-Aslamiy Al-Madaniy. Alikuwa mmoja wa Maswahaba mashujaa, na alikuwa akikimbia kwa kasi zaidi kuliko farasi kwa miguu yake. Alikuwa ni mtu mzuri, Mwenye taqwa, na mkarimu sana. Alifia Al-Madiynah mnamo mwaka wa 74 A.H.

[3] Hadiyth hii inasema wazi kwamba, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akimaliza Swalaah yake ya Ijumaa katika wakati ambao vivuli vya kuta vilikuwa havitoshi kuwafunika watu. Yaani Swalaah ya Ijumaa ni sharti iswaliwe mapema.

[4] Kwa mujibu wa Imaam Ahmad bin Hambal, inaruhusiwa kuanza kuswali Swalaah ya Ijumaa kabla ya Zawaal (jua halijageuka). Maimaamu waliobaki na Wanazuoni wengi wanasema kwamba Swalaah ya Ijumaa sharti ianze kuswaliwa mara baada ya zawaal. Siku hizi imekuwa desturi kuiahirisha Swalaah ya Ijumaa mbele zaidi, hata baada ya Adhuhuri yenyewe, ambaye ni kinyume na mwenendo wa Nabiyy (ﷺ).

[5] Sahl bin Sa'd ndiye Abdul-'Abbaas Al-Khazraji As-Sa'd Al-Answaariy. Aliripoti Hadiyih mia moja, na alifariki mnamo mwaka 91 A.H. akiwa na umri wa takribani miaka mia moja. Inasemekana kuwa alikuwa Swahaba wa mwisho kufariki Al-Madiynah.

[6] Haimaanishi kuwa alikuwa akiswali Swalaah ya Ijumaa hata kabla ya wakati wa zawaal (kugeuka kwa jua). Swalaah ya Ijumaa huitangulia Swalaah ya Adhuhuri. Na kadri inavyohitaji kusomwa khutbah, ni waajibu kuswali haraka, ili Swalaah imalizike ndani ya wakati wa mwanzo wa Adhuhuri.

[7] Usimulizi ambao unanasibishwa na Abuu Hurayrah katika Swahiyh mbili, haikusudii Swalaah ya Ijumaa peke yake, bali umejumuisha Swalaah zote. Madhali mtu kawahi Rakaa kamili na Imaam, anapata thawabu za Swalaah ya jamaa. Hii inahusu Swalaah ya Ijumaa pia. Kisha mtu huyo asimame na kukamilisha sehemu ya Swalaah iliyobakia.

[8] Hadiyih hii inakanusha maoni ya wale wanaodai kuwa Swalaah ya Ijumaa haikubaliki hadi mtu awe kasikiliza sehemu ya khutbah.

[9] Hadiyih hii inadhihirisha kwamba Nabiyy (ﷺ) alikuwa akiwakhutubia watu Msikitini huku amesimama wima. Pia inadhihirisha kwamba, katika Swalaah ya Ijumaa, kutoa khutbah kwa sehemu mbili kunafuata Sunnah, na kwamba ni Sunnah pia kuketi chini kwa muda mfupi katika sehemu mbili hizo za khutbah; na kuikhalifu Sunnah hii ya Nabiyy (ﷺ) kunahesabika kuwa ni bid'ah (iuzushi).

[10] Hadiyih hii inatufunza kwamba, khutbah ni sharti itolewe kwa sauti kubwa, na itolewe kwa njia mbayo itatoa athari ya kutosha kwa wanaosikiliza.

[11] Hayo ni maneno ya ufunguzi wa khutbah ya Kiislamu inayomaanisha: "Baada ya huo utangulizi."

[12] Kwa mujibu wa Shariy'ah, bid'ah ni tendo lolote ambalo halijatajwa au kuthibitishwa na Qur-aan wala Sunnah, wala haitokani na hizo. Maneno yale yasemayo “Kullu bid'ah (kila uzushi)” inaashiria kuwa bid'ah zote ni mbaya au hakuna uzushi (bid'ah) uliokuwa na uzuri wowote, kwa taarifa za kina, rejea kitabu cha Al-I'tiswaam cha Imaam Ash-Shaatwibiyy.

[13] Hii inadhihirisha kwamba, mtu sharti arefushe Swalaah yake na aifupishe khutbah. Baadhi ya Makhatibu siku hizi hurefusha mno khutbah, kiasi kwamba huingilia muda wa Swalaah, na kisha hujaribu kuimaliza Swalaah kwa haraka. Hii ni kinyume na mwenendo wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

[14] Umm Hishaam ndiye Umm Hishaam bint Haarithah bin Nu'umaan, dada (kwa upande wa Mama) wa 'Umrah bint 'Abdir-Rahmaan. Yeye ni Answaariyyah kutoka katika ukoo wa Najjaar. Inasemekana kuwa alishiriki katika Bay'atur-Ridhwaan.

[15] Qaaf (50)

[16] Hii ndiyo Shariy'ah kwetu kuwa, wakati tunawakhutubia watu kabla ya kuwaswalisha Swalaah.

[17] Mtu kama huyo anafanana na punda (mnyama wa kubeba mizigo), kwa vile hapati faida yoyote kwa kule kubeba vitabu vingi mgongoni kwake. Halikadhalika mtu huyo hapati faida yoyote kwa kuswali Swalaah ya Ijumaa.

[18] Zingatia kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakusema Swalaah ya mtu huyo haitakubaliwa, bali atanyimwa fadhila za Swalaah ya Ijumaa. Kwa hivyo Wanazuoni wamebainisha kutoka katika hilo kuwa mtu yeyote atakayeshiriki mazungumzo bila shaka atapata thawabu za Swalaah, lakini atanyimwa thawabu zinazonasibishwa na Swalaah ya Ijumaa.

[19] Usimulizi wa Al-Bukhaariy unao neno: “Khafiyfatayn (Khafifu mbili)” baada ya neno “Raka'tayn (Rakaa mbili)”, yaani inamaanisha kuwa yule mtu aliagizwa aswali Rakaa mbili lakini ziwe nyepesi ili ahifadhi muda mrefu zaidi wa kusikiliza khutbah.

[20] Al-Jumua'ah (62)

[21] Al-Munaafiquwn (63)

[22] Nu'umaan bin Bashiyr ndiye Abuu 'Abdullaah Al-Answaariyy Al-Madaniy, na alikuwa mtoto wa kwanza wa Kianswaar kuzaliwa baada ya Hijrah (kuhama) ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alizaliwa mnamo mwezi wa kumi na tatu wa Hijrah. Alilowea Sham na baadaye akawa

gavana wa Kufa na kisha Hims. Khaalid bin Khali Al-Kilaa'i alimuua yeye Abuu 'Abdullaah Al-Answaariyy katika siku ya Rahit mnamo mwaka 64 A.H.

[23] Miongoni mwa Suwrah hizi alikuwa akisoma Suwrah tofauti nyakati mbalimbali.

[24] [Al-A'laa (87)]

[25] Al-Ghaashiyah (88)

[26] Hii inaleta ushahidi kwamba, iwapo siku kuu ya 'Iyd inaangukia siku ya Ijumaa, siyo lazima kuswali Swalaah ya Ijumaa, lakini ni bora kuswali Ijumaa.

[27] Kuna tofauti ya maoni ya Rakaa ngapi ziswaliwe kama Sunnah baada ya Swalaah ya Ijumaa. Wengine wanatambua Rakaa mbili tu, wakati wengine hupendelea kuswali Rakaa nne. Imaam Shaafi'y na Imaam Ahmad na wengi wa Wanazuoni wameshikilia maoni hayo hayo ambayo ndiyo bora zaidi. Hadiyth ya Rakaa nne ni usemi wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mwenyewe, kwa hivyo watu wautekeleze.

[28] As-Saaib bin Yaziyd ndiye Abuu Yaziyd Al-Kindiy. Alizaliwa mnamo mwaka wa 2 A.H. na alihudhuria ile Hijjatul Wadaa'i pamoja na baba yake. Alikufa mnamo mwaka 80 A.H.

[29] Hadiyth hii inadhihirisha kwamba, endapo mtu ataiswali Swalaah fulani mahali fulani, basi asiswali Swalaah nyingine mahali palepale katika wakati uleule. Lazima uwepo umbali kati ya Swalaah hizo mbali ama kwa kubadilisha mahali au kwa njia ya Adhkaar (Kumdhukuru Allaah). Lengo la niyyah njema la kutenda hivi ni kwamba, rikodi ya matendo yake ipate kuonyeshe kuwa aliswali mahali pengi mbalimbali kadiri iwezekanavyo, au ionyeshe kuwa ameswali mara nyingi.

[30] Hakuna kikomo cha Swalaah za Sunnah (Nawaafil) mtu anazoweza kuziswali wakati akingojea Swalaah ya Ijumaa, na hakuna kikomo cha wakati. Lakini kama Hadiyth nyingine inavyosema kuwa hakukatazwi kuswali Swalaah za khiari siku ya Ijumaa hata iwe ni wakati wa zawaal.

[31] Ni ghuslu (Kuoga joshu) mnamo siku ya Ijumaa ni tendo la Sunnah kwa mujibu wa Wanazuoni wengi, ambayo ndiyo sahihi. Wengine wanaitambua kuwa ni waajib.

[32] Kuna wakati unaopatikana kila siku ya Ijumaa ambapo du'aa ya Muislamu hutakabaliwa bila shaka. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

hakuuutaja wakati huu maalumu. Wakati huo umefichwa kama ulivyofichwa Laylatul-Qadr ili watu watumie muda mwingi zaidi kuutafuta, na kwa hivyo wapate thawabu nyingi zaidi. Kuna nukuu mbili juu ya wakati huu. **Ya kwanza** inasema wakati huo ni kati ya Alasiri na machweo ya jua. **Ya pili** inasema wakati huo umo ndani ya wakati Imaam anapowasomea watu khutbah yake. Waislamu wajitahidi kuutafuta wakati huu nyakati zote za siku ya Ijumaa na khasa nyakati mbili hizo.

[33] Suala kuhusu watu wangapi wakusanyike pahala ili liswihi sharti la kuswali Swalaah ya Ijumaa nalo bado lina khitilafu miongoni mwa Wanazuoni. Tarakimu tofauti zimetolewa na watu mbalimbali watu watatu, wane, tisa, kumi na mbili, ishirini, arubaini, khamsini na sabiini. Ukweli ni kwamba hakuna tarakimu iliyotolewa na Hadiyth. Swalaah zote mbili, Swalaah ya Ijumaa hata kama kuna watu wawili tu wanaoziswali. Hadiyth hii inayotaja tarakimu ni dhaifu. Imeripotiwa katika Hadiyth kwamba, Swalaah ya kwanza kabisa ya Ijumaa katika Usilamu iliswaliwa katika kijiji cha Juwaathaa.

[34] Ameipokea ‘Abdul Aziyz bin ‘Abdir-Rahmaan ambaye Hadiyth zake zimeelezwa na Wanazuoni kuwa ni za “uongo”, za ‘kughush’ na yeye mwenyewe ahisabika kuwa “si wa kutegemewa.” Kwa hivyo sharti hilo kwa Swalaah ya Ijumaa siyo sahihi.

[35] Nabiyy (ﷺ) alikuwa akiwapa mawaidha watu juu ya misingi ya Uislamu, mambo ya msingi ya lazima ya Dini, na alikuwa akiwaonya watu wasighurike na anasa na starehe za dunia hii bali akiwavutia watu waelekee katika maisha ya Aakhirah.

[36] Twaariq bin Shihaab ni wa Ahmusi, Bajali, na wa Kufi, na aliishi muda mrefu katika zama za Jaahiliyyah na zama za Uislamu. Alimuona Nabiyy (ﷺ) lakini hakuwahi kusikia Hadiyth kutoka kwake. Alishiriki katika misafara ya kivita wakati wa Ukhalifa wa Abuu Bakr na ‘Umar. Alikufa mnamo mwaka 82 A.H.

[37] Hadiyth zote hizi zinaelezea kuwa, kuna aina sita za watu ambao kwao wao Swalaah ya Ijumaa siyo lazima. Hao ni watumwa, wanawake, watoto, wasafiri, wagonjwa na wanaohamama, aina zingine mbili zaidi, yaani vipofu na walemavu wametajwa ndani ya Qur-aan. Hao wakiswali Swalaah ya Ijumaa basi hawatawajibika tena Swalaah ya Adhuhuri.

[38] Al-Hakam bin Hazn ndiye Al-Hakam bin Hazn bin Abdil-Waahaab Al-Makhzuwm. Alisilimu katika mwaka ilipokombolewa Makkah. Na kwa

hivyo akahudhuria Swalaah ya Ijumaa pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[39] Hii inathibitisha kwamba, Khatiyb anapotoa khutbah anaweza kugemea kitu ili kuepusha uchovu kutokana na kisimamo cha muda mrefu.

13-Mlango Wa Swalaatul-Khawf (Swalaah Kipindi Cha Ya Khofu)

بَابُ صَلَاةِ الْخَوْفِ

13-Mlango Wa Swalaatul-Khawf (Swalaah Ya Kipindi Cha Khofu)

379.

عَنْ صَالِحِ بْنِ خَوَّاتٍ، {عَمَّنْ صَلَّى مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ ذَاتِ الرِّقَاعِ صَلَاةَ الْخَوْفِ: أَنَّ طَائِفَةً صَلَّتْ مَعَهُ وَطَائِفَةٌ وَجَّاهُ الْعَدُوَّ، فَصَلَّى بِالَّذِينَ مَعَهُ رَكْعَةً، ثُمَّ ثَبَتَ قَائِمًا وَاتَّمُوا لَأَنْفُسِهِمْ، ثُمَّ انْصَرَفُوا فَصَفُّوا وَجَّاهُ الْعَدُوَّ، وَجَاءَتِ الطَّائِفَةُ الْأُخْرَى، فَصَلَّى بِهِمُ الرَّكْعَةَ الَّتِي بَقِيَتْ، ثُمَّ

ثَبَّتَ جَالِسًا وَاتَّمُوا لِأَنْفُسِهِمْ، ثُمَّ سَلَّمَ بِهِمْ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَهَذَا لَفْظُ مُسْلِمٍ

وَوَقَعَ فِي "الْمَعْرِفَةِ" لِابْنِ مَنَدَةَ، عَنْ صَالِحِ بْنِ خَوَّاتٍ، عَنْ أَبِيهِ

Kutoka kwa Swaalih bin Khawwaat[1] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kwa upokezi wa mtu aliyeswali pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى Swalaatul-Khawf (Swalaah ya Khofu) katika vita vya Dhaat Ar-Riqaa'i[2]: “Kuwa kundi la jeshi lilijipanga safu moja pamoja naye, na kundi jingine mkabala na maadui. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaswalisha kundi lililokuwa pamoja naye Rakaa moja, kisha akabaki amesimama wima wakati wanamalizia Swalaah yao wenyewe. Wakaondoka na wakapanga safu mkabala na maadui, na kundi jingine la jeshi likaja. Akawaswalisha Rakaa iliyobaki ya Swalaah yake, kisha akabakia ameketi wakati wao wakimalizia Swalaah yao kisha akatoa nao Salaam.”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Na katika mapokezi ya Al Ma'rifah ya Ibn Mandah kutoka kwa Swaalih bin Khawwaat kutoka kwa babaake.

380.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ قَالَ: { غَزَوْتُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَبْلَ نَجْدٍ، فَوَازَيْنَا الْعَدُوَّ، فَصَافَفْنَاهُمْ، فَقَامَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُصَلِّي بِنَا، فَقَامَتْ طَائِفَةٌ مَعَهُ، وَأَقْبَلَتْ طَائِفَةٌ عَلَى الْعَدُوِّ، وَرَكَعَ بَيْنَ مَعَهُ، وَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ، ثُمَّ انْصَرَفُوا

مَكَانَ الطَّائِفَةِ الَّتِي لَمْ تُصَلِّ فَجَاءُوا، فَرَكَعَ بِهِمْ رَكْعَةً، وَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ، ثُمَّ سَلَّمَ، فَقَامَ كُلُّ وَاحِدٍ مِنْهُمْ، فَرَكَعَ لِنَفْسِهِ رَكْعَةً، وَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَهَذَا لَفْظُ الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) “Nilikwenda vitani pamoja na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) huko Najd[4], tulipofika mbele ya adui tulijipanga msitari tukiwakabili, akasimama Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akatuswalisha. Kundi moja likasimama pamoja naye kundi jingine limesimama mkabala na adui. Akawaswalisha Rakaa moja waliokuwa pamoja naye na akasujudu Sijdah mbili. Kisha wakaondoka wakaenda mahali pa kundi lililokuwa bado halijaswali. Wakaja na akawaswalisha Rakaa moja na akasujudu Sijdah mbili. Kisha akatoa Salaam. Kila mmoja akasimama na kuswali peke yake Rakaa moja na kusujudu Sijdah mbili.[5]” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

381.

وَعَنْ جَابِرٍ قَالَ: { شَهِدْتُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَاةَ الْخَوْفِ، فَصَفَّنَا صَفَّيْنِ: صَفٌّ خَلْفَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَالْعَدُوُّ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقِبْلَةِ، فَكَبَّرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَكَبَّرْنَا جَمِيعًا، ثُمَّ رَكَعَ وَرَكَعْنَا جَمِيعًا، ثُمَّ رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ وَرَفَعْنَا جَمِيعًا، ثُمَّ انْحَدَرَ بِالسُّجُودِ وَالصَّفِّ الَّذِي يَلِيهِ، وَقَامَ الصَّفُّ الْمُوَخَّرُ فِي نَحْرِ الْعَدُوِّ، فَلَمَّا قَضَى السُّجُودَ، قَامَ الصَّفُّ الَّذِي يَلِيهِ... } فَذَكَرَ الْحَدِيثَ

وَفِي رَوَايَةٍ: {ثُمَّ سَجَدَ وَسَجَدَ مَعَهُ الصَّفُّ الْأَوَّلُ، فَلَمَّا قَامُوا
سَجَدَ الصَّفُّ الثَّانِي، ثُمَّ تَأَخَّرَ الصَّفُّ الْأَوَّلُ وَتَقَدَّمَ الصَّفُّ
الثَّانِي...} فَذَكَرَ مِثْلَهُ

وَفِي آخِرِهِ: {ثُمَّ سَلَّمَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَسَلَّمْنَا
جَمِيعًا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَلِأَبِي دَاوُدَ: عَنْ أَبِي عَيَّاشٍ الزُّرْقِيِّ مِثْلَهُ، وَزَادَ: {أَنَّهَا
كَانَتْ بِعُسْفَانَ}

وَالنِّسَائِيُّ مِنْ وَجْهِ آخَرَ عَنْ جَابِرٍ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ صَلَّى بِطَائِفَةٍ مِنْ أَصْحَابِهِ رَكَعَتَيْنِ، ثُمَّ سَلَّمَ، ثُمَّ صَلَّى
بِآخَرِينَ أَيْضًا رَكَعَتَيْنِ، ثُمَّ سَلَّمَ}
وَمِثْلُهُ لِأَبِي دَاوُدَ، عَنْ أَبِي بَكْرَةَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilihudhuria
Swalaatul-Khawf (Swalaah ya Khofu) pamoja na Rasuli wa Allaah
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Tulijipanga safu mbili. Safu nyuma
yake na maadui wakiwa baina yetu na Qiblah. Rasuli wa Allaah
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akapiga Takbiyr nasi sote
tukaitamka, kisha akarukuu na sisi sote tukarukuu, kisha akanyanyua
kichwa chake baada ya kurukuu na sisi sote tukanyanyua vichwa
vyetu, kisha akateremka kusujudu pamoja na safu iliyokuwa karibu
yake wakati safu ya nyuma imesimama mkabala na adui. (Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)) alipomaliza kusujudu ikasimama
safu iliyo karibu yake...” akaitaja Hadiyth yote mfano wake.”[6]
[Imetolewa na Muslim]

Na katika mapokezi mengine: “...kisha safu ya kwanza ikasujudu
pamoja naye, waliposimama, ikasujudu safu ya pili, halafu safu ya

kwanza ikaenda nyuma na safu ya pili ikaenda mbele.” Hadiyth ikatajwa kama hiyo iliyotangulia.

Na mwisho wake inaeleza: “Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akatoa Salaam, kisha nasi sote tukatoa Salaam.” [Imetolewa na Muslim]

Abuu Daawuud amepokea Hadiyth kama hiyo kutoka kwa Abuu ‘Ayyaash Az-Zuraqiyy[7] (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) akaongezea: “Ilikuwa Usfaan.[8]”

An-Nasaaiy amepokea kwa njia nyingine kutoka Hadiyth ya Jaabir (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuwa: “Nabiy (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) aliswalisha kundi la Maswahaba wake Rakaa mbili, kisha akatoa Salaam, kisha akaswalisha kundi jingine Rakaa mbili, kisha akatoa Salaam.”

Hadiyth kama hiyo imepokewa na Abuu Daawuud kutoka kwa Abuu Bakr.

382.

وَعَنْ حُذَيْفَةَ: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى صَلَاةَ
الْخَوْفِ بِهَوْلٍ لَّائِ رَكْعَةٍ، وَبِهَوْلٍ لَّائِ رَكْعَةٍ، وَلَمْ يَقْضُوا } رَوَاهُ
أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ
وَمِثْلُهُ عِنْدَ ابْنِ حُرَيْمَةَ: عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ

Kutoka kwa Khudhayfah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali Swalaatul-Khawf (Swalaah ya Khofu) kwa kuswalisha hawa Rakaa moja na hawa (kundi jingine) Rakaa moja, na hawakukidhi (kulipa).” [Imetolewa na Ahmad, Abu Daawud na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

Mfano wa Hadiyth hiyo ameipokea Ibn Khuzaymah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا)

383.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { صَلَاةُ الْخَوْفِ رَكْعَةٌ عَلَى أَيِّ وَجْهِ كَانَ } رَوَاهُ الْبَزَّازُ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaatul-Khawf (Swalaah ya Khofu) ni Rakaa moja, kwa njia yoyote iwayo.” [Imetolewa na Al-Bazzaar kwa Isnaad dhaifu[9]]

384.

وَعَنْهُ مَرْفُوعًا: { لَيْسَ فِي صَلَاةِ الْخَوْفِ سَهْوٌ } أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) tena katika Hadiyth Marfuw’ amesema: “Katika Swalaatul-Khawf (Swalaah ya Khofu) hakuna (Sijdah ya) kusahau.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy kwa Isnaad dhaifu]

[1] Swaalih bin Khawwaat ndiye Swaalih bin Khawwaat bin Jaabir bin An-Nu’maan Al-Answaariyy Al-Madaniy. Alikuwa ni mmoja wa Maswahaba maarufu, na Ahaadiyth zake zina usahihi wa hali ya juu.

[2] Dhaati Ar-Riqaa’ inaweza kutafsiriwa kuwa ni “iliyo na misitari au milia”. Waislamu walikuwa wana ufukara wa hali ya juu sana, na walikuwa wanatembea pekupeku, bila kuvaa viatu. Miguu yao ikipata malengenge, walikuwa wakiifungiliza kwa marapurapu ya nguo chakavu. Kwa hivyo vita hivi vikaja kujulikana kama ni vita vya Dhaati Ar-Riqaa’.

[3] Hadiyth hii inaeleza kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswalisha Swalaah moja yenye Rakaa mbili, na Hadiyth ya pili inasema aliswalisha Swalaah mbili za Rakaa mbili kila moja kwa makundi mawili tofauti. Kwa kuwa kuswalisha Swalaah mbili kumetajwa, hakuna tofauti ya maoni juu yake. Uhakika wa mambo ni kwamba, katika Swalaatul-Khawf (Swalaah ya Khofu) kama mbinu za vita zimezingatiwa. Imethibitishwa kwamba Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitumia aina mbalimbali za kuswali wakati wa vita. Ibn Hazam alirejea au alizitaja namna kumi na nne mbalimbali za kuswali, kulingana na mahitaji au mazingira ya wakati ule. Wakati mwingine Swalaah ilikuwa ndefu, na wakati mwingine inakuwa fupi. Mara nyingine mtindo mmoja, na mara nyingine mtindo mwingine. Jina la Swahaba wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) huyo lilitajwa kuwa ni Sahl bin Abuu Hathmah.

[4] Najd ni jina la sehemu ya Rasi ya Arabuni ambako kuna nyanda za juu za milima.

[5] Kutokana na Hadiyth hii, inaelekea kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswalisha Rakaa moja kwa kila moja ya makundi mawili tofauti, wakati kila kundi liliswali Rakaa nyingine moja peke yake. Inaelekea kuwa hali hii inaafikiana na Aayah za Qur-aan [An-Nisaa (4: 102-103)]

[6] Sehemu iliyobaki ya Hadiyth inaeleza: "...safu ya nyuma ikaenda chini kusujudu kisha wakasimama. Halafu safu ya nyuma ikaenda mbele na safu ya mbele ikarudi nyuma. Nabiyy (ﷺ) akarukuu nasi sote tukarukuu, akanyanyua kichwa chake baada ya kurukuu na sisi sote tukanyanyua vichwa vyetu. Kisha yeye na safu ya karibu yake lakini ilikuwa nyuma katika Rakaa ya kwanza wakasujudu, wakati safu ya nyuma imesimama mkabala na adui. Kisha Nabiyy (ﷺ) na safu iliyokuwa karibu naye walipomaliza kusujudu, safu ya nyuma nao wakaenda chini kusujudu. Kisha Nabiyy (ﷺ) akatoa Salaam, nasi sote tukafanya hivyo." Mwisho wa Hadiyth.

[7] Abuu 'Ayyaash ndiye Zayd bin Thaabit, ambaye ni Answaariyy na Zuraqiyy. Kundi la Waislamu limeripoti Hadiyth kutoka kwake na alikufa baada ya mwaka 40 A.H.

[8] 'Usfaan ni pahala ambapo pako Nanzil (takribani sawa na safari ya siku mbili) kutoka Makkah.

[9] Hadiyth hii imewafanya wengine waamue kwamba ipo Rakaa moja tu kwa wote Maamuma na Imaam pia. Kwa hivyo Sufyaan anafuata vivyo hivyo.

14-Mlango Wa Swalaatul-'Iydayni (Swalaah Za 'Iyd Mbili)

بَابُ صَلَاةِ الْعِيدَيْنِ

14-Mlango Wa Swalaatul-'Iydayni (Swalaah Za 'IydMbili)[1]

385.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { الْفِطْرُ يَوْمَ يُفْطِرُ النَّاسُ، وَالْأَضْحَى يَوْمَ يُضْحِي النَّاسُ } رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Al-Fitwr ni siku ambapo watu wanakula. Na Al-Adhwhaa ni siku ambapo watu wanachinja.”[2] [Imetolewa na At-Tirmidhiy]

386.

وَعَنْ أَبِي عُمَيْرٍ بْنِ أَنَسٍ، عَنْ عُمُومَةٍ لَهُ مِنَ الصَّحَابَةِ، { أَنَّ رَكْبًا جَاءُوا، فَشَهِدُوا أَنَّهُمْ رَأَوْا الْهَلَالَ بِالْأَمْسِ، فَأَمَرَ هُمُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يُفْطِرُوا، وَإِذَا أَصْبَحُوا يَغْدُوا إِلَى مُصَلَّاهُمْ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ وَهَذَا لَفْظُهُ وَإِسْنَادُهُ صَحِيحٌ

Kutoka kwa Abuu ‘Umayr bin Anas[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kwa upokezi wa maami zake miongoni mwa Maswahaba: “Msafara ulikuja wakashuhudia kuwa wao wameona mwezi mwandamo jana. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaamrisha kula (waache Swawm) na asubuhi waende mahali pa kuswalia.”[4] [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuwd, na tamshi hili ni la Abuu Daawuwd, na Isnaad zake ni Swahiyh]

387.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَا يَغْدُو يَوْمَ الْفِطْرِ حَتَّى يَأْكُلَ تَمْرَاتٍ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

وَفِي رِوَايَةٍ مُعَلَّقَةٍ وَوَصَلَهَا أَحْمَدُ: وَيَأْكُلُهُنَّ أَفْرَادًا

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa hatoki siku ya ‘Iyd Al-Fitwr isipokuwa mpaka ale tende.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na katika mapokezi mengine ni Mu’allaq lakini imeunganishwa na Ahmad: “...Na alikuwa akila moja moja Witr.”

388.

وَعَنْ ابْنِ بُرَيْدَةَ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَا يَخْرُجُ يَوْمَ الْفِطْرِ حَتَّى يَطْعَمَ، وَلَا يَطْعَمُ يَوْمَ الْأَضْحَى حَتَّى يُصَلِّيَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn Buraydah amesema kutoka kwa baba yake kuwa amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa hatoki siku ya ‘Iyd isipokuwa mpaka ale, wala hali kitu siku ya ‘Iyd ya kuchinja[5] mpaka aswali.” [Imetolewa na Ahmad na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

389.

وَعَنْ أُمِّ عَطِيَّةَ قَالَتْ: {أَمَرْنَا أَنْ نُخْرِجَ الْعَوَاتِقَ، وَالْحَيْضَ فِي الْعِيدَيْنِ؛ يَشْهَدْنَ الْخَيْرَ وَدَعْوَةَ الْمُسْلِمِينَ، وَيَعْتَزِلُ الْحَيْضُ الْمُصَلَّى} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ummu ‘Atwiyyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Tumeamrisha[6] siku za ‘Iyd mbili (‘Iydul Fitwr na ‘Iydul Adhwhaa) tuwatoe wasichana na wenye hedhi ili wahudhuriye kheri na du’aa ya Waislamu, isipokuwa wanawake wenye hedhi waepuke mahala pa kuswalia.”[7] [Al-Bukhaariy, Muslim]

390.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَأَبُو بَكْرٍ، وَعُمَرُ: يُصَلُّونَ الْعِيدَيْنِ قَبْلَ الْخُطْبَةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), Abuu Bakr na ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) walikuwa wakiswali ‘Iyd kabla ya Khutbah.” [8] [Al-Bukhaariy, Muslim]

391.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ: {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى يَوْمَ الْعِيدِ رَكَعَتَيْنِ، لَمْ يُصَلِّ قَبْلَهَا وَلَا بَعْدَهَا} أَخْرَجَهُ السَّبْعَةُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali Rakaa mbili[9] siku
ya ‘Iyd na hakuwali kabla wala baada yake.”[10] [Imetolewa na As-
Sab’ah (Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu
Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad)]

392.

وَعَنْهُ: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى الْعِيدَ بِلاَ أَذَانٍ،
وَلَا إِقَامَةٍ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ . وَأَصْلُهُ فِي الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali ‘Iyd bila Adhana
wala Iqaamah.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na chanzo chake ni
katika Al-Bukhaariy]

393.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ قَالَ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
لَا يُصَلِّي قَبْلَ الْعِيدِ شَيْئًا، فَإِذَا رَجَعَ إِلَى مَنْزِلِهِ صَلَّى
رَكْعَتَيْنِ } رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakuwali kamwe Swalaah
yoyote kabla ya Swalaah ya ‘Iyd, lakini aliporejea nyumbani alikuwa
anaswali Rakaa mbili.” [Imetolewa na Ibn Maajah kupitia mlolongo
mzuri wa wapokezi]

394.

وَعَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَخْرُجُ يَوْمَ الْفِطْرِ وَالْأَضْحَى إِلَى الْمُصَلَّى، وَأَوَّلُ شَيْءٍ يَبْدَأُ بِهِ الصَّلَاةُ، ثُمَّ يَنْصَرِفُ فَيَقُومُ مُقَابِلَ النَّاسِ وَالنَّاسُ عَلَى صُفُوفِهِمْ فَيُعِظُهُمْ وَيَأْمُرُهُمْ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anatokea siku ya Fitwr na siku ya Al-Adhwhaa, mpaka mahala pa kuswalia, na jambo la mwanzo alilofanya ni kuswali. Alipomaliza, alisimama wima kuwakabili watu walioketi chini katika safu zao. Kisha aliwakhutubia na kuwaamrisha.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

395.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ عَنْ أَبِيهِ عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ نَبِيُّ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {التَّكْبِيرُ فِي الْفِطْرِ سَبْعٌ فِي الْأُولَى وَخَمْسٌ فِي الْآخِرَةِ، وَالْقِرَاءَةُ بَعْدَهُمَا كِلْتَاهُمَا} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَنَقَلَ التِّرْمِذِيُّ عَنِ الْبُخَارِيِّ تَصْحِيحَهُ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb amesema kutoka kwa baba yake, naye kutoka kwa babu yake, amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Takbiyr katika Swalaah ya ‘Iydul Fitwr ni saba katika Rakaa ya kwanza[11], na tano katika Rakaa ya pili. Na kisomo (cha Qur-aan) katika zote mbili ni baada yake

(Takbiyra).” [Imetolewa na Abuu Daawuud, na At-Tirmidhiy aliisahihisha kutoka kwa Al-Bukhaariy]

396.

وَعَنْ أَبِي وَاqِدِ اللَّيْثِيِّ قَالَ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ فِي الْأَضْحَى وَالْفِطْرِ بِ (ق)، وَ (اَقْتَرَبْتُ) } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Waaqid Al-Laythiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anasoma katika ‘Iydul Adhwhaa na ‘Iyd Al-Fitwr

ق[12]

na,

اَقْتَرَبْتُ[13]

[Imetolewa na Muslim]

397.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا كَانَ يَوْمُ الْعِيدِ خَالَفَ الطَّرِيقَ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ
وَلِأَبِي دَاوُدَ: عَنْ ابْنِ عُمَرَ، نَحْوَهُ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Ilipofika siku ya ‘Iyd, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akibadilisha njia[14]”. [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Naye Abuu Daawuwd amepokea Hadiyth kama hiyo kutoka kwa ‘Umar.

398.

وَعَنْ أَنَسٍ قَالَ: {قَدِمَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْمَدِينَةَ، وَلَهُمْ يَوْمَانِ يَلْعَبُونَ فِيهِمَا. فَقَالَ: "قَدْ أَبْدَلَكُمْ اللَّهُ بِهِمَا خَيْرًا مِنْهُمَا: يَوْمَ الْأَضْحَى، وَيَوْمَ الْفِطْرِ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ بِإِسْنَادٍ صَحِيحٍ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuja Al-Madiynah, watu wakiwa na siku mbili wacheza michezo ndani yake (kusherehekea). Akasema: “Allaah Amewabadilishieni kilicho bora zaidi, siku ya Al-Adhwhaa (kuchinja) na siku ya Al-Fitwr (kufungua Swawm).” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy kwa Isnaad Swahiyh]

399.

وَعَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مِنَ السُّنَّةِ أَنْ يَخْرُجَ إِلَى الْعِيدِ مَاثِيًا} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَحَسَنَهُ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Ni miongoni mwa Sunnah kwenda kwa kuswali ‘Iyd kwa miguu.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaopa daraja la Hasan]

400.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُمْ أَصَابَهُمْ مَطَرٌ فِي يَوْمٍ عِيدٍ. فَصَلَّى بِهِمُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَاةَ الْعِيدِ فِي الْمَسْجِدِ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ لَيِّنٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Mvua ilinyesha siku ya ‘Iyd, kwa hivyo Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akawaswalisha watu ‘Iyd ndani ya Msikiti.”[15] [Imetolewa na Abuu Daawuwd kwa Isnaad layyin (dhaifu)]

[1] Swalaah za Iyd mbili ni Sunnah Muakkadah (Sunnah iliyosisitizwa). Wanazuoni wengine huzitekeleza hizo kama Fardwh Kifaayah (Faradhi ya kutoshelezana). Na wengine wanasema hizo ni Fardhw ‘Ayn (wajibu wa binafsi ambayo ni sharti utekelezwe na kila mtu). Rai ya mwanzo ndio inaonekana ni ya nguvu.

[2] Hadiyth hii inadhihirisha kuwa, ili kuiadhimisha ‘Iydul-Fitwr na ‘Iydul-Adhwhaa kwa Swalaah inahitajika kuswaliwa na ummati wa watu kwa amri ya kiongozi Muislamu. Kama mtu anauona mwezi mchanga wa Shawwaal na watu hawamuamini, basi mtu huyo hawezi kuacha Swawm wala kuswali ‘Iyd hiyo pekee. Anaweza kufanya hivyo pale tu ambapo Waislamu wengine wameshiriki.

[3] Jina la Abuu ‘Umayr ni ‘Abdullaah bin Anas bin Maalik Al-Answaariyy, naye alikuwa ndiye mtoto mkubwa kuliko wote. Alikuwa wa kutegemewa wa daraja la nne, na alikuwa mmoja wa Taabi’iyn. Aliishi muda mrefu baada ya babake.

[4] Hii inathibitisha kuwa ikiwa mwezi haujaonekana mnamo tarehe 29 ya mwezi wa Ramadhwaan, lakini siku inayofuata taarifa za kuthibitisha kuona mwezi zikifika, Swawm sharti isitishwe pale pale. Iwapo uthibitisho huo utafika kabla ya wakati wa Zawaal (Jua linapogeuka), Swalaah ya ‘Iyd ni sharti iswaliwe siku ile ile. Lakini ikiwa uthibitisho umefika baada ya wakati wa Zawaal basi ‘Iyd sharti iswaliwe asubuhi siku inayofuata.

[5] Hadiyth hii inatufunza kuwa ni Sunnah watu kula kitu fulani kabla ya kuswali ‘Iydul-Fitwr na kula baada ya ‘Iydul-Adhwhaa. Hakijapendekezwa chakula chochote maalumu, lakini kwa kuzingatia mwenendo wa Nabiyy (ﷺ), bora kula tende.

[6] Hadiyth hii inatufunza kuwa ni ubora wanawake waende kwenye Muswalla wa ‘Iyd na wakaswali kule pamoja na wanaume. Upendeleo huo wanapewa wanawake ili nao pia washiriki katika du’aa pamoja na Baraka za siku kuu hiyo.

[7] Watu wengine wanaifasiri Hadiyth hii kwamba upendeleo huu ulikuwa kwa siku zile za mwanzo mwanzo tu ili uwingi wa Ummah wa Waislam uonekane mkubwa sana, lakini wanadai kuwa, rukhsa ile kwa wanawake kuja nje ilifutwa baadaye. Lakini kuijibu hoja yao uzuri, yatosheleza kunukuu Hadiyth iliyosimuliwa na ‘Abdullaah bin ‘Abbaas (رضي الله عنه) ambayo inasema, hata baada ya kuiteka Makkah yeye aliwaona wanawake wakienda katika Muswalla wa ‘Iyd.

[8] Kwa mujibu wa Sunnah, Khutbah hutolewa baada ya kuswali, na hakuna kutofautiana maoni juu ya hili. Katika enzi za Baniy Umayyah, Marwaan alileta uzushi kwamba Khutbah itolewe kabla ya kuswali, lakini desturi hiyo haina nafasi katika Uislam.

[9] Iwapo mtu atashindwa kuunga nyuma ya Imaam katika Swalaah ya 'Iyd, akaswali pekee, basi Imaam Ahmad na Ath-Thawriy wana rai kwamba aswali Rakaa nne. Wanazuoni wengine wanaona kwamba aswali Rakkaa mbili. Ama Imaam Abuu Haniyfah ana rai kwamba mtu anaweza kuchagua kati ya kuswali Swalaah ya 'Iyd iliyompita kama ni Rakaa mbili au nne [Rejea Fathul-'Allaam (2/521)]

[10] Kusiswaliwe Naafil (Swalaah ya Sunnah, ya khiari) kabla wala baada ya Swalaah ya 'Iyd katika mahala pa kuswalia 'Iyd. Lakini mtu anaweza kuswali Sunnah nyumbani.

[11] Kuna tofauti ya maoni miongoni mwa Wanazuoni juu ya ripoti kumi kuhusu hizi Takbiyra zaidi mbili. Mchakato sahihi ni huo uliosimuliwa katika Hadiyth hii. Watu wengine wanaegemea katika Hadiyth iliyosimuliwa na Ibn Mas-'uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwa baki ya Takbiyratul-Iftitaah (ya kufungulia Swalaah), na Takbiyratur-Rukuwu' (ya kurukuu) zipo Takbiyra nyenginezo sita; tatu za kutamka ndani ya Rakaa ya kwanza kabla ya kisomo, na tatu zingine za kutamka ndani ya Rakaa ya pili baada ya kisomo. Kwa usahihi, Hadiyth iliyosimuliwa na Ibn Mas-'uwd si ya kutegemewa.

[12] Qaaf (50)

[13] Al-Qamar: (54)

[14] Yaani kama alipokua akienda kuswali ‘Iyd alifuata njia hii, basi aliporudi kutoka huko alirudi kwa njia nyingine, kwa sababu mahala mbalimbali hizo zitashuhudia upitaji njia kuenda kuswali, na hadhi ya Uislam itakuwa juu.

[15] Hadiyth hii inathibitisha kuwa itokeapo ugumu kuswalia Muswalla wa ‘Iyd (Pahala pa kuswalia ‘Iyd), ni rukhsa kuswali ‘Iyd ndani ya Msikiti.

15-Mlango Wa Swalaatul-Kusuwf (Swalaah Ya Kupatwa Jua Au Mwezi)

بَابُ صَلَاةِ الْكُسُوفِ

15-Mlango Wa Swalaatul-Kusuwf [1] (Swalaah Ya Kupatwa Jua Au Mwezi)

401.

عَنْ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {انْكَسَفَتِ الشَّمْسُ عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ مَاتَ إِبْرَاهِيمُ، فَقَالَ النَّاسُ: انْكَسَفَتِ الشَّمْسُ لِمَوْتِ إِبْرَاهِيمَ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "إِنَّ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ آيَتَانِ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ لَا يَنْكَسِفَانِ لِمَوْتِ أَحَدٍ وَلَا لِحَيَاتِهِ، فَإِذَا رَأَيْتُمُوهُمَا، فَادْعُوا اللَّهَ وَصَلُّوا، حَتَّى تَنْكَشِفَ"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: «حَتَّى تَنْجَلِي»
وَالْبُخَارِيُّ مِنْ حَدِيثِ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {فَصَلُّوا
وَادْعُوا حَتَّى يُكْشَفَ مَا بَكُمْ}

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Al-Mughiyrah bin Shu'bah amesema: “Jua lilipatwa wakati wa uhai wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), siku alipofariki (mwanae) Ibraahiym,[2] watu wakasema: Jua limepatwa kwa sababu ya kifo cha Ibraahiym. Akasema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): Jua na mwezi ni Aayaat (ishara) mbili kati ya Aayaat za Allaah. Havipatwi kwa sababu ya kufa yeyote wala kwa uhai wake. [3] Kwa hivyo munapoona kupatwa kwake, muombeni Allaah na mswali hadi kupatwa huko kuondoke.”[4] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Al-Bukhaariy: “Mpaka pawe paangavu.”

Na katika upokezi wa Al-Bukhaariy kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Swalini na ombeni hadi kuondoke kilichokufikeni.”

402.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا: {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ جَهَرَ فِي صَلَاةِ الْكُسُوفِ بِقِرَاءَتِهِ، فَصَلَّى أَرْبَعَ

رَكَعَاتٍ فِي رَكَعَتَيْنِ، وَأَرْبَعَ سَجَدَاتٍ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَهَذَا لَفْظُ مُسْلِمٍ

وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ: {فَبَعَثَ مُنَادِيًا يُنَادِي: الصَّلَاةُ جَامِعَةٌ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisoma kwa sauti[5] kisomo chake cha Swalaatul-Kusuwf (Swalaah ya kupatwa jua au mwezi), akaswali Rakaa mbili ambamo alirukuu mara nne[6] na alisujudu mara nne.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Na katika mapokezi mengine: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akatuma mtu akaenda kutangaza: “Njooni kwenye Swalaah ya Jamaa.”[7]

403.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {إِنْخَسَفَتِ الشَّمْسُ عَلَى عَهْدِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَصَلَّى، فَقَامَ قِيَامًا طَوِيلًا، نَحْوًا مِنْ قِرَاءَةِ سُورَةِ الْبَقَرَةِ، ثُمَّ رَكَعَ رُكُوعًا طَوِيلًا، ثُمَّ رَفَعَ فَقَامَ قِيَامًا طَوِيلًا وَهُوَ دُونَ الْقِيَامِ الْأَوَّلِ، ثُمَّ رَكَعَ رُكُوعًا طَوِيلًا، وَهُوَ دُونَ الرُّكُوعِ الْأَوَّلِ، ثُمَّ سَجَدَ، ثُمَّ قَامَ قِيَامًا طَوِيلًا، وَهُوَ دُونَ الْقِيَامِ الْأَوَّلِ، ثُمَّ رَكَعَ رُكُوعًا طَوِيلًا، وَهُوَ دُونَ الرُّكُوعِ الْأَوَّلِ، ثُمَّ رَفَعَ، فَقَامَ قِيَامًا طَوِيلًا، وَهُوَ دُونَ الْقِيَامِ الْأَوَّلِ، ثُمَّ رَكَعَ رُكُوعًا طَوِيلًا، وَهُوَ دُونَ

الرُّكُوعِ الْأَوَّلِ، ثُمَّ سَجَدَ، ثُمَّ انْصَرَفَ وَقَدْ تَجَلَّتِ الشَّمْسُ.
فَخَطَبَ النَّاسَ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ: {صَلَّى حِينَ كَسَفَتِ الشَّمْسُ ثَمَانِ
رَكَعَاتٍ فِي أَرْبَعِ سَجَدَاتٍ}
وَعَنْ عَلِيٍّ مِثْلُ ذَلِكَ

وَلَهُ: عَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {صَلَّى سِتَّ رَكَعَاتٍ بِأَرْبَعِ
سَجَدَاتٍ}

وَلِأَبِي دَاوُدَ: عَنْ أَبِي بِنِ كَعْبٍ: {صَلَّى، فَرَكَعَ خَمْسَ
رَكَعَاتٍ وَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ، وَفَعَلَ فِي الثَّانِيَةِ مِثْلَ ذَلِكَ}

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Jua lilipatwa wakati wa uhai wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), akaswali na akasimama kisomo kirefu, kadiri ya kuweza kusoma Suwratul-Baqarah, kisha akarukuu Rukuu ndefu, akainua kichwa na kusimama kisimamo kirefu, chini ya kisimamo cha kwanza, kisha akarukuu Rukuu ndefu chini ya Rukuu ya kwanza, akasujudu na akasimama kisimamo kirefu chini ya kisimamo cha kwanza, kisha akarukuu Rukuu ndefu chini ya Rukuu ya kwanza, kisha akainua kichwa, kisha akasujudu, kisha akaondoka, na jua lilishafunguka. Akatoa Khutbah.”[8] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Jua lilipopatwa, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali Rakaa nane katika Sijdah nne.” Na ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alisimulia Hadiyth nyingine kama hiyo.

Yeye (Muslim) tena amemnukuu Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwa:
“(Nabiy صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali kwa Rakaa sita na
Sijdah nne.”

Na Abuu Daawuud amepokea masimulizi ya Ubayy bin Ka'b
(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwa: “(Nabiy صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali na akarukuu mara tano na akasujudu mara mbili, na katika
Rakaa ya pili alifanya hivyo hivyo.”

404.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {مَا هَبَّتْ رِيحٌ قَطُّ
إِلَّا جَنَّا النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى رُكْبَتَيْهِ، وَقَالَ:
"اللَّهُمَّ اجْعَلْهَا رَحْمَةً، وَلَا تَجْعَلْهَا عَذَابًا"} رَوَاهُ الشَّافِعِيُّ
وَالطَّبْرَانِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Upepo
haukuvuma kamwe, isipokuwa Nabiy (رَضِيَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipiga magoti na kusema: Ee Allaah! Ujaalie uwe Rahmah
wala Usiujaalie uwe adhabu.” [Imetolewa na Ash-Shaafi’iyy na Atw-
Twabaraaniyy]

405.

وَعَنْهُ: أَنَّهُ صَلَّى فِي زَلْزَلَةٍ سِتِّ رَكَعَاتٍ، وَأَرْبَعَ سَجَدَاتٍ،
وَقَالَ: هَكَذَا صَلَاةُ الْآيَاتِ رَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ
وَذَكَرَ الشَّافِعِيُّ عَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ مِثْلَهُ دُونَ آخِرِهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena:
“(Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)) aliswali pindi ilipotokea tetemeko la ardhi Rakaa sita na Sijdah nne, na akasema: Hivi ndivyo namna ya kuswali Swalaatul-Aayaat (Swalaah ya ishara (ya Maafa).”[9] [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy]

Na Ash-Shaafi’iyy ametaja Hadiyth ya ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kama hiyo pasi na kutaja mwisho wake.

[1] Maana ya neno hilo ‘Kusuwf’ na ‘Khusuwf’ (kushikwa kwa jua na kushikwa kwa mwezi) ni “kubadilika”. Maneno haya yaweza kuwa kinyume cha hivi.

[2] Mama yake Ibraahiym alikuwa Maria, Mmisri aliyewahi kuwa mtumwa ambaye Al-Muqawqis mtwawala wa Alexandria na Misri alimpa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kama zawadi amuo. Ibraahiym alizaliwa mnamo mwezi wa Jumaadal-Uwlaa mwaka wa 9A.H., na akafariki mnamo tarehe 29 Shawwaal mwaka 11 A.H. akiwa na umri wa miezi kumi na nane. Alizikwa Al-Baqi’, na yeye (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema kuwa: “Anaye wa kumkamilishia kunyonya kwake huko Jannah.”

[3] Siku za Jaahiliyya (kipindi kabla ya ujio wa Uislamu), watu walikuwa wakiamini kuwa kila mtu mashuhuri anapozaliwa au anapokufa, jua au mwezi hupatwa. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikanusha itikadi hii.

[4] Al-Bukhaariy na Muslim.

[5] Hoja ya kama Swalaatul-Kusuwf (Swalaah ya kupatwa kwa jua au mwezi) bora iswaliwe kwa sauti kubwa au sauti ndogo, nayo imetofautiana. Lakini kuswali kwa sauti kubwa ndiko kumethibitishwa kwa Hadiyth Marfuw’.

[6] Kinyume na Swalaah zingine, Swalaah hii ina kurukuu mara mbili kila Rakaa.

[7] Kwa mujibu wa Hadiyth Swahiyh kutangaza au kuita watu kwa ajili ya Swalaah yoyote hairuhusiwi isipokuwa Swalaatul-Kusuwf (Swalaah ya kupatwa kwa jua au mwezi).

[8] Inaeleweka kutokana na Hadiyth kuwa Khutbah hutolewa pia katika Swalaatul-Kusuwf (Swalaah ya kupatwa jua au mwezi).

[9] Hadiyth hii inatufunza kuwa, kukizuka balaa, liwe ni janga la ardhini kama tetemeko la ardhi, au kuporomoka kwa milima ya theluji na barafu, n.k; au maangamizi ya kutoka angani tufani, kimbunga cha mchanga, au kimbunga cha theluji, vinavyoathiri viumbe kwa maumivu na huzuni, watu sharti wajitume wenyewe kuswali Swalaah hii inayoitwa Swalaatul-Aayaat (Swalaah ya ishara za Allaah (عَزَّ وَجَلَّ)).

16-Mlango Wa Swalaatul-Istisqaa (Swalaah Ya Mvua)

بَابُ صَلَاةِ الْإِسْتِسْقَاءِ

406.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {خَرَجَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مُتَوَاضِعًا، مُتَبَذَّلًا، مُتَخَشِّعًا، مُتَرَسِّلًا، مُتَضَرِّعًا، فَصَلَّى رَكْعَتَيْنِ، كَمَا يُصَلِّي فِي الْعِيدِ، لَمْ يَخْطُبْ خُطْبَتَكُمْ هَذِهِ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَأَبُو عَوَانَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitoka (kwenda kuswali Swalaah ya kuomba mvua) huku akiwa mnyonge, amevaa nguo duni na katika hali ya udhalili na mnyenyekevu, anaomba du’aa. Akaswali Rakaa mbili kama za Swalaah ya ‘Iyd,[2] lakini hakukhutubu kama khutbah yenu hii.”[3] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na wakaisahihisha At-Tirmidhiy, Abuu ‘Awaanah na Ibn Hibbaan]

407.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {شَكَاَ النَّاسُ إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قُحُوطَ الْمَطَرِ، فَأَمَرَ بِمَنْبَرٍ، فَوُضِعَ لَهُ فِي الْمُصَلَّى، وَوَعَدَ النَّاسَ يَوْمًا يَخْرُجُونَ فِيهِ، فَخَرَجَ

حِينَ بَدَأَ حَاجِبُ الشَّمْسِ، فَقَعَدَ عَلَى الْمِنْبَرِ، فَكَبَّرَ وَحَمِدَ اللَّهَ، ثُمَّ قَالَ: "إِنَّكُمْ شَكَوْتُمْ جَدَبَ دِيَارِكُمْ، وَقَدْ أَمَرَكُمُ اللَّهُ أَنْ تَدْعُوهُ، وَوَعَدَكُمْ أَنْ يَسْتَجِيبَ لَكُمْ، ثُمَّ قَالَ: الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ، مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ، اَللَّهُمَّ أَنْتَ اللَّهُ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، أَنْتَ الْغَنِيُّ وَنَحْنُ الْفُقَرَاءُ، أَنْزِلْ عَلَيْنَا الْغَيْثَ، وَاجْعَلْ مَا أَنْزَلْتَ قُوَّةً وَبَلَاغًا إِلَى حِينٍ" ثُمَّ رَفَعَ يَدَيْهِ، فَلَمْ يَزَلْ حَتَّى رُئِيَ بَيَاضُ إِبْطِيهِ، ثُمَّ حَوَّلَ إِلَى النَّاسِ ظَهْرَهُ، وَقَلْبَ رِذَائِهِ، وَهُوَ رَافِعٌ يَدَيْهِ، ثُمَّ أَقْبَلَ عَلَى النَّاسِ وَنَزَلَ، وَصَلَّى رَكْعَتَيْنِ، فَأَنْشَأَ اللَّهُ سَحَابَةً، فَرَعَدَتْ، وَبَرَقَتْ، ثُمَّ أَمْطَرَتْ { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَقَالَ: "غَرِيبٌ، وَإِسْنَادُهُ حَيْدٌ"

وَقِصَّةُ التَّحْوِيلِ فِي "الصَّحِيحِ" مِنْ حَدِيثِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدٍ، وَفِيهِ: {فَتَوَجَّهَ إِلَى الْقِبْلَةِ، يَدْعُو، ثُمَّ صَلَّى رَكْعَتَيْنِ، جَهَرَ فِيهِمَا بِالْقِرَاءَةِ}

وَاللِّدَارِ قُطْنِيٍّ مِنْ مُرْسَلِ أَبِي جَعْفَرٍ الْبَاقِرِ: وَحَوْلَ رِذَائِهِ؛ لِيَتَحَوَّلَ الْقَحْطُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Watu walimlalamikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) uhaba wa mvua. Kwa hivyo akaamrisha ijengwe Mimbar, akawekewa hapo Al-Muswallaa, na akaagana na watu siku watakayotoka watu kuja hapo. Akatoka jua lilipoanza kudhihiri. Akakaa juu ya Mimbar, akapiga Takbiyra na akamhimidi Allaah, akasema: Hakika nyinyi mmelalamikia ukame wa maskani zenu, Allaah Amekuamrisheni mumuombe Yeye na Amekuahidini kuwa Atakujibuni. Kisha akasema: “Alhamdulillah, Rabb wa

ulimwengu, Ar-Rahmaan, Mwenye kurehemu, Mfalme wa siku ya malipo, hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, Hufanya Alitakalo. Ee Allaah! Wewe ni Allaah hapana mwabudiwa wa haki ila Wewe, Wewe ni Mkwasi, nasi ni mafukara. Tuteremshie mvua na Ukifanye Utakachotuteremshia kiwe nguvu na chenye kutufikisha mpaka muda (wa mwisho).” Akanyanyua mikono,[4] na akawa anazidi kuinyanyua hadi weupe wa kwapa zake unaonekana. Kisha akawapa mgongo watu, na akageuza ridaa (juba) yake ya juu huku mikono yake kainyanyua juu. Akawageukia watu, akashuka akawaswalisha Rakaa mbili. Kisha Allaah Akaanzisha wingu, radi na umeme, kisha ikanyesha mvua.” [Imetolewa na Abuu Daawuud, ambaye aliipa daraja la Ghaarib, na Isnaad yake ni nzuri]

Kisa cha kugeuza nguo kimetajwa katika Swahiyh Al-Bukhaariy kutokana na usimulizi wa ‘Abdullaah bin Zayd, na kinasema: “(Nabiy ﷺ) alielekea Qiblah huku akiomba du’aa, akaswalisha Rakaa mbili na akasoma kwa sauti.”

Na Ad-Daaraqutwniyy alisimulia vivyo hivyo katika Hadiyth Mursal iliyosimuliwa na Abuu Ja’far Al-Baaqir[5]: “(Nabiy ﷺ) aligeuza ridaa (juba) yake ili ukame ugeuke.”

408.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَجُلًا دَخَلَ الْمَسْجِدَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ، وَالنَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَائِمٌ يَخْطُبُ. فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، هَلَكْتَ الْأَمْوَالُ، وَانْقَطَعَتِ السُّبُلُ، فَادْعُ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يُغِيثُنَا، فَرَفَعَ يَدَيْهِ، ثُمَّ قَالَ: "اللَّهُمَّ اغْنِنَا، اللَّهُمَّ اغْنِنَا..." فَذَكَرَ الْحَدِيثَ، وَفِيهِ الدُّعَاءُ بِإِمْسَاكِهَا { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mtu aliingia Msikitini katika siku ya Ijumaa huku Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akiwa amesimama akikhutubia. Akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Mali imeangamia na njia zimekatika, basi muombe Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Atuletee mvua. (عَزَّ وَجَلَّ) akainua mikono yake, akasema: Ee Allaah! (Tuteremshie mvua), Ee Allaah! Tuteremshie mvua.” Msimulizi akataja Hadiyih yote, ndani yake kuna du’aa za kuzuia mvua.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

409.

وَعَنْ أَنَسٍ: { أَنَّ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ كَانَ إِذَا قَحَطُوا يَسْتَسْقِي بِالْعَبَّاسِ بْنِ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ. وَقَالَ: اللَّهُمَّ إِنَّا كُنَّا نَسْتَسْقِي إِلَيْكَ بِنَبِيِّنَا فَتَسْقِينَا، وَإِنَّا نَتَوَسَّلُ إِلَيْكَ بِعَمِّ نَبِيِّنَا فَاسْقِنَا، فَيُسْقَوْنَ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) tena amesema: “Walikuwa walipofikwa na ukame, ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alikuwa akiomba mvua[6] kwa Al-‘Abbaas bin ‘Abd Al-Mutwallib[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ), naye akasema: Ee Allaah! Tulikuwa tukikuomba kwa Nabiyy wetu, na Ukatuteremshia maji. Sasa tunakuomba kwa Ammi wa Nabiyy wetu. Kwa hivyo tunakuomba mvua. Wakawa wanateremshiwa mvua.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

410.

وَعَنْ أَنَسٍ قَالَ: {أَصَابَنَا وَنَحْنُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَطَرٌ قَالَ: فَحَسَرَ ثَوْبَهُ، حَتَّى أَصَابَهُ مِنَ الْمَطَرِ، وَقَالَ: "إِنَّهُ حَدِيثُ عَهْدٍ بِرَبِّهِ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulipata mvua wakati tulipokuwa pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ), akafunua nguo yake hadi akapata mvua ikamnyeshea na akasema: Imetoka sasa hivi kutoka kwa Rabb wake.” [Imetolewa na Muslim]

411.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا; أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا رَأَى الْمَطَرَ قَالَ: {اللَّهُمَّ صَيِّبًا نَافِعًا} أَخْرَجَاهُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipoona mvua alikuwa akisema: Ee Allah! Tumiminie mvua yenye manufaa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

412.

وَعَنْ سَعْدِ بْنِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ دَعَا فِي الْإِسْتِسْقَاءِ: {اللَّهُمَّ جَلِّلْنَا سَحَابًا، كَثِيفًا، قَصِيفًا،

دَلُوقًا، ضَحُوكًا، تُمْطِرُنَا مِنْهُ رَذَاذًا، قِطْقِطًا، سَجَلًا، يَا ذَا
الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ { رَوَاهُ أَبُو عَوَانَةَ فِي "صَحِيحِهِ"

Kutoka kwa Sa'd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliomba mvua inyeshe[8]: Ee Allaah!
Tufunike kwa mawingu mazito mengi, yenye ngurumo, ya kuteleza,
na yenye umeme na kutokea humo Utushushie mvua ya kumwagika
na ya manyunyuyu. Ee Mwenye Ujalali na Utukufu.” [Imetolewa na
Abuu ‘Awaanah katika Swahiyh yake]

413.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { خَرَجَ سُلَيْمَانُ عَلَيْهِ السَّلَامُ يَسْتَسْقِي،
فَرَأَى نَمْلَةً مُسْتَلْقِيَةً عَلَى ظَهْرِهَا رَافِعَةً قَوَائِمَهَا إِلَى السَّمَاءِ
تَقُولُ: اللَّهُمَّ إِنَّا خَلَقْنَا مِنْ خَلْقِكَ، لَيْسَ بِنَا غِنَى عَنْ سُقْيَاكَ،
فَقَالَ: ارْجِعُوا لَقَدْ سُقِيتُمْ بِدَعْوَةِ غَيْرِكُمْ } رَوَاهُ أَحْمَدُ وَصَحَّحَهُ
الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:
“Sulaymaan (عَلَيْهِ السَّلَامُ) alitoka kuenda kuomba mvua,
akamuona sisimizi amelala chali huku amenyanyua miguu yake
mbinguni akisema:[9] “Ee Allaah! Sisi ni miongoni mwa viumbe
Wako, na hatuwezi kuishi bila mvua Yako.” Akasema (kuwaambia
Maswahaba): “Rudini, kwani mumenyeshewewa kwa du’aa za
wengine.” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Al-Haakim]

414.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
اسْتَسْقَى فَأَشَارَ بِظَهْرِهِ كَفَّيْهِ إِلَى السَّمَاءِ { أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliomba mvua, akaashiria kwa
nyuma ya viganja[10] vyake kuelekea angani.” [Imetolewa na
Muslim]

[1] Maana ya kifasihi ya Istisqaa ni “Kutafuta au kuomba maji.” Katika lugha ya ki Shariy’ah, hutumika kuuswalisha mkusanyiko maalumu ambamo du’aa huombwa ya kuomba mvua. Ziko aina tatu za Istisqaa: (a) Adnaa (ndogo kuliko zote), (b) Awsatw (ya kati), (c) A’alaa (kubwa kuliko zote). Adnaa inamaanisha maombi ya mdomo tu. Awsatw ni maombi ya mdomo katika jamaa baada ya kuswali Swalaah ya Faradhi. A’alaa inahitaji Swalaah maalumu ya jamaa kuomba mvua. Mchakato sahihi wa kuswali Istisqaa ni kuswali Rakaa mbili. Kisomo kiwe kwa sauti kubwa, kikifuatiwa na Khutbah mbili, na mwishowe du’aa iombwe kwa kuelekea Qiblah.

[2] Kuna tofauti ya idadi na mfululizo wa kutamka Takbiyra kati ya Swalaah ya ‘Iyd na Swalaah ya Istisqaa. Khutbah ni sharti ifuatie Swalaah ya Istisqaa, kwa namna ile ile kama katika Swalaah ya ‘Iyd.

[3] Maneno yale yasemayo, “Hakutoa aina yako ya Khutbah” inaashiria kuwa haikuwa Khutbah yake ndefu na ya kuchosha. Shah Waliyullaah katika kitabu chake ‘Hujjatullaahil-Baalighah’ amesema kuwa ziko njia nyingi za Istisqaa ambazo zimehusishwa na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Njia nzuri kuliko zote ambazo watu wanaweza kuzifuata ni kuwa watu wote wakusanyike msituni na Imaam; wawe wamevaa nguo za marapurapu, na wamuombe Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) huku wakilia machozi na nyoyo zilizojaa huzuni. Kisha Imaam aswalishe Swalaah yenye Rakaa mbili kwa kisomo cha sauti kubwa. Baada ya Swalaah, Imaam atoe

Khutbah, kwa kumuomba Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) wakati uso wake umeelekea Qiblah, na kisha ageuze ridaa (juba) lake ndani nje.

[4] Kwa hivyo tunafahamishwa kuwa, katika Swalaah ya Istisqaa, du'aa zisomwe huku mikono imenyanyuliwa juu. Imaam An-Nawawi amekusanya Hadiyth ishirini juu ya jambo hili. Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia kuwa hakuwahi kamwe kumuona Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akinyanyua mikono yake katika du'aa zozote isipokuwa hizo za Istisqaa. Hii inadhihirisha ukweli kwamba hakuwahi kumuona Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akinyanyua mikono yake juu sana katika Swalaah yoyote ile isipokuwa hiyo ya Istisqaa.

[5] Abuu Ja'far Al-Baaqir ndiye Muhamaad Al-Baaqir bin 'Aliy Zainul-'Aabidiyn bin Husayn bin 'Aliy bin Abiy Twaalib, Aliitwa Baaqir kwa ajili ya 'Ilmu au ujuzi wake mpana. Alizaliwa mnamo mwaka 56 A.H. na akafa mnamo mwaka 117 A.H. akiwa na umri wa miaka 63, na akazikwa Al-Baqi'.

[6] Hadiyth hii inadhihirisha kwamba, inafaa kuwataka watu wenye taqwa walio hai watuombe du'aa za Istisqaa, na wala siyo watu waliokwisha kufa. Watu wengi wanaamini kuwa du'aa zinaweza kuombwa kupitia kwa wafu, kwa kuwafanya wao wawe mapitio. Hivi ni kumshirikisha Allaah (رَضِيَ) Ingekuwa ni sahihi kuomba kwa kupitia wafu, Umar (رَضِيَ) asingemuomba 'Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuwaombea du'aa badala ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[7] Al-'Abbaas bin Abd Al-Mutwallib ndiye Ammi yake Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ) na alipewa jina la Abul-Fadhwl. Alikuwa ndiye anayewapa maji mahujaji Makkah na ujenzi wa Ka'bah. Alihudhuria Bay'atul-'Aqabah (mkataba 'Aqabah) kuhakikisha Maanswaar walikuwa waaminifu na wakweli katika ahadi zao, alikuwa hajawa Muislam hadi wakati ule. Alikamatwa pamoja na makafiri katika vita vya Badr, akasilimu kabla ya kuiteka Makkah, naye alishiriki kuiteka, alisimama imara katika vita vya Hunayn. Alikufa mwezi wa Rajab au Ramadhwaan mwaka 32 A.H. na akazikwa Al-Baqi'.

[8] Du'aa nyingi kuhusu Istisqaa zimeripotiwa kutoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na hii ni mojawapo.

[9] Mtindo wa kuwachukua wanyama katika Swalaah ya Istisqaa imethibitishwa kupitia Hadiyth hii. Kwa kuwa Allaah pengine Anaweza kuzikubali du'aa zao.

[10] Wanazuoni wanasema, iwapo du'aa itaombwa ili kupata Baraka za Allaah, mtu sharti anyanyue mikono yake kuomba du'aa kama kawaida (viganja viwe vinamwelekea huyo muombaji du'aa katika Swalaah hiyo). Lakini ikiwa du'aa inaombwa kuliepusha jambo ovu, mnyanyuo wa mikono sharti ugeuzwe (mikono inyanuyuliwe, na viganja vikielekea nje). Inaelekea kuwa Allaah Ageuze ile hali. Kule kugeuza ridaa (juba) ndani kuwe nje pia kunamaanisha hivyo hivyo; na hali kadhalika tendo la kuelekeza nyuma ya viganja nje inaashiria ni kuomba Allaah Ayasogeze mawingu chini (yakiwa yamejaa maji).

17-Mlango Wa Adabu Za Mavazi

بَابُ اللَّبَّاسِ

17-Mlango Wa Adabu Za Mavazi

415.

عَنْ أَبِي عَامِرٍ الْأَشْعَرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَيَكُونَنَّ مِنْ أُمَّتِي أَقْوَامٌ يَسْتَحِلُّونَ الْحَرَ وَالْحَرِيرَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَأَصْلُهُ فِي الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Abuu 'Aamir Al-Ash'ariyy[1] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah amesema: “Kutakuwepo miongoni mwa ummah wangu watu

watakaohalalisha zinaa pamoja na hariri.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na chanzo chake^[2] kimo katika Al-Bukhaariy]

416.

وَعَنْ حُذَيْفَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ نَشْرَبَ فِي أَنْيَةِ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ، وَأَنْ نَأْكُلَ فِيهَا، وَعَنْ لُبْسِ الْحَرِيرِ وَالذِّيْبَاجِ، وَأَنْ نَجْلِسَ عَلَيْهِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Khudhayfah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ametukataza kunywa katika vyombo vya dhahabu na fedha, na kula humo na kuvaa hariri na ad-diybaaj (vitambaa vya hariri vya vito na vilotariziwa kwa dhahabu na fedha) na kukaa juu yake.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

417.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ لُبْسِ الْحَرِيرِ إِلَّا مَوْضِعَ إصْبَعَيْنِ، أَوْ ثَلَاثٍ، أَوْ أَرْبَعٍ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuvaa hariri isipokuwa sehemu ya vidole viwili, vitatu au vinne.”^[3] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

418.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {رَخَّصَ لِعَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَوْفٍ، وَالزُّبَيْرِ فِي قَمِيصِ الْحَرِيرِ، فِي سَفَرٍ، مِنْ حَكَّةٍ كَانَتْ بِهِمَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaruhusu ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Awf na Az-Zubayr[4] wavae kanzu za hariri katika safari kwa sababu ya upele wa kuwashwa ngozi waliokuwa nao.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

419.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَسَانِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حُلَّةً سِيرَاءً، فَخَرَجْتُ فِيهَا، فَرَأَيْتُ الْغَضَبَ فِي وَجْهِهِ، فَشَقَّقْتُهَا بَيْنَ نِسَائِي} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَهَذَا لَفْظُ مُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alinipa mie juba lenye mistari[5] yenye hariri, halafu nikalivaa, nikaona ghadhabu usoni mwake, nililikatakata (na kuligawa) baina ya ahli zangu wanawake.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

420.

وَعَنْ أَبِي مُوسَى رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَحْلَ الذَّهَبُ وَالْحَرِيرُ لِنَاثِ أُمَّتِي، وَحُرِّمَ عَلَى ذُكُورِهِمْ.} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Abuu Muwsaa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Dhahabu na hariri vimeruhusiwa kwa wanawake wa Ummah wangu, na vimekatazwa kwa wanaume wao.” [Imetolewa na Ahmad, An-Nisaa'iy na At-Tirmidhiy, naye aliisahihisha]

421.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا; أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ إِذَا أَنْعَمَ عَلَى عَبْدٍ أَنْ يَرَى أَثَرَ نِعْمَتِهِ عَلَيْهِ} رَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah Anapomneemesha mja Wake hupenda kuona athari ya neema yake juu yake.”[6] [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy]

422.

وَعَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {نَهَى عَنْ لُبْسِ الْقَسِيِّ وَالْمُعْصَفْرِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuvaa hariri na nguo zenye rangi ya zaafarani. [Imetolewa na Muslim]

423.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، قَالَ: {رَأَى عَلِيَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ثَوْبَيْنِ مُعْصَفَرَيْنِ، فَقَالَ: "أُمُّكَ أَمَرَتْكَ بِهَذَا؟"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliniona mimi nikiwa nimevaa nguo mbili za rangi ya zaafarani, akasema: “Mama yako ndiye aliyekuamrisha ufanye hivi?”[7] [Imetolewa na Muslim]

424.

وَعَنْ أَسْمَاءَ بِنْتِ أَبِي بَكْرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {أَنَّهَا أَخْرَجَتْ جُبَّةَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَكْفُوفَةَ الْجَيْبِ وَالْكُمَيْنِ وَالْفَرْجَيْنِ، بِالْذِّيَّاجِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَأَصْلُهُ فِي "مُسْلِمٍ"، وَزَادَ: {كَانَتْ عِنْدَ عَائِشَةَ حَتَّى قُبِضَتْ، فَقَبِضْتُهَا، وَكَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَلْبِسُهَا، فَخُنْ نَغْسِلُهَا لِمَرْضَى نَسْتَشْفِي بِهَا}

وَزَادَ الْبُخَارِيُّ فِي "الْأَدَبِ الْمُفْرَدِ". {وَكَانَ يَلْبَسُهَا لِلْوَفْدِ
وَالْجُمُعَةِ}

Kutoka kwa Asmaa bint Abiy Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Yeye alilitoa joho la Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) lililokuwa limedariziwa kwa hariri nzito mifukoni, mikononi na sehemu mbili zilizo wazi.”[8] [Imetolewa na Abuu Daawuwd]

Na chanzo chake kimo katika Swahiyh Muslim na kina nyongeza: “Lilikuwa kwa ‘Aaishah hadi alipokufa, nikalichukua mimi. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akilivaa, nasi tulikuwa tukiliosha kwa ajili ya wagonjwa waliokuwa wakilitumia kwa kuponywa nalo.”

Na Al-Bukhaariy aliongezea katika kitabu Adab Al-Mufrad[9]: “Alikuwa akilivaa kwa ajili ya wageni[10] na siku za Ijumaa.” [Imetolewa na Muslim]

[1] Abuu ‘Aamir Al-Ash’ariyy ndiye anayeitwa ‘Abdullaah bin Haaniy au ‘Ubayd bin Wahaab. Alikuwa ni Swahaba aliyelowea Sham, na alikuwa wakati wa utawala wa ‘Abdul Maalik bin Marwaan.

[2] Inamaanisha kwamba, watakuwa wakivaa mavazi ya hariri na watakuwa wanatenda zinaa kwa wingi sana ikiwa vitu hivi havitaharamishwa.

[3] Uvaaji wa mavazi ya hariri umekatazwa kwa wanaume. Hata hivyo inaruhusiwa kwa wanaume kuvaa vazi lenye msitari usiozidi sentimita tano hadi kumi. Lakini inaruhusiwa kwa mwanaume kuvaa vazi la hariri iwapo ana maradhi ya kuwashwa ngozi yaani eczema, n.k., au iwapo anashambuliwa na chawa. Kwa kuwa mavazi ya hariri humsaidia mtu anayeumwa magonjwa kama hayo, wanaruhusiwa kuendelea kuyatumia mpaka wapone.

[4] Az-Zubayr hyu ndiye Az-Zubayr bin Al-‘Awwaam bin Khuwaylid bin Asad Al-Qurayshiy Al-Asad, ambaye Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه) alimwita mwenyewe kuwa ni mfuasi mtiifu wake. Ni mtoto wa Swafiyyah bint Abdil-Muttwalib shangazi yake Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). Zubayr ni miongoni mwa Maswahaba kumi waliobashiriwa Jannah. Alikuwa ni miongoni mwa mashujaa katika vita vya Kiislamu. Alifariki mwaka 36H baada ya kurejea kutoka vita vya Al-Jamal.

[5] Vazi hili alipewa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na Mfalme wa jimbo la Aila. Lilikuwa na taraza (nakshi) za nyuzi za dhahabu na hariri.

[6] Hii inaweka wazi kwamba, kula chakula kizuri na kuvaa nguo nzuri sio dhidi ya taqwa. Kwa mujibu wa Hadiyth kwamba Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) Anapenda uzuri na usafi. Imepokelewa kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mas’uwd (رضي الله عنه) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ((Hatoingia Jannah ambaye moyoni mwake mna kiburi uzito wa chembe (au sisimizi)). Mtu mmoja akauliza: “Mtu hupenda nguo yake iwe nzuri na viatu vyake viwe vizuri [itakuwaje?]” Akasema: ((Hakika Allaah ni Mzuri Anapenda Uzuri. Kiburi ni kukataa haki na kudharau watu)). [Muslim]

[7] Hadiyth yote inasema hivi: “‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) alimuomba ruhusa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuenda kuliosha lile vazi. Jibu lake (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikanusha, na akamuamrisha alichome, ambayo bila shaka ni adhabu.”

[8] Diybaaj ni hariri nzito iliyotariziwa kwa dhahabu.

[9] Hili ndilo jina la kitabu kilichoandikwa na Imaam Al-Bukhaariy.

[10] Hii inathibitisha kuwa, kuvaa mavazi mazuri inaruhusiwa siku za Ijumaa, na katika ‘Iyd zote mbili, na katika hadhara za watu.

03-Kitabu Cha Jeneza (Vifo Na Maziko) - كِتَابُ الْجَنَائِزِ

00-Kitabu Cha Jeneza

425.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَكْثَرُ مَا ذَكَرَ هَازِمُ اللَّذَاتِ: الْمَوْتُ } رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Zidisheni kukumbuka kikatisha ladha, yaani kifo.”^[1] [Imetolewa na At-Tirmidhiy, na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

426.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا يَتَمَنَّيَنَّ أَحَدُكُمْ الْمَوْتَ لِيُضْرَّ بِهٖ، فَإِنْ كَانَ لَا بُدَّ مُتَمَنَّيًّا فَلْيَقُلْ: اَللّٰهُمَّ اَحْيِنِيْ مَا كَانَتْ اَلْحَيَاةُ خَيْرًا لِّيْ، وَتَوَفَّنِيْ اِذَا كَانَتْ اَلْوَفَاةُ خَيْرًا لِّيْ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asitamani mmoja wenu mauti[2] kwa sababu ya kufikwa na madhara, ikiwa hana budi kutamani, basi aseme:

اَللّٰهُمَّ اَحْيِنِيْ مَا كَانَتْ اَلْحَيَاةُ خَيْرًا لِّيْ، وَتَوَفَّنِيْ اِذَا كَانَتْ اَلْوَفَاةُ خَيْرًا لِّيْ

Ee Allaah! Nipe uhai, ikiwa uhai ni kheri kwangu, na Unifishe ikiwa mauti hayo ni kheri kwangu.”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim]

427.

وَعَنْ بُرَيْدَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { اَلْمُؤْمِنُ يَمُوتُ بِعَرَقِ الْجَبِينِ } رَوَاهُ اَلثَّلَاثَةُ وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Buraydah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muumini hufa na jasho[4] katika paji la uso wake.” [Imetolewa na Ath-Thalaathah (At-

Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

428.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ وَأَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَقِّنُوا مَوْتَكُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ، وَالْأَرْبَعَةُ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd na Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا)
wamesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
amesema: “Watamkieni wafu wenu “*Laa Ilaaha Illa Allaah*” (hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah).” [Imetolewa na Muslim na Al-Arba'ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah)]

429.

وَعَنْ مَعْقِلِ بْنِ يَسَارٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {اقْرَأُوا عَلَى مَوْتَكُمْ يَس} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ma'qil bin Yasaar[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wasomeni wafu wenu Suwrah Yaasiyn.”[6] [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

430.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {دَخَلَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى أَبِي سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ وَقَدْ شَقَّ بَصَرُهُ فَأَغْمَضَهُ، ثُمَّ قَالَ: "إِنَّ الرُّوحَ إِذَا قُبِضَ، اتَّبَعَهُ الْبَصَرُ" فَضَجَّ نَاسٌ مِنْ أَهْلِهِ، فَقَالَ: "لَا تَدْعُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ إِلَّا بِخَيْرٍ. فَإِنَّ الْمَلَائِكَةَ تُوَمِّنُ عَلَى مَا تَقُولُونَ". ثُمَّ قَالَ: "اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِأَبِي سَلَمَةَ، وَارْفَعْ دَرَجَتَهُ فِي الْمَهْدِيِّينَ، وَافْسَحْ لَهُ فِي قَبْرِهِ، وَنَوِّرْ لَهُ فِيهِ، وَاخْلُفْهُ فِي عَقِبِهِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliingia kwa Abuu Salamah[7] alipofariki huku macho yake yakingali wazi, akayafumba na akasema: “Hakika roho inapochukuliwa, jicho huifuata.”[8] Baadhi ya ahli wake wakalia na kupiga mayowe, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Msijiombee du’aa yoyote isipokuwa kheri, kwani Malaika huitikia Aamiyn kwa mnayoyasema.” Kisha akasema: “Ee Allaah! Mghufirie Abuu Salamah dhambi zake, pandisha daraja yake miongoni mwa walioongoka, mkunjulie katika kaburi lake, na mpe nuru ndani yake,

na mpe warithi katika vizazi vyake vilivyobakia.” [Imetolewa na Muslim]

431.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا: { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حِينَ تُؤَفِّي سَجِّي بِبُرْدٍ حَبْرَةٍ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipofariki, alifunikwa na nguo iliyokuwa na mistari.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

432.

وَعَنْهَا { أَنَّ أَبَا بَكْرٍ الصِّدِّيقَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَبْلَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعْدَ مَوْتِهِ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema tena kuwa: “Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimbusu[9] Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipofariki.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

433.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {نَفْسُ الْمُؤْمِنِ مُعَلَّقَةٌ بِدَيْنِهِ، حَتَّى يُقْضَى عَنْهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Roho ya Muumini imeunganishwa na deni[10] mpaka alipiwe.”[11] [Imetolewa na Ahmad na At-Tirmidhiy, na waliipa daraja la Hasan]

434.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ فِي الَّذِي سَقَطَ عَنْ رَاِحِلَتِهِ فَمَاتَ: {اغْسِلُوهُ بِمَاءٍ وَسِدْرٍ، وَكَفَّنُوهُ فِي ثَوْبَيْنِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu mtu aliyeanguka kutoka juu ya mnyama wake na akafariki: “Muosheni kwa maji na mkunazi[12] na mumvishe sanda[13] ya nguo zake mbili.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

435.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {لَمَّا أَرَادُوا غَسْلَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالُوا: وَاللَّهِ مَا نَذْرِي، نُجَرِّدُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَمَا نُجَرِّدُ مَوْتَانَا، أَمْ لَا؟.....} الْحَدِيثَ، رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Watu walipotaka kumuosha Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) walisema: “Wa-Allaahi hatujui kama tumvue nguo zote Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kama tunavyo wavua nguo wafu wetu.”[14] [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud]

436.

وَعَنْ أُمِّ عَطِيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {دَخَلَ عَلَيْنَا النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَنَحْنُ نَغْسِلُ ابْنَتَهُ، فَقَالَ: "اغْسِلْنَهَا ثَلَاثًا، أَوْ خَمْسًا، أَوْ أَكْثَرَ مِنْ ذَلِكَ، إِنْ رَأَيْتُنَّ ذَلِكَ، بِمَاءٍ وَسِدْرٍ، وَاجْعَلْنَ فِي الْأُخْرَةِ كَافُورًا، أَوْ شَيْئًا مِنْ كَافُورٍ"،

فَلَمَّا فَرَغْنَا أَذْنَاهُ، فَأَلْقَى إِلَيْنَا حِقْوَهُ فَقَالَ: "أَشْعِرْنَهَا إِيَّاهُ" {
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ: {ابْدَأْ بِمِيَامِنِهَا وَمَوَاضِعِ الْوُضُوءِ مِنْهَا}
وَفِي لَفْظٍ لِلْبُخَارِيِّ: {فَضَفَّرْنَا شَعْرَهَا ثَلَاثَةَ قُرُونٍ، فَأَلْقَيْنَاهُ
خَلْفَهَا}

Kutoka kwa Ummu ‘Atwiyyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema:

“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliingia tukiwa tunamuosha binti yake, akasema: “Muosheni kwa maji na mkunazi mara tatu au tano[15] au zaidi ya hivyo mkiona inafaa, na katika mara ya mwisho mtieni kaafuwraa au sehemu ya kaafuwraa.” Tulipomaliza tukamuarifu naye akatutupia kikoi chake, akasema: “Mzungushieni nalo hilo mwilini mwake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyengine: “Anzeni na kuliani kwake na sehemu za kutawadhwa.”

Na katika tamshi la Al-Bukhaariy: “Tulisuka nywele zake mikia mitatu na tukaiweka nyuma ya mgongo wake.”

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كُفِّنَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي ثَلَاثَةِ أَثْوَابٍ بَيْضَ سَحُولِيَّةٍ مِنْ كُرْسُفٍ، لَيْسَ فِيهَا قَمِيصٌ وَلَا عِمَامَةٌ.} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikafiniwa kwa mavazi matatu meupe ya kitambaa cha Sahuwliyyah[16] ambazo miongoni mwake hamkuweko kanzu wala kilemba.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

438.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {لَمَّا تُوفِّيَ عَبْدُ اللَّهِ بْنُ أَبِي جَاءٍ ابْنُهُ إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ . فَقَالَ: أَعْطِنِي قَمِيصَكَ أَكْفَنُهُ فِيهِ، فَأَعْطَاهُ إِيَّاهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Alipofariki ‘Abdullaah bin Ubayy[17] mwanawe[18] alikuja kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na akasema: Nipe kanzu yako nikamkafinie nayo, akampa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

439.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الْبَسُوا مِنْ ثِيَابِكُمُ الْبَيَاضَ، فَإِنَّهَا مِنْ خَيْرِ ثِيَابِكُمْ، وَكَفَّنُوا فِيهَا مَوْتَكُمْ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Vaeni nguo zenu nyeupe kwani ni miongoni mwa nguo zenu nzuri zaidi, na muwakafinieni wafu wenu.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

440.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا كَفَّنَ أَحَدُكُمْ أَخَاهُ فَلْيُحْسِنْ كَفَنَهُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu akimkafini nduguye sharti amkafini kwa sanda nzuri.”[19] [Imetolewa na Muslim]

441.

وَعَنْهُ قَالَ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَجْمَعُ بَيْنَ
الرَّجُلَيْنِ مَنْ قَتَلَى أَحَدٍ فِي ثَوْبٍ وَاحِدٍ، ثُمَّ يَقُولُ: "أَيُّهُمْ أَكْثَرُ
أَخْذًا لِلْقُرْآنِ؟"، فَيَقْدِّمُهُ فِي اللَّحْدِ، وَلَمْ يُغَسَّلُوا، وَلَمْ يُصَلَّ
عَلَيْهِمْ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena: “Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akikusanya baina ya watu
wawili waliouawa Uhud katika nguo moja,[20] halafu akasema:
“Nani kati yao alijua Qur-aan zaidi?” Kisha akamtanguliza kwenye
mwanandani, hawakuoshwa wala hawakuswaliwa.” [Imetolewa na
Al-Bukhaariy]

442.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {سَمِعْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: "لَا تُغَالُوا فِي الْكَفَنِ، فَإِنَّهُ يُسَلَبُ سَرِيعًا"}
رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nimemsikia
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: Msifanye
israafu katika sanda, kwani itaoza haraka.” [Imetolewa na Abuu
Daawuud]

443.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا ، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لَهَا: {لَوْ مِتُّ قَبْلِي فَعَسَلْتُكَ} الْحَدِيثَ. رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia: “Endapo utafariki kabla yangu, Mimi nitakuosha.”[21] [Imetolewa na Ahmad na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

444.

وَعَنْ أَسْمَاءَ بِنْتِ عُمَيْسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا: {أَنَّ فَاطِمَةَ عَلَيْهَا السَّلَامُ أَوْصَتْ أَنْ يُغَسَّلَهَا عَلِيُّ رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ

Kutoka kwa Asmaa bint ‘Umayy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Faatiimah[22] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) aliusia kuwa ‘Aliy[23]

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) ndiye amuoshe yeye (endapo atafariki kabla yake).” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy]

445.

وَعَنْ بُرَيْدَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي قِصَّةِ الْغَامِدِيَّةِ الَّتِي أَمَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِرَجْمِهَا فِي الزَّانَا قَالَ: {ثُمَّ أَمَرَ بِهَا فَصُلِّيَ عَلَيْهَا وَدُفِنَتْ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Buraydah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia habari ya mwanamke wa Ghaamid ambaye Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliamrisha apigwe mawe kwa sababu ya zinaa. Akasema: “Kisha Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliamrisha aswaliwe[24] na akazikwa.” [Imetolewa na Muslim]

446.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {أَتَى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِرَجُلٍ قَتَلَ نَفْسَهُ بِمَشَاقِصٍ، فَلَمْ يُصَلَّ عَلَيْهِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Maiti ya mtu aliyejiua kwa mshale wenye kichwa butu ililetwa
mbele ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), hakumswalia.”[25]
[Imetolewa na Muslim]

447.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي قِصَّةِ الْمَرْأَةِ الَّتِي كَانَتْ
تَقُمُّ الْمَسْجِدَ قَالَ: {فَسَأَلَ عَنْهَا النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
فَقَالُوا: مَاتَتْ، فَقَالَ: "أَفَلَا كُنْتُمْ آذَنْتُمُونِي" ؟ فَكَانَتْهُمْ صَغُرُوا
أَمْرَهَا فَقَالَ: "دُلُونِي عَلَى قَبْرِهَا"، فَدَلُّوهُ، فَصَلَّى عَلَيْهَا {
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ .

وَزَادَ مُسْلِمٌ، ثُمَّ قَالَ: {إِنَّ هَذِهِ الْقُبُورَ مَمْلُوءَةٌ ظُلْمَةً عَلَى
أَهْلِهَا، وَإِنَّ اللَّهَ يُنَوِّرُهَا لَهُمْ بِصَلَاتِي عَلَيْهِمْ }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuhusu
mwanamke aliyekuwa akifagia Msikiti: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
aliuliza khabari zake. Maswahaba wakamuambia
amefariki. Akasema: “Kwa nini hamkuniarifu?” Ikaonekana kana
kwamba waliona jambo lake ni dogo. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
akasema: “Nijulisheni kaburi lake.” Wakamjulisha na
akamswalia.”[26] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Naye Muslim aliongezea: “Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Makaburi haya yamejaa giza kwa waliomo humo. Allaah Atayatia nuru kwa Swalaah yangu niliyowaswalia.”

448.

وَعَنْ حُذَيْفَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
كَانَ يَنْهَى عَنِ النَّعْيِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ

Kutoka kwa Hudhayfah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akikataza kutangaza[27] vifo.” [Imetolewa na Ahmad na At-Tirmidhiy, aliyeipa daraja la Hasan]

449.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
نَعَى النَّجَاشِيَّ فِي الْيَوْمِ الَّذِي مَاتَ فِيهِ، وَخَرَجَ بِهِمْ مِنَ
الْمُصَلَّى، فَصَفَّ بِهِمْ، وَكَبَّرَ عَلَيْهِ أَرْبَعًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitangaza kifo cha An-Najaashiy[28] siku alipofariki, akatoka na watu hadi kwenye Muswalla (uwanja wa kuswalia), akawapanga katika safu, na akapiga Takbiyr mara nne.”[29] [Al-Bukhaariy, Muslim]

450.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: سَمِعْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {مَا مِنْ رَجُلٍ مُسْلِمٍ يَمُوتُ، فَيَقُومُ عَلَى جَنَازَتِهِ أَرْبَعُونَ رَجُلًا، لَا يُشْرِكُونَ بِاللَّهِ شَيْئًا، إِلَّا شَفَعَهُمُ اللَّهُ فِيهِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa
Nimemsikia Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema:
“Muislamu yeyote anapofariki na wakasimama watu arubaini wasio mshirikisha Allaah na chochote wakamswalia, Allaah Atawakubali wawe waombezi[30] wake.” [Imetolewa na Muslim]

451.

وَعَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {صَلَّيْتُ وَرَاءَ
النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى امْرَأَةٍ مَاتَتْ فِي نَفْسِهَا، فَقَامَ
وَسَطَهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Samurah bin Jundub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Niliswali nyuma ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
kumswalia mwanamke aliyefariki baada ya uzazi. Alisimama katikati
ya mwili wake.”[31] [Al-Bukhaariy, Muslim]

452.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {وَاللَّهُ لَقَدْ صَلَّى رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى ابْنِي بَيْضَاءَ فِي الْمَسْجِدِ}
رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswalia maiti wa wana
wawili wa Baydhwaa[32] Msikitini.”[33] [Imetolewa na Muslim]

453.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبِي لَيْلَى قَالَ: {كَانَ زَيْدُ بْنُ أَرْقَمَ يُكَبِّرُ عَلَى جَنَائِزِنَا أَرْبَعًا، وَإِنَّهُ كَبَّرَ عَلَى جَنَازَةِ خُمْسًا، فَسَأَلْتُهُ فَقَالَ: كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُكَبِّرُهَا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَالْأَرْبَعَةُ

Kutoka kwa ‘Abdur-Rahmaan bin Abuu Laylah[34] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Zayd bin Arqam alikuwa akitamka Takbiyr mara nne wakati wa kuwaswalia maiti wao, lakini mara moja aliwahi kutamka mara tano[35] katika kumswalia maiti mmoja.

Nilipomuuliza alisema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitamka Takbiyr hizo.” [Imetolewa na Muslim na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah)]

454.

وَعَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ كَبَّرَ عَلَى سَهْلِ بْنِ حُنَيْفٍ سِتًّا، وَقَالَ: إِنَّهُ بَدْرِي} رَوَاهُ سَعِيدُ بْنُ مَنْصُورٍ وَأَصْلُهُ فِي "الْبُخَارِيِّ"

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nilitamka Takbiyr mara sita katika kuiswalia maiti ya Sahl bin Hunayf.[36] Alikuwa ni mmoja wa Maswahaba waliopigana Vita vya Badr.” [Imetolewa na Sa’iyd bin Manswuwr na chanzo chake ni Al-Bukhaariy]

455.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُكَبِّرُ عَلَى جَنَائِزِنَا أَرْبَعًا وَيَقْرَأُ بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ فِي التَّكْبِيرَةِ الْأُولَى} رَوَاهُ الشَّافِعِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitamka Takbiyr mara nne katika Swalaah za maiti wetu na akawa anasoma Faatihatul-Kitaab (kifunguzi cha Kitaab - Suwratul-Faatihah)[37] baada ya Takbiyr ya kwanza.” [Imetolewa na Ash-Shafi’iyy kwa Isnaad dhaifu]

456.

وَعَنْ طَلْحَةَ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَوْفٍ قَالَ: {صَلَّيْتُ خَلْفَ ابْنِ عَبَّاسٍ عَلَى جَنَازَةٍ، فَقَرَأَ فَاتِحَةَ الْكِتَابِ فَقَالَ: "لِتَعْلَمُوا أَنَّهَا سُنَّةٌ"} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Twalhah bin ‘Abdillaah bin ‘Awf[38] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Niliswali nyuma ya Ibn ‘Abbaas Swalaah ya

jeneza na akasoma Faatihatul-Kitaab (kifunguzi cha Kitabu – Suwratul-Faatihah) kisha akasema: Nilifanya hivyo ili wajue kuwa hiyo ni Sunnah.”[39] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

457.

وَعَنْ عَوْفِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {صَلَّى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى جَنَازَةٍ، فَحَفِظْتُ مِنْ دُعَائِهِ: "اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهُ، وَارْحَمْهُ وَعَافِهِ، وَاعْفُ عَنْهُ، وَأَكْرِمْ نُزُلَهُ، وَوَسِّعْ مَدْخَلَهُ، وَاغْسِلْهُ بِالْمَاءِ وَالتَّلْجِ وَالْبَرَدِ، وَنَقِّهِ مِنَ الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الْأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ، وَأَبْدِلْهُ دَارًا خَيْرًا مِنْ دَارِهِ، وَأَهْلًا خَيْرًا مِنْ أَهْلِهِ، وَأَدْخِلْهُ الْجَنَّةَ، وَفِيهِ فِتْنَةُ الْقَبْرِ وَعَذَابُ النَّارِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Awf bin Maalik[40] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:

“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimswalia maiti nami nikakariri du’aa yake:[41]

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهُ، وَارْحَمْهُ وَعَافِهِ، وَاعْفُ عَنْهُ، وَأَكْرِمْ نُزُلَهُ، وَوَسِّعْ مَدْخَلَهُ، وَاغْسِلْهُ بِالْمَاءِ وَالتَّلْجِ وَالْبَرَدِ، وَنَقِّهِ مِنَ

الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ التُّوبَ الْأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ، وَأَبْدَلَهُ دَارًا
خَيْرًا مِنْ دَارِهِ، وَأَهْلًا خَيْرًا مِنْ أَهْلِهِ، وَأَدْخَلَهُ الْجَنَّةَ، وَقِهِ
فِتْنَةَ الْقَبْرِ وَعَذَابَ النَّارِ

Allaahumma-ghfir lahu warham-hu, wa 'aafihi wa'-fu 'anhu, wa
akrim nuzulahu, wa wassi' mudkhalahu, waghsilhu bilmaai wath-
thalji walbaradi, wanaqqihi minal-khatwaayaa kamaa naqqaytath-
thawbal abyadhwa minad-danas, wa abdilhu daaran khayran min
daarihi, wa ahlan khayran min ahlihi, wa adkhilhul-Jannah, waqihi
fitnatal-qabri wa 'adhaaban-naar

Eee Allaah, Mghufurie na Mrehemu, na Muafu na Msamehe na
Mkirimu kushuka kwake (kaburini) na Mpanulie kuingia kwake, na
Muoshe na maji na kwa theluji na barafu na mtakase dhambi kama
vazi jeupe linavyotakaswa uchafu wake na Mbadilishie nyumba bora
kuliko nyumba yake na ahli bora kuliko ahli zake, na Muingize
Jannah na Mkinge na adhabu ya kaburi na adhabu ya Moto. "[42]
[Imetolewa na Muslim]

458.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا صَلَّى عَلَى جَنَازَةٍ يَقُولُ: "اللَّهُمَّ
اغْفِرْ لِحَيِّنَا، وَمَيِّتِنَا، وَشَاهِدِنَا، وَغَائِبِنَا، وَصَغِيرِنَا، وَكَبِيرِنَا،
وَذَكَرِنَا، وَأَنْتَانَا، اللَّهُمَّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنَّا فَأَحْيِهِ عَلَى الْإِسْلَامِ،

وَمَنْ تَوَفَّيْتَهُ مِنَّا فَتَوَفَّهُ عَلَى الْإِيمَانِ، اللَّهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا أَجْرَهُ،
وَلَا تُضِلَّنَا بَعْدَهُ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ، وَالْأَرْبَعَةُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliposwalia maiti, aliomba
du’aa hii:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِحَيِّنَا وَمَيِّتِنَا وَشَاهِدِنَا، وَغَائِبِنَا، وَصَغِيرِنَا
وَكَبِيرِنَا، وَذَكَرِنَا وَأُنْثَانَا. اللَّهُمَّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنَّا فَأَحْيِهِ عَلَى
الْإِسْلَامِ، وَمَنْ تَوَفَّيْتَهُ مِنَّا فَتَوَفَّهُ عَلَى الْإِيمَانِ، اللَّهُمَّ لَا
تَحْرِمْنَا أَجْرَهُ، وَلَا تُضِلَّنَا بَعْدَهُ

*Allaahumma-ghfir li-hayyinaa wa mayyitinaa, wa shaahidinaa, wa
ghaaibinaa, wa swaghiyrinaa, wa kabiyrinaa, wa dhakarinaa, wa
unthaanaa. Allaahumma man ahyaytahu minnaa fa Ahyihi ‘alal-
Islaami, waman tawaffaytahu minnaa fatawaffahu ‘alal-iymaan.
Allaahumma laa tahrimnaa ajrahu, walaa tudhwillanaa ba’-dahu*

Ee Allaah, Mghufurie aliyehai katika sisi na aliyekufa, aliyepo na
asiyekuwepo, mdogo kati yetu na mkubwa, mwanamume kati yetu
na mwanamke. Ee Allaah, Unayemweka hai kati yetu basi Muweke
katika Uislamu, na Unayemfisha basi mfishe juu ya iymaan. Ee
Allaah, Usitunyime thawabu zake wala usitupoteze baada yake.”[43]
[Imetolewa na Muslim na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy,
Abuu Daawuwd, Ibn Maajah)]

459.

وَعَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا صَلَّيْتُمْ عَلَى الْمَيِّتِ فَأَخْلِصُوا لَهُ الدُّعَاءَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mnapomswalia maiti, mtakasieni du’aa.”[44] [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

460.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَسْرِعُوا بِالْجَنَازَةِ، فَإِنْ تَكُ صَالِحَةً فَخَيْرٌ تُقَدِّمُونَهَا إِلَيْهِ، وَإِنْ تَكُ سَوَى ذَلِكَ فَشَرٌّ تَضَعُونَهُ عَنْ رِقَابِكُمْ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Liharakisheni jeneza, kwani akiwa mwema, mtakuwa mnampeleka mwisho mzuri, na akiwa muovu basi ni uovu huo mnauondoa shingoni mwenu.”[45] [Al-Bukhaariy, Muslim]

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "مَنْ شَهِدَ
الْجَنَازَةَ حَتَّى يُصَلَّى عَلَيْهَا فَلَهُ قِيرَاطٌ، وَمَنْ شَهِدَهَا حَتَّى
تُدْفَنَ فَلَهُ قِيرَاطَانِ". قِيلَ: وَمَا الْقِيرَاطَانِ؟ قَالَ: "مِثْلُ
الْجَبَلَيْنِ الْعَظِيمَيْنِ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِمُسْلِمٍ: { حَتَّى تُوَضَعَ فِي اللَّحْدِ }

وَالْبُخَارِيُّ: { مَنْ تَبَعَ جَنَازَةَ مُسْلِمٍ إِيْمَانًا وَاحْتِسَابًا، وَكَانَ
مَعَهُ حَتَّى يُصَلَّى عَلَيْهَا وَيُفْرَغَ مِنْ دَفْنِهَا فَإِنَّهُ يَرْجِعُ
بِقِيرَاطَيْنِ، كُلُّ قِيرَاطٍ مِثْلُ أَحَدِ }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena

Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:

“Anayehudhuria jeneza mpaka iswaliwe hupata Qiyaatw moja, na anayehudhuria hadi maiti amezikwa, mtu huyo atapata Qiyaatw mbili.” Akaulizwa Qiyaatw ni nini? Akasema: “Ni kama vilima viwili vikubwa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Mpaka awekwe katika mwanandani.”

Na katika Riwaayah ya Al-Bukhaariy pia kutokana na Hadiyth ya Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Mwenye kufuata maziko ya Muislam, kwa Iymaan na kutaka fadhila za Allaah, na akakaa hadi akaswaliwa na akamalizwa kuzikwa, atarejea na thawabu za Qiyaatw mbili, na kila Qiyaatw ni kama mlima wa Uhud.”

462.

وَعَنْ سَالِمٍ، عَنْ أَبِيهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ رَأَى النَّبِيَّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَأَبَا بَكْرٍ وَعُمَرَ، يَمْشُونَ أَمَامَ الْجَنَازَةِ} رَوَاهُ
الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَأَعْلَاهُ النَّسَائِيُّ وَطَائِفَةٌ
بِالْإِسْالِ

Kutoka kwa Saalim[46] alisimulia kutoka kwa baba yake (رَضِيَ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuwa: “Alimuona Nabiyy (اللَّهُ عَنْهُ
Abuu Bakr na ‘Umar wanatembea mbele ya jeneza.”[47] [Imetolewa
na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn
Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Hibbaan, na An-Nasaaiy na
wengine wakasema ina dosari]

463.

وَعَنْ أُمِّ عَطِيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {نُهِينَا عَنْ اتِّبَاعِ
الْجَنَائِزِ، وَلَمْ يُعْزَمْ عَلَيْنَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ummu ‘Atwiyyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema:
“(Wanawake) tumekatazwa kufuata jeneza, lakini haikusisitizwa kwetu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

464.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا رَأَيْتُمُ الْجَنَازَةَ فَقُومُوا، فَمَنْ تَبِعَهَا فَلَا يَجْلِسُ حَتَّى تُوضَعَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkilionajeneza simameni, na yeyote atakayelifuata asiketi[48] chini hadi jeneza hilo liwekwe chini.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

465.

وَعَنْ أَبِي إِسْحَاقَ، أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ يَزِيدَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَدْخَلَ الْمَيِّتَ مِنْ قَبْلِ رِجْلِي الْقَبْرِ، وَقَالَ: هَذَا مِنَ السُّنَّةِ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa Abuu Ishaqa[49] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema
'Abdullaah bin Yaziyd[50] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): Alimtua chini maiti
katika upande wa miguu yake na akasema: "Hii ni Sunnah."
[Imetolewa na Abuu Daawuud]

466.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ قَالَ: { إِذَا وَضَعْتُمْ مَوْتَاكُمْ فِي الْقُبُورِ، فَقُولُوا: بِسْمِ اللَّهِ،
وَعَلَى مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ } أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ،
وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَأَعْلَاهُ
الدَّارَقُطْنِيُّ بِالْوَقْفِ

Kutoka kwa Ibn 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Mkimuweka maiti wenu
kaburini, semeni: BismiLLaahi wa 'alaa millati Rasuwli-LLaah
(Kwa jina la Allaah na kwa kufuata mila ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ))."[51] [Imetolewa na Ahmad, Abuu
Daawuud na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan, na Ad-
Daaraqutwniy aliita Mawquwf (maneno ya Maswahaba)]

467.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {كَسْرُ عَظْمِ الْمَيِّتِ كَكْسَرِهِ حَيًّا} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ عَلَى شَرْطِ مُسْلِمٍ

وَزَادَ ابْنُ مَاجَهَ مِنْ حَدِيثِ أُمِّ سَلَمَةَ: {فِي الْإِثْمِ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuuvunja mfupa wa maiti ni kama kuuvunja akiwa hai.” [Imetolewa na Abuu Daawuud kwa Isnaad inayokidhi masharti ya Muslim]

Na Ibn Maajah ameongezea kutokana na Hadiyth ya Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) yasema: “Katika kupata dhambi.”

468.

وَعَنْ سَعْدِ بْنِ أَبِي وَقَّاصٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {الْحَدُّوا لِي لَحْدًا، وَأَنْصِبُوا عَلَى اللَّبَنِ نُسْبًا، كَمَا صُنِعَ بِرَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

وَالْبَيْهَقِيُّ عَنْ جَابِرِ نَحْوَهُ، وَزَادَ: {وَرُفِعَ قَبْرُهُ عَنِ الْأَرْضِ قَدْرَ شِبْرٍ} وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

وَلِمُسْلِمٍ عَنْهُ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يُجَصَّصَ الْقَبْرُ، وَأَنْ يُقْعَدَ عَلَيْهِ، وَأَنْ يُبْنَى عَلَيْهِ}

Kutoka kwa Sa'd bin Abii Waqqaasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nitengenezeeni mwanandani na mpange matofali juu ya kaburi langu kama alivyofanyiwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) [52].” [Imetolewa na Muslim]

Na Al-Bayhaqiyy alinukuu masimulizi kama hayo kutoka kwa Jaabir, na akaongezea: “Na kaburi lake lilipandishwa juu takribani shubiri moja[53] kutoka ardhini.” [Aliisahihisha Ibn Hibbaan]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza makaburi yasipakwe chokaa, kukaliwa juu yake na kujengwa juu yake.”[54]

469.

وَعَنْ عَامِرِ بْنِ رَبِيعَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى عَلَى عُثْمَانَ بْنِ مَظْعُونٍ، وَأَتَى الْقَبْرَ، فَحَتَّى عَلَيْهِ ثَلَاثَ حَتَّيَاتٍ، وَهُوَ قَائِمٌ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ

Kutoka kwa ‘Aamir bin Rabiyy’ah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswalia maiti ya ‘Uthmaan bin Madhw’uwn,[55] kisha akaenda kwenye kaburi lake na akatupia mikono mitatu ya udongo juu yake huku amesimama wima.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy]

470.

وَعَنْ عُثْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا فَرَغَ مِنْ دَفْنِ الْمَيِّتِ وَقَفَ عَلَيْهِ وَقَالَ: "اسْتَغْفِرُوا لِأَخِيكُمْ وَسَلُّوا لَهُ التَّثْبِيتَ، فَإِنَّهُ الآنَ يُسْأَلُ"}
رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Uthmaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokwisha kuzika maiti, alisimama karibu na kaburi na kusema: “Muombeeni maghfirah ndugu yenu na muombeeni kuthibitishwa[56] kwani hivi sasa anaulizwa.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisaihisha Al-Haakim]

471.

وَعَنْ ضَمْرَةَ بْنِ حَبِيبٍ أَحَدِ التَّابِعِينَ قَالَ: {كَانُوا يَسْتَحِبُّونَ إِذَا سُوِيَ عَلَى الْمَيِّتِ قَبْرُهُ، وَانْصَرَفَ النَّاسُ عَنْهُ، أَنْ يُقَالَ عِنْدَ قَبْرِهِ: يَا فُلَانُ! قُلْ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ. ثَلَاثُ مَرَّاتٍ، يَا فُلَانُ! قُلْ: رَبِّي اللَّهُ، وَدِينِي الْإِسْلَامُ، وَنَبِيِّ مُحَمَّدٌ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ} رَوَاهُ سَعِيدُ بْنُ مَنْصُورٍ مَوْقُوفًا

وَاللَّطَبَرَانِيَّ نَحْوَهُ مِنْ حَدِيثِ أَبِي أَمَامَةَ مَرْفُوعًا مُطَوَّلًا

Kutoka kwa Dhawamrah bin Habiyyb[57], mmoja wa At-Taabi'iyna amesema: Wao (Maswahaba) walipomaliza kusawazisha kaburi na watu wakaondoka, walipendelea kusemwe kaburini pake: "Ee fulani! Sema:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ. ثَلَاثُ مَرَّاتٍ، يَا فُلَانُ! قُلْ: رَبِّي اللَّهُ، وَدِينِي الْإِسْلَامُ، وَنَبِيِّ مُحَمَّدٌ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

Hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah mara tatu; Ee Fulani! Sema: Rabb wangu ni Allaah, Dini yangu ni Uislam, na Nabiy wangu ni Muhammad (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)." [Imetolewa na Sa'iyd bin Manswuwr na akasema ni Mawquwf]

Na Atw-Twabaraaniyy alisimulia vivyo hivyo kupitia kwa Abuu Umaamah, Hadiyth hii ni Marfuw'.

وَعَنْ بُرَيْدَةَ بْنِ الْحَصِيبِ الْأَسْلَمِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {نَهَيْتُكُمْ عَنْ زِيَارَةِ الْقُبُورِ فَزُورُوهَا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

زَادَ التِّرْمِذِيُّ: {فَإِنَّهَا تُذَكِّرُ الْآخِرَةَ}

زَادَ ابْنُ مَاجَةَ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ مَسْعُودٍ: {وَتَزَهَّدُ فِي الدُّنْيَا}

Kutoka kwa Buraydah bin Al-Haswiyb Al-Aslamiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Nilikukatazeni kuzuru makaburi, sasa yazuruni.”[58]
[Imetolewa na Muslim]

Na akaongezea At-Tirmidhiy: “Kwani hiyo inakumbusha Aakhirah.”

Akaongezea Ibn Maajah kutokana na Hadiyth ya Ibn Mas-‘uwd: “Humfanyisha kuipa mgongo dunia.”

473.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَعَنَ زَائِرَاتِ الْقُبُورِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:

“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amewalaani[59]

wanawake wanaozuru makaburi.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

474.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : {لَعَنَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ النَّائِحَةَ ، وَالْمُسْتَمِعَةَ} أَخْرَجَهُ أَبُو
دَاوُدَ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amemlaani
mwanamke anayeomboleza (kwa kelele) na anayemsikiliza.”
[Imetolewa na Abuu Daawuwd]

475.

وَعَنْ أُمِّ عَطِيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : {أَخَذَ عَلَيْنَا رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ لَا نَنُوحَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ummu ‘Atwiyyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alichukua ahadi kwetu kuwa hatutaomboleza tukifiwa.”[60] [Al-Bukhaariy, Muslim]

476.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الْمَيِّتُ يُعَذَّبُ فِي قَبْرِهِ بِمَا نِيحَ عَلَيْهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Maiti huadhibiwa kaburini[61] kwa sababu ya kuombolezwa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

477.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {شَهِدْتُ بِنْتًا لِلنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ تُدْفَنُ ، وَرَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ جَالِسٌ عِنْدَ الْقَبْرِ ، فَرَأَيْتُ عَيْنَيْهِ تَذْمَعَانِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilishuhudia maziko ya binti ya Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikaa karibu na kaburi nikamuona akitokwa na machozi.”[62] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

478.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا تَدْفِنُوا مَوْتَاكُمْ بِاللَّيْلِ إِلَّا أَنْ تُضْطَرُّوا } أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَةَ وَأَصْلُهُ فِي "مُسْلِمٍ"، لَكِنْ قَالَ: زَجَرَ أَنْ يُقْبَرَ الرَّجُلُ بِاللَّيْلِ، حَتَّى يُصَلَّى عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msizike wafu wenu usiku[63] isipokuwa ikilazimika hivyo.” [Imetolewa na Ibn Maajah, na chanzo chake kipo katika Swahiyh Muslim, isipokuwa alisema: Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikemea maiti kuzikwa usiku hadi aswaliwe]

479.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ جَعْفَرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {لَمَّا جَاءَ نَعِيُّ جَعْفَرٍ حِينَ قُتِلَ قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "اصْنَعُوا لَالِ جَعْفَرٍ طَعَامًا، فَقَدْ أَتَاهُمْ مَا يَشْغَلُهُمْ"} أَخْرَجَهُ الْخَمْسَةُ، إِلَّا النَّسَائِيُّ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Ja’far[64] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) ame sema: “Ilipokuja taarifa ya kifo cha Ja’far, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alisema: “Andaeni chakula kwa ajili ya familia ya Ja’far kwani wamepata jambo la kuwashughulisha.”[65] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy]

480.

وَعَنْ سُلَيْمَانَ بْنِ بُرَيْدَةَ عَنْ أَبِيهِ قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُعَلِّمُهُمْ إِذَا خَرَجُوا إِلَى الْمَقَابِرِ: {السَّلَامُ عَلَى أَهْلِ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُسْلِمِينَ، وَإِنَّا إِن شَاءَ اللَّهُ بِكُمْ لِلْآحِقُونَ، أَسْأَلُ اللَّهَ لَنَا وَلَكُمْ الْعَافِيَةَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Sulaymaan bin Buraydah[66] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) ame sema kwa upokezi wa babake kwa kusema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akifunza Swahaba wake wakienda makaburini (waseme):

السَّلَامُ عَلَى أَهْلِ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُسْلِمِينَ، وَإِنَّا إِن
شَاءَ اللَّهُ بِكُمْ لِلْأَحْقُونِ، أَسْأَلُ اللَّهَ لَنَا وَلَكُمْ الْعَافِيَةَ

*As-Salaamu 'alaa ahlid-diyaari minal-Muuminiyna wal-Muslimiyna,
wa innaa In Shaa Allaahu bikum lalaahiquwna, as-alu-Allaah lanaa
wa lakumul-'aafiyah*

(Amani iwe juu yenu mliyomo kwenye makazi haya miongoni mwa
Waumini na Waislamu. Allaah Akipenda na sisi tutajiunga nanyi.
Tunamuomba Allaah Atupe al-'aafiyah[67] sisi na nyinyi.”

[Imetolewa na Muslim]

481.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {مَرَّ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِقُبُورِ الْمَدِينَةِ، فَأَقْبَلَ عَلَيْهِمْ بِوَجْهِهِ
فَقَالَ: "السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَهْلَ الْقُبُورِ، يَغْفِرُ اللَّهُ لَنَا وَلَكُمْ، أَنْتُمْ
سَلَفُنَا وَنَحْنُ بِالْأَثَرِ" { رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَقَالَ: حَسَنٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipita katika makaburi ya
Al-Madiynah, akayaelekea kwa uso wake akasema:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَهْلَ الْقُبُورِ، يَغْفِرُ اللَّهُ لَنَا وَلَكُمْ، أَنْتُمْ سَلَفُنَا
وَنَحْنُ بِالْأَثَرِ

As-salaam 'alaykum yaa Ahlal-qubuwr, Yaghfiru-Allaahu lanaa wa lakum, antum salafunaa wa nahnu bil-athar

(Amani iwe juu yenu enyi wakazi wa makaburi haya. Namuomba Allaah Atughufurie sisi na nyinyi, mumetangulia kabla yetu na sisi tutafuata baada yenu).”[68] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na alisema ni Hasan]

482.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَسُبُّوا الْأَمْوَاتَ، فَإِنَّهُمْ قَدْ أَفْضَوْا إِلَى مَا
قَدَّمُوا } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَرَوَى التِّرْمِذِيُّ عَنِ الْمُغِيرَةِ نَحْوَهُ، لَكِنْ قَالَ: { فَتَوَدُّوا
الْأَحْيَاءَ }

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msitukane wafu
kwani wameshafikia waliyoyatanguliza.” [Imetolewa na al-
Bukhaariy]

Na katika tamshi la At-Tirmidhiy imesimulia vivyo hivyo kupitia kwa Al-Mughiyrah lakini ikaongezea maneno haya: “[Usije ukawadhuru watu walio hai.](#)”[\[69\]](#)

[1] Kutajwa kwa kifo aghalabu huleta hisia ya kujinyima, kujikagua kuhusu matendo yako, na khofu ya Qiyaamah, na humhamasisha mtu kutenda mema na kujikita katika hali ya kiakili ya kujiandaa kwa ajili ya siku ya Hesabu.

[2] Kumekatazwa kuomba au kupendelea kifo kwa sababu ya kawaida ya kidunia, ufukara, ugonjwa, n.k. kuomba kukutana na Allaah (سبحانه) hakika ni dalili ya kukamilika kwa Iymaan ya mtu. Kwa hivyo inaruhusiwa kwa mtu kuomba kifo kwa woga wa kupotoka mbali na njia sahihi ya Dini.

[3] Kwa Muumini, maisha ni zawadi au faida. Hadiyth moja inasema: “Muumini, akiwa mwenye taqwa, atakusanya taqwa zaidi. Maisha ni faida kwa mtenda dhambi pia, kwani anaweza kutubu wakati wa uhai wake.”

[4] Uelewa wa hili umepindishwa kwa njia nyingi. Ufafanuzi sahihi ni kwamba, mtu hutoka jasho kadiri machungu ya kifo yanavyozidi kuwa makali. Na machungu ya Muumini hufanywa kuwa makali ili iwe ni toba kwa madhambi yake yote aliyoyatenda duniani nayo husamehewa papa hapa. Hii pia ni zawadi ya Allaah (سبحانه وتعالى) kwa Waumini.

[5] Ma’qil bin Yasaar ni Swahaba wa Kabila la Muzaynah. Alisilimu kabla ya msafara wa kivita wa Hudaybiyah, na alishiriki katika Bay’atur-Ridhwaan. Mto aliouchimba kule Basra kwa amri ya ‘Umar, uliitwa jina lake. Na tokea wakati ule, ipo mithali isemayo kuwa: “Ikiwa mto wa Allaah utakuja ukibubujika, mto wa Ma’qil utakuwa hauna kazi.” Inasemekana kuwa alifariki Basra mwishoni mwa utawala wa Mu’awiyah mwaka 60A.H. au wakati wa utawala wa Yaziyd.

[6] Hadiyth hii ni dhaifu kwa mujibu wa Shaykh Al-Albani, angalia Al-Irwaa’ (3/150) namba (688).

[7] Huyu Abuu Salamah ndiye ‘Abdullaah bin ‘Abdil-Asad Al-Makhzuwmiy Al-Qurayshiy, mwana wa shangazi (kwa upande wa baba) wa Nabiyy (ﷺ), pia ni ndugu wa Hamzah kwa kunyonya. Wote wawili walinyonyeshwa na Thuwaybah, mjakazi aliyeachwa huru na Abuu Lahab. Abuu Salamah akahamia Uhabeshi (Ethiopia) pamoja na mkewe Ummu Salamah. Alishiriki katika vita vya Badr, na alijeruhiwa katika vita vya Uhud. Jeraha lake likapona, lakini likachipua tena, akafariki mnamo tarehe 3 Jamaadal-Uwlaa mwaka 4.A.H., akamuacha Ummu Salamah ambaye baadaye aliolewa na Rasuli wa Allaah (ﷺ) mnamo mwezi wa Shawwaal mwaka wa 4A.H.

[8] Hii inatufunza sisi kuwa, macho ya mtu anayefariki huwa wazi na hupanuka wakati anapoitazama roho yake wazipendazo ikimtoka. Macho ya mfu yafungwe haraka kwani hayafungiki baada ya mwili kwisha joto lake, na hutia khofu na woga katika akili za watu.

[9] Hii inaonyesha kuwa inaruhusiwa kuubusu mwili wa maiti, ilimradi awe ni Muislam.

[10] Kwa mujibu wa Hadiyih hii, mtu hubaki chini ya deni lake hata baada ya kufariki kwake, kadiri deni lake litavyokuwa bado halijalipwa.

[11] Hii ni kwa sharti kwamba, aliyefariki, licha ya kumiliki mali na kuwa na uwezo wa kulipa deni lake, alifariki bila kulipa. Ikiwa mtu atakufa ghafla na akawa hakuwa na muda wa kutosha kulipa deni hilo, au mtu ambaye hana mali lakini ana niyyah njema ya kulipa deni hilo, hata hivyo husamehewa kulipa deni hilo. Moja ya matumizi ya Zakkah ni kulipa madeni ya watu wanaodaiwa.

[12] Kuyaponda au kusaga majani ya mkunazi huosha uchafu kama ifanyavyo sabuni.

[13] Mtu alikuwa amesimama ‘Arafah pamoja na Nabiyy (ﷺ) (ﷺ). Alianguka chini ya mlima na akapigwa teke na ngamia jike,

halafu akafariki. Nabiyy (ﷺ) akawataka watu waliokuwepo pale wasimfunike kichwa wala wasimnyunyuzie marashi mwilini mwake, kwa kuwa Allaah (عزَّ وجلَّ) Atamwamsha Siku ya Kufufuliwa akiwa katika hali ya kutamka Talbiyah.

[14] Hadiyih inasema: “Rasuli wa Allaah (ﷺ) alipofariki, watu walitaharuki juu ya kama wamvue nguo zake zote ili waoshe maiti yake au wafanyeje. Ghafla, watu wakalemewa na hisia ya usingizi, na sauti isiyojulikana ikasikika ikisema kutokea katika kona ya nyumba ile kuwa maiti isivuliwe nguo zake kamwe, na amri hiyo ikatekelezwa na maiti ikaoshwa kama ilivyotakiwa.”

[15] Inaweka wazi kwamba joshu la maiti sharti kwa uchache mara tatu. Ikitakikana zaidi ya hapo, basi inaweza kuwa mara tano au saba, lakini Wanazuoni wengi wameafikiana kuwa kuoshwa mara moja kunatosheleza.

[16] Sahuwl ni jina la kijiji kule Yemen, na kitambaa hicho kilitoka huko.

[17] ‘Abdullaah bin Ubayy alikuwa ni Sultani wa kabila la Al-Khazraj wakati wa Jaahiliyyah kabla ya Unabiyy wa Rasuli wa Allaah (ﷺ), na akawa mkuu wa wanafiki baada ya Rasuli wa Allaah (ﷺ) kuhamia Al-Madiynah. ‘Abdullaah bin Ubayy pamoja na watu wake mia tatu walijitoa kutoka kwenye vita vya Uhudi, na ndiye aliyechangia zaidi kumsingizia ‘Aaishah (رضي الله عنها). Ndiye pia aliyesema: “Tukirejea Al-Madiynah, mwenye nguvu (yaani yeye) atamfukuza mnyonge (yaani Nabiyy (ﷺ)).” Pia ndiye aliyesema: “Msiwalishe watu walio pamoja na Rasuli wa Allaah (ﷺ) mpaka wasambaratike.” Alifariki mnamo Dhul Qa’dah mwaka wa 9A.H. mama yake aliitwa Saluwl.

[18] Mwanaye ‘Abdullaah bin Ubayy ni ‘Abdullaah bin ‘Abdillaah bin Ubayy bin Saluwl. Alikuwa mmoja wa Maswahaba wema, wadilifu na wakarimu, na alifariki shahidi katika vita vya Al-Yamaamah. Alikuwa ndiye mpinzani mkali kuliko wote dhidi ya baba yake kiasi kwamba aliomba ruhusa amkate kichwa pale baba yake aliposema: “Mwenye

nguvu atamfukuza mnyonge.” Jina lake wakati wa Ujaahiliyyah lilikuwa Hubab lakini Rasuli wa Allaah (ﷺ) alimpa jina jingine, ambalo ni ‘Abdullaah.

[19] Inamaanisha kuwa, hiyo sanda sharti iwe safi na maridadi, isiwe ghali, kwani kuna Hadiyth inayokataza hilo.

[20] Hii ilikuwa ni dharura tu, kwa vile hakukuweco vitambaa vya kutosha kuwakafini mmoja mmoja wakati ule. Ni utaratibu wa kawaida pia kwamba wanaofariki shahidi hawaswaliwi Swalaah ya Janaazah.

[21] Inamaanisha kuwa, mwanaume anaweza kuosha maiti ya mkewe, na kwa hivyo, watu wengi wanafuata mwenendo huu. Watu wengine wanaipinga hiyo, lakini wengi wa Maswahaba wa Rasuli wa Allaah (ﷺ) wanazipinga hoja za wapinzani hao. ‘Aliy (رضي الله عنه) alimuosha Faatwimah (رضي الله عنها), na hali kadhalika ‘Asmaa (رضي الله عنها) alimuosha Abuu Bakr (رضي الله عنه). Matukio haya yanathibitisha kwamba mme anaweza kumuosha mke, na mke pia anaweza kumuosha mme; na wameafikiana wengi kuwa Maswahaba wa Nabiy (ﷺ) waliyanyamazia mambo hayo mawili.

[22] Faatwimah (رضي الله عنها) alikuwa binti mdogo zaidi kuliko mabinti wote wa Rasuli wa Allaah (ﷺ), na ndiye mwanamke mwenye hadhi kubwa zaidi ya Ummah huu. ‘Aliy bin Abiy Twaalib (رضي الله عنه) alimuoa mnamo mwezi wa Ramadhwaan mwaka wa 2 A.H. na wakaanza kuishi pamoja mnamo mwezi wa Dhul Hijjah. Wakati ule alikuwa na umri wa miaka 15 na miezi 5. Alifariki mnamo mwezi wa Ramadhwaan mwaka wa 11 A.H, miezi sita baada ya kifo cha baba yake.

[23] ‘Aliy (رضي الله عنه) alitekeleza wasia wa mke wake.

[24] Tafsiri zingine zinasema neno: “Faswuliya” limetumika, ambalo ni “Majhuwl (haijulikani)”, na inamaanisha kuwa Rasuli wa Allaah (ﷺ) mwenyewe hakushiriki katika Swalaah ya maiti yule,

bali Maswahaba walimswalia. Ukweli ni kwamba Rasuli wa Allaah (ﷺ) mwenyewe alimswalia Swalaatul-Janaazah, maiti yule.

[25] Kuna kutofautiana maoni kuhusu kumswalia mtu aliyejiua mwenyewe. Wengi wanakubali kuwa Swalaah ya Janaaza kwa mtu huyo ni sharti iwepo. Qaadhi ‘Iyaadh anasema kwa mujibu wa chanzo chake, Wanazuoni wote wanaafikiyana juu ya Swalaah Janaazah ya watu walioadhibiwa au wamepigwa mawe hadi wakafariki, kwa kanuni za Shariy’ah, waliojiua wenyewe, na watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Rasuli wa Allaah (ﷺ) alikuwa hahudhurii baadhi ya Swalaah kama hizo za Janaazah, lakini alikuwa akiwaagiza watu wahudhurie.

[26] Inamaanisha kuwa: (a) Ni ruhusa kuswali Swalaah ya Janaazah katika kaburi la mtu, (b) Hakujawekwa kiwango cha muda wa kuweza kumswalia maiti. Hata Rasuli wa Allaah (ﷺ) aliwaswalia mashahidi wa Uhud miaka minane baada ya kifo chao. (c) Pia maiti anaweza kuswaliwa mara mbili hadi tatu.

[27] Maana ya neno “Na’y” ni kuwasilisha khabari za kifo cha mtu, ambayo ilikuwa mila ya kijaahiliyyah kuwa kila mtu maarufu alipofariki, khabari ya kifo chake ilitangazwa mji mzima. Mtindo huo umekatazwa. Hata hivyo, unaweza kuwaarifu ndugu na jamaa na wenye taqwa kushiriki katika kumswalia maiti huyo.

[28] An-Najaashiy kilikuwa cheo cha mtawala wa Uhabeshi (Ethiopia) ambaye jina lake halisi lilikuwa Ashama bin Al-Abjar. Waislam wa Makkaah walikimbilia kwake Uhabeshi kwa ajili ya Iymaan na Dini yao, kukimbia ukandamizaji wa makafiri wa Makkah. Rasuli wa Allaah (ﷺ) alimtuma ‘Amr bin Umayyah Ad-Damar mwishoni mwa mwaka wa 6 A.H. au mwezi wa Muharram mwaka wa 7 A.H. kumpelekea An-Najaashiy ujumbe ili apate kusilimu. Aliipokea barua ile, akaiweka juu ya macho yake, akashuka kutoka kwenye kiti chake cha ufalme, akasilimu. Ja’far bin Abiy Twaalib (رضي الله عنه) alimuandikia barua Nabiyy (ﷺ) kumpa taarifa hiyo. An-Najaashiy alifariki mnamo mwezi wa Rajab mwaka wa 9 A.H. baada ya vita vya

Tabuwk. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswalisha Swalaatul-Janaazah kighaybu (Swalaah ya jeneza ya mbali). Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuandikia barua mrithi wa utawala wake ili naye asilimu.

[29] Inataja kuruhusiwa kumswalia maiti bila ya mwili wake kuwepo hapo anaposwaliwa. Wengine wanaikanusha hii bila ushahidi wowote.

[30] Inafundisha uombezi wa Muislam kwa Muislam, kwa kumuombea du'aa anusurike, inakubaliwa na Allaah.

[31] Ikiwa maiti ni ya mwanaume, Imaam asimame sehemu ya kichwani, na ikiwa mwanamke Imaam sharti asimame sehemu ya katikati ya maiti.

[32] Baydhwaa ni jina la utani la Mama aitwae Da'ad bint Al-Juhdum Al-Fihriyya, na wanawe wavulana wawili wanaitwa Sahl na Suhayl aliowazaa na Wahaab bin Rabi'a Al-Qurayshiy Al-Fihr. Sahl ndiye aliyeikanusha Sahifa iliyoandikwa na Maqurayshi ili wawasuse Banuu Haashim na Waislam. Ilisemekana kuwa yeye alisilimu waziwazi kule Makkah. Inasemekana pia kuwa aliificha Iymaan yake ya Uislam na akalazimishwa kujiunga na jeshi la Maquraysh apigane vita vya Badr. Alitekwa na Waislam, na 'Abdullaah bin Mas-'uwd alimshuhudia kuwa alimuona akiswali kule Makkah. Kwa hivyo aliachiwa, na akafariki Madiynah. Lakini Suhayl alisilimu mapema sana, akashiriki katika Hijratayn (kuhama mara mbili kuenda Uhabeshi), na kuhudhuria vita vya Badr na vingine vyote muhimu. Alifariki Al-Madiynah mnamo mwaka wa 9 A.H. baada ya vita vya Tabuwk. Mwana wa tatu wa Al-Baydhwaa anaitwa Safwaan ambaye alifariki shahidi kule Badr ilisemwa pia kuwa ulipita muda mrefu baada ya kifo cha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[33] Watu wengine wanasema si sawa kuswalia maiti ndani ya Msikiti, lakini hawana ushahidi wowote. Isitoshe, imesimuliwa na Ibn Abiy Shayba (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) kuwa maiti ya Abuu Bakr (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) iliswaliwa Msikitini, Imaam akiwa 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ). Pia imesimuliwa katika Musnad Sa'iyd bin Mas-'uwd kuwa maiti ya 'Umar iliswaliwa Msikitini

Imaam akiwa Suhayb (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) na pia maiti ya Sa'd bin Abiy Waqqaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) iliswaliwa Msikitini.

[34] ‘Abdur-Rahmaan bin Abiy Laylah alikuwa Answaar wa mji wa Madiynah kisha akahamia mji wa Kufa. Alikuwa mmoja wa Taabi’iyna wakongwe katika kusimulia Hadiyth. Alipewa jina la utani la Abuu ‘Iysaa na alisimulia Hadiyth kutoka katika kundi la Maswahaba. Alizaliwa mwanzoni mwa miaka sita ya mwisho ya Ukhalifa wa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ). Alifariki mwaka wa 86 A.H. katika vita vya Al-Jamajim; na ilisemekana kuwa alizama katika mto wa Basra.

[35] Inasemekana kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwahi kutamka Takbiyr mara nne, tano, sita, saba. ‘Umar aliwathibitisha watu katika Takbiyr nne na ndio inayoendelea hadi leo hii.

[36] Sahl bin Hunayf ni Answaar na Aws (kutoka katika kabila la Aws). Alishiriki vita vya Badr na vilivyofuata. Alisimama imara sana na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika vita vya Uhud. Baadaye, ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimteua kuwa mtawala wa Basra, na alishiriki pamoja naye katika vita vya Siffin. Kulikuweko fungamano la udugu kati yake na ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) baada ya Hijra. Alifariki mnamo mwaka wa 38. A.H.

[37] Hadiyth hii ni ushahidi kuwa, kusomwa kwa Suwratul-Faatihah ndani ya Swalaah ya Janaazah ni waajib.

[38] Twalhah bin ‘Abdillaah bin ‘Awf ni Zuhri na Mkurayshi, na ni mwana wa kaka wa ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Awf. Alipewa jina la utani la Twalhah An-Nada, na alikuwa wa kutegemewa, msomi, na alihifadhi Hadiyth nyingi. Alikuwa miongoni mwa Taabi’iyn wa katikati na alifariki mwaka wa 97 A.H akiwa na umri wa miaka 72.

[39] Katika Swalaatul Janaaza, Suwratul-Faatihah husomwa kwa sauti ya chini. Ndiyo sababu Ibn ‘Abbaas aliisoma kwa sauti kubwa na akaeleza: “Niliisoma kwa sauti kubwa ili nyote mjue ni Sunnah.”

[40] ‘Awf bin Maalik alikuwa Swahaba kutoka katika ukoo wa Ashja’, na mwanzoni alishiriki katika vita vya Khaybar, ndiye aliyeshika bendera ya

Ashja' wakati Makkah ilipotekwa. Alilowea Sham na akafariki huko mwaka 73 A.H.

[41] Upo uwezekano kuwa 'Awf (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiisoma du'aa hiyo kwa sauti kubwa, au aliulizia du'aa hii na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamfundisha.

[42] Zipo du'aa mbalimbali zilizosomwa na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika Swalaatul-Janaaza, na mtu anaweza kusoma yoyote anayoitaka. Kama ni maiti ya mtoto, soma:

اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ لَنَا فَرَطًا وَسَلَفًا وَأَجْرًا

Allaahummaj- 'alhu lanaa faratwan wa salafan wa ajraa.

Ee Allaah mfanye kwetu sisi ni kitangulizi cha malipo na dhamana na malipo)

[43] Du'aa nyingi zisomwazo ndani ya Swalaah ya Janaazah zilitoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ); na hii ya hapo juu ni mojawapo. Na kwa vile ni fupi, inapendwa zaidi.

[44] Inaweka wazi, hata kama aliyefariki alikuwa mtu wa dhambi, mtu sharti ulikuze hilo du'aa katika kumuomba kwa Allaah ili Amghufirie madhambi yake. Kuna wengine wanaodai mtu mwenye dhambi ni bora alaaniwe. Maoni kama hayo ni ya makosa na mabaya sana.

[45] Kwa hivyo tunafunzwa kwamba sharti tusikawie kuzika. Wapo watu siku hizi wanaokawiza kuzika maiti, ilhali Shariy'ah ya Kiislam inakataza.

[46] Saalim ndiye Abuu 'Abdullaah au Abuu 'Umar Saalim bin 'Abdillaah bin 'Umar bin Al-Khatwaab, mmoja wa Taabi'iyn na miongoni mwa Maulamaa maarufu. Alikuwa mmoja wa Wanazuoni saba wa Fiqh, na alikuwa mpokezi wa Hadiyth, mwenye ujuzi na muadilifu. Alifanana na baba yake katika elimu na matumizi yake. Alikufa mnamo mwezi wa Dhul Qa'da mwaka 106 A.H.

[47] Wakati wa kuenda mazikoni, ni hiari mtu kuwa mbele ya jeneza, nyuma, kuumeni au kushotoni kwake. Bin Manswuwr kwa upokezi wa Hasan bin 'Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesimulia kuwa, thawabu azipatazo mtu anayetembea nyuma ya jeneza ni kubwa zaidi kuliko za kutembea mbele ya jeneza. Tofauti yake inaweza kulinganishwa na Swalaah ya mtu anayeswali peke yake na Swalaah ya Jamaa.

[48] Neno "Kuketi" linamaanisha tu kuwa watu wote wanatakiwa wachangie kuzika. Wasiachiwe ndugu tu wa aliyefariki kufanya kila kitu ilhali watu wengine wote wanatazama.

[49] Abuu Is-haaq ndiye 'Amr bin 'Abdillaah As-Sabi'i Al-Hamdaaniy Al-Kufi. Ni Taabi'iy maarufu, alisimulia Hadiyth nyingi, lakini alikuwa Mudallis aliyekuja kuwa dhaifu kutokana na uzee katika miaka yake ya mwisho. Alizaliwa miaka miwili kabla ya mwisho wa Ukhalifa wa 'Uthmaan, na akafa mnamo mwaka 129 A.H.

[50] 'Abdullaah bin Yaziyd ni Khutami, Answaar na Aws. Alihudhuria Al-Hudaybiyyah huku akiwa na umri wa miaka 17, na alikuwa na 'Aliy katika vita vya Jamal na Siffin. Aliloweza Kufa, akawa gavana wake katika wakati wa Az-Zuhayr, na akafariki katika utawala wake.

[51] Imaam Bayhaqiyy alisimulia kwa Isnaad dhaifu ya wapokezi kuwa: "Wakati Ummu Kulthum (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) binti wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa akishushwa kaburini, Rasuli wa

Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisoma: “Kutokana nayo (ardhi) Tumekuumbeni, na humo Tutakurudisheni, na kutoka humo Tutakutoeni mara nyingine.” [Suwrah Twaahaa: 55]

بِسْمِ اللَّهِ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَعَلَى مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ

(Kwa jina la Allaah, kwa njia ya Allaah na kwa kufuata mila za Rasuli wa Allaah (maiti huyu hapa anazikwa).” Zipo du’aa nyingi zingine zilizotajwa katika Hadiyth, ambazo mtu anaweza kuzisoma kadiri anavyopenda.

[52] Hadiyth hii ni ushahidi kwamba kaburi alilotayarishiwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) lilikuwa na Lahd. Maswahaba walitofautiana rai zao kuwa kaburi la Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) liwe la Lahd (mwandani wa katikati) au la Shiq (mwanandani wa pembeni). Kulikuweko wachimba kaburi wawili kule Al-Madiynah siku zile, mmoja aliyekuwa stadi wa kuchimba Lahd, na mwingine wa Shiq. Ilikubaliwa miongoni mwa Maswahaba wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuwa mchimba kaburi yeyote atakayekuja kwanza, aanze kazi yake. Kwa hivyo yule stadi wa kuchimba Lahd ndiye aliyekuja kwanza, na akaandaa kaburi ipasavyo.

[53] Shariy’ah ya Kiislam inakataza kuliinua kaburi zaidi ya dhira moja (marefu ya kiganja cha mkono). Hivyo ndivyo lilivyokuwa kaburi la Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Mwanzo lilikuwa na umbile bapa au sawasawa. Lakini kuta za chumba cha Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) zilipoanguka (kwa sababu ya kutokarabatiwa au kuoza), Waliyd bin ‘Abdil-Maalik alikarabati zile kuta na akalijenga kaburi lile kwa umbile la nundu ya mgongoni kwa ngamia. Makaburi ya Abuu Bakr na ‘Umar Faruwq (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) pia yana umbo hilo la ngamia.

[54] At-Tirmidhiy pia anaongeza kuwa makaburi yasiwe na maandishi yoyote, na kusijengwe kitu chochote juu yake, na yasikanyagwekanyagwe. Hadiyth hii imenukuliwa na At-Tirmidhiy kuwa ni sahihi. An-Nasaaiy

alisimulia kuwa kusitupiwe mchanga wowote juu yake isipokuwa mchanga uliochimbwa kutoka humo.

[55] ‘Uthmaan bin Mathw’uwn alikuwa Jumahi na Qurayshi. Alikuwa mmoja wa Maswahaba waadilifu na wajumi; na alijinyima ulevi wakati wa jaahiliyyah. Alikuwa wa kumi na nne kusilimu, alishiriki katika Hijrah mbili, na alipigana Badr. Alikuwa Muhaajir wa kwanza kufariki Al-Madiynah. Kifo chake kilitokea mwezi Sha’baan, mwezi wa thelathini tokea Hijrah, naye akazikwa Al-Baqi’. Nabiy (ﷺ) alibusu uso wake baada ya kufariki, na baada ya kuzikwa akasema: “Huyu ni mtangulizaji mzuri kwetu sisi.” ‘Uthmaan bin Mathw’uwn alikuwa ni ndugu ya Rasuli wa Allaah (ﷺ) kwa kunyonya.

[56] Kwa hivyo tumefunzwa kwamba, baada ya maziko, kumuombea aliyefariki aghufiriwe dhambi zake, na kumuombea athibitike anapokabiliwa na maswali matatu kaburini ni Mustahabb (Inapendeza) na imesuniwa.

[57] Dhawamrah bin Habiyyb ndiye Abuu ‘Utbah Dhawamrah bin Habiyyb bin Suhayb Az-Zubayd Al-Himsi ni Taabi’iy anayetegemewa wa daraja la nne.

[58] Kuzuru makaburi ni miongoni mwa matendo yanayopendeza, lakini si lazima. Lakini kuyazuru makaburi ya wazazi kumesisitizwa sana. Mtu anapaswa kuzuru mara kwa mara na awaombee du’aa kwa Allaah.

[59] Kuna kutofautiana miongoni mwa Wanazuoni kuhusu iwapo wanawake wanaruhusiwa kuzuru makaburi au laa. Ni bora wanawake wasiende huko.

[60] Hadiyth hii inakataza kupiga mayowe, kunung’unika, na kuomboleza kwa ajili ya maiti. Kububujika machozi kwa sababu ya hisia ya huzuni hakukatazwi kwa kuwa kunadhihirisha ulaini wa moyo wa mtu, yaani kukataza hakuhusiani na tendo la macho yake mtu, bali kunahusu matendo ya mikono na ulimi tu.

[61] Maiti hupata mateso kwa ajili watu wanaolia kwa mayowe kwa kupinga Aayah isemayo: “**Na wala nafsi yoyote haitochuma (khayr au shari) ila ni juu yake. Na wala habebi mbebaji, mzigo (wa dhambi) wa mwengine.**” [Al-An’aam: 164]. Hii inahusu hali fulani ambapo kulia

kumeonekana katika baadhi ya majumba ya matajiri kama jambo la fahari na majivuno. Watu wengine huacha wasia kuwa vifo vyao vililiwe, wakati wengine hutoa tu idhini kuwa vifo vyao vyaweza kuliliwa. Katika hali kama hizi maiti ndiye atakayepata mateso. Endapo mtu ataacha maagizo kuwa asililiwe, basi yeye hatoteswa. Kwa hivyo ni bora mtu kuwakataza watu wasimlilie pindi atakapofariki.

[62] Hii inatufunza kwamba, kulia kwa kutokwa machozi kutokana na huzuni haikukatazwa. Mwana wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), Ibrahiym alipofariki, machozi yalikuwa yakibubujika kutoka machoni mwake. Baada ya kuona hivyo, ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Awf akamuuliza: “Ee Rasuli wa Allaah!, hata wewe hulia pia? Naye Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akajibu: “Ndiyo huwa nalia, lakini kwa ajili ya upendo siyo kushindwa uvumilivu.”

[63] Hii ina sababu nyingi: moja ni kwamba si watu wengi wanaoweza kushiriki maziko ya usiku. Sababu nyingine ni kuwaepusha watu na vidudu vihalifu vinavyozuru makaburi nyakati za usiku.

[64] Huyu ni Ja’far bin Abiy Twaalib, na ndiye kaka mkubwa (kwa miaka kumi) wa ‘Aliy bin Abiy Twaalib. Alihamia Uhabeshi ambako alibakia akiishi kule ambako Mfalme wa kule An-Najaashiy na wale waliomfuata walisilimishwa na yeye ‘Abdullaah, baadaye aliamia Al-Madiynah, na akafika Khaybar baada ya kutekwa kwake. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Sijui ni ipi ni furaha kubwa zaidi kumuona Ibn Ja’far au kwa kuiteka Khaybar.” Abuu Ja’far alikuwa mmoja wa watu wakarimu sana. Alikufa shahidi katika vita vya Mut’ah mnamo mwaka wa 8 A.H wakati alipokuwa kamanda wa jeshi. Mikono yake yote miwili ilikatwa, na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah alimpa mbawa mbili badala ya mikono yake iliyokatwa, na kwa mbawa hizo anaweza kuruka kwenda popote anapopataka huko Jannah.” Na kwa sababu hii, alikuwa akiitwa “Ja’far mrukaji” na “Ja’far mwenye mbawa mbili.”

[65] Hadiyth inatufundisha kwamba, kuwalisha ndugu wa maiti ni Sunnah. Kuhusu haki za kuwalisha waliofiwa, ni suala la majirani ambao wako msitari wa mbele. Kutoa vyakula siku ya kwanza ni Sunnah, na siku ya pili ni Makruwh (haipendezi), na imekatazwa pia kwa siku ya tatu. Iwapo

wanawake waliomo katika nyumba ambamo chakula kinaandaliwa wao wenyewe ni wenye kilio, hapo maoni ya Wanazuoni kuhusu chakula hicho hutofautiana. Ile desturi ya ndugu kukusanyika katika nyumba ya wafiwa, na kwa hiyo wao kuwa mzigo usiokuwa wa lazima kwa familia ya maiti. Tabia hii hufanywa na watu wengi, ni mbaya sana.

[66] Sulaymaan bin Buraydah ndiye Al-Husayb na ni Aslami na Marwazi. Alikuwa Taabi'iy ambaye kutegemewa kwake kulithibitishwa na Ibn Ma'in na Abuu Haakim. Al-Haakim amesema: "Hakutaja kama aliwahi kusikia Hadiyth kutoka kwa babake." Naye Al-Khazraji amesema: "Hadiyth alizosimulia kutoka kwa baba yake zimo katika sehemu mbalimbali ndani ya Swahiyh Muslim."

[67] Al-'Aafiyah maana yake ni: Afya, siha, hifadhi ya kila shari, amani, salama ya Dini duniani na Aakhirah.

[68] Kuenda makaburini na kuwaombea maghfirah maiti ni Sunnah kama ilivyothibitishwa na Hadiyth nyingi. Mtu aendae makaburini azingatie mambo mawili: (a) Kuwaombea maiti du'aa (b) Kukumbuka kifo. Mtu yeyote anayekwenda makaburini kwa ajili ya jambo lolote jingine lisilokuwa haya mawili yaliyotajwa hapo juu, yaani kulia, kuomba maghfirah, kurukuu na kusujudu, na kuomba kukidhiwa haja zake, kuzuru kwake makaburi ni shirki na haraam.

[69] Hadiyth hii inatufunza kuwa, si vizuri kuwataja maiti kwa mabaya au madhambi na kuwatangazia watu, lakini hukmu hii imeamrisha hususani kwa Waislamu na wenye taqwa.

كِتَابُ الزَّكَاةِ

Kitabu Cha Zakaah

04-Kitabu Cha Zakaah - كِتَابُ الزَّكَاةِ

01-Mlango Wa Zakaah Ya Mali

Mlango Wa Zakaah Ya Mali

483.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعَثَ مُعَاذًا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ إِلَى الْيَمَنِ... } فَذَكَرَ الْحَدِيثَ، وَفِيهِ: { أَنَّ اللَّهَ قَدْ افْتَرَضَ عَلَيْهِمْ صَدَقَةً فِي أَمْوَالِهِمْ، تُؤْخَذُ مِنْ أَغْنِيَائِهِمْ، فَتُرَدُّ فِي فُقَرَائِهِمْ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma Mu’aadh (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuenda Yaman.” Akaitaja Hadiyth yote, miongoni mwa maneno yaliyomo: “Allaah Aliifanya Zakaah kuwa ni jambo la fardhi kwao, katika mali zao, huchukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kupewa masikini wao.”[2] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni Al-Bukhaariy]

484.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ أَبَا بَكْرَ الصِّدِّيقَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ كَتَبَ لَهُ { هَذِهِ فَرِيضَةُ الصَّدَقَةِ الَّتِي فَرَضَهَا رَسُولُ اللَّهِ

صلى الله عليه وسلم على المسلمين، وأتت أمر الله بها رسوله في أربع وعشرين من الإبل فما دونها الغنم في كل خمس شاة، فإذا بلغت خمسا وعشرين إلى خمس وثلاثين ففيها بنت مخاض أنتى فإن لم تكن فابن لبون ذكر فإذا بلغت ستا وثلاثين إلى خمس وأربعين ففيها بنت لبون أنتى، فإذا بلغت ستا وأربعين إلى ستين ففيها حقة طروقة الجمل فإذا بلغت واحدة وستين إلى خمس وسبعين ففيها جذعة فإذا بلغت ستا وسبعين إلى تسعين ففيها بنتا لبون، فإذا بلغت إحدى وتسعين إلى عشرين ومائة ففيها حقتان طروقتا الجمل، فإذا زادت على عشرين ومائة ففي كل أربعين بنت لبون، وفي كل خمسين حقة، ومن لم يكن معه إلا أربع من الإبل فليس فيها صدقة إلا أن يشاء ربها.

وفي صدقة الغنم سائمتها إذا كانت أربعين إلى عشرين ومائة شاة شاة، فإذا زادت على عشرين ومائة إلى مائتين ففيها شاتان، فإذا زادت على مائتين إلى ثلاثمائة ففيها ثلاث شياه فإذا زادت على ثلاثمائة ففي كل مائة شاة، فإذا كانت سائمة الرجل ناقصة من أربعين شاة واحدة فليس فيها صدقة، إلا أن يشاء ربها.

ولا يجمع بين متفرق ولا يفرق بين مجتمع خشية الصدقة، وما كان من خليطين فإنهما يتراجعان بينهما بالسوية، ولا يخرج في الصدقة هرمة ولا ذات عوار، إلا أن يشاء المصدق، وفي الرقة ربع العشر، فإن لم تكن إلا تسعين ومائة فليس فيها صدقة إلا أن يشاء ربها، ومن بلغت عنده

مِنَ الْإِبِلِ صَدَقَةُ الْجَذَعَةِ وَلَيْسَتْ عِنْدَهُ جَذَعَةٌ وَعِنْدَهُ حِقَّةٌ،
فَإِنَّهَا تُقْبَلُ مِنْهُ الْحِقَّةُ، وَيَجْعَلُ مَعَهَا شَاتَيْنِ إِنْ اسْتَيْسَرَتْ لَهُ،
أَوْ عِشْرِينَ دِرْهَمًا، وَمَنْ بَلَغَتْ عِنْدَهُ صَدَقَةُ الْحِقَّةِ وَلَيْسَتْ
عِنْدَهُ الْحِقَّةُ، وَعِنْدَهُ الْجَذَعَةُ، فَإِنَّهَا تُقْبَلُ مِنْهُ الْجَذَعَةُ، وَيُعْطِيهِ
الْمُصَدِّقُ عِشْرِينَ دِرْهَمًا أَوْ شَاتَيْنِ { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kwamba Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuandikia barua kuwa: “Hii ni Swadaqah ya fardhi ambayo Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliifaridhisha kwa Waislam[3] na ambayo Allaah Alimuamrisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aiamrishe.[4] Kwa kila ngamia ishirini na nne au zaidi, kondoo mmoja atolewe kwa kila tano. Wakitimia kati ya ishirini na tano mpaka thelathini na tano, atolewe ngamia jike wa mwaka wa pili.[5] Iwapo hakuna ngamia jike, basi atolewe ngamia dume wa mwaka wa tatu. Wakitimia thelathini na sita hadi arubaini na tano, atolewe ngamia jike wa mwaka wa tatu. Wakitimia arubaini na sita hadi sitini, atolewe ngamia jike wa mwaka wa nne[6] ambaye yu tayari kupandwa. Wakitimia sitini na moja hadi sabini na tano, atolewe ngamia jike wa mwaka wa tano. Wakitimia sabini na sita hadi tisini, watolewe ngamia wawili majike wa mwaka wa tatu, wakitimia tisini na moja hadi mia na ishirini, watolewe ngamia wawili majike wa mwaka wa nne, ambao wako tayari kupandwa. Wakizidi idadi ya mia na ishirini, ngamia mmoja jike wa mwaka wa tatu atolewe kwa kila arubaini, na ngamia mmoja jike wa mwaka wa nne atolewe kwa kila hamsini. Iwapo mtu anao ngamia wanne tu, hatozwi Swadaqah isipokuwa kama mwenye ngamia anataka kutoa.

Kuhusu Swadaqah ya kondoo wanaolishwa, wakitimia idadi ya arubaini hadi mia moja na ishirini, atolewe kondoo mmoja. Wakizidi mia moja na ishirini hadi mia mbili, watolewe kondoo wawili. Wakiwa zaidi ya mia mbili hadi mia tatu, watolewe kondoo watatu. Wakiwa zaidi ya mia tatu, kondoo mmoja atolewe kwa kila mia

moja. Mtu akiwa na idadi ya kondoo chini ya arubaini, hatozwi Swadaqah isipokuwa kama mwenye kondoo hao anapenda.

Wala hawakusanywi waliotawanyika na waliokusanyika wasitenganishwe[7] kwa sababu ya kuogopa Swadaqah. Na wanaomilikiwa na washirika wawili, watadaiana walipane kwa usawa.[8] Kondoo mzee au kondoo mwenye chongo au kondoo dume asitolewe Swadaqah isipokuwa ikiwa mkusanyaji anataka hivyo.[9] Katika fedha: kwa Dirham mia mbili,[10] ilipwe moja ya arubaini, lakini zikiwepo mia moja na tisini tu, hailipii Zakaah isipokuwa kama mwenye fedha hiyo anataka kutoa. Endapo mtu yeyote mwenye idadi ya ngamia ambayo inahitaji kulipia Zakaah ya ngamia jike wa mwaka wa tano lakini hana ngamia huyo ila anaye ngamia wa mwaka wa nne,[11] mtu huyo alipe ngamia huyu pamoja na kondoo wawili iwapo anaweza kuwapata, vinginevyo alipe Dirham ishirini. Ikiwa mtu ana idadi ya ngamia ambayo inahitaji kulipa ngamia jike wa mwaka wa nne,[12] na hana ngamia kama huyu ila anaye ngamia jike wa mwaka wa tano, amtote ngamia huyu na mkusanyaji lazima amrudishie Dirham ishirini au kondoo wawili.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

485.

وَعَنْ مُعَاذِ بْنِ جَبَلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعَثَهُ إِلَى الْيَمَنِ، فَأَمَرَهُ أَنْ يَأْخُذَ مِنْ كُلِّ ثَلَاثِينَ بَقْرَةً تَبِيعًا أَوْ تَبِيعَةً، وَمِنْ كُلِّ أَرْبَعِينَ مُسِنَّةً، وَمِنْ كُلِّ حَالِمٍ دِينَارًا أَوْ عَدْلَهُ مُعَافِرٍ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَاللَّفْظُ لِأَحْمَدَ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ وَأَشَارَ إِلَى إَخْتِلَافٍ فِي وَصْلِهِ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Mu'aadh bin Jabal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma kuenda Yaman, na akamuamrisha achukue ndama wa ng'ombe mwenye umri wa mwaka mmoja, dume au jike kwa kila ng'ombe telathini, na amchukue ng'ombe jike mmoja wa mwaka wa tatu[13] kwa kila arubaini, na Dinari moja kwa kila mtu mzima asiyekuwa Muislam (kama Jizya),[14] au nguo zenye thamani sawa zilizotengenezwa Yaman.” [imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na tamshi hili ni la Ahmad, na At-Tirmidhiy amesema ni Hasan, na akataja kuwa kuna kutofautiana iwapo hii ni Mawswuwl au laa. Na wakaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

486.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {تُؤْخَذُ صَدَقَاتُ الْمُسْلِمِينَ عَلَى مِيَاهِهِمْ} رَوَاهُ أَحْمَدُ
وَلِأَبِي دَاوُدَ: {وَلَا تُؤْخَذُ صَدَقَاتُهُمْ إِلَّا فِي دُورِهِمْ}

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kwa upokezi wa baba yake kutoka kwa babu yake (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swadaqah za Waislamu zipokewe kwenye manywesheo yao (maji).” [Imetolewa na Ahmad]

Na katika Riwaayah ya Abuu Daawuud: “Swadaqah zao zipokewe majumbani mwao tu.”

487.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَيْسَ عَلَى الْمُسْلِمِ فِي عَبْدِهِ وَلَا فِي فَرَسِهِ صَدَقَةٌ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ
وَلِمُسْلِمٍ: {لَيْسَ فِي الْعَبْدِ صَدَقَةٌ إِلَّا صَدَقَةُ الْفِطْرِ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muislamu hana Swadaqah katika mtumwa wake au farasi wake.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Hakuna Swadaqah kwa mtumwa isipokuwa Swadaqatul-Fitwr.”

488.

وَعَنْ بَهْزِ بْنِ حَكِيمٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {فِي كُلِّ سَائِمَةٍ إِبِلٌ: فِي أَرْبَعِينَ بَنْتُ لَبُونٍ، لَا تُفَرَّقُ إِبِلٌ عَنْ حِسَابِهَا، مَنْ أَعْطَاهَا مُوْتَجِرًا بِهَا فَلَهُ أَجْرُهُ، وَمَنْ مَنَعَهَا فَإِنَّا آخِذُوهَا وَشَطْرَ مَالِهِ، عَزَمَةٌ مِنْ عَزَمَاتِ رَبَّنَا، لَا يَحِلُّ لَالٍ مُحَمَّدٍ مِنْهَا شَيْءٌ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَعَلَّقَ الشَّافِعِيُّ الْقَوْلَ بِهِ عَلَى ثُبُوتِهِ

Kutoka kwa Bahz bin Hakiym[15] kutoka kwa baba yake[16] naye kwa upokezi wa babu yake[17] amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kwa ajili ya ngamia arubaini wanaolishwa,[18] atolewe ngamia mmoja jike wa mwaka wa tatu. Hao ngamia wasitenganishwe wakati wa kuwahesabu. Mtu anayelipa Zakaah kwa kutaka thawabu atapata thawabu na mwenye kuzuia Zakaah sisi tutaichukua pamoja na nusu ya mali yake kama fidia ile Aliyoiweka Rabb wetu. Si halali humo chochote kwa Muhammad.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawud na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Al-Haakim]

Ash-Shaafi’iyy[19] amesema ameongezea kauli juu ya uthibitisho wa kutwaa nusu ya mali ya mtu aliyeikwepa Zakaah.

489.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا كَانَتْ لَكَ مِائَتَا دِرْهَمٍ وَحَالَ عَلَيْهَا الْحَوْلُ فَفِيهَا خُمْسَةٌ دَرَاهِمٍ، وَلَيْسَ عَلَيْكَ شَيْءٌ حَتَّى يَكُونَ لَكَ عِشْرُونَ دِينَارًا، وَحَالَ عَلَيْهَا الْحَوْلُ، فَفِيهَا نِصْفُ دِينَارٍ، فَمَا زَادَ فَبِحِسَابِ ذَلِكَ، وَلَيْسَ فِي مَالٍ زَكَاةٌ حَتَّى يَحُولَ عَلَيْهِ الْحَوْلُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَهُوَ حَسَنٌ، وَقَدْ اخْتَلَفَ فِي رَفْعِهِ وَلِلتِّرْمِذِيِّ، عَنْ ابْنِ عُمَرَ: {مَنْ اسْتَفَادَ مَالًا، فَلَا زَكَاةَ عَلَيْهِ حَتَّى يَحُولَ الْحَوْلُ} وَالرَّاجِحُ وَقْفُهُ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ukiwa na Dirham mia mbili zikapitiwa na mwaka, utazilipia Dirham tano, na hupaswi

kulipa chochote mpaka umemiliki Dinari ishirini kwa muda wa mwaka mzima ambapo utazilipia nusu Dinari,[20] kinachozidi idadi hiyo kitahesabiwa hivyo hivyo. Na hakuna katika mali ya Zakaah mpaka ipitiwe na mwaka.” [Imetolewa na Abuu Daawuud. Ni Hasan na wanazuoni wametofautiana kama ni Marfuw’ au la]

Na At-Tirmidhiy alipokea hivi kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “Mtu anayepata mali hapaswi kuilipia Zakaah mpaka mwaka umepita.” [Hadiyth hii imepewa daraja la Mawquwf]

490.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَيْسَ فِي الْبَقَرِ الْعَوَامِلِ صَدَقَةٌ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَالرَّاجِحُ وَقَفَّهُ أَيْضًا

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Hakuna Swadaqah kwa ng’ombe anayefanyishwa kazi.”[21] [Imetolewa na Abuu Daawuud na Ad-Daaraqutwniyy, na ikaitwa Maawquwf]

491.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ، عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ وَلِيَ يَتِيمًا لَهُ مَالٌ، فَلْيَتَّجِرْ لَهُ، وَلَا يَتْرُكْهُ حَتَّى تَأْكُلَهُ الصَّدَقَةُ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَإِسْنَادُهُ ضَعِيفٌ وَلَهُ شَاهِدٌ مُرْسَلٌ عِنْدَ الشَّافِعِيِّ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kwa upokezi wa baba yake kutoka kwa babu yake ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Endapo waliy wa yatima mwenye mali, ni lazima aifanyie biashara, asiache tu mpaka imalizwe na Zakaah.”[22] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na Ad-Daaraqutwniyy kwa Isnaad dhaifu]

Ina tafsiri inayoiunga mkono ambayo ni Mursal iliyosimuliwa na Ash-Shaafi’iyy

492.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي أَوْفَى رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا أَتَاهُ قَوْمٌ بِصَدَقَتِهِمْ قَالَ: "اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَيْهِمْ"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Abiy Awfaa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Watu walipoleta Swadaqah zao kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisema: Ee Allaah! Wabaarik hawa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

493.

وَعَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ الْعَبَّاسَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {سَأَلَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي تَعْجِيلِ صَدَقَتِهِ قَبْلَ أَنْ تَحِلَّ، فَرَخَّصَ لَهُ فِي ذَلِكَ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema ‘Abbaas (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alimuomba Nabiy (الله عَنْهُ) kuharakiza kutoa Swadaqah yake kabla ya wakati, naye akamruhusu[23] kuilipa.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na Al-Haakim]

494.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَيْسَ فِيمَا دُونَ خُمْسِ أَوَاقٍ مِنَ الْوَرَقِ صَدَقَةٌ، وَلَيْسَ فِيمَا دُونَ خُمْسِ ذَوْدٍ مِنَ الْإِبِلِ صَدَقَةٌ، وَلَيْسَ فِيمَا دُونَ خُمْسَةِ أَوْسُقٍ مِنَ التَّمْرِ صَدَقَةٌ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَلَهُ مِنْ حَدِيثِ أَبِي سَعِيدٍ: {لَيْسَ فِيمَا دُونَ خُمْسَةِ أَوْسَاقٍ مِنَ تَمْرٍ وَلَا حَبٍّ صَدَقَةٌ}
وَأَصْلُ حَدِيثِ أَبِي سَعِيدٍ مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdullaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna Swadaqah chini ya Uqiya[24] tano (yaani gramu 595) za fedha, na chini ya ngamia watano, na kwa idadi chini ya kapu (Wasaq)[25] tano (gramu 652) za tende.”[26] [Imetolewa na Muslim]

Na Abuu Sa’iyd alisimuliwa kuwa: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna Swadaqah (Zakaah) chini ya kapu tano za tende au nafaka.”[27]

495.

وَعَنْ سَالِمِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {فِيمَا سَقَتِ السَّمَاءُ وَالْعُيُونُ، أَوْ كَانَ عَثَرِيًّا: الْعُشْرُ، وَفِيمَا سَقَى بِالنَّضْحِ: نِصْفُ الْعُشْرِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ
وَلِأَبِي دَاوُدَ: {أَوْ كَانَ بَعْلًا: الْعُشْرُ، وَفِيمَا سَقَى بِالسَّوَانِي أَوْ النَّضْحِ: نِصْفُ الْعُشْرِ}

Kutoka kwa Saalim bin ‘Abdillaah amesimulia kutoka kwa baba yake (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) kuwa Nabiy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Katika kilichonyeshewa na mvua au chemchem, au kwa unyevu ni moja ya kumi, na katika kilichonyeshewa kwa njia ya umwagiliaji ni moja ya ishirini au ngamia wa ukame ni moja ya ishirini.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Abuu Daawuwd: “Iwapo hayo mazao ya shambani yatakuwa yalimwagiliwa maji na unyevu wa maji ya chini ya ardhi yatalipiwa moja ya kumi; lakini iwapo yatakuwa yamemwagiliwa kwa mifereji ya umwagiliaji, magurudumu ya maji, au ngamia wa ukame yatalipiwa moja ya ishirini.”

496.

وَعَنْ أَبِي مُوسَى الْأَشْعَرِيِّ، وَمُعَاذِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لَهُمَا: {لَا تَأْخُذَا فِي الصَّدَقَةِ إِلَّا مِنْ هَذِهِ الْأَصْنَافِ الْأَرْبَعَةِ: الشَّعِيرِ، وَالْحِنْطَةِ، وَالزَّيْبِ، وَالتَّمْرِ} رَوَاهُ الطَّبْرَانِيُّ، وَالْحَاكِمُ

وَلِلدَّارِ قُطْنِيٍّ، عَنْ مُعَاذٍ: {فَأَمَّا الْقِتَاءُ، وَالْبِطِيخُ، وَالرُّمَّانُ،
وَالْقَصَبُ، فَقَدْ عَفَا عَنْهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ}
وَإِسْنَادُهُ ضَعِيفٌ

Kutoka kwa Abuu Muwsaa Al-Ash'ariyy na Mu'aadh (رَضِيَ اللَّهُ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wamesema kuwa Nabiyy (عَنْهُمَا)
amesema kuwaambia: “Msikusanye Swadaqah ila kwa aina hizi nne
tu zifuatazo: shayiri, ngano, zabibu kavu, na tende.” [Imetolewa na
Atw-Twabaraaniyy na Al-Haakim

Na katika tafsiri ya pili ya Ad-Daaraqutwniyy kwa upokezi wa
Mu'aadh amesema: “Ama matango, matikiti, makomamanga na
miwa ilisamehewa na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
isilipiwe Swadaqah.” [Isnaad yake ni dhaifu]

497.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ أَبِي حَثْمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: أَمَرَنَا
رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا خَرَصْتُمْ، فَخُذُوا،
وَدَعُوا الثُّلُثَ، فَإِنْ لَمْ تَدَعُوا الثُّلُثَ، فَدَعُوا الرَّبْعَ} رَوَاهُ
الْخَمْسَةُ إِلَّا ابْنَ مَاجَهَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Sahl bin Abuu Hatmah[28] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا)
amesema Rasuli wa Allaah alituamrisha: “Mnapokadiria Swadaqah
ya matunda kama tende, chukueni na muache theluthi moja, basi
acheni robo ya Swadaqah inayokadiriwa kwa wamiliki wake.”[29]
[Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu
Daawuud, Ahmad) isipokuwa Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn
Hibbaan na Al-Haakim]

498.

وَعَنْ عَتَّابِ بْنِ أُسَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: أَمَرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَنْ يُخْرَصَ الْعَنْبُ كَمَا يُخْرَصُ النَّخْلُ، وَتُؤْخَذَ زَكَاةُ زَيْبِيَا } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَفِيهِ انْقِطَاعُ

Kutoka kwa ‘Attaab bin Usayd[30] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliamrisha Zakaah ya mizabibu ikadiriwe kama inavyokadiriwa mitende, na Zakaah yake ilipwe kwa zabibu zilizokaushwa kama Zakaah ya mitende ilipwavyo kwa tende zilizokaushwa.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) lakini ina katika Isnaad]

499.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ، { أَنَّ امْرَأَةً أَتَتْ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَمَعَهَا ابْنَةٌ لَهَا، وَفِي يَدِ ابْنَتِهَا مِسْكَتَانِ مِنْ ذَهَبٍ، فَقَالَ لَهَا: "أَتُعْطِينَ زَكَاةَ هَذَا؟" قَالَتْ: لَا. قَالَ: "أَيَسُرُّكَ أَنْ يُسَوِّرَكَ اللَّهُ بِهِمَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ سَوَارَيْنِ مِنْ نَارٍ؟". فَأَلْقَتْهُمَا. } رَوَاهُ الثَّلَاثَةُ، وَإِسْنَادُهُ قَوِيٌّ وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ: مِنْ حَدِيثِ عَائِشَةَ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kwa upokezi wa baba yake kutoka kwa babu yake amesema: Mwanamke mmoja alikuja kwa Nabiyy

(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), alikuwa pamoja na binti yake aliyejaa bangili za dhahabu mkononi mwake. Akamuambia: “Unalipa Zakaah ya bangili hizo?” Akasema: “Hapana.” Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Je, utafurahi[31] iwapo Allaah Atakuwekea bangili mbili za moto badala yake?” Akazitupa. [Imetolewa na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na Isnaad yake ni imara. Imethibitishwa na Al-Haakim kutokana na Hadiyth ya ‘Aaishah]

500.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّهَا كَانَتْ تَلْبَسُ أَوْضَاحًا مِنْ ذَهَبٍ فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَكُنْزٌ هُوَ؟ فَقَالَ: "إِذَا أَدَّيْتُ زَكَاتَهُ، فَلَيْسَ بِكُنْزٍ" } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Yeye alikua akivaa bangili za dhahabu[32] akauliza: Ee Rasuli wa Allaah! Hii ni hazina? Akasema: “Si hazina iwapo utailipia Zakaah yake.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na Ad-Daaraqutwniyy na akaisahihisha Al-Haakim]

501.

وَعَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَأْمُرُنَا أَنْ نُخْرِجَ الصَّدَقَةَ مِنَ الَّذِي نَعُدُّهُ لِلْبَيْعِ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَإِسْنَادُهُ لَيِّنٌ

Kutoka kwa Samurah bin Jundub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akituamrisha tutoe Swadaqah katika vitu tunavyo viandaa kwa biashara.”[33] [Imetolewa na Abuu Daawuud, na Isnaad yake ni dhaifu]

502.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: "وَفِي الرِّكَازِ: الْخُمْسُ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Na katika hazina iliyofukiwa chini hutozwa moja ya tano.”[34] [Al-Bukhaariy, Muslim]

503.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ فِي كَنْزٍ وَجَدَهُ رَجُلٌ فِي خَرِبَةٍ: "إِنْ وَجَدْتَهُ فِي قَرْيَةٍ مَسْكُونَةٍ، فَعَرِّفْهُ، وَإِنْ وَجَدْتَهُ فِي قَرْيَةٍ غَيْرِ مَسْكُونَةٍ، فَفِيهِ وَفِي الرِّكَازِ: الْخُمْسُ" } أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَةَ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb amemnukuu baba yake, kuwa babu yake (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesimulia kuwa: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

(عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu hazina alioipata mtu mahala pasipotumika: “Ukiipata kwenye makazi ya watu, lazima uwajulishe. Ukiipata pasipo makazi na katika hazina iliyozikwa basi ni moja ya tano.” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa Isnaad nzuri]

504.

وَعَنْ بِلَالِ بْنِ الْحَارِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَخَذَ مِنَ الْمَعَادِنِ الْقَبَلِيَّةِ الصَّدَقَةَ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa Bilaal bin Al-Haarith[35] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokea Swadaqah ya machimbo ya Al-Qabaliyyah.”[36] [Imetolewa na Abuu Daawuwd]

[1] Maana ya Zakaah ni “Kuongezeka na kutakasika.” Kwa sababu malipo ya Zakaah hupelekea kuongezeka kwa mali na kwa hivyo huhesabika kuwa ni sababu ya kutakasika kwake, wajibu huu umepewa jina la Zakaah na Shariy’ah. Zakaah ilifaradhishwa mwaka wa 2 A.H., kabla ya amri ya Swawm.

[2] Hadiyth inatufundisha kuwa Zakaah ni lazima kwa matajiri miongoni mwa Waislam. Zakaah hii ni ya kuwapa msaada Waislam maskini, na hawapewi wasiokuwa Waislam. Tunafunzwa zaidi kuwa, Zakaah inayokusanywa katika mji mmoja sharti wagawiwe maskini wa mji huo huo.

[3] Wakati wa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alipomteua Anas kuwa Gavana wa Bahrayn kwa niaba yake, alimpa maagizo haya yanayohusu Zakaah kwa maandishi.

[4] Kuhusu usahihi wa Hadiyth hii, yaani Isnaad ni sahihi kabisa. Kuhusu maandishi, nayo ni wazi kabisa, na kuna maafikiano ya pamoja ya Maswahaba wa Nabiyy (ﷺ) kuhusu usahihi wake. Hakuna Swahaba hata mmoja wa Rasuli wa Allaah (ﷺ) aliyewahi kuikanusha Hadiyth hii.

[5] بِنْتُ مَخَاضٍ (Bint Makhaadhw) ni neno linalotumika kwa ngamia mwenye umri wa mwaka mmoja na ameingia katika mwaka wa pili wa umri wake.

[6] حِقَّةٌ (Hiqqah) ni neno linalotumika kwa ngamia mwenye umri wa miaka mitatu na ameingia katika mwaka wa nne wa umri wake, na ana uwezo wa kupandwa.

[7] Mfano wa kuunganisha mali ya Zakaah zilizotengana ni kama ifuatavyo: “Kuna watu wawili wana kundi la mbuzi hamsini kila mmoja wao, kwa hivyo wanatakiwa kutoa mbuzi mmoja kila mtu kutoka katika hisa zao. Endapo watu hawa wawili wataunganisha makundi yao mawili kuwa kundi moja, watapata faida ya kutoa mbuzi mmoja tu kwa pamoja kama Zakaah ya mbuzi mia moja, kwa sababu Zakaah ya mbuzi mia moja ni mbuzi mmoja tu.” Mfano wa kutenganisha kesi za Zakaah zilizoungana ni kama ifuatavyo: “Watu wawili wanamiliki kundi moja la mbuzi hamsini kwa ubia wa sawa kwa sawa. Kwa hivyo Zakaah ya mbuzi hawa hamsini itakuwa ni mbuzi mmoja. Lakini wakiligawanya kundi lao na kuwatenganisha ili kila mmoja awe na mbuzi ishirini na tano tu, wataepuka kutoa Zakaah kwa kuwa idadi ya mbuzi wa kila mmoja ni chini ya mbuzi arubaini. Hali kadhalika mkusanyaji wa Zakaah asithubutu kuunganisha wala kutenganisha mali za watu, yaani akiwakuta watu wawili wakiwa na mbuzi thelathini kila mmoja na kwa hivyo wanasamehewa kutoa Zakaah, mkusanyaji hana ruhusa ya kuunganisha hayo makundi mawili mbalimbali ya watu hao wawili na kulifanya liwe kundi moja ili adai wale watu walipe mbuzi mmoja.”

[8] Kwa mfano watu wawili wanamiliki mbuzi mia moja na arubaini. Mmoja anamiliki arubaini wakati mwenziwe anamiliki mia moja. Zakaah hapa inakuwa mbuzi wawili. Lakini ikiwa mmiliki wa mbuzi arubaini anamuambia mwenziwe hivi: “Ni bora ulipe Zakaah ya mbuzi mmoja na nusu, na mimi nilipe nusu ya mbuzi mmoja.” Hivyo haitakuwa sahihi. Shariy’ah yataka mmiliki wa mbuzi arubaini alipe mbuzi mmoja kamili, na

mmiliki wa mbuzi mia pia naye alipe mbuzi mmoja tu kamili kama Zakaah yake.

[9] Hii inamaanisha kwamba, mtu anayetaka kutoa Zakaah asijaribu kutoa vitu vyenye dosari, wala mkusanyaji au mpokeaji naye asijaribu kuchukua vitu vizuri zaidi kuliko vyote. Vitu vitolewe vile vyenye thamani ya wastani.

[10] Moja ya kumi na mbili ya Uqiya moja ya dhahabu, kwa thamani.

[11] جَذْعَةٌ (Jadha'ah) ni neno linalotumika kwa ngamia jike ambaye ana miaka mine na ameingia mwaka wa tano wa umri wake.

[12] حِقَّةٌ (Hiqqah) ni neno linalotumika kwa ngamia jike wa miaka mitatu na ameingia mwaka wa nne wa umri wake.

[13] Ng'ombe na nyati ni jamii moja ya wanyama. Wote hao, wa jinsia zote mbili, wanajumuishwa katika hesabu. Mtu anayemiliki chini ya ng'ombe thelathini hatozwi Zakaah, wakitimia thelathini, hutozwa ndama mwenye umri wa mwaka mmoja. Wanyama anaowamiliki mtu wakiwa kati ya arubaini na sitini na tisa, Zakaah itakuwa ndama wa miaka miwili. Wakitimia sabini Zakaah ni ile ile, yaani ndama mmoja wa miaka miwili pamoja na ndama mmoja wa mwaka mmoja.

[14] Jizyah ni kodi ya kichwa anayoilipa mtu asiyekuwa Muislam anayeishi katika nchi ya Kiislam.

[15] Bahz bin Hakiym ndiye Abuu 'Abdil-Maalik Bahz bin Hakiym bin Mu'aawiya bin Haida Al-Qushayr Al-Basri. Alikuwa Taabi'i wa daraja la sita. Uaminifu au utegemewaji wake umekanushwa. Abuu Daawuwd amesema: "Ahaadiyth zake ni sahihi." Pia Ibn Maa'in, Ibn Al-Madiniy, na An-Nasaaiy walimkubali. Lakini Abuu Haatim amesema: "Huyo siyo mtaalam wa Hadiyth." Naye Ibn Hibbaan amesema: "Alikuwa na makosa mengi katika Hadiyth." Alikufa baada ya miaka ya 140 A.H. au kabla ya miaka sitini.

[16] Na huyu babake Bahz pia ni Taabi'i ambaye Ibn Hibbaan alimhesabu kuwa ni mpokezi na msimuliaji mwaminifu wa Hadiyth.

[17] Babu yake ni Mu'aawiyah bin Hayda bin Mu'aawiya bin Qushayr bin Ka'b Al-Qushayr, na alikuwa Swahaba aliyelowea Basra na alikuwa anazo Ahaadiyth.

[18] Hali ya Zakaah ya ng'ombe ni kwamba sharti wawe wazima na nguvu za kutosha kijilisha wao wenyewe. Hali hii ilitajwa hususan kwa mbuzi na ngamia. Na kanuni hiyo hiyo imeamriwa kwa ajili ya ng'ombe na nyati.

[19] Hadiyth hii inadhihirisha kwamba, iwapo mtu halipi Zakaah kwa hiari yake, Serikali ya ya Kiislam inaweza kumtoza faini yenye thamani ya nusu ya bidhaa zake na wanaweza kuichukua kwa nguvu. Kutozwa hivyo kwa nguvu kutakidhi deni alilonalo huyo mtu, lakini atanyimwa thawabu.

[20] Hadiyth hii inaongelea Zakaah inayotozwa katika dhahabu na fedha. Uzito wa fedha ni kuanzia Dirham mia mbili na zaidi. Uzito hasa wa fedha unaostahili kulipiwa Zakaah ni tola hamsini na nusu (sawa na gramu 611.5) na Zakaah inayotozwa kwa kiasi itakuwa moja ya arubaini. Halikadhalika kiasi cha dhahabu ipaswayo kutolewa Zakaah ni tola saba na nusu (sawa na gramu 87), Zakaah ipaswayo kulipwa kwa kiasi hiki ni moja ya arubaini pia. Na hata kwa pesa za noti hulipiwa hiyo hiyo 1/40.

[21] Ng'ombe wafanyao kazi za kulima, kuchota na kumwagia maji, na wasafirishaji, ndio wanaohusika.

[22] Kuna tofauti za maoni ya Wanazuoni kuhusu iwapo mali ya yatima itolewe Zakaah au laa. Juu ya kuwepo kukhitilafiana, ni bora kuilipia Zakaah.

[23] Siku na nyakati za Hajj, Swalaah na Swawm zote zimepangwa wazi. Lakini kuhusu Zakaah hakuna wakati maalumu. Ulipaji wake unaweza kuahirishwa au pia unaweza kulipwa mapema, ingawa huwa inakuwa deni baada ya muda wa mwaka mmoja tu.

[24] Kwa kuwa thamani ya Uqiya moja ni Dirham 40 (au gramu 128), basi Waqiya tano zitakuwa sawa sawa na Dirham 200.

[25] Takribani kilo kumi na mbili unusu.

[26] Kwa mujibu wa vipimo vya siku hizi, kiasi cha Zakaah ipasavyo kulipwa kwa kila maund 20 za nafaka (yaani quintal 8), itakuwa maund moja ya nafaka (yaani takribani kilo 40). Iwapo kiasi cha nafaka ni chini ya quintal 8, hakuna kuilipia hiyo Zakaah hiyo. Quintal 8 ni sawa na Wasq 5 ambayo imetajwa katika Hadiyth hii. Endapo mtu atamiliki zaidi ya

gramu 87 za dhahabu, huyo analazimika ailipie Zakaah. Na endapo mtu atamiliki zaidi ya gramu 611.5, basi huyu pia inapaswa ailipie Zakaah.

[27] Nafaka yoyote inayoweza kuhifadhiwa kwa mwaka mmoja, inapaswa ilipiwe Zakaah. Ngano, shayiri, mpunga, mtama, mahindi ya Kihindi, mahindi jamii ya kunde na choroko n.k. vyote vinaingia katika kundi hili. Zakaah ya hivi hutegemea kiasi cha kazi na adha itokanayo na kuzalisha hivi. Mazao ya ardhi ambayo yamemwagiliwa maji na ya mafuriko, au mbubujiko wa asili au mito, yatalipiwa moja ya kumi ya kazi ya kuyazalisha. Ikiwa ardhi imemwagiliwa na maji ya kisima au kwa kulipia pesa maji yale kama maji ya mifereji, basi mazao yake yatalipiwa Zakaah ya moja ya ishirini tu ya jumla yake.

[28] Sahl bin Abiy Hatmah, jina lake halisi ni ‘Abdullaah au ‘Aamir bin Sa’ida bin ‘Aamir Al-Answaar Al-Khazraj Al-Madaniy. Alikuwa Swahaba aliyezaliwa mnamo mwaka wa 3A.H. aliloweza Kufa na anahesabika kuwa yu mkazi wa Al-Madiynah ambako alifia wakati wa ugavana wa Mus’ab bin Az-Zubayr.

[29] Maana ya neno la kiarabu “Kharsw” ni kubahatisha au kudhanja, yaani kukisia kiasi cha matunda yanayoweza kuzaliwa baada ya kukomaa na kuiva. Mtu kama huyo ni sharti aifanye kazi yake kwa uaminifu mkubwa sana. Kanuni ya wakusanyaji Zakaah ni kiasi cha theluthi moja ya kiasi hicho alichokikadiria. Kama hakubaliani nacho basi lazima aache robo yake, au mara nyingine mmiliki anaweza kuwapa majirani zake baadhi yake.

[30] ‘Ataab bin Usayd bin Abiy Al-‘Ays bin Umayyah bin ‘Abd Shams Al-Umawi Al-Makki alikuwa Swahaba. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ) alimteua aitawale Makkah katika mwaka wa kuiteka, kwa kuwa alikuwa akienda Humayn na akaendelea kuitawala hadi Abuu Bakr alipofariki. Inasemekana naye alifariki siku hiyo hiyo aliyofariki Abuu Bakr. Inasemwa pia kuwa aliishi hadi mwisho wa Ukhalifa wa ‘Umar.

[31] Suala la Zakaah ya mapambo ya dhahabu lina mvutano. Lakini rai ya wengi ni kuwa iyo Zakaah ni lazima ilipwe, na Hadiyth hii ni ushahidi wake.

[32] أَوْضَاح (Awdhwaah) ni wingi wa وَضْع. Hiyo ilikuwa ni aina ya mapambo ambayo zamani yalikuwa yakitengenezwa kwa fedha. Kwa sababu ya kumeremeta kwake, ikaitwa أَوْضَاح, baadaye ikawa inatengenezwa kwa dhahabu pia. Kwa hivyo Hadiyth hii inathibitisha

kuwa mapambo ya fedha na dhahabu yanapaswa kulipiwa Zakaah. Kuna mapambo mengine yasiyokuwa ya dhahabu na fedha, yasiyostahili kulipiwa Zakaah. Hayo ni mapambo ya lulu, zumaridi, johari, rubi, marijani na vito vingine.

[33] Kwa hivyo hii inatufahamisha, bidhaa zote za biashara hustahili kulipiwa Zakaah.

[34] Mali yoyote iliyofukuliwa kutoka ardhini ni الرِّكَاز (Ar-Rikaaz), yaani ni hazina iliyofichwa ilimradi ni ya kutoka zama za wasiokuwa Waislam, na ni lazima kuweka moja ya tano ya mali hiyo katika hazina ya Kiislam. Hii haina lile sharti la kuwa hiyo moja ya tano iwekwe baada ya kupita mwaka mmoja.

[35] Alipewa jina la utani wa ‘Abdur-Rahmaan, na alikuwa miongoni mwa wajumbe wa kwanza kumzuru Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kule Al-Madiynah kutoka katika kabila la Muzaynah mnamo mwaka wa 5 A.H. alishika bendera ya Muzaynah wakati wa kuiteka Makkah. Aliishi nje ya Al-Madiynah na baadaye akahamia Basra. Alifariki mnamo mwaka wa 60 A.H. huku akiwa na miaka 80.

[36] Qabaliyyah ni jina la mahala iliyo pwani ya bahari umbali wa safari ya siku tano kwa kupanda ngamia kutoka Al-Madiynah.

02-Mlango Wa Zakaatul-Fitwr

بَابُ صَدَقَةِ الْفِطْرِ

Mlango Wa Zakaatul-Fitwr

505.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {فَرَضَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الْفِطْرِ، صَاعًا مِنْ تَمْرٍ، أَوْ صَاعًا مِنْ شَعِيرٍ: عَلَى الْعَبْدِ وَالْحُرِّ، وَالذَّكَرِ، وَالْأُنْثَى، وَالصَّغِيرِ، وَالْكَبِيرِ، مِنَ الْمُسْلِمِينَ، وَأَمَرَ بِهَا أَنْ تُؤَدَّى قَبْلَ خُرُوجِ النَّاسِ إِلَى الصَّلَاةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِابْنِ عَدِيٍّ مِنْ وَجْهِ آخَرَ ، وَالذَّارِقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ: {اغْنَوْهُمْ عَنِ الطَّوَافِ فِي هَذَا الْيَوْمِ}

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliamrisha Zakkaatul-Fitwr kwa mtumwa, mtu huru, mwanaume, mwanamke, kijana, na mzee miongoni mwa Waislam, pishi moja (sawa sawa na takribani kilogramu mbili na nusu) ya tende zilizokaushwa, au Swaa’ moja ya shayiri, na akaamrisha itolewe kabla watu hawajaondoka kuenda kuswali Swalaah ya ‘Iydul-Fitwr.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Ibn ‘Adiyy na Ad-Daaraqutwniy alisimulia Hadiyth hiyo kwa Isnaad dhaifu: “Watosheni (wapeni mahitaji yao) dhidi ya kuenda njiani wakiombaomba katika siku hii.”

506.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كُنَّا نُعْطِيهَا فِي زَمَانِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَاعًا مِنْ طَعَامٍ، أَوْ

صَاعًا مِنْ تَمْرٍ، أَوْ صَاعًا مِنْ شَعِيرٍ، أَوْ صَاعًا مِنْ زَبِيبٍ {
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ: {أَوْ صَاعًا مِنْ أَقِطٍ}
قَالَ أَبُو سَعِيدٍ: {أَمَّا أَنَا فَلَا أَزَالُ أَخْرِجُهُ كَمَا كُنْتُ أَخْرِجُهُ
فِي زَمَنِ رَسُولِ اللَّهِ}
وَلِأَبِي دَاوُدَ: {لَا أَخْرِجُ أَبَدًا إِلَّا صَاعًا}

Kutoka kwa Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Wakati alipokuwepo Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), tulikua
tukitoa Pishi moja ya nafaka[1] kama Zakkaatul-Fitwr, au tende
kavu, au shayiri, au zabibu kavu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine inasema: “Au Swaa’ pishi moja ya
jibini.”

Abuu Sa'iyd amesema: “Mimi sitaacha kutoa kama nilivyokuwa
nikitoa (Pishi) wakati Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
alipokuwa hai.”

Na tafsiri ya Abuu Daawuwd inasema: “Sijawahi kutoa Swadaqah ila
Pishi.”

507.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {فَرَضَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الْفِطْرِ، طُهْرَةً لِلصَّائِمِ مِنَ اللَّغْوِ،

وَالرَّفَثِ، وَطُعْمَةً لِلْمَسَاكِينِ، فَمَنْ أَدَّاهَا قَبْلَ الصَّلَاةِ فَهِيَ زَكَاةٌ مَقْبُولَةٌ، وَمَنْ أَدَّاهَا بَعْدَ الصَّلَاةِ فَهِيَ صَدَقَةٌ مِنَ الصَّدَقَاتِ. { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliamrisha Zakkaatul-Fitwr iwe ndiyo utakaso wa mtu anayefunga Swawm dhidi ya maongezi ya kipuuzi na uchafu, pamoja na kuwa chakula kwa watu maskini. Mtu yeyote atailipa hiyo kabla ya Swalaah ya ‘Iydul-Fitwr itakubaliwa kama Zakaah. Lakini mtu akiilipa hiyo baada ya Swalaah ya ‘Iydul-Fitwr[2] itahesabika kuwa ni Swadaqah miongoni mwa Swadaqah zingine.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na Ibn Maajah na akaisahihisha Al-Haakim]

[1] Neno la Kiarabu: “طَعَامٍ” (Twa’aam) hutumika kwa aina mbalimbali za nafaka. Inaweza kutumika kwa ngano, shairi, na tende pia. Kwa ujumla yaweza kutumika kwa kila zao la kilimo.

[2] Hii inamaanisha kwamba, mtu akiilipa hiyo Zakaatul-Fitwr (Zakaah ya kufungulia Swawm), haimuondoshei wajibu wala hapati thawabu zinazohusiana na malipo hayo kama Zakaah. Hata hivyo ulipaji huu haupotei hivi hivi kwani atapata thawabu za tendo la kawaida tu la Swadaqah. Ni bora kulipa Pishi moja nzima (Kilo 2.6) kama Zakaatul-Fitwr, kwani ule usimulizi unaotaja nusu ya pishi siyo sahihi.

03-Mlango Wa Swadaqah Za Khiari

بَابُ صَدَقَةِ التَّطَوُّعِ

03-Mlango Wa Swadaqah Za Khiari

508.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {سَبْعَةٌ يُظِلُّهُمْ اللَّهُ فِي- ظِلِّهِ يَوْمَ لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّهُ....} فَذَكَرَ الْحَدِيثَ وَفِيهِ: {وَرَجُلٌ تَصَدَّقَ بِصَدَقَةٍ فَأَخْفَاهَا حَتَّى لَا تَعْلَمَ شِمَالُهُ مَا تُنْفِقُ يَمِينُهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu saba Allaah Atawafunika katika kivuli Chake tu, na akawataja miongoni mwao ni mtu anayetoa Swadaqah kwa siri hata mkono wake wa kushoto haujui mkono wake wa kuume umetoa nini.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

509.

وَعَنْ عُقْبَةَ بْنِ عَامِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {كُلُّ إِمْرٍ فِي ظِلِّ صَدَقَتِهِ حَتَّى يُفْصَلَ بَيْنَ النَّاسِ} رَوَاهُ ابْنُ حِبَّانَ وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Uqbah bin ‘Aamir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

akisema: “Kila mmoja atakuwa chini ya kivuli[1] cha Swadaqah yake hadi ihukumiwe baina ya watu.” [Imetolewa na Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

510.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَيُّمَا مُسْلِمٍ كَسَا مُسْلِمًا ثَوْبًا عَلَى عُرِّي كَسَاهُ اللَّهُ مِنْ خُضْرِ الْجَنَّةِ، وَأَيُّمَا مُسْلِمٍ أَطْعَمَ مُسْلِمًا عَلَى جُوعٍ أَطْعَمَهُ اللَّهُ مِنْ ثَمَارِ الْجَنَّةِ، وَأَيُّمَا مُسْلِمٍ سَقَى مُسْلِمًا عَلَى ظَمَأٍ سَقَاهُ اللَّهُ مِنَ الرَّحِيقِ الْمَخْتُومِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَفِي إِسْنَادِهِ لِيْنٌ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muislamu yeyote atakayemvisha Muislam aliye uchi, Allaah Atamvisha huyo nguo za kijani za Al-Jannah. Na Muislam yeyote atakayemlisha Muislam mwenye njaa, Allaah Atamlisha matunda ya Al-Jannah. Na Muislam yeyote atakayemnywesha Muislam mwenye kiu, Allaah Atamnywesha Ar-Rahiq Al-Makhtuwm (kinywaji kizuri cha mvinyo Al-Jannah).” [Imetolewa na Abuu Daawud na kuna udhaifu katika mlolongo wa wapokezi]

511.

وَعَنْ حَكِيمِ بْنِ حِزَامٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الْيَدُ الْعُلْيَا خَيْرٌ مِنَ الْيَدِ السُّفْلَى، وَابْدَأْ بِمَنْ

تَعُولُ، وَخَيْرُ الصَّدَقَةِ عَنْ ظَهْرِ غِنَى، وَمَنْ يَسْتَغْفِرْ يُعَفِّهِ
اللَّهُ، وَمَنْ يَسْتَغْنِ يُغْنِهِ اللَّهُ. { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Hakiym bin Hizaam (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkono wajuu ni
mbora kuliko wa chini, na anza kwa kuwapa Swadaqah
wanaokutegemea.[2] Na Swadaqah bora ni inayotolewa kwa ajili ya
kujitosha, na yeyote anayejizuia kuwaomba watu Swadaqah, Allaah
Atamfanya aridhike, na kila anayeridhika na anachopewa na Allaah,
basi Allaah Atamfanya awe anajitosheleza.” [Al-Bukhaariy, Muslim
na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

512.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { قِيلَ يَا رَسُولَ اللَّهِ:
أَيُّ الصَّدَقَةِ أَفْضَلُ؟ قَالَ: "جُهْدُ الْمُقِلِّ، وَابْدَأْ بِمَنْ تَعُولُ" }
أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ
حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa Swadaqah gani
iliyokuwa bora zaidi? Akasema: “Ni juhudi ya mwenye mali kidogo
sana anayoweza kutoa, na aanze na watu wanaomtegemea yeye.”
[Imetolewa na Ahmad, na Abuu Daawuwd, na wakaisahihisha Ibn
Khuzaymah, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

513.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "تَصَدَّقُوا
 " فَقَالَ رَجُلٌ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، عِنْدِي دِينَارٌ؟ قَالَ: "تَصَدَّقْ بِهِ
 عَلَى نَفْسِكَ " قَالَ: عِنْدِي آخَرُ، قَالَ: "تَصَدَّقْ بِهِ عَلَى وَلَدِكَ
 " قَالَ: عِنْدِي آخَرُ، قَالَ: "تَصَدَّقْ بِهِ عَلَى خَادِمِكَ " قَالَ:
 عِنْدِي آخَرُ، قَالَ: " أَنْتَ أَبْصَرُ " { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ
 وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena kuwa
 Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Toeni
 Swadaqah.” Mtu mmoja akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Ninayo
 dinari moja tu.” Akasema: “Jitolee Swadaqah mwenyewe.” Yule mtu
 akasema: “Ninayo nyingine.” Akasema: “Mtolee Swadaqah
 mwanao.” Yule mtu akasema: “Ninayo nyingine.” Akasema: “Mtolee
 Swadaqah mkeo.” Yule mtu akasema tena: “Ninayo nyingine.”
 Akasema: “Mtolee Swadaqah mtumishi wako.” Yule mtu akasema:
 “Ninayo nyingine.” Akasema: “Wewe unajua zaidi uifanyie nini
 hiyo.” [Imetolewa na Abuu Daawud na An-Nasaaiy, na
 wakaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

514.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ
 عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا أَنْفَقَتِ الْمَرْأَةُ مِنْ طَعَامِ بَيْتِهَا، غَيْرَ مُفْسِدَةٍ،
 كَانَ لَهَا أَجْرُهَا بِمَا أَنْفَقَتْ وَلِزَوْجِهَا أَجْرُهُ بِمَا اكْتَسَبَ
 وَلِلْخَازَنِ مِثْلُ ذَلِكَ، وَلَا يَنْقُصُ بَعْضُهُمْ أَجْرَ بَعْضٍ شَيْئًا {
 مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamke akitoa Swadaqah sehemu ya chakula cha nyumbani mwake bila ubadhirifu,[3] atapata thawabu kwa alichotoa, mumewe atapata thawabu kwa alichochuma, na aliyekihifadhi naye atapata sawa na hizo, wala hakuna atakayepunguziwa thawabu[4] zake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

515.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {جَاءَتْ زَيْنَبُ امْرَأَةُ ابْنِ مَسْعُودٍ، فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّكَ أَمَرْتَ الْيَوْمَ بِالصَّدَقَةِ، وَكَانَ عِنْدِي حُلِيٌّ لِي، فَأَرَدْتُ أَنْ أَتَصَدَّقَ بِهِ، فَزَعَمَ ابْنُ مَسْعُودٍ أَنَّهُ وَوَلَدُهُ أَحَقُّ مَنْ تَصَدَّقْتُ بِهِ عَلَيْهِمْ، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "صَدَقَ ابْنُ مَسْعُودٍ، زَوْجُكَ وَوَلَدُكَ أَحَقُّ مَنْ تَصَدَّقْتُ بِهِ عَلَيْهِمْ".} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Alikuwa Zaynab[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) mke wa Ibn ‘Mas-‘uwd akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Leo umeamrisha Swadaqah, nami nilikuwa na vito vyangu, kwa hivyo ninataka nivitoe hivyo kama Swadaqah, lakini Ibn Mas-‘uwd alidai kuwa yeye na watoto wake wana haki zaidi niwatolee wao Swadaqah.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Ibn Mas-‘uwd amesema kweli, kuwa mumeo na watoto wana haki zaidi ya kunufaishwa na Swadaqah[6] yako.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

516.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا يَزَالُ الرَّجُلُ يَسْأَلُ النَّاسَ حَتَّى يَأْتِيَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَيْسَ فِي وَجْهِهِ مِزْعَةٌ لَحْمٍ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtu hataacha kuomba hadi aje siku ya Qiyaamah hana usoni mwake nyama.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

517.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ سَأَلَ النَّاسَ أَمْوَالَهُمْ تَكَثُّرًا، فَإِنَّمَا يَسْأَلُ جَمْرًا، فَلْيَسْتَقِلَّ أَوْ لِيَسْتَكْثِرْ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayeomba watu mali zao ili aongezee mali yake mwenyewe, huyo anajipalilia makaa ya moto; kwa hivyo hebu aombe kidogo au kingi (na adhabu itamsubiri).”[7] [Imetolewa na Muslim]

518.

وَعَنْ الزُّبَيْرِ بْنِ الْعَوَّامِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَأَنْ يَأْخُذَ أَحَدُكُمْ حَبْلَهُ، فَيَأْتِيَ بِحُزْمَةِ الْخَطْبِ عَلَى ظَهْرِهِ، فَيَبِيعَهَا، فَيَكْفَ اللَّهُ بِهَا وَجْهَهُ، خَيْرٌ لَهُ مِنْ أَنْ يَسْأَلَ النَّاسَ أَعْطَوْهُ أَوْ مَنَعُوهُ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Az-Zubayr bin Al-‘Awwaam amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu kuchukua kamba yake, alete mzigo wa kuni mgongoni kwake, auuze, kwa huo, Allaah Ahifadhie heshima yake ni bora, kuliko kuombaomba watu, wawe wanakupa au wanakunyima.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

519.

وَعَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْمَسْأَلَةُ كَذٌّ يَكْذُبُ بِهَا الرَّجُلُ وَجْهَهُ، إِلَّا أَنْ يَسْأَلَ الرَّجُلُ سُلْطَانًا، أَوْ فِي أَمْرٍ لَا بُدَّ مِنْهُ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Samurah bin Jundub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuomba ni mikwaruzo inayoharibu uso wa mtu isipokuwa akimuomba mtawala,[8] au katika hali ambayo hana budi nayo.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy ambaye pia aliisahihisha]

[1] Hicho ‘Kivuli’ kinamaanisha kuwa kila Swadaqah inayotolewa itageuka kuwa mwavuli kwa mtoaji Swadaqah ambao utamkinga dhidi ya

jua lichomalo sana Siku ya Qiyaamah. Moja ya faida za Swadaqah ya khiari ni kuwa itakuwa kama dawa ya mapungufu katika Zakaah ya fardhi.

[2] Imekatazwa kuwapa Swadaqah watu baki kama watu wa familia yako wana shida kubwa. Kwa mujibu wa Muslim, imesimuliwa na Thawbaan kuwa, sehemu bora ya pesa ni ima ile iliyotomika kwa familia yako, au pesa zilizotumika kwa ajili ya farasi aliyetumika katika vita vya Jihaad (vita ya kidini) au pesa zilizotumika kwa marafiki.

[3] Inamaanisha kuwa, ilimradi mke huyo hana dhamiri ya siri ya kuidhuru nyumba ya mumewe, anaweza kutoa Swadaqah kama ilivyo desturi. Anaweza kumpa muombaji maskini mikate au unga. Ikiwa inahitajika Swadaqah zaidi, basi ni sharti apate idhini kutoka kwa mume wake.

[4] Inamaanisha kwamba, Allaah (سبحانه وتعالى) Atampa kila mtu thawabu au zawadi kamili kwa Ukarimu Wake. Si kama Anayo zawadi moja tu anayoigawanya hiyo hiyo miongoni mwa watu wote. Hii inathibitisha kuwa mtu sharti umsaidie kila mtu kutenda matendo mema ili na yeye apate zawadi.

[5] Zaynab alikuwa anatoka kwa Banuw Thaqiyf, na babake aliitwa Mu'aawiyah, au 'Abdullaah bin Mu'aawiyah, au Abuu Mu'aawiyah. Alisimulia kutoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), mume wake, 'Umar bin Al-Khatwaab, mwanawe, mpwa wake, na wengine walisimuliwa kutoka kwake.

[6] Hilo neno Swadaqah linawahusu watu wote, iwe ni tendo la khiari au la Swadaqah au tendo la lazima la kulipa Zakaah au Swadaqatul-Fitw. Qur-aan tukufu imelitaja neno hili la Swadaqah pale tu ilipokuwa ikieleza mambo kuhusu kugawanya na kusambaza fedha za Zakaah. Inapokuwa hiyo Swadaqah ya khiari siyo kubwa sana, basi kwa kawaida huashiria tendo la wajibu la kutoa Swadaqah (Zakaah). Hapa inaelekea kuwa ni ulipaji wa lazima wa Swadaqah kwani mtu hana haja ya kuomba ruhusa ya mtu yeyote kuhusu Swadaqah ya khiari. Wengi wa Wanazuoni wanaafikiana kuwa mke anaweza kumpa mumewe. Halikadhalika kuna maafikiano ya maoni kuwa mwanaume hawezi kumpa Zakaah mkewe.

[7] Iwapo mtu asiyestahili anakusanya pesa kwa kuombaomba, atapata fedheha na aibu Siku ya Qiyaamah na atakabiliwa na mateso ya motoni. Kuna aina tatu za watu wanaostahili kupewa pesa ya Zakaah:

(a) Mtu ambaye mali yake inateketezwa ghafla na balaa lisilotazamiwa kiasi kwamba hana kitu hata cha kula. Mtu kama huyo anaweza kuomba pesa za Zakaah ili ziweze kumkimu.

(b) Mtu ambaye ameadhibiwa kimaonezi, au mtu aliyemkingia kifua au alisaini dhamana au mkataba fulani kwa ajili ya mtu mwingine na sasa analazimishwa alipe pesa kwa ajili ya huyo mtu mwingine ingawa hana pesa za kutosha kulipia hilo. Mtu kama huyo ana haki ya kupewa pesa za Zakaah ili awe na pesa za kutosha kulipia deni hilo.

(c) Mtu ambaye anafanya kazi au anataka kwa dhati kufanya kazi kwa uaminifu na bidii zote lakini haipati kazi, au mwenye pato dogo kuliko kiwango kinachotosheleza matumizi yake na kwa hivyo analazimika kukabiliwa na njaa.

[8] Hii inatujulisha kwamba kumuendea mfalme na kumuomba msaada wa kipesa inaruhusiwa. Mfalme anaruhusiwa ima kumpa mtu Swadaqah kutoka katika malipo ya Zakaah, au kutoka katika Khumus (moja ya tano ya mali iliyotokana na ngawira za vita na kupangiwa ihifadhiwe katika hazina). Iwapo muombaji ni maskini sana, anaweza kupewa kutoka kwenye Zakaah. Lakini akiwa ni tajiri, asipewe pesa kutoka katika Zakaah, bali apewe kutoka katika Khumus (fedha kutoka hazina ya serikali).

04-Mlango Wa Ugawaji Wa Swadaqah

بَابُ قَسْمِ الصَّدَقَاتِ

04-Mlango Wa Ugawaji Wa Swadaqah

عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَحِلُّ الصَّدَقَةُ لِغَنِيِّ إِلَّا لِخَمْسَةٍ: لِعَامِلٍ عَلَيْهَا، أَوْ رَجُلٍ اشْتَرَاهَا بِمَالِهِ، أَوْ غَارِمٍ، أَوْ غَازٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، أَوْ مَسْكِينٍ تُصَدَّقَ عَلَيْهِ مِنْهَا، فَأَهْدَى مِنْهَا لِغَنِيٍّ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَأَعْلَى بِالْإِسْالِ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swadaqah si halali kwa anayejitosheleza isipokuwa kwa mambo matano: Mtu anayeikusanya, au mtu anayeinunua kwa pesa zake, au alielemewa, au mtu anayepigania Dini ya Allaah, au mtu masikini ambaye baada ya kupewa Swadaqah humpa sehemu yake mtu tajiri kama zawadi.”[1] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na Ibn Maajah, na akaisahihisha Al-Haakim]

521.

وَعَنْ عُبَيْدِ اللَّهِ بْنِ عَدِيٍّ بْنِ الْخِيَارِ، { أَنَّ رَجُلَيْنِ حَدَّثَاهُ أَنَّهُمَا أَتَيَا رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَسْأَلَانِهِ مِنَ الصَّدَقَةِ، فَقَلَّبَ فِيهِمَا الْبَصَرَ، فَرَأَاهُمَا جُلْدَيْنِ، فَقَالَ: "إِنْ شِئْتُمَا، وَلَا حَظَّ فِيهَا لِغَنِيٍّ، وَلَا لِقَوِيٍّ مُكْتَسَبٍ". } رَوَاهُ أَحْمَدُ وَقَوَّاهُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ

Kutoka kwa ‘Ubaydullaah bin ‘Adiyy bin Al-Khiyaar[2] amesema kuwa: “Watu wawili walituarifu kuwa walikwenda kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuomba Swadaqah. Akawatazama juu mpaka chini, na alipowaona wako imara,

akawaambia: “Mkitaka nitawapa, lakini kitu hicho hakipati mtu yeyote ambaye ni tajiri au mtu ambaye ana nguvu mwenye uwezo wa kuchuma.”[3] [Imetolewa na Ahmad na ikaimarishwa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy]

522.

وَعَنْ قَبِيصَةَ بْنِ مُخَارِقٍ الْأَهْلَالِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ الْمَسْأَلَةَ لَا تَحِلُّ إِلَّا لِأَحَدٍ ثَلَاثَةٍ: رَجُلٌ تَحْمَلُ حَمَالَةً، فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ حَتَّى يُصِيبَهَا، ثُمَّ يُمْسِكَ، وَرَجُلٌ أَصَابَتْهُ جَائِحَةٌ، اجْتَاكَ مَالُهُ، فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ حَتَّى يُصِيبَ قَوَامًا مِنْ عَيْشٍ، وَرَجُلٌ أَصَابَتْهُ فَاقَةٌ حَتَّى يَقُومَ ثَلَاثَةٌ مِنْ ذَوِي الْحِجَى مِنْ قَوْمِهِ: لَقَدْ أَصَابَتْ فُلَانًا فَاقَةٌ؛ فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ حَتَّى يُصِيبَ قَوَامًا مِنْ عَيْشٍ، فَمَا سِوَاهُنَّ مِنَ الْمَسْأَلَةِ يَا قَبِيصَةُ سُحَتْ يَأْكُلُهَا صَاحِبُهَا سُحْتًا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Qabiyswah bin Mukhaariq Al-Hilaaliyy[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Kuomba hakuruhusiwi isipokuwa kwa moja kati ya matatu: (a) Mtu aliyeweka dhamana, ambaye huruhusiwa kuomba hadi amepata kisha ajizuie (b) Mtu ambaye mali zake zimeteketezwa na maafa yaliyomsibu. Ameruhusiwa kuomba hadi atakapopata kiasi cha kumkimu. (c) Mtu aliyefilisika na akawa maskini anayethibitishwa na watu watatu werevu, anaruhusiwa kuomba hadi atakapopata cha kumkimu. Sababu yoyote nyingine ya kuomba Ee Qabiyswah ni haramu na mtu anayeomba hivyo, atakuwa anakula

haramu.” [Imetolewa na Muslim, Abuu Daawuud, Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan]

523.

وَعَنْ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ بْنِ رَبِيعَةَ بْنِ الْحَارِثِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ الصَّدَقَةَ لَا تَنْبَغِي لِآلِ مُحَمَّدٍ، إِنَّمَا هِيَ أَوْسَاخُ النَّاسِ} وَفِي رِوَايَةٍ: {وَإِنَّهَا لَا تَحِلُّ لِمُحَمَّدٍ وَلَا آلِ مُحَمَّدٍ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Abdul Mutwalib bin Rabiyy’ah bin Al-Haarith[5] صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) amesema Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Hizi Swadaqah hazifai kwa watu wa Rasuli wa Allaah kwani hizo uchafu wa watu.”[6]

Katika Riwaayah nyingine: “Hizo si halaal kwa Muhammad wala familia yake.” [Imetolewa na Muslim]

524.

وَعَنْ جُبَيْرِ بْنِ مُطْعِمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مَشَيْتُ أَنَا وَعُثْمَانُ بْنُ عَفَّانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقُلْنَا: يَا رَسُولَ اللَّهِ، أُعْطِيتَ بَنِي الْمُطَّلِبِ مِنْ خُمْسِ خَيْبَرَ وَتَرَكَتْنَا، وَنَحْنُ وَهُمْ بِمَنْزِلَةٍ وَاحِدَةٍ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ

صلى الله عليه وسلم "إِنَّمَا بَنُو الْمُطَّلِبِ وَبَنُو هَاشِمٍ شَيْءٌ وَاحِدٌ". { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Jubayri bin Mutw'im (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Uthmaan bin 'Affaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) na mimi tulimuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) tukamuambia: "Ee Rasuli wa Allaah! Umewapa wana wa Al-Mutwalib Khumus (moja ya tano) ya ngawira ya vita vya Khaybar na hukutupa sisi, na sisi na wawo ni daraja moja." [7] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: "Wana wa 'Abdul-Mutwalib na wana wa Haashim wote ni wamoja tu." [8] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

525.

وَعَنْ أَبِي رَافِعٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعَثَ رَجُلًا عَلَى الصَّدَقَةِ مِنْ بَنِي مَخْزُومٍ، فَقَالَ لِأَبِي رَافِعٍ: اصْحَبْنِي، فَإِنَّكَ تُصِيبُ مِنْهَا، قَالَ: حَتَّى آتِيَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَاسْأَلَهُ. فَأَتَاهُ فَسَأَلَهُ، فَقَالَ: "مَوْلَى الْقَوْمِ مِنْ أَنْفُسِهِمْ، وَإِنَّا لَا تَحِلُّ لَنَا الصَّدَقَةُ". { رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالثَّلَاثَةُ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Raafi' [9] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: "Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma mtu wa Banuw Makhzuwm kwenda kukusanya Swadaqah na akamtaka Abuu Raafi' aende naye ili akapate sehemu ya hiyo. Abuu Raafi' akasema: "Hapana siendi hadi nikamuulize Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

صَلَّى اللَّهُ) Alipokwenda kumuuliza Rasuli wa Allaah (وَالِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Swadaqah imeharamishwa kwetu sisi, na mtumwa[10] wa watu ni mmoja wapo.” [Imetolewa na Ahmad, na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud), Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan]

526.

وَعَنْ سَالِمِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ، عَنْ أَبِيهِ، {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يُعْطِي عُمَرَ الْعَطَاءَ، فَيَقُولُ: أَعْطِهِ أَفْقَرَ مِنِّي، فَيَقُولُ: "خُذْهُ فَتَمَوَّلْهُ، أَوْ تَصَدَّقْ بِهِ، وَمَا جَاءَكَ مِنْ هَذَا الْمَالِ، وَأَنْتَ غَيْرُ مُشْرِفٍ وَلَا سَائِلٍ فَخُذْهُ، وَمَا لَا فَلَا تُتْبِعْهُ نَفْسَكَ".} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Saalim bin ‘Abdillaah bin ‘Umar kwa upokezi wa baba yake amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimpa zawadi ‘Umar, naye akamuambia: “Mpe mtu ambaye ni maskini kuliko mimi.” Aliposikia hivyo, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aksema: “Wewe chukua, na uifanye mali yako, au uigawe kama Swadaqah. Chukua kinachokuja katika mali hii wala wewe huna uroho wala huombi, lakini isiyokuwa hiyo usiuache moyo wako uitamani.” [Imetolewa na Muslim]

[1] Imekatazwa kwa mtu tajiri kuchukua pesa zozote kutoka katika Zakaah lakini ikiwa mtu maskini atapata pesa za Zakaah, akanunua kitu kwa pesa hizi na akampa hicho mtu tajiri, inaruhusiwa.

[2] ‘Ubaydullaah bin ‘Adiyy bin Al-Khiyaar alikuwa Mkuraishi kutoka Banuw Nawfal. Alizaliwa wakati Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

(وَسَلَّمَ) bado yu hai, lakini anahesabika miongoni mwa Taabi'iyn. Alisimulia Hadiyth kutoka kwa 'Umar na 'Uthmaan na wengine. Inasemekana kuwa babake aliuawa kule Badr kama kafiri. 'Ubaydullaah anasemekana kuwa alikuwa kijana mkubwa wakati Makkaah ilipotekwa, na kwa hivyo alikuwa Swahaba. Alikuwa miongoni mwa utawala wa Al-Waliyd bin Abdil-Maalik mnamo mwaka wa 90 A.H.

[3] Watu wengine wanaitafsiri Hadiyth hii kwamba, mtu anayeweza kufanya kazi ya kipato, hata kama yeye ni maskini, asipokee Swadaqah. Tafsiri hii siyo sahihi. Hadiyth nyingine inaweka wazi kwa kusema, mtu ambaye yuko karibu na kufa kwa njaa anaweza kuomba Swadaqah.

[4] Qabiyswah bin Mukhaariq Al-Hilaaliyy ndiye Abuu Bishr Qabiyswah bin Al-Mukhaariq bin 'Abdillaah bin Shaddaad Al-'Aamir Al-Hilaal, alikuwa ni Swahaba aliyelowea Basra. Alimzuru Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ) na akasimulia Hadiyth kutoka kwake. Yeye ni msimulizi wa Hadiyth sita.

[5] 'Abdul Mutwalib bin Rabiyy'ah bin Al-Haarith ndiye mwana wa 'Abdul-Mutwalib bin Haashim Al-Qurayashiy. Alilowea Al-Madiynah, kisha akahamia Damascus ambako alifia.

[6] Imekatazwa kwa kila kizazi cha Muhammad (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) kukubali malipo ya Zakaah. Hukmu hii imeafikiwa. Hata hivyo, kuna tofauti ya maoni juu ya hali ya Swadaqah ya khiari. Hawa siyo vizazi vya Muhammaad (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) peke yake wanaoharamishiwa kupokea malipo za Zakaah, bali wamo pia vizazi vya 'Aliy, 'Abbaas, Ja'far, 'Aaqil, 'Abdul-Mutwalib bin 'Abd-Manaaf ambayo inamaanisha kuwa wote hawa wamo katika familia ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[7] Usemi wa Jubayr bin Mutw'im na 'Uthmaan (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) kuwa wao wako sawa au daraja zao sawa una maana mbili: (a) Wote wanamtii Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kwa njia ile ile kama vizazi vya Al-Mutwalib wanavyomtii. (b) Banuw Mutwalib hawawapiti wao katika kustahili kutokana na miungano ya mahusiano na udugu kwa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). 'Uthmaan baki ya kupewa heshima ya kuwa mkwe wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) pia anatoka katika ukoo wa Banuw Umayiyyah. Banuw Umayiyya na Banuw Haashim walihisabika kuwa

makabila yaliyo sawa kwa mujibu wa hadhi yao miongoni mwa vizazi vya Maquraishi.

[8] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Amesema hivi: “Hakuna ubishi kuwa kuhusu daraja, na ukoo, Banuw Haashim na Banuw Umayiyyah wako sawa kabisa. Lakini Banuw Mutwalib waliungana na upande wa Waislam, wakati Banuw Nawfal na Banuw Abdish-Shams waliwapinga Waislam. Kwa sababu hiyo Banuw Haashim na Banuw Mutwalib wako sawa, na wakati ulipofika, walipewa Khumus ya pesa lakini ninyi hamkupewa chochote.”

[9] Abuu Raafi' alikuwa mtumwa wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na jina lake ni Aslam au Hurmuz au Thaabit au Ibraahiym. Alikuwa Mkipti wa Misri na alimilikiwa na Al-'Abbaas aliyemzawadia Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alisilimu kabla ya Badr, na hakuwahi kuishuhudia vita ile. Alishuhudia vita za Uhud na zilizofuata. Al-'Abbaas aliposilimu, Abuu Raafi' ndiye aliyempa habari hizo njema Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ambaye alimuacha huru. Alikufa mwanzo mwanzo wa Ukhalifa wa 'Aliy mnamo mwaka wa 36 A.H. kule Al-Madiynah.

[10] Mtu ambaye kaharamishiwa kupokea Zakaah hata mtumwa wake ni haraam kupokea

كِتَابُ الصِّيَامِ

Kitabu Cha Swiyaam

05-Kitabu Cha Swiyaam - كِتَابُ الصِّيَامِ

01- Kitabu Cha Swiyaam

527.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَقْدَمُوا رَمَضَانَ بِصَوْمِ يَوْمٍ وَلَا يَوْمَيْنِ، إِلَّا رَجُلٌ كَانَ يَصُومُ صَوْمًا، فَلْيَصُْمْهُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msitangulie Ramadhwaan kwa Swawm siku moja au mbili[2] isipokuwa mtu alikuwa ana Swawm basi afunge.”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim]

528.

وَعَنْ عَمَّارِ بْنِ يَاسِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { مَنْ صَامَ الْيَوْمَ الَّذِي يُشَكُّ فِيهِ فَقَدْ عَصَى أَبَا الْقَاسِمِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ } وَذَكَرَهُ الْبُخَارِيُّ تَعْلِيْقًا، وَوَصَلَهُ الْخَمْسَةَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Ammar bin Yaasir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mwenye kufunga siku ambayo inatiliwa mashaka,[4] atakuwa

amemuasi Abul-Qaasim (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) [Al-Bukhaariy aliitaja kuwa ni Mu'allaq, lakini Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) waliifuatilia Hadiyth hii kuwa ni Mawsuwl, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan]

529.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {إِذَا رَأَيْتُمُوهُ فَصُومُوا، وَإِذَا رَأَيْتُمُوهُ فَافْطِرُوا، فَإِنْ غَمَّ عَلَيْكُمْ فَأَقْدُرُوا لَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِمُسْلِمٍ: {فَإِنْ أَغْمِيَ عَلَيْكُمْ فَأَقْدُرُوا لَهُ ثَلَاثِينَ} وَلِلْبُخَارِيِّ: {فَأَكْمِلُوا الْعِدَّةَ ثَلَاثِينَ} وَلَهُ فِي حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {فَأَكْمِلُوا عِدَّةَ شَعْبَانَ ثَلَاثِينَ}

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Mkiuona mwezi mpya fungeni, na msifungue hadi mmeuona. Lakini ikiwa anga ina mawingu, basi ukadirieni.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Muslim amesema: “Ikiwa kuna mawingu, basi hesabuni siku thelathini (ambapo mwezi sharti uandame).”

Na Al-Bukhaariy amesema: “Kamilisheni hesabu siku thelathini.”

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Naye amenukuu Hadiyth ya Abuu Hurayrah kuwa: “Kamilisheni hesabu ya siku thelathini[5] za mwezi wa Sha’baan.”

530.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {تَرَأَى النَّاسُ
الْهَلَالَ، فَأَخْبَرْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنِّي
رَأَيْتُهُ، فَصَامَ، وَأَمَرَ النَّاسَ بِصِيَامِهِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ،
وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Watu waliuona mwezi mwandamo, nikamuarifu Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuwa nimeuona. Kwa hivyo yeye akafunga na akawaamrisha watu wafunge.”[6] [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na wakaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

531.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ أَعْرَابِيًّا جَاءَ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: {إِنِّي رَأَيْتُ الْهَلَالَ، فَقَالَ: " أَتَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ؟ " قَالَ: نَعَمْ. قَالَ: " أَتَشْهَدُ أَنْ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ؟ " قَالَ: نَعَمْ. قَالَ: " فَأَذِّنْ فِي النَّاسِ يَا بِلَالُ أَنْ يَصُومُوا غَدًا " } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ وَرَجَّحَ النَّسَائِيُّ إِسْرَافَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Bedui mmoja alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Nimeona mwezi, Akasema: “Unashahadia kuwa hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah?” Akasema “Ndiyo.” Akasema: “Unashahadia pia kuwa Muhammad ni Rasuli wa Allaah?” Akasema: “Ndiyo.” Akasema: Bilaal! Watangazie watu wafunge kesho.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan, na An-Nasaaiy aliipa daraja ya Mursal]

532.

وَعَنْ حَفْصَةَ أُمِّ الْمُؤْمِنِينَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ لَمْ يُبَيِّتِ الصِّيَامَ قَبْلَ الْفَجْرِ - فَلَا صِيَامَ لَهُ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَمَالِ النَّسَائِيُّ وَالتِّرْمِذِيُّ إِلَى تَرْجِيحِ وَفْقِهِ، وَصَحَّحَهُ مَرْفُوعًا ابْنُ خُزَيْمَةَ وَابْنُ حِبَّانَ وَلِلدَّارَقُطْنِيِّ: {لَا صِيَامَ لِمَنْ لَمْ يَفْرِضْهُ مِنَ اللَّيْلِ}

Kutoka kwa Hafswah[7] Ummul Mu-uminiyna (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asiyelaza niyyah[8] kabla ya alfajiri hana Swawm.”[9] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad), At-Tirmidhiy na An-Nasaaiy wakaisahihisha na kuipa daraja la Mawquwf. Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan wakaipa daraja la Marfuw’]

Na Ad-Daaraqutwniyy amesema: “Hana Swawm ambaye hakuifaradhisha tangu usiku.”

533.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {دَخَلَ عَلَيَّ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ذَاتَ يَوْمٍ. فَقَالَ: " هَلْ عِنْدَكُمْ شَيْءٌ ؟ " قُلْنَا: لَا. قَالَ: " فَإِنِّي إِذَا صَائِمٌ " ثُمَّ أَتَانَا يَوْمًا آخَرَ، فَقُلْنَا: أَهْدِي لَنَا حَيْسٌ، فَقَالَ: " أَرَيْنِيهِ، فَلَقَدْ أَصْبَحْتُ صَائِمًا " فَأَكَلَ }
رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) aliingia kwangu siku moja akasema: “Una kitu chochote cha kula?” Tukasema: “Hapana.” Na akasema (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ): “Basi mie ninafunga leo.”[10] Kisha akanitembelea siku nyingine nami nikamuambia kuwa nimepewa zawadi ya Hays[11], Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Hebu nionyeshe, kwani nimeamka nikiwa na Swawm.” Kisha Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akala.”[12] [Imetolewa na Muslim]

534.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَزَالُ النَّاسُ بِخَيْرٍ مَا عَجَّلُوا الْفِطْرَ }
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِلتَّرمِذِيِّ: مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ أَحَبُّ عِبَادِي إِلَيَّ أَعْجَلُهُمْ فِطْرًا}

Kutoka kwa Sahl bin Sa'd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu wataendelea kuwa katika khayr ilimradi wanaharakisha kufuturu.” [13] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika At-Tirmidhiy kwa upokezi wa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah amesema Mja Nimpendaye sana kati ya waja Wangu ni anayeharakisha kufuturu.”

535.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {تَسَحَّرُوا فَإِنَّ فِي السَّحُورِ بَرَكَاتًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuleni sahuwr (daku) kwani katika sahuwr kuna Baraka.” [14] [Al-Bukhaariy, Muslim]

536.

وَعَنْ سَلْمَانَ بْنِ عَامِرٍ الضَّبِّيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا أَفْطَرَ أَحَدُكُمْ فَلْيُفْطِرْ عَلَى تَمْرٍ، فَإِنْ لَمْ يَجِدْ فَلْيُفْطِرْ عَلَى مَاءٍ، فَإِنَّهُ طَهُورٌ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ وَابْنُ حِبَّانَ وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Salmaan bin ‘Aamir Adhw-Dhwabbiyy[15] (رَضِيَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Nabiy (الله عَنْهُ) amesema: “Endapo mmoja wenu anafuturu, afuturu kwa tende, asipopata (tende), basi kwa maji,[16] kwani maji yanatakasa.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad), akaisahihisha Ibn Khuzaymah, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

537.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ الْوِصَالِ، فَقَالَ رَجُلٌ مِنَ الْمُسْلِمِينَ: فَإِنَّكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ تُوَاصِلُ؟ قَالَ: "وَأَيُّكُمْ مِثْلِي؟ إِنْني أَبِيتُ يُطْعِمُنِي رَبِّي وَيَسْقِينِي". فَلَمَّا أَبَوْا أَنْ يَنْتَهُوا عَنِ الْوِصَالِ وَاصَلَ بِهِمْ يَوْمًا، ثُمَّ يَوْمًا، ثُمَّ رَأَوْا الْهَلَالَ، فَقَالَ: "لَوْ تَأَخَّرَ الْهَلَالُ لَزِدْتُمْ" كَالْمُنْكَلِ لَهُمْ حِينَ أَبَوْا أَنْ يَنْتَهُوا {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza kufunga Swawm mfululizo,[17] akasema mtu mmoja: “Wewe hufunga mfululi’zo Ee

Rasuli wa Allaah! Akasema: “Nani kati yenu yuko kama Mimi? Wakati wa usiku Rabb Wangu Hunilisha na Kuninywesha. Walipokataa wakataka kuendelea kufunga mfululizo, alifunga pamoja nao kwa siku moja na kisha siku moja tena, kisha wakaona mwezi, Akasema: “Mwezi ungechelewa, ningewazidishia”. Alielekea kutaka kuwaadhibu walipokataa kusitisha.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

538.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ لَمْ يَدَعْ
قَوْلَ الزُّورِ وَالْعَمَلَ بِهِ، وَالْجَهْلَ، فَلَيْسَ لِلَّهِ حَاجَةٌ فِي أَنْ يَدَعَ
طَعَامَهُ وَشَرَابَهُ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ، وَأَبُو دَاوُدَ وَاللَّفْظُ لَهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Iwapo mtu hatoacha uongo[18] na matendo yake na ujinga, Allaah Hana haja mtu huyo aache chakula chake na kinywaji chake.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy, na Abuu Daawuwd, na tamshi hili ni lake]

539.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُقْبَلُ وَهُوَ صَائِمٌ، وَيُبَاشِرُ وَهُوَ صَائِمٌ، وَلَكِنَّهُ
أَمْلَكُكُمْ لِإِزْبِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ
وَزَادَ فِي رِوَايَةٍ: {فِي رَمَضَانَ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anabusu[19] na kukumbatia huku akiwa katika Swawm, lakini yeye anamiliki zaidi matamania yake kuliko nyinyi.”[20] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim inasema: “Katika Ramadhwaan”

540.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ اِحْتَجَمَ وَهُوَ مُحْرِمٌ، وَاحْتَجَمَ وَهُوَ صَائِمٌ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliumikwa wakati amevaa Ihraam (wakati wa Hajj au ‘Umrah), na aliumikwa akiwa na Swawm.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

541.

وَعَنْ شَدَّادِ بْنِ أَوْسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَتَى عَلَى رَجُلٍ بِالْبَقِيعِ وَهُوَ يَحْتَجِمُ فِي رَمَضَانَ. فَقَالَ: " أَفْطَرَ الْحَاجِمُ وَالْمَحْجُومُ " } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيَّ، وَصَحَّحَهُ أَحْمَدُ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Shaddaad bin Aws[21] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikutana na mtu Al-Baqiy’ aliyekuwa anaumikwa ndani ya mwezi wa Ramadhwaan, akasema: “Amefungua Swawm aliyeumika na aliyeumikwa wote wamebatilisha Swawm zao.”[22] [Imetolewa na Al-Khamsah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa At-Tirmidhiy, na wakaisahihisha Ahmad, Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan]

542.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَوَّلُ مَا كُرِهَتْ الْحِجَامَةُ لِلصَّائِمِ، أَنَّ جَعْفَرَ بْنَ أَبِي طَالِبٍ اخْتَجَمَ وَهُوَ صَائِمٌ، فَمَرَّ بِهِ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: " أَفْطَرَ هَذَانِ "، ثُمَّ رَخَّصَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعْدُ فِي الْحِجَامَةِ لِلصَّائِمِ، وَكَانَ أَنَسٌ يَخْتَجِمُ وَهُوَ صَائِمٌ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَقَوَّاهُ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mwanzo kukatazwa kuumika kwa mwenye Swawm ilikuwa hivi: Ja’far bin Abiy Twaalib alikwenda kuumikwa wakati akiwa ana Swawm, na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipomuona akasema: “Wote wawili hawa wamebatilisha Swawm zawo.” Baadaye Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaruhusu mtu aweza kuumikwa wakati ana Swawm. Anas alikuwa akienda kuumikwa wakati ana Swawm.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy na akaipa nguvu]

543.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ اِكْتَحَلَ فِي رَمَضَانَ، وَهُوَ صَائِمٌ } رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

قَالَ التِّرْمِذِيُّ: لَا يَصِحُّ فِيهِ شَيْءٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitia Kuhl[23] ndani ya Ramadhwaan akiwa ana Swawm.” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa Isnaad dhaifu]

Na amesema At-Tirmidhiy: “Hakuna lolote katika maudhui haya lililo Swahiyh.”

544.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَنْ نَسِيَ وَهُوَ صَائِمٌ، فَأَكَلَ أَوْ شَرِبَ، فَلْيُتِمَّ صَوْمَهُ، فَإِنَّمَا أَطْعَمَهُ اللَّهُ وَسَقَاهُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَالْحَاكِمُ: { مَنْ أَفْطَرَ فِي رَمَضَانَ نَاسِيًا فَلَا قِضَاءَ عَلَيْهِ وَلَا كَفَّارَةَ } وَهُوَ صَحِيحٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtu yeyote

anayesahau wakati yumo katika Swawm, akala au akanywa kitu, basi akamilishe Swawm yake, kwani Allaah Amemlisha na Kumnywesha yeye.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Al-Haakim amesema: “Mtu yeyote anayefungua Swawm yake kwa kusahau, hana haja ya kulipa Swawm hiyo wala kafara.”[24]
[Usimulizi huo ni Swahiyh]

545.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ ذَرَعَهُ الْقَيْءُ فَلَا قِضَاءَ عَلَيْهِ، وَمَنْ اسْتَقَاءَ فَعَلَيْهِ الْقِضَاءُ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ وَأَعْلَاهُ أَحْمَدُ وَقَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Endapo mtu atajiwa ghafla na kutapika huku yumo ndani ya Swawm, hana haja ya kulipa, na mwenye kujitapisha atalazimika kulipa.”[25]
[Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na Ahmad aliiona ina dosari, na Ad-Daaraqutwniyy aliipa nguvu]

546.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خَرَجَ عَامَ الْفَتْحِ إِلَى مَكَّةَ فِي رَمَضَانَ، فَصَامَ حَتَّى بَلَغَ كُرَاعَ الْغَمِيمِ، فَصَامَ النَّاسُ، ثُمَّ دَعَا بِقَدَحٍ مِنْ

مَاءٍ فَرَفَعَهُ، حَتَّى نَظَرَ النَّاسُ إِلَيْهِ، ثُمَّ شَرِبَ، فَقِيلَ لَهُ بَعْدَ ذَلِكَ: إِنَّ بَعْضَ النَّاسِ قَدْ صَامَ. قَالَ: "أُولَئِكَ الْعُصَاةُ، أُولَئِكَ الْعُصَاةُ" {

وَفِي لَفْظٍ: {فَقِيلَ لَهُ: إِنَّ النَّاسَ قَدْ شَقَّ عَلَيْهِمُ الصِّيَامُ، وَإِنَّمَا يَنْظُرُونَ فِيمَا فَعَلْتَ، فَدَعَا بِقَدَحٍ مِنْ مَاءٍ بَعْدَ الْعَصْرِ، فَشَرِبَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdullaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Aliondoka kuenda Makkah wakati wa Ramadhwaan mwaka wa kuiteka Makkah, na yeye na watu walifunga hadi alipofika Kuraa’ Al-Ghamiym. Kisha akaomba kikombe cha maji akakiinua juu mpaka watu wakakitazama ndipo akanywa.[26] Aliambiwa baadaye kuwa watu waliendelea kufunga akasema: “Hao ni waasi, hao ni waasi.” [27]

Tafsiri nyingine inasema: “Watu wanaona ugumu kufunga na wanangojea utakalofanya wewe.” Hapo akaitisha kikombe cha maji, baada ya Swalaah ya alasiri, akanywa. [Imetolewa na Muslim]

547.

وَعَنْ حَمْزَةَ بْنِ عَمْرِو الْأَسْلَمِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ ، أَنَّهُ قَالَ: {يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَجِدُ بِي قُوَّةَ عَلَى الصِّيَامِ فِي السَّفَرِ، فَهَلْ عَلَيَّ جُنَاحٌ؟ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ " هِيَ رُخْصَةٌ مِنَ اللَّهِ، فَمَنْ أَخَذَ بِهَا فَحَسَنٌ، وَمَنْ أَحَبَّ أَنْ يَصُومَ

فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ " { رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَأَصْلُهُ فِي " الْمُتَّفَقِ " مِنْ حَدِيثِ عَائِشَةَ ، { أَنَّ حَمْزَةَ بْنَ عَمْرِو سَأَلَ }

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Hamzah bin ‘Amr Al-Aslamiyy[28] amesema: “Aliuliza Ee Rasuli wa Allaah! Mimi najiona nina nguvu za kutosha za Swiyaam nikiwa safarini, je nitapata dhambi? Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Hiyo ni ruhsa toka kwa Allaah, na kila atakayeitekeleza atakuwa kafanya vizuri, lakini iwapo mtu yeyote atapenda kufunga, hana dhambi.” [Imetolewa na Muslim na chanzo chake kimo katika Al-Bukhaariy na Muslim kutoka katika ripoti ya ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) ambayo Hamzah bin ‘Amr aliulizia]

548.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { رُخِّصَ لِلشَّيْخِ الْكَبِيرِ أَنْ يُفْطِرَ، وَيُطْعِمَ عَنْ كُلِّ يَوْمٍ مِسْكِينًا، وَلَا قَضَاءَ عَلَيْهِ } رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَالْحَاكِمُ، وَصَحَّاحُهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Mzee anaruhusiwa kula katika mwezi wa Ramadhwaan na kulisha maskini kila siku, na hailipi.”[29] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy na Al-Haakim ambao pia waliithibitisha]

549.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: هَلَكْتُ يَا رَسُولَ اللَّهِ. قَالَ: " وَمَا أَهْلَكَ ؟ " قَالَ: وَقَعْتُ عَلَى امْرَأَتِي فِي رَمَضَانَ، فَقَالَ: " هَلْ تَجِدُ مَا تَعْتِقُ رَقَبَةً ؟ " قَالَ: لَا. قَالَ: " فَهَلْ تَسْتَطِيعُ أَنْ تَصُومَ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ ؟ " قَالَ: لَا. قَالَ: " فَهَلْ تَجِدُ مَا تُطْعِمُ سِتِّينَ مِسْكِينًا ؟ " قَالَ: لَا، ثُمَّ جَلَسَ، فَأَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِعَرَقٍ فِيهِ تَمْرٌ. فَقَالَ: " تَصَدَّقْ بِهَذَا "، فَقَالَ: أَعَلَى أَفْقَرِ مِنَّا ؟ فَمَا بَيْنَ لَابَتَيْهَا أَهْلٌ بَيْتٍ أَحْوَجُ إِلَيْهِ مِنَّا، فَضَحِكَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حَتَّى بَدَتْ أَنْيَابُهُ، ثُمَّ قَالَ: " اذْهَبْ فَأَطْعِمْهُ أَهْلَكَ " } رَوَاهُ السَّبْعَةُ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mtu mmoja[30] alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “ Ee Rasuli wa Allaah! Nimeangamia.” Akasema: “Kitu gani kilichokuangamiza?” Akasema: “Nimemuingilia mke wangu ndani ya Swawm ya Ramadhwaan.” Akasema: “Je unaweza kupata mtumwa wa kumuacha huru?” Akasema: “Hapana.” Akasema tena: “Unaweza kufunga miezi miwili mfululizo?” Akasema: “Hapana.” Akasema tena: “Je unaweza kuwapa chakula maskini sitini?” Akasema: “Hapana.” Kisha akakaa chini. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaletewa ‘Araq[31] moja lenye tende. Akasema: “Lito e hili Swadaqah.” Akasema: “Je kuna maskini kuliko sisi? Hakuna familia iliyo masikini kuliko yangu kati ya milima hii miwili ya Al-Madiynah.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akacheka hadi magego yake yakaonekana, na akasema: “Nenda ukailishe familia yako[32] kwa hizo.”[33] [Imetolewa na As-Sab’ah (Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na tamshi hili ni la Muslim]

550.

وَعَنْ عَائِشَةَ وَأُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يُصْبِحُ جُنُبًا مِنْ جَمَاعٍ، ثُمَّ يَغْتَسِلُ
وَيَصُومُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
زَادَ مُسْلِمٌ فِي حَدِيثِ أُمِّ سَلَمَةَ: وَلَا يَقْضِي

Kutoka kwa ‘Aaishah na Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) wamesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiamka alfajiri[34] akiwa katika hali ya janaba, kisha alikuwa akifanya ghuslu (kuoga josho) na kufunga.” [Al-Bukhaariy, Muslim]
Na akaongezea Muslim katika usimulizi wa Ummu Salamah kuwa: “wala halipi.”

551.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ قَالَ: { مَنْ مَاتَ وَعَلَيْهِ صِيَامٌ صَامَ عَنْهُ وَلِيِّهِ } مُتَّفَقٌ
عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Endapo atakayefariki na deni la Swawm, Waliy wake amfungie.”[35] [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Maana ye neno Swiyaam na Swawm ni “kusitisha” na “kujizuia”. Kwa mujibu wa Istilaahi za Shariy’ah, inamaanisha kujizuia kula, kunywa, na ngono, kuanzia alfajiri hadi machweo ya jua, huku ukiwa na niyyah thabiti ya kutekeleza amri ya Allaah (سبحانه وتعالى). Swawm ni moja ya nguzo tano za Uislaam. Ukiikataa nguzo hii, wewe siyo Muislam, na ukiikwepa, wewe ni muasi. Swawm iliamrisha kuwa ni lazima mnamo mwaka wa 2 A.H.

[2] Hadiyth hii inatufundisha kuwa kule kufunga siku moja kabla ya kuja kwa Ramadhwaan, kama wanavyofanya baadhi ya watu wasiojua, imekatazwa

[3] Endapo mtu ana desturi ya kufunga siku fulani maalumu, na siku hiyo ikaangukia kuwa siku moja kabla ya Ramadhwaan, anaruhusiwa mtu huyo kufunga siku hiyo.

[4] Endapo mwezi wa Ramadhwaan haukuonekana mnamo tarehe 29 ya Sha’baan kwa sababu anga ilikuwa na vumbi au mawingu, ubora mtu akamilishe siku thelathini za Sha’baan ndipo aanze Swiyaam. Kuanza Swiyaam kwa kudhani tu mwezi wa Ramadhwaan unaweza kuwa ulionekana mnamo tarehe 29 ya Sha’baan, kumekatazwa.

[5] Hii inatufunza kwamba usianze kufunga hadi baada ya kuuona mwandamo wa mwezi.

[6] Hii inatufunza kuwa hata shahidi mmoja tu anatosha kutangazwa mwanzo wa mfungo, lakini kuutangaza mwandamo wa mwezi wa ‘Iyd (mfungo mosi) wanahitajika mashahidi wawili, kanuni hii imeafikwa kwa pamoja.

[7] Hafswah alikuwa binti wa ‘Umar bin Al-Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) na akaolewa na Khunays bin Hudhaafah As-Sahmi aliyehama naye kwenda Al-Madiynah. Alipokufa baada ya Badr, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akamuoa mnamo mwaka wa 3 A.H. Alifariki mnamo mwezi Sha’baan mwaka wa 45 A.H akiwa na umri wa miaka 60.

[8] Moja ya masharti ya Swawm ni niyyah. Kwa hivyo kila mtu sharti aweke niyyah ya Swawm kabla ya alfajiri.

[9] Kila mtu ni lazima aweke niyyah ya kufunga kabla ya alfajiri, hasa akiwa anafunga Swawm ya faradhi (ya lazima). Lakini akiwa anafunga Swawm ya Nafl (ya khiari), inatosha kuweka niyyah hata kabla ya saa sita mchana.

[10] Hadiyth hii inatufunza kuwa, niyyah ya kufunga Swawm ya khiari si lazima iwekwe kabla ya Alfajiri, bali niyyah inaweza kuwekwa hata mchana.

[11] Hays ni mchanganyiko wa tende na samli.

[12] Hadiyth hii inatufunza kwamba, Swawm ya khiari inaweza kusitishwa bila sababu yoyote.

[13] Mtu akiwa na hakika kabisa juu ya machweo ya jua, lazima asikawie kufuturu, kwani kuchelewa kufuturu ni desturi ya Mayahudi na Manaswara.

[14] Mayahudi na Wakristo hawana desturi hii ya kula sahuwr (daku). Muslim ameipokea kuwa: “Kula sahuwr ndio tofauti kati yetu na Ahl-al-Kitaab (watu wa kitabu).” Hii inasahilisha Swawm na pia inaleta thawabu zaidi.

[15] Salmaan bin ‘Aamir Adhw-Dhwabbiyy ndiye Ibn Aws bin Hujr bin ‘Amr bin Al-Haarith Adhw-Dhwabbiyy, alikuwa ni Swahaba aliyelowea Basra, na alikuwa mtu mzee wakati wa uhai wa Nabiyy (ﷺ), aliishi hadi kwenye ukhalifa wa Mu’aawiyah, na inasemekana kuwa aliuliwa katika vita vya Al-Jamaal akiwa na umri wa miaka 100. Pia inasemekana kuwa hakuna Swahaba mwingine yoyote kutoka Adhw-Dwabbi isipokuwa yeye.

[16] Kitu kizuri kuliko vyote vya kufungulia Swawm ni tende mbichi, tende kavu, kisha maji, chumvi.

[17] Neno la kiarabu Wiswaal hutumika kwa mtu ambaye hafungui Swawm yake jioni bali anaendelea kufunga mfululizo hadi siku ya pili bila kula wala kunywa katikati. Aina hii ya kufunga Swawm imekatazwa.

[18] Madhumuni ya kufunga Swawm ni kwamba, mtu ajifunze kujidhibiti mwenyewe. Lengo na azma ya kufunga Swawm linapoteza maana iwapo mtu anashindwa kujifunza hilo.

[19] Haijakatazwa kumbusu mkeo au kumkumbatia wakati wa kufunga Swawm, kwani tendo hilo tu halibatilishi Swawm.

[20] ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) anapendekeza kuwa watu wajiepushe kufanya hayo (kubusu na kukumbatia wake/waume), asije mtu akateleza na kubatilisha Swawm yake.

[21] Shaddaad bin Aws ndiye Abuu Ya’laa Al-Answaariy An-Najaariy Al-Madaniy, mpwa wa Hassan bin Thaabit. Alikuwa msomi na mwenye subira sana. Alifia Sham mnamo mwaka 58 A.H. akiwa na umri wa miaka 75.

[22] Hadiyth iliyopita (540) imeruhusu kuumikwa (kunyonywa damu kitabibu) hata kama ni ndani ya Ramadhwaan wakati mtu ana Swawm. Inaelekea kuwa kuna kutofautiana hapa, lakini hakuna. Hadiyth hii iliyosimuliwa na Shaddaad bin Aws imefutwa kwa sababu Shaddaad aliwasili Makkah baada ya mwaka wa kutekwa Makkah. Lakini ‘Abdullaah bin ‘Abbaas alisimulia kuwa hayo hayo yalitokea mnamo mwaka wa Hajjatul-Wadaa’ (Hijjah ya mwisho aliyoitekeleza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kabla hajafariki). Ama kuhusu uhalali wake, kuumika hakubatilishi Swawm kwa mujibu wa ‘Ulamaa walio wengi; lakini kuumika hakupendezi kwa kuwa kuumikwa kunaweza kusababisha udhoofu ambao nao unaweza kupelekea mtu kuvunja Swawm yake. Lakini iwapo mtu ana nguvu za kutosha kuhimili ulegevu au

kusinzia kunakoweza kusababishwa na kuumikwa, basi hiyo nasaha ya kuumikwa kutopendeza haiwi na maana.

[23] Kuhl ni chombo kinachotumiwa kwenye nyusi na kope kwa madhumuni ya kujiremba au kitabibu.

[24] Hii inatujulisha kuwa, kula au kunywa kwa kusahau, hakubatilishi Swawm. Na mtu hana haja ya kuilipa Swawm hiyo wala kuilipia fidia.

[25] Kuna tofauti ya maoni juu ya kama kutapika kunabatilisha Swawm au laa. Rai inayoelekea kuwa sahihi na ina mantiki ni kuwa, iwapo kutapika huko kumetokea kwenyewe, Swawm ni halali, lakini ikiwa ni kwa maksudi Swawm hubatilika.

[26] Inaruhusiwa Swawm wakati wa safari, lakini ni bora zaidi kutofunga. Endapo mtu atahisi kachoka sana wakati wa safari, anaruhusiwa kufungua. Anaweza kulipa kwa kufunga baadaye, lakini halazimiki kufidia au kutubu.

[27] Kwa kawaida inaruhusiwa Swawm kwa mtu akiwa safarini. Wale watu waliokuwa hawakufungua alipofungua Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) waliitwa hawana utii kwa sababu kuwa, kwa vile Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) alifungua Swawm yake, wao ni nani waendelea na Swawm? Utii unahitaji utekelezaji wa kikamilifu kabisa wa amri za Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ). Maswahaba zake walidhani kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) aliwaamrisha kwa kufungua Swawm yake kwa sababu aliwaonea huruma wao Maswahaba, vinginevyo Maswahaba zake wasingesita kamwe kufuata atakavyo.

[28] Hamzah bin ‘Amr Al-Aslamiyy alikuwa Swahaba aliyehesabika kutoka Al-Hijaaz. Aliitwa jina la utani Abuu Muhammad au Abuu Swaalih. Mwanawe Muhammad na ‘Aaishah, Mama wa Waumini walipokea Hadiyth hii kutoka kwake. Alikufa mnamo mwaka wa 61 A.H. akiwa na umri wa miaka 80.

[29] Mzee ambaye hawezi Swawm anaweza kulipia upungufu huu kwa kutoa fidia. Halikadhalika mtu mgonjwa asiyejiweza ambaye haelekei kupona karibuni, anaweza kutoa fidia. Fidia ni kutolewa chakula mara mbili kwa maskini. Pia fidia ya kukosa kufunga Swawm kwa siku moja ni hiyo hiyo.

[30] Huyu aliyemuendea Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ni Salama bin Sakhr.

[31] ‘Araq ni kapu lenye pishi moja ya tende.

[32] Hii inatufahamisha kwamba, endapo mtu ni maskini sana, anaweza kuilisha familia yake yeye mwenyewe kwa kafara yake mwenyewe. Wanazuoni wengu hawaiafiki Hadiyath hii na wanadai kuwa siyo kweli. Wengine wanaihesabu Hadiyath hii kuwa ni agizo maalumu alilopewa bwana huyo mahususi. Lakini maoni yote hayo hayana ushahidi.

[33] Hadiyath hii inatufahamisha kwamba, mwanamke hastahili kutozwa kafara (kafara au fidia ya kosa). Wengi wa Wanazuoni hawaafiki. Kanuni itumikayo ya kuwa, iwapo mme na mke wote walikubaliana kukutana kimwili, basi wote wawili wanastahili kulipa kafara. Lakini ikiwa mme ndiye aliyemlazimisha mke kukutana naye kimwili, basi mme ndiye anayestahili kafara siyo mke.

[34] Iwapo mme atakutana kimwili na mkewe usiku wa Ramadhwaan, lazima aoge asubuhi akiwa ana wasaa wa kutosha na kisha afunge.

[35] Endapo mtu atakufa kabla hajatimiza wajibu wake wa Swiyaam, warithi wake lazima wafunge siku hizo kwa niaba ya aliyefariki ndipo aliyefariki atasamehewa deni lake la Swiyaam.

02-Mlango Wa Swawm Za Sunnah, Na Siku Zilizokatazwa Swawm

بَابُ صَوْمِ التَّطَوُّعِ وَمَا نُهِيَ عَنْ صَوْمِهِ

02-Mlango Wa Swawm Za Sunnah, Na Siku Zilizokatazwa Swawm

552.

عَنْ أَبِي قَتَادَةَ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سُئِلَ عَنْ صَوْمِ يَوْمِ عَرَفَةَ. قَالَ: " يُكْفَرُ السَّنَةُ الْمَاضِيَّةَ وَالْبَاقِيَةَ "، وَسُئِلَ عَنْ صِيَامِ يَوْمِ عَاشُورَاءَ. قَالَ: " يُكْفَرُ السَّنَةُ الْمَاضِيَّةَ " وَسُئِلَ عَنْ صَوْمِ يَوْمِ الْاِثْنَيْنِ، قَالَ: " ذَاكَ يَوْمٌ وَلِدْتُ فِيهِ، وَبُعِثْتُ فِيهِ، أَوْ أُنْزِلَ عَلَيَّ فِيهِ " { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Qataadah Al-Answaariy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa: Rasuli wa Allaah aliulizwa kuhusu Swawm ya siku ya ‘Arafah akasema: “Hufuta madhambi ya mwaka uliopita na unaobakia.” Akaulizwa kuhusu Swawm ya siku ya ‘Aashuwraa akasema: “Inafuta madhambi ya mwaka uliopita.” Akaulizwa kuhusu Swawm ya siku za Jumatatu, akasema: “Hiyo ni siku niliyozaliwa na siku niliyopewa Unabiy na ni siku niliyoteremshiwa Qur-aan.”[1] [Imetolewa na Muslim]

553.

وَعَنْ أَبِي أَيُّوبَ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ صَامَ رَمَضَانَ، ثُمَّ أَتْبَعَهُ سِتًّا مِنْ شَوَّالٍ كَانَ كَصِيَامِ الدَّهْرِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Ayyuwb Al-Answaariyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kufunga Ramadhwaan, kisha akafuatishia siku sita za mwezi Shawwaal,[2] huwa kama Swiyaam ya mwaka mzima.” [Imetolewa na Muslim]

554.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا مِنْ عَبْدٍ يَصُومُ يَوْمًا فِي سَبِيلِ اللَّهِ إِلَّا بَاعَدَ اللَّهُ بِذَلِكَ الْيَوْمِ عَنْ وَجْهِهِ النَّارَ سَبْعِينَ خَرِيفًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna mja yoyote anayefunga siku moja katika njia ya Allaah isipokuwa Allaah Atamuweka mbali na moto miaka sabini elfu kwa sababu ya siku hiyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim][3]

555.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَصُومُ حَتَّى نَقُولَ لَا يُفْطِرُ، وَيُفْطِرُ حَتَّى نَقُولَ لَا يَصُومُ، وَمَا رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ اسْتَكْمَلَ صِيَامَ شَهْرٍ قَطُّ إِلَّا رَمَضَانَ، وَمَا رَأَيْتُهُ فِي شَهْرٍ أَكْثَرَ مِنْهُ صِيَامًا فِي شَعْبَانَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akifunga hadi tunasema kuwa hatofungua; na anakula hadi tunasema hatofunga. Sikuwahi kumuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anafunga mwezi mzima bila kufungua isipokuwa mwezi wa Ramadhwaan tu, na sikumuona anafunga sana katika mwezi wowote zaidi ya Sha’baan.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

556.

وَعَنْ أَبِي ذَرٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَمَرَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ نَصُومَ مِنَ الشَّهْرِ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ: ثَلَاثَ عَشْرَةَ، وَأَرْبَعَ عَشْرَةَ وَخَمْسَ عَشْرَةَ} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Dharri (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituamrisha Swawm siku tatu kila mwezi, siku ya kumi na tatu na kumi na nne na kumi na tano.”[4] [Imetolewa na An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

557.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَحِلُّ لِلْمَرْأَةِ أَنْ تَصُومَ وَزَوْجُهَا شَاهِدٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ .
وَزَادَ أَبُو دَاوُدَ: {غَيْرَ رَمَضَانَ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halali kwa mwanamke kufunga (Swawm ya khiari wakati) mume wake yupo, bila idhini yake.”[5] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na Abuu Daawuwd Akaongezea: “Swawm ambayo si ya Ramadhwaan.”

558.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ صِيَامِ يَوْمَيْنِ: يَوْمِ الْفِطْرِ وَيَوْمِ النَّحْرِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza watu kufunga siku mbili hizi: siku ya ‘Iydu-Fitwr na siku ya ‘Iydu-Adhwhaa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

559.

وَعَنْ نُبَيْشَةَ الْهُذَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَيَّامُ التَّشْرِيقِ أَيَّامُ أَكْلِ وَشُرْبٍ، وَذِكْرِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [6] Kutoka kwa Nubayshah Al-Hudhaliyy[6] amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Siku za At-Tashriyq[7] ni siku za kula, kunywa na za kumdhukuru Allaah (عَزَّ وَجَلَّ).” [Imetolewa na Muslim]

560.

وَعَنْ عَائِشَةَ وَابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَا: { لَمْ يُرَخَّصْ فِي أَيَّامِ التَّشْرِيقِ أَنْ يُصَمَّنَ إِلَّا لِمَنْ لَمْ يَجِدِ الْهَدْيَ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) Kutoka kwa ‘Aaishah na Ibn ‘Umar wamesema: “Hakuna aliyeruhusiwa Swawm siku za At-Tashriyq, isipokuwa yule mtu asiyekuwa na uwezo wa Al-Hadya (mnyama wa kafara).” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

561.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا تَخْتَصُّوا لَيْلَةَ الْجُمُعَةِ بِقِيَامٍ مِنْ بَيْنِ اللَّيَالِي، وَلَا تَخْتَصُّوا يَوْمَ الْجُمُعَةِ بِصِيَامٍ مِنْ بَيْنِ الْأَيَّامِ، إِلَّا أَنْ يَكُونَ فِي صَوْمٍ يَصُومُهُ أَحَدُكُمْ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msiufanye usiku wa Ijumaa miongoni mwa nyusiku nyenginezo kuwa makhsusi kwa Qiyaam (kusimama kuswali), na msiifanye siku ya Ijumaa miongoni mwa siku kuwa makhsusi kwa Swiyaam isipokuwa iwe ni Swawm anayofunga mmoja wenu.” [Imetolewa na Muslim]

562.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا يَصُومَنَّ أَحَدُكُمْ يَوْمَ الْجُمُعَةِ، إِلَّا أَنْ يَصُومَ يَوْمًا قَبْلَهُ، أَوْ يَوْمًا بَعْدَهُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Yeyote kati yenu asifunge siku ya Ijumaa[8] isipokuwa ikiwa anaifunga pamoja na siku kabla yake au siku baada yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

563.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا اِنْتَصَفَ شَعْبَانُ فَلَا تَصُومُوا} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَاسْتَنْكَرَهُ أَحْمَدُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwezi wa Sha’baan ukifikia nusu, msifunge.”[9] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) Ahmad hakuiafiki]

564.

وَعَنْ الصَّمَاءِ بِنْتِ بُسْرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا تَصُومُوا يَوْمَ السَّبْتِ، إِلَّا فِيمَا افْتَرَضَ عَلَيْكُمْ، فَإِنْ لَمْ يَجِدْ أَحَدُكُمْ إِلَّا لِحَاءً عَنِيبًا، أَوْ عُودَ شَجَرَةٍ فَلْيَمِضْغُهَا} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ، إِلَّا أَنَّهُ مُضْطَرَبٌ

وَقَدْ أَنْكَرَهُ مَالِكٌ

وَقَالَ أَبُو دَاوُدَ: هُوَ مَنْسُوخٌ

Kutoka kwa Asw-Swammaai bint Busr[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msifunge siku ya Jumamosi isipokuwa katika mliofaradhishwa, na iwapo mmoja wenu hakupata isipokuwa punje ya zabibu au kijiti cha mti basi na akitafune.”[11] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah,

Ahmad), wapokezi wake wanaaminika, lakini ni Mudhwtwarib (inababaisha)]

Maalik hakuiafiki

Na Abuu Daawuwd amesema: “Hii ni mansuwkh (imefutwa)”

565.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ أَكْثَرَ مَا يَصُومُ مِنَ الْأَيَّامِ يَوْمَ السَّبْتِ، وَيَوْمَ الْأَحَدِ، وَكَانَ يَقُولُ: " إِنَّهُمَا يَوْمَا عِيدٍ لِلْمُشْرِكِينَ، وَأَنَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَهُمْ " } أَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَهَذَا لَفْظُهُ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akifunga zaidi siku ya Jumamosi na Jumapili, na alikuwa akisema: “Hizo ni siku za sikukuu za washirikina, nami nataka kutofautiana nao.” [Imetolewa na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah, na hii ni tafsiri yake]

566.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { نَهَى عَنْ صَوْمِ يَوْمِ عَرَفَةَ بِعَرَفَةَ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ غَيْرَ التِّرْمِذِيِّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَالْحَاكِمُ، وَاسْتَنْكَرَهُ الْعُقَيْلِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza Swawm siku ya ‘Arafah ndani ya ‘Arafah.”[12] [Imetolewa na Al-Khamsah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Al-Haakim, na hakuiafiki Al-‘Uqayliyy]

567.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا صَامَ مَنْ صَامَ الْأَبَدَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِمُسْلِمٍ عَنْ أَبِي قَتَادَةَ بِلَفْظٍ: {لَا صَامَ وَلَا أَفْطَرَ}

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakufunga Swawm anayefunga milele”[13] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Muslim ameandika Hadiyth ya Abuu Qataadah ikiwa na tamshi: “Hakufunga Swawm wala hakula.”

[1] Hii inamaanisha kuwa dhambi ndogo hufutwa kwa sababu ya Swawm, lakini dhambi kubwa hufutwa kwa kutubu tu. Ama kuhusu haki za watu, madeni na wajibu wa kipesa, kuhusiana na mdaiwa, kusamehewa kunategemea matakwa ya watu wanaomdai. ‘Arafah ni jina la siku ya 9 ya mwezi wa Dhul-Hijjah (Mfungo tatu au mwezi wa kumi na mbili wa Kiislam), na ‘Aashuwraa ni siku ya 10 ya mwezi Muharram (Mfungo nne au mwezi wa kwanza wa Kiislam). Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipenda kufunga siku za Jumatatu, lakini hakuelezea juu ya thawabu zake.

[2] Endapo siku 30 za Ramadhwaan zitaunganishwa na siku 6 za kufunga mwezi wa Shawwaal ambayo inaifanya jumla iwe ni siku 36. Kwa mujibu wa Shariy'ah kila jema linalipwa mara kumi. Kwa hivyo tukizidisha siku 36 kwa mara 10 tutapata 360, namba ambayo ni sawa na siku za mwaka mmoja. Wanazuoni wengine wanasema siku hizo 6 za kufunga katika mwezi wa Shawwaal ni sharti zifungwe mfululizo mara baada ya Ramadhwaan. Wengine wanasema inatosha kuzifunga siku zote 6 ndani ya mwezi Shawwaal kwa mpangilio wowote, ama mfululizo au ukajiwekea siku za kufungua baada ya kufunga siku moja. Rai hii ya pili inachukuliwa kuwa sahihi zaidi. Kadhalika Swawm ya Shawwaal hutekelezwa baada ya kukamilisha funga kamili ya Ramadhwaan na kama kuna siku iliyopita basi ifungwe kulipwa kabla ya kuanza Sita za Shawwaal.

[3] Swawm kwa ajili ya Allaah (سبحانه وتعالى) kunaweza kumaanisha kuwa mtu anafunga huku yumo katika uwanja wa vita vya Jihaad. Inaweza pia kumaanisha mfungo wa khiari (Sunnah).

[4] Siku hizo tatu zinaitwa Ayyaamul-biydhw (Masiku meupe), mwanga wa angani unaangaza (kwa sababu ya mwezi mpevu) usiku kucha.

[5] Mwanamke kakatazwa Swiyaam za Sunnah bila ruhusa ya mumewe. Hata kama atataka kufunga siku za fardhi alizozikosa ni sharti aombe ruhusa.

[6] Nubayshah Al-Hudhaliyy ndiye Abuu Twariyf Nubayshah bin 'Abdillaah bin 'Amr bin 'Itaab Al-Hudhali. Huyu ni Swahaba ambaye ana Hadiyth kumi na moja. Alilowe Basra na aliitwa Nubayshah mkarimu.

[7] Siku za Tashriyq ni siku kumi na moja na kumi na mbili na kumi na tatu ya mwezi wa Dhul-Hijjah. Imekatazwa Swiyaam katika siku hizi. Mtu anayehiji anaweza kufunga katika siku hizo iwapo kashindwa kupata mnyama wa kuchinja kama kafara. Watu wengine hawana ruhusa ya kufunga siku hizo. Pia imekatazwa kufunga siku za 'Iyd zote mbili (ya Fitwr na Adhwhaa), iwe ni Swawm ya khiari au ya kulipia Swiyaam za fardhi.

[8] Imekatazwa Swawm siku ya Ijumaa peke yake. Katazo hili ni makhususi la kumsudia mtu anayefunga siku ya Ijumaa kwa kuamini kuwa atapata thawabu zaidi kwa kufunga siku hii.

[9] Mtu anaweza kufunga ilimradi awe analipa Swawm ya faradhi, au Swawm zinazohesabika kuwa ni za Waajib (za lazima). Lakini Swiyaam za khiari zimekatazwa asije mtu akachoshwa au akadhoofishwa mno kiasi cha kuifanya Swawm ya Ramadhwaan inayokuja iwe nzito kwake.

[10] Asw-Swammaai bint Busr alikuwa ni Buhaiya au Bahima bint Busr. Alikuwa Swahaba wa kutoka ukoo wa Mazin. Ikisemekana kuwa ni dada wa au shangazi wa ‘Abdullaah bin Busr.

[11] Kwa kuwa Jumamosi ina umuhimu maalumu kwa Mayahudi na wao hufunga katika siku hii, tunatakiwa tuwe tofauti nao, na kwa kuwa Swawm hiyo inavyofanana na ya Mayahudi, Nabiyy (ﷺ) amekataza kuichagua Jumamosi peke yake kwa Swawm. Lakini Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) anasimulia kuwa Nabiyy (ﷺ) alikuwa akifunga Jumamosi pamoja na Jumapili. Kwa kuwa siku ya Jumamosi ni sikukuu kwa Mayahudi, Nabiyy (ﷺ) alifunga siku hii ili kuharibu kawaida ya Mayahudi na kuongeza thawabu zake, alifunga siku ya Jumapili pia.

[12] Kwa mtu ambaye yumo katika tendo la kuhiji, imekatazwa Swawm siku ya ‘Arafah kwa vile mtu analazimika kukabiliana na taabu na mihangaiko migumu siku hiyo. Kwa hiyo Swawm siku hii atachoka na kudhoofu sana ambako kutapelekea kushindwa kuyafanya uzuri matendo mengine ya Hajj (Hijjah). Watu wengine wote wasiokuwa katika mchakato wa kuhiji siku ile wao hawakatazwi kufunga Swawm siku ile, na kwa yakini Swawm siku ile kwao kuna umuhimu na thawabu nyingi sana.

[13] Watu wengine wasiojua, hung’ang’ania kufunga Swawm mfululizo bila kuacha hata siku moja. Hadiyth hii inadhihirisha kuwa desturi hii imekatazwa. Wengi wa Wanazuoni wanaamini kuwa desturi hii ya kufunga Swawm kila siku milele kwa sababu hii inamdhoofisha mtu kwa hivyo inakuwa kikwazo kwa harakati zake za kidini na kidunia. Hadiyth nyingine inasema mtu anadaiwa au ana deni kwa afya yake na uhai wa mwili wake unahitaji mtu kujipa mapumziko mara kwa mara. Hata Nabiyy (ﷺ) alikuwa akifunga siku moja na anafungua siku nyingine.

03-Mlango Wa Al-I'tikaaf Na Qiyaam: Kisimamo cha Swalaah Za Usiku Wa Ramadhwaan

بَابُ الْإِعْتِكَافِ وَقِيَامِ رَمَضَانَ

03-Mlango Wa Al-I'tikaaf Na Qiyaam: Kisimamo cha Swalaah Za
Usiku Wa Ramadhwaan

568.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ قَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا، غُفِرَ لَهُ مَا
تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:
“Mwenye kusimama katika mwezi wa Ramadhwaan[1] kwa Iymaan
na kutaraji malipo[2] ataghufuriwa dhambi zake zilizotangulia.” [Al-
Bukhaariy, Muslim]

569.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا دَخَلَ الْعَشْرُ أَيُّ: الْعَشْرِ الْآخِرِ مِنْ رَمَضَانَ شَدَّ مِنْزَرَهُ، وَأَحْيَا لَيْلَهُ، وَأَيَّقَظَ أَهْلَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Siku kumi za mwisho wa Ramadhwaan zilipoingia, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alijifunga mkanda wake na alikesha usiku wake na aliiamsha familia yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

570.

وَعَنْهَا: {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَغْتَكِفُ الْعَشْرَ الْآخِرَ مِنْ رَمَضَانَ، حَتَّى تَوَفَّاهُ اللَّهُ، ثُمَّ اغْتَكَفَ أَزْوَاجُهُ مِنْ بَعْدِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema tena kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akikaa I’tikaaf siku kumi za mwisho za Ramadhwaan mpaka alipofishwa na Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) kisha wakeze wakakaa I’tikaaf baada yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

571.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا أَرَادَ أَنْ يَعْتَكِفَ صَلَّى الْفَجْرَ، ثُمَّ دَخَلَ مُعْتَكِفَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anapotaka kukaa I’tikaaf anaswali Alfajiri kisha anaingia I’tikaaf yake.”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim]

572.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {إِنْ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِيَدْخُلَ عَلَى رَأْسِهِ وَهُوَ فِي الْمَسْجِدِ فَأَرْجُلُهُ، وَكَانَ لَا يَدْخُلُ الْبَيْتَ إِلَّا لِحَاجَةٍ، إِذَا كَانَ مُعْتَكِفًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akiweka kichwa chake katika chumba changu wakati alipokuwa Msikitini, nami nikawa namchana nywele zake Msikitini, na alikuwa haingii nyumbani isipokuwa kwa haja tu anapokuwa kwenye I’tikaaf.”[4] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

573.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {السُّنَّةُ عَلَى الْمُعْتَكِفِ أَنْ لَا يَعُودَ مَرِيضًا، وَلَا يَشْهَدَ جَنَازَةً، وَلَا يَمَسَّ امْرَأَةً، وَلَا يُبَاشِرَهَا، وَلَا يَخْرُجَ

لِحَاجَةٍ، إِلَّا لِمَا لَا بُدَّ لَهُ مِنْهُ، وَلَا اِغْتِكَافَ إِلَّا بِصَوْمٍ وَلَا اِغْتِكَافَ إِلَّا فِي مَسْجِدٍ جَامِعٍ { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَلَا بَأْسَ بِرِجَالِهِ، إِلَّا أَنَّ الرَّاجِحَ وَقَفُ آخِرِهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Ni Sunnah kwa mwenye kukaa I’tikaaf asiende kumzuru mgonjwa, wala kuenda mazikoni, na asimuingilie wala kumkumbatia mwanamke,[5] au kutoka kwa haja yoyote ila asiyo budi nayo, iwe dharura muhimu sana kwake. Hakuna I’tikaaf ila kwa Swawm na hakuna I’tikaaf ila ndani ya Msikiti wa jamaa.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd kwa upokezi sahihi, lakini huhesabika Mawquwd]

574.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَيْسَ عَلَى الْمُعْتَكِفِ صِيَامٌ إِلَّا أَنْ يَجْعَلَهُ عَلَى نَفْسِهِ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَالْحَاكِمُ، وَالرَّاجِحُ وَقَفُهُ أَيْضًا

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swiyaam si lazima[6] kwa mwenye kukaa I’tikaaf Msikitini siku kumi za mwisho wa Ramadhwaan isipokuwa kama yeye mwenyewe anataka.”[7] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy na Al-Haakim, pia ni Mawquwf]

575.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: { أَنَّ رَجَالًا مِنْ أَصْحَابِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أُرُوا لَيْلَةَ الْقَدْرِ فِي الْمَنَامِ، فِي السَّبْعِ الْأَوَاخِرِ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "أَرَى رُؤْيَاكُمْ قَدْ تَوَاطَّاتُ فِي السَّبْعِ الْأَوَاخِرِ، فَمَنْ كَانَ مُتَحَرِّيًا فَلْيَتَحَرَّهَا فِي السَّبْعِ الْأَوَاخِرِ" مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Baadhi ya Maswahaba wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) waliona katika ndoto Laylatul-Qadr mnamo usiku wa saba wa mwisho wa Ramadhwaan. Kwa hivyo Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Naona ndoto zenu zinaafikiana na usiku wa saba wa mwisho, kwa hivyo mtu anayeitafuta aitafulite mnamo siku saba za mwisho.”[8] [Al-Bukhaariy, Muslim]

576.

وَعَنْ مُعَاوِيَةَ بْنِ أَبِي سُفْيَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ: { لَيْلَةُ سَبْعٍ وَعِشْرِينَ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالرَّاجِحُ وَقْفُهُ . وَقَدْ اخْتَلَفَ فِي تَعْيِينِهَا عَلَى أَرْبَعِينَ قَوْلًا أوردتها في " فتح الباري "

Kutoka kwa Mu’aawiyah bin Abiy Sufyaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa kuhusu Laylatul Qadr, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ni usiku wa ishirini na saba.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na ni Mawquwf]

577.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {قُلْتُ يَا رَسُولَ اللَّهِ: أَرَأَيْتَ إِنْ عَلِمْتُ أَيَّ لَيْلَةٍ لَيْلَةُ الْقَدْرِ، مَا أَقُولُ فِيهَا؟ قَالَ: "قُولِي: اَللّٰهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌّ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاعْفُ عَنِّي"} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، غَيْرَ أَبِي دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Mimi nilisema: Ee Rasuli wa Allaah! Unaonaje, nikiwa najua Laylatul-Qadr inaangukia usiku gani,[9] niseme nini?” Akasema: Sema:

اَللّٰهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌّ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاعْفُ عَنِّي

Allaahumma Innaka ‘Afuwwun Tuhibul-‘Afwa Fa’fu ‘Anniy

Ee Allaah! Hakia Wewe ni Msamehevu na Unapenda kusamehe, kwa hivyo nisamehe mimi.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa Abuu Daawuwd, na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Al-Haakim]

578.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: {لَا تُشَدُّ الرَّحَالُ إِلَّا إِلَى ثَلَاثَةِ مَسَاجِدَ: الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ، وَمَسْجِدِي هَذَا، وَالْمَسْجِدِ الْأَقْصَى} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msifunge safari isipokuwa ya Misikiti mitatu: Al-Masjid Al-Haraam (Makkah), Msikiti wangu na Al-Masjid Al-Aqswaa.”[10] [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Qiyaam ni kuswali Swalaah za khiari katika usiku. Katika mwezi wa Ramadhwaan, Swalaah inayoswaliwa baada ya 'Ishaa inajulikana kwa Taraawiyh. Kwa kuswali Swalaah hizi, mtu hughufuriwa dhambi zake zote zilizopita, ilimradi mtu huyo ana Iymaan kamili juu ya ahadi ya Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) kuhusu malipo yake.

[2] Inamaanisha kuwa hayo yasifanywe kwa ajili ya riyaa (kujionyesha). Iwapo mtu hafanyi kwa riyaa, basi ataghufuriwa madhambi yake madogomadogo yote. Wanazuoni wengine wanasema kughufuriwa huko kuna masharti ataghufuriwa mtu ikiwa tu anayo 'Aqiydah (Iymaan) thabiti.

[3] Kwa mujibu wa Hadiyth hii, wanawake pia wanafaa kukaa I'tikaaf (kujitenga na kukaa faragha Msikitini kuswali na kumdhukuru Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) mnamo siku 10 za mwisho za Ramadhwaan). Lakini wanawake lazima iwe shariy'ah inamruhusu kukaa I'tikaaf.

[4] Hapa “shida (Haja)” inamaanisha kuenda haja ndogo au kubwa.

[5] Hapa kungusa mwanamke kunamaanisha kukutana naye kimwili, tendo linalobatilisha I'tikaaf. Vinginevyo, kungusa tu mwanamke hakukatazwi.

[6] Inamaanisha siku zile za kawaida, zisizokuwa za Ramadhwaan.

[7] Mtu anayefanya I'tikaaf siyo lazima afunge Swawm, ila kama yeye kaapa kufunga.

[8] Hadiyth ya 'Abdullaah bin 'Umar kupitia kwa Swahiyhayn yasema mtu aitafula Laylatul-Qadr masiku kumi ya mwisho. Vinginevyo aitafula masiku saba ya mwisho, khususani masiku ya Witr kama ya tarehe ishirini na moja, ishirini na tatu, ishirini na tano, ishirini na saba, na tarehe ishirini na tisa.

[9] Maoni ya wengi kuhusu Laylatul-Qadr ni kwamba, usiku huu huangukia usiku wa 10 wa mwisho ya Ramadhwaan, khususan katika

usiku wa Witr, na hubadilika kila Ramadhwaan. Usiku huo huweza kutokea mnamo tarehe 21, 23, 25, n.k. haiwezi kusemwa kwa hakika kabisa, kwa kuwa siku hiyo imegubikwa na siri, ndivyo Hadiyth zinavyoelezea.

[10] Kama ilivyotajwa katika Hadiyth ya hapo nyuma, kuwa I'tikaaf ni sharti iwe Msikitini kutokana na kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ ۖ

Na wala msiwaingilie hali ya kuwa nyinyi wenye kukaa i'tikaaf Misikitini. [Al-Baqarah: 186]

Hadiyth hii pia inatuambia kuwa hairuhusiwi kuenda kutembea popote kwa madhumuni ya kupatia thawabu isipokuwa Misikiti hii mitatu ambayo ina fadhila zake. Mtu akienda katika Msikiti wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), basi na apate fadhila za kulizuru kaburi la Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

كِتَابُ الْحَجِّ

Kitabu Cha Hajj

06-Kitabu Cha Hajj - كِتَابُ الْحَجِّ

01-Mlango Wa Fadhila Zake Na Ubainisho Wa Wale Waliofaradhishiwa

بَابُ فَضْلِهِ وَبَيَانِ مَنْ فُرِضَ عَلَيْهِ

01-Mlango Wa Fadhila Zake Na Ubainisho Wa Wale
Waliofaradhishiwa

579.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الْعُمْرَةُ إِلَى الْعُمْرَةِ كَفَّارَةٌ لِمَا بَيْنَهُمَا، وَالْحَجُّ الْمَبْرُورُ لَيْسَ لَهُ جَزَاءٌ إِلَّا الْجَنَّةُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Umrah mpaka ‘Umrah ni kafara ya madhambi yatendwayo baina yake. Hajjun-Mabruwr (Hijjah iliyokubaliwa) haina malipo isipokuwa Jannah.”[1] [Al-Bukhaariy, Muslim]

580.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! عَلَى النِّسَاءِ جِهَادٌ؟} قَالَ: "نَعَمْ، عَلَيْهِنَّ جِهَادٌ لَا قِتَالَ فِيهِ: الْحَجُّ، وَالْعُمْرَةُ" {رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَابْنُ مَاجَةَ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَإِسْنَادُهُ صَحِيحٌ وَأَصْلُهُ فِي الصَّحِيحِ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilisema: Ee Rasuli wa Allaah! Je Jihaad ni lazima kwa wanawake?” Akasema: “Ndiyo, Jihaad isiyonasibisha mapigano ni lazima kwao, hiyo ni Hijjah na ‘Umrah.”[2] [Imetolewa na Ahmad na Ibn Maajah, na tamshi hili ni la Ibn Maajah, Isnaad yake ni imara, na chanzo chake ni Swahiyh Al-Bukhaariy]

581.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { أَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَعْرَابِيٌّ. فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَخْبِرْنِي عَنْ الْعُمْرَةِ، أَوَاجِبَةٌ هِيَ؟ فَقَالَ: " لَا. وَأَنْ تَعْتَمِرَ خَيْرٌ لَكَ " } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَالرَّاجِحُ وَقَفُّهُ وَأَخْرَجَهُ ابْنُ عَدِيٍّ مِنْ وَجْهِ آخَرَ ضَعِيفٍ عَنْ جَابِرٍ مَرْفُوعًا: { الْحَجُّ وَالْعُمْرَةُ فَرِيضَتَانِ }

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdullaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Bedui mmoja alikuja kwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Niambie juu ya ‘Umrah, je ni lazima?”[3] Akasema: “Hapana, lakini ukifanya ni bora kwako.” [Imetolewa na Ahmad na At-Tirmidhiy. Imeamuliwa kuwa ni Mawquwf]

Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Hijjah na ‘Umrah ni faradhi mbili.” [Imetolewa na Ibn ‘Adiyy kuwa ni dhaifu]

582.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {قِيلَ يَا رَسُولَ اللَّهِ، مَا السَّبِيلُ؟ قَالَ: "الزَّادُ وَالرَّاحِلَةُ"} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَالرَّاجِحُ إِرْسَالُهُ وَأَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عُمَرَ أَيْضًا، وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Ilisemwa: “Ee Rasuli wa Allaah! Nini maana ya As-Sabiyl?”[4] Akasema: “Chakula na kipando.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy na akaisahihisha Al-Haakim, na imeitwa Mursal]

Na tafsiri ya At-Tirmidhiy kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) ni sawa na hiyo, lakini ina udhaifu wa upokezi wake.

583.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَقِيَ رَكْبًا بِالرُّوحَاءِ فَقَالَ: "مَنْ الْقَوْمُ؟" قَالُوا: الْمُسْلِمُونَ. فَقَالُوا: مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ: "رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ" فَرَفَعَتْ إِلَيْهِ امْرَأَةٌ صَبِيًّا. فَقَالَتْ: أَلِهَذَا حَجٌّ؟ قَالَ: "نَعَمْ: وَلَكَ أَجْرٌ"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikutana na wasafiri kule Ar-Rawhaa akasema: “Ninyi ni nani?” Wakasema: “Ni Waislam.” Wakasema: “Wewe ni nani?” Akasema: “Mimi ni Rasuli wa Allaah.” Kisha mwanamke mmoja akamnyanyua mtoto wa kiume

akamsogezea na kusema: “Je huyu ana Hijjah?” Akasema: “Ndiyo na wewe utapata thawabu.”[5] [Imetolewa na Muslim]

584.

وَعَنْهُ قَالَ: {كَانَ الْفَضْلُ بْنُ عَبَّاسٍ رَدِيفَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ. فَجَاءَتْ امْرَأَةٌ مِّنْ خَتَمٍ، فَجَعَلَ الْفَضْلُ يَنْظُرُ إِلَيْهَا وَتَنْظُرُ إِلَيْهِ، وَجَعَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَصْرِفُ وَجْهَ الْفَضْلِ إِلَى الشَّقِّ الْأَخْرِ. فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّ فَرِيضَةَ اللَّهِ عَلَى عِبَادِهِ فِي الْحَجِّ أَذْرَكْتُ أَبِي شَيْخًا كَبِيرًا، لَا يَثْبُتُ عَلَى الرَّاحِلَةِ، أَفَأَحْجُّ عَنْهُ؟ قَالَ: "نَعَمْ" وَذَلِكَ فِي حَجَّةِ الْوَدَاعِ {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena: “Al-Fadhwl bin ‘Abbaas[6] alikuwa amepanda mnyama nyuma ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Mwanamke wa Khath-am alikuja na Al-Fadhwl akawa anamtazama, naye akawa anamtazama. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akageuza uso wa Al-Fadhwl upande mwingine. Kisha yule mwanamke akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Amri ya Allaah kuwa waja Wake wafanye Hijjah imekuja na baba yangu ni mzee mno hawezi kukaa sawa sawa juu ya ngamia. Je, mimi naweza kufanya Hijjah kwa niaba yake?” Akasema: “Ndiyo.” [7] Hiyo ilikuwa katika Hijjatul-Wadaa’ (Hijjah ya kuaga).” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

585.

وَعَنْهُ: { أَنَّ امْرَأَةً مِنْ جُهَيْنَةَ جَاءَتْ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَتْ: إِنَّ أُمِّي نَذَرَتْ أَنْ تَحُجَّ، فَلَمْ تَحُجَّ حَتَّى مَاتَتْ، أَفَأُحُجُّ عَنْهَا؟ قَالَ: "نَعَمْ"، حُجِّي عَنْهَا، أَرَأَيْتَ لَوْ كَانَ عَلَى أَمِّكَ دَيْنٌ، أَكُنْتَ قَاضِيَّتَهُ؟ إِفْضُوا اللَّهَ، فَاللَّهُ أَحَقُّ بِالْوَفَاءِ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena: “Mwanamke mmoja wa Juhaynah alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Mama yangu aliweka nadhiri kuhiji na hakuhihi, mpaka akafariki. Je, naweza kuhiji kwa niaba yake?” Akasema: “Ndiyo nenda kafanye Hijjah kwa niaba yake. Hebu niambie, je iwapo mama yako alikuwa na deni kwa mtu, ungemplipia? Basi lipa deni la mama yako kwa Allaah, kwani Allaah Anastahiki zaidi kulipwa deni alilokopwa Yeye.”[8] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

586.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَيُّمَا صَبِيٍّ حَجَّ، ثُمَّ بَلَغَ الْحِنْثَ، فَعَلَيْهِ أَنْ يَحُجَّ حَجَّةً أُخْرَى، وَأَيُّمَا عَبْدٍ حَجَّ، ثُمَّ أَعْتَقَ، فَعَلَيْهِ أَنْ يَحُجَّ حَجَّةً أُخْرَى } رَوَاهُ ابْنُ أَبِي شَيْبَةَ، وَالْبَيْهَقِيُّ وَرَجَالُهُ ثِقَاتٌ، إِلَّا أَنَّهُ اخْتَلَفَ فِي رَفْعِهِ، وَالْمَحْفُوظُ أَنَّهُ مَوْقُوفٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Endapo mtoto mdogo anafanya Hijjah na baadae anafikia balebale, ni lazima ahiji

tena. Na iwapo mtumwa anafanya Hijjah na baadae anaachwa huru, lazima afanye Hijjah nyingine.” [Imetolewa na Ibn Abuu Shaybah na Al-Bayhaqiyy, na mlolongo wa wapokezi wake ni wa kutegemewa; lakini wametofautiana kama Hadiyth hii ni Marfuw’. Hata hivyo imekubalika kuwa ni Mawquwf]

587.

وَعَنْهُ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَخْطُبُ يَقُولُ: { " لَا يَخْلُونَ رَجُلٌ بِامْرَأَةٍ إِلَّا وَمَعَهَا ذُو مَحْرَمٍ، وَلَا تُسَافِرُ الْمَرْأَةُ إِلَّا مَعَ ذِي مَحْرَمٍ " فَقَامَ رَجُلٌ، فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّ امْرَأَتِي خَرَجَتْ حَاجَّةً، وَإِنِّي اكْتَتَبْتُ فِي غَزْوَةٍ كَذَا وَكَذَا، قَالَ: " اِنْطَلِقْ، فَحُجَّ مَعَ امْرَأَتِكَ " { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akihutubia na kusema: “Mwanamume asikae faragha na mwanamke isipokuwa pamoja na mahram[9] wake. Na mwanamke asisafiri isipokuwa pamoja na mahram.” Mtu mmoja alisimama akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Mke wangu anaazimia kuenda kuhiji, na mimi nimeandikiwa kuenda vita kadha wa kadha.” Akasema: “Nenda kahiji pamoja na mkeo.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

588.

وَعَنْهُ: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَمِعَ رَجُلًا يَقُولُ: لَبَّيْكَ عَنْ شُبْرُمَةَ، قَالَ: " مَنْ شُبْرُمَةُ ؟ " قَالَ: أَخٌ لِي، أَوْ قَرِيبٌ لِي، قَالَ: " حَجَبْتَ عَنْ نَفْسِكَ ؟ " قَالَ: لَا. قَالَ: " حُجَّ عَنْ نَفْسِكَ، ثُمَّ حُجَّ عَنْ شُبْرُمَةَ " { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالرَّاجِحُ عِنْدَ أَحْمَدَ وَقَفُّهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimsikia mtu akisema: “Labbayka[10] kwa niaba ya Shubrumah.” Akasema: “Shubrumah ndiyo nani?” Akasema: “Ni kaka yangu.” Akasema: “Umeshahiji kwa ajili ya nafasi yako?” Akasema: “Hapana.” Hapo akasema: “Basi wewe hiji kwa ajili ya nafsi yako mwenyewe kisha utahiji kwa niaba ya Shubrumah.”[11] [Imetolewa na Abuu Daawuud na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Hibbaan, na Ahmad aliihesabu kuwa ni Mawquwf]

589.

وَعَنْهُ قَالَ: خَطَبَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: { " إِنَّ اللَّهَ كَتَبَ عَلَيْكُمُ الْحَجَّ " فَقَامَ الْأَقْرَعُ بْنُ حَابِسٍ فَقَالَ: أَفِي كُلِّ عَامٍ يَا رَسُولَ اللَّهِ ؟ قَالَ: " لَوْ قُلْتُهَا لَوَجَبْتُ، الْحَجُّ مَرَّةً، فَمَا زَادَ فَهُوَ تَطَوُّعٌ " { رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، غَيْرَ التِّرْمِذِيِّ وَأَصْلُهُ فِي مُسْلِمٍ مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituhutubia na akasema: “Allaah Amekufaradhishieni Hijjah.” Al-Aqra’ bin Haabis[12]

akasimama na akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Hiyo ifanyike kila mwaka?” Akasema: “Ningekuambia kuwa itekelezwe kila mwaka ingekuwa lazima. Hijjah ni mara moja, na ziada ni khiari.” [Imetolewa na Al-Khamsah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa At-Tirmidhiy, na chanzo chake ni Swahiyh Muslim kutoka katika Hadiyth ya Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)]

[1] Hakuna siku maalumu iliyoagizwa kufanya ‘Umrah, bali inaweza kufanywa wakati wowote mtu anaopenda. Hajj Mabruwr (Hijjah kubwa iliyokubaliwa) ni ile inayofanywa na mtu mwenye niyyah njema ya ikhlaasw, na mwaminifu, na ‘ibaadah zake zote zimefanywa kikamilifu na kisahih kabisa, na ambayo matokeo yake humfanya Haji (anayehiji) atake zaidi uadilifu na utendaji sahihi.

[2] Hii inatufahamisha kwamba hakuna ulazima wa wanawake kujiunga au kushiriki katika Jihaad ya kupigana kwenye viwanja vya vita. Hadiyth hii inatufahamisha kuwa, kwa kufanya Hajj wanawake wanastahiki thawabu za Jihaad.

[3] Kiistilahi, ‘Umrah ni “ziara”. Kwa mujibu wa istilahi za ki-shariy’ah, inamaanisha: “Ukiwa katika hali ya Ihraam, uizunguke Ka’bah (utufu), uswali Rakaa mbili kuelekea Maqaam ya Ibraahiym, unywe maji ya zamzam, utembe baina ya Asw-Swafaa na Al-Marwaa, na upunguze au unyoe kabisa nywele.” Kuna tofauti ya maoni ya kuwa ‘Umrah ni waajib au laa. Wanazuoni wengine wanaihesabu kuwa Mustahabb (iliyopendekezwa). Allaah Anajua zaidi.

[4] Allaah Anasema katika Qur-aan kuwa, Hijjah ni lazima kwa wale wenye uwezo kuenda kuhiji. Mtu mmoja akamuuliza Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ): “Nini maana ya neno As-Sabiyl? (njia)” Naye Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akajibu: “Maana yake ni gharama za safari na za kukimu familia ya mtu aendae kuhiji, na upatikanaji wa njia ya usafiri. Haya yote akiwa nayo, mtu huyo analazimika kuenda kuhiji. Lakini gharama zote hizi lazima asizipate kwa kukopa, yaani asibaki na deni, kwani akiwa na deni kwa mtu mwingine halazimiki kufanya Hijjah. Watu wanaoishi pale pale Makkah hawana lile sharti la kuwa na njia ya usafiri.

[5] Hadiyth hii inatufahamisha kuwa, thawabu za tendo jema alitendalo mtoto mdogo huwafikia wazazi wake. Pia inatufahamisha kuwa, kuhusu kufanya ‘ibaadah za Hijjah watoto wadogo wanatawaliwa na shariy’ah zile zile za mama yao, yaani Ihraam ya mama yao inakuwa ndiyo Ihraam yao na wao; na kukimbia kwa mama yao huwa ndiyo kukimbia kwao. Na iwapo mtoto kaifanya Hajj kabla hajabaleghe, atalazimika kufanya Hajj nyingine akisha kubaleghe, ilimradi ana pesa za kutosha kulipia gharama zake na za njia ya usafiri wake.

[6] Al-Fadhwl bin ‘Abbaas alikuwa binami wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na mama yake alikuwa Umm Fadhwl Lubaabah Al-Kubraa bint Al-Haarith Al-Hilaaliyyah. Al-Fadhwl alikuwa mzuri wa sura. Alikuwa imara pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika vita vya Hunayn, na alihudhuria uoshaji wa mwili wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alikuwa ndiye mwana wa kwanza wa Al-‘Abbaas. Alikwenda kwenye Jihaad kule Shaam, na yasemekana kuwa alikufa kwa tauni iitwayo “Amwas” kule Jordan mnamo mwaka wa 18 A.H. Pia inasemekana kuwa alikufa shahidi kule Yarmuk au kule Damascus akiwa amevaa deraya ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[7] Hijjah huwa ni ya lazima kwa mtu aliyekuwa na pesa za kutosha kuenda kuhiji, njia yake inakuwa wazi na salama, anapata idhini ya serikali yake, na anayo njia ya usafiri pia. Na ikiwa mtu huyu ana afya imara, ni lazima aende Hijjah yeye mwenyewe, na kumpeleka mtu mwingine akamfanyie Hijjah yake haitokubaliwa. Iwapo mtu anakuwa mzee mno kujiweza au anaugua ugonjwa mkubwa mno ambao haielekei kupona, inaruhusiwa amtume mtu kuenda kuhiji kwa niaba yake kwa kumpa pesa, na atimize wajibu wake wa Hijjah kwa njia hiyo. Lakini ni sharti kuwa, huyo mtu anayetumwa kuenda kumhijia huyo asiyejiweza awe alikwisha kuhiji yeye mwenyewe kabla ya kutumwa.

[8] Hadiyth hii inatuarifu kuwa, iwapo atakufa mtu ambaye kuhiji kulikuwa lazima kwake alipokuwa hai, basi ni lazima mrithi wake ahiji kwa niaba yake, bila kujali kama aliacha wasia kuhusu hii Hijjah au la. Halikadhalika katika matendo mengine ya ‘ibaadah kama Swawm na Zakaah. (Rejea Ahkaam Al-Janaaiz, cha Shaykh Al-Albaaniy, ukurasa (168-178) kwa maelezo zaidi).

[9] Tunafahamishwa kwamba mwanamume na mwanamke ambao hawajuani wasikutane faragha. Mwanamke asiende safari yoyote, iwe

ndefu au fupi, iwe kwa sababu za kidini au kwa dharura, isipokuwa awe na mume wake au Mahram wake. Mahram ni mtu ambaye asiyeweza kumuoa mwanamke huyo.

[10] “Labbayka Allaahumma Labbayka” maana yake ni “Ninaitikia mwito Wako Ee Allaah!” maneno yarudiwayo kusemwa kwa sauti (wanaume) na wanawake (kimya kimya) baada ya kuingia katika Ihraam mpaka kufikia Makkah kwa ajili ya Twawaaf (kwa mwenye kutekeleza ‘Umrah). Kisha wanapoingia tena Ihraam kwa ajili ya taratibu za Hajj ambayo inaanza tarehe 8 mwezi wa Hajj.

[11] Hii inatufahamisha kuwa, kama mtu hajahiji kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, haruhusiwi kumhijia mwingine, hata ikiwa ana nguvu ya aina gani (nguvu za kiwiliwili na kifedha) ya kutekeleza Hijjah yake mwenyewe. Maimaam wengi wanaafiki maoni haya.

[12] Al-Aqra’ bin Haabis alikuwa Tamiymiy aliyekuwa katika ujumbe wa Banuw Tamiym uliomzuru Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) baada ya kutekwa Makkah. Alikuwa miongoni mwa Mu’allafati Quluwbuhum (ambao nyoyo zao zilizoezwa kwa ajili ya Uislam, na kwa hivyo wakapewa Swadaqah ili wabakie imara katika Uislam). Alikuwa anaheshimika sana katika Jaahiliyyah. Alikufa wakati wa Ukhalifa wa ‘Umar.

02-Mlango Wa Mawaaqiyyt (Vituo Vya Ihraam)

بَابُ الْمَوَاقِيْتِ

02-Mlango Wa Mawaaqiyyt (Vituo Vya Ihraam)

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَقَّتَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ: ذَا الْحُلَيْفَةِ، وَلِأَهْلِ الشَّامِ: الْجُحْفَةَ، وَلِأَهْلِ نَجْدٍ: قَرْنَ الْمَنَازِلِ، وَلِأَهْلِ الْيَمَنِ: يَلَمْلَمَ، هُنَّ لَهُنَّ وَلِمَنْ أَتَى عَلَيْهِنَّ مِنْ غَيْرِهِنَّ مِمَّنْ أَرَادَ الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ، وَمَنْ كَانَ دُونَ ذَلِكَ فَمِنْ حَيْثُ أَنْشَأَ، حَتَّى أَهْلُ مَكَّةَ مِنْ مَكَّةَ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alichagua vituo vifuatavyo kwa ajili ya kuingia katika Ihraam:[1] (a) Dhal-Hulayfah[2] kwa watu wa Al-Madiynah. (b) Al-Juhfah kwa watu wa Syria. (c) Qarna Al-Manaazil kwa watu wa Najd. Na (d) Yalamlam kwa watu wa Yaman. Kwa hivyo vituo hivyo ni kwa kanda hizo na kwa watu wa maeneo mengine wanaokwenda huko kwa niyyah ya Hijjah na ‘Umrah. Mahala ambapo watu wa Makkah wanatakiwa kuingia katika Ihraam ni pale wanapotokea; hata wakazi wa Makkah huvalia Ihraam mumo humo Makkah.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَقَّتَ لِأَهْلِ الْعِرَاقِ ذَاتَ عِرْقٍ { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ وَأَصْلُهُ عِنْدَ مُسْلِمٍ مِنْ حَدِيثِ جَابِرٍ إِلَّا أَنَّ رَاوِيَهُ شَكَّ فِي رَفْعِهِ

وَفِي الْبُخَارِيِّ: {أَنَّ عُمَرَ هُوَ الَّذِي وَقَّتْ ذَاتَ عِرْقٍ}
وَعِنْدَ أَحْمَدَ، وَأَبِي دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيِّ: عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ: {أَنَّ
النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَقَّتْ لِأَهْلِ الْمَشْرِقِ: الْعَقِيقَ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alichagua Dhaata ‘Irq[3] iwe ndio pahala pa kuingia katika Ihraam watu wa Iraaq.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy]

Asili yake ni Hadiyith ya Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) katika upokezi wa Muslim, lakini msimulizi wake ana shaka kama ni Marfuw’.

Na katika Swahiyh Al-Bukhaariy imeelezwa kuwa: “Umar ndiye aliyeteua Dhaata ‘Irq.”

Ahmad, Abuu Daawuud, na At-Tirmidhiy wameipokea hii kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alichagua Al-‘Aqiyqa[4] iwe kituo cha watu wa mashariki kuingia katika Ihraam zao.”

[1] Maana ya Ihraam kilugha: ni haraam, yaani ni jambo lililoharamishwa.

Kiistilahi: Ni kuweka niyyah ya kuingia katika ‘ibaadah ya Hajj au ‘Umrah; kwa maana mtu anapoazimia kutekeleza ‘Umrah au Hajj akaanza taratibu zake *Miyqaat* na kutamka *Talbiyah*, huwa ameshaingia katika Ihraam na kwa hivyo kuna baadhi ya vitendo huwa ni haraam kwake kuvitenda, hadi atakapomaliza taratibu zake na akaitengua na Ihraam .

Na pia wanaume hutakiwa wavae mavazi maalumu ya shuka mbili nyeupe zinazovaliwa na wanaohiji au wenye kutekeleza ‘Umrah wanaponuia. Wanaweza kuvaa mavazi hayo kabla ya kufika Miyqaat kuanza safari ya kuenda kutekeleza Hijjah au ‘Umrah au wanaweza kuyavalia katika Miyqaat.

[2] Dhal Hulayfah ni jina la mahali ambapo ni umbali wa kilomita 15 kutoka Al-Madiynah. Na “Najd” kiistilahi ni “Ardhi iliyonyanyuliwa juu”, na ni ardhi kati ya Tihama na Iraq. “Qarna Al-Manaazil” ni pahala mkabala na Twaafif ambapo sasa panaitwa “Saail”. “Yalamlam” ni jina la mlima ulioko umbali wa safari ya siku mbili kutoka Yaman. Hivi ndivyo vituo vilivyopangiwa Hujaji waingie katika hali zao za Ihraam. Watu wanaoishi nje ya mipaka hii, lazima waingie katika hali ya Ihraam katika vituo hivi, na watu wanaoishi ndani ya mipaka hii waingie katika hali za Ihraam kutokea majumbani kwao wanakoishi. Siyo lazima kwao kuenda hadi kwenye Miyqaat (vituo vilivyotajwa hapo juu) kuingia Ihraam.

[3] Ukweli ni kuwa Dhaat ‘Irq ilichaguliwa na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mwenyewe kuwa Miyqaat kwa ajili ya Hujaji watokao Iraaq, na uamuzi wa hili ulifanyika wakati wa Hajjatul-Wadaa’ (Hijjah ya mwisho au Hijjah ya kuaga aliyoifanya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kabla ya kufa kwake). Ameipokea Al-Bukhaariy kwamba: “Umar ndiye aliyeichagua Dhaat ‘Itq”, ambapo ukweli ni kwamba ‘Umar aliitangaza tu.

[4] Al-‘Aqiyqa ni jina la mahala ambapo ni mkabala na Dhaat-‘Irq

03-Mlango Wa Adabu Na Sifa Za Ihraam

بَابُ وَجُوهِ الْأَحْرَامِ وَصِفَتِهِ

03-Mlango Wa Adabu Na Sifa Za Ihraam

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {خَرَجْنَا مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَامَ حَجَّةِ الْوَدَاعِ، فَمِنَّا مَنْ أَهَلَ بِعُمْرَةٍ، وَمِنَّا
مَنْ أَهَلَ بِحَجٍّ وَعُمْرَةٍ، وَمِنَّا مَنْ أَهَلَ بِحَجٍّ، وَأَهَلَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِالْحَجِّ، فَأَمَّا مَنْ أَهَلَ بِعُمْرَةٍ فَحَلَّ، وَأَمَّا
مَنْ أَهَلَ بِحَجٍّ، أَوْ جَمَعَ الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ فَلَمْ يَحِلُّوا حَتَّى كَانَ
يَوْمَ النَّحْرِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Tulitoka pamoja na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika mwaka wa Hijjah ya kuaga,[1] na wengine wetu wakatamka Talbiyah kwa ajili ya ‘Umrah, wengine kwa ajili ya Hijjah pamoja na ‘Umrah, na wengine kwa ajili ya Hijjah peke yake. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitamka Talbiyah kwa ajili ya Hijjah. Wale waliotamka kwa ajili ya ‘Umrah peke yake wakajitengua Ihraam. Lakini wale waliotamka kwa ajili ya Hijjah peke yake au wale waliounganisha Hijjah na ‘Umrah hawakutengua Ihraam zao hadi siku ya kuchinja.”[2] [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Zipo aina tatu za Ibaada ya Hijjah nazo ni: (a) Ifraad ambapo Haji anaingia katika hali ya Ihraam kwa nia ya kutekeleza Hijjah peke yake. (b) Tamattu’ ambapo Haji hingia katika hali ya Ihraam katika kituo cha Miyqaat kwa nia ya kutekeleza ‘Umrah na kisha atekeleze Twawaaf (kutufu) na Sa’y (kusai). Iwapo kamleta mnyama wa kafara, basi asiivue Ihraam yake; na akiwa hakuleta mnyama basi aivue Ihraam yake wakati huo. Zikianza siku za Hijjah, lazima aingie katika hali ya Ihraam tena na aitekeleze Hijjah. (c) Qiraan ambapo Haji huingia katika hali ya Ihraam kwa nia ya kutekeleza ‘Umrah na Hijjah kwa pamoja. Wakazi wa Makkah hawaruhusiwi kutekeleza au kufanya Tamattu’ na Qiraan.

[2] Yawm An-Nahr ni siku ya kuchinja mnyama wa kafara, yaani tarehe 10 mwezi wa Dhul-Hijjah.

04-Mlango Wa Ihraam Na Yanayohusiana Nayo

بَابُ الْأَحْرَامِ وَمَا يَتَعَلَّقُ بِهِ

04-Mlango Wa Ihraam Na Yanayohusiana Nayo

593.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {مَا أَهْلَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِلَّا مِنْ عِنْدِ الْمَسْجِدِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kamwe hakupaza sauti katika Talbiyah isipokuwa alipo toka Msikitini (Dhul-Hulayfah).”[1] [Al-Bukhaariy, Muslim]

594.

وَعَنْ خَلَادِ بْنِ السَّائِبِ عَنْ أَبِيهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَتَانِي جِبْرِيلُ، فَأَمَرَنِي أَنْ أَمُرَ أَصْحَابِي أَنْ يَرْفَعُوا أَصْوَاتَهُمْ بِالْإِهْلَالِ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Khallaad[2] bin As-Saaib kutoka kwa baba yake[3] (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Jibriyl alikuja kwangu akaniamrisha niwaamrishe Swahaba zangu kupaza sauti[4] zao katika kutamka Talbiyah.”[5] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

595.

وَعَنْ زَيْدِ بْنِ ثَابِتٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ تَجَرَّدَ لِإِهْلَالِهِ وَاغْتَسَلَ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ

Kutoka kwa Zayd bin Thaabit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) alivua nguo zake (za kawaida) ili avae Ihraam zake na akaoga.”[6] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaiita Hasan]

596.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سُئِلَ: مَا يَلْبَسُ الْمُحْرِمُ مِنَ الثِّيَابِ؟ فَقَالَ: "لَا تَلْبَسُوا الْقُمُصَ، وَلَا الْعَمَائِمَ، وَلَا السَّرَاوِيلَاتِ، وَلَا الْبِرَانِسَ، وَلَا الْخِفَافَ، إِلَّا أَحَدٌ لَا يَجِدُ النَّعْلَيْنِ فَلْيَلْبَسْ الْخُفَّيْنِ وَلْيَقْطَعْهُمَا أَسْفَلَ مِنَ الْكَعْبَيْنِ، وَلَا تَلْبَسُوا شَيْئًا مِنَ الثِّيَابِ مَسَّهُ الزَّعْفَرَانُ وَلَا الْوَرَسُ"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa mwenye kuhirimia anavaa nguo gani?[7] Akasema: Asivae shati, kilemba, suruali, vazi lenye vifuniko vya kichwa, wala viatu, isipokuwa kama mtu hawezi kupata ndala na akalazimika kuvaa viatu mbapo ni lazima avikate chini ya tindi ya mguu na asivae nguo zenye kutiwa rangi ya zaafarani (Manjano) au Wars.”[8] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

597.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كُنْتُ أُطِيبُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِإِحْرَامِهِ قَبْلَ أَنْ يُحْرِمَ، وَلِحِلِّهِ قَبْلَ أَنْ يَطُوفَ بِالْبَيْتِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilikuwa ninampaka manukato[9] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kwa ajili ya Ihraam yake[10] kabla hajaivaa, na baada ya kuivua, kabla hajatufu Nyumba (hajaizunguka Ka’bah).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

598.

وَعَنْ عُثْمَانَ بْنِ عَفَّانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَنْكِحُ الْمُحْرِمُ، وَلَا يُنْكَحُ، وَلَا يَخْطُبُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Uthmaan bin ‘Affaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Aliye katika Ihraam asioe, wala asimuozeshe mtu[11], wala asichumbie.” [Imetolewa na Muslim]

599.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {فِي قِصَّةِ صَيْدِهِ الْحِمَارَ الْوَحْشِيِّ، وَهُوَ غَيْرُ مُحْرِمٍ، قَالَ: فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِأَصْحَابِهِ، وَكَانُوا مُحْرِمِينَ: " هَلْ مِنْكُمْ أَحَدٌ أَمَرَهُ أَوْ أَشَارَ إِلَيْهِ بِشَيْءٍ ؟ " قَالُوا: لَا. قَالَ: " فَكُلُوا مَا بَقِيَ مِنْ لَحْمِهِ " { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Qataadah Al-Answaariy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Kuhusu Hadiyth ya yeye kuwinda pundamilia na hakuwa katika hali ya Ihraam, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwauliza Maswahaba wake waliokuwa katika hali ya Ihraam kuwa: “Kuna yeyote kati yenu amependekeza au ameashiria

chochote kwake kuhusu kuwinda?” Wakasema: “Hapana.” Akasema: “Kuleni nyama yake iliyobakia.”[12] [Al-Bukhaariy, Muslim]

600.

وَعَنْ الصَّعْبِ بْنِ جَثَّامَةَ اللَّيْثِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُ أَهْدَى
لِرَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حِمَارًا وَحَشِيًّا، وَهُوَ
بِالْأَبْوَاءِ، أَوْ بِوَدَّانَ، فَرَدَّهُ عَلَيْهِ، وَقَالَ: " إِنَّا لَمْ نَرُدَّهُ عَلَيْكَ
إِلَّا أَنَّا حُرْمٌ " { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Asw-Swa’b bin Jath-thaamah Al-Laythiyy[13] (رَضِيَ
صَلَّى اللَّهُ) amesema kuwa: “Alimpa Rasuli wa Allaah (اللَّهُ عَنْهُ
(عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) nyama ya pundamilia[14] alipokuwa Al-Abwaa
au Waddaan, akaikataa na kusema: “Tulikataa kwa sababu tulikuwa
katika Ihraam.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

601.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { خَمْسٌ مِنَ الدَّوَابِّ كُلُّهُنَّ فَاسِقٌ، يُقْتَلْنَ فِي الْحِلِّ
وَ الْحَرَمِ: الْغُرَابُ، وَالْجِدَاةُ، وَالْعَقْرَبُ، وَالْفَأْرَةُ، وَالْكَلْبُ
الْعَقُورُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuna viumbe
watano wana madhara, na vinaweza kuuliwa nje au ndani ya maeneo

matukufu: (a) Kunguru (b) Kipanga, (c) ‘Nge, (d) Panya na (e) mbwa anayeuma watu.”[15] [Al-Bukhaariy, Muslim]

602.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِخْتَجَمَ وَهُوَ مُحْرِمٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alifanya hijamah (kuumikwa) wakati akiwa katika hali ya Ihraam.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

603.

وَعَنْ كَعْبِ بْنِ عُجْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {حُمِلْتُ إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَالْقَمْلُ يَتَنَازَرُ عَلَى وَجْهِهِ، فَقَالَ: " مَا كُنْتُ أَرَى الْوَجَعَ بَلَغَ بِكَ مَا أَرَى، تَجِدُ شَاةً؟ قُلْتُ: لَا. قَالَ: " فَصُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ، أَوْ أَطْعِمْ سِتَّةَ مَسَاكِينَ، لِكُلِّ مِسْكِينٍ نِصْفُ صَاعٍ " } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ka’b bin ‘Ujrah[16] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilichukuliwa mpaka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na chawa walikuwa wakipuputika usoni mwangu. Akasema: “Sikujua kuwa uchungu umekuathiri kama ninavyoona sasa, unaweza kutoa kafara ya mbuzi?” Nikasema: “Hapana.” Akasema:

“Funga Swawm siku tatu au walishe maskini sita kila masikini nusu pishi.”[17] [Al-Bukhaariy, Muslim]

604.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَمَّا فَتَحَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَكَّةَ، قَامَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي النَّاسِ، فَحَمِدَ اللَّهَ وَأَثْنَى عَلَيْهِ، ثُمَّ قَالَ: " إِنَّ اللَّهَ حَبَسَ عَنْ مَكَّةَ الْفِيلَ، وَسَلَّطَ عَلَيْهَا رَسُولَهُ وَالْمُؤْمِنِينَ، وَإِنَّهَا لَمْ تَحِلَّ لِأَحَدٍ كَانَ قَبْلِي، وَإِنَّمَا أُحِلَّتْ لِي سَاعَةً مِنْ نَهَارٍ، وَإِنَّهَا لَنْ تَحِلَّ لِأَحَدٍ بَعْدِي، فَلَا يُنْفَرُ صَيْدُهَا، وَلَا يُخْتَلَى شَوْكُهَا، وَلَا تَحِلُّ سَاقِطَتُهَا إِلَّا لِمُنْشِدٍ، وَمَنْ قُتِلَ لَهُ قَتِيلٌ فَهُوَ بِخَيْرِ النَّظَرَيْنِ " فَقَالَ الْعَبَّاسُ: إِلَّا الْأَذْخَرَ، يَا رَسُولَ اللَّهِ، فَإِنَّا نَجْعَلُهُ فِي قُبُورِنَا وَبُيُوتِنَا، فَقَالَ: " إِلَّا الْأَذْخَرَ " { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Allaah alipompa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ushindi wa Makkah, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisimama akamhimidi na kumtukuza Allaah kisha akasema: “Allaah Alizuia tembo[18] asiingie Makkah, na Akampa uwezo Rasuli Wake na Waumini wa kushinda. Kupigana ndani yake hakukuruhusiwa kwa mtu yeyote kabla yangu, lakini imeruhusiwa kwangu saa moja ya mchana, na haitoruhusiwa kwa yeyote baada yangu. Wanyama wake hawatumbuliwa, miiba yake haitakatwa, si halali kuokota kinachoangukia ila kwa yule anayekitangaza,[19] na mwenye kuuwawa mtu wake ana chaguo zuri kati ya zaidi kati ya mawili

hayo.”[20] Al-‘Abbaas akasema: “Isipokuwa mti uitwao Al-Idkhir Ee Rasuli wa Allaah! Kwa sababu tunautumia katika makaburi na nyumba zetu.” Naye akasema: “Isipokuwa Al-Idkhir.”[21] [Al-Bukhaariy, Muslim]

605.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدِ بْنِ عَاصِمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِنَّ إِبْرَاهِيمَ حَرَّمَ مَكَّةَ وَدَعَا لِأَهْلِهَا، وَإِنِّي حَرَّمْتُ الْمَدِينَةَ كَمَا حَرَّمَ إِبْرَاهِيمُ مَكَّةَ، وَإِنِّي دَعَوْتُ فِي صَاعِهَا وَمُدَّهَا بِمِثْلِي مَا دَعَا إِبْرَاهِيمُ لِأَهْلِ مَكَّةَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Zayd bin ‘Aaswim (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuwa Ibraahiym alitangaza Makkah kuwa ni tukufu,[22] na kawaombea du’aa watu wake, na mimi naitangaza Al-Madiynah kuwa ni tukufu kama Ibraahiym alivyoitangaza Makkah kuwa ni tukufu, na mimi ninaomba katika pishi na kibaba (ibarikiwe), mara mbili zaidi kuliko Ibraahiym alivyowaombea watu wa Makkah.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

606.

وَعَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْمَدِينَةُ حَرَّمَ مَا بَيْنَ عَيْرٍ إِلَى ثَوْرِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aliy bin Abuu Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Al-Madiynah ni tukufu kutoka ‘Ayr hadi Thawr.”[23] [Imetolewa na Muslim]

[1] Hadiyth hii inadhihirisha Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliingia katika Ihraam ima kule Baida au karibu na mti. Pia tunafahamishwa kuwa kuingia katika Ihraam kabla ya kufika katika Miyqaat kumekatazwa. Hii inapinga maoni ya wengine wanaosema ni sawa kuingia katika hali ya Ihraam kabla.

[2] Khallaad ndiye Khallaad bin As-Saaib bin Khallaad bin Suwayd Al-Answaar Al-Khazraj, ambaye alikuwa Taabi’iy aliyetegemewa sana wa kizazi cha tatu.

[3] Babake Khallaad ni Swahaba aliyepewa jina la utani la Abuu Sahla. Alihudhuria vita vya Badr na akawa gavana wa Mu’aawiyah huko Yaman. Inasemekana pia kuwa ‘Umar alimpeleka kule Yaman. Alikufa mnamo mwaka wa 71 A.H.

[4] Hadiyth hii inatufahamisha kuwa ni lazima kutamka Talbiyah kwa sauti kubwa. Kuhusu wanawake ‘Ulamaa wengi wanaona kuwa waitamke Talbiyah kwa sauti ya chini.

[5] Talbiyah ni kutamka:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ ، لَبَّيْكَ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ ، إِنَّ الْحَمْدَ ، وَالنَّعْمَةَ ، لَكَ وَالْمُلْكَ ،
لَا شَرِيكَ لَكَ ،

Labbayka-Allaahumma Labbayk. Labbayka laa shariyka Laka Labbayk. Innal-Hamda Wan-Ni'imata Laka wal-Mulk laa shariyka Lak.

"Nimekuitikia Ee Allaah nimekuitika, nimekuitika Huna mshirika nimekuitika, hakika Himdi na Neema na Ufalme ni Vyako Huna mshirika."

[6] Hii inatufahamisha kua kuoga kwa ajili ya kuingia katika Ihraam ni Sunnah.

[7] Nguo zote hizi zikishavuliwa, nguo pekee za kuvaa ni shuka mbili ambazo ndiyo nguo za Ihraam yenyewe. Mwanamke anaweza kufunika kichwa chake kwa ushungi, lakini asifunike uso wake kwa ushungi.

[8] Manukato yenye rangi ya manjano.

[9] Kupitia Hadiyth hii inadhihirisha kuwa, manukato yanaweza kupakwa katika mwili wa hujaji kabla hajaingia katika Ihraam, na si ubaya kama mwili wake utaendelea kunukia hata baada ya kuingia katika Ihraam. Pia inaruhusiwa tena kupaka mwili manukato kabla ya Twawaaful-Widaa'i (Twawaaf ya kuaga).

[10] Hali ya kuwania kutekeleza Hijjah na 'Umrah.

[11] Mtu ambaye yumo katika hali ya Ihraam haruhusiwi kufungisha ndoa ya mwanamume au mwanamke au yake mwenyewe au kwa niaba ya mtu mwingine.

[12] Tukio hili lilitokea mnamo mwaka wa Mkataba wa Al-Hudaybiyah. Kama mtu Halal (yaani mtu ambaye hayumo katika hali ya Ihraam) anawinda mnyama kwa niyyah ya kumpa Muhrim, au kwa njia yoyote ile Muhrim alijisaidia yeye mwenyewe kuwinda, anakatazwa kula nyama ya mnyama aliyewindwa hivyo. Inaruhusiwa pale tu ambapo mnyama huyo amewindwa na au kwa niaba ya mtu Halal, bila kusaidiwa na kwa ridhaa ya Muhrim.

[13] Asw-Swa'b bin Jath-thaamah Al-Laythiyy aliishi kule Waddaan na Al-Abwaa na Hadiyth yake ilitajwa na watu wa Al-Hijaz. Alikuwa katika Ukhalifa wa Abuu Bakar au wa 'Uthmaan.

[14] Hii inatuarifu kuwa Nabiyy (ﷺ) alikula nyama ya mnyama aliyewindwa akiwa katika Ihraam kwa kuwa Sa'b aliwinda kwa niyyah ya kumpa Nabiyy (ﷺ).

[15] Kuwaua wanyama hao watano hata wakiwa wamo ndani ya eneo la Msikiti Mtukufu siyo vibaya. Halikadhalika, mtu akiwaua hao wakati yumo katika hali ya Ihraam na yumo ndani ya eneo la Msikiti Mtukufu, hapati adhabu yoyote (kama kutoa kafara ya mnyama au Swadaqah). Kwa kunukuu Hadiyth au tukio hili la mwanzo, Wanazuoni wengine wamekuwa wakiruhusu kuuliwa kwa wanyama wote Haraam (yaani wanyama ambao kuliwa nyama yake kumekatazwa katika Uislam), na hawataji adhabu yoyote kwa mtu kuwaua hao. Inapotokea Muhrim anamuua mnyama baada ya kumshambulia, hapati adhabu yoyote.

[16] Ka'b bin 'Ujrah alikuwa Swahaba maarufu kutoka katika kabila la Al-Bali, na alikuwa rafiki wa Answaar. Aliloweza Kufa na akafia Al-Madiynah mnamo mwaka wa 51 A.H. akiwa na umri wa miaka 75.

[17] Hii inatuarifu kuwa Muhrim analazimika kulipa fidya, hata kama kanyoa kichwa chake kwa sababu maalumu. Na fidya zipo aina tatu: (a) Atoe kafara ya mnyama (b) Afunge Swawm siku tatu (c) Awalishe maskini sita au atoe kilo moja ya nafaka kama Swadaqah kwa kila mtu. Endapo akiwa na uwezo wa kutoa kafara ya mnyama, basi haruhusiwi kutoa fidya hizo mbili za mwisho. Ikiwa hana pesa za kutosha kutoa kafara atachagua moja kati ya haya mawili: (i) Ima afunge Swawm, au (ii) Awalishe maskini.

[18] Hadiyih hii imesimuliwa katika Qur-aan (105: 1-5). Imesemwa kuwa Abraha Al-Athram alipokuwa mfalme wa Manaswara wa Yaman, aliishambulia Makkah kwa jeshi la tembo wengi, kwa lengo la kuibomoa Ka'bah. Maqurayshi hawakuweza kumkabili, kwa hivyo waliondoka Makkah na wakakimbilia mbali. Allaah (سبحانه وتعالى) Akawatuma makundi ya ndege wana vijiwe vidogo mdomoni mwao na kwenye makucha yao. Kila aliyeangukiwa na vijiwe hivi, kwa nguvu za mateso Aliyoyatuma Allaah (سبحانه وتعالى) aliteketea. Abraha, pamoja na majeshi yake yaliyokuwa yakiunguruma wakaishia kuangamizwa. Na hivyo ndivyo Allaah (عز وجل) Alivyoiokoa Nyumba Yake (Ka'bah) isibomolewe.

[19] Hii inamaanisha kuwa iwapo mtu ataokota kitu kitachoanguka au kupotea mle kwa niyyah ya kukichukua yeye mwenyewe, imekatazwa. Lakini akikiokota kwa niyyah ya kutangaza ili kirejeshwe kwa mwenye kukimiliki kihalali, hiyo imeruhusiwa.

[20] Yaani atachagua kati ya haya mawili: (a) Ima atakubali apewe diya (pesa za damu, au malipo kwa kuuliwa mtu wake). (b) Au anaweza kuchagua kulipiza kwa kumuua muuaji yaani kuchukua Qiswaasw (kisasi)

[21] Al-Idkhir ni aina ya majani yanayotumika katika mchakato wa kuyeyusha metali. Hayo hulazwa juu ya mapaa na sakafuni ndani ya majumba, na pia hupandwa makaburini pia.

[22] Nabiyy Ibraahiym (عليه السلام) aliitangaza Makkah kuwa ni patukufu, na aliwaomba watu wake waweze kujikimu. Naye Nabiyy Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) pia aliitangaza Al-Madiynah kuwa ni tukufu na akawaomba watu wake waweze kujikimu.

[23] ‘Ayr na Thawr ni milima miwili inayoizunguka Al-Madiynah. ‘Ayr ni mlima maarufu ulioko kusini mwa Al-Madiynah na kusini Magharibi ya Msikiti wa Qubaa. Watu wengine wameelewa vibaya kwamba mlima wa Thawr uko Makkah, na huenda msimuliaji alikosea huo kwa kuudhani ni mlima mwingine. Ukweli ni kwamba, maoni yao haya yamekosewa. Kuna mlima kule Al-Madiynah pia, mdogo na wa mviringo, ulioko kaskazini mbele zaidi ya mlima wa Uhud ambao pia unaitwa Thawr.

05-Mlango Wa Sifa Za Hijjah Na Kuingia Makkah

بَابُ صِفَةِ الْحَجِّ وَدُخُولِ مَكَّةَ

05-Mlango Wa Sifa Za Hijjah Na Kuingia Makkah

607.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حَجَّ، فَخَرَجْنَا مَعَهُ، حَتَّى أَتَيْنَا ذَا الْحُلَيْفَةِ، فَوَلَدَتْ أَسْمَاءُ بِنْتُ عُمَيْسٍ، فَقَالَ: " اغْتَسِلِي وَاسْتَنْفِرِي بِثَوْبٍ، وَأَحْرِمِي " وَصَلَّى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الْمَسْجِدِ، ثُمَّ رَكِبَ الْقَصَوَاءَ حَتَّى إِذَا اسْتَوَتْ بِهِ عَلَى الْبَيْدَاءِ أَهْلٌ بِالتَّوْحِيدِ: " لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنَّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ، لَا شَرِيكَ لَكَ "

حَتَّى إِذَا أَتَيْنَا الْبَيْتَ اسْتَلَمَ الرُّكْنَ، فَرَمَلَ ثَلَاثًا وَمَشَى أَرْبَعًا،
ثُمَّ أَتَى مَقَامَ إِبْرَاهِيمَ فَصَلَّى، ثُمَّ رَجَعَ إِلَى الرُّكْنِ فَاسْتَلَمَهُ.

ثُمَّ خَرَجَ مِنَ الْبَابِ إِلَى الصَّفَا، فَلَمَّا دَنَا مِنَ الصَّفَا قَرَأَ: " **إِنَّ
الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ** " " أَبْدَأُ بِمَا بَدَأَ اللَّهُ بِهِ " **فَرَقِيَ الصَّفَا، حَتَّى رَأَى الْبَيْتَ، فَاسْتَقْبَلَ الْقِبْلَةَ فَوَحَّدَ اللَّهَ
وَكَبَّرَهُ وَقَالَ: " لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ،
وَلَهُ الْحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ
أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ، وَهَزَمَ الْأَحْزَابَ وَحْدَهُ " . ثُمَّ دَعَا
بَيْنَ ذَلِكَ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، ثُمَّ نَزَلَ إِلَى الْمَرْوَةِ، حَتَّى انْصَبَّتْ
قَدَمَاهُ فِي بَطْنِ الْوَادِي سَعَى حَتَّى إِذَا صَعَدَتَا مَشَى إِلَى
الْمَرْوَةِ فَفَعَلَ عَلَى الْمَرْوَةِ، كَمَا فَعَلَ عَلَى الصَّفَا ... فَذَكَرَ
الْحَدِيثَ. وَفِيهِ:**

فَلَمَّا كَانَ يَوْمَ التَّرْوِيَةِ تَوَجَّهُوا إِلَى مَنَى، وَرَكِبَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَصَلَّى بِهَا الظُّهْرَ، وَالْعَصْرَ،
وَالْمَغْرِبَ، وَالْعِشَاءَ، وَالْفَجْرَ، ثُمَّ مَكَثَ قَلِيلًا حَتَّى طَلَعَتِ
الشَّمْسُ، فَأَجَازَ حَتَّى أَتَى عَرَفَةَ، فَوَجَدَ الْقُبَّةَ قَدْ ضُرِبَتْ لَهُ
بِنَمِرَةٍ فَنَزَلَ بِهَا.

حَتَّى إِذَا زَاغَتِ الشَّمْسُ أَمَرَ بِالْقَصَوَاءِ، فَرُحِلَتْ لَهُ، فَأَتَى
بَطْنَ الْوَادِي، فَخَطَبَ النَّاسَ.

ثُمَّ أَدْنَى ثُمَّ أَقَامَ، فَصَلَّى الظُّهْرَ، ثُمَّ أَقَامَ فَصَلَّى الْعَصْرَ، وَلَمْ
يُصَلِّ بَيْنَهُمَا شَيْئًا.

ثُمَّ رَكِبَ حَتَّى أَتَى الْمَوْقِفَ فَجَعَلَ بَطْنَ نَاقَتِهِ الْقَصَوَاءِ إِلَى الصَّخَرَاتِ، وَجَعَلَ حَبْلَ الْمَشَاةِ بَيْنَ يَدَيْهِ وَاسْتَقْبَلَ الْقِبْلَةَ، فَلَمْ يَزَلْ واقِفًا حَتَّى غَرَبَتِ الشَّمْسُ، وَذَهَبَتِ الصُّفْرَةُ قَلِيلًا، حَتَّى غَابَ الْقُرْصُ، وَدَفَعَ، وَقَدْ شَنَقَ لِلْقَصَوَاءِ الزَّمَامَ حَتَّى إِنَّ رَأْسَهَا لَيُصِيبُ مَوْرِكَ رَحْلِهِ، وَيَقُولُ بِيَدِهِ الْيُمْنَى: " أَيُّهَا النَّاسُ، السَّكِينَةُ، السَّكِينَةُ "، كُلَّمَا أَتَى حَبْلًا أَرَخَى لَهَا قَلِيلًا حَتَّى تَصْعَدَ.

حَتَّى أَتَى الْمُزْدَلِفَةَ، فَصَلَّى بِهَا الْمَغْرِبَ وَالْعِشَاءَ، بِأَذَانٍ وَاحِدٍ وَإِقَامَتَيْنِ، وَلَمْ يُسَبِّحْ بَيْنَهُمَا شَيْئًا، ثُمَّ اضْطَجَعَ حَتَّى طَلَعَ الْفَجْرُ، فَصَلَّى الْفَجْرَ، حِينَ تَبَيَّنَ لَهُ الصُّبْحُ بِأَذَانٍ وَإِقَامَةٍ ثُمَّ رَكِبَ حَتَّى أَتَى الْمَشْعَرَ الْحَرَامَ، فَاسْتَقْبَلَ الْقِبْلَةَ، فَدَعَاهُ، وَكَبَّرَهُ، وَهَلَّلَهُ فَلَمْ يَزَلْ واقِفًا حَتَّى أُسْفَرَ جَدًّا.

فَدَفَعَ قَبْلَ أَنْ تَطْلُعَ الشَّمْسُ، حَتَّى أَتَى بَطْنَ مُحَسَّرٍ فَحَرَكَ قَلِيلًا، ثُمَّ سَلَكَ الطَّرِيقَ الْوُسْطَى الَّتِي تَخْرُجُ عَلَى الْجَمْرَةِ الْكُبْرَى، حَتَّى أَتَى الْجَمْرَةَ الَّتِي عِنْدَ الشَّجَرَةِ، فَرَمَاهَا بِسَبْعِ حَصِيَّاتٍ، يُكَبِّرُ مَعَ كُلِّ حَصَاةٍ مِنْهَا، مِثْلَ حَصَى الْخَذْفِ، رَمَى مِنْ بَطْنِ الْوَادِي، ثُمَّ انْصَرَفَ إِلَى الْمَنْحَرِ، فَنَحَرَ، ثُمَّ رَكِبَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَأَفَاضَ إِلَى الْبَيْتِ، فَصَلَّى بِمَكَّةَ الظُّهْرَ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ مُطَوَّلًا

Kutoka kwa Jaabir Bin ‘Abdullaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alihiji na tulikwenda pamoja naye. Tulipofika Dhul-Hulayfah, Asmaa bint ‘Umays alijifungua mtoto. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

(وَسَلَّمَ) akasema: “Wewe oga, kisha uzingirishe nguo sehemu zako za siri, na uvae Ihraam.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akaswali Msikitini na kisha akampanda Al-Qasw-waa,[1] na aliposimama wima na yeye Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akiwa mgongoni kwake, kule Al-Baydaa,[2] akapaza sauti yake akitangaza Tawhiyd akasema:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ ، لَبَّيْكَ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ ، إِنَّ الْحَمْدَ ،
وَالنُّعْمَةَ ، لَكَ وَالْمُلْكَ ، لَا شَرِيكَ لَكَ

Labbayka-Allaahumma Labbayk. Labbayka laa shariyka Laka Labbayk. Innal-Hamda Wan-Ni'imata Laka wal-Mulk laa shariyka Lak.

"Nimekuitikia Ee Allaah nimekuitika, nimekuitika Huna mshirika nimekuitika, hakika Himdi na Neema na Ufalme ni Vyako Huna mshirika."

Mpaka tukafika katika Al-Ka'bah,[3] akagusa kona,[4] akakimbia mara tatu kuizunguka Nyumba,[5] akatembea mara nne kuizunguka Nyumba. Kisha akaja Maqaam Ibraahiym na kuswali pale. Kisha akarejea kwenye kona akaigusa tena. Kisha akatoka nje mlangoni akakaribia Asw-Swafaa, akasoma:

إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ

“Hakika Asw-Swafaa na Al-Marwaa ni katika alama za Allaah.” [Al-Baqarah (2: 158)] Akasema: “Nnaanza kile Alichianza nacho Allaah”. Kwa hivyo akapanda Swafaa mpaka akaiona Ka'bah, kisha akageukia Qiblah akatangaza Tawhiyd ya Allaah na Akamkabbir akasema:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ، وَلَهُ الْحَمْدُ، وَهُوَ
عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ أَنْجَزَ وَعْدَهُ،
وَنَصَرَ عَبْدَهُ، وَهَزَمَ الْأَحْزَابَ وَحْدَهُ

*Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu laa shariyika Lahu, Lahul-Mulku
Walahul-Hamdu wa Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr. Laa Ilaaha
Illa-Allaahu Wahdahu, Anjaza wa'dahu wa-Naswara 'Abdahu wa-
hazamal-ahzaaba Wahdahu*

“Hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, Hana mshirika, ni Wake Ufalme na Himdi ni Zake, Naye juu ya kila kitu ni Muweza. Hapana mwabudiwa wa haki Allaah, hali ya kuwa Peke Yake, Ametekeleza ahadi Yake, na Amemnusuru mja Wake, na Amevishinda vikosi peke Yake.”

Kisha akaomba du'aa baina yake peke yake kama hivyo mara tatu. Kisha akashuka hadi Al-Marwah. Alipoteremka hadi miguu yake ikakanyaga bonde alikimbia, hadi akapanda, alitembea hadi Al-Marwah. Kama alivyofanya Asw-Swafaa na msimuliaji akataja Hadiyth hivi: “Ilipofika Yawm At-Tarwiyah[6] wakaelekea Minaa, [7] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikwenda akaswali Adhuhuri, Alasiri, Magharibi, ‘Ishaa na Alfajiri. Kisha akakaa kidogo, hadi jua likachomoza, akaenda hadi ‘Arafah akakuta ameshajengewa hema Namirah.[8]

Akashuka, jua lilipopinduka, aliamurisha Al-Qasw-waa aletwe, na alipowekewa matandiko, alikwenda chini bondeni kuhutubia watu. Kisha kukaadhiniwa na kukimiwa, akaswali Swalaah ya Adhuhuri, kisha ikakimiwa na akaswali Alasiri, bila kuswali Swalaah nyingine yoyote baina yake.

Kisha akampanda ngamia wake, akaja mahala pa kisimamo, akauelekeza tumbo la ngamia wake Al-Qasw-waa kwenye mawe,[9] na akatengeneza njia ya wanaoenda kwa miguu. mbele yake. Alielekea Qiblah, akabaki hivyo mpaka jua likazama mwanga wa manjano ukatoweka kidogo, umbo mviringo la jua lilikuwa

limekwisha potea. Alianza kuenda haraka na kuvuta kwa nguvu hatamu ya Al-Qasw-waa huku akiashiria kwa mkono wake wa kuume kwa watu na kusema: “Nyamazeni kimya, nyamazeni kimya” Na kila alipopita pahala palipoinuka juu, alilegeza hatamu ili ngamia aweze kupanda.

Alipofika Al-Muzdalifah aliswali Magharibi na ‘Ishaa kwa Adhana moja tu na Iqaama mbili,[10] hakuleta tasbiyh baina yake.[11] Kisha akalala mpaka alfajiri akaswali Alfajiri kwa Adhana moja na Iqaama moja. Kisha akampanda ngamia wake hadi akafika Al-Mash’aral-Haraam.[12] Akaelekea Qiblah, akamuomba Allaah, akamtukuza na kumpwekesha, na akabakia kusimama hadi kukang’aa sana.

Kisha akaondoka haraka haraka, kabla ya jua halijachomoza, hadi akafika katika bonde la Muhassir.[13] Akaharakisha kidogo kisha akafuata barabara ya katikati[14] ambayo ilikuwa ikitokezea katika Jamrah[15] kubwa, akafika hadi Jamrah jirani na mti. Akatupa vijiwe saba huku akipiga Takbiyr kwa kila kijiwe anachokitupa. Na kila kijiwe kilikuwa kidogo kama kokwa ya tende. Akavitupa bondeni, kisha akaenda mahala pa kuchinja akachinja. Baada ya hivyo, Rasuli wa Allaah akampanda ngamia wake na kuondoka haraka haraka hadi kwenye Al-Ka’bah,[16] na akaswali Adhuhuri Makkah.” [Imetolewa na Muslim kupitia Hadiyth ndefu]

608.

وَعَنْ خُزَيْمَةَ بْنِ ثَابِتٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا فَرَغَ مِنْ تَلْبِيَّتِهِ فِي حَجٍّ أَوْ عُمْرَةٍ سَأَلَ اللَّهَ رِضْوَانَهُ وَالْجَنَّةَ وَاسْتَعَاذَ بِرَحْمَتِهِ مِنَ النَّارِ } رَوَاهُ الشَّافِعِيُّ
بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Khuzaymah bin Thaabit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kila alipomaliza

Talbiyah yake, katika Hijjah au katika ‘Umrah, alikuwa akimuomba Allaah Radhi Zake na Jannah, na aliomba kujilinda na moto kwa Rahmah Yake.”[17] [Imetolewa na Ash-Shaafi’iyy kwa Isnaad dhaifu ya wapokezi]

609.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {نَحَرْتُ هَاهُنَا، وَمِنِّي كُلُّهَا مَنَحَرٍّ، فَأَنْحَرُوا فِي رِحَالِكُمْ، وَوَقِفْتُ هَاهُنَا وَعَرَفْتُ كُلُّهَا مَوْقِفٌ، وَوَقِفْتُ هَاهُنَا وَجَمَعْتُ كُلُّهَا مَوْقِفٌ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Nimechinja hapa, na Minnaa yote ni machinjio, kwa hiyo chinja hapo unapoishi. Nimesimama hapa, na ‘Arafah yote ni mahala pa kusimama. Nimesimama hapa na Jam’ (Al-Muzdalifah) yote ni mahala pa kusimama.”[18] [Imetolewa na Muslim]

610.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا: {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَمَّا جَاءَ إِلَى مَكَّةَ دَخَلَهَا مِنْ أَعْلَاهَا، وَخَرَجَ مِنْ أَسْفَلِهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuja Makkah, aliingilia juu na akatokea chini.”[19] [Al-Bukhaariy, Muslim]

611.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: {أَنَّهُ كَانَ لَا يَقْدُمُ مَكَّةَ إِلَّا بَاتَ بِذِي طُوًى حَتَّى يُصْبِحَ وَيَغْتَسِلَ، وَيَذْكُرُ ذَلِكَ عِنْدَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Yeye (Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا)) Alikuwa haji Makkah bila kulala pale Dhiy Twuwaa[20] hadi alfajiri, na kisha alioga. Alikuwa akisema hivyo ndivyo alivyofanya Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

612.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: {أَنَّهُ كَانَ يُقْبَلُ الْحَجَرَ الْأَسْوَدَ وَيَسْجُدُ عَلَيْهِ} رَوَاهُ الْحَاكِمُ مَرْفُوعًا، وَابْنُ أَبِي مَوْقُوفًا

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Alikuwa akilibusu Hajar Al-Aswad (Jiwe Jeusi) na akisujudu juu yake.”[21] [Imetolewa na Al-Haakim kama ni Marfuw’, na Al-Bayhaqiyy kama Mawquwf]

613.

وَعَنْهُ قَالَ: أَمَرَهُمُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَنْ يَرْمُلُوا ثَلَاثَةَ أَشْوَاطٍ وَيَمْشُوا أَرْبَعًا، مَا بَيْنَ الرُّكْنَيْنِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaamrisha wakimbie mizunguko mitatu,[22] na watembe mizunguko minne,[23] kati ya nguzo mbili.”[24] [Al-Bukhaariy, Muslim]

614.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: "كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا طَافَ الطَّوَافَ الْأَوَّلَ خَبَّ ثَلَاثًا وَمَشَى أَرْبَعًا"

وَفِي رِوَايَةٍ: رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا طَافَ فِي الْحَجِّ وَالْعُمْرَةِ أَوَّلَ مَا يَقْدَمُ فَإِنَّهُ يَسْعَى ثَلَاثَةَ أَطْوَافٍ بِالْبَيْتِ ثُمَّ يَمْشِي أَرْبَعَةً مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Yeye alipokuwa akitufu Nyumba (Al-Ka’bah), alikuwa akikimbia mizunguko mitatu na akitembea mizunguko mine.”

Na katika Riwaayah nyingine inasema: “Nilimuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitufu katika Hijjah au ‘Umrah mara

alipowasili. Alikuwa akikimbia mizunguko mitatu na akawa anatembea mizunguko mine kuzunguka Nyumba.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

615.

وَعَنْهُ قَالَ: {لَمْ أَرِ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَسْتَلِمُ مِنَ الْبَيْتِ غَيْرَ الرُّكْنَيْنِ الْيَمَانِيِّينِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Sikuwahi kumuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akigusa kitu chochote katika Nyumba (Al-Ka’bah) ile isipokuwa zile nguzo za Yamani.” [Imetolewa na Muslim]

616.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ قَبَّلَ الْحَجَرَ الْأَسْوَدَ فَقَالَ: إِنِّي أَعْلَمُ أَنَّكَ حَجَرٌ لَا تَضُرُّ وَلَا تَنْفَعُ، وَلَوْلَا أَنِّي رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْبَلُكَ مَا قَبَّلْتُكَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Alibusu jiwe jeusi akasema: “Ninajua wewe ni jiwe hudhuru wala hunufaishi. Nisingemuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akikubusu, nisingekubusu.”[25] [Al-Bukhaariy, Muslim]

617.

وَعَنْ أَبِي الطُّفَيْلِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَطُوفُ بِالْبَيْتِ وَيَسْتَلِمُ الرُّكْنَ بِمِخْجَنٍ مَعَهُ، وَيُقَبِّلُ الْمِخْجَنَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Atw-Twufayl[26] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilimuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akizunguka Nyumba (Al-Ka’bah) huku anagusa kona kwa Mihjan[27] ambayo alikuwa nayo na kuibusu Mihjan.”[28] [Imetolewa na Muslim]

618.

وَعَنْ يَعْلَى بْنِ أُمَيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {طَافَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مُضْطَبِعًا بِبُرْدٍ أَخْضَرَ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Ya’laa bin Umayyah[29] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitufu akiwa amevaa joho la Kiyemeni rangi ya kijani chini ya kwapa yake ya kuume na ncha yake ikiwa juu ya bega lake la kushoto.”[30] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

619.

وَعَنْ أَنَسٍ - رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ يُهَلُّ - مِنَّا الْمُهَلُّ - فَلَا يُنْكَرُ عَلَيْهِ، وَيُكَبَّرُ مِنَّا الْمُكَبَّرُ فَلَا يُنْكَرُ عَلَيْهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Miongoni mwetu wapo waliopaza sauti katika Talbiyah bila kukatazwa, na miongoni mwetu wapo waliopiga Takbiyra bila kukatazwa.”[31] [Al-Bukhaariy, Muslim]

620.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {بَعَثَنِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الثَّقَلِ، أَوْ قَالَ فِي الضَّعْفَةِ مِنْ جَمْعِ بَلِيلٍ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alinituma (kuenda Minnaa) pamoja na wanawake na watoto, au amesema niende na watu dhaifu wa familia yake[32] kutoka Jam’ wakati wa usiku.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

621.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {إِسْتَأْذَنْتُ سَوْدَةَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَيْلَةَ الْمُزْدَلِفَةِ: أَنْ تَدْفَعَ قَبْلَهُ، وَكَانَتْ تَبِطُهُ تَعْنِي: ثَقِيلَةً فَأَذِنَ لَهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِمَا

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Sawdah[33] (صَلَّى) aliomba ruhusa kwa Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) ili atangulie usiku wa Muzdalifah, alikuwa mnene, kwa hivyo akaruhusiwa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

622.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ لَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَرْمُوا الْجَمْرَةَ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيُّ، وَفِيهِ انْقِطَاعٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Alituambia kuwa: “Msitupe vijiwe pale Jamrah hadi jua lichomoze.”[34] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy, na kuna kukatika]

623.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: { أَرْسَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِأُمِّ سَلَمَةَ لَيْلَةَ النَّحْرِ، فَرَمَتِ الْجَمْرَةَ قَبْلَ الْفَجْرِ، ثُمَّ مَضَتْ فَأَفَاضَتْ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَإِسْنَادُهُ عَلَى شَرْطِ مُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtanguliza Umm Salamah usiku kabla ya siku ya kuchinja, na akatupa vijiwe kule Jamrah kabla ya alfajiri. Kisha akaharakisha kuenda Makkah na akatufu.”[35] [Imetolewa na Abuu Daawuud na wapokezi wake wanakidhi masharti ya Muslim]

624.

وَعَنْ عُرْوَةَ بْنِ مُضَرَّسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ شَهِدَ صَلَاتِنَا هَذِهِ يَغْنِي: بِالْمُزْدَلِفَةِ فَوَقَفَ مَعَنَا حَتَّى نَدْفَعَ، وَقَدْ وَقَفَ بِعَرَفَةَ قَبْلَ ذَلِكَ لَيْلًا أَوْ نَهَارًا، فَقَدْ تَمَّ حَجُّهُ وَقُضِيَ تَفَثُهُ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Urwah bun Mudhwarris[36] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuhudhuria Swalaah yetu hapa Muzdalifah na anasimama nasi hadi tuondoke kuenda Minnaa, na akisimama ‘Arafah kabla mchana au usiku, basi Hijjah yake imekamilika,[37] na ametekeleza Tafathah (taratibu)[38] zake.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Khuzaymah]

625.

وَعَنْ- عُمَرَ رَضِيَ- اللهُ عَنْهُ قَالَ: {إِنَّ الْمُشْرِكِينَ كَانُوا لَا يُفِيضُونَ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ، وَيَقُولُونَ: أَشْرَقَ ثَبِيرٌ وَأَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خَالَفَهُمْ، ثُمَّ أَفَاضَ قَبْلَ أَنْ تَطْلُعَ الشَّمْسُ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) amesema: “Washirikina walikuwa hawarejei kutoka Muzdalifah hadi jua lichomoze na wanasema: Liache jua liangaze juu ya Thabiy.[39] Kwa hivyo Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitofautiana na hao washirikina kwa kurejea upesi kutoka Muzdalifah kabla jua kuchomoza.”[40] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

626.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ وَأُسَامَةَ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَا: {لَمْ يَزَلِ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُلَبِّي حَتَّى رَمَى جَمْرَةَ الْعَقَبَةِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas na Usaamah bin Zayd[41] (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) wamesema: “Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliendelea kupaza sauti yake katika Talbiyah hadi alipotupa vijiwe[42] katika Jamratal-‘Aqabah.”[43] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

627.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ جَعَلَ الْبَيْتَ عَنْ يَسَارِهِ، وَمِنْ يَمِينِهِ، وَرَمَى الْجَمْرَةَ بِسَبْعِ حَصِيَّاتٍ وَقَالَ: هَذَا مَقَامُ الَّذِي أَنْزَلَتْ عَلَيْهِ سُورَةُ الْبَقَرَةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mas-‘uud (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nyumba ikiwa kushoto na Minnaa kuume kwake, alitupa vijiwe saba katika Jamrah amesema: “Hiki ni kisimamo ambacho imeteremkia Suwrah Al-Baqarah.”[44] [Al-Bukhaariy, Muslim]

628.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {رَمَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْجَمْرَةَ يَوْمَ النَّحْرِ ضُحًى، وَأَمَّا بَعْدَ ذَلِكَ فَإِذَا زَادَتْ الشَّمْسُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitupa vijiwe katika Siku ya Kuchinja mchana kabla ya adhuhuri, na baada ya hapo akatupa wakati jua limepinduka.”[45] [Imetolewa na Muslim]

629.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {أَنَّهُ كَانَ يَرْمِي الْجَمْرَةَ الدُّنْيَا، بِسَبْعِ حَصِيَّاتٍ، يُكَبِّرُ عَلَى أَثَرِ كُلِّ حَصَاةٍ، ثُمَّ يَتَقَدَّمُ، ثُمَّ يُسْهَلُ، فَيَقُومُ فَيَسْتَقْبِلُ الْقِبْلَةَ، فَيَقُومُ طَوِيلًا، وَيَدْعُو وَيَرْفَعُ يَدَيْهِ، ثُمَّ يَرْمِي الْوُسْطَى، ثُمَّ يَأْخُذُ ذَاتَ الشَّمَالِ فَيُسْهَلُ،

وَيَقُومُ مُسْتَقْبِلَ الْقِبْلَةِ، ثُمَّ يَدْعُو فَيَرْفَعُ يَدَيْهِ وَيَقُومُ طَوِيلًا، ثُمَّ يَرْمِي جَمْرَةَ ذَاتِ الْعَقَبَةِ مِنْ بَطْنِ الْوَادِي وَلَا يَقِفُ عِنْدَهَا، ثُمَّ يَنْصَرِفُ، فَيَقُولُ: هَكَذَا رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَفْعَلُهُ { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Alikuwa akitupa vijiwe saba katika Jamrah ya karibu,[46] akipiga Takbiyra kila anapotupa. Kisha alikuwa anasogea mbele, anakuenda mpaka ndani ya bonde.[47] Na baada ya kusimama akiwa kaelekea Qiblah akiomba du’aa na kuinua mikono yake akasimama kwa muda mrefu, akitupa vijiwe katika Jamrah ya kati. Kisha aligeukia kushoto na kuenda ndani zaidi kwenye bonde na baada ya kusimama akielekea Qiblah akaomba du’aa na kusimama kwa muda mrefu, akatupa vijiwe katika Jamrah Al-‘Aqabah kutoka bondeni chini, lakini hakusimama karibu yake. Kisha aliondoka na kusema: “Hivi ndivyo nilivyomuona Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akifanya.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

630.

وَعَنْهُ ، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: " اَللّٰهُمَّ اَرْحَمِ الْمَخْلُقِيْنَ " قَالُوا: وَالْمُقَصِّرِيْنَ يَا رَسُولَ اللَّهِ. قَالَ فِي الثَّلَاثَةِ: " وَالْمُقَصِّرِيْنَ " { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:

اَللّٰهُمَّ اَرْحَمِ الْمَخْلُقِيْنَ

“Allaahumma Irham Al-Muhalliqiyna

(Ee Allaah warehemu ambao wamenyoya)

Watu wakapendekeza kuwa Na wale waliopunguza nywele zao[48]
Ee Rasuli wa Allaah! Kisha akasema katika mara ya tatu:

وَالْمُقَصِّرِينَ

“Na waliopunguza.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

631.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو بْنِ الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ
رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَقَفَ فِي حَجَّةِ الْوَدَاعِ،
فَجَعَلُوا يَسْأَلُونَهُ، فَقَالَ رَجُلٌ: لَمْ أَشْعُرْ، فَحَلَقْتُ قَبْلَ أَنْ أَذْبَحَ.
قَالَ: " اذْبَحْ وَلَا حَرَجَ " فَجَاءَ آخَرُ، فَقَالَ: لَمْ أَشْعُرْ، فَتَحَرْتُ
قَبْلَ أَنْ أَرْمِيَ، قَالَ: " اِرْمِ وَلَا حَرَجَ " فَمَا سُئِلَ يَوْمَئِذٍ عَنْ
شَيْءٍ قَدَّمَ وَلَا أَخَّرَ إِلَّا قَالَ: " اِفْعَلْ وَلَا حَرَجَ " { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr bun Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) amesema: “Rasuli wa Allaah (عَنْهُمَا
(وَسَلَّمَ) alisimama katika Hijja ya kuaga, wakawa watu wanamuuliza.
Mtu mmoja akasema: “Sikujua, nimenyoya nywele kabla sijachinja.”
Akasema: “Chinja tu kwani hakuna tatizo.” Mwingine akasema:
“Sikujua nimechinja mnyama kabla sijatupa vijiwe.” Akasema:
“Vitupe tu, kwani hakuna tatizo.” Hakuulizwa kitu chochote
ambacho kilifanywa kabla au baada ya wakati wake maalumu siku
ile bila kusema: “Fanya tu, kwani hakuna tatizo.”[49] [Al-Bukhaariy,
Muslim]

632.

وَعَنْ الْمِسْوَرِ بْنِ مَخْرَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَحَرَ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَ، وَأَمَرَ أَصْحَابَهُ بِذَلِكَ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Al-Miswar bin Makhramah[50] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Rasuli wa Allaah alichinja kabla ya kunyooa, na akaamuru Swahaba zake kufanya vivyo hivyo.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

633.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا رَمَيْتُمْ وَحَلَقْتُمْ فَقَدْ حَلَّ لَكُمْ الطَّيِّبُ وَكُلُّ شَيْءٍ إِلَّا النِّسَاءَ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkishatupa vijiwe na kunyooa, manukato ni halali na kila kitu kingine imeruhusiwa isipokuwa wanawake.”[51] [Imetolewa na Ahmad, na Abuu Daawuwd kwa Isnaad dhaifu]

634.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَيْسَ عَلَى النِّسَاءِ حَلْقٌ، وَإِنَّمَا يُقَصِّرْنَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kunyoa si wajibu kwa wanawake,[52] lakini wanapunguza (nywele zao).” [Imetolewa na Abuu Daawuud kwa Isnaad Hasan]

635.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: {أَنَّ الْعَبَّاسَ بْنَ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ اسْتَأْذَنَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يَبِيتَ بِمَكَّةَ لَيْلِي مَنْى، مِنْ أَجْلِ سِقَايَتِهِ، فَأَذِنَ لَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Abbaas bin ‘Abdul-Mutwalib aliomba ruhusa kutoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) abakie Makkah katika usiku ambao alitakiwa awe Minaa, kwa sababu ya wadhifa wake wa kugawia watu maji, naye akamruhusu.”[53] [Al-Bukhaariy, Muslim]

636.

وَعَنْ عَاصِمِ بْنِ عَدِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَرْخَصَ لِرُعَاةِ الْإِبِلِ فِي الْبَيْتُوتَةِ عَنْ مَنْى،

يَرْمُونَ يَوْمَ النَّحْرِ، ثُمَّ يَرْمُونَ الْغَدَ لِيَوْمَيْنِ، ثُمَّ يَرْمُونَ يَوْمَ
النَّفَرِ { رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Aaswim bin ‘Adiyy[54] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaruhusu
wachungaji wa ngamia wasibakie usiku kucha Minaa na kutupa
vijiwe katika Siku ya Kuchinja kisha watupe siku ya pili yake na
siku ya tatu yake pamoja, kisha watupe katika siku ya watu
kutawanyika kutoka Minaa.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-
Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na
akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

637.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {خَطَبَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ النَّحْرِ...} الْحَدِيثُ مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituhutubia Siku ya
Kuchinja.” Msimuliaji alisimulia sehemu ya Hadiyth iliyosalia. [Al-
Bukhaariy, Muslim]

638.

وَعَنْ سَرَّاءَ بِنْتِ نَبْهَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {خَطَبَنَا
رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ الرُّءُوسِ فَقَالَ: " أَلَيْسَ

هَذَا أَوْسَطُ أَيَّامِ التَّشْرِيقِ ؟ " { الْحَدِيثَ رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ
حَسَنٍ

Kutoka kwa Sarraa bint Nabhaan[55] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitupa mawaidha
baada ya siku ya kuchinja[56] akasema: “Hii si siku ya katikati ya
Siku za Tashriyq?” Msimulizi ameipokea sehemu ya Hadiyth
iliyobakia [Imetolewa na Abuu Daawuwd kwa Isnaad nzuri]

639.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
قَالَ لَهَا: {طَوَأُكَ بِالْبَيْتِ وَبَيْنَ الصَّفَا وَالْمَرْوَةِ يَكْفِيكَ لِحَجَّكَ
وَعُمْرَتِكَ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia: “Kuizunguka Nyumba
(kutufu) na kukimbia kati ya Asw-Swafaa na Al-Marwaa
kunatosheleza kwa Hijjah na ‘Umrah yako.”[57] [Imetolewa na
Muslim]

640.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ {لَمْ يَرْمُلْ فِي السَّبْعِ الَّذِي أَفَاضَ فِيهِ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ
إِلَّا التِّرْمِذِيَّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ.

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Hakukimbia katika kuzunguka Nyumba mara saba[58] aliporudi Makkah.” [Imetolewa na Al-Khamsah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Al-Haakim]

641.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ صَلَّى الظُّهْرَ وَالْعَصْرَ وَالْمَغْرِبَ وَالْعِشَاءَ، ثُمَّ رَقَدَ رَقْدَةً بِالْمُحَصَّبِ، ثُمَّ رَكِبَ إِلَى الْبَيْتِ فَطَافَ بِهِ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliswali Adhuhuri na Alasiri, Maghribi na ‘Ishaa, kisha akalala Al-Muhasw-swab.[59] Kisha akapanda ngamia wake hadi kwenye Al-Ka’bah na akafanya Twawaaf.”[60] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

642.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا: { أَنَّهَا لَمْ تَكُنْ تَفْعَلُ ذَلِكَ أَيَّ: النَّزُولِ بِالْأَبْطَحِ وَتَقُولُ: إِنَّمَا نَزَلَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِأَنَّهُ كَانَ مَنْزِلًا أَسْمَحَ لَخُرُوجِهِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Alikuwa hafanyi hivyo, yaani kushuka Al-Abtwah, amesema Rasuli wa Allaah

(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alishukia pale kwa sababu palikuwa ni mahala rahisi zaidi kuondokea yeye.”[61] [Imetolewa na Muslim]

643.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {أَمَرَ النَّاسُ أَنْ يَكُونَ آخِرَ عَهْدِهِمْ بِالْبَيْتِ، إِلَّا أَنَّهُ خَفَّفَ عَنِ الْحَائِضِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Watu waliamrisha wasiondoke bila kupita katika Nyumba (Al-Ka’bah) ili kutufu Twawaaf Al-Wadaa’i, isipokuwa imesamehewa kwa mwenye hedhi.”[62] [Al-Bukhaariy, Muslim]

644.

وَعَنْ ابْنِ الزُّبَيْرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {صَلَاةٌ فِي مَسْجِدِي هَذَا أَفْضَلُ مِنْ أَلْفِ صَلَاةٍ فِيَمَا سِوَاهُ إِلَّا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ، وَصَلَاةٌ فِي الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَفْضَلُ مِنْ صَلَاةٍ فِي مَسْجِدِي بِمِائَةِ صَلَاةٍ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn Az-Zubayr[63] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swalaah moja katika Msikiti wangu huu ni bora zaidi mara elfu kuliko Swalaah ya popote pengine isipokuwa Swalaah ya Al-Masjid

Al-Haraam (Msikiti Mtukufu wa Makkah). Na Swalaah moja katika Msikiti Mtukufu wa Makkah ni bora zaidi kuliko Swalaah katika Msikiti wangu huu kwa Swalaah mia moja.”[64] [Imetolewa na Ahmad, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

[1] Al-Qasw-waa ni jina la ngamia jike wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

[2] Al-Baydaa maana yake ni msitu au tambarare, na pia kulikuwa na kijiji kilichoitwa Baydaa. Kama ilivyotajwa hapo nyuma, Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alianza kusoma Talbiyah tokea Msikitini. Hii hapa inasema alianza kusoma kule Baydaa. Ukweli ni kwamba usemi wa kwanza ndio sahihi. Kwa kuwa msimuliaji alimuona Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisoma Talbiyah kule Baydaa, alidhani kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alianza kuisoma Talbiyah pale Baydaa, ambapo ukweli ni huo kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikwishaanza kuisoma tokea kabla hata ya kufika Baydaa.

[3] Nyumba hapa ina maana ya “Ka’bah”

[4] Katika lugha ya kiarabu, Rukn maana yake ni Al-Hajar Al-Aswad (Jiwe Jeusi), na Istalaam maana yake ni kulibusu au kuligusa.

[5] Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipofika Makkah pamoja na Maswahaba wake kutekeleza “Umratul-Qada”, Maqurayshi wakaanza kuwashutumu Waislamu kuwa wamekonda na wamedhoofu kuwa vile aina fulani ya homa iliwakumba walipokuwa Al-Madiynah. Baada ya kusikia shutuma hizi, Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaamrisha Maswahaba wake watembe vifua mbele wakiwa wamejaa heshima na majivuno, kama wanavyofanya wapiganaji mieleka, kuwaonyesha Maqurayshi kuwa wao siyo dhaifu. Tokea siku ile mpaka leo hii, hilo tendo la kutembea kwa namna hii katika mizunguko mitatu ya kwanza ya Twawaaf (Kuizunguka Ka’bah) limekuwa tendo la Sunnah.

[6] Yawm At-Tarwiyah ni siku ya nane ya mwezi wa Dhul-Hijjah.

[7] Maana au tafsiri ya neno la Kiarabu “Minaa” ni “kukata au kuangusha”. Kwa sababu mahala pale ndipo zilipokuwa zikimwagwa damu za wanyama wa kafara, paliitwa “Minaa”.

[8] Namirah ni jina la mahala karibu na ‘Arafah, penye Msikiti wenye jina hilo.

[9] Kwa kiarabu, Asw-Swakharah maana yake ni “Mawe”.

[10] Hadiyth hii inaashiria wazi kuwa, kila Swalaah mbili zinaposwaliwa pamoja (kisafari), huhitajika Adhana moja tu, lakini itahitaji kutamka Iqaama mbili tofauti tofauti, moja kwa kila Swalaah moja.

[11] Hadiyth hii pia inatufahamisha kuwa, kila Swalaah mbili zinaposwaliwa moja baada ya nyingine, hairuhusiwi kuswali Swalaah zozote za Sunnah kati yazo.

[12] Al-Mash’aral-Haraam ni eneo la wazi kati ya vilima viwili vya Muzdalifah.

[13] Bonde la Muhassir liko kati ya Al-Muzdalifah na Minaa

[14] Mahujaji huagizwa walivuke lile bonde kwa kasi na mapema sana, bila kujali amepanda kipando au anatembea kwa miguu. Kuna sababu mbili za hili: (a) Wale watu wa tembo waliteketezwa kwa nguvu za Ilaah mahali hapa, kwa hivyo mtu sharti apite pahala hapo kwa haraka na huku akilia machozi. (b) Wakati walipokuwa wakifanya Hijjah, wale washirikina waliokuwa wakiabudu asiyekuwa Allaah, wengi walikuwa wakikaa hapa, na Nabiyy (ﷺ) alitaka kutofautiana nao kwa hilo.

[15] Jamrah maana yake ni “Rundo la mawe”. Yapo majamrah matatu, na ni lazima yote yatupiwe vijiwe. Jamrah lililotajwa hapa ni Jamratul-‘Aqabah.

[16] Khuzaymah bin Thaabit ndiye Ibn Al-Fakiha Al-Khatami Al-Answaariy Al-Aws. Alipewa jina la utani la Abuu ‘Imrata. Alishuhudia Badri na vita vingine vilivyofuata. Ndiye aliyeshika bendera ya Khatama wakati wa kutekwa Makkah, na alishiriki katika vita vya Siffiyn pamoja na ‘Aliy na akauliwa huko.

[17] Hii ina maana mbili: (a) Ya kwanza ni kwamba, baada ya kutamka Labbayk kila mara, sharti mtu umuombe Allaah (سبحانه وتعالى) ridhaa Yake, na kuomba Jannah na Rahma Zake, (b) Pili, mtu sharti amuombe Allaah (سبحانه وتعالى) mwisho wa Talbiyah ambao huishia katika kutupa vijiwe vya Jamratul-‘Aqabah.

[18] Jam' ni jina jingine la Al-Muzdalifah. Uwanja wote wa 'Arafah ni pahala pa kukaa. Kuanzia adhuhuri ya tarehe 9 ya mwezi Dhul-Hijjah (Mfungo tatu) mpaka alfajiri ya tarehe 10 ya Dhul-Hijjah, ni lazima kila Haaji akae kwa muda fulani pale 'Arafah. Haaji atakayeukosa huu msingi mkuu mmojawapo wa Hijjah, atakuwa kaikosa Hijjah yote. Kwa maneno mengine, hakuna Hijjah ya bila kukaa 'Arafah.

[19] Jina la sehemu ya juu ya Makkah ni Ath-Thaaniyatul-Ulyaa, na jina la sehemu ya chini ni Ath-Thaaniyatus-Sufmaa.

[20] Dhiy Twuwaa ni pahala ambapo pako ndani ya mipaka ya ukanda mtukufu na iko karibu na jiji la Makkah.

[21] Kusujudu mbele ya Hajar Al-Aswad (Jiwe Jeusi) haimaanishi kuwa Nabiyy (ﷺ) alilisujudia Al-Hajar Al-Aswad lenyewe. Inaweza kuwa na maana mbili: (a) Ya kwanza ni kuwa alilibusu Al-Hajar Al-Aswad na akagusa paji la uso wake juu yake pia, ambayo hiyo inaashiria kuwa alikuwa akilibusu kikamilifu. (b) Ya pili, baada ya kukamilisha Twawaaf (kutufu au kuzunguka Ka'bah), Nabiyy (ﷺ) alikuwa akiswali Rakaa mbili za Swalaah ya Nafl (Sunnah) mbele ya Al-Hajar Al-Aswad.

[22] Neno linalotumika kwa lugha ya Kiarabu ni "Ashwaatw" ambao ni uwingi wa "Shawtw" na Shawtw moja ni mzunguko mmoja kamili kutufu Ka'bah.

[23] Kutembea mizunguko mine kuitufu Ka'bah

[24] Kona mbili ni Rukn Al-Yaman na Rukn Al-Hajar Al-Aswad

[25] 'Umar amesema hivyo kwa sababu Waarabu ndiyo kwanza walikuwa wameachana na kuabudu masanamu wengi, na katika zama za Jahiliya (kabla ya Uislamu) waliamini kuwa masanamu (ambayo yaliundwa kwa mawe) yalikuwa na nguvu na uwezo wa kuwapa faida wanaadamu. Kwa hivyo 'Umar amesema vile ili kupinga dhana ile ya kuzaliwa nayo ya Waarabu ili wasipotoke.

[26] Abuu Atw-Twufayl ndiye 'Aamir bin Wathila Al-Layth Al-Kinaan. Aliishi miaka minane ya mwisho ya uhai wa Nabiyy (ﷺ). Alifika Makkah mnamo mwaka wa 100 A.H. au 102 au mwaka wa 110 A.H., na alikuwa Swahaba wa mwisho kufariki dunia.

[27] Hii ni fimbo ya kutembelea yenye mshikio uliopinda.

[28] Hadiyth hii inatufahamisa kuwa endapo mtu anashindwa kulifikia Al-Hajar Al-Aswad (Jiwe Jeusi) kwa sababu ya watu wanaolizunguka ni wengi mno, basi inaruhusiwa kuligusa jiwe lile kwa fimbo kisha akaibusu hiyo fimbo. Lakini kwa zama hizi hata hivo haiwezekani kutokana na zahma kubwa mno. Hivyo inatosheleza mtu anapofikia mstari wa Al-Hajar Al-Aswad aashirie tu mkono wake akiwa mbali na kusema: Allaahu Akbar bila ya kubusu mkono, kwani kubusu mkono kila unapofikia hapo ni bid'ah.

[29] Ya'laa bin Umayyah ndiye Abuu Safwaan At-Tamimi Al-Makki, rafiki wa Maqurayshi na Swahaba aliyesilimu wakati wa kutekwa Makkah. Alishuhudia vita vya Hunayn, Twaaf na Tabuwk; na alimtumikia Abuu Bakar na 'Umar, na 'Uthmaan. Aliishi hadi kufikia miaka ya hamsini ya Al-Hijrah.

[30] Hadiyth hii inadhihirisha desturi ya Nabiyy (ﷺ) kuvaa shuka. Nabiyy (ﷺ) alichukua shuka kutoka chini ya kwapa yake ya kuume na akaiweka juu ya bega lake la kushoto. Alifanya hivyo ili kuonyesha afya yake nzuri na nguvu zake. Tendo hilo linafanana na lile tendo la kukimbia wakati akitufu kuzunguka Ka'bah. Haya hayakutakikana baada ya ushindi wa Uislam; lakini tendo la Nabiyy (ﷺ) likawa Sunnah milele.

[31] Mtu huruhusiwa kutamka Takbiyra, lakini ni bora kutamka Talbiyah.

[32] Kisheria, Haaji sharti akeshe usiku mzima pale Muzdalifah: Akae Al-Mash'aral-Haraam baada ya kuswali Swalaah ya Alfajiri, kisha ndipo aendelee kutokea pale. Lakini imeruhusiwa kwa watu dhaifu, wazee, wagonjwa na wanawake kuondoka kutoka Muzdalifah baada ya kukaa pale Muzdalifah kwa sehemu kubwa ya usiku, ili wapate kuwahi kufika Minaa na wakamilishe kitendo kingine cha lazima cha kutupa vijiwe, kabla watu wote hawajafika kule kwani kunajaa watu wengi mno.

[33] Sawdah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) ni Ummul-Mu-uminiyn (Mama wa Waumini) ndiye Sawdah bint Zam'a bin 'Abd-Shams Al-Qurayshiyah Al-Aamiriya. Alisilimu kule Makkah mapema na kuhamia Uhabeshi na mume wake alifika kule. Kisha Nabiyy (ﷺ) alimuoa huko Makkah, baada ya kifo cha Khadija na kabla ya kumchumbia 'Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا). Alifariki mwaka 55 A.H.

[34] Kwa ujumla, watu hawaruhusiwi kutupa vijiwe kule Jamaraat kabla ya jua kuchomoza, lakini watu wenye vilema wanaruhusiwa kutupa.

[35] Hii ni Twawaaf Al-Ifaadhwah.

[36] Ni ‘Urwah bun Mudhwaris bin Aws bin Haarith bin Lam Atta’I aliyekuwa Swahaba aliyeshuhudia Hijjatul-Wadaa na aliloweza Kufa. Ndiye ameipokea Hadiyath hii.

[37] Sehemu muhimu ya Hijjah ambayo ndiyo kule kusimama pale ‘Arafah.

[38] Neno Tafathah maana yake ni taka au uchafu. Hapa neno hilo lina maana hiyo hiyo, kwani watu huenda kunyoa nywele na kuoga taka zote baada ya kukamilisha Hijjah. Huko kujitakasa kunaashiria mwisho wa Hijjah, kila anayetokeleza taratibu zote hizi, Hijjah yake inakuwa imetimilika.

[39] Thabiyr ni moja ya milima mirefu sana Makkah ulioko upande wa kushoto wa barabara iendayo Minaa.

[40] Hilo tendo la kurejea kutoka Muzdalifah kabla ya jua kuchomoza huhesabika kuwa ni Mashruw’ (ni haki kishariy’ah).

[41] Usaamah bin Zayd ndiye Abuu Muhammad au Abuu Zayd Usaamah bin Zayd bin Haarith bin Sharaahil Al-Kalbiy, aliyekuwa kipenzi cha Nabiyy (ﷺ), mtumwa wake aliyemuacha huru na pia ni mtoto wa mtumwa wake aliyemuacha huru. Mama yake alikuwa ni Umm Ayman aliyemlea Nabiyy (ﷺ). Siku chache kabla hajafa, Nabiyy (ﷺ) alimteua aongoze jeshi walimokuwemo Abuu Bakar na ‘Umar, wakati akiwa na umri wa miaka 18 tu. Hata hivyo jeshi lile halikuwahi kupelekwa kwa sababu ya kifo cha Nabiyy (ﷺ), na baadae Abuu Bakr alilipeleka. Usaamah alikufa baada ya kifo cha ‘Uthmaan, mwaka wa 54 H.

[42] Haaji sharti atamke Talbiyah hadi akishatupa vijiwe vya kwanza katika Jamratul-‘Aqabah. Kule kutupa vijiwe vya kwanza ndiko kunaashiria mwisho wa Talbiyah, kwa mujibu wa maoni ya Wanazuoni wengi.

[43] Jamratal-‘Aqabah ndiyo mahala pakubwa pale Minaa ambapo mahujaji hutupa vijiwe kwanza siku ya kuchinja, tarehe 10 ya mwezi wa Dhul-Hijjah.

[44] Nabiyy (ﷺ) alitaja Aayah katika Suwratul-Baqarah kwa sababu Aayah zake nyingi zinatoa maamrisho na makatazo kuhusu Hajj.

[45] Haaji ni sharti akamilishe kutupa vijiwe kabla ya kupinduka jua katika siku ya 'Iyd, ajizuie kutupa vijiwe saa sita mchana. Baada ya jua kupinduka, Ibaada hii inaweza kutekelezwa.

[46] Neno la kiarabu la Ad-Dunyaa linaweza kutafsiriwa kuwa ni “karibu”. Kwa kuwa hio iko karibu na Msikiti wa Khaaif inaitwa Jamratad-dunyaa, lakini pia inaitwa Jamratul-Uwlaa.

[47] Hapa neno la kiarabu Sahl linatumika kwa kipande cha ardhi laini. Hii ina maana kuwa, Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), akitaka kutupa vijiwe katika Jamaraat, hakusimama pale bali alijitokeza nje waziwazi, akasimama pale na kisha akaomba du'aa kwa Allaah (عَزَّ وَجَلَّ).

[48] Ni muhimu kukata nywele baada ya kutekeleza Hijjah au 'Umrah. Kunyoa nywele zote na hata kupunguza zenyewe kunaruhusiwa. Hata mtu ambaye hana nywele kichwani anatakiwa apitishe kijembe kichwa kizima.

[49] Wanaohiji wana mambo manne muhimu katika siku ya 'Iyd: (a) Kurusha vijiwe katika Jamrah (Al-'Aqabah) (b) Kuchinja mnyama, (c) Kunyoa nywele za kichwa, (d) Kutufu Ka'bah. Mpangilio wa kuvitekeleza vitendo hivi vinne ni kama ulivyoonyeshwa hapa, kwa mujibu wa Shariy'ah za Kiislam. Kutimiza mpangilio huu ni Sunnah. Hakuna madhara ikiwa mpangilio huu hautozingatiwa kwa sababu ya kutojua. Lakini iwapo mtu anafanya hivyo kwa makusudi, itakuwa dhambi ingawa haina adhabu.

[50] Al-Miswar bin Makhramah ni Mzuhri na Mquraysh. Alikuwa miongoni mwa watu waadilifu sana. Alihamia Makkah baada ya kuuliwa kwa 'Uthmaan. Alipigwa kwa silaha akafa wakati akiswali wakati Yaziyd bin Mu'aawiyah aliizingira Makkah mnamo mwaka wa 64 A.H.

[51] Hii inaweka wazi kuwa, baada ya kutupa vijiwe katika Jamrah Al-'Aqabah na kunyoa nywele za kichwa, inahusiana kila kitu isipokuwa kujamiiana. Hiyo huruhusiwa baada ya Twawaaf Al-Ifaadhwah tu.

[52] Hii inatufahamisha kuwa wanawake hawana haja ya kunyoa nywele zote, bali lazima wapunguze kidogo nywele zao za chini.

[53] Ni Waajib (lazima) kwa Hujaji kuwapo Minaa usiku ule. Endapo Haaji hawezi kuwepo Minaa usiku mzima, basi awepo angalau kwa sehemu kubwa ya usiku.

[54] 'Aaswim bin 'Adiyy ndiye mwenye jina la utani la Abuu 'Ubaydillaah au Abuu 'Amr, na alikuwa rafiki wa Banu 'Amr bin 'Awf wa Answaar. Alishuhudia vita vya Badri na vita vilivyofuata. Alikuwa ndiye kamanda wa makabila ya Al-'Aaliyah wakati wa vita vya Badr, kwa hivyo

Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimpa sehemu moja ya ngawira. Alikufa mnamo mwaka wa 45 A.H. Pia inasemekana alikufa shahidi katika vita vya Al-Yamaamah akiwa katika umri wa miaka 120.

[55] Huyu ndiye Sarraa bint Nabhaan Al-Ghanawiyyah, ambaye ni Swahaba, naye Rabiyy'a bin Abiy 'Abdir-Rahmaan ameipokea Hadiyth hii kutoka kwake.

[56] Hii ni Yawm Ar-Ru-uws (siku ya Vichwa) ni jina la siku ifuatiayo siku ya 'Iyd

[57] Hadiyth hii inatuarifu, kuifanya Twawaaf moja na Sa'y moja kunatosha kwa zote mbili yaani 'Umrah na Hijjah kwa Haaji anayefanya Hijjah ya Qiraan. Kinyume cha hivi kwa Haaji anayefanya Hijja Tamattu' ni sharti afanye Twawaaf mbili na Sa'y mbili kila moja mbalimbali.

[58] Kwa hivyo tunafahamishwa kwamba hakuna Ramal (kukimbia) katika Twawaaf Al-Ifaadhwah wala Twawaaf Al-Wadaa'i. Ramal hufanywa katika Twawaaf Al-Quduwm tu. Na Twawaaf Al-Quduwm ni ile ambayo hufanywa mara baada ya kuingia Makkah mara ya kwanza. Sharti kuzingatia pia kuwa Ramal (kukimbia) hufanywa na wanaume tu. Endapo Haaji ameshindwa kuifanya katika Twawaaf Al-Quduwm ni sharti aifanye wakati anaifanya Twawaaf Al-Ifaadhwah.

[59] Al-Muhasw-swab ni eneo la wazi kati ya milima miwili iliyo jirani zaidi na Minaa kuliko Makkah. Pia huitwa Abtah, Batha na Khaif Banuw Kinaanah.

[60] Hii ni Twawaaf Al-Wadaa'i (ya kuaga) inayofanywa wakati wa kuondoka Makkah.

[61] Pa kuondokea kuenda Al-Madiynah

[62] Hii ni Twawaaf Al-Wadaa'i (Kuiaga Ka'bah kwa kutufu mara ya mwisho), ambayo ni Waajib (ni lazima) kwa Hujaji kwa mujibu wa Maimaam isipokuwa Imaam Maalik. Hivyo wanawake wenye hedhi wanasamehewa. Mtu yeyote anayeikosa hiyo huwajibika kufanya kafara ya mnyama.

[63] Ibn Az-Zubayr ndiye Abuu Bakr 'Abdillaah bin Az-Zubayr bin Al-'Awwaam Al-Qurayshiy Al-Asad. Mama yake Asmaa bint Abiy Bakr aliamia Al-Madiynah wakati yu mjamzito na akamzaa kule Qubaa, kwa hivyo akawa mtoto wa kwanza kuzaliwa baada ya Hijrah. Alikuwa akifunga Swawm na kuswali sana. Alikuwa mtu mheshimiwa ambaye hakukubali kudhulumiwa, na alikuwa mpiganaji mkali. Alikuwa mbuji, na alikuwa anakubali haki, na alikuwa hodari wa kuwaangalia warithi wake.

Aliapishwa kupokea Ukhalifa baada ya kufa Yaziyd bin Mu'aawiyah mnamo mwaka wa 64 A.H. Kwa hivyo aliziteka Al-Hijaaaz, 'Iraaq zile mbili, Yaman, Misri na sehemu kubwa ya Shaam. Al-Hajjaaj bin Yuwsuf Ath-Thaqafi alimzingira Makkah, na alikufa shahidi na kusulubiwa mnamo mwezi wa Jumaada Al-Ukhraa mnamo mwaka wa 73 A.H.

[64] Imeripotiwa katika Twabaraan kuwa, Swalaah inayoswaliwa katika Msikiti wa Al-Aqswaa (Baytul-Maqdis) huzawadiwa mara 500 (mia tano), na Swalaah inayoswaliwa katika Msikiti wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) (Al-Madiynah) hulipwa mara 1,000 (elfu moja), ambapo Swalaah inayoswaliwa katika Masjid Al-Haraam (Nyumba ya Allaah pale Makkah) hulipwa mara 100,000 (elfu mia moja).

06- Mlango Wa Kukosa Hijjah Na Kuzuilika

بَابُ الْفَوَاتِ وَالْإِخْصَارِ

06-Mlango Wa Kukosa Hijjah Na Kuzuilika

645.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {قَدْ أُخْصِرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَحَلَقَ وَجَامَعَ نِسَاءَهُ، وَنَحَرَ هَذْيَهُ، حَتَّى اِغْتَمَرَ عَامًا قَابِلًا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alizuiliwa.[1] Kwa hivyo akanyoa kichwa chake, akajamiiana na wake zake, na akachinja

wanyama wake. Kisha akafanya ‘Umrah mwaka uliofuata.”
[Imetolewa na Al-Bukhaariy]

646.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {دَخَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى ضُبَاعَةَ بِنْتِ الزُّبَيْرِ بْنِ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي أُرِيدُ الْحَجَّ، وَأَنَا شَاكِيَةٌ، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "حُجِّي وَاشْتَرِطِي: أَنْ مَحَلِّي حَيْثُ حَبَسْتَنِي" {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى) aliingia kwa Dhawubaa’ah[2] bint Az-Zubayr bin ‘Abdil-Mutwalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) na akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Nimeidhamiria kuhiji lakini ninaumwa.” Nabiy (صَلَّى) akasema: “Hiji, lakini omba na uweke sharti kuwa: Mahala nitakapovulia Ihraam ndipo Wewe (Allaah) Utakuwa Umenizuia.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

647.

وَعَنْ عِكْرِمَةَ، عَنْ الْحَجَّاجِ بْنِ عَمْرٍو الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ كُسِرَ، أَوْ عُرِجَ، فَقَدْ حَلَّ وَعَلَيْهِ الْحَجُّ مِنْ قَابِلٍ قَالَ عِكْرِمَةُ. فَسَأَلْتُ

إِبْنُ عَبَّاسٍ وَأَبَا هُرَيْرَةَ عَنْ ذَلِكَ؟ فَقَالَا: صَدَقَ { رَوَاهُ
الْخَمْسَةُ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa ‘Ikrimah[3] amesema kuwa Al-Hajjaaj bin ‘Amr Al-Answaariyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuvunjika mguu au kulemaa, lazima atoke katika hali ya Ihraam na lazima ateleze Hijjah mwaka unaofuata.” ‘Ikrimah amesema: “Nilimuuliza Ibn ‘Abbaas na Abuu Hurayrah juu ya hilo nao walisema: “Amesema kweli.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na At-Tirmidhiy aliipa daraja la Hassan]

[1] Ni mambo gani yanayoweza kuhesabika kuwa kikwazo au kipingamizi katika kufanya Hijjah? Wanazuoni wengi zaidi wana maoni kwamba, chochote kinachoingilia kati Hijjah ya Haaji (mwenye kuhiji) ni kikwazo, iwe ni adui, ugonjwa, vita au kushindwa kusafiri. Wengine wanasema kuwa Ihswaar (kipingamizi) husababishwa na adui tu ambaye kafiri. Kuna kutofautiana miongoni mwa Wanazuoni kuhusu kafara itolewayo na mahujaji wanaopingamizwa kama hao. Wengi wanasema Haaji aliye namna hiyo sharti achinje mnyama wa kafara mahala pale pale anapovulia Ihraam yake, kama mahala hapo pako ndani au nje ya eneo la kuchinja wanyama wa kafara.

[2] Dhawubaa’ah bint Az-Zubayr bin ‘Abdil-Mutwalib alikuwa akiitwa Umm Hakiym Dhawubaa’ah bint Az-Zubayr bin ‘Abdil-Mutwalib bin Haashim bin ‘Abdil-Manaaf, binti wa mjomba wa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Aliolewa na Al-Miqdaad bin Al-Aswad aliyemzalila ‘Abdullaah na Karimah. Alikufa wakati wa Ukhalifa wa ‘Aliy

[3] ‘Ikrimah muachwa huru wa ‘Abdullaah bin ‘Abbaas asili yake ni mberiberi (watu wa Morocco) ni Mwanachuoni wa Tafsiyr ya Qur-aan. Alifariki mwaka wa 107 A.H.

كِتَابُ الْبُيُوعِ

Kitabu Cha Miamala Ya Biashara

07-Kitabu Cha Miamala Ya Biashara - كِتَابُ الْبُيُوعِ

01-Kitabu Cha Biashara: Mlango Masharti Yake Na Yaliokatazwa

بَابُ شُرُوطِهِ وَمَا نُهِيَ عَنْهُ مِنْهُ

01-Mlango Masharti Yake Na Yaliokatazwa

648.

عَنْ رِفَاعَةَ بْنِ رَافِعٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ سُئِلَ: أَيُّ الْكَسْبِ أَطْيَبُ؟ قَالَ: {عَمَلُ الرَّجُلِ
بِيَدِهِ، وَكُلُّ بَيْعٍ مَبْرُورٍ} رَوَاهُ الْبَزَّازُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Rifaa'ah bin Raafi' (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa: Kazi gani bora zaidi?[1] Akasema: “Ni kazi ya mtu kwa mkono wake, na kila biashara halali.” [Imetolewa na Al-Bazaar na akaisahihisha Al-Haakim]

649.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ عَامَ الْفَتْحِ، وَهُوَ بِمَكَّةَ: {إِنَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ حَرَّمَ بَيْعَ الْخَمْرِ، وَالْمَيْتَةِ، وَالْخَنزِيرِ، وَالْأَصْنَامِ. فَقِيلَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَرَأَيْتَ شُحُومَ الْمَيْتَةِ، فَإِنَّهُ تُطْلَى بِهَا السُّفُنُ، وَتُدْهَنُ بِهَا الْجُلُودُ، وَيَسْتَصْبَحُ بِهَا النَّاسُ؟ فَقَالَ: " لَا هُوَ حَرَامٌ "، ثُمَّ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عِنْدَ ذَلِكَ: " قَاتِلِ اللَّهَ الْيَهُودَ، إِنَّ اللَّهَ لَمَّا حَرَّمَ عَلَيْهِمْ شُحُومَهَا جَمَلُوهُ، ثُمَّ بَاعُوهُ، فَأَكَلُوا ثَمَنَهُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa alimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema mwaka wa Fat-hi (Ukombozi wa Makkah) akiwa Makkah: “Hakika Allaah Ameharamisha kuuza (au kununua) pombe, mfu, nguruwe na masanamu.” Akaulizwa Ee Rasuli wa Allaah! Waonaje shahamu ya mfu, kwani majahazi hupakiwa nayo ngozi, hupakwa kwayo na watu wanajiangazia kwayo (wanatia kwenye taa zao). Akasema: “Laa hiyo ni haramu.” Kisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Allaah Awalaani mayahudi. Kwa hakika Allaah Alipowaharamishia shahamu ya mfu, wao

waliiyeyusha wakawa wanaiuza; wakala thamani yake.”[2] [Al-Bukhaariy, Muslim]

650.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {إِذَا اخْتَلَفَ الْمُتَبَايعَانِ لَيْسَ بَيْنَهُمَا بَيِّنَةٌ، فَالْقَوْلُ مَا يَقُولُ رَبُّ السِّلْعَةِ أَوْ يَتَّارَكَانِ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Wawili wenye kuuziana watakapokhitilafiana na hakuna baina yao ubainifu, basi kauli itakayosikilizwa ni ya mwenye bidhaa, au wote wawili waache (biashara hiyo).” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Al-Haakim]

651.

وَعَنْ أَبِي مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ ثَمَنِ الْكَلْبِ، وَمَهْرِ الْبَغِيِّ، وَحُلُوانِ الْكَاهِنِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza

thamani ya mbwa,[3] mahari ya kahaba[4] na bahashishi ya kahini[5] (mpiga ramli).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

652.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّهُ كَانَ يَسِيرُ عَلَى جَمَلٍ لَهُ أَعْيَا. فَأَرَادَ أَنْ يُسَيِّبَهُ. قَالَ: فَلَحِقَنِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَدَعَا لِي، وَضَرَبَهُ، فَسَارَ سَيْرًا لَمْ يَسِرْ مِثْلَهُ، قَالَ: "بِعْنِيهِ بِوُقِيَّةٍ" قُلْتُ: لَا. ثُمَّ قَالَ: "بِعْنِيهِ" فَبِعْتُهُ بِوُقِيَّةٍ، وَاشْتَرَطْتُ حُمْلَانَهُ إِلَى أَهْلِي، فَلَمَّا بَلَغْتُ أَتَيْتُهُ بِالْجَمَلِ، فَنَقَذَنِي ثَمَنَهُ، ثُمَّ رَجَعْتُ فَأَرْسَلْتُ فِي أَثَرِي. فَقَالَ: "أَثَرَانِي مَا كَسْتُكَ لِأَخْذِ جَمَلِكَ؟ خُذْ جَمَلَكَ وَدَرَاهِمَكَ. فَهُوَ لَكَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَهَذَا السِّيَاقُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: Alikuwa juu ya ngamia wake aliyechoka, akataka amuache aende anapotaka. Akasema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaniombea na akampiga (yule ngamia), akaenda mwendo ambao hajawahi kuenda mfano wake. Kisha akasema: Niuzie kwa wakia moja.[6] Nikamuambia: Hapana. Halafu akaniambia: Niuzie. Nikamuuzia kwa wakia moja. Nikashurutisha kunibeba kwake hadi kwa watu wangu (Madiynah). Nilipofika nilimpelekea ngamia. Akalipa thamani yake. Kisha nikarejea. Akatuma mtu nyuma yangu akasema: Wadhani kuwa nimekutaradhilia unipunguzie thamani ili nichukue ngamia wako?[7] Chukua ngamia wako na dirham zako ni milki yako.” [Al-Bukhaariy, Muslim na haya ni maneno ya Muslim]

653.

وَعَنْهُ قَالَ: {أَعْتَقَ رَجُلٌ مِنَّا عَبْدًا لَهُ عَنْ دُبُرٍ لَمْ يَكُنْ لَهُ مَالٌ غَيْرُهُ. فَدَعَا بِهِ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَبَاعَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena: “Mtu miongoni mwenu alitangaza kumuacha huru mtumwa wake baada ya kifo chake, alikuwa hana mali isipokuwa mtumwa huyo. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuita na akamuuzia[8] (na thamani yake akampa mwenyewe).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

654.

وَعَنْ مَيْمُونَةَ زَوْجِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، وَرَضِيَ عَنْهَا {أَنَّ فَارَةً وَقَعَتْ فِي سَمْنٍ، فَمَاتَتْ فِيهِ، فَسُئِلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْهَا. فَقَالَ: " أَلْقُوهَا وَمَا حَوْلَهَا، وَكُلُّوه " } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَزَادَ أَحْمَدُ. وَالنَّسَائِيُّ: {فِي سَمْنٍ جَامِدٍ}

Kutoka kwa Maymuwnah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) mke wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Panya aliingia katika samli akafa humo. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akaulizwa kuhusu panya yule, akasema: Mtupeni na kilicho kando yake na mle (samli hiyo).” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Ahmad na An-Nasaaiy wameongeza: “katika samli iliyoganda”

655.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { إِذَا وَقَعَتُ الْفَأْرَةُ فِي السَّمَنِ، فَإِنْ كَانَ جَامِدًا فَالْقُوْهَا وَمَا حَوْلَهَا، وَإِنْ كَانَ مَائِعًا فَلَا تَقْرُبُوْهُ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَقَدْ حَكَّمَ عَلَيْهِ الْبُخَارِيُّ وَأَبُو حَاتِمٍ بِالْوَهْمِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Panya atakapoingia katika samli, ikiwa imeganda basi mtupeni na kilichomo kando yake, na ikiwa ni maji maji msiikaribie.” [Imetolewa na Ahmad, na Abuu Daawuwd, Al-Bukhaariy na Abuu Haatim wamesema ina shaka]

656.

وَعَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ قَالَ: سَأَلْتُ جَابِرًا عَنْ ثَمَنِ السَّنَّوْرِ وَالْكَلْبِ ؟ فَقَالَ: { زَجَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ ذَلِكَ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ .
وَالنَّسَائِيُّ وَزَادَ: { إِلَّا كَلْبَ صَيْدٍ }

Kutoka kwa Abuu Az-Zubayr[9] amesema kuwa Nilimuuliza Jaabir kuhusu thamani ya paka na mbwa,[10] akasema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza jambo hilo.” [Imetolewa na Muslim]

Na An-Nasaaiy akazidisha: “Isipokuwa mbwa wa kuwinda.”

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {جَاءَتْنِي بِرِيرَةُ، فَقَالَتْ: كَاتَبْتُ أَهْلِي عَلَى تِسْعِ أَوَاقٍ، فِي كُلِّ عَامٍ أَوْقِيَّةً، فَأَعِينَنِي. فَقُلْتُ: إِنَّ أَحَبَّ أَهْلِكَ أَنْ أَعُدَّهَا لَهُمْ وَيَكُونُوا وَلَوْ كُلي فَعَلْتُ، فَذَهَبْتُ بِرِيرَةَ إِلَى أَهْلِهَا. فَقَالَتْ لَهُمْ، فَأَبَوْا عَلَيْهَا، فَجَاءَتْ مِنْ عِنْدِهِمْ، وَرَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ جَالِسٌ. فَقَالَتْ: إِنِّي قَدْ عَرَضْتُ ذَلِكَ عَلَيْهِمْ فَأَبَوْا إِلَّا أَنْ يَكُونَ الْوَلَاءُ لَهُمْ، فَسَمِعَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَأَخْبَرَتْ عَائِشَةُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. فَقَالَ: خُذِيهَا وَاشْتَرِطِي لَهُمُ الْوَلَاءَ، فَإِنَّمَا الْوَلَاءُ لِمَنْ أَعْتَقَ فَفَعَلْتُ عَائِشَةُ، ثُمَّ قَامَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي النَّاسِ خَطِيبًا، فَحَمِدَ اللَّهُ وَأَثْنَى عَلَيْهِ. ثُمَّ قَالَ: "أَمَّا بَعْدُ، مَا بَالُ رِجَالٍ يَشْتَرِطُونَ شُرُوطًا لَيْسَتْ فِي كِتَابِ اللَّهِ مَا كَانَ مِنْ شَرْطٍ لَيْسَ فِي كِتَابِ اللَّهِ فَهُوَ بَاطِلٌ، وَإِنْ كَانَ مِائَةَ شَرْطٍ، قَضَاءُ اللَّهِ أَحَقُّ، وَشَرْطُ اللَّهِ أَوْثَقُ، وَإِنَّمَا الْوَلَاءُ لِمَنْ أَعْتَقَ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ .

وَعِنْدَ مُسْلِمٍ فَقَالَ: {إِشْتَرِيهَا وَأَعْتِقِيهَا وَاشْتَرِطِي لَهُمُ الْوَلَاءَ}

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Bariyrah[11] (mjakazi) alinijia akasema: Nimeandikiana[12] (kuniacha huru) na mabwana zangu kwa wakia tisa; kila mwaka wakia moja; basi nisaidie. Nikamuambia: Mabwana zako wakipenda niwahesabie (hizo) na walaa[13] wako uwe kwangu nitafanya. Bariyrah

akawaendea mabwana wake akawaeleza, wakamkatalia. Akaja kutoka kwako na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameketi. Akasema: nimewaambia jambo hilo wakakataa[14] isipokuwa walaa uwe kwao. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasikia. ‘Aaishah (رَضِيَ اللهُ عَنْهَا) akasema nikamueleza Nabiy (رَضِيَ اللهُ عَنْهَا). Akamuambia ‘Aaishah (رَضِيَ اللهُ عَنْهَا): Mchukue na uwashurutishe walaa, kwani walaa ni wa mwenye kuacha huru.[15] ‘Aaishah (رَضِيَ اللهُ عَنْهَا) akafanya hivyo kisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasimama katika watu Akamhimidi Allaah na Akamsifu kisha akasema: Ammaa ba’d: wana nini watu wanashurutisha masharti yasiyokuwemo katika Kitabu cha Allaah! Sharti isiyokuwemo katika Kitabu cha Allaah ni batili, hata kama ni masharti mia. Hukumu ya Allaah ina nguvu na mno, na walaa ni wa mwenye kuacha huru.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim amesema: “Mnunue umuache huru na uwashururutishie walaa.”

658.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: {نَهَى عُمَرُ عَنْ بَيْعِ أُمَّهَاتِ الْأَوْلَادِ فَقَالَ: لَا تُبَاعُ، وَلَا تُوَهَّبُ، وَلَا تُورَثُ، لَيْسَتْ مَتَاعٌ بِهَا مَا بَدَأَ لَهُ، فَإِذَا مَاتَ فِيهِ حُرَّةٌ} رَوَاهُ مَالِكٌ، وَابْنُ هَشِيمٍ، وَقَالَ: رَفَعَهُ بَعْضُ الرُّوَاةِ، فَوَهَمَ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا) amesema: “Umar amekataza kuuza mama wa watoto,[16] akasema: hawauzwi wala hawatolewi hiba, wala hawarithiwi, atastarehe naye anavyotaka,

atakapokufa (bwana) mwanamke huyo ni huru.” [Imetolewa na Maalik na Al-Bayhaqiyy]

659.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كُنَّا نَبِيعُ سَرَارِينَا، أُمَّهَاتِ الْأَوْلَادِ، وَالنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ حَيًّا، لَا نَرَى بِذَلِكَ بَأْسًا} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَهَ وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulikuwa tukiuzia vijakazi wetu mama wa watoto, na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) yuko hai, haoni ubaya kwa hilo.” [Imetolewa na An-Nasaaiy, Ibn Maajah na Ad-Daaraqutwniy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

660.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ بَيْعِ فَضْلِ الْمَاءِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَزَادَ فِي رِوَايَةٍ: {وَعَنْ بَيْعِ ضِرَابِ الْجَمَلِ}

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza ziada ya maji.” [17] [Imetolewa na Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine akaongeza: “Na kuuza mapigo ya ngamia.”[18]

661.

وَعَنِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ عَسَبِ الْفَحْلِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza mapigo ya ngamia.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

662.

وَعَنْهُ، {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ بَيْعِ حَبْلِ الْحَبْلَةِ، وَكَانَ بَيْعًا يَتَّبَاعُهُ أَهْلُ الْجَاهِلِيَّةِ: كَانَ الرَّجُلُ يَبْتَاعُ الْجَزُورَ إِلَى أَنْ تُنْتَجَ النَّاقَةُ، ثُمَّ تُنْتَجُ الَّتِي فِي بَطْنِهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza mimba ya wenye mimba (Habalil-habalah),[19] na (hiyo) ilikuwa ni biashara wanayouziana watu wa jahiliya. Mtu alikuwa ananunua ngamia mpaka azaliwe ngamia koo kisha kizaliwe kilichomo tumboni mwake.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

663.

وَعَنْهُ، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ
بَيْعِ الْوَلَاءِ، وَعَنْ هَبْتِهِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema tena kuwa:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza
walaa[20] na kuutoa hiba.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

664.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { نَهَى رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ بَيْعِ الْحَصَاةِ، وَعَنْ بَيْعِ
الْغَرَرِ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza biashara ya
kurusha kijiwe na biashara ya udanganyifu.”[21] [Imetolewa na
Muslim]

665.

وَعَنْهُ: أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { مَنْ
اشْتَرَى طَعَاماً فَلَا يَبِيعُهُ حَتَّى يَكْتَالَهُ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kununua chakula, asikiuze mpaka akipime.” [Imetolewa na Muslim]

666.

وَعَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ بَيْعَتَيْنِ فِي بَيْعَةٍ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ
وَلِأَبِي دَاوُدَ: {مَنْ بَاعَ بَيْعَتَيْنِ فِي بَيْعَةٍ فَلَهُ أَوْكُسُهُمَا، أَوْ الرِّبَا}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema tena: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza mauzo mawili katika uzo moja.”[22] [Imetolewa na Ahmad na An-Nasaa'iy na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

Na katika Riwaayah ya Abuu Daawuud inasema: “Yeyote mwenye kuuza mauzo mawili katika uzo moja, basi ima atapata kilicho kichache kati ya viwili au riba.”[23]

667.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يَحِلُّ سَلَفٌ وَبَيْعٌ وَلَا شَرْطَانِ فِي بَيْعٍ، وَلَا رِبْحٌ مَالٌ يُضْمَنُ، وَلَا بَيْعٌ مَالٍ لَيْسَ عِنْدَكَ } رَوَاهُ الْخُمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَالْحَاكِمُ

وَأَخْرَجَهُ فِي "عُلُومِ الْحَدِيثِ" مِنْ رِوَايَةِ أَبِي حَنِيفَةَ، عَنْ عَمْرِو الْمَذْكُورِ بِلَفْظٍ: "نَهَى عَنْ بَيْعٍ وَشَرْطٍ" وَمِنْ هَذَا الْوَجْهِ أَخْرَجَهُ الطَّبْرَانِيُّ فِي "الْأَوْسَطِ" وَهُوَ غَرِيبٌ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb amepokea kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halali kujumuisha mkopo na mauzo,[24] wala masharti mawili katika uzo moja,[25] wala faida katika mali asiyodhamini, wala kuuza kitu usichokimiliki.”[26] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Khuzaymah na Al-Haakim]

Al-Haakim ameitaja katika ‘Uluwmul-Hadiyth’ kutoka kwa Abuu Haniyfah naye kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kwa tamko: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza biashara (iliyochanganywa) iliyokokotezwa kwa sharti.” Atw-Twabaraaniyy ameitaja katika mnyororo wa wapokezi hawa katika Al-Awsatw, na ni Hadiyth ghariyb (iliyotajwa na mpokezi mmoja tu).

وَعَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ بَيْعِ الْعُرْبَانِ} رَوَاهُ مَالِكٌ، قَالَ: بَلَّغْنِي عَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، بِهِ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kutoka kwa baba yake na babu yake amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) amekataza biashara ya ‘Urbaan.”[27] [Imetolewa na Maalik ambaye amesema: Imenifikia (akitaja mnyororo wa wapokezi wake) kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb]

669.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {ابْتِغْتُ زَيْتًا فِي السُّوقِ، فَلَمَّا اسْتَوْجَبْتُهُ لِقَيْنِي رَجُلٌ فَأَعْطَانِي بِهِ رِبْحًا حَسَنًا، فَأَرَدْتُ أَنْ أَضْرِبَ عَلَى يَدِ الرَّجُلِ، فَأَخَذَ رَجُلٌ مِنْ خَلْفِي بِذِرَاعِي، فَالْتَفَتُّ، فَإِذَا هُوَ زَيْدُ بْنُ ثَابِتٍ، فَقَالَ: لَا تَبِعْهُ حَيْثُ ابْتِغْتَهُ حَتَّى تَحُوزَهُ إِلَى رَحْلِكَ؛ فَإِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى أَنْ تُبَاعَ السَّلْعُ حَيْثُ تُبْتَاعُ، حَتَّى يَحُوزَهَا التَّجَارُ إِلَى رِحَالِهِمْ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nilinunua mafuta sokoni, nilipokabidhiwa alikuja mtu (hapo hapo) akanipa faida nzuri, nami nikataka kumuuzia, mara mtu mmoja akanishika kwa nyuma yangu, nilipogeuka alikuwa Zayd bin Thaabit, akasema: Usiuze mahala uliponunua hadi uchukue mahali pako, kwani hakika

Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amakataza bidhaa kuuzwa mahali inaponunuliwa mpaka wafanya biashara wazipeleke maeneo yao (wazikabidhi).”[28] [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud, matni ya Hadiyth ni yake. Na wakaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

670.

وَعَنْهُ قَالَ: {قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي أَبِيعُ بِالْبَقِيعِ، فَأَبِيعُ بِالْذَّنَانِيرِ وَأَخُذُ الدَّرَاهِمَ، وَأَبِيعُ بِالْذَّرَاهِمِ وَأَخُذُ الذَّنَانِيرَ، أَخُذُ هَذَا مِنْ هَذِهِ وَأُعْطِي هَذِهِ مِنْ هَذَا؟ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: لَا بَأْسَ أَنْ تَأْخُذَهَا بِسِعْرِ يَوْمِهَا مَا لَمْ تَتَفَرَّقَا وَبَيْنَكُمَا شَيْءٌ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nilisema: Ee Rasuli wa Allaah! Mimi ninauza ngamia Baqiy’ nikiuza kwa dinari na nikichukua dirham, na nikiuza kwa dirham na nikichukua dinari, nachukua dirhamu badala ya dinari. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Si vibaya kuchukua kwa bei ya siku ile[29] madamu hamujaachana na baina yenu kitu kipo.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Al-Haakim]

671.

وَعَنْهُ قَالَ: {نَهَى صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنِ النَّجْشِ}
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kupandishana bei katika biashara.”[30] [Al-Bukhaariy, Muslim]

672.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنِ الْمُحَاقَلَةِ، وَالْمُزَابَنَةِ، وَالْمُخَابَرَةِ، وَعَنِ التُّنْيَا، إِلَّا أَنْ تُعْلَمَ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا ابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza Muhaaqalah,[31] Muzaabanah,[32] Mukhaabarah[33] na Ath-Thunyaa ila itakapojulikana.”[34] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ahmad) isipokuwa Ibn Maajah, na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

673.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنِ الْمُحَاقَلَةِ، وَالْمُخَاضَرَةِ، وَالْمُلَامَسَةِ، وَالْمُنَابَذَةِ، وَالْمُزَابَنَةِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza Muhaaqalah, Mukhaadhwarah,[35] Mulaamasah,[36] Munaabadhah[37] na Muzaabanah.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

674.

وَعَنْ طَاوُسٍ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا تَلْقُوا الرُّكْبَانَ، وَلَا يَبِيعُ حَاضِرٌ لِبَادٍ } . قُلْتُ لِبْنِ عَبَّاسٍ: مَا قَوْلُهُ: " وَلَا يَبِيعُ حَاضِرٌ لِبَادٍ ؟ " قَالَ: لَا يَكُونُ لَهُ سِمْسَارًا { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Twaawus[38] kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msiwapokee wasafiri, wala mkazi wa mjini asiuze kwa niaba ya mtu wa mashambani.[39] Nikamuambia ‘Abdullaah bin ‘Abbaas: Nini makusudio ya kauli yake “Wala mkazi wa mjini asiuze kwa niaba ya mtu wa mashambani?” Akasema: Asiwe dalali wake.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

675.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا تَلْقُوا الْجَلَبَ، فَمَنْ تُلِقِيَ فَاشْتَرِي مِنْهُ، فَإِذَا أَتَى سَيِّدَهُ السُّوقَ فَهُوَ بِالْخِيَارِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msiwapokee wasafiri, atakayepokezwa bidhaa ikanunuliwa kwake, basi atakapokuja mwenyewe sokoni ana khiyari (ya kutoivunja biashara).” [Imetolewa na Muslim]

676.

وَعَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ يَبِيعَ حَاضِرٌ لِبَادٍ، وَلَا تَنَاجَشُوا، وَلَا يَبِيعُ الرَّجُلُ عَلَى بَيْعِ أَخِيهِ، وَلَا يَخْطُبُ عَلَى خُطْبَةِ أَخِيهِ، وَلَا تُسَالُ الْمَرْأَةُ طَلَاقَ أُخْتِهَا لِتَكْفَأَ مَا فِي إِنْائِهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَلِلْمُسْلِمِ: {لَا يَسُمُّ الْمُسْلِمُ عَلَى سَوْمِ الْمُسْلِمِ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza mkazi wa mjini kumuuzia kwa niaba mtu wa kijijini, wala msipandishiane bei, [40] wala mtu asiuze juu ya biashara ya nduguye, wala asipose juu ya posa ya nduguye (Muislam), wala mwanamke asiombe dada yake kupewa talaka ili afaidike kwa kuachwa kwake.”[41] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Wala Muislam asinunue juu ya biashara ya Muislam (mwenzake).”[42]

677.

وَعَنْ أَبِي أَيُّوبَ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {مَنْ فَرَّقَ بَيْنَ وَالِدَةٍ وَوَلَدِهَا، فَرَّقَ اللَّهُ بَيْنَهُ وَبَيْنَ أَحِبَّتِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالْحَاكِمُ، وَلَكِنْ فِي إِسْنَادِهِ مَقَالٌ وَلَهُ شَاهِدٌ

Kutoka kwa Abuu Ayyuwb Al-Answaariy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Mwenye kufarikisha baina ya mama na mtoto wake, Allaah Atafarikisha baina yake na vipenzi vyake Siku ya Qiyaamah.” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Al-Haakim

678.

وَعَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَمَرَنِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ أَبِيعَ غُلَامَيْنِ أَخَوَيْنِ، فَبِعْتُهُمَا، فَفَرَّقْتُ بَيْنَهُمَا، فَذَكَرْتُ ذَلِكَ لِلنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: أَدْرِكُهُمَا، فَارْتَجِعْهُمَا، وَلَا تَبِعْهُمَا إِلَّا جَمِيعًا} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَرَجَّالُهُ ثِقَاتٌ، وَقَدْ صَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ، وَالطَّبْرَانِيُّ، وَابْنُ الْقَطَّانِ

Kutoka kwa ‘Aliy bin Abiy Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliniamrisha kuwauza vijana wawili ndugu nikawauza kwa kuwatenga. Kisha

nikamuelezea Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) jambo hilo. Akaniambia: watafute uwarudishe,[43] wala usiwauze isipokuwa pamoja.” [Imetolewa na Ahmad. Wapokezi wake ni madhubuti. Na wakaisahihisha Ibn Khuzaymah, Ibn Al-Jaarud, Ibn Hibbaan, Al-Haakim, Atw-Twabaraani na Ibn Al-Qatwaan]

679.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { غَلَا السَّعْرُ بِالْمَدِينَةِ عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ النَّاسُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! غَلَا السَّعْرُ، فَسَعَّرْ لَنَا، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمُسَعِّرُ، الْقَابِضُ، الْبَاسِطُ، الرَّازِقُ، وَإِنِّي لَأَرْجُو أَنْ أَلْقَى اللَّهَ تَعَالَى، وَلَيْسَ أَحَدٌ مِنْكُمْ يَطْلُبُنِي بِمَظْلَمَةٍ فِي دَمٍ وَلَا مَالٍ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Bei zilipanda Madiynah katika zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) watu wakamuambia: Ee Rasuli wa Allaah! Bei zimepanda, tupange bei. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Kwa hakika Allaah Ndiye Mwenye kuwafikia (Mpanga bei), Mwenye kudhikisha, Mwenye Kukunjua, Mwenye Kuruzuku,[44] mimi nataraji kukutana na Allaah na hali hakuna miongoni mwenu mwenye kunidai kwa kudhulumiwa damu wala mali.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

680.

وَعَنْ مَعْمَرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا يَحْتَكِرُ إِلَّا خَاطِيٌّ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Ma'mar bin 'Abdillaah[45] amepokea kutoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuwa amesema: “Halimbikizi ila mkosaji.”[46] [Imetolewa na Muslim]

681.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا تَصُرُّوا الْأِبِلَّ وَالْغَنَمَ، فَمَنْ ابْتَاعَهَا بَعْدُ فَإِنَّهُ بِخَيْرِ النَّظَرَيْنِ بَعْدَ أَنْ يَحْلُبَهَا، إِنْ شَاءَ أَمْسَكَهَا، وَإِنْ شَاءَ رَدَّهَا وَصَاعًا مِنْ تَمْرٍ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِمُسْلِمٍ: { فَهُوَ بِالْخِيَارِ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ }

وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ، عَلَّقَهَا الْبُخَارِيُّ: { رَدَّ مَعَهَا صَاعًا مِنْ طَعَامٍ، لَا سَمْرَاءَ }

قَالَ الْبُخَارِيُّ: وَالتَّمْرُ أَكْثَرُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msivimbishe

chuchu za ngamia na mbuzi (kuonesha yamejaa), na mwenye kumnunua baada ya hapo basi ana khiyari kuchagua moja kati ya mambo mawili, baada ya kumkama; akitaka atabaki nae na akitaka atamrudisha pamoja na pishi ya tende.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “...naye yuko katika khiari kwa muda wa siku tatu.[47] (Ambapo ataamua kuyaweka au hapana).” [48]

Na katika Riwaayah yake nyingine ambayo Bukhaariy ameifanya ni Mu’allaq imesema: “...na atarudisha pamoja na pishi ya chakula isiyokuwa kawahia.”

Bukhaariy amesema katika Riwaayah: “Iliyotaja tende ndio iliyopokewa na wapokezi wengi.”

682.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مَنْ اشْتَرَى شَاةَ مَحْفَلَةٍ، فَرَدَّهَا، فَلْيُرَدَّ مَعَهَا صَاعًا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ .
وَزَادَ الْإِسْمَاعِيلِيُّ: {مِنْ تَمْرٍ}

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mwenye kununua mnyama aliyevimbishwa chuchu na akamrudisha, basi atakapomrudisha amrudishe pamoja na pishi.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na Al-Ismaa’iliyy ameongezea: “...ya tende.”

683.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ مَرَّ عَلَى صُبْرَةِ طَعَامٍ، فَأَدْخَلَ يَدَهُ فِيهَا، فَنَالَتْ أَصَابِعُهُ بَلَلًا ، فَقَالَ: " مَا هَذَا يَا صَاحِبَ الطَّعَامِ ؟ " قَالَ: أَصَابَتْهُ السَّمَاءُ يَا رَسُولَ اللَّهِ. فَقَالَ: أَفَلَا جَعَلْتَهُ فَوْقَ الطَّعَامِ؛ كَيْ يَرَاهُ النَّاسُ ؟ مَنْ غَشَّ فَلَيْسَ مِنِّي } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipita katika lundo la chakula (nafaka), akaingiza mkono wake ndani, vidole vyake vikagusa unyevu. Akasema: Ee mwenye chakula, ni nini hii? Akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Kimepatwa na manyunyu, akamuambia: Si ungekiweka juu ya chakula ili watu wakione! Mwenye kughushi si katika mimi.”[49] [Imetolewa na Muslim]

684.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ بُرَيْدَةَ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { مَنْ حَبَسَ الْعِنَبَ أَيَّامَ الْقَطَافِ، حَتَّى يَبِيعَهُ مِمَّنْ يَتَّخِذُهُ خَمْرًا، فَقَدْ تَقَحَّمَ النَّارَ عَلَى بَصِيرَةٍ } رَوَاهُ الطَّبْرَانِيُّ فِي " الْأَوْسَطِ " بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Buraydah amepokea kutoka kwa baba yake kuwa amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuhifadhi zabibu msimu wa kuchuma (zabibu) ili amuuzie mtengeneza pombe, kwa hakika atakuwa amejiingiza motoni kwa ujuzi.”[50] [Imetolewa na Atw-

Twabaraaniyy katika kitabu chake cha ‘Al-Awsatw’ kwa Isnaad Hasan]

685.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْخَرَجُ بِالضَّمَانِ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَضَعَّفَهُ الْبُخَارِيُّ، وَأَبُو دَاوُدَ وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ، وَابْنُ الْقَطَّانِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kodi ni kwa dhamana.”[51] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na wameidhoofisha Al-Bukhaariy na Abuu Daawuwd, na wakaisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Khuzaymah, Ibn Al-Jaarud, Ibn Hibbaan, Al-Haakim na Ibn Al-Qatwaan]

686.

وَعَنْ عُرْوَةَ الْبَارِقِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَعْطَاهُ دِينَارًا يَشْتَرِي بِهِ أَضْحِيَّةً، أَوْ شَاةً، فَاشْتَرَى شَاتَيْنِ، فَبَاعَ إِحْدَاهُمَا بِدِينَارٍ، فَأَتَاهُ بِشَاةٍ وَدِينَارٍ، فَدَعَا لَهُ بِالْبَرَكَةِ فِي بَيْعِهِ، فَكَانَ لَوْ اشْتَرَى ثُرَابًا لَرَبِحَ فِيهِ { رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا النَّسَائِيُّ

وَقَدْ أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ ضِمْنَ حَدِيثٍ، وَلَمْ يَسُقْ لَفْظَهُ
وَأُورِدَ التِّرْمِذِيُّ لَهُ شَاهِدًا: مِنْ حَدِيثِ حَكِيمِ بْنِ حِزَامٍ

Kutoka kwa ‘Urwah Al-Baariqiyy[52] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimpa dinari (moja) ili anunulie Udhwhiyyah[53] au mbuzi. Akanunua mbuzi wawili kwa dinari hiyo, mbuzi mmoja akamuuza kwa dinari moja, akaenda kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiwa na mbuzi na dinari. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akambariki katika biashara yake (‘Urwah)[54] akawa lau angenunua mchanga basi angepata faida.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy]

Bukhaariy ameileza katika jumla ya Hadiyth nyingine wala hakuitaja tamshi lake.

At-Tirmidhiy ametaja ushahidi wake kutoka katika Hadiyth ya Hakiym bin Hizaam.

687.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ شِرَاءِ مَا فِي بُطُونِ الْأَنْعَامِ حَتَّى تَضَعَ، وَعَنْ بَيْعِ مَا فِي ضُرُوعِهَا، وَعَنْ شِرَاءِ الْعَبْدِ وَهُوَ أَبْقَى، وَعَنْ شِرَاءِ الْمَغَانِمِ حَتَّى تُقَسَمَ، وَعَنْ شِرَاءِ الصَّدَقَاتِ حَتَّى تُقَبَضَ، وَعَنْ ضَرْبَةِ الْغَائِصِ } رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ، وَالْبَزَّازُ، وَالْأَرَقَطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kununua vilivyomo matumboni mwa wanyama mpaka wazae, na amekataza kuuza vilivyomo katika chuchu za wanyama,[55] na kununua mtumwa aliyetoroka, na kununua ghanima mpaka zigawanywe, na kununua Swadaqah mpaka zikadhibiwe, na amekataza kubahatisha mpiga mbizi.”[56] [Imetolewa na Ibn Maajah, Al-Bazzaar na Ad-Daaraqutwniyy kwa Isnaad dhaifu]

688.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا تَشْتَرُوا السَّمَكَ فِي الْمَاءِ; فَإِنَّهُ غَرَرٌ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَشَارَ إِلَى أَنَّ الصَّوَابَ وَقَفُّهُ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msinunue samaki akiwemo majini, kwani ni udanganyifu.” [Imetolewa na Ahmad na ameashiria kuwa Hadiyth hii ni Mawquwf (yaani ni maneno ya Swahaba, yaani Ibn Mas-‘uwd)]

689.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ تُبَاعَ ثَمَرَةٌ حَتَّى تُطْعَمَ، وَلَا يُبَاعَ

صُوفٌ عَلَى ظَهْرٍ، وَلَا لَبَنٌ فِي ضَرْعٍ { رَوَاهُ الطَّبْرَانِيُّ فِي
" الْأَوْسَطِ " وَالْدَّارَقُطْنِيُّ

وَأَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ فِي " الْمَرَاسِيلِ " لِعِكْرِمَةَ، وَهُوَ الرَّاجِحُ.
وَأَخْرَجَهُ أَيْضاً مَوْقُوفاً عَلَى ابْنِ عَبَّاسٍ بِإِسْنَادٍ قَوِيٍّ، وَرَجَّحَهُ
الْبَيْهَقِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza matunda
mpaka yaive, wala manyoya kuuzwa juu ya mgongo, wala maziwa
katika chuchu.”[57] [Imetolewa na Atw-Twabaraaniyy katika kitabu
chake Al-Awsatw na Ad-Daaraqutwniy]

Na Abuu Daawuwd katika Al-Maraasiyl kutoka kwa Ikrimah nayo ni
yenye nguvu.

Vile vile amepokea ikiwa Mawquwf Ibn ‘Abbaas ikiwa na sanadi
yenye nguvu na akaipa nguvu Al-Bayhaqiyy.

690.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ بَيْعِ الْمَضَامِينِ، وَالْمَلَأَقِيحِ { رَوَاهُ
الْبَزَّازُ، وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza mimba
katika matumbo ya ngamia,[58] na manii katika migongo ya

ngamia.”[59] [Imetolewa na Al-Bazaar na katika Isnaad yake kuna udhaifu]

691.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ أَقَالَ مُسْلِمًا بَيْعَتَهُ، أَقَالَهُ اللَّهُ عَثْرَتَهُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَهَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kukubali kurudishiwa kile alichomuuzia Muislamu,[60] Allaah atamsamehe dhambi zake.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

[1] Ni kazi gani au chumo gani lililo bora zaidi? Wanazuoni wametofautiana katika hili. Imaam An-Nawawiy amesema: Sawa ni kuwa chumo bora na inayokuwa kwa kazi ya mkono, japokuwa kilimo ni chumo bora kwa kukusanya kazi ya mkono na kutawakali na ndani yake kuna manufaa ya jumla ya wana Adam, wanyama na ndege. Haafidh bin Hajar amesema: Zaidi ya hivyo ni yanayo chumwa kutokana na mali za makafiri kwenye jihadi, na hilo chumo la Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na hilo ni chumo tukufu zaidi la machumo yote, kwa kuwa ndani yake kuna kuinua neno la Allaah.” Imesemwa Hii inaingia katika chumo la mkono.

[2] Ina maana ya kufanya biashara katika pombe, wanyama wafu, najisi ya maiti na nguruwe, sanamu ni haramu. Hadiyith hii imeweka wazi kuwa faida inayotokana na kitu kilicho haramu ni haramu vile vile, kubadilika kwa namna yake hakuihalalishi kama vile Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alivyohukumu kuhusu faida inayotokana na mafuta.

[3] Kulingana na maoni ya Wanazuoni takriban wote ni kuwa biashara ya mbwa ni haramu.

[4] Mapato yanayotokana na kahaba ni haramu kulingana na maoni ya Wanazuoni wote.

[5] Hul-waan al-kaahin: Wanazuoni wamekubaliana uharamu wa kumpa kahini, na kahini ni ambaye anadai elimu ya ghaibu na kuwaeleza watu yatakayotokea ni haramu. Hali kadhaalika kuimba na kucheza kwa malipo ya kikahini ni haramu.

[6] Wakia mmoja ni sawa na Dirhaam arubaini.

[7] Yaani labda unadhani kuwa nimenunua ngamia wako kwa thamani ndogo.

[8] Hii ina maana ya kumuuzwa mtumwa Mudabbar ni jambo lililoruhusiwa. Mtumwa Mudabbar, mwanamme au mwanamke ni yule anayeambiwa na anayemiliki: “Utakuwa huru baada ya kufa kwangu.”

[9] Jina lake ni Muhammad bin Muslim Tadrus Al-Asadi Al-Makki, muach ahuru wa Hakiym bin Hizaam. Alikuwa ni Taabi’ thiqah aliyekubaliwa na Wanazuoni wa Hadiyth.

[10] Kuuza na kununua paka ni jambo lisiloruhusiwa kishariy’ah. Hivyo hivyo hakuna tofauti kati ya mbwa wa kawaida kuhusu biashara yake kuwa haramu. Hata hivyo mtazamo unakuwa tofauti kuhusu mbwa wa kuwinda, ambapo baadhi ya Wanazuoni wanajuzisha.

[11] Ni mjakazi aliyeachwa huru na ‘Aaishah. Ni Swahaba aliishi hadi katika utawala wa Yaziyd. Aliolewa na Mughiyth, mtumwa katika familia ya Abuu Ahmad bin Jahsh. Alipoachwa huru Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimpa uchaguzi na akachagua kumuacha mume wake ambae alikuwa mtumwa bado na hivyo akawa ameachika.

[12] Kitaabah au Mukaatabah una maana ya mkataba ulioandikwa wa kumuacha huru mtumwa wa kike au wa kiume kwa mkabala wa malipo. Malipo haya yanaweza kupendekezwa kufanyika katika moja ya pande mbili. Kwa mfano mwenye kumiliki mtumwa akadai malipo mkabala na kumuacha huru mtumwa wake na mtumwa akaaridhi malipo mkabala na uhuru wake.

[13] Walaa: mtumwa aliyeachwa huru. Anapokufa, atarithiwa na yule aliyemuacha huru.

[14] Baada ya kifo cha mtumwa Mukattab (mwanamme au mwanamke) mali aliyoacha huitwa Walaa. Ikitokea mtu akalipa hela ya mkataba na kumuacha huru Mukattab (mtumwa mwanamme au mwanamke) katika hali ya kifo cha mtumwa, yule atakayelipa fedha basi atarithi; lakini ikiwa

hela ya mkataba ililipwa na mtumwa mwenyewe mali yake inakwenda kwa jamaa zake.

[15] Ina maana kumuacha huru Mukattab (mtumwa aliyeandika mkataba) kwa gharama fulani inaruhusiwa.

[16] Makusudio ya Ummul-Walad (Mama mtoto) ni mjakazi anaeingiliwa na bwana wake kwa ujakazi na akapata mtoto kwa bwana wake huyo. Mtoto huyo awe ni mume au mke. Ummul-walad (Mama mtoto) atakuwa huru baada ya kufariki bwana wake, wala hastahiki kuuzwa wala kutolewa zawadi wala kurithiwa.

[17] Kuzuia au kuuza maji ya ziada ambayo mtu hana matumizi yake ni jambo lisilokubaliwa kishariy'ah; vyovyote itakavyokuwa asili ya maji yale ni kisima au chemchem, katika ardhi anayoimiliki au katika ardhi ya mtu mwingine. Hata hivyo, maji yaliyohifadhiwa kwa matumizi binafsi yanaweza kuuzwa ni jambo linaloruhusiwa.

[18] Mapigo ya ngamia ni kumchukua ngamia dume na kumkodisha kwa mtu mwenye ngamia jike ili ampande.

[19] Kulikuwa na aina mbili za biashara hii. Aina ya mfano wa kwanza ni kununua kizazi cha mnyama ambaye bado hajazaliwa, nayo hufanyika kwa kulipa malipo kabla. Aina ya pili ni kumuuzwa mnyama kwa sharti la kuchukua mtoto atakayezaliwa. Aina zote za biashara hizi zilikatazwa kwa sababu ya mikataba yake kutokuwa wazi.

[20] Al-Walaa: mtumwa aliyeachwa huru akifa na kama hana wa kumrithi basi atarithiwa na yule aliyemuacha huru. Hadiyth imeweka wazi kuwa Al-Walaa ni kama uzawa wa mtu. Ikiwa kizazi cha mtu hakiwezi kuuzwa au mtu kupewa hiba, basi hivyo hivyo kuuza Walaa au kutoka kama zawadi ni jambo lililokatazwa.

[21] Biashara ya kurusha kijiwe ziko aina nyingi ikiwemo mmoja kumuambia mwengine: “Rusha kijiwe hiki, kitakapoangukia katika nguo yoyote itakuwa ni yako”, kwa kiasi kilichopangwa kabla. Biashara hii ni ya udanganyifu na ni biashara ya kubahatisha, kama vile kuuza njiwa akiwa hewani anaruka au kuuza samaki aliye baharini au kumuuzwa mtumwa aliyepotea au mnyama. Hizi ni aina za biashara zilizokuwa zama za ujahiliya.

[22] Katika sampuli hii ya biashara muuzaji anapanga bei mbili katika uzo moja. Uzo moja kwa malipo taslimu na lingine kwa mkopo. Bei ya mkopo linakuwa juu zaidi, fedha iliyozidi katika bei ya mkopo ni riba ambayo ni haramu.

[23] Baadhi ya Wanazuoni wa Hadiyth hawakubaliani na mapokezi haya ya mwisho ambayo Muhammad bin ‘Amr akiwa mmoja wa wapokezi. Hata hivyo imewekwa katika Hadiyth Hasan na wengine Swahiyh. Angalia ‘Irwaa Al-Ghaliyl, Shaykh Al-Albani 5/149-150.

[24] Biashara hii ina sampuli mbili: aina ya kwanza ni kama mtu anayeuzua farasi kwa riyali mia moja kwa mkopo kwa sharti kuwa mnunuzi atalipa muda fulani. Ikiwa mnunuzi atashindwa kulipa deni lile kwa muda uliopangwa basi muuzaji atamnunua farasi yule kwa shilingi mia na hamsini na kumuacha mnunuzi akidaiwa shilingi mia na hamsini. Hii ni haramu. Sampuli ya pili ni mfano wa nyumba yenye thamani ya shilingi milioni kumi na mbili, huuzwa kwa mtu kwa milioni kumi kwa sharti kuwa mnunuzi atamuazima muuzaji shilingi milioni mbili.

[25] Kama vile kumuambia mtu: “Ntakuuzia nyumba hii kwa shilingi milioni kumi pesa taslimu au kwa shilingi milioni kumi na tatu kwa mkopo.”

[26] Kuuza kitu usichokimiliki mfano wake ni kama vile kuenda sehemu na ukanunua kitu na hapo hapo dukani ukamuuzia mtu na ukamlipa mwenye duka na faida uchukue wewe.

[27] ‘Urbaan ina maana ya kuweka kwa ajili ya kukilinda kitu au kukizuia kwa ajili ya kuginunua kitu. Kwa mfano kama mtu atatoa hela ya kununua mnyama kama hivi na mnunuzi anakaa na hela ile iliyowekwa kama dhamana, kama biashara itakamilika fedha zile zitakatwa katika mauzo. Mauzo haya si halali kulingana na Hadiyth. Hata hivyo, baadhi ya Wanazuoni wanazingatia Hadiyth hii kuwa ni dhaifu. Hivyo basi, imekuwa ni haramu kwa muono wa Imaam Maalik na Shaafiy’ na kukubaliwa na Imaam Ahmad. Fedha hizi ambazo mtu anazitoa ambazo hazitarejeshwa kwake kama biashara haijakamilika huitwa ‘dhamana isiyorejeshwa’.

[28] Ina maana kuwa mtu anaponunua bidhaa sehemu hairuhusiwi kuiuza pale pale tena, hadi itakapohamia katika miliki ya mnunuzi kabla ya kuiuza tena. Hukumu hii ni kwa bidhaa ambayo inaweza kuhamishika. Kwa biashara kama ya nyumba, inawezekana pale tu baada ya kukamilisha taratibu zote za mauzo, hapo naye anaweza kuiuza.

[29] Dirhamu ni sarafu ya fedha, dinari ni sarafu ya dhahabu. Kubadilisha dinari na dirhamu na kinyume chake ni halali madamu mabadilishano haya yatamalizika na kuhitimishwa kwa bei ya siku ile na kila mtu atapokea haki yake kwa ukamilifu. Hii inafahamika kama biashara ya kubadilisha fedha.

[30] An-Najsh ni mtu kuzidisha thamani ya bidhaa kwa kutokuwa na niyyah ya kununua, bali ili watu wainunue kwa bei ya juu.

[31] Muhaaqalah: ni kuuza nafaka katika shuke lake (kabla kuvunwa) kwa kukadiria na nafaka zilizopimwa (zilizovunwa) kama ngano.

[32] Muzaabanah: ni kuuza matunda (au mazao) yaliyo katika shamba (ambayo bado hayajachumwa) kwa matunda yaliyokwisha chumwa. Mauzo haya si halali

[33] Mukhaabarah: ni mtu kukodisha shamba ili malipo yake yawe ni baadhi ya mazao yatakayotoka kama ni nusu ya mazao au theluthi. Kimsingi mauzo haya ni halali na Nabiyy (ﷺ) aliyafanya kwa Mayahudi wa Khaybar. Kinachokatazwa na Hadiyih hii ni kuainisha kipande cha mazao ya ardhi mmiliki na kipande kingine cha ardhi cha aliyekodishwa. Suala hili linaleta mgongano na wamiliki wa ardhi na wakodishaji, ikiwa mazao ya mwenye shamba yasipofanikiwa kuvunwa na ya mkodishaji kuvunwa au kinyume chake. Hata hivyo hakuna tatizo kama watakubaliana kushirikiana mazao yote yaliyovunwa kwa kiwango watakachobaliana.

[34] Thun-yaa ni kuuza mazao shambani yakiwa katika mti kwa bei kadhaa kwa sharti la kuvuna baadhi ya matunda. Hii ni haramu kwa kuwa kilichovunwa hakijulikani. Hata hivyo kama kiwango kitaainishwa basi inaruhusiwa.

[35] Mukhaadhwarah: ni kuuza nafaka au matunda kabla ya kuiva.

[36] Mulaamasah: ni mtu aiguse nguo bila ya kuitazama. Mauzo kwa bei iliyokwishapangwa anainunua akiwa amefunga macho au katika kiza kwa mguso mmoja wa mkono wake. Kwa mfano mtu anakwenda kwa muuza nguo na anapendekeza anunue jora ya kitambaa kwa kiasi cha fedha. Anakubali kununua kwa sharti la kuwa atafunga macho kisha atashika jora la kitambaa, na atanunua jora ambalo atashika mwanzo. Biashara ya sampuli hii imekatazwa.

[37] Munaabadhah: ni mtu kuirusha nguo yake katika hali ya kiza kwa mtu mwingine kabla ya kuikagua au kuitazama na huyo anayerushiwa huinunua.

[38] Jina lake kamili ni Abuu ‘Abdir-Rahmaan Twaawus bin Kisan Al-Faaris, ameachwa na wao (kina Al-Himyaar). Jina lake alikuwa ni Dhakwaan na Twaawus ilikuwa ni lakabu yake. Ni madhubuti, faqihi (Mwanachuoni wa Shariy’ah). Alikuwa ni Taabiy’ wa daraja la tatu. Amepokewa akisema: “Nimekutana na Maswahaba 50 katika uhai

wangu.” Ibn ‘Abbaas amesema: “Sijawahi kumuona mfano wake.” Alifariki mwaka wa 106 Hijriyyah.

[39] Kuwapokea wasafiri nje ya mji, kwa lengo la kununua bidhaa kutoka kwao kwa bei ya chini, na kuwaficha hali halisi ya soko lilivyo ni jambo lisiloruhusiwa. Misafara iruhusiwe kufika katika vituo vyake vya biashara na kujua bei ya soko. Kabla ya hili kuuza na kununua hakutakiwi. Ikiwa mtu atapatana katika mauzo na baadae muuzaji akafahamu kuwa amedanganywa anaweza kuvunja biashara ile.

[40] Najsh imeelezwa hapo kabla. Maelezo mengine ni kuwa ikiwa mtu kanunua kutoka kwa mwenye duka, mwenye duka mwingine hatakiwi kumshawishi mtu yule anunue kutoka kwake kwa kumuuzia kwa bei ya chini zaidi.

[41] Haitakiwi kwa mwanamke kuleta na kusababisha chuki baina ya mke na mume, ili asababishe talaka baina yao ili apate kuolewa yeye na mme huyo. Hali kadhaalika ni haramu kumuoa dada au ndugu ya mtu kwa sharti la kumuacha mke wake wa kwanza.

[42] Kwa mfano mtu akikubaliana na mtu kumuuzia kitu kwa shilingi elfu moja. Hairuhusiwi kwa mtu mwingine kumshawishi muuzaji asiuze kwa shilingi elfu moja, kwa yeye kutaka kununua kwa elfu moja na mia tano kwa kitu kile kile. Hata hivyo ikiwa bidhaa imewekwa kwa ajili ya ushindani kama vile mnadani, inafaa mtu kuongeza thamani.

[43] Hadiyth hii inaashiria kufarakanisha haifai. Hadiyth hii inaweka wazi kama biashara hiyo itaendelea ni haki kuivunja.

[44] Hadiyth hii inaashiria kuwa suala la kupanga bei haliruhusiwi kwani inapelekea hasara wakati mwingine kwa wafanya biashara, kwa upande wa pili inapelekea katika janga la njaa. Mahitaji muhimu ya maisha yanakosekana na uchafu unaibuka katika jamii.

[45] Ma'mar bin 'Abdillaah bin Naafi' bin Nadla bin Harthaan Al-'Adawi ni Swahaba mkubwa, ni miongoni mwa waliohajiri Uhabeshi. Hijra yake Madiynah ilichelewa.

[46] Ihtikaar – Ukiritimba ni kuzuia bidhaa kwa ajili ya mauzo ya faida kubwa zaidi baadae. Ukiritimba umekatazwa na ni haramu kwani inatengeneza uhaba wa mahitaji muhimu wa chakula wakati katika hali halisi vyakula vipo.

[47] Katika Hadiyth, siku tatu zimetajwa kwa sababu kwa uchache siku tatu zinahitajika kutathmini kiasi halisi cha maziwa katika kiwele. Wakati mwingine nyasi kavu na kubadilika kwa sehemu husababisha maziwa kuongezeka. Ikiwa maziwa yataachawa katika kiwele kwa matumizi

binafsi na si kwa kuuza inaruhusiwa. Kwa hali yoyote ile, kuyaacha maziwa katika kiwele cha mnyama humuumiza mnyama.

[48] Ina maana kama mnunuzi ataona ubaya wa muamala huu, anaweza kurudi baada ya siku tatu. Kama mauzo ni maziwa ya ng'ombe, yatarudishwa kwa pishi (sawa na 2.6 kg) kwa nafaka yoyote, sio lazima iwe tende.

[49] Hii ina maana kwamba udanganyifu ni jambo lililokatazwa. Maana ya Hadiyth hii ni Udanganyifu si laiki ya watu wangu. “Ni tabia ya kikafiri.” Haina maana kuwa yeye ni kafiri.

[50] Ni haramu kuuza zabibu kwa mtengeneza mvinyo. Kusaidia kitendo chochote cha ubaya na kwa malengo mabaya ni haramu. Qur-aan Suwrah Al-Maaidah (5: 2) inatuamrisha kufanya na kushirikiana kwa matendo mema na kutukataza kabisa kushirikiana na madhambi na matendo mabaya.

[51] Ina maana hadi wakati wa kurudisha bidhaa (kama haitakiwi) faida na hasara inakuwa kwa mnunuzi. Jaalia mauzo ni ya mnyama, na mnyama akafa katika muda walioahidiana arudishe basi hasara inakuwa kwa mnunuzi, hali kadhalika kama atamuza kwa bei ya juu zaidi wakati ule faida ataichukua yule mnunuzi.

[52] Huyu ni Ibn Ja'ad au Ibn Abiy Ja'ad na inasemekana kuwa baba yake akiitwa 'Iyyaad Al-Baariqiyy, ni sehemu ya ukoo wa Baniy 'Azd ambaye ni Baariqiyy bin 'Adi bin Haaritha. Alikuwa akiitwa Baariqiyy kwa sababu aliishi katika mlima ulioitwa Baariqiyy. 'Urwah alikuwa ni Swahaba aliyemtumikia 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kama Qadhi wa mji wa Kufa, aliishi huko na Hadiyth zake nyingi zilipokewa na watu wa huko.

[53] Udhwhiyyah ni mnyama anayechinjwa katika siku ya 'Iyd ya Hajj.

[54] Hadiyth hii inaweka wazi mambo manne: (i) Wakili anapewa nguvu na mamlaka ya kutumia utajiri wa mdhamini wake. (ii) Huwezi kuuza bidhaa ila kwa ridhaa ya mwenyewe. (iii) Kuwa ni ruhusa kumuza mnyama wa Udhwhiyyah na kumnunua mwingine kwa badala, biashara hii haitakiwi iwe kwa ajili ya faida. Kama kutakuwepo na faida yoyote kutokana na biashara hii basi itolewe kama Swadaqah. (iv) Ya kwamba wema wowote ni lazima ushukuriwe na uwe na malipo yake.

[55] Chuchu la mnyama, yaani kiwele chake.

[56] Katika Hadiyth hii kumetajwa mambo sita yaliyokatazwa katika biashara na sababu zake zinatofautiana. Uharamu wa mawili yaliyotajwa hauna utata ndani yake kwani Wanazuoni wamekubaliana, nazo ni katika

biashara za kubahatisha. La tatu ni haramu kwa sababu ya kutokuwa na hakika na hali ya mtumwa aliyekimbia. La nne ni haramu kwa kuwa haipo katika miliki, la sita ni haramu kwa kuwa hakuna uhakika kama mzamiaji atatoka na chochote anapozamia. Nayo ni hali ya kubahatisha. Kubahatisha kwa mpiga mbizi ni mtu kusema: “Nitapiga mbizi katika maji kwa shilingi kadhaa kitakachotoka ni chako.” Biashara hii imekatazwa kwa sababu ya udanganyifu.

[57] Kiwele: ziwa la mnyama. Katika Hadiyth hii aina tatu za biashara haramu zimetajwa. Ya kwanza ni matunda ambayo bado hayajawiva, matunda yaliyopo mtini kwani kuna uwezekano wa kuharibika hadi yawive. Nukta ya pili ni kuwa mti ni mali ya muuzaji na matunda yake ni mali ya mnunuzi. Ushirikiano wao wa muda mrefu hauwezi kudumu sana. Aina zingine za biashara zilizoharamishwa hapa ni Sufi ya kondoo mgongoni mwake kabla hajanyolewa na maziwa ya mnyama yakiwa katika kiwele chake. Hizi ni haramu kwa sababu kiwango cha sufi na maziwa hayajulikani, ni aina ya bahati nasibu ambayo ni biashara ya kubahatisha.

[58] Madhwaamiyn neno la kiarabu lenye maana ya kizazi kwa maana ya mimba ambayo haijazaliwa katika tumbo la mamake.

[59] Al-Malaaqiyh ni manii katika mgongo wa baba.

[60] Ikiwa wameshakubaliana kuwa mali inaweza kurudishwa, mnunuzi ana haki kamili ya kurejesha. Hata hivyo kama hawajakubaliana hapo kabla na mnunuzi anataka kurejesha, na akamrudishia muuzaji, basi yule muuzaji atakapokubali, kwa khiyari yake, kurudisha bidhaa ile, Allaah atamsamehe madhambi yake.

02- Mlango Wa Khiyari

بَابُ الْخِيَارِ

02-Mlango Wa Khiyari

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا تَبَايَعَ الرَّجُلَانِ، فَكُلُّ وَاحِدٍ مِنْهُمَا بِالْخِيَارِ مَا لَمْ يَتَفَرَّقَا وَكَانَا جَمِيعًا، أَوْ يُخَيَّرُ أَحَدُهُمَا الْآخَرَ، فَإِنْ خَيَّرَ أَحَدُهُمَا الْآخَرَ فَتَبَايَعَا عَلَى ذَلِكَ فَقَدْ وَجَبَ الْبَيْعُ، وَإِنْ تَفَرَّقَا بَعْدَ أَنْ تَبَايَعَا، وَلَمْ يَتْرُكْ وَاحِدٌ مِنْهُمَا الْبَيْعَ فَقَدْ وَجَبَ الْبَيْعُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wakiuziana watu wawili basi kila mmoja miongoni mwao yuko katika khiyari[1] maadamu hawajaachana na wapo pamoja, au mmojawapo amkhiarishe mwingine na wakauziana juu ya maafikiano hayo; basi kuuziana kumeshapasa. Na wakiachana baada ya kuuziana, na mmoja kati yao hakuacha kuuza au kununua, basi kuuziana kumeshapasa.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الْبَائِعُ وَالْمُبْتَاعُ بِالْخِيَارِ حَتَّى يَتَفَرَّقَا، إِلَّا أَنْ تَكُونَ صَفْقَةً خِيَارٍ، وَلَا يَحِلُّ لَهُ أَنْ يُفَارِقَهُ خَشْيَةً أَنْ يَسْتَقِيلَهُ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ إِلَّا ابْنُ مَاجَةَ،

وَالدَّارِقُطْنِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ وَفِي رِوَايَةٍ:
{حَتَّى يَتَفَرَّقَا مِنْ مَكَانِهِمَا}

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb amepokea kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake kuwa amesema Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) amesema: “Muuzaji na mnunuzi wako katika khiyari hadi watakapoachana, isipokuwa iwe na maafikiano ya khiyari, wala si halali kwake kufarikiana naye kwa kuchelea asije akabatilisha mauziano.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ahmad) isipokuwa Ibn Maajah, na imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy, Ibn Khuzaymah na Ibn Al-Jaaruwad]

Katika Riwaayaha nyingine imesema: “...mpaka wafarikiane mahala pao.”

.694

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: ذَكَرَ رَجُلٌ لِلنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ يُخْدَعُ فِي الْبُيُوعِ فَقَالَ: {إِذَا بَايَعْتَ فَقُلْ: لَا خَلَابَةَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa mtu mmoja[2] amemuambia Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuwa yeye hudanganywa katika biashara. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Unapofanya biashara, muambie unayefanya naye hakuna kuhadaana.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Ikhtihaar au Khihaar ni mtu kuwa na haki ya kuvunja mkataba. Kuna aina nyingi za khihaar:

- i. Khihaar Majlis: muda wa kuwa muuzaji na mnunuzi wako pamoja, kila mmoja ana haki ya kukataa au kukubali muamala.
- ii. Khihaar Shartw: Muuzaji na mnunuzi wanaweka sharti kuwa hadi muda fulani, basi kila mmoja wao ana haki ya kukubali au kukataa mauzo.
- iii. Khihaar ‘Ayb: Mnunuzi anasema ikiwa bidhaa ni mbovu atairudisha.
- Iv. Khihaar Ru’yah: Mnunuzi anakamilisha muamala kwa sharti kuwa itakamilika baada ya kuona bidhaa.
- v. Khihaar Ta’ayiyn: Ina maana kuwa mnunuzi anaruhusiwa kuchagua anachokitaka.

[2] Bwana huyu akiitwa Habbaan bin Munqadh. Alipata ajali kichwani na kumbukumbu yake ikawa ndogo, baadhi ya watu walikuwa wakimdanganya katika biashara, kwa hivyo Nabiyy (ﷺ) akamfundisha maneno haya.

03-Mlango Wa Ribaa

بَابُ الرِّبَا

03-Mlango Wa Ribaa

عَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَعَنَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَكِلَ الرَّبَا، وَمُوكِلَهُ، وَكَاتِبَهُ، وَشَاهِدِيَهُ، وَقَالَ: " هُمْ سَوَاءٌ " } رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَلِلْبُخَارِيِّ نَحْوُهُ مِنْ حَدِيثِ أَبِي جُحَيْفَةَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amemlaani mlaji ribaa, mwakilishi wake, mwandishi wake, na mashahidi wake wawili na akasema: “Wote wako sawa.”[1] [Imetolewa na Muslim]

Na katika Al-Bukhaariy amepokea kama hiyo katika Hadiyth ya Abuu Juhayfah

696.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الرِّبَا ثَلَاثَةٌ وَسَبْعُونَ بَابًا أَيْسَرُهَا مِثْلُ أَنْ يَنْكِحَ الرَّجُلُ أُمَّهُ، وَإِنَّ أَرْبَى الرَّبَا عِرْضُ الرَّجُلِ الْمُسْلِمِ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ مُخْتَصَرًا، وَالْحَاكِمُ بِتَمَامِهِ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ribaa ina milango sabini na tatu mwepesi wake ni mfano wa mtu kumuowa mama yake. Kwa hakika ribaa kubwa zaidi ni mtu kuchafua heshima ya Muislam.” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa mukhtasari, na Al-Haakim ameipokea kwa ukamilifu na akaisahihisha]

697.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا تَبِيعُوا الذَّهَبَ بِالذَّهَبِ إِلَّا مِثْلًا بِمِثْلٍ، وَلَا تُشِفُّوا بَعْضَهَا عَلَى بَعْضٍ، وَلَا تَبِيعُوا الْوَرَقَ بِالْوَرَقِ إِلَّا مِثْلًا بِمِثْلٍ، وَلَا تُشِفُّوا بَعْضَهَا عَلَى بَعْضٍ، وَلَا تَبِيعُوا مِنْهَا غَائِبًا بِنَاجِزٍ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah amesema: “Msiuze dhahabu kwa dhahabu isipokuwa sawa kwa sawa, wala msizidishe baadhi yake juu ya baadhi nyingine. Wala msiuze fedha kwa fedha isipokuwa sawa kwa sawa, wala msizidishe baadhi yake juu ya baadhi nyingine, wala msiuze kusichokuwepo kwa kilichopo.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

698.

وَعَنْ عُبَادَةَ بْنِ الصَّامِتِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { الذَّهَبُ بِالذَّهَبِ، وَالْفِضَّةُ بِالْفِضَّةِ، وَالْبُرُّ بِالْبُرِّ، وَالشَّعِيرُ بِالشَّعِيرِ، وَالتَّمْرُ بِالتَّمْرِ، وَالْمِلْحُ بِالْمِلْحِ، مِثْلًا بِمِثْلٍ، سَوَاءٌ بِسَوَاءٍ، يَدًا بِيَدٍ، فَإِذَا اخْتَلَفَتْ هَذِهِ الْأَصْنَافُ فَبِيعُوا كَيْفَ شِئْتُمْ إِذَا كَانَ يَدًا بِيَدٍ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa ‘Ubaadah bin Asw-Swaamit[2] (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah

amesema: “Dhahabu kwa dhahabu, fedha kwa fedha, ngano kwa ngano, shayiri[3] kwa shayiri, tende kwa tende, chumvi kwa chumvi, mfano kwa mfano, sawa kwa sawa, mkono kwa mkono,[4] zitatofautiana aina hizi basi uza unavyotaka muda wa kuwa mauzo yatafanyika mkono kwa mkono.” [Imetolewa na Muslim]

699.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الذَّهَبُ بِالذَّهَبِ وَزَنًا بِوزنٍ مِثْلًا بِمِثْلِ، وَالْفِضَّةُ بِالْفِضَّةِ وَزَنًا بِوزنٍ مِثْلًا بِمِثْلِ، فَمَنْ زَادَ أَوْ اسْتَزَادَ فَهُوَ رِبَا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Dhahabu kwa dhahabu, wizani kwa wizani, mfano kwa mfano, fedha kwa fedha, wizani kwa wizani, mfano kwa mfano, atakayezidisha au akataka kuzidishiwa basi hiyo itakuwa ribaa.” [Imetolewa na Muslim]

700.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ، وَأَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ اسْتَعْمَلَ رَجُلًا عَلَى خَيْرٍ، فَجَاءَهُ بِتَمْرٍ جَنِيبٍ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَكُلْتُ تَمْرَ خَيْرٍ هَكَذَا؟ " فَقَالَ: لَا، وَاللَّهِ يَا رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّا لَنَأْخُذُ الصَّاعَ مِنْ هَذَا بِالصَّاعَيْنِ وَالثَّلَاثَةِ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ

صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " لَا تَفْعَلْ، بَعِ الْجَمْعَ بِالْدَّرَاهِمِ، ثُمَّ
ابْتَغِ بِالْدَّرَاهِمِ جَنِيْبًا } وَقَالَ فِي الْمِيزَانِ مِثْلَ ذَلِكَ. مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَلِمُسْلِمٍ: "وَكَذَلِكَ الْمِيزَانُ"

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd na Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) wamesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtawalisha mtu Khaybar,[5] akamjia na tende nzuri. Akasema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Tende zote za Khaybar ziko hivi?” Akasema: “Hapana. Wa-Allaahi Ee Rasuli wa Allaah! Hakika sisi huchukuwa pishi moja ya tende hizi kwa pishi mbili, au tatu (duni ya hizi).” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Usifanye hivyo, uza tende duni kwa dirhamu kadhaa kisha ununue tende nzuri kwa dirhamu kadhaa.” Na katika mizani alisema kama hivyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim imesema: “...vile vile ilivyopimwa.”

701.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { نَهَى رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ بَيْعِ الصُّبْرَةِ مِنَ التَّمْرِ لَا
يُعْلَمُ مَكِيلُهَا بِالْكَيْلِ الْمُسَمَّى مِنَ التَّمْرِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza lundo la tende lisilojulikana kipimo chake kwa kipimo cha tende kilichotajwa.”[6] [Imetolewa na Muslim]

702.

وَعَنْ مَعْمَرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: إِنِّي كُنْتُ أَسْمَعُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {الطَّعَامُ بِالطَّعَامِ مِثْلًا بِمِثْلِ} "وَكَانَ طَعَامُنَا يَوْمَئِذٍ الشَّعِيرَ" {رَوَاهُ مُسْلِمٌ}

Kutoka kwa Ma'mar bin 'Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Mimi nilikuwa nikimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: "Chakula kwa chakula, sawa kwa sawa, wakati huo chakula chetu kilikuwa ni shayiri." [7] [Imetolewa na Muslim]

703.

وَعَنْ فَضَالَةَ بْنِ عُبَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {إِشْتَرَيْتُ يَوْمَ خَيْبَرَ قِلَادَةً بِاِثْنَيْ عَشَرَ دِينَارًا، فِيهَا ذَهَبٌ وَخَرَزٌ، فَفَصَلْتُهَا فَوَجَدْتُ فِيهَا أَكْثَرَ مِنْ اِثْنَيْ عَشَرَ دِينَارًا، فَذَكَرْتُ ذَلِكَ لِلنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: "لَا تُبَاعُ حَتَّى تُفْصَلَ" {رَوَاهُ مُسْلِمٌ}

Kutoka kwa Fadhwaalah bin 'Ubayd [8] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Nilinunua mkufu Siku ya Khaybar kwa dinari kumi na mbili, ndani yake kuna dhahabu na kito, nikavitenganisha, nikapata zaidi ya dinari kumi na mbili, nikamuelezea jambo hilo Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaniambia: "Haiuzwi mpaka ipambanuliwe." [9] [Imetolewa na Muslim]

704.

وَعَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ بَيْعِ الْحَيَوَانِ بِالْحَيَوَانِ نَسِيئَةً } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ الْجَارُودِ

Kutoka kwa Samurah bin Jun-dub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): amekataza kuuza mnyama kwa mnyama kwa kuchelewesha.”[10] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Al-Jaarud]

705.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { إِذَا تَبَايَعْتُمْ بِالْعِينَةِ، وَأَخَذْتُمْ أَذْنَابَ الْبَقَرِ، وَرَضِيتُمْ بِالزَّرْعِ، وَتَرَكْتُمُ الْجِهَادَ، سَلَّطَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ ذُلًّا لَا يَنْزِعُهُ حَتَّى تَرْجِعُوا إِلَى دِينِكُمْ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ مِنْ رِوَايَةِ نَافِعٍ عَنْهُ، وَفِي إِسْنَادِهِ مَقَالٌ وَلِأَحْمَدَ: نَحْوُهُ مِنْ رِوَايَةِ عَطَاءٍ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْقَطَّانِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Nimemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

akisema: “Mtakapouziana kwa Al-‘Iynah,[11] mkashika mikia ya ng’ombe,[12] mkaridhia kulima na mkaacha Jihaad, Allaah Atawasalitisha udhalili ambao hatauondoa mpaka mrudi katika Dini yenu.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd kutoka katika Riwaayah ya Naafi’[13] na katika Isnaad yake kuna maelezo]

Na Ahmad amepokea kama hivyo kutoka Riwaayah ya ‘Atwaa,[14] wapokezi wake ni madhubuti, na akaisahihisha Ibn Al-Qatwaan

706.

وَعَنْ أَبِي أَمَامَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ شَفَعَ لِأَخِيهِ شَفَاعَةً، فَأَهْدَى لَهُ هَدِيَّةً،
فَقَبَّلَهَا، فَقَدْ أَتَى بَابًا عَظِيمًا مِنْ أَبْوَابِ الرَّبِّ} رَوَاهُ أَحْمَدُ،
وَأَبُو دَاوُدَ، وَفِي إِسْنَادِهِ مَقَالٌ

Kutoka kwa Abuu Umaamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye
kumuomba nduguye uombezi akampa zawadi akaikubali, kwa
hakika atakuwa ameingia mlango mkubwa miongoni mwa milango
ya ribaa.”[15] [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuwd, na katika
Isnaad yake kuna maelezo]

707.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {لَعَنَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ الرَّاشِيَّ وَالْمُرْتَشِيَّ} رَوَاهُ أَبُو
دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amemlaani mtoa rushwa na mpokea rushwa.”[16] [Imetolewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy akaisahihisha]

708.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ رَسُولَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَمَرَهُ أَنْ يُجَهَّزَ جَيْشًا فَنَفَدَتْ الْأَبِلُ، فَأَمَرَهُ أَنْ يَأْخُذَ عَلَى قَلَائِصِ الصَّدَقَةِ. قَالَ: فَكُنْتُ أَخْذُ الْبَعِيرَ بِالْبَعِيرَيْنِ إِلَى إِبِلِ الصَّدَقَةِ } رَوَاهُ الْحَاكِمُ وَالْبَيْهَقِيُّ، وَرَجَّاهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuamrisha kuandaa jeshi, ngamia wakamalizika, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuamrisha kuchukua katika ngamia wa Zakaah. Akasema: “Nikawa nawabadilisha ngamia wawili wadogo wa Zakaah kwa ngamia mmoja mkubwa.” [Imetolewa na Al-Haakim na Al-Bayhaqiyy na wapokezi wake ni madhubuti][17]

709.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنِ الْمُرَابَنَةِ، أَنْ يَبِيعَ ثَمَرُ حَائِطِهِ

إِنْ كَانَ نَخْلًا يَتَمَرُ كَيْلًا، وَإِنْ كَانَ كَرْمًا أَنْ يَبِيعَهُ بِزَبِيبٍ
كَيْلًا، وَإِنْ كَانَ زَرْعًا أَنْ يَبِيعَهُ بِكَيْلِ طَعَامٍ، نَهَى عَنْ ذَلِكَ
كُلُّهُ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza Al-Muzaabanah
kwa kuuza matunda ya shambani mwake ikiwa ni mtende kwa tende
kwa kupimwa na ikiwa ni zabibu kuziua kwa zabibu kwa kupimwa
na ikiwa ni mavuno kuyauza kwa kipimo cha chakula. Ameyakataza
yote hayo.”[18] [Al-Bukhaariy, Muslim]

710.

وَعَنْ سَعْدِ بْنِ أَبِي وَقَّاصٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { سَمِعْتُ
رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ سُئِلَ عَنْ إِشْتِرَاءِ
الرُّطْبِ بِالتَّمْرِ. فَقَالَ: أَيْنَقُصُ الرُّطْبُ إِذَا يَبَسَ؟ " قَالُوا:
نَعَمْ. فَنَهَى عَنْ ذَلِكَ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْمَدِينِيِّ،
وَالْتِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Sa’d bin Abiy Waqqaasw[19] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
amesema: “Nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
akiulizwa kuhusu kununua tende mbivu kwa tende kavu,
akasema: ‘Je mbivu hupungua zinapokauka?’” Wakasema: “Ndio.”
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akakataza kufanya hivyo.”
[Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu
Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Al-Madiyniyy,
At-Tirmidhiyy, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

711.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ بَيْعِ الْكَالِيِّ بِالْكَالِيِّ، يَعْنِي: الدَّيْنِ بِالْدَّيْنِ {
رَوَاهُ إِسْحَاقُ، وَالْبَزَّازُ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza Al-Kaali (kuzuza
deni) kwa Al-Kaali (kwa deni).”[20] [Imetolewa na Ishaaq na Al-
Bazaar kwa Isnaad dhaifu]

[1] Ribaa ni haraam kwa dalili zilizo wazi kabisa katika Qur-aan. Yeyote atakayetoa mkopo kwa sharti la ribaa, na atakayepokea, mwandishi wake na shahidi wake, wote wamelaaniwa.

[2] ‘Ubaadah bin Asw-Swaamit bin Qays Al-Answaar, Al-Khazraj, Abul-Waliyd.

[3] Shayiri: nafaka inayofanana na ngano inayotumika kwa chakula. Ingawaje maeneo ya huku hutumika zaidi kutengeneza bia.

[4] Vitu vilivyotajwa na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) vilikuwa ni dhahabu, fedha, ngano, shayiri, tende na chumvi hakuna nyongeza au punguzo za vitu hivi vilivyotajwa katika kubadilishana navyo. Kwa mfano, mtu anataka aina nzuri ya ngano na mwingine ana aina ya chini, hairuhusiwi kubadilisha kilo 20 za ngano bora kwa kilo 30 za ngano za hali ya chini. Ikiwa mtu anataka kubadilisha aina ya ngano aliyonayo kwa nyingine, ni bora auze aliyonayo kisha kwa thamani ile anunue aina anyingine kwa fedha zile. Mabadilishano ya bidhaa hizi kwa nyongeza au

nuksani hairuhusiwi kabisa. Baadhi ya Wanazuoni wamejuzisha zidisho na punguzo kwa baadhi za bidhaa zisizokuwa hizi sita, hata hivyo Maimaam wane hawakubali mabadilishano haya madamu ni aina moja ya bidhaa kwa bidhaa mfano wake.

[5] Anayezungumziwa hapa ni Sawaad bin Ghaziyya Al-Answaar.

[6] Ina maana ya kwamba bidhaa yoyote inayouzwa kwa kipimo maalumu inabidi iuzwe au kibadilishwe kwa kipimo hicho maalumu na siyo kwa kudhania kipimo au kubahatisha.

[7] Katika Hadiyth nyingine inatajwa kuwa chakula cha wakati ule kilikua ni ngano. Ma'mar anataka kuelezea kuwa ngano na shayiri ni sawa sawa na ichukuliwe kuwa ni aiana moja ya chakula na katika kubadilishana kisipungue au kisizidi. Hata hivyo Maswahaba wengine hawakukubaliana hivi. Kama ilivyoripotiwa na 'Ubaadah bin Swaamit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) ambayo imeweka wazi kuwa ngano na shayiri ni vyakula vya aina mbili tofauti.

[8] Huyu ni Fadhwaalah bin 'Ubayd Al-Answaar Al-Aws, Abuu Muhammad

[9] Hadiyth hii inatoa ushahidi kuwa dhahabu ikichanganywa na kitu kingine isiuzwe isipokuwa iwe imetenganishwa na dhahabu safi nyinginezo, kwani ni vigumu kukadiria uzito wa dhahabu iliyochanganywa na kitu kingine.

[10] Inaruhusiwa kumuuza mmoja kwa thamani ya wanyama wawili lakini kumuuza myama kwa mkopo au kwa kuchelewesha kulipa hakuruhusiwi.

[11] Al-'Iynah: mfano wa Al-'Iynah ni mtu kutaka akopeshe kiasi cha fedha. Hampi huo mkopo bali humpa kilichokuwa na thamani zaidi ya huo mkopo. Kisha ananunua tena kutoka kwake kwa thamani ya chini ambayo ni sawa na mkopo alioumba. Kwa hali hii anamfanya mdaiwa kudaiwa zaidi, yaani fedha aliyompa mkopo na ziada yake. Hii ni ribaa; kufanya

hivi ni haramu kwa sababu inaingia katika ribaa ya kuchelewesha. Na inadhihirisha kuwa mambo mawili hayo ni sababu ya kumdhalilisha Muislamu; moja ni kuiacha jihaad na ya pili ni kughushi na udanganyifu.

[12] “...mkashika mikia ya ng’ombe” yaani mkawa mmeshughulika na mifugo tu.

[13] Huyu ni Abuu ‘Abdillaah Naafi’ bin Sirjis Al-Madani, muachwa huru wa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) aliyetekwa katika vita. Ni mtu madhubuti na Mwanazuoni mkubwa katika Taabi’inya. Amepokea Hadiyth nyingi zilizohadithiwa na Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا). Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) anasema: “Allaah Ametubariki kwa Naafi’.” Imepokewa kuwa Maalik naye amesema: “Nilikuwa sijisumbui kuchukua Hadiyth kwa yeyote maadamu nikiipata kwa Naafi’ kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ).” Al-Bukhaariy vile vile amesema: “Silsila ya upokezi iliyo sahihi zaidi ni ile kutoka kwa Maalik kutoka kwa Naafi’ kutoka kwa Ibn ‘Umar (kutoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)).” Watu wengi wamepokea Hadiyth kutoka kwa Naafi’ alifariki mwaka 117 Hijriyyah.

[14] Uwezekano mkubwa ‘Atwaa huyu akawa ni ‘Atwaa Al-Khurasani ambaye akiitwa Abuu ‘Uthmaan ‘Atwaa bin Abiy Muslim Maysarah, muachwa huru wa Al-Muhalab bin Abiy Sufra. Aliishi Shaam na alikuwa ni mtu mwenye hadhi kubwa. Alikuwa ni mtu madhubuti na alikuwa ni mwenye kudumu katika Swalaah za usiku. Kwa bahati mbaya kumbukumbu yake haikuwa nzuri kwa hiyo alikuwa na makossa katika mapokezi yake. Alifariki mwaka 135 Hijriyyah akiwa na miaka 85.

[15] Ikiwa zawadi hiyo atapewa kabla ya kumuombea pamoja na kumuombea katika yasiyofaa, uharamu wake umekubaliwa na Wanazuoni wote, na inahesabiwa ni rushwa na sio zawadi. Kuunga mkono yasiyofaa na kuchukua zawadi kwa ajili yake ni katika kundi hili hili. Ikiwa mtu amesaidia katika kufanywa kwa mambo mema kisha akapokea zawadi kwa ajili hiyo inaruhusiwa ikiwa halikuwa katika ahadi au kushurutishwa.

[16] Anayepokea rushwa amelaaniwa. Anayelazimishwa kutoa rushwa apate haki yake Allaah atamsamehe. Lakini rushwa ikitolewa kuchepua haki ya mwingine inaelekea mtu kupata laana ya Rabb wake

[17] Hadiyth hii ni dalili kuwa hakuna ribaa katika wanyama.

[18] Hii ni kwa sababu inahusika na kuuza kitu kisichojulikana thamani yake kwa kinachojulikana thamani yake. Kwa sababu biashara hii ni haraam.

[19] Aliitwa Sa'd bin Maalik bin Ahiyb (au Wuhayb) bin 'Abd Manaaf bin Zuhrah bin Kilaab bin Murrah bin Ka'b bin Luay, na alikuwa ni wa kabila la Baniy Zuhrah. Ni wa familia ya Aaminah bint Wahb, mamake Nabiyy (ﷺ) kwa hiyo alikuwa na udugu na 'ammi zake Nabiyy (ﷺ). Ukoo wake unakutana na Rasuli wa Allaah (ﷺ) kwa Kilaab bin Murrah. Jina lake ndilo hilo hila hata kabla ya kusilimu. Lakabu yake ilikuwa Abuu Ishaaq. Rasuli wa Allaah (ﷺ) alimbashiria Sa'd Jannah zaidi ya mara moja. Sa'd alikuwa mmoja wa watu kumi walioahidiwa Jannah na Nabiyy (ﷺ), kumi wamo Jannah: Abuu Bakr yumo Jannah, 'Umar yumo Jannah, 'Uthmaan yumo Jannah, 'Aliy, Az-Zubayr, Twalhah, 'Abdur-Rahmaan bin 'Awf, Abuu 'Ubaydah bin Al-Jarraah na Sa'd bin Abiy Waqqaasw.

[20] Ipo katika aina mbili: kwa mfano: 1. 'Aliy ananunua farasi kutoka kwa Bakr kwa Dirhamu mia moja, na anatoa ahadi kulipa baada ya mwaka mmoja, baada ya mwaka mmoja, anashindwa kulipa deni. Anakuenda kwa Bakr na kumuomba kuuziwa farasi tena kwa thamani ya juu. Hii ina maana kuwa 'Aliy analipa ribaa kwa kuongezewa muda wa ziada wa kulipa. 2. Aina ya pili inaelezwa kwa mfano ufuatao: Jaalia kuwa 'Umar anamdai Dirhamu kumi Zayd, naye Zayd anamdai kitambaa Bakr. Bakr anamuambia Zayd: "Nitakuuzia kipande cha kitambaa ninachomdai 'Umar kwa Dirhamu kumi unayodaiwa na 'Umar." Hivyo basi, 'Umar anampa kitambaa Zayd badala ya Bakr, naye anampa dirhamu kumi Bakr badala ya Zayd. Aina hii ya mauzo inakatazwa.

04-Mlango Wa Ruhusa Katika ‘Araayaa Na Kuuza Matinee Na Matunda

بَابُ الرُّخْصَةِ فِي الْعَرَايَا وَبَيْعِ الْأُصُولِ وَالتَّمَارِ

04-Mlango Wa Ruhusa Katika ‘Araayaa Na Kuuza Mashina Na Matunda

712.

عَنْ زَيْدِ بْنِ ثَابِتٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {رَخَّصَ فِي الْعَرَايَا: أَنْ تُبَاعَ بِخَرْصِهَا كَيْلًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِلْمُسْلِمِ: {رَخَّصَ فِي الْعَرِيَّةِ يَأْخُذُهَا أَهْلُ الْبَيْتِ بِخَرْصِهَا تَمْرًا، يَأْكُلُونَهَا رُطْبًا}

Kutoka kwa Zayd bin Thaabit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Ameruhusu katika ‘Aryaaaa[1] ziuzwe kwa kuzikadiria kwa kipimo.” [Al-Bukaariy, Muslim]

Na katika Muslim imesema: “Ameruhusu katika ‘Ariyyah watu wa nyumbani wanazichukua kwa kuzikadiria na tende, na wale zilizoiva zikichumwa kutoka mtini.”

713.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ رَخَّصَ فِي بَيْعِ الْعَرَايَا بِخَرْصِهَا، فِيمَا دُونَ خَمْسَةِ أَوْسُقٍ، أَوْ فِي خَمْسَةِ أَوْسُقٍ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliruhusu katika biashara ya ‘Araayaa kwa kuzikadiria na tende chini ya wasaqi[2] tano au wasaqi tano.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

714.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ بَيْعِ الثَّمَارِ حَتَّى يَبْدُوَ صَلاَحُهَا، نَهَى الْبَائِعَ وَالْمُبْتَاعَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَفِي رِوَايَةٍ: { وَكَانَ إِذَا سُئِلَ عَنْ صَلاَحِهَا ؟ قَالَ: " حَتَّى تَذْهَبَ عَآهَتُهُ " }

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza matunda hadi yamedhihiri kufaa kwake, amemkataza muuzaji na mnunuzi.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine imesema: “Na alikuwa anapoulizwa kuhusu kufaa kwake husema: mpaka iondoke aibu yake.”[3]

715.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ بَيْعِ الثَّمَارِ حَتَّى تُزْهَى. قِيلَ: وَمَا زَهُوْهَا
؟ قَالَ: " تَحْمَارٌ وَتَصْفَارٌ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza matunda
mpaka yapevuke. Wakasema: Kupevuka kwake ni vipi? Akasema:
Mpaka yawe mekundu au manjano.” [Al-Bukhaariy, Muslim na
tamshi hili ni la^[4] Al-Bukhaariy]

716.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ بَيْعِ الْعِنَبِ حَتَّى يَسْوَدَّ، وَعَنْ بَيْعِ
الْحَبِّ حَتَّى يَشْتَدَّ } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، إِلَّا النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ
حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
“Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuza zabibu
mpaka iwe nyeusi na amekataza kuuza nafaka mpaka iwe ngumu.”
[5] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn
Maajah, Ahmad) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn
Hibbaan na Al-Haakim]

717.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَوْ بَعْتَ مِنْ أَخِيكَ ثَمَرًا فَأَصَابَتْهُ جَائِحَةٌ، فَلَا يَحِلُّ لَكَ أَنْ تَأْخُذَ مِنْهُ شَيْئًا. بِمَ تَأْخُذُ مَالَ أَخِيكَ بِغَيْرِ حَقٍّ؟} رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ: {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَمَرَ بِوَضْعِ الْجَوَائِحِ}

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Lau utamuuzia nduguyo matunda na yakapatwa na maafa basi si halali kwako kuchukua kitu kutoka kwake.[6] Kwa nini uchukue mali ya nduguyo bila haki?” [Imetolewa na Muslim]

Na katika Riwaayah yake nyingine amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameamrisha kutupiliwa mbali malipo ya matunda yaliyopata maafa.”[7]

718.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ ابْتَاعَ نَخْلًا بَعْدَ أَنْ تُؤَبَّرَ، فَتَمَرَتْهَا لِلْبَائِعِ الَّذِي بَاعَهَا، إِلَّا أَنْ يَشْتَرِطَ الْمُبْتَاعُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakayenunua mtende baada ya uchavushi,[8] basi matunda yake ni ya aliyeuza isipokuwa mnunuzi atakaposhurutisha.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] ‘Araayaa (wingi wa ‘Ariyyah) ni mtu kumzawadia maskini tende zake zinazokadiriwa wasaqi tano (kapu tano sawa na kilo 715 takriban) kisha yule mwenye shamba akaona uzito yule maskini kuingia katika shamba lake kwenda kuchuma basi akazinunua kwa kuzikadiria na tende kavu.

[2] Kipimo cha Wasaqi tano: hukisiwa kuwa ni kilo 650 takriban.

[3] Neno la kiarabu ‘Aahat lina maana ya magonjwa ya ghafla, aina hii ya biashara inakatazwa kwa sababu matunda ambao hayajawiva hayafai na matumizi yake si sawa, huenda ugonjwa ukayaangukia na kuyaharibu kwa kuyateketeza. Kwa uwezekano huu wa kuharibika ndio maana ukakatazwa kwa lugha nyingine yasiwe na baka: maradhi ya mimea.

[4] Hadiyth yamalizika hivi: Akasema: “(Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Waonaje Allaah Akizuia (kuosha), matunda ni kwa kitu gani mmoja wenu atahalalisha mali ya nduguye?”

[5] Ina maana hadi ikomae, ndipo inaporuhusiwa kuuzwa. Hadiyth yaonyesha kuwa kuwiva kwa zabibu ni kuwa nyeusi na kuwiva kwa nafaka ni kuwa ngumu. Kila chakula kina namna yake ya kuwiva.

[6] Kama matunda yapo mtini na yakapatwa na maafa, mwenye mti atahusika na hasara ile. Ikiwa maafa ni baada ya kuchumwa kwa matunda basi hasara itabebwa na mnunuzi.

[7] Neno la kiarabu وَضَعَ الْجَوَائِح ina maana hata baada ya kuyachuma yakaonekana ambayo yameharibika muuzaji anatakiwa ampunguzie mteja wake.

[8] Uchavushi ni kupandisha ni kupasua tawi la mtende jike na kupandikiza la mtende dume.

05-Mlango wa As-Salam (Malipo Ya Kabla), Kukopesha Na Kuweka Rahani

أَبْوَابُ السَّلَامِ وَالْقَرْضِ، وَالرَّهْنِ

05-Mlango wa As-Salam (Malipo Ya Kabla),[1] Kukopesha[2] Na
Kuweka Rahani

719.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَدِمَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ الْمَدِينَةَ، وَهُمْ يُسْلِفُونَ فِي الثَّمَارِ السَّنَةَ وَالسَّنَتَيْنِ، فَقَالَ: {مَنْ أَسْلَفَ فِي تَمْرٍ فَلْيُسْلِفْ فِي كَيْلٍ مَعْلُومٍ، وَوَزْنٍ مَعْلُومٍ، إِلَى أَجَلٍ مَعْلُومٍ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ. وَلِلْبُخَارِيِّ: "مَنْ أَسْلَفَ فِي شَيْءٍ"

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliingia Madiynah na wao (wenyeji) wanafanya salaf katika matunda; kwa mwaka mmoja na miaka miwili. Akasema: “Atakayefanya salaf katika matunda basi afanye katika kipimo maalumu, na wizani maalumu na kwa muda maalumu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Al-Bukhaariy imesema: “Atakayefanya salaf katika kitu chochote...”

720.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبْزَى، وَعَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي أَوْفَى رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَا: {كُنَّا نَصِيبُ الْمَغَانِمَ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَكَانَ يَأْتِينَا أَنْبَاطٌ مِنْ أَنْبَاطِ الشَّامِ، فَنُسَلِفُهُمْ فِي الْحِنْطَةِ وَالشَّعِيرِ وَالزَّبِيبِ وَفِي رَوَايَةٍ: وَالزَّيْتِ إِلَى أَجَلٍ مُسَمًّى. قِيلَ: أَكَانَ لَهُمْ زَرْعٌ؟ قَالَا: مَا كُنَّا نَسْأَلُهُمْ عَنْ ذَلِكَ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Abdul-Rahmaan bin Abzaa[3] na ‘Abdullaah bin Abiy Awfaa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) wamesema: “Tulikuwa tukipata ghanima pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na tulikuwa tukijiliwa na Anbaatw[4] wa Sham (Syria, Palestina, Lebanon na Jordan) tulikuwa tukiwalipa kabla kwa ngano, shayiri[5] na zabibu.

Katika Riwaayah nyingine inasema: ...na zeti (ya Zaituni) kwa muda maalumu. Wakasema: Walikuwa na mazao? Akasema: Hatukuwa tukiwauliza swala hilo.”[6] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

721.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ أَخَذَ أَمْوَالَ النَّاسِ يُرِيدُ أَدَاءَهَا، أَدَّى اللَّهُ عَنْهُ، وَمَنْ أَخَذَهَا يُرِيدُ إِتْلَافَهَا، أَتْلَفَهُ اللَّهُ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuchukua mali ya watu anakusudia kuilipa, Allaah atamuwezesha kulipa. Na mwenye kuichukua kwa niyyah ya kuiharibu Allaah Atamuangamiza.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

722.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ فُلَانًا قَدِمَ لَهُ بَزٌّ مِنَ الشَّامِ، فَلَوْ بَعَثْتَ إِلَيْهِ، فَأَخَذْتَ مِنْهُ ثَوْبَيْنِ بِنَسِيئَةٍ إِلَى مَيْسَرَةٍ؟ فَأَرْسَلَ إِلَيْهِ، فَأَمْتَنَعَ} أَخْرَجَهُ الْحَاكِمُ، وَالْبَيْهَقِيُّ، وَرِجَالُهُ ثَقَاتٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilisema: Ee Rasuli wa Allaah! Fulani amekuja na nguo kutoka Sham, waonaje lau ungelimtuma mtu ukachukua kwake nguo mbili kwa mkopo[7] hadi utakapopata? Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamtuma mtu, yule (muuzaji) akakataa.” [Imetolewa na Al-Haakim na Al-Bayhaqiyy. Wapokezi wake ni madhubuti]

723.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الظَّهْرُ يُرْكَبُ بِنَفَقَتِهِ إِذَا كَانَ مَرْهُونًا، وَلَبَنُ الدَّرِّ يُشْرَبُ بِنَفَقَتِهِ إِذَا كَانَ مَرْهُونًا، وَعَلَى الَّذِي يَرْكَبُ وَيَشْرَبُ النَّفَقَةُ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mnyama anapandwa kwa matumizi yake[8] kama mnyama amewekwa rahani[9] na maziwa yatanywewa kwa matumizi yake ikiwa amewekwa rahani, na anayepanda na kukamua ni juu yake matumizi.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

724.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: { لَا يَغْلُقُ الرَّهْنُ مِنْ صَاحِبِهِ الَّذِي رَهْنَهُ، لَهُ غُنْمُهُ، وَعَلَيْهِ غُرْمُهُ } رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَالْحَاكِمُ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ. إِلَّا أَنَّ الْمَحْفُوظَ عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ وَغَيْرِهِ إِرْسَالُهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Rahani haitoki kwenye umiliki wa mwenyewe aliyeweka rahani, nyongeza yake ni yake, matumizi yake ni juu yake.”[10] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy na Al-Haakim. Wapokezi wake ni waaminifu (madhubuti)]

725.

وَعَنْ أَبِي رَافِعٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ اسْتَسْلَفَ مِنْ رَجُلٍ بَكْرًا فَقَدِمَتْ عَلَيْهِ إِبِلٌ مِنَ الصَّدَقَةِ، فَأَمَرَ أَبَا رَافِعٍ أَنْ يَقْضِيَ الرَّجُلَ بَكْرَهُ، فَقَالَ: لَا أَجِدُ

الْأَخْيَارًا قَالَ: "أَعْطِهِ إِيَّاهُ، فَإِنَّ خَيْرَ النَّاسِ أَحْسَنُهُمْ قَضَاءً { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Raafi' (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: "Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikopesha ndama wa ngamia kwa mtu. (Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaletewa ngamia wa Swadaqah. Akamuamuru Abuu Raafi' kumlipa yule ngamia wake. (Abuu Raafi') akasema: Sina isipokuwa ngamia bora mwenye miaka saba. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Mpe huyo kwani ni mbora wao wa kulipa." [11] [Imetolewa na Muslim]

726.

وَعَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {كُلُّ قَرْضٍ جَرٍّ مَنفَعَةٍ، فَهُوَ رَبًّا} رَوَاهُ الْحَارِثُ بْنُ أَبِي أُسَامَةَ، وَإِسْنَادُهُ سَاقِطٌ.
وَلَهُ شَاهِدٌ ضَعِيفٌ عَنْ فَضَالَةَ بْنِ عُبَيْدٍ عِنْدَ الْبَيْهَقِيِّ
وَأَخَرُ مَوْقُوفٌ عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ سَلَامٍ عِنْدَ الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa 'Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Kila mkopo unaoleta manufaa hiyo ni ribaa." [Imetolewa na Al-Haarith bin Abuu Usaamah na katika Isnaad yake kuna mtu ameachwa.

Al-Bayhaqiyy amepokea kama ni ushahidi mwingine ingawaje ni Hadiyth dhaifu kutoka kwa Fadhwaalah bin 'Ubayd.

Al-Bukhaariy ameipokea ikiwa ni Mawquwf kutoka kwa 'Abdullaah bin Salaam.

[1] Salam ina maana ya kununua kitakachozalishwa kwa malipo ya kabla. Kwa mfano mtu anampa mtu mwingine fedha na kumuambia kuwa atampa kitu chenyewe muda fulani kwa bei kadhaa. Hili linaruhusiwa maadamu kuwa bei na thamani yake imekubaliwa hapo kabla. Kwa lugha nyingine inaitwa Salaf.

[2] Kukopesha kwa kiarabu imeitwa Qardhw, ambapo maana yake ni kukata kitu. Mtu anayemkopesha mwenziwe pesa huwa anakata katika zile pesa zake na kumpatia yule anayemkopesha. Katika shariy'ah kukopesha (Qardhw) ni kumpa mtu pesa ambazo zitamsaidia, na mtu huyo anatakiwa kulipa kiwango kile kile alichopewa hapo awali bila ya nyongeza yoyote.

[3] 'Abdul-Rahmaan bin Abzaa Al-Khuzaa'iy, ni muachwa huru wa Banuw Khuzaa' alikuwa ni Swahaba mdogo kwa umri ambaye aliwahi kuswali nyuma ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Aliishi Al-Kufah ('Iraaq), na 'Aliy bin Abiy Twaalib alimfanya kuwa gavana wa Khurasaan. Alifariki Kufa.

[4] Anbaatw ni warabu waliohamia katika miji wa Waajemi na Warumi wakachanganyikana nao.

[5] Shayiri: nafaka inayofanana na ngano inayotumika kuwa chakula.

[6] Hadiyth hii inajuzisha Bayi' As-Salam hata kama mazao hayakuwepo wakati wa mauzo. Cha msingi ni kuwa mazao yawe tayari kwa wakati ule.

[7] Ina maana kuwa kununua kitu kwa mkopo inaruhusiwa. Muuza nguo alikuwa ni Yahudi na alikuwa na uadui na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na ndio maana alikataa.

[8] Ina maana ikiwa mtu ameweka rahani farasi au ng'ombe wake kwa mkopo aliochukua. Kuna tafsiri ya aina mbili: Ima mkopeshaji atamlisha

farasi au ng'ombe na akafaidika nao au mkopaji atamlisha farasi au ng'ombe akafaidika nao. Yeyote atakayewalisha ndio anayestahiki maslahi yao. Hadiyth hii inathibitisha muono wa pili.

[9] Kulingana na Shariy'ah, rahani ni kutoa aina ya miliki au kitu cha anayekopa kama dhamana ya mkopo anaouchukua.

[10] Hii ina maana aliyepewa dhamana si mmiliki wa rahani iliyo kwake. Anaidhibiti tu. Ikiwa rahani imeharibika au kufa, aliyepewa dhamana hana majukumu ya kulipa. Vivyo hivyo kama kutakuwa na ziada ya rahani iliyoongezeka hatokuwa mmiliki wake. Hasara na faida, vyovyote ilivyo inakwenda kwa mmiliki na sio kwa aliyewekewa rahani. Hali hii imebatilisha hali ya kijahiliya ya hapo kabla. Waarabu hapo zamani walikuwa wakiwekeana rahani, yule muweka rahani anaposhindwa kulipa kile kitu chake kinachukuliwa na yule ambaye rahani iko kwake. Iwapo kilichowekwa rahani ni kitu kama matunda au mtoto, basi yule aliyeweka rahani ndiye anayelazimika kusimamia matumizi ya alichoweka rahani ili kiendeleo kuishi.

[11] Ikiwa mdaiwa ametoa faida aliyoipata pamoja na ile fedha aliyokopa si vibaya ni halali kwa mkopeshaji kuchukua. Ama ikiwa mkopeshaji ameweka sharti mkopo urejeshwe na ziada inachukuliwa kama ribaa nayo ni haraam. Kurudisha kilichokua kizuri inaruhusiwa na ni halali kwa mkopeshaji lakini ikilazimishwa kurejesha ziada pamoja na mali aliyokopa ni ribaa na ni haraam. Hadiyth hii yaonesha tabia njema na huwa haihesabiwi kuwa ni mkopo wenye nyongeza, kwa sababu wakati wa kutolewa haukuwa umewekewa sharti. Ni mwenyewe aliyekopa kwa furaha yake anamtunukia zawadi mkopeshaji.

06-Mlango Wa Kufilisiwa Na Kuzuwia (Kutumia Mali)

بَابُ التَّفْلِيسِ وَالْحَجْرِ

06-Mlango Wa Kufilisiwa Na Kuzuwia (Kutumia Mali)

727.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {مَنْ أَدْرَكَ مَالَهُ بِعَيْنِهِ عِنْدَ رَجُلٍ قَدْ أَفْلَسَ، فَهُوَ أَحَقُّ بِهِ مِنْ غَيْرِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَرَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَمَالِكٌ: مِنْ رِوَايَةِ أَبِي بَكْرٍ بْنِ عَبْدِ الرَّحْمَنِ مُرْسَلًا بَلْفَظٍ: {أَيُّمَا رَجُلٍ بَاعَ مَتَاعًا فَأَفْلَسَ الَّذِي ابْتَاعَهُ، وَلَمْ يَقْبِضْ الَّذِي بَاعَهُ مِنْ ثَمَنِهِ شَيْئًا، فَوَجَدَ مَتَاعَهُ بِعَيْنِهِ، فَهُوَ أَحَقُّ بِهِ، وَإِنْ مَاتَ الْمُشْتَرِي فَصَاحِبُ الْمَتَاعِ أَسْوَى الْغُرَمَاءِ} وَوَصَلَهُ الْبَيْهَقِيُّ، وَضَعَفَهُ تَبَعًا لِأَبِي دَاوُدَ

وَرَوَى أَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَهَ: مِنْ رِوَايَةِ عُمَرَ بْنِ خُلْدَةَ قَالَ: أَتَيْنَا أَبَا هُرَيْرَةَ فِي صَاحِبٍ لَنَا قَدْ أَفْلَسَ، فَقَالَ: لَأَقْضِيَنَّ فِيكُمْ بِقَضَاءِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ أَفْلَسَ أَوْ مَاتَ فَوَجَدَ رَجُلٌ مَتَاعَهُ بِعَيْنِهِ فَهُوَ أَحَقُّ بِهِ} وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَضَعَفَ أَبُو دَاوُدَ هَذِهِ الزِّيَادَةَ فِي ذِكْرِ الْمَوْتِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Tulimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Atakayekuta mali yake ile ile kwa mtu aliefilisika, basi yeye ana haki zaidi[1] kuliko mwingine.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Abuu Daawuud na Maalik wameipokea kwa Riwaayah ya Abuu Bakr bin ‘Abdir-Rahmaan[2][3] ikiwa ni Mursal kwa tamshi: “Yeyote mwenye kuuza bidhaa mwenye kuinunua akafilisika wala hakumlipa chochote katika thamani yake akaikuta bidhaa yake ile ile kama ilivyo, basi yeye ana haki zaidi kuichukua. Mnunuzi akifa, mwenye bidhaa akakuta mali yake kwake ana haki zaidi ya kuichukua.”[4] [Al-Bayhaqiyy ameidhoofisha akifuata Abuu Daawuud]

Abuu Daawuud na Ibn Maajah wameipokea kutoka katika Riwaayah ya ‘Umar bin Khaldah[5] amesema: Tulimuendea Abuu Hurayrah tukiwa na sahibu yetu aliyefilisika, akasema kwa hakika nitawahukumu kwa hukumu ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ) amesema: “Mwenye kufilisika au akafa, mtu akakuta mali yake ile ile basi yeye ana haki zaidi kwa mali hiyo.”[6] Ameisahihisha Al-Haakim. Abuu Daawuud ameidhoofisha vile akaidhoofisha ziada hii inayoeleza kifo.

728.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ الشَّرِيدِ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لِيُؤَاغِدَ يُحِلُّ عِرْضَهُ وَعُقُوبَتَهُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَعَلَّقَهُ الْبُخَارِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Amr bin Ash-Shariyd[7] kutoka kwa baba yake[8] amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tajiri kuzuia haki inayofaa kutolewa inamhalalishia kuharibiwa jina na kuadhibiwa[9].”[10] [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaai na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

729.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أُصِيبَ رَجُلٌ فِي عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي ثَمَارِ ابْتِاعَهَا، فَكَثُرَ دَيْنُهُ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "تَصَدَّقُوا عَلَيْهِ" فَتَصَدَّقَ النَّاسُ عَلَيْهِ، وَلَمْ يَبْلُغْ ذَلِكَ وَفَاءَ دَيْنِهِ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ لِعُزْمَائِهِ: "خُذُوا مَا وَجَدْتُمْ، وَلَيْسَ لَكُمْ إِلَّا ذَلِكَ" رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Mtu mmoja katika zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipata hasara katika matunda aliyonunua, deni lake likazidi, akafilisika. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: "Mpeni Swadaqah, haikufikia kiasi cha kulipa deni analodaiwa. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaambia wanaomdai: "Chukueni mlichopata, hamna isipokuwa hicho tu." [11] [Imetolewa na Muslim]

730.

وَعَنْ ابْنِ كَعْبِ بْنِ مَالِكٍ، عَنْ أَبِيهِ، {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ حَجَرَ عَلَى مُعَاذٍ مَالَهُ، وَبَاعَهُ فِي دَيْنٍ

كَانَ عَلَيْهِ { رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَأَخْرَجَهُ أَبُو
دَاوُدَ مُرْسَلًا، وَرُجِّحَ

Kutoka kwa Ibn Ka'b bin Maalik[12] amehadithia kutoka kwa baba
yake[13] kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
alizuia mali ya Mu'aadh akaiuza kulipa deni analodaiwa.”
[Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy, na akaisahihisha Al-Haakim.
Abuu Daawuwd ameipokea ikiwa ni Mursal na kuipa nguvu]

731.

وَعَنِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { عُرِضْتُ عَلَى النَّبِيِّ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ أُحُدٍ، وَأَنَا ابْنُ أَرْبَعِ عَشْرَةَ
سَنَةً، فَلَمْ يُجْزَنِي، وَعُرِضْتُ عَلَيْهِ يَوْمَ الْخَنْدَقِ، وَأَنَا ابْنُ
خَمْسِ عَشْرَةَ سَنَةً، فَأَجَازَنِي { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَفِي رِوَايَةٍ لِلْبَيْهَقِيِّ: "فَلَمْ يُجْزَنِي، وَلَمْ يَرْنِي بَلَّغْتُ".
وَصَحَّحَهَا ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa Ibn 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema:
“Nilipitishwa kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) siku ya vita
vya Uhud[14] nami ni mvulana wa umri wa miaka kumi na nne
hakuniidhinisha. Nikapitishwa kwake siku ya vita vya Khandaq nami
ni mvulana wa miaka kumi na tano akaniidhinisha.”[15] [Al-
Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine ya Al-Bayhaqiyy: “...hakuniidhinisha
wala hakuniona kuwa nimebaleghe.” Ameisahihisha Ibn Khuzaymah

732.

وَعَنْ عَطِيَّةَ الْقُرَظِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {عُرِضْنَا عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ قُرَيْظَةَ، فَكَانَ مَنْ أَنْبَتَ قَتَلَ، وَمَنْ لَمْ يُنْبِتْ خُلِّيَ سَبِيلُهُ، فَكُنْتُ فِيمَنْ لَمْ يُنْبِتْ فَخُلِّيَ سَبِيلِي} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [16] Kutoka kwa ‘Atwiyyah Al-Quradhiyy[16] amesema: “Tulipitishwa kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) siku ya vita vya Quraydhwa, anauwawa aliyeota nywele (za kinena) na ambaye hajaota nywele anaachwa, mimi nilikuwa miongoni mwa ambao hawakuota nywele akaniacha.”[17] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

733.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَجُوزُ لِلْمَرْأَةِ عَطِيَّةٌ إِلَّا بِإِذْنِ زَوْجِهَا}

وَفِي لَفْظٍ: {لَا يَجُوزُ لِلْمَرْأَةِ أَمْرٌ فِي مَالِهَا، إِذَا مَلَكَ زَوْجُهَا عِصْمَتَهَا} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَصْحَابُ السُّنَنِ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb amepokea kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

(عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haifai mwanamke kutoa kitu isipokuwa kwa idhini ya mumewe.”

Katika tamshi lingine: “Haifai mwanamke kufanya lolote katika mali yake[18] endapo mumewe amemiliki hifadhi yake.”[19] [Imetolewa na Ahmad na Maimaam wa Sunan[20] isipokuwa At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Al-Haakim]

734.

وَعَنْ قَبِيصَةَ بْنِ مُخَارِقٍ الْهَلَالِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { إِنَّ الْمَسْأَلَةَ لَا تَحِلُّ إِلَّا لِأَحَدٍ ثَلَاثَةٍ: رَجُلٍ تَحْمَلُ حَمَالَةً فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ حَتَّى يُصِيبَهَا ثُمَّ يُمْسِكَ، وَرَجُلٍ أَصَابَتْهُ جَائِحَةٌ اجْتَاكَ مَالَهُ، فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ حَتَّى يُصِيبَ قِوَامًا مِنْ عَيْشٍ، وَرَجُلٍ أَصَابَتْهُ فَاقَةٌ حَتَّى يَقُولَ ثَلَاثَةً مِنْ ذَوِي الْحِجَى مِنْ قَوْمِهِ: لَقَدْ أَصَابَتْ فُلَانًا فَاقَةٌ، فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Qabiyswah bin Mukhaariq Al-Hilaaliyy[21] (رَضِيَ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah (اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Hakika kuomba si halali kwa yeyote ila kwa moja ya mambo matatu: mtu aliyechukua dhamana, hapo ni halali kwake kuomba mpaka apate kisha atajizuia, mtu iliyoangamia mali yake, ni halali kwake kuomba mpaka apate msimamo wa maisha, na mtu aliyepata na uhitaji kwa umaskini hadi watu watatu wenye busara katika jamaa zake waseme: Hakika fulani amepata umaskini. Ni halali kwake kuomba.”[22] [Imetolewa na Muslim]

[1] Hii ina maana kuwa muuzaji anaweza kuvunja mkataba na mnunuzi na kuchukuwa mali yake ikiwa mnunuzi amefilisika.

[2] Huyu ni Abuu Bakr bin ‘Abdir-Rahmaan bin Al-Haarith bin Al-Mughiyrah Al-Makhzuwm Al-Madaniy, alikuwa ni kadhi wa Madiynah. Inasemekana kuwa jina lake lilikuwa Muhammad Al-Mughiyrah au Abuu Bakr, kun-ya yake ilikuwa ni Abuu Abdir-Rahmaan. Inasemwa hali kadhalika kuwa jina lake na kun-ya yake ilikuwa sawa. Alikuwa mtu madhubuti, Mwanazuoni na mwenye taqwa. Alikuwa ni Taabi’i wa kizazi cha tatu alifariki katika ukhalifa wa Al-Waliyd bin ‘Abdil Maalik.

[3] Abuu Bakr bin ‘Abdir-Rahmaan bin Al-Haarith Al-Makhzuwm Al-Madani. Ni madhubuti, faqihi, mfanya ‘ibaadah. Alifariki mwaka wa 94 Hijriyyah.

[4] Yaani atachukua kama wale wengine wanavyochukua kulingana na mafungu yao.

[5] Huyu ni Abuu Hafsi Al-Answaar Al-Madaniy Al-Qaadhwī. Alikuwa ni mtu mwenye heshima kubwa, mkali, mwenye taqwa na mtu mwenye kutegemewa. Amepokea kutoka kwa Abuu Hurayrah na Rabiyy’a Ar-Raay amepokea kutoka kwake. Inasemekana kuwa Khaldah alikuwa ni babu yake na jina la babake lilikuwa ni ‘Abdur-Rahmaan.

[6] Ikiwa mnunuzi atafilisika baada ya kulipa kiwango cha fedha, muuzaji hana haki ya mali yote. Atachukua hisa ya mali yake tu. Mdaiwa akifa watapewa mali zao bila kujali ni mali ya nani iliyouzwa na ya nani haikuuzwa.

[7] Huyu ni Abul-Waliyd ‘Amr bin Ash-Shariyd bin Suwayd At-Thaqaaf At-Twaaif. Ni madhubuti. Abuu Ash-Shariyd ni Swahaba aliyehudhuria Bay’at Ar-Ridhwaan. Alikuwa ni Taabi’i wa kizazi cha tatu.

[8] Huyu ni Shariyd Suwayd Ath-Thaqaaf. Jina lake ni Maalik, lakini Nabiy (ﷺ) akampa jina Shariyd (aliyetoroka) baada ya kuwa mmoja wa watu wa ukoo wake, alikimbia hadi Makkah na akasilimu. Inasemekana asili yake ni kutoka Hadhramout, ila alijulikana ni wa ukoo wa Banuu Thaqaif yaani watu wa Twaaf.

[9] Ikiwa mdaiwa ana uwezo wa kulipa deni kisha asilipe kwa makusudi, kwa hali hiyo mkopeshaji ana haki ya kumfedhehesha kwa kumkashifu mbele ya kadamnasi na kisha kumfungulia mashtaka.

[10] Kumkashifu ni kusema: “Fulani amezuwia haki yangu.” Na kumuadhibu ni kumfunga.

[11] Rasuli wa Allaah (ﷺ) anakusudia kuwa hizi ni zote zilizokuwepo. Hivyo, aliwataka wadai kugawa alichomiliki sawa kwa sawa.

[12] Abuu Al-Khatwaab ‘Abdir-Rahmaan bin Ka’b bin Maalik Al-Answaar Al-Madaniy, alikuwa madhubuti na ni miongoni mwa taabi’iyna wakubwa. Inasemekana alizaliwa wakati wa Nabiy (ﷺ) na alikuwa wakati wa Khalifa Sulaymaan bin ‘Abdil-Maalik.

[13] Ka’b bin Maalik bin Abuu Ka’b Al-Answaar As-Sulami Al-Madaniy mshairi, alikuwa ni mmoja wa washairi wa Nabiy (ﷺ). Alihudhuria Bay’atul ‘Aqaba ya pili na vita vyote isipokuwa Badr na Tabuwk. Alikuwa mmoja miongoni mwa watatu ambao toba yao ilitajwa katika Suwrat At-Tawbah kwa kubaki Madiynah wakati wa vita vya Tabuwk. Inasemekana kuwa alikufa baada ya kupofuka mwaka 50 au 51 Hijriyyah akiwa na umri wa miaka 77.

[14] Siku ya Uhud alikuenda kwa Nabiy (ﷺ) kuomba ruhusa kupigana katika vita vya Uhud dhidi ya makafiri wa Makkah.

[15] Sababu ya Hadiyth hii kuwekwa hapa ni kuonesha kuwa umri wa kukalifishwa mambo ni umri wa miaka 15 na maamrisha yote ya kishariy'ah yanakuwa wajibu wakati huo. Hivyo basi ambaye hajafikia umri huu muamala wake haukubaliki kama vile kuuza, kununua n.k. isipokuwa kwa ridhaa ya wazazi wake au aliyeteuliwa kuwa msimamizi wake atazuiwa yote hayo mpaka atakapo balebhe. Vivyo hivyo jambo lingine linalotibitisha kukua kwake na kuwajibika ni kuota kwa nywele za kinenani.

[16] 'Atwiyyah Al-Quradhiyy ni Swahaba mdogo aliyeripoti Hadiyth moja tu. Huyu ni kutoka katika kabila la Baniy Quraydhwa. Yasemekana kuwa aliishi Al-Kufah ('Iraq). Ibnu 'Abdil-Barr amesema sikuweza kujua jina la baba yake. Mujaahid na wengineo wamepokea kutoka kwake.

[17] Hadiyth hii ni dalili kuwa anayemea nywele za sehemu ya siri huwa amebalebhe, yaani huchukuliwa kuwa ni mtu mzima anapitishwa hukmu zote.

[18] Mwanamke ana haki zote na mali zake bila ya ruhusa ya mumewe. Mali yake ni nini? Mahari yake, alichorithi, faida za biashara zake anazofanya mwenyewe, hizi ni mali za mke na mume hana mamlaka ya aina yoyote ile kwa mali hii. Mwanamke anaweza kumpa mumewe chochote anachotaka kumpa, na ni halali kwa mumewe. Kisa cha 'Abdullaah bin Mas-'uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) na mkewe kimetajwa huko nyuma, jambo hili lisingetokea kama mke hana haki katika mali yake.

[19] Al-Khattabi amesema: "Hadiyth hii inahimiza uhusiano bora baina ya mtu na mkewe au kwa mke ambaye akili yake haijakaa sawa, kwani imethubutu kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaambia wanawake: Toeni Swadaqah na wanawake wakatoa vipuli, mikufu n.k."

[20] Yaani walioandika vitabu vya Sunan nao ni : At-Tirmidhiy, Abuu Daawud, An-Nasaai na Ibn Maajah. Vitabu vyao ni Sunan At-Tirmidhiy, Sunan Abiy Daawud, Sunan An-Nasaai na Sunan Ibn Maajah.

[21] Qabiyswah bin Mukhaariq bin ‘Abdillaah bin Shaddaads Al-‘Amiri. Ni Swahaba. Alimtembelea Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasilimu. Katika vitabu vya Hadiyith, ana Hadiyith sita. Aliishi Al-Basra (‘Iraaq).

[22] Hadiyith ikamalizikia hivi: “Kuomba kusiko tokana na sababu hizo ni haraam ee Qabiyswa, anayekula anakula haraam.”z

07-Mlango Wa Suluhu

بَابُ الصُّلْحِ

07-Mlango wa Suluhu[1]

735.

عَنْ عَمْرِو بْنِ عَوْفٍ الْمُزَنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الصُّلْحُ جَائِزٌ بَيْنَ الْمُسْلِمِينَ، إِلَّا صُلْحًا حَرَّمَ حَلَالًا وَ أَحَلَّ حَرَامًا، وَالْمُسْلِمُونَ عَلَى شُرُوطِهِمْ، إِلَّا شَرْطًا حَرَّمَ حَلَالًا وَ أَحَلَّ حَرَامًا} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

وَأَنْكَرُوا عَلَيْهِ. لِأَنَّ رَاوِيَهُ كَثِيرَ بَنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرِو بْنِ عَوْفٍ ضَعِيفٌ. وَكَأَنَّهُ إِعْتَبَرَهُ بِكَثْرَةِ طُرُقِهِ وَقَدْ صَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ

Kutoka kwa ‘Amr bin ‘Awf Al-Muzaniyy[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Suluhu[3] inafaa baina ya Waislamu isipokuwa suluhu inayoharamisha halaal[4] au inayohalalisha haraam.[5] Waislamu wako juu ya masharti yao isipokuwa sharti inayoharamisha halaal au inayohalalisha haraam.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha]

Ulamaa wameikataa Hadiyth hii kwa sababu mpokezi wake ni Kathiyr bin ‘Abdillaah bin ‘Amr bin ‘Awf ni dhaifu.[6]

Ibn Hibbaan ameisahihisha kutoka katika Hadiyth iliyopokewa na Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ).

736.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا يَمْنَعُ جَارٌ جَارَهُ أَنْ يَغْرَزَ خَشَبَةً فِي جِدَارِهِ. ثُمَّ يَقُولُ أَبُو هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ مَا لِي أَرَاكُمْ عَنْهَا مُعْرِضِينَ؟ وَاللَّهِ لَا أَرْمِينَّ بِهَا بَيْنَ أَكْتَافِكُمْ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Jirani asimkataze jirani yake kusimamisha mbao katika ukuta wake.”[7] Kisha Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alikuwa akisema: “Mbona nawaona mumeiacha Sunnah hii? Wa-Allaahi mtaibeba baina ya mabega yenu (hata mkichukia)” [Al-Bukhaariy, Muslim]

وَعَنْ أَبِي حُمَيْدٍ السَّاعِدِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يَحِلُّ لِأَمْرِي أَنْ يَأْخُذَ عَصَا أَخِيهِ بِغَيْرِ طَيِّبِ نَفْسٍ مِنْهُ } رَوَاهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ فِي "صَحِيحَيْهِمَا"

Kutoka kwa Abuu Humayd As-Saa'idiyy[8] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah amesema: “Si halaal kwa mtu kuchukua fimbo ya nduguye bila ya nafsi yake kuridhia.”[9] [Imetolewa na Ibn Hibbaan na Al-Haakim katika Swahiyh zao]

[1] Suluhu ni kuweka muafaka baina ya watesi wawili, kama vile mtu kudai haki ya mwengine kwa kuamini kuwa yeye ndiye mwenye haki kuliko mwingine.

[2] Huyu ni ‘Abdullaah ‘Amr bin ‘Awf bin Zayd bin Milha Al-Muzaniyy (kutoka katika kabila la Muzaynah), ni babu wa Kathiyr bin ‘Abdillaah. Alisilimu mapema, alihuduria Badr na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimpa mamlaka ya kusimamia Msikiti wa Madiynah. Alikuwa ni mwenye taqwa na mwenye kububujikwa na machozi katika ‘Ibaadah. Ni Swahaba, alifariki katika utawala wa Mu’aawiyah.

[3] Katika lugha ya kiarabu Sulhu ina maana ya amani. Kuna aina nyingi za suluhu kama vile suluhu baina ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu, suluhu baina ya mke na mume, suluhu baina ya serikali na waasi, magomvi ya kibiashara na suluhu za mambo ya fedha. Katika Hadiyth hii inakusudiwa aina hii ya mwisho ya suluhu. Migogoro ya kifedha ina mikataba ambayo ni halaal na kuna isiyokuwa halaal na masharti ya mikataba yenyewe.

[4] Msingi wa mwanzo muhimu wa mkataba ni kuwa isiwe kinyume na shariy'ah na isibadilishe haraam kuwa halaal na halaal kuwa haraam. Kama vile kusuluhisha juu ya kuchukua mali isiyo halali kwake.

[5] Kama vile kumtaka mume asilale kwa mke wa pili.

[6] Ash-Shaafi na Abuu Daawuud wamemtaja kuwa ni “Msingi wa uongo”. Ahmad amesema: “Hadiyth zake ni Munkar.” An-Nasaaiy naye amemzungumzia kwa kusema: “Haaminiki” na Ibn Hibbaan amesema: “Ana kitabu cha Hadiyth alichokitunga akisingizia kuwa amepokea kutoka kwa baba yake nae kutoka kwa babu yake.”

[7] Shariy'ah imejali maingiliano ya kijamii na kuiwekea miongozo kama hili la jirani kuweka mbao kuegemea ukuta wa jirani yake.

[8] Huyu ni Abuu Humayd As-Saa'idiyy. Jina lake ni Al-Mundhir bin Sa'd. alihudhuria vita vya Uhud na vilivyofuatia baada yake, aliishi hadi mwaka wa 60 Hijriyyah.

[9] Hadiyth hii ni dalili kuwa ni haraam kuchukua mali ya Muislamu hata ikiwa ni kidogo kiasi gani ila kwa radhi yake.

08-Mlango Wa Hawala Na Dhamana

بَابُ الْحَوَالَةِ وَالضَّمَانِ

08-Mlango Wa Hawala[1]Na Dhamana[2]

738.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَطْلُ الْغَنِيِّ ظُلْمٌ، وَإِذَا أَتَبِعُ أَحَدَكُمْ عَلَى مَلِيٍّ فَلْيَتَّبِعْ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَفِي رِوَايَةِ أَحْمَدَ: {فَلْيَحْتَلْ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuchelewesha tajiri (kulipa deni) ni dhulma. Na mmoja wenu atakapofuatishwa kwa mwenye uwezo na afuate.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

739.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {تُوفِّيَ رَجُلٌ مِنَّا، فَغَسَّلْنَاهُ، وَحَنَطْنَاهُ، وَكَفَّنَاهُ، ثُمَّ أَتَيْنَا بِهِ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقُلْنَا: تُصَلِّيْ عَلَيْهِ؟ فَخَطَا خُطًى، ثُمَّ قَالَ: "أَعْلَيْهِ دَيْنٌ؟" قُلْنَا: دِينَارَانِ، فَأَنْصَرَفَ، فَتَحَمَّلَهُمَا أَبُو قَتَادَةَ، فَأَتَيْنَاهُ، فَقَالَ أَبُو قَتَادَةَ: الدِّينَارَانِ عَلَيَّ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "أَحِقَّ الْغَرِيمُ وَبَرَى مِنْهُمَا الْمَيِّتُ؟" قَالَ: نَعَمْ، فَصَلَّى عَلَيْهِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Alikufa mtu miongoni mwetu, tukamuosha, tukamtia dawa na tukamkafini, kisha tukamuendea Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) tukamuambia: Utamswalia? Akaenda hatua chache akasema: Ana

deni? Tukasema: Ana deni la dinari mbili. Akaondoka. Abuu Qataadah akabeba deni lile (akalidhamini) tukamuendea Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), Abuu Qataadah akamuambia: zile dinari mbili juu yangu. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Haki ya mdai (kulipwa) na je maiti ameepukana nayo? Akasema ndio. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamswalia.”[3] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na [An-Nasaa'iy](#), na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

740.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ كَانَ يُؤْتَى بِالرَّجُلِ الْمُتَوَفَّى عَلَيْهِ الدِّينُ، فَيَسْأَلُ: "هَلْ تَرَكَ لِدِينِهِ مِنْ قَضَاءٍ؟ " فَإِنْ حَدَّثَ أَنَّهُ تَرَكَ وَفَاءً صَلَّى عَلَيْهِ، وَإِلَّا قَالَ: "صَلُّوا عَلَى صَاحِبِكُمْ" فَلَمَّا فَتَحَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْفُتُوحَ قَالَ: "أَنَا أَوْلَى بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنْفُسِهِمْ، فَمَنْ تُوَفِّي، وَعَلَيْهِ دَيْنٌ فَعَلِي قَضَاؤُهُ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَفِي رِوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: {فَمَنْ مَاتَ وَلَمْ يَتْرُكْ وَفَاءً {

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa analetewa mtu aliyekufa anayedaiwa Anauliza: Ameacha cha kulipa deni lake? Akiambiwa kuwa ameacha[4] humswalia, la si hivyo alikuwa akisema Mswalieni Swahibu yenu. Allaah alipomfungulia alikuwa akisema: Mimi ni aula kwa Waumini kuliko nafsi zao, atakayekufa

ilhali anadaiwa basi ni juu yangu kulipa deni lake.”[5] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Bukhaariy: “Atakayekufa na hakuacha cha kulipia deni lake...”

741.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا كَفَالَةَ فِي حَدٍّ } رَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna udhamini katika hadd (adhabu).”[6] [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy kwa Isnaad dhaifu]

[1] Hawala ina maana mbili: Ya kwanza ni mtu kumhakikishia tajiri kuwa deni lake litarudi. Hii inaruhusiwa kishariy’ah. Ya pili ni kuhamisha deni kutoka katika dhima ya mmoja hadi kwa mwingine.

[2] Dhamana ni kujitwika deni la mwenye kudaiwa.

[3] Ina maana kuwa deni au haki yoyote ya mwanadamu, haitosamehewa mpaka lilipwe au lisamehewe na mhusika. Hata baada ya kifo chake deni bado linasimama pale pale. Kadhalika tunajifunza katika Hadiyth hii mtu kumdhamini deni la maiti hata kama si jamaa yake.

[4] Yaani ameacha mali ya kutosha.

[5] Ni juu yangu kulilipa haikuwa na maana mali yake binafsi Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Wakati huo hazina ya dola ilikuwa chini ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ndio maana akasema: “Ni juu yangu kumlipia.” Jukumu hili lilikuja kuhamia kwa mkuu wa nchi kama Hadiyith nyingine itakayokuja kufafanua. Hadiyith hii imefuta Hadiyith iliyotangulia. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa hana uwezo alikuwa hamswalii maiti anayedaiwa kwa sababu Swalaah yake ni Shafaa (maombezi) inayokubaliwa moja kwa moja. Lakini alipopata uwezo jukumu la madeni lilikuwa juu yake. Na katika utawala wa Kiislamu kiongozi anawajibika kumlipia maiti deni lake, asipofanya hivyo dhambi ni zake.

[6] Huduwd: adhabu iliyowekwa na Shariy’ah katika Uislam. Hakuna dhamana katika huduwd. Kwa mfano, hakutakiwi kuwepo na dhamana kwa wizi, uzinzi, kumkashifu mtu na ulevi. Kuna sababu nyingi kwa nini hairuhusiwi dhamana kwa makosa haya:

- i. kimsingi dhamana hutumika kutilia nguvu ushahidi, wakati katika utekelezaji wa huduwd, jambo la msingi ni kuwepo kwa ushahidi dhidi ya mtuhumiwa inadhoofishwa na mashtaka yaende kwa mtuhumiwa.
- ii. Dhamana huchelewesha maamuzi, na hakuna hakika kuwa mtuhumiwa atathibitika katika utuhumiwa wake na ataadhibiwa. Ikiwa tuhuma itathibitika, hivyo basi hakuna haja ya maombi ya msamaha wa huduwd.
- iii. Mdhamini anatakiwa amlete mdhaminiwa kwenye hukumu mahakamani; kutokuwepo kwa mtuhumiwa majukumu yake atabebeshwa mdhamini. Hata hivyo adhabu za huduwd zinatekelezwa kwa mhalifu na sio kwa mtu mwingine yeyote. Hadiyith hii ingawa Isnaad yake ni dhaifu lakini maana yake ni sahihi kwa ‘Ulamaa. Iwapo kutakuwepo na udhamini katika adhabu anayopewa mtu bila shaka shariy’ah za adhabu zitabatilika.

09-Mlango Wa Ushirika Na Wakala

بَابُ الشَّرِكَةِ وَالْوَكَالَةِ

09-Mlango Wa Ushirika[1] Na Uwakala[2]

742.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { قَالَ اللَّهُ: أَنَا ثَالِثُ الشَّرِيكَيْنِ مَا لَمْ يَخُنْ أَحَدُهُمَا صَاحِبَهُ، فَإِذَا خَانَ خَرَجْتُ مِنْ بَيْنَهُمَا } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah amesema: Mimi ni wa Tatu wa washirika wawili madamu mmoja wao hajakhini mwenzake, atakapomkhini Nitatoka baina yao.”[3] [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Al-Haakim]

743.

وَعَنْ السَّائِبِ بْنِ يَزِيدَ الْمَخْزُومِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُ كَانَ شَرِيكَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَبْلَ الْبَعْثَةِ، فَجَاءَ يَوْمَ الْفَتْحِ، فَقَالَ: " مَرْحَبًا بِأَخِي وَشَرِيكِي } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ

Kutoka kwa As-Saaib bin Yaziyda Al-Makhzuwmiyy[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Yeye alikuwa ni mshirika wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kabla ya Unabii akamuambia: karibu ndugu

yangu na mshirika wangu.”[5] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na Ibn Maajah]

744.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {إِشْتَرَكْتُ أَنَا وَعَمَّارٌ وَسَعْدٌ فِيمَا نُصِيبُ يَوْمَ بَدْرٍ..} الْحَدِيثُ. رَوَاهُ النَّسَائِيُّ وَغَيْرُهُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mas‘uud (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilishirikiana mimi, ‘Ammar na Sa’d katika tulichopata siku ya vita vya Badr.” Hadi mwisho wa Hadiyth [Imetolewa na An-Nasaaiy]

745.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {قَالَ: أَرَدْتُ الْخُرُوجَ إِلَى خَيْبَرَ، فَأَتَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: "إِذَا أَتَيْتَ وَكِيلِي بِخَيْبَرَ، فَخُذْ مِنْهُ خَمْسَةَ عَشَرَ وَسَقًا} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nilitaka kuenda Khaybar nikamuendea Nabi (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) nikamueleza akasema: Utakapomuendea wakala wangu Khaybar chukua wasaki (kapu) kumi na tano (tende) kutoka kwake.” [6] [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha]

746.

وَعَنْ عُرْوَةَ الْبَارِقِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بَعَثَ مَعَهُ بَدِينَارٍ يَشْتَرِي لَهُ أُضْحِيَّةً.. } الْحَدِيثَ. رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ فِي أَثْنَاءِ حَدِيثٍ، وَقَدْ تَقَدَّمَ

Kutoka kwa ‘Urwah Al-Baariqiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimpa dinari (moja) kununulia udhw-hiyyah.” Mpaka mwisho wa Hadiyth [Imetolewa na Al-Bukhaariy na imetangulia][7]

747.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { بَعَثَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عُمَرَ عَلَى الصَّدَقَةِ.. } الْحَدِيثَ. مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuchukua Zakaah.” Mpaka mwisho wa Hadiyth [Al-Bukhaariy, Muslim][8]

748.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَحَرَ ثَلَاثًا وَسِتِّينَ، وَأَمَرَ عَلِيًّا أَنْ يَذْبَحَ الْبَاقِيَ } الْحَدِيثُ. رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alichinja (ngamia) sitini na tatu akamuamrisha ‘Aliy[9] kuwachinja waliobakia (thelathini na saba).” Mpaka mwisho wa Hadiyth [Imetolewa na Muslim]

749.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي قِصَّةِ الْعَسِيفِ. قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { وَاعْدُ يَا أُنَيْسُ عَلَى امْرَأَةٍ هَذَا، فَإِنْ اعْتَرَفَتْ فَأَرْجُمَهَا.. } الْحَدِيثُ. مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema katika kisa cha muajiriwa kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ee Ubays nenda kwa mke wa bwana huyu, akikiri kosa umpige mawe...”[10] mpaka mwisho wa Hadiyth [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Ushirika ni muafaka baina ya washirika katika asili ya mali na faida. Katika Hadiyth hii kuna dalili kuswihi ushirika katika kuchuma na ushirika huu unaitwa ushirika wa kiwiliwili (Shirkat Al-Abdaan). Ushirika uko katika mafungu manne.

[2] Wakala ni kumpa mtu unaibu atakayekuwa badala yake katika majukumu yake kama vile kuuza, kununua na mfano wake.

[3] Hii ina maana kuwa ushirika wa mali na fedha ni jambo lililoruhusiwa, la kuzingatia ni uaminifu. Ushirika wenye uaminifu ndani yake huleta faida, uaminifu unapoondoka hasara huingia kwa washirika.

[4] Ibn Jawziy ametaja katika At-Taliqiyb jina lake lilikuwa As-Saaib bin ‘Aaidh Al-Makhzuwmiyy. Ibn ‘Abdil-Barr amesema alikuwa miongoni mwa Al-Muallafatul-Quluwb na aliposilimu alikuwa Muislamu mzuri. Ni Swahaba, aliishi hadi katika zama za ukhalifa wa Mu’aawiyah.

[5] Ushirika ulikuwepo hapo kabla na Uislamu ukauielekeza vizuri.

[6] Ina maana mtu anaweza kumuweka wakala wake katika mambo ya fedha. Kuna Hadiyth nyingine ambayo Jaabir anamuuliza Nabiyy (ﷺ) amjibu nini mtu anayemtaka asimamie ukusanyi wa tende. Nabiyy (ﷺ) akamuambia aweke mkono katika mti wa mtende wa anayemuomba, wakati huo Rasuli wa Allaah (ﷺ) alishakuwa na wakala wake. Wasaki 15 ni kilo 2145.

[7] Tazama Hadiyth ya 686.

[8] Hadiyth inamalizikia hivi: Akaambiwa: “Ibn Jamiyl, Khaalid ibn Waliyd na Al ‘Abbaas ami yake Nabiyy (ﷺ) wamezuia (Zakaah). Rasuli wa Allaah (ﷺ) akasema: Ibn Jamiyl hawezi kukataa isipokuwa alikuwa fukara Allaah (Subhaanahu wa Ta’aalaa) Akamtajirisha. Ama Khaalid, nyinyi mnamdhulumu Khaalid. Hakika aliziweka zana zake za kivita katika njia ya Allaah. Ama Al-‘Abbaas [Zakaah](#) yake ninayo mimi na mfano wake.” Kisha akasema: Ee ‘Umar kwani hujui kuwa ami ya mtu ni mfano wa baba yake?” Katika Hadiyth hii muna dalili ya kiongozi kumwakilisha mtu kuchukua Zakaah.

[9] Ina maana kumpa wakala mtu achinje Udhwhiyya (mnyama) ni jambo linalokubalika kishariy’ah

[10] Hii ni dalili nyingine ya kuruhusu uwakala hata katika huduwd. Hadiyth hii ni dalili kuwa anayeamrisha ni wakala wa kiongozi katika kutekeleza hadd (adhabu). Unays ni wakala katika kuhakiki madai ya zinaa, tena ni wakala katika kutekeleza adhabu.

10-Mlango Wa Iqrari (Kukiri Kosa)

بَابُ الْإِقْرَارِ

10-Mlango Wa Iqrari[1] (Kukiri Kosa)

750.

عَنْ أَبِي ذَرٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ لِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {قُلِ الْحَقُّ، وَلَوْ كَانَ مُرًّا} صَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ فِي حَدِيثٍ طَوِيلٍ

Kutoka kwa Abuu Dharr[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameniambia: “Sema haki japo ni chungu.” [Kaisahihisha Ibn Hibbaan kutoka Hadiyth ndefu]

[1] Iqraar ni kuthibitisha kitu fulani, kulingana na Istwilaah ya kishariy’ah ni mtu kukubali aliyoyafanya. Ni kinyume na kukana au kukataa.

[2] Jina lake ni Jundub bin Junaadah, ni Swahaba alisilimu kitambo, imepokewa kuwa yeye alisema: “Mimi ni mtu wa tano katika Uislam.” Hupigiwa mfano katika ukweli, naye ndiye wa kwanza aliyemuamkia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) maakizi ya Kiislamu. Alifariki mwaka wa 32 Hijriyyah. Katika vitabu vya Hadiyth, ana Hadiyth 281.

11-Mlango Wa Kuazima

بَابُ الْعَارِيَةِ

11-Mlango Wa Kuazima[1]

751.

عَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { عَلَى الْيَدِ مَا أَخَذْتُ حَتَّى تُؤَدِّيَهُ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Samurah bin Jundub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ni wajibu wa mkono kwa ulichokichukua hadi ukirudishe.”[2] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha Al-Haakim]

752.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَدَّ الْأَمَانَةَ إِلَى مَنْ أَنْتَمَنَّاكَ، وَلَا تَخُنْ مَنْ خَانَكَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَاسْتَنْكَرَهُ أَبُو حَاتِمٍ الرَّازِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tekeleza amana kwa aliyekuamini, wala usimkhini aliyekukhini.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, na At-Tirmidhiy na amesema ni Hassan, na akaisahihisha Al-Haakim, na ameona ni Munkar (Hadiyth iliokataliwa) Abuu Haatim Ar-Raaziyy]

753.

وَعَنْ يَعْلَى بْنِ أُمَيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {إِذَا أَتَيْتَ رُسُلِي فَأَعْطِهِمْ ثَلَاثِينَ دِرْعًا}، قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَعَارِيَّةٌ مَضْمُونَةٌ أَوْ عَارِيَّةٌ مُؤَدَّاءُ؟ قَالَ: بَلْ عَارِيَّةٌ مُؤَدَّاءُ {رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ya'laa bin Umayyah[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Utakapojiwa na wajumbe wangu, wape deraya (nguo za kivita) thelathini. Nikasema Ee Rasuli wa Allaah! Ni za kuazima zilizodhaminiwa[4] ama ni za kuazima na kurudisha kama kawaida? Akasema: Ni za kuazima na kurudishwa kama kawaida.” [Imetolewa

na Ahmad, Abuu Daawuud na An-Nasaa'iy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

754.

وَعَنْ صَفْوَانَ بْنِ أُمَيَّةَ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ
اسْتَعَارَ مِنْهُ دُرُوعًا يَوْمَ حُنَيْنٍ. فَقَالَ: أَغْصَبُ يَا مُحَمَّدُ؟
قَالَ: بَلْ عَارِيَةٌ مَضْمُونَةٌ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ،
وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ .

وَأَخْرَجَ لَهُ شَاهِدًا ضَعِيفًا عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ

Kutoka kwa Swafwaan bin Umayyah[5] amesema kuwa: “Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliazima kwake deraya siku ya vita
vya Hunayn, akasema: Je unaninyang’anya ee Muhammad? Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Bali ni kuazima kwa
dhamana.”[6] [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaa'iy na
akaisahihisha Al-Haakim]

Na akaishuhudisha kwa Hadiyith dhaifu kutoka kwa Ibn ‘Abbaas

755.

عَنْ سَعِيدِ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { مَنْ اقْتَطَعَ شِبْرًا مِنَ الْأَرْضِ ظُلْمًا
طَوَّقَهُ اللَّهُ إِيَّاهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مِنْ سَبْعِ أَرْضِينَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Sa'iyd bin Zayd[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kukata shubiri moja ya ardhi kwa dhulma, Allaah atamvisha shingoni mwake siku ya Qiyaamah ardhi saba.”[8] [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Katika lugha ya kiarabu مَضْمُونَةُ الْعَارِيَةِ (Al-‘aariyah Madhwmuwnah) ni mkopo uliodhaminiwa na عَارِيَةٌ مُؤَدَّاءٌ (‘Aariyah Muaddah) ni kilichoazimwa (kisicho na dhamana). Kuhusu ya mwanzo ni kuwa dhamana ni muhimu. Jaalia mtu anachukua mkopo wenye dhamana na kilichoazimwa kikaharibika ikiwa kwa aliyekiazima, kilichokubaliwa ni kuwa muazimaji atalipa thamani yake, na ndio maana ikaitwa ‘Aariyah Madhwmuwnah. Hata hivyo ikiwa mtu ataazima kwa kuaminiwa kama ilivyo ‘Aariyah Muaddah (kisichokuwa na dhamana) na kitu chenyewe kikaharibika kwa aliyekiazima (bila uzembe kutoka kwake) hatotakiwa kulipa.

[2] Umetajwa “mkono” lakini makusudio ni mtu. Yaani aliyeazima kitu anawajibika kukirudisha alichokichukua hata kama ni kwa gharama. Hadiyth hii ni dalili kuwa ni wajibu mtu kurudisha mali ya mwenyewe ima kama aliazimia au kwa njia nyingine.

[3] Huyu ni Ya’laa bin Umayyah bin Abiy ‘Ubaydah At-Tamiym. Mama yake anaitwa Mun-yah, kwa hivyo huitwa Ibn Mun-yah. Ni Swahaba mashuhuri, alifariki baada ya mwaka wa 40 Hijriyyah.

[4] Vilivyoazimwa kwa dhamana uharibifu wake utalipwa na mwenye kuazima. Kuazima ni kumruhusu mtu kutumia mali ya mwingine, au faida ya kitu kile, na baada ya kutumia kukirejesha kwa mwenyewe. Lakini katika viazimwavyo ni vitu, hakuna mtu kuazima mkewe. Pia haifai mtu kuazima kitu ili akitumie katika kufanyia kitu cha haraam.

[5] Huyu ni Swafwaan bin Umayyah bin Khalaf bin Wahb Al-Qurayshiy Al-Jumahi Al-Makkiy, ni Swahaba alikuwa miongoni mwa watukufu wa ki

Quraysh. Alikimbia siku ya Fat-hi Makkah (Ukombozi wa Makkah), akapewa Amani, akarudi. Alihudhuria pamoja na Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ) vita vya Hunayn na vita vya Twa'if akiwa ni kafiri, kisha akasilimu, na akawa Muislamu bora. Alifariki siku za mauaji ya 'Uthmaan

[6] Ikiwa mtu ameazima kitu na kikaharibika kwa bahati mbaya, muazimaji hatogharamia kwa hilo, lakini ikithibitika kuwa uharibifu huo ni wa makusudi au ni matokeo ya uzembe wake basi atatakiwa kulipa.

[7] Jina lake ni Sa'iyd bin Zayd bin 'Amr bin Nufayl bin 'Abdul 'Uzza bin Riyaah Al-Qurayshi Al-'Adawi na ukoo wake unakutana na ule wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kwa Ka'b bin Luay. Ni mmojawapo katika waliobashiriwa Jannah, 'Umar bin Al-Katwaab (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) alikuwa ami yake upande wa kuumeni, kwa sababu 'Amr bin Nufayl babake Sa'iyd na Al-Katwaab bin Nufayl babake 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) walikuwa ndugu. Sa'iyd (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) alikuwa mume wa Faatwimah dada yake 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ), alikua chachu iliyomsaidia kumsilimisha 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ) na dada yake Sa'iyd 'Atikah alikuwa mke wa 'Umar (رَضِيَ اللهُ عَنْهُ). Alijulikana kwa jina Sa'iyd kabla ya kuja kwa Uislamu na baada ya kusilimu. Sa'iyd alikuwa katika Muhajirina wa mwanzo.

[8] Hii ina maana ya kupora ardhi ya mtu ni katika madhambi makubwa. Kupora ardhi ya mtu maana yake ni kuichukuwa na kuanza kuilima.

12- Mlango Wa Kuniyang'anya

بَابُ الْغَضَبِ

12-Mlango Wa Kuniyang'anya[1]

756.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ كَانَ عِنْدَ بَعْضِ نِسَائِهِ، فَأَرْسَلَتْ إِحْدَى أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ مَعَ خَادِمٍ لَهَا بِقِصْعَةٍ فِيهَا طَعَامٌ، فَكَسَرَتْ الْقِصْعَةَ، فَضَمَّهَا، وَجَعَلَ فِيهَا الطَّعَامَ. وَقَالَ: " كُلُوا " وَدَفَعَ الْقِصْعَةَ الصَّحِيحَةَ لِلرَّسُولِ، وَحَبَسَ الْمَكْسُورَةَ { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ .
وَالْتِّرْمِذِيُّ، وَسَمَّى الضَّارِبَةَ عَائِشَةَ، وَزَادَ: فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { طَعَامٌ بِطَعَامٍ، وَإِنَاءٌ بِإِنَاءٍ } وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa yuko kwa baadhi ya wakeze, mmoja wa Mama wa Waumini akamtuma mtumishi wake sahani yenye chakula akapiga ile sahani kwa mkono akavunja.[2] Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akavikusanya vipande vile akaweka chakula ndani yake, akasema: Kuleni.[3] Akachukua sahani nzima akampa yule mtumishi, ile iliyovunjika akaizuia.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na At-Tirmidhiy akamtaja aliyepiga ni ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) na akaongeza: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Chakula kwa chakula na chombo kwa chombo.”[4] Ameisahihisa.

757.

وَعَنْ رَافِعِ بْنِ خَدِيجٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ زَرَعَ فِي أَرْضٍ قَوْمٍ بغيرِ إِنْهُمْ، فَلَيْسَ لَهُ مِنَ الزَّرْعِ شَيْءٌ، وَلَهُ نَفَقَتُهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيُّ، وَحَسَنُهُ التِّرْمِذِيُّ. وَيُقَالُ: إِنَّ الْبُخَارِيَّ ضَعَّفَهُ

Kutoka kwa Raafi' bin Khadiyj[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Mwenye kulima katika ardhi ya watu bila ruhusa yao hana haki yoyote katika mazao, na gharama ni yake." [6] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba'ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy, na At-Tirmidhiy akasema ni Hassan] Yasemekana kuwa Al-Bukhaariy ameidhoofisha

758.

وَعَنْ عُرْوَةَ بْنِ الزُّبَيْرِ قَالَ: قَالَ رَجُلٌ مِنَ الصَّحَابَةِ، مِنْ أَصْحَابِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ رَجُلَيْنِ اخْتَصَمَا إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي أَرْضٍ، غَرَسَ أَحَدُهُمَا فِيهَا نَخْلًا، وَالْأُخْرَى لِلْآخَرِ، فَقَضَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بِالْأَرْضِ لِصَاحِبِهَا، وَأَمَرَ صَاحِبَ النَّخْلِ أَنْ يُخْرِجَ نَخْلَهُ. وَقَالَ: "لَيْسَ لِعِرْقٍ ظَالِمٍ حَقٌّ" رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ. وَآخِرُهُ عِنْدَ أَصْحَابِ "السُّنَنِ" مِنْ رِوَايَةِ عُرْوَةَ، عَنْ سَعِيدِ بْنِ زَيْدٍ

وَاخْتَلَفَ فِي وَصْلِهِ وَإِرْسَالِهِ، وَفِي تَعْيِينِ صَحَابِيَّهِ

Kutoka kwa ‘Urwah bin Az-Zubayr[7] amesema: Mmoja wa Maswahaba wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alihadithia: “Watu wawili waligombana na kuenda kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika ardhi ambayo mmojawapo aliolesha mtende kuhusu ardhi ya mwingine. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akahukumu kuwa ardhi ni ya mwenyewe, akamuarisha mwenye mtende kutoa mtende wake na akasema: “Mmea uliopanda kwa dhulma hauna haki.”[8] [Imetolewa na Abuu Daawud na Isnaad yake ni Hassan]

Mwisho wa Hadiyih inapatikana katika vitabu vya As-Sunan, kutoka kwa ‘Urwah naye kutoka kwa Sa’iyd bin Zayd. Hata hivyo wametofautiana ikiwa ni Mawsuwl (iliyounga) au ni Mursal (iliyoishia kwa Taabi’) kadhalika na jina Swahaba aliyesikia na kupokea kutoka kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

759.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ، رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: فِي خُطْبَتِهِ يَوْمَ النَّحْرِ بِمَنَى {إِنَّ دِمَاءَكُمْ وَأَمْوَالَكُمْ وَأَعْرَاضَكُمْ عَلَيْكُمْ حَرَامٌ، كَحُرْمَةِ يَوْمِكُمْ هَذَا، فِي بَلَدِكُمْ هَذَا، فِي شَهْرِكُمْ هَذَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema katika khutbah yake ya siku ya Nahr alipokuwa Minaa alisema: “Hakika damu zenu na mali yenu ni haraam juu yenu kama uharamu wa siku yenu hii, katika mwezi wenu huu katika mji wenu huu.”[9] [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] **الْغَضَبِ** (Al Ghaswb) ina maana ya kuchukua mali ya mtu kwa nguvu bila ridhaa yake.

[2] Alifanya hivyo kwa sababu ya wivu ikiwa wanawake wana wivu na waume wa kawaida.

[3] Akiwaambia wale aliokuwa nao.

[4] Kuna tofauti ya rai baina ya Wanazuoni, ikiwa kimeharibika au kuvunjika kwa aliyekiazima, itabidi alipe thamani yake au kukibadilisha na mfano wake. Hii inahusu vitu vinavyoweza kutiwa thamani tu. Ama vinginevyo lazima virudishwe vilivyo. Hadiyth hii inatilia mkazo vitu kurudishwa kama vilivyo.

[5] Raafi' bin Khadij, Abuu 'Abdillaah, Al-Khazraj Al-Answaariy. Ni mwenyeji wa Madiynah. Hakupigana katika vita vya Badr kwa sababu alikuwa na umri mdogo, lakini alihudhuria vita vya Uhud na vilivyofuatia. Alifariki mwaka wa 73 Hijriyyah.

[6] Ikitokezea mtu akalima shamba la mtu ya ruhusa ya mwenye shamba, hana haki ya mazao yake. Kikubwa anachoweza kudai ni gharama ya mbegu alizotia, na mazao yatakuwa ni ya mwenye kumiliki shamba.

[7] Huyu ni Abuu 'Abdillaah 'Urwah bin Az-Zubayr bin Al-'Awwaam bin Khuwayldi Al-Asad Al-Madaniy. Ni katika Mafuqahaa (Ulamaa wa Shariy'ah) saba wa Madiynah, na ni mmojawapo wa 'Ulamaa wa kitabi'iyna. Alikuwa ni mtu madhubuti amepokea Hadiyth kutoka kwa baba yake, mama yake, Khalati yake ambaye ni 'Aaishah Ummul-Mu-uminiyna (Mama wa Waumini), 'Aliy, Muhammad bin Maslamah na Abuu Hurayrah. Ibn Sa'd amesema: "Ni madhubuti na ana Hadiyth nyingi, Faqihi, Mwanachuoni, thabiti, muaminiwa." Alikuwa akisoma robo ya Qur-aan kila usiku (yaani juzuu saba na nusu). Alizaliwa mwanzoni mwa ukhalifa wa 'Umar katika mwaka wa 23 Hijriyyah. Alifariki mwaka 94 Hijriyyah.

[8] Neno ظَالِمٍ (Dhwaalim) ni neno lenye maana mbaya sana, hapa ina maana ni mtu muovu, asiye na uadilifu. Hadiyth hii ni dalili kuwa anayetumia ardhi ya mwenyewe, ima kwa kupanda mimea, kujenga au kwa jambo lingine, anawajibika kutoa na kubomoa alichojenga, na gharama za kubomoa ni juu yake huyu mnyang'anyi. Lakini ile mimea na majengo ni mwenyewe (mwenye ardhi).

[9] Hadiyth hii imetajwa hapa kuwa kupora mali ya Muislam ni haraam. Na jambo hili limekubaliwa na Wanazuoni wote.

13-Mlango Wa Ash-Shuf'ah (Shufaa)

بَابُ الشُّفْعَةِ

13-Mlango Wa Ash-Shuf'ah (Shufaa)[1]

760.

عَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {قَضَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بِالشُّفْعَةِ فِي كُلِّ مَا لَمْ يُقَسَمْ، فَإِذَا وَقَعَتِ الْحُدُودُ وَصُرِفَتْ الطُّرُقُ فَلَا شُفْعَةَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ .

وَفِي رِوَايَةٍ مُسْلَمٍ: {الشُّفْعَةُ فِي كُلِّ شِرْكَ: أَرْضٌ، أَوْ رَبْعٌ،
أَوْ حَائِطٌ، لَا يَصْلُحُ أَنْ يَبِيعَ حَتَّى يَعْرِضَ عَلَى شَرِيكِهِ}
وَفِي رِوَايَةِ الطَّحَاوِيِّ: {قَضَى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
وَسَلَّمَ بِالشُّفْعَةِ فِي كُلِّ شَيْءٍ} وَرَجَالُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alihukumu shufaa
katika kila mali isiyogawanywa. Itakapowekwa mipaka na njia
zikabainishwa hakuna shufaa.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili
ni la Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Shufaa katika kila ushirika, iwe
ardhi, nyumba ya kuishi na bustani hairuhusiwi.” Katika tamshi
linguine: “si halali (kuzuza mshirika) mpaka amfahamishe mshirika
mwenzake.”

Katika Riwaayah nyingine ya Atw-Twahaawiyy imesema: “Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amehukumu shufaa katika kila kitu.”
Wapokezi wake ni madhubuti.

761.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {جَارُ الدَّارِ أَحَقُّ بِالدَّارِ} رَوَاهُ
النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَلَهُ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema “Jirani wa
nyumba ana haki zaidi ya (kununua) nyumba.” [Imetolewa na An-
Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan lakini ina ila]

762.

وَعَنْ أَبِي رَافِعٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْجَارُ أَحَقُّ بِصَقْبِهِ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ، وَفِيهِ قِصَّةٌ

Kutoka kwa Abuu Raafi' (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Jirani wa nyumba ana haki zaidi kwa nyumba.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy. Hadiyth hii ina kisa chake][2]

763.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْجَارُ أَحَقُّ بِشُفْعَةِ جَارِهِ، يُنْتَظَرُ بِهَا وَإِنْ كَانَ غَائِبًا إِذَا كَانَ طَرِيقُهُمَا وَاحِدًا} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Jirani ana haki zaidi kwa shufaa ya jirani yake atamngojea hata kama hayuko iwapo njia yao ni moja.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba'ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) wapokezi wake ni madubuti (thiqah)]

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الشُّفْعَةُ كَحَلِّ الْعِقَالِ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ وَالْبَزَّازُ، وَزَادَ: "وَلَا شُفْعَةَ لِغَائِبٍ" وَإِسْنَادُهُ ضَعِيفٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Shufaa ni kama kufungua kamba (inayomzuia ngamia).”[3] [Imetolewa na Ibn Maajah na Al-Bazaar akaongezea: “...wala hakuna shufaa kwa asiyekuwepo.” Na Isnaad yake ni dhaifu]

[1] الشُّفْعَةُ (Ash-Shuf’ah) shufaa ni mshirika kuchukua hisa ya mshirika mwenzake ambayo ameiua kwa thamani yake aliyouzia nayo mshirika. uzindushi: Kuna tofauti baina ya Ash-Shufa’ah (shufaa) na Ash-Shafaa’ah (shafaa) na Ash-shifaa’ah. Shufaa ni hii tuliyoieleza. Shafaa ni kuombea mtu msamaha. Shifaa ni poza.

[2] Kisa chenyewe ni hiki: kuwa Abuu Raafi’ akiwa pamoja na Miswaar bin Makhrama alimkabili Sa’d ibn Abii Waqqaasw na kumuaridhia kumuuzia nyumba yake iliyokuwa jirani yake na nyumba ya Sa’d. Miswaar aliongea na Sa’d kuhusu jambo hilo. Sa’d alikubali kulipa Dinari mia nne (sarafu za dhahabu) kwa ajili ya nyumba ya Abuu Raafi’. Alikuwa tayari kulipa malipo ya mara moja au ya kidogo kidogo kama alivyotaka Abuu Raafi’. Aliposikia hivi Abuu Raafi’ akasema hakuuza nyumba hizi kwa fedha alizoahidiwa Dinari mia tano taslimu kwa sababu alimsikia Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema kuwa majirani wana haki zaidi kuliko wengine. Akasema vile vile lau angelisikia kabla asingeuza nyumba zake kwa bei ile.

[3] حَلَّ الْعِقَالِ (Hallil-‘Iqaal) ina maana muda tu magoti ya ngamia yatakapofunguliwa, wakati huo mara moja huamka. Hivyo hivyo, muda wa kuwa nyumba ishauzwa, au mtu ana haki kufahamu kuwa mwenzake

anauza kitu naye asiharakishe mpaka ukapita muda mrefu basi hapo haki yake ya shufaa imeanguka. Na hii ndio maana ya msemu wa Hallil-‘Iqaal kawaida ya kufungua kamba hakuchukui muda mrefu.

14- Mlango Wa Qiraadhw

بَابُ الْقِرَاضِ

14-Mlango Wa Qiraadhw[1]

765.

عَنْ صُهَيْبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {ثَلَاثٌ فِيهِنَّ الْبَرَكَهَةُ: الْبَيْعُ إِلَى أَجَلٍ، وَالْمُقَارَضَةُ، وَخَلْطُ الْبُرِّ بِالشَّعِيرِ لِلْبَيْتِ، لَا لِلْبَيْعِ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Swuhayb[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mambo matatu ndani yake kuna Baraka: kuuza kwa muda maalumu, Muqaaradhwah na kuchanganya ngano na shayiri[3] kwa matumizi ya nyumbani si kwa kuuza.” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa Isnaad dhaifu]

وَعَنْ حَكِيمِ بْنِ حِزَامٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ كَانَ يَشْتَرِطُ عَلَى الرَّجُلِ إِذَا أَعْطَاهُ مَالًا مُقَارَضَةً: أَنْ لَا تَجْعَلَ مَالِي فِي كَيْدِ رَطْبَةٍ، وَلَا تَحْمِلْهُ فِي بَحْرٍ، وَلَا تَنْزِلَ بِهِ فِي بَطْنٍ مَسِيلٍ، فَإِنْ فَعَلْتَ شَيْئًا مِنْ ذَلِكَ فَقَدْ ضَمِنْتَ مَالِي} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَرَجَالُهُ ثِقَاتٌ

وَقَالَ مَالِكٌ فِي "الْمَوْطَأِ" عَنْ الْعَلَاءِ بْنِ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ يَعْقُوبَ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ: {أَنَّهُ عَمِلَ فِي مَالٍ لِعُثْمَانَ عَلَى أَنْ الرِّبْحَ بَيْنَهُمَا} وَهُوَ مَوْقُوفٌ صَحِيحٌ

Kutoka kwa Hakiym bin Hizaam (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Alikuwa anampa mtu masharti anapompa mali kwa Muqaaradhwah akimuambia: Usifanyie biashara mali yangu katika viumbe vyenye uhai, wala usiibebe baharini, wala usiteremke nayo maporomoko ya mito; utakapofanya hivyo utaidhamini mali yangu.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy na wapokezi wake ni madhubuti]

Maalik amesema katika kitabu chake “Al-Muwatwa” kutoka kwa Al-‘Alaa[4] bin ‘Abdir-Rahmaan bin Ya’quwb naye kutoka kwa baba yake[5] kutoka kwa babu yake[6]: “Kwamba yeye alifanyia biashara mali ya ‘Uthmaan kwa sharti ya kugawana faida baina yao.”[7] Hadiyth hii ni Mawquwf.

[1] Qiraadhw na Muqaaradhw yote ni majina ya kitu kimoja; ni mtu ampe mwenzie mali afanyie biashara na mwingine atatoa nguvu za kufanyia kazi, faida itakayopatikana watagawana, kama washirika. Kama kutakuwa na hasara, itaangukia katika rasilimali aliyotoa muekezaji. Kwa jina lingine huitwa Mudhwaarabah.

[2] Huyu ni Abuu Yahya Swuhayb bin Sinaan bin Maalik Ar-Rumi, Abuu Yahya. Alikuwa mwarabu wa kabila la An-Nimir bin Qaasitw bin Waail ambaye alichukuliwa mateka na Waroma na ndipo alipopata jina Ar-Rumi, akakulia kwao, na akawa miongoni mwao. Inasemekana kuwa alipobaleghe na kuwa mkubwa alikimbia na kurudi Makkah na akawa katika wafuasi wa ‘Abdullaah bin Jad’an. Inasemekana kuwa mmoja katika watu wa kabila la Baniy Kalb alimnunua na akamleta Makkah. ‘Abdullaah bin Jad’an akamnunua. Swuhayb alikuwa Swahaba mkubwa ambaye alisilimu mapema, alipata mateso kwa ajili ya dini yake. Alihamia Madiynah na kufariki Madiynah mwaka wa 38 Hijriyyah.

[3] Shayiri: nafaka inayofanana na ngano inayotumika kwa chakula.

[4] Huyu ni Abuu Sibli Al-‘Alaa bin ‘Abdir-Rahmaan bin Ya’quwb Al-Juhani, muachwa huru wa Al-Huraaqa Al-Madaniy. Alikuwa katika Taabi’iyna maarufu wa kizazi cha tano. Alikuwa ni mkweli lakini alikuja kuchanganyikiwa kuhusu Hadiyth. Ahmad na wengineo wanaithibitisha uaminifu wake. Al-Waaqidi anasema kuwa alikufa wakati wa ukhalifa wa Al-Manswuwr.

[5] ‘Abdur-Rahmaan bin Ya’quwb Al-Juhani alikuwa miongoni mwa Taabi’iyna na alikuwa katika kizazi cha tatu. Alichukua Hadiyth za Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kutoka kwa baba yake, Abuu Hurayrah na Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy.

[6] Ya’quwb Al-Juhani alikuwa ni muachwa huru wa Al-Huraaqa na alikuwa kiongozi katika kizazi cha pili katika Taabi’iyna. Aliishi wakati wa ‘Umar bin Al-Khatwaab na miongoni mwa wapokezi wachache wa Hadiyth

[7] Al-Mudhwaarabah au Al-Qiraadhw ni aina za mikataba. Ambayo fidia inasamehewa kwa watu. Kama hasara inatokana na uzembe au makossa ya mfanyakazi, atawajibika kwa hilo. Vinginevyo, hawajibiki. Hivyo hivyo, kutekeleza kinyume na maagizo au maelekezo ya muekezaji, mshirika katika biashara atawajibika na hasara iliyotokea.

15-Mlango Wa Kumwagilia Musaaqaah Na Kukodisha

بَابُ الْمُسَاقَاةِ وَالْإِجَارَةِ

15-Mlango Wa Kumwagilia Musaaqaah[1] Na Kukodisha[2]

767.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَامَلَ أَهْلَ خَيْبَرَ بِشَطْرِ مَا يَخْرُجُ مِنْهَا مِنْ ثَمَرٍ، أَوْ زَرْعٍ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

وَفِي رِوَايَةٍ لَهُمَا: فَسَأَلُوا أَنْ يُقَرَّ هُمْ بِهَا عَلَى أَنْ يَكْفُوا عَمَلَهَا وَلَهُمْ نِصْفُ الثَّمَرِ، فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نُقِرْكُمْ بِهَا عَلَى ذَلِكَ مَا شِئْنَا، فَقَرُّوا بِهَا، حَتَّى أَجَلَاهُمْ عُمَرُ

وَلِمُسْلِمٍ: { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ دَفَعَ إِلَى يَهُودِ خَيْبَرَ نَخْلَ خَيْبَرَ وَأَرْضَهَا عَلَى أَنْ يَغْتَمِلُوهَا مِنْ أَمْوَالِهِمْ، وَلَهُ شَطْرُ ثَمَرِهَا }

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliamiliana na watu wa Khaybar (Mayahudi) kwa makubaliano kuwa atapewa nusu ya kitakachotoka humo kutokana na matunda au mazao.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Katika Riwaayah yao nyingine: “... (Mayahudi) Wakamuomba Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) awaache waishi (Khaybar) kwa sharti walime mali na yao iwe nusu ya tende. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Tumewaruhusu muishi kwa sharti hiyo mpaka tutakapotaka.” Akawaruhusu kuishi humo mpaka ‘Umar alipowafukuza’

Katika Riwaayah ya Muslim: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwapa Mayahudi wa Khaybar mitende ya Khaybar na ardhi ya huko kwa sharti walime kwa mali yao nao wapate nusu ya matunda yake.”[3]

768.

وَعَنْ حَنْظَلَةَ بْنِ قَيْسٍ قَالَ: {سَأَلْتُ رَافِعَ بْنَ خَدِيجٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ كِرَاءِ الْأَرْضِ بِالذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ؟ فَقَالَ: لَا بَأْسَ بِهِ، إِنَّمَا كَانَ النَّاسُ يُؤَاجِرُونَ عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَلَى الْمَادِيَّاتِ، وَأَقْبَالِ الْجَدَاوِلِ، وَأَشْيَاءَ مِنَ الزَّرْعِ، فَيَهْلِكُ هَذَا وَيَسْلَمُ هَذَا، وَيَسْلَمُ هَذَا وَيَهْلِكُ هَذَا، وَلَمْ يَكُنْ لِلنَّاسِ كِرَاءٌ إِلَّا هَذَا، فَلِذَلِكَ زَجَرَ عَنْهُ، فَأَمَّا شَيْءٌ مَعْلُومٌ مَضْمُونٌ فَلَا بَأْسَ بِهِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ .

وَفِيهِ بَيَانٌ لِّمَا أُجْمِلَ فِي الْمُتَّفَقِ عَلَيْهِ مِنْ إِطْلَاقِ النَّهْيِ عَنْ
كَرَاءِ الْأَرْضِ

Kutoka kwa Handhwalah bin Qays[4] amesema: “Nilimuuliza Raafi’ bin Khadiyj (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) juu ya kuikodisha ardhi kwa dhahabu na fedha. Akasema: “Hapana ubaya. Kwani watu walikuwa wakiajiriana wakati wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) sehemu zilizopo juu ya mito mikubwa na katika vianzio vya mito midogo na kwa sehemu ya mazao. Basi sehemu moja inaangamia,[5] na sehemu nyingine ikisalimika, na sehemu hii ikisalimika nyingine inaangamia. Watu walikuwa hawana upangaji isipokuwa huu. Kwa ajili hiyo kakataza. Ama kikikodishwa kwa kitu chenye kujulikana na chenye dhamana basi hakina ubaya.” [Imetolewa na Muslim]

Haya yanathibitisha yaliyokumuishwa katika Al-Bukhaariy na Muslim katika uharamu wa kukodisha ardhi.

769.

وَعَنْ ثَابِتِ بْنِ الضَّحَّاكِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ الْمُزَارَعَةِ وَأَمَرَ بِالْمُوَاجَرَةِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ أَيْضًا

Kutoka kwa Thaabit bin Adhw-Dwahhaak[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza Muzaara’ah[7] na akaamrisha kuajiriana.”[8] [Imetolewa na Muslim]

770.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّهُ قَالَ: {إِخْتَجَمَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَأَعْطَى الَّذِي حَجَمَهُ أَجْرَهُ} وَلَوْ كَانَ حَرَامًا لَمْ يُعْطِهِ. رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliumika na akampa muumikaji ujira wake.” Lau ingalikuwa haraam basi asingalimpa. [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

771.

وَعَنْ رَافِعِ بْنِ خَدِيجٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {كَسَبُ الْحَجَّامِ خَبِيثٌ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Raafi’ bin Khadiyj (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Chumo la muumikaji ni chafu.”[9] [Imetolewa na Muslim]

772.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {قَالَ اللَّهُ (عَزَّ وَجَلَّ) ثَلَاثَةٌ أَنَا خَصْمُهُمْ

يَوْمَ الْقِيَامَةِ: رَجُلٌ أُعْطِيَ بِي ثُمَّ غَدَرَ، وَرَجُلٌ بَاعَ حُرًّا ،
فَأَكَلَ ثَمَنَهُ، وَرَجُلٌ اسْتَأْجَرَ أَجِيرًا ، فَاسْتَوْفَى مِنْهُ، وَلَمْ يُعْطِهِ
أَجْرَهُ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah (عَزَّ
وَجَلَّ) amesema: Watu watatu Mimi ni Mtesi wao siku ya
Qiyaamah: mtu ametoa kwa jina Langu kisha akahini, mtu anamuiza
muungwana na akala thamani yake, na mtu amemuajiri muajiriwa
naye akamkamilishia kazi yake wala hakumpa ujira wake.”[10]
[Imetolewa na Muslim]

773.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { إِنَّ أَحَقَّ مَا أَخَذْتُمْ عَلَيْهِ حَقًّا كِتَابُ اللَّهِ }
أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika cha haki
zaidi mliochukua malipo juu yake ni Kitabu cha Allaah.”[11]
[Imetolewa na Al-Bukhaariy]

774.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَعْطُوا الْأَجِيرَ أَجْرَهُ قَبْلَ أَنْ يَجِفَّ عَرَقُهُ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ

وفي الباب: عن أبي هريرة رضي الله عنه عند أبي يعلى والبيهقي. وجابر عند الطبراني، وكلها ضعاف

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mumpeni muajiriwa malipo yake kabla jasho lake kukauka.”[12] [Imetolewa na Ibn Maajah]

Katika mlangu huu kuna Hadiyth iliyopokewa na Abuu Hurayrah iliyo kwa Abuu Ya’laa na Bayhaqiyy na iliyopokewa kutoka kwa Jaabir iliyo kwa Atw-Twabaraaniy, Riwaayah zote ni dhaifu.

775.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ اسْتَأْجَرَ أَجِيرًا، فَلْيُسَلِّمْ لَهُ أَجْرَتَهُ} رَوَاهُ عَبْدُ الرَّزَّاقِ وَفِيهِ انْقِطَاعٌ، وَوَصَلَهُ الْبَيْهَقِيُّ مِنْ طَرِيقِ أَبِي حَنِيفَةَ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuajiri muajiriwa amkabidhi malipo yake.”[13] [Imetolewa na ‘Abd Ar-Razzaaq, na Isnaadi yake ni Munqatwi’ (imekatika). Na Al-

Bayhaqiyy ameipokea kwa Isnaadi Mawsuwl (iliyounga) kutoka kwa Abuu Haniyfah.

[1] Kumpa mtu kazi ya kumwagilia mti na kuusimamia na kupata malipo katika hilo huitwa Musaaqaah. Kwa jina lingine huitwa Muzaara'ah. Tofauti baina ya Musaaqaah na Muzaara'ah ni kuwa Musaaqaah ni kwa miti ya matunda, wakati Muzaara'ah ni kwa ajili ya nafaka

[2] Kumfanya mtu awe ni mshirika wa faida au kodi inaitwa Ijaarah.

[3] Hadiyth hii inatoa dalili y akuwepo kwa Musaaqaah na Muzaara'ah.

[4] Hanthwalah bin Qays Az-Zurqi Al-Answaar, ni miongoni mwa watu madhubuti Madiynah, na ni katika tabi'iyna wadogo.

[5] Ina maana ya kuwa ardhi ya chini inaweza kuchukuliwa na mafuriko na ardhi ya miinuko ikasalimika na wakati wa ukame ardhi ya chini karibu na maji ikasalimika na ardhi ya kwenye miinuko ikaangamia.

[6] Thaabit bin Adhw-Dwahaak Al-Answaar, Abuu Zayd, naye ni katika walioshuhudia Bay'at Ar-Ridhwaan, alikuwa Hudaybiyah mwaka wa sita Hijriyyah. Alifariki katika balaa ya 'Abdullaah bin Az-Zubayr yakaribia mwaka wa 70 Hijriyyah.

[7] Katika kiarabu Muzaara'ah ni kumpa mtu shamba alime malipo yake ni baadhi ya kitakachovunwa. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakukataza hili, bali ardhi ilipokuwa ndogo kwa Answaar na Muhajiriyna walipoongezeka kwa njia ya dharura walilima ardhi kadiri walivyoweza na akawafundisha kuwa wasigawane mazao kwa njia ya ushirika wa Muzaara'ah bali wakodishe kwani Ijaarah inawapunguzia uzito kwa wapangaji au wakodishaji.

[8] Jina lililotumika Al-Ijaarah lina maana ya kukodisha ardhi kwa muda maalum, jambo ambalo ni la halaal.

[9] Kiarabu neno khabiyth lina maana ya tabia mbaya lakini haina maana ya haraam. Wakati mwingine linatumika kama lina maana ya istiara kwa maana ya bakhili.

[10] Hadiyth hii imehimiza kulipa mishahara kwa wakati wake kwa mfanyakazi. Siku hizi watu wengi wanakuwa siyo waadilifu katika miamala yao na si waaminifu katika malipo yao.

[11] Hadiyth hii inaeleza kwa uwazi kupokea ujira au mishahara kwa kufundisha kitabu cha Allaah na Hadiyth ni halaal. Mwalimu anayefundisha watu kusoma au kuhifadhi Qur-aan anayo haki ya kuchukua malipo.

[12] Ina maana ujira na mashahara kwa mfanyakazi lazima ilipwe mapema. Ambaye hatolipa malipo ya mfanyakazi Allaah atamuadhibu siku ya hukumu.

[13] Ina maana ya kuwa ujira kwa mfanyakazi ushughulikiwe mapema ili kuondosha migogoro. Vivyo hivyo, katika mas-ala kama Mudhwaarabah, Salaam, Muzaara'ah, Muwaajarah, n.k. kanuni ile ile iliyotekelezwa na shariy'ah lazima ifanye kazi na watu wote watekeleze na kufuata.

16-Mlango Wa Kufufua Ardhi Iliyokufa

بَابُ إِحْيَاءِ الْمَوَاتِ

16-Mlango Wa Kufufua Ardhi Iliyokufa[1]

776.

عَنْ عُرْوَةَ، عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ عَمَرَ أَرْضاً لَيْسَتْ لِأَحَدٍ، فَهُوَ أَحَقُّ بِهَا} قَالَ عُرْوَةُ: وَقَضَى بِهِ عُمَرُ فِي خِلَافَتِهِ. رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Urwah naye kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuamrisha (kuendeleza) ardhi isiyo na mwenyewe, basi mtu huyo ana haki zaidi katika ardhi hiyo.” ‘Urwah amesema: ‘Umar alihukumu hukumu hii katika Ukhalifa wake. [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

777.

وَعَنْ سَعِيدِ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ أَحْيَا أَرْضاً مَيْتَةً فَهِيَ لَهُ} رَوَاهُ الثَّلَاثَةُ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ.

وَقَالَ: رُوِيَ مُرْسَلًا. وَهُوَ كَمَا قَالَ، وَاخْتُلِفَ فِي صَحَابِيِّهِ، فَقِيلَ: جَابِرٌ، وَقِيلَ: عَائِشَةُ، وَقِيلَ: عَبْدُ اللَّهِ بْنُ عَمْرٍو، وَالرَّاجِحُ الْأَوَّلُ

Kutoka kwa Sa’iyd bin Zayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuimarisha ardhi iliyokufa, ardhi hiyo ni yake.”[2] [Imetolewa na

Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na At-Tirmidhiy akaipa daraja ya Hassan]

Akisema kuwa imepokewa ikiwa ni Mursal. Hata hivyo hakuna makubaliano kuhusu Maswahaba waliosikia Hadiyth hii kutoka kwa Nabiyy (ﷺ). Inasemekana kuwa ni Jaabir, ‘Aaishah au ‘Abdullaah bin ‘Amr na kauli yenye nguvu ni ya kwanza yaani Jaabir.

778.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ، أَنَّ الصَّعْبَ بْنَ جَثَّامَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَخْبَرَهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا حِمَى إِلَّا لِلَّهِ وَلِرَسُولِهِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas amesema Asw-Swa’b bin Jath-thaamah (ﷺ) alimueleza kuwa Nabiyy (ﷺ) amesema: “Hakuna himaya[3] isipokuwa ya Allaah na Nabiyy Wake.”[4] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

779.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا ضَرَرَ وَلَا ضِرَارَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَابْنُ مَاجَةَ .

وَلَهُ مِنْ حَدِيثِ أَبِي سَعِيدٍ مِثْلُهُ، وَهُوَ فِي الْمُوطَأِ مُرْسَلٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halaal kudhuriana wala kulipiziana madhara.”[5] [Imetolewa na Ahmad na Ibn Maajah]

Kadhalika Ibn Maajah ameripoti Hadiyth mfano wa hii kutoka kwa Abuu Sa’iyd. Hadiyth hii inapatikana katika Muwatwa ikiwa ni Hadiyth Mursal

780.

وَعَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ أَحَاطَ حَائِطًا عَلَى أَرْضٍ فَهِيَ لَهُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْجَارُودِ

Kutoka kwa Samurah bin Jundub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuzungusha ukuta katika ardhi yoyote (ardhi tupu), ardhi hiyo ni yake.”[6] [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Al-Jaaruwd]

781.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مُغَفَّلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ حَفَرَ بَيْرًا فَلَهُ أَرْبَعُونَ ذِرَاعًا عَطْنَا لِمَاشِيَّتِهِ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mughaffal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuchimba kisima basi ana dhira arubaini kwa ajili ya wanyama wake[7] (karibu na maji).” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa Isnaad dhaifu]

782.

وَعَنْ عَلْقَمَةَ بْنِ وَائِلٍ، عَنْ أَبِيهِ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَقْطَعَهُ أَرْضًا بِحَضْرَمَوْتِ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَالتِّرْمِذِيُّ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Alqamah bin Waail[8] naye kutoka kwa baba yake amesema kuwa: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimkatia kipande cha ardhi[9] Hadhwramawt (Yemen).” [Imetolewa na Abuu Daawud na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

783.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَقْطَعَ الزُّبَيْرَ حُضْرَ فَرَسِهِ ، فَأَجْرَى الْفَرَسَ حَتَّى قَامَ ، ثُمَّ رَمَى سَوْطَهُ. فَقَالَ: " أَعْطُوهُ حَيْثُ بَلَغَ السَّوْطُ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَفِيهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimkatia ardhi Az-Zubayr

kiasi cha kuruka farasi wake, akamkimbiza farasi mpaka akasimama kisha (Az-Zubayr) akarusha mjeledi wake, Nabi (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ) akasema:[10] Mpeni (kipande cha ardhi) hadi ulipofika mjeledi.”[11] [Imetolewa na Abuu Daawuud na katika Isnaad yake kuna udhaifu]

784.

وَعَنْ رَجُلٍ مِنَ الصَّحَابَةِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { غَزَوْتُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَسَمِعْتُهُ يَقُولُ: النَّاسُ شُرَكَاءُ فِي ثَلَاثٍ: فِي الْكَلَاءِ ، وَالْمَاءِ ، وَالنَّارِ } رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَأَبُو دَاوُدَ ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

Mtu mmoja katika Maswahaba amesema: “Nilipigana Jihaad pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) nikamsikia anasema: “Watu ni washirika katika mambo matatu: Majani, maji na moto.” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud na wapokezi wake ni madhubuti]

[1] Neno Al-Mawaat nimelitafsiri kwa ‘ardhi iliyokufa’, lakini makusudio ni ardhi ambayo haijaimarishwa, au ardhi isiyo na mmiliki wala hakuna anayenufaika nayo.

[2] Ina maana ya kuwa yeyote atakayelima katika ardhi tupu, basi ni yake, maadamu kuwa ardhi hiyo si miliki ya Muislamu au Dhimmi (asiyekuwa Muislamu anayeishi katika nchi ya Kiislamu). Baadhi ya Wanazuoni wana mtazamo kuwa kuomba ruhusa serikali husika nalo ni jambo la lazima, kwa wengine sivyo.

[3] Wakati wa Jaahiliyya ilikuwa ni ada mkuu wa ukoo au kabila kutenga ardhi yenye rutuba kulishia mifugo yao. Jambo hili limekatazwa katika Uislamu. Hata hivyo, kiongozi au mkuu wa nchi anaweza kutenga ardhi kama Swadaqah katika njia ya Allaah. Ardhi iliyotolewa Swadaqah kwa kulishia mifugo ni ya Allaah na Nabiyy wake. Mkuu wa nchi hawezi kutumia ardhi hii kwa maslahi yake au mifugo yake.

[4] Hima ni ardhi ambayo si milki ya mtu. Kiongozi wa Waislamu huwa anaizuwia kwa ajili ya maslahi fulani kama vile kuwalisha wanyama wa Zakaah na kwa dharura nyinginezo.

[5] Katika lugha ya kiarabu Dhawraar ina maaana ya kumdhuru na kumuumiza mwingine pasina haki, na Dhawraar ni kulipa kisasi kwa aliyeanza kukudhuru. Hadiyyth hii ni kanuni ya msingi. Shariyy'ah haitaki kudhuru au kudhuriwa kwa yeyote. Mbali na haya kuna maelezo mengi kuhusu Hadiyyth hii. Mifano ni mingi katika maisha yetu ambayo watu kwa makusudi wamedhamiria kuwaudhi wenzao mara kwa mara.

[6] Kwa ajili ya ujengaji wa nyumba, kuzungushia ukuta kwa kadiri ya uchache wa futi tatu kuenda juu inathibitisha kuwa ni aliyefanya hivyo, muda wa kuwa ardhi hiyo haina mwenyewe. Hata hivyo, kuthibitisha uhalali wa ardhi ya kilimo ni kwa kulima.

[7] Yaani atakayechimba kisima kwa maslahi ya watu, Shariyy'ah inamruhusu kuwa na nafasi ya dhiraa arubaini kuzunguka kisima kwa ajili ya mifugo yake.

[8] Huyu ni 'Alqamah bin Waail bin Hujr Al-Hudhrami Al-Kufi, alipokea Hadiyyth hii kutoka kwa baba yake na kwa Al-Mughniyah.

[9] Hii ina maana katika dola ya Kiislamu inaruhusiwa kukata kipande cha ardhi kumpa mtu fulani. Kuna aina mbili za hali hii: kutoa kama milki yake na kuruhusu kutumia ardhi kwa muda fulani.

[10] Hapa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akizungumza na wale aliokuwa nao pamoja.

[11] Dola kutoa zawadi au hiba kwa mtu aliyeutumikia Uislamu na Ummah wake, inaruhusiwa na ni halaal kishariy'ah maadamu kuwa ardhi hiyo si milki ya mtu binafsi. Ama mtu kuzawadiwa kwa kusaliti akipewa na dola isiyokuwa ya Kiislamu ni haraam.

17-Mlango Wa Waqf

بَابُ الْوَقْفِ

17-Mlango Wa Waqf[1]

785.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { إِذَا مَاتَ الْإِنْسَانُ انْقَطَعَ عَنْهُ عَمَلُهُ إِلَّا مِنْ
ثَلَاثٍ: صَدَقَةٍ جَارِيَةٍ ، أَوْ عِلْمٍ يُنْتَفَعُ بِهِ، أَوْ وَلَدٍ صَالِحٍ يَدْعُو
لَهُ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:
“Mwanadamu akifa amali yake hukatika ila kwa mambo matatu:
Swadaqah inayoendelea, na ilmu inayonufaisha, au mtoto mwema
anayemuomba du'aa.” [Imetolewa na Muslim]

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {أَصَابَ عُمَرُ أَرْضًا
بِخَيْرٍ ، فَاتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَسْتَأْمِرُهُ
فِيهَا ، فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ ! إِنِّي أَصَبْتُ أَرْضًا بِخَيْرٍ لَمْ
أَصِبْ مَالًا قَطُّ هُوَ أَنفَسُ عِنْدِي مِنْهُ قَالَ: " إِنْ شِئْتَ حَبَسْتَ
أَصْلَهَا ، وَتَصَدَّقْتَ بِهَا " . قَالَ: فَتَصَدَّقَ بِهَا عُمَرُ ، غَيْرَ أَنَّهُ
لَا يُبَاعُ أَصْلُهَا ، وَلَا يُورَثُ ، وَلَا يُوهَبُ ، فَتَصَدَّقَ بِهَا فِي
الْفُقَرَاءِ ، وَفِي الْقُرْبَى ، وَفِي الرِّقَابِ ، وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ ، وَابْنِ
السَّبِيلِ ، وَالضَّيْفِ ، لَا جُنَاحَ عَلَى مَنْ وَلِيَهَا أَنْ يَأْكُلَ مِنْهَا
بِالْمَعْرُوفِ ، وَيُطْعِمَ صَدِيقًا { غَيْرَ مُتَمَوِّلٍ مَالًا مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ ،
وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ .

وَفِي رَوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: {تَصَدَّقْ بِأَصْلِهِ ، لَا يُبَاعُ وَلَا يُوهَبُ ،
وَلَكِنْ يُنْفَقُ ثَمَرُهُ}

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Umar
alipata ardhi huko Khaybar. Akamuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ)
(وَالِإِلَهِ وَسَلَّمَ) akimuomba amri na ushauri katika ardhi hiyo.
Akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Nimepata ardhi Khaybar, sijawahi
kupata mali iliyo nzuri zaidi kwangu kuliko hiyo (utaniamuru
nifanyeje?). Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema:
“Ukipenda, uizuie waqf asili yake na uitoe swadaqah yake.” ‘Umar
(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) akaitoa swadaqah isipokuwa asili yake haiuzwi
wala hairithiwi wala haitolewi hiba. ‘Umar akalitoa swadaqah kwa
mafukara, jamaa zake wa karibu, watumwa na katika Njia ya Allaah,

msafiri na mgeni. Hapana ubaya kwa anayelisimamia kula ndani yake kwa wema na amlishe rafiki ila asilimbikize mali kwa ajili yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Katika Riwaayah nyingine ya Al-Bukhaariy imesema: “Akatoa swadaqah asili yake, lakini kwa sharti isiuzwe[2] wala kutolewa kama hiba ila matunda yake hutolewa (kugawiwa watu).”

787.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {بَعَثَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عُمَرَ عَلَى الصَّدَقَةِ . . } الْحَدِيثُ ، وَفِيهِ: {وَأَمَّا خَالِدٌ فَقَدْ احْتَبَسَ أَدْرَاعَهُ وَأَعْتَادَهُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma ‘Umar kuchukua Zakaah...” mpaka mwisho wa Hadiyth inasesema: “(Nabiy akasema): ...ama Khaalid[3] ametoa Waqf deraya na zana zake za vita katika njia ya Allaah...”[4] [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Waqf ni ile hali ya kuweka mali au feda na kuizuia kwa ajili ya kutumika kwa maslahi ya Ummah, na kubakia asili yake katika uangalizi na siyo kuuzwa, kurithi au kutoa zawadi. Huku ni kama vile mtu kutoa nyumba au sehemu yake kulipia mahitaji ya Msikiti.

[2] Waqf hairuhusiwi kuuzwa. Mdhamini wa Waqf anaweza kuchukua kiasi kidogo cha kuikimu familia yake.

[3] Huyu ni Abuu Sulaymaan Khaalid bin Al-Waliyd bin Al-Mughiyrah Al-Makhzuwm Al-Qurayshi. Mama yake akiitwa Asmaa alikuwa Lubaabah mdogo mtoto wa Al-Haarith na dada wa Ummul-Fadhl. Khaalid alisilimu mwaka wa 8 Hijriyyah kabla ya ufunguzi wa Makkah. Inasemekana vile vile kuwa alisilimu mwaka wa 5 au wa 6 Hijriyyah. Alishiriki katika ufunguzi wa Makkah katika vita vya Hunayn na Tabuwk. Panga tisa zilikatika mkononi mwake alipokuwa akipigana katika vita vya Mu'ta, wakati huo ndipo Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipompa jina la 'Upanga wa Allaah'. Abuu Bakr alimtuma kupigana katika vita vya Ar-Ridda (walioritadi), na baada ya hapo akavamia Fursi. Alitumwa Shaam na akateka ardhi nyingi huko na akaendelea kubaki huko hadi ukhalifa wa 'Umar akiwa kamanda mkuu wa majeshi ya Kiislam Shaam, 'Umar bin Al-Khatwaab alimuzulu Khaalid. Baada ya hapo Khaalid alikuwa ni muangalizi wa kujitolea wa mji wa Hims hadi alipofariki mwaka wa 21 Hijriyyah, alizikwa katika kijiji kimoja umbali wa maili moja nje ya mji wa Hims.

[4] 'Umar alidhanja kuwa Khaalid alibaki na deraya kwa ajili ya kufanyia biashara. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimjulisha 'Umar kuwa Khaalid alizitoa deraya kama zile kama Waqf kwa njia ya Allaah.

18- Mlango Wa Kutoa Hiba

بَابُ الْهَبَةِ

18-Mlango Wa Kutoa Hiba[1]

عَنْ النُّعْمَانَ بْنِ بَشِيرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ أَبَاهُ أَتَى بِهِ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: {إِنِّي نَحَلْتُ ابْنِي هَذَا غُلَامًا كَانَ لِي، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " أَكُلْتُ وَلَدَكَ نَحَلْتَهُ مِثْلَ هَذَا " ؟. فَقَالَ: لَا . فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " فَارْجِعْهُ " }

وَفِي لَفْظٍ: {فَانْطَلَقَ أَبِي إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ لِيُشْهَدَهُ عَلَى صَدَقَتِي. فَقَالَ: " أَفَعَلْتَ هَذَا بِوَلَدِكَ كُلَّهُمْ " ؟. قَالَ: لَا. قَالَ: " اتَّقُوا اللَّهَ، وَاعْدِلُوا بَيْنَ أَوْلَادِكُمْ " فَارْجَعَ أَبِي، فَرَدَّ تِلْكَ الصَّدَقَةَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ قَالَ: {فَأَشْهَدُ عَلَى هَذَا غَيْرِي" ثُمَّ قَالَ: " أَيْسُرُكَ أَنْ يَكُونُوا لَكَ فِي الْبِرِّ سَوَاءً " ؟ قَالَ: بَلَى . قَالَ: " فَلَا إِذَا }

Kutoka kwa An-Nu'maan bin Bashiyr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa baba yake alienda naye kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Mimi nimempa zawadi mtoto wangu huyu mtumwa aliyekuwa wangu. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Watoto wako wote umewazawadia kama hivyo? Akasema: Hapana. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Irudishe.”

Katika tamshi nyingine inasema: “Baba yangu akaenda kwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ili amshuhudishe swadaqah yangu. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Umfanya hivi

kwa wanao wote? Akasema hapana. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Mcheni Allaah na mfanye uadilifu baina ya watoto wenu.[2] Baba yangu akarejea na akairudisha swadaqah hiyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine ya Muslim: “Mshuhudishe jambo hili asiyekuwa mimi. Kisha akasema: Unapendezewa watoto wako wote wakufanyie wema kwa usawa? Akasema: Ndiyo. Akasema: Basi usifanye hivyo.”

789.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْعَائِدُ فِي هَبْتِهِ كَالْكَلْبِ يَقِيءُ، ثُمَّ يَعُودُ فِي قَيْئِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رَوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: {لَيْسَ لَنَا مَثَلُ السَّوِّءِ، الَّذِي يَعُودُ فِي هَبْتِهِ كَالْكَلْبِ يَرْجِعُ فِي قَيْئِهِ}

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayeirudia hiba yake[3] ni kama mbwa anayetapika na kuyarudia matapishi yake.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Al-Bukhaariy inasema: “Sisi hatuna mfano mbaya, ambaye anayerudia hiba yake ni kama mbwa, anatapika kisha anarudia matapishi yake.”[4]

790.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ، وَابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَحِلُّ لِرَجُلٍ مُسْلِمٍ أَنْ يُعْطِيَ الْعَطِيَّةَ، ثُمَّ يَرْجِعَ فِيهَا، إِلَّا الْوَالِدُ فِيمَا يُعْطِي وَلَدَهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) Kutoka kwa Ibn ‘Umar na Ibn ‘Abbaas (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wamesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halaal kwa Muislamu kutoa zawadi kisha akairudia isipokuwa baba katika alichompa mtoto wake.”[5] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

791.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقْبَلُ الْهَدِيَّةَ، وَيُثِيبُ عَلَيْهَا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) Kutoka kwa ‘Aaishah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akikubali zawadi, na akiilipa.”[6] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

792.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {وَهَبَ رَجُلٌ لِرَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَاقَةً، فَأَثَابَهُ عَلَيْهَا، فَقَالَ: "رَضِيتَ"؟ قَالَ: لَا. فَرَادَهُ، فَقَالَ: "رَضِيتَ"؟ قَالَ: لَا. فَرَادَهُ. قَالَ: "رَضِيتَ"؟ قَالَ: نَعَمْ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Mtu mmoja alimpa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hiba ngamia, Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamlipa akasema: Umeridhika? Yule akasema: Hapana. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamzidishia na akasema: Umeridhika? Akasema Hapana. Akamzidishia kisha akasema: Umeridhika? Akasema: Ndiyo.” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

793.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْعُمَرَى لِمَنْ وَهَبَتْ لَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِمُسْلِمٍ: {أَمْسِكُوا عَلَيْكُمْ أَمْوَالَكُمْ وَلَا تُفْسِدُوهَا ، فَإِنَّهُ مَنْ أَعْمَرَ عُمَرَى فَهِيَ لِلَّذِي أَعْمَرَهَا حَيًّا وَمَيِّتًا، وَلِعَقِبِهِ} وَفِي لَفْظٍ: {إِنَّمَا الْعُمَرَى الَّتِي أَجَازَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ يَقُولَ: هِيَ لَكَ وَلِعَقِبِكَ، فَأَمَّا إِذَا قَالَ: هِيَ لَكَ مَا عِشْتَ، فَإِنَّهَا تَرْجِعُ إِلَى صَاحِبِهَا}

وَلِأَبِي دَاوُدَ وَالنَّسَائِيِّ: {لَا تُرْقِبُوا ، وَلَا تُعْمِرُوا، فَمَنْ أَرْقَبَ شَيْئًا أَوْ أَعْمَرَ شَيْئًا فَهُوَ لَوْرَثَتِهِ}

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuzawadia ‘Umraa[7] ni kwa aliyepeewa nyumba hiyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim inasema: “Zuieni mali zenu wala msiharibu,[8] hakika anayetoa ‘Umraa basi ikiwa ni ya yule aliyezawadiwa akiwa hai na akifariki ni ya kizazi chake.”

Katika tamshi linguine inasema: “Hakika ‘Umraa aliyoijuzisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ni kusema: Hiba hii ni yako na vizazi vyako. Ama akisema: Hiba hii ni yako muda wa maisha yako. Basi hiba hiyo humrudia mwenyewe (aliyeitoa).”

Na katika Riwaayah ya Abuu Daawuud na An-Nasaaiy imesema: “Msitoe mali yenu kwa Ruqbaa wala ‘Umraa, atakayepewa chochote kwa njia ya Ruqbaa[9] au ‘Umraa basi ni cha warithi wake.”

794.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {حَمَلْتُ عَلَى فَرَسٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، فَأَضَاعَهُ صَاحِبُهُ، فَظَنَنْتُ أَنَّهُ بَائِعُهُ بِرُخْصٍ، فَسَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ ذَلِكَ. فَقَالَ: " لَا تَبْتَعُهُ ، وَإِنْ أَعْطَاكَه بِدِرْهِمٍ ... } الْحَدِيثُ. مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilitoa hiba farasi katika njia ya Allaah, mwenyewe hakujali (niliyempa). Nikadhani kuwa mwenyewe atamuza kwa bei rahisi (kwa kuwa amedhoofika). Nikamuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

(وَالِهِ وَسَلَّمَ) kuhusu jambo hilo akasema: Usimnunue hata akikupa kwa dirhamu moja....” Mpaka mwisho wa Hadiyth[10] [Al-Bukhaariy, Muslim]

795.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {تَهَادُّوا تَحَابُّوا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ فِي "الْأَدَبِ
الْمُفْرَدِ" وَأَبُو يَعْلَى بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Peaneni
zawadi[11] mutapendana.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy katika ‘Al-
Adab Al-Mufrad’ na Abuu Ya’laa ameipokea kwa Isnaad Hasan]

796.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {تَهَادُّوا، فَإِنَّ الْهَدِيَّةَ تَسُلُّ السَّخِيمَةَ} رَوَاهُ
الْبَزَّازُ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Peaneni zawadi, kwa
hakika zawadi huondoa chuki.” [Imetolewa na Al-Bazzaar kwa
Isnaad dhaifu]

797.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {يَا نِسَاءَ الْمُسْلِمَاتِ! لَا تَحْقِرَنَّ جَارَةً لِّجَارَتِهَا وَلَوْ فَرَسَنَ شَاةٍ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Enyi wanawake Waislamu! Jirani asidharau kamwe kumzawadia jirani yake japo kwa kwato ya mbuzi.”[12] [Al-Bukhaariy, Muslim]

798.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ وَهَبَ هِبَةً، فَهُوَ أَحَقُّ بِهَا، مَا لَمْ يُثَبَّ عَلَيْهَا} رَوَاهُ الْحَاكِمُ وَصَحَّحَهُ، وَالْمَحْفُوظُ مِنْ رِوَايَةِ ابْنِ عُمَرَ، عَنْ عُمَرَ قَوْلُهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kutoa hiba yeye ana haki zaidi madamu hajalipwa.”[13] [Imetolewa na Al-Haakim na akaisahihisha. Hata hivyo kauli yenye nguvu ni kuwa ni mapokezi ya Ibn ‘Umar kutoka kwa ‘Umar]

[1] Hiba ni zawadi kwa ajili ya kupata radhi za Allaah. Waqfu ni milki ya Ummah. ‘Umraa ni mtu kumuachia nyumba yake mtu kama zawadi muda wa umri wake kisha inarudi kwa mwenyewe. Ruqbaa ni nyumba ambayo anapewa zawadi mtu kwa sharti kama mmoja wao atakufa basi nyumba ile itabaki kwa aliye hai katika wao.

[2] Kwa mujibu wa Wanazuoni ni kwamba uadilifu na usawa miongoni mwa watoto ni jambo linalopendeza. Ama kwa mujibu wa Imaam Al-Bukhaariy na Muslim jambo hili ni la wajibu.

[3] Ni makubaliano ya Wanazuoni kuwa baba anaweza kuchukua kitu kutoka kwa mwanae na akamrudishia kama hiba (zawadi); lakini jambo hilo hilo haruhusiwi kulifanya kwa ndugu na jamaa zake wengine na akifanya hivyo itakuwa amefanya jambo la haraam.

[4] Hadiyth hii ni dalili ya uharamu wa mtu kuirudia hiba yake.

[5] Hii ina maana kuwa ni baba peke yake akimpa zawadi mtoto wake, anaweza kuirudia tena na kufanya hivyo hakufanya jambo la haraam. Kwa Wanazuoni wengi mama vile vile anaweza kufanya hivyo katika hiba.

[6] Hii ina maana kupokea zawadi kisha kuitoa zawadi hiyo kwa mwingine ni Sunnah.

[7] ‘Umraa ni kutoa nyumba kumpa mtu kukaa nayo kwa maisha yake kunaitwa ‘Umraa, ipo katika hali tatu i- Ni ile hali ya kutoa moja kwa moja, ii-Kutoa kwa muda wa umri wa mtu, iii-Kutoa kwa masharti (kwamba irudi kwa mwenyewe baada ya kifo cha aliyepewa). Tulichomaanisha hapa ni ile hali ya mwanzo na ya mwisho.

[8] Wakati ule watu walifikiri kuwa ‘Umraa ni mkopo anayepewa mtu kwa muda maalumu, na baada ya muda mwenye mali huichukuwa mali yake. Hata hivyo, Nabiyy (ﷺ) aliweka jambo hili wazi kwa kusema anayeazima kitu chenyewe kinakuwa ni milki yake. Mtoaji anaweza kuwa na niyyah yoyote anapotoa zawadi, hata hivyo jambo hilo

huwa haliangaliwi. Kwa hivyo basi inapendekezwa kwa mtu kabla hajatoa zawadi ya ‘Umraa afikirie vizuri kabla ya kujuta kwake.

[9] Ruqbaa ina maana ya mtu kumpa mtu mwingine nyumba yake (au anachomiliki) ili aishi humo daima, atabaki na nyumba. Hata hivyo, ikiwa aliyeazimwa akifa kabla nyumba itarudi kwa mwenyewe (mmiliki wa asili). Hii inaitwa Ruqbaa kwani kila mmoja anasubiri kifo cha mwenzake.

[10] Hadithi yenyewe inasema hivi: “Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Nilimtoa hiba farasi katika njia ya Allaah (nikampa mmoja katika wapiganaji Jihaadi). Yule aliyekuwa naye hakumsimamia vema (yule farasi akadhoofika). Nikataka kumnunua. Nikadhani kuwa mwenyewe atamuza kwa bei rahisi (kwa kuwa amedhoofika). Nikamuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Usimnunue wala usirudie swadaqah yako hata akikupa kwa dirhamu moja. Kwani anayeirudia hiba yake ni kama anaeyarudia matapishi yake.”

[11] Hii ina maana jambo la kupeleka au kutoa zawadi linapendeza kishariy’ah. Wapokezi wote katika mlolongo wa Hadiyth hii wana ila. Hata hivyo, wengine wanaungwa na wengine na ndio maana Hadiyth ikaonekana kuwa ni nzuri (Hasan). Angalia kitabu Irwaa Al-Ghaliyl cha Sheikh Al-Albaniy (6/44) namba (16010).

[12] Mfano huu unatufundisha mambo ya msingi kuhusu utoaji wa zawadi. Suala la zawadi halijali ukubwa au thamani ya zawadi bali chochote kile. Na atakayepokea aheshimu matakwa ya mtoaji yaani apokee kwa niyyah njema na moyo msafi.

[13] Hadiyth hii imezungumzia nukta mbili muhimu: i-Zawadi itakayotolewa ifidiwe, ii-Mtoaji anaweza kubadilisha mawazo na kuirejesha hiba yake. Hata hivyo, mapokezi haya ni dhaifu.

19-Mlango Wa Al-Luqatwah (Kiokotwa)

بَابُ اللَّقْطَةِ

19-Mlango Wa Al-Luqatwah (Kiokotwa)[1]

799.

عَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مَرَّ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بِتَمْرَةٍ فِي الطَّرِيقِ، فَقَالَ: "لَوْلَا أَنِّي أَخَافُ أَنْ تَكُونَ مِنَ الصَّدَقَةِ لَأَكَلْتُهَا"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipita akaona tende akasema: Lau kama mimi sichelei tende hii kuwa ni swadaqah ningeila.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

800.

وَعَنْ زَيْدِ بْنِ خَالِدٍ الْجُهَنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَسَأَلَهُ عَنِ اللَّقْطَةِ؟

فَقَالَ: " اِعْرِفْ عَفَاصَهَا وَوِكَاءَهَا، ثُمَّ عَرِّفْهَا سَنَةً، فَإِنْ جَاءَ صَاحِبُهَا وَإِلَّا فَشَأْنُكَ بِهَا"

قَالَ: فَضَالَّةُ الْغَنَمِ ؟

قَالَ: "هِيَ لَكَ ، أَوْ لِأَخِيكَ ، أَوْ لِلذُّبِّ "

قَالَ: فَضَالَّةُ الْإِبِلِ؟

قَالَ: " مَا لَكَ وَلَهَا؟ مَعَهَا سِقَاؤُهَا وَحِذَاؤُهَا، تَرِدُ الْمَاءَ، وَتَأْكُلُ الشَّجَرَ، حَتَّى يَلْقَاهَا رَبُّهَا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [2] Kutoka kwa Zayd bin Khaalid Al-Juhaniyy[2] amesema: “Mtu mmoja alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuuliza kuhusu kilichookotwa. Akasema: Kijue chombo chake na uzi wake kisha kitangaze mwaka mzima. Atapokuja mwenyewe utampa, na asipokuja utaangalia wewe. Na akamuuliza kuhusu mbuzi aliyepotea. Akasema: (Mchukue) ni wako au ni wa nduguyo au ni wa mbwa mwitu. Akamuuliza kuhusu ngamia aliyepotea. Akasema: Unataka kuwafanyia nini? Wana matumbo yao na miguu yao. Wanaweza kuenda kwenye maji na kula majani ya miti hadi wakutane na bwana wao.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

801.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { مَنْ أَوَى ضَالَّةً فَهُوَ ضَالٌّ ، مَا لَمْ يُعَرِّفْهَا } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Zayd bin Khaalid Al-Juhaniyy amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

amesema: “Anayezuia mnyama aliyemuokota, mtu huyo amepotea maadamu hajamtolea taarifa.”[3] [Imetolewa na Muslim]

802.

وَعَنْ عِيَّاضِ بْنِ حِمَارٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ وَجَدَ لُقْطَةً فَلْيُشْهَدْ ذَوِي عَدْلٍ، وَلْيَحْفَظْ عِفَاصَهَا وَوِكَاءَهَا، ثُمَّ لَا يَكْتُمْ، وَلَا يُغَيِّبْ، فَإِنْ جَاءَ رَبُّهَا فَهُوَ أَحَقُّ بِهَا، وَإِلَّا فَهُوَ مَالُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Iyaadhw bin Himaar[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayepata kitu alichookota ashuhudishe waadilifu wawili[5] na ahifadhi chombo chake na uzi wake kisha asikifiche wala asikifunike, mwenyewe akija basi ana haki (na kitu chake) na asipokuja hiyo ni mali ya Allaah Humpa Amtakaye.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah, Ibn Al-Jaaruud na Ibn Hibbaan]

803.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عُثْمَانَ التَّيْمِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ
النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنْ لُقْطَةِ الْحَاجِّ {
رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Uthmaan At-Taymiyy[6]
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza mtu kuokota alichopoteza Haajj (mwenye kuhiji).”[7] [Imetolewa na Muslim]

804.

وَعَنْ الْمِقْدَامِ بْنِ مَعْدِيكَرِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { أَلَا لَا يَحِلُّ ذُو نَابٍ مِنَ
السَّبَاعِ، وَلَا الْحِمَارُ الْأَهْلِيُّ، وَلَا اللَّقْطَةُ مِنْ مَالٍ مُعَاهَدٍ، إِلَّا
أَنْ يَسْتَغْنِيَ عَنْهَا { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa Al-Miqdaam bin Ma’d Yakrib[8] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Fahamuni! Si halaal kula wanyama mwitu, wala kula punda wa mjini, wala kuokota kutoka katika mali ya dhimmi[9] isipokuwa kiwe ni kitu kisichohitajika.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd]

[1] Al-Luqatwah ni kitu kilichoanguka au kupotea. Shariy’ah imegawanya katika mafungu matatu: i-kama ni kitu duni au chakula kinaweza kuokotwa na kuliwa. ii-Kitu cha kawaida kisicholiwa; kinaweza kuokotwa na mtu atangaze hadharani siku tatu. iii-Kitu chenye thamani ambacho shariy’ah inaamrisha; Kikiokotwa kitangazwe muda wa mwaka. Kisha ikiwa mweyewe atapatikana arudishiwe. Laa sivyo kinaweza kutumiwa.

Kuna rai za kukhitilafiana kuhusu nukta hii kama kurudishiwa mwenyewe au laa ikiwa atapatikana mwenyewe baada ya kuwa kimeshatumiwa.

[2] Lakabu yake ni ni Abuu ‘Abdir-Rahmaan au Abuu Twalhah Zayd bin Khaalid Al-Juhaniyy Al-Madaniy, ni mkazi wa Madiynah. Swahaba maarufu. Alikuwa amebeba bendera ya watu wa kabila la Juhaynah katika siku ya Fat-h Makkah (Ufunguzi wa Makkah). Aliishi katika mji wa Kufa. Alifariki Madiynah mwaka wa 78 Hijriyyah akiwa na umri wa miaka 85.

[3] Ikiwa mtu ataokota kitu kilichopotea au kumuanguka mtu na akawa na niyyah ya kukitangaza, au kuwazuiwa watu anaodhania wakichukua hawatotangaza inafaa kufanya hivyo. Kuchukua au kuokota kitu kwa niyyah mbaya ya kukihodhi haitakiwi na ni jambo ambalo halipendezi kishariy’ah.

[4] ‘Iyaadhw bin Himaar At-Tamiym Al-Mujashi’ ni Swahaba aliishi Basra (‘Iraq) hadi miaka ya 50 Hijriyyah

[5] Ikiwa kilichookotwa chenyewe ni kitu kilichopotea au kilichodondoka, wanahitajika mashahidi wawili mara moja. Vile vile, wakati wa mwenyewe kuja kukichukua mashahidi waitwe vile vile kushuhudia. Mashahidi wote hao ni muhimu sana. Hii ni kwa sababu mwenye nacho akishachukua anaweza kujitokeza mtu mwingine ambaye atatoa wasifu ule ule wa kiokotwa na kudai kuwa ni chake na hili litapelekea kwenye mzozo.

[6] ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Uthmaan At-Taymiyy Al-Qurayshi, ni mpwa wa Twalhah bin ‘Ubaydillaah, ni Swahaba. Inasemekana kuwa pamoja ya kuwa aliishi katika zama za Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) lakini hakuwahi kukutana naye. Alisilimu wakati wa Hudaybiyyah au katika Fat-h ya Makka. Aliuawa pamoja na ‘Abdullaah bin Az-Zubayr katika mwaka 73 Hijriyyah.

[7] Hii ni kwa sababu Haajj ni msafiri na ni nadra kwa Haaj kukutana na aliyeokota kiokotwa, ndiyo maana ikawekwa amri ya kutookota

alichokipoteza au alichokiangusha Haajj. Na hii ni zaidi kwa mwenye niyyah ya kukimiliki.

[8] Al-Miqdaam bin Ma'd Yakrib bin 'Amr Al-Kindiy, aliyejulikana kwa Abuu Karimah au Abuu Yahya. Alikuwa ni Swahaba maarufu. Aliishi Shaam na Hadiyth yake ilienea kwa watu wengi sana katika watu wake. Alifariki mwaka 47 Hijriyyah akiwa na umri wa miaka 91.

[9] Dhimmi ni kafiri anayeishi katika Dola ya Kiislamu na anayefuata shariy'ah za nchi na Mu'ahid mtu kafiri anayetembelea nchi za Kiislamu akiwa na ruhusa ya kusafiri visa na akifanya shughuli zake kwa amani. Dola ya Kiislamu ni jukumu lake kuangalia amani yake na mali zake n.k. Hakuna tofauti kati ya kiokotwa cha dhimmi, Mu'ahid na Muislamu kadiri ya shariy'ah ya kiokotwa inavyohusika. Hata hivyo kikiwa ni kitu duni kinaweza kuokotwa.

20-Mlango Wa Faraaidhw (Mafungu Ya Wanaorithi)

بَابُ الْفَرَائِضِ

20-Mlango Wa Faraaidhw (Mafungu Ya Wanaorithi)[1]

805.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْحَقُّوا الْفَرَائِضَ بِأَهْلِهَا، فَمَا بَقِيَ فَهُوَ لِأُولَى رَجُلٍ ذَكَرٍ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wapeni mafungu wenye mafungu yao[2] kitakachobaki (baada ya kuwapa wenye mafungu yao) ni cha mwanamume aliye karibu zaidi (na maiti).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

806.

وَعَنْ أُسَامَةَ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَرِثُ الْمُسْلِمُ الْكَافِرَ، وَلَا يَرِثُ الْكَافِرُ الْمُسْلِمَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Usaamah bin Zayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muislamu hamrithi kafiri wala kafiri hamrithi Muislamu.”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim]

807.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي بِنْتٍ، وَبِنْتِ ابْنٍ، وَأُخْتٍ {قَضَى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "لِلْإِبْنَةِ

النِّصْفَ، وَلِابْنَةِ الْإِبْنِ السُّدُسَ تَكْمِلَةَ الثَّلَاثِينَ وَمَا بَقِيَ
فَلِلْأَخْتِ { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesimulia katika
kumrithisha binti, binti ya mtoto wa kiume na dada: “Nabiy (صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alihukumu binti apate nusu, binti ya mtoto wa
kiume apate sudus kukamilisha thuluthi mbili[4] na kilichobakia ni
cha dada.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

808.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يَتَوَارَثُ أَهْلُ مِلَّتَيْنِ } رَوَاهُ
أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ وَأَخْرَجَهُ الْحَاكِمُ بِلَفْظِ أُسَامَةَ.
وَرَوَى النَّسَائِيُّ حَدِيثَ أُسَامَةَ بِهَذَا اللَّفْظِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wenye
dini tofauti hawarithiani.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (An-
Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa At-Tirmidhiy, Al-
Haakim ameipokea kwa maneno ya Usaamah; na An-Nasaaiy
ameitaja Hadiyth ya Usaamah kwa tamshi hili]

809.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: {إِنَّ ابْنَ ابْنِي مَاتَ، فَمَا لِي مِنْ مِيرَاثِهِ؟ فَقَالَ: "لَكَ السُّدُسُ" فَلَمَّا وَلَّى دَعَاهُ، فَقَالَ: "لَكَ سُدُسٌ آخَرُ" فَلَمَّا وَلَّى دَعَاهُ. فَقَالَ: "إِنَّ السُّدُسَ الْآخَرَ طُعْمَةٌ" رَوَاهُ أَحْمَدُ وَالْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ وَهُوَ مِنْ رِوَايَةِ الْحَسَنِ الْبَصْرِيِّ عَنْ عِمْرَانَ، وَقِيلَ: إِنَّهُ لَمْ يَسْمَعْ مِنْهُ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Mtu mmoja alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Mtoto wa mtoto wangu amefariki, nitapata nini katika mirathi yake? Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Utapata sudusi. Alipogeuka alimuita akasema: Utapata sudusi nyingine.[5] Alipogeuka tena alimuita tena akasema: Ile sudusi nyingine ni ziada.”[6] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

Nayo ni katika Riwaayah ya Al-Hassan Al-Baswriyy[7] kutoka kwa ‘Imraan na inasemekana kuwa hajamsikia.

810.

وَعَنْ ابْنِ بُرَيْدَةَ، عَنْ أَبِيهِ، {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ جَعَلَ لِلْجَدَّةِ السُّدُسَ، إِذَا لَمْ يَكُنْ دُونَهَا أُمٌّ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ، وَقَوَّاهُ ابْنُ عَدِيٍّ

Kutoka kwa Ibn Buraydah naye kutoka kwa baba yake amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amempa bibi[8] sudusi iwapo hakuna mama pamoja naye.”[9] [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah, Ibn Al-Jaarud na akaipa nguvu Abn ‘Adiyy

811.

وَعَنْ الْمِقْدَامِ بْنِ مَعْدِيكَرِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْخَالُ وَارِثٌ مَنْ لَا وَارِثَ لَهُ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ سِوَى التِّرْمِذِيِّ، وَحَسَنَهُ أَبُو زُرْعَةَ الرَّازِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Al-Miqdaam bin Ma’d Yakrib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mjomba ni mrithi wa asiye kuwa na mrithi.”[10] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa At-Tirmidhiy, na Abuw Zur’ah Ar-Raaziy amesema ni Hasan, na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim

812.

وَعَنْ أَبِي أُمَامَةَ بْنِ سَهْلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَتَبَ مَعِيَ عُمَرُ إِلَى أَبِي عُبَيْدَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: "اللَّهُ وَرَسُولُهُ مَوْلَى مَنْ لَا مَوْلَى

لَهُ، وَالْخَالُ وَارِثٌ مَنْ لَا وَارِثَ لَهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ
سِوَى أَبِي دَاوُدَ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Umaamah bin Sahl[11] amesema: “Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuandikia barua Abuu صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) ‘Ubaydah[12] kuwa Rasuli wa Allaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Allaah na Rasuli wa Allaah ni Wasimamizi wa asiyekuwa na msimamizi. Mjomba ni mrithi wa asiyekuwa na mrithi.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah) isipokuwa Abuu Daawuud, na At-Tirmidhiy amesema ni Hasan, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

813.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا اسْتَهَلَ الْمَوْلُودُ وَرَّثَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ،
وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema “Mtoto aliyezaliwa akilia, anarithi.”[13] [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

814.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَيْسَ لِلْقَاتِلِ مِنَ الْمِيرَاثِ شَيْءٌ} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَقَوَّاهُ ابْنُ عَبْدِ الْبَرِّ، وَأَعْلَاهُ النَّسَائِيُّ، وَالصَّوَابُ: وَقَفُّهُ عَلَى عُمَرَ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muuaji hana chochote katika mirathi.”[14]
[Imetolewa na An-Nasaaiy, Ad-Daaraqutwniy na akaipa nguvu Ibn ‘Abdi-Barr, na akaidhoofisha An-Nasaaiy. Lakini sawa ni kuwa Hadiyth hii ni Mawquwf]

815.

وَعَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {مَا أَحْرَزَ الْوَالِدُ أَوْ الْوَلَدُ فَهُوَ لِعَصْبَتِهِ مَنْ كَانَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْمَدِينِيِّ، وَابْنُ عَبْدِ الْبَرِّ

Kutoka kwa ‘Umar bin Al-Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Anachochukua baba au mtoto (katika walaa) ni cha ‘Aswabah yake[15] yeyote awaye.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, An-Nasaaiy na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Al-Madiyniy na Ibn ‘Abdil-Barr]

816.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْوَلَاءُ لُحْمَةٌ كُلُّهَا النَّسَبُ، لَا يُبَاعُ، وَلَا يُوهَبُ} رَوَاهُ الْحَاكِمُ: مِنْ طَرِيقِ الشَّافِعِيِّ، عَنْ مُحَمَّدِ بْنِ الْحَسَنِ، عَنْ أَبِي يُوسُفَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَأَعْلَاهُ الْبَيْهَقِيُّ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Walaa[16] ni udugu kama udugu wa nasaba, hauuzwi wala hautolewi hiba (zawadi).” [Imetolewa na Al-Haakim kwa njia ya Ash-Shaafi’iyy kutoka kwa Muhammad bin Al-Hasan[17] kutoka kwa Abuw Yuwsuf,[18] na akaisahihisha Ibn Hibbaan, na akaitia kasoro Al-Bayhaqiyy]

817.

وَعَنْ أَبِي قِلَابَةَ، عَنْ أَنَسٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَفْرَضُكُمْ زَيْدُ بْنُ ثَابِتٍ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ سِوَى أَبِي دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ، وَأَعْلَى بِالْإِسْأَلِ

Kutoka kwa Abuu Qilaabah[19] kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mjuzi wenu katika Faraaidhw (Mirathi) ni Zayd bin Thaabit.”[20] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) isipokuwa Abuu

Daawuud, na akaisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Hibbaan na Al-Haakim, na imepewa dosari kuwa ni Mursal]

[1] Faraaidhw ni wingi wa Fardhw yenye maana ya Shariy'ah inayohusu ugawaji wa mirathi.

[2] Hawa ni watu wenye mafungu kama walivyotajwa katika Qur-aan nao wanaitwa Dhul-Faraaidhw na warithi wengine wanaowezekana kurithi huitwa 'Aswabah. Baadhi ya Dhul-Faraaidhw ni 'Aswabah vile vile. Katika Qur-aan aina sita za mafungu zimetajwa. Hizi ni: Nusu, moja ya nne (robo), moja ya nane (thumuni), theluthi mbili, theluthi moja na sudusi.

[3] Hii ikiwa miongoni mwa waliokufa kuna jamaa wasiokuwa Waislamu hawawezi kumrithi. Yaani Muislamu hawezi kumrithi kafiri kama ilivyo kafiri hawezi kumrithi Muislamu.

[4] Nusu kwa binti na sudusi kwa mjukuu wa kike (upande wa baba) na theluthi itakuenda kwa dada. Hii ina maana ya kuwa dada akiwa pamoja na binti na mjukuu wanakuwa ni 'Aswabah

[5] Maiti aliacha binti wawili na babu yao kama warithi. Binti wawili watapata theluthi mbili, wakati babu atapata sudusi kama Dhul-Faraaidhw na mwingine sudusi kama 'Aswabah. Nabiy (ﷺ) alimjulisha kuhusu sudusi ya mwanzo hapo kabla, ili asifikiri fungu lake kuwa ni theluthi kisha akamuelezea mwishoni.

[6] Mas-ala haya yako hivi. Maiti aliacha mabinti wawili na babu ambaye ndiye muulizaji, wale mabinti wawili wakapata thuluthi mbili, ikabaki thuluthi moja, Nabiy (ﷺ) akampa yule muulizaji (Babu) sudus akamuambia "utapata sudusi nyingine ikiwa ni ziada ('Aswabah)." Kwa hivyo babu amepata sudusi ikiwa ni fungu lake na amepata kilichobakia ikiwa ni 'Aswabah. Tazama: anayerithi kwa ta'siyb (salio) ni mrithi asiye na kiwango maalumu kilichowekwa na Qur-aan na

Hadiyth. Lakini endapo atakuwa yuko peke yake, mali yote itakuwa ni yake, na iwapo atapata fungu na kikabakia kitu hicho kitakuwa ni chake.

[7] Al-Hassan bin Abdil-Hassan Al-Baswriyy alikuwa ni mtumwa wa Kianswaar. Babake akiitwa Yassar. Al-Hassan alikuwa ni Imaam muadilifu. Alikuwa ni madhubuti, mwenye taqwa, Mwanazuoni maarufu, fasaha na mwenye umbuji. Alikua kiongozi wa kizazi cha tatu cha Taabi'iyna, alizaliwa miaka miwili kabla ya ukhalifa wa 'Umar bin Al-Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kuisha. Alipata kumuona 'Uthmaan bin 'Affaan na 'Aliy bin Abiy Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) lakini hakupata kupokea Hadiyth kutoka kwao. Alifariki mwezi wa Rajab mwaka 110 Hijriyyah alipokuwa ana miaka 90 takriban.

[8] Bibi kwa lugha ya kiarabu ni Jaddah Swahiyhah (mama mzaa baba) na Jaddah Fasiydad (mama mzaa mama). Ikiwa mama wa aliyekufa hayupo, fungu la mama litakuenda kwa mama mzaa baba au mama mzaa mama. Ikiwa wote wapo watagawana fungu hilo.

[9] Lau mama atakuwa pamoja naye angalimzuia nyanya kurithi kishariy'ah.

[10] Hadiyth hizi ni dalili kuwa ikiwa hakuna 'Aswabah au Dhul-Faraaidhw (wenye undugu na maiti), kwa hali hiyo basi mjomba anakuwa mrithi. Hii ina maana kwamba mjomba ni mrithi wa mwisho. Ikiwa naye mjomba huyo hayupo mali hiyo itakuenda kwenye Baytul-Maal. Mama mdogo ana nafasi kama nafasi aliyokuwa nayo mjomba.

[11] Jina lake ni As'ad au Sa'd lakini alikuwa akijulikana zaidi kama Abuu Umaamah bin Sahl bin Hunayf bin Wahiyb Al-Answaar Al-Aws Al-Madaniy. Alikuwa ni Swahaba na alimuona Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) lakini hakupata kusikia Hadiyth yoyote kutoka kwake. Alifariki mwaka 100 Hijriyyah akiwa na umri wa miaka 92.

[12] Huyu ni Abuu 'Ubaydah 'Aamir bin 'Abdillaah bin Al-Jarraah bin Hilaal Al-Qurayshi Al-Fihri. Alikuwa ni mmoja katika kumi

waliobashiriwa Jannah. Alisilimu mapema na aliamia Uhabeshi katika Hijrah ya pili. Alishiriki vita vya Badr na vita vinginevyo muhimu pia. Siku ya Uhud alipoteza meno yake mawili alipojaribu kutoa pete ya kofia ya chuma ilipoingia katika kidevu cha Nabiyy (ﷺ). Abuu 'Ubaydah aliliongoza jeshi la Kiislam wakati wa kuiteka Shaam. Alifariki katika ugonjwa wa ndui huko Amwas katika mwaka wa 18 Hijriyyah akiwa na miaka 58.

[13] Hii ina maana mtoto yu hai, mtoto huyu anatakiwa kufanyiwa haki zote kama vile kuswaliwa Swalaah ya maiti kama atakufa baada ya hapo na atakuwa na haki ya kurithi na kurithiwa hali kadhalika.

[14] Muuaji hana haki ya kurithi katika mali ya aliyeuliwa. Muuaji hapati fungu lolote hata kama akiwa ni 'Aswabah au Dhul-Faraaidhw wa aliyeuwawa. Aliyeuwa kwa kukusudia na hata kwa kutokusudia wote wako sawa katika hili kulingana na Maimaam wengi isipokuwa Imaam Maalik pekee yake.

[15] Walaa (Mirathi ya mtumwa aliyeachwa huru) haigawanywi kama mirathi ya Dhul-Faraaidhw. Badili yake, wale 'Aswabah walio karibu wana haki ya mirathi hiyo (Walaa). Hii ndiyo rai sahihi zaidi ingawaje kuna Wanazuoni wenye rai tofauti.

[16] Baada ya kifo cha mtumwa aliyeachwa huru, alichokiacha huitwa Walaa na mwenye kulipa fidia ya uhuru wake huwa ndie mrithi wake baada ya kifo chake aliyekuwa mtumwa ikiwa hana ndugu wa damu wa kumrithi.

[17] Huyu ni Abuu 'Abdullaah Muhammad bin Al-Hassan bin Farqad, Ash-Shaybaan kwa ukoo, alikuwa mmoja wa Maimaam wa dhehebu la Hanafi. Alizaliwa mwaka 132 Hijriyyah huko Waasit na kukulia katika mji wa Kufa huko 'Iraq. Alisafiri ili atafute elimu ya Hadiyth na alikutana na Wanazuoni maarufu. Alihudhuria darasa la Abuu Haniyfah kwa miaka, kisha akajifunza elimu ya Fiqhi kwa Abuu Yuwsuf. Aliandika vitabu vingi muhimu na hivyo kutawanya elimu ya Imaam Haniyfah kwa watu wengi. Kadhalika alipata kusoma kwa Imaam Maalik kwa muda wa miaka mitatu. Wanazuoni wa Hadiyth wanazona Hadiyth alizopokea kama ni dhaifu

kutokana na udhaifu wa kumbukumbu yake ilivyokuwa. Alifariki mwaka 189 Hijriyyah huko Ranbuwaih, kijiji kilichopo Ar-Ray.

[18] Abuw Yuwsuf alikuwa Mwanazuoni wa Fiqhi huko ‘Iraaq. Jina lake kamili ni Imaam Al-Qaadhwi Abuw Yuwsuf Ya’quwb bin Ibrahiym Al-Answaar Al-Kufi, alikua ni mfuasi wa Abuu Haniyfah. Alikulia huku akitafuta elimu. Baba yake alikuwa maskini na Abuu Haniyfah alikuwa akimsaidia baba yake mara kwa mara. Yahya bin Ma’iyn anasema: “Hakuna Mwanazuoni wa Fiqhi ambaye anafahamu Hadiyth au alikuwa madhubuti (katika upokezi wa Hadiyth) kuliko Abuw Yuwsuf.” Yahya bin Yahya At-Tamimi anasema: “Nilimsikia Abuw Yuwsuf akisema wakati wa kifo chake, najikosha na rai ya Fiqhi yoyote niliyotoa wakati wa uhai wangu isipokuwa inayothibitishwa na Qur-aan na Sunnah katika Riwaayah nyingine isipokuwa ile iliyothibitishwa na Qur-aan na makubaliano ya Waislamu.” Alifariki mwezi wa Rabiyy’ Al-Aakhir mwaka 182 akiwa na umri wa miaka 69.

[19] Abuu Qilaabah jina lake sahihi ni Zayd bin ‘Amr au ‘Aamir Al-Jurmi Al-Basri. Alikuwa ni Taabi’ maarufu, ni madhubuti na mpokezi wa Hadiyth nyingi zilizokuwa Mursal. Alikuwa katika kizazi cha sita na alifariki Shaam mwaka 104 Hijriyyah au 106 au 107 kwa kukimbia asije akapewa jukumu la Ukadhi.

[20] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwaminifu wa Ummah huu ni Abuu Bakr; mkali zaidi wa Dini ni ‘Umar bin Al-Khatwaab; mpole zaidi miongoni mwao ni ‘Uthmaan; hakimu mzuri zaidi ni ‘Aliy msomaji mzuri wa Qur-aan ni ‘Ubay bin Ka’b; mwenye kujua halaal na haraam miongoni mwao ni Mu’aadh bin Jabal; mjuzi wao wa Faraaidhw ni Zayd bin Thaabit. Jueni kwamba, katika kila Ummah kuna amini wake na amini wa Ummah huu ni Abuu ‘Ubaydah bin Jaraah.” Katika Hadiyth hii Zayd bin Thaabit anatangulizwa kuhusu mas-ala ya migogoro katika mirathi.

21-Mlango wa Wasia

بَابُ الْوَصَايَا

21-Mlango wa Wasia[1]

818.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَا حَقُّ امْرِئٍ مُسْلِمٍ لَهُ شَيْءٌ يُرِيدُ أَنْ يُوصِيَ فِيهِ يَبِيتُ لَيْلَتَيْنِ إِلَّا وَوَصِيَّتُهُ مَكْتُوبَةٌ عِنْدَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haitakiwi kwa Muislamu iwapo ana jambo linalotakiwa kuusiwa, alale siku mbili ila awe ameshaandika wasia wake[2].”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim]

819.

وَعَنْ سَعْدِ بْنِ أَبِي وَقَّاصٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَنَا ذُو مَالٍ، وَلَا يَرِثُنِي إِلَّا ابْنَةٌ لِي وَاحِدَةٌ، أَفَأَتَصَدَّقُ بِثُلْثِي مَالِي؟ قَالَ: " لَا " قُلْتُ: أَفَأَتَصَدَّقُ بِشَطْرِهِ؟ قَالَ: " لَا " قُلْتُ: أَفَأَتَصَدَّقُ بِثُلْثِهِ؟ قَالَ: " الْثُلْثُ، وَالثُّلُثُ

كَثِيرٌ، إِنَّكَ أَنْ تَذَرَ وَرَثَتَكَ أَغْنِيَاءَ خَيْرٌ مِنْ أَنْ تَذَرَهُمْ عَالَةً
يَتَكَفَّفُونَ النَّاسَ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Sa'd bin Abiy Waqqaasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
alimuambia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Ee
Rasuli wa Allaah! Mimi ni mwenye mali nyingi, wala hakuna
atakayenirithi isipokuwa binti yangu mmoja tu. Je nitoe swadaqah
thuluthi mbili za mali yangu? Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
akasema: “Hapana” nikasema: “Basi nitoe nusu yake?” akasema:
“Hapana” Nikasema: “Je thuluthi (moja)? Akasema: “Thuluthi,[4] na
hiyo thuluthi ni nyingi, kuwaacha warithi wako wakwasi, ni bora
kuliko kuwaacha mafukara wakiomba watu.” [Al-Bukhaariy,
Muslim]

820.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا أَنَّ رَجُلًا أَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ أُمِّي أَفْتَلَتَتْ نَفْسَهَا
وَلَمْ تُوصِ، وَأَظْنُّهَا لَوْ تَكَلَّمَتْ تَصَدَّقْتُ، أَفَلَهَا أَجْرٌ إِنْ
تَصَدَّقْتُ عَنْهَا؟ قَالَ: " نَعَمْ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa mtu
mmoja[5] alimjia Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema:
“Ee Rasuli wa Allaah! Mama yangu amekufa ghafla wala hakuusia
na nadhani lau angelizungumza, angeliamuru itolewe swadaqah, je
atapata ujira nikimtolea swadaqah? Akasema: “Ndio.” [Al-
Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

821.

وَعَنْ أَبِي أُمَامَةَ الْبَاهِلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {إِنَّ اللَّهَ قَدْ أَعْطَى كُلَّ ذِي حَقٍّ حَقَّهُ، فَلَا وَصِيَّةَ لِي وَارِثٍ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَحَسَنَهُ أَحْمَدُ وَالتِّرْمِذِيُّ، وَقَوَّاهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ

وَرَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، وَزَادَ فِي آخِرِهِ: {إِلَّا أَنْ يَشَاءَ الْوَرِثَةُ} وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Umaamah Al-Baahiliyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Kwa hakika Allaah Amempa kila mwenye haki haki yake, kwa hivyo hakuna wasia kwa mwenye kurithi.”[6] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy, Ahmad na At-Tirmidhiy wamesema ni Hasan, Ibn Khuzaymah na Ibn Al-Jaarud wameipa nguvu]

Pia Ad-Daraqutwniyy ameipokea kutoka katika Hadiyth ya Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) mwisho wake akaongeza: “... isipokuwa watakapopenda wanaorithi.” [Isnaad yake ni Hassan]

822.

وَعَنْ مُعَاذِ بْنِ جَبَلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ اللَّهَ تَصَدَّقَ عَلَيْكُمْ بِثُلُثِ أَمْوَالِكُمْ عِنْدَ وَفَاتِكُمْ، زِيَادَةً فِي حَسَنَاتِكُمْ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ

وَأَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْبَزَّازُ مِنْ حَدِيثِ أَبِي الدَّرْدَاءِ
وَابْنِ مَاجَةَ: مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ وَكُلُّهَا ضَعِيفَةٌ، لَكِنْ قَدْ
يَقْوَى بَعْضُهَا بِبَعْضٍ. وَاللَّهُ أَعْلَمُ

Kutoka kwa Mu'aadh bin Jabal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kwa hakika Allaah Amekupeni swadaqah[7] theluthi ya mali yenu mtoe wakati wa kufa kwenu ili kuzidisha mema yenu.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy]

Ahmad na Al-Bazzaar wameipokea kutoka katika Hadiyith ya Abuu Ad-Dardaa.

Na Ibn Maajah ameipokea kutoka katika Hadiyith ya Abuu Hurayrah. Mapokezi yote ni dhaifu. Hata hivyo zimetiliana nguvu zenyewe na zikawa ni Hasan. Allaah ni Mjuzi.

[1] Kilugha Waswiyyah (wasia) ina maana ya kuagiza, kushauri, kupendekeza kitu. Kulingana na Shariy'ah ni wasia anaoacha (kwa theluthi moja) ya mali ya marehemu kutumika baada ya kifo chake.

[2] Kabla ya kuteremka kwa Aayah ya mirathi, kuweka wasia ilikuwa ni wajibu. Hata hivyo baada ya Wahyi huu amri hii ilibatilishwa. Hata hivyo inawezekana mtu akaweka wasia katika yasiyokuwa mambo ya kurithi. Leo hii, suala hili limekuwa muhimu sana, kwa mfano kwa mtu kuwepo na mtoto wake pamoja nae kuweka wasia kwa ajili ya mjukuu wa mtoto wa aliyefariki. Uandishi wa wasia sio muhimu. Hata hivyo ni muhimu kuthibitisha wasia uliotamkwa, ili kuzuia sintofahamu yoyote inayoweza kujitokeza huko mbeleni.

[3] Katika Riwaayah nyingine ya Muslim imesema: “Awe atalala masiku matatu.” Ibn ‘Umar amesema: “Tangu nimsikie Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema maneno hayo sijapitiwa na usiku ila wasia wangu uko kwangu.”

[4] Wasia unaweza kuweka kwa thamani ya juu zaidi isizidi theluthi moja tu kwa mali yote mtu anayomiliki. Ikiwa ni chini ya theluthi ni bora. Hata hivyo kwa niaba ya warithi wengine anaweza kuusia zaidi ya theluthi moja ikiwa warithi wenyewe wako hai, vinginevyo hairuhusiwi kuusia zaidi ya theluthi moja.

[5] Mtu huyu alikuwa ni Sa'd bin 'Ubaadah. Tunajifunza katika Hadiyth hii kuwa watoto wa kike na wa kiume wanaorithi wanaweza kutoa swadaqah katika mali ya mirathi bila ya wasia wa hilo.

[6] Hii ina maana wasia hauwekwi kwa wanaorithi, lakini kwa ruhusa ya warithi wengine, inaruhusiwa, kama ilivyo kuweka wasia wa zaidi ya theluthi moja inaruhusiwa kwa mtu yeyote kwa ruhusa ya warithi wengine.

[7] Katika lugha ya kiarabu neno Ihsaan ni kupendeyesha, mtu akiwa hai mwenye nguvu anatumia mali na utajiri wake autakavyo, baada ya kufa kwake hana mamlaka na mali aliyoacha. Hapa ndipo Allaah Akamtaka mtu kuweka wasia wa theluthi ya mali yake kabla ya kufa kwake ili imuongezee katika amali yake.

22-Mlango Wa Al-Wadiy'ah (Kuweka Amana)

بَابُ الْوَدِيْعَةِ

22-Mlango Wa Al-Wadiy'ah (Kuweka Amana)

823.

عَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ ، عَنْ أَبِيهِ ، عَنْ جَدِّهِ ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ أُوْدِعَ وَدِيعَةً، فَلَيْسَ عَلَيْهِ
ضَمَانٌ} أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَإِسْنَادُهُ ضَعِيفٌ.
وَبَابُ قَسَمِ الصَّدَقَاتِ تَقَدَّمَ فِي آخِرِ الزَّكَاةِ .
وَبَابُ قَسَمِ الْفَيْءِ وَالْغَنِيمَةِ يَأْتِي عَقِبَ الْجِهَادِ إِنْ شَاءَ اللَّهُ
تَعَالَى.

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb naye kutoka kwa baba yake naye
kutoka kwa babu yake (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuwekewa
amana hana dhamana.”[1] [Imetolewa na Ibn Maajah na Isnaad yake
ni dhaifu]

Mlango wa kugawa Zakaah umetangulia katika mwisho wa “Kitabu
cha Zakaah.”.

Mlango wa kugawa Fay na Ghaniymah utakuja baada ya “Kitabu cha
Jihaad” In Shaa Allaah

[1] Tofauti kati ya amaanah (amana) na ‘aariyah (mkopo) ni kuwa pale
mtu anapoazima kwa ajili yake inakuwa ni ‘aariyah wakati amana ni ile
mali mtu anayoiacha kwa mtu mwingine amuwekee. Mtu anaweza
kutumia mali ya ‘aariyah kwa kuazima na kutumia lakini mali ya amaanah
hairuhusiwi. Ikiwa ‘aariyah imeharibika na kupotea, aliyeazima itabidi
alipe. Ama kuhusu mali ya amaanah ikiwa imeharibika au kuangamia kwa
ajali, hatakiwi kulipa aliyewekewa dhamana, hata hivyo ikiwa mali ya

amaanah imetumika au sehemu katika mali ile itabidi ailipe aliyekabidhiwa amaanah ile.

كِتَابُ النِّكَاحِ

Kitabu Cha Nikaah (Ndoa)

08-Kitabu Cha Nikaah - كِتَابُ النِّكَاحِ

01-Buluwgh Al-Maraam: Kitabu Cha Nikaah

824.

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ لَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { يَا مَعْشَرَ الشَّبَابِ! مَنْ اسْتَطَاعَ مِنْكُمُ الْبَاءَةَ فَلْيَتَزَوَّجْ، فَإِنَّهُ أَغْضُّ لِلْبَصَرِ، وَأَحْصَنُ لِلْفَرْجِ، وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَعَلَيْهِ بِالصَّوْمِ، فَإِنَّهُ لَهُ وَجَاءٌ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituambia: “Enyi mkusanyiko wa vijana, anayeweza miongoni mwenu kumudu ndoa

na aoe,[1] kwani huko kuoa huinamisha zaidi macho na huhifadhi zaidi tupu. Na asiyeweza basi ajilazimu swawm; kwani huko swawm kwake ndiko kuyavunja matamanio.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

825.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ حَمِدَ اللَّهَ، وَأَثْنَى عَلَيْهِ، وَقَالَ: " لَكِنِّي أَنَا أَصَلِّي وَأَنَامُ، وَأَصُومُ وَأُفْطِرُ، وَأَتَزَوَّجُ النِّسَاءَ، فَمَنْ رَغِبَ عَنْ سُنَّتِي فَلَيْسَ مِنِّي } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alimhimidi Allaah na akamsifu, akasema... lakini mimi naswali[2] na nalala, nafunga (swawm) na ninakula na naoa wanawake. Basi atakayechukia mwenendo wangu basi si katika mimi.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

826.

وَعَنْهُ قَالَ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَأْمُرُ بِالْبَاءَةِ، وَيَنْهَى عَنِ التَّبَتُّلِ نَهْيًا شَدِيدًا، وَيَقُولُ: " تَزَوَّجُوا الْوُدُودَ الْوُلُودَ . إِنِّي مُكَاثِرٌ بِكُمْ الْأَنْبِيَاءَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

وَلَهُ شَاهِدٌ: عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيِّ، وَابْنِ حِبَّانَ أَيْضًا مِنْ حَدِيثِ مَعْقِلِ بْنِ يَسَارٍ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alikua akituamrisha kuoa na akitukataza kuacha kuoa[3] makatazo makali na akisema: Oweni wanawake wanaozaaa wanaopendeza (kwa waume zao), kwa hakika mimi nitakuwa mwenye kujifakhiri (mbele ya) Manabiy kwa sababu yenu Siku ya Qiyamah.” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

Na ina ushahidi kwa Abuu Daawud, An-Nasaaiy na Ibn Hibbaan kutoka katika Hadiyth ya Ma’qil bin Yasaar

827.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { تُنَكِّحُ الْمَرْأَةَ لِأَرْبَعٍ: لِمَالِهَا، وَلِحَسَبِهَا، وَلِجَمَالِهَا، وَلِدِينِهَا، فَظَفَرُ بَذَاتِ الدِّينِ تَرِبَتْ يَدَاكَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ مَعَ بَقِيَّةِ السَّبْعَةِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamke huolewa kwa mambo manne:[4] kwa mali yake, hadhi yake, uzuri wake na Dini yake. Basi oa aliyeshika Dini (vinginevyo) mikono yako itachafuka.”[5] [Al-Bukhaariy, Muslim pamoja na Maimaam saba (Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawud, Ibn Maajah, Ahmad) waliobakia.

828.

وَعَنْهُ، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا رَفَّأَ إِنْسَانًا إِذَا تَزَوَّجَ قَالَ: {بَارَكَ اللَّهُ لَكَ، وَبَارَكَ عَلَيْكَ، وَجَمَعَ بَيْنَكُمَا فِي خَيْرٍ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alikuwa anapomuombea mtu du’aa njema, akimuombea:[6]

بَارَكَ اللَّهُ لَكَ، وَبَارَكَ عَلَيْكَ، وَجَمَعَ بَيْنَكُمَا فِي خَيْرٍ

Baaraka Allaahu laka, wa baaraka ‘alayka, wa jama’a baynakumaa fiy khayr (Allaah Akubariki (katika mke wako) na Abariki juu yako (uweze kumudu gharama zake) na Awajumuishe katika kheri).” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah), na akaisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan]

829.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {عَلَّمَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ التَّشَهُّدَ فِي الْحَاجَةِ: "إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ، نَحْمَدُهُ، وَنُسْتَعِينُهُ، وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا

إِلَّا اللَّهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ وَيَقْرَأُ ثَلَاثَ آيَاتٍ {
رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
“Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitufundisha
kushahadia katika haja (ndoa na jambo lolote):

إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ، نَحْمَدُهُ، وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ
شُرُورِ أَنْفُسِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ
إِلَّا اللَّهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

*Innal-Hamda liLLaah, nahmaduhu, wa nasta'iynuhu, wa
nastaghfiruhu, wa na'uwdu biLLaahi min shuruwri anfusinaa, man
yahdihi-LLaahu falaa mudhwilla lah, wa ash-hadu an laa ilaaha illa
Allaah, wa ash-hadu anna Muhammadan 'abduhu wa rasuwluhu*

(Hakika Himdi anastahiki Allaah, tunamhimidi, tunamuomba msaada
na tunamuomba maghfirah. Tunajikinga kwa Allaah dhidi ya shari za
nafsi zetu. Anayeongozwa na Allaah hakuna wa kumpoteza na
anayepotezwa Naye hakuna wa kumuongoza. Nashuhudia kuwa
hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah na nashuhudia kuwa
Muhammad ni Mja wake na ni Rasuli wake) baada ya hapo anasoma
Aayah tatu.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy,
An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah), na akaisahihisha At-
Tirmidhiy na Al-Haakim]

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {إِذَا خُطِبَ أَحَدُكُمْ الْمَرْأَةُ، فَإِنْ اسْتَطَاعَ أَنْ يَنْظُرَ مِنْهَا مَا يَدْعُوهُ إِلَى نِكَاحِهَا، فَلْيَفْعَلْ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

وَلَهُ شَاهِدٌ: عِنْدَ التِّرْمِذِيِّ، وَالنَّسَائِيِّ، عَنِ الْمُغِيرَةِ.

وَعِنْدَ ابْنِ مَاجَهَ، وَابْنِ حِبَّانَ: مِنْ حَدِيثِ مُحَمَّدِ بْنِ مَسْلَمَةَ

وَلِمُسْلِمٍ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ لِرَجُلٍ تَزَوَّجَ امْرَأَةً: أَنْظَرْتُ إِلَيْهَا؟} قَالَ: لَا. قَالَ: "إِذْهَبْ فَانْظُرْ إِلَيْهَا"

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Yeyote miongoni mwenu anapomposa mwanamke, iwapo ataweza kumtazama sehemu zinazomvutia ndoa yake[7] basi afanye hivyo.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na wapokezi wake ni madhubuti, na akaisahihisha Al-Haakim]

Hadiyth hii ina ushahidi kwa At-Tirmidhiy na An-Nisaa'iy kutoka kwa Al-Mughiyrah.

Ibn Maajah na Ibn Hibbaan wameipokea kutoka katika Hadiyth ya Muhammad bin Maslamah.[8]

Na kutoka katika Riwaayah ya Muslim kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia mtu alietaka kuoa, “Je umemuangalia?” akasema: “Hapana” Akasema: “Nenda ukamuangalie.”

831.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يَخْطُبُ بَعْضُكُمْ عَلَى خِطْبَةِ أَخِيهِ، حَتَّى يَتْرُكَ الْخَاطِبُ قَبْلَهُ، أَوْ يَأْذَنَ لَهُ الْخَاطِبُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asipose yeyote miongoni mwenu juu ya posa ya nduguye[9] (Muislamu) mpaka yule mposaji aache kabla yake au amruhusu.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

832.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدٍ السَّاعِدِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {جَاءَتْ امْرَأَةٌ إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! جِئْتُ أَهْبُ لَكَ نَفْسِي، فَنَظَرَ إِلَيْهَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَصَعَّدَ النَّظَرَ فِيهَا، وَصَوَّبَهُ، ثُمَّ طَاطَأَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ رَأْسَهُ، فَلَمَّا رَأَتْ الْمَرْأَةُ أَنَّهُ لَمْ يَقْضِ فِيهَا شَيْئًا جَلَسَتْ، فَقَامَ رَجُلٌ مِنْ أَصْحَابِهِ

فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنْ لَمْ يَكُنْ لَكَ بِهَا حَاجَةٌ فَرَوَّجْنِيهَا .

قَالَ: " فَهَلْ عِنْدَكَ مِنْ شَيْءٍ ؟ "

فَقَالَ: لَا، وَاللَّهِ يَا رَسُولَ اللَّهِ .

فَقَالَ: " اِذْهَبْ إِلَى أَهْلِكَ، فَانْظُرْ هَلْ تَجِدُ شَيْئًا ؟ " فَذَهَبَ، ثُمَّ رَجَعَ ؟

فَقَالَ: لَا، وَاللَّهِ يَا رَسُولَ اللَّهِ، مَا وَجَدْتُ شَيْئًا.

فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " انْظُرْ وَلَوْ خَاتَمًا مِنْ حَدِيدٍ "، فَذَهَبَ، ثُمَّ رَجَعَ

فَقَالَ: لَا وَاللَّهِ، يَا رَسُولَ اللَّهِ، وَلَا خَاتَمًا مِنْ حَدِيدٍ، وَلَكِنْ هَذَا إِزَارِي قَالَ سَهْلٌ: مَا لَهُ رِذَاءٌ فَلَهَا نِصْفُهُ.

فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " مَا تَصْنَعُ بِإِزَارِكَ ؟ إِنْ لَبِسْتَهُ لَمْ يَكُنْ عَلَيْهَا مِنْهُ شَيْءٌ، وَإِنْ لَبِسْتَهُ لَمْ يَكُنْ عَلَيْكَ شَيْءٌ " فَجَلَسَ الرَّجُلُ، وَحَتَّى إِذَا طَالَ مَجْلِسُهُ قَامَ، فَرَأَاهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ مُوَلِّيًا، فَأَمَرَ بِهِ، فَدُعِيَ لَهُ، فَلَمَّا جَاءَ.

قَالَ: "مَاذَا مَعَكَ مِنَ الْقُرْآنِ ؟".

قَالَ: مَعِيَ سُورَةٌ كَذَا، وَسُورَةٌ كَذَا، عَدَدَهَا.

فَقَالَ: "تَقْرَأُهُنَّ عَنْ ظَهْرِ قَلْبِكَ ؟".

قَالَ: نَعَمْ، قَالَ: " اِذْهَبْ، فَقَدْ مَلَكَتُكَهَا بِمَا مَعَكَ مِنَ الْقُرْآنِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ.

وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ: { اِنْطَلِقْ، فَقَدْ زَوَّجْتُكَهَا، فَعَلَّمَهَا مِنَ الْقُرْآنِ {

وَفِي رِوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: { اُمْكَنَّاكَهَا بِمَا مَعَكَ مِنَ الْقُرْآنِ {

وَلِأَبِي دَاوُدَ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ قَالَ: { مَا تَحْفَظُ ؟ " قَالَ: سُورَةُ الْبَقَرَةِ، وَالَّتِي تَلِيهَا. قَالَ: " قُمْ . فَعَلَّمَهَا عِشْرِينَ آيَةً {

Kutoka kwa Sahl bin Sa'd As-Saa'idiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Alikuwa mwanamke hadi kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Nimekuja kukupa nafsi yangu.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamtazama juu mpaka chini kisha akainamisha kichwa chake. Yule mwanamke alipoona kuwa hakumuambia lolote aliketi. Mtu mmoja katika Maswahaba akasema: “Ee Rasuli wa Allaah, ikiwa huna haja naye niozeshe mimi.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Una kitu?” Akasema: “Sina Wa-Allaahi Ee Rasuli wa Allaah!” Akasema: “Nenda kwa jamaa zako utazame kama utapata kitu.” Akaenda kisha akarudi, akasema: “Wa-Allaahi sikupata kitu!” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Tafuta hata kama ni pete ya chuma.” Akaenda kisha akarudi, akasema: “Wa-Allaahi Ee Rasuli wa Allaah! Sikupata hata pete ya chuma! Lakini nina hiki kikoi changu.” Sahli (mpokezi wa Hadiyih) amesema: Alikuwa hana shuka. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Atakifanya nini kikoi chako? Ukikivaa yeye hatakuwa na kitu, naye akikivaa wewe hutakuwa na kitu.” Yule mtu akaketi kwa kitambo kirefu kisha akainuka. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuona akienda zake, akaamrisha aitwe, alipokuja akasema: “Umehifadhi kiasi gani cha Qur-aan?” Akasema: “Nimehifadhi Suwrah kadha wa kadhaa.” akazihesabu Suwrah alizohifadhi, akasema: “Umezihifadhi kwa moyo?” Akasema: “Ndiyo” Akasema: “Nimekuoza kwa ulichohifadhi katika Qur-aan.”[10] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Na katika Riwaayah ya Abuu Daawuud aliyoipokea kutoka kwa Abuu Hurayrah: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuuliza umehifadhi nini?” Akasema: “Suwratul-Baqarah na inayofuatia.”

Akasema Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Nenda ukamfundishe Aayah ishirini.”

833.

وَعَنْ عَامِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ الزُّبَيْرِ، عَنْ أَبِيهِ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَعْلِنُوا النِّكَاحَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aamir bin ‘Abdillaah bin Az-Zubayr[11] kutoka kwa baba yake amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tangazeni ndoa.”[12] [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Al-Haakim]

834.

وَعَنْ أَبِي بُرْدَةَ بْنِ أَبِي مُوسَى، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا نِكَاحَ إِلَّا بِوَلِيٍّ} رَوَاهُ أَحْمَدُ وَالْأَرْبَعَةُ وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْمَدِينِيِّ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَأَعْلَى بِالْإِسْأَلِ

Kutoka kwa Abuu Burdah bin Abiy Muwsaa kutoka kwa baba yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ndoa haiswihi ila kwa walii.”[13] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha Ibn Al-Madiyniyy, At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan, na wengine wameiona na ila kwa kuwa ni Mursal]

835.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَيُّمَا امْرَأَةٍ نَكَحْتُ بِغَيْرِ إِذْنٍ وَلِيِّهَا، فَنِكَاحُهَا بَاطِلٌ، فَإِنْ دَخَلَ بِهَا فَلَهَا الْمَهْرُ بِمَا اسْتَحَلَّ مِنْ فَرْجِهَا، فَإِنْ اشْتَجَرُوا فَالسُّلْطَانُ وَلِيُّ مَنْ لَا وَلِيَ لَهُ} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَصَحَّحَهُ أَبُو عَوَانَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamke yeyote anayeolewa bila idhini ya walii wake ndoa yake ni batili. (Mume) akimuingilia mwanamke huyo ana haki ya kupata mahari kwa alichohalalishia tupu yake. Wakishindana,[14] basi sultani (mtawala) ni walii wa asiyekuwa na walii.” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaa’iy, na akaisahihisha Abuw ‘Awaanah, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

836.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا تُنْكَحُ الْأَيِّمُ حَتَّى تُسْتَأْمَرَ، وَلَا تُنْكَحُ الْبَكْرُ حَتَّى تُسْتَأْذَنَ} قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ، وَكَيْفَ إِذْنُهَا؟ قَالَ: " أَنْ تَسْكُتَ {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asiolewe mke mkuu mpaka atakwe amri, wala asiolewe mwanamwali mpaka atakwe idhini.[15] Maswahaba wakasema: Ee Rasuli wa Allaah! Ni vipi idhini yake (huyo mwali)? Akasema: Ni kunyamaza.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

837.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ {الثَّيِّبُ أَحَقُّ بِنَفْسِهَا مِنْ وَلِيِّهَا ، وَالْبَكْرُ تُسْتَأْمَرُ ، وَإِذْنُهَا سَكُونُهَا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ
وَفِي لَفْظٍ: {لَيْسَ لِلْوَلِيِّ مَعَ الثَّيِّبِ أَمْرٌ ، وَالْيَتِيمَةُ تُسْتَأْمَرُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَالنَّسَائِيُّ ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mke mkuu ana haki zaidi kwa nafsi yake kuliko walii wake,[16] na mwanamwali hutakwa idhini, na idhini yake ni kunyamaza.” [Imetolewa na Muslim]

Katika tamshi lingine inasema: “Walii hana amri kwa mke mkuu. Yatima huombwa idhini.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

838.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا تُزَوِّجُ الْمَرْأَةَ الْمَرْأَةَ، وَلَا تُزَوِّجُ الْمَرْأَةَ نَفْسَهَا } رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamke hamuozeshi mwanamke, wala mwanamke hajiozeshi mwenyewe.” [17] [Imetolewa na Ibn Maajah na Ad-Daaraqutwniy na wapokezi wake ni madhubuti]

839.

وَعَنْ نَافِعٍ ، عَنْ ابْنِ عُمَرَ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنِ الشَّغَارِ، وَالشَّغَارُ: أَنْ يُزَوِّجَ الرَّجُلُ ابْنَتَهُ عَلَى أَنْ يُزَوِّجَهُ الْآخَرُ ابْنَتَهُ، وَلَيْسَ بَيْنَهُمَا صَدَاقٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَاتَّفَقَا مِنْ وَجْهِ آخَرَ عَلَى أَنَّ تَفْسِيرَ الشَّغَارِ مِنْ كَلَامٍ نَافِعٍ

Kutoka kwa Naafi’ naye kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza ndoa ya Ash-Shighaar. Ash-Shighaar ni mtu kumuoza binti yake ili yule mwingine naye amuoze binti yake bila mahari baina yao.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Wameafikiana (Al-Bukhaariy na Muslim) wa njia nyingine kuwa tafsiri ya Ash-Shighaar iliyoielezwa ni maneno ya Naafi’]

840.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ جَارِيَةً بَكَرًا أَتَتْ
النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَذَكَرَتْ: أَنَّ أَبَاهَا زَوَّجَهَا
وَهِيَ كَارِهَةٌ، فَخَيَّرَهَا النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {
رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَأَعْلَى بِالْإِسْلاَمِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Kuna
binti mmoja bikra (mwanamwali) alimuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamueleza kuwa baba yake alimuozesha naye
(binti huyo) akiwa amechukia. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
akamkhiyarisha.”[18] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na Ibn
Maajah na imedhoofishwa kwa kuwa ni Mursal]

841.

وَعَنْ الْحَسَنِ، عَنْ سَمُرَةَ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
وَسَلَّمَ قَالَ: { أَيُّمَا امْرَأَةٍ زَوَّجَهَا وَلِيَّانٍ، فَهِيَ لِلأَوَّلِ مِنْهُمَا {
رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَحَسَنُهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Hasan naye kutoka kwa Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:
“Mwanamke yeyote aliyeozeshwa na mawalii wawili, basi yeye ni
mke wa mume aliyeozeshwa na walii wa kwanza.”[19] [Imetolewa
na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu
Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

842.

وَعَنْ جَابِرٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَيُّمَا عَبْدٍ تَزَوَّجَ بِغَيْرِ إِذْنِ مَوَالِيهِ أَوْ أَهْلِهِ، فَهُوَ عَاهِرٌ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ، وَكَذَلِكَ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtumwa yeyote[20] anayeo bila idhini ya mabwana zake au jamaa zake huyo ni mzinifu.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuwd na At-Tirmidhiy na ameisahihisha vile vile Ibn Hibbaan]

843.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يُجْمَعُ بَيْنَ الْمَرْأَةِ وَعَمَّتِهَا، وَلَا بَيْنَ الْمَرْأَةِ وَخَالَتِهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asikusanye (asioe) mtu baina ya mwanamke na shangazi yake wala baina ya mwanamke na mama yake mdogo.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

844.

وَعَنْ عُثْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا يَنْكِحُ الْمُحْرِمُ، وَلَا يُنْكَحُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ. وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ: {وَلَا يَخْطُبُ} وَزَادَ ابْنُ حِبَّانَ: {وَلَا يُخْطَبُ عَلَيْهِ}

Kutoka kwa ‘Uthmaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuhirimia[21] haoi wala kuozaesha.” [Imetolewa na Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine: “...wala kuposa.”

Na Ibn Hibbaan ameongeza: “...wala haposewi.”

845.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {تَزَوَّجَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ مَيْمُونَةَ وَهُوَ مُحْرِمٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِمُسْلِمٍ: عَنْ مَيْمُونَةَ نَفْسِهَا {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ تَزَوَّجَهَا وَهُوَ حَلَالٌ}

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimoa Maymuwnah hali ya kuwa amehirimia.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim kutoka kwa Maymuwnah mwenyewe amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuoa hali ya kuwa ametoka kuhirimia.”

846.

وَعَنْ عُقْبَةَ بْنِ عَامِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ أَحَقَّ الشُّرُوطِ أَنْ يُوفَّى بِهِ، مَا اسْتَحَلَّتُمْ بِهِ الْفُرُوجَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Uqbah bin ‘Aamir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika masharti yalio na haki zaidi kutekelezwa[22] ni yale mnayohalalishia tupu.”[23] [Al-Bukhaariy, Muslim]

847.

وَعَنْ سَلَمَةَ بْنِ الْأَكْوَعِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {رَخَّصَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَامَ أُوطَاسٍ فِي الْمُنْتَعَةِ، ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ، ثُمَّ نَهَى عَنْهَا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Salamah bin Al-Akwa’ (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliruhusu mwaka wa Vita vya Awtwaas ndoa ya Mut’ah[24] siku tatu kisha akaikataza.” [Imetolewa na Muslim]

848.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ الْمُنْتَعَةِ عَامَ خَيْبَرَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza ndoa ya Mut’ah mwaka wa Vita vya Khaybar.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

849.

وَعَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {نَهَى عَنْ مُتْعَةِ
النِّسَاءِ وَعَنْ أَكْلِ الْحُمْرِ الْأَهْلِيَّةِ يَوْمَ خَيْبَرَ} أَخْرَجَهُ السَّبْعَةُ
إِلَّا أَبَا دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza Mut’ah ya wanawake na kula nyama ya punda wa mjini siku ya vita vya Khaybar.” [Imetolewa na As-Sab’ah (Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad) isipokuwa Abuu Daawuwd]

850.

عَنِ الرَّبِيعِ بْنِ سَبْرَةَ، عَنْ أَبِيهِ، رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ:

{إِنِّي كُنْتُ أَذْنِتُ لَكُمْ فِي الْإِسْتِمْتَاعِ مِنَ النِّسَاءِ، وَإِنَّ اللَّهَ قَدْ حَرَّمَ ذَلِكَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، فَمَنْ كَانَ عِنْدَهُ مِنْهُنَّ شَيْءٌ فَلْيُخَلِّ سَبِيلَهَا وَلَا تَأْخُذُوا مِمَّا آتِيَتْموهُنَّ شَيْئًا} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ وَأَبُو دَاوُدَ وَالنَّسَائِيُّ وَابْنُ مَاجَةَ وَ أَحْمَدُ وَ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ar-Rabiy' bin Sabrah[25] kutoka kwa baba yake amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Nilikuwa nimewaruhusu ndoa ya Mut’ah ya wanawake, kwa hakika Allaah Ameiharamisha ndoa hiyo mpaka siku ya Qiyaamah. Ambaye ana mke wa mut’ah basi amuache aende zake wala msichukue chochote mlichowapa.” [Imetolewa na Muslim, Abuu Daawuwd, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad na Ibn Hibbaan]

851.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَعَنَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ الْمُحَلَّلَ وَالْمُحَلَّلَ لَهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ
وَفِي الْبَابِ: عَنْ عَلِيٍّ أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيُّ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amemlaani mwenye kuhalalisha na mwenye kuhalalishwa.”[26] ‘Mwenye kuhalalisha’ ni mtu kumuoa mwanamke aliyeachwa na mume mwingine talaka tatu kwa niyyah ya kumhalalishia yule mume wa kwanza baada ya yeye kumtaliki baada ya kujamiiana naye. [Imetolewa na Ahmad na An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy akaisahihisha]

Katika mlango huu kuna Hadiyth iliyopokewa kutoka kwa ‘Aliy iliyopokewa na Maimaam wane (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy.

852.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يَنْكِحُ الزَّانِي الْمَجْلُودُ إِلَّا مِثْلَهُ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mzinifu aliyepigwa mijeledi asioe isipokuwa mfano wake.”[27] [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuwd na wapokezi wake ni waaminifu (madhubuti)]

853.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، قَالَتْ: { طَلَّقَ رَجُلٌ امْرَأَتَهُ ثَلَاثًا، فَتَزَوَّجَهَا رَجُلٌ، ثُمَّ طَلَّقَهَا قَبْلَ أَنْ يَدْخُلَ بِهَا، فَأَرَادَ زَوْجُهَا أَنْ يَتَزَوَّجَهَا، فَسُئِلَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ ذَلِكَ، فَقَالَ: "لَا. حَتَّى يَذُوقَ الْآخِرُ مِنْ عُسَيْلَتِهَا مَا ذَاقَ الْأَوَّلُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Mtu mmoja alimtaliki mkewe mara tatu, yule mke akaolewa na mwanamme mwingine, kisha akamuacha kabla ya kumuingilia, yule mume wake wa kwanza akataka kumuoa, akamuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuhusu jambo hilo. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Hapana mpaka mwingine aonje asali yake ile aliyoionja wa kwanza.” (yaani baada ya kuoa mpaka mujamiiane).[28] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

[1] Hii ina maanisha ikiwa mmoja wenu ana uwezo na nguvu za kuoa (kimwili na kimali) na aoe. Wanazuoni wengine wanaona kuwa ni jambo la lazima na wengine wanaona ni jambo lenye kupendeza tu.

[2] Hii ina maana kuzidisha sana katika ‘Ibaadah hakutakiwi. Jambo hilo linamfanya mtu kuchoka na kumfanya asiweze kutekeleza Swalaah za faradhi. Mtu anaweza kutoka katika Uislamu anapofikiria kuwa Swalaah zake anazoswali (na kuzidisha sana) ni bora kuliko Swalaah alizoswali Nabiyy (ﷺ).

[3] At-Tabattul ina maana ya kutokuoa, mtu kudhani kuwa kuacha kwake kuoa ni aina ya ‘Ibaadah na kudhani kuwa kuoa kwake ni zuio la kufanya kwake ‘Ibaadah. Tabattul kwa Wanazuoni wote ni jambo lisilofaa na ni tendo lililoharamishwa. Hata hivyo, kutokuoa kwa sababu zisizozuilika ni jambo lingine kabisa.

[4] Nabiyy (ﷺ) amesema kuwa kuna mambo manne yanayomfanya na kumshawishi mtu kuoa. Katika mambo haya manne Muislamu anatakiwa achague mwanamke mwenye Dini. Ikiwa mwanamke ataolewa kwa sifa nyinginezo, kuna uwezekano wa mtu kupotoka na kuacha Dini. Sababu nyingine ya kuchagua Dini ni kuwa mwanamke huyo ndie mwalimu wa mwanzo kwa watoto, hivyo kwa Dini yake atawaongoza watoto katika njia iliyonyooka.

[5] Maana ya neno hili: “Mikono yako itachafuka” Waarabu hulisema kwa njia ya kulaumu, wala siyo kwa kupendelea maana yake halisi ya kumtakia mtu shari. Maana ya Hadiyath hii ni kuwa: kwa kawaida watu huoa mwanamke mwenye sifa hizi nne, basi wewe fanya hima umuoe aliyeshika Dini.

[6] Nabiyy (ﷺ) alikuwa na tabia ya kuwaombea waliofunga ndoa kwa du’aa nzuri nzuri katika umoja wao, mapenzi na kuwaombea Baraka katika maisha yao.

[7] Hizi ni zile sehemu zenye kuonekana kwa nje, kama vile; urefu, uso, mikono na mfano wa hayo.

[8] Alikuwa miongoni mwa Maswahaba wa Answaar, ukoo wa Haarith. Alihudhuria vita vyote isipokuwa vita vya Tabuwk. Alisilimu kupitia kwa Musw'ab bin 'Umayr. Alikufa akiwa na umri wa miaka 77 katika mwaka wa 43 Hijriyyah.

[9] Katazo hili limewekwa ili ile posa ya kwanza ya nduguye ithibiti. Ikiwa msichana alishaposwa na mtu mwingine, mtu wa pili asipeleke posa. Hata hivyo ikiwa posa ya kwanza imekataliwa au kuvunjika, basi ni ruhusa posa nyingine iende.

[10] Hadiyth hii inaweka wazi mambo mengi: Miongoni mwa hayo ni kufundisha Qur-aan kunaweza kuwa ndio mahari ya mtu. Kingine kilichowekwa wazi hapa ni kuwa kiwango cha mahari hakijawekwa. Watu wengine wanatoa dalili ya Hadiyth kuwa kiwango cha chini cha mahari ni Dirham kumi. Hili si sahihi na Hadiyth hiyo haina msingi huo.

[11] Huyu ni 'Aamir bin 'Abdillaah bin Az-Zubayr bin Al-'Awwaam Al-Asadi Al-Qurayshi Al-Madaniy. Alikuwa ni Taabi' na alisikia Hadiyth kutoka kwa baba yake na wengineo. Alikuwa madhubuti na Mwenye taqwa alifariki mwaka wa 124 Hijriyyah.

[12] Sherehe za harusi ni bora zitangazwe ili kuondoa fedheha ya aina yoyote na kadhalika kwa sababu zinginezo. Kuna njia nyingi za matangazo aina hii. Mashahidi katika tukio la ndoa ni matangazo vile. Kutangaza katika kadamnasi ya watu ni aina nyingine ya matangazo.

[13] Hadiyth hii imetajwa na takriban Maswahaba thelathini wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Baadhi ya wapokezi wake ni thiqah (madhubuti). Walii (msimamizi) wa kwanza wa familia ni baba na babu, kisha kaka zake, baada ya hapo baba zake wadogo. Kama kuna rai tofauti kwa mawalii, yeyote aliye karibu zaidi, rai yake itafuatwa zaidi, ikiwa mawalii hao wanalingana kama vile makaka na baba wadogo, kinachofanyika ni mtawala aliyopo ndiye atakayekuwa msimamizi. Vile

vile ikiwa kuna wasimamizi wawili wameozesha mwanamke mmoja sehemu mbili tofauti, ndoa ya kwanza iliyofungwa itakuwa ni sahihi na ya pili itakuwa si sahihi. Ikiwa mwanamke aliyeozwa anakubaliana na msimamizi mmoja na kutofautiana na mwingine, rai ya mwanamke itatangulizwa.

[14] Yaani wale mawalii (wasimamizi wa mke) watakaposhindana wakamzuia mwanamke asiolewe, basi uwalii atakuwa nao sultani/mtawala.

[15] Ridhaa ya mwanamke ni jambo la msingi katika ndoa. Ikiwa walii au hata baba anamuoza binti yake bila ya ridhaa yake, binti ana haki ya kubatilisha ile ndoa na kukataa. Ayyim katika lugha ya kiarabu ni mwanamke aliyekwishawahi kuingiliwa, anaweza kuwa mjane au aliyeachwa. Mzinifu mwanamke ambaye hajaolewa ni Ayyim, lakini kulingana na Shariy'ah siyo Ayyim. Ayyim ni lazima athibitishe ndoa yake kwa kutamka, vinginevyo ndoa haitosihi. Ama bikra ambaye hajabaleghe, ridhaa yake siyo muhimu bali ni ruhusa ya walii wake.

[16] Hii ina maana ya kuwa Ayyim hawezi kuoza bila ya ridhaa yake, lakini haina maana kuwa anaweza kuolewa bila ya walii. Ikiwa kuna rai tofauti kati ya Ayyim na walii kuhusu mchumba wake na uchaguzi wa mwanamke ukawa ni kutoka katika jamaa zake wa karibu na hakuwa na uhusiano wowote nae mbaya, wakati huo walii atalazimishwa kukubaliana na Ayyim, kama walii hatokubali hilo mwanamke anaweza kuomba msaada wa mtawala wa kumuoza. Dhul Arhaam (ndugu upande wa mama) hawezi kuwa walii.

[17] Kuhusu ndoa mwanamke hawezi kuwa msimamizi au walii, hawezi kujioza wala hawezi kuoza mwanamke mwingine.

[18] Ina maana bila ridhaa ya mwanamke, awe bikra au mkuu (Ayyim), hawezi kuoza, akiolewa bila ya ridhaa yake, ana haki ya kukataa na kuvunja, hata ikiwa ni baba yake au kaka yake ndiye msimamizi wa ndoa ile.

[19] Ikiwa mawalii wawili wamemuoza mwanamke kwa waume wawili basi ndoa itakayopita ni ya yule mume aliyoozeshwa na walii wa kwanza na ndoa ya pili itakuwa sio sahihi. Ama kama ndoa hizo zitakuwa zimefungwa kwa wakati mmoja, zote zitakuwa ni batili. Kuna rai mbalimbali katika hili.

[20] Kwa ndoa ya mtumwa ni wajibu kupatikana radhi za bwana wake, bila ya ruhusa yake, ndoa haitafungwa. Ikiwa mtumwa hajui ukweli huu kuwa ruhusa ya bwana inatakiwa ni muhimu na akamuingilia mkewe, hatoadhibiwa kwa hilo, lakini kama alikuwa anajua basi ataadhibiwa.

[21] Mtu akiwa katika hali ya Ihraam, kuoa au kuoza hairuhusiwi. Hii ni kulingana na Wanazuoni takribani wote. Ama kuhusu Hadiyth iliyopokewa na Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) sanad yake ni sahihi, lakini alikosea kusema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuoa Maymuwnah alipokuwa katika Ihraam. Maymuwnah mwenyewe amethibitisha hili katika Hadiyth iliyofuatia.

[22] Ina maana suala la mahari ni la msingi katika ndoa.

[23] Maana ya Hadiyth hii ni kuwa masharti yaliyo na haki zaidi kutekelezwa ni masharti ya ndoa, bora yasipite mipaka, Al-Khatwaab amesema: ‘Masharti katika ndoa, yako tofauti, muna masharti yanayopasa kutimizwa kwa itifaki ya ‘Ulamaa, nayo ni Aliyoamrisha Allaah ya kushikamana kwa wema au kwa kuachana kwa ihsani, na kwa maana hii Ulamaa wengine wameisherehesha Hadiyth hii. Kuna na masharti yasiyofaa kutekelezwa aslan kama vile mwanamke kuweka sharti mke mwenza atalikiwe. Kuna masharti yaliyo na khitilafu miongoni mwa ‘Ulamaa, kama vile kushaurisha asimuolee mke mwingine’

[24] Mut’ah ni ndoa ya muda maalumu. Aina hii ya ndoa ilikuwepo katika zama za Jaahiliyyah. Kuna wakati Uislamu ulikataza na wakati uliruhusu kwa masharti maalumu, mwishowe ndoa hii iliharamishwa katika Hijjatul-Wada’ (Hijjah ya mwisho ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ))

[25] Ar-Rabiy' bin Sabrah bin Ma'bad Al-Juhani Al-Madaniy alikuwa ni mtu madhubuti kulingana na An-Nasaaiy na Al-'Ajli.

[26] Al-Muhallil “mwenye kuhalalisha” ni mtu kumuoa mwanamke aliyeachwa na mume mwingine talaka tatu kwa niyyah ya kumhalalishia yule mume wa kwanza baada na yeye kumtaliki baada ya kujamiana naye. Ndoa iliyosimama kwa malengo haya ni haramu, iwe ni kwa muda uliotajwa au isiwe hivyo.

[27] Hii ina maana mwenye taqwa asimue mwanamke ambaye ameshatuhumiwa na kuthibitishwa kuwa ni mzinifu na vivyo hivyo mwanamke mwenye taqwa asiolewe na mwanamme mzinifu.

[28] Ina maana mwanamke aliyeachwa talaka tatu akiolewa na mtu mwingine na akawa keshaingiliwa na mume yule kisha mume akamuacha au akafariki hapo ndipo anaweza tena kuolewa na yule mume wake wa mwanzo. Kama hajakutana naye kimwili na mume wake wa pili hawezi kuolewa na yule mume wake wa mwanzo.

02-Mlango Wa Kutangamana Na Wake

بَابُ عَشْرَةِ النِّسَاءِ

02-Mlango Wa Kutangamana Na Wake

865.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَلْعُونٌ مَنْ أَتَى امْرَأَةً فِي دُبْرِهَا} رَوَاهُ

أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَرَجَالُهُ ثِقَاتٌ، وَلَكِنْ أَعْلَى
بِالْإِسْأَلِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Amelaaniwa mwenye kumjamii mkewe katika duburi yake.”[1] [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy, matini ya Hadiyth ni yake. Wapokezi wake ni madhubuti lakini imedhoofishwa kwa kuwa ni Mursal]

866.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يَنْظُرُ اللَّهُ إِلَى رَجُلٍ أَتَى رَجُلًا أَوْ امْرَأَةً فِي دُبْرِهَا } رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالنَّسَائِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَأَعْلَى بِالْوَقْفِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah Hamtazami mwanamume aliyemjamii mwanamume au mwanamke katika uchi wake wa nyuma.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan na imedhoofishwa kwa kuwa ni Mawquwf]

867.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلَا يُؤْذِي
جَارَهُ، وَاسْتَوْصُوا بِالنِّسَاءِ خَيْرًا، فَإِنَّهُنَّ خُلِقْنَ مِنْ ضِلْعٍ،
وَإِنَّ أَعْوَجَ شَيْءٍ فِي الضِّلْعِ أَعْلَاهُ، فَإِنْ ذَهَبَتْ تَقِيمُهُ كَسَرَتْهُ،
وَإِنْ تَرَكَتْهُ لَمْ يَزَلْ أَعْوَجَ، فَاسْتَوْصُوا بِالنِّسَاءِ خَيْرًا} مُتَّفَقٌ
عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

وَلِمُسْلِمٍ: {فَإِنْ اسْتَمْتَعْتَ بِهَا اسْتَمْتَعْتَ وَبِهَا عِوَجٌ، وَإِنْ
ذَهَبَتْ تَقِيمُهَا كَسَرَتْهَا، وَكَسَرُهَا طَلَاقُهَا}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayemuamini
Allaah na siku ya mwisho, asimuudhi jirani yake.[2] Wafanyieni
kheri wanawake, hakika wao wameumbwa kwa ubavu, na hakika
kitu kilichopotoka zaidi katika ubavu ni ule wa juu, ukitaka
kuunyosha utauvunja[3] na ukiuwacha utaendelea kupotoka, kwa
hivyo wafanyieni wema wanawake.” [Al-Bukhaariy, Muslim na
tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “Ukistarehe naye utastarehe naye
akiwa na upotofu. Na ukitaka kumnyoosha utamvunja na kumvunja
kwake ni kumtaliki.”

868.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كُنَّا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي غَزَاةٍ، فَلَمَّا قَدِمْنَا الْمَدِينَةَ، ذَهَبْنَا

لِنَدْخُلَ. فَقَالَ: " أَمْهَلُوا حَتَّى تَدْخُلُوا لَيْلًا يَغْنِي: عِشَاءً لِكَي تَمْتَشِطَ الشَّعِثَةُ، وَتَسْتَحِدَّ الْمَغِيبَةُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَفِي رِوَايَةٍ لِلْبُخَارِيِّ: { إِذَا أَطَالَ أَحَدُكُمْ الْغَيْبَةَ، فَلَا يَطْرُقُ أَهْلَهُ لَيْلًا }

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulikuwa pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika vita, tuliporudi Madiynah tulitaka kuingia (majumbani mwetu) Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akatuambia: Subirini,[4] ili muingie usiku yaani wakati wa ‘Ishaa ili (mke) mwenye nywele timtim apate kujichana, na yule aliyempoteza mumewe apate kujinyoa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Katika Riwaayah ya Bukhaariy imesema: “Mmoja wenu atakapokuwa safarini muda mrefu basi asiwagongee katu watu wake wakati wa usiku.”

869.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { إِنَّ شَرَّ النَّاسِ مَنْزِلَةً عِنْدَ اللَّهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، الرَّجُلُ يُفْضِي إِلَى امْرَأَتِهِ وَتُفْضِي إِلَيْهِ، ثُمَّ يَنْشُرُ سِرَّهَا } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika uovu wa watu kwa daraja kubwa mbele ya Allaah siku ya Qiyamah ni mwanamume anamjamii mkewe kisha akaeneza siri yake, na

mwanaamke anamjamii mme wake kisha anaeneza siri yake.”[5]
[Imetolewa na Muslim]

870.

وَعَنْ حَكِيمِ بْنِ مُعَاوِيَةَ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: {قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! مَا حَقُّ زَوْجِ أَحَدِنَا عَلَيْهِ؟} قَالَ: "تُطْعِمُهَا إِذَا أَكَلْتَ، وَتَكْسُوهَا إِذَا اكْتَسَيْتَ، وَلَا تَضْرِبُ الْوَجْهَ، وَلَا تُقَبِّحُ، وَلَا تَهْجُرُ إِلَّا فِي الْبَيْتِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَهَ، وَعَلَّقَ الْبُخَارِيُّ بَعْضَهُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Hakiym bin Mu'aawiyah kutoka kwa baba yake amesema: "Niliuliza: Ee Rasuli wa Allaah! Ni nini wajibu wa mke kwa mumewe? Akasema: Ni umlishe unapokula, umvishe unapovaa, wala usimpige uso, wala usimkaripie wala usimgure ila nyumbani tu." [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuwd, An-Nasaa'iy na Ibn Maajah. Al-Bukhaariy ameifanya ni Mu'alaqqah baadhi yake. Akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

871.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَتْ الْيَهُودُ تَقُولُ: إِذَا أَتَى الرَّجُلُ امْرَأَتَهُ مِنْ دُبْرِهَا فِي قُبْلِهَا، كَانَ الْوَلَدُ أَحْوَلَ. فَانْزَلَتْ: "نِسَاؤُكُمْ حَرْتُ لَكُمْ فَأَتُوا حَرَّتْكُمْ أَنَّى شِئْتُمْ" [الْبَقَرَةُ : 223]} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Mayahudi walikuwa wakisema: Mwanamume akimjamii mkewe kinyume nyume kwa uchi wa mbele mtoto akizaliwa atakuwa makengeza. Ikateremka Aayah hii: “Wake zenu ni konde kwenu. Basi ziendeeni konde zenu (panapotoka kizazi) vyovyote mpendavyo” [Al-Baqarah: 223] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

872.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ إِذَا أَرَادَ أَنْ يَأْتِيَ أَهْلَهُ قَالَ: بِسْمِ اللَّهِ. اللَّهُمَّ جَنِّبْنَا الشَّيْطَانَ وَجَنِّبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْتَنَا، فَإِنَّهُ إِنْ يُقَدَّرَ بَيْنَهُمَا وَلَدٌ فِي ذَلِكَ، لَمْ يَضُرَّهُ الشَّيْطَانُ أَبَدًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Lau mmoja wenu anapomuendea mkewe (amjamii) aseme:

اللَّهُمَّ جَنِّبْنَا الشَّيْطَانَ وَجَنِّبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْتَنَا

BismiLlaah, Allaahumma jannibnaa ash-shaytwaana wa jannibi ash-shaytwaana maa razaqtanaa (Kwa jina la Allaah, Ee Allaah Tuepushe na shaytwaan, na umuepushe shaytwaan katika Utakachoturuzuku). Kisha wakajaaliwa kupata mtoto, shaytwaan hawezi kumdhuru (mtoto huyo) milele.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

873.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا دَعَا الرَّجُلُ امْرَأَتَهُ إِلَى فِرَاشِهِ فَأَبَتْ أَنْ
تَجِيءَ، لَعَنَتْهَا الْمَلَائِكَةُ حَتَّى تُصْبِحَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ
لِلْبُخَارِيِّ
وَلِمُسْلِمٍ: {كَانَ الَّذِي فِي السَّمَاءِ سَاخِطًا عَلَيْهَا حَتَّى يَرْضَى
عَنْهَا}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamume
atakapomuita mkewe kitandani akakataa kumuendea, akalala,
Malaika wanamlaani (mke huyo) mpaka apambazukiwe.” [Al-
Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim imesema: “...Aliye mbinguni
Atamkasirikia (mke huyo) mpaka mumewe amridhie.”

874.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ {لَعَنَ الْوَاصِلَةَ وَالْمُسْتَوْصِلَةَ، وَالْوَاشِمَةَ
وَالْمُسْتَوْشِمَةَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Amemlaani mwanamke[6]

mwenye kuunga na mwenye kuungwa nywele na mwenye kuchanja na mwenye kuchanjwa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

875.

وَعَنْ جُذَامَةَ بِنْتِ وَهَبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {حَضَرْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي أَنَاسٍ، وَهُوَ يَقُولُ: لَقَدْ هَمَمْتُ أَنْ أَنْهَى عَنِ الْغِيلَةِ، فَنَظَرْتُ فِي الرُّومِ وَفَارِسَ، فَإِذَا هُمْ يُغِيلُونَ أَوْلَادَهُمْ فَلَا يَضُرُّ ذَلِكَ أَوْلَادَهُمْ شَيْئًا. ثُمَّ سَأَلُوهُ عَنِ الْعَزْلِ؟ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "ذَلِكَ الْوَادُ الْخَفِيُّ" رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Judhaamah bint Wahb[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilikuwa pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipowaambia watu: Nilitamani kukataza Ghiylah,[8] Nikatazama Warumi na Wafursi nikawakuta wanawafanyia Ghiylah watoto wao wala hilo halidhuru chochote watoto wao. Kisha Maswahaba wakamuuliza kuhusu ‘Azli’[9] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaambia Huko ndiko kuua kwa siri.” [Imetolewa na Muslim]

876.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَجُلًا قَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ لِي جَارِيَةً، وَأَنَا أَعْزِلُ عَنْهَا، وَأَنَا أَكْرَهُ أَنْ

تَحْمِلَ، وَأَنَا أُرِيدُ مَا يُرِيدُ الرَّجَالُ، وَإِنَّ الْيَهُودَ تُحَدِّثُ: أَنَّ الْعَزَلَ الْمَوْوَدَّةَ الصُّغْرَى. قَالَ: " كَذَبَتْ يَهُودُ، لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَخْلُقَهُ مَا اسْتَطَاعَتْ أَنْ تَصْرِفَهُ { رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَالطَّحَاوِيُّ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa "Mtu mmoja alimjia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Mimi nina mjakazi, nami namfanyia 'azli nachukia kubeba kwake mimba, nami nataka wanayotaka wanaume (kujimai) na Mayahudi huwa wanasema kuwa kufanya 'azli ni mauaji madogo. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akasema: Wayahudi wamedanganya, lau Allaah Angalitaka kumuumba mtoto wewe usingaliweza kumzuia." [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud, An-Nasaa'iy na Atw-Twahaawiyy, na wapokezi wake ni madhubuti]

877.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كُنَّا نَعَزِلُ عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَالْقُرْآنُ يَنْزِلُ، وَلَوْ كَانَ شَيْئًا يُنْهَى عَنْهُ لَنَهَانَا عَنْهُ الْقُرْآنُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِمُسْلِمٍ: {فَبَلَغَ ذَلِكَ نَبِيَّ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَلَمْ يَنْهَنَا}

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Tulikuwa tukifanya 'Azl katika zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ)

(وَالَيْهِ وَسَلَّمَ) na Qur-aan inateremka. Lau kama (‘azl) ingekuwa ni jambo analokataza basi Qur-aan ingelitukataza.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim inasema: “...habari hiyo ikamfikia Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wala hakutukataza.”

878.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَطُوفُ عَلَى نِسَائِهِ بِغُسْلٍ وَاحِدٍ } أَخْرَجَاهُ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alikuwa akiwazungukia wakeze kwa joshu moja.”[10] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

[1] Wanazuoni wote wamekubaliana kuwa kumuingilia mwanamke nyuma ni haraam.

[2] Kumkera na kumuudhi Muislamu ni jambo lisilotakiwa, ama kumuudhi jirani ni katika madhambi makubwa.

[3] Hadiyth hii inatufundisha kuwa wanawake waamiliwe kwa wema. Tabia ya mwanamke ni tofauti na ya mwanamume. Kuna sababu nyingi za matatizo anayoyapata mwanamke. Mwanamke ni kama ubavu, ambao ukiunyoosha utauvunja. Tabia ya maumbile aliyoubwa nayo mwanamke haiwezi kubadilika.

[4] Hii ina maana ikiwa mtu ametoka safari ya mbali, si vizuri kuenda nyumbani kwake moja kwa moja. Ni vizuri kutuma taarifa ya kufika kwako kwanza. Kuna sababu nyingi kuhusu jambo hili. Mume

anapoondoka, mwanamke hajiangelii kwa kujiremba na kujiweka vizuri kama kunyoa sehemu zake na usafi mzima wa mwili wake. Suala hili linaweza kuonekana dogo lakini linaweza kumfanya mume akapunguza mapenzi kwa mke wake.

[5] Ina maana ya kuelezea lile tendo kwa watu wengine, kwa hakika kufanya jambo hili kunapelekea katika kufanya jambo la haraam.

[6] Katika Hadiyth hii wamelaaniwa wanawake aina nne: 1-Wenye kuunga nywele, 2-Wenye kuungwa nywele, 3-Wenye kuchanja (tattoo), 4- Wenye kuchanjwa (tattoo) katika miili yao.

[7] Judhaamah bint Wahb ni dada yake ‘Ukaashah bin Mihdhan kwa mama, jina lake lingine ni Jundal Al-Asadiyyah. Alikuwa ni Swahaba miongoni mwa Waislamu wa mwanzo. Alihajiri Madiynah. Alikuwa ni mke wa Anis bin Qataadah.

[8] Ghiylah ni mwanamume amjamii mkewe naye ananyonyesha au akiwa ni mjamzito.

[9] ‘Azl ni kumjamii mkewe na ukifika wakati wa kushusha manii akayamwaga nje kwa ajili ya kupanga kizazi. Suala la uhalaal na uharaam wa ‘Azl ni kuwa kuna Hadiyth kuhusiana na suala hili. Ikiwa imeamuliwa kuwa ‘Azl ni halaal na kwa wakati huo huo Shariy’ah haipendekezi. Kwa kadhia ya mwanamke ambaye afya yake ni mbaya hapa ‘Azl itakuwa lina lengo la kuokoa maisha.

[10] Lengo la Hadiyth hii kuwa ugawaji wa muda haukuwa wajibu kwa Nabiyy (ﷺ). Ingalikuwa ni wajibu kwake kama kwa watu wengine asingelazimika kuwazunguka wote kwa usiku mmoja.z

03-Mlango Wa Mahari

بَابُ الصَّدَاقِ

03-Mlango Wa Mahari

879.

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَنَّهُ أَعْتَقَ صَفِيَّةً، وَجَعَلَ عِتْقَهَا صَدَاقَهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “alimuacha huru Swafiyyah[1] na akafanya kumuacha huru kwake ndio mahari yake.”[2] [Al-Bukhaariy, Muslim]

880.

وَعَنْ أَبِي سَلَمَةَ بْنِ عَبْدِ الرَّحْمَنِ، رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ قَالَ: {سَأَلْتُ عَائِشَةَ زَوْجَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ كَمْ كَانَ صَدَاقُ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَتْ: كَانَ صَدَاقُهُ لِأَزْوَاجِهِ ثِنْتِي عَشْرَةَ أُوقِيَّةً وَنَشَأُ. قَالَتْ: أَتَدْرِي مَا النَّشْ؟ قَالَ: قُلْتُ: لَا. قَالَتْ: نِصْفُ أُوقِيَّةٍ. فَتِلْكَ خَمْسُمِائَةٍ دِرْهَمٍ، فَهَذَا صَدَاقُ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ لِأَزْوَاجِهِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Salamah bin ‘Abdir-Rahmaan[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilimuuliza ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) mahari

ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ilikuwa kiasi gani?[4]
Akasema: Mahari ya wakeze yalikuwa ni wakia kumi na mbili na An-Nash. Akasema: Unajua ni nini An-Nash? Akasema Hapana. Akasema: ni nusu wakia. Kwa hivyo hizo ni dirhamu mia tano (500) haya ndiyo mahari ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kwa wakeze.” [Imetolewa na Muslim]

881.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : { لَمَّا تَزَوَّجَ عَلِيٌّ فَاطِمَةَ عَلَيْهِمَا السَّلَامُ . قَالَ لَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " أَعْطَيْتَهَا شَيْئًا " ، قَالَ : مَا عِنْدِي شَيْءٌ . قَالَ : " فَأَيْنَ دِرْعُكَ الْخُطْمِيَّةُ ؟ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ ، وَالنَّسَائِيُّ ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Aliy alipomuoa Faatwimah عَلَيْهِمَا السَّلَامُ, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia: Mpe kitu (kama mahari yake), ‘Aliy akasema: Sina kitu, Rasuli wa Allaah akasema: Iko wapi ile deraya yako ya Al-Hutwamiyyah?.”[5] [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na akaisahihisha Al-Haakim]

882.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { أَيُّمَا امْرَأَةٍ نَكَحْتَ عَلَى صَدَاقٍ، أَوْ حِبَاءٍ، أَوْ عِدَّةٍ، قَبْلَ عِصْمَةِ النِّكَاحِ، فَهُوَ لَهَا، وَمَا كَانَ بَعْدَ عِصْمَةِ النِّكَاحِ، فَهُوَ لِمَنْ أُعْطِيَ، وَأَحَقُّ مَا أُكْرِمَ الرَّجُلُ عَلَيْهِ ابْنَتُهُ، أَوْ أُخْتُه } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamke yeyote anayeolewa kwa mahari, zawadi au kwa ahadi ya kupewa zawadi kabla ya kifungo cha ndoa, basi kitu hicho ni chake.[6] Na kinachotolewa baada ya kifungo cha ndoa hicho ni cha aliyepewa. Na kilicho haki zaidi mtu kukirimiwa kwa sababu yake ni binti yake au dada yake.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa At-Tirmidhiy.

883.

وَعَنْ عَلْقَمَةَ، عَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُ سُئِلَ عَنْ رَجُلٍ تَزَوَّجَ امْرَأَةً، وَلَمْ يَفْرِضْ لَهَا صَدَاقًا، وَلَمْ يَدْخُلْ بِهَا حَتَّى مَاتَ، فَقَالَ ابْنُ مَسْعُودٍ: لَهَا مِثْلُ صَدَاقِ نِسَائِهَا، لَا وَكُسٍ، وَلَا شَطْطٌ، وَعَلَيْهَا الْعِدَّةُ، وَلَهَا الْمِيرَاثُ، فَقَامَ مَعْقِلُ بْنُ سِنَانٍ الْأَشْجَعِيُّ فَقَالَ: قَضَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي بَرُوعَ بِنْتِ وَاشِقٍ امْرَأَةً مِثْلَ مَا قَضَيْتَ،

885.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَامِرٍ بْنِ رَبِيعَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ ، عَنْ أَبِيهِ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَجَازَ نِكَاحَ امْرَأَةٍ عَلَى نَعْلَيْنِ } أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ، وَخُولِفَ فِي ذَلِكَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Aamir bin Rabiyy’ah[10] kutoka kwa baba yake (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Ameruhusu mwanamke kuolewa kwa (mahari ya) viatu.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha na amekhalifiwa katika hilo (la kufanya Hadiyth kuwa ni sahihi)

886.

وَعَنْ سَهْلٍ بْنِ سَعْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { زَوَّجَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ رَجُلًا امْرَأَةً بِخَاتِمٍ مِنْ حَدِيدٍ } أَخْرَجَهُ الْحَاكِمُ.

وَهُوَ طَرَفٌ مِنَ الْحَدِيثِ الطَّوِيلِ الْمُتَقَدِّمِ فِي أَوَائِلِ النِّكَاحِ

Kutoka kwa Sahl bin Sa’d (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuoza mtu mwanamke kwa (mahari ya) pete ya chuma.” [Imetolewa na Al-Haakim nayo ni sehemu katika Hadiyth ndefu iliyotangulia mwanzo wa Mlango wa Ndoa][11]

887.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَا يَكُونُ الْمَهْرُ أَقَلَّ مِنْ عَشْرَةِ دَرَاهِمٍ} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ مَوْقُوفًا، وَفِي سَنَدِهِ مَقَالٌ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mahari haiwi chini ya dirhamu kumi.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy ikiwa ni Mawquwf na katika Isnaad yake kuna maelezo]

888.

وَعَنْ عُقْبَةَ بْنِ عَامِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {خَيْرُ الصَّدَاقِ أَيْسَرُهُ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Uqbah bin ‘Aamir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mahari yalio na kheri ni yalio mepesi.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Al-Haakim]

889.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا {أَنَّ عَمْرَةَ بِنْتَ الْجَوْنِ تَعَوَّذَتْ مِنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ حِينَ أُدْخِلَتْ عَلَيْهِ تَعْنِي: لَمَّا تَزَوَّجَهَا فَقَالَ: "لَقَدْ عُدْتُ بِمَعَاذٍ"، فَطَلَّقَهَا، وَأَمَرَ

أَسَامَةُ فَمَتَّعَهَا بِثَلَاثَةِ أَثْوَابٍ { أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَفِي إِسْنَادِهِ
رَأَوْ مَثْرُوكٌ

وَأَصْلُ الْقِصَّةِ فِي "الصَّحِيحِ" مِنْ حَدِيثِ أَبِي أُسَيْدٍ السَّاعِدِيِّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Amrah bint
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ Al-Jawn alijilinda dhidi ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّم) wakati alipoingia kwake (siku aliyomuoa). Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّم) akasema: Kwa hakika umejilinda kwa kinga.
Akamtaliki na akamuamrisha Usaamah ampe (mwanamke yule) nguo tatu.” [Imetolewa na Ibn Maajah na katika Isnaad yake kuna mpokezi anayeachwa. Asili ya kisa chenyewe kimo katika Swahiyh Al-Bukhaariy kutoka katika Hadiyth ya Abuu Usayd As-Saa’idiy]

[1] Huyu ni Mama wa Waumini Swafiyyah bint Huyai bin Al-Akhtwab, ni kutoka katika kizazi cha Nabiyy Haaruwn. Mwanzoni alikuwa ameolewa na Kinaanah bin Abdil-Huqaiq ambaye aliuwawa katika vita vya Khaybar. Swafiyyah alitekwa, kisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّم) alimchagua kuwa mke wake na akasilimu. Aliachwa huru na uhuru wake ndiyo iliyokuwa mahari yake. Alifariki mwaka 50 Hijriyyah na alizikwa katika makaburi ya Baqi’

[2] Hii ina maana mahari inaweza kuwa kitu kisichokuwa fedha.

[3] Huyu ni Abuu Salamah bin ‘Abdir-Rahmaan bin ‘Awf Az-Zuhri Al-Qurayshiy. Huyu ni mmoja katika Mafuqahaa saba wakubwa katika mji wa Madiynah na ni miongoni mwa Taabii’ wakubwa. Ni madhubuti na amepokea Hadiyth nyingi ambazo alizisikia kutoka katika makundi mbalimbali ya Maswahaba na kutoka kwa waliopokea kutoka kwake. Alifariki mwaka 94 au 104 katika mapokezi mengine akiwa na umri wa miaka 70.

[4] Hakuna kiwango maalumu cha mahari katika Shariy'ah, hata hivyo kuifanya ndogo zaidi kunapendeza, ili kuifanya ndoa kuwa ni nyepesi kwa watu wengi.

[5] Ni deraya iliyotengenezwa na watu wa kabila la Al-Hutwamah, walikuwa mahodari wa kutengeneza maderaya ya kivita. Hadiyth hii ni dalili kuwa bwana arusi anatakiwa ampe mkewe kitu kabla ya kumuingilia.

[6] Hii ina maana kila kilichoamuliwa kabla ya ndoa ni mahari, na yote yanakuwa ni ya muolewa. Ikiwa zawadi hiyo ni ya fedha, dhahabu, nguo, ardhi, nyumba au kitu kingine chochote, yeye ndiye mmiliki kamili wa kitu hicho. Ikiwa kuna kitu chochote watachopewa jamaa za binti baada ya kuolewa kwake, hilo halitazingatiwa kuwa ni mahari, na si milki ya binti. Ni zawadi aliyopewa mtu tu.

[7] Huyu ni 'Alqamah bin Qays Abu Shibl bin Maalik katika kabila la Banu Bakr bin An-Nakha, amepokea Hadiyth nyingi kutoka kwa 'Umar na Ibn Mas-'uwd. Alikuwa ni Taabi' mkubwa, alikuwa maarufu kwa Hadiyth ya Abdullaah bin Mas'uwd na kuwa na usuluba naye, alikuwa ni mjomba wa Al-Aswad bin An-Nakahi alifariki mwaka 61 Hijriyyah.

[8] Jina hili la Birwa' lina ikhtilafu kwa Wanazuoni wa lugha ambao wao humuita Barwa' na Wanazuoni wa Hadiyth humuita Birwa'

[9] Sawiyq ni unga wa mtama au wa mahindi au wa shayiri uliokaangwa.

[10] Huyu ni Abuu 'Imraan 'Abdillaah bin 'Aamir bin Rabiyy'ah Al-Anzi. Alikuwa ni mwenye umri wa miaka minne au mitano pindi Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipofariki. Alifariki mwaka wa 85 Hijriyyah.

[11] Tazama Hadiyth ya 832.

04-Mlango Wa Waliymah (Karamu Ya Harusi)

بَابُ الْوَلِيْمَةِ

04-Mlango Wa Waliymah (Karamu Ya Harusi)

890.

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ رَأَى عَلَى عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَوْفٍ أَثَرَ صُفْرَةٍ، قَالَ: { " مَا هَذَا؟ " ، قَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي تَزَوَّجْتُ امْرَأَةً عَلَى وَزْنِ نَوَافٍ مِنْ ذَهَبٍ. فَقَالَ: " فَبَارَكَ اللَّهُ لَكَ، أَوْلِمَ وَلَوْ بِشَاةٍ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alimuona ‘Abdir-Rahmaan bin ‘Awf ana athari ya manukato ya zafarani, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Una jambo gani? Akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Nimeoa mwanamke (fulani) kwa uzito wa kokwa ya dhahabu.[1] Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Allaah Akubarikie. Fanya waliymah (karamu) japo mbuzi.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

891.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {إِذَا دُعِيَ أَحَدُكُمْ إِلَى الْوَلِيمَةِ فَلْيَأْتِهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِمُسْلِمٍ: {إِذَا دَعَا أَحَدُكُمْ أَخَاهُ، فَلْيُجِبْ، عُرْسًا كَانَ أَوْ نَحْوَهُ}

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anapoalikwa mmoja wenu katika waliymah (karamu) aende.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim inasema: “Mmoja wenu anapomualika nduguye ajibu (aende) iwe ni harusi au mfano wake.” [2]

892.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {شَرُّ الطَّعَامِ طَعَامُ الْوَلِيمَةِ: يُمْنَعُهَا مَنْ يَأْتِيهَا، وَيُدْعَى إِلَيْهَا مَنْ يَأْبَاهَا، وَمَنْ لَمْ يُجِبِ الدَّعْوَةَ فَقَدْ عَصَى اللَّهَ وَرَسُولَهُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Chakula kibaya ni chakula cha waliymah (karamu ya harusi) kinanyimwa anayekiendea na hualikwa anayekikataa. Na asiyejibu mualiko atakuwa amemuasi Allaah na Rasuli wake.” [Imetolewa na Muslim]

893.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {إِذَا دُعِيَ أَحَدُكُمْ فَلْيُجِبْ، فَإِنْ كَانَ صَائِمًا فَلْيُصَلِّ، وَإِنْ كَانَ مُفْطِرًا فَلْيُطْعَمْ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ أَيْضًا
وَلَهُ مِنْ حَدِيثِ جَابِرٍ نَحْوُهُ. وَقَالَ: {فَإِنْ شَاءَ طَعِمَ وَإِنْ شَاءَ تَرَكَ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anapoalikwa mmoja wenu aitike, akiwa ana swawm aombe du’aa na akiwa hana swawm basi ale.” [Imetolewa na Muslim]

Vile vile Muslim amepokea kutoka katika Hadiyth ya Jaabir kama hiyo na akasema: “Akipenda atakula na akipenda ataacha”

894.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {طَعَامُ الْوَلِيمَةِ أَوَّلَ يَوْمٍ حَقٌّ، وَطَعَامُ يَوْمِ الثَّانِي سُنَّةٌ، وَطَعَامُ يَوْمِ الثَّلَاثِ سُمْعَةٌ، وَمَنْ سَمِعَ سَمِعَ اللَّهُ بِهِ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَاسْتَغْرَبَهُ، وَرِجَالُهُ رِجَالُ الصَّحِيحِ
وَلَهُ شَاهِدٌ: عَنْ أَنَسٍ عِنْدَ ابْنِ مَاجَةَ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Chakula cha waliymah (karamu) siku ya kwanza ni haki, chakula cha siku ya pili

ni Sunnah, na chakula cha siku ya tatu ni riyaa. Mwenye kuidhihirisha amali yake kwa riyaa Allaah Atamfedhehesha Siku ya Qiyaamah.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy]

895.

وَعَنْ صَفِيَّةَ بِنْتِ شَيْبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {أَوْلَمَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَلَى بَعْضِ نِسَائِهِ بِمُدَّيْنٍ مِنْ شَعِيرٍ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Swafiyyah bint Shaybah[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alifanya waliymah (karamu) alipomuowa mmoja katika wakeze kwa pishi mbili za shayiri.”[4] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

896.

وَعَنْ أَنَسٍ قَالَ: {أَقَامَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بَيْنَ خَيْبَرَ وَالْمَدِينَةِ ثَلَاثَ لَيَالٍ، يُبْنَى عَلَيْهِ بِصَفِيَّةَ، فَدَعَوْتُ الْمُسْلِمِينَ إِلَى وَلِيمَتِهِ، فَمَا كَانَ فِيهَا مِنْ خُبْزٍ وَلَا لَحْمٍ، وَمَا كَانَ فِيهَا إِلَّا أَنْ أَمَرَ بِالْأَنْطَاعِ، فَبُسِطَتْ، فَأُلْقِيَ عَلَيْهَا التَّمْرُ، وَالْأَقِطُ، وَالسَّمْنُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Anas amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikaa siku tatu baina ya Khaybar na Madiynah akimkamilishia Swafiyyah ndoa yake. Nikawaalika Waislamu katika waliymah (karamu) yake, hakukuwa na mkate wala nyama. Akaamrisha iletwe

busati la ngozi likatandikwa ikawekwa juu yake tende, aqitw[5] na samli.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

897.

وَعَنْ رَجُلٍ مِنْ أَصْحَابِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا اجْتَمَعَ دَاعِيَانِ، فَأَجِبْ أَقْرَبَهُمَا بَابًا، فَإِنْ سَبَقَ أَحَدُهُمَا فَأَجِبِ الَّذِي سَبَقَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَسَنَدُهُ ضَعِيفٌ

Kutoka kwa mtu mmoja katika Maswahaba amehadithia kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wanapojumuika waalikaji wawili nenda kwa yule ambaye mlango wake uko karibu zaidi (nawe), mmoja kati yao atakapotangulia (kukualika) nenda kwa yule aliyetangulia.”[6] [Imetolewa na Abuu Daawuud na Isnaad yake ni dhaifu]

898.

وَعَنْ أَبِي جُحَيْفَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا أَكُلُ مُتَكِنًا} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Juhayfah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mimi sili nikiwa nimeegemea.”[7] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

899.

وَعَنْ عُمَرَ بْنِ أَبِي سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { يَا غُلَامُ! سَمِّ اللَّهَ، وَكُلْ بِيَمِينِكَ، وَكُلْ مِمَّا يَلِيكَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [8] Kutoka kwa ‘Umar bin Abuu Salamah[8] amesema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ee kijana! Mtaje Allaah, na kula kwa mkono wako wa kuume, na kula kinachokuelekea.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

900.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَتَى بِقِصْعَةٍ مِنْ ثَرِيدٍ، فَقَالَ: "كُلُوا مِنْ جَوَانِبِهَا، وَلَا تَأْكُلُوا مِنْ وَسْطِهَا، فَإِنَّ الْبَرَكَةَ تَنْزِلُ فِي وَسْطِهَا } رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ، وَهَذَا لَفْظُ النَّسَائِيِّ، وَسَنَدُهُ صَحِيحٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliletewa sahani ya thariyd[9] akasema: kuleni kando yake wala msile katikati yake, kwa hakika Baraka huteremka kati kati yake” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na tamshi hili ni la An-Nisaa’iy na Isnaad yake ni Swahiyh]

901.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مَا عَابَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ طَعَامًا قَطُّ، كَانَ إِذَا إِشْتَهَى شَيْئًا أَكَلَهُ، وَإِنْ كَرِهَهُ تَرَكَهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hajapatapo kamwe hakukiaibisha chakula, alikuwa akitamani kitu hula na asipokipenda hukiacha.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

902.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا تَأْكُلُوا بِالشَّمَالِ، فَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَأْكُلُ بِالشَّمَالِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msile kwa kushoto, hakika shaytwaan hula kwa kushoto.” [Imetolewa na Muslim]

903.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا شَرِبَ أَحَدُكُمْ، فَلَا يَتَنَفَّسْ فِي الْإِنَاءِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِأَبِي دَاوُدَ: عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ نَحْوَهُ، وَزَادَ: {أَوْ يَنْفُخُ فِيهِ} وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Abuu Qataadah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Yeyote kati yenu anapokunywa asipumue ndani ya chombo.”[10] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Abuu Daawuwd amepokea Riwaayah kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Abbaas Hadiyth kama hii na akaongezea: “...wala asipumulie humo.” [Na ameisahihisha At-Tirmidhiy]

[1] Nawaah ya dhahabu ni takribani gramu 18.4 za dhahabu

[2] Kujibu mwito wa sherehe ya harusi au jambo lingine ni wajibu, isipokuwa kuwe kuna yenye kuchukiza, hapo haifai kwenda. Na iwapo atenda na akaona chukizo hilo anawajibika kuukanya, wasipokatazika wanapaswa waondoke.

[3] Huyu ni Swafiyyah bint Shaybah bin ‘Uthmaan bin Abiy Twalhah Al-‘Abadariy wa ukoo wa Banuu ‘Abdid-Daar. Inasemekana kuwa alimuona Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wakati wengine wanakataa hilo. Ibn Sa’d anakiri kuwa alikuwa Taabi’iy

[4] Shayiri nafaka inayofanana na ngano inayotumika kuwa chakula

[5] Aqitw ni maziwa yaliyogandishwa kwa moto

[6] Hadiyth hii ni dalili kuwa mtu anapoalikwa na watu wawili kwa pamoja basi aliye na haki ya kujibiwa ni yule aliyetangulia, wakilingana katika hilo atatangulizwa jirani. Na majirani wako kwa daraja, mwenye haki zaidi ni yule ambaye mlango wake uko karibu zaidi na mlango wako, wakilingana kwa hilo itapigwa kura.

[7] Al-Khatwabi amesema: “Makusudio ya ‘kuegemea’ katika Hadiyth hii ni kuketi juu ya tandiko laini kama yule aliyekusudia kula sana bali alikuwa akiketi bila kujituliza (ili asile sana) na huwa akila kidogo.”

Wengine wamesema kuwa ‘kuegemea’ ni mtu kula kwa kuegemea kwa ubavu wake.

[8] ‘Umar bin Abiy Salamah ‘Abdillaah bin ‘Abdil-Asad bin Hilaal Al-Makhzuwm, alikuwa ni mtoto wa Ummul-Muuminiyna Ummu Salamah. Alizaliwa katika nchi ya Uhabeshi (Ethiopia) baina ya Hijrah ya Uhabeshi na ile ya Madiynah. Alifariki katika mji wa Madiynah mwaka 83 Hijriyyah.

[9] ‘*Thariyd*’, ni mikate mepesi mikavu inayopikwa kwa unga wa shayiri (talbiynah/barley) na inakatwakatwa na kuchanganywa na supu ya nyama au mchuzi. Inasemekana ni chakula tokea zama za Nabiyy Ibraahiym (‘Alayhis-Salaam) mpaka zama za Nabiyy Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam). Ni chakula waliokuwa wakikaribishwa Hujaji wa Makkah kabla ya Uislamu.

[10] Hii ina maana ni pale anapokunywa mtu asipumulie kwenye chombo, kwani ni sababu ya kueneza magonjwa.

05-Mlango Wa Kugawa (Zamu)

بَابُ الْقَسَمِ

05-Mlango Wa Kugawa (Zamu)

904.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقْسِمُ، فَيَعْدِلُ، وَيَقُولُ: "اللَّهُمَّ هَذَا قَسَمِي

فِيمَا أَمْلِكُ، فَلَا تَلْمَنِي فِيمَا تَمْلِكُ وَلَا أَمْلِكُ { رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ،
وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَالْحَاكِمُ، وَلَكِنْ رَجَّحَ التِّرْمِذِيُّ إِسْرَافَهُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akigawa muda baina ya wakeze, na akifanya uadilifu na anasema: Ee Allaah! Huu ni mgao wangu[1] katika ninachokimiliki, usinilaumu kwa kile unachomiliki nami sikimiliki.” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisa Ibn Hibbaan na Al-Haakim, lakini At-Tirmidhiy ametilia nguvu kuwa ni Mursal]

905.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { مَنْ كَانَتْ لَهُ إِمْرَاتَانِ، فَمَالَ إِلَى أَحَدَاهُمَا،
جَاءَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَشِقُّهُ مَائِلٌ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَسَنَدُهُ
صَحِيحٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye wake wawili, na akaegemea zaidi kwa mmojawapo,[2] Siku ya Qiyaamah atakuja ilhali ubavu wake mmoja umeinama.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na Isnaad yake ni sahihi]

906.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مِنَ السُّنَّةِ إِذَا تَزَوَّجَ الرَّجُلُ الْبَكَرَ عَلَى النَّثِيبِ أَقَامَ عِنْدَهَا سَبْعًا، ثُمَّ قَسَمَ، وَإِذَا تَزَوَّجَ النَّثِيبَ أَقَامَ عِنْدَهَا ثَلَاثًا، ثُمَّ قَسَمَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Katika Sunnah (mtu) anapooa mwanamwali juu ya mke mkuu akalale kwake siku saba kisha agawanye (siku). Na anapooa mke mkuu akae kwake siku tatu kisha agawanye (siku).” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

907.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ لَمَّا تَزَوَّجَهَا أَقَامَ عِنْدَهَا ثَلَاثًا، وَقَالَ: "إِنَّهُ لَيْسَ بِكَ عَلَى أَهْلِكَ هَوَانٌ، إِنْ شِئْتَ سَبَعْتُ لَكَ، وَإِنْ سَبَعْتُ لَكَ سَبَعْتُ لِنِسَائِي} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipomuoa alikaa kwake siku tatu na akamuambia: Hutapata udhalilifu kwangu, nikipenda nitakukamilishia siku saba na iwapo nitakukamilishia siku saba vile vile nitawakamilishia wake zangu wote siku saba.” [Imetolewa na Muslim]

908.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا { أَنَّ سَوْدَةَ بِنْتَ زَمْعَةَ وَهَبَتْ
يَوْمَهَا لِعَائِشَةَ، وَكَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقْسِمُ
لِعَائِشَةَ يَوْمَهَا وَيَوْمَ سَوْدَةَ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Sawdah bint Zam’ah aliitoa siku yake[3] kumpa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akimgawia ‘Aaishah siku yake na siku ya Sawdah.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

909.

وَعَنْ عُرْوَةَ قَالَ: { قَالَتْ عَائِشَةُ: يَا ابْنَ أُخْتِي! كَانَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ لَا يُفْضِلُ بَعْضَنَا عَلَى بَعْضٍ
فِي الْقِسْمِ مِنْ مَكْتَبِهِ عِنْدَنَا، وَكَانَ قَلَّ يَوْمٌ إِلَّا وَهُوَ يَطُوفُ
عَلَيْنَا جَمِيعًا، فَيَذْنُو مِنْ كُلِّ امْرَأَةٍ مِنْ غَيْرِ مَسِيسٍ، حَتَّى يَبْلُغَ
الَّتِي هُوَ يَوْمُهَا، فَيَبِيتُ عِنْدَهَا { رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ
وَاللَّفْظُ لَهُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

وَلِمُسْلِمٍ: عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ إِذَا صَلَّى الْعَصْرَ دَارَ عَلَى نِسَائِهِ،
ثُمَّ يَذْنُو مِنْهُنَّ { الْحَدِيثُ

Kutoka kwa ‘Urwah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Aaishah aliniambia: Ee mpwa wangu! Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa hamfadhilishi yeyote miongoni mwetu katika mgawo wa kukaa kwake kwetu. Alikuwa akitutembelea sisi sote,

akimkaribia kila mke bila ya kufanya jimai mpaka afike kwa yule ambaye ni siku yake[4] akalala kwake.” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawud na matini ya Hadiyth ni yake, na akaisahisha Al-Haakim]

Na katika Riwaayah ya Muslim kutoka kwa ‘Aaishah inasema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anapomaliza kuswali alasiri akiwazungukia wakeze na akiwakaribia (kwa kuwabusu na kuwakumbatia)...” Mpaka mwisho wa Hadiyth

910.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَسْأَلُ فِي مَرَضِهِ الَّذِي مَاتَ فِيهِ: " أَيْنَ أَنَا غَدًا ؟ " ، يُرِيدُ: يَوْمَ عَائِشَةَ، فَأَذِنَ لَهُ أَنْ يَزُوجَهُ يَكُونُ حَيْثُ شَاءَ، فَكَانَ فِي بَيْتِ عَائِشَةَ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa katika maradhi yake aliyofia alikuwa akiuliza: “Kesho nitakuwa wapi?”[5] akikusudia siku ya ‘Aaishah. Wakeze wakamruhusu abaki pale anapopapenda. Akakaa katika nyumba ya ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

911.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ إِذَا أَرَادَ سَفَرًا أَقْرَعَ بَيْنَ نِسَائِهِ، فَأَيَّتُهُنَّ خَرَجَ سَهْمُهَا، خَرَجَ بِهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipokuwa anataka kusafiri hupiga kura baina ya wakeze, yoyote atakayepata kura husafiri pamoja naye.”[6] [Al-Bukhaariy, Muslim]

912.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَمْعَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا يَجْلِدُ أَحَدُكُمْ امْرَأَتَهُ جَلْدَ الْعَبْدِ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Zam’ah[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu asimpige mkewe kipigo cha mtumwa.”[8] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

[1] Haikuwa muhimu kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuenda kwa wake zake kwa zamu, pamoja na kuwa alikuwa na mapenzi zaidi kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا), lakini aliendelea kufanya uadilifu kwa wake zake wengine. Kila mara alimuomba Allaah Amsamehe.

[2] Katika hali hii uadilifu hapa unakusudiwa ni ule wa vitu na kuwahudumia kwa usawa katika mahitaji mengine na kutoa zamu. Yote haya mtu ana uwezo wa kuyafanya au kutoyafanya, na haya ndio ataulizwa kama ameyafanyia uadilifu. Kumpenda mtu na moyo kutekwa na mtu huyo si dhambi, maadamu halimzuii kufanya uadilifu.

[3] Hadiyth hii ina maana kwamba ikiwa mwanamke atakubaliwa mwenyewe kupunguziwa fedha zake za matumizi au zamu ya mumewe kwake, ni jambo linaloruhusiwa na mwanamme katika jambo hili si wa kulaumiwa, hata hivyo, ana haki ya kudai kurejeshewa haki yake wakati wowote.

[4] Hapa zamu inakusudiwa kulala kwake. Vinginevyo, mmoja anaweza kuruhusiwa kuongea na wengine na kuenda katika nyumba zao.

[5] Hii ina maana wakati wa ugonjwa wake, kuwepo kwa niyyah tu ya kubaki kwa mmoja sio tatizo. Hii ina maana ya ruhusa ya wake wengine, mtu anaweza kukaa kwa mmoja wao. Ugonjwa huu wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ulianzia kwa Maymwunah.

[6] Jina linalotokeza katika kura basi ndie wa kufuatana na Nabiyy katika safari zake. Siku zote za safari hazihesabiwi katika zamu. Hata hivyo wake wanaweza kukubaliana wenyewe bila ya kuwepo kwa kura.

[7] Huyu ni ‘Abdullaah bin Zam’ah bin Al-Aswad bin ‘Abdil-Mutwalib bin Asad bin ‘Abdil-‘Uzza Al-Asadi, ni kaka wa Ummul Muuminiyina Sawdah bint Zam’ah. Alikuwa ni Swahaba mkubwa katika wakazi wa Madiynah. Aliuawa katika siku ya Ad-Daar.

[8] Ni haraam kumpiga mwanamke katika hali zozote isipokuwa moja tu la kufanya uzinifu. Haifai kumpiga usoni au kumpiga kiasi cha kumvunja, katika hali kama hiyo mume ataadhibiwa.

06-Mlango Wa Mlango Wa Khul’

بَابُ الْخُلْعِ

Mlango Wa Khul’[1]

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ امْرَأَةً ثَابِتِ بْنِ قَيْسٍ أَتَتْ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! ثَابِتُ بْنُ قَيْسٍ مَا أَعِيبُ عَلَيْهِ فِي خُلُقٍ وَلَا دِينٍ، وَلَكِنِّي أَكْرَهُ الْكُفْرَ فِي الْإِسْلَامِ، قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " أَتُرَدِّينَ عَلَيْهِ حَدِيثَهُ؟ "، قَالَتْ: نَعَمْ. قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ " إِقْبِلِ الْحَدِيثَ، وَطَلِّقِيهَا تَطْلِيقًا " رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ.

وَفِي رِوَايَةٍ لَهُ: { وَأَمْرُهُ بِطَلَاقِهَا }

وَلِأَبِي دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيِّ وَحَسَنَهُ: { أَنَّ امْرَأَةً ثَابِتِ بْنِ قَيْسٍ اخْتَلَعَتْ مِنْهُ، فَجَعَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عِدَّتَهَا حَيْضَةً }

وَفِي رِوَايَةٍ عَمْرٍو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ عِنْدَ ابْنِ مَاجَةَ: { أَنَّ ثَابِتَ بْنَ قَيْسٍ كَانَ دَمِيمًا وَأَنَّ امْرَأَتَهُ قَالَتْ: لَوْلَا مَخَافَةُ اللَّهِ إِذَا دَخَلَ عَلَيَّ لَبَسَقْتُ فِي وَجْهِهِ }

وَلِأَحْمَدَ: مِنْ حَدِيثِ سَهْلِ بْنِ أَبِي حَثْمَةَ: { وَكَانَ ذَلِكَ أَوَّلَ خُلْعٍ فِي الْإِسْلَامِ }

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa:

“Mke wa Thaabit bin Qays[2] alimuendea Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ)

(وَالِإِسْلَامِ) na akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Thaabit bin Qays simtii kasoro katika tabia wala Dini lakini nachukia kukufuru nikiwa

Muislamu. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Utamrudishia shamba lake?” Akasema: Ndio. Rasuli wa Allaah akasema: (kumwambia Thaabit): “Kubali shamba lako na umuache talaka moja.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Katika Riwaayah yake nyingine imesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuamrisha ampe talaka.”

Katika Riwaayah ya Abuu Daawuwd na At-Tirmidhiy ambayo imesema ni Hasan: “Mke wa Thaabit bin Qays alipewa talaka kwa kurudisha shamba, Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaamuru Eda yake iwe ni kipindi kimoja cha hedhi.”

Katika Riwaayah iliyo kwa Ibn Maajah kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb amepokea kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake amesema: “Thaabit bin Qays alikuwa na sura mbaya, mkewe akasema: “Lau si kwa sababu ya kumuogopa Allaah, ningalimtemea mate usoni mwakwe wakati anapoingia!”

Ahmad amepokea kutoka Hadiyth ya Sahl bin Hathmah: “Hiyo ndiyo ilikuwa Khulu’ ya kwanza katika Uislamu.”

[1] Khulu’ maana yake kilugha ni kuvua nguo. Kulingana na Shariy’ah khulu’ ina maana ya haki aliyonayo mwanamke kuvunja ndoa. Ana haki ya kuvunja ndoa baada ya kurudisha mahari. Mtu anaweza kutoa talaka akiwa na sababu za msingi. Vivyo hivyo, mwanamke naye ana haki ya kujivua (khulu’) baada ya kurejesha mahari kama ana haki ya msingi. Kulingana na ‘Ulamaa wengine, Khulu’ ni talaka, wakati wengine wakiichukulia kuwa ni kuvunja ndoa. Kuna rai tofauti kuhusu kurudisha mahari na haswa ile ya awali. Hivyo kimsingi mwanamme hawezi kudai mahari makubwa kurejeshewa zaidi ya mahari ile aliyotoa ya asili.

[2] Thaabit bin Qays Al-Ansaar Al-Khazraj alikuwa mmoja wa Maswahaba wakubwa na alikuwa ni msemaji mkuu wa Answaar na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alishuhudia vita vya Uhud na vita vingine vilivyofuatia baada yake. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimthibitishia Jannah na aliuwawa katika vita vya Al-Yamaamah.

07-Mlango Wa Talaka

بَابُ الطَّلَاقِ

Mlango Wa Talaka-07

914.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَبْغَضُ الْحَلَالِ عِنْدَ اللَّهِ الطَّلَاقُ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَرَجَّحَ أَبُو حَاتِمٍ إِرْسَالَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Halali ichukizayo kwa Allaah ni talaka.”[1] [Imetolewa na Abuu Daawuwd na Ibn Maajah, na akaisahihisha Al-Haakim na Abuu Haatim anaiona kuwa ni Mursal]

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {أَنَّهُ طَلَّقَ امْرَأَتَهُ وَهِيَ حَائِضٌ فِي عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَسَأَلَ عُمَرُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ ذَلِكَ؟ فَقَالَ: "مُرَهُ فَلْيُرَاجِعْهَا، ثُمَّ لِيُمْسِكْهَا حَتَّى تَطْهُرَ، ثُمَّ تَحِيضَ، ثُمَّ تَطْهُرَ، ثُمَّ إِنْ شَاءَ أَمْسَكَ بَعْدُ، وَإِنْ شَاءَ طَلَّقَ بَعْدَ أَنْ يَمَسَّ، فَتِلْكَ الْعِدَّةُ الَّتِي أَمَرَ اللَّهُ أَنْ تُطَلَّقَ لَهَا النِّسَاءُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ: {مُرَهُ فَلْيُرَاجِعْهَا، ثُمَّ لِيُطَلِّقَهَا طَاهِرًا أَوْ حَامِلًا}

وَفِي رِوَايَةٍ أُخْرَى لِلْبُخَارِيِّ: {وَحُسِبَتْ عَلَيْهِ تَطْلِيقَةٌ}
وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ: قَالَ ابْنُ عُمَرَ: {أَمَّا أَنْتَ طَلَّقْتَهَا وَاحِدَةً أَوْ اثْنَتَيْنِ، فَإِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَمَرَنِي أَنْ أُرَاجِعَهَا، ثُمَّ أُمَهِّلَهَا حَتَّى تَحِيضَ حَيْضَةً أُخْرَى، وَأَمَّا أَنْتَ طَلَّقْتَهَا ثَلَاثًا، فَقَدْ عَصَيْتَ رَبَّكَ فِيمَا أَمَرَكَ مِنْ طَلَاقِ امْرَأَتِكَ}

وَفِي رِوَايَةٍ أُخْرَى: قَالَ عَبْدُ اللَّهِ بْنُ عُمَرَ: {فَرَدَّهَا عَلَيَّ، وَلَمْ يَرَهَا شَيْئًا، وَقَالَ: "إِذَا طَهُرْتَ فَلْيُطَلِّقْ أَوْ لِيُمْسِكْ}

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Alimtaliki mkewe akiwa katika hedhi zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), ‘Umar akamuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) jambo hili. Akasema: “Muamrishe amrejee kisha akae naye mpaka atwaharike, halafu akipenda atakuwa naye, na kumuingilia. Hiyo ndiyo Eda aliyoiamrisha Allaah, wanawake waachwe namna hiyo.”[2] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Katika Riwaayah nyengine ya Muslim inasema: “Muamrishe amrejee kisha amtaliki akiwa ni twahara au ana mimba.”

Katika Riwaayah nyengine ya Bukhaariy imesema: “...na itahesabiwa kuwa ni talaka moja.”

Katika Riwaayah nyengine ya Muslim kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar (alimuambia muulizaji): “Ama wewe umementaliki talaka moja au mbili, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliniamrisha nimrejee kisha niishi naye mpaka apate hedhi nyengine, kisha nimpe muda ili atwahirike, kisha nimaliki kabla ya kumgusa (kumingilia). Ama wewe umemuacha talaka tatu umemuasi Rabb wako katika Alivyokuamrisha kumtaliki mkeo.”

Katika Riwaayah nyengine imesema: “Abdullaah Ibn ‘Umar (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisema: Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamrudisha kwangu wala hakuihisabu hiyo kuwa ni talaka. Akasema: “Atakapotwahirika umtaliki au ubaki naye (akiwa ni mkewe).”

916.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَ الطَّلَاقُ عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَأَبِي بَكْرٍ، وَسَنَتَيْنِ مِنْ خِلَافَةِ عُمَرَ، طَلَاقُ الثَّلَاثِ وَاحِدَةً، فَقَالَ عُمَرُ بْنُ الْخَطَّابِ: إِنَّ النَّاسَ قَدْ اسْتَعْجَلُوا فِي أَمْرِ كَانَتْ لَهُمْ فِيهِ أُنَاةٌ، فَلَوْ أَمْضَيْنَاهُ عَلَيْهِمْ؟ فَأَمْضَاهُ عَلَيْهِمْ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: Katika zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), Abuu Bakar na miaka miwili ya mwanzo wa Ukhalifa wa ‘Umar, talaka tatu zilikuwa ni moja.[3] ‘Umar akasema: “Hakika watu wanalifanyia haraka jambo ambalo ndani yake linatakiwa upole. Itakuwa bora tukiwapitishia.” Akawapitishia. [Imetolewa na Muslim]

917.

وَعَنْ مَحْمُودِ بْنِ لَبِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أُخْبِرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ رَجُلٍ طَلَّقَ امْرَأَتَهُ ثَلَاثَ تَطْلِيقَاتٍ جَمِيعًا، فَقَامَ غَضَبَانِ ثُمَّ قَالَ: "أَيُّلَعَبُ بِكِتَابِ اللَّهِ تَعَالَى، وَأَنَا بَيْنَ أَظْهَرِكُمْ" حَتَّى قَامَ رَجُلٌ، فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَلَا أَقْتُلُهُ؟} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ وَرَوَاتُهُ مُوْتَقُونَ

Kutoka kwa Mahmuwd bin Labiyd[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliambiwa kuhusu mtu aliyemtaliki mkewe talaka tatu pamoja, akasimama kwa hasira akasema: “Kitabu cha Allaah kinachezewa nami niko miongoni mwenu?” Mtu mmoja akasimama na akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Waonaje nikamuua?” [Imetolewa na An-Nasaaiy na wapokezi wake ni madhubuti]

918.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {طَلَّقَ أَبُو رُكَانَةَ أُمَّ رُكَانَةَ}. فَقَالَ لَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "رَاجِعْ أَمْرَاتَكَ"، فَقَالَ: إِنِّي طَلَّقْتُهَا ثَلَاثًا. قَالَ: "قَدْ عَلِمْتُ، رَاجِعُهَا" رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

وَفِي لَفْظٍ لِأَحْمَدَ: {طَلَّقَ أَبُو رُكَانَةَ أَمْرَاتَهُ فِي مَجْلِسٍ وَاحِدٍ ثَلَاثًا، فَحَزَنَ عَلَيْهَا، فَقَالَ لَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "فَإِنَّهَا وَاحِدَةٌ"} وَفِي سَنَدِهَا ابْنُ إِسْحَاقَ، وَفِيهِ مَقَالٌ وَقَدْ رَوَى أَبُو دَاوُدَ مِنْ وَجْهِ آخَرَ أَحْسَنَ مِنْهُ: {أَنَّ رُكَانَةَ طَلَّقَ أَمْرَاتَهُ سُهَيْمَةَ الْبَتَّةَ، فَقَالَ: "وَاللَّهِ مَا أَرَدْتُ بِهَا إِلَّا وَاحِدَةً، فَرَدَّهَا إِلَيْهِ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ"}.

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Abuu Rukaanah alimtaliki Ummu Rukaanah. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Mrudie mkeo”. Abuu Rukaanah akamuambia: “Nimemtaliki talaka tatu.” Akamuambia: “Najua mrejee (mkeo).” [Imetolewa na Abuu Daawuwd]

Katika tamshi lingine la Ahmad imesema: “Abuu Rukaanah alimtaliki mkewe talaka tatu katika kikao kimoja, halafu akahuzunika kule kumtaliki mkewe. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Hiyo ni talaka moja.” Katika Isnaad zake kuna Ibn Ishaaqa^[5] ambaye ndani yake kuna maelezo.

Abuu Daawuwd amepokea kwa njia nyengine bora zaidi kuliko hiyo ikisema: “Abuu Rukaanah alimtaliki mkewe anayeitwa Suhaymah talaka isiyorudiwa akasema: “Wallaahi nimekusudia talaka moja tu.”

Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamrudishia mkewe.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {ثَلَاثُ جُذُوهِنَّ جُذٌّ، وَهَزْلُهُنَّ جُذٌّ: النِّكَاحُ، وَالطَّلَاقُ، وَالرَّجْعَةُ} رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

وَفِي رِوَايَةٍ لِابْنِ عَدِيٍّ مِنْ وَجْهِ آخَرَ ضَعِيفٍ: {الطَّلَاقُ، وَالْعِتَاقُ، وَالنِّكَاحُ}

وَلِلْحَارِثِ ابْنِ أَبِي أُسَامَةَ: مِنْ حَدِيثِ عُبَادَةَ بْنِ الصَّامِتِ رَفَعَهُ: {لَا يَجُوزُ اللَّعِبُ فِي ثَلَاثٍ: الطَّلَاقُ، وَالنِّكَاحُ، وَالْعِتَاقُ، فَمَنْ قَالَهُنَّ فَقَدْ وَجَبْنَ} وَسَنَدُهُ ضَعِيفٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mambo matatu kweli yake ni kweli na mzaha wake ni kweli:[6] nikaah, talaka na kumrejea mke.” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha Al-Haakim]

Na katika Riwaayah nyengine ya Ibn ‘Adiyy imepokewa kwa njia nyengine dhaifu: “...talaka, kuacha huru na ndoa.”

Al-Haarith Ibn Abuu Usaamah amepokea kutoka katika Hadiyth ya ‘Ubaadah bin Asw-Swaamit ambayo ni Marfuw’: “Haifai kufanya mchezo katika mambo matatu: talaka, ndoa na kuacha huru, atakayesema maneno hayo itakuwa imepasa.” Isnaad yake ni dhaifu.

920.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِنَّ اللَّهَ تَجَاوَزَ عَنْ أُمَّتِي مَا حَدَّثَتْ بِهِ
أَنْفُسَهَا، مَا لَمْ تَعْمَلْ أَوْ تَكَلِّمْ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah
Amesamehe Ummah wangu wanayoyazungumza nafsini mwao
maadamu hawajatenda au kuyazungumza.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

921.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى وَضَعَ عَنْ أُمَّتِي الْخَطَأَ،
وَالنِّسْيَانَ، وَمَا اسْتُكْرِهُوا عَلَيْهِ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَالْحَاكِمُ،
وَقَالَ أَبُو حَاتِمٍ: لَا يَثْبُتُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kwa hakika
Allaah Amewasamehe umati wangu kukosea, kusahau na
walilolazimishwa.”[7] [Imetolewa na Ibn Maajah na Al-Haakim. Na
akasamea Abuu Haatim kuwa ‘Haikuthibitu’]

922.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {إِذَا حَرَّمَ امْرَأَتُهُ لَيْسَ بِشَيْءٍ} وَقَالَ: لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَلِمُسْلِمٍ: {إِذَا حَرَّمَ الرَّجُلُ عَلَيْهِ امْرَأَتَهُ ، فَهِيَ يَمِينٌ يُكْفَرُهَا}

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Mtu anapojiharamishia mkewe[8] hakuna kitu.” Na akasema: “Kwa hakika mna mfano mzuri kwa Rasuli wa Allaah.”[9] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na katika Riwaayah ya Muslim inasema: “Mtu anapojiharamishia mkewe hiyo ni yamini na ataitolea kafara.”

923.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا {أَنَّ ابْنَةَ الْجَوْنِ لَمَّا أُدْخِلَتْ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَدَنَا مِنْهَا. قَالَتْ: أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْكَ، قَالَ: "لَقَدْ عُدْتُ بِعَظِيمٍ، الْحَقِّي بِأَهْلِكَ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Bint Al-Jawn alipoingizwa kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na akamkaribia (Amrah) alisema: “Najilinda kwa Allaah kwa sababu yako.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

akamuambia: “Kwa hakika umejilinda kwa Mtukufu. Nenda kwa jamaa zako.”[10] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

924.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا طَلَّاقَ إِلَّا بَعْدَ نِكَاحٍ، وَلَا عِتْقَ إِلَّا بَعْدَ مِلْكٍ } رَوَاهُ أَبُو يَعْلَى، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَهُوَ مَعْلُولٌ وَأَخْرَجَ ابْنُ مَاجَهَ: عَنِ الْمِسْوَرِ بْنِ مَخْرَمَةَ مِثْلَهُ، وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ، لَكِنَّهُ مَعْلُولٌ أَيْضًا

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna talaka ila baada ya ndoa, wala hakuna kuacha huru ila baada ya kumiliki.”[11] [Imetolewa na Abuu Ya’laa, na akaisahihisha Al-Haakim nayo ni Ma’luwl

Ibn Maajah amepokea Hadiyth kama hii kutoka kwa Al-Miswar bin Makhramah, sanad yake ni hasan lakini bado inabaki kuwa ni Ma’luwl (yenye ‘illah iliyojificha)

925.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ لَا نَذَرَ لِابْنِ آدَمَ فِيمَا لَا يَمْلِكُ، وَلَا عِتْقَ لَهُ فِيمَا لَا يَمْلِكُ، وَلَا طَلَّاقَ لَهُ فِيمَا لَا يَمْلِكُ {

أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ، وَنُقِلَ عَنِ الْبُخَارِيِّ
أَنَّهُ أَصَحُّ مَا وَرَدَ فِيهِ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka
kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) amesema: “Hakuna nadhiri kwa mwana Adam katika
asichomiliki, wala kuacha huru (mtumwa) katika asiyemiliki, wala
kutoa talaka asiyoimiliki.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na At-
Tirmidhiy na wakaisahihisha.

Imenakiliwa kutoka kwa Bukhaariy kuwa Hadiyth hii ndio sahihi
zaidi iliyopokewa katika mas-ala haya.

926.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
وَسَلَّمَ قَالَ: {رُفِعَ الْقَلَمُ عَنْ ثَلَاثَةٍ: عَنِ النَّائِمِ حَتَّى يَسْتَيْقِظَ،
وَعَنِ الصَّغِيرِ حَتَّى يَكْبُرَ، وَعَنِ الْمَجْنُونِ حَتَّى يَعْقِلَ، أَوْ
يَفِيْقَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy
(صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kalamu zimeinuliwa
kwa watu watatu:[12] aliyelala mpaka atakapoamka, mtoto mdogo
mpaka atakapobaleghe na mwenda wazimu mpaka akili
itakapomrudia.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (An-Nasaaiy,
Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) isipokuwa At-Tirmidhiy, na
akaisahihisha Al-Haakim

[1] Hadiyth hii ina mafundisho mengi (kama ingethibitishwa kuwa ni Swahiyh). Kuwa siyo vitu vyote vilivyokuwa halaal vinapendezesha kwa Allaah, kwa mfano talaka ni jambo la halaal lakini siyo kila mara huwa ni jambo zuri. Ni halaal kwa kuwa katika mazingira mengine jambo linakuwa gumu na mtu kulazimishwa kuacha. Katika hali kama hizo, jambo hilo linakubaliwa, kama hakuna njia nyingine. Talaka ni kitu kisichokuwa kizuri, ni jambo linalopelekea uadui na ni furaha ya shaytwaan. Maana ya talaka ni kukiacha kitu huru kishariy'ah, na kumtoa mwanamke katika kifungo cha ndoa.

[2] Hadiyth hii nayo ina mafundisho kadhaa ndani yake: 1. Ni haraam kumuacha mwanamke akiwa katika hedhi, 2. Bila ushauri wa mwanamke, mtu anaweza kubadilisha uamuzi wake, 3. Ni Bid'ah kumuacha mwanamke katika hali ya Twuhr (ni pale mwanamke anapomaliza hedhi yake) ambapo ni ruhusa kufanya tendo la ndoa, ambapo ni sawa na wakati ule wa kumuacha akiwa na hedhi. Kuna aina nne za talaka, mbili katika hizo ni halaal na mbili zingine siyo halaal. Kumuacha wakati akiwa na mimba akiwa katika hali ya Twuhr ambapo kumuingilia hakuruhusiwi ni halaal, wakati kumuacha akiwa katika hedhi katika hali ya Twuhr ambapo huruhusiwa kumuingilia talaka ni haraam. Kwa upande mwingine kuna aina tatu za talaka: (i) Ahsan (ii) Hasan (iii) Bid'ah. **Ahsan** ni kumuacha tu pindi anapokuwa mjamzito au wakati wa Twuhr na kuacha eda ipite (eda ni muda uliopangwa wa kusubiri baada ya mwanamke kuachwa ambapo hawezi kuolewa, inatofautiana katika hali mbali mbali). **Hasan** ni kuacha mara tatu, katika ya tatu, katika nyakati tatu tofauti za Twuhr. Hadi talaka mbili au tohara mbili, mtu anaweza kuvunja talaka na kuoa tena. Akishatamka talaka ya tatu hawezi kuvunja talaka wala hawezi kumuoa tena mke wake aliyemuacha kabla ya kuolewa na mtu mwingine, ambaye inabidi amuingilie na ikija kutokea akaja kumuacha baadae ndipo anaweza kumuoa au afiwe na mumewe wa pili. **Bid'ah** ni talaka mbili au tatu kwa mara moja, 'Ulamaa wengi wana rai kuwa talaka inayotolewa wakati wa hedhi huhesabiwa.

[3] Ni nini hukumu ya talaka tatu zinazotolewa mara moja? Kuna rai mbali mbali za 'Ulamaa kuhusu suala hili. 1. Talaka tatu zinazotolewa mara moja na hazina nguvu zozote kishariy'ah. 2. Talaka tatu za mara moja zinahesabiwa na mwanamke anaachika. 3. Rai ya tatu ni kuwa talaka tatu zinazotolewa wakati mmoja zinazingatiwa kuwa ni talaka moja. 4. Rai ya nne ni kuwa ikiwa mwanamke alishaingiliwa, talaka zitahesabiwa, na kama hakingiliwa, itakuwa ni moja tu. Miongoni mwa rai hizi rai ya tatu ndiyo yenye nguvu zaidi na inayoingia akilini zaidi. Hukumu hii ndiyo

iliyokuwa wakati wa Nabiy (ﷺ), hivyo basi Abuu Rukaanah aliamrisha kumrudia mkewe baada ya kutoa talaka tatu kwa mara moja. Ingekuwa zile talaka tatu zingehesabiwa, basi Nabiy (ﷺ) asingemuamrisha kumrudia mkewe. Aina hii ya talaka inaingia katika mantiki ya watu. Kwa talaka tatu, Nabiy (ﷺ) ameweka muda wa miezi mitatu.

[4] Mahmuwd bin Labiyd bin Abuu Rafi Al-Answaaar Al-Ash-hal. Alizaliwa katika zama za Nabiy (ﷺ), ni Swahaba. Abuu Haatim amesema kuwa uswahaba wake haujulikani. Ama Imaam Muslim anamuona kuwa ni miongoni mwa Taabi'iyah. Alikuwa ni miongoni mwa 'Ulamaa, alifariki mwaka wa 96 Hijriyyah.

[5] Huyu ni Abuu 'Abdillaah Muhammad bin Ishaq bin Yassar Al-Mutwalibi, muachwa huru wa Qayd bin Makhrama Al-Madani ambaye alikuwa ni mtaalamu katika historia na medani ya vita wa Nabiy (ﷺ) na Maswahaba zake. Alikufa mwaka 51 Hijriyyah.

[6] Kuwa vitu hivi vinne kwa namna vilivyo havifanyiwi mzaha navyo ni: 1. Ndoa, 2. Talaka, 3. Kutengua talaka, 4. Kumuacha huru mtumwa.

[7] Hii ina maana kufikiria tu talaka bila ya kutenda hakuhesabiwi. Hii ina maana vile vile talaka inayotolewa kwa kulazimishwa sio talaka. Vivyo hivyo, ndoa ya kulazimishwa nayo si ndoa.

[8] Ikiwa mtu atamuambia mke wake kuwa hataendelea na uhusiano naye na kujiharamishia mke wake haizingatiwi kuwa ni talaka bali ni kiapo ambacho kinabidi kilipiwe fidia.

[9] Mfano wa Nabiy (ﷺ) hapa ni pindi alipowagomea wake zake kwa muda fulani.

[10] Aina nyingine ya talaka imewekwa wazi katika Hadiyth hii, ambayo ni 1. Ushahidi na talaka ya wazi: katika hali hii hakuna haja ya nia kulingana na maneno kuwa wazi. Ni maneno pekee yanakamilisha talaka. 2. Iwe ni moja kwa moja au kwa kuashiria: katika hali hii maneno yanakuwa kwa mafumbo, na yanaweza kuwa hayana maana ya talaka. Kwa mfano: “uko huru” au “Nenda kwa wazazi wako” n.k. maneno kama haya yanapotolewa niyyah zao zitazingatiwa lakini siyo maneno yao.

Ikiwa mzungumzaji ana maana ya talaka, basi itathibiti, na ikiwa hana niyyah hiyo basi haitothibitu.

[11] Hii ina maana kuwa mtu anaweza kumuacha mwanamke aliyemuoa tu.

[12] Hii ina maana ikiwa kuna aliyetoa talaka akiwa na usingizi talaka haiswihi. Kadhalika kichaa hatoi talaka, haitozingatiwa kuwa ni talaka.

08-Mlango Wa (Talaka Ya) Rejea

بَابُ الرَّجْعَةِ

08-Mlango Wa (Talaka Ya) Rejea

927.

عَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، {أَنَّهُ سُئِلَ عَنْ
الرَّجُلِ يُطَلَّقُ، ثُمَّ يُرَاجِعُ، وَلَا يُشْهَدُ؟ فَقَالَ: أَشْهَدُ عَلَى
طَلَاقِهَا، وَعَلَى رَجْعَتِهَا} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ هَكَذَا مَوْقُوفًا، وَسَنَدُهُ
صَحِيحٌ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Aliulizwa kuhusu mtu aliyemtaliki mkewe kisha akamrejea wala hakushuhudisha mtu. Akasema: “Shuhudisha talaka yake na kumrejea kwake.”[1] [Imetolewa na Abuu Daawuwd na ikiwa ni Mawquwf na Isnaad yake ni swahiyh]

928.

وَعَنِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّهُ لَمَّا طَلَّقَ امْرَأَتَهُ، قَالَ
النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ، لِعُمَرَ: "مُرْهُ فَلْيُرَاجِعْهَا"
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa:
Alipomtaliki mkewe, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
alimuambia: “Muamrishe amrejee.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Ina maana talaka na kumrejea mashahidi wawili ni lazima wawepo.
Kama hakuna mashahidi, mwanaume au mwanamke anaweza kufanya kitu
kwa kudanganya na ikasababisha matatizo zaidi. Kuita mashahidi ni
lazima na ni jambo lenye kupendeza. Rai ya ‘Ulamaa wengi ni kuwa ni
jambo linalopendeza kulifanya, lakini kwa ukweli haswa ni jambo la
lazima.

09-Mlango Wa Al-Iylaa, Dhwihaar, Kafaara

بَابُ الْإِيْلَاءِ وَالظُّهَارِ وَالْكَفَّارَةِ

09-Mlango Wa Al-Iylaa,[1] Dhwihaar[2], Kafaara[3]

929.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {أَلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ مِنْ نِسَائِهِ وَحَرَّمَ، فَجَعَلَ الْحَرَامَ حَلَالًا، وَجَعَلَ لِلْيَمِينِ كَفَّارَةً} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَرَوَاتُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliapa (kuwa hatawaingilia) wakeze kwa muda. Hivyo akajiharamishia (baadhi ya vitu) akafanya haraam kuwa halaal, na akafanya kafara kwa ajili ya kiapo.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na wapokezi wake ni madhubuti]

930.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {إِذَا مَضَتْ أَرْبَعَةُ أَشْهُرٍ وَقَفَ الْمُؤَلِّي حَتَّى يُطْلَقَ، وَلَا يَقَعُ عَلَيْهِ الطَّلَاقُ حَتَّى يُطْلَقَ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Inapopita miezi minne muapaji atasimama ili atoe talaka, na talaka haipiti mpaka mume atoe talaka.”[4] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

931.

وَعَنْ سُلَيْمَانَ بْنِ يَسَارٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَذْرَكْتُ بَضْعَةَ عَشَرَ مِنْ أَصْحَابِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ كُلُّهُمْ يَقِفُونَ الْمُؤَلِّي} رَوَاهُ الشَّافِعِيُّ

Kutoka kwa Sulaymaan bin Yasaar[5] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: "Nimewakuta zaidi ya Maswahaba kumi wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) wote wakimsimamisha aliyeapa." [Imetolewa na Ash-Shafi'iiyy]

932.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَ إِيلَاءُ الْجَاهِلِيَّةِ السَّنَةِ وَالسَّنَتَيْنِ، فَوَقَّتَ اللَّهُ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ، فَإِنْ كَانَ أَقَلَّ مِنْ أَرْبَعَةِ أَشْهُرٍ، فَلَيْسَ بِإِيلَاءٍ} أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ

Kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: "Ilikuwa kiapo cha Jahiliyyah[6] ni mwaka mmoja au miaka miwili, Allaah Akaweka muda wa miezi minne, inapokuwa ni uchache wa miezi minne hicho si kiapo." [7] [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy]

933.

وَعَنْهُ رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُمَا، {أَنَّ رَجُلًا ظَاهَرَ مِنْ أَمْرَاتِهِ، ثُمَّ وَقَعَ عَلَيْهَا، فَأَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: إِنِّي وَقَعْتُ عَلَيْهَا قَبْلَ أَنْ أَكْفِّرَ، قَالَ: "فَلَا تَقْرُبُهَا حَتَّى تَفْعَلَ مَا أَمَرَكَ اللَّهُ"} رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَرَجَّحَ النَّسَائِيُّ إِرْسَالَهُ

وَرَوَاهُ الْبَزَّازُ: مِنْ وَجْهِ آخَرَ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ وَزَادَ فِيهِ:
{كَفَّرَ وَلَا تَعُدْ}

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Mtu mmoja alimfanyia Dhwihaar mkewe kisha akamjamii, akamuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Mimi nimemjamii kabla ya kutoa kafara.” Akamuambia: “Usimkaribie mpaka utende Alilokuamrisha Allaah.” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy amesema ni Mursal]

Al-Bazaar ameipokea kwa njia nyingine kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) na akaongezea: “...toa kafara wala usirudie.”

934.

وَعَنْ سَلَمَةَ بْنِ صَخْرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {دَخَلَ رَمَضَانَ، فَخِفْتُ أَنْ أُصِيبَ امْرَأَتِي، فَظَاهَرْتُ مِنْهَا، فَاِنْكَشَفَ لِي مِنْهَا شَيْءٌ لَيْلَةً، فَوَقَعْتُ عَلَيْهَا، فَقَالَ لِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "حَرِّ رَقَبَةً" قُلْتُ: مَا أَمْلِكُ إِلَّا رَقَبَتِي. قَالَ: "فَصُمْ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ"، قُلْتُ: وَهَلْ أَصَبْتُ الَّذِي أَصَبْتُ إِلَّا مِنَ الصِّيَامِ؟ قَالَ: "أَطْعِمْ عِرْقًا مِنْ تَمْرٍ بَيْنَ سِتْنَيْنِ مَسْكِينًا" { أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ

Kutoka kwa Salamah bin Swakhr[8] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Uliingia mwezi wa Ramadhwaan, nikahofia kumjamii mke wangu

nikamfanyia Dhwihaar, usiku mmoja kitu kikanifunikia mwilini mwake, nikamjamii. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaniambia: “Acha mtumwa huru.” Nikamuambia: “Similiki ila shingo yangu”. Akaniambia: “Funga (Swiyaam) miezi miwili mfululizo.” Nikamuambia: “Yale yaliyonifikia ni kwa sababu ya Swiyaam.” Akaniambia: “Lisha maskini tende (vikapu) sitini.”[9]
[Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaa’iy, na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Al-Jaaruwd]

[1] Al-Iylaa ni kiapo anachoapa mtu kuwa hatomuingilia mke wake; au kumuambia mke wake moja kwa moja kwa kuapa kwa Allaah kuwa hatomuingilia tena. Allaah Ameweka muda wa miezi mine ya kurudisha uhusiano baina ya mume na mke. Ni vizuri kurudisha uhusiano, kwa kutoa kafaara kwa kiapo kwa muda uliopangwa. Vinginevyo talaka itakuwa imeshatoka; au kulingana na ‘Ulamaa wengine, mtu atalazimishwa kumuacha mkewe au kurudisha uhusiano kama mwanzoni.

[2] Dhwihaar imetokana na neno **Dhwahr** kwa maana ya mgongo au nyuma, ni kumfananisha mke wa mtu na mgongo wa mama yake. Aina hii ya mazungumzo katika lugha ya kiarabu ina maana ya kuwa: “Wewe ni kama mama yangu na ni haraam kwa ndoa yangu au kukuoa au kukuingilia”. Kulingana na Istwilahi za kishariy’ah Adhw-Dhwihaar ni kumfananisha mke wa mtu na mama wa mtu na hivyo kumfanya kuwa ni haraam kwake. Jambo hili kishariy’ah halizingatiwi kuwa ni talaka lakini ni lazima mtu atoe kafaara kabla ya kumrudia mke wake. Kafaara yake ni kumuacha huru mtu mtumwa au kufunga Swiyaam siku sitini kwa mfululizo au kuwalisha maskini sitini. Ni wajibu kutekeleza moja ya adhabu hii.

[3] Kaffaarah ina maana ya kutubia kwa madhambi hayo mawili yaliyotajwa hapo juu.

[4] Katika hali ya kuapa mtu huulizwa aache au aendeleo na mahusiano, nayo hufanyika baada ya miezi minne. Kama hataki kufanya hivyo,

anaweza kutengua ndoa yake kwa msaada wa mtawala, na baada ya kumalizia eda yake ataruhusiwa kuolewa tena.

[5] Huyu ni Abuu Ayuwb Sulaymaan bin Yasaar, muachwa huru wa Ummul-Mu'miniyn Maymuwnah. Alikuwa ni mmoja wa 'Ulamaa saba wakubwa wa Fiqhi na ni Taabi' mkubwa katika mji wa Madiynah. Ni mtu madhubuti, mwenye taqwa na Mwanazuoni. Alifariki mwaka 107H akiwa na umri wa miaka 73.

[6] Wakati wa Ujahiliyah, mwanamke alionewa sana. Wakati mwingine kwa miaka, hajulikani yuko wapi si muolewa wala si aliyeachwa, yupo katikati. Vile vile haruhusiwi kuolewa baada ya kwisha Eda yake. Mwanamke alikuwa akionewa katika hili na kuachwa kwa muda wa miaka, nayo ilikuwa aina ya kumkomoa, ndipo Allaah Alipoweka miezi minne.

[7] Hadiyth hii inaweka wazi kuwa kama mahusiano yatarudi kabla ya miezi minne, basi itakuwa siyo Iylaa na hakutokuwepo na adhabu.

[8] Huyu ni Salamah bin Swakhr bin Sulaymaan Bin As-Samma Al-Bayadi anatokana na kizazi cha Banu Bayaad, ukoo wa Al-Khazraj, mmoja katika Al-Bukauwn miongoni mwa Swahaba.

[9] Araq moja ni pishi 15 (mfuko mmoja wa tende)

10-Mlango Wa Kulaaniana

بَابُ اللَّعَانِ

Mlango Wa Kulaaniana[1]-10

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {سَأَلَ فُلَانٌ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَرَأَيْتَ أَنْ لَوْ وَجَدَ أَحَدُنَا إِمْرَأَتَهُ عَلَى فَاحِشَةٍ، كَيْفَ يَصْنَعُ؟} إِنْ تَكَلَّمَ تَكَلَّمَ بِأَمْرِ عَظِيمٍ، وَإِنْ سَكَتَ سَكَتَ عَلَى مِثْلِ ذَلِكَ! فَلَمْ يُجِبْهُ، فَلَمَّا كَانَ بَعْدَ ذَلِكَ أَتَاهُ، فَقَالَ: إِنَّ الَّذِي سَأَلْتُكَ عَنْهُ قَدْ ابْتُلِيتُ بِهِ، فَأَنْزَلَ اللَّهُ الْآيَاتِ فِي سُورَةِ النُّورِ، فَتَلَاهُنَّ عَلَيْهِ وَوَعَظَهُ وَذَكَّرَهُ، وَأَخْبَرَهُ أَنَّ عَذَابَ الدُّنْيَا أَهْوَنُ مِنْ عَذَابِ الْآخِرَةِ. قَالَ: لَا، وَالَّذِي بَعَثَكَ بِالْحَقِّ مَا كَذَبْتُ عَلَيْهَا، ثُمَّ دَعَاهَا النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَوَعَظَهَا كَذَلِكَ، قَالَتْ: لَا، وَالَّذِي بَعَثَكَ بِالْحَقِّ إِنَّهُ لَكَاذِبٌ، فَبَدَأَ بِالرَّجُلِ، فَشَهِدَ أَرْبَعَ شَهَادَاتٍ، ثُمَّ ثَنَّى بِالْمَرْأَةِ، ثُمَّ فَرَّقَ بَيْنَهُمَا {رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Fulani aliuliza: “Ee Rasuli wa Allaah! Nieleze lau mmoja wetu atamkuta mkewe katika machafu (zinaa) afanye nini? Ikiwa atazungumza basi atasema jambo kubwa, na ikiwa atanyamaza, atanyamazia kitu kibaya.” Wala hakumjibu. Baada ya hapo akamuendea tena, akasema: “Lile swali nililokuuliza mimi nimejaribiwa nalo.” Allaah akateremsha Aayah katika Suwrah An-Nuwr, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamsomea Aayah hizo akamnasihi akamkumbusha na akamueleza kuwa adhabu ya duniani ni sahali kuliko adhabu ya Aakhirah. Akasema: “Hapana, naapa kwa aliyekutuma kwa haki sikumzulia uongo!” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuita (mwanamke) akamnasihi vile

vile. Mwanamke akasema: “Hapana naapa kwa Aliyekutuma kwa haki yeye ni muongo!” Akaanza kwa mwanamume, akashuhudia mara nne kwa kiapo cha Allaah. Halafu akamgeukia yule mwanamke (akashuhudia kama yule mume), kisha akawaachanisha.” [Imetolewa na Muslim]

936.

وَعَنِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَيْضًا { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ لِلْمُتَلَاعِنَيْنِ: "حِسَابُكُمَا عَلَى اللَّهِ تَعَالَى، أَحَدُكُمَا كَاذِبٌ، لَا سَبِيلَ لَكَ عَلَيْهَا" قَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! مَالِي؟ قَالَ: "إِنْ كُنْتَ صَدَقْتَ عَلَيْهَا، فَهُوَ بِمَا اسْتَحْلَلْتَ مِنْ فَرْجِهَا، وَإِنْ كُنْتَ كَذَبْتَ عَلَيْهَا، فَذَلِكَ أَبْعَدُ لَكَ مِنْهَا" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) alisema tena kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaambia wale waliolaaniana: “Hisabu yenu iko kwa Allaah.[2] Mmoja wenu ni muongo, wewe (mume) huna njia ya kumrudia mkeo.” Yule mume akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Mali yangu?” Akasema: “Ikiwa ulisema kweli kumhusu yeye (mwanamke) basi mali hiyo ni kwa uchi wake uliojihalalishia.[3] Na ikiwa umemzulia uongo basi mali hiyo iko mbali nawe zaidi kuliko huyo (mwanamke).” [Al-Bukaariy, Muslim]

937.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَبْصِرُوهَا، فَإِنْ جَاءَتْ بِهِ أَبْيَضَ سَبْطًا فَهُوَ لِزَوْجِهَا، وَإِنْ جَاءَتْ بِهِ أَكْحَلَ جَعْدًا، فَهُوَ الَّذِي رَمَاهَا بِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtizameni, ikiwa aliyezaliwa ni mweupe maumbile yake yamekamiliwa basi ni wa mume wake, na akiwa macho yake ni kama yaliyopaka wanja na nywele koto basi huyo ni wa aliyemsingizia uzinifu (uzinzi).”[4] [Al-Bukhaariy, Muslim]

938.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَمَرَ رَجُلًا أَنْ يَضَعَ يَدَهُ عِنْدَ الْخَامِسَةِ عَلَى فِيهِ، وَقَالَ: "إِنَّهَا مُوجِبَةٌ" } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuamrisha mtu aweke mkono wake mdomoni[5] mwake katika ile mara ya tano na akasema: “Itawajibisha.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nisaa’iy na wapokezi wake ni Madhubuti]

939.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي قِصَّةِ الْمُتَلَاعِنِينَ قَالَ: {فَلَمَّا فَرَّغَا مِنْ تَلَاْعُنِهِمَا قَالَ: كَذَبْتُ عَلَيْهَا يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ أَمْسَكْتُهَا، فَطَلَّقَهَا ثَلَاثًا قَبْلَ أَنْ يَأْمُرَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Sahl bin Sa'd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kisa cha wale waliolaaniana: “Walipomaliza kulaaniana kwao mume alisema: “Nitakuwa nimemsingizia Ee Rasuli wa Allaah! Kama nitakuwa naye.” Akamtaliki talaka tatu[6] kabla ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kumuamrisha kufanya hivyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim

940.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {أَنَّ رَجُلًا جَاءَ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: إِنَّ أَمْرًا آتَى- لَا تَرُدُّ يَدَ لَامِسٍ. قَالَ: "غَرِّبَهَا". قَالَ: أَخَافُ أَنْ تَتَّبِعَهَا نَفْسِي. قَالَ: "فَاسْتَمْتِعْ بِهَا"} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالْبُزَّارُ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ.

وَأَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ مِنْ وَجْهِ آخَرَ: عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ بِأَلْفُظٍ {قَالَ: طَلَّقَهَا. قَالَ: لَا أَصْبِرُ عَنْهَا. قَالَ: "فَأَمْسِكُهَا"}.

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Mtu mmoja alimuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Mke wangu harudishi mkono wa mwenye kugusa.” [7] Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Mhamishe.” Akasema: “Nahofia kumfuata.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Basi starehe naye.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na Al-Bazzaar, na wapokezi wake ni waaminifu (madhubuti)]

Na An-Nasaaiy ameipokea kwa njia nyingine kutoka kwa Ibn ‘Abbaas kwa lafdhi: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Mtaliki.” Yule mtu akasema: “Siwezi kuwa mbali naye.” Akamuambia: “Basi baki naye.”

941.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ حِينَ نَزَلَتْ آيَةُ الْمُتَلَاعِنِينَ: "أَيُّمَا امْرَأَةٍ ادْخَلْتُ عَلَى قَوْمٍ مِنْ لَيْسَ مِنْهُمْ، فَلَيْسَتْ مِنَ اللَّهِ فِي شَيْءٍ، وَلَنْ يُدْخِلَهَا اللَّهُ جَنَّتَهُ، وَأَيُّمَا رَجُلٍ جَدَّ وَلَدَهُ وَهُوَ يَنْظُرُ إِلَيْهِ احْتَجَبَ اللَّهُ عَنْهُ، وَفَضَحَهُ اللَّهُ عَلَى رُءُوسِ الْخَلَائِقِ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ { أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Alimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema iliposhuka Aayah[8] ya wanaolaaniana: “Mwanamke yeyote amemuingiza katika watu asiye miongoni mwao[9] basi mwanamke huyo hana kitu kwa Allaah na Allaah Hatamuingiza katika Jannah Yake, na mwanaume yeyote anayekana mtoto wake naye anamuangalia, Allaah Atajitenga naye na Atamfedhehesha mbele ya watu wa mwanzo na wa mwisho.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, An-Nasaaiy na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

942.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {مَنْ أَقْرَبُ بَوْلِدٍ طَرْفَةَ عَيْنٍ، فَلَيْسَ لَهُ أَنْ يَنْفِيَهُ} أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ، وَهُوَ حَسَنٌ مَوْقُوفٌ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mwenye kumkiri mtoto wake japo kwa kupepesa jicho hana haki ya kumkana.”[10] [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy, na Hadiyth hii ni Hasan na Mawquwf]

943.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَجُلًا قَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ امْرَأَتِي وَلَدَتْ غُلَامًا أَسْوَدَ؟ قَالَ: "هَلْ لَكَ مِنْ إِبِلٍ؟" قَالَ: نَعَمْ. قَالَ: "فَمَا أَلْوَانُهَا؟" قَالَ:

حُمْرٌ. قَالَ: "هَلْ فِيهَا مَنْ أَوْرَقَ؟"، قَالَ: نَعَمْ. قَالَ: "فَأَنَّى ذَٰلِكَ؟"، قَالَ: لَعَلَّهُ نَزَعَهُ عِرْقٌ. قَالَ: "فَلَعَلَّ ابْنَكَ هَٰذَا نَزَعَهُ عِرْقٌ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ: { وَهُوَ يُعَرِّضُ بَأْنَ يَنْفِيهِ } ، وَقَالَ فِي آخِرِهِ: { وَلَمْ يُرَخِّصْ لَهُ فِي الْإِنْتِفَاءِ مِنْهُ }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: Mtu mmoja alimuendea Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Mke wangu amejiifungua mtoto mweusi.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Je, una ngamia?” Akasema: “Ndio.” Akasema: “Ni rangi gani?” Akasema: “Ni wekundu.” Akasema: “Je kuna mwenye rangi nyeusi miongoni mwao?” akasema: “Ndio.” Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Imekuwaje hilo?” Akasema: “Pengine amerithi hilo.” Akasema: “Na huyu (pia) yawezekana katika baba (na babu) zake yuko aliyekuwa na rangi hiyo na pia ikampata.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah nyingine ya Muslim inasema: “Naye anazungumza kwa mafumbo ili amkane mtoto wake.” Amesema mwisho wake: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakumkubalia kumkana mtoto wake.”

[1] Al-Li’aan inamaanisha kumtuhumu mmoja wa wanandoa kuwa amezini, bila ya kuwepo kwa ushahidi madhubuti. Ikiwa mwanamke anakana tuhuma, mwanamme analazimika kuapa viapo vine akirejea tuhuma katika kila kiapo, cha tano atasema: “Ghadhabu ya Allaah inishukie ikiwa nimesema uongo.” Ikiwa mwanamke atakaa kimya ataadhibiwa. Hata hivyo akikana hutuma, atawajibika kuapa viapo vinne

akikana tuhuma ile katika kila kiapo na katika kiapo cha tano atasema: “Ikiwa anasema kweli basi laana ya Allaah iniangukie.” Laana hii inayokusudiwa hapa inarejea katika Li’aan. Li’aan maana yake ni kuwajibisha kutengana, hakuna njia nyingine ya hawa wawili kuoana tena.

[2] Katika Hadiyth hii umuhimu umewekwa katika kufanya toba ya dhambi aliyokuwa nayo mtu.

[3] Hii ina maana kwamba mahari ya mwanamke haiwezi kurejeshwa tena kwa mume.

[4] Hadiyth hii inahusu mambo matatu: Kwanza, kuhusu mas-ala ambayo hayajawekwa wazi na wahyi, mambo hayo huwa yanatolewa ufafanuzi na Nabiyy (ﷺ). Pili: Ikiwa dalili za msingi ya maamuzi ya jambo hayapo, kuamua kwa kudhania kunakubaliwa. Tatu: kuhusu suala la Li’aan, hata ikiwa kudhania kumesibu, mwanamke hawezi kuadhibiwa kwa uzinifu.

[5] Kuweka mkono mdomoni ni dalili ya kumzindua mtu kwa kiapo cha mwisho; baada ya kiapo hiki majukumu yanarudi kwao katika maisha haya na ya kesho Aakhirah. Ikiwa mwanamme atanyamaza kwenye kiapo cha tano ataadhibiwa kwa kumsingizia na kumkashifu. mwanamke ana haki ya kufanya Li’aan akitaka.

[6] Baada ya Li’aan hakuna haja tena ya kutoa talaka, wakati huo talaka inakuwa imeshatoka. Baada ya Li’aan mwanamke hana haki ya kupokea masrufu yoyote.

[7] Ina maana nyingi: Kwanza, ni hajali anapokutana na ajnabi. Pili: ni mzinifu. Tatu: si muangalizi mzuri wa mali ya mume wake. Maana ya kwanza ndio inayoelekea kuwa sahihi zaidi. Ingekuwa maana ya pili ni sahihi basi mwenye kutuhumu inabidi aje na mashahidi, na hapo basi Li’aan itabidi ifanyike, au mwanamke angeadhibiwa. Hata hivyo yote haya hayakufanyika. Kinyume chake Nabiyy (ﷺ) alimtaka avumilie. Lau maana ya pili ingekuwa sahihi, basi Nabiyy (ﷺ) angekuwa ameruhusu yule bwana kuwa Dayyuwth (mtu asiyejali tabia mbaya aliyouwa nayo mwanamke ambaye yumo katika himaya yake)

[8] Angalia Suwrah An-Nuwr aayah ya 6 (24:6)

[9] Hii ina maana ya kuzaa mtoto ambaye si halaal kisha kuonesha kuwa ni halaal. Suala hili linaleta matatizo mengi katika mirathi, mambo ya kishariy'ah na mas-ala ya ndoa, n.k.

[10] Hatakiwi mtu kumkana mtoto wake, muda wa kuwa uzazi umeshakubalika, ikiwa hali imejitokeza hivyo, kwa upande mmoja, atakuwa ni mtoto wa kitendo cha haraam, na kwa upande wa pili mama yake atakuwa ametuhumiwa uzinifu na mtoto atatengwa na mirathi.

11-Mlango Wa: Al-'Iddah (Kukaa Eda) Na Al-Ihdaad (Matanga)

بَابُ الْعِدَّةِ وَالْإِحْدَادِ

11-Mlango Wa Al-'Iddah (Kukaa Eda)[1] Na Al-Ihdaad (Matanga)
[2]

944.

عَنْ الْمِسْوَرِ بْنِ مَخْرَمَةَ { أَنَّ سُبَيْعَةَ الْأَسْلَمِيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا
نُفِسَتْ بَعْدَ وَفَاةِ زَوْجِهَا بِلَيَالٍ، فَجَاءَتْ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ فَاسْتَأْذَنْتَهُ أَنْ تَنْكِحَ، فَأَذِنَ لَهَا، فَانْكَحَتْ { رَوَاهُ
الْبُخَارِيُّ وَأَصْلُهُ فِي "الصَّحِيحَيْنِ"
وَفِي لَفْظٍ: { أَنَّهَا وَضَعَتْ بَعْدَ وَفَاةِ زَوْجِهَا بِأَرْبَعِينَ لَيْلَةً }

وَفِي لَفْظٍ لِمُسْلِمٍ، قَالَ الزُّهْرِيُّ: {وَلَا أَرَى بَأْسًا أَنْ تَزَوَّجَ
وَهِيَ فِي دَمِهَا، غَيْرَ أَنَّهُ لَا يَقْرِبُهَا زَوْجُهَا حَتَّى تَطْهَرَ}

Kutoka kwa Al-Mis-war bin Makhramah amesema kuwa Subay'a Al-Aslamiyyah[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) alijifungua baada tu ya kufariki mumewe kwa siku chache, akamuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akimuomba idhini aolewe, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamruhusu akaolewa.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy na asili ya Hadiyth hii imo katika Swahiyh Al-Bukhaariy na Swahiyh Muslim]

Katika tamshi lingine: “...alijifungua baada ya mumewe kufariki kwa siku arubaini.”

Katika tamshi lingine la Muslim inasema: Az-Zuhriy[4] amesema: “Sioni kama pana ubaya akiolewa baada ya kujifungua hata kama yuko damuni (Nifaas), isipokuwa tu mumewe hawezi kumkaribia (kumjamii) mpaka atwahirike.”

945.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {أُمِرْتُ بِرِيرَةَ أَنْ تَعْتَدَ
بِثَلَاثِ حَيْضٍ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَةَ، وَرَوَاتُهُ ثِقَاتٌ، لَكِنَّهُ مَعْلُوفٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Bariyrah aliamrishwa akae eda hedhi tatu.”[5] [Imetolewa na Ibn Maajah, Wapokezi wake ni madhubuti lakini ina ‘illah]

946.

وَعَنْ الشَّعْبِيِّ، عَنْ فَاطِمَةَ بِنْتِ قَيْسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي الْمُطَلَّاقَةِ ثَلَاثًا: "لَيْسَ لَهَا سُكْنَى وَلَا نَفَقَةٌ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ash-Sha'biyy[6] kutoka kwa Faatwimah bint Qays (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusu mwanamke aliyeachwa talaka tatu: "Hana maskani wala chakula." [7] [Imetolewa na Muslim]

947.

وَعَنْ أُمِّ عَطِيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا تَحِدْ امْرَأَةً عَلَى مَيِّتٍ فَوْقَ ثَلَاثٍ إِلَّا عَلَى زَوْجٍ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ - وَعَشْرًا، وَلَا تَلْبَسْ ثَوْبًا مَصْبُوغًا، إِلَّا ثَوْبَ عَصَبٍ، وَلَا تَكْتَحِلْ، وَلَا تَمَسَّ طَبِيًّا، إِلَّا إِذَا طَهَّرْتَ نُبْدَةً مِنْ قُسْطٍ أَوْ أَظْفَارَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَهَذَا لَفْظُ مُسْلِمٍ وَلِأَبِي دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيِّ مِنَ الزِّيَادَةِ: { وَلَا تَخْتَضِبُ } وَلِلنَّسَائِيِّ: "وَلَا تَمْتَشِطُ"

Kutoka kwa Umami 'Atwiyyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Mwanamke haombolezi maiti zaidi ya siku tatu, isipokuwa juu ya mumewe miezi minne na siku kumi.[8] Wala asivae nguo ya rangi isipokuwa nguo ya 'aswbi,[9] wala asijipake wanja, wala asiguse manukato isipokuwa atakapotwahirika (atajipaka) kiasi kidogo tu cha

Qustwi au adhwfaari.”[10] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Katika Riwaayah ya Abuu Daawuud na An-Nisaa'iy amezidisha: “...wala asipake hina.”

Na kwa An-Nasaa'iy: “...wala asijichane.”

948.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {جَعَلْتُ عَلَى عَيْنِي صَبْرًا، بَعْدَ أَنْ تُوفِّيَ أَبُو سَلَمَةَ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ} "إِنَّهُ يَشِبُّ الْوَجْهَ، فَلَا تَجْعَلِيهِ إِلَّا بِاللَّيْلِ، وَانْزِعِيهِ بِالنَّهَارِ، وَلَا تَمْتَشِطِي بِالطَّيِّبِ، وَلَا بِالْحِنَاءِ، فَإِنَّهُ خِضَابٌ". قُلْتُ: بِأَيِّ شَيْءٍ أَمْتَشِطُ؟ قَالَ: "بِالسَّدْرِ" { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ

Kutoka kwa Ummi Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: Nilipaka swabira (aina ya dawa) machoni mwangu baada ya Abuu Salamah kufariki. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaniambia: “Hiyo hurembesha uso kwa hiyo jipake usiku, na mchana iondoe. Wala usijichane kwa manukato wala kwa hina,[11] kwani hiyo ni rangi.” Nikasema: “Nijichane kwa nini?” Akasema: “Kwa majani ya mkunazi.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaa'iy na Isnaad yake ni hasan]

949.

وَعَنْهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّ امْرَأَةً قَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ ابْنَتِي مَاتَ عَنْهَا زَوْجُهَا، وَقَدْ إِشْتَكَّتْ عَيْنُهَا، أَفَنَكْحُهَا؟ قَالَ: "لَا" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: Mwanamke mmoja alisema Ee Rasuli wa Allaah! Binti yangu amefiwa na mumewe na jicho lake linauma, je tumpake wanja? Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Hapana.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

950.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { طَلَّقْتُ خَالَتِي، فَأَرَادَتْ أَنْ تَجِدَ نَخْلَهَا فَزَجَرَهَا رَجُلٌ أَنْ تَخْرُجَ، فَأَتَتْ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: بَلْ جُدِّي نَخْلِكِ، فَإِنَّكَ عَسَى أَنْ تَصَدَّقِي، أَوْ تَفْعَلِي مَعْرُوفًا { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Khaalat wangu (Mama mdogo/mkubwa) alitalikiwa, akataka kuenda kukata mitende yake, mtu mmoja akamkanya asitoke.[12] Akamuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Akasema: “Nenda ukakate mitende yako kwani pengine ukatoa Swadaqah au ukafanya wema.”[13] [Imetolewa na Muslim]

951.

وَعَنْ فُرَيْعَةَ بِنْتِ مَالِكٍ، { أَنَّ زَوْجَهَا خَرَجَ فِي طَلَبِ عَبْدٍ لَهُ
فَقَتَلُوهُ. قَالَتْ: فَسَأَلْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ
أَرْجِعَ إِلَى أَهْلِي; فَإِنَّ زَوْجِي لَمْ يَتْرُكْ لِي مَسْكَنًا يَمْلِكُهُ وَلَا
نَفَقَةً، فَقَالَ: "نَعَمْ". فَلَمَّا كُنْتُ فِي الْحُجْرَةِ نَادَانِي، فَقَالَ: "
أَمْكُثِي فِي بَيْتِكَ حَتَّى يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ". قَالَتْ: فَأَعْتَدْتُ فِيهِ
أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا، قَالَتْ: فَقَضَى بِهِ بَعْدَ ذَلِكَ عُثْمَانُ {
أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالدُّهْلِيُّ،
وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ وَغَيْرُهُمْ

Kutoka kwa Furay'ah bint Maalik[14] amesema: Mumewe alitoka kuenda kuwatafuta watumwa wake, wakamuua. Akaeleza: Nikamuuliza Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuhusu kurudi kwa jamaa zangu kwani mume wangu hakuniachia maskani anayomiliki wala matumizi. Nabiy akaniambia: "Sawa." Nilipokuwa chumbani aliniita akaniambia: "Kaa nyumbani mwako mpaka eda imalizike." [15] Nikakaa Eda humo miezi minne na siku kumi. (Furay'ah) akasema: "Baada ya hapo 'Uthmaan akahukumu kwa hukumu hiyo." [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba'ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy, Adh-Dhuhliyy, Ibn Hibbaan, Al-Haakim na wengineo]

952.

وَعَنْ فَاطِمَةَ بِنْتِ قَيْسٍ قَالَتْ: { يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ زَوْجِي
طَلَّقَنِي ثَلَاثًا، وَأَخَافُ أَنْ يُقْتَحَمَ عَلَيَّ، قَالَ: فَأَمَرَهَا،
فَتَحَوَّلَتْ { رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Faatwimah bint Qays amesema: "Ee Rasuli wa Allaah! Mume wangu ameniacha talaka tatu nami nachelea kushambuliwa."

Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuamrisha ahame.
[Imetolewa na Muslim]

953.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { لَا تُلْبِسُوا عَلَيْنَا سُنَّةَ نَبِيِّنَا، عِدَّةُ أُمِّ الْوَلَدِ إِذَا تُؤْفِّي عَنْهَا سَيِّدُهَا أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَأَعْلَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِالْإِنْقِطَاعِ

Kutoka kwa ‘Amr bin Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Msituchanganye na Sunnah ya Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wetu. Eda ya mjakazi (aliyezalishwa na bwana wake) bwana wake akifa ni miezi minne na siku kumi.”[16] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na Ibn Maajah, na akaisahihisha Al-Haakim, na akaidhoofisha kwa kuwa Munqatw Ad-Daaraqutwniy]

954.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: { إِنَّمَا الْأَقْرَاءُ، الْأَطْهَارُ } أَخْرَجَهُ مَالِكٌ فِي قِصَّةٍ بِسَنَدٍ صَحِيحٍ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Quruwu tatu ni twahara.”[17] [Imetolewa na Maalik kwa Isnaad sahihi katika kisa fulani]

955.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {طَلَقُ الْأُمَةِ
تَطْلِيقَتَانِ، وَعِدَّتُهَا حَيْضَتَانِ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَأَخْرَجَهُ
مَرْفُوعًا وَضَعَفَهُ

وَأَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ مَاجَةَ: مِنْ حَدِيثِ
عَائِشَةَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَخَالَفُوهُ، فَاتَّفَقُوا عَلَى ضَعْفِهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Talaka ya
mjakazi ni talaka mbili, na Eda yake ni hedhi mbili.”[18] [Imetolewa
na Ad-Daaraqutwniyy ikiwa Marfuw’ na ameidhoofisha]

Na wameipokea Abuu Daawuwd, At-Tirmidhiy na Ibn Maajah
kutoka katika Hadiyth ya ‘Aaishah, na akaisahihisha Al-Haakim.
(Wanazuoni wa Hadiyth) wametofautiana nae, wameafikiana kuwa
ni dhaifu.

956.

وَعَنْ رُوَيْفِعِ بْنِ ثَابِتٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَحِلُّ لِامْرِئٍ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ
الْآخِرِ أَنْ يَسْقِيَ مَاءَهُ زَرْعَ غَيْرِهِ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ،
وَالتِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَحَسَّنَهُ الْبَزَّازُ

Kutoka kwa Ruwyfi’ bin Thaabit[19] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema
kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halaal
kwa mtu anayemuamini Allaah na siku ya mwisho kunyosheleza

maji yake katika mmea wa mtu mwingine.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan, na Al-Bazaar akasema ni Hasan]

957.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { فِي امْرَأَةِ الْمَفْقُودِ تَرَبَّصُ أَرْبَعِ سِنِينَ، ثُمَّ تَعْتَدُ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا } أَخْرَجَهُ مَالِكٌ، وَالشَّافِعِيُّ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Kuhusu mwanamke ambaye mumewe ametoweka (hajulikani aliko): “Asubiri kwa miaka minne kisha ataketi eda miezi minne na siku kumi.”[20] [Imetolewa na Maalik na Ash-Shaafi’yy]

958.

وَعَنْ الْمُغِيرَةِ بْنِ شُعْبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { امْرَأَةُ الْمَفْقُودِ امْرَأَتُهُ حَتَّى يَأْتِيَهَا الْبَيَانُ } أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Al-Mughiyrah bin Shu’bah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mke wa mume aliyetoweka (asiyejulikana aliko) anabaki kuwa ni mkewe mpaka ajiwe na ubainifu.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy kwa isnaad dhaifu]

959.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا يَبِيتَنَّ رَجُلٌ عِنْدَ امْرَأَةٍ، إِلَّا أَنْ يَكُونَ نَاكِحًا، أَوْ ذَا مَحْرَمٍ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamume yeyote asilale kwa mwanamke[21] isipokuwa awe amemuoa au ni maharimu wake.”[22] [Imetolewa na Muslim]

960.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَخْلُونَ رَجُلٌ بِامْرَأَةٍ، إِلَّا مَعَ ذِي مَحْرَمٍ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asikae faragha mwanamume na mwanamke ila awe pamoja naye maharimu.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

961.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ فِي سَبَايَا أُوطَاسٍ: {لَا تُوطَأُ حَامِلٌ حَتَّى تَضَعَ،

وَلَا غَيْرُ ذَاتِ حَمْلٍ حَتَّى تَحِيضَ حَيْضَةً { أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ،
وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ وَلَهُ شَاهِدٌ: عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ فِي الدَّارِ قُطْنِيٍّ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema katika mateka wa kabila la Awtwaas: “Mjamzito asijamiwe mpaka ajifunguwe, na asiyekuwa mjamzito asijamiwe mpaka apate hedhi moja.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha Al-Haakim nayo ina ushahidi katika Hadiyth ya ‘Abdullaah bin ‘Abbaas iliyopokewa na Ad-Daaraqutwniy]

962.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الْوَلَدُ لِلْفِرَاشِ، وَلِلْعَاهِرِ الْحَجَرُ} مُتَّفَقٌ
عَلَيْهِ مِنْ حَدِيثِهِ

وَمِنْ حَدِيثِ عَائِشَةَ فِي قِصَّةٍ وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ، عِنْدَ
النَّسَائِيِّ وَعَنْ عُثْمَانَ. عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtoto ni wa kitanda,[23] mzinifu lake ni jiwe.” [Al-Bukhaariy, Muslim kutoka katika Hadiyth yake (Abuu Hurayrah)]

Na kutoka katika Hadiyth ya ‘Aaishah katika kisa kimoja kimepokewa kwa ‘Abdullaah bin Mas-‘uud na An-Nasaaiy vile vile kimepokewa ‘Uthmaan kwa Abuu Daawuud

[1] Eda ni muda wa kusubiri ambapo mwanamke haruhusiwi kuolewa, baada ya kifo cha mumewe au kuachika. Kuna aina tatu za Eda: 1. Eda ya kuzaliwa. 2. Eda ya hedhi, na 3. Eda ya mwezi. Kwa mwanamke mwenye mimba, katika hali yoyote iwe ni kifo cha mumewe au kuachika, eda yake ni baada ya kuzaliwa mtoto. Kwa mfano ameachika au mumewe amefariki leo, na siku inayofuata akajifungua mtoto, eda yake huisha kwa kuzaliwa mtoto. Hapo anaruhusiwa kuolewa wakati wowote, lakini kwa muda wote ambapo atakuwa yupo katika nifaas hatoruhusiwa kuingiliwa na mumewe.

[2] Al-Ihdaad ni ile hali ya kuangalilia msiba, kwa mwanamke aliyefiwa na mumewe.

[3] Huyu ni Subay'a ni binti wa Al-Haarith Al-Aslamiyyah wa Banu Aslam. Alikuwa ni Swahaabiyyah. Ibn Sa'd anamtaja kuwa alikuwa ni miongoni mwa waliohajiri. Aliolewa na Sa'd bin Khawlah ambaye alifariki katika Hajjatul Wadaai' baada ya hapo akaolewa na kijana katika jamaa zake. Imetajwa katika mapokezi mengine kuwa aliolewa na Abuu Sanaabil.

[4] Huyu ni Muhammad bin Muslim bin 'Ubaidillaah bin Abdillaah bin Shihaab Al-Quraysh Az-Zuhriy, mmoja katika Maimaamu wakubwa na Mwanazuoni mkubwa katika Hijaaz na Shaam. Alikua ni kiongozi wa kizazi cha nne cha Taabi'iyna uwezo wake ulifahamika na kukubaliwa. Al-Layth anasema hakuwahi kumuona Mwanazuoni aliyekusanya elimu nyingi kama Ibn Shihaab. Maalik anaeleza Ibn Shihaab alikuwa katika watu karimu na hakuwa na mfano wake. Alifariki mwaka 124H.

[5] Mume wake Bariyrah alikuwa ni mtumwa. Baada ya kuachwa huru kutoka utumwani kama mwanamke huru, alipewa khiyari ya kuchagua kuhusu ndoa yake. Bariyrah alichagua kuvunja ndoa yake. Kwa hivyo ilibidi kukaa eda ya hedhi tatu. Hadiyth hii inamaanisha kuwa muda wa eda unaotakiwa ni kwa kuangalia hali ya mke sio ya mume.

[6] Huyu ni Abuu 'Amr 'Aamir bin Sharahil bin 'Abdillaah Ash-Sha'biyy Al-Hamdani Al-Kufi. Ni taabi' na maarufu na Mwanazuoni mkubwa. Az-Zuhri anamueleza kuwa: "Ulamaa ni wanne: Ibn Al-Musayab wa Madiynah, ASH-Sha'b wa Kufa, Hasan Al-Baswri aliyepo Baswra na Mak-hul wa Shaam". Ash-Sha'biyy alizaliwa wakati wa Ukhalifa wa 'Umar na inasemekana kuwa alizaliwa miaka sita kabla ya kuanza kwa Ukhalifa wa 'Uthmaan.

[7] Hukumu ya kishariy'ah kuhusu talaka ni kuwa ni jukumu la mwanamme kugharamia maskani na chakula hadi muda wa eda wa mwanamke unapomalizika. Lakini mwanamme huyo huyo hana haki ya kumgharamia maskani na chakula pindi anapotoa talaka tatu. (ambayo si talaka rejea)

[8] Muda wa eda kwa mjane (asiyekuwa mjamzito) ni miezi mine na siku kumi. Eda ya mwanamke aliyeachika ni hedhi tatu kamili, maadamu ni bado kijana. Ama ikiwa ni ajuza hedhi yake imeshakatika au ni msichana mdogo eda yake ni miezi mitatu.

[9] 'Aswbi ni aina ya nguo kutoka Yemen

[10] Qustwi ni aina ya udi au manukato.

[11] Maelekezo yaliyopo wakati wa eda ni kuwa hairuhusiwi kwa mwanamke kutumia manukato, kuvaa nguo za rangi rangi, kupaka wanja na kuingia katika mkataba au mazungumzo yoyote ya posa na mwanamme. Hali hii inahusu wanawake wote walioolewa kwa ujumla.

[12] Furay'ah bint Maalik ni dada yake Abuu Sa'd AL-Khudriyy alishuhudia Bay'ah Ar-Ridhwaan. Amepokea baadhi ya Hadiyth

[13] Wanawake walioachika wanatakiwa wakae eda zao katika nyumba za waume zao, iwe wameachika au ni wajane. Hata hivyo mwanamke aliyeachika talaka tatu haiwi hivyo. Mwanamke aliyeachika talaka tatu hakai katika nyumba ya mume wake.

[14] Jina lake ni Furay'ah bint wa Maalik bin Sinaan Al-Khudriyah, dada wa Swahaba maarufu Sa'd Al-Khudriyy. Alihudhuria Bay'ah Ar-Ridhwaan.

[15] Mjane anatakiwa amalize muda wake wa eda katika nyumba ya mumewe. Hii ndio hukumu iliyotolewa na 'Ulamaa wengi.

[16] Muda wa Eda wa Ummul Walad (kijakazi aliyejifungua mtoto wa bwana wake), kama ni mjane, baadhi ya 'Ulamaa wanaona kuwa ni miezi mine na siku kumi, wengine wanaona kuwa ni hedhi moja, ambayo ndiyo hukumu iliyo sahihi.

[17] Kuna maneno kadha ya kiarabu ambayo ina maana ya neno na kinyume chake. Maneno kama hayo yanaitwa Dhawaatul-‘Addad (ni maneno na kinyume chake). Moja katika maneno hayo ni Al-Qar-u ambayo maana yake ni kipindi cha hedi, na wakati huo huo ina maana ya Twuhr na kadhalika.

[18] Hii ina maana kijana wa kiume (mtumwa) anaacha kwa talaka mbili na mwanamke muda wake wa eda ni hedhi mbili.

[19] Ruwyfi’ bin Thaabit Al-Answaar ni wa kabila la Baniy Maalik bin An-Najjar, anahisabiwa ni katika wakazi wa Misri. Alifariki mwaka wa 46 Hijriyyah.

[20] Mwanamke aliyepotewa na mume wake asubiri miaka mine (kabla ya kuolewa tena. Muda huu uliwekwa na ‘Umar bin Al-Khatwaab. Baadaye Maswahaba walikubaliana na hukumu hii na ndio hukumu ambayo inafuatwa na ‘Ulamaa wote.

[21] Hadiyth hii inakataza mwanamme kuwa na mwanamke ajnabi peke yake. Hukumu ya Hadiyth hii kadhalika imetajwa katika Hadiyth nyingine, ushawishi wa shaytwaan unaweza kuingia katikati yao na kufanya jambo lisilotakiwa la uzinifu. Hata kama hawawezi au wasifanye jambo hili lakini kuna uwezekano mkubwa wa kutuhumiwa katika hilo, ni vizuri watu wakawa mbali na tuhuma kama hizi.

[22] Maharimu ni jamaa wa karibu wa mwanamke ambao ndoa baina yao ni haraam, uharaam wa milele.

[23] Hii ina maana mtoto wa mwanamke atanasibishwa kwa mume wake na atakuwa chini ya ulezi wake, ikiwa mtu atadai kuwa alikuwa na uhusiano na mwanamke fulani na ya kuwa mtoto ni wake, katika hali hii bado mtoto atakuwa chini ya ulezi wa mumewe na yule mwanamme aliyethibitisha kuzini, shariy’ah itamhukumu kwa hilo. Hakuna hukumu yoyote itakayochukuliwa dhidi ya mwanamke kwa maneno ya mtu bila ushahidi wa wazi wa watu wane. Vinginevyo hukumu itamuendea aliyemtuhumu na kuadhibiwa yeye.

12-Mlango Wa Kunyonya (Mtoto Kunyonyeshwa Na Asiye Mamake)

بَابُ الرِّضَاعِ

12-Mlango Wa Kunyonya (Mtoto Kunyonyeshwa Na Asiye Mamake)

963.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا تُحَرِّمُ الْمَصَّةَ وَالْمَصَّتَانِ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kunyonya mara moja na mbili hakuhamishi.”[1] [Imetolewa na Muslim]

964.

وَعَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { أَنْظُرْنَ مَنْ إِخْوَانُكُنَّ، فَإِنَّمَا الرِّضَاعَةُ مِنَ الْمَجَاعَةِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Angalieni vizuri ndugu zenu ni nani.[2] Hakika kunyonyesha (kunakoleta udugu) ni kutokana na kumaliza njaa (ya mtoto).” [Al-Bukhaariy, Muslim]

965.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {جَاءَتْ سَهْلَةُ بِنْتُ سُهَيْلٍ. فَقَالَتْ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ سَالِمًا مَوْلَى أَبِي حُذَيْفَةَ مَعَنَا فِي بَيْتِنَا، وَقَدْ بَلَغَ مَا يَبْلُغُ الرِّجَالُ. قَالَ: "أَرْضِعِيهِ. تَحْرُمِي عَلَيْهِ"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Sahlah bint Suhayl[3] alikuja kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Saalim[4] muachwa huru wa Abuu Hudhayfah[5] yuko pamoja nasi nyumbani mwetu na amefikia yanayofikiwa na wanaume. Nabiy akasema: “Mnyonyeshe utakuwa haraam kwake.”[6] [Imetolewa na Muslim]

966.

وَعَنْهَا: {أَنَّ أَفْلَحَ أَخَا أَبِي الْقُعَيْسِ جَاءَ يَسْتَأْذِنُ عَلَيْهَا بَعْدَ الْحِجَابِ. قَالَتْ: فَأَبَيْتُ أَنْ أَدْنَ لَهُ، فَلَمَّا جَاءَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَخْبَرْتُهُ بِالَّذِي صَنَعْتُ، فَأَمَرَنِي أَنْ أَدْنَ لَهُ عَلَيَّ. وَقَالَ: "إِنَّهُ عَمُّكَ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Aflah (mjomba aliyenyonya naye) nduguye Abuu Al-Qu’ays,[7] aliomba ruhusa kuingia kwangu baada ya kuteremka Aayah ya hijaab. Nikakataa kumruhusu. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ)

(وَسَلَّمَ) alipokuja nilimueleza nililotenda, akaniamurisha nimruhusu na akaniambia: “Huyo ni ami yako.”[8] [Al-Bukhaariy, Muslim]

967.

وَعَنْهَا قَالَتْ: {كَانَ فِيمَا أَنْزَلَ فِي الْقُرْآنِ: عَشْرُ رَضَعَاتٍ مَعْلُومَاتٍ يُحَرِّمْنَ، ثُمَّ نُسِخْنَ بِخَمْسِ مَعْلُومَاتٍ، فَتُوفِّي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَهِيَ فِيمَا يُقْرَأُ مِنَ الْقُرْآنِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Miongoni mwa Aayah za Qur-aan zilizoteremka ilikuwa ni Aayah hii: “Manyonyesho kumi yanayojulikana yanafanya mtu kuwa maharimu wa mnyonyeshaji.” Kisha zikafutwa kwa manyonyesho matano yanayojulikana....” [Imetolewa na Muslim]

968.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَرِيدَ عَلَى ابْنَةِ حَمْزَةَ. فَقَالَ: "إِنَّهَا لَا تَحِلُّ لِي، إِنَّهَا ابْنَةُ أَخِي مِنَ الرِّضَاعَةِ} وَيَحْرُمُ مِنَ الرِّضَاعَةِ مَا يَحْرُمُ مِنَ النَّسَبِ. مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipewa binti wa Hamzah. Alisema: Yeye si halaal kwangu kumuoa, yeye ni binti ya ndugu

yangu wa kunyonya, na yale[9] yanayoharamishwa katika kunyonya yanaharamishwa katika nasaba.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

969.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يُحَرِّمُ مِنَ الرِّضَاعَةِ إِلَّا مَا فَتَقَ الْأُمَمَاءُ، وَكَانَ قَبْلَ الْفِطَامِ } رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ هُوَ وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ummi Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haiharamishi katika kunyonya ila kiasi kilichopenya matumboni na ikawa kabla ya kuachishwa kunyonya.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Al-Haakim]

970.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { لَا رِضَاعَ إِلَّا فِي الْحَوْلَيْنِ } رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَابْنُ عَدِيٍّ مَرْفُوعًا وَمَوْقُوفًا، وَرَجَّحَا الْمَوْقُوفَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Hakuna kunyonyesha isipokuwa ile miaka miwili ya mwanzo.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy na Ibn ‘Adiyy ikiwa ni Marfuw’ na Mawquwf, wameitilia nguvu kuwa ni Mawquwf]

971.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَا رِضَاعَ إِلَّا مَا أَنْشَرَ الْعَظْمَ، وَأَنْبَتَ اللَّحْمَ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna kunyonyesha ila yanayoimarisha mfupa na kuotesha nyama.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd]

972.

وَعَنْ عُقْبَةَ بْنِ الْحَارِثِ، {أَنَّهُ تَزَوَّجَ أُمَّ يَحْيَى بِنْتَ أَبِي إِيَّابٍ، فَجَاءَتْ امْرَأَةً. فَقَالَتْ: قَدْ أَرْضَعْتُكُمَا، فَسَأَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: "كَيْفَ وَقَدْ قِيلَ ؟ " فَفَارَقَهَا عُقْبَةُ. وَنَكَحَتْ زَوْجًا غَيْرَهُ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Uqbah bin Al-Haarith[10] anasema kuwa: Yeye alimuoa Umami Yahya[11] binti Abuu Ihaab. Akaja mwanamke mmoja akasema: “Nimekunyonyesheni wewe na huyo mkeo.” Akaja akamuuliza Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) jambo hilo. Akasema: “Itakuwaje (unasita) na imeshasemwa (kuwa amewanyonyesha?)”[12] ‘Uqbah akamtaliki yule mke akaolewa na mtu mwingine.[13] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

973.

وَعَنْ زِيَادِ السَّهْمِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ تُسْتَرْضَعَ الْحَمَقَى} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَهُوَ مُرْسَلٌ، وَلَيْسَتْ لَزِيَادٍ صُحْبَةٌ

Kutoka kwa Ziyaad As-Sahmiyy[14] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza watu wasiwape wapumbavu kuwanyonyeshea watoto wao.” [Imetolewa na Abuu Daawuud nayo ni mursal na Ziyaad si Swahaba]

[1] Hadiyth hii inatujulisha kuwa kitendo cha kunyonya ziwa la mwanamke mara moja au mbili halithibitisha umaharim. Hadiyth iliyopokewa na ‘Aaishah anaeleza kuwa ili kuthibitisha makatazo hayo mwanamke anatakiwa anyonyeshe kwa uchache mara tano.

[2] Ilitokea wakati fulani mtu alikuwa amekaa karibu na Mama ‘Aaishah. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakupenda hali hiyo. ‘Aaishah alimjulisha kuwa yule aliyekaa naye alikuwa ni nduguye kwa kunyonya. Baada ya kusikia hivi Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akalitolea ufafanuzi suala hili la kunyonya kwa watoto pamoja utotoni.

[3] Sahlah binti wa Suhayl bin ‘Amr Al-Qushariyah alikuwa wa kabila la Banuu ‘Aamir bin Lu’ayy. Alisilimu mapema na alihama pamoja na Abuu Hudhayfah kuenda Uhabeshi na akamzalia Muhammad bin Abiy Hudhayfah.

[4] Huyu ni Saalim bin Ma’qil muachwa huru wa Abuu Hudhayfah. Alilelewa na mwanamke wa Ki-answaar akiitwa Layla au Thubayta, binti wa Ya’ar, pindi Abuu Hudhayfah alipomuoa alikuja pamoja na Saalim ambaye Abuu Hudhayfah alimfanya katika watu wake. Saalim alihudhuria Badr na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaamurrisha Maswahaba zake wasikilize Qur-aan kutoka kwa watu wane na miongoni mwa hao watu wane Saalim alikuwemo. Alikuwa na mazowea ya kuwaongoza Muhajiruwna, akiwemo ‘Umar, katika Swalaah Msikiti wa Quba kabla ya

Rasuli wa Allaah (ﷺ) kuwasili Madiynah. Hadiyth hii inamhusu Sahlah bint Suhayl. ‘Ulamaa wote wakiwemo Taabi’iyna na Fuqahaa wana msimamo kuwa mtu mkubwa hanyonyeshwi. Na wana msimamo kuwa Hadiyth hii ni Mansuwkh (Hukumu yake imefutwa)

[5] Inasemekana kuwa jina lake lilikuwa ni Muhaashim au Hishaam bin ‘Utbah bin Rabiyy’ah bin ‘Abd Shams. Alikuwa ni Swahaba maarufu aliyehudhuria Badr, Uhud na vita vyote muhimu. Aliuwawa katika vita vya Al-Yamaamah akiwa na umri wa miaka 53.

[6] ‘Ulamaa wengi wamekubaliana na rai kuwa kunyonyesha kunakofanya uharaam wa watu wawili ni ule wa miaka miwili ya mwanzo wa umri wa mtoto. Ama kadhia hii ya Saalim katika Hadiyth hii ni maalum, haitumiki kwa mtu mwingine yeyote.

[7] Jina lake kamili ni Abul-Ja’d Aflah, muachwa huru wa Nabiyy (ﷺ) au muachwa huru wa Ummu Salamah. Kaka yake Abul-Qu’ays alikuwa akiitwa Al-Ja’d au Wail bin Aflah Al-Ash’ari, hivyo basi jina la kaka yake Aflah ni sawa sawa na jina la baba yake. ‘Aaishah alikuwa na wajomba wawili wa kunyonya, miongoni mwao akiwemo kaka zake Abuu Bakr kwa kunyonya ambao walifariki katika zama za Nabiyy (ﷺ) na wa pili alikuwa ni Aflah ambaye ni kwa kaka wa baba yake kwa kunyonya.

[8] Mwanamke ananyonyesha maziwa yake, atakuwa ni mama halisi wa mtoto, kama kwamba yeye ndiye aliyemzaa na baba halikadhalika ataonekana hivyo. Na ichukuliwe hivyo kwa watoto wote watakaonyonya nao pamoja nao katika makatazo ya maharim kuoana.

[9] Yatupasa kufahamu kuwa mtoto anaelekea kwa mama yake aliyemyonyesha. Hata hivyo mama huyo hatokuwa na uhusiano wa ndugu wa damu wa mtoto yule. Uharaam huu utakuwa na wenzake walionyonya.

[10] Alikua akiitwa Sirwa’ta ‘Uqbah bin Al-Haarith bin ‘Aamir bin Nawfal bin ‘Abd Manaaf Al-Makkiy. Alikuwa ni Swahaba miongoni mwa waliosilimu siku ya Fat-h Makkah. Aliishi hadi miaka ya hamsini ya Hijrah.

[11] Jina lake ni Ghaniyah, binti wa Abiy Ihaab bin ‘Uwair At-Tamiymiy. Inasemekana kuwa jina lake lilikuwa Zaynab vile vile.

[12] Hadiyth hii inatufahamisha kuwa tukitaka kuthibitisha uhusiano wa walionyonyeshwa pamoja (ukaka na udada), ushahidi wa mtu mmoja unatosha kuthibitisha. Hili linaonesha vile vile kuwa ushahidi utakaotolewa na mwanamke, katika mas-ala yanayohusiana na mwanamke, ana nguvu zaidi kuliko itakayotolewa na mwanamume.

[13] Imeandikwa katika kitabu At-Taqriyb kuwa alikuwa ni Taabi’ wa kizazi cha tatu na anajulikana kama ni thiqah (madhubuti). Ameripoti Hadiyth ambayo ni Mursal. Na inasemekana kuwa ni muacha huru wa ‘Amr bin Al-‘Aasw. Waandishi wote wa Usudul Al-Ghaba na Al-Isti’aba hakutajwa miongoni mwa Maswahaba.

[14] Hind bin ‘Utbah bint Rabiyy’ah bin ‘Abd Shams alisilimu mwaka wa Fat-h Makkah baada ya mume wake kusilimu katika mwaka huo huo wa Fat-h Makkah. Kifo cha baba yake ‘Utbah mjomba wake Shaybah na kaka yake Al-Waliyd huko Badr vilimshtua sana na alifurahi sana pindi Hamza alipouawawa katika vita vya Uhud.

13-Mlango Wa Matumizi

بَابُ النَّفَقَاتِ

13-Mlango Wa Matumizi

974.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: { دَخَلْتُ هِنْدُ بِنْتُ عُثْبَةَ امْرَأَةً أَبِي سُفْيَانَ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ . فَقَالَتْ: يَا

رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ أَبَا سُفْيَانَ رَجُلٌ شَحِيحٌ لَا يُعْطِينِي مِنْ النِّفَقَةِ مَا يَكْفِينِي وَيَكْفِي بَنِيَّ، إِلَّا مَا أَخَذْتُ مِنْ مَالِهِ بِغَيْرِ عِلْمِهِ، فَهَلْ عَلَيَّ فِي ذَلِكَ مِنْ جُنَاحٍ؟ فَقَالَ: "خُذِي مِنْ مَالِهِ بِالْمَعْرُوفِ مَا يَكْفِيكَ، وَيَكْفِي بَنِيكَ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Siku moja Hind bint ‘Utbah[1] mke wa Abuu Sufyaan[2] aliingia kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Kwa hakika Abuu Sufyaan ni mtu bakhili mwenye tamaa, wala hanipi kinachonitosha mimi na wanangu ila ninachokichukua katika mali yake ilhali hajui, je nikifanya hivyo nina dhambi? Akasema: “Chukua kwa wema katika mali yake kinachokutosha wewe na wanao.”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim]

975.

وَعَنْ طَارِقِ الْمُحَارِبِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {قَدِمْنَا الْمَدِينَةَ، فَإِذَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَائِمٌ يَخْطُبُ وَيَقُولُ: "يَدُ الْمُعْطَى الْعُلْيَا، وَابْدَأْ بِمَنْ تَعُولُ: أُمَّكَ وَأَبَاكَ، وَأُخْتُكَ وَأَخَاكَ، ثُمَّ أَذْنَاكَ أَذْنَاكَ" { رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْدَّارَقُطْنِيُّ

Kutoka kwa Twaariq Al-Muhaaribiyy[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulienda Madiynah tukamkuta Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) yuko juu ya mimbari amesimama anawahutubia watu: “Mkono wa mtoaji ni wa juu,[5] anza kwa unayemlisha: mama yako, baba yako, dada yako na ndugu yako, halafu aliye karibu nawe zaidi.” [Imetolewa na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Ad-Daaraqutwniy]

976.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لِلْمَمْلُوكِ طَعَامُهُ وَكِسْوَتُهُ، وَلَا يُكَلَّفُ مِنَ الْعَمَلِ إِلَّا مَا يُطِيقُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtumwa ana haki kwa bwana wake kupata chakula chake na nguo zake[6] wala halazimishwi kufanya kazi ila anayoiweza.” [Imetolewa na Muslim]

977.

وَعَنْ حَكِيمِ بْنِ مُعَاوِيَةَ الْقُشَيْرِيِّ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: {قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! مَا حَقُّ زَوْجَةٍ أَحَدِنَا عَلَيْهِ؟} قَالَ: "أَنْ تُطْعِمَهَا إِذَا طَعِمْتَ، وَتَكْسُوَهَا إِذَا اكْتَسَيْتَ، وَلَا تَضْرِبَ الْوَجْهَ، وَلَا تُقَبِّحَ...". {الْحَدِيثُ. وَتَقَدَّمَ فِي عَشْرَةِ النَّسَاءِ.

Kutoka kwa Hakiym bin Mu’aawiyah Al-Qushayriyy amepokea kutoka kwa baba yake amesema: “Nilisema Ee Rasuli wa Allaah! Ni ipi haki ya mke wa mmoja wetu juu ya mumewe? Akasema: ‘Ni kumlisha unapokula na kumvisha unapovaa’.” Hadiyth imetangulia katika mlango wa matengamano ya waume kwa wake zao.

978.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ فِي حَدِيثِ الْحَجِّ بِطُولِهِ قَالَ فِي ذِكْرِ النِّسَاءِ: {وَلَهُنَّ
عَلَيْكُمْ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdullaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kutoka katika Hadiyith
ya Hajj iliyotajwa kwa urefu alisema alipowataja wanawake: “Wao
(wanawake) wana haki inayowapasa nyinyi chakula chao na nguo
zao kwa wema.”[7] [Imetolewa na Muslim]

979.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {كَفَى بِالْمَرْءِ إِثْمًا أَنْ يُضَيِّعَ مَنْ
يَقُوتُ} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ
وَهُوَ عِنْدَ مُسْلِمٍ بِلَفْظٍ: "أَنْ يَحْبِسَ عَمَّنْ يَمْلِكُ قُوَّتَهُ"

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Yatosha
mtu kuwa ana dhambi kwa kumtelekeza anayemlisha.”[8]
[Imetolewa na An-Nasaaiy].

Nayo iko kwa Muslim kwa tamshi: “Kuzuia chakula kwa yule
anayekimiliki.”

980.

وَعَنْ جَابِرِ يَرْفَعُهُ، فِي الْحَامِلِ الْمُتَوَفَّى عَنْهَا قَالَ: {لَا نَفَقَةَ لَهَا}
أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ، لَكِنْ قَالَ: الْمَحْفُوظُ وَقَفُّهُ

وَتَبَّتْ نَفْيُ النَّفَقَةِ فِي حَدِيثِ فَاطِمَةَ بِنْتِ قَيْسٍ كَمَا تَقَدَّمَ. رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir amesema kuhusu mwanamke mjamzito aliyefiwa na mumewe, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hana matumizi.”[9] [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy na wapokezi wake ni madhubuti lakini amesema: Ilivyohifadhiwa ni kuwa Hadiyth hii ni Mawquwf]

Na imethibiti mwanamke huyo kutopewa matumizi katika Hadiyth ya Faatwimah bint Qays kama iliyotangulia. [Imetolewa na Muslim]

981.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {الْيَدِ الْعُلْيَا خَيْرٌ مِنَ الْيَدِ السُّفْلَى، وَيَبْدَأُ أَحَدُكُمْ بِمَنْ يَعُولُ. تَقُولُ الْمَرْأَةُ: أَطْعَمَنِي، أَوْ طَلَّقَنِي} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini, mmoja wenu aanze na anayemlisha. Mwanamke husema[10]: “Nilishe au nipe talaka.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy na Isnaad yake ni hasan]

982.

وَعَنْ سَعِيدِ بْنِ الْمُسَيَّبِ فِي الرَّجُلِ لَا يَجِدُ مَا يُنْفِقُ عَلَى أَهْلِهِ قَالَ: {يُفَرِّقُ بَيْنَهُمَا} أَخْرَجَهُ سَعِيدُ بْنُ مَنْصُورٍ: عَنْ سُفْيَانَ، عَنْ أَبِي

الزَّيْنَادِ، عَنْهُ. قَالَ: {فَقُلْتُ لِسَعِيدِ بْنِ الْمُسَيَّبِ: سُنَّةٌ؟ فَقَالَ: سُنَّةٌ} وَهَذَا مُرْسَلٌ قَوِيٌّ

Kutoka kwa Sa'iyd bin Al-Musayyib amesema kuhusu mtu aliyekuwa hapati matumizi ya mkewe: "Watatenganishwa." [Imetolewa na Sa'iyd bin Manswuwr kutoka kwa Sufyaan[11] naye kutoka kwa Abuu Az-Zinaad[12]]

Kutoka kwa Sa'iyd bin Al-Musayyib amesema: "Nilisema kumuambia Sa'iyd bin Al-Musayyib je hii ni Sunnah? Akasema: ndiyo ni sunnah." [Hadiyth hii ni Mursal yenye nguvu]

983.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّهُ كَتَبَ إِلَى أُمَرَاءِ الْأَجْنَادِ فِي رَجَالٍ غَابُوا عَنْ نِسَائِهِمْ: أَنْ يَأْخُذُوهُمْ بَأَنِّ يُنْفِقُوا أَوْ يُطَلَّقُوا، فَإِنْ طَلَّقُوا بَعَثُوا بِنَفَقَةٍ مَا حَبَسُوا} أَخْرَجَهُ الشَّافِعِيُّ. ثُمَّ الْبَيْهَقِيُّ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: "Aliwaandikia viongozi wa majeshi kuhusu watu walio mbali na wake zao muda mrefu, kuwa watoe matumizi au wawataliki wake zao, ikiwa watawataliki watume gharama[13] za zile siku walizozuwia kutoa." [Imetolewa na Ash-Shaafi'iyy na Al-Bayhaqiyy kwa Isnaad hasan]

984.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! عِنْدِي دِينَارٌ؟ قَالَ: "أَنْفَقْهُ عَلَى نَفْسِكَ". قَالَ: عِنْدِي آخَرُ؟ قَالَ: "أَنْفَقْهُ عَلَى وَلَدِكَ". قَالَ: عِنْدِي آخَرُ؟ قَالَ: "أَنْفَقْهُ عَلَى أَهْلِكَ". قَالَ: عِنْدِي آخَرُ، قَالَ:

"أَنْفَقَهُ عَلَى خَادِمِكَ". قَالَ عِنْدِي آخَرُ، قَالَ: "أَنْتَ أَعْلَمُ" { أَخْرَجَهُ الشَّافِعِيُّ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَأَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ وَالْحَاكِمُ بِتَقْدِيمِ الزَّوْجَةِ عَلَى الْوَلَدِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Alikuwa mtu kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Nina dinari moja (niifanyeje?) akasema: Jitolee mwenyewe. Akasema: Ninayo nyingine. Akasema: Mpe mwanao. Akasema: Ninayo nyingine. Akasema: Mpe mkeo. Akasema: Ninayo nyingine. Akasema: Mpe mtumishi wako. Akasema: Ninayo nyingine. Akasema: Wewe ndiye unajua zaidi (cha kuifanyia).” [Imetolewa na Ash-Shaafi’iyy na Abuu Daawuud. Matini ya Hadiyth ni ya Abuu Daawuud, vile vile An-Nasaaiy na Al-Haakim wameipokea kwa kumtanguliza mke mbele ya mtoto]

985.

وَعَنْ بَهْزِ بْنِ حَكِيمٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: { قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! مَنْ أَبْرُ؟ قَالَ: "أُمَّكَ". قُلْتُ: ثُمَّ مَنْ؟ قَالَ: "أُمَّكَ". قُلْتُ: ثُمَّ مَنْ؟ قَالَ: "أُمَّكَ". قُلْتُ: ثُمَّ مَنْ؟ قَالَ: "أَبَاكَ، ثُمَّ الْأَقْرَبَ فَالْأَقْرَبَ" { أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحُسْنَهُ

Kutoka kwa Bahz bin Hakiym kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake amesema: Nilisema Ee Rasuli wa Allaah! Nimfanyie nani wema? Akasema: “Mama yako.” Nikasema: Kisha nani? Akasema: “Mama yako.” Nikasema kisha nani? Akasema “Mama yako.” Nikasema kisha nani? Akasema: “Baba yako, kisha jamaa wa karibu zaidi.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy amesema ni sahihi]

[1] Hind bint ‘Utbah bint Rabiyy’a bin ‘Abd Shams alisilimu mwaka wa Fat-h Makkah baada ya mume wake kusilimu katika mwaka huo huo wa Fat-h Makkah. Kifo cha baba yake ‘Utbah, mjomba wake Shaiba na kaka yake Al-Waliyd huko Badr vilimshtua sana na alifurahi sana pindi Hamza alipouwawa katika vita vya Uhud.

[2] Jina lake ni Sakhr bin Harb bin Umaiyah bin ‘Abd Shams ambaye alibeba bendera ya ukafiri na alikuwa kiongozi aliyepigana na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Alisilimu katika Fat-h Makkah pindi Al-‘Abbaas alipomchukuwa kwa Nabiyy kabla ya kuingia Makkah. Aliishi akiwa ni Muislamu mzuri.

[3] Lengo la Hadiyth hii kuwekwa hapa ni kuonesha majukumu aliyokuwa nayo mtu katika kusimamia mahitaji ya mkewe au wakeze na watoto wake. Inaonyesha hali kadhalika kuwa ikiwa mtu atakataa kutoa haki anayotakiwa kutoa, basi Shariyy’ah itaruhusu haki hiyo itolewe kwa njia nyingine. Kwa maneno mengine, ikiwa mtu amedhulumiwa anaweza kutafuta haki yake kupitia njia nyingine.

[4] Twaariq bin ‘Abdillaah Al-Muhaaribiyy alikuwa ni Swahaba ambaye alipokea baadhi ya Hadiyth. Alikuwa Muhaaribiyy bin Khasfa, katika kabila la Banu Ghatafan.

[5] Mkono unaotoa ni bora kuliko mkono unaopokea. Ni vizuri mtu kutokopa fedha. Hadiyth hii haikutaja mke na watoto kwani wao wameshaingizwa katika matumizi ya familia. Maelezo ya ziada ni kuwa familia ya mtu tajiri inajumuisha jamaa zake wa karibu kama kaka na dada zake walio masikini ili nao waishi maisha mazuri.

[6] Kilichokuwa kizuri katika muamala wa mtu na watumwa au wafanyakazi ni pale anapokula amlishe anachokula na amvishe anachovaa. Kadhalika asizidishiwe kazi ila anachoweza kufanya kama kuna uzito basi asaidiwe.

[7] Lengo la kuwekwa kwa Hadiyth hii ni matumizi yatachukuliwa kulingana na kipato cha mtu. Ikiwa mtu ni tajiri mkewe anaweza kuomba ziada ya matumizi, inayolingana na uwezo wa mumewe. Ikiwa hali yake ni ya umasikini atapata kile kinacholingana na uwezo wa mumewe.

[8] Maelezo ya Hadiyth hii yanasisitiza kuwa ni dhambi kuwatekeleza wale ambao umeamrisha kuwahudumia. Watu ambao ni lazima kishariy'ah kuwahudumia kwa daraja la mwanzo kabisa ni mke, watoto, wafanyakazi wake na wazazi wake.

[9] Mwanamke asiye kuwa na mimba na aliyeachika talaka tatu, kwa makubaliano ya 'Ulamaa, hana haki ya kupewa nyumba na gharama zake. Mjamzito, aliyeachika talaka tatu anayo haki ya kupewa chakula lakini siyo nyumba. Mjane asiye na mimba anapewa nyumba lakini siyo chakula. Mjane mwenye mimba ana haki ya nyumba, kuna tofauti ya rai kutokana na 'Ulamaa ikiwa ana haki ya kupewa chakula na gharama zingine za maisha. Mjadala upo katika huduma za nyumba na maisha kwa mwanamke aliyekuwa katika eda. Pindi eda yake inapomalizilka, hana haki ya chochote katika yaliyotangulia.

[10] Hadiythi hii inatupambanulia kwamba ikiwa mwanamme hawezi gharama za mke wake, wataachanishwa ikiwa mwanamke ametaka hivyo. Hata hivyo, ikiwa mwanamke atapendelea asubiri kwa matamu ya maisha na machungu yake, atakuwa ni mwenye kupata ujira.

[11] Huyu ni Sufyaan bin Sa'iyd bin Masruq Ath-Thawriy Abuu 'Abdillaah Al-Kufi. Alikuwa ni Imaam maarufu na makini, Hafidhi na mwenye elimu kubwa ya Hadiyth, alikuwa ni mwenye taqwa. Alizaliwa mwaka 77H na alikufa katika mji wa Basra mwaka 161H.

[12] Jina lake halisi ni 'Abdullaah bin Dhakwaan, ni katika ukoo wa Al-Amawi wa Madiynah. Alikuwa ni miongoni mwa maimaam wakubwa, Ahmad anamuelezea kwa kusema: "Alikuwa ni mtu madhubuti na kamanda wa Waumini." Al-Bukhaariy naye anamuelezea kwa kusema: "Isnaad iliyokuwa bora zaidi ni kutoka kwa Abuu Az-Zinaad naye kutoka kwa Al-A'raaj kutoka kwa Abuu Hurayrah (ambaye amepokea kutoka kwa Nabiy)." Alifariki mwaka 130 Hijriya au 131.

[13] Katika Hadiyth nyingine inasisitiza kuwa fedha inayotumiwa na mtu kwa ajili ya mke wake na watoto wake ndiyo yenye ujira mkubwa na ni bora kuliko ile inayotumika katika kuwapa maskini wa mbali (wasiokuwa ndugu).

14-Mlango Wa Al-Hadhwaanah Malezi

بَابُ الْحَضَانَةِ

14-Mlango Wa Al-Hadhwaanah Malezi[1]

986.

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ امْرَأَةً قَالَتْ: {يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ ابْنِي هَذَا كَانَ بَطْنِي لَهُ وَعَاءٌ، وَتَذْيِي لَهُ سِقَاءٌ، وَحَجْرِي لَهُ حِوَاءٌ، وَإِنَّ أَبَاهُ طَلَّقَنِي، وَأَرَادَ أَنْ يَنْتَزِعَهُ مِنِّي. فَقَالَ لَهَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "أَنْتِ أَحَقُّ بِهِ، مَا لَمْ تَنْكِحِي".} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdillaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Mwanamke mmoja alikuja akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Kwa hakika mwanangu huyu tumbo langu lilikuwa ndio mfuko wake, ziwa langu lilikuwa ni kiriba chake cha maji, na paja langu lilikuwa kitanda chake. Baba yake alinitaliki na anataka kunipokonya mtoto huyu!” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Wewe una haki zaidi kwake maadamu hujaolewa.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na akaisahihisha Al-Haakim]

987.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ امْرَأَةً قَالَتْ: { يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّ زَوْجِي يُرِيدُ أَنْ يَذْهَبَ بِابْنِي، وَقَدْ نَفَعَنِي، وَسَقَانِي مِنْ بئرِ أَبِي عَنبَةَ فَجَاءَ زَوْجُهَا، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "يَا غُلَامُ! هَذَا أَبُوكَ وَهَذِهِ أُمُّكَ، فَخُذْ بِيَدِ أَيُّهُمَا شِئْتَ" فَأَخَذَ بِيَدِ أُمِّهِ، فَانْطَلَقَتْ بِهِ. } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: Mwanamke mmoja alikuja akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Mume wangu anataka kumchukua mwanangu na ananisaidia kuchotea maji katika kisima cha Abiy ‘Inabah, mumewe akaja, akasema Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kumuambia yule kijana: “Ee mtoto, huyu ni baba yako na huyu ni mama yako, mshike mkono umtakae.” [2] Yule kijana akashika mkono wa mama yake na akaondoka naye.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

988.

وَعَنْ رَافِعِ بْنِ سِنَانَ، { أَنَّهُ أَسْلَمَ، وَأَبَتْ امْرَأَتُهُ أَنْ تُسَلَّمَ. فَأَقْعَدَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ الْأُمَّ نَاحِيَةً، وَالْأَبَ نَاحِيَةً، وَأَقْعَدَ الصَّبِيَّ بَيْنَهُمَا. فَمَالَ إِلَى أُمِّهِ، فَقَالَ: "اللَّهُمَّ اهْدِهِ". فَمَالَ إِلَى أَبِيهِ، فَأَخَذَهُ. } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Raafi' bin Sinaan[3] amesema kuwa: Yeye alisilimu, na mkewe akakataa kusilimu. Nabiyy (ﷺ) akamkalisha mama upande mmoja na baba upande mwingine, na akamkalisha mtoto katikati yao, yule mtoto akawa ameegemea upande wa mama yake, Rasuli wa Allaah (ﷺ) akaomba: “Ee Allaah! Muongoze (mtoto huyu).” Yule mtoto akaegemea upande wa baba yake akamchukua.[4] [Imetolewa na Abuu Daawuud, An-Nasaaiy na Al-Haakim]

989.

وَعَنْ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَضَى فِي ابْنَةِ حَمْزَةَ لِخَالَتِهَا، وَقَالَ: الْخَالَةُ بِمَنْزِلَةِ الْأُمِّ. } أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ
وَأَخْرَجَهُ أَحْمَدُ: مِنْ حَدِيثِ عَلِيٍّ فَقَالَ: { وَالْجَارِيَةُ عِنْدَ خَالَتِهَا، فَإِنَّ الْخَالََةَ وَالِدَةٌ }

Kutoka kwa Al-Baraai bin ‘Aazib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: Nabiyy (ﷺ) alihukumu kuhusu binti wa Hamza kwa mama yake mdogo na akasema: “Mama mdogo ni katika daraja yake mama.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Na kutoka kwa Ahmad ameipokea hadiyth ya ‘Aliy alisema: “Binti mdogo anafaa kulelewa na mama yake mdogo kwani mama mdogo ni mama.”

990.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { إِذَا أَتَى أَحَدَكُمْ خَادِمُهُ بِطَعَامِهِ، فَإِنْ لَمْ يُجْلِسْهُ مَعَهُ، فَلْيُنَاوِلْهُ لُقْمَةً أَوْ لُقْمَتَيْنِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu atakapoletewa chakula na mtumishi wake iwapo hakumkalisha ale pamoja naye basi ampe tonge moja au matonge mawili.”[5] [Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Bukhaariy]

991.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { عُذِّبَتْ امْرَأَةٌ فِي هِرَّةٍ سَجَنَتْهَا حَتَّى مَاتَتْ، فَدَخَلَتْ النَّارَ فِيهَا، لَا هِيَ أَطْعَمَتْهَا وَسَقَتْهَا إِذْ هِيَ حَبَسَتْهَا، وَلَا هِيَ تَرَكَتْهَا، تَأْكُلُ مِنْ خَشَاشِ الْأَرْضِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwanamke kaadhibiwa kwa sababu ya paka, alimfunga hadi akafa, akaingizwa motoni kwa ajili ya paka. Hakumlisha wala hakumpa maji, wala hakumuacha ale vidudu vya ardhini.” [Bukhaariy, Muslim]

[1] Al-Hadhwaanah kwa lugha ya kiarabu ina maana ya kuhifadhi na kulinda. Kulingana na Istilahi ya kishariy'ah ina maana ya malezi na maangalizi anayopewa mtoto. Ikiwa mtu kamuacha mkewe na wote ni Waislamu na wana watoto, katika hali hii mwanamke huwa ana haki zaidi ya malezi ya mtoto. Mwanamme hawezi kuwachukua na kuwaweka mbali na mama yao kwa nguvu. Ikiwa mtoto au watoto wapo katika hatua ya kunyonyeshwa ni haki ya baba kumgharimia mahitaji na matumizi ya yule mtoto kwa muda wote akiwa ni mtoto anayenyonya. Mtoto ataendelea kuhudumiwa na baba yake ikiwa anakaa naye au anakaa na mama yake. Akiwa anakaa na mama yake itaendelea kuwa hivyo maadamu mama yule atakuwa hajaolewa tena hadi atakapofikia balebhe. Ikiwa mama kaolewa ulezi wa mtoto utahamia kwa baba yake. Kulingana na madhehebu ya Hanafi ni kuwa, atakapoolewa na jamaa wa mtoto, malezi na uangalizi wake utabaki kwa mama yake.

[2] Hadiyth iliyotangulia, mama ametangulizwa zaidi kwa ulezi wa mwanawe, wakati katika Hadiyth hii mwana anapewa uhuru wa kuchagua baina ya wazazi wake wawili. Sababu ni kuwa katika Hadiyth hii mtoto ameshakuwa mkubwa na mwenye uwezo zaidi wa kuchagua wapi pa kumfaa zaidi. Kwa hali hii tunajifunza kuwa mtoto anapokuwa ameshakuwa na hana haja ya ulezi na ulinzi wa wazazi wake ana khiyari ya kuchagua pa kuenda kati ya kwa baba na kwa mama.

[3] Huyu ni Abul-Hakam Al-Answaar Al-Madaniy ambaye alikuwa Swahaba, Abul-Qaasim bin Salam amesema katika Al-Answaab kuwa walikuwa ni kizazi cha Al-'Atbun ambaye ni 'Aamir bin Tha'alabah.

[4] Hadiyth hii inathibitisha kuwa hata ikiwa mama ni kafiri hakumnyima haki ya mwanawe, ikiwa mtoto keshapambanukiwa, hatoendelea kukaa nae.

[5] Hadiyth hii inatuhimiza kuwa bwana mwenye nyumba ampe mfanyakazi wake chakula.

كِتَابُ الْجَنَائَاتِ

Kitabu Cha Jinai (Na Kisasi)

09-Kitabu Cha Jinai (Na Kisasi) - كِتَابُ الْجَنَائَاتِ

00-Buluwgh Al-Maraam: Kitabu Cha Jinai: Mlango Wa Makosa Ya Jinai

بَابُ الْجَنَائَاتِ

00-Mlango Wa Makosa Ya Jinai[1]

992.

عَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا يَحِلُّ دَمُ امْرِيٍّ مُسْلِمٍ، يَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ
إِلَّا اللَّهُ، وَأَنِّي رَسُولُ اللَّهِ، إِلَّا بِأَحَدٍ ثَلَاثٍ: الثَّيِّبُ الزَّانِي،

وَالنَّفْسُ بِالنَّفْسِ، وَالتَّارِكُ لِدِينِهِ، الْمُفَارِقُ لِلْجَمَاعَةِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn Mas-'uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halaal damu ya mtu Muislam anayeshuhudia kuwa hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah na kuwa mimi ni Rasuli wa Allaah ila kwa mojawapo ya mambo matatu:[2] Mzinifu aliyeoa, nafsi kwa nafsi na aliyeacha Dini yake (aliyeritadi) aliyefarikiana na jamaa (umoja wa Waislam).” [Bukhaariy, Muslim]

993.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا يَحِلُّ قَتْلُ مُسْلِمٍ إِلَّا فِي إِحْدَى ثَلَاثِ خِصَالٍ: زَانٌ مُحْصَنٌ فَيُرْجَمُ، وَرَجُلٌ يَقْتُلُ مُسْلِمًا مُتَعَمِّدًا، فَيُقْتَلُ، وَرَجُلٌ يَخْرُجُ مِنَ الْإِسْلَامِ فَيُحَارِبُ اللَّهَ وَرَسُولَهُ، فَيُقْتَلُ، أَوْ يُصَلَّبُ، أَوْ يُنْفَى مِنَ الْأَرْضِ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa 'Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halaal kumuua Muislam ila kwa mojawapo ya mambo matatu: mzinifu aliyehifadhika atapigwa mawe, mtu anayemuua Muislam kwa makusudi naye atauawa, na mtu anayetoka katika Uislam, akawa anampiga vita Allaah na Rasuli wake atauawa, au atasulubiwa na atatolewa katika nchi.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy na akaisahihisha Al-Haakim]

994.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَوَّلُ مَا يُقْضَى بَيْنَ النَّاسِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِي الدِّمَاءِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdillaah bin Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Jambo la kwanza watakalohukumiwa watu siku ya Qiyaamah ni katika damu.”[3] [Bukhaariy, Muslim]

995.

وَعَنْ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ قَتَلَ عَبْدَهُ قَتْلَنَاهُ، وَمَنْ جَدَعَ عَبْدَهُ جَدَعْنَاهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ، وَحَسَنَةُ التِّرْمِذِيُّ، وَهُوَ مِنْ رَوَايَةِ الْحَسَنِ الْبَصْرِيِّ عَنْ سَمُرَةَ، وَقَدْ اخْتَلَفَ فِي سَمَاعِهِ مِنْهُ

وَفِي رَوَايَةٍ لِأَبِي دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيِّ: {وَمَنْ خَصَى عَبْدَهُ خَصَيْنَاهُ} وَصَحَّ الْحَاكِمُ هَذِهِ الزِّيَادَةُ

Kutoka kwa Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kumuua mtumwa wake, nasi tutamuua, na mwenye kumkata pua mtumwa

wake na si tutamkata.”[4] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah), na At-Tirmidhiy amesema ni Hasan nayo ni katika Riwaayah ya Al-Hasan Al-Baswriy kutoka kwa Samurah, wametofautiana katika kusikia kwake kwa Samurah au sivyo]

Katika Riwaayah ya Abuu Daawuud na An-Nasaaiy kuna ziada hii: “...na mwenye kumhasi mtumwa wake na sisi tutamhasi.” Al-Haakim ameipa daraja ya sahihi ziada hii.

996.

وَعَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {لَا يُقَادُ الْوَالِدُ بِالْوَلَدِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْجَارُودِ وَالْبَيْهَقِيُّ، وَقَالَ التِّرْمِذِيُّ: إِنَّهُ مُضْطَرَبٌ

Kutoka kwa ‘Umar bin Al Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Baba halipizwi kisasi kwa mwanawe.”[5] [Imetolewa na Ahmad, At-Tirmidhiy na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Al-Jaarud na Al-Bayhaqiyy. Na akasema At-Tirmidhiy ni ‘Mudhwtwarib’][6]

997.

وَعَنْ أَبِي جُحَيْفَةَ قَالَ: {قُلْتُ لَعَلِّي رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: هَلْ عِنْدَكُمْ شَيْءٌ مِنَ الْوَحْيِ غَيْرَ الْقُرْآنِ؟ قَالَ: لَا وَالَّذِي فَلَقَ الْحَبَّةَ وَبَرَأَ النَّسَمَةَ، إِلَّا فَهُمْ يُعْطِيهِ اللَّهُ رَجُلًا فِي الْقُرْآنِ، وَمَا

فِي هَذِهِ الصَّحِيفَةِ قُلْتُ: وَمَا فِي هَذِهِ الصَّحِيفَةِ؟ قَالَ: "الْعَقْلُ، وَفِكَائُ الْأُسَيْرِ، وَلَا يُقْتَلُ مُسْلِمٌ بِكَافِرٍ { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

وَأَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ: مِنْ وَجْهِ آخَرَ عَنْ عَلِيٍّ وَقَالَ فِيهِ: {الْمُؤْمِنُونَ تَتَكَافَأُ دِمَاؤُهُمْ، وَيَسْعَى بِذِمَّتِهِمْ أَدْنَاهُمْ، وَهُمْ يَدُّ عَلَى مَنْ سِوَاهُمْ، وَلَا يُقْتَلُ مُؤْمِنٌ بِكَافِرٍ، وَلَا ذُو عَهْدٍ فِي عَهْدِهِ} وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Juhayfah amesema: Nilisema kumuambia ‘Aliy: Nyinyi mna chochote katika Wahyi isiyokuwa Qur-aan?[7] Akasema: Hapana naapa kwa Aliyepasua mbegu na Akaumba nafsi, isipokuwa fahamu Allaah Humpa mtu katika Qur-aan (kuielewa), na yaliyomo katika sahifa (karatasi) hii. Nikasema katika sahifa hii kuna nini? Akasema: ‘Al ‘aqlu (kanuni za malipo ya damu), diya, kumfungua mateka na Muislam hauwawi kwa kumuua kafiri.[8] [Imetolewa na Al Bukhaariy]

Na wameipokea Ahmad, Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy kwa njia nyingine kutoka kwa ‘Aliy amesema: “Waumini damu zao zinalingana, na anaenda kwa dhima yao aliye karibu nao, nao wako juu ya wengine wala Muumini hauwawi kwa (kumuua) kafiri, wala mwenye mkataba katika mkataba wake.” [Ameisahihisha Al-Haakim]

998.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ جَارِيَةً وَجَدَ رَأْسَهَا قَدْ رُضَّ بَيْنَ حَجْرَيْنِ، فَسَأَلُوهَا: مَنْ صَنَعَ بِكَ هَذَا؟ فَلَانَّ. فَلَانَّ. حَتَّى ذَكَرُوا يَهُودِيًّا. فَأَوْمَأَتْ بِرَأْسِهَا، فَأَخَذَ الْيَهُودِيُّ،

فَأَقْرَ، فَأَمَرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ يُرَضَّ
رَأْسُهُ بَيْنَ حَجَرَيْنِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
Mjakazi mmoja alipatikana hali ya kuwa kichwa chake kimepondwa
katikati ya mawe mawili. Akaulizwa ni nani aliyekufanyia hivi? Ni
fulani? Ni fulani? Hadi wakamtaja Myahudi, akaashiria kwa kichwa.
“Ndiye” yule Myahudi akashikwa na akaungama. Rasuli wa Allaah
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaamuru kichwa chake kipondwe
baina ya mawe mawili.[9] [Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la
Muslim]

999.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ غُلَامًا لِلْأَنْسِ
فُقَرَاءَ قَطَعَ أُذُنَ غُلَامٍ لِلْأَنْسِ أَغْنِيَاءَ، فَأَتَوْا النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَلَمْ يَجْعَلْ لَهُمْ شَيْئًا { رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالثَّلَاثَةُ،
بِإِسْنَادٍ صَحِيحٍ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema
kuwa: Kijana wa watu mafukara[10] alikata sikio la watu matajiri,
wakamuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) basi
hawakuwapa chochote. [Imetolewa na Ahmad na Ath-Thalaathah
(At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) kwa isnaad Swahiyh]

1000.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ، رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَجُلًا طَعَنَ رَجُلًا بِقَرْنٍ فِي رُكْبَتِهِ، فَجَاءَ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: أَقْدِنِي. فَقَالَ: "حَتَّى تَبْرَأَ". ثُمَّ جَاءَ إِلَيْهِ. فَقَالَ: أَقْدِنِي، فَأَقَادَهُ، ثُمَّ جَاءَ إِلَيْهِ. فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! عَرَجْتُ، فَقَالَ: "قَدْ نَهَيْتُكَ فَعَصَيْتَنِي، فَأَبْعَدَكَ اللَّهُ، وَبَطَلَ عَرَجُكَ". ثُمَّ نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "أَنْ يُقْتَصَّ مِنْ جُرْحٍ حَتَّى يَبْرَأَ صَاحِبُهُ" { رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالدَّارَقُطْنِيُّ، وَأَعْلَى بِالْإِسْأَلِ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: Mtu mmoja alimchoma mtu kwa pembe katika goti lake, (yule aliyedungwa) akamuendea Nabi (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Nilipizie kisasi.?” Akamuambia: “Subiri mpaka upone.” Yule mtu akasisitiza: “Nilipizie kisasi.?” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamlipizia kisasi, kisha akamjia tena akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Nimekuwa kiwete.” Akamuambia: “Nilikukataza ukaniasi, Allaah Akakuweke mbali (na Rahma Zake), na ulemavu wako umebatilika.”[11] Kisha Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza mtu kulipiziwa kisasi cha jeraha mpaka aliyejeruhiwa apone. [Imetolewa na Ahmad na Ad-Daaraqutwniy na imetiwa ila kuwa ni Mursal]

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {اِقْتَتَلَتْ اِمْرَأَتَانِ مِنْ هُذَيْلٍ، فَرَمَتْ اِحْدَاهُمَا الْاُخْرَى بِحَجَرٍ، فَقَتَلَتْهَا وَمَا فِي بَطْنِهَا، فَاخْتَصَمُوا إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَضَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنَّ دِيَّةَ جَنِينِهَا: غُرَّةٌ، عَبْدٌ أَوْ وَلِيدَةٌ، وَقَضَى بِدِيَّةِ الْمَرْأَةِ عَلَى عَاقِلَتِهَا. وَوَرَّثَهَا وَلَدَهَا وَمَنْ مَعَهُمْ. فَقَالَ حَمَلُ بْنُ النَّابِغَةِ الْهُذَلِيُّ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! كَيْفَ يَغْرَمُ مَنْ لَا شَرِبَ، وَلَا أَكَلَ، وَلَا نَطَقَ، وَلَا اسْتَهَلَ، فَمِثْلُ ذَلِكَ يُطَلُّ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "إِنَّمَا هَذَا مِنْ إِخْوَانِ الْكُفَّانِ"، مِنْ أَجْلِ سَجْعِهِ الَّذِي سَجَعَ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَأَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ: مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عَبَّاسٍ، أَنَّ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ سَأَلَ مَنْ شَهِدَ قِضَاءَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي الْجَنِينِ ؟ قَالَ: فَقَامَ حَمَلُ بْنُ النَّابِغَةِ، فَقَالَ: كُنْتُ بَيْنَ اِمْرَأَتَيْنِ، فَضَرَبْتُ اِحْدَاهُمَا الْاُخْرَى... فَذَكَرَهُ مُخْتَصَرًا. وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Wanawake wawili wa Hudhayl walipigana, mmoja akamrushia jiwe mwenzie akamuuwa pamoja na kilicho tumboni mwake. Wakashtakiana kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akahukumu: Diya ya mtoto wake (aliyekuwa tumboni)[12] ni mtumwa au mjakazi. Na akahukumu Diya ya mwanamke iwe juu ya jamaa zake (kwa baba). Akamrithisha mwanaye (yule mwanamke) na jamaa zao. Hamal bin An-Naabighat Al Hudhaliy[13] akasema Ee Rasuli wa Allaah! Vipi nimlipe ambaye hajanywa wala hajala, wala hakutamka wala hakulia? Na mfano wao hawalipwi. Rasuli wa

Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema kuhusu mtu huyu: "Huyu ni ndugu wa makuhani." [14] Kwa sababu ya mizani ya maneno yake anayotoa. [Bukhaariy, Muslim]

Na imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy kutoka katika Hadiyth ya Ibn 'Abbaas kuwa: 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) aliuliza: Ni nani aliyeshuhudia hukumu ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika mtoto aliye tumboni? Hamal bin-An Naabighat akasimama akasema: Nilikuwa ni baina ya wanawake na mmoja kati yao akampiga mwenzie. Akaitaja Hadiyth hii kwa mukhtasari. Na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim

1002.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ الرَّبِيعَ بِنْتَ النَّضْرِ عَمَّتَهُ كَسَرَتْ ثَنِيَّةَ جَارِيَةٍ، فَطَلَبُوا إِلَيْهَا الْعَفْوَ، فَأَبَوْا، فَعَرَضُوا الْأَرْضَ، فَأَبَوْا، فَأَتَوْا رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَأَبَوْا إِلَّا الْقِصَاصَ، فَأَمَرَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بِالْقِصَاصِ، فَقَالَ أَنَسُ بْنُ النَّضْرِ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَتُكْسَرُ ثَنِيَّةُ الرَّبِيعِ؟ لَا، وَالَّذِي بَعَثَكَ بِالْحَقِّ، لَا تُكْسَرُ ثَنِيَّتُهَا، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "يَا أَنَسُ! كِتَابُ اللَّهِ: الْقِصَاصُ". فَرَضِيَ الْقَوْمُ، فَعَفَوْا، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ: "إِنَّ مِنْ عِبَادِ اللَّهِ مَنْ لَوْ أَقْسَمَ عَلَى اللَّهِ لِأَبْرَهُ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: Ar-Rubayyi' bint An-Nadhwr [15] shangazi yake alivunja meno ya msichana

mmoja, wakamuombea msamaha, wakakataa, wakawapa fidia ya jeraha, wakakataa, wakaenda kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wakakataa ila kisasi. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaamuru walipiziwe kisasi. Anas bin An-Nadhwr[16] akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Meno ya mbele ya Ar-Rubayyi' yavunjwe, haiwezekani! Naapa kwa Alyekutuma kwa haki meno yake hayatavunjwa. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Ee Anas Kitabu cha Allaah ni kulipa kisasi.” Watu wakaridhia wakamsamehe. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Hakika miongoni mwa waja wa Allaah kuna ambao lau atamuapia Allaah (kwa jambo) Anamfanyia.”[17]
[Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

1003.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ قُتِلَ فِي عِمِّيٍّ أَوْ رَمِيًّا بِحَجَرٍ، أَوْ سَوْطٍ، أَوْ عَصَا، فَعَلَيْهِ عَقْلُ الْخَطَا، وَمِنْ قُتِلَ عَمْدًا فَهُوَ قَوْدٌ، وَمَنْ حَالَ دُونَهُ فَعَلَيْهِ لَعْنَةُ اللَّهِ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَهَ، بِإِسْنَادٍ قَوِيٍّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuuwawa kwa (‘Immiyyan)[18] au kwa kurushiwa jiwe, mjeledi au fimbo, basi diya yake ni diya ya kuuwawa kimakosa. Na mwenye kuuwawa kwa makusudi atalipiziwa kisasi. Atakayeweka pingamizi baina ya hayo yaliyotajwa na baina ya msimamizi wa aliyeuwawa

basi laana ya Allaah Iwe juu yake.” [Imetolewa na Abuu Daawuud, An-Nasaaiy na Ibn Maajah kwa isnaad ya nguvu]

1004.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا أَمْسَكَ الرَّجُلُ الرَّجُلَ، وَقَتْلَهُ الْآخَرُ،
يُقْتَلُ الَّذِي قَتَلَ، وَيُحْبَسُ الَّذِي أَمْسَكَ} رَوَاهُ الدَّارَقُطْنِيُّ
مَوْصُولًا وَمُرْسَلًا، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْقَطَّانِ، وَرَجَّاهُ ثِقَاتٌ، إِلَّا
أَنَّ الْبَيْهَقِيَّ رَجَّحَ الْمُرْسَلَ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtu atakapomzuia mtu,
na mtu mwingine akamuuwa, aliyeuwa atauwawa na yule
aliyemzuia[19] atafungwa.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy ikiwa
ni Mursal na akaisahihisha Ibn Al-Qatwaan, wapokezi wake ni
madhubuti lakini Al-Bayhaqiyy ametilia nguvu kuwa ni Mursal]

1005.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ الْبَيْلَمَانِيِّ، {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَتَلَ مُسْلِمًا بِمَعَاهِدٍ. وَقَالَ: "أَنَا أَوْلَى مَنْ وَفَى
بِذِمَّتِهِ} أَخْرَجَهُ عَبْدُ الرَّزَّاقِ هَكَذَا مُرْسَلًا. وَوَصَلَهُ
الدَّارَقُطْنِيُّ، بِذِكْرِ ابْنِ عُمَرَ فِيهِ، وَإِسْنَادُ الْمَوْصُولِ وَاهٍ

Kutoka kwa ‘Abdi Rahmaan bin Al-Baylamaaniy[20] amesema kuwa: Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuuwa Muislam kwa kumlipizia kafiri mwenye mkataba[21] na akasema: “Mimi ni aula wa kutekeleza dhima yake.” [Imetolewa na ‘Abdu Razzaaq ameipokea ikiwa ni Mursal. Ad-Daaraqutwniy amesema ni Mawsuwl kwa kutajwa Ibn ‘Umar ndani yake. Isnaad yake Mawsuwl ni dhaifu sana]

1006.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {قُتِلَ غُلَامٌ غِيْلَةً، فَقَالَ عُمَرُ: لَوْ إِشْتَرَكْتُ فِيهِ أَهْلُ صَنْعَاءَ لَقَتَلْتُهُمْ بِهِ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Kijana mmoja aliuwawa kwa kuviziwa,[22] ‘Umar akasema lau watu wa Swan’aa wanalishirikiana katika mauaji yake ningaliwauwa kwa sababu yake. [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1007.

وَعَنْ أَبِي شُرَيْحٍ الْخُزَاعِيِّ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {فَمَنْ قُتِلَ لَهُ قَتِيلٌ بَعْدَ مَقَالَتِي هَذِهِ، فَأَهْلُهُ بَيْنَ خَيْرَتَيْنِ: إِمَّا أَنْ يَأْخُذُوا بِالْعَقْلِ. أَوْ يَقْتُلُوا} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ وَأَصْلُهُ فِي "الصَّحِيحَيْنِ" مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ بِمَعْنَاهُ

Kutoka kwa Abuu Shurayh Al-Khuzaa'iy[23] amesema Rasuli wa Allaah (ﷺ) amesema: “Mwenye kuuawa mtu wake baada ya maneno yangu haya basi watu wake wako baina ya khiyari mbili: ima wachukue diya au nao waue.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na An-Nasaa'iy. Asili ya hadiyth hii iko katika sahihi mbili kutoka katika hadiyth ya Abuu Hurayrah kwa maana kama hiyo]

[1] Jinayaat ni wingi wa Jinaya yenye maana ya “Kumdhuru mtu kwa kumpa adhabu ya kiwiliwili.” Vyovyote iwavyo kama ni kwa bahati mbaya au kwa makusudi.

[2] Hairuhusiwi kumuua aliyetoa Shahaadah. Mzinifu aliyeoa, muuwaji, na aliyeritadi wanauliwa. Katika Hadiyth moja tunajifunza kuwa ni ruhusa kuuwa kwa kujilinda ikitokezea mtu kuja kwa niyyah ya kuuwa. Hili ni jambo la nne katika yanayoruhusiwa kwa aliyetoa Shahaadah. Neno nafsi kwa nafsi iliyotajwa kwa Hadiyth hii ni kuuwa kwa kulipiza kisasi.

[3] Hii inaonyesha kuwa kuuwa ni moja katika madhambi makubwa sana. Ni kanuni ya msingi kuwa jambo kubwa zaidi huwa linatangulizwa zaidi, na madamu ya kuwa mauwaji ni dhambi kubwa zaidi basi na hukumu yake ndiyo itakayokuwa ya mwanzo siku ya Qiyaamah. Vivyo hivyo kwa kuwa majukumu ya watu kuswali hutangulizwa kuliko kingine chochote nacho ndicho kitakachoulizwa mwanzo hali kadhalika.

[4] ‘Ulamaa wamekubaliana kuwa mtumwa atakatwa kichwa chake kwa mauaji ya muungwana. Hata hivyo kuna rai tofauti ya ‘Ulamaa ikiwa naye muungwana atakatwa kichwa kwa kumuua mtumwa.

[5] ‘Ulamaa wengi wa mwanzo wamefuata rai ya kuwa ikiwa baba kamuuwa mwanawe, hawezi kuuliwa kwa kulipizwa kisasi cha mwanawe. Hata hivyo hawezi kukwepa adhabu inayomsubiri siku ya Qiyammaah. Sababu kubwa ya ubaguzi huu ni kuwa baba ndiye msingi na chanzo cha kuwepo kwa mtoto na sio kinyume chake na hivyo hawezi kuwa na haki ya kusitisha maisha ya baba yake.

[6] Al-Khatwaab amesema: “Makusudio ni kuwa zawadi haistahiki ila katika mashindano ya farasi, ngamia na mfano wa wanyama hao na kurusha mishale kwa sababu mambo haya ni maandalizi ya kupambana na adui na kutoa zawadi katika mashindano haya ni kuhimiza watu katika Jihaad.”

[7] Abuu Juhayfah aliuliza swali hili kwa sababu moja katika madhehebu ya Kishia linaamini kuwa pamoja na kuwa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa ni Rasuli wa Allaah aliyekuwa akishushiwa Wahyi na familia yake vile vile walikuwa na sehemu ya wahyi uliokuwa ukiteremka kwao. Abuu Juhayfah alikua anataka muono huu ufutwe kutoka kwao.

[8] Hadiyth hii inajulisha kuwa Muislam hauliwi kwa kulipiza kisasi kwa kumuuwa kafiri. Ikiwa imethibitika kuwa kafiri yule anahusika na nchi iliyo na vita na dola ya Kiislam basi hatouwawa kwa kuuwa kwake. Hii ni kwa mujibu wa kongamano la ‘Ulamaa. Ama ikithibitika kuwa aliyeuwawa ni dhimmi (kafiri anayeishi katika dola ya Kiislam na anayelipa kodi na ambaye yupo chini ya dola ya Kiislam), Maimaam watatu wana rai kuwa Muislam hatouwawa kwa mauaji haya ambapo Imaam wa nne Abuu Hanifa ana rai kuwa ni lazima auwawe.

[9] Hadiyth hii inathibitisha kuwa mtu huuliwa kwa kumuuwa mwanamke. Vivyo hivyo hakuna ubaguzi kwa misingi ya utajiri na umaskini wa mtu baina ya kijana na mtu mzima.

[10] Mtumwa alikata sikio la mtumwa. Sasa watu wakawa wana chaguo: Ni kisasi au kulipa diya. Bwana wa yule mtumwa hakutaka kisasi bali diya. Bwana wa yule mtumwa aliyetenda kosa hakuwa na uwezo wa kulipa na mtumwa mwenyewe hakuwa na uwezo wowote. Aliyeshtakia akawa hajapata chochote. Hii inamaanisha kuwa mwenye kuomba (maskini) hana jukumu la kulipa diya kwa yeyote na familia yake haishurutishwi kwa hilo vile vile. Kulipa fidia inakuwa ni wajibu kwa familia inayotarajia kurithi kutoka kwa mtu huyo. Madamu mtu mwenyewe hana cha kurithiwa, suala la kulipa fidia linakuwa halipo.

[11] Hadiyth hii inatujavya kuwa mtu asipokee fidia yoyote na asubiri hadi atakapopona kabisa. Hikmah ya jambo hili ni kuthibitika kwa jeraha lenyewe kwa kupona au kutokupona. Suala la fidia litategemea hali atakayokuwa nayo aliyejuruhiwa.

[12] Ikiwa mtoto aliye tumboni alikufa kabla ya kuzaliwa fidiya yake itakuwa ni bei ya kijakazi au mtumwa. Ikiwa mtoto alikufa baada ya kuzaliwa, fidia itakayolipwa itakuwa ni sawa na ngamia mia moja. Mauaji ya kukusudia au mauaji ya bahati mbaya hayahitaji kisasi, bali fidiya tu. Jina la kiarabu ‘Aaqila inafasiriwa kama ni ‘Asaba (jamaa wa karibu) ina maana kuwa fidiya haiwajibiki kwa muuaji peke yake bali kwa jamaa zake wa karibu.

[13] Hamal bin Maalik bin An-Naabighat Al-Hudhaliy Abuu Nadla Al-Basri alikuwa ni Swahaba.

[14] Ni wingi wa kuhani, mpiga ramli.

[15] Ar-Rubayyi’ ni mtoto wa Nadhr bin Damdam bin Zaid bin Haram, alikuwa ni shangazi wa Anas bin Maalik, Swahaba mkubwa aliyekuwa mtumishi wa Nabiyy (ﷺ) na alikuwa ni mama wa Haarith bin Suraaqa aliyekufa katika vita vya Badr.

[16] Alikuwa ni kaka yake Ar-Rubayyi’ na alikuwa ni ami yake Anas bin Maalik. Hakushiriki katika vita vya Badr na alikua akijutia hilo kila mara. Hivyo basi, katika siku ya vita vya Uhud, [baadhi ya Waislam walipokimbia, alikuenda mstari wa mbele wa maadui mushirikina na kujutia hali ya Waislam na kusema kwa sauti: ”Nasikia harufu ya Jannah katika mlima wa Uhud” alipigana hadi akauwawa.](#)

[17] Maneno haya aliyoyatoa Anas hayakuwa kupinga Shariy’ah ya Allaah. Alifanya kila jitihada lakini alikuwa na Iymaan kubwa na huruma ya Allaah. Kama ingalikuwa vinginevyo basi Rasuli wa Allaah asingemsifu bali angesema kinyume chake. Hadiyth hii inaeleza kuwa kisasi kinachukuliwa hata kwa kutolewa jino la mtu.

[18] ‘Immiyyan ni mtu kuuawa kwa kuchinjwa bila kujulikana muuaji wake au sababu zilizopelekea hilo kutofahamika. Vivyo hivyo, ikiwa mtu atauwawa katika vurugu, kisasi hakitahusika, kwa kuwa hukumu ihusikayo hapa ni Diya (fidiya ya fedha kwa mauaji). Ikiwa mtu amekufa kwa kupigwa na rungu, kupigwa mijeledi, au jiwe, aina hiyo ya mauaji inazingatiwa kuwa ni mauaji ya kukusudia ambayo inahitaji fidiya.

[19] Hadiyth hii inathibitisha kuwa mtu atakayemzuia mtu ili auwawe hauwawi bali atafungwa. Aina ya kifungo itatolewa na Qaadhw, inaweza kuwa ndefu au fupi kulingana na mazingira ya mauaji yenyewe.

[20] Huyu ni ‘Abdur-Rahmaan bin Abuu Zayd, muachwa huru wa ‘Umar bin Al-Khatwaab. Alikuwa ni mkazi wa Madiynah ambaye aliishi Haran. Alikuwa Taabi’i wa kizazi cha sita. Abuu Haatim anamuelezea: “Alikuwa ni dhaifu (katika mapokezi ya hadiyth)” Ibn Hibbaan anamtaja kuwa alikuwa madhubuti. Al Haafidh Abdul-‘Azim anasema kuhusiana naye: “Hakuwa katika watu wenye mamlaka kuhusu Hadiyth.”

[21] Neno la kiarabu lililotumika ni Mu’aahid ambalo lina maana ya kafiri ambaye hana makazi ya kudumu katika dola ya Kiislam na amekwenda katika dola hiyo kwa sababu maalumu baada ya kupata ruhusa kutoka katika dola hiyo. Mauaji ya mtu kama huyo kwa makubaliano ya kongomano la ‘Ulamaa ni haraam. Hata hivyo muuaji Muislam hatolipiziwa kisasi kulingana na ‘Ulamaa wote isipokuwa Abuu Haniyfah.

[22] Tukio lilikua ni watu watatu waliomuuwa kijana mmoja kwa pamoja na kwa kumvizia. ‘Umar alitoa hukmu ya kuuwawa kwa wote. Kuna rai tofauti kama inafaa kwa watu wengi waliomuua mtu mmoja kwa kuuwawa wote. Kauli yenye nguvu ni ile hukumu ya ‘Umar.

[23] Huyu ni ‘Amr bin Khuwaylid bin ‘Amr Al-Kabi Al-‘Adawi Al-Khuzaa’iy alisilimu baada ya Fat-h ya Makkah na alifariki Madiynah katika mwaka wa 68 Hijriyyah.

01-Mlango Wa Diya

بَابُ الدِّيَاتِ

01-Mlango Wa Diya[1]

عَنْ أَبِي بَكْرٍ بْنِ مُحَمَّدٍ بْنِ عَمْرِو بْنِ حَزْمٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ
جَدِّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ
كَتَبَ إِلَى أَهْلِ الْيَمَنِ... فَذَكَرَ الْحَدِيثَ، وَفِيهِ: {أَنَّ مَنْ اغْتَبَطَ
مُؤْمِنًا قَتْلًا عَنْ بَيِّنَةٍ، فَإِنَّهُ قَوْدٌ، إِلَّا أَنْ يَرْضَى أَوْلِيَاءُ
الْمَقْتُولِ، وَإِنْ فِي النَّفْسِ الدِّيَّةُ مِائَةً مِنَ الْإِبِلِ، وَفِي الْأَنْفِ إِذَا
أَوْعَبَ جَذْعُهُ الدِّيَّةُ، وَفِي اللِّسَانِ الدِّيَّةُ، وَفِي الشَّفَتَيْنِ الدِّيَّةُ،
وَفِي الذِّكْرِ الدِّيَّةُ، وَفِي الْبَيْضَتَيْنِ الدِّيَّةُ، وَفِي الصُّلْبِ الدِّيَّةُ،
وَفِي الْعَيْنَيْنِ الدِّيَّةُ، وَفِي الرَّجْلِ الْوَاحِدَةِ نِصْفُ الدِّيَّةِ، وَفِي
الْمَأْمُومَةِ ثُلُثُ الدِّيَّةِ، وَفِي الْجَائِفَةِ ثُلُثُ الدِّيَّةِ، وَفِي الْمُنْقَلَةِ
خَمْسَ عَشْرَةَ مِنَ الْإِبِلِ، وَفِي كُلِّ إصْبَعٍ مِنْ أَصَابِعِ الْيَدِ
وَالرَّجْلِ عَشْرٌ مِنَ الْإِبِلِ، وَفِي السِّنِّ خَمْسٌ مِنَ الْإِبِلِ وَفِي
الْمُوضِحَةِ خَمْسٌ مِنَ الْإِبِلِ، وَإِنَّ الرَّجُلَ يُقْتَلُ بِالْمَرْأَةِ، وَعَلَى
أَهْلِ الذَّهَبِ أَلْفُ دِينَارٍ { أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ فِي "الْمَرَّاسِيلِ"
وَالنِّسَائِيُّ، وَابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ، وَابْنُ حِبَّانَ،
وَأَحْمَدُ، وَاخْتَلَفُوا فِي صِحَّتِهِ

Kutoka kwa Abuu Bakr bin Muhammad bin ‘Amr bin Hazm[2]
kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake (رَضِيَ اللَّهُ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa: Nabiyy (عَنْهُ
aliwaandikia watu wa Yemen akaitaja Hadiyith ndani yake inasema:
“Kwa hakika mwenye kumuua Muumin bila ushahidi wa kupasa
kuuwawa, basi atalipiziwa kisasi, isipokuwa watakaporidhia
wasimamizi wa aliyeuwawa.”[3] Katika kuuwa nafsi kuna diya
kamili, nayo ni ngamia mia. Katika pua inapokatwa yote kuna diya
kamili. Katika macho mawili kuna diya kamili, katika ulimi kuna
diya kamili, katika midomo kuna diya kamili. Katika dhakar (uume)
kuna diya kamili, katika dhakari ya mwanamume kuna diya kamili,

katika uti wa mgongo kuna diya kamili, katika mguu mmoja kuna nusu ya diya. Katika mpasuko uliokaribia ubongo ni thuluthi ya diya. Katika jeraha lililovunja mifupa ni ngamia kumi na tano. Katika kila kidole miongoni mwa vidole vya mikononi na miguuni ni ngamia kumi. Katika jino ni ngamia watano. Katika jeraha linaloonyesha mfupa ni ngamia watano. Na kwa hakika mwanamume anauawa kwa kuuwa mwanamke. Na wenye dhahabu watatoa dinari elfu moja.”[4]
[Imetolewa na Abuu Daawud katika kitabu cha [Al-Maraasiyl](#), na An-Nasaaiy, Ibn Khuzaymah, Ibn Al-Jaarud, Ibn Hibbaan na Ahmad wamekhitilafiana katika kuswihi kwake]

1009.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {دِيَةُ الْخَطَا أُمَاسًا: عَشْرُونَ حِقَّةً،
وَعَشْرُونَ جَذَعَةً، وَعَشْرُونَ بَنَاتٍ مَخَاضٍ، وَعَشْرُونَ بَنَاتٍ
لَبُونٍ، وَعَشْرُونَ بَنِي لَبُونٍ} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ.
وَأَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، بِلَفْظٍ: {وَعَشْرُونَ بَنِي مَخَاضٍ} ، بَدَلًا:
{بَنِي لَبُونٍ} وَإِسْنَادُ الْأَوَّلِ أَقْوَى.
وَأَخْرَجَهُ ابْنُ أَبِي شَيْبَةَ مِنْ وَجْهِ آخَرٍ مَوْقُوفًا، وَهُوَ أَصَحُّ
مِنَ الْمَرْفُوعِ
وَأَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ: مِنْ طَرِيقِ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ،
عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ رَفَعَهُ: {الدِّيَةُ ثَلَاثُونَ حِقَّةً، وَثَلَاثُونَ
جَذَعَةً، وَأَرْبَعُونَ خِلْفَةً. فِي بَطُونِهَا أَوْلَادُهَا}

Kutoka kwa Ibn Mas-‘ud (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Diya ya bahati

mbaya ni aina tano: hiqqah[5] ishirini, jadha'ah[6] ishirini, banaati makhaadhw[7] ishirini, banaati labuwni[8] ishirini na baniy labuwni[9] ishirini.” [Imetolewa na Ad Daaraqutwniyy]

Na imepokewa na Al-Arba'ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) kwa tamshi: “...na baniy makhaadhw ishirini.” Badala ya: “...bin labuwni.” Isnaad ya Hadiyth ya kwanza ina nguvu.

Na Ibn Abiy Shaybah ameipokea kwa njia nyingine mawquwf ndiyo sahihi zaidi kuliko Marfuw’.

Abuu Daawuwd na At-Tirmidhiy wameipokea kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb naye kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake ikiwa ni Marfuw’: “Ad Diyyah ni hiqqah thalathini na jadha'ah thalathini na ngamia arubaini wenye mimba.”

1010.

وَعَنْ ابْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِنَّ أَعْتَى النَّاسِ عَلَى اللَّهِ ثَلَاثَةٌ: مَنْ قَتَلَ فِي حَرَمِ اللَّهِ، أَوْ قَتَلَ غَيْرَ قَاتِلِهِ، أَوْ قَتَلَ لِدُخْلِ الْجَاهِلِيَّةِ} أَخْرَجَهُ ابْنُ حِبَّانَ فِي حَدِيثٍ صَحَّحَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika watu wenye majivuno zaidi kwa Allaah ni watatu: mwenye kuuwa katika Haram ya Allaah (Makkah), au akamuuwa asiyeuwa au akauwa kwa kisasi cha kijahiliya.” [Imetolewa na Ibn Hibbaan katika hadiyth aliyoisahihisha]

1011.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو بْنِ الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَلَا إِنَّ دِيَةَ الْخَطَا شِبْهَ الْعَمْدِ مَا كَانَ بِالسَّوْطِ وَالْعَصَا مِائَةً مِنَ الْإِبِلِ، مِنْهَا أَرْبَعُونَ فِي بُطُونِهَا أَوْ لَادُهَا} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr bin Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (عَنْهُمَا) amesema: “Jueni diya ya kuuwa (bahati mbaya)[10] na kuuwa kunakofanana na makusudi inayokuwa kwa mjeledi au fimbo (diya yake ni) ngamia mia, katika hao arubaini wenye mimba.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd, An-Nasaa'iy na Ibn Maajah, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1012.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {هَذِهِ وَهَذِهِ سَوَاءٌ يَعْنِي: الْخُنْصَرُ وَالْإِبْهَامُ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ
وَلِأَبِي دَاوُدَ وَالتِّرْمِذِيِّ: {دِيَةُ الْأَصَابِعِ سَوَاءٌ، وَالْأَسْنَانُ سَوَاءٌ: الثَّنِيَّةُ وَالضَّرْسُ سَوَاءٌ}
وَلِابْنِ حِبَّانَ: {دِيَةُ أَصَابِعِ الْيَدَيْنِ وَالرِّجْلَيْنِ سَوَاءٌ، عَشْرَةٌ مِنَ الْإِبِلِ لِكُلِّ إصْبَعٍ}

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hiki kwa hiki ni sawa yaani kidole kidogo na kidole gumba.”[11] [Imetolewa na Al Bukhaariy]

Na kutoka kwa Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy: “Diya ya vidole ni sawa, na diya ya meno ni sawa, na diya ya meno ya mbele na magego ni sawa.”

Na Ibn Hibbaan ameipokea: “Diya ya vidole vya mikono na miguu ni sawa na ngamia kumi katika kila kidole.”

1013.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ رَفَعَهُ قَالَ: {مَنْ تَطَبَّبَ وَلَمْ يَكُنْ بِالطَّبِّ مَعْرُوفًا فَأَصَابَ نَفْسًا فَمَا دُونَهَا، فَهُوَ ضَامِنٌ} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَهُوَ عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيِّ وَغَيْرِهِمَا، إِلَّا أَنَّ مَنْ أَرْسَلَهُ أَقْوَى مِمَّنْ وَصَلَهُ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kutibu na si mjuzi wa tiba, akauwa nafsi na kusababisha madhara mengine basi atalipa.”[12] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy na akaisahihisha Al-Haakim. Nayo iko kwa Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na wengine. Isipokuwa alieifanya kuwa ni Mursal ana nguvu zaidi kuliko aliyeifanya Mawsuwl]

1014.

وَعَنْهُ، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {فِي الْمَوَاضِحِ خَمْسٌ، خَمْسٌ مِنَ الْإِبِلِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ. وَالْأَرْبَعَةُ. وَزَادَ أَحْمَدُ: {وَالْأَصَابِعُ سَوَاءٌ، كُلُّهُنَّ عَشْرٌ، عَشْرٌ مِنَ الْإِبِلِ} وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ.

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Katika majeraha yanayoonesha mfupa ni ngamia watano.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah)]

Na akaongezea Ahmad: “Na vidole vyote ni sawa ngamia kumi kumi.” Na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Al-Jaarud.

1015.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {عَقْلُ أَهْلِ الذِّمَّةِ نِصْفُ عَقْلِ الْمُسْلِمِينَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ وَالْأَرْبَعَةُ وَلَفَظُ أَبِي دَاوُدَ: {دِيَةُ الْمُعَاهِدِ نِصْفُ دِيَةِ الْحُرِّ} وَلِلنِّسَائِيِّ: {عَقْلُ الْمَرْأَةِ مِثْلُ عَقْلِ الرَّجُلِ، حَتَّى يَبْلُغَ الثُّلُثُ مِنْ دِيَّتِهَا} وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Diya ya ahlu adh-dhimmah[13] ni nusu ya diya ya Waislam.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah)]

Na katika tamshi la Abuu Daawuud: “Diya ya aliyewekeana mkataba (Mu’aahid) ni nusu ya diya ya aliye huru.”

Na katika An-Nasaaiy: “Diya ya mwanamke ni sawa na diya ya mwanamume hadi ifikie thuluthi katika diya yake.” Na akaisahihisha Ibn Khuzaymah

1016.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {عَقْلُ شِبْهِ الْعَمْدِ مُغْلَظٌ مِثْلُ عَقْلِ الْعَمْدِ، وَلَا يَقْتُلُ صَاحِبُهُ، وَذَلِكَ أَنْ يَنْزُرَ الشَّيْطَانُ، فَتَكُونَ دِمَاءٌ بَيْنَ النَّاسِ فِي غَيْرِ ضَعِيفَةٍ، وَلَا حَمَلٍ سِلَاحٍ} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ وَضَعَفَهُ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Diya ya kuuwa kunakofanana na makusudi ni diya nzito, mfano wa diya ya kuuwa kwa makusudi aliyeuwa hauwawi,[14] ni shari ya shaytwaan, damu ikamwagika baina ya watu bila ya kuwepo chuki wala kubeba silaha.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy na ameidhoofisha]

1017.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {قَتَلَ رَجُلٌ رَجُلًا عَلَى عَهْدِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَجَعَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ دِيَّتَهُ إِثْنَيْ عَشَرَ أَلْفًا} رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ، وَرَجَّحَ النَّسَائِيُّ وَأَبُو حَاتِمٍ إِرْسَالَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Mtu mmoja aliuwa mtu katika zama za Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akahukumu diya yake dirhamu elfu kumi na mbili. [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah)

1018.

وَعَنْ أَبِي رَمْثَةَ قَالَ: { أَتَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَمَعِيَ ابْنِي فَقَالَ: "مَنْ هَذَا؟" قُلْتُ: ابْنِي. أَشْهَدُ بِهِ. قَالَ: "أَمَّا إِنَّهُ لَا يَجْنِي عَلَيْكَ، وَلَا تَجْنِي عَلَيْهِ" رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ

Kutoka kwa Abuu Rimthah[15] amesema: Nilimuendea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) pamoja na mtoto wangu, akasema: “Huyu ni nani?” Nikasema ni mtoto wangu nami namshuhudia kuwa huyu ni mwanangu. Akasema: “Hutoulizwa kwa kosa lake, naye hatoulizwa kwa kosa lako.”[16] [Imetolewa na An-Nasaaiy na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Al-Jaarud]

[1] Diya ni malipo ya damu iliyomwagwa. Malipo haya yanalipwa kwa warithi wake.

[2] Huyu ni Abuu Bakr bin Muhammad bin ‘Amr bin Hazm Al-Ansari An-Najari Al-Madaniy Al-Qadhwi. Alikuwa madhubuti, mwenye taqwa na alikuwa mmoja katika waliochangia kwa vitabu sita vya Hadiyth. Alikuwa ni taabi’i wa kizazi cha tano. Mke wake anamuelezea kuwa hakuweza kulala kitandani mwake kwa muda wa miaka arubaini, akimaanisha kuwa alikua akiamka visimamo vya usiku. Ibn Ma’in amemtaja kuwa ni madhubuti, na Ibn Sa’ad amesema kuwa alifariki mwaka 120 Hijriyyah.

[3] Katika hii inamaanisha kuwa katika mauaji ya kukusudia, mrithi wa aliyeuwawa bila kujali kama ni wa damu au wa kupanga, wana hiari aina nne: (a) kisasi kwa kuuwawa kwa mkosaji, (b) fidiya, (c) kumsamehe muuwaji, (d) kuwa na utaratibu mwingine wa kulipa zaidi au pungufu ya fidiya.

[4] Hadiyth hii inaelezea misingi ya Shariy'ah na wanaostahiki, kwa mfano mrithi wa aliyeuwawa, aliyeuwawa bila ya kuwepo kwa makosa kwa upande wake, ana uchaguzi ima achukue fidiya au alipe kisasa. Kiwango cha fidiya ni ngamia mia moja au thamani yake. Kuna ibara inayotaja kila jina la kiungo. [Al-Ma-muwamah ni pigo linaloathiri akili ya mtu.](#) [Al-Jaaifah](#) ni jeraha linalotokana na koo hadi tumboni na kumalizia kienani na kutokozea tumboni. Al-Muwdhwihah ni jeraha linalopasua nyama ya mtu katika mwili na kufanya mfupa uonekane.

[5] Hiqqah ni ngamia jike akiwa katika mwaka wake wa nne

[6] Jadha'ah ni ngamia jike akiwa katika mwaka wake wa tano.

[7] Banaati makhaadhw ni ngamia jike wanaoingia mwaka wao wa pili.

[8] Banaati labuwni ni ngamia jike wanaoingia katika mwaka wao wa tatu.

[9] Baniy labuwni ni ngamia dume anaoingia katika mwaka wake wa tatu.

[10] Hadiyth iliyopokelewa na Ibn Mas-'uwd kuhusu diya inayolipwa kwa tukio la mauaji kimakosa imetajwa hapo kabla. Baadhi ya watu wakitumia Hadiyth hii wanachukulia fidiya hii kuwa ni sahihi na inaweza kutumika katika hali zote. Mantiki yake ni kuwa kila kesi ya mauaji hushughulikiwa peke yake kulingana na mazingira na hali ya aliyeuliwa. Kwa mfano ikiwa mtu kauwawa katika tukio lisilo la umwagaji damu katika hali iliyokuwa ya amani, basi adhabu yake itakuwa ni kali zaidi. Mauaji ya makusudi ni yale mtu ambayo anadhimiria na kutumia silaha yenye kuuwa na kusababisha mauti kwa mtu. Mauaji ya bahati mbaya ni yale ya mtu kutumia kitu chenye kuuwa lakini hakuwa amekusudia kumuuwa. Kwa mfano mshale, ambao umerushwa kumpiga kiwindwa, ambao ulimkosa na kumpata mwana Adam. Mauaji ya kukusudia ni yale ya kumkusudia mtu fulani lakin silaha au ala iliyotumika kufanya jambo lile si aghlabu kusababisha kifo kama vile; mjeledi, kirungu na tofali, na kadhalika.

[11] Vidole vyote vina thamani moja katika suala la malipo ya fidiya.

[12] Maadamu si mtaalamu wa tiba, haruhusiwi kufanya kazi yenyewe kwa hatari anayoweza kusababisha. Ikiwa mgonjwa alikuwa anatibiwa na daktari kama huyu akapata matatizo kutokana na operesheni au dawa alizoandikiwa zikamuuwa ni juu ya daktari yule kulipa fidiya.

[13] Hadiyth hii inabainisha mambo mawili. Kwanza, diya kwa Ahl Adh-dhimma ni nusu anayolipwa Muislam. Dhimmi ni neno linalotumiwa kwa maana ya kafiri anayeishi katika dola ya Kiislam. Pili, fidiya kwa mwanamke aliyejeruhiwa ni sawa na ya mwanamme, hadi itakapofikia kiwango cha theluthi ya fidiya. Chochote kinachozidi theluthi kitaingia katika nusu kama ni fidiya atakayolipwa mtu.

[14] Thamani ya fidiya kwa adhabu hii inategemea hukumu. Katika hali ya matukio ya mauaji yaliyoenea sehemu fulani au ya kwamba mauaji ametokea kuwa ni mtu mwenye tabia mbaya sana ya kikatili, ni juu ya Qadhwi kukadiria fidiya kama ya mauaji ya makusudi. Lakini kama tukio linaonesha kinyume na hivyo, Qadhwi ana uwezo wa kukadiria fidiya ndogo zaidi kama ilivyo katika mauaji yaliyofanyika kwa bahati mbaya na kwa makosa.

[15] Abuu Rimthah: Inasemekana kuwa jina lake ni Habib bin Haiyaan au Rifa'a bin Yathrib au 'Amaarah bin Yathrib, Balwiyy au Taym wa Banu Taym Ar-Rabaab. Inasemekana vile vile kuwa alikuwa Tamimi kizazi cha Amru Al-Qais bin Zayd Manaath bin Tamiym. Alikuwa ni Swahaba aliyekuwa akiishi mji wa Kufa Iraq.

[16] Lengo la kutajwa Hadiyth hii ni kuelezea kuwa mtoto habebi majukumu ya makosa aliyofanya baba yake na vivyo hivyo baba habebi dhambi ya mwanaye. Mtu haadhibiwi kwa makosa ya mwenzake.

02-Mlango Wa Kudai Damu Na Kiapo

بَابُ دَعْوَى الدِّمِّ وَالْقَسَامَةِ

1019.

عَنْ سَهْلِ بْنِ أَبِي حَثْمَةَ، عَنْ رَجَالٍ مِنْ كُبَرَاءِ قَوْمِهِ، أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ سَهْلٍ وَمُحَيِّصَةَ بْنَ مَسْعُودٍ خَرَجَا إِلَى خَيْبَرَ مِنْ جَهْدِ أَصَابِهِمْ، فَأَتَى مُحَيِّصَةُ فَأَخْبَرَ أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ سَهْلٍ قَدْ قُتِلَ، وَطُرِحَ فِي عَيْنٍ، فَأَتَى يَهُودَ، فَقَالَ: أَنْتُمْ وَاللَّهِ قَتَلْتُمُوهُ. قَالُوا: وَاللَّهِ مَا قَتَلْنَاهُ، فَأَقْبَلَ هُوَ وَأَخُوهُ حُوَيْصَةُ وَعَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ سَهْلٍ، فَذَهَبَ مُحَيِّصَةُ لِيَتَكَلَّمَ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { "كَبُرَ كَبْرٌ" يُرِيدُ: أَلَسَنَ، فَتَكَلَّمَ حُوَيْصَةُ، ثُمَّ تَكَلَّمَ مُحَيِّصَةُ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "إِنَّمَا أَنْ يَدُوا صَاحِبَكُمْ، وَإِنَّمَا أَنْ يَأْذَنُوا بِحَرْبٍ". فَكَتَبَ إِلَيْهِمْ فِي ذَلِكَ [كِتَابًا]. فَكَتَبُوا: إِنَّا وَاللَّهِ مَا قَتَلْنَاهُ، فَقَالَ لِحُوَيْصَةَ، وَمُحَيِّصَةَ، وَعَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ سَهْلٍ: "أَتَحْلِفُونَ، وَتَسْتَحِقُّونَ دَمَ صَاحِبِكُمْ؟" قَالُوا: لَا. قَالَ: "فَتَحْلِفُ لَكُمْ يَهُودُ؟" قَالُوا: لَيْسُوا مُسْلِمِينَ فَوَدَّاهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ مِنْ عِنْدِهِ، فَبَعَثَ إِلَيْهِمْ مَائَةَ نَاقَةٍ. قَالَ سَهْلٌ: فَلَقَدْ رَكُضْتَنِي مِنْهَا نَاقَةٌ حَمْرَاءُ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

Kutoka kwa Sahli bin Abuu Hathmah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kutoka kwa wakubwa wa kabila lake kuwa: 'Abdullaah bin Sahl[1] na Muhayyiswah[2] bin Mas-'uwd walienda Khaybar kwa sababu ya

ukame uliowapata. Muhayyiswah akamuendea ‘Abdullaah bin Sahl akaambiwa kuwa ameuliwa na ametupwa katika kisima. Akawaendea Mayahudi na akawaambia: “Wa-Allaahi nyinyi mumemuuwa.” Mayahudi wakasema: “Wa-Allaahi hatukumuuwa.” Yeye na ndugu yake Huwayyiswah[3] na ‘Abdur-Rahmaan bin Sahl[4] walifika na Muhayyiswah alikuwa anataka kuzungumza na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamkatisha kwa kusema: “Mtangulize mkubwa, mtangulize mkubwa.” Huwayyiswah akazungumza kisha Muhayyisah naye akazungumza. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaambia: “Ima waondoe diya ya mwenzenu au watangaziwe vita.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaandikia barua, nao wakajibu: “Wa-Allaahi sisi hatukumuuwa.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia Huwayyiswah, Muhayyiswah na ‘Abdur-Rahmaan bin Sahl: “Mtaapa ili mstahiki damu ya mwenzenu?” Wakasema: “Hapana.” Akawaambia: “Basi Mayahudi wataapa.” (kuwa hawakuhusika) wakasema: “Wao sio Waislamu.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ) binafsi yake akamlipia diya, [5] akawapelekea ngamia mia. Sahli amesema: “Katika ngamia hao kuna ngamia mwekundu aliyenikanyaga.” [Bukhaariy, Muslim]

1020.

وَعَنْ رَجُلٍ مِنَ الْأَنْصَارِ، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَقْرَّ الْقَسَامَةِ عَلَى مَا كَانَتْ عَلَيْهِ فِي الْجَاهِلِيَّةِ، وَقَضَى بِهَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بَيْنَ نَاسٍ مِنَ الْأَنْصَارِ فِي قَتِيلٍ ادَّعَوْهُ عَلَى الْيَهُودِ } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa mtu mmoja katika Answaar amesema kuwa: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekiri Qasaamah iliyokuwa katika zama za ujahiliya[6] na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amehukumu kwa hiyo Qasaamah (kiapo katika kesi za mauaji) baina ya watu mongoni mwa Answaar kuhusu mtu wao aliyeuwawa waliodai kuwa waliomuuwa ni mayahudi. [Imetolewa na Muslim]

[1] 'Abdullaah bin Sahl bin Zaid bin Ka'ab bin 'Aamir Al-Answaar Al-Haarith aliuwawa Khaybar na mwili wake ulipatikana katika chemchem huku shingo yake ikionekana imevunjwa.

[2] Abu Sa'iyd Muhayyiswah bin Mas-'uwd bin Ka'ab Al-Haarith Al-Answaar Al-Madaniy, ni jamaa wa Swahaba aliyeuwawa; 'Abdullaah ambaye alisilimu kabla ya Hijra na alishiriki katika vita vya Uhud, Al-Khandaq na vita vingine muhimu vilivyobakia. Rasuli wa Allaah alimtuma Fadak kuenda kuwalingania watu katika Uislamu.

[3] Huyu alikuwa ni kaka wa Muhayyiswah alisilimu kwa msaada wa ndugu yake. Inasemekana alishiriki katika vita vya Khandaq, Uhud na vita vingine muhimu pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).

[4] Huyu ni kaka yake 'Abdullaah bin Sahl mama yake akiitwa Laylah, binti wa Nafi bin 'Aamir. Inasemekana kuwa alipigana katika vita vya Badr, Uhud na vita vingine vyote muhimu. Aliumwa na nyoka na 'Amaara bin Hazm alimtibu kwa Ruqyah kwa maelekezo kutoka kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Hata hivyo, Ibn Hajar aliingiwa na wasiwasi wa kuipokea na kuweka katika kitabu chake Al-Isaabah.

[5] Qasaamah ina maana ya masharti ambapo muuaji hajafahamika, mtuhumiwa au watu husika au watu wa kabila fulani wanatakiwa watoe kiapo. Tukio kama hili linapotokea, watu hamsini wanatakiwa wajitokeze ili waape ya kwamba wao au watu wa kijiji hawajafanya mauaji hayo. Aina hii ya viapo vinatumika mahakamani tu. Viapo hivi havitumiki katika aina zingine za adhabu (huduud). Qasaamah inatekelezwa na watu wawili (mlalamikaji au mlalamikiwa). Ikiwa mlalamikaji (warithi wa marehemu) watatoa ushahidi, au watatumia kiapo kama ushahidi haupo kuwa hawa ndio wauaji wenyewe, bila shaka itakuwa wazi kwa wanaojitetea kuwa ni

wajibu kwao kulipa fidiya kwa walalamikaji. Walalamikaji wakishindwa kufanya hivyo, walalamikiwa wanatakiwa kuleta watu wapatao hamsini kisha waape kuwa hawajaua. Kiapo kilichotajwa kitatolewa na wale watu waliochaguliwa na muombaji mwenyewe. Hii ndio hukumu pekee inayohalalisha kiapo kwa upande wa muombaji vile vile.

[6] Katika hali hii, Shariy'ah inakubali kiapo kitakachoapwa na kafiri. Qasaamah haifanyi kazi kwa tuhuma zitakazoletwa na muombaji ila itakapokuwa imeambatanishwa na ushahidi mzito unaohusiana na mauaji.

03-Mlango Wa Kuwapiga Vita Waasi (Wa Kiongozi)

بَابُ قِتَالِ أَهْلِ الْبَغْيِ

03-Mlango Wa Kuwapiga Vita Waasi (Wa Kiongozi)

1021.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ حَمَلَ عَلَيْنَا السَّلَاحَ، فَلَيْسَ مِنَّا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kutubebea silaha si katika sisi.”[1] [Bukaariy, Muslim]

1022.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَالِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ خَرَجَ عَنِ الطَّاعَةِ، وَفَارَقَ الْجَمَاعَةَ،
وَمَاتَ، فَمِيتَتُهُ مِيتَةُ جَاهِلِيَّةٍ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kutoka
katika utiifu (wa kiongozi) na akajitenga na jamaa na akafariki, basi
kifo chake ni kifo cha kijahiliya.”[2] [Imetolewa na Muslim]

1023.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {تَقْتُلُ عَمَّارًا أَلْفَنَةُ الْبَاغِيَةِ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ammaar
atauwawa na kikundi kilichoasi (kiovu).”[3] [Imetolewa na Muslim]

1024.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {هَلْ تَدْرِي يَا ابْنَ أُمِّ عَبْدِ، كَيْفَ حُكِّمَ اللَّهُ
فِي مَنْ بَغَى مِنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ؟}، قَالَ: اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَعْلَمُ. قَالَ:

"لَا يُجْهَزُ عَلَى جَرِيحِهَا، وَلَا يُقْتَلُ أَسِيرُهَا، وَلَا يُطْلَبُ هَارِبُهَا، وَلَا يُقْسَمُ فَيُؤْهَى { رَوَاهُ الْبَزَّازُ وَ الْحَاكِمُ وَصَحَّحَهُ فَوْهَمٌ، فَإِنَّ فِي إِسْنَادِهِ كَوْثَرَ بَنَ حَكِيمٍ، وَهُوَ مَثْرُوكٌ وَصَحَّ عَنْ عَلِيٍّ مِنْ طَرُقٍ نَحْوُهُ مَوْقُوفًا. أَخْرَجَهُ ابْنُ أَبِي شَيْبَةَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ee mwana wa Ummi ‘Abd (‘Abdullaah bin Mas-‘uwd), unajua nini hukumu ya Allaah kwa aliyeasi katika ummah huu? Akasema Allaah na Rasuli wa Allaah Wanajua. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Aliyejeruhiwa hamalizwi, mateka wake hauliwi, aliyekimbia hafuatwi na mali yake haigawanywi.”[4] [Imetolewa na Al-Bazaar na Al-Haakim na akaisahihisha akaghafilika kwa sababu katika isnaad yake yumo Kawthar[5] bin Hakiym ambaye Hadiyth zake zinaachwa. Lakini imeswihi kutoka kwa ‘Aliy kwa njia nyingine mfano wa Hadiyth kama hii ikiwa ni Mawquwf iliyopokewa na Ibn Abiy Shaybah na Al-Haakim]

1025.

وَعَنْ عَرْفَجَةَ بْنِ شَرِيحٍ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { مَنْ أَتَاكُمْ وَأَمَرَكُمْ جَمِيعٌ، يُرِيدُ أَنْ يُفَرِّقَ جَمَاعَتَكُمْ، فَاقْتُلُوهُ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Arfajah bin Shurayh[6] amesema kuwa alimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Atakayewajia nyinyi na jambo lenu ni moja, na anataka

kuwatenganisha katika umoja wenu, basi mpigeni vita.” [Imetolewa na Muslim]

[1] Kupigana dhidi ya Shariy’ah ni dhambi kubwa. Vivyo hivyo, kumtishia Muislam kumuuwa au kumtolea silaha ni dhambi kubwa. Ikiwa mtu amehalalisha damu ya Muislam au kumuuwa kwa kuona kuwa ni halaal kufanya hivyo, bila shaka mtu huyu atakuwa ameritadi. Mtu huyu anazingatiwa kuwa amekufuru kwa makubaliano ya Jamhuri ya ‘Uamaa. Hata hivyo ni halaal kuwapiga Waislam walioasi dhidi ya mamlaka ya Shariy’ah kama ilivyokuja katika Qur-aan:

فَقَاتِلُوا الَّتِي تَبْغِي حَتَّى تَفِيءَ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ ﷻ

“...basi piganeni na ambalo linakandamiza mpaka lielemee kwenye amri ya Allaah...” [Al-Hujuraat: 9]. Kadhalika tunajifunza hayo katika Hadiyth mbalimbali.

[2] Utiifu kwa Amiri (mtawala) ni wajibu madamu hajakwenda kinyume na Shariy’ah za Kiislam. Vivyo hivyo, hairuhusiwi kutoka katika jamaa, maadamu hafanyi yanayoweza kumtoa katika Uislam. Kwa kumkaidi Amiri anayetawala kwa misingi ya Shariy’ah ya Kiislam ni uasi. Yeyote anayevunja mamlaka ya Amiri au kujitoa katika kundi pamoja na kuwa hatonekana kuwa ni kafiri lakini ataonekana kuwa amekwenda kombo. Tofauti yao ni kuwa si katika wao mwenye Imaam au mamlaka ya kishariy’ah.

[3] Aliuwawa katika vita vya Swiffiyn na wale waliokuwa wakipigana dhidi ya ‘Aliy.

[4] Hakuna kutokubaliana kuhusu uhalali wa kuwapiga vita watu waliodhulumu. Hata hivyo, kuna tofauti ya maoni kwa ‘Ulamaa katika kumata mali zao, kuwaacha waliojeruhiwa na kuwashawishi wanaotaka kutoroka.

[5] Alikuwa ni mkazi wa mji wa Kufa uliopo ‘Iraq na baadae akahamia Halab. Ibn Ma’iyn anamzungumzia, “Si chochote katika Hadiyth.” Ahmad bin Hanbal naye anamsema: “Hadiyth zake ni za uongo.”

[6] ‘Arfajah bin Shurayh Ashja’i alikuwa ni Swahaba aliyekuwa akiishi Kufa (mji uliopo Iraq).

04-Mlango Wa Kupigana Na Anayefanya Jinai Na Kumuuwa Aliyeritadi

بَابُ قِتَالِ الْجَانِي وَقَتْلُ الْمُرْتَدِّ

04-Mlango Wa Kupigana Na Anayefanya Jinai Na Kumuuwa Aliyeritadi

1026.

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ قُتِلَ دُونَ مَالِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayeuliwa kwa kutetea mali yake, huyo ni Shahiyd.”[1] [Imetolewa na Abuu Daawuwd, An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

1027.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {قَاتَلَ يُعْلَى بْنُ أُمَيَّةَ رَجُلًا، فَعَضَّ أَحَدُهُمَا صَاحِبَهُ، فَنَزَعَ ثَنِيَّتَهُ،

فَاخْتَصَمَا إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ:
 "أَيَعَضُّ أَحَدُكُمْ أَخَاهُ كَمَا يَعَضُّ الْفَحْلُ ؟ لَا دِيَّةَ لَهُ" { مُتَّفَقٌ
 عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: Yu’laa bin Ummyyah alipigana na mtu, mmoja wao akang’ata mkono wa mwingine, akauvuta mkono wake kutoka mdomoni mwake, meno yake ya mbele yakadondoka. Wakashtakiana kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Mmoja wenu anang’ata kama fahali ang’atavyo, mtu huyo hana diya.”[2] [Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

1028.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ أَبُو الْقَاسِمِ
 صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَوْ أَنَّ إِمْرَأًا اطَّلَعَ عَلَيْكَ بِغَيْرِ
 إِذْنٍ، فَحَذَفْتَهُ بِحَصَاةٍ، فَفَقَاتَ عَيْنَهُ، لَمْ يَكُنْ عَلَيْكَ جُنَاحٌ}
 مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ .

وَفِي لَفْظٍ لِأَحْمَدَ، وَالنَّسَائِيَّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ: {فَلَا دِيَّةَ
 لَهُ وَلَا قِصَاصَ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Lau mtu atakuchungulia bila ruhusa na ukamrushia kijiwe ukaliharibu jicho lake, basi huna dhambi.”[3] [Bukhaariy, Muslim]

Na katika tamshi la Ahmad na An-Nasaa'iy na akaisahihisha Ibn Hibbaan imesema: “Hana diya wala kulipiza kisasi.”

1029.

وَعَنْ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {قَضَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنْ حِفْظَ الْحَوَائِطِ بِالنَّهَارِ عَلَى أَهْلِهَا، وَأَنْ حِفْظَ الْمَاشِيَةِ بِاللَّيْلِ عَلَى أَهْلِهَا، وَأَنْ عَلَى أَهْلِ الْمَاشِيَةِ مَا أَصَابَتْ مَاشِيَتُهُمْ بِاللَّيْلِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ إِلَّا التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَفِي إِسْنَادِهِ اخْتِلَافٌ

Kutoka kwa Al-Baraa bin ‘Aazib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alihukumu kuwa kuhifadhi mashamba wakati wa mchana ni jukumu la wenyewe, na kuhifadhi wanyama wakati wa usiku ni jukumu la wenyewe, na kwamba wenye wanyama watalipa kilichoharibiwa na wanyama wao iwapo wameharibu wakati wa usiku.[4] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa At-Tirmidhiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan na katika isnaad yake kuna tofauti]

1030.

وَعَنْ مُعَاذِ بْنِ جَبَلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي رَجُلٍ أَسْلَمَ ثُمَّ تَهَوَّدَ: {لَا أَجْلِسُ حَتَّى يُقْتَلَ، قَضَاءُ اللَّهِ وَرَسُولِهِ، فَأَمْرٌ بِهِ، فَقُتِلَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِأَبِي دَاوُدَ: {وَكَانَ قَدْ أُسْتُتِبَ قَبْلَ ذَلِكَ}

Kutoka kwa Mu'aadh bin Jabl (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuhusu mtu aliyasilimu kisha akawa myahudi: "Sitakaa hadi auwawe,[5] hiyo ndiyo hukumu ya Allaah na Rasuli wa Allaah." Baada ya hapo ikaamriwa auwawe. [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika riwaayah ya Abuu Daawuwd inasema: "Kabla ya kuuwawa alipewa nafasi ya kutubia."

1031.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ بَدَّلَ دِينَهُ فَاقْتُلُوهُ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Mwenye kuritadi (kuacha Uislam- anaingia katika Uislam kwa hadaa kwa lengo la kurudi katika dini yake na kuanza kukejeli na kuutukana Uislam) muuweni." [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1032.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ، {أَنَّ أَعْمَى كَانَتْ لَهُ أُمٌّ وَلَدَ تَشْتُمُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَتَقَعُ فِيهِ، فَيَنْهَاهَا، فَلَا تَنْتَهِي، فَلَمَّا كَانَ ذَاتَ لَيْلَةٍ أَخَذَ الْمِعْوَلَ، فَجَعَلَهُ فِي بَطْنِهَا، وَاتَّكَأَ عَلَيْهَا فَقَتَلَهَا فَبَلَغَ ذَلِكَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: "أَلَا إِشْهَدُوا أَنَّ دَمَهَا هَذَرٌ" رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَرَوَاتُهُ ثِقَاتٌ.

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Kulikuwa kuna kipofu aliyekuwa na mjakazi, mjakazi huyu alikuwa akimtukana Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na akimdhalilisha. Alikuwa akimkataza bila kukatazika. Usiku mmoja alichukua mtaimbo akauweka juu ya tumbo lake (mjakazi) akaliegemea juu yake akamuuwa. Hili likamfikia Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Fahamuni! Shuhudieni kwa hakika damu yake (mjakazi huyo) ni halaal.” [Imetolewa na Abuu Daawuud wapokezi wake ni madhubuti]

[1] Katika Hadiyth nyingine yenye mnasaba kama huu inasema: “Atakayeuwawa kwa ajili ya mali yake, nafsi, familia na dini yake huyo ni shahidi, na hivyo anastahiki Jannah.” Ikiwa jambazi atamshambulia mtu na kutaka kuchukua mali yake, mke au watoto wake, na mtu yule akajilinda na kumuuwa yule adui katika hali ile hatokuwa ni mwenye dhambi. Hukumu hii ni makubaliano ya Jamhuri ya ‘Ulamaa.

[2] Ikiwa mtu atajilinda na jambo fulani kisha mwenzake akapata madhara kwa ajili hiyo huwa hakuna fidiya.

[3] Hii inahusu sehemu ambazo huwezi kuingia bila ya ruhusa kama vile nyumba ya mtu au sehemu ya mtu maalum.

[4] Hadiyth hii inamaanisha kuwa ikiwa kundi la wanyama litaharibu mazao au shamba la mtu wakati wa mchana, basi mwenye wanyama hatolipa chochote. Hii ni kwa sababu kwa ada ya wanyama ni kupata malisho yao wakati wa mchana. Katika hali hii mwenye shamba ndiye anayetakiwa kuwa makini na shamba lake zaidi. Vivyo hivyo ni muhimu mtu kulinda wanyama wake usiku kwani kwa wakati huo wanyama wakisababisha madhara ni wajibu wake kulipa.

[5] Hadiyth hii na inayofuatia imepokewa na Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) ambazo zinaeleza kwa uwazi kabisa kuwa adhabu ya aliyeritadi ni kuuliwa. Ikiwa mtu kalazimishwa kuwa hivyo au kusema maneno ya kuonyesha kuwa ameritadi, mtu huyo atasamehewa na Shariy’ah. Baadhi ya ‘Ulamaa wanaona kuwa mwanamke aliyeritadi haadhibiwi. Muono huu sio sahihi kwani naye anaadhibiwa kwa makubaliano ya ‘Ulamaa.

كِتَابُ الْحُدُودِ

Kitabu Cha Al-Huduwd (Adhabu)

كِتَابُ - 10-Kitabu Cha Al-Huduwd (Adhabu) الْحُدُودِ

01-Mlango Wa Adhabu Ya Uzinifu

بَابُ حَدِّ الزَّانِي

01-Mlango Wa Adhabu Ya Uzinifu

1033.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ وَزَيْدِ بْنِ خَالِدٍ الْجُهَنِيِّ
رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا { أَنَّ رَجُلًا مِنَ الْأَعْرَابِ أَتَى رَسُولَ اللَّهِ

صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! أَنْشُدْكَ بِاللَّهِ
 الْأَقْضَيْتَ لِي بكِتَابِ اللَّهِ، فَقَالَ الْآخَرُ وَهُوَ أَفْقَهُ مِنْهُ نَعَمْ.
 فَأَقْضَ بَيْنَنَا بكِتَابِ اللَّهِ، وَأَذِنَ لِي، فَقَالَ: "قُلْ". قَالَ: إِنَّ ابْنِي
 كَانَ عَسِيفًا عَلَى هَذَا فَرَزَنِي بِأَمْرَاتِهِ، وَإِنِّي أُخْبِرْتُ أَنَّ عَلَى
 ابْنِي الرَّجْمَ، فَافْتَدَيْتُ مِنْهُ بِمِائَةِ شَاةٍ وَوَلِيدَةٍ، فَسَأَلْتُ أَهْلَ
 الْعِلْمِ، فَأَخْبَرُونِي: أَنَّ مَا عَلَى ابْنِي جَلْدُ مِائَةٍ وَتَغْرِيْبُ عَامٍ،
 وَأَنَّ عَلَى امْرَأَةِ هَذَا الرَّجْمَ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
 وَآلِهِ وَسَلَّمَ "وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَا أَقْضِيَنَّ بَيْنَكُمَا بِكِتَابِ اللَّهِ،
 الْوَلِيدَةُ وَالْغَنَمُ رَدٌّ عَلَيْكَ، وَعَلَى ابْنِكَ جَلْدُ مِائَةٍ وَتَغْرِيْبُ عَامٍ،
 وَاغْدُ يَا أُنَيْسُ إِلَى امْرَأَةِ هَذَا، فَإِنْ اعْتَرَفَتْ فَارْجُمُهَا" { مُتَّفَقٌ
 عَلَيْهِ، هَذَا وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah na Zayd bin Khaalid Al-Juhaniyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) wamesema: Mtu mmoja katika mabedui alimjia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: "Ee Rasuli wa Allaah! Nakuomba kwa Allaah unihukumu kwa Kitabu Cha Allaah". Mwingine ambaye ni mjuzi kuliko yeye akasema: "Ndio, hukumu baina yetu kwa Kitabu Cha Allaah, na uniruhusu niseme." Akasema Rasuli wa Allaah: "Sema." Akasema: "Mwanangu alikuwa ni muajiriwa wa huyu, akazini na mkewe, nami nilikuwa nimeambiwa kuwa mwanangu atarujumiwa, nimeamtolea fidia ya mbuzi mia na mjakazi. Nikawauliza wenye ilmu wakaniambia kuwa mwanangu achapwe mijeledi mia na atolewe mjini mwaka mmoja na mke wa huyu arujumiwe. Akasema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): "Naapa kwa Ambaye nafsi yangu imo Mkononi mwake! Nitahukumu baina yenu kwa Kitabu Cha Allaah. Mjakazi na mbuzi warudishwe kwako. Na mwanao achapwe mijeledi mia na kutolewa mjini mwaka mmoja. Ee Unays, nenda hadi kwa mke wa bwana huyu, akiungama umrajimu

(umpige mawe).”[2] [Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

1034.

وَعَنْ عُبَادَةَ بْنِ الصَّامِتِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {خُذُوا عَنِّي، خُذُوا عَنِّي، فَقَدْ جَعَلَ اللَّهُ لَهُنَّ سَبِيلًا، الْبِكْرُ بِالْبِكْرِ جَلْدُ مِائَةٍ، وَنَفْيُ سَنَةٍ، وَالتَّيِّبُ بِالتَّيِّبِ جَلْدُ مِائَةٍ، وَالرَّجْمُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ.

Kutoka kwa ‘Ubaadah bin Asw-Swaamit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Chukueni kutoka kwangu, chukueni kutoka kwangu. Allaah Amewajaalia (wanawake) kupata njia.[3] Mume asiye na mke, na mke asiye na mume (watakapozini) watapigwa mijeledi mia na kutolewa mjini mwaka mmoja. Mume aliyeowa na mke aliyeolewa (wakizini) watapigwa mijeledi mia[4] na kupigwa mawe (Rajm).” [Imetolewa na Muslim]

1035.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَتَى رَجُلٌ مِنَ الْمُسْلِمِينَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَهُوَ فِي الْمَسْجِدِ فَنَادَاهُ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي زَنَيْتُ، فَأَعْرَضَ عَنْهُ، فَتَنَحَّى تَلْقَاءَ وَجْهِهِ، فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي زَنَيْتُ، فَأَعْرَضَ عَنْهُ، حَتَّى ثَنَى ذَلِكَ عَلَيْهِ أَرْبَعَ مَرَّاتٍ، فَلَمَّا شَهِدَ

عَلَى. نَفْسِهِ أَرْبَعَ شَهَادَاتٍ. دَعَاهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ "أَبُكَ جُنُونٌ؟" قَالَ. لَا. قَالَ: "فَهَلْ أَحْصَنْتَ؟" قَالَ: نَعَمْ. فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "إِذْهَبُوا بِهِ فَارْجُمُوهُ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Mtu mmoja katika Waislamu alimjia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiwa Msikitini, akamnadia: “Ee Rasuli wa Allaah! Mimi nimezini.” Rasuli wa Allaah akampa mgongo, akamuendea akamuambia: “Ee Rasuli wa Allaah! Mimi nimezini!” Rasuli wa Allaah akampa mgongo, hata akaikariri kauli hiyo mara nne. Alipojishuhudia zinaa yeye mwenyewe mara nne, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuita akamuuliza: “Una wazimu?” Akasema: “Laa (hapana).” Akasema: “Umehifadhika (una mke)?” Akasema: “Ndio.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Mchukueni na mumrajimu.”[5] [Bukhaariy, Muslim]

1036.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {لَمَّا أَتَى مَا عِزُّ بْنُ مَالِكٍ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ لَهُ: "لَعَلَّكَ قَبَّلْتَ، أَوْ غَمَزْتَ، أَوْ نَظَرْتَ؟" قَالَ: لَا يَا رَسُولَ اللَّهِ} رَوَاهُ
الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ [6] Nabiy[6] Maa’iz bin Maalik alipokuja kwa Nabiy[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) akasema: “Pengine ulibusu au uligusa au ulitazama.” Akasema Maa’iz: “Sivyo Ee Rasuli wa Allaah!” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1037.

وَعَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُ خَطَبَ فَقَالَ: إِنَّ اللَّهَ بَعَثَ مُحَمَّدًا بِالْحَقِّ، وَأَنْزَلَ عَلَيْهِ الْكِتَابَ، فَكَانَ فِيهَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَيْهِ آيَةَ الرَّجْمِ. قَرَأْنَاهَا وَوَعَيْنَاهَا وَعَقَلْنَاهَا، فَرَجَّمَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَرَجَمْنَا بَعْدَهُ، فَأَخْشَى أَنْ طَالَ بِالنَّاسِ زَمَانٌ أَنْ يَقُولَ قَائِلٌ: مَا نَجِدُ الرَّجْمَ فِي كِتَابِ اللَّهِ، فَيَضِلُّوا بِتَرْكِ فَرِيضَةِ أَنْزَلَهَا اللَّهُ، وَإِنَّ الرَّجْمَ حَقٌّ فِي كِتَابِ اللَّهِ عَلَى مَنْ زَنَى، إِذَا أَحْصَيْنَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ، إِذَا قَامَتِ الْبَيِّنَةُ، أَوْ كَانَ الْحَبْلُ، أَوْ الْإِعْتِرَافُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Umar bin Al-Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alihutubia akasema: “Kwa hakika Allaah Alimtuma Muhammad (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kwa haki, Akamteremshia Kitabu, ikawa katika Aliyomteremshia ni Aayah ya Rajmi, tuliisoma tukaihifadhi na tukaizingatia. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akapiga kwa mawe (Rajm), na sisi baada yake tukapiga kwa mawe. Kwa hivyo nachelea isije zama zikawa ndefu kwa watu akaja kusema mwenye kusema: “Mbona hatuoni kupiga kwa mawe (Rajm) katika Kitabu Cha Allaah!” Kwa ajili hiyo wakapotea kwa kuacha

faradhi Aliyoiteremsha Allaah. Na kwa hakika Rajm kumethubutu katika Kitabu Cha Allaah[7] kwa mwenye kuzini aliyeoa au ameolewa miongoni mwa wanaume na wanawake utakaposimama ubainifu au kwa kushika mimba au kwa kukiri.” [Bukhaariy, Muslim]

1038.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "إِذَا زَنَتُ أَمَةً أَحَدِكُمْ، فَتَبَيَّنَ زَنَاهَا، فَلْيَجْلِدْهَا الْحَدَّ، وَلَا يُثْرَبْ عَلَيْهَا، ثُمَّ إِنْ زَنَتُ فَلْيَجْلِدْهَا الْحَدَّ، وَلَا يُثْرَبْ عَلَيْهَا، ثُمَّ إِنْ زَنَتِ الثَّلَاثَةَ، فَتَبَيَّنَ زَنَاهَا، فَلْيَبِيعْهَا وَلَوْ بِحَبْلٍ مِنْ شَعْرِ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَهَذَا لَفْظُ مُسْلِمٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Nimemsikia Rasuli wa Allaah akisema: “Atakapozini mjakazi wa mmoja wenu[8] na uzinifu wake ukabainika, basi ampe adhabu kwa kumchapa mijeledi wala asimkaripie. Atakapozini tena amchape mijeledi wala asimkaripie. Atakapozini mara ya tatu uzinifu wake ukabainika basi amuuze japo kwa kamba ya nywele.” [Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

1039.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {أَقِيمُوا الْحُدُودَ عَلَى مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wasimamishieni adhabu iliyowamiliki mikono yenu.” [Imetolewa na Abuu Daawuud]

1040.

وَعَنْ عُمَرَ بْنِ حَصِينٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ امْرَأَةً مِنْ جُهَيْنَةَ أَتَتْ نَبِيَّ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَهِيَ حُبْلَى مِنَ الزَّانَفَقَالَتْ: يَا نَبِيَّ اللَّهِ! أَصَبْتُ حَدًّا، فَأَقِمْهُ عَلَيَّ، فَدَعَا نَبِيُّ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَلِيَّهَا. فَقَالَ: "أَحْسِنِ إِلَيْهَا فَإِذَا وَضَعْتَ فَأَتِنِي بِهَا" ففعل. فَأَمَرَ بِهَا فَشَكَّتْ عَلَيْهَا ثِيَابُهَا، ثُمَّ أَمَرَ بِهَا فَرُجِمَتْ، ثُمَّ صَلَّى عَلَيْهَا، فَقَالَ عُمَرُ: أَنْصَلِي عَلَيْهَا يَا نَبِيَّ اللَّهِ وَقَدْ زَنْتِ؟ فَقَالَ: "لَقَدْ تَابَتْ تَوْبَةً لَوْ قُسِّمَتْ بَيْنَ سَبْعِينَ مِنْ أَهْلِ الْمَدِينَةِ لَوَسِعَتْهُمْ، وَهَلْ وَجَدْتُ أَفْضَلَ مِنْ أَنْ جَادَتْ بِنَفْسِهَا لِلَّهِ؟". رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: Mwanamke wa kabila la Juhaynah (Al-Ghamidiya) alienda kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiwa na mimba ya zinaa, akamuambia: “Ee Nabiyy wa Allaah! Nimestahiki haddi (adhabu) kwa hivyo nisimamishie.” Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ

(عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuita msimamizi wake akamuambia: “Mfanyie wema, atakapojifungua[9] mlete.” Akafanya hivyo akaja naye, akaamuru, akafungwa kwa nguo zake kisha akaamuru akarajumiwa kisha akamswalia. ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) akamuambia: “Ee Nabiy wa Allaah! Unamswalia na hali amezini?” Akasema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) : “Kwa yakini ametubia tawbah ambayo lau ingaligawanyiwa kwa watu sabini mongoni mwa watu wa Madiynah, ingaliwatosha. Je ushawahi kuona lililo bora kuliko yeye kujileta mwenyewe kwa Allaah?” [Imetolewa na Muslim]

1041.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {رَجَمَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ رَجُلًا مِّنْ أَسْلَمَ، وَرَجُلًا مِّنْ الْيَهُودِ، وَإِمْرَأَةً} رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَقِصَّةُ رَجْمِ الْيَهُودِيِّينَ فِي "الصَّحِيحَيْنِ" مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عُمَرَ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimpiga mawe (Rajm) mtu wa kabila la Aslam, na mtu mwigine wa Kiyahudi na mwanamke.[10] [Imetolewa na Muslim]

Kisa cha Mayahudi wawili kiko katika Swahiyh mbili; Swahiyh Al-Bukhaariy na Swahiyh Muslim kutoka katika Hadiyth ya ‘Ibn Umar

1042.

وَعَنْ سَعِيدِ بْنِ سَعْدِ بْنِ عِبَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَ بَيْنَ أَبْيَاتِنَا رُوَيْجِلٌ ضَعِيفٌ، فَخَبَثَ بِأَمَةٍ مِنْ إِمَائِهِمْ، فَذَكَرَ ذَلِكَ سَعْدٌ لِرَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: "إِضْرِبُوهُ حَدَّه". فَقَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّهُ أَضْعَفُ مِنْ ذَلِكَ، فَقَالَ: "خُذُوا عَتَكَالًا فِيهِ مِائَةُ شِمْرَاخٍ، ثُمَّ إِضْرِبُوهُ بِهِ ضَرْبَةً وَاحِدَةً". فَفَعَلُوا} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَةَ، وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ. لَكِنْ اخْتَلَفَ فِي وَصْلِهِ وَإِرْسَالِهِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) [11] Kutoka kwa Sa'iyd bin Sa'd bin 'Ubaadah[11] amesema kuwa: Katika nyumba zetu kulikuwa na mtu dhaifu akazini na kijakazi miongoni mwa vijakazi vyao. Sa'd akamueleza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) khabari hiyo, akasema Rasuli wa Allaah: "Mmpigeni haddi (adhabu) yake." [12] Maswahaba wakamuambia: "Ee Rasuli wa Allaah! Yeye ni dhaifu mno kuliko hiyo (haddi)." Rasuli akasema: "Chukueni shina la mtende lenye vitawi mia na mumpige nalo mara moja." Maswahaba wakafanya hivyo. [Imetolewa na Ahmad, An-Nasaaiy na Ibn Maajah. Sanad ya wapokezi wake ni Hasan. Hata hivyo wametofautiana kama ni mawsuwl au mursal]

1043.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ وَجَدْتُمُوهُ يَعْمَلُ عَمَلَ قَوْمِ لُوطٍ، فَاقْتُلُوا الْفَاعِلَ وَالْمَفْعُولَ بِهِ، وَمَنْ وَجَدْتُمُوهُ وَقَعَ عَلَى بَهِيمَةٍ،

فَاقْتُلُوهُ وَاقْتُلُوا الْبَهِيمَةَ { رَوَاهُ أَحْمَدُ وَالْأَرْبَعَةُ، وَرِجَالُهُ مُوْتَقُونَ، إِلَّا أَنَّ فِيهِ اخْتِلَافًا

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtakayemkuta akifanya kitendo cha uliwati muuweni mwenye kufanya na kufanyiwa,[13] na mtu akimkuta akimuingilia mnyama basi muuweni yeye na muuweni mnyama.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah). Wapokezi wake ni madhubuti lakini ndani yake kuna ikhtilafu]

1044.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ضَرَبَ وَغَرَّبَ وَأَنَّ أَبَا بَكْرٍ ضَرَبَ وَغَرَّبَ { رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ، إِلَّا أَنَّهُ اخْتَلَفَ فِي رَفْعِهِ، وَوَقْفِهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alichapa mijeledi na akawatoa[14] mjini. Abuu Bakr alichapa na akatoa mjini. [Imetolewa na At-Tirmidhiy na wapokezi wake ni madhubuti, isipokuwa wamekhitilafiana kuwa ni mawquwf au Marfuw’]

1045.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: لَعَنَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ الْمُخَنَّثِينَ مِنَ الرِّجَالِ، وَالْمُتَرَجَّلَاتِ مِنَ النِّسَاءِ، وَقَالَ: {أَخْرِجُوهُمْ مِنْ بُيُوتِكُمْ} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake, na wanawake wanaojifananisha na wanaume.[15] Na akasema: “Watoeni majumbani mwenu.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1046.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {ادْفَعُوا الْحُدُودَ، مَا وَجَدْتُمْ لَهَا مَدْفَعًا} أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَإِسْنَادُهُ ضَعِيفٌ وَأَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالْحَاكِمُ: مِنْ حَدِيثِ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا بِلَفْظٍ {ادْرَأُوا الْحُدُودَ عَنِ الْمُسْلِمِينَ مَا اسْتَطَعْتُمْ} " وَهُوَ ضَعِيفٌ أَيْضًا وَرَوَاهُ الْبَيْهَقِيُّ: عَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ (مِنْ) قَوْلِهِ بِلَفْظٍ: {ادْرَأُوا الْحُدُودَ بِالشُّبُهَاتِ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Zuieni adhabu mnapopata njia ya kuzizuia.” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa isnaad dhaifu]

Na At-Tirmidhiy amepokea na Al-Haakim kutoka katika Hadiyth ya ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) kwa tamshi: “Waepushieni adhabu[16] Waislam kadiri muwezavyo.” [nayo pia ni dhaifu]

Al-Bayhaqiyy amepokea kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwa kauli yake: “Epusheni haddi (adhabu) kwa shubha (utata).”

1047.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {اجْتَنِبُوا هَذِهِ الْقَادُورَاتِ الَّتِي نَهَى اللَّهُ تَعَالَى عَنْهَا، فَمَنْ أَلَمَ بِهَا فَلْيَسْتَتِرْ بِسِتْرِ اللَّهِ تَعَالَى، وَلْيَتُبْ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى، فَإِنَّهُ مَنْ يَبْدِ لَنَا صَفْحَتَهُ نُقِمَ عَلَيْهِ كِتَابَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ} رَوَاهُ الْحَاكِمُ، وَهُوَ فِي "الْمَوْطَأِ" مِنْ مَرَّاسِيلِ زَيْدِ بْنِ أَسْلَمَ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Jiepusheni na machafu haya Aliyokataza Allaah. Atakayetenda basi ajisitiri kwa sitara ya Allaah na atubu kwa Allaah, kwani atakayetudhihirishia hakika yake tutamsimamishia Kitabu Cha Allaah.” [Imetolewa na Al-Haakim, hadiyth hii iko katika kitabu cha Al-Muwatwa ya Imaam Malik kutoka katika Ahaadiyth za Zayd bin Aslama[17]]

[1] Huduwd ni wingi wa Hadd, ambayo ina maana ya ‘Kuzuia’. Ni adhabu ya kishariy’ah kwa wazinifu na mfano wa adhabu hizo huitwa kuwa ni Huduwd kwani zinaonesha adhabu kwa aina za watu waliotajwa. Wakati mwingine neno Hadd hutumika kutaja aina fulani ya tendo la dhambi.

[2] Hadiyth hii inaonesha hukumu ya mtu aliyezini kwa Bikra awe ni mwanamme au mwanamke ni mijeledi mia moja na kuhamishwa kwenye nje ya dola ya Kiislam kwa muda wa mwaka mmoja. Kupigwa mijeledi

mia moja ni kutokana na hukumu ya Qur-aan wakati adhabu kuhamishwa ni ziada inayokubaliwa na wapokezi wote wa Hadiyth. Adhabu ya mzinifu aliyekuishaoa au kuolewa ni Rajm (adhabu ya kupigwa mawe mpaka kufa) hadi kufa kulingana na makubaliano ya ‘Ulamaa. Hii inathibitisha vile vile kuwa kukiri kwa mmoja katika wazinifu kunatosha kusimamisha adhabu.

[3] Hii inakusudia maelezo ya Allaah katika Suwrah Al-Maaidah (5) Aayah 15:

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ كَثِيرًا مِّمَّا كُنْتُمْ تُخْفُونَ مِنَ الْكِتَابِ وَيَعْفُو عَنْ كَثِيرٍ ۖ قَدْ جَاءَكُمْ مِنَ اللَّهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُبِينٌ (١٥)

“Enyi Ahlal-Kitaab! Hakika amekwisha kujieni Rasuli Wetu anayekubainishieni mengi katika yale mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anasamehe mengi. Kwa yakini imekufikieni kutoka kwa Allaah Nuru na Kitabu kinachobainisha”

[4] Hadiyth hii inamaanisha kuwa mzinifu wa kike na mzinifu wa kiume watapigwa mijeledi kisha wapigwe mawe (Rajm) hadi kufa. Hata hivyo, maoni ya ‘Ulamaa wengi ni kuwa suala la kupigwa mijeledi mia moja halina haja bali Rajm itatosheleza. Wamesema kuwa suala hili halina nguvu kwa sababu Nabi hakumpiga Maa’iz na wengine, bali ni kupigwa mawe tu.

[5] Mtu ambaye alitoa uthibitisho huu alikuwa ni Maa’iz Aslami. Hadiyth hii inaelezea kuwa Qadhi ni lazima afanye uchunguzi wa kutosha kabla ya kutoa hukumu yake kuhusu adhabu fulani, kwani huenda maisha ya mtu yakakatishwa kwa hukumu yenye makossa.

[6] Maa’iz ndiye aliyekiri kufanya kosa hili wakati akiwa na mke.

[7] Hadiyth hii imetajwa na Muhadithina wote isipokuwa An-Nasaai, kadhalika imepokewa na Maswahaba wengi wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Iliripotiwa na Ubay bin Ka’ab kuwa Suwrah Ahzaab ilikaribiana na Suwrah Baqarah. Nyingi katika Aayah za Suwrah hizo zilifanywa Nasikh au zilikuwa Mansuwkh. Ubay bin Ka’ab anahadithia: “Tulikuwa tunasoma Aayah hizi katika Suwrah hii hadi tunapofikia katika Aayah:

‘Pindi mwanamme aliyeowa na mwanamke aliyeolewa wanapozini warujumuni’ baadae, usomaji wa Aayah hii ukafutwa lakini hukumu yake ikabaki pale pale, ambayo vile vile ni aina ya naskh.

Hukumu ya uzinifu unahitaji ushahidi ufuatao: (a) mashahidi wane, (b) kukiri kwa mhusika, na (c) mimba. Sharti hili la tatu linawahusu wanawake tu, lakini Imaam Shaafi’iy na Imaam Abuu Haniyfah hawakubaliani nalo. Kwa wanaolikubali kama ni ushahidi, mwanamke ambaye hakuolewa (asiyekuwa mtumwa) ataadhibiwa ikiwa mimba yake itakuwa wazi.

[8] Suala la mamlaka ya mtumwa mwanamke au mwanamme limeachwa kwa anayemiliki. Watu wote walobakia wanahukumiwa na Dola. Ikiwa mtumwa mwanamme alikuwa ameshaoa, hapa kutakuwa na rai tofauti miongoni mwa ‘Ulamaa ya kuwa mamlaka ya kumpa adhabu yatakuwa kwenye Dola au kwa mwenyewe mwenye kummiliki. Ama kijakazi akizini basi atachapwa mijeledi na adhabu ya kumpiga mawe haitotekelezwa kwake. Hata kupigwa kwake mijeledi haitozidi hamsini. Ushahidi wa hili ni Aayah katika Qur-aan inayosema:

فَإِذَا أَحْصَيْنَ فَإِنَّ أَتَيْنَ بِفَاحِشَةٍ فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ مِنَ الْعَذَابِ

Na watakapohifadhiwa katika ndoa, kisha wakafanya uchafu basi adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu ya waliyowekewa wanawake walio huru (wasioolewa).

[An-Nisaa: 4: 25]

[9] Hadiyth hii inabainisha kuwa suala la adhabu la uzinifu halitakiwi kufanyika mapema kwa mwanamke ili iangaliwe kwanza kama ana mimba. Ikiwa kama ana mimba anatakiwa asubiriwe hadi atakapojifungua. Pindi mwanamke atakapojifungua, mwanamke anaweza kupewa adhabu kwa sharti kuwa suala la kumnyonyesha mtoto na kumlea limekadhibiwa mwanamke mwingine. Ikiwa mwanamke huyo hajapatikana suala la adhabu litaakhirishwa hadi mtoto atakapoachishwa ziwa. Hata kama mwanamke huyo hakuwahi kuolewa adhabu itaakhirishwa mpaka atakapojifungua. Katika hali hiyo inatakiwa atendewe wema na jamaa zake na si vizuri kumshutumu na kumtukana ambapo Shariy’ah hairuhusu.

[10] Nabiyy (ﷺ) aliwahukumu watu wane kupigwa Rajm katika wakati wake. Wa kwanza ni lile tukio la mwanamke, wa pili alikuwa mtu wa kabila la Banu Aslam (Maa’iz bin Maalik) na Mayahudi wawili (mwanamke na mwanamme). Hili linamaanisha kuwa hukumu za

Shariy'ah zinahusika pia kwa makafiri kama zinavyotekelezwa kwa Waislam.

[11] Sa'iyd bin Sa'd bin 'Ubaadah Al Answaar As-Sa'iyd alikuwa ni Swahaba. Inasemekana kwa wengine alikuwa ni Taabi'i, alikuwa ni madhubuti aliyepokea baadhi za Ahaadiyth. Alikuwa gavana wa Yemen wakati wa Ukhalifa wa 'Aliy bin Abi Twaalib.

[12] Hadiyth hii inaelezea ikiwa mtu ambaye hajaoa akazini, lakini kulingana na hali yake ya udhaifu au maradhi, na pindi itakaposimamishwa adhabu kwake anaweza kufa kama atapigwa mijeledi mia moja, inatakiwa upole katika kutekeleza adhabu yenyewe. Idadi ya mijeledi mia moja haitopunguzwa, bali huenda fimbo ya kupigia ikawa ni ndogo zaidi. Hata hivyo kunaweza kuwa na tofauti ya kupiga na isiwe kwa nguvu zaidi kama katika hali ya kawaida.

[13] Kuna rai tofauti kwa 'Ulamaa kuhusu adhabu ya liwati kwa mwanamme kumfanyia mwanamke, pamoja na kuwa hakuna Hadiyth maalum inayoainisha hilo zaidi ya adhabu ya kifo. Hii ina maana tofauti iliyopo ni jinsi ya kutekeleza adhabu yenyewe tu. Baadhi wanaona kuwa adhabu ni Rajm (kupigwa kwa mawe). Wengine wanaona kuwa watupwe kutoka umbali wa juu na kurushwa chini. Kundi lingine linaona kuwa wawashiwe moto. Rai nyingine inaona kuwa hukumu ya mzinifu ipite kwake; Kama ameo aarajimiwe; vinginevyo, apigwe mijeledi mia moja na atolewe nje ya mji. Allaah ndiye Mjuzi.

[14] Baadhi ya 'Ulamaa wana muono kuwa adhabu ya kuhamishwa mji imefutwa na haifanyi kazi tena. Hadiyth hii inapinga ile rai ya kuwa ikiwa wazinifu walihamishwa miji wakati wa Makhalifa waongofu, dalili ipi inayoonesha kuwa hukumu hii imefutwa?

[15] Hadiyth hii inathibitisha kuwa mwanamke au mwanamme ambaye anaiga tabia ya jinsia ya pili ni watu wenye kulaaniwa na jambo hili ni katika madhambi. Matowashi wapo wa aina mbili: ni wale matowashi ambao maumbile yao ya kiwiliwili yanafanana na wanawake na wakati wengine wanafanana na wanaume. Matowashi lazima wavae nguo zinazofanana na jinsia yao na kufanana nao zaidi.

[16] Ikiwa kuna shaka kuhusu ukweli fulani wa ushahidi unaopelekea katika hukumu ya adhabu, hukumu ile inabidi itenguliwe. Hadiyth hii haikusudii kuwa hakuna hukumu itakayotolewa, bali inamaanisha kuwa hukumu ya adhabu haitopitishwa hadi tatizo liwe la wazi uwazi usio na shaka. Watu wanashauriwa kuwa wasipeleke kesi yoyote mahakamani hadi wajenge ushahidi wa kutosha unaowaunga katika madai yao ili kuthibitisha kuwa fulani ni mwenye kosa.

[17] Alikuwa ni Swahaba kutoka kabila la Al-Balawi. Alikuwa katika ukoo wa Banuu Al-‘Ajlan, washirika wa Banuu ‘Amr bin ‘Awf katika Al-Answaar. Alishuhudia Badr na kadhalika Swiffiyn akiwa pamoja na ‘Aliy. Hata hivyo, Hishaam Al-Kalabi amesema, (Zaid) aliuwawa na Twulayha bin Khuwaylid Al-Asad katika siku ya Bazakha katika mwaka wa 11 Hijriyyah mwanzoni mwa Ukhalifa wa Abuu Bakr.

02-Mlango Wa Adhabu Ya Kusingizia

بَابُ حَدِّ الْقَذْفِ

02-Mlango Wa Adhabu Ya Kusingizia

1048.

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {لَمَّا نَزَلَ عُذْرِي، قَامَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَلَى الْمِنْبَرِ، فَذَكَرَ

ذَلِكَ وَتَلَا الْقُرْآنَ، فَلَمَّا نَزَلَ أَمَرَ بِرَجُلَيْنِ وَإِمْرَأَةٍ فَضْرَبُوا
الْحَدَّ { أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ وَالْأَرْبَعَةُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: Udhuru wangu ulipoteremka (kutoka mbinguni)[1] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisimama juu ya mimbari akaeleza hilo akasoma Qur-aan, alipoteremka aliamuru wanaume wawili na mwanamke mmoja[2] wapigwe haddi (adhabu).[3] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah)]

1049.

وَعَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَوَّلَ لِعَانٍ كَانَ فِي الْإِسْلَامِ أَنَّ شَرِيكَ بْنَ سَمْحَاءٍ قَذَفَهُ هِلَالُ بْنُ أُمَيَّةَ بِأَمْرَاتِهِ، فَقَالَ لَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "الْبَيِّنَةُ وَالْأَفْحَدُّ فِي ظَهْرِكَ" { الْحَدِيثُ أَخْرَجَهُ أَبُو يَعْلَى، وَرَجَالُهُ ثِقَاتٌ

وَهُوَ فِي الْبُخَارِيِّ نَحْوُهُ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عَبَّاسٍ

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: Kulaaniana kwa kwanza katika Uislam ni Hilaal bin Umayyah[4] alipomsingizia mke wake kuzini na Shariyka bin Samhaa,[5] Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Leta ushahidi vinginevyo utapigwa mijeledi mgongoni mwako...”[6] mpaka mwisho wa Hadiyth [Imetolewa na Abuu Ya’laa na wapokezi wake ni madhubuti, na katika Al-Bukhaariy kuna Hadiyth kama hii kutoka kwa Ibn ‘Abbaas]

1050.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَامِرٍ بْنِ رَبِيعَةَ قَالَ: {لَقَدْ أَدْرَكْتُ أَبَا بَكْرٍ، وَعُمَرَ، وَعُثْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ، وَمِنْ بَعْدَهُمْ، فَلَمْ أَرَهُمْ يَضْرِبُونَ الْمَمْلُوكَ فِي الْقَذْفِ إِلَّا أَرْبَعِينَ} رَوَاهُ مَالِكٌ، وَالثَّوْرِيُّ فِي "جَامِعِهِ"

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Aamir bin Rabiyy’ah amesema: Nilimkuta Abuu Bakr, ‘Umar na ‘Uthmaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ) na waliokuja baada yao sikuwaona wakimpiga mtumwa katika adhabu ya kusingizia uzinifu isipokuwa mijeledi arubaini tu.[7] [Imetolewa na Maalik na Ath-Thawriy katika kitabu chake cha Al-Jaami’i]

1051.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {مَنْ قَذَفَ مَمْلُوكَهُ يُقَامُ عَلَيْهِ الْحَدُّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، إِلَّا أَنْ يَكُونَ كَمَا قَالَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakaemsingizia (uzinifu) mtumwa wake atasimamishiwa haddi Siku Ya Qiyaamah[8] isipokuwa iwe ni kama alivyosema.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

[1] Soma Suwrah An-Nuwr Aayah ya 11 (na zinazofuatia)

إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنْكُمْ ۚ لَا تَحْسَبُوهُ شَرًّا لَّكُم بَلْ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۚ
لِكُلِّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ مَا اكْتَسَبَ مِنَ الْإِثْمِ ۚ وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ لَهُ عَذَابٌ
عَظِيمٌ (١١)

“Hakika wale walioleta singizo la kashfa; (kumzulia mama wa waumini ‘Aaishah رضي الله عنها) ni kundi miongoni mwenu. Msiichukulie kuwa ni shari kwenu, bali ni khayr kwenu. Kila mtu katika wao atapata yale aliyochuma katika dhambi. Na yule aliyejitwika sehemu yake kubwa miongoni mwao atapata adhabu kuu.”

[2] Mwanamme anayetajwa hapa ni Mistwah bin Uthaathah na Hassan bin Thaabit na mwanamke aliyekuwa akiitwa Hamna bin Jahsh.

[3] Ikiwa mtu kamtuhumu mtu kwa uzinifu na akashindwa kuthibitisha, itabidi alete mashahidi wane, adhabu yake itakuwa mijeledi themanini. Baadhi ya wanafiki walimsingizia Mama ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) kwa uzinifu. Walitangaza na jambo hilo likawaathiri watu wengi na minong’ono ikawa mingi kuhusu jambo hilo. Pindi ‘Aaishah alipokoshwa na Aayah za Allaah, Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitangaza adhabu kali kwa Waumini lakini hakusema chochote kuhusu wanafiki, kwani aliacha adhabu yao wapewe na Allaah. Waumini watatu walioadhibiwa kwa kusingizia huku walikuwa ni Hassan bin Thaabit, Mistwah bin Uthaathah na Hamna bint Jahsh (Radhwiya-Allaahu ‘anhum).

[4] Alikuwa katika Al-Answaar, Aws na Waqifi alikuwa Swahaba mashuhuri. Alisilimu mapema na alikuwa na tabia ya kuyavunja masanamu ya Baniy Waqifu. Alishuhudia vita vya Badr, Uhud na alibeba bendera ya Banu Waqifu katika siku ya Fat-hu Makkah. Alikuwa mmoja kati ya watatu walioshindwa kuhudhuria vita vya Tabuwk ambae altengwa kwa muda wa siku hamsini na baadae walisamehewa na Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

[5] Alikuwa katika kabila la Balawi waliokuwa na ushirika na Answaar. Hilaal bin Umayyah alimtuhumu kuzini na mke wake. Inasemekana kuwa alishiriki katika vita va Uhud na baba yake. Alikuwa na udugu upande wa

mama ni pamoja na Baraa bin Maalik, jina la baba yake ni ‘Abaadah bin Mu’tib na As-Sahma lilikuwa ni jina la mama yake.

[6] Ikiwa mtu atamtuhumu mke wake kuzini ni lazima athibitishe kwa ushahidi, vinginevyo au apate laana ya Allaah kwake kwa kumsingizia mke wake. Vinginevyo ataadhibiwa kwa kusingizia. Akimtaja mtu kama ndio mshirika wake katika jinai ile, anatakiwa atoe ushahidi hadi mwisho wake. Kwa kuwa ni mke wake anaweza kukwepa adhabu ya mijeledi lakini hatokwepa laana ya Allaah kwake (ikiwa atakuwa amemsingizia). Nini hali ya mtu aliyetuhumiwa kuwa mshirika wa jinai hii? Hana uchaguzi isipokuwa: (a) Atoe ushahidi kuunga madai yake, au (b) awe tayari kukabiliana na adhabu ya kusingizia.

[7] Hii inathibitisha kuwa adhabu anayopewa mtumwa mwanamme au mwanamke ni nusu ya adhabu apewayo mtu aliyekuwa huru, na hii ni kwa mujibu wa Jamhuri ya ‘Ulamaa.

[8] Hii ina maana kama mtu atamsingizia mtumwa au kijakazi wake kwa uzinifu hatoadhibiwa hapa duniani.

03-Mlango Wa Adhabu Ya Kuiba

بَابُ حَدِّ السَّرِقَةِ

03-Mlango Wa Adhabu Ya Kuiba

عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ: { لَا تُقْطَعُ يَدُ سَارِقٍ إِلَّا فِي رُبْعِ دِينَارٍ فَصَاعِدًا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ. وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ . وَلَفْظُ الْبُخَارِيِّ: "تُقْطَعُ الْيَدُ فِي رُبْعِ دِينَارٍ فَصَاعِدًا "

وَفِي رِوَايَةٍ لِأَحْمَدَ "اقْطَعُوا فِي رُبْعِ دِينَارٍ، وَلَا تَقْطَعُوا فِيمَا هُوَ أَدْنَى مِنْ ذَلِكَ"

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mkono wa mwizi haukatwi ila kwa robo dinari na zaidi.”[1] [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Na Matini ya Bukhaariy inasema: “Mkono wa mwizi unakatwa kwa robo dinari na zaidi.”

Na katika riwaayah nyingine ya Ahmad: “Kateni (mkono) katika robo dinari wala msikate chini ya hiyo.”

1053.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا: { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَطَعَ فِي مَجَنٍّ، ثَمَنُهُ ثَلَاثَةُ دَرَاهِمٍ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikata (mkono) katika (kuiba) ngao thamani yake ni dirhamu tatu.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1054.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ {لَعَنَ اللَّهُ السَّارِقَ ؛ يَسْرِقُ الْبَيْضَةَ ، فَتُقَطَّعُ يَدُهُ ، وَيَسْرِقُ الْحَبْلَ ، فَتُقَطَّعُ يَدُهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ أَيْضًا

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah Amlaani mwizi! Anaiba yai mkono wake ukakatwa, na anaiba kamba mkono wake ukakatwa.”[2] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1055.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا ؛ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَتَشْفَعُ فِي حَدِّ مِنْ حُدُودِ اللَّهِ؟} ثُمَّ قَامَ فَاخْتَطَبَ ، فَقَالَ : " أَيُّهَا النَّاسُ ! إِنَّمَا هَلَكَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ أَنَّهُمْ كَانُوا إِذَا سَرَقَ فِيهِمُ الشَّرِيفُ تَرَكَوهُ ، وَإِذَا سَرَقَ فِيهِمُ الضَّعِيفُ أَقَامُوا عَلَيْهِ الْحَدَّ . . . } الْحَدِيثُ . مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ وَلَهُ مِنْ وَجْهِ آخَرَ : عَنْ عَائِشَةَ : كَانَتْ امْرَأَةً تَسْتَعِيرُ الْمَتَاعَ ، وَتَجَحِّدُهُ ، فَأَمَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بِقَطْعِ يَدِهَا

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema (kwa Usaamah Bin Zayd): “Unaomba[3] katika haddi (adhabu) miongoni mwa haddi za Allaah? Halafu akasimama kuwakhutubia watu: ‘Enyi watu! Kwa yakini waliangamia waliokuwa kabla yenu, kwani anapoiba mtukufu

wao wanamuacha, na akiiba mnyonge wanamsimamishia haddi.”[4]
[Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Naye Muslim amepokea kwa njia nyingine kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا): “Mwanamke alikuwa akiazima vyombo na anakanusha, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaamuru akatwe mkono.”

1056.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَيْسَ عَلَى خَائِنٍ وَلَا مُنْتَهَبٍ ، وَلَا مُخْتَلِسٍ ، قَطْعٌ} رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَالْأَرْبَعَةُ ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Jabair (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kufanya khiyana, mwenye kudokoa na mwenye kunyang’anya, hawakatwi mkono.”[5] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

1057.

وَعَنْ رَافِعِ بْنِ خَدِيجٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ ، قَالَ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {لَا قَطْعَ فِي ثَمَرٍ وَلَا

كثُرَ { رَوَاهُ الْمَذْكُورُونَ، وَصَحَّحَهُ أَيْضًا التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Raafi' bin Khadiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa amemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Hakuna kukata mkono kwa aliyechukua matunda wala joyo la mtende.”[6] [Imetolewa na hao waliotajwa, vile vile At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan wameisahihisha]

1058.

وَعَنْ أَبِي أُمَيَّةَ الْمَخْزُومِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { أَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ بِلِصٍّ قَدْ اعْتَرَفَ اعْتِرَافًا، وَلَمْ يُوَجِدْ مَعَهُ مَتَاعٌ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ "مَا إِخَالِكَ سَرَقْتَ". قَالَ: بَلَى، فَأَعَادَ عَلَيْهِ مَرَّتَيْنِ أَوْ ثَلَاثًا، فَأَمَرَ بِهِ فَقُطِعَ. وَجِيءَ بِهِ، فَقَالَ: "اسْتَغْفِرُ اللَّهَ وَتُبْ إِلَيْهِ"، فَقَالَ: أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ، فَقَالَ: "اللَّهُمَّ تُبْ عَلَيْهِ" ثَلَاثًا { أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَأَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ وَأَخْرَجَهُ الْحَاكِمُ مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ، فَسَاقَهُ بِمَعْنَاهُ، وَقَالَ فِيهِ: { اذْهَبُوا بِهِ، فَاقْطَعُوهُ، ثُمَّ احْسِمُوهُ } . وَأَخْرَجَهُ الْبَزَّازُ أَيْضًا، وَقَالَ: لَا بَأْسَ بِإِسْنَادِهِ

Kutoka kwa Abiy Umayyah Al-Makhzuwmiy[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliletewa mwizi aliyeungama kuwa aliiba lakini hakuwa na alichocha, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: ‘Sidhani kama

umeiba' yule mtu akasema: 'Nimeiba,[8] akarudia kusema hivyo mara mbili au mara tatu. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaamrisha akatwe mkono kisha akaletwa, akamuambia: 'Omba msamaha kwa Allaah na utubie Kwake' yule mtu akasema: 'Naomba msamaha kwa Allaah na natubia Kwake' Rasuli wa Allaah akasema: 'Ee Allaah! Mkubalie tawbah yake' alisema hivyo mara tatu." [Imetolewa na Abuu Daawud, na matini ya hadiyth ni yake, vile vile imepokewa na Ahmad na An-Nasaaiy na wapokezi wake ni madhubuti]

Pia Al-Haakim ameipokea kutoka katika hadiyth ya Abuu Hurayrah akayieleza ki maana, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaambia: "Mchukueni mumkate kisha mumpisheni." Vile vile Al-Bazaar ameipokea na amesema: Isnaad yake haina ubaya.

1059.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَوْفٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ؛ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { لَا يَغْرَمُ السَّارِقُ إِذَا أُقِيمَ عَلَيْهِ الْحَدُّ } رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَبَيَّنَّ أَنَّهُ مُنْقَطِعٌ. وَقَالَ أَبُو حَاتِمٍ: هُوَ مُنْكَرٌ

Kutoka kwa 'Abd Ar-Rahmaan bin 'Awf (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Mwizi harudishi alichokiiba atakaposimamishiwa[9] haddi." [Imetolewa na An-Nasaaiy na ameeleza kuwa Hadiyth hii ni Munqatwi'. Na amesema Abuu Haatim: "Hadiyth hii ni Munkar."]

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو بْنِ الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ؛ { أَنَّهُ سُئِلَ عَنِ الثَّمْرِ الْمُعَلَّقِ؟ فَقَالَ: "مَنْ أَصَابَ بِفِيهِ مِنْ ذِي حَاجَةٍ، غَيْرَ مُتَّخِذٍ خُبْنَةً، فَلَا شَيْءَ عَلَيْهِ، وَمَنْ خَرَجَ بِشَيْءٍ مِنْهُ، فَعَلَيْهِ الْغَرَامَةُ وَالْعُقُوبَةُ، وَمَنْ خَرَجَ بِشَيْءٍ مِنْهُ بَعْدَ أَنْ يُؤْوِيَهُ الْجَرِينُ، فَبَلَغَ ثَمَنَ الْمَجَنِّ فَعَلَيْهِ الْقَطْعُ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr bin Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa kuhusu tende zilizotundikwa, akasema: “Mwenye haja akila kiasi cha haja bila ya kuchukua hana lawama. Na mwenye kutoka na kitu basi atapata kulipa na kuadhibiwa. Na mwenye kuchukua sehemu (katika hiyo tende) baada ya kuingizwa sehemu inayokaushiwa na ikafikia thamani ya tende zinazotiwa sehemu hiyo, basi atakatwa (mkono).” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na An-Nasaa'iy na akaisahihisha Al-Haakim]

وَعَنْ صَفْوَانَ بْنِ أُمَيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ لَهُ لَمَّا أَمَرَ بِقَطْعِ الَّذِي سَرَقَ رِدَاءَهُ، فَشَفَعَ فِيهِ: { هَلَّا كَانَ ذَلِكَ قَبْلَ أَنْ تَأْتِيَنِي بِهِ } أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ. وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْجَارُودِ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Swafwaan bin Ummyyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipoamrisha kukatwa mkono wa aliyeiba shuka yake (Safwaan). Safwaan alimuomba yule mwizi asikatwe. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: ‘Ungalifanya hivyo kabla ya kumleta kwangu).’ [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha Ibn Al-Jaarud na Al-Haakim]

1062.

وَعَنْ جَابِرٍ قَالَ: جِيءَ بِسَارِقٍ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: {“أَقْتُلُوهُ”. فَقَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنَّمَا سَرَقَ. قَالَ: “اقْطَعُوهُ” فَقَطَعَ، ثُمَّ جِيءَ بِهِ الثَّانِيَةَ، فَقَالَ “أَقْتُلُوهُ” فَذَكَرَ مِثْلَهُ، ثُمَّ جِيءَ بِهِ الرَّابِعَةَ كَذَلِكَ، ثُمَّ جِيءَ بِهِ الْخَامِسَةَ فَقَالَ: “أَقْتُلُوهُ” { أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَاسْتَنْكَرَهُ وَأَخْرَجَ مِنْ حَدِيثِ الْحَارِثِ بْنِ حَاطِبٍ نَحْوَهُ. وَذَكَرَ الشَّافِعِيُّ أَنَّ الْقَتْلَ فِي الْخَامِسَةِ مَنْسُوخٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliletewa mwizi akasema: ‘Muuweni’. Maswahaba wakasema: Ee Rasuli wa Allaah! Ameiba. Akasema: ‘Mkatani (mkono)’ akakatwa mkono, kisha akaletwa mara ya pili akasema: ‘Muuweni’. Akataja mfano wake. Kisha akaletwa mara ya tatu. Akaeleza kama alivyotangulia. Kisha akaletwa mara ya nne. Akataja mfano wake. Alipoletwa mara ya tano, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: ‘Muuweni’.”[10]

[Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na amesema ni Munkar]

An-Nasaaiy alipokea mfano wake kutoka kwa Al-Haarith bin Haatwib.[11] Ash-Shaafi'iy amesema kuwa kuuwawa kwa mara ya tano kumefutwa (mansuwkh)

[1] Kuna rai tofauti miongoni mwa ‘Ulamaa kuhusu kiasi cha thamani ya kitu kilichoibiwa ili mkono wa mwizi ukatwe. Tukisoma Ahaadiyth mbali mbali na maelezo ya ‘Ulamaa mbali mbali kinathibitisha kuwa wizi wa bidhaa zenye thamani chini ya moja ya nne ya dinari (ambayo ni sawa na dirhamu 3 wakati wa Maswahaba wa Nabiy) haihalalishi mkono wa mwizi ule kukatwa. Robo dinari ni chini ya gramu moja na nusu ya dhahabu.

[2] Hadiyth ikamalizikia: “Ikateremka Aayah:

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا أُولَٰئِكَ لَا خَلَاقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ (٧٧)

“Hakika wale wanaobadilisha ahadi ya Allaah na viapo vyao kwa thamani ndogo; hao hawana sehemu yoyote katika Aakhirah na wala Allaah Hatowasemesha na wala Hatowatazama Siku Ya Qiyaamah na wala Hatowatakasa na watapata adhabu iumizayo” [Aal-‘Imraan: 77]

[3] Tukio hili lilitokea kwa bibi mmoja aitwae Faatwimah bint Aswad Makhzuwmiyah, ambae ni mwanamama kutoka katika familia kubwa inayoheshimika aliyeiba. Ilipotajwa hukumu ya kumkata mkono, watu wakaanza kutafuta wa kumuombea msamaha. Usaamah alionekana wa kutumika kumuombea. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitoa khutbah kali ambayo baadhi yake ipo katika hadiyth hii. Kishariy’ah mtu aliyeibiwa ana haki ya kumsamehe mwizi wake kabla ya jambo lile kupelekwa mahakamani. Hata hivyo kesi ikishapelekwa mahakamani hakuna njia ya kumsamehe tena mhusika. Mkono wake ni lazima ukatwe, na kumuombea kwa wakati huu haina maana kwani hairuhusiwi.

[4] Yaani wote watakuwa ni wamiliki wa mnyama huyo.

[5] Wizi wa kutumia silaha, ubadhirifu wa mali na udanganyifu haviingii katika adhabu ya kukata mkono. Udanganyifu unakusudia mtu aliyepatiwa amana kwa kuilinda anaitumia na kuondoka na mali ile huku akionesha sura nyingine. Ama wizi kwa njia ya ujambazi ni kuchukua mali ya mtu kwa nguvu na kwa uwazi kabisa. Ubadhirifu ni kutumia mali ya mtu mwingine vibaya kwa kutokuwepo kwake. Hata hivyo, ikiwa mtu ataazima kitu kwa mtu na mwisho akakana kuwa hajaazima, mtu huyu atachukuliwa kama ni mwizi na atakatwa mkono.

[6] Kuiba matunda hailazimishi mtu kukatwa mkono maadamu katika shamba lile hakukuwa na ukuta uliozungushiwa. Likiwa shamba au bustani lenyewe lina ukuta uliozungushwa basi atawajibika na adhabu ile. Hivyo, msafiri ambae ameshaanza kupewa chakula na watu wa mji anaruhusiwa kula katika bustani iliyo na matunda pembezoni mwa ukuta.

[7] Ni Swahaba kutoka Al-Hijaaz ambae amepokea Hadiyth moja tu. Hammaad bin Salamah anamuelezea: “Alikuwa ni katika ukoo wa Al-Makhzuwm” wakati wa Humam bin Yahya amesema: ‘Alikuwa ni Answaar’

[8] Hadiyth hii inaelezea mambo mawili yaliyozingatiwa katika kutoa hukumu ya adhabu ya mwizi. Kwanza mali ya wizi ikombolewe kutoka kwake, au mwenyewe kukiri kuhusu hilo, siyo lazima kukiri mara mbili, mara moja inatosha kumuingiza hatiani na hukumu kutekelezwa kwake. Kuna tofauti ya rai ikiwa ushahidi unahitajika katika suala la wizi unapotokea. Kwa maneno mengine ni kuwa ikiwa mtuhumiwa hajakiri kuiba na hakuna kidhibiti kilichopatikana kwake na mashahidi wakapatikana kuwa ndie aliyeiba. Hukumu ya kesi kama hiyo siyo katika makubaliano ya ‘Ulamaa. Baada ya mkono kukatwa mafuta ya moto humwagwa ili kuzuia kutoka kwa damu. Ikiwa katika hali kama hii damu ikaendelea kumiminika na mtu akafa, kwa ajili hiyo ni jukumu la Hazina ya dola (Baytul-Maal) kulipa fidia kwa warithi wa aliyefariki.

[9] Ikiwa vitu vilivyoibwa vitapatikana kwa mwizi, vitarejeshwa kwa mwenyewe na mkono wa mwizi utakatwa kwa makubaliano ya ‘Ulamaa. Katika hali ya vitu vilivyoibwa kuharibika, hapa kuna tofauti ya rai kwa ‘Ulamaa kama alipe faini au laa.

[10] ‘Ulamaa wengi wanaona kuwa njia iliyoelezwa ya kumkata mwizi mkono na mguu ni kuwa kwa mara ya kwanza akiiba atakatwa kiganja cha mkono wa kuume. Kwa mara ya pili atakatwa fundo la mguu wa kushoto,

mara ya tatu kiganja cha mkono wa kushoto na mara ya nne ni kifundo cha mguu wa kushoto.

[11] Huyu alikuwa Jumahi, Mqurayshi aliyezaliwa Ethiopia. Alikuwa gavana wa Makkah mwaka wa 66 Hijriyyah wakati wa ‘Abdullaah bin Az-Zubayr. Alimtumikia kwa muda wa miaka 6 na baada ya hapo akawa msimamizi wa Al-Masai wakati wa Marwaan alipokuwa gavana wa Madiynah wakati wa Mu’aawiyah.

04-Mlango Wa Adhabu Ya Mnywaji Pombe Na Kubainisha Kileo (Ni Nini)

بَابُ حَدِّ الشَّارِبِ وَبَيَانِ الْمُسْكِرِ

04-Mlango Wa Adhabu Ya Mnywaji Pombe Na Kubainisha Kileo (Ni Nini)

1063.

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَتَى بِرَجُلٍ قَدْ شَرِبَ الْخَمْرَ، فَجَلَدَهُ بِجَرِيدَتَيْنِ نَحْوَ أَرْبَعِينَ. قَالَ: وَفَعَلَهُ أَبُو بَكْرٍ، فَلَمَّا كَانَ عُمَرُ اسْتَشَارَ النَّاسَ، فَقَالَ عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ عَوْفٍ: أَخَفَّ الْحُدُودِ ثَمَانُونَ، فَأَمَرَ بِهِ عُمَرُ { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِمُسْلِمٍ: عَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي قِصَّةِ الْوَلِيدِ بْنِ عَقْبَةَ
 {جَلَدَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَرْبَعِينَ، وَأَبُو بَكْرٍ
 أَرْبَعِينَ، وَعُمَرُ ثَمَانِينَ، وَكُلُّ سُنَّةٍ، وَهَذَا أَحَبُّ إِلَيَّ}
 وَفِي هَذَا الْحَدِيثِ: {أَنَّ رَجُلًا شَهِدَ عَلَيْهِ أَنَّهُ رَأَاهُ يَتَقَيَّ
 الْخَمْرَ، فَقَالَ عُثْمَانُ: إِنَّهُ لَمْ يَتَقَيَّهَا حَتَّى شَرِبَهَا}

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa:
 (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) “Mtu mmoja aliletwa kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
 akiwa amekunywa khamr[1] (pombe), akamtandika kwa matawi
 mawili ya mtende mara arubaini hivi. Na Abuu Bakr naye alifanya
 hivyo. Ulipokuwa wakati wa ‘Umar aliwashauri watu. ‘Abdur-
 Rahmaan bin ‘Awf amesema: ‘Adhabu hafifu zaidi ni mijeledi
 themanini.’ ‘Umar akaamuru iwe hivyo.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Katika Riwaayah ya Muslim kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
 katika kisa cha Al-Waliyd bin ‘Uqbah[2]: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
 alipiga mijeledi arubaini, Abuu Bakr alipiga mijeledi
 arubaini, ‘Umar alipiga mijeledi thamanini. Yote hayo ni Sunnah na
 hii yapendeza mno kwangu.”

Na katika hadiyth hii: “Mtu mmoja alimshuhudia (Al-Waliyd)
 akitapika pombe. ‘Uthmaan akasema: ‘Yeye hakutapika pombe ila
 baada ya kuwa amekunywa.’

1064.

وَعَنْ مُعَاوِيَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
 وَآلِهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ قَالَ فِي شَارِبِ الْخَمْرِ: {إِذَا شَرِبَ فَاجْلِدُوهُ،
 ثُمَّ إِذَا شَرِبَ الثَّانِيَةَ فَاجْلِدُوهُ، ثُمَّ إِذَا شَرِبَ الثَّلَاثَةَ فَاجْلِدُوهُ، ثُمَّ

إِذَا شَرِبَ الرَّابِعَةَ فَاضْرِبُوا عُنُقَهُ { أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ وَهَذَا لَفْظُهُ،
وَالْأَرْبَعَةُ

وَذَكَرَ التِّرْمِذِيُّ مَا يَدُلُّ عَلَى أَنَّهُ مَنسُوخٌ، وَأَخْرَجَ ذَلِكَ أَبُو
دَاوُدَ صَرِيحًا عَنْ الزُّهْرِيِّ

Kutoka kwa Mu'aawiyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisema kuhusu mnywaji pombe:
“Atakapokunywa (mara ya kwanza) mtandikeni, kisha
atakapokunywa mara ya pili mtandikeni, kisha atakapokunywa mara ya
tatu mtandikeni, kisha atakapokunywa mara ya nne mkateni shingo
yake.” [Imetolewa na Ahmad, matini hii ni ya Maimaam wane (At-
Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah). At-Tirmidhiy
amesema kuwa ni mansuwkh.[3] Abuu Daawuud pia amepokea kwa
uwazi kutoka kwa Az-Zuhriyy]

1065.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { " إِذَا ضَرَبَ أَحَدُكُمْ فَلْيَتَّقِ
الْوَجْهَ " } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakapopiga
mmoja wenu aepuke kupiga uso.”[4] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1066.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { لَا تُقَامُ الْحُدُودُ فِي الْمَسَاجِدِ }
رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haddi (adhabu) hazitekelezwi ndani ya Msikiti.”[5] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na Al-Haakim]

1067.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { لَقَدْ أَنْزَلَ اللَّهُ تَحْرِيمَ الْخَمْرِ، وَمَا بِالْمَدِينَةِ شَرَابٌ يَشْرَبُ إِلَّا مِنْ تَمْرٍ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Allaah Ameteremsha kuharamisha pombe na Madiynah hakuna pombe inayonywewa ila pombe ya tende.” [Imetolewa na Muslim]

1068.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { نَزَلَ تَحْرِيمُ الْخَمْرِ، وَهِيَ مِنْ خَمْسَةِ: مِنَ الْعِنَبِ، وَالتَّمْرِ، وَالْعَسَلِ، وَالْحِنْطَةِ، وَالشَّعِيرِ. وَالْخَمْرُ: مَا خَامَرَ الْعَقْلَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Imeteremka amri ya kuharamisha pombe, inayotokana na vitu vitano: Zabibu, tende,

asali, ngano na shayiri.[6] Pombe ni kila kinachofunika akili.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1069.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "كُلُّ مُسْكِرٍ خَمْرٌ، وَكُلُّ مُسْكِرٍ حَرَامٌ" } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ.

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kila kileo ni pombe na kila kileo ni haraam.” [Imetolewa na Muslim]

1070.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "مَا أَسْكَرَ كَثِيرُهُ، فَقَلِيلُهُ حَرَامٌ" } أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Chochote kinacholeweshwa kwa wingi, uchache wake[7] ni haraam.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1071.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يُنْبِذُ لَهُ الزَّبِيبُ فِي السَّقَاءِ، فَيَشْرِبُهُ يَوْمَهُ، وَالْغَدَ، وَبَعْدَ الْغَدِ، فَإِذَا كَانَ مَسَاءَ الثَّلَاثَةِ شَرِبَهُ وَسَقَاهُ، فَإِنْ فَضَلَ شَيْءٌ أَهْرَاقَهُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akitengenezewa kinywaji cha (kurowekwa) zabibu na akitiliwa katika chombo akinywa siku ile, siku inayofwatia na siku baada yake. Inapofika jioni ya siku ya tatu alikuwa akinywa na akimpa mtu mwingine anywe kinapobakia kitu anamwaga.”[8] [Imetolewa na Muslim]

1072.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "إِنَّ اللَّهَ لَمْ يَجْعَلْ شِفَاءَكُمْ فِيمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمْ" } أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Allaah Hakujaalia ponyo lenu katika Alivyoharamisha.”[9] [Imetolewa na Al-Bayhaqiyy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1073.

وَعَنْ وَائِلِ الْحَضْرَمِيِّ، أَنَّ طَارِقَ بْنَ سُوَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {سَأَلَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ عَنْ الْخَمْرِ يَصْنَعُهَا لِلدَّوَاءِ؟ فَقَالَ: " إِنَّهَا لَيْسَتْ بِدَوَاءٍ، وَلَكِنَّهَا دَاءٌ" } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ. وَأَبُو دَاوُدَ وَغَيْرُهُمْ

Kutoka kwa Waa-il Al-Hadhwramiyy amesema kuwa Twaariqa bin Suwayd[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا): Alimuuliza Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuhusu pombe inayotengenezwa kwa ajili ya dawa? Akasema: “Hiyo (pombe) sio dawa lakini ni ugonjwa.” [Imetolewa na Muslim na Abuu Daawuwd na wengineo]

[1] Khamr kwa Kiarabu maana yake ni kuficha, kufinika. Mtu anapolewa kile kilevi hufunika akili yake na hii ndio maana ya Khamr. Katika istwilaah ya Shariy’ah kila kilevi ni haraam. Na kila kinachopelekea katika kilevi ni haraam. Kuna makubaliano ya ‘Ulamaa kwa athari ya kilevi na adhabu ya mtu anayopewa. Hata hivyo, kuna rai tofauti kwa mnywaji pombe. Wakati wa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na Abuu Bakr, adhabu kwa mnywaji pombe ilikuwa ni mijeledi arubaini. ‘Umar aliongeza kufikia themanini na ndio uliyokuwa msimamo uliokuja chukuliwa. Kwa hivyo basi baadhi ya Maimaam wametoa hukumu zao adhabu ya mijeledi themanini. Kwa kuwa adhabu ya mijeledi themanini haikuwepo wakati wa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), baadhi ya ‘Ulamaa wanaona kuwa adhabu ni mijeledi arubaini tu. Nukta nyingine ya tafaruku baina ya ‘Ulamaa kulingana na adhabu ni je, suala la adhabu ni lazima kutumia mijeledi au kopo au kiatu kinatosheleza. Kulingana na muono wa ‘Ulamaa wengi, ni sawa kutumia chombo chochote (mjeledi, kiatu, kopo na kadhalika) wakati wa kumuadhibu mtu mwenyewe.

[2] Al-Waliyd bin ‘Uqbah bin Abiy Mu’ait Al-Qurayshiy alikuwa ni ndugu wa ‘Uthmaan bin ‘Affaan upande wa mama. Alisilimu siku ya Fat-h Makkah. Alikuwa miongoni mwa ma-Quraysh wacheshi, mvumilivu, jasiri na mshairi. ‘Uthmaan alimfanya gavana wa mji wa Kufa nchini ‘Iraq kisha akamuuzulu kwa tuhuma za kunywa pombe. Alijzuia kuingia katika

fitnah baada ya kuuwawa kwa ‘Uthmaan, aliishi Ruqa na alifia huko na kuzikwa kwa maeneo ya Bulaykh.

[3] Imam Shaafi’iy anaripoti makubaliano ya ‘Ulamaa (isipokuwa madhehebu ya Zuhri na Imaam Ibn Hazm) kuwa mnywa pombe kwa hali yoyote hawezi kuuwawa, bila kujali amekunywa mara ngapi. Vivyo hivyo, kila atakapokamatwa akinywa pombe hukumu mpya itatolewa dhidi yake, bila kujali kama aliadhibiwa kabla ya hapo na hukumu hiyo hiyo. Kuna makubaliano ya hukumu hii kwa ‘Ulamaa.

[4] Muda wowote pindi mtu anapopigwa kwa adhabu yoyote iliyotolewa dhidi yake, mtu huyo anayetokeleza hukumu ile asipige usoni kwa yeyote atakayeadhibiwa.

[5] Hii ni kwa sababu Misikiti imesimamishwa kwa lengo maalum la kumuabudu Allaah. Hivyo basi, inatakiwa iwe safi muda wote kwa ajili ya jukumu lile la kumuabudu Allaah. Damu ya mtu aliyeadhibiwa (aliyekukumiwa) haitakiwi kutapakaa maeneo ya Msikiti. Maeneo haya ni matukufu na sehemu ya kusubiri Rahmah za Allaah, wakati adhabu iliyotolewa ni kulipa kisasi cha Allaah.

[6] Lengo la kutaja Hadiyth hii ni kuelezea kuwa sio tu kwamba pombe inayotokana na mzabibu ndio iliyoharamishwa bali zote zinazoleweshwa ni haraam.

[7] Ina maana chochote kinacholeweshwa kwa kunywa kwa wingi wake basi ni haraam kukichukuwa kwa uchache wake. Hata kama kichache chake hakilevi.

[8] Huenda kile kilichobaki kikawa kilevi baada ya muda. Kinywaji kile kinapoanza kubadilika ni lazima kimwagwe. Haswa ikiwa ni zaidi ya siku tatu, kinywaji kile kisitumike kikianza kuonekana kimeharibika hata kama ni siku ya pili.

[9] Hii inamaanisha kuwa ni haraam kutumia vitu vilivyoharamishwa, hata kwa ajili ya tiba. Vitu hivi ni kama vile pombe, bangi, madawa ya kulevyo na mfano wake.

[10] Huyu ni Swahaba aliyekuwa akijulikana kwa jina la Twaariqa bin Suwayd. Alikuwa mhadharami na inasemekana alikuwa Ju’fi. Ana Hadiyth moja ambayo watu wa mji wa Kufa walikuwa wakipokea kutoka kwake.

05-Mlango Wa Ta'ziyr Na Hukumu Ya Mshambuliaji

بَابُ التَّعْزِيرِ وَحُكْمِ الصَّائِلِ

05-Mlango Wa Ta'ziyr[1] Na Hukumu Ya Mshambuliaji

1074.

عَنْ أَبِي بُرْدَةَ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { لَا يُجْلَدُ فَوْقَ عَشْرَةِ أَسْوَاطٍ، إِلَّا فِي حَدٍّ مِنْ حُدُودِ اللَّهِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Burdah[2] Al-Answaariyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alisema kuwa alimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Asichapwe mtu zaidi ya mijeledi kumi[3] isipokuwa katika haddi (adhabu) miongoni mwa haddi za Allaah.” [Bukhaariy, Muslim]

1075.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "أَقِيلُوا ذَوِي الْهَيْئَاتِ عَثَرَاتِهِمْ إِلَّا الْحُدُودَ" }
رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wasameheni wenye tabia nzuri[4] kuteleza kwao isipokuwa katika haddi.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy]

1076.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { مَا كُنْتُ لِأُقِيمَ عَلَى أَحَدٍ حَدًّا، فَيَمُوتُ، فَأَجِدُ فِي نَفْسِي، إِلَّا شَارِبَ الْخَمْرِ، فَإِنَّهُ لَوْ مَاتَ وَدَيْتُهُ } أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Msimamishieni haddi yeyote na akifa nikahuzunika isipokuwa mnywaji pombe, kwani lau atakufa nitamtotea diya.”[5] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1077.

وَعَنْ سَعِيدِ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ { "مَنْ قُتِلَ دُونَ مَالِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ" } رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Sa'd bin Zayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayeuwawa kwa kutetea mali zake huyo ni Shahidi.” [Imetolewa na Al-Arba'ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

1078.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ خَبَّابٍ قَالَ: سَمِعْتُ أَبِي رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ يَقُولُ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "تَكُونُ فِتْنٌ، فَكُنْ فِيهَا عَبْدَ اللَّهِ الْمَقْتُولَ، وَلَا تَكُنْ الْقَاتِلَ" } أَخْرَجَهُ ابْنُ أَبِي خَيْثَمَةَ. وَالِدَّارَقُطْنِيُّ وَأَخْرَجَ أَحْمَدُ نَحْوَهُ: عَنْ خَالِدِ بْنِ عُرْفُطَةَ

Kutoka kwa ‘Abdillaah[6] bin Khabbaab[7] amesema amemsikia Baba yangu (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) akisema kuwa alimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Kutakuwa na fitnah,[8] kuwa mja wa Allaah mwenye kuuwawa wala usiwe mwenye kuua.”[9] [Imetolewa na Abiy Khaythamah na Ad-Daaraqutwniy]

Na Ahmad ameipokea Hadiyth kama hii kutoka kwa Khaalid bin ‘Urfutwah[10]

[1] Kuadhiri na kuadhibu.

[2] Huyu ni Hani bin Niyaar aliyekuwa Swahaba kutoka katika kabila la Balawi. Alikuwa ni mshirika wa Al-Answaar na alishuhudia vita vya Badr na vita vinginevyo. Alifariki mwaka 41, na inasemekana 42 na wengine 45 Hijriyyah.

[3] Hadiyth hii imefahamika na baadhi ya Fuqahaa kuwa ni dalili hawezi mtu kuchapwa zaidi ya mijeledi kumi isipokuwa mtu huyo ameingia katika adhabu ya haddi. Imaam Shaafi'iy na Maalik kuongeza inaruhusiwa ilimradi isifikie kile kiwango cha haddi kilichotajwa. Wengine wanaona kuwa huwezi kuongeza maadamu adhabu imetajwa. Wengine wanaona kuwa inaweza kuongezeka zaidi ya mijeledi kumi ikiwa ni adhabu ya kosa kubwa, wakati makosa madogo huwezi kzidisha zaidi ya mijeledi kumi.

[4] Katika adhabu za haddi zilizoainishwa kulingana na makatazo, adhabu hizo zitawahusu wote bila kubagua, tajiri au masikini, mtu wa kawaida au yule mwenye nafasi kubwa katika jamii. Katika makosa madogo madogo hali inaangaliwa kulingana na muda, aina ya kosa, na mtu aliyehusika na kosa lenyewe.

[5] Hadiyth hii inaonesha pia kuwepo kwa tofauti ya rai baina ya Maswahaba wa Nabiy (ﷺ) ikiwa kumchapa mnywa pombe kwa mijeledi arubaini ilikuwa ni adhabu ya haddi au ilikuwa ni Ta'ziyr (kumuadhibu kwa kumuadhiri). Hilo vile vile lilikuwa ni adhabu ya kumuadhiri mtu mzima kwa sababu adhabu ile haipo katika Qur-aan. Hakuna cha kufanya kwa wale ambao watakufa kwa kutekelezewa adhabu ile kwao. Hata hivyo, ikiwa kama mtu atakufa akipitishiwa hukumu hiyo ya kumwadhiri ni juu ya Dola kutoa fidiya kutoka katika hazina wa warithi wa aliyefariki. Tokea hapo, ikawa kila mnywa pombe atakapoadhibiwa na akafa katika adhabu ile, Fuqahaa wana rai kuwa itolewe fidia walipwe warithi wake.

[6] 'Abdullaah alikua ni miongoni mwa Taabi'iyna na mkazi wa Madiyna. Hururiya (Khawaarij) walimuuwa katika mwaka wa 27 Hijriyyah baada ya kumuasi 'Aliy na alikuwa njiani akielekea An-Naharwaan. Baada ya kumuuwa waliingia nyumbani kwake, walimuuwa mjakazi wake na kukatakata kichanga kilichokuwa tumboni mwake. Hili lilipelekea vita maarufu vya An-Naharwaan ambapo 'Aliy aliwauwa Khawaarij wote isipokuwa tisa miongoni mwao ambao walisababishia fitnah kubwa huko mbele.

[7] Khabbaab bin Al-Arat bin Jandala At-Tamiymi alikuwa mmoja wa Maswahaba walioteswa kwa ajili ya Dini yao. Alishiriki katika vita vya Badr. Alikufa katika mji wa Kufa uliopo 'Iraaq alipokataa kushiriki katika vita vya Siffin katika mwaka wa 37 Hijriyyah akiwa na umri wa miaka 73.

[8] Fitnah ni mitihani mbalimbali ni ule mtafaruku uliokuwa ukitokea katika Ummah na katika Dini.

[9] Imetajwa katika Hadiyth iliyotangulia kuwa mwenye kufa akitetea nafsi yake, mali na familia yake atakuwa amekufa Shahidi. Akimuua adui kwa njia ya kujilinda hatopata dhambi kwa mauaji yale. Hukumu hii hutekelezwa ikiwa hali ipo kwa uwazi na sababu zimefahamika. Ikiwa jambo halipo wazi na kuna ukinzani na ugomvi hatakiwi mtu kunyanyua mkono wake kuuwa. Njia nzuri kwa mtu za kuwa salama ni kuacha kuuwa, kwa kuwa muuwaji hukabiliwa na adhabu ya moto, ama aliyeuliwa huingia Jannah. Ikiwa wote watapigana na kila mmoja kupupia kumuuwa mwenzake wote watakabiliwa na adhabu ya moto atakapo Allaah.

[10] Huyu ni Swahaba kabila lake ni Quda katika koo za ‘Udhr. Alikuwa ni wakilishi wa Sa’d bin Abiy Waqqaas katika mji wa Kufa. Alifariki mwaka 61 Hijriyyah na inasemekana kuwa Al-Mukhtar bin Abuu ‘Ubayd alimuuwa baada ya kifo cha Yaziyd mwaka 64 Hijriyyah.

كِتَابُ الْجِهَادِ

Kitabu cha Jihaad

11-Kitabu Cha Jihaad - كِتَابُ الْجِهَادِ

01-Kitabu Cha Jihaad

1079.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "مَنْ مَاتَ وَلَمْ يَغْزُ، وَلَمْ يُحَدِّثْ نَفْسَهُ بِهِ، مَاتَ عَلَى شُعْبَةٍ مِنْ نِفَاقٍ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayekufa na hakupigana Jihaad, wala asiizungumzise nafsi yake hilo, amekufa akiwa na sehemu ya unafiki.”[2] [Imetolewa na Muslim]

1080.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "جَاهِدُوا الْمُشْرِكِينَ بِأَمْوَالِكُمْ، وَأَنْفُسِكُمْ، وَالسِّنَتِكُمْ" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Piganeni na washirikina[3] kwa mali yenu, nafsi zenu na ndimi zenu.” [Imetolewa na Ahmad na An-Nasaaiy na akaisahihisha Al-Haakim]

1081.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! عَلَى النِّسَاءِ جِهَادٌ؟ قَالَ: "نَعَمْ. جِهَادٌ لَا قِتَالَ فِيهِ، الْحَجُّ وَالْعُمْرَةُ"}. رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ وَأَصْلُهُ فِي الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Nilisema Ee Rasuli wa Allaah! Je ni juu ya wanawake Jihaad? Akasema ndio jihaad isiyokuwa na mapambano ndani yake,[4] nayo ni Hajj na ‘Umrah.” [Imetolewa na Ibn Maajah na asili ya Hadiyth imo katika Swahiyh Al-Bukhaariy]

1082.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَسْتَأْذِنُهُ فِي الْجِهَادِ. فَقَالَ: "أَحْيٍ وَالِدَاكَ؟" ، قَالَ: نَعَمْ: قَالَ: "فَفِيهِمَا فَجَاهِدْ"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَلِأَحْمَدَ، وَأَبِي دَاوُدَ: مِنْ حَدِيثِ أَبِي سَعِيدٍ نَحْوُهُ، وَزَادَ: { "ارْجِعْ فَاسْتَأْذِنْهُمَا، فَإِنْ أَذِنَا لَكَ، وَإِلَّا فَبِرَّهُمَا" }

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Mtu mmoja alikuja kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anaomba idhini aende katika Jihaad. Akasema: ‘Je wazazi wako wako hai?’ Akasema: ‘Ndio’ Akasema: ‘kwao wao pigana Jihaad.” [5] [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na Ahmad na Abuu Daawuud wameipokea Hadiyth kama hii kutoka kwa Abuu Sa’iyd na wakaongezea: “Rudi kawaombe idhini, wakikupa idhini sawa, vinginevyo watendee wema.”

1083.

وَعَنْ جَرِيرِ الْبَجَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "أَنَا بَرِيٌّ مِنْ كُلِّ مُسْلِمٍ يُقِيمُ بَيْنَ الْمُشْرِكِينَ" } رَوَاهُ الثَّلَاثَةُ وَإِسْنَادُهُ صَحِيحٌ، وَرَجَّحَ الْبُخَارِيُّ إِسْنَادَهُ

Kutoka kwa Jariyr Al-Bajaliyy[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mimi niko mbali na kila Muislam anayeishi miongoni mwa washirikina.” [7] [Imetolewa na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd) na isnaad yake ni sahihi. Na Al-Bukhaariy ameitilia nguvu kuwa ni Mursal]

1084.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { " لَا هِجْرَةَ بَعْدَ الْفَتْحِ، وَلَكِنْ جِهَادٌ وَنِيَّةٌ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna Hijrah[8] baada ya Fat-h[9] kilichobakia ni Jihaad na niyyah.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1085.

وَعَنْ أَبِي مُوسَى الْأَشْعَرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "مَنْ قَاتَلَ لِتَكُونَ كَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا، فَهُوَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Muwsaa Al-Ash'ariyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
amesema: “Anayepigana ili neno la Allaah liwe juu basi huyo yuko katika Njia ya Allaah.”[10] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1086.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ السَّعْدِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "لَا تَنْقَطِعُ الْهَجْرَةُ مَا قُوتِلَ الْعَدُوُّ" } رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin As-Sa’diyy[11] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)
amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
amesema: “Hijrah[12] haikatiki maadamu adui keshapigwa vita.”
[Imetolewa na An-Nasaaiy, na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1087.

وَعَنْ نَافِعٍ قَالَ: { أَغَارُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى بَنِي الْمُصْطَلِقِ، وَهُمْ غَارُونَ، فَقَتَلَ مُقَاتِلَتَهُمْ، وَسَبَى

ذَرَارِيَّهُمْ. حَدَّثَنِي بِذَلِكَ عَبْدُ اللَّهِ بْنُ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا {
مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) Kutoka kwa Naafi' amesema: "Rasuli wa Allaah (aliwavamia Baniy Muswtwaliq nao wakiwa wameghafilika[13] akawauwa wapiganao nae na akiteka wanawake na watoto wao.[14] Alimhadithia hivyo 'Abdullaah bin 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) [Al-Bukhaariy, Muslim]

1088.

وَعَنْ سُلَيْمَانَ بْنِ بُرَيْدَةَ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا أَمَرَ أَمِيرًا عَلَى جَيْشٍ أَوْصَاهُ بِتَقْوَى اللَّهِ، وَبِمَنْ مَعَهُ مِنَ الْمُسْلِمِينَ خَيْرًا، ثُمَّ قَالَ: "أَغْزُوا بِسْمِ اللَّهِ، فِي سَبِيلِ اللَّهِ، قَاتِلُوا مَنْ كَفَرَ بِاللَّهِ، أَغْزُوا، وَلَا تَغْلُوا، وَلَا تَغْدُرُوا، وَلَا تُمَثِّلُوا، وَلَا تَقْتُلُوا وَلِيدًا، وَإِذَا لَقِيتَ عَدُوَّكَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ فَادْعُهُمْ إِلَى ثَلَاثِ خِصَالٍ، فَأَيُّتَهُنَّ أَجَابُوكَ إِلَيْهَا، فَاقْبَلْ مِنْهُمْ، وَكَفَّ عَنْهُمْ: ادْعُهُمْ إِلَى الْإِسْلَامِ فَإِنْ أَجَابُوكَ فَاقْبَلْ مِنْهُمْ.

ثُمَّ ادْعُهُمْ إِلَى التَّحَوُّلِ مِنْ دَارِهِمْ إِلَى دَارِ الْمُهَاجِرِينَ، فَإِنْ أَبَوْا فَأَخْبِرْهُمْ أَنَّهُمْ يَكُونُونَ كَأَعْرَابِ الْمُسْلِمِينَ، وَلَا يَكُونُ لَهُمْ . فِي الْغَنِيمَةِ وَالْفَيْءِ شَيْءٌ إِلَّا أَنْ يُجَاهِدُوا مَعَ الْمُسْلِمِينَ. فَإِنْ هُمْ أَبَوْا فَاسْأَلْهُمْ الْجِزْيَةَ، فَإِنْ هُمْ أَجَابُوكَ فَاقْبَلْ مِنْهُمْ، فَإِنْ أَبَوْا فَاسْتَعِنَ بِاللَّهِ وَقَاتِلْهُمْ. وَإِذَا حَاصَرْتَ أَهْلَ حِصْنٍ

فَأَرَادُوكَ أَنْ تَجْعَلَ لَهُمْ ذِمَّةَ اللَّهِ وَذِمَّةَ نَبِيِّهِ، فَلَا تَفْعَلْ، وَلَكِنْ
اجْعَلْ لَهُمْ ذِمَّتَكَ، فَإِنَّكُمْ إِنْ تَخْفِرُوا ذِمَّتَكُمْ. أَهْوَنُ مِنْ أَنْ
تُخْفِرُوا ذِمَّةَ اللَّهِ، وَإِذَا أَرَادُوكَ أَنْ تُنْزِلَهُمْ عَلَى حُكْمِ اللَّهِ، فَلَا
تَفْعَلْ، بَلْ عَلَى حُكْمِكَ، فَإِنَّكَ لَا تَدْرِي أَتُصِيبُ فِيهِمْ حُكْمَ اللَّهِ
أَمْ لَا" { أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Sulaymaan bin Buraydah naye kutoka kwa baba yake kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa anapomueka Amiri katika jeshi au kikosi[15] humuusia kheri na kuwa na Taqwa na huwausia Waislam walio pamoja nae kheri pia. Kisha anasema: ‘Piganeni kwa Jina la Allaah, katika Njia ya Allaah, piganeni na anayemkufuru Allaah, piganeni na wala msifanye udanganyifu,[16] wala msivunje ahadi, wala msitese,[17] wala msiue mtoto mdogo. Utakapokutana na adui yako miongoni mwa washirikana walinganie katika mambo matatu, lolote kati ya hayo watakapokujibu wakubalie na ujizuwie; walinganie katika Uislam, wakikujibu wakubalie, kisha walinganie wahame kutoka katika mji wao wahamie mji wa Muhaajiriyna[18] (Madiynah), wakikataa waambie kuwa wao watakuwa kama wale mabedui Waislam, hawatapata kitu katika ngawira[19] wala katika fai[20] isipokuwa watakapopigana Jihaad pamoja na Waislam. Wakikataa waombe watoe Jizya,[21] wakikujibu wakubalie, wakikataa basi omba msaada kwa Allaah dhidi yao na upigane nao. Utakapowazingira watu katika ngome, wakakuomba uwajaalie dhima ya Allaah na dhima ya Nabiy wake usifanye, lakini wajalie dhima yako, kwani nyinyi kutangua dhima zenu ni rahisi kuliko kutangua dhima ya Allaah. Na akikuomba uwaweke katika hukumu ya Allaah usifanye, bali katika hukumu yako, kwani wewe hujui utapata usawa Hukumu ya Allaah miongoni mwao au la.”

[Imetolewa na Muslim]

1089.

وَعَنْ كَعْبِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا أَرَادَ غَزْوَةً وَرَى بِغَيْرِهَا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ka'b bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anapotaka kuenda vitani huficha (kusudio lake) kwa jambo jingine.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1090.

وَعَنْ مَعْقِلٍ، أَنَّ النُّعْمَانَ بْنَ مُقَرَّرٍ قَالَ: { شَهِدْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا لَمْ يُقَاتِلْ أَوَّلَ النَّهَارِ آخَرَ الْقِتَالِ حَتَّى تَزُولَ الشَّمْسُ، وَتَهْبُ الرِّيَّاحُ، وَيَنْزِلَ النَّصْرُ } رَوَاهُ أَحْمَدُ وَالثَّلَاثَةُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ. وَأَصْلُهُ فِي الْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Ma'qil amesema kuwa An-Nu'maan bin Muqarrin[22] amesema: “Nilishuhudia vita pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى) alikuwa asipopigana mwanzo wa mchana huakhirisha vita mpaka jua lipinduke upepo uvume na nusura iteremke.”[23] [Imetolewa na Ahmad na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaa'iy, Abuu Daawuud) na akaisahihisha Al-Haakim, na asili yake iko katika Al-Bukhaariy]

1091.

وَعَنْ الصَّعْبِ بْنِ جَثَامَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {سُئِلَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ الدَّارِ مِنَ الْمُشْرِكِينَ. يُبَيِّتُونَ، فَيُصَيَّبُونَ مِنْ نِسَائِهِمْ وَذُرَارِيهِمْ، فَقَالَ: "هُم مِّنْهُمْ"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Asw-Swa'b bin Jathaamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliulizwa kuhusu wanawake na watoto miongoni mwa washirikina wanaovamiwa ghafla wakauwawa au wakadhuriwa wanawake na watoto wao. Akasema wao ni miongoni mwao.”[24] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1092.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لِرَجُلٍ تَبِعَهُ يَوْمَ بَدْرٍ: "إِرْجِعْ. فَلَنْ أَسْتَعِينَ بِمُشْرِكٍ"} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuambia mtu aliyemfuata katika vita vya Badr: ‘Rudi kwani sitaomba msaada kwa mshirikina’.”[25] [Imetolewa na Muslim]

1093.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَأَى امْرَأَةً مَقْتُولَةً فِي بَعْضِ مَغَارِيهِ، فَأَنْكَرَ قَتْلَ النِّسَاءِ وَالصِّبْيَانِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimuona mwanamke ameuwawa katika baadhi ya vita alivyopigana, akakataa kuua wanawake na watoto.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1094.

وَعَنْ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { " أَقْتُلُوا شُيُوخَ الْمُشْرِكِينَ، وَاسْتَبْقُوا شَرَّخَهُمْ " } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wauweni wazee[26] wa mushirikina na waacheni watoto wao.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

1095.

وَعَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُمْ تَبَارَزُوا يَوْمَ بَدْرٍ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ وَأَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ مُطَوَّلًا

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Wao walibariziana[27] siku ya Badri.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy na Abuu Daawuud ameipokea kwa urefu]

1096.

وَعَنْ أَبِي أَيُّوبَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: إِنَّمَا أُنْزِلَتْ هَذِهِ الْآيَةُ
فِينَا مَعْشَرَ الْأَنْصَارِ، يَعْنِي: (وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ)
قَالَهُ رَدًّا عَلَى مَنْ أَنْكَرَ عَلَى مَنْ حَمَلَ عَلَى صَفِ الرُّومِ
حَتَّى دَخَلَ فِيهِمْ . رَوَاهُ الثَّلَاثَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ
حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Ayyuwb (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Aayah hii iliteremka kwetu kongamano la Answaar: {...wala msijitupe katika maangamizi kwa (kuzuia) mikono yenu (isitoe)...} [Qur-aan2: 195] alisema hivyo akamrudi aliyejiingiza ndani ya safu ya Warumi akaingia katikati yao.”[28] [Imetolewa na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na akaisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

1097.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { حَرَقَ رَسُولُ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَخْلَ بَنِي النَّضِيرِ، وَقَطَعَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliichoma mitende[29] ya Baniy An-Nadhwiyr na akaikata.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1098.

وَعَنْ عُبَادَةَ بْنِ الصَّامِتِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "لَا تَغْلُوا، فَإِنَّ الْغُلُولَ نَارٌ وَعَارٌ عَلَى أَصْحَابِهِ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa ‘Ubaadah bin Asw-Swaamit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msifanye khiyana katika ghanima (kabla ya kugawiwa), kwa hakika khiyana ni moto na ni aibu kwa wanaoifanya duniani na Aakhirah.” [Imetolewa na Ahmad na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1099.

وَعَنْ عَوْفِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَضَى بِالسَّلْبِ لِلْقَاتِلِ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَأَصْلُهُ عِنْدَ مُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Awf bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alihukumu kilichoachwa na

aliyeuwawa ni cha aliyeuwa.”[30] [Imetolewa na Abuu Daawuud na asili yake iko katika Muslim]

1100.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَوْفٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فِي قِصَّةِ قَتْلِ أَبِي جَهْلٍ قَالَ: {فَابْتَدَرَاهُ بِسَيْفَيْهِمَا حَتَّى قَتَلَاهُ، ثُمَّ انْصَرَفَا إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَأَخْبَرَاهُ، فَقَالَ: "أَيُّكُمَا قَتَلَهُ؟ هَلْ مَسَحْتُمَا سَيْفَيْكُمَا؟" قَالَا: لَا. قَالَ: فَنَظَرَ فِيهِمَا، فَقَالَ: "كِلَاكُمَا قَتَلَهُ، سَلَبُهُ لِمُعَاذِ بْنِ عَمْرٍو بْنِ الْجَمُوحِ" {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Awf (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema katika kisa cha Abuu Jahl akasema: “Wakamkimbilia kwa panga zao wakamuuwa, kisha wakaenda kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) wakamueleza. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawauliza: ‘Ni nani kati yenu aliyemuua? Je mumezipangusa panga zenu? Wakasema bado. Nabiy akazitazama panga zao akawaambia: ‘Nyote mumemuua’. Nabiy akahukumu salab yake kwa Mu’aadh bin ‘Amr bin Al-Jamuwh.”[31] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1101.

وَعَنْ مَكْهُولٍ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَصَبَ
الْمَنْجَنِيْقَ عَلَى أَهْلِ الطَّائِفِ } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ فِي
"الْمَرَّاسِيلِ" وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

وَوَصَلَهُ الْعُقَيْلِيُّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ عَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ

Kutoka kwa Makhuwl[32] amesema: “kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) aliwashambulia[33] watu wa Atw-Twaaif kwa Manjaniyq.” [Imetolewa na Abuu Daawuud katika kitabu chake cha Al-Maraasiyl na wapokezi wake ni madhubuti]

Al-‘Uqayliyy ameipokea ikiwa ni mawsuwl dhaifu kutoka kwa ‘Aliyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)

1102.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
دَخَلَ مَكَّةَ وَعَلَى رَأْسِهِ الْمَغْفَرُ، فَلَمَّا نَزَعَهُ جَاءَهُ رَجُلٌ، فَقَالَ:
ابْنُ خَطْلٍ مُتَعَلِّقٌ بِأَسْتَارِ الْكَعْبَةِ، فَقَالَ: "أُقْتُلُوهُ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) aliingia Makkah na juu ya kichwa chake ana kofia ya chuma, alipoivua mtu mmoja alimjia akasema: ‘Ibn Khatwal ameikumbatia nguzo ya Al-Ka’bah’ Nabiy akasema: Muuweni.”[34] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1103.

وَعَنْ سَعِيدِ بْنِ جُبَيْرٍ، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَتَلَ يَوْمَ بَدْرٍ ثَلَاثَةً صَبْرًا } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ فِي "الْمَرَّاسِيلِ" وَرِجَالَهُ ثَقَاتٌ

Kutoka kwa Sa'iyd bin Jubayr[35] amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliua watu watatu katika vita vya Badr.”[36] [Imetolewa na Abuu Daawuud katika kitabu chake cha Al-Maraasil na wapokezi wake ni madhubuti]

1104.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَدَى رَجُلَيْنِ مِنَ الْمُسْلِمِينَ بِرَجُلٍ مِنَ الْمُشْرِكِينَ } أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ. وَأَصْلُهُ عِنْدَ مُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwatolea fidia watu wawili Waislamu[37] kwa mtu mmoja mshirikina.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha, na asili yake iko katika Muslim]

1105.

وَعَنْ صَخْرِ بْنِ الْعَيْلَةِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "إِنَّ الْقَوْمَ إِذَا أَسْلَمُوا ؛ أَحْرَزُوا دِمَاءَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ" } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَرِجَالُهُ مُوْتَقُونَ

Kutoka kwa Swakhr bin Al-‘Aylah[38] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu wanaosilimu, wamehifadhi damu zao na mali yao.”[39] [Imetolewa na Abuu Daawuud na wapokezi wake ni madhubuti]

1106.

وَعَنْ جُبَيْرِ بْنِ مُطْعَمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ فِي أُسَارَى بَدْرٍ: { "لَوْ كَانَ الْمُطْعَمُ بْنُ عَدِيٍّ حَيًّا، ثُمَّ كَلَّمَنِي فِي هَؤُلَاءِ النَّتْنَى لَتَرَكْتُهُمْ لَهُ" } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Khubayr bin Mutw’am (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuhusiana na mateka wa vita vya Badr: “Lau Al-Mutw’am bin ‘Adiyy[40] angekuwa hai, kisha akazungumza nami ili niwaache hawa wanaonuka, ningalimwachia.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1107.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { أَصَبْنَا سَبَايَا يَوْمَ أُوطَاسٍ لَهُنَّ أَزْوَاجٌ، فَتَحَرَّجُوا، فَأَنْزَلَ اللَّهُ تَعَالَى: (وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ) } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulipata mateka waliokuwa na waume zao katika vita vya Awtwaas wakaona uzito juu ya hali hili,[41] Allaah Akateremsha Aayah hii: {Na (Mmeharamishiwa pia) wanawake walio katika ndoa isipokuwa iliyowamiliki mikono yenu ya kuume...}.” Mpaka mwisho wa Aayah hii [Qur4: 24] [Imetolewa na Muslim]

1108.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {بَعَثَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَرِيَّةً وَأَنَا فِيهِمْ، قَبْلَ نَجْدٍ، فَغَنِمُوا إِبِلًا كَثِيرَةً، فَكَانَتْ سُهُمَانُهُمْ اثْنِي عَشَرَ بَعِيرًا، وَنُفِّلُوا بَعِيرًا بَعِيرًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituma kikosi nami nikiwa ndani yake upande wa Najd, wakapata ngamia wengi, mafungu yao yakafikia ngamia kumi na mbili kila mmoja.”[42] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1109.

وَعَنْهُ قَالَ: {قَسَمَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ خَيْبَرَ لِلْفَرَسِ سَهْمَيْنِ، وَلِلرَّاحِلِ سَهْمًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ. وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

وَلِأَبِي دَاوُدَ: {أَسْهَمَ لِرَجُلٍ وَلِفَرَسِهِ ثَلَاثَةَ أَسْهُمٍ: سَهْمَيْنِ لِفَرَسِهِ، وَسَهْمًا لَهُ}

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aligawa (ngawira) katika vita vya Khaybar, mpanda farasi mafungu mawili na wa miguu ana fungu moja.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Bukhaariy]

Katika riwaayah ya Abuu Daawuud imesema: “Rasuli wa Allaah alimgawia mpiganaji na farasi wake mafungu matatu, mafungu mawili ni ya farasi wake na fungu moja ni lake.”

1110.

وَعَنْ مَعْنِ بْنِ يَزِيدَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: "لَا نَفْلَ إِلَّا بَعْدَ الْخُمْسِ"} رَوَاهُ أَحْمَدُ ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الطَّحَاوِيُّ

Kutoka kwa Ma'n bin Yaziyd[43] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Hakuna ziada isipokuwa baada ya khumus.”[44] [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud na akaisahihisha Atw-Twahaawiy]

1111.

وَعَنْ حَبِيبِ بْنِ مَسْلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {شَهِدْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَفْلَ الرَّبْعِ فِي الْبَدَاةِ، وَالثُّلُثِ فِي

الرَّجْعَةَ { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْجَارُودِ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [45] Kutoka kwa Habiyy bin Maslamah amesema: “Nilimshuhudia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akiongeza ngawira robo katika kuanza safari na thuluthi katika kurejea.” [46] [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Ibn Al-Jaaruwd, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

1112.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُنْفِلُ بَعْضَ مَنْ يَبْعَثُ مِنَ السَّرَايَا لِأَنْفُسِهِمْ خَاصَّةً، سِوَى قَسَمِ عَامَّةِ الْجَيْشِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alikuwa akiongeza baadhi ya aliowatuma katika vikosi kwa ajili yao makhsusi [47] usiokuwa mgao wa jeshi lote.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1113.

وَعَنْهُ قَالَ: { كُنَّا نُصِيبُ فِي مَغَارِينَا الْعَسَلَ وَالْعِنَبَ ، فَتَأْكُلُهُ وَلَا نَرْفَعُهُ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ وَلِأَبِي دَاوُدَ: { فَلَمْ يُؤْخَذْ مِنْهُمْ الْخُمْسُ } وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Katika vita vyetu tulikuwa tunapata asali na zabibu tukizila wala hatuzichukui.” [48] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

Katika riwaayah ya Abuu Daawuwd: “...wala humo haikuchukuliwa khumus.” [Na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1114.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي أَوْفَى رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {أَصَبْنَا طَعَاماً يَوْمَ خَيْبَرَ، فَكَانَ الرَّجُلُ يَجِيءُ، فَيَأْخُذُ مِنْهُ مِقْدَارَ مَا يَكْفِيهِ، ثُمَّ يَنْصَرِفُ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ الْجَارُودِ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdillaah bin Abiy Awfa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Katika vita vya Khaybar tulipata chakula ikawa mtu anachukua kiasi kinachomtosha na kisha anaondoka.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Ibn Al-Jaaruwd na Al-Haakim]

1115.

وَعَنْ رُوَيْفِعِ بْنِ ثَابِتٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {“مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلَا يَرْكَبُ دَابَّةً مِنْ فِيءِ الْمُسْلِمِينَ، حَتَّى إِذَا أَعْجَفَهَا رَدَّهَا فِيهِ، وَلَا يَلْبَسُ ثَوْباً مِنْ فِيءِ الْمُسْلِمِينَ حَتَّى إِذَا أَخْلَقَهُ رَدَّهُ فِيهِ”} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالدَّارِمِيُّ، وَرِجَالُهُ لَا بَأْسَ بِهِمْ

Kutoka kwa Ruwayfi' bin Thaabit (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kumuamini Allaah na Siku ya mwisho, asipande myama katika ghanima ya Waislamu mpaka akamdhoofisha na kumrudisha humo,[49] wala asivae nguo katika ngawira ya Waislam mpaka akaichakaza na kuirudisha.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na Ad-Daarimiyy na wapokezi wake hawana ubaya.

1116.

وَعَنْ أَبِي عُبَيْدَةَ بْنِ الْجَرَّاحِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "يُجِيرُ عَلَى الْمُسْلِمِينَ بَعْضُهُمْ" } أَخْرَجَهُ ابْنُ أَبِي شَيْبَةَ، وَأَحْمَدُ، وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ

وَلِلْطَيَالِسِيِّ: مِنْ حَدِيثِ عَمْرِو بْنِ الْعَاصِ: { "يُجِيرُ عَلَى الْمُسْلِمِينَ أَدْنَاهُمْ" }

وَفِي "الصَّحِيحَيْنِ" : عَنْ عَلِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { "ذِمَّةُ الْمُسْلِمِينَ وَاحِدَةٌ يَسْعَى بِهَا أَدْنَاهُمْ" }

زَادَ ابْنُ مَاجَهَ مِنْ وَجْهِ آخَرَ: { "يُجِيرُ عَلَيْهِمْ أَقْصَاهُمْ" }

وَفِي "الصَّحِيحَيْنِ" مِنْ حَدِيثِ أُمِّ هَانِيٍّ: { قَدْ أَجَرْنَا مَنْ أَجَرْتَ }

Kutoka kwa Abiy ‘Ubaydah bin Al-Jarraah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Waislam[50] wanawakinga baadhi yao.”

[Imetolewa na Ibn Abiy Shaybah na Ahmad na katika isnaad yake kuna udhaifu]

Na amepokea Atwayaalisiy kutoka katika Hadiyth ya ‘Amr bin Al-’Aasw: “Waislam wanawakinga walio karibu nao.”

Na katika Swahiyh Al-Bukhaariy na Swahiyh Muslim imepokewa kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Dhima ya Waislam ni mmoja anaenda katika dhima yao aliye karibu nao.”

Ibn Maajah ameongezea kwa njia nyingine: “Anaenda katika dhima yao aliye mbali nao.”

Na katika Swahiyh Al-Bukhaariy na Swahiyh Muslim kutoka katika Hadiyth ya Ummu Haaniy[51]: “Kwa hakika tumemhami uliyemhami.”

1117.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "لَا أَخْرَجَنَّ الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى مِنْ جَزِيرَةِ الْعَرَبِ، حَتَّى لَا أَدْعَ إِلَّا مُسْلِمًا" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa alimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Nitawatoa Mayahudi na Manaswara katika rasi ya Arabuni[52] hadi nisibakishe isipokuwa Muislam.” [Imetolewa na Muslim]

1118.

وَعَنْهُ قَالَ: {كَانَتْ أَمْوَالُ بَنِي النَّضِيرِ مِمَّا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ، مِمَّا لَمْ يُوجِفْ عَلَيْهِ الْمُسْلِمُونَ بِخَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ، فَكَانَتْ لِلنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خَاصَّةً، فَكَانَ يُنْفِقُ عَلَى أَهْلِهِ نَفَقَةً سَنَةً، وَمَا بَقِيَ يَجْعَلُهُ فِي الْكُرَاعِ وَالسَّلَاحِ، عُدَّةً فِي سَبِيلِ اللَّهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mali ya baniiy An-Nadhwiyr miongoni mwa mali ambayo Allaah Alimrudishia Rasuli wake, ambayo Waislamu hawakuendea kwa farasi wala ngamia, ilikuwa ni ya Nabiiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) pekee: Nabiiy alikuwa anatenga chakula cha ahli zake mwaka mzima, kinachobaki[53] anakifanya kwenye farasi na silaha, maandalizi njia ya Allaah.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1119.

وَعَنْ مُعَاذٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {غَزَوْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خَيْبَرَ، فَأَصَبْنَا فِيهَا غَنَمًا، فَقَسَمَ فِيْنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ طَائِفَةً، وَجَعَلَ بَقِيَّتَهَا فِي الْمَغْنَمِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَرِجَالُهُ لَا بَأْسَ بِهِمْ

Kutoka kwa Mu’aadh (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Tulipigana Jihaad pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Khaybar tukapata ndani yake mbuzi, Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akatugawia fungu, na kilichobaki alikigawa katika ghanima.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na wapokezi wake hawana ubaya]

1120.

وَعَنْ أَبِي رَافِعٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "إِنِّي لَا أَخِيسُ بِالْعَهْدِ، وَلَا أَحْبِسُ الرَّسُلَ" } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Raafi' (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kwa hakika mimi sivunji ahadi[54] wala sifungi wajumbe.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1121.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "أَيُّمَا قَرْيَةٍ أَتَيْتُمُوهَا، فَأَقَمْتُمْ فِيهَا، فَسَهْمُكُمْ فِيهَا، وَأَيُّمَا قَرْيَةٍ عَصَتْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ، فَإِنْ خُمِسَهَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ، ثُمَّ هِيَ لَكُمْ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ.

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mji wowote mliouenda mkakaa humo[55] fungu lenu limo humo. Na mji wowote uliomuasi Allaah na Rasuli wake, kwa hakika khumus yake ni ya Allaah na Rasuli wake, kitakachobaki ni chenu.” [Imetolewa na Muslim]

[1] Jihaad kilugha ina maana ya juhudi na jitihada kuendea jambo fulani. Katika Istwilaah ya kishariy'ah neno hili hutumika kwa maana ya vita dhidi ya makafiri. Wakati mwingine hutumika kwa maana ya jitihada dhidi ya shaytwaan au dhidi ya uadui unaoelekezwa kwa Uislamu na Waislam.

[2] Jihaad linatumika kila wakati, wakati mwingine ni kwa panga, wakati mwingine kwa kutumia fedha na wakati mwingine kwa maneno na maandishi. Muislam akipata wasaa huo basi na aweke niyyah kuhusiana nayo. Mtu ambaye hakufikiria kabisa na hakulipa uzito jambo hili ni mnafiki.

[3] Hadiyth hii inazungumzia kulingana na mahitaji ya wakati uliopo, Jihaad ni faradhi kwa kila Muumin, hiyo ni katika kila zama. Ikiwa mtu huyo hajali wala haoni umuhimu wake, basi hakuna tofauti yake kuwa kwake Muumin na wengine kuwa kwao makafiri. Jihaad ya ulimi inahusisha kutumia hoja na hekima katika kuwalingania watu katika ukweli na kwa Allaah.

[4] Katika hali hii ni kuwa Jihaad ya silaha, mapigano na vita si wajibu kwa mwanamke. Kwa kufanya kwake Hijjah na 'Umrah mwanamke anapata malipo kama ya mwanamme aliyeshiriki vita vya Jihaad.

[5] Hadiyth hii ni dalili kuwa kabla ya kuenda vitani ni vizuri mtu kuomba ruhsa ya wazazi wawili maadamu ni Waislam. Hairuhusiwi kwa yeyote kuenda kwenye uwanja wa vita kama wazazi wake hawataki, kwa kuwa katika kuwahudumia wao kadhalika ni katika wajibu wake binafsi. Hata hivyo, ruhsa yao haitakiwi katika Jihaad ya wajibu, pindi mtu atakapoitwa na kiongozi wa Kiislam.

[6] Huyu ni Abuu 'Amr Jariyr bin 'Abdillaah bin Jaabir Al-Bajaliyy ambaye alisilimu mwaka wa 10 Hijriyyah. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) alimtandikia kitambaa akalie na akamtuma kwa watu wa Dhil Khalasa na kuwaangamiza. Alikaa Yaman akiitumikia Dola ya Kiislam wakati wa Nabiy. Anaelezea hali yake kwa kusema: "Tokea niliposilimu kila mara Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) anaponiona hutabasamu." Alishiriki katika kuifungua Al-Madayn na alikuwa katika kamandi ya kuume katika jeshi la Waislam katika vita vya Al-Qadisiya. Alikuwa akijulikana kama Yuwsuf wa Ummat huu. Alikufa mwaka 52 au 54 Hijriyyah.

[7] Wakati huo Waislam walikuwa ni wachache sana na ilikuwa ni muhimu sana kwao kuimarisha ngome yao Madiynah. Uislam usingewezekana bila ya kuhama. Kuhama ilikuwa ni wajibu kwa waliyoweza. Hadiyth hii iliyopokewa na Jariyr ilizungumzwa wakati huo. Hata hivyo, pindi ufunguzi wa Makkah ulipofanikiwa na makabila mbalimbali ya kiarabu kuanza kuingia katika Uislam kwa makundi makundi kila siku, na hivyo kuifanya dola ya Kiislam ipanuke, wakati huo tena suala la kuhamia kuenda Madiynah halikuwa la lazima. Tunasoma katika Hadiyth ifuatayo iliyoripotiwa na Ibn ‘Abbaas inahusu jambo hili hili. Hadi leo hii, ikiwa mtu kachoshwa na ni mwenye dhiki kubwa katika Daarul-kufr (Miji na chi za makafiri), ni wajibu kwake kuhamia katika Daarul-Islaam (nchi za Kiislam).

[8] Makkah kuelekea Madiynah.

[9] Ufunguzi wa mji wa Makkah.

[10] Hii ina maana ya kuwa vita vyote kwa malengo ya, (i) Kuthibitisha ujasiri au ushujaa wa watu, (ii) Kulinda heshima, (iii) Utekaji nyara, (iv) Unafiki na utekaji wa ardhi n.k si katika vita vya Kiislam pamoja na kuwa vinaweza kuwa vinapiganwa na jeshi la Waislam. Lengo la vita vya Kiislamu ni kupigana kwa ajili ya nia ya kuutangaza Uislam (Da’wah). Katika hali hiyo inaweza kutokea kukapatikana kwa maslahi mengine kwa wapiganaji wa Kiislam na Uislam hauwakatazi kunufaika na maslahi hayo.

[11] Alikuwa ni Swahaba kutoka katika ukoo wa ‘Aamir wa Kikureshi. Al-Waqiyd amesema: “Alifariki mwaka 57 Hijriyyah”. Jina lake lilikuwa ‘Amr au Qudaamah au ‘Abdullaah bin Waqdaan.

[12] Yaani kutoka katika ardhi zilizokamatwa na makafiri kuelekea katika ardhi za Waislam.

[13] Nabiyy (ﷺ) alipojulishwa kuwa Banu Mustwaliq walikuwa wamejitayarisha kumvamia na kumpiga, yeye akawahi kuwavamia, akawauwa watu kumi miongoni mwao na kuteka mateka waliobakia. Nabiyy (ﷺ) alipowaachia huru na kumuoa Juwayriyya, Maswahaba nao wakawaachia mateka wote waliobakia na kisha wote wakasilimu.

[14] Hii inaelezea kuwa ikiwa watu wameshalinganiwa, na wakakataa ulingano huo, sio wajibu tena kuwatumia lingano la vita kabla ya kupigana nao. Hadiyth hii inaelezea vile vile kumshambulia adui katika mipaka yao ni jambo linaloruhusiwa na mwisho inaonesha kuwa hata waarabu wakichukuliwa mateka.

[15] Sariya ni kikosi maalumu cha uchunguzi kinachofanya kazi yake usiku.

[16] Katika kuchukuwa ngawira kabla ya mgao.

[17] Katika lugha ya kiarabu Muthla ni kukata kiungo kimoja kimoja. Kama vile kukata pua, sikio, na viungo vingine mwilini.

[18] Hii ina maana kuwa suala la kuhama ni jambo la kuendelea daima, kwa kua kuendelea kukaa katika nchi za makafiri kunazuiwa kutekelezwa kwa shariy'ah za Kiislaam.

[19] Katika lugha ya kiarabu ni Ghaniyma kwa maana ya mabaki yanayoachwa au yanayotekwa kutoka kwa adui vitani. Moja ya tano inachukuliwa na kuhifadhiwa katika hazina na zilizobaki zinagawiwa kwa wapiganajii. Askari wa miguu hupata hisa moja na yule wa farasi hupata hisa tatu.

[20] Fai ni istwilaah inayotumiwa kwa maana ya ngawira inayopatikana kutoka kwa makafiri bila ya mapigano. Moja ya tano inayopatikana haigawiwi bali inapelekwa kwa yatima, maskini, wasafiri, wanaohama, na fiy sabiliLLaah kwa amri ya Khalifa.

[21] Jizya ni malipo ya kodi ya kichwa ambayo inachukuliwa na serikali ya Kiislam kutoka kwa wakazi wake wasio kuwa Waislaam.

[22] Huyu alikua ni Swahaba kutoka katika kabila la Muzaynah na alikuwa ni mmoja katika makamanda wa Waislam wakati wa Khalifa Abuu Bakr na 'Umar bin Al-Khatwaab. Alihama pamoja na ndugu zake wengine saba. Alifungua Asbahan na aliuwawa katika vita vya Nahawand katika mwaka wa 21 Hijriyyah.

[23] Muda mzuri wa kushambulia ni asubuhi, wakati muda mzuri wa kupigana ni mchana, wakati huo nusra za Allaah hushuka kwa Waumini wakati wa Swalaah. Du'aa zinazosomwa muda huu ni mustajaabu.

[24] Wanawake na watoto wa kikafiri hawatakiwi kuuwawa katika vita. Hata hivyo, ikiwa imetokezea mashambulizi yakifanyika usiku na bahati mbaya wakauwawa hakuna lawama katika hilo.

[25] Mwanzoni, ilikatazwa kuchukua msaada kutoka kwa makafiri wakati wa vita. Katazo hili lilikuja kuondoshwa huko mbele. Kuna Hadiyth inayoeleza kuwa: “Mtafanya mkataba wa amani na Warumi, Waislaam na Warumi wataungana kupigana na adui.”

[26] Ni haraam kabisa kuuwa watoto. Ni ruhusa kuuwa wanawake kama wanawake hao watashambulia, vinginevyo ni haraam kuwauwa. Wazee miongoni mwa washirikina (kama wana nguvu na wanaweza kupigana) na wanaoweza kusaidea adui katika hali yoyote hata kama watatoa ushauri inaruhusiwa kuwauwa. Vinginevyo wazee wasioingia vitani haifai kuuwawa.

[27] Mubaaraza ni mapigano ya mtu kwa mtu (kwa wenye uwezo wa kupigana). Mara nyingi hufanyika wito wa kupigana wa mtu na mtu kwa sauti za majigambo. Pamoja na kuwa jambo hili linaonekana la kujigamba na kujiamini kupita kiasi na kuonesha ujasiri wa hali ya juu, ni jambo ambalo hukubaliwa tu kwa lengo la kumtisha adui.

[28] Hadiyth hii ina maelezo kuwa wakati wapiganaji wanataka kushambulia, ifikiriwe pia idadi ya adui kwa kulinganisha. Ikiwa wapiganaji wa kikafiri ni mara mbili ya wale Waumini, Waislam wanaamrisha kupigana nao. Hata hivyo, ikiwa idadi ni zaidi ya hapo ni wajibu wa Waislam kupigana nao. Hadiyth hii inathibitisha dalili ya ruhusa ya mpiganaji mmoja kushambulia kundi la adui, akiwa anajua kuwa anaweza kufanya hivyo.

[29] Hadiyth hii inaelezea kuwa ikiwa kuna kitu kinacholeta kikwazo vitani hata ikiwa kina manufaa na watu na kitu hicho kikatumika kama ngome ya adui ni ruhusa kukiangamiza.

[30] Katika lugha ya kiarabu Salb ni kitu kilichohusishwa na mwili wa aliyeuwawa, kama nguo, silaha na kipando. ‘Ulamaa wengi ni wenye rai kuwa hivyo ni haki kwa aliyeuwa.

[31] Huyu alikuwa katika Answaar wa Khazraj wa ukoo wa Sulami. Alihudhuria Al-‘Aqaba na Badr. Alikuwa ni mmoja aliyemkata mguu Abuu Jahl na kumuangusha kutoka katika farasi wake kisha Ikrimah mtoto wa Abuu Jahl akamkata Mu’aadh mkono wake, lakini hilo halikumzuia kupigana hadi vita vilivyokwisha. Alifariki wakati wa Ukhaliifa wa ‘Uthmaan.

[32] Makhuwl Ad-Dimashqi alikuwa ‘Aalim (Mwanazuoni) wa Fiqhi huko Sham na katika watu mashuhuri. Abuu Haatim anamuelezea: “Simjui mwenye ufahamu wa Fiqhi kumzidi.” Alifariki katika mwaka 113 Hujriyyah.

[33] Manjaniyq ni mtambo wa kutupa mawe vitani katika ngome ya adui. Lengo la kutaja Hadiyth hii ni kuwa kuna uwezekano wa kuuwawa watoto, wanawake na watu wazima katika vita vya namna hii ambapo adui anajificha katika ngome na hakuna njia nyingine ila kuwasha Manjaniyq ili kuwashinda.

[34] Jina la Ibn Khatal lilikuwa ni ‘Abdullaah. Mtu huyu dhaifu alisilimu mwanzoni. Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma akakusanye Zakaah pamoja na mtu mwingine katika Ansaar ndipo aliporitadi na kumuuwa jamaa wa kianswaar. Aliiba fedha za Zakaah na kukimbilia Makkah. Baada tu ya Waislamu kuifungua Makkah, Ibn Khatal alijificha maeneo ya Ka’bah. Rasuli alituma Maswahaba zake wakamuuwe. Hii inathibitisha kuwa msaliti na muuwaji hapati msamaha hata akiwa Ka’bah.

[35] Alikuwa katika ukoo wa Al-Walibi na akiishi mji wa Kufa ‘Iraaq. Alikuwa ‘Aalim (Mwanazuoni) mkubwa wa Fiqhi na Imaam mwenye mamlaka katika tafsiri ya Qur-aan na Hadiyth. Alikuwa ni mtu wa mwisho kuuwawa na Hajjaaj bin Yusuf. Maimun bin Mahraan anasema: “Sa’iyd bin Jubayr alikufa wakati kila mmoja wakati ule akihitajia elimu yake.” Aliuwawa mwaka 95 Hijriyyah. Akiwa ni mzee sana.

[36] Watu hawa watatu walikuwa ni: Tua’ma bin ‘Adl, Nadr bin Harith na ‘Uqbat bin Abi Mu’ait. Hili linaelezea kuwa ni ruhusa kuwauwa watu wa aina hii (wanaokaribia kufa kwa njaa au kiu)

[37] Maelezo ya Hadiyth hii ni kuonesha kuwa kubadilishana wafungwa ni ruhsa. Watu wa Banu Thaqiyf waliwateka Maswahaba wawili wa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Kwa kuwa Banu ‘Aql walikuwa ni washirika

wa Banu Thaqiyf Maswahaba wakamteka mtu mmoja wa Banu ‘Aql. Makafiri walipowaachia nae Nabiyy (ﷺ) akamuachia huru waliyemteka.

[38] Huyu ni Swakhr bin Al-‘Aylah Al-Ahmas Abuu Haazim alikuwa ni Swahaba aliyepokea Hadiyih.

[39] Itakapokuwa Al-Harbi (mtu kutoka katika ardhi ya makafiri) atakaposilimu kwa khiyari yake, utajiri wake unabaki kwake. Ama akisilimu kwa nguvu ya kushindwa vita, maisha yake yatabakizwa lakini mali yake itagawiwa kama ni ngawira kwa wapiganaji.

[40] Ni pale Nabiyy (ﷺ) alipokua akirejea kutoka Twaaf baada ya kujeruhiwa huko, Al-Mutw’am bin ‘Adiyy alimuhifadhi na akawa anamhudumia. Hapa Nabiyy (ﷺ) anakumbuka fadhila zake.

[41] Ndoa zilizotanguliwa za wanawake wanaotekwa vitani, zimetanguka. Ikiwa mwanamke huyo ana mimba, inaruhusiwa kumingilia baada ya kujifungua. Kama hana mimba inafaa kumjamii baada ya kupita twahaarah moja. Hii bila ya kujali kuwa kasilimu au hajasilimu.

[42] Askari wa kuenda kwa miguu ana haki ya hisa moja katika mgawo wa ngawira, wakati askari wa farasi ana hisa tatu. Kamanda amepewa haki ya kumpa mpiganaji yeyote kutokana na uwezo alioonesha vitani.

[43] Kutoka kwa Ma’n bin Yazid bin Al-Akhnas As-Sulami alikuwa ni Swahaba na mtoto wa Swahaba. Alihudhuria ufunguzi wa Damascus na alikuwa akiishi katika mji wa Kufa uliopo ‘Iraq. Alikuenda Misri na kuenda kuishi Damascus. Alishiriki katika vita vya Marj Rahit akiwa na Adh-Dhahaq bin Qays mwaka 64 Hijriyyah. Aliuwawa katika vita hivyo. Inasemekana kuwa alikuwa akipenda kuwa na Mu’aawiyah katika vita alivyokuwa akipigana.

[44] Khumus ni moja ya tano ya mapato ya vita ambayo Allaah Amemuwekea Nabiyy wake Muhammad (ﷺ) pamoja na familia yake na kwa ajili ya Waislam wenye shida na fiy sabili LLaah

[45] Huyu ni Abuu ‘Abdir-Rahmaan Al-Fihri Al-Makki alikuwa ni Swahaba akijulikana kama Habiyy wa Roma kutokana na vita vingi alivyopigana huko. Alifariki Armenia katika mwaka 41 au 42 Hijriyyah akiwa kama gavana wa huko.

[46] Kiasi kikubwa walichopewa ilikuwa ni kwa sababu ya hatari kubwa iliyowakabili walipokuwa wakipigana na adui kwa mara ya pili, walipokuwa wakirejea katika ardhi za Waislam.

[47] Hadiyth hii inaonesha kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akigawa zawadi kwa baadhi ya watu.

[48] Moja ya tano (khumus) haichukuliwi kutoka katika chakula, hukusudiwa kuliwa na sio kuhifadhiwa. Kila mpiganaji anaweza na ana ruhusa kuchukuwa kabla hata ya mgawo wenyewe.

[49] Farasi na silaha zinazokamatwa zinaweza kutumika kisha zikarejeshwa kama ngawira. Vinginevyo, ni haraam kuvitumia. Baadhi ya ‘Ulamaa wana rai kuwa vitu hivi havifai kutumiwa hata kwa muda tu, ila kwa masharti ya kupata ruhusa maalum kutoka kwa Amiri jeshi.

[50] Hadiyth hii inaonesha sio tu Imaam mwenye uwezo wa kutoa haki ya amani. Muislam yoyote ana haki hiyo, iwe ni mwanamke au mwanamme, kijana kwa mtu mzima, tajiri kwa maskini, mpiganaji wa kawaida, kamanda wana haki ya kutoa haki hiyo ya kuwalinda na kuwapa amani wasio kuwa Waislam, ni heshima waliyopewa wote na shariy’ah. Hata Imaam hana haki ya kutengua haki ya kumlinda na kumpa amani mtu.

[51] Huyu alikuwa ni binti wa Abuu Twaalib Al-Hashimiy na dada wa ‘Aliy bin Abiy Twaalib. Jina lake lilikuwa ni Fakhita au Hind na alisilimu wakati wa Fat-h Makkah.

[52] Bara Arabuni ile sehemu ya ardhi iliyozunguka bahari ya Hindi, bahari ya kati na mito ya Tigri na Furati. Kwa urefu wake inaelekea hadi ‘Aden hadi Syria. Kwa upana wake, kutoka Jeddah hadi ‘Iraq. Watu wengine wanadhani kuwa Bara Arabu lina maana ya Hijazi iliyokusanya Makkah, Madiynah na Yamama, Taif na pembezoni mwake tu. Hili ndilo haswa maana ya eneo la Hijaaz lilivyokuwa likitumika huko nyuma. Kwa

hivyo ilikuwa kujulikana kuwa kuwafukuza Mayahudi katika bara lote na haswa zaidi katika eneo la Hijaaz.

[53] Wapiganaji hawana hisia katika Fai - mali iliyotekwa na Waislaam bila ya kupigana. Wakati wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hadi wakati wa Makhalifa kufuatana na maelekezo ya Shariy'ah, walikuwa wakigawa mali hii katika matumizi ya nyumba ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na jamaa wa karibu na Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Kadhalika mayatima, maskini, wasafiri na katika njia ya Allaah. Mali inayobaki hutumika kununulia silaha pamoja na farasi kwa ajili ya maandalizi ya vita.

[54] Hadiyth hii inaashiria kuwa kuvunja mkataba uliowekwa wa kivita kisha kuwakamata makafiri hairuhusiwi. Kisa cha suala hili linarudi kwa Abuu Raafi' (muachwa huru wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)) alikuenda kwa Nabiyy kabla hajasilimu, kama ni mjumbe aliyetumwa na makafiri. Mara tu alipomuona Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasilimu. Kisha akamtaka Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kumkataza asirudi kule na kubaki, kwani hakutaka kurudi kwa makafiri tena. Baada ya Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kusikia haya ndipo aliposema Hadiyth hii.

[55] Mji wa kwanza ambao haukupiganwa vita. Hisa za wapiganaji wanazopata katika mji huo ni sawa na za Waislam wengine. Mji wa pili ni ule ambao mapigano yalifanyika. Moja ya tano ya ngawira inayopatikana inabidi itolewe kwanza, kisha baada ya hapo igawiwe kwa wapiganaji.

02-Mlango Wa Jizya Na Kusitisha Vita

بَابُ الْجِزْيَةِ وَالْهُدْنَةِ

02-Mlango Wa Jizya Na Kusitisha Vita[1]

1122.

عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَوْفٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَخَذَهَا يَغْنِي: الْجِزْيَةُ مِنْ مَجُوسِ هَجَرَ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ وَلَهُ طَرِيقٌ فِي "الْمَوْطَأِ" فِيهَا انْقِطَاعُ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Awf amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alichukua Jizya kutoka kwa Majusi wa Hajar.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]. Nayo ina njia nyingine iliyopokewa katika kitabu cha Al-Mawtwa ambayo ni Munqatwi’.

1123.

وَعَنْ عَاصِمِ بْنِ عُمَرَ، عَنْ أَنَسٍ، وَعَنْ عُثْمَانَ بْنِ أَبِي سُلَيْمَانَ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعَثَ خَالِدَ بْنَ الْوَلِيدِ إِلَى أَكْيَدِرِ دَوْمَةَ، فَأَخَذُوهُ ، فَحَقَنَ دَمَهُ، وَصَالَحَهُ عَلَى الْجِزْيَةِ } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Aaswim[2] bin ‘Umar naye kutoka kwa Anas na kutoka kwa ‘Uthmaan bin Abiy Sulaymaan[3] amesema kuwa: “Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimtuma Khaalid bin Al-Waliyd aende kwa Ukaydir Duwmah,[4] wakamchukua, wakamleta kwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) naye akahifadhi damu yake na

akasuluhishiana naye kwa kutoa Jizya.” [Imetolewa na Abuu Daawuud]

1124.

وَعَنْ مُعَاذِ بْنِ جَبَلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {بَعَثَنِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِلَى الْيَمَنِ، وَأَمَرَنِي أَنْ أَخُذَ مِنْ كُلِّ حَالِمٍ دِينَارًا، أَوْ عَدْلَهُ مَعَافِرِيًّا} أَخْرَجَهُ الثَّلَاثَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Mu’aadh bin Jabal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alinituma Yemen akaniamrisha nichukue dinari moja (Jizya)[5] kwa kila aliyebaleghe au kinacholingana na dinari katika nguo za makafiri.”[6] [Imetolewa na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

1125.

وَعَنْ عَائِذِ بْنِ عَمْرٍو الْمُزْنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {“الْإِسْلَامُ يَغْلُو، وَلَا يُغْلَى”} أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaidh bin ‘Amr Al-Muzaniyy[7] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Uislamu unakuwa juu wala haukaliwi juu.”[8] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniy]

1126.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { " لَا تَبْدُؤُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى بِالسَّلَامِ، وَإِذَا لَقِيتُمْ أَحَدَهُمْ فِي طَرِيقٍ، فَاضْطَرُّوهُ إِلَى أَضْيَقِهِ " } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msianze kuwasalimia Mayahudi na Manaswaara[9] mtakapokutana na mmoja wao njiani msongeni kwenye dhiki zaidi.” [Imetolewa na Muslim]

1127.

وَعَنْ الْمِسْوَرِ بْنِ مَخْرَمَةَ. وَمَرْوَانَ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ خَرَجَ عَامَ الْحُدَيْبِيَّةِ. فَذَكَرَ الْحَدِيثَ بِطَوْلِهِ، وَفِيهِ: " هَذَا مَا صَالَحَ عَلَيْهِ مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ سُهَيْلُ بْنُ عَمْرٍو: عَلَى وَضْعِ الْحَرْبِ عَشْرَ سِنِينَ، يَأْمَنُ فِيهَا النَّاسُ، وَيَكْفُ بَعْضُهُمْ عَنْ بَعْضٍ " } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَأَصْلُهُ فِي الْبُخَارِيِّ

وَأَخْرَجَ مُسْلِمٌ بَعْضَهُ مِنْ حَدِيثِ أَنَسٍ، وَفِيهِ: { أَنَّ مَنْ جَاءَ مِنْكُمْ لَمْ نَرُدَّهُ عَلَيْكُمْ، وَمَنْ جَاءَكُمْ مِنَّْا رَدَدْتُمُوهُ عَلَيْنَا. فَقَالُوا:

أَنْكُتُبُ هَذَا يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: "نَعَمْ. إِنَّهُ مِنْ ذَهَبٍ مِّنَّا إِلَيْهِمْ فَأَبْعَدَهُ اللَّهُ، وَمَنْ جَاءَنَا مِنْهُمْ، فَسَيَجْعَلُ اللَّهُ لَهُ فَرْجًا وَمُخْرَجًا"

Kutoka kwa Al-Miswari bin Makhramah na Marwaan[10] wamesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alitoka mwaka wa vita vya Hudaybiyah... akataja Hadiyth kwa urefu wake: “Hivi ndivyo[11] Muhammad bin ‘Abdillaah alivyosulihishana na Suhayl bin ‘Amr[12] juu ya kuacha vita kwa muda wa miaka kumi ndani yake watu watakuwa na amani, na baadhi yao watajizuia kushambulia wengine.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na asili yake imo katika Al-Bukhaariy]

Na Muslim amepokea baadhi yake kutoka katika Hadiyth ya Anas: “Anayetujia kutoka kwenu, sisi hatumrudishi na atakayewajia nyinyi miongoni mwetu mutamrudisha kwetu. Maswahaba wakamuuliza: ‘Unaandika hili Ee Rasuli wa Allaah! Akasema ndiyo. Atakayewaendea wao miongoni mwetu, Allaah Amuepushe na Rahmah Zake, na atakayetujia sisi miongoni mwao, basi Allaah Amjaalie faraja na pa kutokea.”

1128.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو ، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "مَنْ قَتَلَ مُعَاهِدًا لَمْ يَرَحْ رَائِحَةَ الْجَنَّةِ، وَإِنَّ رِيحَهَا لِيُوجَدَ مِنْ مَسِيرَةِ أَرْبَعِينَ عَامًا" } أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Abdillaah bin ‘Amr amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kumuua Mu’aahid,[13] hatanusa harufu ya Al-Jannah, kwa hakika harufu yake husikika

masafa ya mwendo wa maisha arubaini.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

[1] Jizya ni kodi ya kichwa inayopatikana kutokana na kodi zinazolipwa na wasio kuwa Waislamu wanaoishi katika dola ya Kiislamu. Fedha hizo ambazo zinatumika katika usalama na ulinzi wao wenyewe na mahitaji ya jamii kwa ujumla. Ama Hudna ni mikataba ya amani ya muda ya kusitisha vita.

[2] Huyu ni Abuu 'Umar 'Aaswim bin 'Umar bin Qataadah bin An-Nu'maan Al-Answaar alikuwa ni madhubuti. Taabi' ambaye amepokea Hadiyth nyingi. Elimu yake ni hazina kubwa. Wametofautiana wengi kuhusu mwaka wa kifo chake, tarehe zifuatazo zimerikodiwa kuhusu mwaka wa kifo chake, 119 Hijriyyah, 120, 121, 127 na 129 Hijriyyah.

[3] 'Uthmaan bin Abiy Sulaymaan bin Jubayr bin Mut'im alikuwa ni Qadhi wa Makkah; Ahmad, Ibn Ma'in na Abuu Haatim wanamzingatia kuwa ni madhubuti.

[4] Duwmah Al-Jandal lilikuwa ni ngome karibu na Tabuwk lililokuwa likikaliwa na Ukaydir ambaye alikuwa ni mkristo, tukio hili lilitokea mwaka wa 9 Hijriyyah, wakati wa harakati za kuenda Tabuwk.

[5] Jizya zipo za aina mbili: ya binafsi, na ya pamoja. Ikiwa ni kutoka kwa mtu binafsi basi inawahusu wote maskini na tajiri. Kiwango cha chini kwa mwaka kutoka kwa mtu binafsi ni dinari moja. Hata hivyo, watoto na wale bado hawajawa watu wazima hawalipi. Kodi nyinginezo zitakazokatwa na serikali zinatakiwa ziwe juu ya kiwango hicho na si chini ya hapo. Ikiwa wasio kuwa Waislam wakaamua kulipa kwa pamoja basi kodi hiyo itatakiwa kutoka kwa matajiri peke yao tu.

[6] Hizi ni nguo zinazotengenezwa Yemen.

[7] Huyu ni Abuu Hubayrah aliyekuwa akikaa Basra, alikuwa miongoni mwa Maswahaba. Alihudhuria Bay'atur-Ridhwaan na alifariki wakati wa ukhalifa wa Yazid bin Mu'aawiyah.

[8] Hadiyth hii imetajwa kama ni kitangulizi cha kuweka mkataba. Hata kama kuna kipengele kimoja kinaonekana kuwa kiko dhidi ya maslahi ya Waislam basi watu wasivunjike moyo, kwani Allaah ndiye Atakayeunusuru Uislam.

[9] Hadiyth hii iko wazi inaonyesha kuwa Muislam hatakiwi kuanza kuwasalimia kwa “As-Salaam ‘alaykum” na Muislam anatakiwa amdhiki Myahudi na Mnaswaara akiwa njiani.

[10] Marwaan bin Al-Hakam Al-Umawl alikuwa ni baba wa ‘Abdul Maalik (Khalifa). Alikuwa gavana wa Madiynah wakati wa Mu’aawiyah. Alishindana na ‘Abdullaah bin Az-Zubayr katika ukhalifa baada ya kufa kwa Yazid na kung’atuka kwa mtoto wa Mu’aawiyah. Aliteka Misri na Shaam. Alikufa Damascus katika mwaka 65 Hijriyyah.

[11] Hii inaonesha ushariy’ah wa mkataba waliowekeana baina ya Waislam na wasio kuwa Waislam. Inaeleza pia kuwa Amiri ana uwezo wa kuendelea na kusaini mkataba ambao anaona kuwa utakuwa na faida na Waislam kwa siku za usoni.

[12] Alikuwa katika watukufu wa ki-Qurayshi, alikuwa ni mtu mwenye hikmah, mshairi na kiongozi. Alikamatwa katika vita vya Badr akiwa bado ni kafiri, alisilimu katika Fat-h ya Makkah. Maquraysh walibaki wakiwa Waislam wakati wa Ar-Ridda (fitna za baadhi kuritadi) kutokana na yeye Suhayl kuwashauri. Inasemekana alikufa katika vita vya Yarmuk katika mwaka 14 Hijriyyah. Mapokezi mengine yanasema kuwa alikufa katika Marj As-Safr au katika ugonjwa wa tauni wa Amwaas mwaka 18 Hijriyyah.

[13] Mu’aahid ni kafiri anayeishi nje ya mipaka ya dola ya Kiislam na ambaye amepata ruhusa ya kuishi katika dola ya Kiislam. Kumuuwa Mu’aahid ni suala zito kwa maana ya matokeo yake kwani hutoa jina baya la Uislam nje. Kumuuwa Mu’aahid ni haraam kwa mujibu wa kongomano la ‘Ulamaa wote.

03-Mlango Wa Mashindano Ya Farasi Na Kurusha Mishale

بَابُ السَّبْقِ وَالرَّمْيِ

03-Mlango Wa Mashindano Ya Farasi Na Kurusha Mishale

1129.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {سَابَقَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِالْخَيْلِ الَّتِي قَدْ أُضْمِرَتْ، مِنَ الْحَفِيَاءِ، وَكَانَ أَمْدُهَا ثَنِيَّةَ الْوَدَاعِ. وَسَابَقَ بَيْنَ الْخَيْلِ الَّتِي لَمْ تُضْمَرْ مِنَ الثَّنِيَّةِ إِلَى مَسْجِدِ بَنِي زُرَيْقٍ، وَكَانَ ابْنُ عُمَرَ فِيهِمَا سَابِقٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ زَادَ الْبُخَارِيُّ، قَالَ سُفْيَانُ: مِنَ الْحَفِيَاءِ إِلَى ثَنِيَّةِ الْوَدَاعِ خَمْسَةَ أَمْيَالٍ، أَوْ سِتَّةَ، وَمِنْ الثَّنِيَّةِ إِلَى مَسْجِدِ بَنِي زُرَيْقٍ مِيلٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alishindanisha farasi[1] wepesi (wa kukimbia) kutoka Hafyaa mpaka Thaniyyah Al-Wadaa’.[2] Ambao siyo wepesi akawashindanisha Thaniyyah Al-Wadaa’ mpaka katika Msikiti wa Baniy Zurayq. Na Ibn ‘Umar alikuwa miongoni mwa walioshindanishwa.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Al-Bukhaariy ameongeza: “Sufyaan amesema: “Kutoka Hafyaa'i hadi Thaniyyah Al-Wadaa' ni maili tano au sita. Na kutoka Thaniyyah hadi Msikiti wa Baniy Zurayq ni maili moja.”

1130.

وَعَنْهُ، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَبَقَ بَيْنَ الْخَيْلِ، وَفَضْلِ الْقَرْحُ فِي الْغَايَةِ } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn 'Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alishindanisha farasi, akaweka kikomo ni kwa farasi anayekimbia masafa marefu zaidi.” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1131.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "لَا سَبَقَ إِلَّا فِي خُفٍّ، أَوْ نَصْلٍ، أَوْ حَافِرٍ" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالثَّلَاثَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna mashindano ila katika farasi au kulenga shabaha au ngamia.”[3] [Imetolewa na Ahmad na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1132.

وَعَنْهُ، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "مَنْ أَدْخُلَ
فَرَسًا بَيْنَ فَرَسَيْنِ وَهُوَ لَا يَأْمَنُ أَنْ يَسْبِقَ فَلَا بَأْسَ بِهِ، وَإِنْ
أَمِنَ فَهُوَ قِمَارٌ" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَإِسْنَادُهُ ضَعِيفٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye
kumuingiza farasi mashindanoni[4] baina ya farasi wawili na
haijulikani kama atashindwa, basi hapana ubaya. Na kama
itajulikana (kama atashindwa) hiyo ni kamari.”[5] [Imetolewa na
Ahmad na Abuu Daawuwd na isnaadi yake ni Dhwaiyf]

1133.

وَعَنْ عَقَبَةَ بْنِ عَامِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَهُوَ عَلَى الْمِنْبَرِ يَقْرَأُ: (وَأَعِدُّوا
لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ) "أَلَا إِنَّ الْقُوَّةَ الرَّمْيُ، أَلَا إِنَّ الْقُوَّةَ
الرَّمْيُ، أَلَا إِنَّ الْقُوَّةَ الرَّمْيُ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aqabah bin ‘Aamir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema:
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) “Nilimsikia Rasuli wa Allaah
akisema naye yuko juu ya minbar: “Na waandalieni nguvu zozote
mziwezazo na farasi waliofungwa tayari (kwa vita)...” [Al-Anfaal:
60] mpaka mwisho wa Aayah (kisha akasema): “Jueni kuwa, nguvu
ni kurusha mishale, jueni kuwa, nguvu ni kurusha mishale, jueni
kuwa, nguvu ni kurusha mishale.”[6] [Imetolewa na Muslim]

[1] Hadiyth hii inaonyesha uhalaali wa kushindanisha farasi. Hata hivyo cha kuangalia ni nguvu na umri wa farasi ni vizuri ukatiliwa maanani katika kuwashindanisha. Farasi wa kawaida anaweza kukimbia maili moja kwa hadhari wakati farasi aliyefundishwa anaweza kukimbia kwa urefu wa maili tano bila matatizo.

[2] Njia ya mlimani karibu na Madiynah kuelekea Al-‘Aqabah.

[3] Hili linajulisha kuwa mashindano na zawadi inakuwa kwa kuwashindanisha ngamia na farasi kwa sharti kwamba zawadi itakayotolewa ni kutoka kwa mmoja wa washindani, kulingana na ‘Ulamaa wengi. Kama zawadi itatolewa na wasio kuwa washindani (mtu au kundi la nje) hakuna tofauti katika uhalaali wake.

[4] Lengo la mashindano ya farasi ni kupima nguvu na uwezo wa farasi wa kukimbia, ama suala la zawadi ni jambo linalofuatia tu lakini si la msingi. Ikiwa masharti ya mashindano ni kuwashindanisha kwa msingi ufuatao, “Ikiwa farasi wake atashinda nitakulipa shilingi elfu kumi au farasi wangu atakuwa wako, au useme kinyume chake. ‘unilipe elfu kumi au farasi wako awe wangu’.” Katika hali kama hii hairuhusiwi na imekataliwa na ‘Ulamaa wengi. Ikiwa mashindano yamesimama kwa sharti la upande mmoja tu kwa kusema: “Nitakulipa elfu ishirini, ikiwa farasi wako atashinda.” Kitu hiki ni halaal (kulingana na rai za ‘Ulamaa wengi). Kingine kinachoruhusiwa ni maelekezo yafuatayo: ‘Nitamlipa atakayeshinda kiasi kadha’.

[5] Ikiwa inafahamika kuwa farasi fulani atashinda kwa hali yoyote ile, basi hairuhusiwi kushindana kwa sababu tu ya kupata zawadi.

[6] Kutupa mishale ndio iliyokuwa silaha kuu ya wakati ule. Katika hali yetu leo hii unaweza kulinganisha na silaha za kisasa na silaha za kijeshi zinazotumia teknolojia ya hali ya juu iliyokuwa na nguvu zaidi.

كِتَابُ الْأَطْعِمَةِ

Kitabu Cha Vyakula

12- Buluwgh Al-Maraam: Kitabu Cha Vyakula - كِتَابُ الْأَطْعِمَةِ

00-Kitabu Cha Vyakula

1134.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "كُلْ ذِي نَابٍ مِنَ السَّبَاعِ، فَأَكَلَهُ حَرَامٌ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ وَأَخْرَجَهُ: مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عَبَّاسٍ بِلَفْظٍ: نَهَى. وَزَادَ: { "وَكُلْ ذِي مَخْلَبٍ مِنَ الطَّيْرِ" }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kila mnyama mwenye kuwinda kwa meno, kumla kwake ni haraam.”[1] [Imetolewa na Muslim]

Pia amepokea kutoka katika hadiyth ya ‘Abdullaah ibn ‘Abbaas kwa tamshi hili: “Amekataza.” Na akaongeza: “Na kila ndege anayewinda kwa kucha.”

1135.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ خَيْبَرَ عَنْ لُحُومِ الْحُمْرِ الْأَهْلِيَّةِ، وَأَذْنٍ فِي لُحُومِ الْخَيْلِ {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ. وَفِي لَفْظِ الْبُخَارِيِّ: {وَرَخَّصَ {

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza nyama za punda kihongwe (wa mjini)[2] siku ya Vita vya Khaybar, akaruhusu nyama za farasi.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

Na katika tamshi la Bukhaariy: “Na ameruhusu.”

1136.

وَعَنْ ابْنِ أَبِي أَوْفَى قَالَ: {غَزَوْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَبْعَ غَزَوَاتٍ، نَأْكُلُ الْجَرَادَ {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn Abiy Awfaa amesema: “Tumepigana pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) vita saba, tunakula nzige.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1137.

وَعَنْ أَنَسٍ فِي قِصَّةِ الْأَرْزَبِ {قَالَ: فَذَبَحَهَا، فَبَعَثَ بِوَرِكَيْهَا إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَبِلَهُ {مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas katika kisa cha sungura: “...akamchinja, akampelekea Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) paja lake naye akalikubali.”[3] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1138.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ قَتْلِ أَرْبَعٍ مِنَ الدَّوَابِّ: النَّمْلَةُ، وَالنَّحْلَةُ، وَالْهُدُودُ، وَالصُّرَدُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kuuwa wanyama wanne sisimizi, nyuki, hudihudi na kipwe (ndege).” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1139.

وَعَنْ ابْنِ أَبِي عَمَّارٍ قَالَ: {قُلْتُ لِحَبِيبِ بْنِ أَبِي عَمَّارٍ: أَلَمْ يَنْهَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ قَتْلِ أَرْبَعٍ مِنَ الدَّوَابِّ: النَّمْلَةَ، وَالنَّحْلَةَ، وَالْهُدُودَ، وَالصُّرَدَ؟} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ وَصَحَّحَهُ الْبُخَارِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn Abiy ‘Ammar[4] amesema: “Nilimuuliza Jaabir fisi analiwa? Akasema Ndiyo.[5] Nikasema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema hivyo? Akasema ndiyo.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha Al-Bukhaariy na Ibn Hibbaan]

1140.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ ، أَنَّهُ سُئِلَ عَنْ الْقَنْفُذِ ، فَقَالَ : (قُلْ لَا أَجِدُ فِي مَا أُوْحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلَى طَاعِمٍ) فَقَالَ شَيْخٌ عِنْدَهُ :

سَمِعْتُ أَبَا هُرَيْرَةَ يَقُولُ: {ذَكَرَ عِنْدَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: خِبْنَةُ مِنَ الْخَبَائِثِ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَإِسْنَادُهُ ضَعِيفٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Aliulizwa kuhusu nungu akasema kwa kusoma Aayah hii: (Sema: Sipati katika yale niliyofunuliwa Wahyi kwangu kilichoharamishwa kwa mlaji...) Qur-aan 6: 145. Mzee mmoja aliye kwake akasema: ‘Nilimsikia Abuu Hurayrah anasema alitajwa mbele ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) akasema: “Ni mchafu miongoni mwa vichafu’.” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud na isnaad yake ni dwaifu]

1141.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ الْجَلَّالَةِ وَالْبَانِيهَا} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيَّ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza kula mnyama anayekula uchafu na kunywa maziwa yake.”[6] [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy, na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

1142.

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {فِي قِصَّةِ الْحِمَارِ الْوَحْشِيِّ فَأَكَلَ مِنْهُ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abiy Qataadah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema katika kisa cha punda milia: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamla.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1143.

وَعَنْ أَسْمَاءِ بِنْتِ أَبِي بَكْرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: {نَحَرْنَا عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَرَسَاءً، فَأَكْلَنَاهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Asmaa bint Abiy Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Katika zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) tulichinja farasi na tukamla.”[7] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1144.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {أَكُلَّ الضَّبَّ عَلَى مَائِدَةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Kenge aliliwa katika meza ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).”[8] [Al-Bukhaariy, Muslim]

1145.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عُثْمَانَ الْقُرَشِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ طَبِيبًا سَأَلَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ الضَّفْدَعِ يَجْعَلُهَا فِي دَوَاءٍ، فَنَهَى عَنْ قَتْلِهَا} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdir-Rahmaan bin ‘Uthmaan Al-Qurashiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Kuwa tabibu mmoja alimuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuhusu chura kumfanya dawa. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akakataza kuuwa chura.”[9]
[Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Al-Haakim]

[1] Hadiyth hii inatoa maelezo kwamba kila mnyama mwenye kula mnyama na mwenye chonge ni haraam kuliwa. Vivyo kwa ndege anayenyofoa kiwindwa chake na kutumia ukucha ndege wa aina hiyo ni haraam kuliwa.

[2] Punda wa porinini (Pundamilia) ni halaal kuliwa.

[3] Sungura ni halaal kwa mujibu wa ‘Ulamaa wengi.

[4] Huyu ni ‘Abdur-Rahmaan bin ‘Abdillaah bin Abuu ‘Ammmaar Al-Qurayshiy Al-Makkiy. Alikuwa ni Mwenye Taqwa na An-Nasaaiy anamthibitisha kuwa ni madhubuti.

[5] Hadiyth inaonesha kuwa kumla fisi kumeruhusiwa. Kulingana na baadhi ya Maimaam (kama vile Shaafi’y) ni halaal. Wengine kama Hanafiy wanaona kuwa ni haraam. Sababu ya kuwa kwake ni haraam ni kuwa anapenda kula nyama ya mwana Adam na kuichimbia chini.

[6] Katika lugha ya Kiarabu Jallaala ina maana ya wanyama wenye kula kwenye vinyaa, uchafu, awe mnyama huyo ni ngamia jike, ng’ombe au mbuzi. Hata ikiwa ni halaal kutumia nyama au maziwa yake, hili ni jambo lenye tofauti ya rai kati ya Wanazuoni tokea awali. Baadhi ya Wanazuoni wanaona kwamba ni halaali na wengine wakiona kuwa ni haraam. Mnyama ataonekana kuwa ni Jallaala ikiwa kiasi kikubwa cha chakula chake ni uchafu wa mwana Adam. Ama ikiwa kiwango kikubwa cha chakula chake ni kinachoruhusiwa basi hatoingia katika kundi hili la Jallaala.

[7] Kuna Hadiyth iliyotangulia kabla ya hii ikisisitiza kuwa kula farasi ni halaal. Na hadiyth hii inathibitisha jambo hilo hilo.

[8] Tunajifunza katika baadhi ya Hadiyth kuwa Dhabbu (mburukenge) analiwa, pamoja na kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mwenyewe hakumla, lakini Maswahaba wake walimla mbele yake katika meza yake. Alialikwa kumla lakini hakushiriki. Hakuwakataza watu kumla. Wanazuoni wanataja katika maandiko yao kuwa ni chukizo la Tanzihi (vile vilivyokuwa chini ya daraja la makatazo).

[9] Tunajifunza katika Hadiyth hii kuwa ni haraam kuuwa chura na kadhalika kumla.

01-Mlango Wa Kuwinda Na Kuchinja

بَابُ الصَّيْدِ وَالذَّبَائِحِ

01-Mlango Wa Kuwinda Na Kuchinja

1146.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "مَنْ اتَّخَذَ كَلْبًا، إِلَّا كَلْبَ مَاشِيَةٍ، أَوْ صَيْدٍ، أَوْ زَرْعٍ، انْتَقَصَ مِنْ أَجْرِهِ كُلِّ يَوْمٍ قِيرَاطٌ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kufuga mbwa isipokuwa mbwa wa kuwinda au wa mifugo au wa kulima[1]

hakika kila siku anapunguziwa Qiyaatw kutoka katika ujira wake.”
[Al-Bukhaariy, Muslim]

1147.

وَعَنْ عَدِيِّ بْنِ حَاتِمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ لِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "إِذَا أُرْسِلْتَ كَلْبَكَ فَادْكُرْ اسْمَ اللَّهِ، فَإِنْ أَمْسَكَ عَلَيْكَ فَادْكُتْهُ حَيًّا فَادْبَحْهُ، وَإِنْ أَدْرَكَتْهُ قَدْ قُتِلَ وَلَمْ يُؤْكَلْ مِنْهُ فَكُلْهُ، وَإِنْ وَجَدْتَ مَعَ كَلْبِكَ كَلْبًا غَيْرَهُ وَقَدْ قُتِلَ فَلَا تَأْكُلْ: فَإِنَّكَ لَا تَدْرِي أَيُّهُمَا قَتَلَهُ، وَإِنْ رَمَيْتَ سَهْمَكَ فَادْكُرْ اسْمَ اللَّهِ، فَإِنْ غَابَ عَنْكَ يَوْمًا، فَلَمْ تَجِدْ فِيهِ إِلَّا أَثَرَ سَهْمِكَ، فَكُلْ إِنْ شِئْتَ، وَإِنْ وَجَدْتَهُ غَرِيقًا فِي الْمَاءِ، فَلَا تَأْكُلْ " } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَهَذَا لَفْظُ مُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Adiyy bin Haatim[2] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisema: “Unapomtuma mbwa wako, taja jina la Allaah[3] juu yake, akikukamatia (mnyama) nawe ukamkuta hai, basi mchinje na ukikuta ameuwa naye hakula chochote humo, basi kula, na ukikuta pamoja na mbwa wako kuna mbwa mwingine naye ameuwa basi usile, kwani hujui ni yupi aliyemuwa. Na utakaporusha mshale wako taja Jina la Allaah. Itakapokupotea siku moja na (ukalipata halafu) usikute ila athari ya mshale wako, kula ukipenda. Na atakapompata ameghariki kwenye maji, usile.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

1148.

وَعَنْ عَدِيِّ قَالَ: {سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ صَيْدِ الْمِعْرَاضِ فَقَالَ: "إِذَا أَصَبْتَ بِحَدِّهِ فَكُلْ، وَإِذَا أَصَبْتَ بِعَرْضِهِ، فُقُتِلْ، فَإِنَّهُ وَقِيدٌ، فَلَا تَأْكُلْ"} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Adiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilimuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kuhusu kuwinda kwa Mi’raadhw (mshale). Akasema: ‘Utakapolenga katika ukali wake,[4] kula na utakapolenga kwa ubavu wake na ikauwa, basi mnyama huyo ni mawquwdha[5] usile.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1149.

وَعَنْ أَبِي ثَعْلَبَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "إِذَا رَمَيْتَ بِسَهْمِكَ، فَغَابَ عَنْكَ، فَأَذْرَكْتَهُ فَكُلْهُ، مَا لَمْ يُنْتِنْ" } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abiy Tha’labah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Utakaporusha mshale wako ukakupotea[6] ukaukuta (umeua windo), basi lile maadam halikuvunda harufu mbaya.” [Imetolewa na Muslim]

1150.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، {أَنَّ قَوْمًا قَالُوا لِلنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِنَّ قَوْمًا يَأْتُونَنَا بِاللَّحْمِ، لَا نَدْرِي أَذْكَرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ أَمْ لَا؟ فَقَالَ: " سَمُّوا اللَّهَ عَلَيْهِ أَنْتُمْ، وَكُلُّوهُ" } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Watu walimuambia Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) watu wanatujia na

nyama hatujui kama wametaja Jina la Allaah juu yake ama hawakutaja? Nabiyy (ﷺ) akasema: ‘Nyinyi tajeni Jina la Allaah juu yake na muile.’[7] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1151.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مُغَفَّلٍ الْمُزْنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَهَى عَنِ الْخُذْفِ، وَقَالَ: "إِنَّهَا لَا تَصِيدُ صَيْدًا، وَلَا تَنَكُّ عَدُوًّا، وَلَكِنَّهَا تَكْسِرُ السِّنَّ، وَتَفْقَأُ الْعَيْنَ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ. وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ

Kutoka kwa ‘Abdillaah bin Mughaffal Al-Muzaniyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (ﷺ) amekataza mtu kurusha kijiwe na akasema: ‘Kwani kurusha kijiwe[8] hakuwindi windo wala hakuui adui, lakini huvunja jino na kupofua.’ [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

1152.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "لَا تَتَّخِذُوا شَيْئًا فِيهِ الرُّوحُ غَرَضًا" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (ﷺ) amesema: “Msichukue kitu chenye roho kulengea shabaha.” [Imetolewa na Muslim]

1153.

وَعَنْ كَعْبِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ امْرَأَةً ذَبَحَتْ شَاةً بِحَجَرٍ، فَسُئِلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ ذَلِكَ، فَأَمَرَ بِأَكْلِهَا } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ka'b bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: "Mwanamke mmoja alichinja mbuzi kwa jiwe. Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akaulizwa kuhusu hilo akaamuru kuliwa kwake." [9] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1154.

وَعَنْ رَافِعِ بْنِ خَدِيجٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "مَا أَنْهَرَ الدَّمَ، وَذَكَرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ، فَكُلْ لَيْسَ أَلْسَنَ وَالظُّفْرَ، أَمَّا أَلْسَنُ، فَعَظْمٌ، وَأَمَّا الظُّفْرُ: فَمُدَى الْحَبَشِ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Raafi' bin Khadiyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) amesema: "Kinachomwaga damu na Jina la Allaah likatajwa juu yake, kula. Isipokuwa jino na kucha. [10] Ama jino ni mfupa. Na ama kucha ni kisu cha Wahabeshi." [Al-Bukhaariy, Muslim]

1155.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يُقْتَلَ شَيْءٌ مِنَ الدَّوَابِّ صَبْرًا } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amekataza mnyama kuuwawa kwa kutesa.”[11] [Imetolewa na Muslim]

1156.

وَعَنْ شَدَّادِ بْنِ أَوْسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "إِنَّ اللَّهَ كَتَبَ الْإِحْسَانَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ، فَإِذَا قَتَلْتُمْ فَأَحْسِنُوا الْقِتْلَةَ، وَإِذَا ذَبَحْتُمْ فَأَحْسِنُوا الذَّبْحَةَ، وَلْيُحِدَّ أَحَدُكُمْ شَفْرَتَهُ، وَلْيُرِخْ ذَبِيحَتَهُ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Shaddaad bin Aws (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Allaah Ameandika hisani juu yake kila jambo. Mnapouwa, uweni kwa namna nzuri, na mnapochinja chinjeni kwa uzuri. Mmoja wenu akinoe kisu chake na amuondolee mashaka mnyama anayemchinja.” [12] [Imetolewa na Muslim]

1157.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "ذَكَاةُ الْجَنِينِ ذَكَاةُ أُمِّهِ" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abiy Sa’iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kumchinja mtoto tumboni ni kwa kumchinja mama yake.”[13] [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1158.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "الْمُسْلِمُ يَكْفِيهِ اسْمُهُ، فَإِنْ نَسِيَ أَنْ يُسَمِّيَ حِينَ يَذْبَحُ، فَلْيُسَمِّ، ثُمَّ لِيَأْكُلْ" } أَخْرَجَهُ الدَّارَقُطْنِيُّ، وَفِي إِسْنَادِهِ مُحَمَّدُ بْنُ يَزِيدَ بْنِ سِنَانَ، وَهُوَ صَدُوقٌ ضَعِيفُ الْحِفْظِ

وَأَخْرَجَهُ عَبْدُ الرَّزَّاقِ بِإِسْنَادٍ صَحِيحٍ إِلَى ابْنِ عَبَّاسٍ، مَوْقُوفًا عَلَيْهِ وَلَهُ شَاهِدٌ عِنْدَ أَبِي دَاوُدَ فِي "مَرَّاسِيلِهِ" بِلَفْظٍ: { "ذَبِيحَةُ الْمُسْلِمِ حَلَالٌ، ذَكَرَ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا أَوْ لَمْ يَذْكُرْ" } وَرِجَالُهُ مُوْتَقُونَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muislam linamtosha jina lake, akisahau BismiLLaah wakati wa kuchinja, basi aseme BismiLLaah kisha ale.”[14] [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy]

Katika Hadiyith hii kuna mpokezi hifadhi yake ni dhaifu ambaye ni Muhammad bin Yaziyd bin Sinaan[15] ni mkweli mwenye udhaifu wa kuhifadhi.

Abdur-Razzaaq ameipokea kwa isnaad sahihi ikinasibishwa kwa ‘Abdullaah bin ‘Abbaas ikiwa ni Marfuw’.

Ina ushahidi kwa Abuu Daawuwd katika Maraasil kwa tamshi: “Chinjo la Muislam ni halaal, ataje Jina la Allaah wakati wa kuchinja ama asitaje.” Wapokezi wake ni madhubuti.

[1] Kwa sababu zisizokuwa za kuwinda na kuchunga vitu, ni haraam kumfuga mbwa kama mnyama wa nyumbani. Qiraatw ni kitu chenye thamani kubwa.

[2] ‘Adiyy bin Haatim bin At-Ta’i na baba yake walikuwa mashuhuri kwa ukarimu wao. Alimtembelea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mwaka wa

7 Hijriyyah. Yeye pamoja na watu wake walithibitisha Uislam wao zaidi wakati wa Ar-Ridda. Zakkaah ya kwanza kumfikia Abuu Bakr ilikuwa kutoka kwa ‘Adiyy na watu wake. Alihudhuria ufunguzi wa Madain na alikuwa pamoja na ‘Aliy wakati wa vita vya Al-Jamaal, alifariki mwaka 120 Hijriyyah akiwa na miaka 68.

[3] Kuwinda kwa sababu ya kutafuta chakula au kuuza ni ruhusa. Ama ikiwa hilo linafanyika kwa sababu ya kutembea, kufurahi na kupoteza muda haitakiwi. Ni ruhusa kutumia mbwa au wanyama wengine kwa ajili ya kuwindia. Hata hivyo, kuna mambo mawili yanayotawala jambo hili: Kwanza unapomtuma mbwa wako unataja Jina la Allaah na pili, mbwa aliyetumwa anatakiwa yule aliyefundishwa kuwinda. Ikiwa mbwa yule kamla yule aliyemkamata anakuwa si halaal kwako kwani atakuwa amejiwindia na hakukuwindia.

[4] Moja katika hukumu ya uhalaal wa kuliwa kwa kiwindo ni kuwa ikiwa mnyama amekufa kwa kupigwa na kitu chenye ncha kali, basi ni halaal kuliwa ama ikiwa amekufa kwa kupigwa na kitu kikafa (kisichokuwa na ncha) usile kwani kitakuwa kimekufa kwa kupigwa.

[5] Yaani mnyama anayekufa kwa kupigwa na kitu kama vile fimbo au jiwe bila ya kuchinjwa.

[6] Ikiwa mnyama amepigwa mshale, kisha akakimbia usimuone na baadae ukakuta amekufa katika maji, hairuhusiwi kuliwa. Hata hivyo, ikiwa mnyama huyo huyo amepatikana akiwa hai, anatakiwa achinjwe. Ikiwa amekufa amelala chini na hana majeraha mengine zaidi ya mshale wako, ni halaal kumla. Ama akikutwa na jeraha lingine lisilokuwa la mshale wako basi ni haraam kumla.

[7] Hadiyth hii inatoa kanuni ya msingi kuwa mwana Aadam hakuna hakika kuwa nyama fulani si halaal, huna haja ya kusema kuwa si halaal maadamu huna hakika, na haswa zaidi ikiwa inatoka kwa Muislam.

[8] Hadiyth inaonesha kuwa vijiwe vinavyokusudiwa hapa ni vile vidogo visivyokuwa na manufaa.

[9] Mafundisho tuyapatayo katika Hadiyth hii yanaonesha kuwa ni halaal kwa mwanamke kuchinja kwa masharti kuwa: (a) Awe ni Muislam (b)

Kabla ya akuchinja ataje Jina la Allaah kwa kusema BismiLLaah Allaahu Akbar.

[10] Kitu chochote chenye ncha kali (mbali na ukucha, mfupa au meno) ambayo itafanya damu ya mnyama kutiririka katika mwili wake, ni halaal kutumika kuchinja.

[11] Katika lugha ya Kiarabu Swabr ina maana mbili: (a) kumuuwa mnyama kwa kumzuilia na maji au kufa kwa njaa, (b) Kumtumia mnyama kama kitu cha kulengea shabaha au kumtumia katika mazoezi ya kulenga shabaha. Yote haya ni haraam.

[12] Hata kama ni mtu anatakiwa kuuwawa basi anatakiwa auwawe kwa haraka bila kupata masumbuko yoyote ili afe kwa haraka.

[13] Hadiyth hii inaonesha kuwa kichanga kinafuata hukumu ya mama yake. Ikiwa mama ni halaal basi na kilicho ndani yake kinafuata hukumu hiyo. Ikiwa kichanga katika tumbo la mama ni hai basi atachinjwa kwa mujibu wa Wanazuoni.

[14] Ikiwa Muislam hakutaja Allaahu Akbar kwa makusudi wakati wa kuchinja basi nyama ile inakuwa ni haraam. Kama atakuwa amesahau basi ni halaal. Na hii ndio rai ya Wanazuoni.

[15] Huyu ni Abuu ‘Abdillaah alikuwa katika kabila la At-Tamiym. Abuu Haatim anamuelezea: ‘Hakuwa makini katika Hadiyth lakini pamoja na hayo alikuwa Mwenye Taqwa.’ Abuu Daawud anamuelezea: ‘Si wa kutegemewa’ na An-Nasaaiy anasema: ‘Hakuwa madhubuti.’ Ama Ibn Hibbaan amemtaja kuwa alikuwa Ath-Thiqah (kuwa alikuwa madhubuti). Alikufa mwaka 220 Hijriyyah.

02-Mlango Wa Kuchinja Udhw-hiyyah

بَابُ الْأَضَاجِ

02-Mlango Wa Kuchinja Udhw-hiyyah[1]

عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يُضْحِي بِكَبْشَيْنِ أَمْلَحَيْنِ أَقْرَنَيْنِ، وَيُسَمِّي، وَيُكَبِّرُ، وَيَضَعُ رِجْلَهُ عَلَى صِفَاحِهِمَا. وَفِي لَفْظٍ: ذَبَحَهُمَا بِيَدِهِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ. وَفِي لَفْظٍ: { سَمِينَيْنِ } وَلِأَبِي عَوَانَةَ فِي "صَحِيحِهِ": { ثَمِينَيْنِ }. بِالْمُثَلَّثَةِ بَدَلِ السَّيْنِ

وَفِي لَفْظٍ لِمُسْلِمٍ، وَيَقُولُ: { بِسْمِ اللَّهِ. وَاللَّهُ أَكْبَرُ } وَلَهُ: مِنْ حَدِيثِ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَمَرَ بِكَبْشٍ أَقْرَنٍ، يَطَأُ فِي سَوَادٍ، وَيَبْرُكُ فِي سَوَادٍ، وَيَنْظُرُ فِي سَوَادٍ، لِيُضْحِيَ بِهِ، فَقَالَ: "اشْحِذِي الْمُدِيَّةَ"، ثُمَّ أَخَذَهَا، فَأَضْجَعَهُ، ثُمَّ ذَبَحَهُ، وَقَالَ: "بِسْمِ اللَّهِ، اللَّهُمَّ تَقَبَّلْ مِنْ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَمِنْ أُمَّةٍ مُحَمَّدٍ" }

Kutoka kwa Anas bin Maalik (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: "Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akichinja kondoo wawili madume wa kijivu walio na pembe. Akipiga BismiLLaah na akipiga Takbiyr, na akiweka mguu wake juu ya pambizo za shingo zao. Katika tamshi lingine: "Aliwachinja kwa mkono wake." Katika tamshi lingine: "...walionona." Abuu 'Awaanah amepokea katika Swahiyh yake: "...wenye thamani kubwa."

Vile vile katika tamshi lingine la Muslim: "Na alikuwa akisema: BismiLLaah Wa-Allaahu Akbar."

Pia Muslim amepokea kutoka kwa Hadiyth ya 'Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا): "Ameamrisha kondoo mwenye pembe, mwenye miguu nyeusi, mwenye tumbo leusi, na kando ya macho yake ni weusi pia. Akaletewa ili amchinje, akamuambia 'Aaishah: 'Ee 'Aaishah niletee kisu' kisha akaniambia: 'Kinoe kwa jiwe', nikafanya hivyo. Akachukua kisu kile na akamchukua kondoo akamlaza, akamchinja akasema:

بِسْمِ اللَّهِ، اللَّهُمَّ تَقَبَّلْ مِنْ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَمِنْ أُمَّةِ مُحَمَّدٍ

“BismiLLaah, Allaahumma taqabbal min Muhammad wa aali Muhammad, wa min ummati Muhammad.” Kisha akamchinja

1160.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {“مَنْ كَانَ لَهُ سَعَةٌ وَلَمْ يُضَحَّ، فَلَا يَقْرَبَنَّ مُصَلَّانَا”} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَابْنُ مَاجَهَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، لَكِنْ رَجَّحَ الْأَيْمَنُ غَيْرُهُ وَقَفَّهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye uwezo na hakuchinja basi asikaribie katu Muswallaa[2] wetu.” [Imetolewa na Ahmad na Ibn Maajah na akaisahihisha Al-Haakim. Maimaam wengine wametilia nguvu kuwa ni Mawquwf]

1161.

وَعَنْ جُنْدُبِ بْنِ سُفْيَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {شَهِدْتُ الْأَضْحَى مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَلَمَّا قَضَى صَلَاتَهُ بِالنَّاسِ، نَظَرَ إِلَى غَنَمٍ قَدْ ذُبِحَتْ، فَقَالَ: “مَنْ ذَبَحَ قَبْلَ الصَّلَاةِ فَلْيَذْبَحْ شَاةً مَكَانَهَا، وَمَنْ لَمْ يَكُنْ ذَبَحَ فَلْيَذْبَحْ عَلَى اسْمِ اللَّهِ”} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jundub bin Sufyaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilishuhudia Udhw-hiyyah pamoja na Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipomaliza kuswalisha watu alitazama mbuzi

aliyekuwa amechinjwa, akasema: “Aliyechinja kabla kuswali achinje mnyama mwingine mahala pake na ambaye hajachinja basi achinje kwa Jina la Allaah.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1162.

وَعَنْ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَامَ فِينَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: {“أَرْبَعٌ لَا تَجُوزُ فِي الضَّحَايَا: الْعَوْرَاءُ الْبَيِّنُ عَوْرُهَا، وَالْمَرِيضَةُ الْبَيِّنُ مَرَضُهَا، وَالْعَرَجَاءُ الْبَيِّنُ ظَلْعُهَا وَالْكَسِيرَةُ الَّتِي لَا تُنْقِي”} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ . وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Al-Baraa bin ‘Aazib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alisimama akatuhutubia: “Wanyama aina nne[3] hawafai katika Udhw-hiyyah: mwenye chongo, inayoonekana wazi chongo yake, mgonjwa anayeonekana dhahiri ugonjwa wake, kiwete anayeonekana waz ulemavu wake na mkongwe ambaye hana uboho.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha At-Tirmidhiy na Ibn Hibbaan]

1163.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {“لَا تَذْبَحُوا إِلَّا مُسِنَّةً، إِلَّا أَنْ يَعْسُرَ عَلَيْكُمْ فَتَذْبَحُوا جَذْعَةً مِنَ الضَّأْنِ”} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msichinje (Udhw-hiyyah)

isipokuwa musinnah,[4] isipokuwa ikiwa uzito kwenu, hapo mtachinja koo la kondoo (mwenye umri wa miezi sita hadi kumi).”
[Imetolewa na Muslim]

1164.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَمَرَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ نَسْتَشْرِفَ الْعَيْنَ وَالْأُذْنَ، وَلَا نُضْحِي بِعَوْرَاءَ، وَلَا مُقَابِلَةً، وَلَا مُدَابِرَةً، وَلَا خَرْمَاءَ، وَلَا ثَرْمَاءَ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ. وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alituamuru kuchunguza macho na masikio, wala tusidhahi mnyama chongo, wala aliyekatwa ncha ya sikio, wala aliyekatwa masikio kwa upana wala asiye na meno ya mbele.”[5] [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy, Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

1165.

وَعَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {أَمَرَنِي النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ أَقُومَ عَلَى بُدْنِهِ، وَأَنْ أَقْسِمَ لِحُومِهَا وَجُلُودِهَا وَجِلَالِهَا عَلَى الْمَسَاكِينِ، وَلَا أُعْطِيَ فِي جِزَارَتِهَا مِنْهَا شَيْئًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aliy bin Abiy Twaalib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliniamuru nimsimamie ngamia wake (wa Udhw-hiyyah) na nigawe nyama yao, ngozi yake na

masaruji yake kwa masikini.[6] Na nisimpe chochote mchinjaji kutokana na ngamia hao.” [Al-Bukhaariy, Muslim]

1166.

وَعَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {نَحَرْنَا مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَامَ الْحُدَيْبِيَّةِ: الْبَدَنَةَ عَنْ سَبْعَةٍ، وَالْبَقَرَةَ عَنْ سَبْعَةٍ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdillaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Tulichinja pamoja na Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) mwaka wa Vita Vya Hudaybiyah watu saba kwa kuchinja ngamia mmoja na watu saba wakishirikiana kwa kuchinja ng’ombe mmoja.”[7] [Imetolewa na Muslim]

[1] Kuchinja ni aina mbili: Ya kwanza ni Hady na ya pili ni Udhw-hiyyah. Hady ni ile inayotolewa na Hujaji Minaa. Ama Udhw-hiyyah ni ile inayotolewa na Waislamu maeneo mengine ulimwenguni wakati wa ‘Iydu Adhw-haa au wakati wa Tashriyq. Kulingana na Wanazuoni wengi, kutoa Udhw-hiyyah ni Sunnah, kwa Wanazuoni wengine ni waajib. ‘Ibaadah hii inaitwa udhw-hiyyah kwa sababu inafanyika wakati wa dhwuha.

[2] Baadhi ya Wanazuoni wanahitimisha katika Hadiyth hii kuwa swala la kuchinja udhw-hiyyah ni la waajib. Hata hivyo Wanazuoni wengi wanaona kuwa ni Sunnah Muakkada. (Sunnah iliyosisitizwa).

[3] Mgonjwa, kiguru, chongo na dhaifu hawaruhusiwi kuchinjwa kwa ajili ya Udhw-hiyyah. Wanazuoni wanaona kuwa hukumu hii inahusu pia magonjwa mengine mwilini.

[4] Katika lugha ya Kiarabu Musinnah ni mnyama ambaye meno yake ya mwanzo yameshaondoka na kuanguka na kubadilishwa kwa meno mengine ya kawaida. Kila mnyama ana muda wake wa kutoka kwa meno. Mbuzi, kondoo na kondoo dume aliyehasiwa wanapokuwa mwaka wa kwanza na kuingia mwaka wa pili wanakuwa musinnah. Ng’ombe na

jamusi wanakuwa katika hali hii wanapoingia mwaka wa tatu wa umri wao. Ngamia anakuwa anakuwa katika hali hiyo anapoingia mwaka wa sita wa umri wake.

[5] Mnyama ambaye amekakwa sikio au hata kukaruzwa, au aliyekakwa pembe haruhusiwi kuchinjwa. Hukumu inayohusu sikio na pembe ni ikiwa nusu ya viungo hivi kama vimekatwa basi hairuhusiwi kuchinjwa. Lakini ikiwa zaidi ya nusu ya viungo hivi vikiwa katika hali nzuri basi wanyama hawa wanafaa kuchinjwa. Ikiwa mnyama atakuwa amezaliwa bila ya pembe haizingatiwi kama ni ila, hata hivyo ikiwa pembe yenyewe imekatika baada ya kuzaliwa itakuwa ni ila.

[6] Ngozi, sufi na nyama ya mnyama inabidi itolewe kama Swadaqah. Mtu anayetoa Udhw-hiyyah anaruhusiwa kula nyama ile na anaweza kutumia ngozi yake. Kumpa mchinjaji nyama kama ujira wake ni jambo lenye kukatazwa. Watu wengine hawawalipi wachinjaji ujira wao, ambalo ni jambo lisilopendeza. Katika hali ambayo mchinjaji hachukui ujira wake kwa mapenzi yake basi inaruhusiwa.

[7] Udhw-hiyyah wa kondoo mmoja inatosheleza hata kwa watu ishirini wa nyumba moja. Ama udhw-hiyyah wa ng'ombe, jamusi na ngamia mmoja wanashirikiana watu saba kwa maana hiyo nyumba saba zitafaidika na udhw-hiyyah hiyo. Ikiwa udhw-hiyyah hiyo ni ya Sunnah au ni ya waajib, yote ni sawa hakuna tofauti. Siyo lazima ikawa kwa watu saba hata mtu mmoja anaweza kufanya hivyo.

03-Mlango Wa"Aqiyqah

بَابُ الْعَقِيقَةِ

03-Mlango Wa 'Aqiyqah[1]

1167.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَقَّ عَنْ الْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ كَبْشًا كَبْشًا } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ الْجَارُودِ، وَعَبْدُ الْحَقِّ لَكِنْ رَجَّحَ أَبُو حَاتِمٍ إِرْسَالَهُ وَأَخْرَجَ ابْنُ حِبَّانَ: مِنْ حَدِيثِ أَنَسٍ نَحْوَهُ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alimfayia ‘Aqiyqah Hasan na Husayn[2] kondoo mmoja mmoja.”[3] [Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha Ibn Khuzaymah, Ibn Al-Jaarud na ‘Abdul Haqq. Lakini Abuu Haatim ameitilia nguvu kuwa ni Mursal] Na amepokea Ibn Hibbaan kutoka kwa Anas mfano wake.

.1168

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَمَرَهُمْ، أَنْ يُعَقَّ عَنْ الْغُلَامِ شَاتَانِ مُكَافِئَتَانِ، وَعَنْ الْجَارِيَةِ شَاةٌ } رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ وَأَخْرَجَ الْخَمْسَةُ عَنْ أُمِّ كُرْزٍ الْكَعْبِيَّةِ نَحْوَهُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliwaamrisha mvulana

afanyiwe ‘aqiyqah kwa mbuzi wawili wanaolingana, na mtoto wa kike afanyiwe ‘Aqiyqah mbuzi mmoja.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha]

Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) wameipokea kutoka kwa Ummu Kurzi Al-Ka’biyyah[4] Hadiyth kama hii.

.1169

وَعَنْ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {كُلُّ غُلَامٍ مُرْتَهَنٌ بِعَقِيقَتِهِ، تُذَبِّحُ عَنْهُ يَوْمَ سَابِعِهِ، وَيُحْلَقُ، وَيُسَمَّى} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kila kijana amewekwa rahani[5] kwa ‘Aqiyqah yake, huchinjiwa siku yake ya saba,[6] hunyolewa na hupewa jina.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

[1] ‘Aqiyqah ni istwilaah inayotumika kwa wanyama, ni kichinjo kwa ajili ya mtoto mchanga anayezaliwa.

[2] Husayn alikuwa ni mdogo kuliko Hasan na takriban alikuwa mdogo kwa mwaka mmoja. Alikuwa ni mjukuu wa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

(وَسَلَّمَ) na maarufu kwa taqwa yake. Aliuwawa Karbala ‘Iraq tarehe kumi ya Muharram, 61 Hijriyyah.

[3] ‘Aqiyqah ni Sunnah. Hadiyth inayofuata inaelezea kuwa kuchinja kondoo wawili anachinjiwa ikiwa mtoto mwenyewe ni wa kiume, wakati Hadiythi hii inaeleza kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameeleza kuwa kondoo mmoja ni kwa ajili ya mtoto mmoja. Hii inawezekana kuwa hapakuwepo na kondoo wengine wa kuchinja kwa wakati ule. Vinginevyo, ni kuwa kuchinja kondoo wawili kwa mtoto mmoja wa kiume ndiyo Sunnah.

[4] Ummu Kurzi Al-Ka’biyyah alikuwa ni Swahaabiyya katika kabila la Khuza’a na amepokea baadhi za Hadiyth.

[5] Hii ina maana ya kitu kilichowekwa kama dhamana, hakitumiwi. Kwa maelezo hayo ni kuwa huyo mtoto hawezi kumuomba baba yake siku ya Qiyaamah.

[6] Ni sawa sawa kama amechinjwa ng’ombe katika ‘Aqiyqah. Siku mtoto anapozaliwa ndipo atakaposomewa adhaana kwa sikio lake la kuume na Iqaamah katika sikio lake la kushoto, kulingana na baadhi ya ‘Ulamaa. Hata hivyo, Hadiyth iliyoripotiwa na Abuu Daawud na At-Tirmidhiy kuwa maelezo haya si sahihi. ‘Aqiyqah itekelezwe siku ya saba baada ya kuzaliwa kwa mtoto. Katika siku hiyo hiyo mtoto anapewa jina na ananyolewa nywele zake. Baada ya hapo, nywele zilizotolewa zinapimwa na thamani yake ya fedha inatolewa kama swadaqah. Vivyo hivyo, mtoto ataombewa du’aa na kufanyiwa tahniyk (kulainishiwa tende na kupewa mdomoni).

كِتَابُ الْأَيْمَانِ وَالنُّذُورِ

Kitabu Cha Yamini Na Nadhiri

13- Kitabu Cha Yamini (Viapo) Na Nadhiri - كِتَابُ الْأَيْمَانِ وَالنُّدُورِ

00-Kitabu Cha Yamini Na Nadhiri

كِتَابُ الْأَيْمَانِ وَالنُّدُورِ

Kitabu Cha Yamini Na Nadhiri

1170.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ أَدْرَكَ عُمَرَ بْنَ الْخَطَّابِ فِي رَكْبٍ، وَعُمَرُ يَخْلِفُ بِأَبِيهِ، فَنَادَاهُمْ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "أَلَا إِنَّ اللَّهَ يَنْهَاكُمْ أَنْ تَخْلِفُوا بِأَبَائِكُمْ، فَمَنْ كَانَ حَالِفًا فَلْيَخْلِفْ بِاللَّهِ، أَوْ لِيَصْمُتْ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

وَفِي رِوَايَةٍ لِأَبِي دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيِّ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { لَا تَخْلِفُوا بِأَبَائِكُمْ، وَلَا بِأُمَّهَاتِكُمْ، وَلَا بِأَنْدَادٍ، وَلَا تَخْلِفُوا إِلَّا بِاللَّهِ، وَلَا تَخْلِفُوا بِاللَّهِ إِلَّا وَأَنْتُمْ صَادِقُونَ" }

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimkuta ‘Umar bin Al-Khatwaab katika kundi la watu, na ‘Umar anaapa kwa baba yake. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaita

akawaambia: Kwa Yaqini Allaah Anawakataza kuapa kwa baba zenu. [1] Ambaye ataapa basi aape kwa Allaah au anyamaze.” [Bukhaariy, Muslim]

Na katika riwaayah nyingine ya Abuu Daawuwd na An-Nasaaiy kutoka kwa Abuu Hurayrah: “Msiape kwa baba zenu wala kwa mama zenu wala kwa masanamu. Na msiape kwa Allaah isipokuwa muwe wakweli.”

1171.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "يَمِينُكَ عَلَى مَا يُصَدِّقُكَ بِهِ صَاحِبُكَ" } وَفِي رِوَايَةٍ: { "الْيَمِينُ عَلَى نِيَّةِ الْمُسْتَحْلِفِ" } أَخْرَجَهُمَا مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Yamini yako ni kwa jambo analokusadiki mwenzio.”[2]

Na katika riwaayah nyingine: “Yamini ni kwa niyyah ya aliyeapisha (Al-Mustahlif).” [Riwaayah zote zimetolewa na Muslim]

1172.

وَعَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { وَإِذَا حَلَفْتَ عَلَى يَمِينٍ، فَرَأَيْتُ غَيْرَهَا خَيْرًا مِنْهَا، فَكْفَرُ عَنْ يَمِينِكَ، وَأَنْتَ الَّذِي هُوَ

خَيْرٌ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ . وَفِي لَفْظٍ لِلْبُخَارِيِّ: { "فَأَيْتَ الَّذِي هُوَ خَيْرٌ، وَكَفَّرَ عَنْ يَمِينِكَ" } وَفِي رِوَايَةٍ لِأَبِي دَاوُدَ: { "فَكَفَّرَ عَنْ يَمِينِكَ، ثُمَّ أَنْتَ الَّذِي هُوَ خَيْرٌ" } وَإِسْنَادُهَا صَحِيحٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [3] Kutoka kwa ‘Abdur-Rahmaan bin Samurah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema Rasuli wa Allaah amesema: “Utakapoapa kiapo kasha ukaona vinginevyo ni kheri kuliko hilo, basi utolee kafara[4] yamini yako na utende lililo bora.” [Bukhaariy, Muslim]

Na katika tamshi la Al-Bukhaariy: “...tolea kafara yamini yako kisha ufanye lililo bora.”

Na katika riwaayah ya Abuu Daawuwd: “...basi utolee kafara yamini yako kisha ufanye lililo bora.” [Isnaadi zake ni sahihi]

1173.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "مَنْ حَلَفَ عَلَى يَمِينٍ فَقَالَ: إِنْ شَاءَ اللَّهُ، فَلَا حَنْثَ عَلَيْهِ" } رَوَاهُ الْخَمْسَةُ . وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuapa yamini na akasema In Shaa Allaah (Allaah Akipenda) atakuwa hakuvunja yamini.”[5] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1174.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {كَانَتْ يَمِينُ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "لَا، وَمُقَلَّبِ الْقُلُوبِ"} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Ilikuwa yamini ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: Naapa kwa Anayezigeuza nyoyo.”[6] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1175.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {جَاءَ أَعْرَابِيٌّ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! مَا الْكَبَائِرُ؟ ... فَذَكَرَ الْحَدِيثَ، وَفِيهِ قُلْتُ: وَمَا الْيَمِينُ الْغَمُوسُ؟ قَالَ: "الَّذِي يَقْتَطِعُ مَالَ امْرِئٍ مُسْلِمٍ، هُوَ فِيهَا كَاذِبٌ"} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ.

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Mbedui mmoja alimjia Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Ee Rasuli wa Allaah! Ni yapi madhambi makubwa? Akataja Hadiyth yote, ndani yake: Yamini ya uongo.[7] Nikasema ni ipi yamini ya uongo? akasema: ni ambayo mtu huchukua mali ya mtu Muislaam naye ndani ya kiapo chake anakusudia uongo.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1176.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا { فِي قَوْلِهِ تَعَالَى: (لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ) }
قَالَتْ: هُوَ قَوْلُ الرَّجُلِ: لَا وَاللَّهِ. بَلَى وَاللَّهِ { أَخْرَجَهُ
الْبُخَارِيُّ . وَأُورِدَهُ أَبُو دَاوُدَ مَرْفُوعاً

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuhusiana na aayah hii: “Allaah Hatokuchukulieni kwa viapo vyenu vya upuuzi... [8] [Al-Maaidah: 89] imeteremshwa kuhusu mtu anavyosema Hapana Wa-Allaahi! Ndio Wa-Allaahi.”[9] [Imetolewa na Al-Bukhaariy, na Abuu Daawuud ameipokea ikiwa ni marfuw’a]

1177.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "إِنَّ لِلَّهِ تِسْعًا وَتِسْعِينَ إِسْمًا، مَنْ أَحْصَاهَا دَخَلَ الْجَنَّةَ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ . وَسَاقَ التِّرْمِذِيُّ وَابْنُ حِبَّانَ الْأَسْمَاءَ، وَالتَّحْقِيقُ أَنَّ سَرْدَهَا إِدْرَاجٌ مِنْ بَعْضِ الرُّوَاةِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kwa hakika Allaah Ana Majina tisini na tisa,[10] mwenye kuyahifadhi ataingia Al-Jannah.”[11] [Bukhaariy, Muslim. Tirmidhiy na Ibn Hibbaan wametaja majina hayo. Lakini uhakiki ni kuwa utajo wake ni (Idraaj) si Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)]

1178.

وَعَنْ أُسَامَةَ بْنِ زَيْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "مَنْ صُنِعَ إِلَيْهِ مَعْرُوفٌ، فَقَالَ لِفَاعِلِهِ: جَزَاكَ اللَّهُ خَيْرًا. فَقَدْ أَبْلَغَ فِي الثَّنَاءِ" } أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Usaamah bin Zayd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayefanyiwa wema na akamuambia aliyemfanyia Jazaaka-Allaahu khayran (Allaah Akujaze kheri) hakika atakuwa amekamilisha hisani kwa ukamilifu.”[12] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1179.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ نَهَى عَنْ النَّذْرِ وَقَالَ: " إِنَّهُ لَا يَأْتِي بِخَيْرٍ وَإِنَّمَا يُسْتَخْرَجُ بِهِ مِنَ الْبَخِيلِ " } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikataza kuweka nadhiri[13] na akasema: Haileti kheri bali kutoka kwa bakhili hutolewa nadhiri.” [Bukhaariy, Muslim]

1180.

وَعَنْ عُقْبَةَ بْنِ عَامِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "كَفَّارَةُ النَّذْرِ كَفَّارَةُ يَمِينٍ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ. وَزَادَ التِّرْمِذِيُّ فِيهِ: { إِذَا لَمْ يُسَمَّ } ، وَصَحَّحَهُ.

وَلِأَبِي دَاوُدَ: مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عَبَّاسٍ مَرْفُوعاً: { "مَنْ نَذَرَ نَذْرًا لَمْ يُسَمِّهِ، فَكَفَّارَتُهُ كَفَّارَةُ يَمِينٍ، وَمَنْ نَذَرَ نَذْرًا فِي مَعْصِيَةٍ، فَكَفَّارَتُهُ كَفَّارَةُ يَمِينٍ، وَمَنْ نَذَرَ نَذْرًا لَا يُطِيقُهُ، فَكَفَّارَتُهُ كَفَّارَةُ يَمِينٍ" } وَإِسْنَادُهُ صَحِيحٌ، إِلَّا أَنَّ الْحُفَّاطَ رَجَّحُوا وَقْفَهُ. وَلِلْبُخَارِيِّ: مِنْ حَدِيثِ عَائِشَةَ: { "وَمَنْ نَذَرَ أَنْ يَعْصِيَ اللَّهَ فَلَا يَعْصِيهِ" }

وَلِمُسْلِمٍ: مِنْ حَدِيثِ عِمْرَانَ: { " لَا وَفَاءَ لِنَذْرِ فِي مَعْصِيَةٍ" }

Kutoka kwa ‘Uqbah bin ‘Aamir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kafara ya nadhiri ndio kafara ya yamini.”[14] [Imetolewa na Muslim] na akazidisha At-Tirmidhiy: “...asipoitaja.” [Na ameisahihisha]

Na Abuu Daawuud ameipokea kutoka katika Hadiyth ya Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) ikiwa ni Marfuw’: “Mwenye kuweka nadhiri ambayo haikutajwa, basi kafara yake ni kafara ya yamini. Na mwenye kuweka nadhiri ya katika maasi, basi kafara yake ni kafara ya yamini. Na mwenye kuweka nadhiri ya jambo asiloweza, basi kafara yake ni kafara ya yamini.” [Isnaad yake ni sahihi isipokuwa Wanazuoni wa Hadiyth wameitilia nguvu kuwa ni Mawquwf]

Bukhaariy ameipokea kutoka katika Hadiyth ya ‘Aaishah: “... na mwenye kuweka nadhiri ya kumuasi Allaah asimuasi.”

Muslim amepokea katika Hadiyth ya ‘Imraan: “Hakuna kutekeleza nadhiri katika maasia.”

1181.

وَعَنْ عُقْبَةَ بْنِ عَامِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَذَرْتُ أُخْتِي أَنْ تَمْشِيَ إِلَى بَيْتِ اللَّهِ حَافِيَةً، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "لِتَمْشِ وَلْتَرْكَبْ"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ. وَلِلْخَمْسَةِ. فَقَالَ: { "إِنَّ اللَّهَ لَا يَصْنَعُ بِشَقَاءِ أُخْتِكَ شَيْئًا، مُرَهَا: فَلْتُخْتَمِرْ ، وَلْتَرْكَبْ، وَلْتَصُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ" }

Kutoka kwa ‘Uqbah bin ‘Aamir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Dada yangu aliweka nadhiri ya kutembea hadi katika nyumba ya Allaah bila viatu. Akaniamuru kutaka Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) fatwa yake. Nami nikamuuliza, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Atembee na apande.” [Al-Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) wamepokea: “Kwa hakika Allaah Hana haja ya Kumtesa dada yako kwa jambo lolote. Muambie avae mtandio, apande (mnyama) na afunge siku tatu.”

1182.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {اسْتَفْتَى سَعْدُ بْنُ عُبَادَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي نَذْرٍ كَانَ عَلَى أُمِّهِ، تُؤَفِّيْتُ قَبْلَ أَنْ تَقْضِيَهُ ؟ فَقَالَ: "إِقْضِهِ عَنْهَا"} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Sa’d bin ‘Ubaada[15] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alimuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) juu ya nadhiri iliyompasa mama yake,[16] akafariki kabla ya kuilipa. Akasema: “Mlipie.” [Bukhaariy, Muslim]

1183.

وَعَنْ ثَابِتِ بْنِ الضَّحَّاكِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {نَذَرَ رَجُلٌ عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ يَنْحَرَ إِبِلًا بِبُؤَانَةٍ، فَأَتَى رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَسَأَلَهُ: فَقَالَ: "هَلْ كَانَ فِيهَا وَثْنٌ يُعْبَدُ؟". قَالَ: لَا. قَالَ: "فَهَلْ كَانَ فِيهَا عِيدٌ مِنْ أَعْيَادِهِمْ؟" فَقَالَ: لَا. فَقَالَ: "أَوْفٍ بِنَذْرِكَ، فَإِنَّهُ لَا وَفَاءَ لِنَذْرٍ فِي مَعْصِيَةِ اللَّهِ، وَلَا فِي قَطِيعَةِ رَحِمٍ، وَلَا فِيمَا لَا يَمْلِكُ ابْنُ آدَمَ" { رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتَّبَرَانِيُّ وَاللَّفْظُ لَهُ، وَهُوَ صَحِيحُ الْإِسْنَادِ.

وَلَهُ شَاهِدٌ مِنْ حَدِيثِ كَرْدَمٍ. عِنْدَ أَحْمَدَ

Kutoka kwa Thaabit bin Adw-Dwahhaak (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Mtu mmoja katika zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliweka nadhiri ya kuchinja ngamia Buwaanah, akamuendea Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuuliza. Akasema: Je ndani yake kulikuwa na sanamu anayeabudiwa?[17] Akasema: Hapana. Akasema: Tekeleza nadhiri yako, kwa hakika si ruhusa kutekeleza nadhiri katika kumuasi Allaah

wala katika kukata kizazi wala katika asichomiliki mwana Aadam.”
[Imetolewa na Abuu Daawuud na Atw-Twabaraaniyy. Isnaad yake ni sahihi na ina ushahidi kutoka katika Hadiyth ya Kardam^[18] kwa Ahmad]

1184.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَجُلًا قَالَ يَوْمَ الْفَتْحِ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي نَذَرْتُ أَنْ فَتَحَ اللَّهُ عَلَيْكَ مَكَّةَ أَنْ أَصَلِّيَ فِي بَيْتِ الْمَقْدِسِ، فَقَالَ: "صَلِّ هَا هُنَا". فَسَأَلَهُ، فَقَالَ: "صَلِّ هَا هُنَا". فَسَأَلَهُ، فَقَالَ: "شَأْنُكَ إِذَا" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Mtu mmoja siku ya Fat-h Makkah alisema: Ee Rasuli wa Allaah! Mimi nimeweka nadhiri iwapo Allaah Atakufungulia mji wa Makkah nitaswali katika Msikiti wa Baytul-Maqdis (Jerusalem). Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Swali hapa hapa. [19] Akamuuliza tena, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: Swali hapa hapa. Akamuuliza tena, Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: kwa hivyo ni shauri yako.” [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud na akaisahihisha Al-Haakim]

1185.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "لَا تُشَدُّ الرَّحَالُ إِلَّا إِلَى ثَلَاثَةِ مَسَاجِدَ: مَسْجِدِ الْحَرَامِ، وَمَسْجِدِ الْأَقْصَى، وَمَسْجِدِي" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِلْبُخَارِيِّ

Kutoka kwa Abiy Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si ruhusa kufunga safari ila katika Miskiti mitatu: Masjidil-Haraam, Masjidil-Aqswaa na Msikiti wangu huu.” [Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Al-Bukhaariy]

1186.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: { قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! إِنِّي نَذَرْتُ فِي الْجَاهِلِيَّةِ، أَنْ أَعْتَكِفَ لَيْلَةً فِي الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ. قَالَ: "فَأَوْفِ بِنَذْرِكَ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَزَادَ الْبُخَارِيُّ فِي رِوَايَةٍ { فَأَعْتَكِفَ لَيْلَةً }

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilisema: Ee Rasuli wa Allaah! Nilikuwa nimeweka nadhiri zama za ujahiliya,[20] nikakaa I’tikaaf usiku mmoja katika Al-Masjid Al-Haraam. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaniambia: tekeleza nadhiri yako.” [Bukhaariy, Muslim]

Katika riwaayah nyingine Bukhaariy ameongezea: “...akakaa I’tikaaf usiku mmoja.”

[1] Ilikuwa ni tabia ya Waarabu kuapa kwa majina ya baba zao na babu zao. ‘Umar alipoapa mbele ya Nabiyy (ﷺ) alikatazwa kufanya hivyo, na kuwa akitaka kuapa na aape kwa jina la Allaah. Maelezo kama ‘Nakuapia’, ‘Naapa kwa kichwa chako’ ‘Naapa kwa Husain’ ‘Naapa kwa Nabiyy (ﷺ)’. Matumizi ya viapo vyote hivi havifai, bali viapo kama hivyo huwa ni shirki.

[2] Hadiyth hii inaelezea ikiwa muapaji (Al-Halif) kwa kumtaka anayeambiwa (Al-Mustahlif) mwenye haki, kiapo kitachukuliwa kuwa ni cha jambo maalumu tu. Niyyah iliyojificha ya anayeapa (Al-Halif) haitozingatiwa. Kitakachozingatiwa ni ile niyyah ya Al-Mustahlif aliyeomba kiapo kifanyike. Hata hivyo ikiwa mtu ataapa mwenyewe bila ya kutakiwa kiapo, basi chochote atakachofanya ndicho kitakachozingatiwa.

[3] ‘Abdur-Rahmaan bin Samurah: Lakabu yake ni Abuu Sa’iyd alikuwa ni Swahaba. Alisilimu baada ya Fat-h na alifungua Sijistan na Kabul. Aliishi Basra ‘Iraaq na alifariki mwaka 50 Hijriyyah

[4] Kafara ya kiapo ni a: Kumuachia huru mtumwa, b) kulisha watu kumi, c) Kuwapa nguo watu, d) Kufunga (Swiyaam) siku tatu.

[5] Hadiyth hii inataka watu wafungamanishe viapo vyao na Atakavyo Allaah kwa kusema In Shaa Allaah wakati wa kuapa.

[6] Hadiyth hii inaonesha kuwa suala la kuapia si kwa majina ya Allaah (Al-Asmaa) peke yake. Inaruhusiwa kuapia kwa sifa zake (Asw-Swifaat). Hili linaruhusiwa kama mtu ataapia kwa sifa zake (Asw-Swifaat Adh-dhaatiyya) kama vile elimu, nguvu na sifa za Ilaah (Asw-Swifaat Al-Fi’liyyah) kama vile hasira, ridhaa n.k.

[7] Katika lugha ya Kiarabu, Yamiyn ghamuws (Kiapo cha uongo) ni kile kiapo kinachokusudia kuhadaa, kudanganya kwa niyyah ya kuchuka mali ya mtu bila ya haki. Ikiwa jambo hilo la kuapa halikusudii mali basi kiapo chenyewe kitajulikana kama Yamiyn faajir. Hakuna kafara kwa Yamiyn ghamuws. Kafara pekee ya hili ni kurudisha mali ya watu, kumuomba Allaah maghfirah.

[8] Rejea Suwrat Al-Maaidah Aayah ya 89.

[9] Mazungumzo anayotoa mtu bila ya kufikiriwa hayazigatiwi, hayachukuliwi kama ni viapo. Katika hali hii hamna kafara au adhabu, hata hivyo ni tabia ambayo haipendezi.

[10] Mbali na majina haya kuna majina mengine yanayonasibishwa na Allaah. Majina mengine ni nyongeza lakini nayo ni Matukufu

[11] Maana yake na inakusudiwa vile vile kuyahifadhi na kuyatumia mara kwa mara na kuyatumia maana yake kiutekelezaji katika maisha ya kila siku.

[12] Mtu aliyefanyiwa jambo fulani nae ajitahidi amfanyie aliyemfanyia vizuri zaidi. Kama hatoweza kufanya basi na amuombee du'aa.

[13] Nadhiri iliyokatazwa ni kama vile mtu kusema: “Ikiwa mgonjwa wangu atapona, nitatoa swadaqah kiasi kadhaa.” Hii ina maana kuwa hatoi Swadaqah kwa dhati ya Allaah bali ameifungamanisha na anachokitaka. Vivyo hivyo, ndiyo hali ya bakhili kwani mara nyingi hatoi mali yake ila kwa makusudio ya kupata kitu fulani. Inabidi watu kufahamu kuwa kuweka nadhiri hakubadilishi Qadar ya mtu. Hili linahusu nadhiri iliyokokotezwa kwa jina la Allaah, sembuse nadhiri zilizoapiwa kwa kaburi la fulani, au mtu kuamini kuwa aliyelala katika kaburi fulani ndiye mwenye uwezo wa kubadilisha hali ya fulani au kuleta maslahi fulani? kwa hakika siyo kwamba aina hii ya nadhiri zinakatazwa bali ni ushirikina kwa dhati yake.

[14] Ikiwa nadhiri inajitegemea bila kuainisha na jambo lolote kama vile mtu kusema: “Nimeweka nadhiri kwa Jina la Allaah.” Nadhiri au kiapo cha aina hii hakijakamilika, atalazimika kutoa kafara ya kiapo. Ikiwa kiapo chenyewe kimeainishwa, na mtu ana uwezo wa kuitekeleza basi ni wajibu kwake kuitekeleza. Ikiwa aliyeapa hana uwezo wa kutekeleza, itabidi atoe kafara ya kiapo kama ilivyo ya yamini. Ikiwa kiapo chenyewe kimefungamanishwa na kumuasi Allaah au kufanya jambo lolote la dhambi, baadhi ya Wanazuoni wana rai ya kutotolewa kafara yoyote, wakati wengine wana rai kuwa ni lazima atoe kafara ya kiapo (Kaffaarah Al-Yamiyn)

[15] Sa'd bin 'Ubaada: Alikuwa kiongozi wa Al-Khazraj, mbeba bendera wa Answaar katika vita vyote na kiongozi wa msafara wa Bay'atul-'Aqaba. Alikuwa mtu mwenye heshima, mkarimu na alikuwa mwandishi. Alikuwa hodari katika kuogelea na kutupa mishale, alijulikana kwa jina Al-Kaamil (mkamilifu) kwa sababu ya tabia na sifa alizokuwa nazo. Alikuwa akitoa swadaqah nyingi mara kwa mara. Aliwahi kuondoka Madiynah kabla ya Abuu Bakr kutoa kiapo cha ukhalifa. Alikufa mwaka 14 Hijriyyah na wengine wanasema 15 au 16.

[16] Mapokezi haya hayakuelezea aina ya kiapo kilichotolewa. Katika Hadiyth nyingine inaonesha ni kiapo cha kuacha mtumwa. Hii inaelezea kuwa mtu aliyekufa katika hali hii warithi wake wanatakiwa wamlipie kiapo chake.

[17] Hadiyth inatuelezea kuwa ikiwa mtu ameweka nadhiri au kiapo cha kufanya 'ibaadah katika sehemu fulani, basi ni wajibu kwake kutekeleza kiapo kile, maadamu ya kuwa sehemu ile anayotaka kufanyia 'ibaadah hakuna 'ibaadah za kijahiliya zinazofanyika. Hata hivyo pamoja na kukubalika huko, si lazima atekeleze 'ibaadah ile sehemu ile ile.

[18] Kardam bin Sufyaan Ath-Thaqafi alikuwa Swahaba na binti yake Maymuwna aliyekuwa Swahabiya na aliyepokea Hadiyth kutoka kwake alikuwa ni 'Abdullaah bin 'Amr bin Al-'Aasw.

[19] Hadiyth hii inagusia kanuni ya msingi kuwa ikiwa mtu ameapa kuwa atafanya 'ibaadah sehemu fulani, ni wajibu kutekeleza kiapo kile kwa kiwango cha 'ibaadah cha Msikiti mwingine wenye hadhi kama Msikiti ule. Kama ataswali Msikiti wenye hadhi ya chini basi atakuwa hajatekeleza kiapo kile. Hapa kuswali kwake katika Msikiti wa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Madiynah au Al-Ka'bah atakuwa ametekeleza kile kiapo. Ama akitoa kiapo cha kuswali katika Masjid Al-Haram Makkah hawezi kutekeleza kiapo kile kwa kuswali Baytul-Maqdis au Masjid Nabawi Madiynah. Ni lazima aswali katika Masjid Al-Haram Makkah.

[20] Watu wanaona kuwa kiapo cha kafiri hakina nafasi katika Uislaam. Katika Hadiyth hii ni dalili kama kafiri atakuwa ameweka kiapo chake kisha akasilimu ni lazima atekeleze kile kiapo chake. Huu ni muono wa Al-Bukhaariy, Ibn Jariyr na wengineo.

كِتَابُ الْقَضَاءِ

Kitabu Cha Kuhukumu

كِتَابُ الْقَضَاءِ - 14-Kitabu Cha Kuhukumu

00-Kitabu Cha Kuhukumu

1188.

عَنْ بُرَيْدَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "الْقُضَاءُ ثَلَاثَةٌ: اِثْنَانِ فِي النَّارِ، وَوَاحِدٌ فِي الْجَنَّةِ. رَجُلٌ عَرَفَ الْحَقَّ، فَقَضَى بِهِ، فَهُوَ فِي الْجَنَّةِ. وَرَجُلٌ عَرَفَ الْحَقَّ، فَلَمْ يَقْضِ بِهِ، وَجَارَ فِي الْحُكْمِ، فَهُوَ فِي النَّارِ. وَرَجُلٌ لَمْ يَعْرِفِ الْحَقَّ، فَقَضَى لِلنَّاسِ عَلَى جَهْلٍ، فَهُوَ فِي النَّارِ " } رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Buraydah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Maqaadhwi ni watatu, wawili[1] ni wa motoni na mmoja ni wa katika Jannah. (Wa kwanza) Ni mtu amejua haki akahukumu kwayo; huyo ni wa katika Jannah. (Wa pili) ni mtu amejua haki wala hakuhukumu kwayo, na akafanya jeuri katika hukumu, huyo ni wa motoni. (Wa tatu) ni mtu ambaye hakujuwa haki, akahukumu watu kwa ujinga, huyo ni wa

motoni.” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) na akaisahihisha Al-Haakim]

1189.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: {“مَنْ وَلِيَ الْقَضَاءَ فَقَدْ ذُبِحَ بِغَيْرِ سِكِّينٍ”} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ وَصَحَّحَهُ ابْنُ خُزَيْمَةَ، وَابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kutawalia ukadhi, kwa hakika amechinjwa bila ya kisu.”[2] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan]

1190.

وَعَنْهُ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {“إِنَّكُمْ سَتَحْرِصُونَ عَلَى الْأَمَارَةِ، وَسَتَكُونُ نَدَامَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ، فَنِعْمَ الْمُرْضِعَةُ، وَبِئْسَتِ الْفَاطِمَةُ”} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika nyinyi mtapupia uongozi, na utakuwa majuto siku ya Qiyaamah. Ni neema iliyoje (kwa mnyonyeshaji (duniani)! Na ubaya ulioje wa muachishaji (kunyonya).”[3] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1191.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "إِذَا حَكَمَ الْحَاكِمُ، فَاجْتَهَدَ، ثُمَّ أَصَابَ، فَلَهُ أَجْرَانِ. وَإِذَا حَكَمَ، فَاجْتَهَدَ، ثُمَّ أَخْطَأَ، فَلَهُ أَجْرٌ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Amr bin Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa amemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Hakimu akihukumu akajitahidi akapatia, ana (malipo mawili), na akihukumu akajitahidi akakosea, ana ujira mmoja.” [Bukhaariy, Muslim]

1192.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "لَا يَحْكُمُ أَحَدٌ بَيْنَ اثْنَيْنِ، وَهُوَ غَضَبَانُ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa amemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Asihukumu yoyote baina ya wawili huku ameghadhibika.” [4] [Bukhaariy, Muslim]

1193.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { " إِذَا تَقَاضَى إِلَيْكَ رَجُلَانِ، فَلَا تَقْضِ لِلأَوَّلِ، حَتَّى تَسْمَعَ كَلَامَ الآخرِ، فَسَوْفَ تَدْرِي كَيْفَ تَقْضِي " } . قَالَ عَلِيٌّ: فَمَا زِلْتُ قَاضِيًا بَعْدُ { رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ، وَقَوَّاهُ ابْنُ الْمَدِينِيِّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَلَهُ شَاهِدٌ عِنْدَ الْحَاكِمِ: مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عَبَّاسٍ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu wawili wakishtakiana kwako, usimhukumu wa kwanza mpaka usikie maneno ya mwingine[5] pengine ndio utajua utakavyo hukumu. ‘Aliy akasema ‘baada ya mafundisho haya nikawa nahukumu hivyo.” [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy ameifanya ni Hasan na akaipa nguvu Ibn Al-Madaniyy. Na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

Na ina ushahidi kwa Al-Haakim kutoka katika Hadiyith ya Ibn ‘Abbaas

1194.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: { " إِنَّكُمْ تَخْتَصِمُونَ إِلَيَّ، وَلَعَلَّ بَعْضَكُمْ أَنْ يَكُونَ أَلْحَنَ بِحُجَّتِهِ مِنْ بَعْضٍ، فَأَقْضِي لَهُ عَلَى نَحْوِ مِمَّا

أَسْمَعُ، مِنْهُ فَمَنْ قَطَعْتُ لَهُ مِنْ حَقِّ أَخِيهِ شَيْئًا، فَإِنَّمَا أَقْطَعُ لَهُ
قِطْعَةً مِنَ النَّارِ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika nyinyi
mnakuja kwangu kushtakiana na huenda mmoja wenu akawa fasaha
zaidi katika hoja yake kuliko mwingine, hivyo nikamhukumu yeye
kulingana na nilivyosikia. Basi nitakayemkatia chochote katika haki
ya nduguye hakika ninamkatia kipande cha moto.”[6] [Bukhaariy,
Muslim]

1195.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "كَيْفَ تُقَدِّسُ أُمَّةٌ، لَا يُؤْخَذُ مِنْ شَدِيدِهِمْ
لِضَعِيفِهِمْ؟" } رَوَاهُ ابْنُ حِبَّانَ
وَلَهُ شَاهِدٌ: مِنْ حَدِيثِ بُرَيْدَةَ، عِنْدَ الْبَزَّازِ
وَأَخَرُ: مِنْ حَدِيثِ أَبِي سَعِيدٍ عِنْدَ ابْنِ مَاجَهَ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nimemsikia Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Vipi ummah utasafishwa
ilhali haki ya mnyonge haichukuliwi kutoka kwa mwenye nguvu?”
[7] [Imetolewa na Ibn Hibbaan]

Na ina ushahidi kutoka katika Hadiyath ya Buraydah kwa Al-Bazzaar.

Na ina ushahidi mwingine kutoka katika Hadiyath ya Abuu Sa’iyd
kwa Ibn Maajah.

1196.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: { "يُدْعَى بِالْقَاضِي الْعَادِلِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، فَيُلْقَى مِنْ شِدَّةِ الْحِسَابِ مَا يَتَمَنَّى أَنَّهُ لَمْ يَقْضَ بَيْنَ اثْنَيْنِ فِي عُمْرِهِ" } رَوَاهُ ابْنُ حِبَّانَ وَأَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ، وَلَفْظُهُ: { فِي تَمْرَةٍ }

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema amemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Siku ya Qiyaamah ataitwa Qadhwi muadilifu, kutokana na ugumu wa hesabu atatamani kuwa asingehukumu baina ya watu wawili katika umri wake.” [Imetolewa na Ibn Hibbaan, na Al-Bayhaqiyy ameitaja kwa tamko: ‘hata kama ni tende’]

1197.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "لَنْ يُفْلِحَ قَوْمٌ وَلَّوْا أَمْرَهُمْ امْرَأَةً" } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu hawatafaulu watakapomtawalisha mwanamke jambo lao.”[8] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1198.

وَعَنْ أَبِي مَرْيَمَ الْأَزْدِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ {قَالَ: "مَنْ وَلَّاهُ اللَّهُ شَيْئًا مِنْ أَمْرِ الْمُسْلِمِينَ، فَاحْتَجَبَ عَنْ حَاجَتِهِمْ وَفَقِيرِهِمْ، احْتَجَبَ اللَّهُ دُونَ حَاجَتِهِ" } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) [9] Kutoka kwa Abuu Maryam Al-Azdiyy [9] amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa: “Ambaye Allaah Atamtawalisha katika chochote cha Waislaam, akajificha dhidi ya haja zao na mafukara wao, Allaah Atajitenga naye katika haja zake.” [10] [Imetolewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy]

1199.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {لَعَنَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الرَّاشِيَّ وَالْمُرْتَشِيَّ فِي الْحُكْمِ} رَوَاهُ الْخُمْسَةُ، وَحَسَنَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ وَلَهُ شَاهِدٌ: مِنْ حَدِيثِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو. عِنْدَ الْأَرْبَعَةِ إِلَّا النَّسَائِيَّ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Hurayrah [11] amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amemlaani [11] mtoa rushwa na mchukua rushwa katika hukumu.” [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah,

Ahmad) na At-Tirmidhiy amesema ni Hasan. Na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

Na ina ushahidi wa Hadiyth ya Abdullaah bin ‘Amr kwa Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy.

1200.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ الزُّبَيْرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {قَضَى
رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّ الْخَصْمَيْنِ يَقْعُدَانِ بَيْنَ
يَدَيِ الْحَاكِمِ} رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Az-Zubayr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا)
amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
amehukumu kuwa watesi wawili wanakaa[12] mbele ya hakimu.”
[Imetolewa na Abuu Daawuud na akaisahihisha Al-Haakim]

[1] Hadiyth hii inaelezea nukta mbili: Nukta ya kwanza, mtu ambaye hajui ukweli. Na mtu mwingine, ambaye hatekelezi ukweli ule pamoja na kuujua, mtu huyu ataadhibiwa. Hii ina maana kuwa elimu isiyokuwa na utekelezaji haina maana. Pili, kuna uwezekano wa kukosea katika kutoa hukumu. Kama isingekuwa hivyo basi watu wasingegawanyika katika hali ile na kila mmoja kujiona yuko sawa.

[2] Kwa kusoma Hadiyth hii adhabu na ukali ulio dhidi ya Qadhwi anayekwenda kinyume na maamrisho. Kila anayepewa nafasi ya Qadhwi ameiweka nafsi yake katika kichinjo. Ikiwa Qadhwi ni mwenye taqwa ni juu yake kutafuta hukumu yenye uadilifu zaidi. Vinginevyo anatarajiwa kupata hukumu kali mbele ya Allaah huko Aakhirah. Hadiyth nyingine inaelezea kuwa Qadhwi mwenye taqwa ataitwa na kuulizwa maswali katika Siku ya Hukmu, kiasi cha yule Qadhwi kusema: ‘Wa-Allaahi ni

bora ningehukumu walau kati ya watu wawili'. Ikiwa Qadhwi huyo atakuwa ni dhalimu, mla rushwa, mara noja atatupwa motoni.

[3] Hii ina maana kuwa utawala huo unawaridhia watawala wengi hapa duniani. Hata hivyo, anapokufa anaachishwa, anakosa raha zile na anasubiri hukumu yake. Ubaya ndio mwisho wake kwa aliyeshindwa kutekeleza majukumu yake.

[4] Qadhwi au jaji asitoe hukumu yake akiwa ameghadhibika, au mfano wa hali kama hizo; kusikia kiu, njaa, ugonjwa, wasiwasi, kusikia usingizi na mfano wa hayo. Akifanya hivyo huenda akatoa hukumu isiyo adilifu. Jambo hili ni katazo la uharaam katika istwilahi ya kishariy'ah. Ikiwa Qadhwi ametoa hukumu katika hali ya ghadhabu hukumu hiyo itakuwa na utata wa kuzingatiwa uhalaal wake.

[5] Hadiyth hii inatahadharisha kutoa hukumu kwa kumsikiliza mlalamikaji pekee kuwa si sahihi, ila atakapopewa anayelalamikiwa nafasi ya kujitetea. Katika kesi ambayo mlalamikiwa amekaa kimya, anakataa kujibu maswali au hajibu, kujieleza na hajali chochote na haji kusikiliza kesi yake hapo ni ruhusa kwa Qadhwi, hakimumu au jaji kutoa hukumu ya kesi ile.

[6] Hadiyth hii inabainishia nukta muhimu zifuatazo: ikiwa Qadhwi atatoa hukumu kinyume na hukumu yenyewe basi Allaah Ataiandika kuwa ni hukumu batili na hukumu sahihi Allaah Ataitoa siku ya Hukmu (Aakhirah). Pili, Nabiyy (ﷺ) hakuwa na elimu ya ghaibu. Vinginevyo, asingetoa maneno kama hayo.

[7] Hadiyth hii inasisitiza haki za wanyonge kutoka kwa watu wenye nguvu na mamlaka kuwa haki zao ni wajibu kupewa. Ikiwa kuna dhuluma inayofanyika katika nchi, basi watu wote watawajibika na dhulma ile.

[8] Nabiyy (ﷺ) amesema maneno hayo pindi watu wa Iran walipomtawalisha Khosru (binti wa Kisrah) akiwa kama mtawala wao. Suala la mwanamke kutawazwa kuwa ni jaji katika mahakama ni suala lenye utata miongoni mwa Wanazuoni. Hata hivyo, Wanazuoni wengi wana rai kuwa mwanamke hawezi kuwa jaji katika mahakama ya jinai.

[9] Swahaba anaitwa Al-Asadi, alikuwa Mhadhramiy. Alimtembelea Mu'aawiyah Shaam na akamsomea Hadiyth hii.

[10] Hadiyth hii inatupa fundisho kuwa ni haraam kwa mtawala kuwazuia watu wake na haja zao. Vivyo hivyo, hatakiwi kufunga milango ya

hukumu kwao, badili yake watu wote, maskini kwa tajiri waweze kuingia kwake katika mashauri yao bila kuzuiwa.

[11] Wote kwa pamoja mtoa rushwa na mpokea rushwa wamelaaniwa. Hali hii inajumuisha hali zote. Hali ya kwanza kwa anayetoa rushwa ili apate haki zake zinazomuhusu. Katika hali hii uharaam ni kwa anayechukuwa si kwa anayetoa. Hali ya pili ni ya yule mtu anayetoa rushwa ili apate zaidi ya kile anachostahiki kupata na kwa hiyo anatwaa haki ya mwingine. Rushwa katika hali hii inakuwa ni haraam kwa anayetoa na anayepokea.

[12] Tunapata mafundisho yafuatayo: (a) Kuwa mlalamikaji na mlalamikiwa wafanyiwe usawa, yeyote asipendelewe. (b) Kila mmoja kati ya mlalamikaji na mlalamikiwa watoe maelezo yao kwa hakim hali wakiwa wamekaa.

01-Mlango Wa Ushahidi

بَابُ الشَّهَادَاتِ

01-Mlango Wa Ushahidi

1201.

عَنْ زَيْدِ بْنِ خَالِدِ الْجُهَنِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "أَلَا أُخْبِرُكُمْ بِخَيْرِ الشُّهَدَاءِ؟ الَّذِي يَأْتِي بِشَهَادَتِهِ قَبْلَ أَنْ يُسْأَلَهَا" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Zayd bi Khaalid Al-Juhaniyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Je nikuambieni shahidi bora? Ni yule anayetoa ushahidi kabla hajaulizwa.”[1] [Imetolewa na Muslim]

1202.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "إِنَّ خَيْرَكُمْ قَرْنِي، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، ثُمَّ يَكُونُ قَوْمٌ يَشْهَدُونَ وَلَا يُسْتَشْهَدُونَ، وَيَخُونُونَ وَلَا يُؤْتَمَنُونَ، وَيَنْذَرُونَ وَلَا يُؤْفُونَ، وَيَظْهَرُ فِيهِمُ السَّمَنُ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika wabora wenu ni karne yangu, kisha wanaowafuatia, kisha wanaowafuatia. Kisha kutakuwa na watu wanaotoa ushahidi (wa uongo) wala hawakutakiwa kutoa ushahidi,[2] wanakhini wala hawaaminiwi, wanaweka nadhiri wala hawatekelezi, unene utadhihiri ndani yao.” [Bukhaariy, Muslim]

1203.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "لَا تَجُوزُ شَهَادَةُ خَائِنٍ، وَلَا خَائِنَةٍ، وَلَا ذِي غَمْرٍ عَلَى أَخِيهِ، وَلَا تَجُوزُ شَهَادَةُ الْقَانِعِ لِأَهْلِ الْبَيْتِ" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haufai ushahidi wa mfanya khiyana mwanamme wala mwanamke, wala mwenye chuki dhidi ya nduguye, wala haufai ushahidi wa mtumishi wa nyumbani.”[3] [Imetolewa na Ahmad na Abuu Daawuud]

1204.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "لَا تَجُوزُ شَهَادَةُ بَدَوِيٍّ عَلَى صَاحِبِ قَرْيَةٍ" } رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ، وَابْنُ مَاجَةَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa amemsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Ushahidi wa bedui dhidi ya mtu wa kijijini (au mjini) haufai.”[4] [Imetolewa na Abuu Daawuwd na Ibn Maajah]

1205.

وَعَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّهُ خَطَبَ فَقَالَ: إِنَّ أَنْاسًا كَانُوا يُؤْخَذُونَ بِالْوَحْيِ فِي عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَإِنَّ الْوَحْيَ قَدْ انْقَطَعَ، وَإِنَّمَا نَأْخُذُكُمْ الْآنَ بِمَا ظَهَرَ لَنَا مِنْ أَعْمَالِكُمْ } رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Umar bin Al-Khatwaab (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alikhutubia akasema: “Hakika baadhi ya watu katika zama za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) walipatilizwa kutokana na Wahyi. Na Wahyi umekatika si vinginevyo. Sasa tutawapatiliza kutokana na matendo yenu yanayotudhihirikia.”[5] [Imetolewa na Al-Bukaariy]

1206.

وَعَنْ أَبِي بَكْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ عَدَّ شَهَادَةَ الزُّورِ فِي أَكْبَرِ الْكَبَائِرِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ فِي حَدِيثٍ

Kutoka kwa Abuu Bakr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Aliuhesabu ushahidi wa uzushi katika dhambi kubwa.” [Bukhaariy, Muslim katika Hadiyth]

1207.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لِرَجُلٍ: "تَرَى الشَّمْسَ ؟" قَالَ: نَعَمْ. قَالَ: "عَلَى مِثْلِهَا فَاشْهَدْ، أَوْ دَعْ" } أَخْرَجَهُ ابْنُ عَدِيٍّ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ فَأَخْطَأَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alimuambia mtu mmoja: Unaona jua? Akasema: ‘Ndiyo’ akamuambia: kwa mfano wake toa ushahidi au wacha.”[6] [Imetolewa na Ibn ‘Adiyy kwa isnaad dhaifu. Akaisahihisha Al-Haakim lakini alikosea]

1208.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، { أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَضَى بِيَمِينٍ وَشَاهِدٍ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ. وَأَبُو دَاوُدَ. وَالنَّسَائِيُّ وَقَالَ: إِسْنَادُهُ جَيِّدٌ

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ. أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alihukumu kwa yamini na

wa shahidi mmoja.”[7] [Imetolewa na Muslim na Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na amesema: ‘Isnaad yake ni nzuri’

Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amepokea Hadiyth kama hii. Imepokewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan

1209.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ مِثْلَهُ. أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Hadiyth mfano wake imepokewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan

[1] Hawa ni wale wanaotoa ushahidi kwa ajili ya Allaah na kwa lengo la kupatikana kwa haki. Hawasubiri hadi dhalimu awakabili na kutoa ushahidi.

[2] Hawa ni wale wenye kutoa ushahidi tu kwa njia yoyote iwe ni haki au batili. Haya yanatoka katika undani wao ili kuupoteza ukweli. Hawa ni mashahidi wa aina mbaya sana.

[3] Ushahidi unaotolewa na mtu asiyekuwa mwaminifu haukubaliki, adui au mtu atakayetoa ushahidi kwa kumpendelea jamaa yake haukubaliki, kwani ushahidi kama huo mara nyingi unaelekea upande mmoja. Vivyo hivyo, hairuhusiwi kwa mtu kutoa ushahidi kwa mtu anayemkirimu kwa uwezekano mkubwa wa kumpendelea katika ushahidi wake. Ushahidi unatakiwa utolewe na mtu mwaminifu ambaye hatompendelea mmoja dhidi ya mwengine.

[4] Hii ni kwa sababu bedui hajui hali na mazingira ya watu wa mjini au kijijini na ndiyo maana wamekatazwa kutoa ushahidi kwao (kwa ajili au dhidi yao). Kwa mtu wa mjini kutoa kwa watu wa mjini mfano wao inaruhusiwa kwa kufahamu kwao mazingira ya wenzao wanaokaa mjini.

Ikiwa bedui anafahamu vizuri mazingira ya watu wa mjini basi anaruhusiwa kutoa ushahidi.

[5] Hadiyth hii inaelezea kuwa hukumu itatolewa kwa lililodhaniwa kuwa ni sawa. Ikiwa katika mashahidi kuna aliyesema uongo (pamoja na kuwa aliapa kuwa atasema kweli) dhambi itakuwa ni kwa yule aliyesema uongo. Kadhi au jaji hatohusika na makosa yale.

[6] Mtu anatakiwa atoe ushahidi kwa kile alichokuwa na hakika nacho au vinginevyo aache kutoa ushahidi wake. Kwa hali hiyo hatakiwi atoe ushahidi kwa kukisia au kudhanika au kwa kusikia maneno yasiyokuwa ya uhakika.

[7] Tunapata uthibitisho wa Hadiyth hii kuwa kama hakuna mashahidi wawili basi mmoja anatosheleza pamoja na kiapo cha mdai. Ikiwa katika hali ambayo hakuna shahidi, wakati huo kiapo cha madai hakitotosheleza katika kusimamisha madai yake. Katika hali hiyo, mdaiwa atatakiwa kuleta kiapo cha kukana mashtaka dhidi yake.

02-Mlango Wa Madai na Ushahidi

بَابُ الدَّعْوَى وَالْبَيِّنَاتِ

02-Mlango Wa Madai na Ushahidi[1]

1210.

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَوْ يُعْطَى النَّاسُ بِدَعْوَاهُمْ، لَادَّعَى نَاسٌ دِمَاءَ

رَجَالٍ، وَأَمْوَالَهُمْ، وَلَكِنَّ الْيَمِينَ عَلَى الْمُدَّعَى عَلَيْهِ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِلْبَيْهَقِيِّ بِإِسْنَادٍ صَحِيحٍ: { "الْبَيِّنَةُ عَلَى الْمُدَّعَى، وَالْيَمِينَ عَلَى مَنْ أَنْكَرَ {

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Lau watu wangepewa kulingana na madai yao, basi watu wengine wangedai damu za watu na mali zao.[2] Lakini yamini ni juu ya mdaiwa.” [Bukhaariy, Muslim]

Na amepokea Al-Bayhaqiyy kwa isnaad sahihi: “Ushahidi ni juu ya mdai na yamini ni juu ya aliyekana.”

1211.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَرَضَ عَلَى قَوْمِ الْيَمِينَ، فَأَسْرَعُوا، فَأَمَرَ أَنْ يُسْهَمَ بَيْنَهُمْ فِي الْيَمِينَ، أَيُّهُمْ يَخْلِفُ { رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Aliwaambia watu fulani waape, wakaharakisha. Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akaamrisha kupiga kura[3] baina yao nani kati yao aape.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1212.

وَعَنْ أَبِي أُمَامَةَ الْخَارِثِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "مَنْ اقْتَطَعَ حَقَّ امْرِئٍ مُسْلِمٍ بِيَمِينِهِ، فَقَدْ أَوْجَبَ اللَّهُ لَهُ النَّارَ، وَحَرَّمَ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ" } . فَقَالَ لَهُ رَجُلٌ: وَإِنْ كَانَ شَيْئًا يَسِيرًا يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: "وَإِنْ قَضَيْتُ مِنْ أَرَاكِ" { رَوَاهُ مُسْلِمٌ }

Kutoka kwa Abuu Umaamah Al-Haarithiy[4] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakayejichukulia haki ya mtu Muislaam kwa kiapo chake, hakika Allaah Amekwishamuajibishia moto na Amemharamishia Jannah. Mtu mmoja akasema: ‘Ee Rasuli wa Allaah! Hata kama ni kitu kidogo? Akasema: hata kama ni kipande cha mswaki.”[5] [Imetolewa na Muslim]

1213.

وَعَنْ الْأَشْعَثِ بْنِ قَيْسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { "مَنْ حَلَفَ عَلَى يَمِينٍ، يَقْتَطِعُ بِهَا مَالَ امْرِئٍ مُسْلِمٍ، هُوَ فِيهَا فَاجِرٌ، لَقِيَ اللَّهَ وَهُوَ عَلَيْهِ غَضَبَانُ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Al-Ash’ath bin Qays[6] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakayeapa yamini ili ajikatie mali ya mtu Muislaam ilihali katika hilo ni muovu; atakutana na Allaah ilihali Amemghadhibikia.” [Bukhaariy, Muslim]

1214.

وَعَنْ أَبِي مُوسَى الْأَشْعَرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَجُلَيْنِ
اخْتَصَمَا إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي دَابَّةٍ، لَيْسَ
لِوَاحِدٍ مِنْهُمَا بَيِّنَةٌ، فَقَضَىٰ بِهَا رَسُولُ اللَّهِ بَيْنَهُمَا نِصْفَيْنِ {
رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ وَهَذَا لَفْظُهُ، وَقَالَ: إِسْنَادُهُ
جَيِّدٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Muwsaa Al-Ash'ariyy amesema kuwa: “Watu wawili waligombania mnyama, wala hakuna yeyote kati yao mwenye ushahidi. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akahukumu baina yao nusu mbili.”[7] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na An-Nasaaiy, Hadiyth hii ni tamshi lake na akasema: Isnaad yake ni nzuri]

1215.

وَعَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
قَالَ: { "مَنْ حَلَفَ عَلَى مَنْبَرِي هَذَا بِيَمِينِ آثِمَةٍ، تَبَوَّأَ مَقْعَدَهُ
مِنَ النَّارِ" } رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ
حِبَّانَ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy amesema kuwa: “Atakayeapa juu ya mimbari yangu hii kwa yamini ya dhambi, basi ameandaa makazi yake motoni.”[8] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1216.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {ثَلَاثَةٌ لَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ، وَلَا يُزَكِّيهِمْ، وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ: رَجُلٌ عَلَى فَضْلِ مَاءٍ بِالْفَلَاةِ، يَمْنَعُهُ مِنْ ابْنِ السَّبِيلِ; وَرَجُلٌ بَايَعَ رَجُلًا بَسْلَعَةً بَعْدَ الْعَصْرِ، فَحَلَفَ لَهُ بِاللَّهِ: لَا أَخَذَهَا بَكْذَا وَكَذَا، فَصَدَّقَهُ، وَهُوَ عَلَى غَيْرِ ذَلِكَ; وَرَجُلٌ بَايَعَ إِمَامًا لَا يُبَايِعُهُ إِلَّا لِلدُّنْيَا، فَإِنْ أَعْطَاهُ مِنْهَا، وَفَى، وَإِنْ لَمْ يُعْطِهِ مِنْهَا، لَمْ يَفِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu watatu[9] Allaah Hatawasemesha Siku ya Qiyaamah wala Hatawatazama wala Hatawatakasa na wana adhabu kali: (a) mtu mwenye maji ya ziada jangwani na anamyima msafiri, (b)mtu aliyeuziana bidhaa na mtu baada ya Al-‘Aswr akaapa kwa kadha wa kadha, akamuamini na yeye si hivyo, (c) na mtu aliyembai kiongozi kwa ajili ya dunia tu akimpa kitu hutekeleza na asipompa kitu hatekelezi.” [Bukhaariy, Muslim]

1217.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {أَنَّ رَجُلَيْنِ اخْتَصَمَا فِي نَاقَةٍ، فَقَالَ كُلُّ وَاحِدٍ مِنْهُمَا نُتِجْتُ عِنْدِي، وَأَقَامَا بَيْنَهُ، فَقَضَى بِهَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِمَنْ هِيَ فِي يَدِهِ}

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Watu wawili waligombania ngamia, kila mmojawapo akasema: ‘Ngamia huyu amezaliwa kwangu’ na wao wakaleta uthibitisho. Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akahukumu ngamia huyo ni wa ambaye yuko mkononi mwake.”

1218.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَدَّ الْيَمِينَ عَلَى طَالِبِ الْحَقِّ} رَوَاهُمَا الدَّارَقُطْنِيُّ، وَفِي إِسْنَادِهِمَا ضَعْفٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alirudisha yamini ya mwenye kutafuta haki.” [Imetolewa na Ad-Daaraqutwniyy na katika isnaadi zake kuna udhaifu]

1219.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا {قَالَتْ: دَخَلَ عَلَيَّ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ذَاتَ يَوْمٍ مَسْرُورًا، تَبَرَّقَ أَسَارِيرُ وَجْهِهِ. فَقَالَ: "أَلَمْ تَرِي إِلَى مُجَزَّزِ الْمُدْلَجِيِّ؟ نَظَرَ أَنْفًا إِلَى زَيْدِ بْنِ حَارِثَةَ، وَأَسَامَةَ بْنِ زَيْدٍ، فَقَالَ: " هَذِهِ أَقْدَامُ بَعْضِهَا مِنْ بَعْضٍ " } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliingia kwangu hali ni mwenye furaha, uso wake wameremeta. Akasema: “Je umemuona Mujazzizin Al-Mudlijiyy?[10] Muda mfupi amemtazama Zayd bin Haarithah na Usaamah bin Zayd akasema: “Hakika nyayo hizi baadhi yake zinatokana na baadhi nyingine.” [Bukhaariy, Muslim]

[1] Maana ya Da’waa (mashtaka au ulingano) ni kuweka madai ya mtu katika kitu kwa kusema: “Ni haki ya kitu kadha wa kadha.” Bila kujali madai hayo yaliyowekwa ni kweli au si kweli. Bayyinah ina maana ya jambo lililo wazi, bayana, maadamu inathibitisha haki ya kishariy’ah ya mmiliki katika kitu kinachogombewa.

[2] Moja katika kanuni za msingi za shariy’ah ni kuwa mdai ni lazima athibitishe ukweli wa madai yake kwa kuleta vithibitisho, kuleta mashahidi n.k. mdaiwa au mshtakiwa ni lazima athibitishe ukweli wa madai yake kwa kuthibitisha au kwa kukana. Kama hili halijafanyika, mdaiwa anatakiwa alete ushahidi wa kukana madai au aape. Katika kesi ya mtuhumiwa mauaji ni kuwa mdaiwa (kama hali itaruhusu) anatakiwa alete mashahidi 50 watakaotoa kiapo. Akishindwa mdaiwa kufanya hivyo, au mdai kutoamini viapo vile, basi wakati huo anaweza kuleta viapo kama vile na kutaka alipwe fidia.

[3] Ikiwa mazingira ya madai ni imetokea kuwa makundi yote hasimu kila kimoja ni mdai na mdaiwa kwa wakati huo mmoja, basi makundi yote yanawajibika kutoa kiapo. Ikiwa kundi moja limekataa kutoa kiapo, kundi hasimu linatakiwa lifanye hivyo na kuchukua kinachogombaniwa. Kama hali itakuwa ni kwa makundi yote kuwa tayari kutoa viapo, mwenye kustahiki ataamuliwa kwa kura. Jina lolote litakalotokeza katika utaratibu huo atachukua kiapo kisha atachukuwa kitu kinachogombewa.

[4] Huyu ni Abuu Umaamah Iyaas bin Tha’labah Al-Answaar Al-Haarith Al-Khazraji. Inasemekana ni katika kabila la Balawi lililokuwa mshirika na Answaar. Alikuwa ni Swahaba wa kitambo, hakushiriki Badr kwa kuwa alikuwa akimuuguza mama yake.

[5] Hadiyth hii inathibitisha kuwa mtu akitoa kiapo cha uongo na kuchukua kitu cha mtu (hata kikiwa ni kidogo kiasi gani) au akamkosesha mtu mwenye haki na kitu chake, mtu huyo ataharamishiwa Jannah.

[6] Al-Ash'ath bin Qays bin Ma'dikarib Al-Kindi, Abuu Muhammad kwa jina lingine alikuwa ni Swahaba aliyeishi katika mji wa Kufa 'Iraq. Alipoteza macho yake mawili katika vita vya Yarmuk. Alikuwa ni mtu karimu na mwema. Alichaguliwa kuwa ni gavana wa Azerbaijan na alihudhuria Siffin akiwa na 'Aliy. Alifariki baada ya siku arubaini ya kifo cha 'Aliy katika mwaka 40 Hijriyyah akiwa na umri wa miaka 63.

[7] Hii ni hali ambayo makundi yote mawili yanadai kitu kimoja. Ima hawakuwa tayari kuapa, au hawakuwa na mashahidi wa kuthibitisha madai yao. Hii ina maana walikuwa katika hadhi moja kuhusu madai yao. Ikiwa jambo katika mazingira kama haya litatokea, basi kitu kinachogombewa kitabaki kwa aliye nacho. Ikiwa hakuna aliyekuwa nacho, au kitu hicho kipo katika umiliki wa nusu kwa nusu, basi hukumu ni kukigawa kitu kinachogombewa mara mbili na kila mmoja kupata nusu yake.

[8] Hadiyth hii inaonesha kuwa uzito wa dhambi unategemea ni sehemu mtu aliyefanyia kitu kile na wakati alioufanya.

[9] Hadiyth hii inalinganisha watu wenye madhambi, kuwa hali zao zitakuwa mbaya sana, na wanastahiki ghadhabu za Allaah.

[10] Imepokelewa kuwa Zayd bin Haarith muachwa huru wa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alielekea kuwa mweupe zaidi ilihali mwanae Usaamah alikuwa mweusi. Kwa ajili ya hili baadhi ya makafiri wakashuku nasaba ile. Mujazzizin Al-Mudlijiyy aliwaona wakiwa wamelala, wamejifunika nyuso zao na miguu yao ikiwa wazi. Alipoona miguu yao alisema maneno hayo ambayo yalimfurahisha Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Hii ni dalili ya kuwa mtu anapopata mashaka na kitu ni bora akapata ushauri wa wataalamu kama huyo bwana mtaalamu wa nasaba alivyofanya.

كِتَابُ الْعِتْقِ

Kitabu Cha Ukombozi

كِتَابُ الْعِتْقِ - 15-Kitabu Cha Ukombozi

00-Kitabu Cha Ukombozi

1220.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "أَيُّمَا امْرِئٍ مُسْلِمٍ أَعْتَقَ امْرَأً مُسْلِمًا، اسْتَنْقَذَ اللَّهُ بِكُلِّ عُضْوٍ مِنْهُ عُضْوًا مِنْهُ مِنَ النَّارِ" } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ وَلِلتِّرْمِذِيِّ وَصَحَّحَهُ، عَنْ أَبِي أُمَامَةَ: { "وَأَيُّمَا امْرِئٍ مُسْلِمٍ أَعْتَقَ امْرَأَتَيْنِ مُسْلِمَتَيْنِ، كَانَتَا فِكَاهَهُ مِنَ النَّارِ" } وَلِأَبِي دَاوُدَ: مِنْ حَدِيثِ كَعْبِ بْنِ مُرَّةَ: { "وَأَيُّمَا امْرَأَةٍ أَعْتَقْتَ امْرَأَةً مُسْلِمَةً، كَانَتْ فِكَاهَهَا مِنَ النَّارِ" }

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muislaam yeyote atakayemkomboa Muislaam mwenzake, Allaah Atamuacha huru na moto,[1] kila kiungo chake kwa kila kiungo cha mtu huyo.” [Bukhaariy, Muslim]

At-Tirmidhiy amepokea na ameisahihisha kutoka kwa Abuu Umaamah: “Na mtu yeyote Muislaam atakayekomboa wanawake wawili Waislaam basi watakuwa ni kuokoka kwake dhidi ya moto.”

Abuu Daawuwd amepokea kutoka katika Hadiyth ya Ka’b bin Murrah[2]: “Na mwanamke yeyote Muislaam atakayemkomboa mwanamke Muislaam basi atakuwa ni kuokoka kwake dhidi ya moto.”

1221.

وَعَنْ أَبِي ذَرٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { قَالَ: سَأَلْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَيُّ الْعَمَلِ أَفْضَلُ؟ قَالَ: "إِيمَانُ بِاللَّهِ، وَجِهَادٌ فِي سَبِيلِهِ". قُلْتُ: فَأَيُّ الرِّقَابِ أَفْضَلُ؟ قَالَ: "أَعْلَاهَا تَمَنَّا، وَأَنْفُسُهَا عِنْدَ أَهْلِهَا" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Dharr (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilimuuliza Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ni amali gani bora zaidi? Akasema: ‘Ni kumuamini Allaah na jihaad katika njia yake’ Nikasema: ni kuacha kupi mtumwa huru kuliko bora? Akasema: “Mwenye thamani kubwa na mzuri zaidi kwa watu wake.” [Bukhaariy, Muslim]

1222.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "مَنْ أَعْتَقَ شِرْكًَا لَهُ فِي عَبْدٍ، فَكَانَ لَهُ مَالٌ

يَبْلُغُ ثَمَنَ الْعَبْدِ، قَوْمَ قِيَمَةِ عَدْلٍ، فَأَعْطَى شُرَكَاءَهُ حِصَصَهُمْ،
وَعَتَّقَ عَلَيْهِ الْعَبْدُ، وَإِلَّا فَقَدْ عَتَّقَ مِنْهُ مَا عَتَّقَ" { مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ -
وَلَهُمَا: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { "وَإِلَّا قَوْمٌ عَلَيْهِ،
وَاسْتُسْعِيَ غَيْرَ مَشْقُوقٍ عَلَيْهِ" } وَقِيلَ: إِنَّ السَّعَايَةَ مُدْرَجَةٌ
فِي الْخَبَرِ -

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuacha
huru fungu lake katika mtumwa akawa na mali inayofikia thamani ya
mtumwa (yule), atathaminishwa thamani ya uadilifu awape
washirika wake mafungu yao na atamuacha huru mtumwa.[3]
Vinginevyo atakuwa ameacha huru katika fungu lake.” [Bukhaariy,
Muslim]

Wamepokea kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ): “La si
hivyo atathaminishwa na aombwe kufanya kazi ili alipie ushuru
wake bila kumtia uzito.” Imesemwa haya ya kufanya kazi ni maneno
Mudrajaah (yaliyoingizwa na siyo ya Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ
وَسَلَّمَ

1223.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { " لَا يَجْزِي وَلَدٌ وَالِدَهُ، إِلَّا أَنْ يَجِدَهُ مَمْلُوكًا
فَيُعْتِقَهُ" } رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa
Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtoto hawezi

kumlipa mzazi wake isipokuwa amkute ni mtumwa amnunue na amuache huru.”[4] [Imetolewa na Muslim]

1224.

وَعَنْ سَمُرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {“مَنْ مَلَكَ ذَا رَحِمٍ مَحْرَمٍ، فَهُوَ حُرٌّ”} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْأَرْبَعَةُ وَرَجَّحَ جَمْعٌ مِنَ الْحُفَّازِ أَنَّهُ مَوْقُوفٌ^{٢٤}

Kutoka kwa Samurah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kumiliki mwenye kizazi ambaye ni maharimu,[5] basi yuko huru.” [Imetolewa na Ahmad na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah). Kundi la wahifadhi Hadiyth wametilia nguvu kuwa ni Mawquwf]

1225.

وَعَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، {أَنَّ رَجُلًا أَعْتَقَ سِتَّةَ مَمْلُوكِينَ لَهُ، عِنْدَ مَوْتِهِ، لَمْ يَكُنْ لَهُ مَالٌ غَيْرَهُمْ، فَدَعَا بِهِمْ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَجَزَّاهُمْ أَثْلَاثًا، ثُمَّ أَقْرَعَ بَيْنَهُمْ، فَأَعْتَقَ اثْنَيْنِ، وَأَرَقَّ أَرْبَعَةً، وَقَالَ لَهُ قَوْلًا شَدِيدًا} رَوَاهُ مُسْلِمٌ^{٢٥}

Kutoka kwa ‘Imraan bin Huswayn (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa: “Mtu mmoja aliwaacha huru watumwa sita wakati wa kifo chake wala hakuwa na mali zaidi ya hiyo.[6] Rasuli wa Allaah

(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akawaita akawagawa mafungu matatu kisha akapiga kura miongoni mwao, akawaacha huru wawili na wanne akawabakisha kwenye utumwa. Na akamuambia maneno mazito yule mwenyewe.”[7] [Imetolewa na Muslim]

1226.

وَعَنْ سَفِينَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ {قَالَ: كُنْتُ مَمْلُوكًا لِأُمِّ سَلَمَةَ فَقَالَتْ: أَعْتَقُكَ، وَأَشْتَرِطُ عَلَيْكَ أَنْ تَخْدِمَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَا عِشْتَ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Safiynah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Nilikuwa mtumwa wa Ummu Salamah akaniambia: ‘Nitakuacha huru na nitakupa sharti uwe ukimtumikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) katika maisha yako.”[8] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuwd, An-Nasaaiy na Al-Haakim]

1227.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {“إِنَّمَا أَلَوْلَاءُ لِمَنْ أَعْتَقَ”} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ فِي حَدِيثٍ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Al-

Walaau ni wa mwenye kuacha huru.”[9] [Bukhaariy, Muslim katika Hadiyth ndefu]

1228.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { "الْوَلَاءُ لِحِمَّةٍ كُلِّحِمَةٍ النَّسَبِ، لَا يُبَاعُ وَلَا يُوهَبُ" } رَوَاهُ الشَّافِعِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ وَأَصْلُهُ فِي "الصَّحِيحَيْنِ" بِغَيْرِ هَذَا اللَّفْظِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Al-Walaau ni undugu kama undugu wa nasaba, hauuzwi wala hautolewi bure (hiba/zawadi).” [Imetolewa na Ash-Shaafi’iy na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim. Asili yake imo katika Swahiyh Al-Bukhaariy na Swahiyh Al-Muslim kwa tamshi [lingine](#) lisilokuwa hili]

[1] Malipo na thawabu ayapatayo mtu ni yale ya kumuacha huru mtumwa Muumini, Pamoja na kuwa kuna malipo na fadhila za kumuacha huru mtumwa kafiri. Hata hivyo kumuacha huru mtumwa Muumini kuna malipo makubwa zaidi.

[2] Ka’b bin Murrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) alikuwa ni Swahaba na inasemekana kuwa alikuwa akiitwa Murrah bin Ka’b. Aliishi Basra kisha akahamia Jordan hadi yalipomkuta mauti yake mwaka 57 au 59 Hijriyyah.

[3] Hadiyth hii inatujulisha kuwa mtumwa ambae ameacha huru nusu ana hadhi ya dhamana iliyoziwa hawezi kuuzwa au kutolewa kama zawadi.

[4] Kulingana na Hadiyth hii Wanazuoni wa Zahiriyah wana muono kuwa baba hawezi kuzingatiwa kuwa yuko huru kwa sharti la kulipiwa na mwanae, bali atakuwa huru hadi mwanae atakapotamka hivyo. Wanazuoni wengine wanaona kuwa baba keshakuwa huru madamu amenunuliwa na mwanae. Hukumu hii pia inamhusu mama. Hadiyth hii kwa upande mmoja

inatuelezea nafasi za wazazi wawili na kwa upande mwingine inaelezea fadhila za kumuacha huru mtumwa.

[5] Ndugu wa karibu kama vile baba, mtoto, kaka, dada, ndugu ya baba, kaka wa mama n.k. ambao wapo karibu kiasi cha kuwa huwezi kuoa (au kuolewa) hawawezi kuwa katika hadhi ya mtumwa na bwana wake. Ikiwa aliyekuwa utumwani ni mwanamke, basi hukumu inakuwa ni wazi zaidi. Katika hali hiyo itaangaliwa kama wanaweza kuoana au sivyo. Kama ni sawa, basi hukumu ile inatumika kwao, kwani watakuwa ni Mahram.

[6] Mafundisho tunayoyapata katika Hadiyth hii ni kuwa swadaqah inayotolewa na mtu mgonjwa ni kama vile kuacha wasia. Mtu haruhusiwi kuacha wasia zaidi ya theluthi ya mali yake au kama ni zawadi au wakfu. Maneno makali aliyoyasema Nabiyy (ﷺ) kwa mtu yule yalikuwa: “Kama ningejulishwa habari za mtu yule hapo kabla basi nisingeruhusu kuzikwa katika makaburi ya Waislaam.”

[7] Kwa sababu theluthi mbili za mali ya marehemu yanatakiwa kuenda kwa warithi wake.

[8] Kuwa inawezekana kuweka sharti unapoacha huru mtumwa kama alivyofanya Ummu Salamah kuwa aendeleo kumtumikia Nabiyy (ﷺ) kwa muda uliokubaliwa. Uhalaal wa hili unaonekana pale Nabiyy (ﷺ) alipokuwa hakulikataza jambo hili.

[9] Al-Walaau ni mirathi ya mtumwa aliyeachwa huru inamilikiwa na aliyemuacha huru. Haitakiwi kuuzwa wala kutolewa zawadi.

كِتَابُ الْعِتْقِ

Kitabu Cha Ukombozi

01-Mlango Wa Mudabbar, Al-Mukaatab Na Ummul-Walad

بَابُ الْمُدَبَّرِ وَالْمُكَاتَّبِ وَأُمِّ الْوَلَدِ

01-Mlango Wa Mudabbar,[1] Al-Mukaatab[2] Na Ummul-Walad[3]

1229.

عَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ { أَنَّ رَجُلًا مِنْ الْأَنْصَارِ
أَعْتَقَ غُلَامًا لَهُ عَنْ دُبُرٍ، لَمْ يَكُنْ لَهُ مَالٌ غَيْرُهُ، فَبَلَغَ
ذَلِكَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ . فَقَالَ: "مَنْ يَشْتَرِيهِ
مِنِّْي؟" فَاشْتَرَاهُ نَعِيمُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ بِثَمَانِمِائَةِ دِرْهَمٍ { مُتَّفَقٌ
عَلَيْهِ . وَفِي لَفْظٍ لِلْبُخَارِيِّ: فَاحْتَاجَ وَفِي رِوَايَةٍ لِلنَّسَائِيِّ:
{ وَكَانَ عَلَيْهِ دَيْنٌ، فَبَاعَهُ بِثَمَانِمِائَةِ دِرْهَمٍ، فَأَعْطَاهُ
وَقَالَ: " إِقْضِ دَيْنَكَ" }

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa: “Mtu mmoja miongoni mwa Answaar aliahidi uhuru wa mtumwa wake[4] baada ya kufa hakuwa na mali isipokuwa mtumwa huyo. Habari hiyo ikamfikia Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: ‘Ni nani atakayemnunua?’ Nu’aym bin ‘Abdillaah[5] akamnunua kwa dirhamu mia nane.” [Bukhaariy, Muslim, katika tamshi lingine la Al-Bukhaariy: ‘akahitajia’]

Katika Riwaayah ya An-Nisaa’iy: “Alikuwa ana deni akamuuzwa kwa dirhamu mia nane na akampa mwenyewe akamuambia: ‘lipa deni lako’.”

1230.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {قَالَ: " الْمُكَاتَبُ عَبْدٌ مَا بَقِيَ عَلَيْهِ مِنْ مُكَاتَبَتِهِ دِرْهَمٌ " } أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ وَأَصْلُهُ عِنْدَ أَحْمَدَ، وَالثَّلَاثَةُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb amepokea kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ) amesema: “Al-Mukaatab ni mtumwa madamu katika mkataba wake imebakia dirhamu moja.”[6] [Imetolewa na Abuu Daawuud kwa Isnaad Hasan. Asili yake imo kwa Ahmad na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na akaisahihisha Al-Haakim]

1231.

وَعَنْ أُمِّ سَلَمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا كَانَ لِإِحْدَاكُنَّ مُكَاتَبٌ، وَكَانَ عِنْدَهُ مَا يُؤَدِّي، فَلْتَحْتَجِبِي مِنْهُ} رَوَاهُ الْخَمْسَةُ وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

Kutoka kwa Ummu Salamah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Iwapo mmoja wenu ana Mukaatab naye anacho cha kutoa basi ajisitiri kwake.”[7] [Imetolewa na Al-Khamsah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy,

Abuu Daawuud, Ibn Maajah, Ahmad) na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

1232.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {يُودَى الْمُكَاتَبُ بِقَدْرِ مَا عَتَقَ مِنْهُ دِيَّةَ الْحُرِّ، وَبِقَدْرِ مَا رَقَّ مِنْهُ دِيَّةَ الْعَبْدِ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَأَبُو دَاوُدَ، وَالنَّسَائِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Al-Mukaatab hufidiwa fidiya ya muungwana kiasi alicholipia katika mali ya kuandikiana na hufidiwa fidiya ya mtumwa kiasi kilichobakia katika deni.”[8] [Imetolewa na Ahmad, Abuu Daawuud na An-Nisaiy]

1233.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ الْحَارِثِ أَخِي جُوَيْرِيَةَ أُمِّ الْمُؤْمِنِينَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {مَا تَرَكَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عِنْدَ مَوْتِهِ دِرْهَمًا، وَلَا دِينَارًا، وَلَا عَبْدًا، وَلَا أَمَةً، وَلَا شَيْئًا، إِلَّا بَغَلَتُهُ الْبَيْضَاءُ، وَسِلَاحُهُ، وَأَرْضًا جَعَلَهَا صَدَقَةً} رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Amr bin Al-Haarith[9] nduguye Juwayriyah Ummul-Mu-miniyna (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alipofariki hakuacha dirhamu wala dinari wala mtumwa wala mjakazi wala chochote isipokuwa nyumbu wake mweupe, silaha yake na ardhi aliyoitoa swadaqah.” [10] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1234.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَيُّمَا أَمَةٍ وَلَدْتُ مِنْ سَيِّدِهَا، فَهِيَ حُرَّةٌ بَعْدَ مَوْتِهِ} أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَالْحَاكِمُ بِإِسْنَادٍ ضَعِيفٍ وَرَجَّحَ جَمَاعَةٌ وَقَفَّهٖ عَلَى عُمَرَ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mjakazi yeyote aliyezaa na bwana wake, basi yuko huru baada ya kufa kwake.” [Imetolewa na Ibn Maajah na Al-Haakim kwa Isnaad Dhaifu. Kundi la Wanazuoni wa Hadiyth wana mtazamo kuwa Hadiyth hii ni Mawquwf kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ)]

1235.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ حُنَيْفٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ أَعَانَ مُجَاهِدًا فِي

سَبِيلَ اللَّهِ، أَوْ غَارِمًا فِي عُسْرَتِهِ، أَوْ مُكَاتِبًا فِي رَقَبَتِهِ،
أَظْلَهُ اللَّهُ يَوْمَ لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّهُ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَصَحَّحَهُ
الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Sahl bin Hunayaf (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:
“Mwenye kumsaidia mpigana jihaad katika Njia ya Allaah, au
mwenye deni katika uzito wake, au Mukaatab katika utumwa wake,
Allaah Atamfunika kivuli siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa
kivuli Chake.” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Al-Haakim]

[1] Ni maneno anayoambiwa mtumwa na bwana wake, “Uko huru baada ya kufa kwangu.”

[2] Mtumwa anapoingia katika mkataba na bwana wake ili anunue uhuru wake.

[3] Kijakazi anayemzalia bwana wake.

[4] Tumejifunza katika Hadiyth hii kuwa bwana anaweza kumuacha mtumwa wake Mudabbar, maadamu ya kuwa hayuko katika hali ya ugonjwa. Wanazuoni wana muono kuwa ichukuliwe kutoka katika theluthi ya mali yake kama usia. Wanazuoni wengine wanaona kuwa ruhusa kumuuza Mudabbar ila kwa mahitaji, au kulipa madeni ya bwana wake.

[5] Kun-ya yake ilikuwa ni An-Nakhkham, alikuwa Mqurayshi wa ukoo wa ‘Aad. Alisilimu mda mrefu akafanya kuwa ni siri, alipotaka kuhama watu wa kabila lake wakamtaka akae na afuate dini aitakayo, kwani alikuwa akiwasaidia wajane wao na mayatima wao, hivyo alibaki. Alihama katika mwaka wa Hudaybiyah. Aliuwawa katika Fat-hi ya Shaam wakati wa Ukhalifa wa Abuu Bakr Asw-Swidiq au wa ‘Umar Al-Faruwq.

[6] Ina maana kuwa ikiwa Al-Mukaatab hajamaliza deni lake kulipa dhamana yake, ataendelea kubaki kuwa ni mtumwa. Hili linathibitisha nukta moja kuwa mtumwa anamiliki anachopata. Haina maana kuwa mtumwa hawezi kumiliki kitu. Al-Mukaatab ni mwanamme au mwanamke mtumwa ambaye anaingia katika mkataba na bwana wake kuwa iwapo atamuacha huru atampa kadha na kadha kwa ajili ya uhuru wake. Aina hii ya mkataba unaitwa Mukaatabah na mtumwa anayeingia katika mkataba huu anaitwa Al-Mukaatab.

[7] Bi mkubwa kishariy'ah hana haja ya kuficha uso wake kwa mtumwa wake, kwani anakuwa kama mtoto wake. Lakini ikiwa Al-Mukaatab ameshakusanya kiasi cha fedha cha kujikomboa, itabidi aanze kuvaa hijab kamili kwake. Hadiyth hii inabainisha kuwa maadamu Al-Mukaatab hajakamilisha malipo kamili katika mkataba wake bado anahesabiwa kuwa ni mtumwa.

[8] Al-Khatwaab amesema: “Makubaliano ya Wanazuoni wa Fiqh ni kuwa Al-Mukaatab ni mtumwa kulingana na adhabu pamoja na fidiya, muda wa kuwa bado hajakamilisha dirhamu moja. Hata hivyo, Ibraahiym An-Nakhai na rai kutoka kwa ‘Aliy wanakubaliana na maana ya wazi yaliyopokewa kutoka kwenye Hadiyth hii.”

[9] Huyu ni Al-Haarith bin Abuu Dhirar bin Habib Al-Khuza'i Al-Mustwaliqi. Alikuwa ni Swahaba na ana Hadiyth moja tu kulingana na Wanazuoni wa Hadiyth.

[10] Nabiyy (ﷺ) alipofariki, Maria Qibtwiyyah mama wa mtoto wa Nabiyy (ﷺ) Ibraahiym alikuwa bado yu hai. Alikuwa ni mtumwa wa Nabiyy (ﷺ). Kwa kuwa alikuwa mama wa mtoto wa Nabiyy (ﷺ), alikuwa huru baada ya Rasuli wa Allaah (ﷺ) kufariki. Lengo la kutaja Hadiyth hii ni kuwa Ummul-Walad (mtumwa wa kike aliyemzalia bwana wake), anakuwa huru baada ya kufariki bwana mwenyewe.

كِتَابُ الْجَامِعِ

Kitabu Cha Mjumuisho

16-Kitabu Cha Mjumuisho - كِتَابُ الْجَامِعِ

01-Mlango Wa Adabu

بَابُ الْأَدَبِ

01-Mlango Wa Adabu

1236.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {حَقُّ الْمُسْلِمِ عَلَى الْمُسْلِمِ سِتٌّ: إِذَا لَقِيْتَهُ فَسَلَّمَ عَلَيْهِ، وَإِذَا دَعَاكَ فَأَجِبْهُ، وَإِذَا اسْتَنْصَحَكَ فَاَنْصَحْهُ، وَإِذَا عَطَسَ فَحَمِدَ اللَّهَ فَسَمِّتْهُ وَإِذَا مَرِضَ فَعُدْهُ، وَإِذَا مَاتَ فَاتَّبِعْهُ} رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haki ya

Muislaam juu ya Muislaam ni sita:[1] unapokutana naye msalimie, anapokualika muitike, anapokutaka nasaha mnasihi, anapopiga chafya na akamhimidi Allaah mrehemu, anapougua mtembelee na akifa msindiize.” [Imetolewa na Muslim]

1237.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {انْظُرُوا إِلَى مَنْ هُوَ أَسْفَلَ مِنْكُمْ، وَلَا تَنْظُرُوا إِلَى مَنْ هُوَ فَوْقَكُمْ، فَهُوَ أَجْدَرُ أَنْ لَا تَزْدَرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtazameni ambaye yuko chini yenu[2] wala msimtazame ambaye yuko juu yenu, kwani kufanya hivyo hamtadharau neema za Allaah juu yenu.” [Bukhaariy, Muslim]

1238.

وَعَنْ النَّوَّاسِ بْنِ سَمْعَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ الْبِرِّ وَالْإِثْمِ؟ فَقَالَ: {الْبِرُّ: حُسْنُ الْخُلُقِ، وَالْإِثْمُ: مَا حَاكَ فِي صَدْرِكَ، وَكَرِهْتَ أَنْ يَطَّلَعَ عَلَيْهِ النَّاسُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Anawwaas bin Sam'aan[3] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nilimuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) (وَسَلَّمَ): “Kuhusu wema na dhambi, akasema: “Wema ni tabia njema, [4] na dhambi[5] ni inayotia shaka katika nafsi yako na ukachukia watu kuona.” [Imetolewa na Muslim]

1239.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا كُنْتُمْ ثَلَاثَةً، فَلَا يَتَنَاجَى اثْنَانِ دُونَ الْآخَرِ، حَتَّى تَخْتَلِطُوا بِالنَّاسِ؛ مِنْ أَجْلِ أَنْ ذَلِكَ يُحْزِنُهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ، وَاللَّفْظُ لِمُسْلِمٍ.

Kutoka kwa Ibn Mas-'uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mnapokuwa watatu, wawili wasinong'one bila yule mwingine (kusikia)[6] mpaka mchanganyike na watu, kwani hilo litamhuzunisha.” [Bukhaariy, Muslim na tamshi hili ni la Muslim]

1240.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا يُقِيمُ الرَّجُلُ الرَّجُلَ مِنْ مَجْلِسِهِ، ثُمَّ يَجْلِسُ فِيهِ، وَلَكِنْ تَفَسَّحُوا، وَتَوَسَّعُوا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mmoja wenu asimsimamishie mtu kwenye kikao chake kisha akaketi yeye,[7] lakini kunjukeni na toeni nafasi.” [Bukhaariy, Muslim]

1241.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا أَكَلَ أَحَدُكُمْ طَعَامًا، فَلَا يَمْسَحْ يَدَهُ، حَتَّى يُلْعَقَهَا، أَوْ يُلْعِقَهَا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anapomaliza kula mmoja wenu asipanguse vidole vyake mpaka avirambe au avirambishe.”[8] [Bukhaariy, Muslim]

1242.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَيْسَ لِلصَّغِيرِ عَلَى الْكَبِيرِ، وَالْمَارِّ عَلَى الْقَاعِدِ، وَالْقَلِيلِ عَلَى الْكَثِيرِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ
وَفِي رِوَايَةٍ لِمُسْلِمٍ: {وَالرَّاكِبُ عَلَى الْمَاشِي}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mdogo amsalimie

mkubwa, anayetembea amsalimie aliye kaa,[9] na wachache wawasalimie wengi.” [Bukhaariy, Muslim]

Na katika Riwaayah ya Muslim: “...na aliyepanda amsalimie anayetembea.”

1243.

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يُجْزَى عَنْ الْجَمَاعَةِ إِذَا مَرُّوا أَنْ يُسَلِّمَ أَحَدُهُمْ، وَيُجْزَى عَنْ الْجَمَاعَةِ أَنْ يَرُدَّ أَحَدُهُمْ} رَوَاهُ أَحْمَدُ، وَالْبَيْهَقِيُّ

Kutoka kwa ‘Aliy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kundi linatoshelezwa kwa mtu mmoja wao kusalimia, na mtu mmoja wao hutosheleza anapojibu salaam.”[10] [Imetolewa na Ahmad na Al-Bayhaqiyy]

.1244

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا تَبْدُؤُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى بِالسَّلَامِ، وَإِذَا لَقِيتُمُوهُمْ فِي طَرِيقٍ، فَاضْطَرُّوهُمْ إِلَى أَضْيَقِهِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msianze kuwasalimia Mayahudi wala Manaswara,[11] munapokutana na

mmoja wao njiani msogezeni upande wenye dhiki zaidi.”[12]
[Imetolewa na Muslim]

1245.

وَعَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِذَا عَطَسَ أَحَدُكُمْ فَلْيَقُلْ: الْحَمْدُ لِلَّهِ، وَلْيَقُلْ لَهُ أَخُوهُ يَرْحَمُكَ اللَّهُ، فَإِذَا قَالَ لَهُ: يَرْحَمُكَ اللَّهُ، فَلْيَقُلْ: يَهْدِيكُمُ اللَّهُ، وَيُصْلِحْ بَالَكُمْ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Akipiga chafya mmoja wenu aseme:

الْحَمْدُ لِلَّهِ

Alhamdulillah[13]

na nduguye au mwenzie amuambie

يَرْحَمُكَ اللَّهُ

(Allaah Akurehemu).

Atakapomuambia

يَرْحَمُكَ اللَّهُ

naye amuambie:

يَهْدِيكُمُ اللَّهُ، وَيُصْلِحْ بَالَكُمْ

(Allaah Awaongeze na Awatengenezee mambo yenu).” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1246.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا يَشْرَبَنَّ أَحَدٌ مِنْكُمْ قَائِمًا} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asinywe mmoja wenu kwa kusimama.”[14] [Imetolewa na Muslim]

1247.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِذَا انْتَعَلَ أَحَدُكُمْ فَلْيَبْدَأْ بِالْيَمِينِ، وَإِذَا نَزَعَ فَلْيَبْدَأْ بِالشَّمَالِ، وَلْتَكُنَّ الْيُمْنَى أَوْلَهُمَا تَنْعَلُ، وَآخِرُهُمَا تُنْزَعُ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anapovaa mmoja wenu viatu aanze kulia, na anapovua aanze kushoto. Upande wa kulia uwe wa kwanza kuvaliwa na wa mwisho kuvuliwa.”[15]

1248.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا يَمْشِ أَحَدُكُمْ فِي نَعْلٍ وَاحِدَةٍ، وَلْيُنْعِلْهُمَا جَمِيعًا، أَوْ لِيَخْلَعْهُمَا جَمِيعًا} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Asitembee mmoja wenu kwa kiatu kimoja, avae vyote au avue vyote.”[16] [Bukhaariy, Muslim]

1249.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا يَنْظُرُ اللَّهُ إِلَى مَنْ جَرَّ ثَوْبَهُ خِيَلَاءَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah Hamtazami anayeburuta nguo yake kwa kibri.”[17] [Bukhaariy, Muslim]

1250.

وَعَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { إِذَا أَكَلَ أَحَدُكُمْ فَلْيَأْكُلْ بِيَمِينِهِ، وَإِذَا شَرِبَ فَلْيَشْرَبْ بِيَمِينِهِ، فَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَأْكُلُ بِشِمَالِهِ، وَيَشْرَبُ بِشِمَالِهِ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anapokula mmoja wenu ale kwa mkono wa kulia. Na anapokunywa anywe kwa kulia kwake. Kwa hakika shaytwaan hula anapotumia kushoto na

hunywa anapokunywa kwa kushoto kwake.”[18] [Imetolewa na Muslim]

1251.

وَعَنْ عَمْرِو بْنِ شُعَيْبٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {كُلْ، وَاشْرَبْ، وَالْبَسْ، وَتَصَدَّقْ فِي غَيْرِ سَرَافٍ، وَلَا مَخِيلَةٍ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَأَحْمَدُ، وَعَلَّقَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake, naye kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) amesema: “Kula, kunywa, vaa na utoe swadaqah bila ya israfu wala kibri.”[19] [Imetolewa na Abuu Daawuud na Ahmad. Bukhaariy ameitaja kuwa ni Mu’allaq]

[1] Tunajifunza katika Hadiyith hii kuwa kusimamia majukumu haya ni wajibu. Baadhi ya Wanazuoni wanaona kuwa ni Mandub ambayo haitakiwi kuachwa hata mara moja.

[2] Hili ni hamasisho kwa watu kulinganisha hali zao kiuchumi na wale walio chini yao, kwani kufanya hivyo kunajenga iymaan na kuwa na taqwa zaidi katika moyo wa mtu. Mara nyingi kuwaangalia watu walio juu na hadhi kunapelekea katika tamaa, ambayo inapelekea katika hisia ya kutoridhika na husuda na wivu juu yao.

[3] Anawwaas bin Sam’aan bin Khaalid Al-Kilabi Al-‘Amiri alikuwa ni Swahaba katika watu wa Shaam. Inasemekana kuwa baba yake alimtembelea Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ambaye alimuomba. Alimpa pea za ndara ambazo Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alizipokea.

[4] Tabia njema inahusisha utii kwa Allaah, kutoa swadaqah, kuwatendea watu vizuri, kuwavumilia wanaokukosea, kuhusubiana nao kwa wema, kuimarisha ujamaa na udugu na watu n.k.

[5] Kuna madhambi ya aina mbili: (a) Ni yale makatazo ya kishariy'ah yaliyokuwa wazi. Ni wajibu kwa watu wote kuachana nayo. (b) Ni yale ambayo makatazo yake hayako wazi ila ni mambo ambayo hayapendwi kufanywa, na watu wanayachukia na kuhusu uzito juu yake. Hivyo basi, ni bora kuyaacha.

[6] Hadiyth hii inathibitisha Uislaam kuheshimu hisia za watu. Watu hawatakiwi kufanya vitu vitakavyowaletea watu wengine hisia mbaya.

[7] Hii inathibitisha kuwa ni haki ya mtu aliyekaa katika kikao cha awali kuendelea kukaa pale mwanzo. Haruhusiwi mtu mwingine kukaa sehemu aliyokwisha kaa mwenzake hata kama atakuwa ametoka kidogo basi ni haki yake pale atakaporudi. Au hawezi kumuondoa sehemu aliyekwisha kaa isipokuwa kwa kuomba kusogezana nae apate nafasi.

[8] Sababu ya tukio hili limeelezwa na maneno ya Rasuli wa Allaah (ﷺ): **“Hujui ni sehemu gani katika chakula chako chenye baraka.”**

[9] Hadiyth nyingine inaelezea kuwa waliopanda wawasalimie wanaotembea na anayepita amsalimie aliyesimama. Ikiwa kuna watu wawili wanatembea, mmoja inapasa amsalimie mwenzake. Hata hivyo, mbora ni yule anayeanza kutoa salaam. Wanazuoni wamekubaliana kuwa suala hili sio suala la mtu kutaka au kutotaka bali ni suala la lazima.

[10] Kuanza kutoa salaam ni suala la lazima kwa wote na kujibu ni suala la lazima kwa wote. Hata hivyo inatosheleza kama mmoja atasalimia na wengine kujibu.

[11] Wanazuoni wengi wa mwanzo wana rai kuwa Muislaam asitangulie kumsalimia kafiri. Akitoa salaam basi salaam yake ijibiwe. Wanazuoni

wengine ni wenye rai kuwa ni ruhusa Waislaam kuanza kuwasalimia makafiri kama si jambo linaloweza kuzuilika.

[12] Kuwabana kwenye njia ya dhiki ni kutowapa heshima yao. Kama sehemu ina zahama basi amruhusu kwanza Muislaam apite kisha afuatie kafiri.

[13] Mtu anatakiwa aendelee kujibu hadi chafya ya tatu (zenye kufuatana). Chafya ikiongezeka zaidi ya hapo hatakiwi kujibu.

[14] Kunywa maji kwa kusimama hakuingii katika makatazo makubwa, bali ni makatazo ya kushauri, ila ikiwa mtu ana sababu za kishariy'ah.

[15] Kimsingi kila jambo zuri linatakiwa lianze kwa upande wa kuume, wakati mambo mengine ni kwa upande wa kushoto. Kwa mfano, kuvaa viatu, kuchana nywele na kuchukua 'udwuu yote yanatakiwa yaanze kwa upande wa kuume, kuvua viatu, kujisafisha katika sehemu za siri yaanze upande wa kushoto.

[16] Hili vile vile ni katazo la kushauri, silo tatizo kubwa, na huu ndio muono wa Wanazuoni wengi.

[17] Mtu ambaye nguo yake inaburuza chini ya kifundo kwa kusahau au kwa kuwa tumbo lake ni kubwa kiasi cha kuwa hawezi kuzuia nguo yake kuanguka, ni watu wasio husika na hukumu hii. Pamoja na kuwa adhabu inahusisha suala la kibri lakini kuna makatazo ya jumla (bila hata kuhusisha kibri cha mtu) ya kutoruhusu nguo kuwa chini ya vifundo viwili, kulingana na Hadiyth zingine Swahiyh. Hukumu hii inawahusu wanaume peke yao, kwani wanawake wanaelekezwa washushe nguo zao kiasi cha kufunika miguu yao.

[18] Hadiyth hii inasisitiza matumizi ya mkono wa kulia kwa kulia na kunywea, ama makatazo ni kwa ajili ya mkono wa kushoto kufanyia mambo hayo.

[19] Katika Hadiyth hii tunapata maelezo ya ndani zaidi kuhusu aayah ya Qur-aan inayosema:

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا

(...na kuleni na kunyweni...) [Al-A'raaf: 31].

Hadiyth hii inasisitiza maadamu ni haraam kufanya matumizi ya kupindukia kwa vitu vilivyokuwa ni halaal kwa mtu, iweje iruhusiwe kwa vitu ambavyo vimekatazwa kabisa. Matumizi haya ya kupindukia katika lugha ya Kiarabu yanaitwa Israaf.

02-Mlango Wa Wema Na Kuunga Kizazi

بَابُ الْبِرِّ وَالصَّلَةِ

02-Mlango Wa Wema Na Kuunga Kizazi

1252.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ أَحَبَّ أَنْ يُبْسَطَ عَلَيْهِ فِي رِزْقِهِ، وَأَنْ يُنْسَأَ لَهُ فِي أَثَرِهِ، فَلْيَصِلْ رَحِمَهُ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayependa kukunjuliwa rizki yake na kurefushwa umri wake na aunge kizazi chake.”[1] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1253.

وَعَنْ جُبَيْرِ بْنِ مُطْعِمٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ قَاطِعٌ } يَعْنِي: قَاطِعٌ رَحِمٍ. مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Jubayr bin Mutw'im (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hataingia Jannah mkataji (yaani mkata udugu).”[2] [Bukhaariy, Muslim]

1254.

وَعَنْ الْمُغِيرَةِ بْنِ سَعِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: { إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَ عَلَيْكُمْ عُقُوقَ الْأُمَّهَاتِ، وَوَادَ الْبَنَاتِ، وَمَنْعًا وَهَاتِ، وَكَرِهَ لَكُمْ قِيلَ وَقَالَ، وَكَثْرَةَ السُّؤَالِ وَإِضَاعَةَ الْمَالِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Al-Mughiyrah bin Sa'iyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Allaah Amewaharamishia kuwaasi mama (zenu), na kuzuia na kukusanya (mali), kuzika mabinti (wakiwa hai). Na Amechukia kwenu: maneno ya uzushi, kuuliza kwingi na kuharibu mali.” [Bukhaariy, Muslim]

1255.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {رَضَا اللَّهُ فِي رَضَا الْوَالِدَيْنِ، وَسَخَطُ
اللَّهُ فِي سَخَطِ الْوَالِدَيْنِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ
حِبَّانَ وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema
kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Radhi ya
Allaah iko katika radhi ya wazazi wawili, na hasira za Allaah ziko
katika hasira za wazazi wawili.”[3] [Imetolewa na At-Tirmidhiy, na
akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

1256.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
قَالَ: {وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يُؤْمِنُ عَبْدٌ حَتَّى يُحِبَّ لِجَارِهِ أَوْ
لِأَخِيهِ مَا يُحِبُّ لِنَفْسِهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Naapa kwa Ambaye nafsi yangu
imo Mkononi Mwake, haamini mja yeyote mpaka ampendelee jirani
yake au nduguye (Muislamu) analopendelea nafsi yake.”[4]
[Bukhaariy, Muslim]

1257.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَيُّ الذَّنْبِ أَعْظَمُ؟ قَالَ: {أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ نِدَاءً، وَهُوَ خَلْقَكَ. قُلْتُ ثُمَّ أَيُّ؟ قَالَ: ثُمَّ أَنْ تَقْتُلَ وَلَدَكَ خَشْيَةً أَنْ يَأْكُلَ مَعَكَ. قُلْتُ: ثُمَّ أَيُّ؟ قَالَ: ثُمَّ أَنْ تُزَانِيَ حَلِيلَةَ جَارِكَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nilimuuliza Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Ni dhambi gani kubwa zaidi? Akasema: ni kumfanyia Allaah mshirika hali Yeye Amekuumba. Nikasema: kisha ni dhambi gani? Akasema: ni kumuua mwanao kwa kuogopa asije kula pamoja nawe. Nikasema: kisha ni dhambi gani? Akasema: ni kuzini na mke wa jirani yako.”[5]
[Bukhaariy, Muslim]

1258.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَمْرٍو بْنِ الْعَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مِنْ الْكَبَائِرِ شَتْمُ الرَّجُلِ وَالِدَيْهِ. قِيلَ: وَهَلْ يَسُبُّ الرَّجُلُ وَالِدَيْهِ؟ قَالَ: نَعَمْ. يَسُبُّ أَبَا الرَّجُلِ، فَيَسُبُّ أَبَاهُ، وَيَسُبُّ أُمَّهُ، فَيَسُبُّ أُمَّهُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Amr bin Al-‘Aasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Miongoni mwa madhambi makubwa ni mtu kutukana wazazi wake. Maswahaba wakasema: mtu anaweza kutukana wazazi wake? Akasema: “Ndiyo, atamtukana baba wa mtu

naye anamtukana baba yake, na atamtukana mama wa mtu naye atamtukana mama yake.”[6] [Bukhaariy, Muslim]

1259.

وَعَنْ أَبِي أَيُّوبَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {لَا يَحِلُّ لِمُسْلِمٍ أَنْ يَهْجُرَ أَخَاهُ فَوْقَ ثَلَاثِ لَيَالٍ يَلْتَقِيَانِ، فَيُعْرِضُ هَذَا، وَيُعْرِضُ هَذَا، وَخَيْرُهُمَا الَّذِي يَبْدَأُ بِالسَّلَامِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Ayyuwb (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si halaal kwa Muislaam kumhama nduguye zaidi ya siku tatu;[7] anakutana naye, huyu akampa mgongo na huyo akampa mgongo, na mbora kati yao ni yule anayeanza kutoa salaam.” [Bukhaariy, Muslim]

1260.

عَنْ جَابِرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {كُلُّ مَعْرُوفٍ صَدَقَةٌ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kila jema ni swadaqah.” [8] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1261.

وَعَنْ أَبِي ذَرٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَحْقِرَنَّ مِنَ الْمَعْرُوفِ شَيْئًا، وَلَوْ أَنْ تَلْقَى أَخَاكَ بِوَجْهِ طَلْقٍ }

Kutoka kwa Abuu Dharri (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Usidharau chochote katika wema[9] hata kama ni kukutana na nduguyo kwa uso mkunjufu.” [Imetolewa na Muslim]

1262.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا طَبَخْتَ مَرَقَةً، فَأَكْثِرْ مَاءَهَا، وَتَعَاهَدْ جِيرَانَكَ } أَخْرَجَهُمَا مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Dharri (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Unapopika mchuzi zidisha maji yake na umpe jirani yako.”[10] [Imetolewa na Muslim]

1263.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَنْ نَفَسَ عَنْ مُؤْمِنٍ كُرْبَةً مِنْ كُرْبِ الدُّنْيَا، نَفَسَ اللَّهُ عَنْهُ كُرْبَةً مِنْ كُرْبِ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ، وَمَنْ يَسَّرَ عَلَى

مُعْسِرٌ، يَسِّرَ اللَّهُ عَلَيْهِ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَمَنْ سَتَرَ مُسْلِمًا،
 سَتَرَهُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَاللَّهُ فِي عَوْنِ الْعَبْدِ مَا كَانَ
 الْعَبْدُ فِي عَوْنِ أَخِيهِ { أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa
 Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye
 kumfariji katika dhiki Muumini miongoni mwa dhiki za duniani,[11]
 Allaah Atamfariji katika dhiki miongoni mwa dhiki za Siku ya
 Qiyaamah. Mwenye kumrahisishia mwenye uzito, Allaah
 Atamrahisishia duniani na Aakhirah. Mwenye kumsitiri Muislaam,
 Allaah Atamsitiri duniani na Aakhirah. Allaah Yumo katika
 kumsaidia mja madamu mja huyo yumo katika kumsaidia nduguye.”
 [Imetolewa na Muslim]

1264.

وَعَنْ أَبِي مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
 اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { مَنْ دَلَّ عَلَى خَيْرٍ، فَلَهُ مِثْلُ أَجْرِ فَاعِلِهِ }
 أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli
 wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye
 kujulisha kheri atapata mfano wa ujira (malipo) wa mwenye
 kuifanya.” [Imetolewa na Muslim]

1265.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ اسْتَعَاذَكُمْ بِاللَّهِ فَأَعِيدُوهُ، وَمَنْ سَأَلَكُمْ بِاللَّهِ فَأَعْطُوهُ، وَمَنْ أَتَى إِلَيْكُمْ مَعْرُوفًا فَكَافِئُوهُ، فَإِنْ لَمْ تَجِدُوا، فَادْعُوا لَهُ} أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ.

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kujilinda kwenu kwa Allaah, basi mlindeni na mwenye kuwaomba kwa Jina la Allaah mpeni, na mwenye kuwatendea wema mlipeni, msipopata cha kumlipa muombeeni du’aa.” [Imetolewa na Al-Bayhaqiy]

[1] Swali linalojitokeza hapa ni kuwa maadamu ya kuwa umri ulishapangwa, iweje wema kwa ndugu na jamaa kutaongeza umri wa mtu? Jibu la swali hili ni kuwa umri wa mtu upo katika elimu ya Allaah, hubaki wala haubadiliki, lakini ule ambao upo katika elimu ya Malaika muhusika wa maisha ya watu unaweza kupungua na kuongezeka vivyo hivyo. Kwa maneno mengine ni kuwa, Malaika wanapewa elimu ya Qadar iliyowekwa na siyo ile ya mwisho na yenyewe kabisa. Kwa mfano, anaambiwa ikiwa mtu fulani anawafanyia wema jamaa zake, atapewa umri wa miaka mia moja, vinginevyo utapunguzwa hadi miaka sitini.

[2] Hiki ni kitisho kikali kwa mwenye kukata udugu. Neno la Kiarabu linalotumika ni Rahm, neno hili linakusanya mahusiano yote na watu ambao ni Mahram na wale wote wenye haki ya kurithi.

[3] Kutomtii mzazi ni katika madhambi makubwa, madamu tu hakukulazimisha kufanya jambo linalopingana na Shariy’ah.

[4] Hadiyth hii inaelezea majukumu makubwa aliyonayo mtu kwa jirani zake.

[5] Hadiyth hii inatupa mafundisho kuwa madhambi makubwa yanatofautiana, kulingana na adhabu zake. Madhambi ya kuzini yanakatazwa kwa ujumla, lakini kulifanya jambo hilo kwa mke wa jirani ni jambo baya zaidi.

[6] Hukmu inayopatikana katika Hadiyth hii ni kuwa jambo lolote ambalo linapelekea katika makatazo linakatazwa vile vile. Hata kama aliyefanya jambo lile hakukusudia kufanya jambo lililokatazwa.

[7] Ikiwa sababu ya jambo hilo ni mambo binafsi, haitakiwi mfarakano huo udumu zaidi ya masiku tatu. Lakini ikiwa jambo hilo linahusiana na jambo la Dini, hakuna makadirio ya muda kwani jambo hilo ni sehemu ya iymaan.

[8] Swadaqah haina maana finyu ya mtu kutoa chochote tu katika mali yake. Bali maana yake ni pana, yaani mtu kufanya tendo lolote zuri na kuacha jambo lolote baya nayo ni Swadaqah.

[9] Bashasha inaweza kuonekana ni jambo dogo machoni mwa watu, jambo hili limepewa nafasi kubwa katika malipo na fadhila zake.

[10] Hukumu hii inakuwa ni ya faradhi ikiwa jirani yako ni mtu maskini. Ikiwa jirani ni tajiri basi hukumu hii inakuwa ni kwa kufadhilisha na kupendzesha zaidi. **نَبِيٌّ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)** amesema: “Kila Jibriyl anaposhuka kwangu huniusia kuhusu kumfanyia wema jirani kiasi cha kufikiri kuwa huenda jirani akanirithi.”

[11] Mahimizo tunayoyapata hapa ni ule ubora na umuhimu wa kumsaidia Muumini.

03-Mlango Wa Kuipa Mgongo Dunia

بَابُ الزُّهْدِ وَالْوَرَعِ

03-Mlango Wa Kuipa Mgongo Dunia[1]

عَنْ النُّعْمَانِ بْنِ بَشِيرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ وَأَهْوَى النُّعْمَانُ بِإِصْبَعَيْهِ إِلَى أُذُنَيْهِ: {إِنَّ الْحَلَالَ بَيْنَ، وَإِنَّ الْحَرَامَ بَيْنَ، وَبَيْنَهُمَا مُشْتَبِهَاتٌ، لَا يَعْلَمُهُنَّ كَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ، فَمَنْ اتَّقَى الشُّبُهَاتِ، فَقَدْ اسْتَبْرَأَ لِدِينِهِ وَعِرْضِهِ، وَمَنْ وَقَعَ فِي الشُّبُهَاتِ وَقَعَ فِي الْحَرَامِ، كَالرَّاعِي يَرْعَى حَوْلَ الْحِمَى، يُوشِكُ أَنْ يَقَعَ فِيهِ، أَلَا وَإِنَّ لِكُلِّ مَلِكٍ حِمًى، أَلَا وَإِنَّ حِمَى اللَّهِ مَحَارِمُهُ، أَلَا وَإِنَّ فِي الْجَسَدِ مُضْغَةً، إِذَا صَلَحَتْ، صَلَحَ الْجَسَدُ كُلُّهُ، وَإِذَا فَسَدَتْ فَسَدَ الْجَسَدُ كُلُّهُ، أَلَا وَهِيَ الْقَلْبُ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) Kutoka kwa An-Nu'maan bin Bashiyr (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) amesema kuwa alimsikia Rasuli wa Allaah (وَسَلَّمَ) akisema: (Nu'maan akaashiria vidole vyake kwenye masikio yake): “Hakika halaal iko wazi na haraam iko wazi, baina ya mawili hayo kuna mambo yenye utata.[2] Wengi katika watu hawayajui. Basi atakayejeiepusha na yenye utata amejeiepusha kwa Dini yake na heshima yake. Na ataketumbukia katika yenye utata atatumbukia kwenye haraam. Kama mchungu anayechunga pembeni ya mipaka, ni haraka kulisha humo. Fahamuni! Kila mfalme ana mipaka. Fahamuni! Hakika mipaka ya Allaah ni maharamisho. Zindukeni! Hakika katika mwili kuna kinofu, kinapotengamaa mwili wote unatengamaa. Kinapoaribika mwili wote unaharibika. Fahamuni! Hicho ni moyo.” [Bukhaariy, Muslim]

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {تَعَسَ عَبْدُ الدِّينَارِ، وَالذَّرْهَمِ، وَالْقَطِيفَةِ، إِنْ أُعْطِيَ رَضِيَ، وَإِنْ لَمْ يُعْطَ لَمْ يَرْضَ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ameangamia mtumwa wa dinari na dirhamu, mahameli na khamisa; akipewa huridhika, asipopewa haridhiki.”[3] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1268.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: أَخَذَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِمَنْكَبِي، فَقَالَ: {كُنْ فِي الدُّنْيَا كَأَنَّكَ غَرِيبٌ، أَوْ عَابِرُ سَبِيلٍ} وَكَانَ ابْنُ عُمَرَ يَقُولُ: إِذَا أَمْسَيْتَ فَلَا تَنْتَظِرِ الصَّبَاحَ، وَإِذَا أَصْبَحْتَ فَلَا تَنْتَظِرِ الْمَسَاءَ، وَخُذْ مِنْ صِحَّتِكَ لِسَقَمِكَ، وَمِنْ حَيَاتِكَ لِمَوْتِكَ. أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alishika mabega yangu akaniambia: “Kuwa katika dunia kana kwamba ni mgeni au mpita njia. Ibn ‘Umar alikuwa akisema: ‘Unapochwewa usingoje asubuhi, na unapopambazukiwa usingoje jioni, chukua siha yako kwa ajili ya ugonjwa wako, na uhai wako kwa kifo chako.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1269.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ تَشَبَّهَ بِقَوْمٍ، فَهُوَ مِنْهُمْ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kujifananisha na watu basi yeye ni miongoni mwao.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1270.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ: كُنْتُ خَلْفَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمًا، فَقَالَ: {يَا غُلَامُ! احْفَظِ اللَّهَ يَحْفَظْكَ، احْفَظِ اللَّهَ تَجِدْهُ تُجَاهَكَ، وَإِذَا سَأَلْتَ فَاسْأَلِ اللَّهَ، وَإِذَا اسْتَعَنْتَ فَاسْتَعِنْ بِاللَّهِ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَقَالَ: حَسَنٌ صَحِيحٌ.

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema siku moja nilikuwa nyuma ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akasema: “Ewe kijana! Mhifadhi Allaah [4]Atakuhifadhi. Mhifadhi Allaah utamkuta mbele yako. Unapoomba muombe Allaah. Unapotaka msaada mtake msaada Allaah.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na amesema Hadiyth hii ni Swahiyy Hasan]

1271.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدٍ قَالَ: {جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ! ذُلَّنِي عَلَى عَمَلٍ إِذَا عَمَلْتُهُ أَحَبَّنِي اللَّهُ، وَأَحَبَّنِي النَّاسُ. فَقَالَ: ازْهَدْ فِي الدُّنْيَا يُحِبُّكَ اللَّهُ، وَازْهَدْ فِيمَا عِنْدَ النَّاسِ يُحِبُّكَ النَّاسُ} رَوَاهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَسَنَدُهُ حَسَنٌ

Kutoka kwa Sahl bin Sa'd amesema alikuja mtu kwa Nabiyy (صَلَّى) akasema: “Ee Rasuli wa Allaah! Nijulishe amali ambayo nikiifanya Allaah Atanipenda na watu pia watanipenda. Akasema: “Chukia dunia Allaah Atakupenda[5] na chukia vilivyo kwa watu, watu watakupenda.” [Imetolewa na Ibn Maajah na isnaad yake ni hasan]

1272.

وَعَنْ سَعْدِ بْنِ أَبِي وَقَّاصٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْعَبْدَ التَّقِيَّ، الْغَنِيَّ، الْخَفِيَّ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Sa'd bin Abiy Waqqaasw (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Hakika Allaah Anampenda mja mwenye Taqwa mwenye kujitosha na mwenye kujificha.”[6] [Imetolewa na Muslim]

1273.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مِنْ حُسْنِ إِسْلَامِ الْمَرْءِ، تَرْكُهُ مَا لَا يَغْنِيهِ} رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَقَالَ حَسَنٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Katika uzuri wa Uislaam wa mtu ni kuacha lisilomhusu.”[7] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akasema ni Hadiyith hii ni Hasan]

1274.

وَعَنْ الْمِقْدَامِ بْنِ مَعْدِيكَرِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا مَلَأَ ابْنُ آدَمَ وَعَاءً شَرًّا مِنْ بَطْنٍ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ

Kutoka kwa Al-Miqdaam bin Ma'd Yakrib (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwana Adam hakujaza chombo chenye shari zaidi kuliko tumbo lake.”[8] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akasema kuwa Hadiyith hii ni Hasan]

1275.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {كُلُّ بَنِي آدَمَ خَطَّاءٌ، وَخَيْرُ الْخَطَّائِينَ التَّوَّابُونَ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَابْنُ مَاجَهَ، وَسَنَدُهُ قَوِيٌّ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kila mwana Adam ni mkosaji na bora wa wacosaji ni wanayetubia.”[9] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na Ibn Maajah, na Isnaad yake ina nguvu]

1276.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الصَّمْتُ حِكْمَةٌ، وَقَلِيلٌ فَاعِلُهُ} أَخْرَجَهُ الْبَيْهَقِيُّ فِي "الشُّعَبِ" بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ وَصَحَّحَ أَنَّهُ مَوْقُوفٌ مِنْ قَوْلِ لُقْمَانَ الْحَكِيمِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kunyamaza ni hekima, [10] na ni wachache wafanyaji wake.” [Imetolewa na Al-Bayhaqi katika Kitabu ‘Ash-Shu’ab’ kwa Isnaad dhaifu. Na imeswihi kuwa ni Mawquwf ni kauli ya Luqmaan mwenye hekima]

[1] Neno la Kiarabu linalotumika hapa ni الْوَرَع yenye maana ya kujitenga na mambo yenye shaka mtu asije angukia kwenye haraam.

[2] Hadiyth hii inatufungamanisha na hukmu muhimu za Kiislaam. Mushtabihaat ni yale mambo ambayo yana utata, yapo baina ya halaal na haraam. Wanazuoni wametofautiana kuhusu makatazo yake. Kuharibika kwa kiungo kimoja mwilini kunatokana na kuharibika kwa moyo wa mtu. Kwa sababu moyo wa mtu ndiyo unaongoza matendo ya mtu. Ikiwa mfalme amepotoka kimaadili basi uwezekano wa raia zake kupotoka vile vile ni mkubwa. Vivyo hivyo, ikiwa mfalme ni mwenye Taqwa raia zake watakuwa mfano wake.

[3] Hili linarejea kwa mtu mwenye tamaa. Akiendelea kufurahia neema za ulimwengu huu, atakuwa na furaha naye atamridhisha Allaah. Ikiwa ni kinyume chake hatopata vitu hivi basi hatofurahi kwa alichopewa na Allaah, na hatojiridhia vile vile.

[4] Kumhifadhi Allaah ni kufahamu mafundisho ya Allaah na kukatazika na makatazo yake. Kuwa ni mtu uliyehifadhiwa na Allaah ni kuwa Allaah Atakulipa malipo mazuri siku ya Qiyaamah na utapata jaza na kusahau tabu za duniani. Hadiyth hii inaingiza hisia za Tawhiyd katika mioyo ya waja na ya kuwa hakuna kinachoweza kukudhuru kama Allaah Hakutaka.

[5] Njia sahihi na pekee ya mtu kujikurubisha na Allaah ni kujitenga na dunia hii, na kuweka iymaan ya juu kwa Allaah na kuachana na tamaa ya yaliyokuwa kwa watu.

[6] Allaah Anapompenda mja wake Humtakia mema, Humuongoza katika haki. Mwenye Taqwa ni yule ambaye anatekeleza maamrisho ya Allaah na kukatazika na makatazo yake. Tajiri ni yule aiye kuwa tajiri katika moyo wake na anamshkuru Allaah kwa kila alichopewa. Khafiyy ni yule mtu asiye mnafiki na wala hajioneshi, hujishughulisha tu na 'ibaadah ya Allaah.

[7] Ikiwa mtu ana hakika kuwa Allaah Anamuona kwa kile anachofanya na kusema na ni mwenye elimu ya hilo, mtu huyo atakuwa ni mwepesi kujizuia na kuzungumza vibaya au na mazungumzo yasiyo na faida yoyote.

[8] Hadiyth hii inaelezea kuwa kuelekea katika kuzidisha jambo hakufai. Suala la chakula ni muhimu lakini himizo tunalopata hapa ni jinsi gani lilivyobeba shari ya mwana Adam.

[9] Hadiyth hii imethibitisha kuwa wana Aadam wote ni wakoaji isipokuwa Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Allaah Hachukii sana kwa yule anayefanya dhambi, bali Anamfurahia zaidi yule anayeomba maghfirah na tawbah. Imepokewa na Abuu Hurayrah katika Swahiyh Muslim ikiwa wana Aadam wote watamuasi Allaah kisha wasiombe maghfirah kwake baada ya madhambi yale, Allaah Ataungamiza ulimwengu huu na kuabadilisha na watu wengine watakaotubu na kumuomba Allaah maghfirah baada ya kuyafanya madhambi.

[10] Hadiyth nyingi zimepokelewa zikionesha umuhimu wa mtu kunyamaza kama hana zuri la kusema. Hadiyth mojawapo inaelezea kuwa ikiwa hakuna cha kuzungumza bora kukaa kimya.

04-Mlango Wa Onyo Dhidi Ya Akhlaaq (Tabia) Mbaya

بَابُ الرَّهَبِ مِنْ مَسَاوِي الْأَخْلَاقِ

04-Mlango Wa Onyo Dhidi Ya Akhlaaq (Tabia) Mbaya

1277.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِيَّاكُمْ وَالْحَسَدَ، فَإِنَّ الْحَسَدَ يَأْكُلُ الْحَسَنَاتِ، كَمَا تَأْكُلُ النَّارُ الْحَطَبَ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ
وَلَاِبْنِ مَاجَهَ: مِنْ حَدِيثِ أَنَسٍ نَحْوُهُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tahadharini na hasadi,[1] hakika hasadi hula mema kama vile moto unavyokula kuni.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd. Ibn Maajah aliripoti mfano wa Hadiyth hii kutoka katika Hadiyth za Anas]

1278.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَيْسَ الشَّدِيدُ بِالصُّرْعَةِ، إِنَّمَا الشَّدِيدُ الَّذِي يَمْلِكُ نَفْسَهُ عِنْدَ الْغَضَبِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Si mwenye nguvu mwenye kushinda mieleka, bali mwenye nguvu ni anaemiliki nafsi yake wakati wa ghadhabu.”[2] [Bukhaariy, Muslim]

1279.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الظُّلُمُ ظُلُمَاتٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Dhulma[3] ni giza Siku ya Qiyaama.” [Bukhaariy, Muslim]

1280.

وَعَنْ جَابِرِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ : {اتَّقُوا الظُّلْمَ، فَإِنَّ الظُّلْمَ ظُلُمَاتٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَاتَّقُوا الشَّحَّ، فَإِنَّهُ أَهْلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ.

Kutoka kwa Jaabir (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ogopeni dhulma, hakika kudhulumu ni giza Siku ya Qiyaamah, na ogopeni ubakhili, hakika ubakhili uliangamiza waliokuwa kabla yenu.” [Imetolewa na Muslim]

1281.

وَعَنْ مَحْمُودِ بْنِ لَبِيدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ أَخُوفَ مَا أَخَافُ عَلَيْكُمُ الشِّرْكَ الْأَصْغَرُ: الرِّيَاءُ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ بِسَنَدٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa Mahmuwd bin Labiyd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kwa hakika jambo ninalowahofia zaidi ni shirki ndogo (nayo ni) riyaa.” [4] [Imetolewa na Ahmad kwa Isnaad hasan]

1282.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا اتَّخَذَ خَانَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Alama za mnafiki

ni tatu:[5] akizungumza anaongopa, akitoa ahadi anakhalifu na akiaminiwa anakhini.” [Bukhaariy, Muslim]

1283.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {سَبَابُ الْمُسْلِمِ فُسُوقٌ، وَقِتَالُهُ كُفْرٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kumtukana Muislaam ni ufasiki na kupigana naye ni ukafiri.”[6] [Bukhaariy, Muslim]

1284.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِيَّاكُمْ وَالظَّنَّ، فَإِنَّ الظَّنَّ أَكْذَبُ الْحَدِيثِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tahadharini kudhania,[7] hakika dhana ni mazungumzo ya uongo.” [Bukhaariy, Muslim]

1285.

وَعَنْ مَعْقِلِ بْنِ يَسَارٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {مَا مِنْ عَبْدٍ يَسْتَرْعِيهِ اللَّهُ رَعِيَّةً، يَمُوتُ يَوْمَ يَمُوتُ، وَهُوَ غَاشٌّ لِرَعِيَّتِهِ، إِلَّا حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ma'qil bin Yasaar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema nilimsikia Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akisema: “Hakuna mja yeyote Allaah Amempa kuwaongoza raia, siku ya kufa akafa ilihali ni mwenye kughushi raia zake isipokuwa Allaah Atamharamishia Jannah.”[8] [Bukhaariy, Muslim]

1286.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {اللَّهُمَّ مَنْ وَلِيَ مِنْ أَمْرِ أُمَّتِي شَيْئًا، فَشَقَّ عَلَيْهِ، فَاشْقُقْ عَلَيْهِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ee Allaah! Atakayesimamia jambo katika mambo ya ummah wangu na akawafanyia uzito, basi Nawe Mfanyie uzito.” [Imetolewa na Muslim]

1287.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِذَا قَاتَلَ أَحَدُكُمْ، فَلْيَتَجَنَّبِ الْوَجْهَ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anapopigana mmoja wenu na ajiepushe (kulenga) uso.”[9] [Bukhaariy, Muslim]

1288.

وَعَنْهُ أَنَّ رَجُلًا قَالَ: { يَا-رَسُولَ اللَّهِ! أَوْصِنِي. فَقَالَ: لَا تَغْضَبْ، فَرَدَّدَ مِرَارًا. قَالَ: لَا تَغْضَبْ } أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa mtu mmoja alimuambia Ee Rasuli wa Allaah! Niusie: “Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamuambia: “Usighadhibike.”[10] Akarudia mara nyingi (Nabiy) akasema: “Usighadhibike.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1289.

وَعَنْ خَوْلَةَ الْأَنْصَارِيَّةِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { إِنَّ رَجُلًا يَتَخَوِّضُونَ فِي مَالِ اللَّهِ بِغَيْرِ حَقٍّ، فَلَهُمُ النَّارُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ } أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Khawlah Al-Answaariy[11] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

amesema: “Hakika watu wanaotumia mali ya Allaah[12] bila haki wana moto Siku ya Qiyaamah.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1290.

وَعَنْ أَبِي ذَرٍّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
فِيمَا يَرْوِي عَنْ رَبِّهِ قَالَ: {يَا عِبَادِي! إِنِّي حَرَّمْتُ الظُّلْمَ
عَلَى نَفْسِي، وَجَعَلْتُهُ بَيْنَكُمْ مُحَرَّمًا، فَلَا تَظَالَمُوا} أَخْرَجَهُ
مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Dharri (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy
(صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) katika anayoyapokea kutoka kwa
Rabb wake, amesema: “Enyi waja Wangu, Hakika Mimi
Nimejiharamishia dhulma katika Nafsi yangu na Nimeijaalia haraam
miongoni mwenu; kwa hivyo msidhulumiane.” [Imetolewa na
Muslim]

1291.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {أَتَذَرُونَ مَا الْغَيْبَةُ؟} قَالُوا: اللَّهُ وَرَسُولُهُ
أَعْلَمُ قَالَ: ذِكْرُكَ أَخَاكَ بِمَا يَكْرَهُ. قِيلَ: أَرَأَيْتَ إِنْ كَانَ فِي
أَخِي مَا أَقُولُ؟ قَالَ: إِنْ كَانَ فِيهِ مَا تَقُولُ فَقَدْ اغْتَبْتَهُ، وَإِنْ لَمْ
يَكُنْ فَقَدْ بَهْتَهُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mnajua nini Ghiybah (kusengenywa)? Wakasema Allaah na Rasuli wake Wanajua. Akasema: ‘ni kumtaja nduguyo kwa analochukia’ ikasemwa: unaonaje iwapo kwa ndugu yangu yapo nisemayo? Akasema: “Ikiwa analo usemalo umemsengenywa[13] na ikiwa hana ulisemalo umemzulia.” [Imetolewa na Muslim]

1292.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَحَاسَدُوا وَلَا تَنَاجَشُوا، وَلَا تَبَاغَضُوا، وَلَا تَدَابَرُوا، وَلَا يَبِغْ بَعْضُكُمْ عَلَى بَعْضٍ، وَكُونُوا عِبَادَ اللَّهِ إِخْوَانًا، الْمُسْلِمُ أَخُو الْمُسْلِمِ، لَا يَظْلِمُهُ، وَلَا يَخْذُلُهُ، وَلَا يَحْقِرُهُ، التَّقْوَى هَاهُنَا، وَيُشِيرُ إِلَى صَدْرِهِ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، بِحَسَبِ امْرِئٍ مِنَ الشَّرِّ أَنْ يَحْقِرَ أَخَاهُ الْمُسْلِمَ، كُلُّ الْمُسْلِمِ عَلَى الْمُسْلِمِ حَرَامٌ، دَمُهُ، وَمَالُهُ، وَعَرِضُهُ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msihusudiane wala msipandishiane bei, wala msichukiane, wala msikatane. Wala baadhi yenu asiuze kwa mauzo ya nduguye; nyote kuweni waja wa Allaah hali ya kuwa ni ndugu. Muislaam ni ndugu wa Muislaam; hamdhulumu wala hamdharau wa hamtelekezi. Taqwa ipo hapa.” Akaashiria mara tatu kifuani mwake. “Yatosha mtu kutenda shari atakapomdharau nduguye Muislaam. Kila Muislaam juu ya Muislaam mwenzie ni haraam: damu yake, mali yake na heshima yake.”[14] [Imetolewa na Muslim]

1293.

وَعَنْ قُطْبَةَ بْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {اللَّهُمَّ جَنِّبْنِي مُنْكَرَاتِ الْأَخْلَاقِ، وَالْأَعْمَالِ، وَالْأَهْوَاءِ، وَالْأَدْوَاءِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ وَاللَّفْظُ لَهُ

Kutoka kwa Qutwbah bin Maalik[15] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: اللَّهُمَّ جَنِّبْنِي مُنْكَرَاتِ الْأَخْلَاقِ، وَالْأَعْمَالِ، وَالْأَهْوَاءِ، وَالْأَدْوَاءِ

“Ee Allaah! Niepushe na akhlaaq (tabia) mbaya, na amali mbaya, na matamanio na magonjwa.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Al-Haakim

1294.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا تُمَارِ أَخَاكَ، وَلَا تُمَارِضْهُ، وَلَا تَعِدْهُ مَوْعِدًا فَتُخْلِفْهُ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ بِسَنَدٍ فِيهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Usishindane na nduguyo, wala usimfanyie mzaha, wala usimuahidi ahadi na ukamkhalifu.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy kwa isnaad dhaifu]

1295.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {خَصَلْتَانِ لَا يَجْتَمِعَانِ فِي مُؤْمِنٍ: الْبُخْلُ، وَسُوءُ الْخُلُقِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَفِي سَنَدِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mambo mawili hayakutani kwa Muumini: ubakhili na khulqa (tabia) mbaya.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na katika isnaad yake kuna udhaifu]

1296.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ: {الْمُسْتَبَانِ مَا قَالَا، فَعَلَى الْبَادِي، مَا لَمْ يَعْتَدِ الْمَظْلُومُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wawili wenye kutukanana wana dhambi (kiasi wanavyosema), aliyeanza ni mwenye dhambi nyingi zaidi madamu aliyedhulumiwa hajavuka mpaka (katika kujibu).” [16] [Imetolewa na Muslim]

1297.

وَعَنْ أَبِي صِرْمَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ ضَارَّ مُسْلِمًا ضَارَّهُ اللَّهُ، وَمَنْ شَاقَّ مُسْلِمًا شَقَّ اللَّهُ عَلَيْهِ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ وَالتِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ

Kutoka kwa Abuu Swirmah[17] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kumdhuru Muislaam, Allaah Atamdhuru,[18] na mwenye kumsumbua Muislaam Allaah Atamsumbua.” [Imetolewa na Abuu Daawuud na At-Tirmidhiy na kwa isnaad Hasan]

1298.

وَعَنْ أَبِي الدَّرْدَاءِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ اللَّهَ يُبْغِضُ الْفَاحِشَ الْبَذِيءَ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ

وَلَهُ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ مَسْعُودٍ رَفَعَهُ: {لَيْسَ الْمُؤْمِنُ بِالطَّعَّانِ، وَلَا اللَّعَّانِ، وَلَا الْفَاحِشِ، وَلَا الْبَذِيءِ} وَحَسَنَهُ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ، وَرَجَّحَ الدَّارَقُطْنِيُّ وَقَفَّهُ

Kutoka kwa Abuu Ad-Dardaa[19] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Allaah Anamchukia muovu, mwenye maneno mabaya.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha]

Pia amepokea kutoka katika Hadiyth ya Ibn Mas-‘uud marfuw’: “Muumini si mtukanaji, wala si mlaanifu,[20] wala mchafu, wala si mwenye maneno mabaya.” [Na amesema ni Hasan na akaisahihisha Al-Haakim. Ad-Daaraqutwniy ameitilia nguvu kuwa ni Marfuw’]

1299.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا تَسُبُّوا الْأَمْوَاتَ، فَإِنَّهُمْ قَدْ أَفْضَوْا إِلَى مَا قَدَّمُوا } أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Msishutumu wafu,[21] hakika wao wameshayaendea waliyoyatanguliza.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1300.

وَعَنْ حُذَيْفَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ قَتَاتٌ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Hudhayfah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mchonganishi hataingia Jannah.”[22] [Bukhaariy, Muslim]

1301.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ كَفَّ غَضَبَهُ، كَفَّ اللَّهُ عَنْهُ عَذَابَهُ} أَخْرَجَهُ الطَّبْرَانِيُّ فِي " الْأَوْسَطِ "

وَلَهُ شَاهِدٌ: مِنْ حَدِيثِ ابْنِ عُمَرَ عِنْدَ ابْنِ أَبِي الدُّنْيَا

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kuzuwia ghadhabu zake, Allaah Atamzuilia adhabu Yake.” [Imetolewa na Atw-twabaraaniy katika kitabu cha ‘Al-Awsatw’. Nayo ina Ushahidi wa Hadiyth ya ‘Abdullaah ibn ‘Umar kwa Ibn Abuu Ad-Dunyaa]

1302.

وَعَنْ أَبِي بَكْرٍ الصِّدِّيقِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ خَبٌّ، وَلَا بَخِيلٌ، وَلَا سَيِّئُ الْمَلَكَةِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَفَرَّقَهُ حَدِيثَيْنِ، وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa Abuu Bakr Asw-Swiddiyq (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haingii Jannah mwenye hadaa wala bakhili wala mbaya wa kumiliki.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na ameigawa katika Hadiyth mbili, na katika isnaad yake kuna udhaifu]

1303.

وَعَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ تَسَمَّعَ حَدِيثَ قَوْمٍ، وَهُمْ لَهُ كَارُهُونَ، صُبَّ فِي أُذُنَيْهِ الْأَنْكُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ} يَعْنِي: الرِّصَاصَ. أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayesikiliza mazungumzo ya watu na ilihali wenyewe wanachukia siku ya Qiyaamah atamiminiwa risasi masikioni mwake.” [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1304.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {طُوبَى لِمَنْ شَغَلَهُ عَيْبُهُ عَنْ عُيُوبِ النَّاسِ} أَخْرَجَهُ الْبَزْزَارُ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Furaha ni ya ambaye aibu zake zimemshughulisha, akaachana na aibu za watu.” [Imetolewa na Al-Bazaar kwa isnaad Hasan]

1305.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ تَعَازَمَ فِي نَفْسِهِ، وَاخْتَالَ فِي مَشِيَّتِهِ، لَقِيَ اللَّهَ وَهُوَ عَلَيْهِ غَضَبَانُ} أَخْرَجَهُ الْحَاكِمُ وَرِجَالُهُ ثِقَاتٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kujikweza nafsini mwake, akaringa katika kutembea kwake, atakutana na Allaah ilihali Amemghadhibikia.”[23] [Imetolewa na Al-Haakim na wapokezi wake ni Madhubuti]

1306.

وَعَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْعَجَلَةُ مِنَ الشَّيْطَانِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَقَالَ: حَسَنٌ

Kutoka kwa Sahl bin Sa’d (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Haraka inatokana na shaytwaan.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na amesema ni Hasan]

1307.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {الشُّؤْمُ: سُوءُ الْخُلُقِ} أَخْرَجَهُ أَحْمَدُ وَفِي إِسْنَادِهِ ضَعْفٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ukorofi ni khulqa (tabia) mbaya.”[24] [Imetolewa na Ahmad na katika isnaad yake kuna udhaifu]

1308.

وَعَنْ أَبِي الدَّرْدَاءِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ اللَّعَّانِينَ لَا يَكُونُونَ شُفَعَاءَ، وَلَا شُهَدَاءَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Ad-Dardaa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Wenye kulaani hawawi waombezi wala Mashahidi Siku ya Qiyaamah.” [Imetolewa na Muslim]

1309.

وَعَنْ مُعَاذِ بْنِ جَبَلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ عَيَّرَ أَخَاهُ بِذَنْبٍ، لَمْ يَمُتْ حَتَّى يَعْمَلَهُ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَحَسَنَهُ، وَسَنَدُهُ مُنْقَطِعٌ

Kutoka kwa Mu’aadh bin Jabal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwenye kumuaibisha nduguye kwa dhambi hatakufa hadi aifanye.”[25]

[Imetolewa na At-Tirmidhiy na amesema ni Hasan na isnaad yake imekatika]

1310.

وَعَنْ بَهْزِ بْنِ حَكِيمٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ: قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {وَيْلٌ لِلَّذِي يُحَدِّثُ، فَيَكْذِبُ؛ لِيَضْحَكَ بِهِ الْقَوْمُ، وَيِلُّ لَهُ، ثُمَّ وَيِلُّ لَهُ} أَخْرَجَهُ الثَّلَاثَةُ، وَإِسْنَادُهُ قَوِيٌّ

Kutoka kwa Bahz bin Hakiym kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) amesema: “Ole wake anayezungumza akadanganya ili kuwachekesha watu.[26] Ole wake! Kisha ole wake!” [Imetolewa na Ath-Thalaathah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuud) na isnaad yake ina nguvu]

1311.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {كَفَّارَةٌ مَنْ اغْتَبَتَهُ أَنْ تَسْتَغْفِرَ لَهُ} رَوَاهُ الْحَارِثُ بْنُ أَبِي أُسَامَةَ بِسَنَدٍ ضَعِيفٍ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kafara ya uliyemsengenya ni kumuomba maghfirah.”[27] [Imetolewa na Al-Haarith bin Abuu Usaamah kwa isnaad dhaifu]

1312.

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَبْغَضُ الرِّجَالِ إِلَى اللَّهِ الْأَلَدُّ الْخَصِيمُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mtu anayechukiwa kabisa na Allaah ni katili mwingi wa ugomvi.” [Imetolewa na Muslim]

[1] Katika lugha ya kiarabu ‘Hasad’ (husuda na wivu) hurejea kwa mtu anayemuonea wivu mwenzake na kuhusudu alichokuwa nacho na kutamani neema ile imuondokee na ije kwake. Jambo hili limekatazwa. Ikiwa mtu anatamani apate kitu fulani lakini hataki vile vile kimuondokee mwenzake, jambo hili linaitwa ‘Hiqd’. Hisia hii inahitajika katika mambo ya kidini.

[2] Hili linathibitisha umuhimu wa kusamehe, na kutopendelea kulipa kisasi haswa unapoghadhibishwa na jambo. Watu wanatakiwa wajifunze namna ya kujizuia na ghadhabu au hasira kwani hasira hasara. Mambo yanayoweza kuzuia hasira ni: Kujikinga na Allaah dhidi ya shaytaan kwa kusema:

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

Na kuchukua wudhuu na kukaa chini kama utakuwa umesimama na kulala kama utakuwa umekaa.

[3] Dhulma, maana yake ni kuweka kitu sehemu isiyokuwa yake, au kuficha ukweli ili usitokeze. Katika Siku ya Hukmu (Qiyaamah) itaonekana na rangi yake itakuwa ni nyeusi. Hadiyth hii inatufundisha kuwa dhulma ni kitu kibaya na ni haraam ikiwa kwa mtu, katika heshima au utajiri wake.

[4] Riyaa ni kujionyesha. Ni pale mja anapofanya tendo lolote la ki ‘ibaadah kama la kuacha makatazo na kutekeleza maamrisho, lakini mtu anafanya hivyo ili watu wamuone kuwa ni mtiifu, hivyo anaridhisha watu badala ya kumridhisha Allaah. Au anaweza kufanya tendo la ‘ibaadah kwa malengo ya kidunia. Riyaa ina namna mbili: Ya kwanza ni kutenda jambo la ‘ibaadah, na kulionyesha kwa watu. Ya pili ni kufanya ‘ibaadah ambayo watu hawajui kisha anawajulisha watu kuwa kafanya. Aina hii ya riyaa inaitwa ‘Sum’ah’ na ile ya kwanza ndio riyaa yenyewe. Zote hazitakiwi.

[5] Unafiki ni aina mbili: a) Unafiki wa matendo na b) Unafiki katika Iymaan. Unafiki wa matendo umeshatajwa katika Hadiyth hii. Unafiki wa Iymaan pindi anapoficha ukafiri na kudhihirisha Uislaam. Unafiki wa Iymaan ni mbaya na hatari zaidi kuliko ukafiri wenyewe. Unafiki wa kimatendo ni moja ya madhambi makubwa ambao unaweza kusamehewa.

[6] ‘Fisq’ ni mtu kuangukia katika kumuasi Allaah. Kwa mfano, Allaah Amekataza Muislaam kutumia maneno machafu, na kuwa mtu anamuasi Allaah kwa kumuita nduguye majina mabaya, mtu huyo anakuwa ‘Faasiq’ (mwenye dhambi). Lakini ikiwa mtu huyo huyo au mwingine akaamua kupigana na mwenzake ambaye ni Muislaam, katika Hadiyth hii mtu huyo ni ‘Kufr’ (kufanya jambo la ukafiri). Ikiwa mambo haya mawili hayamhusu mtu mmoja basi neno hili litakuwa limetumika kama fumbo, yaani kufanya jambo la kikafiri.

[7] Dhana (kufikiria kitu kisichokuwepo). Limeelezwa kama ni mazungumzo ya uongo na Wanazuoni na ni uzushi na ni moja kati ya madhambi makubwa.

[8] Hali hii ya ‘Ghasb’, kunyanga’nya ni katika madhambi makubwa, kwani ni jambo linaloweza kumzuia kuingia Jannah. Watawala wanatakiwa wawahukumu watu kwa uadilifu. Inaonya kuwa adhabu kali zinawakabili watawala dhalimu.

[9] Hadiyth hii inaonyesha makatazo ya kupiga uso, hata kama ni adhabu ya makosa ya mtu. Hata wanyama wasipigwe usoni.

[10] Hadiyth hii ni mfano halisi wa wema ambao unataka uonyeshwe katika maisha haya ya duniani. Hili linatokana na ukweli kuwa mtu anayeepushwa na khulqa (tabia) njema ya huruma na kuwa na khulqa ya hasira kwa upande mmoja na upande wa pili khulqa ile ya hasira huwakera watu wengine. Hali hii ni mbaya kwani inamuathiri yule mtu mwenyewe na inawaathiri waliomzunguka.

[11] Khawlah, binti wa Thamir Al-Answariy akiitwa Umm Muhammad na baba yake akiitwa Qays bin Qahad. Alikuwa katika Banuu Maalik bin An-Najjaar, aliolewa na Hamza bin ‘Abdil-Mutwalib, mumewe alipouwawa katika Uhud aliolewa na An-Nu’maan bin Al-‘Ajlaan Al-Answariy Az-Zuraqi.

[12] Hadiyth hii ni dalili kuwa hata watawala wanaweza kutumia mali za ‘Baytul Maal’ vibaya, hili ni katika madhambi makubwa.

[13] Hadiyth hii imetajwa na Maswahaba wengi, na imepokelewa katika njia nyingi. Kuna makubaliano ya Wanazuoni kuwa kusengenya ni haraam.

[14] Tunajifunza katika Hadiyth hii Muislaam hatakiwi kuwa na kinyongo kwa Muislaam mwenzake.

[15] Alikuwa ni Swahaba kutoka kwa Banuu Tha’laba bin Sa’d bin Dhubyaan, alikuwa pia akiitwa Adh-Dhubyaan. Alikuwa ni mkazi wa Kufa mji uliopo ‘Iraq, baadhi ya Hadiyth zake zilipokewa na mpwawe Ziyaad bin ‘Alaqa.

[16] Hadiyth hii inabainisha mambo mawili: a) Suala la kulipa ubaya uliyofanyiwa na mwingine, ni suala linarohusiwa, b) suala la dhambi litamuhusu yule aliyeanzisha hali ile, maadamu yule wa pili hajavuka mipaka kwa kufanya uadui. Pamoja na yote hayo lililo bora zaidi ni kumsamehe aliyefanya makosa.

[17] Huyu ni Maalik bin Qays au Qays bin Maalik, alikuwa ni Swahaba kutoka katika kabila la Maazin. Alishiriki vita vya Badr na vita vingine vilivyofuatia na amepokea baadhi ya Hadiyth.

[18] Hadiyth hii inaonyesha kumdhuru Muislaam kwa jambo lolote lile hata kama litaonekana ni dogo kiasi gani hairuhusiwi.

[19] Jina halisi la Abuu Ad-Dardaa lilikuwa ni ‘Uwaymir bin Zayd au Ibn ‘Aamir au Ibn Maalik bin ‘Abdillaah bin Qays. Alikuwa ni Answaar wa kabila la Khazraj. Alikuwa ni Swahaba aliyejinyima raha na anasa za kidunia. Alisilimu katika siku ya vita vya Badr na alishiriki vita vya Uhud. ‘Umar alimhusisha katika watu waliyoshiriki Badr. Alikuwa ni katika watu walioikusanya Qur-aan na alifanywa kuwa ni Qaadhi wa Damascus. Ana fadhila nyingi. Amesikika akisema: “Umaarufu na riyaa ya saa moja inaweza kusababisha huzuni ya muda mrefu.” Alifariki 32 Hijriyyah.

[20] Hadiyth hii inatuelekeza kuwa si katika khulqa (tabia) ya Muumini kuwaita nduguze majina mabaya au kuwalaani. Hata hivyo inaruhusiwa kumtukana na kumlaani yule aliyelaaniwa na Allaah na Rasuli wake. Au kutaja kwa ujumla laana ya Allaah kwa makafiri. Watu wenye kufanya mambo mabaya na machafu. Vinginevyo si halaal kumlaani mtu kwa kumtaja jina lake.

[21] Hapa tunajifunza kuwa hairuhusiwi kabisa kuwaita waliokufa kwa majina mabaya, kuwasema vibaya. Hili linahusu kwa Waislaam hususan na hata kwa makafiri ambao wana udugu na baadhi ya Waislaam kwani kuwatusi au kuwasema vibaya kutawasikitisha ndugu zao Waislaam.

[22] Hafiydh Mundhir anaona kuwa makubaliano ya Wanazuoni wa Ummah huu ni kuwa mchochezi au mchukua maneno hapa na kuyapeleka kule ili kuleta utesi baina ya watu amefanya jambo la haraam na baya sana na linahesabiwa kuwa ni katika madhambi makubwa.

[23] Maelezo tunayopata kwenye Hadiyth hii ni makemeo kuhusu kibri na ni katika madhambi makubwa. Imepokewa na At-Tirmidhiy kuwa: [“Mwenye sehemu ndogo ya kibri katika nafsi yake hatoingia Jannah.”](#)

[24] Shari anazopata mwana Aadam ni kutokana na khulqa (tabia) zake mbaya. Hadiyth hii inaonyesha kuwa khulqa nzuri au mbaya za mtu zinatokana na chaguo lake binafsi.

[25] Tunajua kuwa kutaja maovu ya mtu ni dhambi. Ni vibaya sana kutaja udhaifu wa mtu na matatizo yake mbele za watu, ili kumuumbua au kumuaibisha. Hadiyth hii inatuhimiza kuwa mtu asitaje madhambi ya fulani eti kwa sababu naye amekashifiwa.

[26] Kusema uongo hata ikiwa ni kwa utani tu ili watu wacheke ni katika makatazo makubwa na ni sifa mojawapo ya unafiki. Uongo ambao haumnufaishi mtu hapa duniani na hata huko Aakhirah hauna maana na ni uongo mbaya sana. Kusikiliza uongo vile vile ni jambo lisilokubalika, aidha mtu azungumze ubaya wake au aondoke kwenye kikao hicho.

[27] Tawbah ya kusengenya ni: ikiwa mtu atamsengenya mtu mwingine ni bora amuombe msamaha. Kama hatompata mtu mwenyewe basi amuombee du’aa kwa Allaah Amghufurie madhambi yake.

05-Mlango Wa Mahimizo Ya Akhlaaq (Tabia) Njema

بَابُ التَّرْغِيبِ فِي مَكَارِمِ الْأَخْلَاقِ

05-Mlango wa Mahimizo Ya Akhlaaq (Tabia) Njema

1313.

عَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { عَلَيْكُمْ بِالصِّدْقِ، فَإِنَّ الصِّدْقَ يَهْدِي إِلَى الْبِرِّ، وَإِنَّ الْبِرَّ يَهْدِي إِلَى الْجَنَّةِ، وَمَا يَزَالُ الرَّجُلُ يَصْدُقُ، وَيَتَحَرَّى الصِّدْقَ، حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ صَدِيقًا، وَإِيَّاكُمْ وَالْكَذِبَ، فَإِنَّ الْكَذِبَ يَهْدِي إِلَى الْفُجُورِ، وَإِنَّ الْفُجُورَ يَهْدِي إِلَى النَّارِ، وَمَا يَزَالُ الرَّجُلُ يَكْذِبُ، وَيَتَحَرَّى الْكَذِبَ، حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ كَذَّابًا } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Shikamaneni na ukweli. Hakika ukweli unaongoza kwenye wema na wema unaongoza Jannah. Mtu hataacha kusema kweli na anachagua ukweli mpaka aandikwe mbele ya Allaah kuwa ni mkweli. Nawatahadharisheni na uongo. Hakika uongo huongoza kwenye uovu, na uovu huongoza motoni. Mtu hataacha kudanganya na anaendelea kudanganya mpaka aandikwe mbele ya Allaah kuwa ni mdanganyifu.” [Bukhaariy, Muslim]

1314.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِيَّاكُمْ وَالظَّنَّ، فَإِنَّ الظَّنَّ أَكْذَبُ الْحَدِيثِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tahadharini na dhana, hakika dhana ni mazungumzo ya uongo.” [Bukhaariy, Muslim]

1315.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِيَّاكُمْ وَالْجُلُوسَ بِالطَّرِيقَاتِ. قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ! مَا لَنَا بُدٌّ مِنْ مَجَالِسِنَا، نَتَحَدَّثُ فِيهَا. قَالَ " فَأَمَّا إِذَا أَبَيْتُمْ، فَأَعْطُوا الطَّرِيقَ حَقَّهُ. قَالُوا: وَمَا حَقُّهُ؟ قَالَ: " غَضُّ الْبَصَرِ، وَكَفُّ الْأَدَى، وَرَدُّ السَّلَامِ، وَالْأَمْرُ بِالْمَعْرُوفِ، وَالنَّهْيُ عَنِ الْمُنْكَرِ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Tahadharini kukaa njiani.[1] Wakasema: Ee Rasuli wa Allaah! Hatuna budi na vikao vyetu. Akasema: “Iwapo mtakataa isipokuwa kukaa basi ipeni njia haki yake. Wakasema: Ni ipi haki ya njia? Akasema: ni kuinamisha macho (kutotazama yalio haramishwa), kuondoa udhia, kurudisha salaam, kuamrisha mema na kukataza mabaya.” [Bukhaariy, Muslim]

1316.

وَعَنْ مُعَاوِيَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ يُرِدِ اللَّهُ بِهِ خَيْرًا، يُفَقِّهُهُ فِي الدِّينِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Mu'aawiyah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Anayemtakia Allaah kheri Humjaalia ufaqihi (‘ilmu ya kina) katika Dini.”[2] [Bukhaariy, Muslim]

1317.

وَعَنْ أَبِي الدَّرْدَاءِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا مِنْ شَيْءٍ فِي الْمِيزَانِ أَثْقَلُ مِنْ حُسْنِ الْخُلُقِ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ، وَالتِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa Abuu Ad-Dardaa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakuna jambo zito katika mizani ya Muumini Siku ya Qiyaamah kama khulqa (tabia) njema.” [Imetolewa na Abuu Daawuwd na At-Tirmidhiy na akaisahihisha]

1318.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْحَيَاءُ مِنَ الْإِيمَانِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hayaa ni katika iymaan.”[3] [Bukhaariy, Muslim]

1319.

وَعَنْ أَبِي مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ مِمَّا أَدْرَكَ النَّاسُ مِنْ كَلَامِ النَّبُوءَةِ الْأُولَى: إِذَا لَمْ تَسْتَحْ، فَاصْنَعْ مَا شِئْتَ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Abuu Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika miongoni mwa waliyopata watu kutoka katika mafundisho ya Manabiy wa mwanzo ni: usipostahi fanya utakalo.”[4] [Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1320.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْمُؤْمِنُ الْقَوِيُّ خَيْرٌ وَأَحَبُّ إِلَى اللَّهِ مِنَ الْمُؤْمِنِ الضَّعِيفِ، وَفِي كُلِّ خَيْرٍ، إِحْرَصْ عَلَى مَا يَنْفَعُكَ، وَاسْتَعِنْ بِاللَّهِ، وَلَا تَعْجَزْ، وَإِنْ أَصَابَكَ شَيْءٌ فَلَا تَقُلْ: لَوْ أَنِّي فَعَلْتُ كَانَ كَذَا وَكَذَا، وَلَكِنْ قُلْ: قَدَّرَ اللَّهُ وَمَا شَاءَ فَعَلَ; فَإِنْ لَوْ تَفْتَحُ عَمَلَ الشَّيْطَانِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendeza mno kwa Allaah[5] kuliko Muumini dhaifu, na katika wote (hao) muna kheri. Jali linalokunufaisha na muombe Allaah msaada wala usichoke. Utakapopatwa na jambo usiseme ‘Lau ningalifanya kadha wa kadha’ isipokuwa sema:

قَدَّرَ اللَّهُ وَمَا شَاءَ فَعَلَ

‘Allaah Amekadiria, na Atakalo huwa’

kwani neno ‘lau’ hufungua amali ya shaytwaan.” [Imetolewa na Muslim]

1321.

وَعَنْ عِيَّاضِ بْنِ حِمَارٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ اللَّهَ أَوْحَى إِلَيَّ أَنْ تَوَاضَعُوا، حَتَّى لَا يَبْغِيَ أَحَدٌ عَلَى أَحَدٍ، وَلَا يَفْخَرَ أَحَدٌ عَلَى أَحَدٍ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa ‘Iyaadw bin Himaar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Allaah Amenifunulia Wahy kwamba nyenyekeeni ili yeyote asimdhumu yeyote wala yeyote asijifakhiri juu ya yeyote.”[6] [Imetolewa na Muslim]

1322.

وَعَنْ أَبِي الدَّرْدَاءِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {مَنْ رَدَّ عَنْ عَرَضِ أَخِيهِ بِالْغَيْبِ، رَدَّ اللَّهُ عَنْ وَجْهِهِ النَّارَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَحَسَّنَهُ
وَلِأَحْمَدَ، مِنْ حَدِيثِ أَسْمَاءَ بِنْتِ يَزِيدَ نَحْوَهُ

Kutoka kwa Abuu Ad-Dardaa (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakayerudisha heshima ya nduguye asiyekuwepo,[7] Allaah Ataepusha uso wake dhidi ya moto siku ya Qiyaamah.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na

amesema ni Hasan. Ahmad ana Hadiyth inayofanana kutoka kwa Asmaa[8] bint Yaziyd]

1323.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا نَقَصْتُ صَدَقَةً مِنْ مَالٍ، وَمَا زَادَ اللَّهُ عَبْدًا بِعَفْوٍ إِلَّا عِزًّا، وَمَا تَوَاضَعَ أَحَدٌ لِلَّهِ إِلَّا رَفَعَهُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Swadaqah haijapunguza mali, Allaah Hamzidishii mja kwa msamaha ila utukufu, na hanyenyekei yeyote kwa ajili ya Allaah isipokuwa Allaah (عز وجل) Atamuinua.”[9] [Imetolewa na Muslim]

1324.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ سَلَامٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يَا أَيُّهَا النَّاسُ! أَفْشُوا السَّلَامَ، وَصَلُّوا الْأَرْحَامَ، وَأَطْعِمُوا الطَّعَامَ، وَصَلُّوا بِاللَّيْلِ وَالنَّاسُ نِيَامَ، تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ بِسَلَامٍ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin Salaam (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Enyi watu! Enezeni salaam, na lisheni chakula, na ungeni kizazi na mswali (usiku) hali ya watu wamelala, mtaingia Jannah kwa amani.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha]

1325.

وَعَنْ تَمِيمِ الدَّارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الدِّينُ النَّصِيحَةُ} ثَلَاثًا. قُلْنَا: لِمَنْ يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: "لِلَّهِ وَلِكِتَابِهِ وَلِرَسُولِهِ وَلِأَيِّمَةِ الْمُسْلِمِينَ وَعَامَّتِهِمْ" أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Tamiym Ad-Daariy[10] (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Dini ni nasaha.[11] Amesema mara tatu. Tukasema: ‘kwa nani Ee Rasuli wa Allaah! Akasema: “Hiyo ni kwa ajili ya Allaah, na Kitabu Chake, Rasuli Wake, viongozi wa Waislaam na watu wote.” [Imetolewa na Muslim]

1326.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {أَكْثَرُ مَا يُدْخِلُ الْجَنَّةَ تَقْوَى اللَّهِ وَحُسْنُ الْخُلُقِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mengi yanayowaingiza watu Jannah ni kuwa na taqwa Allaah[12] na khulqa (tabia) njema.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Al-Haakim]

1327.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّكُمْ لَا تَسْعُونَ النَّاسَ بِأَمْوَالِكُمْ، وَلَكِنْ لِيَسْعَهُمْ بَسْطُ الْوَجْهِ، وَحُسْنُ الْخُلُقِ} أَخْرَجَهُ أَبُو يَعْلَى، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Nyinyi hamuwezi kuwatosheleza watu kwa mali zenu, lakini iwatoshe wao kutoka kwenu uchangamfu wa uso na khulqa (tabia) njema.” [Imetolewa na Abuu Ya’laa na akaisahihisha Al-Haakim]

1328.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْمُؤْمِنُ مِرَاةُ الْمُؤْمِنِ} أَخْرَجَهُ أَبُو دَاوُدَ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muumini ni kioo[13] cha ndugu yake Muumini.” [Imetolewa na Abuu Daawud kwa isnaad Hasan]

1329.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْمُؤْمِنُ الَّذِي يُخَالِطُ النَّاسَ، وَيَصْبِرُ عَلَى أَذَاهُمْ خَيْرٌ مِنَ الَّذِي لَا يُخَالِطُ النَّاسَ وَلَا يَصْبِرُ عَلَى أَذَاهُمْ} أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَةَ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ، وَهُوَ عِنْدَ التِّرْمِذِيِّ: إِلَّا أَنَّهُ لَمْ يُسَمِّ الصَّحَابِيَّ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Muumini

anayetangamana na watu na anasubiri maudhi yao, ni bora kuliko Muumini asiyetangamana na watu wala hasubiri maudhi yao.” [Imetolewa na Ibn Maajah kwa Isnaad Hasan nayo iko kwa At-Tirmidhiy lakini hakutaja Swahaba]

1330.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {اللَّهُمَّ كَمَا أَحْسَنْتَ خُلُقِي، فَحَسِّنْ خُلُقِي} رَوَاهُ أَحْمَدُ وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uwd (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema:

اللَّهُمَّ كَمَا أَحْسَنْتَ خُلُقِي، فَحَسِّنْ خُلُقِي

“Ee Allaah! Kama Ulivyofanya umbo langu kuwa bora nitengenezee tabia yangu.” [Imetolewa na Ahmad na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

[1] Majukumu matano ya kuketi njiani yametajwa hapa. Kadhalika kuna mengine yaliyotajwa kama vile kumuelekeza mpita njia na kumjibu mwenye kupiga chafya n.k. majukumu haya yanafikia kumi na nne. katika lugha ya Kiarabu غَضُّ الْبَصَرِ ina maana kuinamisha macho chini na kutowaangalia wanawake, na mengine yaliyoharamishwa.

[2] Elimu ya halaal na haraam katika Shariy’ah inaitwa Fiqh. Maelezo haya yanaonesha utukufu na ukubwa wa somo hili muhimu. Kilichoelezwa hapa ni elimu ya Qur-aan na Sunnah ya Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), siyo mijadala ya kifalsafa yaliyopo katika masomo ya Shariy’ah leo hii, ambayo hayawezi kufahamika na akili ya mtu wa kawaida.

[3] Hadiyth hii inaonyesha kuwa kutojikweza kwa mtu na hayaa ni katika mambo yanayomsaidia na kutofanya madhambi, au kushindwa kutekeleza

haki za wengine, kwa hakika hili linamfanya afikirie jina lake katika jamii lau baadhi ya madhambi yake yatadhihirika. Katika lugha nyingine, khulqa (tabia) njema na mtu kuwa na hayaa yanamfanya kutokariri mambo mabaya. Kwa hakika hayaa ni msingi wa khulqa (tabia) njema na ni sehemu katika iymaan ya mja.

[4] Pamoja na kuwa Shariy'ah za Rasuli waliyopita zimetenguliwa, suala la staha, ambalo ni moja ya taratibu zilizopita haikufutwa. Staha ni kigingi kinachomsaidia mtu katika kujizuia na kufanya mambo yoyote ayatakayo.

[5] Nini maana ya Muumini mwenye nguvu? Hii haimaanishi nguvu za kiwili wili. Badili yake inatujulisha utashi wa mtu kwa anayoyafanya katika mambo mema na kutaraji thawabu na malipo huko Aakhirah.

[6] Katika Hadiyth hii tunaona kuwa dhulma, kibr ni khulqa (tabia) zisizopendeza kwa mtu. Katika Hadiyth mojawapo inaelezwa kuwa dhulma ni katika mabaya zaidi ambayo mtu anaadhibiwa kwayo zaidi hapa duniani na huko Aakhirah. Hata hivyo kiini cha tatizo hili ni mtu kujikweza na kujiona.

[7] Ikiwa mtu atamsengenya mtu, anayesikia ni lazima amkataze anayesengenya, na kama inawezekana mtu aeleze mazuri yake badala ya mabaya yake.

[8] Huyu ni Asmaa binti wa Yaziyd bin As-Sakan Al-Ash-haliya. Alikuwa ni msemaji wa wanawake. Alishiriki katika vita vya Yarmuk na peke yake aliuwa watu tisa siku ile akiwa na upondo.

[9] Sifa tatu zilizotajwa katika Hadiyth hii zinaitwa kuwa ni 'Misingi ya khulqa (tabia) njema'. Ambayo inafundisha usamehevu na unyenyekevu.

[10] Huyu ni Abuu Ruqaiyah, Tamiym bin Aws bin Kharija Ad-Dar. Alisilimu mwaka wa tisa Hijriyyah. Aliishi Baytul-Maqdis (Jerusalem). Ibn Siriyn anasema kuwa: "Alikusanya Qur-aan na alikuwa akiisoma kwa usiku mmoja." Alifariki mwaka wa 40 Hijriyyah.

[11] Hadiyth hii ni kiini cha msingi wa Dini hii. Ni Hadiyth inayohitaji maelezo marefu, ingawaje hapa si penyewe kwa hilo. Nasaha kwa Allaah ni mtu kuwa na iymaan kwa Allaah, asimshirikishe na chochote na afuate mafundisho yake. Nasaha katika kitabu cha Allaah ni kuamini kuwa ni maneno ya Allaah, kuchukuwa kulichokatazwa na kukatazika nalo na kulifanyia kazi lililoamrisha, kusoma kwa umakini na kufahamu maana

yake na kufanya kazi. Nasaha kwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) ni kukiri Unabii wake na kufuata Sunnah zake. Ama nasaha kwa watawala Waislaam ni kuwasaidia katika yaliyo ya haki, kufuata amri zao, kuwakumbusha na mahitaji ya raia zake, kuwashauri katika wema na kuwaheshimu na kuwahamasisha kuendelea kufanya uadilifu. Na mwisho ni nasaha kwa Waislaam wote nayo ni kuwaelezea maslahi yao katika maisha yao hapa duniani na kesho Aakhirah, kuwalinda na uharibifu wowote au madhara yoyote, kuwaamrisha mema na kuwakataza maovu.

[12] Khulqa (tabia) njema hapa inahusisha: kutengamana na watu kwa wema, kutowafanyia ubaya, na kutabasamu kila unapokutana nao. Neno la Kiarabu تَقْوَى linasimama kwa maana ya kufuata yaliyoamrishwa na kuacha yaliyokatazwa.

[13] Mtu anajifunza kuonekana kwake iwe ni uzuri au ubaya pindi anapojiangalia katika kioo. Vivyo hivyo, Muislaam ndio kioo cha Muislaam mwenzake na anatakiwa ajifunze kutoka kwa mwenzake kwa khulqa (tabia) alizonazo ili apendeze kwa Allaah na kwa watu baada ya kuondokana na khulqa yake mbaya.

06-Mlango Wa Adhkaar Na Du'aa

بَابُ الذِّكْرِ وَالذُّعَاءِ

06-Mlango Wa Adhkaar Na Du'aa

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: أَنَا مَعَ عَبْدِي مَا ذَكَرَنِي، وَتَحَرَّكَتْ بِي شَفَتَاهُ} أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَذَكَرَهُ الْبُخَارِيُّ تَعْلِيْقًا

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Allaah (تعالى) Anasema: “Mimi Niko katika dhana ya mja wangu[1] anaponitaja na midomo yake inatikisika kwa sababu Yangu.” [Imetolewa na Ibn Maajah na akaisahihisha Ibn Hibbaan. Al-Bukhaariy ameitaja kuwa ni Mu’allaq]

1332.

وَعَنْ مُعَاذِ بْنِ جَبَلٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا عَمِلَ ابْنُ آدَمَ عَمَلًا أَنْجَى لَهُ مِنْ عَذَابِ اللَّهِ مِنْ ذِكْرِ اللَّهِ} أَخْرَجَهُ ابْنُ أَبِي شَيْبَةَ، وَالطَّبْرَانِيُّ بِإِسْنَادٍ حَسَنٍ

Kutoka kwa Mu’aadh bin Jabal (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Mwana Adam hajatenda amali yenye kumuokoa zaidi na adhabu ya Allaah kuliko kumdhukuru Allaah.” [Imetolewa na Ibn Abuu Shaybah na Atw-Twabaraaniy kwa isnaad nzuri]

1333.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا جَلَسَ قَوْمٌ مَجْلِسًا، يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا حَفَّتْ بِهِمُ الْمَلَائِكَةُ، وَغَشِيَتْهُمْ الرَّحْمَةُ، وَذَكَرَهُمُ اللَّهُ فِيمَنْ عِنْدَهُ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ^{٢٨}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu hawakai wakamdhukuru Allaah isipokuwa Malaika Huwazunguka,[2] na rahmah huwaenea na utulivu huwateremkia, na Allaah Huwataja kwa walioko Kwake.” [Imetolewa na Muslim]

1334.

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَا قَعَدَ قَوْمٌ مَقْعَدًا لَمْ يَذْكُرُوا اللَّهَ، وَلَمْ يُصَلُّوا عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِلَّا كَانَ عَلَيْهِمْ حَسْرَةٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ، وَقَالَ: "حَسَنٌ"

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Watu hawakai kikao chochote na ikatokea hawamdhukuru Allaah katika kikao hicho wala hawamswalii Nabiy[3] (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) isipokuwa kitakuwa ni majuto kwao Siku ya Qiyaamah.” [Imetolewa na At-Tirmidhiy na amesema Hadiyth hii ni Hasan]

1335.

وَعَنْ أَبِي أَيُّوبَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ قَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ عَشْرَ مَرَّاتٍ، كَانَ كَمَنْ أَعْتَقَ أَرْبَعَةَ أَنْفُسٍ مِنْ وَلَدِ إِسْمَاعِيلَ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Ayyuwb (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakayesema لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ

Hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, peke yake hana mshirika Ni kama mwenye kuacha huru nafsi nne katika wana wa Ismaa’iyl.” [4] [Bukhaariy, Muslim]

1336.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {مَنْ قَالَ: سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ مِائَةَ مَرَّةٍ حُطَّتْ خَطَايَاهُ، وَإِنْ كَانَتْ مِثْلَ زَبَدِ الْبَحْرِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakayesema: سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ

Kutakasika ni kwa Allaah na Kuhimidiwa ni Kwake Mara mia kwa siku atafutiwa dhambi zake hata kama ni mfano wa povu la bahari.” [Bukhaariy, Muslim]

1337.

وَعَنْ جُوَيْرِيَةَ بِنْتِ الْحَارِثِ قَالَتْ: قَالَ لِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {لَقَدْ قُلْتُ بَعْدَكَ أَرْبَعَ كَلِمَاتٍ، لَوْ وُزِنْتُ بِمَا قُلْتُ مِنْذُ الْيَوْمِ لَوَزَنْتُهُنَّ: سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ، عَدَدَ خَلْقِهِ، وَرِضَا نَفْسِهِ، وَزِينَةَ عَرْشِهِ، وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) [5] Kutoka kwa Juwayriyah bint Al-Haarith[5] amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliniambia: “Nimesema maneno manne baada yako lau yangelinganishwa na uliosema tangu leo, ya kwangu yangeyashinda: [6]

سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ، عَدَدَ خَلْقِهِ، وَرِضَا نَفْسِهِ، وَزِينَةَ عَرْشِهِ، وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ

Kutakasika ni kwa Allaah, na kuhimidiwa ni Kwake, kwa idadi ya viumbe Vyake na radhi ya nafsi Yake na uzito wa ‘Arshi Yake na wingi wa (kuandikia) maneno Yake.” [Imetolewa na Muslim]

1338.

وَعَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الْبَاقِيَاتُ الصَّالِحَاتُ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَسُبْحَانَ اللَّهِ، وَاللَّهُ أَكْبَرُ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ} أَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa Abuu Sa'iyd Al-Khudriy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Amali njema yenye kubakia:[7]

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَسُبْحَانَ اللَّهِ، وَاللَّهُ أَكْبَرُ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

Hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, na Kutakasika ni kwa Allaah, na Allaah ni Mkubwa, na sifa njema ni za Allaah na hapana uwezo wala nguvu ila vyote vinatokana na Allaah.”

[Imetolewa na An-Nasaaiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

1339.

وَعَنْ سَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ { أَحَبُّ الْكَلَامِ إِلَى اللَّهِ أَرْبَعٌ، لَا يَضُرُّكَ بِأَيِّهِنَّ بَدَأْتَ: سُبْحَانَ اللَّهِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَاللَّهُ أَكْبَرُ } أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Samurah bin Jundub (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Maneno yapendwayo mno kwa Allaah ni manne hakitakudhuru lolote utakaloanza

سُبْحَانَ اللَّهِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَاللَّهُ أَكْبَرُ

Kutakasika ni kwa Allaah, sifa njema ni za Allaah, Hapana mwabudiwa wa haki ila Allaah, Allaah ni Mkubwa.” [Imetolewa na Muslim]

1340.

وَعَنْ أَبِي مُوسَى الْأَشْعَرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ لِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {يَا عَبْدَ اللَّهِ بْنَ قَيْسٍ! أَلَا أَدُلُّكَ عَلَى كَنْزٍ مِنْ كُنُوزِ الْجَنَّةِ؟ لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

زَادَ النَّسَائِيُّ: {وَلَا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ}

Kutoka kwa Abuu Muwsaa Al-Ash'ariyy (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Ee Abdullaah bin Qays! Nikujulishe hazina za Jannah? [8]

لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

Hapana uwezo wala nguvu ila vyote vinatokana na Allaah.” [Bukhaariy, Muslim]

An-Nasaaiy ameongezea:

لَا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ

Hakuna pa kukimbilia ila ni kwake (Allaah).”

1341.

وَعَنِ النَّعْمَانِ بْنِ بَشِيرٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: {إِنَّ الدُّعَاءَ هُوَ الْعِبَادَةُ} رَوَاهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ التِّرْمِذِيُّ

وَلَهُ مِنْ حَدِيثِ أَنَسٍ بَلْفَظٍ: {الدُّعَاءُ مَخُّ الْعِبَادَةِ}
وَلَهُ مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ رَفَعَهُ: {لَيْسَ شَيْءٌ أَكْرَمَ عَلَى اللَّهِ
مِنَ الدُّعَاءِ} وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) Kutoka kwa An-Nu'maan bin Bashiyr (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika du’aa ndio ‘ibaadah.”[9] [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha At-Tirmidhiy]

Naye amepokea kutoka katika Hadiyth ya Anas kwa tamshi: “Du’aa ni ubongo wa ‘ibaadah.”

Vile vile amepokea katika Hadiyth ya Abuu Hurayrah Marfuw’: “Hakuna kitu kilicho kitukufu kwa Allaah kuliko du’aa.” Na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim

1342.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {الدُّعَاءُ بَيْنَ الْأَذَانِ وَالْإِقَامَةِ لَا يُرَدُّ} أَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ، وَغَيْرُهُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَغَيْرُهُ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Du’aa baina ya Adhaan na Iqaamah hairudishwi.”[10] [Imetolewa na An-Nasaaiy na wengine na akaisahihisha Ibn Hibbaan na wengine]

1343.

وَعَنْ سَلْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ رَبَّكُمْ حَيٌّ كَرِيمٌ، يَسْتَجِي مِنْ عَبْدِهِ إِذَا رَفَعَ إِلَيْهِ يَدَيْهِ أَنْ يَرُدَّهُمَا صِفْرًا} أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ إِلَّا النَّسَائِيُّ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Salmaan (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Hakika Rabb Wenu ni mwenye hayaa Mkarimu Anamstahi mja Wake anapoinua mikono yake Kwake kuirudisha patupu.”[11] [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, Abuu Daawuud, Ibn Maajah) isipokuwa An-Nasaaiy na akaisahihisha Al-Haakim]

1344.

وَعَنْ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا مَدَّ يَدَيْهِ فِي الدُّعَاءِ، لَمْ يَرُدَّهُمَا، حَتَّى يَمْسَحَ بِهِمَا وَجْهَهُ} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَلَهُ شَوَاهِدٌ مِنْهَا: حَدِيثُ ابْنِ عَبَّاسٍ: عَنْ أَبِي دَاوُدَ وَمَجْمُوعُهَا يَقْتَضِي أَنَّهُ حَدِيثٌ حَسَنٌ

Kutoka kwa ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): “Alikua anaponyoosha mikono yake katika du’aa hairudishi hadi aipangusie uso wake.”[12] [Imetolewa na At-Tirmidhiy]

Nayo ina ushahidi mwingi ikiwemo Hadiyth ya Ibn ‘Abbaas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) iliyoko kwa Abuu Daawuud na wengineo. Jumla ya ushahidi wote unapelekea kuwa hii ni Hadiyth Hasan.

1345.

وَعَنْ ابْنِ مَسْعُودٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ، أَكْثَرُهُمْ عَلَيَّ صَلَاةً} أَخْرَجَهُ التِّرْمِذِيُّ وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Ibn Mas-‘uud (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Atakayekuwa karibu zaidi nami siku ya Qiyaamah ni yule anayeniswalia kwa wingi zaidi.”[13] [Imetolewa na At-Tirmidhiy na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1346.

وَعَنْ شَدَّادِ بْنِ أَوْسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {سَيِّدُ الْإِسْتِغْفَارِ، أَنْ يَقُولَ الْعَبْدُ: اللَّهُمَّ أَنْتَ رَبِّي، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، خَلَقْتَنِي، وَأَنَا عَبْدُكَ، وَأَنَا عَلَى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ مَا اسْتَطَعْتُ، أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا صَنَعْتُ، أَبُوءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ، وَأَبُوءُ لَكَ بِذَنْبِي، فَاغْفِرْ لِي؛ فَإِنَّهُ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ} أَخْرَجَهُ الْبُخَارِيُّ

Kutoka kwa Shaddaad bin Aws (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Bwana wa Istighfaar[14] ni mja kusema:

اللَّهُمَّ أَنْتَ رَبِّي، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، خَلَقْتَنِي، وَأَنَا عَبْدُكَ، وَأَنَا عَلَى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ مَا اسْتَطَعْتُ، أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا صَنَعْتُ، أَبُوءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ، وَأَبُوءُ لَكَ بِذَنْبِي، فَاغْفِرْ لِي؛ فَإِنَّهُ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ

Ee Allaah, Wewe ni Rabb wangu, hapana mwabudiwa wa haki ila Wewe, umeniumba mimi na mimi ni mja Wako, nami niko juu ya ahadi Yako, na agano Lako, kiasi cha uwezo wangu, najikinga Kwako kutokana na shari ya nilichokifanya, nakiri Kwako kwa kunineemesha, na nakiri kwa madhambi yangu, basi nakuomba unighufurie kwani hakuna wa kughufuria madhambi ila Wewe.”
[Imetolewa na Al-Bukhaariy]

1347.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: {لَمْ يَكُنْ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَدْعُ هَؤُلَاءِ الْكَلِمَاتِ حِينَ يُمَسِّي وَحِينَ يُصْبِحُ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ فِي دِينِي، وَدُنْيَايَ، وَأَهْلِي، وَمَالِي، اللَّهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَاتِي، وَآمِنْ رَوْعَاتِي، وَاحْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ يَدَيْ، وَمِنْ خَلْفِي، وَعَنْ يَمِينِي، وَعَنْ شِمَالِي، وَمِنْ فَوْقِي، وَأَعُوذُ بِعَظَمَتِكَ أَنْ أُغْتَالَ مِنْ تَحْتِي} أَخْرَجَهُ النَّسَائِيُّ، وَابْنُ مَاجَهَ، وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) hakuwa anaacha maneno haya anapochwewa[15] na anapopambazuka:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ فِي دِينِي، وَدُنْيَايَ، وَأَهْلِي، وَمَالِي،
اللَّهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَاتِي، وَأَمِنْ رَوْعَاتِي، وَاحْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ
يَدَيَّ، وَمِنْ خَلْفِي، وَعَنْ يَمِينِي، وَعَنْ شِمَالِي، وَمِنْ فَوْقِي،
وَأَعُوذُ بِعَظَمَتِكَ أَنْ أُغْتَالَ مِنْ تَحْتِي

“Ee Allaah, hakika nakuomba msamaha na Al’-Aafiyah (hifadhi, amani, salama) duniani na Aakhirah, na ahli wangu, na mali yangu. Ee Allaah nisitiri aibu zangu na nitulize khofu yangu. Ee Allaah, nihifadhi mbele yangu, na nyuma yangu, na kulia kwangu, na kushoto kwangu, na juu yangu, na najikinga kwa Uadhimu Wako kwa kutekwa chini yangu.”

[Imetolewa na An-Nasaa’iy na Ibn Maajah na akaisahihisha Al-Haakim]

1348.

وَعَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: {اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ زَوَالِ نِعْمَتِكَ،
وَتَحَوُّلِ عَافِيَتِكَ، وَفَجْأَةِ نِقْمَتِكَ، وَجَمِيعِ سَخَطِكَ} أَخْرَجَهُ
مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Ibn ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisema:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ زَوَالِ نِعْمَتِكَ، وَتَحَوُّلِ عَافِيَتِكَ، وَفَجْأَةِ
نِقْمَتِكَ، وَجَمِيعِ سَخَطِكَ

“Ee Allaah! Najilinda Kwako kutokana na kuondoka neema Zako, [16] kubadilika uzima wangu, na adhabu yako ya ghafla, najilinda Kwako kutokana na hasira Zako zote.” [Imetolewa na Muslim]

1349.

وَعَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: { كَانَ رَسُولُ
اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ غَلَبَةِ
الدِّينِ، وَغَلَبَةِ الْعَدُوِّ، وَشِمَاتَةِ الْأَعْدَاءِ } رَوَاهُ النَّسَائِيُّ،
وَصَحَّحَهُ الْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Abdullaah bin ‘Umar (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا) amesema
kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa
akisema:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ غَلَبَةِ الدِّينِ، وَغَلَبَةِ الْعَدُوِّ، وَشِمَاتَةِ
الْأَعْدَاءِ

“Ee Allaah! Najilinda Kwako kushindwa na madeni, kushindwa na
adui[17] na kuchekwa na maadui.” [Imetolewa na An-Nasaa'iy na
akaisahihisha Al-Haakim]

1350.

وَعَنْ بُرَيْدَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {سَمِعَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَجُلًا يَقُولُ: اَللّٰهُمَّ اِنِّيْ اَسْأَلُكَ بِاَنِّيْ اَشْهَدُ اَنَّكَ اَنْتَ اللَّهُ لَا اِلَهَ اِلَّا اَنْتَ، اَلْأَحَدُ الصَّمَدُ، الَّذِي لَمْ يَلِدْ، وَلَمْ يُولَدْ، وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا اَحَدٌ. فَقَالَ " لَقَدْ سَأَلَ اللَّهُ بِاسْمِهِ الَّذِي إِذَا سُئِلَ بِهِ أُعْطِيَ، وَإِذَا دُعِيَ بِهِ أُجَابَ } أَخْرَجَهُ الْأَرْبَعَةُ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ

Kutoka kwa Buraydah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Nabiyy alimsikia mtu anaomba:

اَللّٰهُمَّ اِنِّيْ اَسْأَلُكَ بِاَنِّيْ اَشْهَدُ اَنَّكَ اَنْتَ اللَّهُ لَا اِلَهَ اِلَّا اَنْتَ، اَلْأَحَدُ الصَّمَدُ، الَّذِي لَمْ يَلِدْ، وَلَمْ يُولَدْ، وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا اَحَدٌ

“Ee Allaah! Hakika mimi nakuomba kuwa mimi nashuhudia kuwa Wewe ni Allaah, hapana mwabudiwa wa haki ila Wewe, Wewe Peke Yako, Mkusudiwa wa yote, Ambaye Hakuzaa wala Hakuzaliwa na wala hakuna mfano Wake chochote.”

Akasema Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ): Kwa hakika amemuomba Allaah kwa Jina lake ambalo Akiombwa nalo Hutoa[18] na Akiombwa kwalo Hujibu.” [Imetolewa na Al-Arba’ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu Daawuwd, Ibn Maajah) na akaisahihisha Ibn Hibbaan]

1351.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا أَصْبَحَ، يَقُولُ: اَللّٰهُمَّ بِكَ اَصْبَحْنَا، وَبِكَ اَمْسَيْنَا، وَبِكَ نَحْيَا، وَبِكَ نَمُوتُ، وَإِلَيْكَ النُّشُورُ } وَإِذَا

أَمْسَى قَالَ مِثْلَ ذَلِكَ ; إِلَّا أَنَّهُ قَالَ: {وَالَيْكَ الْمَصِيرُ} أَخْرَجَهُ
الْأَرْبَعَةُ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa
Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa
anapopambazuka anasema:

اللَّهُمَّ بِكَ أَصْبَحْنَا، وَبِكَ أَمْسَيْنَا، وَبِكَ نَحْيَا، وَبِكَ نَمُوتُ،
وَإِلَيْكَ النُّشُورُ

“Ee Allaah! Kwako tumepambazuka na Kwako tunakuchwa, Kwako
tunaishi, na Kwako tutakufa,[19] na Kwako tutafululiwa.”

Na anapofikia jioni akisema vivo hivyo isipokuwa mwisho husema

وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ

Na marejeo ya mwisho ni Kwako.

[Imetolewa na Al-Arba'ah (At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Abuu
Daawuud, Ibn Maajah)]

1352.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ أَكْثَرُ دُعَاءِ رَسُولِ اللَّهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً، وَفِي الْآخِرَةِ
حَسَنَةً، وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema: “Du’aa ya Rasuli
wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliyokuwa akikithiri mno
kuisoma ilikuwa

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً، وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً، وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

Ee Rabb! Tupe mema duniani na (Tupe) mema Aakhirah[20] na Utukinge na adhabu ya moto.”[21] [Bukhaariy, Muslim]

1353.

وَعَنْ أَبِي مُوسَى الْأَشْعَرِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَدْعُو: اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي خَطِيئَتِي، وَجَهْلِي، وَإِسْرَافِي فِي أَمْرِي، وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي جِدِّي، وَهَزْلِي، وَخَطِيئِي، وَعَمْدِي، وَكُلُّ ذَلِكَ عِنْدِي، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي مَا قَدَّمْتُ، وَمَا أَخَّرْتُ، وَمَا أَسْرَرْتُ، وَمَا أَعْلَنْتُ، وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي، أَنْتَ الْمُقَدِّمُ وَالْمُؤَخِّرُ، وَأَنْتَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ} مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

(رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) Kutoka kwa Abuu Muwsaa Al-Ash'ariyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema kuwa Nabiyy alikuwa anaomba du'aa hii:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي خَطِيئَتِي، وَجَهْلِي، وَإِسْرَافِي فِي أَمْرِي، وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي جِدِّي، وَهَزْلِي، وَخَطِيئِي، وَعَمْدِي، وَكُلُّ ذَلِكَ عِنْدِي، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي مَا قَدَّمْتُ، وَمَا أَخَّرْتُ، وَمَا أَسْرَرْتُ، وَمَا أَعْلَنْتُ، وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي، أَنْتَ الْمُقَدِّمُ وَالْمُؤَخِّرُ، وَأَنْتَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Ee Allaah! Nighufurie makosa yangu, ujahili (ujinga) wangu, na israaf (upindukaji mipaka) katika mambo yangu, Unayoyajua Wewe

kutoka kwangu. Ee Allaah! Nighufurie niliyoyafanya kwa kudhamiria, na niliyoyafanya kwa kukosea, na makosa yangu yote. Ee Allaah! Nighufurie niliyoyatanguliza na niliyoyachelewesha, na niliyoyaficha, na niliyoyadhihirisha, na ambayo Wewe Unayajua kuliko mimi, Wewe ni Mwenye kutanguliza, na Wewe ni mwenye kuchelewesha. Wewe ni Muweza juu ya kila kitu.” [Bukhaariy, Muslim]

1354.

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: اللَّهُمَّ أَصْلِحْ لِي دِينِي الَّذِي هُوَ عِصْمَةُ أَمْرِي، وَأَصْلِحْ لِي دُنْيَايَ الَّتِي فِيهَا مَعَاشِي، وَأَصْلِحْ لِي آخِرَتِي الَّتِي إِلَيْهَا مَعَادِي، وَاجْعَلْ الْحَيَاةَ زِيَادَةً لِي فِي كُلِّ خَيْرٍ، وَاجْعَلْ الْمَوْتَ رَاحَةً لِي مِنْ كُلِّ شَرٍّ} أَخْرَجَهُ مُسْلِمٌ

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisema:

اللَّهُمَّ أَصْلِحْ لِي دِينِي الَّذِي هُوَ عِصْمَةُ أَمْرِي، وَأَصْلِحْ لِي دُنْيَايَ الَّتِي فِيهَا مَعَاشِي، وَأَصْلِحْ لِي آخِرَتِي الَّتِي إِلَيْهَا مَعَادِي، وَاجْعَلْ الْحَيَاةَ زِيَادَةً لِي فِي كُلِّ خَيْرٍ، وَاجْعَلْ الْمَوْتَ رَاحَةً لِي مِنْ كُلِّ شَرٍّ

“Ee Allaah! Nitengenezee Dini yangu ambayo ndio hifadhi ya mambo yangu, na Nitengenezee dunia yangu ambayo ndani yake ni maisha yangu. Na nitengenezee Aakhirah yangu ambayo ndio marejeo kwangu. Yafanye maisha ni ziada kwangu katika kila kheri,

na mauti ni raha yangu kutokana na kila shari.”[22] [Imetolewa na Muslim]

1355.

وَعَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: {كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: "اللَّهُمَّ إِنْفَعْنِي بِمَا عَلَّمْتَنِي، وَعَلَّمْنِي مَا يَنْفَعُنِي، وَارْزُقْنِي عِلْمًا يَنْفَعُنِي} رَوَاهُ النَّسَائِيُّ، وَالْحَاكِمُ وَلِلتِّرْمِذِيِّ: مِنْ حَدِيثِ أَبِي هُرَيْرَةَ نَحْوَهُ، وَقَالَ فِي آخِرِهِ: {وَزِدْنِي عِلْمًا، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى كُلِّ حَالٍ، وَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ حَالِ أَهْلِ النَّارِ} وَإِسْنَادُهُ حَسَنٌ

Kutoka kwa Anas (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema kuwa Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alikuwa akisema:

اللَّهُمَّ إِنْفَعْنِي بِمَا عَلَّمْتَنِي، وَعَلَّمْنِي مَا يَنْفَعُنِي، وَارْزُقْنِي عِلْمًا يَنْفَعُنِي

“Ee Allaah! Ninufaishe kwa Ulichonifundisha, Unifundishe kitakachonifaa na Uniruzuku elimu itakayoninufaisha.”[23] [Imetolewa na An-Nasaaiy na Al-Haakim]

At-Tirmidhiy amepokea kutoka katika Hadiyth ya Abuu Hurayrah mfano wake mwisho wake akasema:

وَزِدْنِي عِلْمًا، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى كُلِّ حَالٍ، وَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ حَالِ أَهْلِ النَّارِ

“Na Unizidishie elimu. Kuhimidiwa ni kwa Allaah kwa hali zote, na najilinda kwa Allaah kwa hali ya watu wa motoni.” [Isnaad yake ni Hasan]

وَعَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَّمَهَا هَذَا الدُّعَاءَ: {اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنَ الْخَيْرِ كُلِّهِ، عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ، مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الشَّرِّ كُلِّهِ، عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ، مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ مَا سَأَلَكَ عَبْدُكَ وَنَبِيُّكَ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا عَادَ بِهِ عَبْدُكَ وَنَبِيُّكَ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّةَ، وَمَا قَرَّبَ إِلَيْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّارِ، وَمَا قَرَّبَ مِنْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ، وَأَسْأَلُكَ أَنْ تَجْعَلَ كُلَّ قَضَاءٍ قَضَيْتَهُ لِي خَيْرًا} أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَهَ، وَصَحَّحَهُ ابْنُ حِبَّانَ، وَالْحَاكِمُ

Kutoka kwa ‘Aaishah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) amesema kuwa Nabiyy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimfundisha du’aa hii:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنَ الْخَيْرِ كُلِّهِ، عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ، مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الشَّرِّ كُلِّهِ، عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ، مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ مَا سَأَلَكَ عَبْدُكَ وَنَبِيُّكَ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا عَادَ بِهِ عَبْدُكَ وَنَبِيُّكَ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّةَ، وَمَا قَرَّبَ إِلَيْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّارِ، وَمَا قَرَّبَ مِنْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ، وَأَسْأَلُكَ أَنْ تَجْعَلَ كُلَّ قَضَاءٍ قَضَيْتَهُ لِي خَيْرًا

“Ee Allaah! Nakuomba kheri zote za dunia na Aakhirah, ninazozijua na nisizozijua. Najilinda Kwako na shari zote za dunia na Aakhirah,

ninazozijua humo na nisizozijua. Ee Allaah! Nakuomba kheri aliyokuomba mja Wako na Nabiy Wako, na najilinda Kwako na shari aliyokuomba mja Wako na Nabiy Wako. Ee Allaah! Nakuomba Jannah na kinachokaribisha Jannah kwa kauli au kitendo, na najilinda Kwako na moto na kinachokaribisha motoni kwa kauli au kitendo. Nakuomba Ufanye kila hukumu Uliyohukumu kwangu iwe ya kheri.” [Imetolewa na Ibn Maajah na akaisahihisha Ibn Hibbaan na Al-Haakim]

1357.

وَأَخْرَجَ الشَّيْخَانِ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ {كَلِمَتَانِ حَبِيبَتَانِ إِلَى الرَّحْمَنِ، خَفِيفَتَانِ عَلَى اللِّسَانِ، ثَقِيلَتَانِ فِي الْمِيزَانِ، سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ ، سُبْحَانَ اللَّهِ الْعَظِيمِ}

Kutoka kwa Abuu Hurayrah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) amesema Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) amesema: “Kuna maneno mawili yanapendwa mno na Ar-Rahmaan, mepesi katika ulimi, mazito katika mizani:

سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ ، سُبْحَانَ اللَّهِ الْعَظِيمِ

Kutakasika ni kwa Allaah na Kuhimidiwa ni Kwake, Kutakasika ni kwa Allaah Mtukufu.”[24] [Bukhaariy, Muslim]

[1] Katika Hadiyth hii Allaah (عز وجل) Anatangaza kuwa yu Pamoja na mja Wake si kwa kiwiliwili chake bali kwa elimu yake na kwa uweza Wake. Allaah Yupo katika ‘Arshi Yake.

[2] Tunajifunza kupitia Hadiyth hii tukufu kuwa Malaika wanavizungukia vikao vya kumdhukuru Allaah na huenezwa rahmah za Allaah ndani yake.

Allaah (عَزَّ وَجَلَّ) Anaweza kukumbukwa kupitia vikao hivi, kwa kumuomba Yeye tu na kusoma Qur-aan.

[3] Hadiyth nyingine inasema hivi: “[Atawaadhibu, na Akipenda Atawasamehe.](#)” Maneno haya ya kumdhukuru Allaah na kumswalia Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ni ya lazima kufanywa.

[4] Hadiyth hii na Hadiyth za mfano huu, zenye maneno ya kuwa atakayefanya hivi na vile, atapata malipo haya na yale na kughufuriwa madhambi yake. Kuna rai tofauti kwa Wanazuoni kwa maana haswa ya Hadiyth hizi. Baadhi wanaona kuwa malipo yatalipwa kwa yule atakayefanya matendo yale siku zote, wakati Wanazuoni wengine hawahusishi sharti hili. Wanaona kuwa atakayefanya jambo lile la kulipwa ni vizuri ajizuie na madhambi makubwa kwanza. Hii ina maana ya kuwa matendo yale mazuri yatafuta madhambi madogo tu na sio makubwa. Wanazuoni wengine wanaona kuwa hayaingiliani kuwa ni madhambi madogo na makubwa, bali ni suala tu la malipo ayapatayo mtu. Baadhi ya Wanazuoni wana muono kuwa madhambi madogo yanaghufuriwa na kufutika kwa mambo mema ayafanyayo mtu, ama madhambi makubwa kifutio chake ni kutubia na kuomba maghfirah wa Allaah.

[5] Juwayriyah: Huyu ni Ummul-Mu’uminiyn, alikuwa katika mateka wa vita vya Al-Murais. Alikuwa ni katika fungu la hisa la Thaabit bin Qays bin Shammās, ambaye alikubaliana naye kumuuzia uhuru wake. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alimlipa na akamuoa. Baada ya hapo Swahaba wakawaacha huru jamaa za Juwayriyah wakisema: “Hizi ni Shariy’ah za Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ).” Alikuwa ni mwanamke mwenye msaada mkubwa kwa watu wake. Alifariki mwaka 56 Hijriyyah.

[6] Maelezo ni kuwa Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliondoka na kumuacha Juwayriyah akiendelea na ‘ibaadah. Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) aliporudi katika ‘ibaadah wakati wa Dhawuḥā alimuona Juwayriyah akiendelea na ‘ibaadah. Wakati huo Nabiyy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akamtajia maneno yale.

[7] Maelezo mengi yanaonesha kuwa malipo ya matendo yote ya utiifu kwa Allaah na kufanya wema, yatabakia katika amali za aliyefanya

matendo hayo. Miongoni mwa hayo ni maneno haya manne yaliyotajwa katika Hadiyth hii.

[8] Ina maana ya kuwa malipo ya kusema maneno haya ni makubwa, malipo yenyewe Allaah Ameyahifadhi Jannah. Kama zilivyo hazina zozote zenye thamani kubwa zinahifadhiwa katika sehemu yenye usalama.

[9] Du'aa ni sehemu ya 'ibaadah. Kadhalika inaweza kuwa na maana kuwa Du'aa katika aayah ya Allaah:

وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ (٦٠)

“Na Rabb wenu Amesema: Niombeni, Nitakuitikieni. Hakika wale wanaotakabari katika kuniabudu wataingia Jahanam wadhalilike” [Al Ghaafir: 60] ina maana ‘Niabudu nami Nitajibu du’aa zako...’

[10] Tunabainishiwa hapa kuwa kuna baadhi ya muda du’aa zinajibiwa, kama vile katikati ya usiku na baada ya Swalaah ya fardhi. Watu walimuuliza Nabiyy (ﷺ) ni nini cha kuomba katikati ya Adhana na Iqaamah. Nabiyy (ﷺ) aliwaambia wamuombe Allaah al-‘aafiyah (afya na salama) katika maisha yao ya kila siku na Iymaan yao katika kuyaendea mambo yao ya Dini.

[11] Katika Hadiyth hii tunajifunza kuwa ni Sunnah kunyanyua mikono wakati wa kuomba du’aa

[12] Kutokana na mapokezi ya Hadiyth hii ni kuwa baada ya kumaliza du’aa ni vizuri kupangusa uso kwa matumbo ya mkono.

[13] Kwa hakika kumswalia Nabiyy (ﷺ) ni du’aa kwa Allaah ya kumuomba rahmah Nabiyy wake (ﷺ) katika kongamano la Malaika, na ni tendo kubwa la ki’ibaadah. Baada ya du’aa tukufu ya

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

inafuatiwa na ‘ibaadah ya kumuomba Nabiyy (ﷺ) wetu na kumswalia.

[14] Du'aa hii imeitwa kuwa ni bwana wa Istighfaar (kuomba maghfirah). Ina hisia kubwa ya mja kujidhalilisha kwa Bwana wake apate kile anachokiomba.

[15] Al-'Aafiyah ni neno linalujumuisha Allaah (عز وجل) kumjaalia mja Wake salama na na kumpa amani na kumlinda na maradhi, balaa, majanga, madhara, misukosuko, na kila ya aina za shari za wana Adam na majini na kubakia salama katika Dini yake na Aakhirah yake; Katika Dini ni ile hali ya kuacha madhambi na bid'ah, au kupuuzia majukumu ya mtu ya Dini au kuyaacha moja kwa moja. Al-'Aafiyah kwa familia ni kutokupata maradhi, na mahitaji makubwa ya matamano ya dunia. Al-'Aafiyah katika utajiri na mali ni mtu kuokolewa na yanayoangamiza. Katika Hadiyth hii na du'aa Allaah Anatulinda na majanga yote yanayotokana na kukosa Al-'Aafiyah. Tukizingatia kuwa mwana Adam amezungukwa na maadui wake wengi kutokana na mashaytwaan wa kibin Adam na mashaytwaan wa kijini, mwana Adam ni kama kondoo katikati ya mbwa mwitu; kama hana ulinzi kutoka kwa Allaah, hawezi kujilinda yeye mwenyewe.

[16] Neema za Allaah zinaondoshwa na madhambi ya mtu. Kwa maneno mengine, kama kwamba maneno yaliyo katika du'aa hii ni kama kumuomba Allaah Atukinge na ubaya wa matendo yetu. Kwa hakika haya ni maneno tunayofundishwa na Nabiy (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na sio ya kuwa yeye ndie aliyekuwa muhitaji zaidi kwani hakuwa na dhambi.

[17] Kuzidiwa na madeni na ile hali ya kuwa mtu anashindwa tena kuyalipa madeni yale na hali hii huondoa hata nia ya kulipa deni lenyewe. Kwa hakika mwenye niyyah halisi ya kulipa deni lake Allaah Atamsahilishia njia ya kulilipa na kumpa nguvu ya kulipa kama ilivyotajwa katika Hadiyth. Ama kushindwa na maadui ni ile hali ya mtu kushindwa kujitetea au kulipa kisasi cha uadui uliofanywa.

[18] Katika lugha ya Kiarabu kuomba ina maana ya kuomba jambo fulani makhsusi, wakati du'aa ni ya jumla jamala (kuomba chochote). Vile vile kumuomba Allaah kitu, inatakiwa kutumiwa maneno yale yale yaliyokuja katika Hadiyth ambayo yatapata hadhi zaidi ya kujibiwa au kukubaliwa.

[19] Inasemwa, ‘Kulala ni nusu ya mauti’. Kutokana na uhusiano uliyopo wa maneno haya. Muda wowote mtu anapolala, ni kama anarejesha roho yake katika asili yake. Vivyo hivyo, neno la Kiarabu الْمَصِيرُ (mwisho wa kitu) limetumika katika Hadiyth hii (mwisho wako) kwa yule anayejitayarisha kulala. Mfano huo huo, mtu anapoamka, kama kwamba anarejesha uhai baada ya kifo. Katika lugha ya Kiarabu النُّشُورُ (ufufuo) umetumika katika Hadiyth hii kwa maana ya (ufufuo wako) kwa yule ambaye anaamka kutoka usingizini.

[20] حَسَنَةً Mema ya maisha haya yanahusisha vitu vizuri vyema kama vile: mwenza wa maisha (mke/mume), Taqwah, watoto wema, utajiri na kujitosha, matumizi mazuri ya elimu ya mtu, n.k. mema ya Aakhirah ni mja kuingia Jannah, na mengine mfano wake kama vile kuwa mbali na wasiwasi, hesabu ya mtu kuwa nyepesi na kuokolewa na moto. Hadiyth iliyopokelewa na Abuu Hurayrah kwamba mtu anamuomba Allaah na anajikinga na moto mara saba, nao moto unamuomba Allaah kwa kusema: ‘Mja wako fulani anaomba ulinzi wako dhidi yangu, hivyo mpe ulinzi wako.’

[21] Al-Baqarah aayah ya 201

[22] Katika du’aa hii, uzuri wa maisha yote mawili ni yenye kutafutwa. Haina maana kuwa mtu aombee kifo chake. Bali matamanio aina gani ya kifo ikibidi yawe, ambayo ayatampa mja malazi na makazi mazuri baada ya hapo kutokana na kila jambo la shari kabla ya kufa katika maisha haya na baada yake (kaburini).

[23] Hadiyth hii inatufungua macho kuwa tuombe elimu yenye manufaa, na tuombe kwa Allaah na tujikinge na elimu isiyokuwa na manufaa. Elimu isiyokuwa na manufaa n ile isiyokuwa na manufaa na wewe katika Aakhirah yako.

[24] Imaam Al-Bukhaariy alihitimisha Swahiyh Al-Bukhaariy kwa kutaja Hadiyth hii. Kwa kufuata mfano wake waandishi wengi na wakusanyaji wengi wamemaliza Hadiyth kwa Hadiyth hii. Hadiyth hii inathibitisha kuwepo kwa Miyzaan (kipimo cha kupima matendo ya siku ya hukumu) kama yalivyotajwa kwa uwazi katika Qur-aan. Kuna mgongano wa rai miongoni mwa Wanazuoni katika upimaji wa matendo ya watu. Baadhi ya Wanazuoni wana muono kuwa hata ile rekodi ya matendo ya watu itapimwa, kama ilivyothibitishwa na Hadiyth ya “Bitaqa” iliyoripotiwa na Ahmad, Tirmidhiy, Ibn Maajah na wengineo. (Silsilah Ahadiyth Asw-

Swahiyhah 1/212 namba 135). Wanazuoni wengine wana rai kwamba kila tendo lina maana yake, kwa maana kila tendo litapimwa kivyake, kama ilivyothibitishwa na Hadiyth ya mwisho katika Buluwgh Al-Maraam (namba 1358). Hadiyth hii inatuelezea upana wa rahmah ya Allaah, kuwa anatoa malipo makubwa sana kwa matendo madogo sana, na watu kusamehewa kwa makosa yao mara kwa mara.

Ee Allaah! Al-Ghafuwr na Ar-Rahiym, Muokoe mja wako katika asiyoyaona na Mkubalie Tawbah yake kwa huruma yako. Aamiyn, Ee Allaah! Mhifadhi wa dunia na Aakhirah. Ee Allaah! Msamehe madhambi ya mwandishi wa kitabu hiki Aamiyn.